# FASIRI YA BIBLIA ISIYOGHARAMIWA

UNAWEZA KUIELEWA BIBLIA!

*Nyaraka za Paulo kwa Kanisa Lenye Mateso:*

*1 & 2Wakorintho*

Na Dr. Bob Utley, Profesa mstaafu wa kanuni za ufasiri (utafasili wa Biblia)

**ORODHA YA YALIYOMO**

Vifupisho Vilivyotumika Katika Fasiri Hii

Neno Toka kwa Mwandishi: Ni kwa Namna Gani Fasihi Inaweza Kukusaidia

Mwongozo Mzuri wa Usomaji wa Biblia:Utafiti Binafsi kwa Ukweli Uliothibitika

**Fasiri:**

Utangulizi wa 1 Wakorintho

Utangulizi wa 2 Wakorintho

1 Wakorintho 1
1 Wakorintho 2
1 Wakorintho 3
1 Wakorintho 4
1 Wakorintho 5
1 Wakorintho 6
1 Wakorintho 7
1 Wakorintho 8
1 Wakorintho 9
1 Wakorintho 10
1 Wakorintho 11
1 Wakorintho 12
1 Wakorintho 13
1 Wakorintho 14
1 Wakorintho 15
1 Wakorintho 16
2 Wakorintho 1
2 Wakorintho 2
2 Wakorintho 3
2 Wakorintho 4
2 Wakorintho 5
2 Wakorintho 6
2 Wakorintho 7
2 Wakorintho 8
2 Wakorintho 9
2 Wakorintho 10
2 Wakorintho 11
2 Wakorintho 12
2 Wakorintho 13

**Viambatisho:**

Maelezo Mafupi ya Muundo wa Kisarufi wa Kiyunani.

Uhakiki wa Tofauti za Kiuandishi

Ufafanuzi/Faharasa

Maelezo ya Kimaandiko

Copyright © 2013 Bible Lessons International. Haki zote zimehifaziwa. Nukuu au usambazaji wowote wa sehemu ya maandishi haya lazima utolewe pasipo malipo yoyote. Nukuu au usambazaji huo lazima pongezi zimwendee mwandaaji Dr. Bob Utley na ikijumuisha nukuu toka www.freebiblecommentary.org

Msingi wa Mandiko ya Kibiblia yaliyotumika katika fasihi hii yametoka katika toleo la: New American Standard Bible (lililoboreshwa, 1995) Copyright ©1960, 1962, 1963, 1968, 1971, 1972, 1973, 1975, 1977, 1995 by The Lockman Foundation, P. O. Box2279, La Habra, CA 90632-2279

# VIFUPISHO VILIVYOTUMIKA KATIKA FASIRI HII

| | |
|---|---|
| AB | Anchor Bible Commentaries, ed. William Foxwell Albright and David Noel Freedman |
| ABD | Anchor Bible Dictionary (6 vols.), ed. David Noel Freedman |
| ABPS | American Baptist Publication Society |
| AKOT | Analytical Key to the Old Testament by John Joseph Owens |
| ANE | Ancient Near East |
| ANET | Ancient Near Eastern Texts, James B. Pritchard |
| ASV | American Standard Version |
| AV | Authorized Version |
| BAGD | A Greek-English Lexicon of the New Testament and Early Christian Literature, Walter Bauer, 2nd ed. by F. W. Gingrich and Fredrick Danker |
| BDB | A Hebrew and English Lexicon of the Old Testament by F. Brown, S. R. Driver and C. A. Briggs |
| BHS | Biblia Hebraica Stuttgartensia, GBS, 1997 |
| DSS | Dead Sea Scrolls |
| EJ | Encyclopedia Judaica |
| IDB | The Interpreter's Dictionary of the Bible (4 vols.), ed. George A. Buttrick |
| ISBE | International Standard Bible Encyclopedia (5 vols.), ed. James Orr |
| JB | Jerusalem Bible |
| JPSOA | The Holy Scriptures According to the Masoretic Text: A New Translation (The Jewish Publication Society of America) |
| KB | The Hebrew and Aramaic Lexicon of the Old Testament by Ludwig Koehler and Walter Baumgartner |
| KJV | King James Version |
| LAM | The Holy Bible From Ancient Eastern Manuscripts (the Peshitta) by George M. Lamsa |
| LXX | Septuagint (Greek-English) by Zondervan, 1970 |
| MOF | A New Translation of the Bible by James Moffatt |
| MT | Masoretic Hebrew Text |
| NAB | New American Bible Text |
| NASB | New American Standard Bible |
| NEB | New English Bible |
| NET | NET Bible: New English Translation, Second Beta Edition |
| NIDNTT | New International Dictionary of New Testament Theology (4 vol.s), by Colin Brown |
| NIDOTTE | New International Dictionary of Old Testament Theology and Exegesis (5 vols.), ed. Willem VanGemeren |
| NIV | New International Version |
| NJB | New Jerusalem Bible |

| | |
|---|---|
| NKJV | New King James Version |
| NRSV | New Revised Standard Bible |
| OTPG | Old Testament Passing Guide by Todd S. Beall, William A. Banks and Colin Smith |
| REB | Revised English Bible |
| RSV | Revised Standard Version |
| SEPT | The Septuagint (Greek-English) by Zondervan, 1970 |
| TCNT | The Twentieth Century New Testament |
| TEV | Today's English Version from United Bible Societies |
| $UBS^4$ | United Bible Societies' The Greek New Testament, fourth revised edition |
| YLT | Young's Literal Translation of the Holy Bible by Robert Young |
| ZPEB | Zondervan Pictorial Encyclopedia of the Bible (5 vols.), ed. Merrill C. Tenney |

# NENO TOKA KWA MWANDISHI
# NI KWA NAMNA GANI FASIHI HII ITAKUSAIDIA?

Kutafasiri Biblia ni uwiano wa wastani na wa kiroho ambao unajaribu kumwelewa mwandishi wa kale aliyevuviwa kuandika ili kuwezesha ujumbe wa Mungu uweze kueleweka na kutumiwa katika zama hizi.

Mchakato wa kiroho ni muhimu sana lakini mugumu sana kuelezea. Unahusisha kujitoa na kuwa wazi kwa Mungu. Lazima pawepo na njaa (1) kwa ajili yake (2) ya kumjua yeye na (3) kumtumkia yeye. Mchakato huu unahusisha maombi, ukiri na kuwa tayari kubadili mfumo wa kuishi. Roho Mtakatifu ni wa muhimu sana katika mchakato wa utafasiri, lakini kwa nini wakristo waaminifu, wanaompenda Mungu wanaielewa Biblia tofauti kabisa na kuitafasiri visivyo.

Mchakato wa uwiano huu ni rahisi kuuelezea. Lazima tuwe na msimamo na haki kwa maandiko badala ya kuathiriwa na hali ya upendeleo binafsi au wa ki-madhehebu. Sote tumefungamanishwa ki-historia. Hakuna yeyote mtafasiri miongoni mwetu awezae kubisha. Fahiri hii inatoa kwa uangalifu uwiano ulio sahihi wenye kanuni tatu za tafasiri zilizoundwa kusaidia kudhibiti hali zetu za upendeleo.

## KANUNI YA KWANZA

Kanuni ya kwanza ni kuona muundo wa kihistoria ambao kwayo Biblia iliandikwa na tukio zima la kihistoria katika uandishi wake. Mwandishi wa mwanzo alikuwa na kusudi, ujumbe wa kuwakilisha. Andiko haliwezi kumaanisha kitu kwetu ambacho hakikumaanishwa na ile asili, na mwandishi aliyevuviwa wa zama hizo. Kusudi lake na wala sio mahitaji yetu ki-historia, ki-musisimko, ki-tamaduni na mapokeo ya ki-madhehebu yetu ni—ufunguo.

Matumizi ni mbia mkubwa wa tafasiri, lakini tafasiri sahihi lazima ipate kipaumbele kwa matumizi. Lazima isisitizwe kwamba, kila andiko la Biblia lina tafasiri moja tu, na si vinginevyo. Maana hii ndiyo mwandishi wa mwanzo wa Biblia alivyokusudia akiongozwa na roho kuiwasilisha katika enzi zake. Maana hii moja yaweza kuwa na matumizi anwai, katika tamaduni na mazingira tofauti. Matumizi haya lazima yaambatane na ukweli halisi wa mwandishi wa awali. Kwa sababu hii, mwongozo wa fasiri hii imetayalishwa kwa namna ya kutoa utangulizi kwa kila kitabu cha Biblia.

## KANUNI YA PILI

Kanuni ya pili ni kuibainisha fasihi moja. Kila kitabu cha Biblia ni hati ya kumbukumbu iliyounganishwa. Wafasiri hawana haki ya kutenganisha hoja moja ya ukweli kwa nyingine. Kwa hiyo hatuna budi kujaribu kuelewa kusudi la kitabu kizima cha Biblia kabla ya kutafasiri fasihi ya kitabu kimoja kimoja. Sehemu moja—sura, aya, au mistari haiwezi kumaanisha ambacho kitabu kizima hakimaanishi. Tafsiri sharti iwiane na mtizamo mzima kuelekea mtimzamo wa sehemu ya vifungu vya Biblia. Kwa hiyo mwongozo huu wa fasiri ya mafunzo haya umelenga kuwasaidia wanafunzi kuchambua muundo wa kila andiko ki-aya. Mgawanyo wa ibara na sura havikuvuviwa bali ni kutusaidia tu ili kubaini mawazo.

Kutafasiri katika ngazi ya aya na sio sentesi, ibara,kifungu au ngazi ya neno ndio ufunguo katika kufuata maana ya mwandishi aliyokusudia. Aya zimejengwa kwenye mada iliyounganishwa pamoja, mara nyingi huitwa sentesi yenye dhamira au mada. Kila neno, kifungu, ibara na sentesi katika aya kwa kiasi fulani vinahusiana na dhamira iliyo pamoja. Aidha haya huweka ukomo, inapanua , kuieleza na/ au kuihoji. Maelekezo sahihi (ufunguo) kwa tafsiri sahihi ni kufuata wazo la mwandishi wa awali aya kwa aya kufuatana na fasihi binafsi ambayo inatengeneza Biblia nzima..Tafsiri hizi zimechaguliwa kwa sababu zinatumia nadharia mbalimbali za tafsiri.

1. Andiko la Kiyunani la United Bible Society ni rekebisho la chapisho la Nne la (UBS[4]). Andiko hili liliandikwa ki-aya na wasomi wa maandiko ya kisasa.

2. Toleo la New King James Version (NKJV) ni utafsiri wa fasihi wa neno kwa neno uliosimamia kwenye mapokeo ya machapisho ya Kiyunani yaliyojulikana kama "Upokeaji wa Maandishi". Mgawanyo wa aya zake ni mrefu kuliko tafasiri zinginezo. Urefu wa aya hizi unamwezesha wasomi kuona mada zilizo pamoja.
3. Toleo la New Revised English Version(NRSV) ni tafsiri ya neno kwa neno lililoboreshwa. Inatengeneza pointi ya kati baina ya matoleo mawili ya kisasa yanayofuata. Mgawanyo wa aya zake ni wa msaada mkubwa katika kubainisha masomo.
4. Toleo Today's English Version(TEV) ni utafsiri sawia wenye nguvu uliyochapishwa na muungano wa vyama vya Biblia. Unajaribu kutafasiri Biblia kwa njia ya kumwezesha msomaji au mnenaji wa kiingereza cha kisasa kuelewa maana iliyomo katika andiko la Kigiriki. Mara nyingi, hasa hasa katika injili, inagawanya aya kufuatana na mnenaji hata kuliko somo lenyewe, sawa na NIV. Kwa kusudi la mtafasiri, hili halina msaada. Inapendeza kuona kuwa vitabu vya UBS[4] na TEV vimechapishwa na mtu yule yule lakini aya zake zinatofautiana.
5. The Jerusalem Bible(JB) ni tafsiri sawia yenye mlinganyo wa nguvu iliyosimamia kwenye tafasiri ya Katoriki ya Ufaransa. Ni nzuri mno katika kufanya ulinganifu wa aya kutoka katika mtizamo wa ki-Ulaya.
6. Chapisho la andiko ni uboreshaji wa mwaka 1995 wa toleo la Biblia New American Standard Bible (NASB) ambalo ni tafasili ya neno kwa neno. Pia maoni ya mstari kwa mstari yanafuata aya hizi.

## KANUNI YA TATU

Kanuni ya tatu ni kusoma Biblia tofauti tofauti ili kupata uwezekano mpana wa maana (somo la maana ya maneno) kwamba maneno ya Kibiblia au vifungu yanaweza kuwa nayo. Daima, neno au fungu la maneno katika Kiyunani yanaweza kueleweka kwa njia mbalimbali. Tafsiri hizi tofauti husaidia kubaini na kuelezea utofauti uliopo katika maandiko ya awali ya Kiyunani. Lakini haya hayaathiri mafundisho, bali husaidia katika kujaribu kurejelea maandiko asili yaliyoandikwa na mwandishi wa kwanza aliyevuviwa.

Fasiri hii humpa mwanafunzi njia ya haraka ya kuchunguza fasiri zake. Hii haina maana kuwa ni ya kumalizia, bali ni ya utoaji taarifa na udadisi kimawazo. Mara nyingi tafsiri nyingine hutusaidia tusiwe ving'ang'anizi na wafinyu wa mawazo na mapokeo ya kimadhehebu. Watafasili wanapaswa kuwa na upana mkubwa wa kuelewa tafsiri tofauti tofauti na kuweza kubaini ni kwa ugumu upi maandiko ya kale yanaweza kuwa. Inashangaza kuona ni kwa kiasi kidogo kilioje cha makubaliano yaliopo kati ya Wakristo ambao wanadai kuamini biblia kama chanzo chao pekee cha ukweli. Kanuni hizi zimenisaidia kushinda hali yangu ya kufungwa kihistoria na kunifanya nipambane na maandiko ya zama hizo. Ni matumaini yangu kuwa kanuni hizi zitakuwa za Baraka kwako.

Bob Utley
June 27, 1 996
Haki Miliki © 2013 Bible Lessons International

# MWONGOZO KWA USOMAJI MZURI WA BIBLIA:

# UTAFITI BINAFSI KWA UKWELI ULIOTHIBITIKA

Kinachofuata ni maelezo mafupi ya Dr. Bob Utley mwana falsafa wa kanuni za ufasili na njia alizotumia katika fasihi yake.

Tunaweza kuufahamu ukweli? Unapatikana wapi? Tunaweza kuuthibitisha kimantiki? Kweli, kuna mamlaka ya kimsingi? Kuna imani kamili inayoweza kulinda maisha yetu, na ulimwengu wetu tuliomo? Kuna maana yeyote katika maisha? Kwa nini tuko hapa? Tunakwenda wapi? Maswali haya yanauliza kwa watu wote wenye tafakuri zenye uwiano—wameyatawala maarifa ya binadamu tangu mwanzoni mwa nyakati (Mhu. 1:13-18; 3:9-11). Naweza kukumbuka utafiti wangu binafsi kwa ajili ya ungamanisho la maisha yangu. Nimekuwa mwamini katika Kristo kwenye umri mdogo, awali kabisa nikizingatia juu ya ushahidi wa watu wengine muhimu kwenye familia yangu. Nilivyokuwa kufikia utu uzima, maswali juu yangu na ulimwengu ninamoishi ulivyokuwa.Tamaduni za kawaida na dini hazikuleta maana yeyote kwenye uzoefu niliousoma au kukutana nao. Ulikuwa ni muda wa kuchanganyikiwa, kutafuta, kutamani, na mara nyingi fikra zisizokuwa na tumaini katika uso wa ulimwengu mgumu, usiojali nilimoishi.

Wengi walidai kuwa na majibu kwa maswali haya ya msingi, lakini baada ya utafiti na kufikiri nikapata majibu yao yamelenga juu ya (1) falsafa binafsi, (2) hadithi za kubuniwa za kale, (3) uzoefu binafsi, au (4) Saikolojia zilizojichomoza. Nilihitaji digrii fulani ya uthibitisho, baadhi ya vielelezo, kiasi cha busara ambamo ningelenga mtazamo wangu wa kidunia, kiini cha uzima wangu, sababu yangu ya kuishi.

Niliyapata haya katika usomaji wangu wa biblia. Nilianza kutafuta ushahidi wa udhamini nilioupata katika (1) utegemezi wa historia ya biblia kama ulivyothibitishwa na elimu kale, (2) usahihi wa Nabii za Agano la Kale, (3) umoja wa jumbe za Biblia zaidi ya miaka 1600 ya kutolewa kwake na (4) shuhuda binafsi za watu ambao maisha yao yalibadilika moja kwa moja baada ya kusoma biblia. Ukristo, kama mfumo wa imani na kuamini uliounganishwa, una uweo wa kukabiliana na maswali magumu ya maisha ya mwanadamu. Siyo haya tu yanaweza kutoa muundo kazi, lakini mwelekeo unaotokana na uzoefu wa imani za kibiblia uliniletea furaha zenye hisia na ustahimili.

Nilijiridhisha ya kuwa nimepata kiini cha uzima wa maisha yangu—Kristo, kama ninavyoelewa kupitia maandiko.Ulikuwa ni uzoefu mgumu, msukumo wenye kuweka huru. Ingawa, naweza kukumbuka mshituko na maumivu yalipoanza kunifahamisha juu ya tafasiri ngapi tofauti ya kitabu hiki zimetetewa, wakati mwingine hata ndani ya makanisa hayo ya aina moja. Nikithibitisha mwongozo wa Ki-Mungu na uaminifu wa biblia haukuwa mwisho, lakini ni mwanzo pekee. Ni kwa vipi naweza kuthibitisha au kukataa tafsiri zinazotofautiana na kugongana za kurasa nyingi ngumu ndani ya maandiko kwa wale waliokuwa wakidai mamlaka yake na uaminifu?

Kazi hii imekuwa lengo la maisha yangu na hija ya imani. Nilifahamu ya kuwa imani katika Kristo imeniletea furaha na amani kubwa. Mawazo yangu yametamani baadhi ya imani kamili katikati ya nadharia ya utamaduni wangu na mfumo wa imani gonganishi wa dini na majivuno ya kimadhehebu. Katika utafiti wangu wa mitazamo halali kwenye utafsiri wa fasihi ya kale, nilishangaa kuvumbua historia yangu, ya kitamaduni, ya kimadhehebu na uzoefu wa kipendeleo. Kwa kawaida kabisa, mara nyingi, nimesoma Biblia ili kuimarisha mtizamo wangu. Nimeutumia kama chanzo cha mfumo wa imani kuvamia imani nyingine wakati nikijihakikishia usalama wangu na utoshelevu. Ni kwa namna gani utambuzi wa maumivu haya yalikuwa kwangu!

Ingawa siwezi kuwa kipingamizi moja kwa moja, naweza kuwa msomaji mzuri wa biblia. Naweza kuweka ukomo wa upendeleo kwa kutambua na kukubali uwepo wao. Sijawaweka huru,lakini nimeukabiri udhaifu wangu. Mtafsiri mara nyingi ndio adui mbaya wa usomaji mzuri wa biblia! Ngoja nitaje baadhi ya dhanio nilizoleta kwenye usomaji wa biblia ili, msomaji, aweze kuzichunguza pamoja nami:


## I. DHANIO

1. Ninaamini biblia ni uvuvio wa ki-pekee wa ufunuo binafsi wa Mungu mmoja na aliye wa kweli. Kwa hiyo, ni lazima itafsiriwe katika mwanga wa kusudi la Ki-Ungu la mwandishi wa mwanzo (yaani Roho) kupitia mwandishi wa kibinadamu katika muundo wa historia uliokusudiwa.
   - Wapokeaji wa mwanzo
   - Ujumbe ulioandikwa
   - Kusudi la mwandishi wa mwanzo
2. Ninaamini biblia iliandikwa kwa ajili ya mtu wa kawaida—kwa watu wote! Mungu alilazimika mwenyewe kuongea kwetu waziwazi kupitia historia na tamaduni zilizomo. Mungu hakuuficha ukweli, anatutaka sisi kuelewa! Kwa hiyo, inalazimika kutafsiriwa katika (uwazi) katika siku hizo, na siku hizi tulizomo. Biblia haitakiwi kumaanisha kwetu yale ambayo hayakumaanisha kwa wale wa mwanzo walioisoma au kuisikia. Inaeleweka kwa wastani wa mawazo ya kibinadamu na kutumia aina ya njeo mbadala za kawaida za mawasiliano ya ki-binadamu.
3. Ninaamini Biblia inakusudi na ujumbe uliowekwa pamoja. Haina mkanganyiko ndani yake, ingawa inajumuisha (njia ngumu na zinazokinzana). Hivyo basi, mtafsiri mzuri wa biblia ni biblia yenyewe.
4. Ninaamini kwa kila kurasa (pasipo kujumuisha unabii) ina maana moja iliyosimama kwenye kusudi la mwanzo la mwaandishi aliyevuviwa. Ingawa hatuwezi kutia shaka kutambua kusudi la mwandishi wa mwanzo, viashirio vingi daima vimeelekeza katika uelekeo wake;
   a. Aina ya fasihi tanzu uliochaguliwa kuelezea ujumbe
   b. Mtindo wa kihistoria na/au muda maalumu ulioshawishi maandiko kuandikwa
   c. Muundo wa fasihi wa kitabu husika pamoja na kila fasihi moja
   d. Muundo wa maandishi (elezewa kwa fasaha) wa fasihi moja kama zinavyo husiana na ujumbe
   e. Umbo la kisarufi husika lililowekwa kuwasilisha ujumbe
   f. Maana zilizochaguliwa kuwakilisha ujumbe


Mafunzo ya kila eneo hili liwe chanzo cha mafunzo yetu katika aya. Kabla sijaelezea njia zangu za usomaji mzuri wa biblia, hebu nielezee angalau njia zisizosahihi zinazotumiwa siku hizi zilizopelekea kuwepo kwa tafsiri tofauti nyingi na hivyo basi zinatakiwa kuepukika.

## II. Mbinu zisizofaa

1. Kutojali mazingira ya fasihi ya vitabu vya Biblia na kutumia kila sentesi, ibara, au maneno binafsi kama maelezo ya kweli yasiyohusiana na kusudi la mwandishi wa mwanzo au mtindo mpana. Hii mara nyingi huitwa “uhakiki wa andiko”
2. Kutoujali muundo wa ki-hisoria wa vitabu kwa kubadilisha muundo wa ki-historia unaodhaniwa kuwa ni mdogo au usiosaidika kutoka kwenye andiko lenyewe.
3. Kutojali muundo wa kihistoria wa vitabu na kusoma kama gazeti la mtaani lililoandikwa asili kwa wakristo binafsi wa kisasa.
4. Kuupa muundo wa kihistoria wa vitabu kwa kuliistiari andiko ndani ya ujumbe wa falsafa/theolojia isioendana na wasikiaji wa kwanza na kusudi la mwandishi wa mwanzo.
5. Kutojali muundo wa mwanzo kwa kubadilisha mtindo wa theolojia ya mtu, mafundisho yanayopendeka, au mambo ya kisasa yasiyoendana na kusudi la mwandishi wa mwanzo na ujumbe uliotolewa. Tabia hii mara nyingi hufuata usomaji wa mwanzo wa biblia kama kigezo cha kuanzisha mamlaka ya mnenaji. Hii mara nyingi hurejewa kama “mwitikio wa msomaji” (utafsiri wa-andiko-lililomaanisha-kwangu). Kwa wastani, vitu vitatu vinavyoendana vinaweza kupatikana katika mawasiliano ya binadamu yalioandikwa.



Siku za nyuma, mbinu tofauti za usomaji zimenitazamisha juu ya moja kati ya vitu vitatu. Lakini kweli tunatamka kwa dhati uhuisho wa Biblia wa kipekee na mchora uliofanyiwa mabadiliko unaofaa zaidi:




Kwa kweli vitu hivi nyote vitatu lazima vijumulishwe katika mchakato wa ufasiri. Kwa kusudi la uthibitisho, ufasiri wangu unalenga juu ya moja kati ya vitu viwili: mwandishi wa mwanzo na maandiko. Ninayamkinika kujibu matusi mabaya niliyoyachunguza (1) shutumu au kutakasa maandiko na (2) tafasili ya "mwitikio wa msomaji" (unamaanishwa nini kwangu).Matusi yanaweza kutokea katika kila hatua. Ni lazima kila mara tuchunguze mienendo yetu, upendeleo wetu, mbinu na matumizi. Lakini ni kwa jinsi gani tunaweza kuyachunguza kama hapatakuwepo na mipaka ya ufasihi, ukomo au kigezo? Hapa ni pale kusudi la mwandishi na muundo wa maandiko yaliponipa baadhi ya vigezo kuzuia maeneo ya fasiri zilizo halali. Katika kuangazia hizi mbinu za usomaji zisizofaa, zipi ni baadhi ya mitazamo mizuri ya usomaji mzuri wa biblia ambao unatoa digri ya uthibitisho na misimamo?

## III. Mitazamo inayofaa katika usomaji mzuri wa Biblia

Katika hatua hii sijadili mbinu pekee za ufasiri wa namna mahususi lakini kwa pamoja kanuni halali kwa aina yote ya maandiko ya kibiblia. Kitabu kizuri kwa namna ya mitazamo mahususi ni *How To Read The Bible For All Its Worth*, ya Gordon Fee na Douglas Stuart, kilichochapishwa na Zondervan.

Utaratibu wangu mwanzoni ulinitizamisha juu ya msomaji aliyemruhusu Roho Mtakatifu kuangaza biblia kupitia kwa miduara minne ya usomaji binafsi. Hii inamfanya Roho, andiko na msomaji wawe kiwango cha mwanzo, na siyo cha juu. Vile vile hii inamlinda msomaji kutokuwa na mwanya wa kushawishiwa na mtoa maoni. Nimesikia ikisemwa: "Biblia inaangazia zaidi katika fasihi". Hii haimaanishi kukashifu maoni juu ya msaada wa usomaji lakini ni ombi kwa muda unaofaa kwa matumizi yao. Tunalazimika kuusaidia ufasiri wetu kutoka katika andiko lenyewe. Maeneo matatu yanatoa angalau ukomo wa uthibitisho:

1. muundo wa kihistoria
2. mazingira ya fasihi
3. muundo wa kisarufi (vipashio)
4. matumizi ya maneno ya kisasa
5. milango muhimu iliyo sambamba
6. namna tanzu ya uwasilishaji

Tunahitajika kuweza kutoa sababu na mantiki zilizo nyuma ya ufasii wetu. Biblia ndiyo chanzo pekee cha imani yetu na mazoezi. Kwa huzuni, mara nyingi wakristo hawakubali juu ya kile kinachofundishwa au kukiri. Ni kushindwa kudai uhuisho juu ya Biblia na kupelekea waamini washindwe kukubali juu ya kile kinachofundishwa na kutakiwa! Miduara mine ya usomaji imeundwa kutupatia utambuzi wa ufasili ufuatao:

### 1. Mduara wa kwanza wa usomaji

a. Soma kitabu katika mkao mmoja. Soma tena katika fasili tofauti , kwa matumaini kutoka katika fasili tofauti za nadharia
   1) Neno kwa neno (NKJV, NASB, NRSV)
   2) Mlinganyo wenye nguvu (TEV, JB)
   3) Ufafanuzi (Living Bible, Amplified Bible)
b. Angalia kiini cha kusudi la uandishi mzima. Tambua dhamira yake.

c. Tenga (ikiwezekana) fasihi moja, sura, ibara au sentesi inayoelezea waziwazi Kiini cha kusudi au dhamira
d. Tambua fasihi tanzu yenye nguvu
    1) Agano la kale
        a) Simulizi za waebrania
        b) Mashairi ya waebrania (fasihi za hekima, zaburi)
        c) Unabii wa ki-Ebrania (lugha ya mjazo, shairi)
        d) Alama za siri za ki-sheria
    2) Agano jipya
        a) Simulizi (Injili, matendo)
        b) Hadithi za mafumbo (Injili)
        c) Barua/nyaraka
        d) Fasihi za mafunuo

## 2. Mduara wa pili wa usomaji

a. Soma kitabu kizima tena, ukitafuta kufahamu mada muhimu au masomo.
b. Elezea kwa muhtasari wa mada muhimu na elezea kwa kifupi yaliomo kwa maelezo rahisi
c. Angalia kusudi la maelezo yako na eleza kwa mapana kwa msaada wa usomaji.

## 3. Mduara wa tatu wa usomaji.

a. Soma tena kitabu kizima, ukitafuta kutambua muundo wa ki-historia na Matukio lengwa kwa ajili ya uandishi kutoka katika kitabu cha Biblia yenyewe.
b. Taja vipengele vya ki-historia ambavyo vinatajwa katika kitabu cha Biblia.
    1) Mwandishi
    2) Tarehe
    3) Wapokeaji
    4) Kusudu mahsusi la uandishi
    5) Mwelekeo muundo wa kitamaduni unaorandana na kusudi la mwandishi
    6) Marejeo toka kwenye matukio na watu wa kihistoria/ kale
c. Panua maelezo yako kwa kiwango cha aya kutoka katika sehemu ya kitabu cha biblia unayotafasiri. Mara nyingi tambua na kuelezea fasihi. Inaweza kuwa na vifungu na aya nyingi. Hii inakuwezesha wewe kufuata wazo na muundo wa maandiko ya mwandishi wa mwanzo.
d. Angalia muundo wako wa kihistoria kwa kutumia msaada wa usomaji

## 4. Mduara wa nne wa usomaji

a. Soma tena bayana fasihi moja katika tafasiri nyinginezo nyingi
    1) Neno kwa neno (NKJV, NASB, NRSV)
    2) Mwenendo linganifu (TEV, JB)
    3) Ufafanuzi (Living Bible, Amplified Bible)
b. Angalia fahisi au muundo wa kisarufi
    1) Misemo ya kujirudia Waefeso.1:6, 12, 14
    2) Muundo wa kisarufi unaojirudia Warumi 8:31
    3) Mbinyo wa mawazo (dhana zinazoafikiana)
c. Taja vipengele vifuatavyo:-
    1) Istilahi muhimu
    2) Istahili zisizo za kawaida
    3) Muundo muhimu wa kisarufi
    4) Maneno magumu, ibara, na sentesi
d. Angalia njia muhimu zilizosambamba
    1) Angalia njia za wazi za ufundishaji kwenye somo lako kwa kutumia
        a) Vitabu vya thiolojia
        b) Biblia za marejeo
        c) Itifaki

2) Angalia maneno mawili yanayokinzana katika somo lako. Kweli nyingi za ki-Biblia zinatolewa katika rahaja mbili zinazofanana. Migongano mingi ya ki-madhehebu hutokea kutokana na uthibitisho nusu wa maandiko ya Biblia. Biblia zote zimevuviwa. Ni lazima tutafute ujumbe mzima ili kutoa mlinganyo wa ki-maandiko katika tafasiri zetu.
3) Angalia milinganisho ndani ya kitabu, kile kile, mwandishi Yule Yule, au namna ileile, Biblia ina mfasiri wake mzuri kwa sababu ina mwandishi mmoja ambaye ni Roho Mtakatifu.

e. Tumia misaada ya kusoma kuangalia uchunguzi wako wa muundo wa kihistoria na tukio.
1) Soma biblia
2) Ensaikolopidia za biblia, vitabu vya mkononi na kamusi
3) Tangulizi za biblia
4) Fasihi za biblia (katika hatua hii kwenye usomaji wako ruhusu jamii ya waamini, waliopita na waliopo, kusaidia na kusahihisha usomaji wako binafsi)

## IV. Matumizi ya utafasiri wa Biblia.

Katika hatua hii tunageukia matumizi, umechukua muda kuelewa andiko katika muundo wake, sasa lazima utumie katika maisha yako, utamaduni wako, na elezea mamlaka ya Ki-biblia kama "uelewa ule mwandishi wa ki-biblia wa mwanzo alivyosema katika zama zake na kutumia ukweli huo katika zama hizi". Matumizi lazima yafuate utafasiri wa kusudi la mwandishi wa mwanzo katika muda na mantiki.

Hatuwezi kutumia njia ya Biblia katika zama zetu mpaka pale tutakapo fahamu kile alichokuwa akikisema katika zama hizo. Njia ya Biblia isimaanishe kile asicho kimaanisha!
Maelezo yako kwa kirefu, kwa kiwango cha aya (mzunguko wa usomaji≠3) yatakuwa mwongozo wako. Matumizi lazima yafanyike katika kiwango cha aya, na sio kiwango cha neno, maneno yana maana pekee katika mazingira, ibara zina maana pekee katika mazingira na sentensi zina maana pekee katika mazingira. Mtu pekee aliyevuviwa ambaye amejumuishwa katika mchakato wa utafsiri ni mwandishi wa mwanzo. Kipekee unafuata utangulizi wake kwa mwanga wa Roho Mtakatifu. Lakini nuru sio uvuvio. Kusema "asema Bwana"lazima, tufungamane na kusudi la mwandishi wa mwanzo. Matumizi lazima yaendane bayana na kusudi lote la uandishi mzima, maandishi bayana, na muendelezo wa kiwango cha aya.

Usiruhusu mambo ya zama hizi yatafasiri Biblia, iruhusu Biblia ijiongee yenyewe. Hii itatuhitaji kuvuta kanuni kutoka kwenye andiko. Hii itakubalika kama andiko litaiwezesha kanuni. Bahati mbaya wakati mwingi kanuni zetu ni "zetu" na si kanuni za ki-maandiko.

Katika kutumia Bibilia, ni muhimu kukumbuka kuwa (isipokuwa katika unabii) maana moja na moja pekee itakubalika kwa andiko la Kibiblia pekee. Maana hiyo iendane na kusudi la mwandishi wa mwanzo kama alivyo eleza tatizo au hitaji katika zama zake. Mengi ya matumizi yanayowezekana yanaweza kutolewa kutoka katika maana hii moja. Matumizi yatategemea mahitaji ya wapokeaji lakini ni lazima yaendane na maana ya mwandishi wa mwanzo.

## V. Sura ya utafasiri wa kiroho.

Zaidi ya hapo nimejadili mantiki na mchakato wa ki-maandiko uliojumuishwa kwenye utafasiri na matumizi. Sasa ngoja nijadili kwa kinaga ubaga mwelekeo wa kiroho wa utafasiri. Mfuatano ufuatao umekuwa wa msaada sana kwangu.

1. Omba kwa ajili ya msaada wa Roho (kama vile 1Kor. 1:26-2:16)
2. Omba kwa ajili ya msaada binafsi na kusafishwa kutoka katika dhambi inayojulikana (kama vile 1 Yohana 1:9)
3. Omba kwa ajili ya hamu kubwa ya kumjua Mungu (kama vile Zab. 19:7-14, 42:1, 119:1)
4. Tumia utambuzi wowote mpya mara moja katika maisha yako.
5. Baki mnyenyekevu na anayefundishika.

Ni vigumu kuweka mlinganyo kati ya mchakato wa kimantiki na uongozi wa kiroho wa Roho Mtakatifu. Dondoo zifuatazo zimesaidia kulinganisha hizi mbili:

1. Kutoka kwa mwandishi James W.Sire, *scripture twisting*,kr. 17-18
   "Nuru huja kwenye mawazo ya watu wa Mungu na sio tabaka la watu wa kiroho. Hakuna daraja la ualimu katika ukristo wa kibiblia. Hakuna kuongoza, hapana mtu awaye yote ambaye tafsiri zote nzuri zitoke kwake. Na hivyo, wakati roho mtakatifu anatoa karama maalumu ya hekima, maarifa na utambuzi wa kiroho huwa pamoja. Hakutoa hizi kwa wakristo waliokirimiwa kuwa wao ndo pekee watafsiri wenye mamlaka ya Neno lake. Ni juu ya kila watu wake kujifunza, kuamua na kutambua kwa kufanya marejeo kwenye Biblia ambayo inasimama kama yenye mamlaka hata kwa wale ambao Mungu amewapa uwezo pekee. Kwa kufupisha, wazo mnalofanya kupitia kitabu kizima ni kuwa Biblia ni ufunuo wa kweli wa Mungu kwa watu wote, ya kuwa ni mamlaka yetu ya mwisho katika mambo yote ambayo inayaongelea, kuwa sio fumbo lote lakini inaweza kueleweka vya kutosha na watu wa kawaida kwa kila tamaduni."
2. Juu ya Kierkegaard, inayopatikana toka kwa Benard Ramm, *Protestant Biblical Interpretation (tafsiri ya biblia ya ki-protestanti*) Uk.75:
   Kutokana na Kierkegaard, kisarufi, misamiati na usomaji wa kihistoria wa Biblia ulikuwa ni muhimu lakini utangulizi wa usomaji wa kweli wa Biblia na kusoma Biblia kama neno la Mungu mmoja lazima alisome kwa moyo wake wote mdomoni mwake, kutoka ncha ya kidole, na shauku ya matarajio katika mazungumzo na Mungu. Usomaji wa Biblia pasipo tafakari, kutojali au kielimu, au weledi sio usomaji wa Biblia kama neno la Mungu, kama mmojawapo asomavyo barua ya mapenzi isemavyo, tena mmoja asoma kama neno la Mungu.
3. H.H Rawley katika *The Relevance of the Bible*, Uk.19:
   Hakuna uelewa mdogo wa kisomi wa Biblia, ingawa yote, inaweza kumiliki hazina yote. Haidharau uelewa huo, kwa kuwa ni muhimu kwa uelewa wote. Lakini ni lazima iongeze uelewa wa kiroho wa hazina ya kiroho ya kitabu hiki kwa ujumla. Kwa huo uelewa wa kiroho kitu fulani ambacho ni zaidi ya hadhari ya kiroho ni muhimu. Mambo ya kiroho ni utambuzi wa kiroho, na wanafunzi wa Biblia wanahitaji fikra za upokeaji wa kiroho. Ile hamu ya kumtafuta Mungu ambayo inaweza kumsababisha ajitoe kwake. Ni kama kupita zaidi ya usomaji wa kisayansi kuingia kwenye urithi wa utajiri wa hiki kitabu kikubwa kuliko vyote.

## VI. Njia hizi za Fasiri

*Study Guide Commentary (Mwongozo wa usomaji) wa* fasihi umeundwa kusaidia njia zako za utafsiri katika njia zifuatazo:

1. Maelezo fasaha ya kihistoria yanayotambulisha kila kitabu baada ya kufanya "mduara wa usomaji #3" angalia taarifa hizi.
2. Utambuzi wa ki-mazingira unapatikana katika kila kurasa. Hii itakusaidia kuona jinsi gani maandishi/fasihi imeundwa.
3. Katika kila mwanzo wa kifungu au fasihi kubwa inaunganisha mgawawanyo wa aya na maelezo ya kichwa cha makala yanatolewa kutoka katika tafsiri za kisasa.
   a. United Bible Society Greek Text.Toleo la nne lililobadilishwa (UBC)
   b. The New American Standard Bible 1995 ya kisasa (NASB)
   c. The New King James Version (NKJV)
   d. The New Revised Standard Version (NRSV)
   e. Today's English Version (TEV)
   f. The Jerusalem Bible (JB)

Aya zilizogawanywa hazikuvuviwa. Lazima ziyakinishwe kutoka katika mazingira fulani. Kwa kulinganisha tafsiri nyingi za kisasa kutoka tafsiri nyingi za ki-nadharia na mitizamo ya kitheolojia, tunaweza kuchanganua muundo unaokusudiwa wa mawazo ya mwandishi wa mwanzo, kwani kila aya ina ukweli mmoja mkubwa. Huu uliitwa "mada ya sentensi" au wazo la kati la andiko, hilo wazo lililounganishwa ni ufunguo kwa tafsiri nzuri ya kihistoria na kisarufi. Mmojawapo asitafsiri, kuhubiri au kufundisha chini ya aya, vilevile ukumbuke ya kuwa kila aya inahusiana na aya zingine. Hii ndo maana kiwango cha aya kinachoelezea kitabu kizima ni muhimu. Ni lazima tuweze kufuata mtiririko wa kimantiki wa somo lililotolewa na mwandishi wa mwanzo aliyevuviwa.

4. Muhtasari wa Bob unafuata mtazamo wa kifungu kwa kifungu kwa utafsiri wake. Hii inatulazimisha kufuata mawazo ya mwandishi wa mwanzo. Muhtasari unatoa habari kutoka sehemu nyingi.
   a. Mazingira ya fasihi

b. Utambuzi wa kihistoria na tamaduni
c. Habari za kisarufi
d. Usomaji wa neno
e. Njia muhimu zilizo sambamba

5. Mahali fulani katika fasihi, andiko lililochapishwa toka toleo jipya la Marekani (1995 mpaka sasa hivi) litaongezewa na tafsiri za matoleo mbalimbali ya kisasa.
   a. New King James Version (NKJV) ambayo unafuata mswaada wa "Upokeaji wa Maandiko halisi".
   b. The New Revised Standard Version (NRSV) ambayo ni rudio la neno-kwa-neno Kutoka katika Umoja makanisa asili ya Revised Standard Version
   c. The Today's English Version (TEV) ambayo ni tafsiri ya mlinganyo wa nguvu Kutoka American Bible Society.
   d. The Jerusalem Bible (JB) ambayo ni tafsiri ya Kiingereza inayotegemea kutoka tafsiri ya Mlinganyo wa nguvu wa Katoriki ya Ufaransa.
6. Kwa wale wote ambao hawasomi ki-giriki, ukilinganisha na tafsiri za kiingereza inaweza kusaidia kutambua matatizo katika andiko:
   a. Tofauti za mswada
   b. Maana ya maneno mbadala
   c. Muundo na maandiko magumu ya kisarufi Ingawa tafsiri za kiingereza haziwezi kuleta suluhu kwenye matatizo hayo yanayalenga kama sehemu ya ndani na usomaji kamili.
   d. Karibia kila kifungu, maswali muhimu ya majadiliano yanatolewa ambayo yanajaribu kulenga maswala muhimu ya utafsiri wa kifungu hicho

# UTANGULIZI WA 1 WAKORINTHO

## (USHAURI WA KIUTENDAJI KWENYE KANISA LENYE MISUKOSUKO)

I. UHALISIA WA 1 WAKORINTHO

A. Umenukuliwa mara nyingi zaidi na mwanzoni kabisa na makasisi wa kanisa la mwanzo kuliko maandiko yeyote ya Paulo ambayo yanaonyesha umuhimu wake na matumizi yake

B. Katika orodha ya sheria za kanisa, ambazo zilikuwa ni sheria za taratibu za kanisa toka huko Rumi (Mwaka 200 K.K), zimeorodheshwa kama maandiko ya kwanza ya Paulo ambayo pia yameonyesha umuhimu wake.

C. Paulo analeta utofauti katika waraka huu wa kiutendaji kati ya maoni yake binafsi na amri za Mungu. Hata hivyo, hii inasimamia juu ya maarifa yake ya mafundisho ya Yesu juu ya somo lililotolewa. Kama angaliweza angepitia kwenye maneno ya Yesu. Aliamini pia maoni yake yalikuwa yamevuviwa na ya kimamlaka (k.v 1 Kor. 7:25,40)

D. Kanuni za mwongozo wa Paulo kwa ajili ya ushirika wa kanisa ni juu ya uhuru wa mwamini pekee, lakini pia kutimiliza uwajibikaji wao wa pamoja haukusimamia kwenye sheria, lakini katika upendo, nguvu na makuzi ya kanisa lote yalizidi upendeleo binafsi au faida (k.v 1 Kor.12:7)

E. Waraka huu (ukiwa pamoja na 2 Wakorintho) unatupatia mtazamo wa haraka ndani ya kanisa la Agano Jipya, muundo wake, namna na ujumbe wake. Hata hivyo, ni lazima pia ikumbukwe kuwa kanisa hili lilikuwa la kimatatizo, sio kusanyiko halisia.

II. MJI WA KORINTHO

A. Njia ya usafiri kipindi cha majira ya baridi maeneo ya sehemu muhimu za kusini mwa Uyunani (yaani, Cape Malea) zilikuwa za hatari mno kwa hiyo njia za ardhini zilikuwa za muhimu sana. Kijografia kitongoji cha Korintho kilikuwa maili nne ndani ya shingo ya nchi kati ya Ghuba ya Korintho ?(yaani., Ziwa ionia) na Ghuba ya Saranic (yaani, Ziwa Aegea) na kuufanya mji kuwa mji mkubwa wa kibiashara(ulibobea kwenye aina ya vyungu na aina maalumu ya shaba nyeupe), na kituo cha kijeshi. Katika siku za Paulo, hii kiuhalisia ulikuwa ni utamaduni wa Mashariki na Magharibi kukutana.

B. Korintho pia ulikuwa ni kitovu kikubwa cha tamaduni za ulimwengu wa Kiyunani na Kirumi kwa sababu ulikuwa ni mwenyeji wa michuano ya Mabara ya mwaka 581 K.K (kwenye Hekalu la Poseidon). Michezo ya Olympic huko Anthens, Uturuki, kila baada ya miaka minne, zilishindanishwa katika saizi na uwezo (Thucydides, *Hist,* 1.13.5)

C. Katika mwaka wa 146 K.K Korintho ilijihusisha na mapinduzi (yaani, Shirikisho la Achani) dhidi ya Rumi na uliharibiwa na mtawala wa Kirumi Lucius Mummius na kundi kubwa la Kiyunani liligawanyika kwenye utumwa. Kwa sababu ya umuhimu wake wa kibiashara na kijeshi ulijengwa upya huenda mwaka wa 46 au 48 K.K na Julius Kaisari. Na ukajakuwa koloni kubwa la Rumi pale wanajeshi wa Kirumi walipostaafu. Ulikuwa ni mji ulioingizwa kama mji wa kumi kwa usanifu wa majengo na utamaduni na ulikuwa ni kitovu cha utawala wa Rumi (yaani, Maseneta) jimbo la Achani katika mwaka 27 K.K. lilikuja kuwa jimbo la kifalme mwaka 15 B.K.

D. Mji wa zamani wa Korinto ni mji uliokuwa umeimarishwa na kujengwa juu ya vilima, ukiinuka yapata futi 1880 toka usawa wa bahari, ulikuwa ni eneo la Hekalu la Aphrodito. Hekalu hili lilihusishwa kuwa na makahaba 1000 (Strabo, Geograpy, 8.6.20-22). Kuitwa "Wakorintho" (yaani, *Korinthiazesthai,* ukiwa na sarafu ya Aristophanes [450-385 K.K]) kwanza ulistahili kuacha maisha mfanano ya vurugu. Hekalu hili, kama lilivyojulikana kwenye mji, liliharibiwa na tetemeko yapata miaka 150 kabla ya Paulo kuwasili pale, kama ilivyokuwa tena katika mwaka wa 77 B.K, haijulikani kama makundi ya dini yaliendelea kustawi katika siku za Paulo. Kwa vile Warumi katika mwaka wa 146 K.K waliuharibu mji na kuuwa au kuwafanya watumwa wenyeji wote wa pale. Uzuri wa mji wa Kiyunani ulichukuwa nafasi na hadhi ya kikoloni ya Warumi (Pausani II 3.7). Utamaduni huu wa Kirumi badala ya utamaduni wa Kiyahudi, ulitengeneza tofauti muhimu katika kuitafasiri 1 Wakorintho.

## III. MWANDISHI

A. Ilikuwa katika mji huu pale Paulo alipokuja mara ya pili katika safari yake; maelezo yake yanapatikana katika Mdo. 18:1-21. Kupitia kwenye maono Bwana akamfunulia Paulo kuwa wengi wataamini na kuwa hapatakuwepo na upinzani utakaofanikiwa katika huduma yake (k.v Mdo. 18:9-10)

B. Mpango wa safari ya Paulo ulikuwa ni kusimika makanisa katika miji mikubwa katika kipindi cha siku zake, akitambua kuwa wageni, wasafiri na wachuuzi wanaookoka wataihubiri injili kila sehemu wanakokwenda. Ilikuwa hata kwenye kanisa la mahali kuchukuwa wajibu kwa ajili ya uinjilisti na uwanafunzi wa eneo husika.

C. Paulo akawapata Aquila na Priscalla, pia watengeneza mahema walioamini au watengeneza ngozi, katika Korinto. Walifukuzwa kutoka Rumi katika mwaka 49 kwa tamko la Claudio (Orosias, *Hist*, 7:6:15-16) kwa kwenda kinyume na kipato chochote cha Myahudi au sherehe zozote (k.v Mdo. 18:2). Paulo alikuwa mwenyewe Korintho. Wote Silas na Timotheo walikuwa na shughuli nyingine huko Macedonia (k.v Mdo. 18:5). Alikatishwa na tama (k.v Mdo. 18:9-19; 1 Kor. 2:3). Hata hivyo alivumilia na kuendelea kukaa huko Korintho miezi 18 (k.v Mdo. 18:11)

D. Uandishi wa Paulo wa kitabu hiki umethibitishwa na Clement wa Rumi ambaye aliandika waraka kwa Wakorinto katika mwaka wa 95/96 B.K (I Clement 37:5; 47:1-3; 49:5). Uandishi wa Paulo wa waraka huu haukuwahi kutiliwa mashaka, hata na wasomi mahili wa kisasa.

## IV. TAREHE

A. Tarehe ya Paulo kuzuru Korintho iligunduliwa kwa ujumbe wa mtawala Claudio uliopatikana huko Delphi, unaoonyesha tarehe ya Ugavana wa Gallio kama ulianza mwezi wa saba , 52 (k.v Mdo. 18:12-17), ambao utafanya kuonesha tarehe ya kuwasili kwa Paulo kuwa mwaka wa 49-50 B.K.

B. tarehe ya waraka wa Paulo wakati mwingine unaweza kuwa katikati ya mwaka wa 50. Aliuwandika akiwa Efeso alipohudumu kwa muda kati ya miaka miwili (k.v Mdo. 19:10) na miaka mitatu (k.v Mdo. 20:31)

C. uwezekano wa mfanano wa maandiko ya Paulo ukiufatisha F.F Bruce na Murry Harris ulikuwa na mwitikio mdogo.

| <u>Kitabu</u> | <u>Tarehe</u> | <u>Mahali pa kuandikia</u> | <u>Uhusiano wa Mdo</u>. |
|---|---|---|---|
| 1. Wagalatia | 48 | Antiokia huko Syria | Mdo. 14:28; 15:2 |
| 2. 1 Thesalonike | 50 | Korinto | Mdo. 18:5 |
| 3. 2 Thesalonike | 50 | Korinto | |
| 4. 1 Wakorinto | 55 | Efeso | Mdo. 19:20 |
| 5. 2 Wakorinto | 56 | Makedonia | Mdo 20:2 |
| 6. Warumi | 57 | Korinto | Mdo. 20:3 |
| 7-10 Nyaraka magerezani | | | |
| Wakolosai | Mwanzoni mwa 60 | Rumi | |
| Filemoni | Mwanzoni mwa 60 | Rumi | |
| Waefeso | Mwanzoni mwa 60 | Rumi | |
| Wafilipi | Baadaye miaka ya 62-63 | Rumi | Mdo 28:30-31 |
| 11-13 Safari ya nne ya Kimisionari | | Efeso(?) | |
| 1 Timotheo | 63 (au baadaye, | Makedonia | |
| Tito | 63 lakini kabla | | |
| 2 Timotheo | 64 B.K 68) | Rumi | |

## V. WAPOKEAJI WA WARAKA

A. Wapokeaji wa waraka lilikuwa kanisa changa hasa lilikuwa ni la watu wa mataifa. Idadi ya Wakorinto ilikuwa kijamii na kitamaduni imechanganyikana. Tunayafahamu haya toka kwa watu wa mambo ya kale na maandiko (k.v 18:4-8) kuwa palikuwapo na Sinagogi huko Korinto.

B. Maaskari wa Kirumi walistaafia huko baada ya kumaliza miaka 20 ya kulitumikia jeshi. Korinto ulikuwa mji huru, koloni la Kirumi na mji mkuu wa jimbo la Kirumi, Achani.

C. Waraka unaonekana kuaksi kwenye makundi mbali mbali ndani ya kanisa
   1. Wasomi wa Kiyunani walikuwa bado wana majivuno ya tamaduni zao za kifalsafa na walijaribu kung'ang'ania mafunuo ya Kikristo kwa taratibu hizi za kizamani na taratibu za kisomi
   2. Wafadhiri wa Kirumi na wale tabaka la wasomi kwenye jamii
   3. Kundi lililotengenezwa la Wayahudi wanaoamini hasa watu wa mataifa "wenye hofu ya Mungu" waliokuwa wanahudhulia kwenye Sinagogi.
   4. Kundi kubwa la watumwa walioongoka

## VI. DHUMUNI LA WARAKA

A. Paulo alisikia matatizo yaliyoibuka huko Korinto toka kwa vyanzo vine
   1. Watu wa Chloe, 1 Kor. 1:11
   2. Waraka toka kanisani uliouliza maswali, 1 Kor. 7:1,25; 8:1; 12:1; 16:1,12
   3. Matembezi binafsi toka kwa Stephano, Fortunatus na Achaicus, 1 Kor. 16:17

Yawezekana kuwa waraka wa (#2) uliletwa na hawa watu wa (#3)

Inafurahisha kuona kuwa Murry Hurris amefafanua kitabu cha 1 Wakorinto akilenga juu ya maelezo ya Paulo aliyoyapokea kuhusu kanisa.
   1. Taarifa ya kusimuliwa toka kwa wanajumuiya wa nyumbani mwa Chloe, ikisababisha katika maandiko ya Paulo ya sura ya 1 Kor. 1-4 kupatikana
   2. Taarifa ya kusimuliwa toka kwa wawakilishi wa kanisa (yaani., Stephano, Fortinatus, na Achaica), iliyosababisha sura ya 1 Kor. 5-6 kupatikana
   3. Maswali yalioandikwa toka kanisani yaliyosababisha sura ya 1 Kor. 7-16 kupatikana

B. Kanisa likajakuwa lenye vikundi vidogo vidogo likiwatetea viongozi tofauti: Apollo, Petro na yumkini chama cha Kikristo (k.v 1 Kor. 1:12). Sio tu kanisa liliweza kugawika kwa aina ya viongozi, lakini pia kwa maswala ya kimaadili na matumizi ya karama za rohoni. Sababu kubwa hapa ya mabishano ni kuhusu mamlaka ya Kitume ya Paulo (hasa kwenye 2 Wakorinto)

## VII. KUKUTANA KWA PAULO NA KANISA LA KORINTO-MAPENDEKEZO YA MAJARIBIO

A. Ni nyaraka ngapi Paulo aliandika kwa ajili ya Wakorinto?
   1. Huenda mbili, 1 & 2 Wakorinto
   2. Huenda tatu ikiwa moja ilipotea
   3. Nne ikiwa mbili kati yake zilipotea
   4. Baadhi ya wasomi walipata sehemu kati ya zile mbili zilizopotea katika 2 Wakorinto
      a. Waraka wa nyuma (1 Kor. 5:9) katika 2 Kor. 6:14-17:1)
      b. Waraka mchungu (2 Kor. 2:3-4,9; 7:8-12) katika 2 Wakorinto 10-13)
   5. Tano, ukiwa na 2 Kor. 10-13 ukiwa waraka wa tano, uliotumwa baada ya taarifa ya Tito ukihusishwa na taarifa mbaya

B. Nadharia ya #3 inaonekana kuwa nzuri zaidi kwa
   1. Waraka wa nyuma uliopotea (1 Kor. 5:9)
   2. 1 Wakorinto
   3. Waraka mchungu uliopotea (yumkini ni sehemu ya ule uliowekwa kama kumbu kumbu katika 2 Kor. 2:1-11; 7:8-12)
   4. 2 Wakorinto

C. Mapendekezo ya uundaji

| TAREHE | SAFARI | WARAKA |
|---|---|---|
| 50-52 B.K safari ya pili ya Paulo | a. katika safari ya pili ya Paulo alikaa Miezi 18 (k.v Mdo. 18:1-11) | |
| 52 B.K Gallio alikuwa Gavana wa Rumi mwaka 51 B.K (k.v Mdo.18: | | a. 1 Kor. 5:9-11 inaonekana kurejea kwenye waraka kuhusu hali isiyo |

12-17)

ya kiadilifu katika kanisa. Waraka Huo haujulikani isipokuwa
(1) Baadhi wanadai kuwa 2 Kor. 6:14-7:1 ni moja ya sehemu yake au
(2) Kuwa 2 Kor. 2:3,4,9 ni nyaraka za wakati uliopita usiotimilifu na unarejerea kwenye 2 Korinto

Mwaka wa 56 B.K
(majira ya kuchipua)

b. Paulo anayosikia kuhusu matatizo ndani ya kanisa wakati akiwa Efeso toka kwa vyanzo viwili
(1) Watu wa Chloe,1 Kor. 1:11 na
(2) Stephano, Fortunatus, na Achaicus 1 Kor. 16:17. Inaonekana kuwa walileta Waraka toka makanisa ya Korinto ukiwa Na maswali

Mwaka wa 56 B.K
(majira ya baridi) au
Mwaka wa 57 B.K
(majira ya baridi)

b. Paulo anajibu maswali haya (k.v 1 Kor. 7:1,25; 8:1; 12:1; 16:1,2) kwa kuandika 1 Wakorinto, Timotheo (k.v 1 Kor. 4:17) anawajibika toka kwa Waefeso kwenda kwa wakorinto. Timotheo hakuweza kuleta Suluhu ya matatizo ndani ya Kanisa

c. Paulo anafanya safari ya dharura yenye maumivu huko Korinto (haikuwekwa kumbu kumbu katika matendo, k.v 2 Kor. 2:1). Haikuwa na mafanikio lakini aliapa kurudi

c.Paulo anaandika waraka mchungu (k.v 2 Kor. 2:3-4:9; 7:8-12) kwa Makanisa ya Korinto uliopokelewa Na Tito (k.v 2 Kor. 2:3; 7:13-15). Waraka huu haujulikani isipokuwa baadhi wanadhani moja ya sehemu yake ipo katika 2 Kor. 10-13

d.Paulo anapanga kumwona Tito huko Troa, lakini Tito hakuonekana, kwa hiyo Paulo akaamua kwenda Makedonia (k.v 2 Kor. 2:13; 7:5,13), yumkini Filipo(k.v Mss B$^c$,L,P)

d.Alimpata Tito na kusikia kuwa kanisa limeitikia kwenye uongozi wake na tena akaandika 2 Korinto katika shukrani kubwa(k.v 7:11-16) ukapokelewa na Tito.

Mwaka 57-58 B.K

e. Safari ya mwisho ya Paulo kwenda Korinto

(majira ya baridi) iliyoandikwa inaonekana kurejerewa Kwenye Mdo. 20:2-3. Ingawa haitaji Jina la Korinto, kama ilivyofikiliwa aliamua Kubaki huko kipindi cha majira ya baridi

e. Hali ya alama inayobadilika kati ya sura ya 1-9 na 10-13 imeelezewa na wasomi kama taarifa mbaya (yumkini ufufuaji wa upinzani wa Kale na kuongeza upinzani mpya) Kutoka kwa makanisa ya Korinto Baada ya sura ya 1-9 kuwa Imeandikwa

## VIII. HITIMISHO

A. Katika 1 Wakorinto tunamwona Paulo, Mchungaji, akishughulika na tatizo la kanisa. Katika waraka huu na katika Wagalatia, tunamwona akitumia ukweli wa injili ya pamoja katika Nyanja tofauti, akilenga kwenye hitaji la kanisa: uhuru kwa makanisa ya Galatia/vikwazo kwa makanisa ya Wakorinto.

B. Kitabu hiki huenda ni mtiririko wa "tamaduni za kinyama" au utajiri wa kweli ya kikanuni uliotumika kiwenye muundo fulani wa kihistoria/ kitamaduni. Lazima tuwe waangalifu kutochanganya ukweli na matumizi ya kitamaduni ya ukweli huu. Kwa majadiliano mazuri ya hili, suala muhimu la kanuni za ufasiri tazama Gordon Fee na Doglas Sturt juu ya *How To Read The Bible For All Its Worth,* kr. 65-76 na Gordon Fee, *Gospel And Spirit*

C. Kitabu hiki kitakupeleka mpaka kwenye ukomo wa uwezo wako wa kiroho kuweza kutafasiri Biblia. Kitakulazimisha kufikiria upya dhana ya thiolojia yako. Kitakufungulia dirisha kwenda kwenye mapenzi ya Mungu katika hizi siku zetu, kikiongea kiutendaji, kama maandishi mengine machache ya ki-Biblia.

## IX. UFAFANUZI FASAHA WA 1 WAKORINTO

A. Utangulizi wa 1 Korinto 1:1-9
   1. Salamu, 1 Kor. 1:1-3
   2. Shukrani, 1 Kor. 1:4-9

B. Matatizo yaliyowakilishwa katika Korinto, 1 Kor. 1:10-6:20
   1. Makundi madogo madogo ndani ya kanisa kwa sababu ya kutokuelewa visivyo juu ya nia ya uongozi wa Kikristo (yaani., Paulo, Apollo, Petro) na ujumbe 1 Kor. 1:10-4:12
   2. Zinaa ya kushangaza, 1 Kor. 5:1-13
   3. Madai ya Wakristo, 1 Kor. 6:1-10
   4. Uhuru wa Wakristo ukizuiwa na uajibikaji, 1 Kor. 6:12-20

C. Barua toka Korinto ikiuliza maswali ya usumbufu, 1 Kor. 7:1-16:4
   1. Uasherati wa mwanadamu, 1Kor. 7:1-40
   2. Uhusiano wa tamaduni za kizinzi na uhuru wa Mkristo, 1 Kor.8:1-11:1
   3. Ibada ya wakristo na mambo ya rohoni, 1 Kor. 11:2-14:40
   4. Mtazamo juu ya mambo ya siku za mwisho, hasa ufufuo, 1 Kor. 15:1-58
   5. Mchango wa kanisa Mama huko Yerusalem, 1 Kor. 16:1-4

D. Maoni ya kuhitimisha
   1. Mpango wa Paulo kusafiri (na wahudumu wenza)
   2. Ushawishi wa mwisho na salamu, 1 Kor. 16:13-24

## X. MAANDIKO YALIYOPENDEKEZWA JUU YA FIKRA ZA PAULO

A. *The Mind of St. Paul*, William Barclay, published by Harper & Row

B. *Paul, Apostle of the Heart Set Free*, F. F. Bruce, published by Eerdmans

C. *The Origins of Paul's Religion*, J. Gresham Machen, published by Eerdmans

D. *Paul, An Outline of His Theology*, Herman Ridderbos (translated by John De Witt), published by Eerdmans
E. *Epochs in the Life of Paul*, A. T. Robertson, published by Baker
F. *A Man In Christ*, James S. Stewart, published by Harper & Row
G. *Dictionary of Paul and His Letters*, published by IVP
H. *Paul in the Roman World, The Conflict at Corinth*, Robert M. Grant, published by Westminister, John Knox Press
I. *Philo and Paul Among the Sophists*, Bruce W. Winter, published by Eerdmans
J. *After Paul Left Corinth*, Bruce W. Winter

## MZUNGUKO WA KWANZA WA USOMAJI

Hili ni somo la mwongozo wa ufasiri, ambalo linamaanisha kwamba una wajibika kuitafsiri Biblia. Kila mmoja wetu anapaswakutembea katika nuru tulio nayo. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usiiache hii kwa mtoa maoni pekee.

Soma sura kwa wakati mmoja.elezea kiini cha dhamira ya kitabu chote kwa maneno yako mwenyewe.

1. Dhamira ya kitabu kizima
2. Aina ya fasihi iliyotumika (tanzu)

## MZUNGUKO WA PILI WA USOMAJI (Angalia **Mwongozo wa Usomaji Mzuri wa Biblia (A Guide to Good Bible Reading**

Hili ni somo la mwongozo wa ufasiri, ambalo linamaanisha kwamba una wajibika kuitafsiri Biblia. Kila mmoja wetu anapaswa kutembea katika nuru tulio nayo. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usiiache hii kwa mtoa maoni pekee.

Soma kitabu chote cha Biblia mara ya pili kwa wakati mmoja. Fafanua vichwa vya habari na uelezee ujumbe wa somo kwa sentensi moja.

1. Somo la kwanza la sehemu ya fasihi
2. Somo la pili la sehemu ya fasihi
3. Somo la tatu la sehemu ya fasihi
4. Somo la nne la sehemu ya fasihi

# 1 WAKORINTHO 1

| MGAWANYO WA AYA WA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **UBS[4]** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB** |
| Salamu na Shukrani | Salamu | Salamu | Salamu | Utambulisho na Salamu |
| 1:1-3 | 1:1-3 | 1:1-3 | 1:1 | 1:1-3 |
| | | | 1:2 | |
| | | | 1:3 | |
| | Karama za Rohoni huko Korintho | Shukrani | Baraka ndani ya Kristo | Shukrani |
| 1:4-9 | 1:4-9 | 1:4-9 | 1:4-9 | 1:4-9 |
| Mgawanyiko Kanisani | Utengano wa Kivikundi ni Dhambi | mgawanyiko huko Korintho | Mgawanyiko ndani ya kanisa | Mifarakano kati ya waaminifu |
| 1:10-17 | 1:10-17 | 1:10-17 | 1:10-13 | 1:10-16 |
| | | | 1:14-17 | Hekima ya kweli Na ya uongo |
| Kristo nguvu na Hekima ya Mungu | Kristo nguvu na Hekima ya Mungu | Kristo aliyesulubiwa (1:18-2:5) | Kristo Nguvu na Hekima ya Mungu | (1:17-3:4) |
| | | | | 1:17-25 |
| 1:18-25 | 1:18-25 | 1:18-25 | 1:18-20 | |
| | | | 1:21-25 | |
| 1:26-31 | 1:26-31 | 1:26-31 | 1:26-31 | 1:26-31 |

* Ingawa hazijavuviwa, migawanyo ya aya ndiyo ufunguo wa kuelewa na kufuata kusudio la awali la mwandishi. Kila tafsiri ya kisasa imegawanya na kufanya muhtasari wa aya. Kila aya ina mada kuu, kweli, au wazo. Kila toleo hufupisha mada hiyo kwa namna yake ya pekee. Unaposoma andiko, jiulize ni tafsiri gani inashabihiana na uelewa wako wa mada na mgawanyo wa aya. Katika kila sura lazima tusome Biblia kwanza na kujaribu kutambua somo (aya), kisha tulinganishe uelewa wetu na matoleo ya kisasa. Ni pale tu tunapoelewa kusudio la asili la mwandishi kwa kufuata mantiki yake na uwasilishaji wake, ndipo tunapoweza kuielewa Biblia kiukweli. Ni mwandishi wa asili tu aliyevuviwa—wasomaji hawana haki ya kubadili au kurekebisha ujumbe. Wasomaji wa biblia wana wajibu wa kutumia kweli iliyovuviwa kwenye siku na maisha yao. Fahamu kwamba maneno yote ya kiufundi na vifupisho vimefafanuliwa kikamilifu kwenye nyaraka zifuatazo: Maelezo Fasaha ya Muundo wa Sarufi za Kiyunani (Brief Definitions of Greek Grammatical Structure), Uhakiki wa Tofauti za Kiuandishi (Textual Criticism) na Ufafanuzi (Grossary).

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (kutoka "**Mwongozo wa Usomaji Mzuri wa Biblia"("A Guide to Good Bible Reading")**

### *KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo wa usomaji wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako binafsi ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika nuru tuliyonayo. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hupaswi kumwachia kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo. Linganisha mgawanyo wa masomo yako na tafsiri tano hapo juu. Kugawanya katika aya hakuna uvuvio, isipokuwa ni ufunguo wa kufuatilia kusudio la asili la mwandishi ambalo ndilo kiini cha ukalimani. Kila aya ina somo moja na ni moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA):1 WAKORINTHO 1:1**
**1 Paulo, aliyeitwa kuwa mtume wa Yesu Kristo kwa mapenzi ya Mungu, na Sosthene ndugu yetu,**

**1:1 "Paulo"** Wengi miongoni mwa Wayahudi wa siku za Paulo walioishi nje ya Palestina walikuwa na majina ya kwanza mawili, moja la Kiyahudi na moja la Kirumi (kama vile Matendo 13:9) Jina la Paulo la Kiyahudi lilikuwa Sauli. Yeye kama mfalme wa kwanza wa Waisraeli alikuwa wa kabila la Benjamini (kama vile Rum. 11:1; Flp. 3:5). Jina lake la Kirumi ama Kiyunani, Paulo lilimaanisha "mdogo".

1. Hii ilihusu aidha urefu wa umbile lake, ambalo lilihusianishwa na kitabu cha karne ya pili kisichohusu sheria za kanisa, *The Acts of Paul,* katika sura inayohusiana na Wathesalonike ikiitwa "Paulo na Tekla"
2. Kwa hisia yake binafsi ya kuwa mdogo kuliko wote miongoni mwa watakatifu kwa sababu hapo mwanzoni alilitesa kanisa (kama vile1 Kor. 15:9; Efe. 3:8; 1 Tim. 1:15)
3. Kwa sababu tu ya jina alilopewa na wazazi wake wakati wa kuzaliwa.

◙ **"aliyeitwa"** Angalia Mada Maalum ifuatayo.

**MADA MAALUMU: ALIYEITWA (SPECIAL TOPIC: CALLED)**

◙ **"mtume"** Hili ni neno la kawaida la Kiyunani kwa "upelekwa" (yaani *apostellō*). Angalia Mada Maalum katika 1 Wakorintho 4:9.
Neno lina matumizi kadhaa ya Kitheolojia.

1. Walimu wa sheria za Kiyahudi (Rabbis) walilitumia kama mtu aliyeitwa na kutumwa kama mwakilishi rasmi wa mwingine, kitu kama kwa kiingereza chetu "balozi" (kama vile 2 Kor. 5:20)
2. Injili mara nyingi hutumia neno hili kuhusu Yesu akiwa ametumwa na Baba (kama vile Mt. 10:40; 15:24; Marko 9:37; Luka 9:48) katika Yohana neno kuchukua vidokezo vya maana halisi vya ki-Masihi (kama vile Yohana 4:34; 5:24,30,36,37,38; 6:29,38,39,40,57; 7:29; 8:42; 10:36; 11:42; 17:3,8,18,21,23,25; 20:21). Limetumika kwa Yesu akiwatuma waaminio (kama vile Yohana 17:18; 20:21).
3. Agano Jipya lilitumika kwa wanafunzi.
    a. Wale kumi na wawili wa awali waliokuwa kiini cha wanafunzi (kama vile Luka 6:13; Matendo 1:21-22)
    b. Kundi maalum la wasaidizi wa kitume na watenda kazi wenzao.
        1) Barnaba (kama vile Matendo 14:4,14)

2) Androniko na Yunia (KJV Junia, kama vile Rum 16:7)
3) Apolo (1 Kor. 4:6-9)
4) Yakobo mdogo wake Bwana (Gal. 1:19)
5) Silivanusi na Timotheo (kama vile 1 The. 2:6)
6) Yawezekana Tito (kama vile 2 Kor. 8:23)
7) Yawezekana Epaprodito (kama vile Flp. 2:25)

c. Karama zinazoendelea ndani ya kanisa (kama vile 1 Kor. 12:28-29; Efe. 4:11)

4. Paulo hutumia wadhifa huu kwa ajili yake miongoni mwa nyaraka zake kama njia ya kutetea wito wake aliopewa na Mungu na mamlaka yake kama mwakilishi wa Yesu Kristo (kama vile Rum. 1:1; 1 Kor. 1:1; 2 Kor. 1:1; Gal. 1:1; Efe. 1:1; Kol. 1:1; 1 Tim. 1:1; 2 Tim. 1:1; Tito 1:1).

◙ **"Yesu Kristo"**Maneno haya ni sehemu ya cheo kamili cha "Bwana Yesu Kristo" (kama vile 1 Kor. 1:2,3,7,8,9,10) Nyadhifa hizi tatu zote zina umuhimu wa kila mmoja.

1. "Yesu" ndilo jina lililopewa mtoto na malaika huko Bethlehemu, Mathayo 1:21. Kutokana na nomino mbili za Kiebrania "YHWH," Jina la Agano la "Uungu" na "Wokovu" (yaani Hosea). Ni jina la Kiebrania linalofanana na Yoshua. Linapotumika peke yake mara nyingi linamtambulisha mwanaume, Yesu wa Nazareti, mwana wa Mariamu (mf, Mt.1:16, 25; 2:1; 3:13,15,16).
2. "Kristo" Ni tafsiri ya Kiyunani ya Masihi wa Kiebrania (yaani aliyepakwa mafuta) linathibitisha jina la Yesu la Agano la Kale la mtu aliyekuwa ameahidiwa kutumwa na YHWH kuanzisha kizazi kipya cha haki.
3. "Bwana" (lililotumika katika 1 Kor. 1:1 katika KJV) ndiyo tafsiri ya neno la Kiebrania *Adon* ambalo linamaanisha "mmiliki mume, bwana ama mtawala" Wayahudi wakawa na hofu kulitamka jina la YHWH wasije wakaharibu na kuvunja mojawapo ya amri kumi za Mungu na kila waliposoma maandiko waliweka jina *Adon* badala kwa YHWH. Hii ndiyo maana tafsiri zetu za kiingereza hutumia herufi zote kubwa BWANA kwa YHWH katika Agano la Kale. Kuhamisha wadhifa huu (*kurios* kwa Kiyunani) kuwa Yesu, katika Agano Jipya waandishi wanathibitisha Uungu wake na usawa wake na Baba.

◙ **"kwa mapenzi ya Mungu"** Hii ni habari ya kwanza miongoni mwa nyingi zenye kusisitiza katika utangulizi huu ikihusu mamlaka ya Paulo (yaani "aliyeitwa kuwa mtume" 1 Kor. 1:1 "kwa mapenzi ya Mungu," 1 Kor. 1:1, na "kwa jina la Bwana wetu Yesu Kristo" 1 Kor. 1:10). Mamlaka ya kitume ya Paulo ndilo swala kuu la kithiolojia katika nyaraka za Wakorintho, hasa 2 Wakorintho.
Aya ile ile ya utangulizi imetumika kwenye Kol. 1:1; 1 Kor. 1:1; 2 Kor. 1:1; na 2 Tim. 1:1 Paulo alikuwa amejiridhisha kwamba Mungu alikuwa amemchagua kuwa mtume. Hii fasihi maalumu ya dhana akilini ilianza pale alipoongoka njiani akielekea Dameski (kama vile Matendo 9:22, 26)

◙ **"Sosthene"** Yawezekana huyu ndiye alikuwa kiongozi wa Kiyahudi aliyetajwa katika Matendo 18:17, aliyepigwa na lile kundi la watu wenye fujo na yawezekana baadaye aliamini na kuwa kiongozi wa kanisa. Yawezekana alikuwa (1) msaidizi wa Paulo; (2) mwandishi (mtaalamu wa dini) (3) chanzo cha habari kuhusu kanisa ama (4) mtu ambaye kanisa lilimjua vizuri.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA):1 WAKORINTHO 1:2**
**2 kwa kanisa la Mungu lililoko Korintho, wale waliotakaswa katika Kristo Yesu, walioitwa wawe watakatifu, pamoja na wote wanaoliitia jina la Bwana wetu Yesu Kristo kila mahali, Bwana wao na wetu.**

**1:2 "kwa kanisa"** Angalia Mada Maalum chini

## MADA MAALUMU:KANISA (*EKKLESIA*) (SPECIAL TOPIC: CHURCH (*EKKLESIA)*

◙ "**la Mungu lililoko Korintho"** aya hii inafafanua dhana mbili zilizo dhahiri kuhusu "kanisa"

Ni udhihirisho wa mwili wa Kristo ulioenea kote. Hili linaonekana katika Mathayo 16:18 (yaani mmoja wa kwanza miongoni mwa matumizi adimu ya neno hili alilolitumia Yesu (kama vile Mt. 18:17 [mara mbili]); Matendo 9:31 hutumia umoja wa neno"kanisa" kwa makusanyiko yote ya mahali katika Uyahudi, Galilaya na Samaria; na mwishowe matumizi ya neno katika Waefeso ambalo ni waraka wa kuzunguka katika makanisa yote ya Asia ndogo (Efe. 1:22; 3:10,21; 5:23-32) kuna moja ya chombo kikubwa cha Kristo kinachoundwa na waamini wote (wengine sasa wamekufa, wengine wako hai) na kuna maelezo ya kimahala ya chombo hiki cha pamoja.

◙ "**wale waliotakaswa**" Hii ni KAULI TIMILIFU TENDWA ENDELEVU Ambayo inamaanisha wamekwisha na wanaendelea kutangazwa kuwa watakatifu kwa kazi ya Yesu Kristo kupitia uwakala wa roho (kama vile 1 Kor. 6:11) neno hili (*hagiazō*) linahusiana na neno "takatifu" (*hagios*) na "watakatifu" (yaani, "walio watakatifu" *hagioi* ). Anazungumzia kuhusu kutengwa kwetu kwa ajili ya kumtumikia Mungu. Hapa anazungumzia mahali petu katika yeye kama 1 Kor. 1:3 inavyozungumzia, lakini sehemu nyingine kwenye Agano Jipya waaminio wanawajibika kujitahidi kuelekea "utakatifu" (mf. Mt. 5:48). Ni mahali panapopaswa kumilikiwa. Paulo analitia moyo kanisa hili la bandia lenye kiburi kwa kuwaita watakatifu hata katikati ya kushindwa kwao na dhambi.

## MADA MAALUMU: UTAKATIFU/UTAKASO WA AGANO JIPYA (SPECIAL TOPIC: NEW TESTAMENT HOLINESS/SANCTIFICATION

◙ **"katika Kristo Yesu"** Mfumo huu wa sarufi unadhihirisha MAZINGIRA YA MAHALI YA waamini wanatakaswa na baba (yaani, chanzo kama vile Yohana 17:7; 1 The. 5:23) kupitia Yesu Kristo (yaani sababu kama vile1 Kor. 1:2; Efe. 5:26) vipengele vyote vinakuja pamoja katika Ebr. 2:11 ni roho mtakatifu ambaye kwa kawaida anadhaniwa kuwa sababu, yaani wakili, kama vile Rum. 15:16; 2 The. 2:13).
Hii ndiyo njia ipendwayo na Paulo kwa kuwadhihirisha waamini. Mfano mzuri wa jambo hili ni Efe.1:3,4,7,9,10,12,13.
Angalia William Barclay, *The Mind of St*. Paul, uk. 121 -132. Inamaanisha umuhimu wa jambo, muunganiko binafsi na Yesu (kama vile Matendo 17:28)

Inapendeza kutambua jinsi waandishi wakati mwingine wako

1. "ndani ya Kristo Yesu - MSS $P^{46}$, B, D, F, G
2. "ndani ya Yesu Christo - MSS א, A

Aina hii ya utofauti hutokea mara nyingi katika mchakato wa kusoma na kunakiri. Haiathiri maana lakini huonesha kwamba waandishi wa awali walikuwa wanahusika sana na maana ya msingi ya maneno halisi ya mwandishi na sio kujua kusoma kulikoshawishika.

◙ **"walioitwa"** Hii ni KAULI YA KATI ENDELEVU YA WAKATI ULIOPO. Kama jinsi Paulo alivyoitwa mtume, ndivyo pia Wakristo wa Korintho walivyoitwa watakatifu (kama vile Rum. 1:7). Tambua uzito wa msisitizo juu ya fundisho la uchaguzi katika sura hii ya 1 Kor. 1:9,24,26,27,28. Muundo huu unahusu kitendo cha awali cha Mungu kuwaita pamoja na kuitwa baadaye na Yesu katika maombi kwa ajili ya wokovu, kulikosababisha uwepo wa maombi endelevu, kuabudu na utii. Wokovu ni imani ya mwanzoni/mwitikio wa toba na kuendelea kuamini/kuitika kwenye toba. Tazama Mada Maalumu: Kuitwa katika 1 Kor. 1:1.

◙ **"watakatifu"** "Watakatifu" (*hagioi*) linahusiana kitheolojia na neno la Agano la Kale "takatifu," (*kados*h) linalomaanisha "kutengwa kwa ajili ya kazi ya Mungu" (kama vile 1 Kor. 1:2; 2 Kor. 1:1; Rum. 1:1; Flp. 1:1; Kol. 1:2). Neno hili lipo katika WINGI kwenye Agano Jipya isipokuwa mara moja kwenye Wafilipi (4:21),lakini hata hapo limetumika katika hali ya kiushirika. Kuokolewa ni kuwa sehemu ya imani ya jumuiya ya agano la imani, familia ya waaminio, mwili wa Kristo.

Watu wa Mungu ni watakatifu kwa sababu ya haki ya Yesu iliyozuliwa (kama vile Warumi 4; 2 Kor. 5:21; Wagalatia 3). Ni mapenzi ya Mungu kwamba waishi maisha matakatifu (kama vile 1 Kor. 1:4; 4:1; 5:27; Kol. 1:22; 3:12).

Waamini wanatangazwa kuwa watakatifu (utakaso wa mahali) na wameitwa kwenye mfumo wa maisha matakatifu (utakaso endelevu). Kuhesabiwa haki na kutakasika lazima vidaiwe pamoja!

## MADA MAALUM: WATAKATIFU (SPECIAL TOPIC: SAINTS)

◙ **"pamoja na wote wanaoliitia jina la Bwana wetu Yesu Kristo kila mahali"** Paulo hutumia aya hii kuwakumbuka waamini wa Korintho kwamba wao ni sehemu ya kanisa kubwa la kifamilia. Hawana haki ya upekee ama wapewe huduma maalum. Lazima wafanane na mwili wote wa Kristo katika mafundisho na utendaji (kama vile 1 Kor. 4:17; 7:17; 11:16; 14:33).

◙ **"anaoliitia jina la Bwana wetu"** Hii inahusu mtu anapojiunga kuwa mkristo (kama vile Matendo 2:21; 22:16; Rum. 10:9-13), lakini pia akaendelea kuabudu (yaani, matumizi ya Agano la Kale ya jina, kama vile Mwa. 4:26; 12:8; 26:25). Hii hapa ni KAULI YA KATI ENDELEVU YA WAKATI ULIOPO, ambapo inaelezea uhusiano wa ki-imani wa hatua kwa hatua na kristo (yaani, inafanana kitheolojia na ile ya paulo "ndani ya kristo") na msisitizo juu ya chaguo la mtu. Tazama Mada Maalum katika 1 Kor. 1:10.

◙ **"*Bwana wao* na wetu"** Hii ni aya nyingine inayotamka umoja wa waaminio wote na makanisa yote. Yesu ni Bwana wa makusanyiko yote ya wakristo ambao ni pamoja na Wakorintho. Paulo anajitambulisha mwenyewe na Sosthene na waamini wengine walioko Korintho katika aya hii. Wanapaswa kukumbushwa kwamba (1) wao ni mojawapo ya makusanyiko mengi na (2) kwamba Paulo ni mmoja wao na kwa ajili yao!

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA):1 WAKORINTHO 1:3**
**3 Neema na iwe kwenu na amani, zitokazo kwa Mungu Baba yetu, na kwa Bwana Yesu Kristo.**

**1:3 "Neema"** Paulo amebadili namna ya kawaida ya kuanza kuandika waraka wa Kiyunani wa neno "salamu," *charein,* kuwa neno la kipekee la Kikristo ambalo linaonekana kuwa sawa na, *charis* (kama viloe Rum. 1:7; 2 Kor. 1:2; Gal. 1:3 Efe. 1:2; Flp. 1:2; 2 The. 1:2; Filemoni 1:3).

◙ **"amani"** Yawezekana kwamba kama vile neema ilivyoaksi salaam ya asili ya Kiyunani hivyo "amani" iliaksi salamu ya asili ya Kiebrania, *shalom*. Neno *shalom* ni neno la Kiebrania kwa ajili ya salamu na kusema kwa heri. Inaonesha sio tu kwamba hakuna matatizo, bali uwepo wa wema na afya njema ya mafanikio. Inawezekana kwamba salamu ya kawaida ya Paulo yatoka katika Hes. 6:25-26, ambapo vyote viwili neema na amani vinaonekana. Kitheolojia mara zote neema hutangulia amani, lakini vyote vinapatikana tu pale palipo na uhusiano wa imani na Yesu, (yaani, kwa ushirika na mtu binafsi).

## MADA MAALUM: AMANI (*SHALOM*) (SPECIAL TOPIC: PEACE (*SHALOM*))

◙ **"zitokazo kwa Mungu Baba yetu, na kwa Bwana Yesu Kristo"** vyote viwili "neema" na "amani" huja kutoka kwa Baba na mwana. Baba na Yesu kisarufi wameungana kama kitu kimoja (yaani, kihusishi kimoja lakini vitu viwili). Hii ni njia ya kawaida kwa waandishi wa Agano Jipya kutangaza Uungu wa Yesu. (kama vile 1 The. 1:1; 3:11; 2 The. 1:2,12; 2:16). Matumizi ya vyeo vya Mungu kwenye Agano la Kale kutumika kwa Yesu ni njia moja ya kutangaza ukweli ule ule (yaani, BWANA);Pia tukio moja la Agano la Kale "Siku ya Bwana," sasa inaelekezewa kwa Yesu ("siku ya Bwana wetu Yesu Kristo," kama vile 1 Kor. 1:8).
Kwa ajili ya cheo cha neno "Bwana Yesu Kristo" angalia nukuu katika 1 Kor. 1:1.

## MADA MAALUM: UBABA WA MUNGU (SPECIAL TOPIC: FATHERHOOD OF GOD)

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) :1 WAKORINTHO 1: 4-9**

**4 Namshukuru Mungu sikuzote kwa ajili yenu, kwa sababu ya neema ya Mungu mliyopewa katika Kristo Yesu; 5 kwa kuwa katika kila jambo mlitajirika katika yeye, katika maneno yote, na maarifa yote; 6 kama ushuhuda wa Kristo ulivyothibitika kwenu; 7 hata hamkupungukiwa na karama yo yote, mkikutazamia sana kufunuliwa kwake Bwana wetu Yesu Kristo; 8 ambaye atawathibitisha hata mwisho, ili msilaumiwe siku ile ya Bwana wetu Yesu Kristo. 9 Mungu ni mwaminifu ambaye mliitwa na yeye mwingie katika ushirika wa Mwanawe, Yesu Kristo Bwana wetu.**

**1:4 "Namshukuru Mungu sikuzote kwa ajili yenu"** Hii ni KAULI TENDAJI YENYE KUARIFU YA WAKATI ULIOPO, ambayo inafafanua kitendo kinachoendelea. Aya 4-9 ni upanuaji wa mambo ambayo Paulo anamshukuru Mungu kwayo katika maisha ya kanisa hili lililotaabishwa. Kutoa shukrani katika utangulizi kilikuwa kitu kilichotegemewa kiutamaduni katika barua zilizoandikwa kwenye karne ya kwanza. Hakuna shukrani kwenye utangulizi wa 2 Wakorintho (wala Wagalatia).
Kuna maandishi ya Kiyunani ya kale yenye herufi kubwa (yaani, א* na B) pamoja na toleo la Kilatin, P[61], א[2], A, C, D, F, G, toleo la ki-Shamu, Coptic, na Tafsiri za ki -America zimo ndani yake. Maandiko la Kiyunani ya toleo la UBS[4] yanatoa hitimisho la kiwango “A”(yaani, yenye uhakika).

## MADA MAADA: SHUKRANI (SPECIAL TOPIC: THANKSGIVING)

◙ **" kwa sababu ya neema ya Mungu mliyopewa katika Kristo Yesu"** Paulo anasisitiza kwamba kusimama kwao na karama zao kulikuwa ni kwa neema ya Mungu kupitia kazi iliyokamilishwa ya Yesu Kristo na sio juhudi zao binafsi (yaani, KAULI TENDWA ENDELEVU YA WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFU, kama vile Efe. 2:8-9). Huu ulikuwa mlango uliohitajika kuondoa kiburi chao cha kiroho katika

1. Viongozi wao waliokuwa na karama
2. karama zao binafsi za kiroho
3. msingi wao wa kisomi (yaani, utamaduni wa Kiyunani)
4. maisha yao ya kijamii (yaani, utamaduni wa Kirumi)

**1:5 "katika kila jambo mlitajirika katika yeye"** Hii ni KAULI TENDWA ELEKEZI YA WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFU inayoendelea na msisitizo wa kitheolojia 1 Kor. 1:4 (yaani, neema ya Mungu mliyopewa katika Kristo). Katika VITENZI VYOTE TENDWA kwenye 1 Kor. 1:4-9 mwakilishi atamkwaye ni Mungu. Nafsi tatu za Mungu zimewapa waamini kila kitu wanachohitaji (yaani, karama zote za rohoni, kama vile. 1 Kor. 1:7). Tazama Mada Maalum: Utatu katika 1 Kor. 2:10.
Angalia matumizi ya Paulo kwenye aya hii ya *pas* tatu (yaani, "yote" au "kila kitu"). Mungu ndiye Yeye atoaye. Hahitaji welevu, akili, au msimamo wa kijamii wa wanadamu.

**NASB "katika maneno yote, na maarifa yote"**
**NKJV "katika kutamka kote na maarifa yote"**
**NRSV "katika maneno na maarifa ya kila aina"**
**TEV "katika mambo yote pamoja na maneno na maarifa yote"**
**NJB "katika kila aina ya maneno na maarifa yote"**

Tafsiri ya Phillips inayo kauli "kutoka maneno ya kinywa chako hadi uelewa wa moyo wako."Hii ni mitazamo miwili ya asili ya kiyunani (yaani, wale wenye mafunuo wa mwanzo) yenye kiburi cha kiroho ambacho kilikuwa kinakuwa ndani ya kanisa la Korintho (kama vile 1 Kor. 13:1-3). Walikuwa wanajitukuza katika vipawa vyao na utendaji badala ya Kristo. Mungu ndiye alikuwa amewapa karama hizi. Hapakuwepo na nafasi kwa kiburi cha kibinadamu (kama vile Efe. 2:9). Angalia **MADA MAALUM: MAJIVUNO (SPECIAL TOPIC: BOASTING)** katika 1 Kor. 5:6.
Elimu ambayo Paulo anayohusisha sio elimu ya nadharia, wala elimu ya shuleni bali ukweli wa Kikristo na jinsi inavyotumika katika maisha (kama vile 1 Kor. 1:8-10; Rum. 14:1-15:13). Elimu ya kibinadamu hujenga, lakini elimu

ya Mungu huinua umaarufu wa mtu na huelekeza kwenye amani na upatanifu kwenye ushirika wa Kikristo. Ni jinsi gani wanahitaji karama ya Mungu ya maarifa katika kanisa lao!

**1:6 "kama ushuhuda wa Kristo"** Kuhubiri injili kwa mitume, kukitiwa nguvu na roho, kuliwatajirisha hawa waaminio katika karama za rohoni, Kama Baraka na karama zote za Mungu, hutiririka kupitia Kristo hadi kwa wahitaji, mioyo inayoitikia.

**NASB, NKJV "ulivyothibitika kwenu"**
**NRSV "umetiwa nguvu miongoni mwenu"**
**TEV "umeshikanishwa kwa nguvu ndani yenu"**
**NJB "umeota mzizi ndani yenu"**

Hili ni neno la Kiyunani *bebaios*, ambalo lina vidokezo vitatu.

1. Kile ambacho ni hakika, bila mashaka ama chaweza kutegemewa (kama Rum. 4:16; 2 Kor. 1:7; Hebr. 2:20; 3:6,14; 6:19; 2 Pet. 1:10,19).
2. Mchakato ambao uaminifu wa kitu unaonyeshwa au kuanzishwa (kama vile Rum. 15:8; Hebr. 2:2, kama vile Louw na Nida, *Greek-English Lexicon of the New Testament*, Juzuu. 1, kur. 340,377,670).
3. Katika karne ya kwanza maandishi kwenye mafunjo ya lugha ya Koine yaliyopatikana misri yalikuwa ni maneno ya kitaalamu kwa dhamana ya kisheria (kama vile Moulton na Milligan, *The Vocabulary of the Greek New Testament*, kur. 107-8).

Hapa inahusu nguvu ya Mungu ikidhihirishwa miongoni mwao (yaani, karama za rohoni) . Ingeweza kuhusu dhihirisho nyingine za rohoni, kwa sababu ni kauli nyingine TENDAJI YENYE KUARIFU YA WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFU KATIKA 1 Kor. 1:5 (ingeweza pia kuhusu matendo ya Mungu kupitia Roho mtakatifu kwenye kuongoka kwao 1 Kor. 1:4).

**1:7**
**NASB, NJB "hamkupungukiwa na karama yo yote"**
**NKJV "ili msiwe na upungufu katika karama yoyote"**
**NRSV "ili msiwe mnapungukiwa karama yoyote ya kiroho"**
**TEV "kwamba hamjashindwa kupokea baraka moja"**
Neno “karama," ni *charisma*.Neno hili linahusiana na neno “neema” *charis* linalosisitiza kwamba karama za kiroho zinatolewa na Mungu kwa nia njema (kama vile 1 Kor. 12:7,11). Zimekusudiwa kumtukuza Kristo, sio roho ama Mkristo binafsi (kama vile sura 12-14). Karama zote zilikuwemo ndani ya kanisa la Wakorintho kama zilivyo kwa kila Kanisa (kama vile 1 kor. 1:5). Mungu ametoa kwa wingi (yaani, HASI MARA MBILI yenye nguvu ukihusianishwa na neno "kupungukiwa") kwa watu wake wakati wa kuja kwa Kristo mara ya pili kupitia huduma ya Roho Mtakatifu.

◙ "**mkikutazamia sana**" Neno hili la Kiyunani linaweza kumaanisha

1. Kungojea kwa ustahimilivu kwa jambo linalotazamiwa kwenye tukio la baadaye (kama vile Ebr. 10:13; 1 Pet. 3:20)
2. Kutazamia tukio la baadaye kwa shauku kubwa (kama vile Rum. 8:19,23,25; Flp 3:20; Ebr. 9:28)

Tafsiri za NKJV, NASB, na tafasiri ya NIV inafuata #2, ambapo tafsiri za NRSV, TEV, na NJB zinafuata na #1.

◙ "**kufunuliwa kwake Bwana wetu Yesu Kristo**" Hili ni neno la Kiyunani *apocalupsis*. Mara nyingi limetafsiriwa kama "ufunuo." Neno hili kimsingi linamaanisha kurudisha nyuma pazia ili kudhihilisha kitu fulani. Ndiyo sifa ya kitabu cha mwisho katika Agano Jipya. hapa kinarejea juu ya kurudi kwa Yesu (kama vile 1 Kor. 1:8). Angalia **MADA MAADA: MANENO YA AGANO JIPYA JUU YA KURUDI KWA YESU (SPECIAL TOPIC: NT TERMS FOR CHRIST RETURN)**katika 1 Kor. 15:23.

**1:8**
**NASB, NKJV " ambaye atawathibitisha hata mwisho"**
**NRSV "Yeye pia atawaimarisha hata mwisho"**
**TEV "Atawafanya imara hata mwisho"**
**NJB "Ataendelea kuwapa ninyi nguvu hata mwisho"**

1 Kor. 1:4-9 yote, wakala mtendaji wa VITENZI TENDWA amekuwa ni Mungu. Hata hivyo, 1 Kor. 1:8 ni tata. Baadhi ya watoa maoni wanadhani kwamba kwa mara ya kwanza katika sehemu hii Kristo ndiye anayerejelewa "ambaye" yaonekana kimuktadha ni bora kuchukulia kwamba Mungu Baba bado ndiye wakala mtendaji ambaye anawatia nguvu waamini na anasimika kukubalika kwao.

Neno "thibitisha" lilitumika katika 1 Kor. 1:6. Kanisa hili lilihitaji kuimarishwa liwe lisilo badilika na bila kuyumbayumba. Hii ndiyo sababu kubwa ya barua za Paulo kuletwa kwao. Injili ya Kristo ilikuwa imethibitishwa (yaani 1 Kor. 1:8). Katika 2 Kor. 2:8 Paulo anataka upendo wao kwake uthibitike.

Biblia inaonekana kuwa na kweli mbili kinzani kuhusu uhusiano wa waamini na Mungu.

1. Ni wa Ki-Agano kwa asili; kwa hiyo, unahusu imani ya awali na endelevu pamoja na mwitikio wa toba. Lazima uwe wenye juhudi kudumisha uhusiano wetu.
2. Uko salama katika uaminifu wa Mungu (kama vile Yuda 24) hakuna awezaye kuiba uhusiano wetu kutoka kwetu (kama vile Yohana 6:37,39; 10:28; Rum. 8:38-39) Usalama na ustahimilivu yote mawili ni ki-biblia (kama vile Efe. 2:8-9,10 na Flp. 2:12-13) hiyo ndiyo mionekano miwili ya lazima ya "agano"

◙ "**msilaumiwe"** Angalia Mada Maalum ifuatayo.

## MADA MAALUMU: ISIYO LAUMIWA, ISIYO NA HATIA, ISIYO NA KOSA, PASIPO LAWAMA (SPECIAL TOPIC: BLAMELESS, INNOCENT, GUILTLESS, WITHOUT REPROACH)

◙ **"siku ile ya Bwana wetu Yesu Kristo"** Waandishi wote wa Agano Jipya wamechukua "siku ya YHWH ya Agano la Kale na kuitumia kwenye kuja mara ya pili kwa Yesu Kristo. Yesu Kristo ni mbadala wa YWHW katika uumbaji, ukombozi na hukumu.

**1:9 "Mungu ni mwaminifu"** Neno hili "imani" kwenye Agano la Kale ni upanuaji wa sitiari wa msimamo imara au thabiti. Ulikuja kuwa alama kistiari kwa kile kilicho hakika, chenye kuaminika, chenye kutegemewa na cha uaminifu. Kati ya vyote hivi hakuna kinachoelezea hata ukombozi wa mwanadamu aliyeanguka. Sio kuaminika kwa mwanadamu, au uaminifu au kutegemewa bali ni kwa Mungu (kama vile Kumb. 7:9; Zab. 36:5; 40:10; 89:1,2,5,8; 92:2; 119:90; Isa. 49:7; Rum. 3:3; 1 Kor. 10:13; 2 Kor. 1:18; 1 The. 5:24; 2 Tim. 2:13) Tunatumaini ahadi zake za kuaminika, sio tunavyo aminika! Utii wa ki-agano unabubujika kutoka kwenye shukrani. Mtazamo wa kibiblia wakati wote umekuwa juu ya uaminifu wake, sio imani ya waaminio! Imani haiwezi kumwokoa yeyote. Neema tu ndiyo huokoa, lakini inapokelewa kwa imani (kama vile Efe. 2:8-9). Mtazamo kamwe hauwezi kuwa juu ya kiasi cha imani (kama vile Mt. 17:20) bali juu ya jambo (Yesu). Tumaini letu ni katika tabia ya Mungu isiyobadilika ambaye huita na kuaidi (kama vile Mal. 3:6; 2 Kor. 1:20). Imani hupokea kipawa cha bila malipo cha Mungu katika Kristo (kama vile Rum. 3:22,25; 4:5; 6:23; 9:30; Gal. 2:16; 1 Pet. 1:5) Mungu anashugulikia mwanadamu aliyeanguka kwa njia ya agano. Kila mara huchukua ari (kama vile Yohana 1:12; 3:16-17,36; 6:40; 11:25-26; Rum. 10:9-13) na huandaa agenda na mipaka (kama vile Yohana 6:44,65) Huruhusu mwanadamu aliyeanguka kushiriki katika wokovu wake kwa kuitikia kwenye ahadi aliyoitoa kwenye agano lake. Mwitikio wa kile alichokitoa kama dhamana ni imani tangu mwanzo pamoja na imani inayodumu, toba, utii, huduma, ibada na ustahimilivu.
Michael Magill, *New Testament Transline*, uk. 577, #24, ina ushauri mkubwa:

"Angalia njeo ya wakati uliopita katika 1 Kor. 1:5-6, Mungu ni mwaminifu katika fahamu zote tatu.

## MADA MAALUM: KUSADIKI, AMINI, IMANI NA UAMINIFU KATIKA AGANO LA KALE (אמן) (SPECIAL TOPIC: BELIEVE, TRUST, FAITH AND FAITHFULNESS IN THE OLD TESTAMENT אמן)

◙ **"ambaye mliitwa"** Huu ni msisitizo unaoendelea kuhusu uchaguzi wa Mungu kwa waaminio wa Korintho (kama vile 1 Kor. 1:2,9,24,26; Matendo 18:9)

◙ **"ushirika wa Mwanawe"** Hili ni neno la Kiyunani *koinonia* linalomaanisha ushiriki wa pamoja. Mungu ametuita kuwa na ushirika katika mwana wake vyote kimahali (Angalia Mada Maalum: Utakaso katika 1 Kor. 1:2) na Kimahusiano. lengo la Ukristo ni kufanana na Kristo (kama vile Rum. 8:29; Gal. 4:19; Efe. 1:4; 2:10).

Mtindo wa maisha wa waaminio baada ya kukutana na Yesu ni ushahidi tosha kwa wokovu wao (kama vile vitabu vya Agano JIpya vya Yakobo na 1 Yohana). Wanaokolewa kwa neema kwa njia ya imani ili watende kazi (kama vile Efe. 2:8-9,10)! Wanaokolewa ili kutumikia (kama vile Rum. 6:11)! Imani pasipo matendo imekufa, kama matendo pasipo imani (kama vile Mt. 7:21-23 na Yakobo 2:14-26). Lengo la uchanguzi wa baba ni kwamba waaminio wawe "watakatifu pasipo lawama" (kama vile Efe. 1:4; Mt. 5:48).

Paulo alishambuliwa mara nyingi kwa injili yake ambayo ilikuwa huru kwa sababu ilionekana kuchochea maisha yasiyo matakatifu. Injili inaonekana kutohusiana na utendaji usio wa kiadilifu ambao waweza kuwaelekeza watu kwenye uovu. Injili ya Paulo ilikuwa huru katika neema ya Mungu na kazi iliyokamilishwa ya Yesu pamoja na kubembeleza kwa roho mtakatifu, lakini, pia ilihitaji pia mwitikio stahiki, sio tu katika toba ya awali tu, bali katika kuendelea kutubu. Maisha ya kumcha Mungu ndiyo matokeo sio kuishi pasipo utii wa sheria. Kufanya matendo mema sio njia ya kupata wokovu, bali ni matokeo, hii kweli kinzani ya wokovu wa bure na usio na gharama ni ngumu kuwasilishwa kimawasiliano, lakini mawili hayo lazima yabebwe kiuwiano katika mazingira ya watu waliojaa msongo wa mawazo na kweli inayokwenda kinyume na mantiki isiyoeleweka. Mtu anapaswa asitenge kuhesabiwa haki na kufanywa mtakatifu.

### MADA MAALUM: *KOINŌNIA* (SPECIAL TOPIC: *KOINŌNIA)*

◙ **" Mwanawe"** Yesu kama mwana wa Mungu ndiyo dhana yenye kujirudia rudia ya maandishi ya Paulo (kama vile Rum. 1:3,4,9; 5:10; 8:3,29,32; 1 Cor. 1:9; 2 Kor. 1:19; Gal. 1:16; 2:20; 4:4,6; Efe. 4:13; Kol. 1:13; 1 The. 1:10). Yeye si "mwana"kwa muda tu, bali "Mwana" katika umilele (kama vile Ebr. 1:2; 3:6; 5:8; 7:28). Haijawahi kutokea muda ambao Yesu hakuwa Mwana. Kuinuliwa kwa Yesu kwenye ufufuo na kupalizwa kwake kumerejesha na kutukuza uwepo wake wa kabla, na utukufu wa kufanyika kwake mwanadamu kabla.

### MADA MAALUM: MWANA WA MUNGU (SPECIAL TOPIC: SON OF GOD)

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA):1 WAKORINTHO 1:10-17**

**10 Basi ndugu, nawasihi, kwa jina la Bwana wetu Yesu Kristo, kwamba nyote mnene mamoja; wala pasiwe kwenu faraka, bali mhitimu katika nia moja na shauri moja. 11 Kwa maana, ndugu zangu, nimearifiwa habari zenu na wale walio wa nyumbani mwa Kloe, ya kwamba iko fitina kwenu. 12 Basi, maana yangu ni hii, ya kwamba kila mtu wa kwenu kusema, Mimi ni wa Paulo, na, Mimi ni wa Apolo, na, Mimi ni wa Kefa, na, Mimi ni wa Kristo. 13 Je! Kristo amegawanyika? Je! Paulo alisulibiwa kwa ajili yenu? Au je! Mlibatizwa kwa jina la Paulo? 14 Nashukuru, kwa sababu sikumbatiza mtu kwenu, ila Krispo na Gayo; 15 mtu asije akasema kwamba mlibatizwa kwa jina langu. 16 Tena naliwabatiza watu wa nyumbani mwa Stefana; zaidi ya hao, sijui kama nalimbatiza mtu ye yote mwingine. 17 Maana Kristo hakunituma ili nibatize, bali niihubiri Habari Njema; wala si kwa hekima ya maneno, msalaba wa Kristo usije ukabatilika.**

**1:10 "Basi"** Hii ni KAULI ILIYO KINYUME. Paulo anaanza na ujumbe mahsusi wa barua.

◙ **"nawasihi"** Aya hii ilikuwa nyepesi na ngumu. Ulikuwa ni mwito kwa maisha stahiki na vilevile changamoto ya kimamlaka. Paulo mara nyingi alitumia neno hili (kama vile 1 Kor. 1:10; 4:16; 16:15; 2 Kor. 2:8; 5:20; 6:1; 10:1; 12:1,8; 15:30; Efe. 4:1; Flp. 4:2; 1 The. 4:10; 1 Tim. 1:3; Filemoni 1:9-10). Tazama nukuu katika 2 Kor. 1:4-11.

### MADA MAALUM: FARIJI (SPECIAL TOPIC: CONFORT)

◙ **"ndugu"**Paulo hutumia neno "wapenzi" au "ndugu” mara nyingi. Ingawa Paulo alilazimika kusihi kundi hili kwa maneno mazito bado walibaki kuwa ndugu zake wa kiume na wa kike katika Kristo.
Paulo mara nyingi hutumia neno hili kutambulisha somo jipya, lakini ndani ya kitabu hiki anautumia kuonyesha umoja wa kanisa wakiwa na Paulo pamoja na makanisa mengine.

◙ **"kwa jina la Bwana wetu Yesu Kristo"** Katika maisha ya Wayahudi jina liliwakilisha tabia ya mtu na mamlaka. Hapa tafsiri ya Filipo ilikamata uzito wa maneno"yale yote ambayo Bwana wetu Yesu Kristo alimaanisha kwako."

**MADA MAALUM : JINA LA BWANA (SPECIAL TOPIC: THE NAME OF THE LORD)**

◙ **" kwamba nyote mnene mamoja"** Kuna kauli mbili TENDAJI TEGEMEZI ZA WAKATI ULIOPO katika kusudi la Paulo (yaani., *hina*) la sura hii.

1. Kuwa asiweze kuendelea na mifarakano (KAULI TENDAJI TEGEMEZI YA WAKATI ULIOPO)
2. Kuwa waweze (KAULI TENDAJI TEGEMEZI YA WAKATI ULIOPO) kuungana na kuwa kitu kimoja (YAANI., KAULI TIMILIFU TENDWA YA HALI YA KUENDELEA, ambayo inatengeneza FUMBO).

UTEGEMEZI huu unaongeza hali ya udharura. Palikuwepo na migawanyiko na makundi madogo madogo haya hayakuweza kuwa kitu kimoja. Kitu muhimu hapa ni mtizamo na matendo kuweza kuendeleza umoja uliowekwa katika Efe. 4:2-3.
Dhamira ya Paulo katika kanisa hili ni kuyatazamisha maombi ya Yesu yaliyoko katika Yohana 17:11,21-23, "kuwa waweze kuwa wamoja, kama tulivyo sisi." Huu pia ni msukumo wa Efe. 4:1-6. Umoja (sio ulinganifu) ni muhimu kwa ajili ya ustawi, makuzi, na agizo kuu la kanisa (k.v. Phil. 1:27). Ukosefu wa mshikamano unapelekea kuwepo na fikra finyu (cf. 2 Cor. 3:14; 4:4; 11:3).

▣ **"wala pasiwe kwenu faraka"** Neno hili (yaani, *schismata*) lilitumika katika lugha ya kawaida ya Koine juu ya vyama vidogo vya kisiasa (kama vile Matendo 14:4; 23:7). Tunapata neno la kiingereza "mfarakano," kutoka neno hili la Kiyunani. Hili lilikuwa mojawapo ya matatizo makuu ndani ya kanisa hili (kama vile 1 Kor. 11:18-19; 12:25). Makundi haya yalitokana na

1. Upendeleo binafsi wa waamini kwa ujuzi fulani wa kiuongozi (yaani, ujuzi wa kuongea)
2. Wivu na majivuno ya mwamini juu ya karama za rohoni
3. Utambuaji wa mwamini kuhusu tabaka za kiuchumi (yaani, matajiri na maskini)
4. Dhuluma ya mwamini kwenye ngazi ya kijamii (yaani, mtumwa na aliye huru)
5. kiburi cha kimbali cha mwamini (yaani, Myahudi na Mataifa)
6. majivuno au kiburi cha mwamini juu ya habari ya kuoa/kuolewa (yaani, mwenye ndoa na asiye na ndoa)
7. kiburi cha mwamini juu ya umahiri ki elimu (yaani, kundi la wasomi wa karne ya kwanza na wapotoshaji,)

Katika njia nyingi huu msisitizo kuhusu hali ya kujiona mkubwa kupindukia, kiburi, kung’ang’ania imani fulani, kuchagua kile unacho kipendelea unaelezea jinsi machafuko ya kimadhehebu katika kanisa la leo. Kila kundi linadai kuwa la kwanza likifuata viongozi wao wa kibinadamu (yaani, Luther, Calvin, Arminius, Wesley, n.k). kila kundi hudhani kwamba wao pekee ndio wanaakisi fikra za Mungu. Haswa, kuna hitaji linaloendelea la kumnyenyekea na kuwa tiyari kufundishika. Wale wengine wanaoendelea kuliita jina la Yesu wao ni Kanisa Lake!

◙ **" bali mhitimu katika nia moja na shauri moja"** Toleo la Today's English Version (TEV) tafsiri yake ina "mkiwa mmeungana kikamilifu, mkiwa na wazo moja na kusudi moja." Kusudi hilo ni ufalme wa Mungu, injili, agizo kuu, utakatifu wa kila mtu, sio kujipendelea kufanyaa uchaguzi wa upande mmoja, ama ajenda za binafsi!

**1:11 "nyumbani mwa Kloe"** Hatujui lolote kuhusu mwanamke huyu ila kwamba pengine alikuwa mshirika wa kanisa pale Korintho ama angalau wafanyakazi wake walikuwa washirika. Jina lake lilikuwa jina la utani la mungu wa kike wa Kloe Demetri. Watumishi wake ni chanzo kimoja cha Paulo cha kujua kuhusu matatizo ambayo yaliendelea kuwepo miongoni mwa makanisa ya nyumbani katika Korintho. Tazama utangulizi, VI. A.

◙ **"ya kwamba iko fitina kwenu"** Neno lile lile (yaani, *eris*) limeorodheshwa kwenye orodha nyingine za Paulo za dhambi Gal. 5:20, (kama vile 1 Kor. 3:3; 2 Kor. 12:20; 1 Tim. 6:4). Kamwe haipaswi kuwa kielelezo cha kanisa la Yesu Kristo!

**1:12** Hii inaonekana kuwa orodha ya vikundi vidogo vidogo (yaani, kundi la Paulo, Apollo, kundi la Petro na kundi la Yesu). Mengi yamekwisha kufanyika kuhusu tabia za viongozi (yaani, Paulo = chama cha uhuru ambacho kilijumuisha mataifa kwa imani pekee Apollos = chama cha wana falsafa; Wa-Kefa = wana mapokeo ya Kiyahudi ama chama cha washikiliaji mno wa sheria, kama vile 2 Kor. 11:18-33); wa - Kristo = wale wenye wadhifa maalum, wito, wenye karama au hali ya kuwa mtu wa Kiroho sana (kama vile 2 Kor. 12:1). Hata hivyo, hakuna habari ya hakika kwenye Agano Jipya kuhusu theolojia ama maisha ya kila kikundi. Viongozi hawa wenyewe hawakuwa na makundi.Hivi vikundi pale Korintho ndivyo vilidai kuwa wao ndiyo mabingwa wa kuanzisha vikundi.

◙ **"Apolo"** Huyu alikuwa mhubiri aliyekuwa msomi wa hali ya juu mwenye ufasaha katika kunena akitokea Alexandria, nchini Misri. Alikuwa pale Korintho (kama vile Matendo 18:24-19:1), Alikuwa mfano wa kiongozi ambaye kanisa hili lilivutwa kwake (kama vile 1 Kor. 16:12).

◙ **"Kefa"** Hili ni jina la Kiaramu ambalo ni sawa na jina la Kiyunani, Petro. Hakuna hakika kama Petro alifika Korintho. Kama sivyo, hii inaweza kuakisi "chama cha Kiyahudi" (kama vile Wagalatia na pengine 2 Wakorintho).

◙ **"Mimi ni wa Kristo"** Hakuna hakika kama huu ulikuwa mjibizo wa Paulo kwa waanzisha vikundi wenye kupenda uongozi ama kikundi kingine kilichodai kwamba Kristo ndiye kiongozi wao. Klement wa Rumi, aliyewaandikia Wakorintho katika mwaka 95 b.k (yaani, I Klem. 48) hataji chama cha Kristo, ingawa anataja makundi mengine ya vikundi hivyo hivyo. Hii inakubaliana na mtazamo kwamba hii ingeweza kuwa mshangao wa Paulo. Wanaweza kuchambua,kutambua na kufuata viongozi wa kibinadamu lakini yeye humwinua Kristo pekee na ni wa Kristo pekee!

Wasomi wengine wanadhani kwamba hili lingeweza kuwa kundi lililodai elimu maalum ya Yesu ama ufunuo maalum kutoka kwa Yesu ama uhusiano maalum kwa Yesu (yaani wasomi, aina ya vikundi vyenye mafunuo)Lakini tena, hili halina hakika na ni kisio tu. Kuna mengi sana tusio yajua kuhusu kanisa la karne ya kwanza na ya pili.

**1:13** Aya hii inaandika mjibizo wa kushutusha wa Paulo. "Je Yesu amekatwa katwa vipande?" Hii ni KAULI TIMILIFU TENDWA YENYE KUALIFU, ikidokeza Kristo amekuwa na anaendelea kugawanywa kwa mienendo na matendo ya hivi vikundi vidogo vidogo hapo Korintho.Kama hili ni swali, basi tarajia jibu la"ndiyo."

Machapisho ya kwenye mafunjo yaliyoandikwa mwaka 200's, B.K yana tofauti ya kimaandiko, "Kristo hawezi kugawanyika" (lakini mafunjo haya yamekwisha kuhahiribiwa na maandiko hayana uhakika). Miswada ya Kiyunani inayoaminika sana iliyo ya kale kuliko yote yenye herufi kubwa, א, A, B, C, D, F, na G, inafuta ile hasi na, hapo inatengeneza, (1) swali; (2) mshangao; au (3) maelezo. UBS[4] hutoa andiko fupi zaidi kipimo cha (bila hakika).

◙ **"Paulo alisulibiwa kwa ajili yenu? Au je! Mlibatizwa kwa jina la Paulo"** Hizi ni kauli za Paulo zenye msisitizo wa ukuu wa Kristo (yaani, akijishusha thamani mwenyewe) yawezekana akizielekeza kwa makundi haya

yanayoanzisha vikundi ama yumkini hata kundi lililoitwa kwa jina lake. Swali hili linatarajia jibu la “hapana".

**1:14 "Krispo"** Huyu ndiye aliyetajwa katika Matendo 18:8 ambaye alikuwa kiongozi wa sinagogi la Korintho aliyemkubali Kristo. Matendo 18:8 pia anatamka kwamba alibatizwa pamoja na nyumba yake (kama vile 1 Kor. 1:16). Yaonekana alifanya ubatizo huu wa "nyumbani" katika ulimwengu wa awali pale alipoamini dini pia. Hii kwa kawaida ilijumuisha watoto na watumishi kama walikuwepo kwa maelezo kamili tazama nukuu katika Matendo 16:5 kwenye mtandao www.freebiblecommentary.org.

◙ **"Gayo"** Mtu huyu aweza kuwa Yule aliyetajwa katika Rum. 16:23, ambaye nyumba yake kanisa la Korintho lilikutanika. Jina lake kamili la Kirumi lingekuwa Gaius Titus Justus.

**1:16 "Stefana"** Mtu huyu ametajwa katika 1 Kor. 16:15,17. Ni mmojawapo kwa wale wahusika watatu wa kanisa walioleta barua kutoka kwa Waefeso kwenda kwa Paulo. Utangulizi, VI. A.

**1:17 "Maana Kristo hakunituma ili nibatize, bali niihubiri"** Hii haimaanishi kushusha hadhi ya ubatizo bali kukabiri roho ya kusababisha vikundi katika kanisa la Korintho iliyokuwa inawainua viongozi Fulani. Hata hivyo kauli hii inaonesha kwamba ubatizo haukuonekana kama wakala wa "kisakramenti" wa neema. Inashangaza kwamba wengine hutafsiri maandiko ya Paulo katika mtazamo wa Sakramenti wakati katika maandiko yote anataja dhahiri meza ya Bwana mara moja tu katika 1 Kor. 11 na ubatizo mara mbili, katika Rum. 6:1-11 na Kol. 2:12. Kwa hali yoyote ubatizo ni mapenzi ya Mungu kwa kila aaminiye (Mt: 3:13-17)

1. ni agizo la Yesu (Mt. 28:28-10)
2. Ni kitu kinachotarajiwa, utaratibu wa kawaida kwa wote waaminio (Warumi 6; Matendo 2:38)

Siamini katika mtiririko wa kupokea neema ya Mungu ama Roho. Ilikuwa fursa ya watu wote kwa waaminio wapya kuweka wazi imani yao kwa njia ya hadhara na ya uchaguzi. Hakuna anayeamini Agano Jipya ambaye angeuliza "lazima nibatizwe ili niokoke? Yesu alifanya hivyo! Fanya hivyo.

## MADA MAALUM:UBATIZO (SPECIAL TOPIC: BAPTISM)

**NASB "sio kwa werevu wa kunena"**
**NKJV " si kwa hekima ya maneno"**
**NRSV "sio katika hekima ya ufasaha wa kusema"**
**TEV "bila kutumia hekima ya lugha ya binadamu"**
**NJB "sio kwa njia ya hekima ya lugha"**

Neno *sophia* (yaani, werevu au hekima) katika 1 Kor. 1:17-24 limetumika katika maelekezo ya mazingira (yaani, hekima ya ulimwengu, hekima ya kibinadamu, hekima iliyoanguka). Ufasaha wa kuzungumza wa kibinadamu na hekima haviwezi kuwa mbadala wa habari njema za Mungu zilizo katika kifo cha Yesu badala yetu. Nguvu imo ndani ya ujumbe, sio ndani ya mpeleka ujumbe (yaani, si hata ndani ya Paulo kama vile, 2 Kor. 10:10; 11:6). Kisehemu cha kanisa kilijipa kiburi katika ustadi wa elimu na ufasaha wa kusema katika (Tazama Bruce W. Winter, *Philo and Paul Among the Sophists*). 2 Wakolintho 10-13. Hakuna mwili utakaojitukuza mbele za Mungu (kama vile 1 Kor. 1:29; Efe. 2:9).

◙ **" msalaba wa Kristo usije ukabatilika"** Kama wanadamu wangeweza kujiokoa wenyewe kutokana na matendo yao ama akili, basi kifo cha Kristo kisingekuwa lazima! Lakini hawakuweza! Nguvu ya msalaba ni utoaji kamili wa Mungu kupitia Kristo. Kila jambo linalohitaji kufanyika kwa ajili ya ulimwengu wote kuokolewa limekamilika na linapatikana ndani ya maisha, mafundisho, kifo, ufufuo, kupaa mbingiuni na kurudi kwa Kristo ambako wanadamu wanaweza tu kuitikia kwa imani.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA):1 WAKORINTHO 1:26-31**
**18 Kwa sababu neno la msalaba kwao wanaopotea ni upuzi, bali kwetu sisi tunaookolewa ni nguvu ya Mungu. 19 Kwa kuwa imeandikwa, Nitaiharibu hekima yao wenye hekima, Na akili zao wenye akili nitazikataa. 20 Yu wapi mwenye hekima? Yu wapi mwandishi? Yu wapi mlete hoja wa zamani hizi? Je! Mungu hakuifanya hekima ya dunia kuwa ni upumbavu? 21 Kwa maana katika hekima ya Mungu, dunia isipopata kumjua Mungu kwa hekima yake, Mungu alipenda kuwaokoa waaminio kwa upuzi wa lile neno linalohubiriwa. 22 Kwa sababu Wayahudi wanataka ishara, na Wayunani wanatafuta hekima; 23 bali sisi tunamhubiri Kristo, aliyesulibiwa; kwa Wayahudi ni kikwazo, na kwa Wayunani ni upuzi; 24 bali kwao waitwao, Wayahudi kwa Wayunani, ni Kristo, nguvu ya Mungu, na hekima ya Mungu. 25 Kwa sababu upumbavu wa Mungu una hekima zaidi ya wanadamu, na udhaifu wa Mungu una nguvu zaidi ya wanadamu.**

**1:18 "neno la msalaba"** Hili "neno" (yaani, *logos*) linahusiana na maudhui wa mahubiri ya Paulo (kama vile 1 Kor. 1:17 na 23). Kwa kawaida kwenye mahubiri yake Paulo husisitiza kusulubishwa na ufufuo wa Kristo. Lakini kwenye muktadha anaelekeza kwenye kusulubishwa (kama vile Mwa. 3:15; Zaburi 22; Isaya 53; Zekaria 9-14) na matokeo yake (kama vile 1 Kor. 1:30).

**NASB, NKJV,**
**NRSV "upuzi"**
**TEV "ni upuzi"**
**NJB "tendo la ujinga"**

Neno la Kiyunani huja katika kiingereza kama "moron." Kama ndicho kigezo cha msingi kwenye ufafanuzi wa Paulo wa hekima ya mwanadamu iliyoanguka (kama vile 1 Kor. 1:18,21,23,25), pia tambua 2:14; 3:18-19; 4:10. Injili ni ufunuo (yaani, inayojifunua yenyewe) kutoka kwa Mungu, sio uvumbuzi wa binadamu!

◙ **"bali kwetu sisi tunaookolewa ni nguvu ya Mungu"** Kuna kauli mbili ENDELEVU ZA WAKATI ULIOPO. Ya kwanza ni KAULI YA KATI ENDELEVU YA WAKATI ULIOPO nay a pili ni KAULI TENDWA ENDELEVU YA WAKATI ULIOPO. Angalia MADA MAALUM: WOKOVU (NJEO ZA VITENZI VYA KIYUNANI) SPECIAL TOPIC: SALVATION (GREEK VERB TENSES) katika 1 Kor. 3:15. Kuna aina mbili za watu: wale wanaopotea na wale wanaookolewa (karama 2 Kor. 2:15; 4:3). Neno "potea"halimaanishi kuangamia kwa mwili, lakini ni kupoteza moja kwa moja ushirika na Mungu, kwa ule walioumbiwa kwao. Tazama mada maalumu katika 1 Kor. 1:28. Watafasiri wa kisasa wamechukua tafsida za Kiebrania na kuzifasihi. Mifano miwili ni:

1. "lala" = kifo, bila ufahamu hadi ufufuo
2. "potea" = kupotea kwa kiroho, sio kuteketea au kuangamia

Baadhi wanasema kupotea (yaani, kumalizika kwa uhai) ni kibinadamu zaidi kuliko moto wa milele (kama vile Fudge, *The Fire That consumes*). Tatizo linaibuka pale neno hilo hilo linalotumika kueleza moto wa milele linatumika mbinguni (yaani, "milele," kama vile Mt. 25:46) na ufufuo mara mbili kama katika Dan. 12:2; Yohana 5:28-20; na Matendo 24:15. Wala si Mungu awapelekaye watu motoni bali kukataa kwao wenyewe kwa (1) nuru walio nayo yaani (yaani, Zab. 19:1-6; Warumi 1-2) au (2) injili (yaani, dhambi isiyo sameheka na dhambi ya mauti ni dhambi ya kutokuamini). Kutokuamini katika maisha haya unaathiri umilele.

Agano Jipya huelezea wokovu kama

1. kitendo cha kuamua kuacha uasi uliopita (yaani, NJEO YA WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFU, Matendo 15:11; Rum. 8:24; 2 Tim. 1:9; Tito 3:5)
2. mchakato unaoendelea kwenye maisha (yaani, NJEO YA WAKATI ULIOPO, 1 Kor. 1:18; 15:2; 2 Kor. 2:15)
3. tukio lililopita linakuwaja kuwa kwenye hali ya uhalisia (yaani, NJEO YA WAKATI TIMILIFU Efe. 2:5,8)
4. ukamilishaji ujao (yaani, NJEO YA WAKATI UJAO, Rum. 5:9,10; 10:9; 13:11; 1 Kor. 3:15; Flp. 1:28; 1 Thes. 5:8-9; Hebr. 1:14; 9:28)

Hatari ya kitheolojia ni kutenga mojawapo ya hivi kama vitu vya lazima sana katika wokovu. Lazima kila wakati tuwe macho dhidi ya kujiaminisha kiurahisi kunakosisitiza kitendo cha mwanzoni tu ama ukamilifu ambayo unasisitiza uzaaji wa tunda pekee. Wokovu ni mwitikio wa hiari wa awali wa zawadi ya Mungu ya bure katika Kristo unaotoa mfanano wa Yesu kila siku. Sio tu mtu akaribishwaye, bali ujumbe kuhusu mtu Yule apokelewaye, na maisha ya mashindano ajaribuyo mtu huyo kuishi kwayo. Sio tunda, hati ya bima, au tiketi ya kwenda mbinguni, bali uhusiano wa kila siku unaokua pamoja na Yesu. Agano Jipya haliweki msisitizo wa kufanya maamuzi, bali kuwa mwanafunzi (kama vile Mt. 28:19-20).

Muujiza halisi ni kwamba injili inapohubiliwa wengine husema "ndiyo" na wanaokolewa, lakini wengine husema "hapana" na uasi wao unahakikishwa tena (kama vile Luka 2:34; Yohana 9:39; 1 Pet. 2:7). Hainishangazi kusikia watu kusema ndiyo, lakini nashangaa kwamba pamoja kwa

1. shauku ya Mungu watu wote wapate kuokolewa
2. kazi ya Kristo aliyokamilishwa
3. ubembelezi wa Roho Mtakatifu
4. hisia ya uovu wa binadamu
5. hali ya maisha ya kukosa matumaini bila Mungu

Kwamba watu waseme “hapana”! Haya ni maajabu ya uchaguzi (kama vile 2 Kor. 3:14; 4:4; 11:3).

◙ **"nguvu ya Mungu"** Injili ni uweza wa Mungu (kama 1 Kor. 1:24; Rum. 1:16). Injili inadhihirisha na kuelekeza nguvu ya Mungu. Inazaa imani,nazaa toba,inazaa hekima,haki utakaso, na ukombozi (kama 1 Kor. 1:30). Injili ya msalaba inazaa haya yote. Ni uweza wa Mungu nyuma ya neno lililoandikwa (yaani., Biblia), neno linaloishi (yaani., Kristo), neno linalohubiliwa (yaani, injili), na neno lililoasisiwa (yaani, kuwa kama Kristo

**1:19** Hii ni nukuu ya Isa. 29:14. Ni usawa wa wa Agano la Kale. Msisitizo upo kwenye ujinga wa hekima ya mwanadamu pasipo Mungu (kama vile Isa. 29:13; Mhu. 1:12-18; 12:12).

◙ **"NITAIHARIBU"** Hii ni sehemu ya nukuu ya Agano la Kale (yaani, Isa. 29:14).Angalia Mada Maalum: *Apollumi* katika 1 Kor. 8:11.

**1:20** Hii ni orodha ya mizanini ya kibinadamu (yaani, Wayahudi na Mataifa). Inaweza kuwa kidokezo kwa Isa. 33:18katika LXX (*Jerome Biblical Commentary*, uk. 257). Wanadamu hawawezi kuvumbua injili. Ni fumbo la Mungu lililofichwa toka vizazi (kama Efe. 2:11-3:13). Mpango wa Mungu na utoaji wake vinaonekanana ni upumbavu kwa sababu vinashusha heshima na hekima ya mwanadamu.

◙ **"wa zamani hizi. . .dunia"** Aya hizi mbili zinaaksi dhana inayofanana kwamba kipindi hiki cha wakati huu kimeanguka. Huu sio ulimwengu ambao Mungu alikusudia, Mungu alikusudia lakini injili itakibadili kizazi hiki kilichoanguka ili kiwe uumbaji uliokusudiwa na Mungu (yaani, Mwanzo 1-2 na Ufunuo 21-22).
Neno "ulimwengu"limetumika katika tafsiri mbili kwenye Agano Jipya: (1) sayari hii kama ilivyo (kama vile Yohana 3:16) na (2) jamii ya binadamu iliyoanguka inayojiongoza na kuishi tofauti na mapenzi ya Mungu (kama vile Yakobo 1:27; 4:4; 1 Yohana 2:15-17). Katika maandiko ya Paulo neno la Kiebrania *'olam*, limetafsiriwa kwenda Kiyunani kama *aiōn*, likiwa kisawe cha neno *kosmos* (kama vile 1 Kor. 1:20; 2:6; 3:19; Efe. 2:2). Neno *kosmos* angalia Mada Maalumu: Matumizi ya Paulo ya Neno *Kosmos* (ulimwengu) katika 1 Kor. 3:21b-22.

## MADA MAALUM:ENZI HII NA ENZI IJAYO (SPECIAL TOPIC: THIS AGE AND THE AGE TO COME)

◙ **"Mungu hakuifanya hekima ya dunia kuwa ni upumbavu?"** Maneno ya sarufi yanaonyesha kuwa Paulo anategemea jibu la "hapana."

**1:21 "Kwa maana katika hekima ya Mungu"** Hiki kinaweza kuwa kidokezo kwa Mith. 8:22-31, katika Yohana 1:1-5,9-14. Pia inahusu mpango wa Mungu kumkomboa mwanadamu aliyeanguka. Ukombozi ulipangwa moyoni mwa Mungu kabla ya uumbaji (kama vile Mt. 25:34; Matendo 2:23; 3:18; 4:28; 13:29; Efe. 1:4; 1 Pet. 1:19-20; Ufu. 13:8). Mpango huu ulihusu

1. Kujua kabla ya kuanguka kwa mwanadamu kutimiza mapenzi ya Mungu
2. Kutokuweza kwa mwanadamu kutimiza mapenzi ya Mungu (kama vile Kumb. 31:27-29; Jos. 24:19; Gal. 3)
3. Utoaji wa Mungu katika Kristo (yaani, the new covenant, kama vile Yer. 31:31-34)
4. Kuwaunganisha Wayahudi na mataifa kwa imani katika Kristo (kama vile 1 Kor. 1:21; Efe. 2:11-3:13)

## MADA MAALUM: MPANGO WA YWHW WA UKOMBOZI WA MILELE (SPECIAL TOPIC: YHWH's ETERNAL REDEMPTIVE PLAN)

▣ **"Asipopata kumjua Mungu"** Wayunani hawakuamini kuwa Mungu anajulikana.miungu yao ilikuwa na udhaifu wa kibinadamu na haikuhusiana na ulimwengu huu. Mwanadamu aliyeanguka hawezi kutambua Mungu, lakini Mungu amechagua kujidhihilisha Mwenyewe kupitia Kristo, (yaani., neno la uzima) na kupitia Biblia (yaani., Neno lililoandikwa), vile vile pia kupitia mwanadamu aliyekombolewa (yaani., Neno lililoanzishwa)!

▣ **"Mungu alipenda kuwaokoa waaminio kwa upuzi wa lile neno linalohubiriwa"** Sio uwasilishaji, lakini maudhui ya injili ambayo ni upuuzi kwa fikra zilizoanguka (k.v. 1 Cor. 2:14).

▣ **"Kuokoa wale wanaoamini"** Hii ni KAULI TENDAJI ISIO NA UKOMO YA WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFU ikifuatiwa na KAULI TENDAJI ENDELEVU YA WAKATI ULIOPO. Hili ndio dhumuni la kuitangaza injili! Neno "okoa" lilitumika katika Agano la Kale kwa ukombozi wa kimwili, lakini katika Agano Jipya likawa likitumika kwa ajili ya msamaha wa kiroho na ukubalifu. Ukubalifu wetu kwa Mungu kupitia Kristo ni ukweli uliotimilizwa, lakini kwa upande wetu ni mwendelezo wa ushirika wa kimaagano. Mambo yote kati ya mwanadamu na Mungu ni ya kimaagano. Siku zote Mungu huanzisha agano na kutengeneza mahitaji yake, lakini ameisha kuchagua kuwa binafsi lazima tuitikie na kuendelea kuitika. Tazama Mada Maalumu katika 1 Cor. 3:15.

**MADA MAALUMU: HITAJI LA USTAHIMILIVU (SPECIAL TOPIC: PERSEVERENCE)**

**1:22 "Wayahudi wanataka ishara"** Hii inaaksi ufahamu wake wa maisha ya Kristo (kama vile Mt. 12:38; 16:1,4; Marko 8:11-12; Yohana 4:48; 6:30).

◙ **"Wayunani wanatafuta hekima"** Neno"Wayunani" (*Hellēnes*) linarejea juu ya watu wote ambao si Wayahudi, hili linaonekana waziwazi katika matumizi yake Katika Matendo 18:16-21,32; Rum. 1:13.

**1:23** Aya hii inapaswa kuanza na KAULI YENYE KINYUME "lakini." Jawabu la Paulo kwa shauku ya yote mawili"ishara" na "hekima" ilikuwa injili.

◙ **"aliyesulibiwa"** Hii ni KAULI TIMILIFU TENDWA ENDELEVU. Kusulubiwa kwa Yesu sio mantiki wala miujiza, ni moyo wa injili ya Paulo. NJEO YA WAKATI TIMILIFU inadai kwamba Yesu atabaki kuwa "msulubiwa." Tutakapomwona Yesu mbinguni atakuwa amebakiza alama za kusulibiwa kwake (kama vile Yohana 20:25) kwa sababu zimekuwa vielelezo vya ushirika wake wa kusulibiwa vya heshima na utukufu. Yesu ni sehemu pekee ya Utatu ambao una mwili.
Hakika inawezekana kwamba NJEO YA WAKATI TIMILIFU ni WAKATI TIMILIFU ULIOTIMILIZWA ambao unatazama kwenye kukamilisha tukio ama kitendo, kikidokeza matokeo (kama vile Daner and Mantey, *A Manual Grammar of the Greek New Testament*, kur. 202-203). Yesu alisulibiwa kuweka muhuri wa wokovu wetu. Ulikuwa utimilifu wa Mwa. 3:15; Zaburi 22; Isaya 53; na Zek. 12:10. Masihi anayeteseka akawa mshituko wa kithiolojia kwa Wayahudi!
Angalia vyeo vya kimasihi vilivyotumiwa na watangazaji wa awali na wale waliokiri.

1. Yesu ndiye Kristo (Masihi) – Matendo 5:42; 9:22; 17:3; 18:5,28; 1 Kor. 1:23
2. Yesu ni Mwana wa Mungu – Matendo 9:20; Rum. 1:3-4
3. Yesu ni Bwana (akiaksi BWANA, YHWH) - Matendo 2:36; 10:36; 11:20; Rum. 10:9; 2 Kor. 4:5; Kol. 2:6

Hii ni mihtasari iliyotumika kuthibitisha mantiki ya Ukristo (tazama James D. G. Dunn, *Unity and Diversity in the NT*, kur. 34-63).

**NASB, NKJV,**
**NRSV "kikwazo"**
**TEV " kuvunja sheria"**
**NJB "kizuizi"**

Neno hili la Kiyunani (yaani, *skandalon*) lilitumika kwa chombo cha kufyatulia mtambo kwenye mtego wa mnyama (kama vile Gal. 5:11). Wayunani walimkataa Kristo kwa sababu ya dhana ya kufufuka (kama vile Kumb. 21:23). Walitarajia Mesiha kuwa kiongozi mshindi wa vita (na atakuwa siku akirudi!). Wayahudi hawakumtambua Masiha anayeteseka (kama vile Mwa. 3:15; Zaburi 22; Isa. 52:13-53:12) na hatua mbili zinazokuja (yaani., tendo la kubadilika kuwa mwanadamu na kurudi kwa utukufu).

**MADA MAALUM: MASIHI (SPECIAL TOPIC: MESSAIH)**

**NASB, NJB "na upumbavu wa Mataifa"**
**NKJV "kwa Wayunani ni upuzi"**

**NRSV "upumbavu kwa Mataifa"**
**TEV "upuzi wa Mataifa"**

Neno hili la Kiyunani (yaani, kwa sababu kwao mwili ndio chanzo cha uovu) halikuyafaa mawazo yao ya kifalsafa yaliyofikiliwa kwanza. Maelezo haya ya Paulo pia yanaonyesha kuwa mtarajiwa "mwokozi aliyekufa na kufufuka" wa ustawi wa makundi ya kimadhehebu na maajabu ya dini haukuwa mtizamo wa fikra za Wayahudi na hakika hakikuwa chanzo cha mtizamo wa Paulo kwa Yesu. uwe mwangalifu kuihukumu injili kwa namna ya utaifa au tamaduni zako!toleo la NKJV, likifuata upokeaji wa maandiko, lina "Kiyunani" kinachofuata machapisho sahihi ya herufi kubwa za Kiyunani $C^3$ na $D^c$. maandiko mengine yote ya Kiyunani yana "watu wa mataifa" (*ethnesiu*). Neno "Kiyunani" linaonekana katika 1 Cor. 1:22 and 24. Yumkini waandishi wa kale walibadili 1 Cor. 1:23 kulifanya kuwa la kutegemewa.
Kwa ajili ya neno "ujinga" angalia kumbukumbu kwenye 1 Cor. 1:25.

**1:24 "bali kwao waitwao"** Mwanzo wa 1 Wakorintho unasisitiza wito wa Mungu (yaani, kuchaguliwa) na neema ya Mungu kama msingi pekee kwa wokovu wa kanisa la Wakorintho (kama vile 1 Kor. 1:2,9,26,27; Efe. 1-2). Tunajifunza kutoka Yohana 6:44,65 kwamba hakuna anayekuja kwa Mungu mpaka Roho amvute yeye me/ke. Wito wa Mungu hauondoi ama kupunguza hitaji la mwitikio wa binadamu pale mwanzoni na kuendelea.

**MADA MAALUM: UCHAGUZI/MAJAALIWA NA HITAJI LA ULINGANIFU WA KITHIOLOJIA (SPECIAL TOPIC: ELECTION/ PREDESTINATION AND THE NEED FOR THEOLOGICAL BALANCE)**

◙ **"Wayahudi kwa Wayunani"** Hii inaonesha kusudi la injili ni kuwaunganisha binadamu wote katika Kristo. Hili ndilo fumbo lililofichwa tokea vizazi, bali sasa limefunuliwa waziwazi (kama vile Efe. 2:11-3:13).

◙ **"Kristo, nguvu ya Mungu, na hekima ya Mungu"** Aya ya kwanza inaweza kuhusu ufufuo wa Kristo kwa sababu ya kutumia "nguvu ya Mungu" katika Rum. 1:4.
Aya ya pili kipekee inahusu tatizo la kanisa la Korintho kusisitiza juu ya maarifa. Dhahili kwa vyovyote vile ingeweza kuwa marejeo ya Mith. 8:22-31 (yaani hekima ya uumbaji iliyowekwa kwenye mfano wa mwanadamu, kama vile 1 Kor. 8:6; Kol. 1:15-17; Ebr. 1:2).

**1:25 "upumbavu wa Mungu una hekima zaidi ya wanadamu"** Hii ni dhamira ya Agano la Kale (kama vile Isa. 55:8-9). Imerejewa katika 1 Kor. 1:18,21,23. Hili ni neno *mōros*. Lenyewe na kwa namna nyingine linatumiwa mara nyingi na Paulo kwenye nyaraka zake za Wakorintho Tazama Mada Maalum katika 1 Kor. 15:36.

1. *mōros* (mpumbavu), 1 Kor. 1:25,27; 3:18; 4:10
2. *mōria* (upumbavu), 1 Kor. 1:18,21,23; 2:14; 3:19
3. *mopainō* (fanywa mpumbavu), 1 Kor. 1:20

◙ **" na udhaifu wa Mungu una nguvu zaidi ya wanadamu"** Hii kimsingi ni kuthibitisha ukuu wa Mungu usio na kifani Yeye amekuzwa kwa njia ya udhaifu wa binadamu. (kama vile 1 Kor. 12:5,7-10). Inaweza kuhusu kule kuonekana kushindwa kwa kifo cha Yesu kutokana na mtazamo wa "kibinadamu" (kama vile 2 Kor. 13:4), bado katika uhalisia ulikuwa ushindi wa matokeo ya milele!
Injili, ushindi, wote ni wa Mungu na si wa mwanadamu angalia Mada Maalum: udhaifu katika 2 Kor. 12:9.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA):1 WAKORINTHO 1:26-31**

**26 Maana, ndugu zangu, angalieni mwito wenu, ya kwamba si wengi wenye hekima ya mwilini, si wengi wenye nguvu, si wengi wenye cheo walioitwa; 27 bali Mungu aliyachagua mambo mapumbavu ya dunia awaaibishe wenye hekima; tena Mungu alivichagua vitu dhaifu vya dunia ili aviaibishe vyenye nguvu; 28 tena Mungu alivichagua vitu vinyonge vya dunia na vilivyodharauliwa, naam, vitu ambavyo haviko, ili avibatilishe vile vilivyoko; 29 mwenye mwili awaye yote asije akajisifu mbele za Mungu. 30 Bali kwa yeye ninyi mmepata kuwa katika Kristo Yesu, aliyefanywa kwetu hekima itokayo kwa Mungu, na haki, na utakatifu, na ukombozi; 31 kusudi, kama ilivyoandikwa, Yeye aonaye fahari na aone fahari juu ya Bwana.**

**1:26-31** Aya hii ya mwisho ya sura ya kwanza yatuonesha uhusiano wa “hekima” na “maarifa” uliojaa wasi wasi unapohusishwa na injili. Kwa maana moja ni "mbaya," na kwa maana nyingine ni "nzuri." Hebu ninukuu aya ya ajabu kutoka Herman Ridderbos' *Paul, An Outline of His Theology*:

> "Kusema kweli,uhusiano wa imani na maarifa, *pistis* and *gnosis*, kama ilivyo imani na matendo, havina uhakika.kwa upande mmoja maarifa husimama kwenye njia ya imani, yaani kama vile, matendo mema kwa Wayahudi, kuwakilisha mapenzi ya Wanadamu kwa ukombozi binafsi. Namna hii kinzani inavyoendelea ndani ya Wagalatia na Warumi 1 kuhusiana na matendo, tishio hili kwenye imani ya Mkristo toka upande wa *gnosis* imewekwa wazi hasa katika 1 Wakorintho (yaani, mf, 1 Kor. 1:26-29). Na hatari hii ilidumu sio tu kutoka upande wa kile ambacho Paulo hukiita "Hekima ya ulimwengu" (1 Kor. 1:21), bali pia kutoka kwenye aina maalum ya *gnosis* ya Kikristo. Paulo anatambua kwamba *gnosis* ndani ya hiyo: twajua kwamba sote tunayo maarifa (1 Kor. 8:1). Lakini ghafla anaongeza katika hilo: maarifa huleta majivuno, upendo hujenga. Kilicho swala hapa ni *gnosis*, ya kikristo ilivyotumiwa kwa makosa, inavyojiinua; juu ya jirani wa mtu, walio dhaifu.Maarifa ambayo kwa uhakika yako kwenye huduma ya uhuru wa mtu binafsi, lakini ile isiyolijenga kanisa. Hii *gnosis* pekee huongeza kiburi cha ubinafsi na husimama kinyume na upendo. Kwa jinsi hiyo inajeruhi na haina faida (1 Kor. 13:2,3)" uk . 242.

**1:26**
**NASB, NRSV,**
**NJB "fikilia"**
**NKJV "angalia"**
**TEV "kumbuka"**

Hii ni aidha KAULI TENDAJI SHURUTISHI WA WAKATI ULIOPO au KAULI TENDAJI YENYE KUARIFU YA WAKATI ULIOPO. Moffatt anatafasiri hiyo kama, "tazama kiwango chako mwenyewe." Aya hii haikukusudiwa kuwa kitu cha kukatisha tamaa kwa kanisa la awali kwa uongozi wake, bali uthibitisho wa upendo na nguvu ya Mungu. Ilimaanisha kuvunjavunja kiburi cha kanisa. Hili lenye kiburi kilichopitiliza. Kanisa la awali lilijawa na hasa jamii ya “wasio navyo". Hata hivyo, inaonekana mojawapo ya vikundi vidogo pale Korintho vilitokana na watu maarufu wa kirumi ambao kiutamaduni walikuwa wenye heshima. Kwa kuwatumia hawa ambao hawakuwa na hadhi ya kidunia, Mungu hukuza uweza wake.

◙ "**sio wengi wenye hekima ya kimwili"** Hii inahusu hekima ya kibinadamu ama viwango vya kiulimwengu (kama vile 1 Kor. 1:20; 2:6,8; 3:18).

## MADA MAALUM: MWILI (*sarx*) (SPECIAL TOPIC: BODY (*sarx*)

◙ **"si wengi wenye nguvu"** Hii inahusu nguvu za kimwili ama hadhi nafasi ama cheo.

◙ **"si wengi wenye hekima"** Hii inahusu msingi wa familia ya mtu binafsi ambayo ingehusisha utajiri, elimu, na fursa za kijamii. Hizi sifa tatu zinaoana sana na wapotoshaji ambao walijivunia sana elimu zao, vyeo na ustaharabu wa kisasa wa wakati ule.

**1:27 "Mungu aliyachagua mambo mapumbavu ya dunia"** Hii ni KAULI YA KATI YENYE KUARIFU YA WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFU. Mungu mwenyewe amechagua kudhihirisha nguvu yake kupitia wanyonge ili kwamba pasiwe na mashaka ya nani atakayepokea utukufu (kama vile 2 Wakolintho 12). Ushindi umo ndani ya rasilimali ya Mungu sio mafanikio ya binadamu (kama vile 1 Kor. 1:29; Efe 2:9) au hadhi kijamii kwa “wapumbavu” tazama maelezo katika.1 Kor. 1:25. Ya "kidunia" angalia Mada Maalum katika 1 Kor. 3:21b-22.

**1:28**
**NASB "vitu vinyonge vya dunia na vilivyodharauliwa"**

**NKJV " vitu vinyonge vya dunia na vilivyodharauliwa"**
**NRSV "kile kilicho chini na kinachodharauliwa ulimwenguni"**
**TEV "kile ambacho ulimwengu hukishusha na kukidharau"**
**NJB "wale ambao kwa viwango vya kibinadamu ni wa kawaida wenye kustahili kutokuthaminiwa"**

Aya hii inalingana na "wenye hekima…..wenye nguvu…..wenye hadhi" katika 1 Kor. 1:26. Neno "hali ya chini" kiuhalisia ni "wale wenye uzao hali ya chini," ambayo ni rejeo jingine kwa ukuu wa Warumi.

**NASB, NRSV "mambo yasiyokuwepo"**
**NKJV "vitu visivyokuwepo"**
**TEV "vitu si kitu"**
**NJB "wale wasio thaminika"**

Je hili ni kundi jingine la mambo/watu wa chini ama muhtasari? Kwasababu hakuna *kai* (yaani, na; MSS P[46], א[*], A, C[*], D, F, G) kabla ya aya hii kama ilivyo kwenye nyingine zote, pengine ni taarifa ya muhtasari. Mungu huita na kutumia watu ambao ulimwengu hauna habari nao! Vigezo vya kitheolojia ni

1. "hakuna mwenye mwili atakayejisifu mbele za Mungu" (kama vile 1 Kor. 1:29)
2. Nguvu ya Mungu na uandaaji wake unatukuzwa katika udhaifu wa vyombo vya kibinadamu (kama vile 2 Kor. 12:1-10)
3. Upatanisho wa Kristo unatukuzwa (kama vile. 1 Kor. 1:30)

Katika yeye, kila kitu ambacho Wayahudi na Wayunani walikitafuta na kukihangaikia ni kipawa kutoka kwa YHWH, kwa njia ya Masihi, ikitiwa nguvu na roho mtakatifu!

◙ "**avibatilishe vile vilivyoko**" Hili ni neno la Kiyunani, *katargeō*. Angalia nukuu katika 1 Kor. 1:18 na Mada Maalumu ifuatayo.

## MADA MAALUM: ISIYO KWELI NA TUPU (*KATARGEŌ*) (SPECIAL TOPIC: NULL AND VOID (*KATARGEŌ*)

**1:29 "mwenye mwili awaye yote asije akajisifu mbele za Mungu"** Kitenzi ni KAULI YA KATI TEGEMEZI YA WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFU inayomaanisha uchaguzi binafsi uliokwisha kamilishwa. Hakuna kiumbe chochote chenye mwili kitakachojivuna mbele ya muumbaji (kama vile Efe. 2:9)! Huu ndio ulikuwa ukweli mkuu wa ujumbe wa Paulo kwa Wakorintho wenye kiburi na kwa binadamu aliye anguka kwa ujumla, Myahudi na Mataifa (kama vile Rum. 3:27; Efe. 2:9). Angalia **MADA MAALUM: MAJIVUNO (SPECIAL TOPIC: BOASTING)** katka 1 Kor. 5:6.

◙ **"mwanadamu"** Neno hili kwa uhalisia "mwili." Angalia Mada Maalum katika 1 Kor. 1:26.

**1:30**
**NASB "kwa kufanya kwake"**
**NKJV "wa yeye"**
**NRSV "Yeye ndiye chanzo"**
**TEV "Mungu"**
**NJB "kwa yeye"**

Hili kwa uhalisia ni neno "kutoka ndani yake," ambayo ni lahaja ya Kiyunani ikielezea msababishi wa kwanza, Msogezaji Mkuu. Baba alikitumia, Yesu akakileta na Roho akakitia nguvu. Kinachofuata ni orodha ya vipawa wa Mungu kwa waaminio kwa njia ya Kristo.

◙ "**hekima itokayo kwa Mungu**"Katika fikra za Kiyahudi hekima inafanya kuwa kama binadamu katika Mithali 8:22-31 na Kol. 2:2-3. Hekima ni mtu. Kweli ni mtu. Injili ni mtu-Yesu! (kama vile Yohana 14:6).

Ikiwa kwa vyovyote, Paulo alikuwa anawaeleza vitu vya msingi kifalsafa ndani ya kanisa, basi *sophia* angekuwa na ushirika na kiburi chao kwenye desturi za utamaduni wao (yaani, Plato, Socrates, Aristotle, n.k). Ingekuwa kutoka shule ya masomo maalum. Inawezekana pia kwamba upokeaji wa mafunuo ya uongo yalikuwepo kwenye mazingira yasiyofuata mfumo wa kidini wa Korintho na inawezekana yalikuwa yamekwisha kupenya ndani ya kanisa (kama vile 1 Kor. 1:18-2:8; 3:18-23; 8:1-2). Kama ndivyo basi ushauri wa Paulo katika Wakolosai unahusika (yaani, Kristo, Mwenyewe, ni hekima, kama vile Kol. 1:9; 2:3).
Nadhani maneno yote haya yanahusiana na kile ambacho Kristo amekifanya kwa waamini kwa njia ya Yesu.

1. Yeye ni hekima ya Mungu kwetu
2. Yeye ni haki ya Mungu kwetu
3. Yeye ni utakaso wa Mungu kwetu
4. Yeye ni ukombozi wa Mungu kwetu

Yote ni ya Mungu Baba kwa njia ya Mwana.

◙ "**haki**" Hii ni sitiari kutoka mahakama ya sheria (kama vile Rum. 3:21-26; 2 Kor. 5:21). Katika siku za Paulo waalimu wa sheria za Kiyahudi walikwisha hamisha kiasi binafsi cha hekima ya Mithali 8 kwenda kwenye sheria za Mungu. Kama Paulo alikuwa anafikiri kuhusu msingi wa Kiyahudi ndani ya kanisa la Korintho, lilikuwa jina lenye nguvu na la mwisho.

**MADA MAALUM: HAKI (SPECIAL TOPIC: RIGHTEOUSNESS)**

◙ **"utakatifu"** Hii ilikuwa sitiari kutoka kwenye mfumo wa kidhabihu wa Israel (kama vile Rum. 6:19-23). Hii ni kutoka kwenye mzizi wa neno "takatifu" au "kilichowakifishwa." Katika Agano la Kale ilihusu mtu, mahali, ama kitu kilichokuwa kimetengwa kwa ajili ya kutumika kwa kazi ya Mungu. Kitheolojia yahusu nafasi ya aaminiye ndani ya Kristo. Mara mtu anapo weka imani ndani yake, anahesabiwa kuwa kwenye haki na anatakaswa (kama vile Rum. 8:30). Angalia Mada Maalum katika 1 Kor. 1:2.

◙ "**ukombozi**" Hii inamaanisha "kurejesha" (kama vile Rum. 3:24). Hii ilikuwa sitiari kutoka kwenye soko la watumwa ndiyo dhana kuu ya wokovu katika Agano la Kale.

**MADA MAALUM: FIDIA/UKOMBOZI (SPECIAL TOPIC: RANSOM/REDEEM)**

**1:31** Hii ni nukuu kutoka Yer. 9:23-24. Paulo anarudia nukuu hii katika 2 Kor. 10:17. "Bwana"katika aya ya Yeremia inahusu YHWH, lakini hapa ni kwa Yesu! Hii ni namna ya kawaida ya Agano Jipya kuthibitisha Uungu wa Kristo.
Hatujivuni ndani ya nafsi zetu bali kwa yeye ambaye ndani yake ukamilifu wote wa Mungu wakaa kimwili! Nukuu hizi mbili za Yeremia zaonesha umoja kati ya 1 Wakolintho 1-4 na 2 Wakolintho 10-13. Wapinzani ni wapotoshaji wa Kiyahudi waliojigamba kuhusu elimu yao ya ujuzi ya kusema kwa mtindo wao huo (kama vile Bruce W. Winter, *Philo and Paul Among the Sophists).*

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa usomaji wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako binafsi ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika nuru tuliyonayo. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hupaswi kumwachia kazi hii mfasiri.

Maswali haya ya kujadili yanatolewa kukusaidia mambo muhimu ya kipengele cha kitabu hiki. Yamekusudiwa kukuchokonoa mawazo na sio ya mwisho.

1. Kwanini wito wa Mungu umesisitizwa mara nyingi sana na Paulo?
2. Mungu anawezaje kuwaita watu wenye dhambi "watakatifu"?
3. Karama za kiroho zina kusudi gani katika kanisa?
4. Kwanini kanisa la Korintho lilikuwa na vikundi vingi ndani ya kanisa lote?
5. 1 Kor. 1:12 Inahusishwaje na madhehebu ya kisasa?

6. Je Paulo anashusha hadhi ya ubatizo katika 1 Kor. 1:17?
7. Kwanini Wayahudi walikataa injili?
8. Kwanini Wayunani walikataa injili?
9. Kwanini Mungu amekubali kutumia watu dhaifu wasio na sifa kubwa kijamii ama kielimu kusambaza injili?

# 1 WAKORINTHO 2

| MGAWANYO WA AYA WA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **UBS[4]** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB** |
| Kumtangaaza Kristo Aliyesulibiwa | Kristo Aliyesulibiwa | Kristo Aliyesulibiwa | Habari Kuhusu Kristo alipokuwa Msalabani | Hekima ya Kweli na ile ya Uongo (1:17-3:4) |
| 2:1-5 | 2:1-5 | 2:1-5 | 2:1-5 | 2:1-5 |
| Ufunuo Utokanao na Roho wa Mungu | Hekima ya Kiroho | Hekima ya Koroho | Hekima ya Mungu | |
| 2:6-16 | 2:6-16 | 2:6-13 | 2:6-12 | 2:6-9 |
| | | | | 2:10-16 |
| | | | 2:13-16 | |
| | | 2:14-16 | | |

**MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI** (Kutoka "**Mwongozo wa Usomaji Mzuri wa Biblia" (A Guide to Good Bible Reading)**

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Haya ni maoni ya mwongozo kwa kujisomea, ikiwa na maana kuwa unawajibika binafsi kwa tafsiri ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mtoa maoni tu.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

5. Aya ya kwanza
6. Aya ya pili
7. Aya tatu
8. N.k

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA KWA 1 WAKORINTHO 2:1-16

A. Kulikuwa na baadhi ya watu katika kanisa la Korintho waliokuwa na muelekeo wa akili sana (yaani, mila za kistiari za karne ya kwanza). Katika muktadha huu wa msisitizo mkubwa wa ujuzi wa mwanadamu na utendaji, Katika Sura ya 1 Paulo alianza na msisitizo kuhusiana na neema ya Mungu ( kama alivyofanya pia katika Efe. 2:1-10). Bado, alikubali kwamba hekima na ujuzi pia ni miongoni mwa vipawa vya Mungu. Katika Sura ya 2, Paulo aliendelea katika dhamira hii kwenye dhaminra hii kwa kusisitiza ufunuo dhidi ya ugunduzi wa mwanadamu. Wao kama Wakorintho hawakuwa na madai juu ya ujuzi walionao, kwa usawa wao hawakuwa na madai juu ya upatikanaji wa ujuzi huo.
B. Kimsingi, 1 Kor. 2:1-16 ni kichocheo cha Sura ya 1 Kor. 1:18-25.

C. Mistari ya 10-16 inaweza kueleweka kama yenye kurejelea katika baadhi ya vipengele vya ndani vya kiroho au ufunuo. Mungu alifanya hivyo ili kujifunua Mwenyewe kwetu ( yaani, ufunuo, 1 Kor. 2:10-12); Amechagua watu fulani kuandika na kuelezea matendo yake (yaani, uvuvio, juzuu. 13), na mwisho Roho huwawezesha wasomaji wa Biblia kuielewa kweli iliyo kuu ya ufunuo wake (yaani, mwangaza, 1 Kor. 2:14-16).

**MADA MAALUMU: NURU ( SPECIAL TOPIC: ILLUMINATION)**

**MADA MAALUMU: UVUVIO (SPECIAL TOPIC: INSPIRATION)**

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 1 WAKORINTHO 2:1-5**
**[1]Basi, ndugu zangu, mimi nilipokuja kwenu, sikuja niwahubiri siri ya Mungu kwa ufasaha wa maneno, wala kwa hekima. [2]Maana naliazimu nisijue neno lo lote kwenu ila Yesu Kristo, naye amesulibiwa. [3]Nami nalikuwako kwenu katika hali ya udhaifu na hofu na matetemeko mengi. [4]Na neno langu na kuhubiri kwangu hakukuwa kwa maneno ya hekima yenye kushawishi akili za watu, bali kwa dalili za Roho na za nguvu, [5]ili imani yenu isiwe katika hekima ya wanadamu, bali katika nguvu za Mungu.**

**2:1 "ndugu zangu"** Haya maelezo yanayowahusu wale waaminio yametumiwa na Paulo mara kwa mara, kwa ufahamu au akili iliyofichika, ili kuonyesha hatua inayofuata katika uwasilishaji wa kweli au uwasilishaji wa ukweli mpya (kama vile 1 Kor. 2:1; 3:1; 4:6; 7:24; 10:1; 11:33; 12:1; 14:6, 20, 35; 15:1, 31, 50, 58; 16:15). Neno lingemaanisha waume na wake wa kanisa la Korintho.

**NASB "sikuja niwahubiri siri ya Mungu kwa ufasaha wa maneno,wala kwa hekima"**
**NKJV "sikuja kwa uzuri wa kauli hekima"**
**NRSV "sikuja kutangaza…kwa maneno ya juu au hekima"**
**TEV "sikuja na maneno marefu na mafundisho makubwa"**
**NJB "sikuja na uzuri wo wote wa maelezo au hoja ya hekima "**

Paulo anaonyesha tofauti yake mwenyewe (yaani, Paulo huko Korintho, kama vile Matendo 18:1-18) na uongo wa wale wanaosisitiza sana juu ya ujuzi na sitiari za baadhi ya Wakoritho ambao baadaye walikuja kuwa viongozi wa kanisa. Apolo, si Paulo, alikuwa mwana-stiari aliyeng'arishwa ambapo wao walimtaka Paulo kuiga mtindo wake wa kuzungumza na makusanyiko (angalia Bruce W. Winter, *Philo and Paul Among the Sophists*. Kwa "Ubora" (*huperochē*) angalia Mada Maalumu ifuatayo.

**MADA MAALUMU: MATUMIZI YA PAULO YA NENO *HUPER* (SPECIAL TOPIC: PAUL'S USE OF *HUPER* COMPOUNDS)**

**NASB, NKJV "siri ya Mungu"**
**NRSV, NJB "siri ya ujumbe wa Mungu"**
**TEV "siri ya ukweli wa Mungu"**

Kuna Tofauti ya machapisho ya Kiyunani hapa. Neno la Kiyunani *musterion* (siri) linaonekana katika MSS $P^{46}$, א*, A, na C. Neno *marturion* (ushuhuda) linaonekna katika Machapisho ya kale א$^2$, B, C, D. Ikiwa ni "siri," dhana hii inaelezewa katika 1 Kor. 2:7; Efe. 2:11-3:13; na Kol. 1:26-27, ambayo ni umoja wa Wayahudi na Wayunani kupitia Kristo ndani ya familia moja (yaani, kanisa. Ikiwa ni "siri," inaunganisha 1:6, ambayo ingekuwa na maana zinazofanana na "injili." $UBS^4$ inatoa dalaja B la neno "muujiza" (yaani, karibu na hakika).

Neno "siri" lilitumika mara nyingi katika mafunjo ya lugha ya Koine ya karne ya kwanza iliyopatikana Misri huku ikirejea kwa kuanza upya ujuzi wa siri unaopatikana pekee kwa kundi maalumu (yaani, siri ya dini). Paulo analichukua neno hili la kiufundi na kulitumia katika uhusiano na wale ambao wana Roho (yaani, waaminio) na

wale ambao hawana. Hakuna tofauti katika hatua hii katika uwasilisho wa Paulo kati ya waaminio (kama vile1 Kor. 3:1). Yote yatazingatiwa "wenye kupevuka" (kama vile 1 Kor. 2:6).

**MADA MAALUMU: FUMBO (SPECIAL TOPIC: MYSTERY)**

**2:2 "mimi"** Katika mstari wa 1-5 Paulo anaonekana kujilinganisha mwenyewe na

1. uwasilishaji wake wa nyuma wa injili huko Ethene ambako alitimua mantiki ya Kiyunani, hata aliwanukuu washairi wao (yaani, kwanza ilipendekezwa na Origen, kama vile Mdo. 17:16-34)
2. uwasilishaji wake wa injili dhidi ya wale katika Korintho ambao waliongea kwa hekima ya binadamu na sitiari za binadamu kuhusu mambo ya Kiroho

◙ **"Yesu Kristo, naye amesulibiwa"** Hii ni KAULI TENDWA ENDELEVU YA WAKATI TIMILIFU (kama vile 1 Kor. 1:23). Kuna vipengele viwili vya kitheolojia vilivyofunuliwa katika NJEO ENDELEVU hii:

1. WAKATI TIMILIFU unafunua kwamba Yesu alibaki kuwa aliyesulubiwa. Pale tutakapo muona, bado atakuwa na makovu. Imekuwa ishara ya utukufu (angalia maelezo katika 1 Kor. 1:23).
2. IRABU TENDWA inafunua kwamba kifo cha Yesu kilikuwa
   a. kwa ushirika/uwakala wa Baba na Mpango wake wa milele (kama vile Mdo. 2:23; 3:18; 4:28; 13:29) kwa ukombozi (kama vile Isa. 53:10)
   b. kwa dhambi za binadamu na uasi wa kudai dhabihu (kama vile Rum. 5:14-15,18-19)
   Ujumbe kuhusu kifo cha Kristo kwa niaba ya Mwanadamu ni ujumbe wa kati wa theolojia ya Paulo. Dhana ya kuteseka na Kufa kwa Masihi ilikuwa mila ya kigeni kwa mawazo ya Wayahudi. Kipengele hiki cha injili lazima mwanzo kilimsumbua Paulo. Ni jinsi gani mtiwa mafuta wa YHWH angewaza kulaaniwa na Mungu (kama vile Kum. 21:23). Bado, hii ilikuwa sehemu ya ufunuo wa Agano la Kale (kama vile Mwa. 3:15; Zaburi 22; Isaya 53; Zek. 12:10). Yesu, Mwana wa Mungu asiye na dhambi, alikufa kwa nafasi yetu (kama vile Rum. 5:18-19; 2 Kor. 5:21). Yeye alikuwa laana kwa ajili yetu (kama vile Gal. 3:13). Kristo alisulIbiwa kwa wote ni siri ya Mungu iliyofichika (kama vile Kol. 1:26-28; 2:2-4).

**2:3 "Nami nalikuwako kwenu katika hali ya udhaifu na hofu na matetemeko mengi"** Hii inaweza kuwa kidokezo toka kwenye Kut. 15:16 katika maandiko ya kale ya Kiyunani (LXX). Paulo anatuonyesha upungufu wake.

1. alikuwa na hofu kwa sababu ya utendaji wake mbaya huko Filipi, Thessalonika, na Berea (kama vile Mdo. 16-17)
2. alikatishwa tamaa katika matokeo na labda mbinu zake alizotumia katika Ethene (yaani, mtazamo wa Origen kutoka Mdo. 17:22-34)
3. matatizo yake ya mwili, labda shida ya jicho, kulimsababishia shida kubwa (kama vile 2 Kor. 12:7-9)
4. Ukosefu wa Paulo wa imani na kukata tamaa wakati akiwa Korintho

Kristo alimtokea Paulo mara kadhaa kwa kumuhimiza/kumtia moyo (kama vile Mdo. 18:9-10;23:11;27:23). Maneno yake na hali ya mwili wake sio vilivyowabadilisha watu kuwa na imani katika Kristo, lakini kusihi kwa injili na nguvu ya Roho (kama vile 1 Kor. 2:4; 1:17; 2 Kor. 10:10). Ni yenye msaada kwangu kama mchungaji wa Yesu Kristo kutambua

1. Yesu alikuwa na muda wake mwenyewe wa kukata tamaa (yaani, Gethsemane)
2. Mitume mara nyingi hawakuweza kuelewa kimamilifu mafundisho ya Yesu
3. Paulo alihisi kuwa na hofu na Mdhaifu.
   Lazima daima tukiri udhaifu wa mwili pia nguvu kubwa ya injili na uwepo wa Roho! Tabia ya Mungu na utoaji wake umekuzwa kupitia udhaifu wa binadamu (kama vile 1 Kor. 1:26-29; 2 Kor. 12).
   Udhaifu wa Paulo ni wa mambo haya kwamba walimu wa uongo katika 2 Kor . 10-13 walimshambulia Paulo. Walikuza uwezo wao (yaani, Elimu, nafasi katika jamii, waliojaliwa kiroho, ujuzi wa kuzungumza). Inavyoonekana maandiko ya Paulo yalikuwa yameundwa kwa ufasaha zaidi (yaani, 2 Kor. 10-13) na yenye nguvu zaidi ya ujumbe wake wa mdomo. Angalia MADA MAALUMU: UDHAIFU (SPECIAL TOPIC: WEAKNESS) katika 2 Kor. 12:9.

**2:4**
**NASB "hakukuwa na maneno ya hekima"**
**NKJV "sio na maneno ya kuvutia ya hekima ya mwanadamu"**
**NRSV "sikuyatoa kwamaneno ya kuvutia na ya hekima"**
**TEV "hayakufika na maneno ya ujuzi wa hekima ya mwanadamu"**
**NJB "hayakumanisha kushawishi kwa hoja za kifalsafa"**

Kuna mfanano mwingi wa kifungu hiki katika mswada wa Kiyunani.

1. Tatizo la kwanza linahusisha KIVUMISHI adimu *peithois* (kama vile MSS $P^{46}$, א, A, B, C, D), ambacho hakipatikani kwingine kokote katika Maandiko ya Agano la Kale, mafunjo ya lugha ya Koine, au Agano Jipya.
2. Baadhi walidhani utofauti ulisababishwa na waandishi ambao walikua wageni na KIVUMISHI hiki. Wanaweza kuwa wamebadilisha kidogo mfumo wake kwa *peithoi*, ambao unamaanisha "ushawishi."
3. Baadhi ya miswada ya Kiyunani imeongeza "ushawishi wa wanaume" (kama vile 1 Kor. 2:13 na MSS א [2], A, C).
4. Katika baadhi ya miswada neno "maneno" " (yaani., *logois* au *logos*) hayapo (kama vile MSS $P^{46}$, F, G na maandishi ya Kiyunani yaliyotumiwa na Chrysostom).

Inaonekana bora kutoka mazingira ya jumla kuunganisha kifungu hiki na Kukataa kwa Paulo kwa ufasaha wa binadamu, mantiki, na hekima (kama vile 1 Kor. 1:17; 2:1,13). Hata hivyo, maana kamili ya neno *peithois* inabaki isiyojulikana (angalia NIDNTT, juzuu. 1, kr. 588-593).

◙ **"bali kwa dalili za Roho na za nguvu"** Hii inarejea kwa kubabilishwa maisha ya Wakoritho waongofu. Na pia inaweza kuhusishwa na uwepo wa ishara zilizothibitisha kwamba mara nyingi walihudhuria mahubiri ya Paulo ya injili (kama vile Mdo. 13:11; 14:10; 16:18,28; 19:11-12; 20:10). Angalia maelezo kwenye herufi kubwa au herufi ndogo "r" Roho katika 1 Kor. 2:11.

**2:5** Kwa Paulo, tumaini pekee la mwanadamu lilikuwa katika neema ya Baba, kazi iliyomalizwa na Mwana, na nguvu ya Roho. Katika maneno mengine, Mungu mwenyewe ndiye msingi pekee wa kweli kwa wokovu. Ufunuo wa Mungu, sio ugunduzi wa mwanadamu; hekima ya Mungu, sio lugha ya kushawishi ya mwanadamu au mantiki, ni chanzo pekee cha imani.

Kwa Paulo, Injili ya Mungu na mwanadamu aliyeanguka ni majibu ya kufahamu Agano (yaani, toba, imani, utii, na uvumilivu) ni ufunguo wa maisha ya milele

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 1 WAKORINTHO 2:6-13**
**6 Walakini iko hekima tusemayo kati ya wakamilifu; ila si hekima ya dunia hii, wala ya hao wanaoitawala dunia hii, wanaobatilika; 7bali twanena hekima ya Mungu katika siri, ile hekima iliyofichwa, ambayo Mungu aliiazimu tangu milele, kwa utukufu wetu; 8 ambayo wenye kuitawala dunia hii hawaijui hata mmoja; maana kama wangaliijua, wasingalimsulibisha Bwana wa utukufu; 9lakini, kama ilivyoandikwa, Mambo ambayo jicho halikuyaona wala sikio halikuyasikia, (Wala hayakuingia katika moyo wa mwanadamu,) Mambo ambayo Mungu aliwaandalia wampendao. 10Lakini Mungu ametufunulia sisi kwa Roho. Maana Roho huchunguza yote, hata mafumbo ya Mungu. 11Maana ni nani katika binadamu ayajuaye mambo ya binadamu ila roho yabinadamu iliyo ndani yake? Vivyo hivyo na mambo ya Mungu hakuna ayafahamuye ila Roho waMungu. 12Lakini sisi hatukuipokea roho ya dunia, bali Roho atokaye kwa Mungu, makusudi tupate kuyajua tuliyokirimiwa na Mungu. 13Nayo twayanena, si kwa maneno yanayofundishwa kwa hekima ya kibinadamu, bali yanayofundishwa na roho, tukiyafasiri mambo ya rohoni kwa maneno ya rohoni.**

**2:6 "** Walakini iko hekima tusemayo kati ya wakamilifu" Paulo anaweza

1. kutumia kejeli hapa kuhusisha msisitizo mkubwa wa Wakorintho juu ya hekima ya mwanadamu na mtazamo wao wenyewe "kukomaa" (kama vile George E. Ladd, *A Theology of the New Testament*, kr. 383-385)

2. hii inaweza kuhusiana na waaminio wachanga wa 1 Kor. 3:1-4 ambao Paulo anawahusisha na kikundi kidogo ndani ya kundi zima la ulimwengu wa Kiroho katika kanisa
3. katika Efe. 4:13 neno hili sana, *teleios*, linaelezea waaaminio waliokomaa dhidi ya watoto (yaani, kihalisia "watoto wachanga" Efe. 4:14). Angalia pia 14:20; Flp. 3:15 na Ebr. 5:14

Angalia jinsi neno linavyotumika katika Waebrania kutoka Mada Maalumu hapa chini.

**MADA MAALUMU: MWISHO AU UTIMILIFU *(TELOS)*** **(SPECIAL TOPIC: END OR FULL *(TELOS)*)**

◙ **"ila si hekima ya dunia hii"** Haya ni madai ya Paulo ya dhana ya kibiblia ya Wayahudi ya enzi mbili: enzi ya uovu ya sasa, inayotawaliwa na mwanadamu aliyeanguka, na enzi ya haki inayokuja, inayotawaliwa na Masihi. Ulimwengu wa Hekima ya mwandamu kimsingi ni dhanio na mabadiliko kutoka kwa utamaduni kwa utamaduni na wakati kwa wakati.Tazama Mada Maalumu juu ya dhana ya enzi mbili za Wayahudi katika 1 Kor. 1:20.

◙ **"wala ya hao wanaoitawala dunia hii"** Inawezekana kwamba hiki kifungu kinarejea kwa safu ya malaika au mafunuo ya *aeons* (kama vile Rum. 8:38-39; Efe. 1:21; 3:10; 6:12; Kol. 1:16; 2:10,15, BAGD,uk. 114, #3; F. F. Bruce, *Answers to Questions*, uk. 90). Inaonekana zaidi katika mstari wa pamoja na muktadha huu kutafsiri hili kama viongozi wa kibinadamu (kama vile 1 Kor. 2:8; Mdo. 3:17; Rum. 13:1-2; angalia Grant Osborne, *The Hermeneutical Spiral*, kr. 82-83). Ni vigumu sana kujua kama Paulo anazungumza kabisa kwa mantiki ya Binadamu au shughuli yenye pepo mbaya nyuma ya mantiki ya Binadamu: wote wawili wapo. Binadamu anaathiriwa kwa sababu ya kuanguka kwao (kama vile Rum. 12:2; Gal. 1:14; Efe. 2:2), lakini pia wanaathiriwa na uwepo wa uovu usio wa kawaida (yaani, ya malaika na wenye pepo mbaya, kama vile 2 Kor. 4:4; Dan. 10).

**NASB"wanaobatilika"**
**NKJV"ambao wanakuja bure"**
**NRSV"ambao wako katika mkumbo wa kupotea "**
**TEV"nguvu ambazo zinapoteza nguvu zao "**
**NJB"ambaye hawezi kudumu kwa muda mrefu "**

Hii ni KAULI TENDEWA ENDELEVU YA WAKATI ULIOPO ya neno ambalo lina maanisha “kufanya isivyosawa” (kama vile 1 Kor. 1:28; Rum. 6:6). Paulo alitumia neno hili mara ishirini na saba. Ikiwa hii inarejea kwa mamlaka ya binadamu, watakufa. Ikiwa hii inarejea kwa mamlaka ya malaika, enzi hii itapita ndani ya enzi mpya ya haki. Angalia Mada Maalum: Batili na utupu (*Katarge*ō) katika 1 Kor. 1:28.

**2:7 "bali"** Huu ni USHINDANI mkubwa ULIO KINYUME wa neno "*alla*." Hekima ya Paulo na nguvu ilikuwa kutoka kwa Mungu.

◙ **"twanena hekima ya Mungu katika siri, ile hekima iliyofichwa"** Hekima hii ni kutoka kwa Mungu (yaani, *Theos* iko mbele, au imewekwa kwanza, katika maandishi ya Kiyunani kwa kusisitiza); Hii ni hekima iliyofichwa (yaani., KAULI TENDEWA ENDELEVU YA WAKATI TIMILIFU, kama vile Efe. 3:9); siri hii sasa imedhihirishwa wazi katika Kristo (kama vile Rum. 16:25; Efe. 3:3-5; Kol. 1:26). Hii ni siri iliyowekwa wazi (yaani,injili) inasisitiza ufunuo wa Mungu dhidi ya ugunduzi wa Binadamu (kama vile Rum. 16:25-26; Efe. 1:9-10; 3:3-5; Kol. 1:26; 2:2-3). Ufafanuzi mpana zaidi wa siri hii ni kwamba Myahudi na watu wa Mataifa wameungana katika kuwa watu wapya wa Mungu (yaani, kanisa, kama vile Efe. 2:11:-3:13). Angalia Mada Maalumu: Siri katika 1 Kor. 2:1.

**NASB"ambayo Mungu aliiazimu tangu milele"**
**NKJV"ambayo Mungu aliwaagiza"**
**NRSV"ambayo Mungu aliagiza "**
**TEV"ambayo tayari alikua amechagua "**
**NJB"ambayo Mungu aliiazimia tangu mwanzo"**

Hata kabla ya uumbaji Mungu tayari alikuwa na mpango wa ukombozi (kama vile Mt. 25:34; Yohana 17:24; Efe. 1:4; 1 Pet. 1:20; Ufu. 13:8 napiaMdo 2:13; 3:18; 4:28; 13:29). Neno lililotafsiriwa hapa "lililojaaliwa" ni msombo wa KIHUSISHI cha neno "kabla" na "kuweka mipaka" (kama vile Mdo. 4:28; Rum. 8:29,30; Efe. 1:5,11).

Kifungu dhahiri juu ya mambo yaliyoamuliwa kabla katika Agano Jipya ni Rum. 8:28-30; Rum. 9; na Efe. 1:3-14. Maandishi haya dhahiri yana mkazo kwamba Mungu ni Mtawala. Yeye yu katika udhibiti kamili wa vitu vyote, ikiwa ni pamoja na historia ya Binadamu.

Kuna mpango wa ukombozi wa Mungu uliowekwa tayari kufanywa kwa wakati. Hata hivyo, huu mpango ni ule usio na mantiki au wenye uwezo wa kuchagua. Haitegemei pekee juu ya utawala wa Mungu na ujuzi wa mbele, lakini pia juu ya tabia yake isiyobadilisha ya upendo, huruma, na neema zisizostahili.

Lazima tuwe wangalifu kwa ubinafsi wetu wa magharibi (Mmarekani) au moyo wetu wa kiinjili kutia rangi ukweli huu wa ajabu. Lazima pia tulinde dhidi ya kukingamizwa katika historia, migogoro ya kitheolojia kati ya Augustino dhidi ya Pelegius au Calvinism dhidi ya Arminianism.

Mambo yaliyoamuliwa kabla sio mafundisho yaliyomanisha kupunguza mapenzi ya Mungu, neema, na huruma, wala kuwatenga baadhi kutoka kwenye injili. Inamaanisha kuwapa uwezo waaminio kwa kuumba maoni yao ya Kidunia. Mapenzi ya Mungu ni kwa wanadamu wote (kama vile 1 Tim. 2:4; 2 Pet. 3:9). Mungu ni mtawala wa kila kitu. Nani au nini kinaweza kututenganisha sisi na yeye (kama vile Rum. 8:31-39)? Majaaliwa hufanya moja ya njia mbili kuangalia maisha. Mungu huangalia historia yote kama ilivyo sasa; Binadamu amefungwa kwa wakati. Mtazamo wetu na uwezo wa akili ni mdogo. Hakuna ukinzani kati ya mamlaka ya Mungu na mapenzi huru ya mwanadamu. Ni mfumo wa Agano. Huu ni mfano mwingine wa ukweli wa kibiblia uliotolewa katika fumbo la maneno, mbinu pembuzi, jozi zilizojaa mvutano. Mafundisho ya kibiblia yamewasilishwa kutoka katika mitazamo tofauti. Mara nyingi huonekana kwa fumbo la maneno/kweli kinzani. Ukweli ni uwiano/usawa kati ya jozi inayoonekana kinyume. Lazima tusiondoe wasiwasi/mvutano kwa kuchagua moja ya ukweli. Hatupaswi kutenganisha ukweli wowote wa kibiblia ndani ya vyumba peke yake.

Pia ni muhimu kuongeza kwamba lengo la uchaguzi sio mbinguni pekee wakati tutakapokufa, bali kuwa kama Kristo sasa (kama vile Efe. 1:4; 2:10! Tulichaguliwa kuwa "watakatifu na wasio na lawama." Mungu alichagua kutubadilisha sisi ili wengine waweze kuona mabadiliko na kujibu kwa imani kwa Mungu katika Kristo. Majaaliwa sio upendeleo wa kibinafsi, bali wajibu wa Agano! Tunatakiwa kutumika, tumeokolewa kutumika!

◙**" tangu milele,"** kifungu cha maneno "tangu milele" ni lahaja ya Agano la kale inayorejelea kwenye umilele uliopita. Inafanana na neno la kiebrania *'olam*, ambalo linaweza maanisha milele, iliyopita au ijayo.inaweza pia kuonyesha kipindi kidogo cha wakati/muda mdogo. Ni lazima kutafsiriwa katika mazingira.Tafsiri yake inahusiana na jambo lake (yaani,Mungu, ahadi za agano, maisha ya ulimwengu, waovu, n.k.).

Hii pia ni kweli kwa tafsiri ya Kiyunani ya Agano Jipya ya neno *aiōn*, *aiōnios*, *eis ton aiōna*, amabayo yanafuata tafsiri ya Maandiko ya Agano la Kale ya neno *'olam*. Mungu ni milele, bali vitu vya kimwili (yaani, mbinguni na dunia) vitapita (kama vile 2 Pet. 3:10). Kama pamoja na maneno yote, lakini hasa maneno *'olam* na *aiōn,* mazingira ni muhimu na huamua tafsiri.

Kwa majadiliano ya kuvutia ya neno "milele" angalia Robert B. Girdlestone's *Synonyms of the Old Testament*, kr. 312-319 na F. F. Bruce's, *Answers to Questions*, kr. 202-203.

## MADA MAALUMU: MILELE *('OLAM)* (SPECIAL TOPIC: FOREVER *('OLAM))*

◙ **"kwa utukufu wet"** angalia mada maalumu chini.

## MADA MAALUMU: UTUKUFU (AGANO LA KALE*)* ( SPECIAL TOPIC: GLORY *(OT))*

**2:8 "kama"** A. T. Robertson, katika *Word Pictures in the New Testament*, uk.85, huita hii SENTENSI YENYE MASHARTI DARAJA LA PILI inayoitwa "kinyume na kweli."Kauli ya uongo imefanywa kuonyesha hitimisho la uongo, "kama watawala wa enzi hizi wangeelewa (yaani, KAULI TENDAJI ELEKEZI YA WAKATI TIMLIFU), ambavyo

hawakuelewa, basi wasingeweza kumsulibisha (yaani, KAULI TENDAJI ELEKEZI YA WAKATI ULIOPO USIOTIMILIFU) Bwana wa utukufu, ambavyo walifanya."

◙ **"Bwana wa utukufu"** Kifungu hiki cha maneno kilitumika kwa YHWH katika Matendo 7:2; Efe. 1:17 na labda ni dokezo kwa Kut. 24:16. Kifungu sawa kinatumika kwa Yesu katika Yakobo 2:1. Huu ni mfano mwingine wa waandishi wa Agano Jipya kutumia sifa ya YHWH kwa Yesu na, hivyo, wanadai yeye ni sawa na YHWH (kama vile 2 Kor. 4:6).

## MADA MAALUMU: MAJINA YA UUNGU (SPECIAL TOPIC: NAMES FOR DEITY)

**2:9 "kama ilivyoandikwa"** Hii ni nahau ya Kiebrania (yaani, KAULI TENDEWA ELEKEZIYA WAKATI TIMILIFU) kwa kutambulisha nukuu ya Agano la Kale. Clement wa Roma (yaani, Waraka wa Kwanza wa Clement kwa Wakorintho XXXIV), iliandika katika K.K. 95, inasema ni nukuu kutoka Maandiko ya Agano la Kale ya Isa. 64:4 au labda iliunganishwa pamoja na 65:17 (kama vile Isa. 52:15 na Yer. 3:16). Origen na Jarome walidhani Paulo alinukuu kutoka katika kitabu cha kuhusu sheria za kanisa kinachoitwa *Apocalypse of Elijah*, ambacho karibu kabisa kupotea. Ukweli ni kwamba nukuu /dokezo hili linafaa, hakuna maandiko yanayojulikana ya Agano la kale (hata hivyo ni kweli yana ufanano ule ule ni wa kweli Mt. 2:23; Yohana 7:38; Yakobo 4:5).

Mungu alitenda katika njia ambayo mwanadamu asingeweza kufikiria kamwe (kama vile Isa. 55:8-9), lakini sasa kwa kupitia injili na Roho wanaweza kwa imani! Ni ahadi ya Ajabu!

◙ **"MOYO"** Angalia Mada Maalumu katika 1 Kor. 14:25.

**2:10 "Lakini Mungu ametufunulia sisi kwa Roho"** Baba, kupitia Roho, alijifunua (yaani, *apokaluptō,* KAULI TENDAJI ELEKEZI YA WAKATI ULIOPO USIOTIMILIFU) siri hii iliyofichwa katika Kristo. Hekima zote ni katika Kristo (kama vile 1 Kor. 1:18-25,30).
Angalia Mungu wa Utatu 1 Kor. 2:8-10: Bwana wa utukufu aliyesulubiwa (yaani,Yesu), Mungu (yaani, Baba), na Roho.

## MADA MAALUMU: UTATU (SPECIAL TOPIC: THE TRINITY)

◙ **" Maana Roho huchunguza yote, hata mafumbo ya Mungu"**Msisitizo hapa ni juu ya Utatu kamili wa Roho (kama vile Isa. 63:10; Efe. 4:30). Roho ni njia yetu pekee ya kumjua Mungu (kama vile Rum. 8:26-27; 11:33-36). Huu ni msisitizo unaoendelea wa mazingira yote kwamba njia ya mwanadamu ni ile ya kutokuwa na nguvu ya kumjua Mungu au mambo (yaani, mipango) ya Mungu. Neno "Yenye kina" ni sitiari ambayo ni (1) nzito yenye kupingana na iliyo nyepesi (2) iiyofichwa ndani zaidi ya mwanadamu kuweza kufikia au kugundua/ugunduzi. Kazi ya Roho ni muhimu katika kusadikisha, wokovu, na kuishi kama (kama vile Yohana 16:7-14).

Kifungu cha maneno "mambo yenye kina ya Mungu" (NKJV) kinachoweza kushika moja vikundi vidogo vidogo katika Korintho. Mambo yenye kina ya Mungu yapo kwa wote ambao wanafanya imani katika Kristo.Hakuna siri iliyofichwa tena. Injili inafunuliwa kwa wote ambao watapokea. Hakuna "mambo ya kina zaidi," hakuna imani kwamba tabaka fulani linapaswa kutawala, hakuna asiyechanganyika na mwingine!
Imani hii ya ajabu ya kutoka kwa Mungu na kujali ilinyonywa na Mafunuo ya baadaye, ambao walidai ni uthibitisho wa maandishi kwa maarifa maalumu (kwa mfano sio ya kuhusu sheria za kanisa na kitabu cha mafunuo ya *Ascension of Isaiah).*

## MADA MAALUMU:UBINADAMU WA ROHO (SPECIAL TOPIC: THE PERSONHOOD OF THE SPIRIT)

**2:11-12** Huu ni mfano wa ukweli uliosemwa awali. Angalia matumizi ya kwanza ya Utatu wa "roho" katika aya hii ina "r" ndogo, wakati matumizi ya pili ya "Roho" yana herufi kubwa "R." Katika maandiko ya kiyunani hakuna njia ya kutofautisha herufi kubwa, kwa hivyo, hii ni fasiri. Herufi kubwa "R" ingeweza rejea kwa Roho Mtakatifu na

herufi ndogo “r” kwa roho ya mwanadamu (kama vile 1 Kor. 6:18; Rum. 8:16; 2 Kor. 2:13; 7:13; 12:18; Gal. 6:18; Flp. 4:23). Hilii linaweza kuwa dokezo la Mit. 20:27.

**2:12 " roho ya dunia"** Hiki ni kidokezo kingine cha neno *kosmos* (yaani, Ulimwengu, angalia Mada Maalumu katika 1 Kor. 3:21b-22), jamii ya mwanadamu iliyoanzishwa na kufanya kazi pasipo na Mungu (ni kawaida sana katika maandiko ya Yohana). Leo tungeweza kuyaita "ufuasi wa binadamu kutoamini uwepo wa Mungu” (kama vile 1 Kor. 2:6).Pia inaitwa “roho ya utumwa” katika Rum. 8:15.

◙ **"makusudi tupate kuyajua tuliyokirimiwa na Mungu"** Waaminio wanaweza kuelewa injili ya Kristo na mibaraka yao katika yeye pekee kupitia Roho Mtakatifu.

Ni ukweli hakika kwamba katika kuanguka kwao na hali ya muda hata waaminio hawawezi kukamilisha, kumaliza kabisa kumjua Mungu, lakini wanaweza kujua na kuelewa kila kitu kinachohitajika kwa wokovu na kuishi ki-Mungu kupitia ufunuo wa Baba, mtu na kazi ya Mwana na mwangaza wa Roho. Kwa sababu hatuwezi kujua kila kitu si udhuru wa kutokukumbatia ukweli halisi wa Biblia na kutembea ndani yake.

Pia ni muhimu kwamba wanaoamini wanatambua kwamba hekima ya Mungu ilikuwa “imetolewa bure” "(kama vile Rum. 8:32). Ni zawadi ya Mungu ambayo yeye alitamani kuitoa kwa kila mwanadamu aliyemfanya katika mfano wake (kama vile Mwa. 1:26-27), lakini sasa kupitia uasi wanatenganishwa na Yeye (yaani Mwanzo 3). Hekima ya Mungu sio matokeo ya akili za mwanadamu, kusimama kijamii, au iliyofanywa kwa maarifa, bali ufunuo wa mapenzi ya Mungu na huruma kupitia kazi ya Kristo na wakala wa Roho. Tangu Kristo, ujinga ulikuwa umekusudiwa! Roho Mtakatifu huleta mwanga, ukweli, na wokovu. Roho ya huu ulimwengu ulileta giza, udanganyifu, na kifo.

**2:13 "Nayo twayanena"** Ni muhimu kwamba waaminio wapate kushiriki ukweli huu uliotolewa na Mungu. Wao ni uzima na nuru kwenye ulimwengu unaokufa na kupotea, kwenye ulimwengu uliopendwa ambao utakombolewa ikiwa watampokea Mwana wa Mungu pekee, Mungu wa ukweli! Ufunuo ni mwanzo wa ukombozi (kama vile 2 Tim. 2:15) na kisha mabadiliko (kama vile 2 Tim. 3:16-17).

**NASB "kwa walio fundishwa na Roho, kuunganisha mawazo ya kiroho na maneno ya kiroho"**
**NKJV "ambacho Roho Mtakatifu anafundisha, kulinganisha na mambo ya kiroho na kiroho"**
**NRSV "tuliyofundishwa na Roho, yanafasiri mambo ya kiroho kwa walio na huyo Roho "**
**TEV "nayo twayanenasi kwa maneno tuliyofundishwa na hekima ya binadamu, bali kwa maneno tuliyofundishwa na Roho”**
**NJB "kwa maneno tuliyojifunza kutoka kwa Roho,ya kustahiki lugha ya kiroho kwa mambo ya kiroho "**

Hiki ni Kifungu cha maneno chenye maana nyingi sana kwa baadhi ya sababu. Kabla ya kujaribu kufanya hili kukumbuka mazingira makubwa ni muhimu na sio maelezo yenye maana nyingi ya Sarufi ya Kiyunani na taaluma ya kukua. Mazingira makubwa yanahusiana na waaminio waliokomaa (kama vile 1 Kor. 2:6). Inatofautisha hekima ya mwanadamu na ujuzi/maarifa pamoja na hekima ya Mungu, ambayo ni Kristo, na maarifa ya Mungu, ambayo yanaelezewa katika injili. Huu ni ukweli mkuu wa Sura 1 na 2.

Roho Mtakatifu ni njia ya lazima ya mawasiliano (kama vile Yohana 16:8-14). Yeye alifunua ukweli wa kiroho kwa wale ambao wanamuamini Kristo na kupokea Roho. Katika baadhi ya njia za majadiliano ya Paulo hapa ni sawa na mfano wa Yesu wa mpanzi au udongo (kama vile Mathayo 13). Ujumbe wa injili umeeleweka na kujibiwa na wasikilizaji waliopokea, lakini ulikataliwa na wasikilizaji wasiokubali.

Neno *pneumatikois* linaweza kuwa LISILO CHUKUA SHAMIRISHO (yaani,mambo ya kiroho) au jinsia ya kiume (yaani,watu wa kiroho). Kundi lingine la wasikilizaji limetajwa katika aya inayofuta, *psuchikos* (yaani,asili ya mtu aliyepotea). Yumkini kwamba neno katika 1 Kor. 2:13 waaminio waliokomaa au waliotayarishwa) pamoja na 1 Kor. 2:15 (yaani,ambapo walikuwa wanaitwa *pneumaikos*). Inaonekana kuwepo kwa makundi matatu ya watu wanaorejelewa pia katika mazingira haya.

1. watu waliopotea
2. waliookolewa, lakini waamini wachanga
3. waamini waliokomaa

Mara nyingi hakuna tofauti inayoonekana kati ya # 1 na #2.

Ikiwa hivyo, basi jinsi gani Roho inawasiliana na ukweli wa kiroho? KAULI TENDAJI ENDELEVU YA WAKATI ULIOPO,*sunkrinontes*, inatumika katika Maandiko ya Agano la Kale kwa kufasiri ndoto (kama vile Mwa. 40:8,16,22; 41:12,15; Amu. 7:15; Dan. 5:12; 7:15,16). Hata hivyo, neno hili sawa la kiyunani linatumika hapa pekee na katika 2 Kor. 10:12 katika Agano Jipya lina hali yake ya kawaida "kulinganisha." Hakika jinsi Roho anavyowasilisha ukweli wa kiroho kwa watu wa kiroho ni ngumu na kwa sababu hiyo hatupaswi kuwa wagumu juu ya namna ya kuweza kulitafasiri andiko hili. Ukweli mkubwa ni kwmba Mungu Mtakatifu anatafuta na kufanikisha mawasiliano na mwanadamu aliyeanguka (kama vile 1 Kor. 2:12). Mungu anazungumza, tunasikiliza?

Kuna makala inavutia juu ya "Ufunuo na maandiko matakatifu" katika *Expositor's Bible Commentary*, juzuu. 1, kr. 461-462. Hii hapa lakini ni aya moja.

> "kwa waandishi wa Agano Jipya, ufunuo unahusu ukweli. Ukweli ni kazi ya lugha. Katika njia hii ufunuo na maandiko matakatifu yasiodadavulika kuunganishwa katika theolojia ya Agano Jipya. Matukio na fasiri huenda sambamba. Ufunuo wa Agano jipya kama unavyomuhusisha Yesu Kristo unahusisha sio tu dhahania na bila wakati wa maadili ya kweli, au uzoefu wa kujitegemea wa wanafunzi, lakini unahusika na matukio ambayo ni thabiti, hasa ya sehemu, ya hali halisi. Kauli ya Mitume na fasiri ya matukio ni ukweli wa jambo. Waandishi walikusudia kuwasilisha kwa wasomaji hasa kile kihusucho, kusema nini kinaendelea juu ya mambo ambayo yalikuwa yanatokea. Shitaka lolote linaweza kufanywa dhidi ya waandishi wa Agano Jipya kama kwenye imani yao ya kidini, tunapaswa kutambua kwamba wanadai kutupa sisi ufunuo wa kimungu ulioelezewa katika lugha ya mwanadamu (1 Kor. 2:13)."

**ANDIKO LA NASB(LILILOBORESHWA) : 1 WAKORINTHO 2:14-16**
**14 Basi mwanadamu wa tabia ya asili hayapokei mambo ya Roho wa Mungu; maana kwake huyo ni upuzi, wala hawezi kuyafahamu, kwa kuwa yatambulikana kwa jinsi ya rohoni. 15 Lakini mtu wa rohoni huyatambua yote, wala yeye hatambuliwi na mtu. 16 Maana, Ni nani aliyeifahamu nia ya Bwana, amwelimishe? Lakini sisi tunayo nia ya Kristo.**

**2:14**
**NASB"mwanadamu wa tabia ya asili"**
**NKJV"mwanadamu wa tabia ya asili"**
**NRSV"wale ambao hawapokei mambo ya Roho wa Mungu"**
**TEV"mwanadamu amabaye hana Roho"**
**NJB"mwanadamu wa tabia ya asili"**

Hii ni kinyume na "mtu wa kiroho" inarejelea pia katika 1 Kor. 2:6,13 na 3:1. Neno (yaani, *psuchikos*) linatumika mara kadhaa katika Agano Jipya ambapo linarejea kwa maisha juu ya ulimwengu, maisha waishiyo katika uhusiano na hisia tano pekee (yaani, maisha ya *bios*, dhidi ya maisha ya *zoē*,). Neno lenye kuishia na *ikos* mwishoni linamaanisha "elezewa kwa" (kama vile 1 Kor. 3:3). Basi inaweza kumaanisha vya duniani dhidi vya mbinguni au visivyo vya kiroho dhidi ya kiroho (kama vile 1 Kor. 15:44,46; Yakobo 3:15; na Yuda 1:19).

**NASB "hapokei"**
**NKJV, NRSV "hayapokei"**
**TEV "hawezi kuyapokea"**
**NJB "hayana nafasi kwa"**

Neno kanushi la Kiyunani linamaanisha "kukataa," "kukataa kukubali," "hawezi kutambua," au "kutoweza kutambua" au "kutoleta maana." Neno hili pasipo kukanusha mara nyingi hutumika kwa kumkaribisha mgeni. Neno hili (yaani, *dechomai,* kama vile Luka 8:13; Matendo 8:14; 11:1; 17:11; 2 Kor. 11:4; 1 The. 1:6; Yakobo 1:21) linafanana na *lamban*ō (kama vileYohana 1:12; 12:48; 14:17). Halihusiani na ujinga wa mwanadamu, lakini kutoweza kuelewa ukweli wa kiroho!

Hii ni siri ya jinsi gani/kwanini baadhi ambao wanasikia injili wanajibu na wengine hawajibu. Kukataliwa huku kulihusiana na majaaliwa au ridhaa/hiari ya mwanadamu? Jibu ni"ndio," lakini hasa jinsi gani kuhusiana kwa kauli

hizi mbili ni sehemu ya upembuzi asili wa ufunuo wenyewe (kama vile Flp. 2:12-13, angalia Mada Maalumu katika 2 Kor. 8:16-17). Napenda kile anachokisema Frank Stagg, katika *New Testament Theology*, anasema, "katika Agano Jipya, kinyume cha uchaguzi sio kusudio na uchaguzi, lakini ni kukataa kwa mwandamu wokovu wa Mungu " (uk. 87).

◙**" upuzi"** Angalia maelezo katika 1 Kor. 1:25.

◙ **"kwa kuwa yatambulikana kwa jinsi ya rohoni"** Hili ni neno halali ambalo linazungumzia kwa ukamilifu wa mtihani wa mwanzo kabla ya majaribu (kama vile Luka 23:14; Matendo 12:19;24:8; 25:26; 28:18) au kuchunguza kitu fulani kwa umakini (yaani, maandiko Matakatifu, kama vile Mdo. 17:11; chakula, kama vile 1 Kor. 10:25,27). Neno sawa hutokea mara mbili zaidi katika 1 Kor. 2:15.

◙ Waaminio waliojaliwa na Roho wanaweza kuamua ipasavyo mambo yote katika ulimwengu wa kimwili na kiroho (kama vile 1 Kor. 1:22-25 na 2:2, pia maelezo katika 14:29 na 1 The. 5:20-21). Hata hivyo, asiye wa rohoni wa 1 Kor. 2:14 hawezi kutambua vizuri mambo ya kiroho, ukweli wa kiroho, au watu wa kiroho.

**2:15 "wala yeye hatambuliwi na mtu"** Hii, bila shaka, ni mtindo wa pamoja wa JINSIA YA KIUME. Waaminio hawawezi kuhukumiwa, hata kuelewa na wasioamini (kama vile 1 Kor. 4:3-4). Hii inaweza kurejea kwa baadhi ya maadui wa Paulo katika Korintho (kama vile 1 Kor. 9:3). Ni Roho iishio ndani ambayo inaleta nuru kupita injili kuelekea kwenye ukweli, sio ukweli wa enzi hii au ukweli wa kimwili, lakini ukweli wa Mungu!

**2:16** Hili ni dokezo kwa Isa. 40:13 katika Maandiko ya Agano la Kale. Katika Isa. 40:3 neno "BWANA" ni jina la Mungu YHWH, lakini hapa Paulo hutumia nukuu kwa kurejea kwa Yesu (pia angalia maelezo katika Rum. 10:13 na Flp. 2:10-11).

Hii huendelea kusisitiza taratibu juu ya hitaji la Roho kwa mwanadamu kwa “kusikia” injili na kuelewa ukweli wa kiroho. Mazingira haya na Yohana 14-16 ni muhimu katika kuelewa kazi ya Roho ya Mungu. Pasipo na Roho mwanadamu aliyeanguka anajishughulisha katika makisio, hadithi zinazoelezea asili ya watu, hata wenye pepo mbaya walitia msukumo kwenye ukweli wa uongo! Ah, jambo liletalo huzuni la dini za ulimwengu na falsafa ya mwandamu.

◙ **"Lakini sisi tunayo nia ya Kristo"** KIWAKILISHI NOMINO Neno "sisi" ni mkazo! Hi inaweza kurejea kwa (1) Paulo na wezi wake; (2) wahubiri wa kikristo; au (3) Wakristo waliokomaa. Hii haimaanishi waaminio kujua kila kitu ambacho Kristo anajua, lakini kwamba Roho imefunua nafsi zetu kwa mtazamo wake, vipaumbele vyake, moyo wake (kama vile Rum. 12:2; Flp 2:5).

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni <u>mwongozo</u> wa maoni ya usomaji, ukiwa na maana kuwa, unawajibika kwa fasiri binafsi ya Biblia. Kila mmoja wetu yampasa atembee katika nuru tulionayo, na Roho Mtakatifu ndiye kipaumbele katika fasiri yetu. Usimwachie hili mtoa maoni pekee.

Maswali haya ya kujadili yanatolewa ili kukusaidia kufikiri mambo muhimu yaliyoko katika kipengele cha kitabu hiki. Yanamaanisha kuwa maswali ya kichokonozi, yasio na ukomo.

1. Fafanua matumizi ya Paulo ya neno, “siri” katika mazingira haya.
2. Nini ambacho Paulo alimaanisha kwamba amekuja katika hofu na mashaka makubwa kwa Wakorintho?
3. Nini ushahidi kwamba mahubiri ya Paulo yaliwezeshwa na Mungu?
4. Kwanini waandishi wa Agano Jipya walikaidi kuelezea habari zihusuzo mambo ya mbinguni au jehanam kwa undani?
5. Elezea tofauti kati ya “ufunuo,” “uvuvio,” na “mwangaza.”
6. Orodhesha njia tofauti tatu ambazo Paulo anatumia kulielezea neno “roho” katika sura hii.
7. Orodhesha njia tofauti nne amabazo Paulo anatumia kuelezea neno “hekima’ katika sura hii.
8. Tazama 1 Kor. 2:13 katika tafsiri baadhi za Kiingereza. Unafikiria mstari huu unafundisha nini?

# 1 WAKORINTHO 3

| MGAWANYO WA AYA WA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **UBS[4]** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB** |
| Watenda kazi Pamoja na Mungu | Ufuasi wa kimadhe -hebu ni hali ya Mwili | Mafarakano juu ya Viongozi | Watumishi wa Mungu | Hekima ya Kweli na ya Uongo (1:17-3:4) |
| 3:19 | 3:14 | 3:14 | 3:14 | 3:14 |
| | Kumwagilia, Kutenda Kazi, na Kuonya | | | Nafasi ya Mhubiri wa Kikristo |
| | 3:5-17 | 3:5-9 | 3:5-9a<br>3:9b-15 | 3:5-9 |
| | | Walimu na Kanisa Chini ya Mungu | | |
| 3:10-17 | | 3:10-15 | | 3:10-15 |
| | | 3:16-17 | 3:16-17 | 3:16-17 |
| | Epuka Hekima ya Kidunia | | | Hitimisho (3:18-4:13) |
| 3:18-23 | 3:18-23 | 3:18-23 | 3:18-23 | 3:18-23 |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (Kutoka "Mwongozo wa Usomaji Mzuri wa Biblia"(A Guide to Good Bible Reading")

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Haya ni maoni ya mwongozo kwa kujisomea, ikiwa na maana kuwa unawajibika binafsi kwa tafsiri ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mtoa maoni tu.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa,lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

9. Aya ya kwanza
10. Aya ya pili
11. Aya tatu
12. N.k

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA KWA 1 WAKORINTHO 3:1-23

A. Katika sura hii, Paulo anaendelea kuzikuza sifa pambanuzi za Wakristo wa Kikorintho kama wasiokomaa kama ilivyo katika sura ya 2.

B. Mwonekano wa haya makundi yaliyotazamiwa ambayo kwa mara nyingine yanatajwa bayana katika sura 3. Hii inaonyesha kwamba sura ya 1-3 ni hoja zilizoidhinishwa kuhusu hekima ya mwanadamu na uongozi wa Mkristo.
C. Angalia haya makundi matatu.
   1. mwanadamu wa asili, 1 Kor. 2:1
   2. mwanadamu wa kiroho, 1 Kor. 3:1
   3. watoto wachanga katika Kristo, 1 Kor. 3:1
D. Mistari ya 10-17 imeangaliwa kwa urefu kama yenye kumpambanua mtu, Wakristo wa kimwili. Hii inawezekana kwa kulinganisha muktadha uliompana wa 1 Kor. 1:12 kupitia 3:4-5. Uthibitisho mwingine wa hoja hii ungeliweza kuwa Paulo analieleza kanisa (katika hali ya WINGI "ninyi") katika 1 Kor. 3:1 na 16. Matumizi ya mara kwa mara ya maneno "kila mtu," "hakuna mtu," "kama mtu" katika 1 Kor. 3:10,11,12,13, 14,15, 17,18 pia inaleta imani ya fasiri hii.

Hata hivyo, inawezekana kuhusianisha andiko hili na viongozi wa kanisa (kama vile 1 Kor. 3:10). Haya makundi madogo madogo hayarejelei kwa Wakristo wote wa Korintho (yaani, waliokomaa wale wa 1 Kor. 2:6), bado baadhi yao (yaani, "watu wenye tabia ya mwilini," "watoto wachanga katika Kristo," 3:1). Hawa ni viongozi wa haya makundi madogo madogo ambapo Paulo anajilinganisha mwenyewe na Apolo katika1 Kor. 3:6-9. Muktadha wa moja kwa moja unahusiana na 1 Kor. 3:10-15 kwa viongozi, namna wanavyozitumia karama zao za kiroho katika kulitumika kanisa. Huu ni msistizo wa onyo la 1 Kor. 3:17.

Ni vigumu kuamua kati ya hoja hizi mbili: (1) Kitabu cha Agano Jipya hakijadili hali ya kiroho na hatima ya Wakristo wa kimwili na (2) ule "uharibifu" wa 1 Kor. 3:17 haueleżwi bayana. Mistari ya 15 na 17 lazima ielezwe katika hali ya mvutano. Maneno yote yenye neno"kama" katika muktadha huu ni SENTENSI YENYE MASHARTI DARAJA LA KWANZA, ambayo inadhaniwa kuwa ya kweli kwa kusudi la mwandishi. Mstari wa 14 hudhani kuwa hao ni waamini ya kweli, ambapo 1 Kor. 3:15 hudhani kwamba baadhi watateketea kwa kuipoteza thawabu. Neno "kujaribu" katika 1 Kor. 3:13 linamaanisha jaribio liletalo matokeo ya ukubalifu. Hata hivyo, muktadha huu unamaanisha kwamba Paulo anawashutumu kwa sababu ya kutoilewa injili, kwa sababu ya wao kutokuwa wa kiroho, kuwa wenye wivu, na kuibua makundi madogo madogo miongoni mwao.
Kwangu hili linaonekana bora zaidi kutohusianisha andiko hili kwa Wakristo wote, lakini pia, hata kuzuia hili kwa viongozi. Andiko hili kwa uhalisia linahusiana na wale ambao wanachangia kuibuka kwa makundi madogo madogo na migawanyo ndani ya kanisa. Waamini wote watatoa hesabu zao kwa Mungu kwa ajili ya huduma njema ama kwa ajili ya kuuharibu mwili Wake, kanisa (kama vile 2 Kor. 5:10; Gal. 5:10)

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : 1 WAKORINTHO 3:1-4**
[1]**Lakini, ndugu zangu, mimi sikuweza kusema nanyi kama na watu wenye tabia ya rohoni, bali kama na watu wenye tabia ya mwilini, kama na watoto wachanga katika Kristo.** [2] **Naliwanywesha maziwa sikuwalisha chakula; kwa kuwa mlikuwa hamjakiweza. Naam, hata sasa hamkiwezi,** [3] **kwa maana hata sasa ninyi ni watu wa tabia ya mwilini. Maana, ikiwa kwenu kuna husuda na fitina, je! Si watu wa tabia ya mwilini ninyi; tena mnaenenda kwa jinsi ya kibinadamu?** [4] **Maana hapo mtu mmoja asemapo, Mimi ni wa Paulo; na mwingine, Mimi ni wa Apolo, je! Ninyi si wanadamu?**

**3:1 "ndugu"** Angalia maelezo kamili katika 1 Kor. 2:6.

◙**"mimi sikuweza kusema nanyi"** Hii ni KAULI ELEKEZI YA WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFU na KAULI ISIO NA UKOMO YA WAKATI ULIOPITA ISIO TIMILIFU ambayo inayarejelea mahubiri ya mwanzo ya Paulo huko Korintho (kama vile Matendo 18:1-18).

**NASB "kama na watu wenye tabia ya rohoni"**
**NKJV, NRSV "kama watu wa kiroho"**
**TEV "kama watu walio na huyo Roho"**
**NJB "kama watu wa kiroho"**

Paulo anaielekeza mistari hii kwa nani: (1) kwa waamini wote au (2) kwa wale ambao hawajakomaa kiroho (yaani, yale makundi madogo madogo kama vile 1 Kor. 3:4)? Jibu la swali hili linahusisha namna mtu anavyofasiri 2:6. Kulikuwa na mwongozo mwingine wa huyo Roho, waamini waliokomaa katika kanisa la Korintho au wote walikuwa hawajakomaa?

◙**"bali"** Hii ni kauli nzito ya KINYUME *alla*. Kuna tofauti kati ya neno "kukomaa" la 1 Kor. 2:6 (yaani, watu wenye tabia ya rohoni) na wale "watu wenye tabia ya mwilini" katika 1 Kor. 3:1-4. Makundi yote yanaye huyo Roho (yaani, Wakristo), lakini kundi la kwanza linaonyesha kuwa na yule Roho, ambapo kundi la pili linaonyesha kuwa la kidunia.

**NASB " watu wenye tabia ya mwilini"**
**NKJV "kama wa kimwili"**
**NRSV "kama watu wa mwili"**
**TEV "kama watu wa kidunia"**
**NJB "kama watu waishio bado kwa mielekeo ya asili zenu"**

Hili ni neno "*sarkinos*" katika Kiyunani. Hii inayoishia na *inos* inamaanisha "kuundwa kwa" au "kukombolewa kutoka katika" (m.f. "mioyo ya nyama," kama vile 2 Kor. 3:3) hivyo hii inamaanisha "waliumbwa kwa mwili." Paulo anatumia "mwili" katika njia kadhaa na tofauti (angalia Mada Maalum katika 1 Kor. 1:26). Muktadha huu (yaani, "kama watoto wachanga katika Kristo") anaonekana kulitumia neno hili kwa waamini walio na yule Roho, lakini wenye kuenenda badala ya njia za ulimwengu huu.

Hii si kauli ya Paulo ya mwili dhidi ya Roho (kama vile Rum. 8:1-11), bali ni aina ya waamini. Kama hili ni la kweli muktadha huu ni moja ya nafasi chache katika Agano Jipya ambamo utofauti huu unatengenezwa. Hii ni huzuni ya wokovu usio na utakaso. Kumtaja Kristo kama Mwokozi, lakini si kuishi kana kwamba Kristo ni Bwana. Ikiwa hali hii ya kiroho yenye kutisha inabainishwa na wivu, migongano, na roho ya mgawanyiko wa makundi madogo madogo, vipi kuhusu kanisa la sasa? haswa, huzuni ya "Mkristo aliye kama mtoto" katika Ufalme wa Mungu na moyo wa Mfalme!

◙**"kama na watoto wachanga katika Kristo"** Kila mwamini huanza kama Mkristo mchanga. Katika hili hakuna aibu. Hii ni asili ya sitiari ya kifamilia iliyotokana na dhana ya neno "kuzaliwa upya" (kama vile Yohana 3:3; 2 Kor. 5:17; 1 Pet. 1:3,23), lakini haitupasi kubaki kama watoto wachanga!

**3:2 "Naliwanywesha maziwa"** Hii ni sitiari endelevu ya Mkristo mpya kama kiumbe mwenye chapa mpya mwenye kubainishwa kwa sifa ya kuwa kama mtoto (kama vile Ebr. 5:12-14; 1 Pet. 2:2). Tertullian na Hippolytus wanatwambia kwamba kanisa la kale lilikuwa likigawa bilauli ya maziwa kwa wale waliochukuwa maamuzi ya kubadili dini kwa wakati wao wa kwanza wa kuipokea meza ya Bwana kama ishara ya ukweli halisi.

◙**"kwa kuwa mlikuwa hamjakiweza"** Kwa kipindi kile Paulo alipoiandika barua hii, miezi mingi ilikuwa imepita. Ingawa yafaa kuwa kama Mkristo aliye kama mtoto mwanzoni mwa maisha ya Ukristo, ni huzuni kuendelea kukaa kama Mristo aliye kama mtoto kwa miaka mingi.
Hii mistari ya ufunguzi ya sura ya 3 lazima itakuwa imewajeruhi viongozi wenye matendo ya hujivunia usomi. Pana mchezo wa kimshangao juu ya NJEO YA WAKATI USIOTIMILIFU (yaani, " kwa kuwa mlikuwa hamjakiweza") na huu <u>njeo ya wakati uliopo</u> (yaani, "hata sasa hamkiwezi "). Hili neno "kuweza" ni neno la Kiyunani *dunamai*, ambalo linamaanisha nguvu ya kutenda, kukamilisha, kutenda hadi kufikia matokeo yaliyotamaniwa. Waamini wanaokolewa ili kutumika; hawa sasa wanaitwa wanaomfanana Kristo, si baadaye kwenda mbinguni pekee. Hawa "waamini" hawana nguvu ya Ufalme, ni nguvu za mwili, ambazo ziko, katika ukweli, wasioweza!

**3:3**
**NASB "ninyi ni watu wa tabia ya mwilini"**
**NKJV " ninyi bado ni wa mwilini"**
**NRSV " ninyi bado ni watu wa kimwili"**
**TEV "bado ninyi ni watu wa kidunia"**
**NJB "ninyi bado mnaishi kwa asili zenu za mwili"**

Hili ni neno *sarkikos* katika Kiyunani. Hili linaloishia na *ikos* linamaanisha "kubainishwa na " (kama vile 1 Kor. 2:14-15). Paulo anaumba neno kuleta mchezo juu ya neno *sarks* (mwili) katika 1 Kor. 3:1 na 3 kufafanua juu ya Wakristo wengi kama walivyookolewa huko Korintho, lakini wakiwa hali ya uchanga sana. Hawa walikuwa na ubinafsi, si wasiokuwa wabinafsi! Kwa neno "kimwili" angalia Mada Maalum katika 1 Kor. 1:26.

◙**"husuda na fitina"** Hizi ni kazi mbili za mwili zilizoorodheshwa katika Gal. 5:19-21. Hizi zilithibitisha kwamba baadhi ya Wakristo wa ki- Korintho walikuwa katika hali ya kimwili.

Katika machapisho ya kale ya Kiyunani (yaani, $P^{46}$, D, na tafsiri ya ki-Syria) kuna neno la nyongeza lenye kueleza, "faraka," ambalo pia linapatikana katika Gal. 5:20. Kwa uhakika hili halielezi tatizo la huko Korintho. Hata hivyo, hili neno linalokosekana katika MSS $P^{11}$, א, A, B, C, na P na lile toleo la Biblia ya Kilatini, Coptic, na tafsiri za lugha ya Armenia. Inaonekana kuwa nyongeza ya kiuandishi (yaani, $UBS^4$ inatoza ondoleo kwa daraja B (takribani ni yumkini).

◙ **"mnaenenda kwa jinsi ya kibinadamu"** Muundo wa kisarufi wa swali hili unatarajia jibu la "ndiyo". Hii ni maana ya kimwili. Ukomavu unaonekana kwa matunda yake, katika hali zote mtazamo na matendo (kama vile Rum. 8:1-11; Mt. 7:1na kuendelea).

3:**4** Aya hii inaaksi faraka ya 1 Kor. 1:10-17.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA ) : 1 WAKORINTHO 3:5-9**

**5Basi Apolo ni nani? Na Paulo ni nani? Ni wahudumu ambao kwao mliamini; na kila mtu kama Bwana alivyompa ambao kwao mliamini. 6Mimi nilipanda, Apolo akatia maji; bali mwenye kukuza ni Mungu. 7 Hivyo, apandaye si kitu, wala atiaye maji, bali Mungu akuzaye. 8 Basi yeye apandaye, na yeye atiaye maji ni wamoja, lakini kila mtu atapata thawabu yake mwenyewe sawasawa na taabu yake mwenyewe. 9Maana sisi tu wafanya kazi pamoja na Mungu; ninyi ni shamba la Mungu, ni jengo la Mungu.**

**3:5**
**NASB, NRSV,**
**NJB "nini"**
**NKJV, TEV "nani"**

Toleo la King James lina neno "nani" (yaani, *tis*), kufuatia machapisho ya Kiyunani $P^{46}$, C, D, na G. Tafsiri nyingi za Kiingereza zina neno "nini" (yaani, *ti*), ambalo linaonekana kuwa la makusudi kwa ajili ya kutoyachukulia maanani maneno yasiyofaa (yaani, Apolo, Paulo, Petro). Hili linathibitishwa na *ti* katika mstari wa 7. Tazama Bruce Metzger, *A Textual Commentary On the Greek NT*, uk. 548.

◙ **"wahudumu"** Hili ni neno (yaani, *diakonos*) ambapo tunalipata neno letu la Kiingereza "shemasi" (kama vile Flp. 1:1; 1 Tim. 3:8,12). Hili linakuwa moja ya maneno ya Kiyunani (yaani, *therapeuō, hupēreteō* na *diakoneō*) linalotumika kudokeza kutumika, msaada, au huduma (neno lingine la kawaida *latreuō* linadokeza huduma ya kikuhani). Angalia MADA MAALUM: UONGOZI WA KITUMISHI (SPECIAL TOPIC: SERVANT LEADERSHIP katika 1 Kor. 4:1.

◙**"ambao kwao mliamini"** Ukristo huanza kwa maamuzi ya hiari katika kuupokea (yaani, KITENZI KAULI TENDAJI ELEKEZI) injili ya Mungu, ambayo ni Yesu Kristo, mafundisho yake, matendo yake ya ukombozi, ufufuo wake, na kurudi kwake. Mtu hawezi kusukumwa katika wokovu. Hili si suala la wazazi wa mtu, taifa la mtu, akili nyingi za

mtu. Ni suala la neema ya agano la Mungu na mwitikio wetu wa kimaagano (yaani, toba, imani, utii, huduma, na ustahimilivu). Watu huwa Wakristo kwa kumpokea Kristo, kuiamini injili, na kuenenda katika Kristo. Haya yamefanya mawili kwanza, lakini la tatu lilikosekana. Habari njema ni Mtu, ukweli, na maisha. Yote haya ni muhimu kwa ajili ya ukomavu.

Neno la Kiyunani kuamini (yaani, *pisteuō)* linatafsiriwa katika Kiingereza kama sadiki, tumaini, au imani. Kifanani cha neno hili katika Agano la Kale kilimaanisha "kuaminiwa" na, ambapo neno hili lilikuja kutumika ki-istiari juu ya yule ambaye aliaminiwa, mtiifu, wa kutegemewa, au mwaminifu (tazama Mada Maalumu katika 1 Kor. 1:9). Kama kidokezo cha ufunuo wa muktadha huu, mwanadamu anaweza kuliitikia tumaini la Mungu pekee, uaminifu wa Mungu, agano la Mungu utii wa agano la Mungu. Imani ya mwanadamu ni mwitikio wa uaminifu wa Mungu! Ni jambo la kiimani, ahadi ya imani ni Mungu! Neema yake, huruma yake, wito wake, Mwanae, Roho wake, haya ndiyo matumaini pekee ya mwanadamu wa uasi.

◙ **"ambao kwao mliamini"** Msistizo ulioko hapa ni juu ya sehemu ya ki-Ungu, si mwitikio wa kibinadamu au utendaji. Lakini lengo la majaaliwa ya Mungu ni utakatifu (kama vile Efe. 1:4; 2:10), si nafasi za upendeleo, si zoezi la upendeleo binafsi au uteule binafsi. Kila mwamini ametayarishwa na Mungu kwa ajili ya huduma ya ndani na kwa ajili ya kanisa (kama vile 1 Kor. 12:7,11; Efe. 4:11-13).

Utambulisho kamili wa neno "Bwana" ni mgumu. Aghalabu huyu ni Mungu Baba ambaye hutoa wito wa wokovu. Lakini Paulo amekuwa akitumia neno "Bwana" mara kadhaa katika 1 Wakorintho kumrejelea Yesu (kama vile 1 Kor. 1:2,3,7,8,9,10; 2:8). Hata hivyo, mara kadhaa Paulo amekuwa akinukuu kifungu cha Agano Jipya ambapo Bwana humaanisha kumrejelea YHWH (kama vile 1 Kor. 1:31; 2:16; 3:20). Huu utata unaonekana dhahiri katika 1 Kor. 2:16 ambapo neno Bwana katika nukuu ya Agano la Kale linatumika katika ufanano wa "maana ya Kristo."

Hiki kifungu "na kila mtu" kwa uwazi pia huonyesha ugumu katika kupambanua juu ya yule anayezungumziwa. Ni kama viongozi hawa yaani Paulo na Apolo, waaamini wa huko Korintho, au waamini wote?

1. Waamini wote wameitwa na wamejaliwa vipawa, lakini wengine pia wameitwa na kujaliwa karama ya kuongoza (kama vile Hes.16:3).
2. Haya ni mazingira ya pamoja tenganifu au kuna msistizo binafsi (yaani, viongozi fulani)?

**3:6 "nilipanda. . . akatia maji"** Paulo anatumia sitiari za kilimo. Injili ni mbegu (yaani, Mathayo 13), bali wanadamu huipanda na kuitunza.

Agizo Kuu (yaani, Mt. 28:19-20) lina majukumu mawili sawa sawa.

1. uinjilisti
2. uanafunzi

Paulo alianzisha kanisa kwa kuihubiri injili na Apolo alilifundisha kanisa. Wote ni muhimu na hawatenganishwi!

◙ **"bali mwenye kukuza ni Mungu"** Hii ni NJEO YA WAKATI USIO TIMILIFU, ambao inamaanisha tendo endelevu katika wakati uliopita. Matendo ya Apolo na Paulo yalikuwa ya matukio ya wakati ulelule, bali matendo ya Mungu ni endelevu (kama vile 1 Kor. 3:7).

**3:8**
**NASB, NKJV" ni wamoja"**
**NRSV "wana kusudi moja"**
**TEV "hakuna tofauti kati yao"**
**NJB "wote ni wamoja"**

Swali la kifungu hiki cha Kiyunani kifupi na chenye utata (yaani, NASB, NKJV) ni (1) je! Viongozi wote ni sawa (2) je! Viongozi wote hugawana majukumu sawa ya kuikuza huduma ya kanisa? Utofauti wa kweli hauko baina ya karama za kiroho (yaani, mwinjilisti wa kwanza au mkufunzi, mchungaji/mwalimu, n.k.,kama vile Efe. 4:11), bali baina ya kazi ya Mungu na vitu vya kibinadamu. Mungu ndiye jawabu!

◙ **"lakini kila mtu atapata thawabu yake mwenyewe sawasawa na taabu yake mwenyewe"** Hii dhana ya thawabu imefafanuliwa vema katika 1 Kor. 3:10-15. Katika kujadili kuhusiana na dhana ya thawabu angalia maelezo kamili katika 1 Kor. 3:14.
Wazo hili la thawabu kwa ajili ya huduma linahusiana na kanuni ya kiroho iliyofafanuliwa katika 1 Kor. 3:13 na Gal. 6:7. Tunavuna kile tulichokipanda (kama vile 2 Kor. 9:6).

Jambo la kitheolojia linalohusika ni vile viwango vya thawabu. Maarifa ya injili yalioongezewa nguvu na Roho na wito wa uongozi ndani ya kanisa la Mungu ulileta mwitikio mkubwa (kama vile Luka 12:48). Kitabu cha Agano Jipya Kale kinaonekana kufundisha viwango na adhabu zitolewazo (kama vile Mt. 10:15; 11:22,24; 18:6; 25:21,23; Marko 12:40; Luka 12:47-48; 20:47; Yakobo 3:1). Angalia Mada Maalum katika 1 Kor. 9:24.

**3:9**
**NASB, NKJV " sisi tu wafanya kazi pamoja na Mungu"**
**NRSV" sisi tu watumishi wa Mungu, tufanyao kazi pamoja naye"**
**TEV" sisi ni ndugu, wafanyakazi pamoja na Mungu"**
**NJB" tunachangia katika kuifanya kazi ya Mungu"**
**REB"sisi ni wamoja katika huduma ya Mungu"**

Hizi tafsiri mbali mbali zinajaribu kuonyesha kwamba kazi ya Apolo na Paulo "kwa" Mungu, si kwamba wote ni wafanyakazi wa kazi tatu zile zile. Kipaumbele lazima kibaki na Mungu, si viongozi wa kibinadamu wa muda!
Aya hii inarejea juu ya Paulo na Apolo. Hii ni sitiari ya huko karibia na Mashariki ya familia yenye kufanyakazi shambani kwa pamoja (yaani 2 Kor. 6:1). Mstari huu una VIMILIKISHI miliki vitatu: Paulo na Apolo ni wa Mungu Baba, kama kanisa lilivyofanya huko Korintho.

◙ **"ninyi ni shamba la Mungu, ni jengo la Mungu"** Aya hii inalirejelea kanisa la Korintho. Paulo anatumia sitiari ya ukuaji wa kilimo (kama vile Isa. 61:3; Mt. 15:13) na ujenzi wa jengo (kama vile Efe. 2:20-22; Kol. 2:7; 1 Pet. 2:5) kutoa ufafanuzi unaolihusu kanisa. Kitheolojia lazima ikumbukwe kwamba kanisa ni watu, si jengo.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : 1 WAKORINTHO 3:10-15**
**[10]Kwa kadiri ya neema ya Mungu niliyopewa, mimi, kama mkuu wa wajenzi mwenye hekima, naliuweka msingi, na mtu mwingine anajenga juu yake. Lakini kila mtu na aangalie jinsi anavyojenga juu yake. [11] Maana msingi mwingine hakuna mtu awezaye kuuweka, isipokuwa ni ule uliokwisha kuwekwa, yaani, Yesu Kristo. [12]Lakini kama mtu akijenga juu ya msingi huo, dhahabu au fedha au mawe ya thamani, au miti au majani au manyasi, kazi ya kila mtu itakuwa dhahiri. [13]Maana siku ile itaidhihirisha, kwa kuwa yafunuliwa katika moto; na ule moto wenyewe utaijaribu kazi ya kila mtu, ni ya namna gani. [14] Kazi ya mtu aliyoijenga juu yake ikikaa, atapata thawabu. [15]Kazi ya mtu ikiteketea, atapata hasara; ila yeye mwenyewe ataokolewa; lakini ni kama kwa moto.**

**3:10 "Kwa kadiri ya neema ya Mungu niliyopewa"** Paulo anautetea wokovu, wito wake, na kipawa chake kama Mtume wa Mataifa (kama vile 1 Kor. 15:10).

◙ **"mkuu wa wajenzi mwenye hekima"** Hili pia lingeweza kumaanisha "msimamizi wa jengo" Hapa tupata neno la Kiingereza "msanifu majengo" kutona na neno hili la Kiyunani. Katika maana iliyopo Paulo anaitetea mamlaka yake kama Mtume aliyeitwa na Kristo kwa ajili ya Mataifa na mtu wa kwanza kuishirikisha injili kwa Wakorintho hawa.

◙ **"naliuweka msingi"** Aya hii inarejea juu ya mahubiri ya awali ya injili ya Paulo huko Korintho. Hili linaweza kuwa dokezo la Isa. 28:16. Yesu ndiye msingi!

◙ **"na mtu mwingine anajenga juu yake"** Paulo alianzisha kanisa, lakini wengine walichangia katika ukuaji wake. Apolo ni mfano (kama vile1 Kor. 3:5-9). Hata hivyo, katika muktadha huu hili lazima lihusiane na wale viongozi

waliomo ndani ya kanisa ambao waliunga mkono roho ya kuwepo kwa makundi madogo madogo yenye utengano. Hawa wanaweza kuwa viongozi wa makanisa tofauti ya nyumbani.

◙ **"kila mtu na aangalie"** Kiuhalisia hii ni KAULI TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO ya neno *blepō*, "Naona." Hili ni tahadharisho kwamba viongozi wa kanisa watatoa hesabu za kazi ya kanisa lao kwa Mungu, kama itakavyokuwa kwa waamini wote (kama vile 2 Kor. 5:10).

**3:11** Kuna sifa tatu zinazohusiana na kanisa zilizotajwa katika kifungu hiki.

1. ujumbe wa viongozi/waamini lazima uwe wa kitovu cha Kristo (kama vile 1 Kor. 3:11-12 na Efe. 2:20-21)
2. maisha ya viongozi/waamini lazima yawe na ufanano wa Kristo (kama vile 1 Kor. 3:12-15)

**3:12 "kama"** Huu ni mtirirko wa kwanza wa SENTENSI YENYE MASHARTI DARAJA LA KWANZA ambayo inadhaniwa kuwa ya kweli kutokana na mtazamo wa mwandishi au kwa ajili ya kusudi lake la kiuandishi (kama vile 1 Kor. 3:12,14,15,17,18). Kulikuwa na (na hata sasa wapo) viongozi wenye kuzaa matunda na wenye thamani na wenye kujeruhi na waharibifu!

◙ **"mtu akijenga juu ya msingi huo"** Swali kuu la kufasirika hapa ni hili ni msingi gani anaouzungumzia Paulo: (1) injili, 1 Kor. 3:11 au (2) lile kanisa lililoko huko Korintho, 1 Kor. 3:10? Je! Anawaelekeza viongozi au waamini kwa ujumla? Fasiri yake ya 1 Kor. 3:10-15 lazima ihusiane na 1 Kor. 3:16-17, ambayo inatoa ufafanuzi wa kanisa kama utimilifu na kama hekalu la Mungu.

◙ **"dhahabu au fedha au mawe ya thamani"** Msistizo uliopo hapa ni huu kitu gani kinadumu, urembo, na gharama na vile visivyoweza kuharibiwa kwa moto. Mawe ya thamani yana weza kuwa vito, mawe yenye thamani ndogo, mawe yaliyong'arishwa kwa marumaru.

**3:13**
**NASB " itaidhihirisha"**
**NKJV "itathibitisha"**
**NRSV "itakapoonekana"**
**TEV "itakapofichua"**
**NJB "itakapoonyeshwa"**

Udhihirisho huu wa wazi wa huduma ya mwamini au kiongozi (yaani, shauku, matendo, kusudi) unasisitizwa na marudio matatu fungamano ya VITENZI katika 1 Kor. 3:13.

1. kuwa dhahiri (yaani, *phainō*)
2. kuonyesha (yaani, *dēloō*)
3. kufunua (yaani, *apokaluptō*)

Maonyesho haya ya wazi na hukumu ya waamini lazima yahusiane na kiti cha hukumu cha Kristo katika 2 Kor. 5:10.

◙**"yafunuliwa katika"** Aya hii inarejea katika Kitabu cha Agano la Kale "Siku ya Bwana," ambayo itahusisha vyote yaani kutukuzwa na thawabu kwa waamini na hukumu kwa wale wasio amini. Hata hivyo, hata wale waaminio watatoa hesabu zao mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo (kama vile 2 Kor. 5:10; Mt. 12:36-37; 25:31 na kuendelea; Rum. 2:16; 14:12; Gal. 5:10; Efe. 13:17).

◙ **"moto"** Angalia Mada Maalum ifuatayo.

**MADA MAALUM: MOTO (SPECIAL TOPIC: FIRE)**

◙ **"utaijaribu"** Aya hii inarejea juu ya moto wa tanuru (kama vile1 Kor. 4:5), ambao hujaribu kwa lengo la kuthibitishwa (yaani, *dokimazō*).

## [MADA MAALUM: MANENO YA KIYUNANI YA NENO KUJARIBU NA MAANA ZAKE (SPECIAL TOPIC: GREEK TERMS FOR TESTING AND THEIR CONNOTATIONS)]

◙**"kazi ya kila mtu, ni ya namna gani"** Katika muktadha huu lazima aya hii irejee juu ya uhusika wa mtu ndani ya kanisa. Karama zote za kiroho ni kwa ajili ya kulijenga kanisa (kama vile 1 Kor. 12:7). Hakuna tofauti zo zote za kiroho kati ya wachungaji /makasisi wa kanisa na walei, kiongozi na mfuasi, bali kuna utofauti wa majukumuu (kama vile Hes. 16:3). Viongozi ni wawajibikaji (kama vile Yakobo 3:1).

**3:14 "ikikaa"** Hii aya ni ya pili katika mtirirko wa SENTENSI YENYE MASHARTI DARAJA LA PILI, inayodhaniwa kuwa ya kweli kutokana na mtazamo wa mwandishi au kutokana kusudi lake la kiuandishi (kama vile 1 Kor. 3:12,14,15,17,18).

◙**"atapata thawabu"** Kifungu hiki kinaamisha kutoa thawabu, si wokovu. Watu wote wanaoambiwa wanadhaniwa kuwa waamini!
Dhana ya Agano Jipya kuhusiana na thawabu lazima itofautishwe na wokovu kwa kuzibainisha faida (kama vile Rum. 6:23). Katika Agano la Kale neno thawabu au baraka yaliunganishwa na utii (kama vile Kumb. 11:13-32,27-29; Zaburi 1). Katika maana hii, hili bado liko sawa. Hata hivyo, wokovu ni neema, si thawabu.

Maisha ya imani na utii ni matokeo ya wokovu, si kwa ajili ya wokovu. Thawabu inaweza kupotezwa, bado wokovu ukatunzwa. Thawabu ni utambuzi wa huduma endelevu ya waamini. Sasa Paulo ameiweka katika mtazamo wa kiulimwengu tathmini yake ihusuyo matukio ya siku za mwisho (kiama) (kama vile 1 The. 2:19-20; Flp. 2:14-16) ili kuwajumuisha waamini wote. Thawabu ni njia ya kuwatambua wale waliokwisha kudhihirishwa katika namna ya kufaa na kwa uaminifu katika kuiendeleza injili. Thawabu ni vipawa vya Mungu kupitia kuuinua Ufalme wake. Bado, kama ulivyo uhusiano wa maagano yote, waamini lazima waitikie kwa ukubalifu na kwa uendelevu (kama vile 1 Kor. 9:24-27). Angalia [MADA MAALUM: VIWANGO VYA THAWABU NA ADHABU (SPECIAL TOPIC: DEGREES OF REWARDS AND PUNISHMENT)] katika 1 Kor. 9:24-27.

**3:15 "Kazi ya mtu ikiteketea"** Haswa, huzuni ya kutokuzaa matunda, ubinafsi, maisha ya Mkristo yenye utengano – huzuni kwa mtu, huzuni kwa kanisa, na huzuni kwa wale wasiokolewa!

◙ **"ila yeye mwenyewe ataokolewa"** Aya hii inaonyesha upendeleo wa neema hata uwezekano wa kuipoteza thawabu.
Dhana hii inaweza kujibu mkanganyiko wa kitheolojia wa wokovu huru katika neema ya Mungu, kazi ya Kristo iliyokwisha kumalizika, na maombolezo ya Roho yaliyotofautisha kila kitu kilichokuwa katika hukumu ya maisha ya Mkristo.

Naweza kuwa na woga wa kulitumia andiko hili kama dhana ya ufunguzi pekee kutokana na uchache wa Andiko katika namna ya kitheolojia ya neno "marudio," ya maneno umbo-mwili, Mkristo aliye kama mtoto yanavyotumika! Makanisa ya leo huitumia dhana hii kutoa maelezo katika namna isiyokutakiwa, katika hali ya kutojali, kanisa la kidunia, lakini kwa nadra Agano Jipya linafafanua hukumu ya ukuaji wa kiroho (kama vile Ebr. 5:11-14).

◙ **"ataokolewa"** Huu ni uelekeo wa matukio ya siku za mwisho. Angalia Mada Maalum hapa chini.

## [MADA MAALUM: WOKOVU (NJEO ZA VITENZI VYA KIYUNANI) (SPECIAL TOPIC: SALVATION (GREEK VERB TENSES)]

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : 1 WAKORINTHO 3:16-17**
**[16] Hamjui ya kuwa ninyi mmekuwa hekalu la Mungu, na ya kuwa Roho wa Mungu anakaa ndani yenu? [17]Kama mtu akiliharibu hekalu la Mungu, Mungu atamharibu mtu huyo. Kwa maana hekalu la Mungu ni takatifu, ambalo ndilo ninyi.**

**3:16 " Hamjui ya kuwa ninyi mmekuwa hekalu la Mungu"** Hapa hakuna KIAMBATA kilicho na neno "hekalu" (yaani, *naos*, katikati ya sehemu yenyewe iliyo takatifu). Hiki KIWAKILISHI cha neno "ninyi" ni wingi, ambapo "hekalu" ni UMOJA, kwa hiyo, katika muktadha huu "hekalu"lazima lirejelee juu ya kanisa zima la huko Korintho (kama vile 2 Kor. 6:16; Efe. 2:21-22), ambalo linaweza kuwa limehusishwa makanisa kadhaa ya nyumbani.

Mtazamo wa imani ya Kiyahudi uliendelezwa katika taratibu za Hekalu na liturujia (kanuni za ibada) (kama vileYeremia 7) badala ya imani katika YHWH. Hii si wapi au lini au ni kwa namna gani mtu huabudu, bali Nani mtu huyo anahusiana naye, Mungu. Yesu aliuona mwili wake kama hekalu la Mungu (kama vile Yohana 2:21) Yesu ni mkuu kuliko lile hekalu la Agano la Kale (kama vile Mt. 12:6). Kazi ya Mungu imesogea kutoka jengo takatifu hadi katika utakatifu (yaani, kuokolewa, utakatifu) wa miili ya waamini. Mtazamo wa kazi ya Mungu katika ulimwengu ni watu! Mwili wa Kristo sasa ni mahala, vyote viko katika hali ya umoja na ni vya kibinafsi.

◙**"ya kuwa Roho wa Mungu anakaa ndani yenu"** "Hukaa" NI KAULI TENDAJI ELEKEZI YA WAKATI ULIOPO. Neno "Yenu" ni WINGI. Dhana ya hekalu kama sehemu pekee ya kuishi ya YHWH katika Agano la Kale hapa inafanana na dhana ya lile kanisa kama mahala pa kuishi Roho Mtakatifu.
Hii dhana ya Uungu iishio ndani inarudiwa katika Agano Jipya. Nafsi zote tatu za Utatu zinazungumziwa kuwa zinaishi ndani ya waamini.

1. huyo Roho (kama vile Yohana 14:16-17; Rum. 8:9,11; 1 Kor. 3:16; 6:19; 2 Tim. 1:14)
2. huyo Mwana (kamavile Mt. 28:20; Yohana 14:20,23; 15:4-5; Rum. 8:10; 2 Kor. 13:5; Gal. 2:20; Efe. 3:17; Kol. 1:27)
3. wote Mwana na Baba (kama vile Yohana 14:23 na 2 Kor. 6:16)

**3:17 "Kama mtu akiliharibu hekalu la Mungu, Mungu atamharibu mtu huyo"** HII NISENTENSI YENYE MASHARTI DARAJA LA TATU, ambayo hudhani juu ya ukweli wa waamini wasio wa kiroho waiharibuyo kazi ya kanisa (yaani, viongozi au kazi). Hapa msistizo uko katika matendo ya mwamini binafsi. Hili haliuathiri wokovu wao, 1 Kor. 3:15, bali urefu na thawabu.

Huzuni kuu ya waamini waishio kwa ubinafsi, walioishi pasipo kuzaa matunda ni uwezekano wa vyanzo vya kuondoshwa kwao. Wao wanaijua injili; wanaye huyo Roho, bado wao wenyewe na kanisa linaathiriwa na matendo yao. Hapa ndipo Luka 12:48 huzungumza kama kipaza sauti! Hii inazungumza nawe?
Hili neno *phtheirō* (kuharibu) lina matumizi kadhaa katika Agano Jipya.

1. dhuru au chafua kimwonekano (yaani, matunda maovu au nyama iliyooza, hata kistiari neno hili linazungumzia kuwa na madhara kifedha)
2. dhuru au chafua kimaadili (yaani, kuvunja sheria za mashindano ya riadha au kumshawishi mtu kiuasherati)
3. kuangamiza
   a. kimwonekano/kimwili
   b. kiroho
   c. katika maisha ya umilele

Ni muktadha wa moja kwa moja peeke yanayoweza kubainisha maana halisi ya hili neno. Hapa vinatumika vishazi vyenye ufanano, lakini si yumkini ikiwa lina maana sawa katika kila kishazi kwa sababu marejeo ya kwanza yanalihusu na yale ya pili yanamhusu mtu. Katika muktadha huu hili neno linarejelea juu ya kuokolewa, lakini pasipo ukomavu, waamini wanaosababisha kukua kwa roho ya makundi madogo madogo yenye utengano katika kanisa la huko Korintho. Tazama Mada Maalumu katika 1 Kor. 15:42.

Ni vigumu kutoa ufafanuzi unaohusu maana ya neno "kuharibu" katika muktadha huu (kama vile Mt. 18:6; Luka 17:1-2; Rum. 14:15; 1 Kor. 5:5; 8:11; 1 Tim. 1:20).
Nikiwa katika somo hili, Mimi binafsi siliamini neno hili (na maneno yanayohusiana) kwa uhalisia linaweza kutumika katika kuhakikisha kuwaangamiza watu waliopotea (Fudge, *The Fire That Consumes*), lakini kwa namna fulani ya utambuzi wao, utengano na Mungu wa milele (yaani, jehanamu, kama vile Dan. 12:2; Mt. 25:46; Matendo 24:15).

Inawekana kwamba hata kile Paulo anachokizungumzia hapa kinahusiana na 1 Kor. 5:5 na 1 Tim. 1:20, ambapo kanisa humwadibisha yule aliye nje ya ushirika wake (lakini wenye tumaini la mara kwa mara na ombi la urejesho utofautishao toba).

◙**"hekalu la Mungu ni takatifu, ambalo ndilo ninyi"** Hii ni dhana ya pamoja. Ile iliyohusika na uingizwaji wa kimantiki ni kwamba muumini binafsi pia ni hekalu la Mungu (yaani 1 Kor. 6:19). Wakristo wanaitwa katika utakatifu (yaani Mt. 5:48; Efe. 1:4).

**MADA MAALUM: UTAKATIFU (SPECIAL TOPIC: HOLY)**

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 1 CORINTHIANS 3:18-23**
**[18] Mtu asijidanganye mwenyewe; kama mtu akijiona kuwa mwenye hekima miongoni mwenu katika dunia hii, na awe mpumbavu, ili apate kuwa mwenye hekima. [19] Maana hekima ya dunia hii ni upuzi mbele za Mungu. Kwa maana imeandikwa, Yeye ndiye awanasaye wenye hekima katika hila yao. [20]Na tena, Bwana anayafahamu mawazo ya wenye hekima ya kwamba ni ya ubatili. [21]Basi, mtu ye yote na asijisifie wanadamu. Kwa maana vyote ni vyenu; [22]kwamba ni Paulo, au Apolo, au Kefa; au dunia, au uzima, au mauti; au vile vilivyopo sasa, au vile vitakavyokuwapo; vyote ni vyenu; [23] nanyi ni wa Kristo, na Kristo ni wa Mungu.**

**3:18 "Mtu asijidanganye mwenyewe"** HII NI KAULI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO yenye KIAMBATA HASI, ambacho mara kwa mara humaanisha kustisha tendo lililotayari kwenye mchakato. Waamini wengine wa huko Korintho walijivunia ushirika wao wa ndani au wafuasi wa viongozi fulani/maarifa maalumu.

Hili neno "danganya" ni muundo uliochochewa na neno *apataō* (yaani Efe. 5:6; 1 Tim. 2:14; Yakobo 1:26) wenye kiambishi awali *ek* (yaani Rum. 7:11; 16:8; 2 The. 2:3). Hili neno lina ufanano na *planaō* (yaani, kupotea, kukengeuka, kupotea), ambalo linatumika kwenye vidokezo vya Injili , maandiko ya Yohana, na Paulo (yaani, 1 Kor. 6:9; 15:33 na VIVUMISHI katika 2 Kor. 6:8). Kujidanganya mwenyewe ni huzuni ya kiroho (yaani Rum. 12:16; Gal. 6:3; 2 Tim. 3:13; 1 Yohana 1:8). Paulo anaweza kuwa anadokeza Mit. 3:7 au Isa. 5:21 au hata Yer. 9:23-24. Kazi ya viongozi walio wengi waliofannya kazi huko Korintho walikuwa wakomavu na wenye hekima, lakini walikuwa wakijidanganya.

◙ **"kama"** Hii HII NI SENTENSI YENYE MASHARTI DARAJA LA TATU. Wengi waliokuwa katika kanisa la Korintho walijisifu na kujidhania kuwa wa kiroho au kuwa na karama za kiroho au maarifa. Mielekeo hii ni sawa na kile ambacho baadaye kilikuja kuitwa Mafunuo. Kihistoria hii si yumkini kama Korintho ilishawishiwa na kujitenga kwa wasomi wa Kiyunani walioendelea. Mfumo huu wa fikra (kiini cha uwili kati ya roho na vitu) haukuandikwa kwa ukamilifu hadi karne ya pili, huu ulikuwa uasi mkubwa wa kanisa la kwanza.

◙**"mtu akijiona kuwa mwenye hekima miongoni mwenu katika dunia hii"** Hii aya inarejea juu ya mtu anayedhani yeye kama mwanaume/mwanamke ni wa kipekee au amesimama imara. Katika kanisa kulikuwa na wale waliodai kuwa ukuu wao umeegemea juu ya hali yao ya kiroho, maarifa, msimamo wa kijamii, au akili nyingi. Hii inawezekana kwamba aya hii inarejea juu ya zile kazi za kundi la viongozi zilizotajwa katika 1 Kor. 1:12; 3:5,21.

◙**"na awe mpumbavu"** Hii ni KAULI YA KATI (chenye ushahidi) SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFU. Injili ya Mungu,Kristo Mwenywe, ndiyo hekima pekee ya kweli. Mara nyingi hili neno linatumika kueleza maana ya aya "hekima ya dunia hii" (kama vile 1 Kor. 1:18,27; na hapa). Hata Paulo analitumia katika 1 Kor. 4:10 kwa maana ya kejeli katika uhusianao wa Wakristo Korintho ambao walidai na kuichochea hekima ya mwanadamu. Angalia Mada Maalum: Maneno ya Watu Wapumbavu 1 Kor. 15:36.

**3:19 "hekima ya dunia hii ni upuzi mbele za Mungu"** Hii ni kwa sababu aya hii iliyoegemea juu ya ile hekima yenye mipaka, ya kidunia, finyu, maarifa yaliyoanguka (kama vile 1 Kor. 1:18,21,23,25). Ili kuifahamu maana ya neno hili "upuuzi" tazama 1 Kor. 1:25.

**3:19-20** Nukuu zifuatazo zilizobadilishwa kwa uchache zinatoka katika Ayubu 5:13 na Zaburi 94:11. Kwa neno "hila"tazama nukuu kamili katika 2 Kor. 4:2.

**3:21**
**NASB " mtu ye yote na asijisifie wanadamu"**
**NKJV "hivyo mtu ye yote asijitukuze kwa wanadamu"**
**NRSV "Basi, mtu asijivunie wanadamu"**
**TEV "na asiwepo ye yote, hata, anayepaswa kujivuna juu ya yale wawezayo kufanya wanadamu"**
**NJB "hivyo haipaswi kujivuna juu ya wanadamu"**

Hii inaweza kuwa hata dokezo la Yer. 9:23-24. Kujivuna kwa mwanadamu kumetajwa mara kadhaa katika 1 Kor. (kama vile 1 Kor. 1:29,31; 3:21; 4:7; na 2 Kor. 5:12; 10:17; 11:12,18,30; 12:1,5,6,9). Tazama Mada Maalumu katika 1 Kor. 5:6. Hili lilikuwa tatizo kubwa katika Korintho (na la wanadamu kwa ujumla). Tatizo hili lilihusisha kanisa zaidi kuliko viongozi wachache; pia wafuasi wanawajibika. Hii huwa na maana sana kama kile kiburi cha madhehebu ya sasa na majivuno (yaani, Mimi ni wa Calvin; Mimi ni wa Wesley; Mimi ni wa . . ., kama vile 1 Kor. 4:6).

**3:21b-22** Paulo anadai kwamba vitu vyote (yaani, orodha ndefu kama ile ya Rum. 8:38-39) inahusika na waamini kupitia Kristo wakiwemo wahubiri wote walioorodheshwa. Hili neno *kosmos* (yaani, ulimwengu) hapa linatumika katika maana chanya ya mpangilio wa uumbaji (kama vile LXX wa Mwa. 1:31). Waamini ni warithi mojawapo wa vitu vyote na nyakati zote kupitia Kristo (yaani Rum. 8:12-17). Usijiwekee mipaka mwenyewe.

**MADA MAALUM: MATUMIZI YA PAULO YA NENO *KOSMOS* (ULIMWENGU) (SPECIAL TOPIC: PAUL'S USE OF KOSMOS (WORLD)**

**3:23 "nanyi ni wa Kristo"** Hili neno "nanyi" ni la mkazo na ni WINGI. Hii inaonyesha nafasi ya kutukuzwa kwa Kristo ndani ya kanisa (yaani 1 Kor. 1:29-31). Hii inaelekea hadi kwenye jukumu lao kama waamini.

◙**"Kristo ni wa Mungu"** Aya hii inarejea juu ya maisha ya unyenyekevu ya Kristo kwa Baba (kama vile 1 Kor. 11:3; 15:28). Hili si sual la asili (kama vile Yohana 1:1-3), bali suala la kazi. Utatu (tazama Mada Maalum katika 1 Kor. 2:10) ni uelekeo wa kazi.

## MASWALI YA MJADALA

Haya ni maoni na mwongozo wa kujisomea, ambao una maana kuwa, wewe unawajibika kwa tafsiri yako binafsi ya Biblia. Kila mmoja wetu anapaswa kutembea katika mwanga tulionao. Wewe, Biblia na Roho Mtakatifu ndiyo vipaumbele katika kutafsiri. Usimwachie kazi hii mtoa maoni tu.

Maswali haya ya majadiliano yanatoa tu, msaada wa wewe kufikiria kupitia masuala nyeti ya sehemu ya kitabu hiki. Yamekusudiwa kuwa ya kukuchokonoa/kuchokoza akili, na yasiyo na ukomo

1. Nini tofauti kati ya maziwa na chakula kigumu kama inavyohusiana na mahubiri ya Mkristo?
2. Je! Wakristo watasimama mbele za Mungu katka hukumu? Ikiwa ni hivyo, kwa nini?
3. Nani anaelezwa katika 1 Kor. 3:10-15?
4. Je! 1 Kor. 3:16 waamini binafsi au wafuasi wa kanisa?
5. Neno"kuharibu" linamaanisha nini katika 1 Kor. 3:17? Je! Linahusianaje na 1 Kor. 3:15?
6. Je!Usaidizi wa Kristo kwa Baba, ambao unaoneka dhahiri katika 1 Kor. 3:23 na 15:28, unamaanisha kwamba yeye si Uungu?

# 1 WAKORINTHO 4

| MGAWANYO WA AYA WA TAFASIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **UBS[4]** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB** |
| Huduma ya Mitume | Watumishi wa siri za Mungu | Matumizi | Mitume wa Kristo | Hitimisho<br>(3:18-4:13) |
| 4:1-5 | 4:1-5 | 4:1-5 | 4:1-5 | 4:1-5 |
| | Kughiribiwa kwa ajili Ya Kristo | | | |
| 4:6-13 | 4:6-13 | 4:6-7<br>4:8-13 | 4:6-7<br>4:8-13 | 4:6-13 |
| | Malezi ya kibaba ya Paulo | Kuasa na kuonya kwa Kibaba | | Hali ya kusihi |
| 4:14-21 | 4:14-21 | 4:14-21 | 4:14-17<br>4:18-21 | 4:14-17<br>4:18-21 |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (Kutoka "**Mwongozo wa Usomaji Mzuri wa Biblia**"**A Guide to Good Bible Reading**")

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Haya ni maoni ya mwongozo kwa kujisomea, ikiwa na maana kuwa unawajibika binafsi kwa tafsiri ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mtoa maoni tu.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa,lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

13. Aya ya kwanza
14. Aya ya pili
15. Aya tatu
16. N.k

## MAELEZO FASAHA YA SURA YA 4

A. Mistari 1-5 inahusika na hukumu ya Wakristo na kuhukumiwa.
B. Mistari ya 1-6 inatofautisha majivuno ya viongozi wa Kikorintho na mitume wa kweli.
C. Katika mistari ya 14-21 Paulo anaongelea juu ya mamlaka yake na mipango yake wazi ya safari mbele ya madai ya wapinzani wake.

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : 1 WAKORINTHO 4:1-5**

**[1] Mtu na atuhesabu hivi, kuwa tu watumishi wa Kristo, na mawakili wa siri za Mungu. [2] Hapo tena**

**inayohitajiwa katika mawakili, ndiyo mtu aonekane kuwa mwaminifu. [3]Lakini, kwangu mimi, si kitu kabisa nihukumiwe na ninyi, wala kwa hukumu ya kibinadamu, wala sijihukumu hata nafsi yangu. [4]Maana sijui sababu ya kujishitaki nafsi yangu, lakini sihesabiwi haki kwa ajili hiyo; ila anihukumuye mimi ni Bwana. [5] Basi ninyi msihukumu neno kabla ya wakati wake, hata ajapo Bwana; ambaye atayamulikisha yaliyositirika ya giza, na kuyadhihirisha mashauri ya mioyo; ndipo kila mtu atakapoipata sifa yake kwa Mungu.**

**4:1**"**Mtu na atuhesabu hivi"** Hii ni KAULI YA KATI (yenye ushahidi) SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO. Waamini lazima watathimini au kufikiria hadhi ya uongozi. Kwa ajili ya Ufalme wa Mungu, uongozi ni utumishi/uwakili (k.v Marko 10:42-44). Thiolojia ya Paulo inafuatisha maneno ya Yesu.

◙"**watumishi wa Kristo"** Agalia Mada Maalum hapa chini

## MADA MAALUM: UONGOZI WA KITUMISHI (SPECIAL TOPIC: SERVANT LEADERSHIP)

◙"**mawakili"** Huu ni muunganiko wa neno la Kiyunani "nyumba" na "sheria." Mhudumu ndiye aliyetunza nyumba/shamba na kutoa taarifa kwa mmiliki (yaani, neno katika Mt. 25:14-46; Luk. 16:1, na dhana ya "kuteua" "kile kilichopangwa kwa ajili ya mtu fulani"). Huu ni msisitizo juu ya uwajibikaji na uaminifu wa injili (Kama vile 1 Kor. 4:2; 4:1; 9:17; Kol. 1:25; 1 The. 2:4; Tit. 1:7; 1 Petr. 4:10). Mungu atawahukumu watumishi wake (kama vile 1 Kor. 4:4,5; 3:13). Ni upendeleo na wajibu wa namna gani!

◙"**wa siri za Mungu"** Neno hili linatumiwa na Paulo katika njia kadhaa na tofauti tofauti. Msukumo wa msingi unaonesha kuwa Mungu pekee ndiye atakayewaunganisha Wayahudi na watu wa Mataifa katika familia moja kupitia Kristo, kwa kufanya hivyo anatimiza andiko la Mwa. 3:158 na 12:3. Angalia Mada Maalum: Fumbo katika 1 Kor. 2:1

◙ "**Ndiyo mtu aonekane kuwa mwaminifu"** Hiki ni KIWAKILISHI cha neno *pistol.* Yesu alitumia dhana ya Mtumishi mwaminifu katika Mt. 24:45; 25:21,23!

## MADA MAALUM: KUAMINI, SADIKI, IMANI NA UAMINIFU KATIKA AGANO LA KALE (SPECIAL TOPIC: BELIEVE, TRUST, FAITH, AND FAITHFULNESS IN THE OLD TESTAMENT)

◙"**Lakini, kwangu mimi, si kitu kabisa nihukumiwe na ninyi"** Paulo alikuwa chini ya mavamizi binafsi toka kwa kundi fulani (yaani, watoto wachanga katika Kristo, kama vile 1 Kor.3:1, au hata upinzani wa Wayahudi unaofanana na ule wa wale Washika desturi za Kiyahudi wa Wagalatia) kule Korintho. Fikra zao juu ya gharama ya kitume halikuwa jambo la kutilia maanani (bado yalikuwa maumivu). Alihusika kuhusu namna gani watu wanaiona injili na kanisa (kama vile 1 Kor. 8:13; 9:19-23; 10:23,33; 2 Kor. 4:2; 5:11; Rum. 14:1-15:13).

◙"**wala kwa hukumu ya kibinadamu"** Hii kihalisia ni "hukumu ya kibinadamu." Inarejea juu ya utaratibu ya hukumu ya kibinadamu kama ilivyo 3:13 inavyorejea juu ya utaratibu wa hukumu ya "ki-Ungu" ile siku ya mwisho (kama vile 1 Kor. 1:8; 5:5). Kama ilivyo 4:3a inavyorejerea juu ya neno *sarkinois* (yaani, waumini wachanga wa 1 Kor.3:1). Kifungu hiki kinarejea juu ya *psuchikos* (yaani, watu wa asili wasio na Roho) katika 1 Kor. 2:14.

◙"**wala sijihukumu hata nafsi yangu"** Ni vigumu kuweza kuchunguza kwa usahihi ukiroho wa mtu. Mara nyingi waumini ni wagumu juu yao wenyewe na wepesi kwa wengine. Mara nyingi tunajilinganisha sisi wenyewe na watu wengine (kama vile 2 Kor. 10:12-18). Lazima tumwachie Mungu ahukumu mwenyewe (k.v 1 Kor. 4:5). Yeye anaujua moyo na matukio ya mtu (kama vile 1 Sam. 16:7; 1 Fal. 8:39; 1 Nya. 28:9; Yer. 17:10; Lk. 16:15; Mdo. 1:24).

**4:4**“**Maana sijui sababu ya kujishitaki nafsi yangu”** Kabla ya Paulo kuongoka alifikiria namna gani kuhusu uhusiano wake na sheria za Musa (kama vile Mdo. 23:1; Flp. 3:5-6). Roho ilifunua matamanio yake (kama vile Rum. 7:7) na Paulo aliongoka toka dhambini na kuitikia katika neema ya Mungu kupitia Kristo pekee (kama vile Rum. 3:19-26). Aliishi na kutumika katika neema kama mtumishi. Katika fumbo la neema ya bure, lakini utumishi wa kuajibika, alikuwa na dhamira iliyojaa amani, lakini hakimu wa ki-Ungu pekee katika muundo wa mambo ya siku ya mwisho aweza kufanya sawa

**NASB, NRSV"kuachiliwa pasipo kosa"**
**NKJV"kuhesabiwa haki"**
**TEV"kutokuwa na hatia"**
**NJB"kumhesabia haki”**

Hii ni KAULI TIMILIFU TENDWA INAYO ARIFU. Hili ni neno la kiufundi la kisheria kwa mtu kuachiliwa huru kutokana na matokeo ya kufanya kosa (kama vile Rum. 3:24). Kithiolojia hili linafanana na “hakuna hukumu” katika Rum. 8:1 na muktadha wa kisheria wa Rum. 8:31-35. Katika muktadha huu inamaanisha kuwa Paulo hayuko huru toka kwenye hukumu ya ki-Ungu (kama vile 2 Kor.5:10) kwa sababu tu dhamira yake ilikuwa sawa.

◙ “**ila anihukumuye mimi ni Bwana”** Watumishi watatoa hesabu zao juu ya uaminifu wao (kama vile. 1 Kor. 4:2; 3:11; 2 Kor. 5:10; 10:18).

**4:5**
**NASB, NKJV,**
**NRSV"Kwa hiyo"**
**TEV"Hivyo"**
**NJB"kwa sababu hiyo"**

Huu ni uhitimisho wa mazungumzo ya Paulo juu ya somo hili na ni amri kwa wale watu wachanga watoao tathimini.

◙“**Basi ninyi msihukumu neno kabla ya wakati wake”** Hii ni KAULI TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO yenye KIAMBATA HASI, ambayo mara nyingi humaanisha kuzuia tendo ambalo tayari lipo kwenye mchakato (kama vile Mt. 7:1-5). Haya makundi madogo madogo au washabiki wa walimu wa uongo walikuwa tayari wamemhukumu Paulo. Paulo lazima alikuwa amepata wakosoaji wengi huko Korintho kwa miaka yote (kama vile 2 Kor.10-12)

◙**“hata ajapo Bwana”** Kurudi kwa mara ya Pili kunajulikana; lakini muda na namna gani haijulikani. Tathimini ya kweli lazima ingoje mpaka wakati muafaka (kama vile Mt. 13:24-30, 36-43).

◙“**hata ajapo Bwana; ambaye atayamulikisha yaliyositirika ya giza”** Hata waamini watatoa hesabu zao juu ya mienendo yao, mipango na tabia (kama vile 1 Kor. 3:13; Yohana 3:17-21; Rum. 2:16; 2 Kor. 5:10), lakini tushukuru Mungu, si dhambi zao! Paulo anatumia neno hili hili “vitu vya sirini” (*krupta*) mara kadhaa.

1. Warumi 2:16-“mambo ya sirini ya watu”
2. 1 Wakorintho 4:26-“mambo yaliyositirika ya giza”
3. 1 Wakorintho 14:25- “mambo yaliyo sirini ya moyoni”
4. 2 Wakorintho 4:2-“mambo yaliyo sirini ya aibu”

◙“**ambaye atayamulikisha yaliyositirika ya giza”** Hili ni la muhimu. Hii ndio sababu Mungu pekee aweza kuhukumu pasipo upendeleo. Waamini wanawajibika tu kwa yale wanayoyatambua, lakini mara zote wanawajibika kwa mienendo na tabia zao. Wale waaminifu ndio watazawadiwa (kama vile 1 Kor. 3:8,14,15), Wale walio waaminifu watapokea thawabu (kama vile 1 Kor.3:16-17). Angalia MADA MAALUM: MOYO (SPECIAL TOPIC: THE HEART) katika 1 Kor. 14:25

◙"**Ndipo kila mtu atakapoipata sifa yake kwa Mungu"** Hii ni mada inayojirudia (kama vilea Ayubu.34:11; Zab. 62:12; Wimb. 12:14; Yer. 17:10; 32:19; Mt. 16:27; 25:31-40; Rum. 2:16; 14:12; 1 Kor. 3:8; 2 Kor.5:10; 1 Petr. 1:17; Ufu. 2:23; 20:12; 22:12) yenye kuegamia katika kanuni za Gal.6:7

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) :1 WAKORINTHO 4:6-7**

**6 Basi ndugu, mambo hayo nimeyafanya kuwa mfano wa mimi na Apolo kwa ajili yenu, ili kwamba kwa mfano wetu mpate kujifunza kutokupita yale yaliyoandikwa; ili mmoja wenu asijivune kwa ajili ya huyu, kinyume cha mwenziwe. 7 Maana ni nani anayekupambanua na mwingine? Nawe una nini usichokipokea? Lakini iwapo ulipokea, wajisifia nini kana kwamba hukupokea?**

**4:6**

**NASB "Mambo haya nimeyafanya kwa mfano wa Mimi na Apollo"**
**NKJV "yamebadilishwa kwa mfano"**
**NRSV, TEV,**
**NJB "yamefanyika"**

Hili neno la Kiyunani "yamefanyika kwa mfano" (yaani, *meteschēmatisa*, ambayo ni KAULI TENDAJI YENYE KUARIFU YA WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFU) ni gumu kuliitafasiri katika muktadha huu. Katika muktadha wa mazingira mengine, Wafilipi 3:21, IRABU TENDAJI inamaanisha "kubadili" na katika 2 Kor. 11:13-15, IRABU YA KATI inamaanisha "kuficha ukweli." Wazo la msingi ni kubadili jozi ya matukio toka kundi moja hadi kundi jingine. Paulo anajitumia mwenyewe na Apollo kama mfano wa kuigwa kwa viongozi wote.

**NASB "kwa mfano wetu mpate kujifunza kutopita yale yalioandikwa"**
**NKJV "ili mpate kujifunza kutofikilia zaidi kuliko kile kilichoandikwa"**
**NRSV "kwa mfano wetu mpate kujifunza maana ya msemo "zaidi ya kile kilichoandikwa'"**
**TEV "kuzichunguza sheria zilizo sahihi"**
**NJB "kuliko zaidi ya kile kilichoandikwa"**

Hiki kifungu "imeaandikwa" kimetumika mara kwa mara katika Agano Jipya kuzitambulisha nukuu za Agano la Kale. Hapa kinaonekana kutambulisha mithali inayofahamika sana. Fasiri zinazowezekana ni

1. utangulizi wa nukuu itokanayo na Agano la Kale (kama vile 1 Kor.1:19;31; 3:19)
2. msemo wa kikosi kimoja miongoni mwa yale makundi madogo madogo katika Korintho
3. kuzichunguza sheria zilizo sahihi" (yaani, waamini wanatakiwa kuishi kufuatana na maandiko:
   a. hasa yale ambayo Paulo ameyanukuu katika sura ya 1-3
   b. kutokwenda zaidi ya Maandiko kama baadhi ya walimu wa uongo wa Kiyahudi)

**NASB" ili mmoja wenu asijivune kwa ajili ya huyu, kinyume cha mwenziwe"**
**NKJV" ili mmoja wenu asijekuwa na kiburi kwa ajili ya huyu, kinyume cha mwenziwe"**
**NRSV" ili mmoja wenu asijekuwa na kiburi kwa ajili ya upendeleo, kinyume cha mwenziwe"**
**TEV" ili mmoja wenu asijivune kwa ajili ya huyu, na kuwadharau wengine"**
**NJB"ili asiwepo mmoja wenu atakayejiona wa maana na kujilinganisha na maumivu ya mwingine"**

Hili neno la Kiyunani *phusioō* kwa asili yake linamaanisha kuongeza kitu fulani (yaani, Robertson, *Word Pictures in the New Testament*, uk. 105, na Vincent, *Word Studies*, uk. 766 toka *phusa* - miungurumo). Hili lilikuja kuanza kutumika katika fasihi ya Kikristo (yumkini lilibuniwa na Paulo) kisitiari kwa maana ya kiburi au kujivuna. Hili lilikuwa tatizo kubwa la kiroho kwa kanisa la Korintho. Paulo analitumia neno hili katika 1 Kor. 4:6,18,19; 5:2; 8:1; 13:4 na katika orodha ya dhambi katika 2 kor. 12:20. Hili kipekee linatumika nje ya nyaraka za Wakorintho katika Agano Jipya katika Kol. 2:18, pale linaporejea juu ya maono ya Mafunuo ya maarifa maalumu.

Waamini hawapaswi kuchagua kwa majivuno waalimu fulani dhidi ya waalimu wengine. Hawa lazima wawahukumu wapiga mbiu kwa maudhui ya jumbe zao (1 Yohana 4:1-6) na mifumo yao ya maisha (Mt. 7:1 na kuendelea), sio kwa namna ya kujiwasilisha kwao wala utanashati wao wala kwa upendeleo wao binafsi wala si kwa viongozi wanaodai ni wa kwao (yaani, udini).

**4:7**
**NASB"nani anayekupambanua na mwingine"**
**NKJV"naam nani anayekutofautisha na mwingine"**
**NRSV"Nani amekupendelea wewe?"**
**TEV"Nani akikufanya uwe zaidi kuliko wengine"**
**NJB"Nani alikufanya wewe uwe wa muhimu"**

KIWAKILISHI "wewe" na vitenzi vyote viko katika UMOJA katika 1 Kor. 4:7, lakini bado kinaonekana kuwa na mazingira ya "mmoja kati yenu." UWINGI wa "wewe" unaendelea katika 1 Kor.4:8.

Neno ambatano la Kiyunani *diakrinō* linatumika mara nyingi katika 1 Wakorintho na katika maana kadhaa.

1. kupendelea au kuondoa ukubwa (kama vile 1 Kor. 4:7)
2. kuhukumu (kama vile 1 Kor. 6:5)
3. kuweka utofauti (kama vile 1 Kor. 11:29)
4. kuchunguza (kama vile 1 Kor. 11:31; 14:29)
5. kutambua (muundo wa nomino *diakrisis*, kama vile 1 Kor. 12:10)

Uambatano unaohusiana na neno *anakrinō* unatumika katika 1 Kor. 2:15 (mara mbili); 4:3,4 na 14:24. Mchakato wa tathmini halisi kati ya waamini na viongozi na kati ya viongozi na viongozi ulikuwa wa muhimu kwa kanisa la Korintho. Mfumo wa swali /jibu hili ni njia dhahili ya mafundisho ya Paulo inayojulikana kama "makemeo." Huu ni wa kawaida katika Agano la Kale (kama vile Malaki) na mbinu za Mafundisho ya dini ya Kiyahudi. Paulo anaonekana kueleza viongozi wa makundi madogo madogo wanaojivuna (makanisa ya nyumbani).

◙ **"Nawe una nini usichokipokea"** Paulo unawakumbushia hawa viongozi wenye majivuno kuwa wao hawakuwa waanzilishi au wavumbuzi wa ile kweli, bali wapokeaji wa huduma za wengine.

◙**"ikiwa"** Hii ni SENTESI MASHARTI DARAJA LA KWANZA, ambayo inasadikiwa kuwa kweli kutokana na mtazamo wa mwandishi au kusudio lake la kifasihi. Hili ni swali la tatu la kisitiari la 1 Kor. 4:7. Baadhi ya viongozi na wafuasi wao walikuwa wakitenda kama vile wao walikuwa chanzo cha ukweli walioutangaza. Tatizo lingine la Wakorintho lilikuwa majivuno ya kibinadamu (kama vile 1 Kor. 1:29,31; 3:21; 4:7; 13:4). Angalia Mada Maalum katika 1 Kor. 5:6.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : 1 WAKORINTHO 4:8-13**

**8 Mmekwisha kushiba, mmekwisha kupata utajiri, mmemiliki pasipo sisi. Naam, laiti mngemiliki, ili sisi nasi tumiliki pamoja nanyi! 9 Maana nadhani ya kuwa Mungu ametutoa sisi mitume mwisho, kama watu waliohukumiwa wauawe; kwa sababu tumekuwa tamasha kwa dunia; kwa malaika na wanadamu. 10 Sisi tu wapumbavu kwa ajili ya Kristo, lakini ninyi ni wenye akili katika Kristo; sisi tu dhaifu, lakini ninyi mna nguvu; ninyi mna utukufu, lakini sisi hatupati heshima. 11 Hata saa hii ya sasa, tuna njaa na kiu, tu uchi, twapigwa ngumi, tena hatuna makao; 12 kisha twataabika tukifanya kazi kwa mikono yetu wenyewe. Tukitukanwa twabariki, tukiudhiwa twastahimili; 13 tukisingiziwa twasihi; tumefanywa kama takataka za dunia, na tama ya vitu vyote hata sasa.**

**4:8-13** Hii ni kejeli ya kushangaza!

**4:8**
**NASB"Mmekwisha kushiba"**
**NKJV"tayari mmekwisha shiba"**
**NRSV"Tayari mmeshakuwa na vyote mlivyohitaji"**
**TEV"mmekuwa na vyote mlivyohitaji"**
**NJB"mmekuwa na vyote"**

KIWAKILISHI "ninyi" Ni UWINGI katika 1 Kor. 4:8,10. Hili neno"kushiba" kawaida linatumika kwa tendo la kula kimwili (kama vile Mdo. 27:38), lakini hapa ni sitiari (kama vile Mt. 5:6) ya majivuno ya kiroho. Mstari wa 8 unaweza kuwa na maswali matatu (kama vile toleo la TEV) au semi tatu (kama vile NASB, NKJV, RSV na REB). Hii

ni milolongo ya maelezo ya kejeli au maswali ambayo yanafunua kiburi cha viongozi wa makundi madogo madogo ya Wakorintho. Hawa wanafikiria kana kwamba wamekwishafika (yaani, KAULI TIMILIFU TENDEWA ZENYE MAFUMBO). Paulo aliviitamani walivyokuwa navyo, lakini haikuwa kweli; matendo yao yalikifunua kiwango cha ukomavu wao (yaani, watoto wachanga katika Kristo)

◙**"Mmemilki…ili mmngeiliki"** Paulo anatumia taswira ya matukio ya siku za mwisho kuwashtua viongozi wenye majivuno na wasioridhika. Katika Kristo waamini wote watatawala pamoja na Mfalme Yesu, lakini ni baada ya kuja mara ya pili tu. Viongozi hawa walichukulia wenyewe kama wanatawalawaliokwisha tawala, wakiongea mambo ya rohoni.

**4:9"Mungu ametutoa sisi mitume mwisho, kama watu waliohukumiwa wauawe"** Mstari huu ni kielelezo kilichochukuliwa toka kwenye sherehe na ibada za kidini huko Rumi baada ya ushidi (kama vile Kol. 2:5), ambapo wafungwa waliopatikana na hatia (yaani, baadaye wakauwawa katika uwanja wa kimaonyesho wa Kirumi, kama vile 1 Kor. 15:32) walionyeshwa mwishoni katika gwaride la ushindi la Kirumi.

## MADA MAALUM: UPELEKWA *(APOSTELLŌ)* SPECIAL TOPIC: SEND (*APOSTELLŌ*)

◙**"Tumekuwa tamasha kwa dunia; kwa malaika na wanadamu"** Paulo anarejea juu ya kazi ngumu ya kuihubiri injili (kama vile 2 Kor. 4:7-12; 6:3-10; 11:23-30). Kifungu "kwa malaika" chaweza kuhusishwa na Waefeso 2:7; 3:10. Mungu amejidhihirisha mwenyewe kwenye ulimwengu wa kimalaika kwa matendo yake dhidi ya mwanadamu (kama vile 1 Pet. 1:12)

**4:10"Sisi tu wapumbavu kwa ajili ya Kristo"** Hekima ya Mungu ni upuuzi kwa ulimwengu, hata wakati mwingine kwa Wakristo wenye majivuno. Kwa "wapumbavu" angalia muhtasari katika 1 Kor. 1:25 na Mada Maalum katika 1 Kor. 15:36.

◙ **" lakini ninyi ni wenye akili katika Kristo; sisi tu dhaifu, lakini ninyi mna nguvu"** Hii ni kejeli inayoendelea toka 1 Kor. 4:7-9

◙ **"Dhaifu"**Angalia MADA MAALUM: UDHAIFU (SPECIAL TOPIC: WEAKNESS) katika 2 Kor.12:9.

**4:11** "**Hata saa hii ya sasa, tuna njaa na kiu, tu uchi, twapigwa ngumi, tena hatuna makao"** Mistari hii inaurejelea ule uzoefu wa Paulo (kama vile 2 Kor. 4:7-12; 6:3-10 na 11:23-30, pia angalia Waebrania 11:34-38). Yeye aliandika 1 Wakorintho akiwa Efeso.

4:**12 "kisha twataabika tukifanya kazi kwa mikono yetu wenyewe"** Hii inaaksi misisitizo ya Kiyahudi juu ya usahihi wa kazi ya mikono (kama vile Mdo. 18:3; 20:34; 1 The. 2:9; 2 The. 3:8). Hii ilishushwa hadhi na tamaduni za Kiyahudi, ikijumuishwa na kanisa la Korintho.

◙ **"Tukitukanwa twabariki"** Paulo anaaksi mafundisho ya Yesu (kama vile Mt. 5:10-12; 1 Pet. 2:23). Neno "kutukanwa" (yaani, *loidoreō*) pia limejumuishwa kwenye orodha ya dhambi katika 1 Kor. 5:11 na 6:10 (yaani, *loidoros*). Vincent, *Word Studies*, anasema neno hili linarejea matusi binafsi ya maneno, wakati neno "kashifiwa" (yaani, *dusphēmeō*, kama vile 1 Kor. 4:13) inamaanisha kashfa ya wazi (kama vile 1 Kor. 4:13; 2 Kor. 6:8). sijawahi weza kuthibitisha utofauti huu. Yote ni sehemu ya herufi kubwa ya maneno ya lugha ya kawaida ya Koine iliyotumika katika namna ya ki-elimu ya maana ya neno "kutukana na kashifiwa" (kama vile Louw na Nida, *Greek-English Lexicon*, juzuu. 1, kur. 433-434). Paulo anakabiliwa na maneno ya kashfa toka kwa walimu wa uongo, lakini lilikuwa ni kanisa la Korintho ambalo lilimshangaa zaidi. Kundi la watu ambalo binafsi aliliongoza kwa Kristo likawa lenye kumkashfu zaidi.

**4:13 "patanisha"** Angalia muhtasari mzima kwenye 2 Kor.1:4-11

**NASB" tumefanywa kama takataka za dunia, na tama ya vitu vyote hata sasa"**
**NKJV" tumefanywa kama takataka za dunia, na tukisafisha vitu vyote hata sasa"**
**NRSV" tumefanywa kama takataka za dunia, makapi ya vitu vyote"**
**TEV"Sisi si kitu zaidi ya takataka ya dunia, watu wasio na thamani duniani"**
**NJB"tunatendewa hata sasa kama makapi ya dunia, yenye thamani ndogo"**

Aya hii (1 Kor. 4:8-13) inaonyesha maumivu binafsi ya Paulo yaliyohusiana na kipindi cha kuihubiri injili. Alijisikia kufedheheshwa na kukataliwa sio tu na wale wasio amini, lakini pia na viongozi wa Kikorintho wenye majivuno.

Kifungu cha kwanza "watu duni kabisa" inarejea juu ya kile kilichobaki juu ya vyombo baada ya kusafisha vyombo vya jikoni. Kiuhalisia ni "kusafisha pande zote ndani na nje." Katika kuvielezea hivi visawe vichache swali la mwanzo la Paulo kistiari ni la msingi.

1. Kama anatumia Agano la Kale kama lilivyoelezewa katika tafasiri ya Kiyunani, ya maandiko ya kale, andiko hili linatumika kwa kusafisha kikamilifu na kwa hali hiyo linalipa fidia ya mtu (kama vile Mit. 21:18). Bauer, Arndt, Gingrich, na Danker's *Greek/English Lexicon*, uk. 647, na A. T. Robertson's *Word Pictures*, uk. 108, anashauri inaweza kueleweka kama "mbuzi wa kafara," yumkini katika matumizi yake katika kitabu cha Tobiti 5:19
2. Kama anatumia usuli halisi wa Kiyunani maneno yote mawili katika 1 Kor. 4:13 ni visawe vya yale yalioondolewa kwa kujisafisha kikamilifu.
3. Kama anayatumia kisitiari kwa hiyo yote kimsingi yanarejea juu ya unyenyekevu (kama vile Bauer, Arndt, Gingrich, na Danker's *Greek/English Lexicon*, uk. 653).

Kifungu cha pili "makapi ya vitu" pia linarejea juu ya vile ambavyo vimekwanguliwa na kupangusa wakati wa mchakato wa kukisafisha. Maneno haya mawili ni visawe. Ni maneno yenye nguvu, lakini yalikuwa yakitumika kama nahau. Yumkini ni ya nguvu na ya kupendeza kwetu kwa vile ni maneno haba. Yalisaidia kumuimalisha Paulo kutokana na kejeli alizozipata.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : 1 WAKORINTHO 4:14-21**
**[14] Siyaandiki hayo ili kuwatahayarisha; bali kuwaonya kama watoto niwapendao. [15]Kwa kuwa ijapokuwa mna waalimu kumi elfu katika Kristo, walakini hamna baba wengi. Maana mimi ndimi niliyewazaa katika Kristo Yesu kwa njia ya Injili. [16] Basi, nawasihi mnifuate mimi. [17] Kwa sababu hii nimemtuma Timotheo kwenu, aliye mwanangu mpendwa, mwaminifu katika Bwana, atakayewakumbusha njia zangu zilizo katika Kristo, kama vile nifundishavyo kila mahali katika kila kanisa. [18] Basi wengine wamejivuna kana kwamba siji kwenu. [19]Lakini nitakuja kwenu upesi, nikijaliwa, nami nitafahamu, si neno lao tu waliojivuna, bali nguvu zao. [20]Maana ufalme wa Mungu hauwi katika neno, bali katika nguvu. [21] Mnataka vipi? Nije kwenu na fimbo, au nije katika upendo na roho ya upole?**

**4:14** "**Siyaandiki hayo ili kuwatahayarisha"** Mistari ya 8-13 zimekuwa na upigaji wa vijembe. Paulo anahisi wanastahili kuabishwa (kama vile 1 Kor. 6:5; 15:34). Haijulikani kama aya hii (yaani, 1 Kor. 4:14-24) inaelekeza huko nyuma (yaani, sura ya 1-4) au mbele. Wana mengi ya kuyaonelea aibu.

◙ "**bali kuwaonya kama watoto niwapendao"** Paulo anatumia sitiari ya mafunzo ya mtoto kuwatia moyo Wakorintho (kama vile Efe. 6:4). Hili ni neno la pamoja la Kiyunani (yaani, "fikra" pamoja "kuweka") yaliyotumika kukumbushia (kama vile 1 Kor. 10:11 na 3:10). Neno linalohusiana nalo (yaani, "pamoja na" pamoja "kumbukumbu") limetumika katika 1 Kor. 4:17; 11:24-25; 2 Kor. 7:15.

**4:15 "Ikiwa"** Hii ni SENTENSI YENYE MASHARTI DARAJA LA TATU inayomaanisha juu ya tendo kuu.

**NASB"walimu wasiohesabika"**
**NKJV"waelekezaji elfu kumi"**
**NRSV, TEV"walezi elfu kumi"**
**NJB"watumwa elfu kumi wa kuwaangalia"**

Kiuhalisia inamaanisha "wakufunzi watumwa" (kama vile Gal. 3:24) watumwa hawa waliwajibika kwa ajili ya kuwasindikiza vijana wenye umri mkubwa kwenda shule, kuwafundisha majumbani kwao, na kuwalinda na hatari yeyote.

◙ **"Baba wengi……..baba"** Hii ni sitiari ya Paulo kwa ajili ya kujielezea mwenyewe kama mwinjilisti ambaye mwanzo aliwaongoza kwenda kwa Kristo. Hili linastahili heshima na upendeleo!

**4:16 "nawasihi mnifuate Mimi"** Hii ni KAULI YA KATI (yenye ushahidi) SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO. Tunapata neno letu la Kiingereza "kuiga" toka kwa neno la Kiyunani "mwigizaji." Paulo aliishi ndani ya imani yake (kama vile 1 Kor. 11:1; Flp. 3:17; 4:9; 1 The. 1:6; 3:9) na aliwaagiza hawa viongozi wa kanisa wa Korintho kufanya kama vile vile.

◙ **"Kutia moyo"** MADA MAALUM: FARAJA (SPECIAL TOPIC: COMFORT) katika 1 Kor. 1:10

**4:17 "Nimewatumieni Timotheo"** Hatuna taarifa zingine za Kibiblia juu ya ziara hii. Timotheo aliongoka wakati wa ziara ya kwanza ya Paulo na kumtengeneza kama msaidizi kwenye ziara ya pili. Alikuja kuwa rafiki mwaminifu, mwenza, mfanyakazi mwenza, na mwakilishi wa Kitume.

Kumtuma Timotheo kunaonyesha upendo wa Paulo na kujishughulisha na kanisa lake. Lakini hofu ya Paulo kuhusu baadhi ya watu katika kanisa watawatendea wenzao wadogo na wawakilishi binafsi, Timotheo (kama vile 1 Kor. 16:10-11). Tazama MADA MAALUM: TIMOTHEO (SPECIAL TOPIC: TIMOTH) katika 2 Kor. 1:1.

◙ "**kama vile nifundishavyo kila mahali katika kila kanisa"** Paulo alitaka kusisitiza kuwa kanisa la Korintho lingepewa mafundisho yale yale kama kwa makanisa mengine (k.v 1 Kor. 7:17; 11:16; 14:33). Hawakuwa watu maalumu au walioendelea, hawakuwa na haki ya kuwa tofauti na wengine, watu wa hadhi ya juu. Tazama Mada Maalum: Kanisa katika 1 Kor. 1:2

**4:18-21** Hii ilikuwa ni mipango ya mbele ya safari ya Paulo, kwa namna alivyohusiana na Korintho. Alifanya hili kwa vile baadhi ya watu kanisani walitumia mwanya wa kutokuwepo kwa Paulo kama njia ya mashambulizi (k.v 1 Kor. 4:18). Walikuwa wakidai kuwa (1) kutokuwepo kwa Paulo ni ishara kuwa alikuwa hajali kuhusu kanisa au (2) hakuweza kufuatilia kuhusu ahadi zake.

**4:18 "Basi wengine wamejivuna"** Paulo ametumia neno hili mara tatu katika sura hii (yaani., 1 Kor. 4:6,18,19) na mara nyingi katika nyaraka za Wakorintho (kama vile 1 Kor. 5:2; 8:1; 13:4 na 2 Kor. 12:20). Hili lilikuwa tatizo tofauti kwa kanisa hili. Angalia maelezo katika 1 Kor. 4:6.

**4:19 "Lakini nitakuja kwenu upesi"** Paulo alirudi tena na tena kuyatia nguvu makanisa aliyoyaanzisha (k.v 1 Kor. 11:34; 16:5). Paulo alipenda kwenda kuwatembelea, lakini umri wake ulikuwa umesonga mno. Kwa hiyo alipaswa kusikiliza na kufuata maongozo ya Roho (kama vile Mdo. 16:6).

◙ **"Kama Bwana akipenda"** Hii ni SENTENSI YENYE MASHARTI DARAJA LA TATU, inayomaanisha tendo kuu. Hiki kilikuwa ni kifungu kisichokuwa na maana kwa Paulo (kama vile 1 Kor. 16:7; Mdo. 18:21; Rum. 1:10; 15:32).

**NASB " Nitalazimika kufahamu, si neno lao tu waliojivuna, bali nguvu zao"**
**NKJV " nami nitafahamu, si neno lao tu waliojivuna, bali nguvu zao"**
**NRSV "Nitafahamu sio neno lao tu waliojivuna bali nguvu zao"**
**TEV "Nitafahamu mwenyewe nguvu walionayo hawa wanaojivuna, na si kile wanachosema"**
**NJB "Nami nitafahamu si neno lao tu wanaojiona kuwa bora, bali nguvu zao"**

Walimu wa uongo walikuwa na nguvu kwenye hotuba zao lakini matokeo yake yalikuwa hafifu (Mathayo 7)

**4:20 "Ufalme wa Mungu"** Paulo hatumii dhana hii zaidi kama vile Yesu alivyoitumia (yaani., hasa hasa kwenye vidokezo vya injili). Unarejea juu ya utawala wa Mungu kwa mioyo ya mwanadamu sasa (kama vile Mt. 14:17),

ambao siku moja utatimizwa duniani kama ilivyo huko Mbinguni (kama vile Mt. 6:10). Paulo anatumia kifungu hiki zaidi katika 1 Wakorintho (kama vile 1 Kor. 4:20; 6:9; 15:24,50) kuliko sehemu nyingine ya maandiko yake. Waamini hawa walihitaji kujua kuwa walikuwa sehemu ya agenda kubwa ya Kikristo (kama vile 1 Kor. 4:17)

**MADA MAALUM: UFALME WA MUNGU (SPECIAL TOPIC: THE KINGDOM OF GOD)**

◙ "**hauwi katika neno, bali katika nguvu"** Kuiweka kweli hii katika Mithali ya Waamerika, "matendo yanaongea zaidi kuliko maneno" au "ukweli uko kwenye uso wa mtu."

**4:21 "Fimbo"** Hii inarejea juu ya fimbo ya mwalimu (Kama vile Kor. 4:15). Kanisa hili lilipaswa kuamua kama Paulo angetakiwa kuja kama Baba mwenye kutia adabu wanae au Baba mwenye kusamehe. Matendo yao ndio yalipaswa kuamua mtazamo wake.

◙ **"roho ya upole"** Katika *Synonyms of the Old Testament* Robert Girdlestone ana maelezo ya kufurahisha juu ya utumiaji wa neno "roho" katika Agano Jipya (kur. 61-63)

1. roho wabaya
2. roho ya binadamu
3. Roho Mtakatifu
4. Vitu vinavyzalisha Roho ndani na kupitia kwa roho za wanadamu
   a. Asiye roho wa utumwa dhidi ya roho wa uasili-Rum. 8:15
   b. roho wa upole- 1 Kor. 4:21
   c. roho wa imani- 2 Kor. 4:13
   d. roho wa hekima na ufunuo katika maarifa yake-Efe. 1:17
   e. sio roho wa uoga dhidi ya yule wa nguvu, upendo na heshima-2 Tim. 1:7
   f. Roho wa makosa dhidi ya roho wa ukweli

Angalia nukuu zingine juu ya "roho" katika 2 Kor. 4:13.

*The Jerome Bible Commentary, NT*, uk. 260, unataja kuwa sentensi hii ya mwisho katika 1 Wakorintho 4:21 yaweza kuwa ni dokezo la Ayubu 37:13.

## MASWALI YA MJADALA

Haya ni maoni na mwongozo wa kujisomea, ambao una maana kuwa, wewe unawajibika kwa tafsiri yako binafsi ya Biblia. Kila mmoja wetu anapaswa kutembea katika mwanga tulionao. Wewe, Biblia na Roho Mtakatifu ndiyo vipaumbele katika kutafsiri. Usimwachie kazi hii mtoa maoni tu.

Maswali haya ya majadiliano yanatoa tu, msaada wa wewe kufikiria kupitia masuala nyeti ya sehemu ya kitabu hiki. Yamekusudiwa kuwa ya kukuchokonoa/kuchokoza akili, na yasiyo na ukomo.

1. kwa nini waamini hawastahili kuhukumiana wao wenyewe wala kuwaruhusu wengine kufanya hivyo? Hili linahusianaje na ushuhuda wetu wa Kikristo?
2. Ni nini aya, mistari ya 6-13, inasema kuhusu juu ya mienendo na miundo ya maisha ya wahudumu wa leo?
3. Elezea maana ya "ufalme wa Mungu"
4. Tambua na kuelezea juu ya matumizi ya Paulo ya vijembe vya kejeli katika sura hii.

# 1 WAKORINTHO 5

| MGAWANYO WA AYA WA TAFASIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **UBS[4]** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB** |
| | | Machafuko katika Korintho<br><br>(5:1-6:20) | | |
| Hukumu Dhidi ya Uzinifu | Uzinifu ulinajisio Kanisa | Jambo lihusulo Nidhamu ya Kanisa | Uzinifu katika Kanisa | Uasherati wa Nasaba |
| 5:18 | 5:1-8 | 5:1-2 | 5:1-5 | 5:1-5 |
| | | 5:3-5 | | |
| | | 5:6-8 | 5:6-8 | 5:6-8 |
| | Wazinzi Yawapasa Kuhukumiwa | | | |
| 5:9-13 | 5:9-13 | 5:9-13 | 5:9-11 | 5:9-13a |
| | | | 5:12-13 | 5:13b |

**MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI** (*kutoka* "**Mwongozo wa Usomaji Mzuri wa Biblia"(A Guide to Good Bbible Reading")**)

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILIA LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo wa usomaji wa hitifaki, ambayo inamaanisha kwamba unao wajibu wa tafsiri yako mwenyewe ya Biblia. Kila mmoja wetu lazima aenende katika nuru tuliyo nayo. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Unalazimika kutokuondoa hili toka kwa msemaji.

Soma sura katika mkao mmoja. Yatambue masomo. Linganisha mgawanyiko wa mada zako kwa ulinganifu wa tafsiri tano za hapo juu. Aya haijavuviwa, lakini ni ufunguo wa kufuata kusudi la msingi wa mwandishi, ambao ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya inayo moja na katika hilo ni somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya ya tatu
4. N.k

## MAZINGIRA YA KITHEOLOJIA YA NIDHAMU YA MKRISTO

A. Hii ni moja ya kurasa kadhaa katika kitabu cha Agano Jipya kuhusiana na nidhamu (kama vile 1 Kor. 5:2,7,13; 2 Kor. 2:5-7; 2 The. 3:14-15; 1 Tim. 1:20; Tito 3:10).
B. Nidhamu ya kanisa ina makusudi matatu.
   1. kudumisha sifa njema na uadilifu wa kanisa la mahala
   2. kumsaidia mwanafunzi na kumrejesha kaka ama dada aliyepotoka katika agano (kama vile 2 Kor. 2:5-11; 2 The. 3:14-15)

3. kuwasababisha Wakristo wasitende dhambi (kama vile 1 Tim. 5:20)

C. kuna mtazamo unaoonyeshwa.

1. kwanza, makubaliano binafsi na ikiwa si yenye kufanikiwa, matengano binafsi (kama vile Mt. 18:15; Gal. 6:1; 2 The. 3:14-15; Tito 3:10)
2. pili, makubaliano ya kundi dogo (kama vile Mt. 18:16)
3. tatu, matengano ya wengi kutoka katika ushirika wa ki-Kristo (kama vile Mt. 18:17; 1 Kor. 5:1; 1 Tim. 1:20)
4. mara kwa mara lazima lengo liwe kwa ajili ya toba na urejesho, si utengano na adhabu (kama vile 2 Kor. 2:6-8; Gal. 6:1)

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : 1 WAKORINTHO 5:1-2**

[1]**Yakini habari imeenea ya kuwa kwenu kuna zinaa, na zinaa ya namna isiyokuwako hata katika Mataifa, kwamba mtu awe na mke wa babaye.** [2]**Nanyi mwajivuna, wala hamkusikitika, ili kwamba aondolewe miongoni mwenu huyo aliyetenda jambo hilo.**

**5:1 "Yakini habari imeenea"** Neno la Kiingereza "yamkini" ni Kiyunani *holōs*, ni muundo haba uliotokea mara kadhaa katika 1 Wakorintho (kama vile 1 Kor. 5:1; 6:7; 15:29). Ni muundo wa neno *holos*, ambalo linamanisha "kabisa" "kwa jumla" Muundo huu haba unaonekana kumaanisha "kujulikana kwa upana" (kama vile NJB). Hii inaweza kuwa moja ya sababu za Paulo kuwatisha juu ya uovu huu wa wazi. Kanisa la ki-korintho lilijitukuza lenyewe na taarifa ilitolewa kwa mapana kwa makanisa mengine kulihusu. Paulo ilimpasa kuhusisha na tendo hili lililokuwa limevuka mipaka na mtazamo wa kanisa hili waliobaki waliyaathiri makanisa yote (yaani, kanuni ya chachu, kama vile 1 kor. 5:6-8).

◙ **"zinaa"** Neno hili la Kiyunani "*porneia*" ambalo lilikuwa neno la jumla la upotevu wa kizinaa. Tunalipata neno la Kiingereza, picha ya ngono, kutokana na neno la Kiyunani. Korintho ya Kiyunani ilijulikana kwa uzinzi wake wa ovyo ovyo. Hata watu wengine wasiomjua Mungu walitiwa wasi wasi na leseni ya uzinzi wa jamii ya ki-Korintho. Angalia Bruce W. Winter, *After Paul Left Corinth*.

Katika kitabu cha Agano la Kale kuna tofauti kati ya neno "uasherati" (yaani, mmoja au wote walio katika ndoa) na "uzinifu" (yaani, aidha ni mwanandoa), lakini hii si sababu katika lugha ya kawaida ya Koine (kama vile Matendo 15:20,29). Neno hili linarejelea juu ya uchafu wo wote wa kingono (yaani, uasherati, uzinzi, ngono za jinsia moja, hata ukatili). Hapa kuna uvunjaji wa sheria ya Law. 18:8; Kumb. 27:20.

◙ **"namna isiyokuwako hata katika Mataifa,"** Huu uhusiano wa kiuzinifu wa ndugu wa nasaba ulizuiliwa na Sheria ya Musa (kama vile Law. 18:8 na Kumb. 22:30), lakini pia hii lazima iwe ya kuchukiza hata kwa wapagani walio waovu wa huko Korintho. Hili lilikuwa "mbali zaidi" hata kwa karne ya kwanza ya utamaduni wa Kirumi kama vile Gaius, *Inst.* I, 63 na *Oxford Classical Dictionary*8, 539-540).

**NASB, NKJV “Mataifa"**
**NRSV " watu wasiomjua Mungu"**
**TEV " walio mbali na Mungu"**
**NJB "Mataifa"**

Paulo analitumia neno hili katika maana mahususi. Katika kitabu cha Agano Jipya kilikuwa na tofauti iliyokuwa wazi kati ya Myahudi na Mtu wa Mataifa. Yale "mataifa" yalikuwa na maana nyingine iliyo hasi. Paulo anatumia neno Mataifa katika maana ya yule asiyeamini. Wengi wao aliokuwa akiwaandikia hawakuwa Wayahudi.

**NASB "kwamba mtu awe na mke wa babaye"**
**NKJV "kwamba ni mzinifu na mke wa babaye"**
**NRSV "mmoja wenu anaishi na mke wa baba yake"**

**TEV "ya kwamba mtu anazini na mke mwingine wa babaye"**
**NJB "kwamba mmoja wenu anafanya uasherati na mke wa babaye"**

Kwa udhihirisho aya hii inarejelea juu ya mtu kuishi na mke wa babaye. Mtu huyo

1. alimshawishi mke wa babaye kinyume na babaye
2. alikuwa akiishi na mke wa babaye aliyetarakishwa
3. alikuwa akiishi na mke wa babaye aliye mjane

**5:2** Inawezekana kuuchukulia mstari huu kama (1) maswali matatu (2) semi tatu (NASB, NKJV); au (3) kama muunganiko (yaani NRSV, TEV, NJB, NIV).

**NASB "Nanyi mwajivuna"**
**NKJV "ninyi mna majivuno"**
**NRSV "mna majivuno"**
**TEV "mnawezaje kujivuna"**
**NJB "na mmejaa maivuno ninyi wenyewe"**

Hii ni KAULI TENDWA ENDELEVU YA WAKATI ULIOPO ya neno "kujivuna," hili linatumika mara kwa mara katika barua ya Wakorintho (yaani 1 Kor. 4:6,18,19; 5:2; 8:1; 13:4; 2 Kor. 12:20).Ina KITENZI-JINA “kuwa” kilichohusianishwa nacho, ambacho kinaifanya kauli hii kuwa TIMILIFU YENYE MAFUMBO, ambacho kinaaamisha hali iliyoamriwa. Tatizo halisi lilikuwa kwa sababu ya ule msimamo wa kanisa (yaani, KIWAKILISHI CHA WINGI na VITENZI). Walijivunia hali hii iliyokuwepo.

**NASB “wala hamkusikitika "**
**NKJV "na wala kwa namna fulani hamkusikitika"**
**NRSV "Haiwapasi kuwa na masikitiko?**
**TEV "Kwa upande mwingine, mwatakiwa kuwa na huzuni"**
**NJB "Ingekuwa afadhali kwenu kuomboleza”**

Neno hili la Kiyunani (yaani, *pentheō*, kama vile Mt. 5:4; 9:15; 2 Kor. 12:21; Yakobo 4:9) lilitumika kama kuomboleza kwa ajili ya aliye kufa (kama vile Ufu. 18:8,11). Katika jamii ya Kiyahudi maombolezo yalifanyika kwa ajili ya Yule aliyekufa, kwa wengine ilikuwa kwa ajili ya madhara, au kwa ajili ya kufuru iliyofanyika (kama vile Marko 14:63).

**NASB “ili kwamba aondolewe miongoni mwenu"**
**NKJV "yampasa kuondolewa kati yenu"**
**NRSV "aondolewe miongoni mwenu"**
**TEV "yampasa kuondolewa katika ushirika wenu"**
**NJB "na awe mbali na jumuiiya yenu"**

Hii ni KAULI TENDWA TEGEMEZI YA WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFU. Neno hili la Kiyunani linamaanisha "kunyanyua kitu na kuondoka nacho," mara nyingi huhusisha hukumu (kama vile Mt. 24:39) na mkazo (kama vile Yohana 11:48). Kusudi la kanisa lililoadibishwa ni kufungamana kwa namna tatu.

1. kulitakasa kanisa la mahali fulani (yaani, katika hatua zote kutoka dhambini na urejesho wa taswira yake katika jumuia asilia)
2. Matengenezo mapya na ukombozi wa waamini waliopotoka. Hili linawezekana kwa sababu ya 1 Kor. 5:5 (maneno yale yale yanatumika katika Luka 23:18) ambayo yanarejelea juu ya kifo cha waamini waliopotoka (s).
3. waamini wengine wanaoliona adibisho la Mungu wanasisitizwa kutotenda dhambi

**ANDIKO LA NASB (LLILILOBORESHWA ) : 1 WAKORINTHO 5:3-5**
**[3] Kwa maana kweli, nisipokuwapo kwa mwili, lakini nikiwapo kwa roho, mimi mwenyewe nimekwisha kumhukumu yeye aliyetenda jambo hilo, kana kwamba nikiwapo. [4] Katika jina la Bwana wetu Yesu, ninyi mkiwa mmekusanyika pamoja na roho yangu, pamoja na uweza wa Bwana wetu Yesu; [5] kumtolea Shetani mtu huyo, ili mwili uadhibiwe, ili na roho iokolewe katika siku ya Bwana Yesu.**

**5:3-5** Aya hii ni sitiari ya kisheria. Paulo analiunga mkono kanisa lile lililoitwa "kanisa la kimahakama" (kama vile Yakobo 2:1-4). Kanisa la kale lilifuata mfumo wa utawala na mpangilio wa sinagogi. Mahakama hizi zilikuwa za kawaida na zilizo nyingi zilijitenga na sinagogi.

**5:3 "Kwa maana kweli, nisipokuwapo kwa mwili, lakini nikiwapo kwa roho."** Zote hizi ni KAULI TENDAJI ENDELEVU YA WAKATI ULIOPO. Kwa uwazi inaonyesha maana ya Paulo ya mamlaka yake ya ki-utume (kama vile 1 Kor. 5:3 & 5). Lakini kumbuka kwamba yeye analitaka kanisa kuuhakiki uamuzi wake (kama vile 1 Kor. 5:4).
**MADA MAALUM: ROHO (*PNEUMA*) KATIKA AGANO JIPYA** **(SPECIAL TOPIC : SPIRIT(PNEUMA) IN THE NT**

◙ **"nimekwisha kumhukumu yeye aliyetenda jambo hilo"** Hii ni KAULI TENDAJI ELEKEZI. Paulo anaitetea mamlaka yake hata katika kutokuwepo kwake kimwili na msimamo wa maamuzi yake.

**5:4 "Katika jina la Bwana wetu Yesu"** Hii ni njia ya Kiebrania ya kuitetea heshima na nguvu ya Kristo aliyeinuliwa kama chanzo cha mamlaka ya Paulo ya ki-utume. Paulo anamwakilisha Kristo na kumfatisha Yeye.

Kuna miundo mbali mbali ya "jina la —" katika mamchapisho ya Kiyunani ya mstari huu.

1. "wetu Kristo" katika machapisho ya herufi kubwa B, D*
2. "Yesu Kristo" katika machapisho ya herufi kubwa א
3. "wetu Yesu Kristo" katika machapisho ya herufi kubwa $D^2$, F, G
4. "wetu" sehemu ya maandiko katika chapisho dogo 1021 (karne ya 12)
5. "Yesu Kristo Bwana wetu" katika machapisho ya herufi ndogo za Kirumi 81 (11karne ya)

Shirika la Umoja wa Biblia ya Agano Jipya la Kiyunani, toleo la nne ($UBS^4$) linasema kuwa ni vigumu kuamua, bali kupendelea #1.
Tatizo hili hili limetokea kwa mara nyingine tena katika 1 Kor. 5:5 (na pia 1 Kor. 5:11).

1. " Bwana" katika MSS $P^{46}$, B
2. "Bwana Yesu" katika MS א
3. "Bwana Yesu Kristo" katika MS D
4. "Bwana wetu Yesu Kristo" katika MSS A, F, G, P

UBS4 inatoa dalaja #1 kama yenye uhakika wa mara kwa mara.

**5:5 "kumtolea Shetani mtu huyo, ili mwili uadhibiwe"** "Kumtolea" ni neno la Kiyunani *paradidōmi*, ambalo lintumika katika Injili za kumgeuza mtu kwa mamlaka kwa ajili ya adhabu yenye kumfaa (kama vile Mt. 4:12; 5:25; 10:4,17; 18:34; 20:19; 26:15; 27:2,18,26) na katika Warumi (kama vile Rum. 1:24,26,28) kwa ajili ya kumgeuza mtu kutoka nguvu za giza. Matumizi haya yanaendana zaidi na muktadha huu (kama vile, Ibilisi kubainishwa).

Aya hii ni sawa na 1 Tim. 1:20. Kumekuwa na mjadala mwingi kati ya wasomi na watoa maoni kuhusiana na kile kilichohusishwa na aya hii. Wengine wanaona kwamba hii aya ina matokeo ya adhabu ya kudumu ya kimwili (yaani, kifo), kama ilivyo katika Matendo 5 na 1 Kor. 3:17; 11:30.Wengine wanaliona hili kama matengano ya moja kwa moja, yanayomweka mtu katika uhalisia wa kazi ya Ibilisi, ambayo ni ulimwengu (kama vile Yohana 12:31; 16:11; 1 Kor. 4:4; 1 Yohana 5:19), ambapo kujitenga kwake na ushirika wa Mungu na watu Wake kunaweza kumgeuza kumwelekea Mungu na kuiepuka hukumu ya mwisho. Paulo aliuona ulimwengu kama milki ya Ibilisi (kama vile Efe. 2:2). Uovu unaotokea duniani (yaani, kifo, magonjwa, upotevu, n.k.) unasababishwa na yule aliye mwovu, Ibilisi (kama vile 2 Kor. 12:7; 1 The. 2:18). Hii inawezekana kwamba "mwili" unarejea juu ya uasi wa mwanadamu katika maisha ya uzinifu (yaani, asili ya Nadharia iliyoanguka). Angalia Mada Maalum: Uovu Binafsi katika 1 Kor. 7:5.Kwa maelezo zaidi kuhusiana na neno "mwili" tazama Mada Maalum katika 1 Kor. 1:26.

◙ **"ili na roho iokolewe"** Nidhamu ya kanisa lazima iwe ya kiukombozi na urejesho, si kulipiza kisasi (kama vile 2 Kor. 2:5-11; 2 The. 3:14-15). Hii ni maana nyingine ya Agano la Kale ya neno "kuokolewa," ambayo inamaanisha ukombozi wa kimwili. Mtu, ingawa hutenda kwa namna ya ki-uovu, ni mshirika wa kanisa. Huyo anahitaji ukombazi wa kiroho, si wokovu.

Kama ilivyo kawaida katika maandiko ya Paulo umbo la kimwili na roho vimewekwa katika namana tofauti (yaani, Rum. 8:1-11). Hivi vinawasilisha miundo miwili tofauti ya mamlaka, mawazo mawili ya kiulimwengu, uaminifu wa aina mbili (kama vile Mt. 6:19-34; 1 Yohana 2:15-17).

Hoja moja ya kitheolojia zaidi kuhusiana na 1 Kor. 5:5: Ibilisi ni wa Mungu, anayeyatumikia makusudi ya Mungu ya wokovu. Katika Agano Jipya Ibilisi ni adui wa mwanadamu, lakini ni wa Mungu (kama vile A. B. Davidson, *An OT Theology*, kr. 300-306). Ni uhusiano unaochochewa katika Agano Jipya. Ibilisi ni adui wa Mungu, lakini si mtumishi asiye tayari. Kazi ya Ibilisi katika 1 Kor. 5:5 ni kuleta wokovu wa milele kwa wale washirika wa kanisa waliopotea.

◙ **"katika siku ya Bwana Yesu"** Kwa udhihirisho aya hii inarejea juu ya siku ya mwisho, mpangilio wa nyakati za mwisho. Hukumu ya Mungu yenye mtiririko kuwaelekea Wakristo inaweza kuonekana katika Kor. 11:30-32; Matendo, na 1 Tim. 1:20. Je! Andiko hili linadokeza juu ya (1) kifo cha mwili, bali wokovu kwenye siku ya mwisho, 1:8 au (2) yeye kuutegemea wokovu katika toba yake?

Kuna msistizo wa sasa kuhusiana na hukumu katika 1 Wakorintho (kama vile 1 kor. 1:7-8; 3:13; 4:5; 5:5; 6:14; 11:26; 13:12; 15:50-54; 16:22). Bila shaka moja ya matatizo yaliyohusiana na siku ya hukumu katika kanisa la Wakorintho lilikuwa juu ya siku ya hukumu iliyotambuliwa kwa kuunganishwa na mwanzo wake.

Wanamafunuo hawa walifikiri kuwa kiroho wamefika (kama vile1 Kor. 4:7-10) na kwamba mwili ni mwovu (yaani, mawazo ya Kiyunani) na, hivyo, mawazo haya kutohusiana na mambo ya kiroho. Paulo anakanusha kuhusiana na uelekeo huu kwa

1. Kuithibitisha hukumu ijayo na vile ya wakati huu (kama vile 1 Kor. 5:5)
2. kusisitiza juu ya zinaa isiofaa kwa waamini (kama vile 1 Kor. 5:5-6)

Pia tambua kwamba vifungu vya Agano la Kale vinavyorejea juu ya YHWH sasa vimehamishiwa kwa Yesu (kama vile 1 Kor. 1:8; 2 Kor. 1:14; 1 The. 5:2; 2 The. 2:2; 2 Tim. 4:8). Hii ni moja ya njia ya kimaandishi ambayo waandishi wa Agano Jipya wanatumia kuutetea Uungu wa Yesu wa Nazarethi.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : 1 WAKORINTHO 5: 6-8**

**6 Kujisifu kwenu si kuzuri. Hamjui kwamba chachu kidogo hulichachusha donge zima? 7 Basi, jisafisheni, mkatoe ile chachu ya kale, mpate kuwa donge jipya, kama vile mlivyo hamkutiwa chachu. Kwa maana Pasaka wetu amekwisha kutolewa kuwa sadaka, yaani, Kristo; 8 basi na tuifanye karamu, si kwa chachu ya kale, wala kwa chachu ya uovu na ubaya, bali kwa yasiyochachika, ndio weupe wa moyo na kweli.**

**5:6 "Kujisifu kwenu si kuzuri"** Haya maoni yanasaidia kufasiri mtazamo wa kanisa la Korintho. Hawa walidai uhuru na kibali kilichojikita katika injili. Wao walitaka kuonyesha uhuru wao mpya badala ya kutoa ushahidi wa injili kwa jumuiya yao.

**MADA MAALUM: KUJISIFU (SPECIAL TOPIC: BOASTING)**

◙ **"Hamjui kwamba"** Hii ni tabia ya aya iliyotumiwa na Paulo mara kwa mara ili kurejea yale mambo ambayo yawapasa waamini kuyajua, mambo waliojihusisha nayo hapo awali, lakini yale yaliyokuwa na udhihirisho (yaani, kwa sababu ya matendo na mitazamo yao) kuwa yasahaulike (kama vile Rum. 6:16; 11:2; 1 Kor. 3:16; 5:6; 6:2,3,9,15,19; 9:13,24).

◙ **"chachu"** Aya hii inarejea juu ya mithali ya Kiyunani (kama vile Mt. 16:6,12; Gal. 5:9) kuhusiana na chachu, mara nyingi ni katika maana hasi, iliyoungamanishwa na uozo kwa sababu ya tendo la kuchachusha. Hata hivyo, wakati mwingine hii stiari ina kipengele chanya (kama vile Mt. 13:33; Luka 13:20-21), kinachoonyesha kwamba ile maana inahusiana na muktadha.

**MADA MAALUM: CHACHU (SPECIAL TOPIC: LEAVEN)**

**5:7 "hulichachusha donge zima"** Hii ni KAULI TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPITA USIO TIMILIFU. Hili ni dokezo kwa desturi za Kiyahudi za kuondoa chachu ndani ya nyumba kabla ya Pasaka ya kila mwaka (kama vile Kut. 12:15).Taratibu za ibada ya kila mwaka ilikuwa ishara ya toba.

**NASB "mpate kuwa donge jipya, kama vile mlivyo hamkutiwa chachu"**
**NKJV "mpate kuwa donge jipya, kwa kuwa hakutiwa chachu kabisa"**
**NRSV "mapate kuwa mikate mipya, kama ambavyo hamkutiwa chachu kabisa"**
**TEV "mpate kuwa donge jipya lisilotiwa chachu. Yawapasa kuwa kama mlivyokuwa"**
**NJB "mpate kuwa donge jipya, kama mlivyokuwa"**

Hii inaonyesha ni muunganiko wenye ufanano kamili wa Paulo juu ya amri ya MAADILI iliyohusianishwa na maelezo ya MAHALI. Nafasi tuliyonayo katika Kristo, yatupasa kuwa katika maisha ya kumfanana Kristo. Hawa walikuwa watu wa Mungu (yani, wasiotiwa chachu), lakini wangeza kuwa watu wa hukumu ya Mungu (yaani, donge jipya).

**NASB "maana Pasaka wetu amekwisha kutolewa kuwa sadaka"**
**NKJV "maana, Kristo, Pasaka, yetu, amekwisha tolewa kuwa sadaka"**
**NRSV "kwa kuwa sikukuu ya Pasaka i tayari, na sasa yule Kristo, Mwana-Kondoo wa Pasaka, amekwisha tolewa Sadaka"**
**TEV "kwa maana sikukuu ya Pasaka i tayari, na sasa yule Kristo, Mwana -Kondoo wa Pasaka yetu, amekwisha kuwa sadaka"**
**NJB "Pasaka yetu imekwisha tolewa sadaka, naye ni, Kristo"**

Paulo anahusianisha kifo cha Kristo na dhana ya Agano la Kale ya Mwana- Kondoo wa Pasaka (kama vile Kut. 12:15 na kuendelea; 13:7). Hii ni moja ya maeneo machache katika Agano Jipya ambayo yamehusinishwa na semi zilizozungumzwa kwa njia mahususi:

1. Yohana Mbatizaji uliuona uhusiano huu na kumuita Yesu "Mwana – Kondoo wa Mungu azichukuaye dhambi za ulimwengu" katika Yohana 1:29.
2. Yohana 19:36 anatumia nukuu toka kwenye Pasaka ya kutoka Misri, Kut. 12:46.

**5:8 "basi na tuifanye karamu"** Hii ni KAULI TENDAJI TEGEMEZI YA WAKATI ULIOPO (UHIMIZAJI TEGEMEZI inayotoa wito wa tendo). Inahusiana na Agano la Kale pekee juu ya siku ya kufunga (kama vile Mambo ya Walawi 16), iliyoitwa Siku ya Upatanisho katika 1 Kor. 5:7, ambapo 1 Kor. 5:7b na 8 inahusiana na Sikukuu ya Pasaka (kama vile Kutoka 12). Hii inarejea juu ya maisha endelevu kwa sababu ya kazi ya Kristo kwetu na kati yetu, lakini ikiwa na dalili za udharura (yaani, DHAMIRA TEGEMEZI).

◙ **"si kwa chachu ya kale"** Hii inarejea juu ya Agano la Kale katika Kristo (kama vile Yer. 31:31-34; Eze. 36:22-38). Hili agano jipya limeyatenga majisifu ya mwanadamu na kiburi. Kifo cha Kristo ni kumwagwa kwa maji ya ufunuo wa biblia.

◙ **"wala kwa chachu ya uovu na ubaya"** Katika muktadha na kwa namna tofauti, Paulo anaeleza juu ya yale yasiyo sahihi, hata uovu, shauku na matendo ya baadhi ya makanisa ya nyumbani ya huko Korintho.

◙ **"bali kwa yasiyochachika"** Hili neno haba bila shaka ni muungano wa neno linalotokana na "mwangaza wa jua" na "hukumu." Neno hili linaeleza dhana ya kutofichika, nia iliyo safi (kama vile 1 Kor. 5:8; 2 Kor. 1:12; 2:17; Flp. 1:10; 2 Pet. 3:1).

◙ **"Ukweli"** Asili ya neno *alētheia* ni "kutambua, isiyofichika, iliyodhihirishwa wazi," ambalo lina ufanano na mzizi wa maana ya neno "unyofu." Paulo anahusika na nia! Tazama Mada Maalum katika 2 Kor. 13:8.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : 1 WAKORINTHO 5:9-13**
**[9] Naliwaandikia katika waraka wangu, kwamba msichangamane na wazinzi. [10] Sisemi msichangamane kabisa na wazinzi wa dunia hii, au na wenye kutamani, au na wanyang'anyi, au na wenye kuabudu sanamu; maana hapo ingewalazimu kutoka katika dunia. [11] Lakini, mambo yalivyo, naliwaandikia kwamba msichangamane na mtu aitwaye ndugu, akiwa ni mzinzi au mwenye kutamani au mwenye kuabudu sanamu au mtukanaji au mlevi au mnyang'anyi; mtu wa namna hii msikubali hata kula naye. [12] Maana yanihusu nini kuwahukumu wale walio**

**nje? Ninyi hamwahukumu hao walio ndani? [1]*3* Lakini hao walio nje Mungu atawahukumu. Ninyi mwondoeni yule mbaya miongoni mwenu.**

**5:9 "Naliwaandikia katika waraka wangu"** Bila shaka aya hii inarejea juu ya waraka uliopotea (kama vile A, T, Robertson, *Word Pictures in the New Testament*, uk. 115, na M. R. Vincent, *Word Studies in the New Testament*, uk. 769). Inawezekana kwamba nyaraka kadhaa za Paulo zimepotea (kama vile Kol. 4:16) au inaweza kuwa KAULI YA KIWARAKA (kama vile 1 Kor. 9:15), ambayo ingeweza krejea kwa 1 Wakorintho, ambayo ilikuwa imeandikwa kwa wakati huohuo (kama vile 1 Kor. 5:11). Angalia *Introduction to 1 Corinthians*, VII. C.

◙ **"wazinzi"** Hili ni neno la Kiyunani *pornos* (kama vile 1 Kor. 5:9,10,11; 6:9). Hili linahusiana na "upotovu" (yaani, *porneia* kama vile 1 Kor. 5:1 [mara mbili]; 6:13,18; 7:2; 2 Kor. 12:21) na "kutenda yaliyo maovu" (yaani, *porneuō,* kama vile 1 Kor. 6:18; 10:8).

Waamini hawa wa huko Korintho wengi wao walikuwa wa Mataifa (bila shaka Warumi). Watu wasiomjua Mungu walikuwa wakiabudu huku wakiwa walevi na wenye matendo ya uzinifu katika mahekalu ya miungu yao huku wakiwa na milo maalumu binafsi na ya watu wengine. Imani yao mpya katika Kristo bado imechanganyikana na mila za wakati ule wa Mataifa.

### MADA MAALUM: MAOVU NA WEMA KATIKA AGANO LA KALE (SPECIAL TOPIC: VICES AND VIRTUES IN NT)

**5:10** Waraka wa Paulo umekuwa si wa kueleweka. Paulo anawasisitiza waamini wapya kuuepuka uovu. Hata hivyo, wengine hulitafsiri hili kama "kamwe msihusiane nao." Paulo alipaswa kuweka bayana maana yake aliyokuwa ameikusudia. Waamini wanaishi katika ulimwengu ulioanguka; haiwezekani kuwatenga watu walio waovu (hasa ikiwa tutawachukulia kwa umakini Mt. 28:19). Kile alichokimaanisha Paulo ni kwamba msile maagano na ndugu wasiomjua Mungu, washirika wenza wa kanisa, au hata kuwa nao katika urafiki uliopindukia. HIKI NI KITENZI JINA CHA KATI CHA WAKATI ULIOPO cha neno *sunanamignumi*, ambacho kinamaanisha "kuweka pamoja" (kama vile 1 Kor. 5:9,11; 2 The. 3:6,14). Mistari ya 10-11 inatoa mtazamo kamili mazingira ya kiutamaduni ya kanisa huko Korintho.

**5:11**
**NASB "mtu aitwaye ndugu"**
**NKJV "ye yote aitwaye ndugu"**
**NRSV "mtu anayelikubali jina la kaka ama dada"**
**TEV "mtu anajiita ndugu"**
**NJB "ye yote aenendaye kwa jina la ndugu"**

Kifungu hiki ni ni KAULI TENDWA ENDELEVU YA WAKATI ULIOPO, inayohusianishwa na SENTENSI YENYE MASHARTI DARAJA LA TATU (kama vile Efe. 5:3) au kuliita jina la Yesu (kama vile Rum. 10:9-13; Flp. 2:11). Kulichukuwa jina la Yesu ilimaanisha kuzichukua tabia zake. Hii ni wazi kwamba Paulo (kama Yesu) aliamini kuwa maisha ya mtu huufunua utu wake ulivyo (kama vile Mt. 7:15-23). Weledi lazima uoanishwe na maarifa ya injili, yule Roho akaaye ndani, utii binafsi, na ustahimilivu.

◙ **"mtukanaji"** Tazama 1 Kor. 4:12.

◙ **"akiwa"** Hii ni SENTENSI YENYE MASHARTI DARAJA LA TATU, ambayo inamaanisha tendo lenye uwezekano. Kuna orodha kadhaa katika maandiko ya Paulo kuhusiana na dhambi ya mwili (kama vile Warumi 1:29-37; 1 Kor. 5:10-11; 6:9-10; 2 Kor. 12:20; Gal. 5:19-21; Efe. 4:31; 5:3-4; Kol. 3:5-9).

◙ **"msikubali hata kula naye"** Hii inaweza kuwa inarejea juu ya Karamu ya Bwana, lakini pia ingeweza kurejea juu ya uhusiano wa kijamii (kama vile 1 Kor. 10:27). Katika utamaduni wa Kirumi mara kwa mara milo ilipata nafasi ya

kuendana na uovu.

**5:12** Paulo na kanisa lazima wajihusishe na washirika (1 Kor. 5:12 inatarajia jibu la "ndiyo"), lakini waamini lazima wamruhusu Mungu ili ashughulike na wale wasio washirika. Waamini hawapaswi kuhukumiana (kama vile Mt. 7:1 na kuendelea; Rum. 14:1-15:13), bali

1. yatupasa kuyapima matunda ya kila mmoja wetu kwa nafasi za uongozi (kama vile 1 Kor. 6:1-3; Mathayo 7)
2. yatupasa kujizoeza kuifatisha nidhamu ya kanisa wakati marejesho ya kanisa lililokuwa katika hatari ya kuangamia

Mara nyingi huu ni mstari ulionyooka! Kwa maana nyingine Paulo anadai kuwa mwanadamu mwenye dhambi wa 1 Kor. 5:1 awekwe katika kweli ya hukumu ya Mungu (yaani, nje ya kanisa).

Moja ya maajabu ni kwa namna muktadha huu unavyohusiana na jamii za sasa ambapo waamini na wale wasio amini wana fursa ya kurekebisha desturi za kijamii. Je! Yawapasa waamini kushiriki kwa bidii katika tendo la kisiasa? Muktadha huu umewekewa kizuizi cha hukumu inayohusiana na nidhamu ya kanisa na si ya Kimagharibi, demokrasia ya sasa. Waamini ni raia katika uthibitisho wa aina mbili wenye majukumu na upendeleo ndani ya aina hizi zote! Roho wa Mungu , Mapenzi ya Mungu, na kitabu cha Mungu kinachotusaidia sisi kama waamini kuitafakari njia yetu katika ulimwengu huu ulioanguka, lakini wale wasioamini wananyonywa na kuteswa na dhambi, wenyewe, na Ibilisi. Hawa wanahitaji ushahidi wetu na ushirikiano wetu, si hukumu ya haki yetu wenyewe. Hawa hawana uwezo wa kuzielewa nia zetu, makusudi, na matendo.

Tatizo la wakati gani na namna gani Wakristo wanapaswa "kuhukumu" mmoja baada ya mwingine lilisababishwa na machapisho ya Kiyunani kwa madhabahu ya andiko.
Machapisho ya kale ya mafunjo $P^{46}$ (mnamo 200 B.C) pamoja na ile tafsiri ya matoleo ya Biblia magharibi mwa Misri (karne ya 3) na tafsiri ya toleo la Biblia ya makanisa ya Syria (karne ya 5) ambazo zinaondoa hali hasi na kutafsiri sentensi kama YENYE MASHARTI, "Hukumu ya wale walio ndani [kanisa]" (kama vile Bruce M. Metzger, *A Textual Commentary on the Greek New Testament*, uk. 551).

1. Tafsiri ya toleo la biblia kusini mwa Misri (karne ya 3) inayoweka hali hasi yenye sentensi ya awali, "Nifanye kipi ikiwa nitawahukumu wale walioko nje na kuwaacha walioko ndani? Hukumu wale walioko ndani
2. Ile andiko la $UB^{S4}$ halikubali uwezekano wa tofauti hizi kama ni halisi.

**5:13** Paulo anakamilisha majadiliano yake kutokana na mtazamo wa Kiyunani kwa kudokeza maandiko ya Musa (kama vile Kumb. 13:5; 17:7,12; 19:19; 21:21; 22:21,24; 24:7). Kama kanisa litavumilia (hata kusifu ndani ya) washirika waovu wataliathiri kanisa zima (kama vile 1 Kor. 5:11).

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa usomaji wa hitifaki, ambayo inamaanisha kwamba unao wajibu wa tafsiri yako mwenyewe ya Biblia. Kila mmoja wetu lazima aenende katika nuru tuliyo nayo. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Unalazimika kutokuondoa hili toka kwa msemaji.

Maswali haya ya majadiliano yanatoa tu, msaada wa wewe kufikiria kupitia masuala nyeti ya sehemu ya kitabu hiki. Yamekusudiwa kuwa ya kukuchokonoa/kuchokoza akili, na yasiyo na ukomo.

1. Kwa nini makanisa hayatembei katika nidhamu ya kanisa katika zama hizi?
2. Ni kwa namna gani tunahusianisha mamlaka ya ki-utume ya Paulo na kanisa asilia?
3. Je! nini maana ya kumtoa mtu kwa Ibilisi kwa ajili ya uharibifu wa mwilli wake?
4. Ni nyaraka ngapi azilizoziandika Paulo kwa Korinth?

# 1 WAKORINTHO 6

| MGAWANYO WA AYA WA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| UBS[4] | NKJV | NRSV | TEV | NJB |
| Kwenda kwenye sheria mbele ya wasioamini | Msiwashtaki wapendwa wenzenu | Mashtaka katika mahakama za kipagani | Mashtaka dhidi ya Wakristo wenzio | Msaada katika mahakama za kipagani |
| 6:1-11 | 6:1-11 | 6:1-6 | 6:1-6 | 6:1-8 |
| | | 6:7-8 | 6:7-11 | |
| | | | | 6:9-11 |
| Mtukuze Mungu katika Mwili wako | Kumtukuza Mungu katika Mwili na Roho | Onyo dhidi ya uzembe 6:9-11 | Tumia mwili wako kwa Utukufu wa Mungu | Uasherati |
| 6:12-20 | 6:12-20 | 6:12-20 | 6:12-14 | 6:12-17 |
| | | | 6:15-17 | |
| | | | 6:18-20 | 6:18-20 |

**MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI** (Kutoka" **Mwongozo wa Usomaji Mzuri wa Biblia"("A Guide to Good Bible Reading")**

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILIA LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo wa usomaji wa hitifaki, ambayo inamaanisha kwamba unao wajibu wa tafsiri yako mwenyewe ya Biblia. Kila mmoja wetu lazima aenende katika nuru tuliyo nayo. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Unalazimika kutokuondoa hili toka kwa msemaji.

Soma sura katika mkao mmoja. Yatambue masomo. Linganisha mgawanyiko wa mada zako kwa ulinganifu wa tafsiri tano za hapo juu. Aya haijavuviwa, lakini ni ufunguo wa kufuata kusudi la msingi wa mwandishi, ambao ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya inayo moja na katika hilo ni somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya ya tatu
4. N.K

## MAONI YA UFUNGUZI

Kwa miaka mingi, nimekuwa na wanasheria kadhaa wakiniuliza kuhusu jinsi mazingira haya yanavyohusiana na jamii yetu ya kisasa. Kwanza, katazo la kumpeleka mwenzio (hata Mkristo mwingine) mahakamani lazima lishughulikiwe. Mtu anaweza kujadili kwamba mahakama za kisasa ni tofauti na mahakama za kipagani, lakini kwa jinsi gani? Sheria zetu nyingi zinaegemea juu ya Sheria za Kirumi. Baadhi ya waamuzi leo ni waaminio, lakini hilo lisiathiri maamuzi yao ya kimahakama.-

Kunaonekana kuwepo mambo kadhaa yanayohusishwa.

1. Azimio na kusudi la kufungua madai mahakamani ni muhimu, si tu msingi wa kisheria wadaawa hiyo. Tunaishi katika jamii yenye kuleta ubishi, kama vile Athene ya kale. Mara nyingi kiburi, pesa, au visasi yalikuwa ni masuala ya kweli.

2. Matokeo ya athari za kijamii yenye uroho, mambo madogo madogo,au hasira za wakristo katika mahakama ya wazi lazima kuepukwa. Kila muamini ana wajibu wa ushirika kwenye ufalme wa Mungu. Mashahidi wetu ni muhimu.
3. Hata hivyo, kanisa halikutoa njia ifaayo ya suluhisho kati ya waaminio.hakuna baraza la kanisa la kikristo kwa waaminio kuangalia na kushughulikia mambo amabyo ni muhimu kwao au amabayo yasio haki kiasili.
4. Kwa kadri iwezekanavyo moja ya ufumbuzi ni ushirikiano wa wanasheria wa kikristo wakiwa na mtaji wa kiroho (yaani, maandiko matakatifu, hekima ya kiroho, n.k.), sio tu vigezo vya kisheria, ambavyo vinajishughulisha na mambo halali yanayowahusu waaminio. Waamini (yaani, kuwaamini wanasheria) ambao wanaojifikiria kujihusisha katika mambo ya madai wanapaswa kuuliza mwongozo wa Mungu na kuanzisha miongozo ambayo wanachagua kutekeleza sheria.Hii ingaliweza kuanzia kwenye mijadala ya usuluhisi kati ya waaminio.

Ingawa Agano Jipya kihistoria na kiutamaduni limewekewa masharti, matatizo ya kimsingi na mwelekeo wa kibinadamu sio. Mungu anazungumza kupitia maandiko haya na waaminio lazima kusikia maneno na mapenzi yake, ingawa sio katika karne ya kwanza ya makundi ya Kirumi na Kiyunani. Maandishi haya yanawahitaji waaminio kutokuwa wabishi na kuwa zaidi kama Kristo. Wanaliomba kanisa kuleta majadiliano (kama Mahakama za sinagogi). Wamatupigia kelele kwamba hasara ya kibinafsi ni bora kuliko ufalme wa Mungu (yaani, injili) kupotea!

Katika siku ya kuliadibisha kanisa dogo, taraka nyingi za waamini zilizotapakaa, zikiambatana na uroho, jamii yenye kuleta ubishi, sura 5 na 6 ni maandiko muhimu kwetu sisi kuyasoma na kuyatekeleza, yote kwa ushirikiano (kanisa na makanisa) na kibinafsi. Uhuru wa Wamarekani hutegemea usawa ulio chini ya sheria. Hii inamaanisha kama waamini tunaishi kwenye ulimwengu au dunia ya vitu viwili, moja wa pamoja na mwingine wa kiroho. Hatuwezi thubutu kukomesha mfumo wetu wa kisheria, lakini tunapaswa kukumbuka uraia wetu wa mbinguni. Tawala zote zina haki na wajibu. Lakini utawala mmoja huwa na kipaumbele (kama vile 1 Kor. 6:19-20)!

Baadhi ya waamini wanaweza kuliona suala la madai mahakamani na sababu sahihi ya kufungua madai kiutofauti.Sisi sote tunapaswa kutembea katika mwanga tulionao.Mazingira haya yanaweza kuongeza hiyo nuru.

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 1 WAKORINTHO 6:1-6**
**1 Je! Mtu wa kwenu akiwa ana daawa juu ya mwenzake athubutu kushitaki mbele ya wasio haki, wala si**
**mbele ya watakatifu? 2 Au hamjui ya kwamba watakatifu watauhukumu ulimwengu? Na ikiwa ulimwengu**
**utahukumiwa na ninyi, je! Hamstahili kukata hukumu zilizo ndogo? 3 Hamjui ya kuwa mtawahukumu malaika,**
**basi si zaidi sana mambo ya maisha haya? 4 Basi, mkiwa na mahali panapohukumiwa mambo ya maisha haya,**
**mwawaweka kuwa waamuzi hao waliohesabiwa kuwa si kitu; katika kanisa? 5 Nasema hayo nipate**
**kuwatahayarisha. Je! Ndivyo, kwamba kwenu hakuna hata mtu mmoja mwenye hekima, awezaye kukata**
**maneno ya ndugu zake? 6 Bali mwashitakiana, ndugu kwa ndugu, tena mbele yao wasioamini.**

**6:1**
**NASB"shitaka"**
**NKJV"daawa"**
**NRSV"Shutma"**
**TEV “Mabishano”**
**NJB"malalamiko"**

Hii hutumika katika lugha ya kawaida ya Koine huko Uyunani kwenye mafunjo yaliyopatikana Misri kwa kumaanisha (1) "kitendo" au "tendo"; (2) "madai"; (3) "shida" au "matatizo"; (4) "shughuli" au "biashara" (kama vile Moulton na Milligan, *The Vocabulary of the Greek New Testament*, uk. 532). Hoja namba mbili inafaa zaidi kwenye muktadha huu.Tunajua kutoka katika nyaraka za wa-Athene kwamba Wayunani kiutamaduni walianguka kifudi fudi mbele ya maswala ya madai. Hivyo hivyo, kwa kiasi fulani, ilitumika kwa Warumi. Korintho ya siku za Paulo ulikuwa sio wa Kiyunani, bali wa Kirumi (tazama Bruce W. Winter, *After Paul Left Corinth*, Eerdmans, 2001).

**NASB"jirani yake"**
**NKJV, NRSV,**
**NJB"mwenzake"**
**TEV"ndugu muumini"**

Hili kihalisia ni neno *heteros* (kama vile 1 Kor. 10:24; 14:17; Gal. 6:4). Katika Kiyunani cha kawaida kulikuwa na tofauti kati ya neno *alla* (yaani, nyinngine ya aina moja) na *heteros* (yaani, nyingine ya aina tofauti). Hii tofauti katika lugha ya kawaida ya Koine (kama kulivyokuwa na tofauti nyingi kwa sarufi za kawaida za Kiyunani na matumizi yake) ilianza kutoweka. Mazingira haya ni mfano mzuri. Matumizi hapa ya neno *heteros*, yanayorejelea kwa muamini mwenza, yanafanana katika Rum. 13:8. Katika Rum. 2:1 neno lina maana pana, yumkini jirani, raia mwenza, au Myahudi. Mthibitishaji wa kimktadha wa vidokezo hivi katika mstari huu wa kifungu "mbele ya watakatifu." Jirani aliyepotea yumkini hawezi kubali kwenda mbele ya mahakama ya kanisa (kama vile Mt. 18:17; Yakobo 2:1-4) katika kupingana na muamini.

Ni hakika inawezekana kwamba Paulo alikuwa na ngazi mbili za utofauti. Ni tatizo kwa muamini dhidi ya asioamini kwenda mbele ya mahakama ya kipagani. Ni mbaya zaidi kwa muamini kumpeleka muamini mwingine mbele ya mahakama ya kipagani. Napendeleza itafasiliwe kwamba "jirani" 1 Kor. 6:1 pia imaanishe "mwenzi wa Agano " au "muumini mwenza."

◙ **" athubutu "** Hili neno la Kiyunani (i.e., *tolmaō*) hutumika wakati kadhaa katika barua ya Wakorintho kwa maana ya "kudhania " au "kuhakikisha ujasiri " (kama vile 1 Kor. 6:1; 2 Kor. 6:2,10; 11:21; na Rum. 5:7; 15:15,18; Yuda 9).

**NASB, NKJV"kushitaki mbele ya wasio haki"**
**NRSV"mbele ya mahakama ya watu wasiomjua Mungu"**
**TEV"kwenda mbele ya waamuzi wa kipagani"**
**NJB"kutafuta hukumu kutoka kwa wenye dhambi"**

Paulo hakuwa na wasiwasi kuhusu waaminio kutendewa isivyo sawa, lakini ni kuhusu kuyaweka wazi matatizo ya Wakristo mbele ya wasioamini. Roho ni mwongozo kwa uhusiano wa kibinafsi katika kanisa, sio sheria ya kipagani. Uinjilisti ni muhimu zaidi kuliko haki ya mtu binafsi!

**6:2 "Au hamjui"** Tazama maelezo katika 1 Kor. 5:6.

◙ **"Watakatifu"**Neno "Watakatifu" (*hogioi*) ni kutoka katika neno la Agano la Kale "utakatifu," (*kadosh*) ambalo linamaanisha "kilichotengwa kwa ajili ya huduma ya Mungu " (kama vile Kut. 19:6; Kum. 7:6; 1 Kor. 1:2; 2 Kor. 1:1; Rum. 1:1;Efe. 1:1; Flp. 1:1; Kol. 1:2). Daima liko katika WINGI kwenye Agano Jipya isipokuwa mara moja katika Wafilipi (4:21), lakini hata hapo, limetumika kiushirikiano. Kuokolewa ni kuwa sehemu ya jamii ya Agano la imani, familia ya waaminio. Angalia **MADA MAALUM: WATAKATIFU (SPECIAL TOPIC: SAINTS)** katika 1 Kor. 1:2.

Watu wa Mungu ni watakatifu kwa sababu ya haki aliyoshutumiwa nayo Yesu (yaani, kauli ELEKEZI, kama vile Warumi 4; 2 Kor. 5:21). Ni mapenzi ya Mungu kwamba waishi maisha ya utakatifu (yaani, amri shurutishi, kama vile Efe. 1:4; 4:1; 5:27; Kol. 1:22; 3:12). Waaminio wanatangaziwa utakatifu (utakaso wa mahali) na pia kuitwa kwenye mfumo wa maisha ya utakatifu (utakaso endelevu). Kuhesabiwa haki na utakaso lazima viendane pamoja! Angalia **MADA MAALUM: UTAKATIFU /UTAKASO WA AGANO JIPYA (SPECIAL TOPIC: NEW TESTAMENT HOLINESS/SANCTIFICATION)** katika 1 Kor. 1:2.

◙ **"watauhukumu ulimwengu"** ingawa Yesu alitaja wazi kwamba mitume watatenda kama waamuzi, mwendelezo wa kimantiki wa ukweli huu ni kwamba watakatifu watahukumu pia (kama vile Dan. 7:22,27; Mt. 19:28; Luka 22:28-30; Ufu. 2:26, 3:21, 20:4). Lini na jinsi gani ni maswali magumu.

◙ **"ikiwa"** Hii ni SENTENSI YENYE MASHARTI DARAJA LA KWANZA, ambayo hudhani watakatifu watashiriki kama waamuzi katika matukio ya wakati wa mwisho

**NASB " je! Hamstahili kukata hukumu zilizo ndogo"**
**NKJV "je! Hamstahili kukata hukumu zilizo ndogo"**
**NRSV "je! hamna uwezo wa kuamua daawa zilizo ndogo"**
**TEV "kwa nni hamstahili kuhukumu hata katika mambo madogo"**
**NJB "je! Hamuwezi kuamua daawa zilizo ndogo"**

Hii ni kejeli inayochoma iliyoelekezwa kwa wale ambao walidai kuwa na hekima iliyo bora zaidi! Neno hilo hilo (yaani, *anaxios*) hutumika kwa tabia isiofaa ya makanisa ya Wakorintho katika karamu ya Bwana (kama vile 1 Kor. 11:27,29). Hawa waaminio wachanga, ambao walidai sana utambuzi muhimu wa kiroho, katika ukweli hawakujua jinsi gani ya kufanya tathmini vizuri au kutenda vizuri!

Neno "ndogo zaidi" ni umbo la sifa ya juu kabisa ya neno *mikros*. Paulo alitumia mwanzoni katika 1 Kor. 4:3.matumizi yake yalizidisha kejeli.

**6:3 "Hamjui ya kuwa mtawahukumu malaika"** Sarufi ilitegemea jibu la "ndio". Waaminio ni wenye mamlaka ya juu ya kiroho kuliko malaika. Ni vigumu kwa waaminio kunaswa katika huu ulimwengu ulioanguka, kutambua msimamo wetu wa kweli wa kiroho (kama vile 1 Kor. 13:12).Malaika waliumbwa kama watumishi wa Mungu na wa kumkomboa mwanadamu (kama vile Ebr. 1:14). Ni binadamu ambaye aliumbwa katika sura na mfano wa Mungu (kama vile Mwa. 1:26-27), sio malaika. Ni kwa binadamu ambao Yesu alitoa maisha yake, sio kwa malaika (kama vile Ebr. 2:14-16). Waaminio siku moja watahukumu malaika (yaani., malaika waasi, kama vile Mwa. 6; Mt. 25:41; 2 Pet. 2:4-9;Yuda 6 au malaika wote kama sitiari ya utawala wa ulimwengu, Dan. 7:22, 27).

Kulingana na theolojia ya walimu wa sheria za kiyunanai malaikak daima wamekuwa na wivu wa Upendo wa Mungu,uangalizi, na utoaji kwa biadamu aliyeanguka.maandiko mbali mbali ya Kiyahudi juu ya maangamizo ya siku ya mwisho yanadai kwamba uasi wa Shetani ulihusiana na amri ya Mungu juu ya kuitumikia jamii ya Adamu.

◙ **"basi si zaidi sana"** Hii inahaksi KIANGAMA KISHIRIKISHI cha nguvu (yaani, *ge*), ambacho hutumika kuonyesha msisitizo (kama vile Moulton's *Analytical Lexicon*, Revised, uk. 75). Utofauti wa kejeli uko dhahiri.

**6:4 "mkiwa"** Hii ni SENTENSI YENYE MASHARTI DARAJA LA TATU, ambayo ina maana ya uwezekano wa kitendo.

◙ " **mwawaweka"** Kuna njia nyingi zinazowezekana kukitafsiri kifungu hiki. Nadharia ni

1. KAULI ELEKEZI (kauli), "unaanzisha"
2. KAULI YA KUULIZA (swali), "Je! unaanzisha?"
3. KAULI YA MSHANGAO (kama vile NJB, NIV), "umeanzisha!"
4. KAULI SHURUTISHI (amri), "kuanzisha"

Jambo ni kwamba angalau Mkristo anapaswa kuwa na uwezo wa kuhukumu mambo rahisi na ya kawaida ya kidunia. Kujaribu kufafanua chaguzi zaidi, kuna njia mbili za kutazama maandishi haya: (1) inarejelea kwa waamuzi wa kipagani au (2) inarejelea angalau kwa washirika muhimu wa Kanisa.Ikiwa hivyo basi, inaendeleza kejeli.

**NASB, NJB" hao waliohesabiwa kuwa si kitu "**
**NKJV"hao waliohesabiwa kuwa sio kitu"**
**NRSV, TEV"Hao wasiokuwa na nafasi"**

Neno hili (yaani, *exoutheneō*, KAULI TENDEWA ENDELEVU YA WAKATI TIMILIFU) sana lilitumiwa na Paulo katika 1 Kor. 1:28 kuonyesha kwamba Mungu hutumia "mambo ya msingi," "ya kudharauliwa," "mambo ambayo siyo" kufadhaisha hekima ya ulimwengu ili Mungu mwenyewe akapate kutukuzwa. Hapa inaonyesha kudokeza wale walioko kanisani na wasio na nafasi au ujuzi wa uongozi. Kwa kiasi kidogo cha watu wa Mungu zaidi wametosheka kwa sababu ya hekima ya Mungu na Roho yule ashughulikae na matatizo kuliko waamuzi waioamini wa kidunia walioelimika na wenye uzoefu.

◙ **"kanisa"** Angalia Mada Maalumu katika 1 Kor. 1:2.

**6:5 "Nasema hayo nipate kuwatahayarisha"** Paulo hutumia neno hili mara nyingi (kama vile 1 Kor. 4:14; 6:5; 15:34; 2 The. 3:14; Tito 2:8). Kuaibisha ni moja ya zana za Roho ili kuleta badiliko na kuruhusu matendo ya imani na uaminifu na tabia kujengeka.Hii aya huendeleza kejeli inayoumiza.

◙ **"Je! Ndivyo, kwamba kwenu hakuna hata mtu mmoja mwenye hekima"** Hii ilikuwa kejeli inayoumiza kwa kanisa hili la wasomi wenye kiburi. Hili ni swali lenye kusisitiza likiwa na ukandamizi mara mbili ambalo linategemea jibu la"ndio." Angalia maelezo katika 1 Kor. 4:7.

**6:6 "tena mbele yao wasioamini"** Hakuna KIBAINISHI, kwa sababu hiyo, msisitizo ni juu ya ubora wa waamuzi wa kidunia wa "kipagani".-

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 1 WAKORINTHO 6:7-8**

**[7] Basi imekuwa upungufu kwenu kabisa kwamba mnashitakiana ninyi kwa ninyi. Maana si afadhali kudhulumiwa? Maana si afadhali kunyang'anywa mali zenu? [8] Bali kinyume cha hayo ninyi wenyewe mwadhulumu watu na kunyang'anya mali zao; naam, hata za ndugu zenu.**

**6:7 " Basi "** Tazama maelezo katika 1 Kor. 5:1.

◙**" imekuwa"** Kifungu hiki (yaani., *ēdē men oun*) kinadokeza kwamba kanisa hili tayari lilifanya mambo haya sana. Walikuwa tayari wameshindwa!

**NASB, NRSV"upungufu kwenu kabisa"**
**NKJV"upungufu kwenu kabisa"**
**TEV"mmeshindwa kabisa"**
**NJB"upungufu"**

Hii kiuhalisia ni "upungufu," lakini hutumika katika maana ya kushindwa au kutofaulu (kama vile 2 Kor. 12:13; Rum. 11:12; 2 Pet. 2:19-20).

**NASB, NRSV "Maana si afadhali kudhulumiwa? Maana si afadhali kunyang'anywa mali zenu"**
**NKJV "Maana si afadhali kudhulumiwa? Maana si afadhali kunyang'anywa mali zenu "**
**TEV "Je! Haingekuwa jambo bora zaidi kwenu kudhulumiwa? Haingekuwa bora zaidi kwenu kunyang'anywa mali zenu "**
**NJB "Kwa nini hampendelei udhalimu, Kwa nini hampendelei kunyang'anywa mali zenu"**

Hizi ni Kauli mbili TENDEWA ELEKEZI ZA WAKATI ULIOPO. Haki binafsi za waaminio sio muhimu kama mienendo na wito wa kanisa. Je! Pana Mkristo yeyote atakayeshinda ikiwa ufalme atapotea?

**6:8** kanisa la magharibi, likiwa na msisitizo wake juu ya ubinafsi, limeondoka nje ya kweli ya injili. Tumekosa muendelezo wa msisitizo wake juu ya yote, ushiriki, na mwili! Tunaona ukristo kama kitu fulani kwa sisi binafsi badala ya kitu fulani kwa injili.Tumeokolewa (ubinafsi) kuutumikia mwili (kama vile 1 Kor. 12:7). Waaminio wanapaswa kuendeleza mtazamo wa ulimwengu wa Agano Jipya, wautazame ulimwengu kupitia macho ya Mungu na ushirika, makusudi ya kiulimwengu (yaani, Mt. 28:18-20; Lk 24:47; Mdo1:8).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 1 WAKORINTHO 6:9-14**

**[9] Au hamjui ya kuwa wadhalimu hawataurithi ufalme wa Mungu? Msidanganyike; waasherati hawataurithi ufalme wa Mungu, wala waabudu sanamu, wala wazinzi, wala wafiraji, wala walawiti, [10] wala wevi, wala watamanio, wala walevi, wala watukanaji, wala wanyang'anyi. [11] Na baadhi yenu mlikuwa watu wa namna hii; lakini mlioshwa, lakini mlitakaswa, lakini mlihesabiwa haki katika jina la Bwana Yesu Kristo, na katika Roho wa Mungu wetu.**

**6:9-10** Paulo anahusika dhahili na maisha ya Wakristo binafsi (kama vile 1 Kor. 5 :10,11; 6:9-10), ambao wanatafakari juu ya kanisa. Wokovu sio tu tendo la kimahakama (yaani, uthibitisho kwa imani), ni maisha yaliyobadilika (yaani., utakaso au kuwa kama Kristo, kama vile Gal. 6:7). Angalia **MADA MAALUM: UTUKUFU/UTAKASO WA AGANO JIPYA (SPECIAL TOPIC: NEW TESTAMENT HOLINESS/SANCTIFICATION)** katika 1 Kor. 1:2.

Kanisa lilikuwa, na lina "danganyika" Hii ni KAULI TENDEWA SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO, ikiwa na KIAMBATA HASI, ambayo kwa kawaida inamaanisha kuzuia kitendo kilichoko katika mchakato.

**6:9 "Au hamjui"** Angalia maelezo katika 1 Kor. 5:6. Kidokezo ni kwamba waaminio, kwa sababu ya wokovu wao na Roho aishie ndani yao, wanapaswa kujua mambo haya! Lakini, watoto (wale walio wachanga), waaminio wa kimwili hawayajui!!! Kifikra wametawaliwa na mfumo wa ulimwengu huu ulioanguka na pepo wabaya (yaani, kujidanganya, kudanganyika kitamaduni, na kudanganyika kishetani, kama vile 1 Kor. 12:2).

◙ **" kuwa wadhalimu hawataurithi ufalme wa Mungu"** Paulo alisema hili mara mbili kwa ajili ya kusisitiza (1 Kor. 6:9, 10).Hii huleta mkanganyiko wa injili kwenye utofauti wa wazi. Wakovu ni bure katika kazi iliyomalizika ya Kristo, lakini wokovu wa kimaagano huhitaji mwitikio endelevu na unaofaa. Waaminio ambao wanadai "haki" katika Kristo wanapaswa kukomaa katika ufanano wa Kristo.Lengo la Mungu daima limekuwa juu ya watu wenye haki ambao wanaaksi tabia yake. Agano Jipya ni kama tu Agano la Kale katika mawazo haya. Asili ya msingi wa Agano Jipya (kama vile Yer. 31:31-34; Eze. 36:22-38) ni kwamba utendaji wa binadamu kwa ajili ya wokovu umechukuliwa nafasi yake na utendaji wa Kristo. Lakini hii haiathiri shauku ya Mungu kwa watu wenye haki. Inabadilisha tu utaratibu wa kufanya jambo. Katika wakati huu wa injili, waaminio wanahamasishwa kwa shukrani, sio kwa thawabu.

Hata hivyo, kanuni ya kiroho ya "kupanda na kuvuna" (kama vile Gal. 6:7) bado inafanya kazi kwa waaminio na wasioamini (kama vile sura 3). Haswa, ni msiba wa wakristo wasio na matunda (kama vile Yohana 15; Yakobo 2:14-26; 1 Petro; 1 Yohana). Inaathiri Ufalme, kanisa la mahali, mtu binafsi, na waliopotea.

Je! Mkristo ambaye amefanya dhambi iliyoorodheshwa katika 1 Kor. 6:9-10 ataokolewa? Kwa hakika (kama vile 1 Kor. 6:11)! Je! Mkristo aendelee kutenda hii dhambi na ataokolewa? Sio pasipo kupoteza matokeo ya ki-Mungu na ushirika pamoja na Mungu, kupoteza mwongozo wa Roho, kupotenza imani, kupoteza amani, kupoteza furaha, kupoteza mashahidi! Ni gharama gani hiyo tutakayolipa!

Kuna maandishi kadhaa katika Matendo na maandiko ya Paulo (kama vile Mdo 20:32; 26:18; 1 Kor. 6:9-10; 15:50; Gal. 5:21; Efe. 5:5) ambayo yanaaksi maneno ya Yesu juu ya kurithi ufalme wa Mungu (kama vile Mt. 25:34).

## MADA MAALUM: UASI *(APHISTĒMI) [*SPECIAL TOPIC: APOSTASY *(APHISTĒMI)*

## MADA MAALUM: URITHI WA WAAMINIO (SPECIAL TOPIC: BELIEVERS' INHERITANCE)

◙ **"Msidanganyike"** Hii ni KAULI TENDEWA SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO (*The Expositor's Bible Commentary*, juzuu. 10, uk. 223, husema ni KAULI YA KATI YA WAKATI ULIOPO, yaani, "acha kujidanganya mwenyewe ") na KIAMBATA HASI, ambacho kawaida kinamaanisha "zuia kitendo kilichoko katika utaratibu." Hii ni *asyndeton* kama 1 Kor. 6:18, ambacho kilikuwa ni kisarufi cha lugha ya kawaida ya Koine huko Uyunani juu ya msisitizo ambao ulileta kwa ajili ya usikivu wa msomaji au msikilizaji.

**NASB, NKJV,**
**NRSV"waasherati"**
**TEV"watu wasio waadilifu"**
**NJB"Asiye mwadilifu kimapenzi"**

Hili ni neno la pamoja likimaanisha zinaa (kama vile 1 Kor. 5:1 [mara mbili],9,10; 6:9,11,13,18; 7:2; 10:8; 2 Kor. 12:21). Aya 9-10 imeorodhesha dhambi zinazohusishwa kwenye karne ya kwanza na taratibu za ibada ya kipagani (kama vile 1 Kor. 5:9-11), ambayo mara kwa mara ilihusisha shughuli za kiuzinzi kwa jina la mungu wa anasa.

◙ **"waasherati"** Kwa muamini mwenye mtazamo wa Agano la Kale, hakuna chochote kibaya zaidi kuliko hiki. Matumizi ya neno hili katika orodha ya dhambi inathibitisha kwamba hii ni orodha ya utaratibu wa ibada za kipagani. Waamini wote wa mataifa katika Korintho wametokea kwenye mazingira haya (kama vile1 Kor. 6:11). Paulo alitumia hii dhana (yaani., ibada na kuiabudu miungu wa uwongo) mara nyingi katika barua za Wakorintho (kama vile1 Kor. 5:10,11; 6:9; 8:4,7,10; 10:7,14,19,28; 12:2; 2 Cor. 6:16).

◙ **"wazinzi"** Hili ni neno la Kiyunani *moichos*, ambalo linarejea juu ya kutokuwa mwaminifu kwenye mapenzi ya ndoa.Hii ndiyo sehemu pekee ambayo hutumiwa katika Barua ya Wakorintho.

**NASB" wala wafiraji"**
**NKJV, NJB" wala mfiraji "**
**NRSV"makahaba wa kiume"**
**TEV"Walawiti"**
**NJB “kujidekeza"**

Neno (*malakos*) kihalisia linamanisha kitu laini. Linaweza kutumiwa kwenye Nguo (kama vile Mt. 11:8). Wakati likitumiwa kisitiari kwa mtu linarejelea kwa kahaba wa Kiume, hasa vijana.Kwa makala nzuri juu ya ubasha tazama *Dictionary of Paul and His Letters*, kr. 413-414.

**NASB"ubasha"**
**NKJV, NRSV,**
**NJB"mfiraji"**
**TEV"(maneno yote hutafsiriwa pamoja kama 'ulawiti’)"**

Hili neno (*arsenokoitēs*, kutoka kwa *arsēn*, kiume, na *keitē*, mtu anayelala naye) inarejea juu ya ubasha/ngono ya jinsia moja ya kiume (kama vile 1 Tim. 1:10; Rum. 1:27). Hili lilikuwa tatizo kubwa katika jamii ya Warumi (kama vile Rum. 1:26-27; 1 Tim. 1:10) kama ilivyokuwa karibu na Mashariki ya kale (kama vile Law. 18:22; 20:13; Kum. 23:18). Maneno haya mawili yanayohusiana katika 1 Kor. 6:9 kwa ajili ya ulawiti yanaweza kurejea juu ya sura ya kiutendaji (*arsenokoitai*) na kutendewa (*malakoi*) ya dhambi hii.

Kuna shinikizo kubwa la kiutamaduni wa kisasa kukubali mapenzi ya jinsia moja kama mfumo wa maisha unaokubalika. Biblia inaishutumu kitendo hicho kama uharibifu wa mfumo wa maisha, nje ya mapenzi ya Mungu kwa uumbaji wake.

1. inakiuka amri ya Mwanzo 1 kuwa ya kuzaa matunda na kuongezeka
2. inaainisha ibada na utamaduni wa kipagani (kama vile Law. 18:22; 20:13; Rum. 1:26-27; na Yuda 7)
3. inafunua ubinafsi wa kujitegemea kutoka kwa Mungu (kama vile 1 Kor. 6:9-10)

Hata hivyo, kabla ya kuacha hii mada napenda nionyeshe mapenzi ya Mungu na msamaha kwa wanadamu wote waasi. Wakristo hawana haki ya kutenda kwa chuki na majivuno dhidi ya dhambi hii, hasa pale inapojulikana kuwa wote tunatenda dhambi. Maombi, mashaka, ushahidi, na huruma hufanya zaidi katika eneo hili kuliko laana kali. Maneno ya Mungu na Roho yake italaani ikiwa tutaviacha. Dhambi zote za kujamiiana, sio tu hii moja, ni za kuchukiza mno mbele za Mungu na zinapelekea hukumu. Tendo la ndoa ni zawadi kutoka kwa Mungu kwa ajili ya ustawi wa wanadamu, furaha, na jamii imara. Lakini nguvu hii, ushauri uliotolewa na Mungu mara nyingi hugeuka kuwa maisha ya uasi, ubinafsi, kutafuta anasa, "kujipendelea zaidi kwa gharama yoyote.” (kama vile Rum. 8:1-8; Gal. 6:7-8).

◙ **"watukanaji "** Angalia maelezo katika 1 Kor. 4:12.

**6:11 "Na baadhi yenu mlikuwa watu wa namna hii "** Hii ni KAULI ELEKEZI YA WAKATI USIOTIMILIFU, ambayo huelezea kitendo kinachoendelea cha wakati uliopita. Hii huonyesha maadili ya uchungu ya utamaduni wa

kipagani wa siku za Paulo (kama vile 1 Kor. 12:2), lakini pia huonesha neema ya kushangaza na nguvu ya kubadilika ya injili ya Mungu katika Kristo.

Maisha yaliyobadilishwa ya hawa wapagani walioongoka yalikuwa ushahidi wa nguvu sana kwa injili. Lakini mabadiliko lazima yawe ya kudumu na makamilifu, sio ya muda na kiuchaguzi.Wamekuwa tofauti sasa, wenye kuishi sasa, wenye kutaarifiwa sasa. Hawapaswi kurudi kama mbwa kwenye matapishi yake au nguruwe kwenye matope (kama vile 2 Pet. 2:22). Ulimwengu uliopotea unaangalia!

◙ **"lakini"** Angalia matoleo matatu yaliyo pamoja ya neno *alla* katika maandishi ya Kiyunani kuonyesha tofauti hizi tatu za matukio ya kiroho:

1. Kuosha
2. Kutakasa
3. kuhesabiwa haki kulikofanywa na Mwana na Roho kupitia mwitikio wetu wa imani na toba

◙ **"lakini mlioshwa"** Hii ni KAULI YA KATI ELEKEZI YA WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFU. Hii inaweza kurejea kwenye ubatizo kama alama ya tendo la ndani la utakaso wa awali, hiari, na unaoonekana (kama vile Mdo 2:38; 22:16; Tito 3:5). Tafsiri nyingi zinatafsiri hiki kifungu kama IRABU TENDWA isipokuwa tafsiri ya Williams yenye maneno "mmejitakasa wenyewe." Wabadili dini wa Kiyahudi walijibatiza wenyewe wakati wakijiunga na sinagogi. Ikiwa neno hili ni irabu ya kati kama Matendo 22:16, hii inaweza kuwa dokezo la kitheolojia kwa mjadala wa wajibu wa Agano katika Eze. 18:31 uliounganishwa wa mamlaka ya ki-Mungu (kama vile Eze. 36:25-27). Hii yaweza kuwa ni sitiari ya utakaso (kama vile Tito 3:15).

◙ **"lakini mlitakaswa"** Hii ni KAULI TENDEWA ELEKEZI YA WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFU Kwa njia ya kifo cha Kristo na upatanisho wa Roho (kama vile 1 Kor. 1:2,30). Angalia **MADA MAALUM: UTAKATIFU/UTAKASO WA AGANO JIPYA (SPECIAL TOPIC: NEW TESTAMENT HOLINESS/SANCTIFICATION** katika 1 Kor. 1:2.

◙ **"lakini mlihesabiwa haki"** Hii ni KAULI TENDEWA ELEKEZI YA WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFU. Waaminio wote watahesabiwa haki na kutakaswa wakiamini (kama vile Rum. 8:29). Msimamo huu wa kithiolojia wa mahali unaruhusu kuishi maisha yanayofanana kama Kristo Angalia **MADA MAALUM: HAKI (SPECIAL TOPIC: RIGHTEOUSNESS)** katika 1 Kor. 1:30.

◙ **"haki katika jina la Bwana Yesu Kristo, na katika Roho wa Mungu wetu"** Kifungu hiki yumkini kinathibitisha ufasiri ya kwamba "kuoshwa" au "kujitakasa" katika 1 Kor. 6:11 inarejerea kwenye ubatizo (kama vile Rum. 10:9-13).Kazi ya wazi ya kanisa la awali kuhusu imani ilikuwa ni ubatizo. Waliochaguliwa wanathibitisha imani yao kwa kutamka kwa maneno "Na amini Yesu ni Bwana" au ukiri unaofanana wa kiluturujia.

Kifungu cha pili kinachotaja neno "Roho" kinaweza kuwa dokezo au njia ya kiliturujia iliyoegamia kwenye Mt. 28:19, "wakibatiza katika jina la Baba na la Mwana na Roho Mtakatifu." Inafurahisha jinsi gani Paulo mara nyingi anavyorejea kwenye neno "kwa jina "katika sura za ufunguzi wa 1 Wakorintho (angalia Mada Maalumu katika 1 Kor. 1:10).

1. njia ya kurejelea kwa waaminio ("ambao. . .wanaliita jina la Bwana," kama vile 1 Kor. 1:2)
2. njia nya kuwatia moyo waaminio (kama vile 1 Kor. 1:10)
3. njia ya kutetea mamlaka ya Paulo (kama vile 1 Kor. 5:4)
4. njia ya kurejelea kitendo cha awali cha waamini cha kulitumia jina la Bwana(kama vile 1 Kor. 6:11)

Jina la Bwana huwakilisha Utu wa Yesu, mamalaka, sifa, na hadhi.

Hii ni rejea dhahiri ya kazi ya ukombozi ya utatu wa Mungu (kama vile 1 Kor. 6:10-11). Neno "utatu" sio neno la kibiblia, lakini dhana ni kuwa. Ikiwa Yesu ni Mungu na Roho ni mtu, basi asili moja ya Roho wa Uungu ina utatu wa milele, udhihilisho binafsi. Angalia **MADA MAALUM: UTATU (SPECIAL TOPIC: TRINITY)** katika 1 Kor. 2:10.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 1 WAKORINTHO 6:12-20**

**[12] Vitu vyote ni halali kwangu, lakini si vyote vifaavyo; vitu vyote ni halali kwangu, lakini mimi sitatiwa chini ya uwezo wa kitu cho chote. [13] Vyakula ni kwa tumbo, na tumbo ni kwa vyakula; lakini Mungu atavitowesha**

**vyote viwili, tumbo na vyakula. Lakini mwili si kwa zinaa, bali ni kwa Bwana, naye Bwana ni kwa mwili. [14] Naye Mungu alimfufua Bwana, na tena atatufufua sisi kwa uweza wake. [15] Je! Hamjui ya kuwa miili yenu ni viungo vya Kristo? Basi nivitwae viungo vya Kristo na kuvifanya viungo vya kahaba? Hasha! [16] Au hamjui ya kuwa yeye aliyeungwa na kahaba ni mwili mmoja naye? Maana asema, Wale wawili watakuwa mwili mmoja. [17] Lakini yeye aliyeungwa na Bwana ni roho moja naye. [18] Ikimbieni zinaa. Kila dhambi aitendayo mwanadamu ni nje ya mwili wake; ila yeye afanyaye zinaa hutenda dhambi juu ya mwili wake mwenyewe. [19] Au hamjui ya kuwa mwili wenu ni hekalu la Roho Mtakatifu aliye ndani yenu, mliyepewa na Mungu? Wala ninyi si mali yenu wenyewe; [20] maana mlinunuliwa kwa thamani. Sasa basi, mtukuzeni Mungu katika miili yenu.**

**6:12**
**NASB, NKJV**
**NRSV" Vitu vyote ni halali kwangu"**
**TEV"mtu anaweza kusema, 'nimekubalika kufanya chochote"**
**NJB"Kwang Mimi vitu vyote vimeruhusiwa"**

Hii inaweza kurejea kwa kitu fulani Paulo alichosema juu ya tukio la awali (kama vile 1 Kor. 10:23; Rum. 14:2,14,20) lakini imeondolewa katika mazingira haya kwa (1) ushikiliaji wa sheria kwa waamini wa kiyahudi au (2) walimu wakware wa uongo ambao hutumia uhuru wa mkristo kama kibali cha kutenda dhambi (kama vile Gal. 5:13; 1 Pet. 2:16). Paulo alijaribu kutembea vyema kati ya wakatili wawil na bado akazungumza na wote.

Hii inaweza kuwa nukuu ya kwanza ya Paulo ya wito wa walimu wa uongo au walimu wa uongo wanaongea kitu fulani nje ya mazingira aliyohubiri na kueneza misemo yake katika meneneo mengine (kama vile 1 Kor. 6:12,13; 7:1; 8:1,4; 10:23, tazama (1) *The Cambridge History of the Bible*, vol. 1, uk. 244, na (2) Klein, Blomberg, na Hubbard, *Introduction to Biblical Interpretation*, kur. 362-363).Sio kwamba walichokisema kilikuwa sio kweli, lakini walichukulia ukweli nyuma ya mipaka ya kisheria. Ni vigumu kujua wakati gani Paulo hutumia mbinu hii.Inawezekana vigezo vifuatavyo vinaweza kusaidia.

1. Ni kitu fulani Paulo mwenyewe alikisema katika maandiko mengine (kama vile 1 Kor. 10:23; Rum. 14:2,14,20).
2. Ni maelezo mafupi ya ujumla ya ukweli (kama mithali).
3. Sitiari zote za kibiblia ni kweli, lakini zina kikomo kwenye matumizi yake muhimu. Hakuna mfano au sitari ambayo inaweza kusogezwa mbele kwa kila ngazi. Mara kwa mara pamekuwepo na tumizi moja kubwa.

Paulo anajaribu kurudia tena ukweli uliokusudiwa na kuzuiya mwendelezo usio sahihi. Hili ni jambo la kanuni za ufasiri katika kila enzi!

◙ **"lakini si vyote vifaavyo"** Aya hii inazungumza juu ya matumizi mazuri ya uhuru wa mkristo ambao lazima kutumiwa katika upendo wa kujizuia (kama vile 1 Kor. 10:23; 14:26; Rum. 14:19; 15:2). Kujenga mwili wa Kristo ni muhimu zaidi kuliko haki binafsi na uhuru.

◙ **"vifaavyo"** Hili ni neno ambatani la Kiyunani ambalo linamaanisha "weka pamoja kwa manufaa ya mtu" (kama v ile 1 Kor. 6:12; 7:35; 10:23; 12:7; 2 Kor. 8:10, kinyume katika 1 Kor. 12:1).Haya ni maelezo ya Paulo yanayofanana katika katika Rum. 14:19; 15:2; 1 Kor. 10:23; 14:26; 2 Kor. 12:19; Efe. 4:12,29. Kwa sababu tu kuwa muamini huru katika Kristo haimaanishi kwamba kila jambo huadilisha waaminio wengine. Tunazuilia uhuru wetu katika upendo kwa ajili ya Bwana na Kanisa lake. Daima tunatafuta na kukuza afya na uzima wa mwili wote wa Kristo (kama vile 1 Kor. 12:7).

**NASB" lakini mimi sitatiwa chini ya uwezo wa kitu cho chote "**
**NKJV"lakini sitaki kutawaliwa na kitu chochote"**
**NRSV"lakini siwezi kuongozwa na kitu chochote"**
**TEV"sitaki kuruhusu chochote kinifanye mtumwa wake"**
**NJB"lakini nimeamua kutokutawaliwa na kitu chochote"**

Hii ni KAULI TENDWA ELEKEZI YA WAKATI UJAO ya neno la Kiyunani *exousia*. Neno hili lina mawanda mapana ya matumizi

1. Mamlaka
2. Utekelezaji wa sheria
3. Madaraka ya kuongoza
4. Nguvu
5. Nguvu ya ajabu

Paulo angeweza kuwa na baadhi ya vidokezo hivi katika fikra kwenye muundo huu. Kuna dhihaka ya wazi kati ya neno "kuhalishwa kisheria" (*exestin*) na "mwenye ustadi mkubwa" (*exousiasthēsomai*). Yeye hakuwa na hisia kwamba

1. Mwandamu yoyote hana haki ya kumuhukumu (kama vile 1 Kor. 2:14-15; 3:4-5)
2. Hakuna kiumbe mwenye mamlaka juu yake (kama vile 1 Kor. 12:2, wasioamini wanaongozwa na pepo wabaya)
3. Hakuna uhuru wa kibinafsi au upendeleo wa kibinafsi au majaribu ya kibinafsi (yaani., *tinos*, ni KIVUMISHI CHA KIWAKILISHI NOMINO CHA UMOJA KISICHO CHA WAZI katika utofauti wa matumizi mawili ya *panta* katika aya hii)

Mamlaka ya Paulo yalikuwa kutoka kwa Kristo. Alikuwa Kristo na Roho wake aliyemthibiti na kumpa nguvu. Kujizuia hakika ni moja ya matunda ya Roho (kama vile Gal. 5:23; Mdo24:25; 2 Pet. 1:6).Paulo alithibiti uhuru wake ili kwamba injili iweze kuendelea mbele na hivyo tunapaswa nasi!

Paulo anadai kwamba uhuru wa Mkristo usipewe kipaumbele kwa kibali binafsi. Mambo mengi ambayo ni mazuri yanaweza kuwa malengo, mitazamo, au hali zisizofaa (kama vile Rum. 14:23). Hili sula la uhuru wa Mkristo na wajibu wa mkristo ni suala mtambuka kwa barua za Wakorintho. Suala hili pia linashughulika na Rum. 14:1-15:13. Ningependa kunukuu maoni yangu ya ufunguzi juu ya somo hili kutoka kwenye fasiri ya Warumi.

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA KUTOKA KWA WARUMI 14:1-15:13

A. Sura hii hujaribu kulinganisha mkanganyiko uliopo kati ya uhuru wa mkristo na wajibu wa Mkristo. Sehemu ya fasihi hushughulika kupitia 15:13.

B. Tatizo ambalo huhimiza sura hii yumkini ni mvutano kati ya watu wa mataifa na waamini wa Kiyahudi katika kanisa la Warumi. Kabla ya kuongoka Wayahudi walijifanya kuwa washikiliaji mno wa sheria na wapagani walijifanya kuwa wasio na maadili. Kumbuka, sura hii imehutubiwa kwa wafuasi waaminifu wa Yesu. Sura hii haikuhutubia kwa ajili waamini walio mwilini (kama vile1 Kor. 3:1). Lengo kubwa zaidi limewekwa kwa ajili ya makundi yote. Kuna hatari kwenye miisho ya pande zote.Mjadala huu sio ruksa ya uhakiki wa ushikiliaji mno wa sheria au kutamba kwa ukarimu.

C. Waaminio wanapaswa kuwa waangalifu kutokufanya theolojia au maadili yao kuwa kipimo kwa waamini wengine (kama vile 2 Kor. 10:12). Waaminio wanapaswa kutembea katika mwanga walionao, lakini wakielewa kwamba theolojia yao sio ya moja kwa moja ndiyo theolojia ya Mungu. Waaminio bado wanaathiriwa na dhambi. Tunapaswa kuwatia moyo, kuwashawishi, na kufundishana kutoka kwenye Maandiko Matakatifu, sababu, na uzoefu, lakini daima katika upendo. Kwa namna mtu anavyojua kuwa anajua kumbe ndivyo anavyojua kuwa hajui (kama vile 1 Kor. 13:12)!

D. Mtazamo na malengo ya mtu mbele za Mungu ni funguo halisi katika kutathmini matendo yake. Wakristo watasimama mbele ya Kristo ili kuhukumiwa kwa namna waliyotendeana (kama vile 1 Kor. 6:10,12 na 2 Kor. 5:10).

E. Martin Luther alisema, "Mwanaume Mkristo ni Bwana aliye huru kwa wote, hahusiki kwa yeyote; mwanaume mkristo ni mtumishi mwajibikaji kwa wote, anahusika kwa wote." Ukweli wa kibiblia mara nyingi umewasilishwa katika mkanganyiko iliyojazwa wasiwasi.

F. Somo hili ngumu lakini muhimu linashughulika na sehemu ya fasihi yote ya Warumi 14:1-15:13 na pia katika 1 Wakorintho 8-10 na Wakolosai 2:8-23.

G. Hata hivyo, inahitaji kuelezwa kwamba hali ya uwingi miongoni mwa waaaminio watiifu sio kitu kibaya. Kila muamini ana nguvu na madhaifu yake.kila mtu anapaswa kutembea katika nuru aliyonayo yeye, daima jiweke wazi kwa Roho na Biblia kwa ajili ya uelewa zaidi. Katika wakati huu wa kuangalia kupitia kioo kilichotia giza (1 Kor. 13:8-13) mtu lazima atembee katika upendo (1 Kor. 6:15), na amani (1 kor. 6:17,19) kwa ujenzi wa maadii wa pande mbili.

H. sifa ya, ya neno “mwenye nguvu” na “aliye dhaifu” ambayo Paulo huwapa makundi haya, huwaathiri wao kwetu sisi.Hii hakika ilikuwa sio nia ya Paulo.Makundi yote walikua waamini watiifu. Hatutajaribu kuwachambua Wakristo wenginetoka ndani mwetu! Tunaridhiana sisi kwa sisi katika Kristo!

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA KWA WARUMI 15:1-13

A. Mjadala kuhusu uhuru wa Mkristo na wajibu wake unaendelea kutoka kwenye sura ya 14.
B. hoja yote inaweza kuelezewa kama
   1. Kukubaliana sisi kwa sisi kwa sababu Mungu anatukubali katika Kristo (kama vile 1 Kor. 14:1,3; 15:7);
   2. Tusiukumiane kwa sababu Kristo ndiye Bwana wetu na mwamuzi (kama vile 1 Kor. 14:3-12);
   3. Upendo ni muhimu zaidi kuliko uhuru wa kibinafsi (kama vile 1 Kor. 14:13-23);
   4. Kuufuata mfano wa Kristo na kuweka haki zako kwa ajili ya ujenzi wa maadili na uzuri kwa wengine (kama vile 1 Kor. 15:1-13).
C. Rum. 15:5-6 inahaksi kusudi fungamani la mazingira yote ya 1 Kor. 14:1-15:13
   1. kuishi katika amani na mtu mwingine;
   2. kuishi kwa mujibu wa mfano wa Kristo;
   3. Kwa uunganishaji wa mioyo na midomo hutoa sifa ya umoja kwa Mungu.
D. Mvutano huo huo kati ya uhuru binafsi na wajibu wa pamoja unajihusisha na 1 Kor. 8-10 na Kol. 2:8-23.

**6:13**
**NASB"vyakula ni kwa tumbo "**
**NKJV"vyakula ni kwa tumbo na tumbo kwa vyakula"**
**NRSV"chakula ni kwa ajili ya tumbo, na tumbo ni kwa ajili ya chakula"**
**TEV"unaweza sema, 'chakula ni kwa ajili ya tumbo, na tumbo ni kwa ajili ya chakula'"**
**NJB"vyakula ni kwa tumbo, na tumbo ni kwa vyakula"**

Hii inaweza kuwa kauli wito mwingine. Inaonekeana kurejea kwenye mvutano usiofaa, wa kanuni za ufasiri kwa walimu wakware wa uongo. Paulo anadai kuwapo na chembe chembe ya ukweli katika kile wanachokisema (kama vile Marko 7:19). Paulo ni mojawapo

1. Hutumia mbinu ya kifasihi ya makemeo, mahali pale ambapo wapinzani hutumia thiolojia yake kutengeneza hoja
2. Hunukuu wito wa walimu wa uogo, baadhi ya sehemu zinazotokana na mafundisho ya Yesu au mafundisho ya Paulo

◙ **"lakini Mungu atavitowesha vyote viwili"** Hili ni dokezo kwa ufalme uliokamilishwa. Chakula ni sehemu tu ya wakati, sio umilele. Yesu alikula samaki baada ya Ufufuo wake (yaani., Yohana 21), lakini hiyo ilikuwa nafasi ya kuwatembelea wanafunzi wake wenye hofu,halikuwa hitaji lake muhimu la wazi. Yesu pia aliongelea kuhusu kuandaa dhifa ya Kimasihi (yaani, Luka 22:30), lakini hili, pia, ni sitiari ya ushirika, sio muhimu kimwili ili kurudiwa.

Kifungu "kuondoa" (kama vile NASB) au"kuharibu" (kama vile NKJV) ni *katargeō*. Paulo hutumia neno hili mara ishirini na saba, lakini katika maana tofauti. Tazama Mada Maalumu: *Katargeō* katika 1 Kor. 1:28.

◙ **"Lakini mwili si kwa zinaa"** Hii wazi inaonyesha uenezi wa uongo. Binadamu ameumbwa kwa ajabu kwa ajili ya maisha na maendeleo yake katika sayari hii. Hata hivyo, kuna baadhi ya mipaka aliyopewa na Mungu kuhakikisha kuweza kuishi maisha marefu, yenye furaha, na ya kuzaa matunda.Tangia kwenyeanguko (kama vile Mwanzo 3), binadamu anajaribu kunyakua kilicho cha haraka, kinachomtosha binafsi, kinachomfurahisha binafsi kwa gharama yoyote!

◙ **"mwili. . . bali ni kwa Bwana, naye Bwana ni kwa mwili"** Vifungu hivi viko kwenye uhusiano unaofanana. Msukumo unaonekana kwamba waamini ni wa Bwana (kama vile 1 Kor. 6:20; 7:23; Mdo 20:28). Anataka kutumia miili yao kwa huduma yake, makusudi yake. Hili linaweza kuwa dhihaka juu ya mwili wa binadamu na kanisa la Kristo kama mwili.

**6:14** Sura bora kabisa katika Agano Jipya juu ya ufunuo wa Kristo na ufunuo wa waaminio ni 1 Wakorintho 15.

Katika uelewa wa kifikra za Wayahudi (yaani., mwili wa nyama ni mwovu) inahitaji kusisitizwa kuwa fikra za kibiblia hazipunguzi mwili. Katika mazingira haya mwili

1. Uliumbwa " kwa ajili ya Bwana " (kama vile 1 Kor. 6:13)
2. "washirika wa Christo " (kama vile 1 Kor. 6:15)
3. Hekalu ambamo Roho hukaa ndani yake (kama vile 1 Kor. 6:19)
4. Kumtukuza Kristo (kama vile 1 Kor. 6:20)

Mwili sio muovu. Utafufuliwa na utakuwa sehemu ya ufalme wa milele. Hata hivyo, pia ni ulimwengu wa majaribu na uwanja wa mapambano ya maadili ya dhambi. Yesu alijitoa kimwili kwa kanisa. Waaminio wanapaswa kufuata mfano wake (kama vile 1 Yohana 3:16).

◙ **"Naye Mungu alimfufua Bwana"** Katika *A Textual Commentary of the Greek New Testament* Bruce M. Metzger huelezea utofauti wa machapisho ya Kiyunani yaliyohusianishwa kwenye NJEO YA KITENZI:

1. WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFU katika MSS $P^{46}$, $C^2$, B
2. WAKATI ULIOPO katika MSS $P^{11}$, $P^{46}$, A, $D^*$
3. WAKATI UJAO katika MSS $P^{46}$, $C^1$, א, C, $D^3$

Njeo ya WAKATI UJAO inaendana na mazingira na mfanano wa 2 Kor. 4:14" (uk. 552; $UBS^4$ inaipa daraja "B" [karibu na hakika]).

Kifungu hiki ni nafasi nzuri sana kuonyesha kwamba Agano Jipya mara nyingi linamatokeo ya kazi za ukombozi kwa Uungu wa wote watatu.

1. Mungu Baba alimuinua Yesu (kama vile Mdo 2:24; 3:15; 4:10; 5:30; 10:40; 13:30,33,34,37; 17:31; Rum. 6:4,9; 10:9; 1 Kor. 6:14; 2 Kor. 4:14; Gal. 1:1; Efe. 1:20; Kol. 2:12; 1 The. 1:10)
2. Mungu Mwana alijiinua mwenyewe (kama vile Yohana 2:19-22; 10:17-18)
3. Mungu Roho alimuinua Yesu (kama vile Rum. 8:11)

◙ **"na tena atatufufua sisi kwa uweza wake"** Paulo anafurahia uhusiano wake binafsi wa sasa akiwa na Kristo (kama vile 1 Kor. 6:17). Huu ni uelewa wa Paulo wa matukio ya siku za mwisho au kiyama (kama vile C. H. Dodd). Katika maana halisi mbingu ilimwijilia Paulo ndani ya maisha yake na pia ataongezewa katika maisha yake ya baadaye.

Paulo pia aliamini kwamba Yesu atarudi hivi karibuni. Katika baadhi ya maandishi Paulo anadai kwamba atakuwa hai wakati wa kurudi kwa Kristo (kama vile 1 The. 4:17; 1 Kor. 15:51-52; Flp. 3:20). Hata hivyo, katika maandishi mengine anajihusianisha na wale ambao watafufuliwa kutoka kwenye wafu (kama vile 1 Kor. 6:14; 2 Kor. 4:14). Kitabu chote cha 2 Wathesalonike hutarajia kucheleweshwa kwa ujio wa mara ya pili, kama kulivyofanyika katika sehemu za Mathayo 24, Marka 13, na Luka 21.

Kuja kwa Yesu mara ya pili ni tumaini la kila kizazi cha mkristo, lakini unabaki kuwa ukweli wa kizazi kimoja pekee. Hata hivyo, ufufuo pamojana mwili wake mpya na ushirika wa moyoni ni ukweli kwa waaminio wote!

**MADA MAALUMU:UTAYARI WA YESU KURUDI WAKATI WOWOTE DHIDI YA UCHELEWAJI WA KURUDI (SPECIAL TOPIC: THE ANY-MOMENT RETURN OF JESUS CHRIST VERSUS THE NOT YET)**

**6:15 "Je! Hamjui "** Angalia maelezo katika 1 Kor. 5:6.

◙ **"miili yenu ni viungo vya Kristo"** Paulo hutumia mfanano wa kutoka Mwa. 2:24 kama msingi kwa onyo kuhusu umoja wa waaminio kwenye zinaa ya aina yoyote. Waaminio wamekuwa mwili wa Kristo (kama vile 1 Kor. 12:20,27; Rum. 12:5; Efe. 4:12,16,25).

◙ **" kahaba"** Hili ni neno la Kiyunani *pornē*, ambalo linalotoka kwenye KITENZI "kuuza" (yaani., *pernēmi,* kama vile Kittel, *Theological Dictionary of the New Testament*, juzuu. 6, uk. 580). Katika Korintho (Karibu na Mashariki ya Kale) kuna aina mbili ya ukahaba, moja wa kimadhehebu (yaani., ibada ya kipagani) na utumwa (yaani.,iliyoendeshwa kwa faida). Paulo mara kwa mara alijadili *porneia* (kama vile 1 Kor. 5:1 [mara mbili]; 9,10,11; 6:9,13,15, 16,18; 7:2; 10:8; 2 Kor. 11:21).ustawi wa ibada za kipagani ilielezewa katika tendo la kujamiiana.

Wasikiaji katika siku za Paulo walikuwa wakishiriki katika matambiko haya na taratibu za ibada hizi, lakini sasa ni wakristo!

**NASB"hasa"**
**NKJV"hakika sio"**
**NRSV"kamwe"**
**TEV"hata kidogo"**
**NJB"nje ya swali"**

Kifungi hiki cha kimshangao (nadra DHAMIRA YENYE UCHAGUZI huonyesha matakwa makubwa,tamaa, au maombi) hutumiwa mara nyingi na Paulo kuelezea wasiwasi wake kwa namna baadhi yao wanavyoitikia (yaani., makemeo) kwenye kauli zake au maswali yasiodai majibu (kama vile Rum. 3:4; 6:31; 6:2,15; 7:7,13; 9:14; 11:1,11; 1 Kor. 6:15; Gal. 2:17; 3:21; 6:14).

**6:16 "WALE WAWILI WATAKUWA MWILI MMOJA"** Hii ni nukuu kutoka Mwa. 2:24. Katika ndoa watu wawili kwa hiari watakuwa mwili mmoja. Urafiki wa karibu sana wa kimwili ni uzoefu wa uhusiano wa nguvu.Ina nafasi sahihi, iliyowekwa na Mungu katika maisha.kama zilivyo zawadi zingine zilizotolewa na Mungu,inaweza kutumika vibaya na kuchukuliwa zaidi ya mipaka ya Mungu iliyotolewa.

**6:17** Huu ni mfanano wa kiroho ulichukuliwa toka Mwa. 2:24. Kama mume na mke watakuwa mwili mmoja kimwili, muamini na Bwana wake watakuwa kitu kimoja kiroho (kama vile Yohana 17:11,23; Gal. 2:20; Efe. 5:21-33). Mfano mzuri wa dhana hii ya kitheolojia ni Rum. 6:1-11. Waaminio wanafao katika Kristo, watazikwa (katika ubatizo) na Kristo, na watafufuliwa pamoja na Kristo.

**NASB"lakini yeye aliyeungwa"**
**NKJV"yeye aliyejiunga"**
**NRSV"yoyote aliyejiunga"**
**TEV"yeye atakayejiunga"**
**NJB"yeyote ambaye atajiunga"**

Hii haswa inafanana na 6:16. Uundwaji wa kisarufi ni

1. KAULI TENDWA ENDELEVU YA WAKATI ULIOPO kama 1 Kor. 6:16 (kama vile Zerwick na Grosvenor, *A Grammatical Analysis of the Greek New Testament*, uk. 508)
2. KAULI YA KATI ENDELEVU YA WAKATI ULIOPO (kama vile Harold K. Moulton, *The analytical Greek Lexicon Revised*, uk. 236)

Ufasiri mlinganyo wenye nguvu (yaani., TEV, NJB), vivyo hivyo pia na toleo la NASB, inaitafsiri kama IRABU YA KATI. Ni dhahiri kwamba mazingira yanalenga juu ya sehemu za hiari zinazohusika

**6:18 "Ikimbieni zinaa "** Hii ni KAULI TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO ikiwa bila kiunganishi cha kisarufi kwa kile kinachoendela kabla au baada (yaani., *asyndeton*), ambayo kwa wasomaji wa lugha ya kawaida ya Koine huko Uyunani ilikuwa njia ya kusisitiza iliyosababisha kifungu kusimama.

Tendo la ndoa ni zawadi toka kwa Mungu mwenye rehema, lakini kuna vipengele vinavyofaa na visivyofaa kwa namna gani mtu hutumia zawadi hii ya Mungu. Paulo anathibitisha ndoa kwa nukuu yake ya Mwa. 2:24, lakini anaweka mipaka imara juu ya uasherati kabla ya ndoa au uzizi nje ya ndoa. Waaminio wanapaswa siku zote kuwa waangalifu katika eneo hili, hasa utamaduni unapokosa maadili. Dhambi ya kujamiiana ni tatizo kubwa kwa maisha ya imani. Waamini wanapaswa kuishi kijinsia katika maisha sahihi yaliyobadilishwa (kama vile 2 Kor. 12:21; Efe. 5:3; Kol. 3:5).

◙ **" Kila dhambi aitendayo mwanadamu ni nje ya mwili wake "** Hii ni hoja ngeni. Natamani niielewe vizuri . Inaweza kuaksi

1. Utamaduni wa wapagani wa Korintho
2. Mafundisho ya kusisitiza ya walimu wa uongo
3. Kuhubiri msisitizo wa Paulo (kama vile 1 Kor. 6:12, 13)

Mwanadamu hana roho, wao ni roho (kama vile Mwa. 2:7). Ikihusianishwa na uelewa wa Paulo waamini hawana mwili, bali wao ni mwili. Yumkini haya ni maendeleo ya kitheolojia kutoka Mwanzo na kinyume na fikra za Wayunani kwamba kuupunguza mwili ni kosa. Agano la Kale na Agano Jipya huthibitisha ufufuo wa kimwili ambao ni njia ya kuthibitisha uzuri na umilele wa adhabu ya kuishi kwa binadamu. Baadaye waalimu wenye mafunuo ya ukware wangetofautisha vipengele vya kimwili kutoka kwenye vipengele vya kifikra, hivyo kuthibitisha wokovu kama maarifa mbadala yenye kumcha mungu au yenye haki. Paulo huthibitisha kwamba injili ni

1. Mtu kuwakaribisha
2. Ukweli kuhusu mtu huyo kuamini
3. maisha ya mtu huyo kuiga

Hizi haziwezi kutenganishwa! Binadamu ni wamoja. Wakovu umetimilizwa. Ufalmewa Mungu umetujilia. Kuna dhamana isiovunjika kati ya imani na utii. Utakaso wa mwanzo lazima uuongoze ule utakaso endelevu. Haki ni vyote zawadi (ELEKEZI) na amri (SHURUTISHI).

Mwenzangu katika Chuo Kikuu cha Texas baptisti huko Mashariki, Dr. Bruce Tankersley, alinikumbusha kwamba katika ukahaba wa kimadhehebu, kahaba ni mbadala kwa Uungu. Kwa hiyo, uhusiano wa kijinsia ulikuwa sio uovu pekee, lakini pia wa kuabudu sanamu

**6:19 "Au hamjui "** Angalia maelezo katika 1 Kor. 5:6.

◙ **" ya kuwa mwili wenu ni hekalu la Roho Mtakatifu "** Ukristo hubadilisha hekalu la kimwili la Wayahudi na hekalu la kiroho la mwili wa Kristo (kama vile Yohana 2:21) kama mwili wake wa ushirika, ambao ni kanisa (kama vile 1 Kor. 10:16,17; 11:29; 12:12-27).Dhana hii ya hekalu hutumika katika maana mbili katika 1 Wakorintho.

1. Katika 1 Kor. 3:16-17 hutumika kwa kanisa lote la mahali
2. Hapa hutumika kwa muamini binafsi

Hii huelezea uhusiano usio imara kati ya sura ya ushirika na sura ya kibinafsi.

Jambo kuu la Paulo katika mazingira haya ni wito wa utakatifu. Waaminio wanatakiwa kuwa tofauti kwa kiasi kikubwa kutokana na tamaduni zinazowazunguka. Hili lina makusudi mawili.

1. Inakamilisha lengo la kufanana na kristo
2. Inawavutia watu kuingia kwenye imani kupitia kristo, ambayo ndiyo kitovu pacha cha agizo kuu (kama vile Mt. 28:19-20)

◙ **"Roho Mtakatifu aliye ndani yenu"** Huu ni msisitizo juu ya Roho Mtakatifu akaaye ndani mwetu. Nguvu kwa maisha ya Mkristo ni zawadi ya Mungu, kama ulivyo wokovu. Tunapaswa kujitoa wenyewe kwa kazi ya Roho. Watu wote wa utatu hukaa ndani ya muamini.

1. Roho (kama vile Yohana 14:16-17; Rum.8:9,11; 1Kor. 3:16; 6:19; 2 Tim. 1:14)
2. Mwana (kama vile Mt. 28:20; Yohana 14:20,23; 15:4-5; Rum. 8:10; 2 Kor. 13:5; Gal. 2:20; Efe. 3:17; Kol. 1:27)
3. Baba (kama vile Yohana 14:23; 2 Kor. 6:16)

Waaminio ni watu wanaomilikiwa na Mungu. Hii kwa hiari ni tofauti toka kwenye kuwa na pepo wabaya kwamba ushirikiano wa hiari kwa muamini ni wa muhimu katika kila hatua na ngazi. Pepo huharibu mapenzi binafsi, lakini mamlaka kuu ya Mungu imechagua kuheshimu uhuru wa uumbaji wake wa binadamu. Ukomavu wa Mkristo (yaani., kuwa kama kristo ) unafanya mapenzi ya Mungu kuwa mwongozo wa nguvu unaomiliki!

**6:20 "maana mlinunuliwa kwa thamani "** Hii ni KAULI TENDWA ELEKEZI YA WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFU. Sitiari hii ilikuja kutoka katika soko la watumwa (kama vile 1 Kor. 7:22-23; Rum. 3:24; Gal. 3:13; 4:5). Katika Agano la Kale hii inajulikana kama *go'el*, ambaye alikuwa jamaa wa karibu aliyemrudisha mtu mmoja toka katika utumwa (kama vile Law. 25:25). Hii inarejea juu ya Kristo kama mbadala wa upatanisho wa kushangaza (kama vile Isaya 53; Mk 10:45; 2 Kor. 5:21). Wakati mtu akimkubali Kristo yeye huachilia haki zake binafsi kwa ajili ya mwili wake na huchukua wajibu kwa kushiriki kiafya na nguvu ya hekalu lote, ambao ni mwili (kama vile 1 Kor. 12:7).

◙ **"mtukuzeni Mungu katika miili yenu "** Hii ni KAULI TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFU,ni amri ya kushurutisha,na sio ya kuomba . Jinsi waamini waishivyo ni muhimu kwa ajili ya uhakika wao, kwa amani, kwa ushuhuda! Angalia **MADA MAALUMU: UTUKUFU *(AK)*** **(SPECIAL TOPIC: GLORY (OT**) katika 1 Kor. 2:7.

Kuna vitu viwili vya kuviepuka katika maisha ya mkristo: (1) kila kitu si sahihi; (2) kila kitu ni sahihi. Miili yetu ni kwa ajili ya Mungu, sio kwa ajili ya nafsi zetu;ni kwa ajili ya huduma, sio kwa ajili ya dhambi (kama vile Warumi 6). Mtazamo huu wa mwili ni tofauti sana toka kwenye mtazamo wa Kiyunani juu ya mwili kama nyumba ya gereza la nafsi. Mwili sio mwovu, lakini ni uwanja wa vita wa maisha ya kiroho (kama vile Efe. 6:10-20).
Kuna kifungu cha ziada katika NKJV, "na katika roho zenu, ambacho ni cha Mungu," chenye herufi kubwa chache mwishoni na katika miswada midogo ya machapisho ya Kiyunani ya huko nyuma. Hata hivyo, maandiko ya zamani hayana. Haipo katika $P^{46}$, א, A, B., $C^*$, $D^*$, F,au G. $UBS^4$ hutoa andiko fupi daraja "A" (hakika).

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni <u>mwongozo</u> wa usomaji wa hitifaki, ambayo inamaanisha kwamba unao wajibu wa tafsiri yako mwenyewe ya Biblia. Kila mmoja wetu lazima aenende katika nuru tuliyo nayo. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Unalazimika kutokuondoa hili toka kwa msemaji.

Maswali haya ya kujadili yanatolewa ili kukusaidia kufikiri mambo muhimu yaliyoko katika kipengele cha kitabu hiki. Yanamaanisha kuwa maswali ya kichokonozi, yasio na ukomo.

1. Je! Sura hii inafundisha wakristo katika siku zetu hawapaswi kwenda mahakamani?
2. Jinsi gani na lini watakatifu watawahukumu malaika?
3. Je! Orodha ya dhambi katika aya ya 9 na 10 inarejea katika matendo binafsi au mazoea ya maisha?
4. Wakati Paulo anaonyeha kwamba kila kitu kinaruhusika kwangu, alikuwa na maana gani hasa kwa kauli hiyo katika kurejea kwenye uzoefu binafsi na amri maalumu katika Biblia?
5. Kwanini dhambi ya uashearati ni tatizo muhimu la Kiroho?
6. Elezea tofauti kati ya mtazamo wa Kiyunani wa mwili na mtazamo wa Mkristo wa mwili

# 1 WAKORINTHO 7

| MGAWANYO WA AYA WA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **UBS[4]** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB** |
| Matatizo kuhusu Ndoa | kanuni za Ndoa | Maagizo kuhusu ndoa | Maswali kuhusu Ndoa | Ndoa na Ubikra |
| 7:1-7 | 7:1-9 | 7:1-7 | 7:1a<br>7:1b-5<br>7:6-7 | 7:1-7 |
| 7:8-16 | Timiza viapo vya Ndoa yako | 7:8-9 | 7:8-9 | 7:8-9 |
| | 7:10-16 | 7:10-11<br>7:12-16 | 7:10-11<br>7:12-16 | 7:10-11<br>7:12-16 |
| Maisha ambayo Bwana ameyapanga | Ishi kama ulivyoitwa | Mambo ya siku Za mwisho na mabadiliko katika hali ya kijamii na kindoa | Ishi kama Mungu alivyokuita | |
| 7:17-24 | 7:17-24 | 7:17-20<br>7:17-24 | 7:17-24 | 7:17-24 |
| Wasio na ndoa Na Wajane | Kwa wasio olewa na Wajane | | Maswali kuhusu Wajane wasioolewa | |
| 7:25-35 | 7:25-40 | 7:25-31 | 7:25<br>7:26-28<br>7:29-31<br>7:32-34<br>7:35<br>7:36-38 | 7:25-28 |
| 7:39-40 | | 7:39-40 | 7:39-40 | 7:39-40 |

**MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI** (Kutoka **"Mwongozo wa Usomaji Mzuri wa Biblia" ("A Guide to Good Bible Reading"**)

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo wa usomaji wa fasiri, Ikiwa na maana kwamba unawajibika kwa ukalimani wako wa biblia mwenyewe. Kila mmoja wetu sharti atembee katika nuru tuliyonayo.Wewe, Biblia na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika kutafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua mada. Linganisha mgawanyo wa somo lako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika kiaya sio uvuvio, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la asili la mwandishi ambalo ndilo kiini cha ukalimani. Kila aya ina mada moja na mada ni moja tu.

5. Aya ya kwanza
6. Aya ya pili
7. Aya ya tatu
8. N.K

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA KWA 7:1-40

A. Huu ndio mjadala mpana wa Paulo kuhusu mahusiano ya nyumbani. Anashughulikia
   1. Kuporomoka kwa maadili ya kimapenzi, 6:9-20; 7:2
   2. ndoa, 1 Kor. 7:2-5, 10-16, 28
   3. ambao hawajaoa na kuolewa, 1 Kor. 7:6-9, 25-26, 29-35
   4. mabikra, 1 Kor. 7:36-38
   5. Kurejea kwa ndoa za wajane na wagane, 1 Kor. 7:39-40
   6. Dhamira rejewa ni, "kubaki kama ulivyo," 1 Kor. 7:1, 6-7, 8, 10, 17-24, 26-35, 37, 40; kwa sababu ya mgogoro uliopo sasa na *parousia*, inayotarajiwa ingawa anaruhusu udhuru

B. Sura ya 7 ni mfano mzuri wa jinsi ya hali ya mahali na mazingira ya muda yanavyopaswa kutiliwa maanani kabla mtu kuweza kutafsiri Biblia kwa usahihi na kuweka kanuni za kutumiwa na wote. Ni vigumu katika kitabu cha 1 Wakorintho kujua mpangilio wa kihistoria kwa sababu
   1. Hatujui kwa hakika tatizo lililokuwa linawakabili watu katika Korintho (yawezekana njaa)
   2. hatujui ni kundi gani dogo ndani ya kusanyiko ambalo Paulo anawaandikia na katika aya zipi (yaani wanao jinyima anasa za mwili)
   3. Hatunayo barua ambayo kanisa walimwandikia Paulo wakimuuliza maswali haya (kama vile 1 Kor. 7:1,25; 8:1; 12:1; 16:1,12)

C. Panaonekana kuwepo na tabia/vikundi vidogo ndani ya kanisa la Korintho vilivyokuwa vinasababisha mtafaruku Mkubwa. La kwanza walikuwa wale walioelekea kujinyima anasa za mwili (kama vile 1 Kor. 7:1). Kundi la pili walikuwa wale waliojilegeza kwenye mambo ya uadilifu ama wa wale wasiofungwa na sheria (kama vile 1 kor. 6:12; 10:23). Kweli yote inashambuliwa na waliovuka viwango. Katika 1 wakorintho 7, paulo anajaribu kutembea kIvitendo na mbano wa kitheolojia katikati ya viwango hivi vilivyozidi, wakati akiwa bado anaongea na vikundi vyote viwili.

D. Kuna dhamira inayojirudia rudia ikikimbilia kwenye sura yote ya saba 7. Inadhihirishwa na aya ya 17, 20, 24, 26, 40 na ilidokeza kwenye aya ya 8. Dhamira hiyo ni "baki kama ulivyo" kwasababu muda ni mfupi. Hii haiwezi kuwa kanuni ya watu wote kwasababu
   1. Hii inahusu kipindi cha mateso
   2. ndoa ni mpango wa Mungu kwa mwanadamu (kama vile Mwa. 1:28)
   3. kanisa hili lilipambana na matatizo ya ndani na walimu wa uongo

   Mtu atashangaa ni kundi gani (yaani, wale hawajaolewa, waliowahi kuolewa, ama kuoana na asiyeamini) Paulo mwenyewe alipitia. Labda aliwajua kiuhalisia. Wayahudi wengi walifunga ndoa kwa tafsiri ya Mwa.1:28 sawa sawa na mapokeo. Mke wa Paulo aidha alikufa (yaani, alikuwa mgane) ama alimwacha kutokana na imani yake mpya (yaani alkuwa ameachwa). Katika kipindi cha wito wake kuokolewa na huduma (yaani, njia ya Dameski) yeye mwenyewe alichagua kuishi bila ndoa kama vile Barnaba alivyofanya lakini hakumlaumu Petro kwa ndoa yake (kama vile 1 Kor. 9:5).

E. Ndoa katika Biblia ni tendo la kawaida (kama vile Mwa. 1:28; 2:18). Paulo labda alikuwa ameoa wakati Fulani (yaani, kidokezo cha Matendo 26:10, ikiwa Paulo alikuwa mjumbe wa wakuu wa Sinagogi, basi alipaswa kuwa ameoa). Anatamka kwamba ndoa ni kitu cha heshima kwa aaminiye (kama vile 1 Kor. 6:16; 7:14; 2 Kor. 11:2 na Efe. 5:22-31). Lazima tukumbuke kwamba Paulo anaelezea hali ya vikundi vidogo ndani ya kanisa la kwanza hali ya watu wa kanisa la karne ya kwanza hali ya watu kutoka sehemu zote.

F. Mjadala wa Paulo kuhusu kutahiriwa katika aya ya 19 unathibitisha kwamba kwa Paulo kawaida za Agano la Kale zimetoweka katika injili ya Bwana wetu Yesu Kristo kwa waamini wa mataifa (k.v matendo 15) na kwa hiyo, hawafungwi. Tukiongea kithiolojia mara nyingi inaelezewa kuwa Paulo anathibitisha kipengele cha kimaadili cha Agano la Kale, na kukanusha kipengele cha taratibu za kidini.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 1 WAKORINTHO 7:1-7**

**[1] Basi kwa habari ya mambo yale mliyoandika, ni heri mwanamume asimguse mwanamke. [2] Lakini kwa sababu ya zinaa kila mwanamume na awe na mke wake mwenyewe, na kila mwanamke na awe na mume wake mwenyewe. [3] Mume na ampe mkewe haki yake, na vivyo hivyo mke na ampe mumewe haki yake. [4] Mke hana amri juu ya mwili wake, bali mumewe; vivyo hivyo mume hana amri juu ya mwili wake, bali mkewe. [5] Msinyimane isipokuwa mmepatana kwa muda, ili mpate faragha kwa kusali; mkajiane tena, Shetani asije akawajaribu kwa kutokuwa na kiasi kwenu. [6] Lakini nasema hayo, kwa kutoa idhini yangu, si kwa amri. [7] Ila nipendalo ni kwamba watu wote wawe kama mimi nilivyo; walakini kila mtu ana karama yake mwenyewe itokayo kwa Mungu, huyu hivi, na huyu hivi.**

**7:1** "**Basi kwa habari ya mambo yale mliyoandika**" Yawezekana mambo yaliyoandikwa katika sura ya 1-6 yalikuwa yanahusu Paulo kwa watu wa leo. Na aya "sasa kuhusu" yahusu maswali mahususi ambayo kanisa la Korintho liliyatuma kwa Paulo labda kupitia kwa Stefano, Fortunatus, and Achaicus (kama vile 1 Kor. 7:25; 8:1; 12:1; 16:1,12). Ni vigumu sana kutafsiri sura hii bila kujua sawasawa ni maswali gani Wakorintho waliuliza na ni nani aliyeuliza (yaani, waaminio waaminifu, kundi la waasherati, kundi la wanaojinyima anasa za mwili, au mmoja wa walioanzisha vikundi vidogo).

**NASB, NKJV "ni heri mwanamume asimguse mwanamke"**
**NRSV "ni heri mwanamume asimguse mwanamke"**
**TEV "Mwanaume hufanya vema kuacha kuoa"**
**NJB "Ndiyo ni jambo jema kwa mwanaume kuacha kumgusa mwanamke"**

Neno “vizuri" lina uwanja mkubwa wa elimu maana lakini kwenye mazingira haya linamaanisha "enye faida ama"kwa manufaa ya mtu" (kama vile 1 Kor. 7:1,8,26). Linatumika Kwenye maana hii hii katika maandiko ya kale katika Mwa. 2:18. Kusudi lote la Paulo ni kile kilicho bora zaidi kwa mtu katika nyakati za mateso yatokanayo na maumivu, wasi wasi, magonjwa ama kuchoka na kile kilicho bora zaidi kwa ufalme wa Mungu.
Hili linaweza kuhusu

1. Nukuu kutoka kwenye barua ambayo Wakorintho walimwandikia Paulo
2. Neno au aya itumikayo kuhamasisha nia ya kikundi kutoka kwa mojawapo ya vikundi vidogo ndani ya Kanisa
3. Kirai/fungu la maneno kutoka kwenye mahubiri ya Paulo lakini likaelekea isivyo na likatumiwa na wanaojinyima anasa za mwili, wale wanaoshikilia mno sheria ama wale waasherati

Neno hili "gusa" lina vidokezo vingi, "kuweka mikono juu ya," "kushika," "kutawala." Lilikuja kutumika ki-sitiari kwenye tendo la ndoa (kama vile LXX Mwa. 20:6; Mith. 6:29; Josephus' Antiquities 1.163; pia Plato, Leges 8.840a; na Plutarch, Alex. M. 21.4. Tazama Bauer, Arndt, Gingrich na Danker's Lexicon, uk. 102, lakini halikutumika kumaanisha tendo la ndoa katika mafunzo ya lugha ya Koine kutoka Misri).
Paulo hajaribu kushusha thamani ya ndoa au tendo la ndoa. Mwanadamu kila wakati hutumia karama za Mungu zaidi ya mipaka ya Mungu. Hali ya mazingira ya Korintho ilikuwa yenye uovu kupindukia (kama vile 1 Kor. 7:2a).

**NASB "Lakini kwa sababu ya zinaa"**
**NKJV "Lakini kwa sababu ya zinaa"**
**NRSV "Hata hivyo kwa sababu ya zinaa"**
**TEV "Lakini kwa sababu kuna zinaa sana"**
**NJB "ili kujiepusha na zinaa"**

Ndoa haikuwa tatizo kwa Paulo. Hii ni KAULI TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO, UMOJA WA MTU WA TATU. Watu wengi wanaamini kwamba alikuwa rabbi kwa sababu alifundishwa chini ya mwalimu wa sheria

Gamaliel na alikuwa mwenye ari kwa ajili ya sheria. Alijua kuwa ndoa iliyoeleweka ni jambo la lazima ili kutimiza Mwanzo, "zaeni mkaongezeke" (kama vile Mwa. 1:28; 9:1,7). Tendo la ndoa ni zawadi kutoka kwa Mungu. Jamii ya watu wa mataifa ilikuwa imeruhusu zinaa na uchafu kwa sababu tendo la ndoa lilitumika kwenye ibada za kipagani za kuzidisha uzao ndiyo maana Paulo alihisi kwamba lazima aeleze swala hilo.

Paulo anaelezea mada ya kithiolojia ya watu kujitenga na kuoa ama kuolewa na hali ya mateso iliyokuwa inapangwa. Kipo kipawa cha kiroho cha kujizuia kuoa ama kuolewa chenyewe si cha kiroho zaidi kuliko kuwa na ndoa. Mtu akiwa peke yake anaweza kutoa muda mrefu zaidi. Nguvu na rasilimali zaidi kwa ajili ya huduma, hili ni jema lakini sio kwa watu wote, sio kwa wengi sana!

Swala kuu la Paulo katika muktadha huu wa 1 Kor. 7:2 sio kule kuwa bila mwenza bali "kaa kama ulivyo." Nyakati zilikuwa ngumu. Mateso yalikuwa yanaongezeka. Historia yatuambia kuhusu njaa zilizo kabili ukubwa wa falme kubwa tatu katika kipindi hiki. Paulo anathibitisha ndoa (kama vile 1 Kor. 6:16), lakini katika mfumo wa kijamii wakati huu unatetea kuwa kukaa mwenyewe tu. Hii sio kanuni ya watu wote onyo dogo la muda la kitamaduni.
Shughuli ya Paulo katika 1 Kor. 7:2 ni zinaa inayoenea kote katika karne ya kwanza kwenye utamaduni wa Kiyunani – Kirumi. Katika jamii iliyochangamana bila utaratibu, ndoa ya mume mmoja kwa mke mmoja yenye uaminifu yafaa sana kiroho, kimihemko, na kimwili kuliko ibada za kipagani, si tu kwamba ndoa inathibitishwa bali wajibu unaostahili kila mwanandoa unathibitishwa.

**7:2"mwanamume na awe na mke wake mwenyewe, na kila mwanamke na awe na mume wake mwenyewe**"Hizi ni KAULI SHURUTISHI ZA WAKATI ULIOPO mbili, lakini hazitendi kimamlaka, mpaka hii itarajie 1 Kor. 7:5. Huu ni muundo ulio unaofanana kisarufi kama zisivyo 1 Kor. 7:3 na 4. (kama vile 1 Tim. 4:3; Ebr. 13:4).

**7:3** Aya hii pia ina kauli mbili TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO. Paulo anatoa miongozo minne katika aya mbili. Inawezekana kwamba Paulo anashughulika na matatizo mawili kwenye eneo hili la mambo ya ngono ya binadamu (kama vile Gordon D. Fee, *To What End Exegesis*, kr. 88-98).

1. Wakristo wasio na utaratibu waliendelea na utaratibu wao wa kipagani wa awali hasa kwenye mahekalu na kwenye sherehe (yaani, wazinzi),
2. Wakristo ambao wamefanya hata ngono ya ndoa kama mila ya kiroho (yaani wanaojinyima anasa za mwili kama vile 1 Kor. 7:5 na hivyo 1 Kor. 7:1 inakuwa neno la kuhamasisha nia/kusudi kusudi ama moja ya vikundi vidogo kanisani)

**7:4** Aya hii inaonyesha uwezo wa Paulo wa kuweka uwiano katika mila yake isiyofaa (kama vile Efe. 5:21,22-33). Katika siku za Paulo wanawake walikuwa na haki chache. Paulo anawaambia wanandoa wawili wawe na wajibu wa pamoja. Mahitaji ya ngono sio uovu. Ni hamu iliyowekwa na Mungu.

**7:5 "Msinyimane"** Hii ni KAULI TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO ikiwa na KIAMBATA HASI, ambacho mara nyingi hudokeza "kuzuia kitendo kilicho kwenye mchakato." Hii inahusu tatizo la kujinyima anasa za mwili kwenye kanisa la Korintho. Pia inadai kwamba ngono ama kukataa kushiriki ngono, kisiwe kigezo cha kumthibiti mwenzi!

◙**"isipokuwa mmepatana"** Kifungu hiki kinaanza na *ei mēti*, ikimaanisha “isipokuwa labda" au "mpaka ikiwa " (kama vile Luka 9:13). Inatoa kisingizio kimoja kinaachowezekana kwenye kanuni (yaani sheria baadaye udhuru) kimetumika kwenye aya nzima. Paulo anatembelea kwenye mkazo wa kithiolojia kati ya mtu anayeshika sheria sana/mtu anayejinyima raha na mwasherati/ mtu ambaye asiyeshika sheria. Kila kikundi kidogo kidogo kina ajenda yao na wito!
Tambua Paulo anaelezea mfano wa wazi. Mwanaume hana mamlaka ya kuchagua peke yake! Kibiblia usimamizi wa kiuanaume kwa bahati mbaya umeeleweka vibaya. Mme lazima atende kwa namna ya utoaji kwa ukomavu wa familia (kama vile Efe. 5:25-29), sio kwa faida ya mtu binafsi ama kujipendelea bali katika uwakili wa kiroho.

**MADA MAALUM: WANAWAKE KATIKA BIBLIA (SPECIAL TOPIC: WOMEN IN THE BIBLE)**

**NASB, NRSV "ili mpate kujitoa kwa ajili ya maombi"**
**NKJV "kwamba muweze kujitoa nafsi zenu kwa kufunga"**

**TEV "ili mtumie muda wenu kwenye maombi"**
**NJB "kuacha nafsi zenu huru kwa maombi"**

"Kufunga" kumo ndani ya Upokeaji wa Maandiko kafuatia MSS אc, K, na L na toleo la Biblia ya ki-Syria (Peshitta). Hata hivyo idadi kubwa ya Kiyunani cha kale, P11, P46, א*, A, B, C, D, G, P, tafsiri nyingi za kale na tafsiri nyingi za kisasa za Kiingereza <u>hazijumuishi</u> hili. UBS[4] hutoa maandiko mafupi zaidi ya katika daraja "A" (hakika).

Kanuni ya Agano Jipya kuhusu kufunga kwa hiari kwa kipindi fulani kwa makusudi ya Kiroho imefananishwa hapa na kujitenga na masuala ya ngono katika ndoa kwa vipindi kwa makusudi ya kiroho. Kama vile kufunga na kuelekeza fikra kwenye mapenzi ya Mungu, ndivyo pia kujitenga na ngono kwenye ukomo kunaweza, ukajitenga na mambo ya kujamiiana.

## [MADA MAALUM: KUFUNGA (SPECIAL TOPIC: FASTING)]

◙"**Shetani asije akawajaribu**" Hata wanandoa wanahitaji kuwa waangalifu sana kuhusu vishawishi vya shetani vyenye kudhuru kwa siri ndani ya ndoa. Ngono ya wanadamu ingawa ni zawadi kutoka kwa Mungu ni msukumo wenye nguvu wa binadamu, Shetani hutumia kipengere hiki cha hitaji la kibaiolojia kama chombo cha kumtenganisha mwanadamu aliyeanguka na Mungu (kama vile 1 Tim. 5:14-15).
Katika muktadha huu ni dhahiri kuna tatizo linaloonyesha thiolojia ya zinaa ya mwanadamu ndani ya kanisa la Korintho labda lilikuwa na kiasi cha kupitiliza cha tabia ya kujinyima anasa za mwili na wanaume kutokuwajibika na kuishi maisha machafu.

## [MADA MAALUM: UOVU BINAFSI (SPECIAL TOPIC: PERSONAL EVIL)]

◙"**kwa kutokuwa na kiasi kwenu**" Hili ni neno la *kratos*, lilimaanisha "uwezo," "nguvu," "tawala," pamoja na,
1. Mathayo 23:25 kuhusiana waandishi na Mafarisayo
2. 1 Wakorintho 7:5 kuhusiana na wanandoa
3. 2 Timotheo 3:3 kwenye orodha ya maovu

Neno linalofanana, *egkrateia*, lina kidokezo cha kujizuia mwenyewe, hasa kuhusiana na mambo ya kujamiiana.
1. Matendo 24:25 kwenye orodha ya maadili/wema
2. 1 Wakorintho 7:9 kwenye mjadala wa Paulo kuhusu haki ya ndoa
3. 1 Wakorintho 9:25 kuhusiana na mazoezi ya mbio
4. Wagalatia 5:23 katika orodha ya Paulo ya matunda ya Roho
5. 2 Petro 1:6 kwenye orodha ya tabia pambanuzi ziletazo ukomavu

Kujithibiti ni (1) tunda la roho na (2) mazoea ya ndani ya kudhibiti tamaa za asili. Kutawala roho ya mtu iliyokombolewa juu ya mwili inawezekana kwa msaada wa roho mtakatifu anayekaa ndani. Tamaa za asili sio mbaya isipokuwa zinapochukuliwa nje ya mipaka ambayo Mungu ameitoa.

**7:6**
**NASB "Lakini hili nalisema kwa njia ya kukubali sio agizo"**
**NKJV "lakini nasema hili kama kukubali sio amri"**
**NRSV "Hili nalisema kwa njia kukubali sio amri"**
**TEV "Nawambieni hili si kama agizo bali tu kama ruhusa"**
**NJB "Nawambia hili kama kukubali sio agizo"**

Je! 1 Kor. 7:6 inahusu (1) 1 Kor. 7:1-5; (2) 1 Kor. 7:3-5; (3) 1 Kor. 7:5; au (4) 1 Kor. 7:7? Paulo anatoa maoni juu ya maongozi ya roho. Anatarajia
1. Kuja kwa mara ya pili wakati wowote
2. Kuongezeka kwa mateso wakati wowote

3. Mwendelezo wa njaa

Kusudi lake lilikuwa kuwasaidia waaminio kwenda sambamba na mazingira yaliyokuwepo, na sio kuwazuia

**7:7 "Ila nipendalo ni kwamba watu wote wawe kama mimi nilivyo"** Hii ingeweza kuhusu (1) Paulo kama mtu mmoja; (2) Paulo kama mtu aliyeridhika; au (3) Paulo kama aliyejithibiti (kama vile 1 Kor. 7:9). Paulo labda alikuwa ameoa wakati Fulani kwa sababu ya shinikizo la utamaduni kutoka kwa misingi na kuingizwa lawamani wa Matendo 26:10, ambapo Paulo anaonekana kuwa mjumbe wa wakuu wa Sinagogi (yaani, "Napiga kura"). Kama alikuwa sehemu ya wakuu wa Sinagogi, ilimpasa kuoa. Shauku ya Paulo kwamba waaminio wote wabaki kama alivyo inahitaji kuelezewa kwa namna mbalimbali

1. Paulo alitarajia kuja kwa mara ya pili katika uhai wake kama walivyotarajia Wakristo wote wa karne ya kwanza. Kurudi kwa Yesu wakati wowote (angalia Mada katika 1 Kor. 6:14) kunamaanisha kuleta motisha ya nguvu kuelekea kufanana na Kristo na uinjilisti katika kila kizazi.
2. Mtazamo wa Paulo lazima uangaliwe katika nuru ya amri ya Mungu “kuzaa na kuongezeka" ya Mwa. 1:28. Kama Wakristo wote wangeweza kuishi bila ndoa ingetokeaje kwenye kizazi kilicho fuata
3. Paulo mwenyewe alikuwa na mtazamo wa juu kuhusu ndoa (kama vile 1 Kor. 6:16), Angewezaje tena kuitumia kama analojia ya Kristo na kanisa kulilinganisha kama mume na mke katika Efe 5:22-33?

◙**"kila mtu ana karama yake mwenyewe itokayo kwa Mungu"** Hii inaonekana kurejea juu ya kujitenga na kuoa au kuolewa kama mojawapo ya karama nyingi za kiroho (kama vile Mt. 19:12). Haikuorodhesha miongoni mwa orodha ya karama (Warumi 12; 1 Wakorintho 12; Waefeso 4). Haionekani kuwa kitendo kinachofanana sana ama kutenda kama “karama” nyingine. Paulo anatumia neno “karama”kwa maana maalumu.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 1 WAKORINTHO: 7:8-9**
**[8] Lakini nawaambia wale wasiooa bado, na wajane, Ni heri wakae kama mimi nilivyo. [9]Lakini ikiwa hawawezi kujizuia, na waoe; maana ni afadhali kuoa kuliko kuwaka tamaa.**

**7:8 "wasiooa bado, na wajane"** Neno hili liko kwenye JINSIA YA KIUME na lingeweza kurejea kwa (1) wale wote wasiooa au (2) ama wagane. Neno la pili ni JINSIA YA KIKE na lingeweza kurejea kwa (1) wale ambao wengi wao walikwisha kufa (2) wajane.

◙**"Ni heri kwao"** Angalia nukuu katika 1 Kor. 7:1 juu ya neno "vema."

◙**"ikiwa"** Hii ni SENTENSI YENYE MASHARTI DARAJA LA TATU, ambayo inahusu tendo MUHIMU.

◙**"wakae kama mimi nilivyo"** Paulo amemaliza tu kutaja karama za kiroho katika 1 Kor. 7:7, lakini aya hii inataja hali iliyopo katika maisha, sio karama. Yawezekana "karama" imetumika kwenye muktadha huu katika dhana ya fikra ama taswira.

**7:9 "ikiwa"** Hii ni SENTENSI YENYE MASHARTI DARAJA LA KWANZA. Ambayo inachukuliwa kuwa kweli kutokana na mtizamo wa mwandishi ama makusudi yake kifasihi. Wengi watapenda kuoa sio kwa sababu ni maovu bali kwasababu hawama karama ya useja

◙**"hawawezi kujizuia"** Hili linasikika kinyume kwenye masikio ya watu wa leo. Je Paulo anasema kuoa ni ishara ya kupungukiwa na hali ya kujithibiti kwa aaminiye? Je ni kuwa na upungufu katika hali ya kiroho? Kutokana na mwanga wa mafundisho ya maandiko yote hii haiwezi kuwa kweli. Paulo anaelekeza maoni yake kwenye hali ya muda mfupi ya mahali pale. Huu sio ushauri wa ndoa na useja kwa watu wote. Ndoa sio kitu cha hali ya chini zaidi kati ya maovu mawili; ngono isiyo na utaratibu, hata hivyo wakati wote inakuwa nje ya mipaka.

◙**"na waoe"** Hii ni KAULI TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFU. Paulo aliafiki ndoa (kama vile 1 Tim. 5:14).

**NASB " kwani ni afadhari kuoa kuliko kuwaka tamaa"**
**NKJV, TEV "kwani ni afadhari kuoa kuliko kuwaka tamaa"**
**NRSV "kwani ni afadhari kuoa kuliko kuwashwa na tamaa"**
**NJB "kwakuwa ni afadhari kuoa kuliko kuwakwa na tamaa"**

Tambua tofauti inayoonekana dhahiri kati ya "kati ya kuoa" (KAULI TENDAJI ISIO NA KIKOMO YA WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFU) na "kuungua" (KAULI TENDWA ISIO NA KIKOMO YA WAKATI ULIOPO). Ndoa inasababisha ile hali ya kuendelea kutamani kuthibitiwe. Hii pia sio kudhhirisha maoni kuhusu ndoa, bali ni uchunguzi kiutendaji. Ndoa ndiyo njia ya kawaida kutimiliza hamu yenye nguvu na yenye kujirudia rudia iliyotolewa na Mungu. Neno hilo hilo "kuwaka" linatumiwa na Paulo mwenyewe katika 2 Kor. 11:29, kwa hiyo sio neno sanifiwa lililo kinyume.

**ANDIKO LA NASB(LILILOBORESHWA): 1 WAKORINTHO 7:10-11**

**[10] Lakini wale waliokwisha kuoana nawaagiza; wala hapo si mimi, ila Bwana; mke asiachane na mumewe; [11] lakini, ikiwa ameachana naye, na akae asiolewe, au apatane na mumewe; tena mume asimwache mkewe.**

**7:10 "waliokwisha kuoana"** Hili ni kundi la tatu lililokwisha ambiwa: "wasio na ndoa," "walio tengana," walio ooana."

◙**"wala hapo si mimi ila Bwana"** Kwa kirai hiki Paulo anahusisha maneno ya Yesu, mengi, lakini sio yote yalionakiliwa kwenye injili za muhtasari kuhusu kuachana (kama vile Mt. 5:32, 19:6; Marko 10:11-12; Luka 16:8).
Huu ni mfano mzuri wa ukweli kwamba Paulo hashugulikii mambo yote ya mafundisho ya Bwana kuhusu kuachana, moja ya Nyaraka za Paulo ni "Nyaraka za muda." Anaonyesha hisia kwenye thiolojia dhaifu ya waasherati na wenye kujinyima anasa za kimwili. Hali hii inaendeleza maelezo ya Paulo kuthibitisha baadhi ya kauli za waalimu wa uongo ama wenye vikundi vidogo vidogo kanisani, lakini pia kuonyesha mipaka ya nia na makusudi yao. Mambo ambayo ni ya nusu ukweli ni magumu kusahihisha hasa ikiwa yana maudhi yenye tatizo pande zote mbili!

◙**"mke asiachane na mumewe"** Hii inaonyesha kwamba wote ni waaminio (kama vile 1 Kor. 7:12-16). Wanawake hawakuwa na haki ya kuvunja ndoa katika dini ya Kiyahudi, lakini walikuwa na haki kwenye jamii ya Warumi. Kwa sababu utamaduni fulani unaoruhusu ama hauruhussu jambo haimaanishi kwamba waaminio lazima wafaidike wao kutumia fursa hiyo au wabadili uwe mwiko kwao. Kwasababu mtu anaweza kufanya haimaanishi kwamba mtu mwingine anapaswa naye kufanya (kama vile Rum. 14:1-15:13). Yapo mazingira fulani ambayo yanapelekea kuachana kuonekane kunafaa zaidi.

1. Kosa dogo miongoni mwa makosa mawili
2. Upatanisho umeshindikana
3. Hatari ya kimwili kwa mwenza na mtoto kuonekana ndio chanzo

Katika sehemu hii nataka kuongeza msisitizo juu ya umakini wa kibiblia wa kuweka viapo kwa jina la Mungu. Ndoa za Kikristo ni viapo vya kidini! Mungu, zaidi ya jamii inayotuzunguka anawajibisha waaminio kwa jinsi tunavyolitumia jina lake. Ndoa ilikusudiwa kuwa ya kudumu. Ndoa ni kanuni, sio jambo la udhuru. Katika mwaka wa 2002 asilimia iliyokuwepo ya mila za kifamilia kule Amerika ya kaskazini kwa wakati huo (yaani, Mume, mke, na watoto) ilikuwa chini ya 23%! Unaona tatizo la kuachana kwa urahisi? Ndoa kimsingi ni ahadi kwa Mungu na kisha kwa kwa mtu mwingine. Nyumba zilizosimama imara za Kikristo zinaweza kuwa mojawapo ya ushuhuda wenye nguvu kuliko zote katika siku zote.

`**7:11 "ikiwa"** Hii ni SENTENSI YENYE MASHARTI DARAJA LA TATU inayomaanisha juu ya tendo muhimu. NASB inaweka kishazi hiki kwenye mabano kama maoni ya pembeni. DHAMIRA TEGEMEZI inamaanisha
kwamba kuachana kulikuwa kunatokea siku zile za jumuiya ya Kikristo.

◙**"na akae asiolewe"** Hii ni KAULI TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO. Swali la ndoa ya Kikristo ni gumu. Kumbukumbu 24 ilioandikwa na Musa kusaidia ndoa. Majibu ya Yesu kuhusu maswali ya Mafarisayo, hayashughulikii somo lenyewe hasa. Mtu angeweza kusema vipi kuhusu Marko 10:11-12. Tatizo ni kwamba injili hii haihusishi kishazi isipokuwa kama Mathayo inavyofanya Mt. 5:32. Kwa namna gani kishazi chenye udhuru kinahusiana na kuolewa tena? 1 Timotheo 5:14-15 inahitaji kupanuliwa zaidi katika siku zetu kwenye upana wa kundi kuliko "wajane wenye umri mdogo." Hakika anawajali wale waishio wenyewe wanaotamani kuoa katika 1 Kor. 7:9 lazima ihusiane na jamii yetu iliyo na matatizo. Binadamu aliumbwa na Mungu kama viumbe vinavyojamiiana. Ili mpaka pawepo na karama ya useja, na /au ukomavu wa kujizuia mwenyewe, lazima pawepo na uchaguzi unaofaa wa kujamiiana kwa watu wa Mungu; zinaa kamwe haiwezi kuwa uchaguzi mzuri, lakini kuoa/kuolewa tena kwa Mkristo kwaweza kuwa suluhisho linalokubalika. Neema na ufunuo lazima vyote vitumike hapa.

◙**"au apatane na mumewe;"** Hii ni KAULI TENDWA SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFU. Katika mazingira haya ya kitamaduni, chaguzi za Paulo kwa wale waliokwisha kuoana zilikuwa (1) kuwa mmoja au (2) upatanisho.
Aya hii imekuwa ikitumika kama sheria ngumu na haraka kwa waaminio wengi wa kisasa. Upatanisho mara zote ni tumaini mpaka pale kurjeana kwa wanandoa kunapotokea. Katika hali hiyo inahitimisha kuwa matokeo yaliyotamaniwa (yaani, imekatazwa kwenye huduma ya Agano la Kale).

Ni kazi kuitafsiri 1 Wakorintho
1. Ikiwa ni dhahiri maswala ya kitamaduni ambayo utamaduni wa magharibi hauyashughulikii (yaani, vyakula vilivyotolewa kwa miungu mabikra, washirika kwenye huduma, n.k.).
2. Kuna makundi mawili ya aina za nafsi (yaani, waliojitenga na anasa za mwili na waasherati ama wana vikundi vya kithiolojia). Maneno ya Paulo ni kujaribu kuthibitisha kweli zinazohusika lakini yanaweka mpaka yale yaliyozidi (yaani, wenye maagizo ya kimamlaka ya kisheria, msioe; na uhuru usio na sheria, kama unajisikia vizuri, fanya tu).

Hakuna hakika kama yaliyovuka viwango yanaaksi (1) Wayahudi/Mataifa; (2) washikaji sana wa sheria; (3) wenye aina za tabia; ama (4) Miundo miwili ya fikra za Kiyunani (baadaye imeonekana kwenye vikundi vya wale wenye mafunuo ya uongo). Mkanganyiko huja pale watafsiri wa kisasa hawajui
1. Wito wao ulikuwa nini
2. Chanzo cha miito
    a. Mahubiri ya awali ya Paulo
    b. Dini ya Kiyahudi
    c. Wanaovumilia mateso/wapokeaji wa mafunuo ya uongo

Paulo anawaambia wote waliovuka viwango! Ugumu ni kuamua maneno yapi yanaelekezwa kwa waaminio wa kweli na yapi kwa vikundi vidogo kanisani, watafsiri wa kisasa kusikiliza yale wanayotaka kusikia na kulaani wasiotaka. Tafsiri zetu kusema zaidi kuhusu thiolojia yetu kuliko waraka wa Paulo kwa mji wa Roma karne ya kwanza ya Akaya.
◙**"mume asimwache mkewe"** Kumbuka muktadha huu unawawekea waaminio wenye ndoa. Kuna visingizio viwili katika Agano jipya kwenye agizo hili: (1) tendo la ndoa lisilofaa (kama vile Mt. 5:32, 19:9) na (2) kutokuamini (kama vile 1 Kor. 7:12,13).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 1 WAKORINTHO 7:12-16**
**12 Lakini watu wengine nawaambia mimi, wala si Bwana, ya kwamba iwapo ndugu mmoja ana mke asiyeamini, na mke huyo anakubali kukaa naye asimwache. 13 Na mwanamke, ambaye ana mume asiyeamini, na mume huyo anakubali kukaa naye, asimwache mumewe. 14 Kwa maana yule mume asiyeamini hutakaswa katika mkewe; na yule mke asiyeamini hutakaswa katika mumewe; kama isingekuwa hivyo, watoto wenu wangekuwa si safi; bali sasa ni watakatifu. 15 Lakini yule asiyeamini akiondoka, na aondoke. Hapo huyo ndugu mume au ndugu mke hafungiki. Lakini Mungu ametuita katika amani. 16 Kwa maana wajuaje, wewe mwanamke, kama utamwokoa mumeo? Au wajuaje, wewe mwanamume, kama utamwokoa mkeo?**

**7:12 "wengine"** Hili lingehusu wale wanandoa ambao waliooana wakingali wapagani ambapo mmoja alikwisha kuwa aaminiye. Hii haiwezi kutumika kama uhakiki wa maandiko kwa aaminiye akifunga ndoa na asiyeamini. Hii inahusu hali ambayo wote wawili hapo awali walikuwa si waaminio. Mmoja alimpokea Kristo kwa matarajio ya muda, na mwingine pia angempokea Yesu (kama vile 1 Kor. 7:16).

**NASB, NRSV "Nasema, sio Bwana"**
**NKJV "Mimi, sio Bwana"**
**TEV "(Mimi, mwenyewe sio Bwana)"**
**NJB "maagizo haya ni yangu mwenyewe sio ya Bwana"**

Hii sio hali ya kukataa ya mfano wa kuvutia wa Paulo bali kutambua kwamba Paulo hakujua kuhusu mafundisho ya Yesu kwenye swala hili 1 Kor. 7:25 na 40 ya sura hii.

◙**"iwapo"** Hii ni SENTENSI YENYE MASHARTI DARAJA LA KWANZA. Kulikuwa Na Wanandoa waliochanganyika katika Korintho. Hii inaonesha matokeo ya mahubiri ya Paulo na ugumu uliohusika katika kuoa/kuolewa na asiyeamini.

◙**"asimwache"** Hii ni KAULI TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO kama ufanano katika 1 Kor. 7:13.

**7:14**
**NASB, NKJV,**
**NJB "Kwa kuwa mume asiye amini ametakaswa"**
**NRSV "Kwa kuwa mume asiyeamini amefanywa kuwa mtakatifu"**
**TEV "Mimi mwenyewe sio Bwana"**

Hii ni KAULI TIMILIFU TENDWA YENYE KUARIFU kama kifungu mfanano katika 1 Kor. 7:14. Hii haimaanishi kwamba mwenza asiyeamini ameokolewa. Hii inahusu Wakorintho wengine wajue kwamba kuoa/kuolewa na asiyeamini kungelinganishwa na dhambi. Labda walikwisha sikia mahubiri ya Paulo kuhusu mwili mmoja (kama vile 1 Kor. 6:16-20). Hii lazima ihusu ushawishi wa Ki-Mungu wa mwenza aaminiye kwenye familia. Hii haiwezi kuhusu nafasi ya mwenza asiyeamini kwa Kristo. Uinjilisti ndilo lengo la aaminiye kwa mwenza wake (kama vile 1 Kor. 7:16).

**NASB, NIV "mke asiyeamini kutakaswa kupitia mume wake anayeamini"**
**NKJV, NRSV "mke asiyeamini kutakaswa kupitia mumewe anayeamini"**
**NJB " mke asiyeamini kutakaswa kupitia kwa kaka"**
**REB "mke kupitia mume wake Mkristo"**

Kuna tofauti ya kwenye kirai hiki katika maswala ya Kiyunani. Nyingi miongoni mwa miswada ya Kiyunani ina "kaka" badala ya "mume aaminiye" (kama vile MSS $P^{46}$, א*, A, B, C, D*, G, na P). Waandishi waliibadili kuilinganisha na Kirai cha awali kilicho sambamba (kama vile MSS א$^{c}$, $D^{C}$, K, na L). UBS[4] Hutathimini "ndugu" kama "A" (hakika).

◙**"kama isingekuwa hivyo, watoto wenu wangekuwa si safi; bali sasa ni watakatifu."** Kumekuwepo na tafsiri nyingi kwa kirai hiki; kinachohusu

1. Uhalalishaji wa watoto (yaani, dhana ya kisheria)
2. Utakaso wa kiibada (yaani, dhana ya Kiyahudi)
3. mwenza asiye amini na watoto wakilishiriki baraka za Mkristo mmoja kwenye nyumba moja (yaani, maana ya kiroho)

Wengi wamejaribu kutafsiri aya hii wakihusisha ubatizo wa watoto, lakini inaonekana kabisa sivyo kwani uhusiano wa aaminiye na ule wa mwenza asiye amini. Angalia MADA MAALUM: TAKATIFU (SPECIAL TOPIC: HOLY) katika 1 kor. 3:17.

**7:15 "Ikiwa"** Hii ni SENTENSI YENYE MASHARTI DARAJA LA DARAJA LA KWANZA. Ukristo ulisababisha baadhi ya nyumba kuvunjika (kama vile Mt. 10:34-36; Luka 12:49-53).

**NASB, NKJV "hafungwi kwenye maswala kama hayo"**
**NRSV "katika swala kama hilo ndugu wa kike au wa kiume au kike hafungwi"**
**TEV "katika maswala kama hayo mwenza wa Kikristo kama ni mume ama mke, yuko huru kutenda"**
**NJB "kwenye mazingira haya kaka au dada hafungwi tena"**

Hii ni KAULI TIMILIFU TENDWA YENYE KUARIFU ya neno "kufungwa." Hii inadokeza kwamba Wakristo kwenye mazingira maalum ya kitamaduni hawaruhusiwi kuchochea suala la talaka, lakini kama mwenza asiyeamini anaifanya inaruhusiwa. Hii ina uhusiano kwa waaminio kuoana na wasio amini; katika mazingira haya hii inarejerea matengano, na sio kurudiana (kama vile 1 Kor. 7:11), ingawa istilahi ya Paulo inafanana na "kufunga na kufungua" kwa falsafa ya sheria ya Kiyahudi kwa namna ndoa ilivyofikiliwa Kumb. 24:1-4. James S. Jeffers, *The Greco-Roman World*, husema,
"neno" lililotafsiriwa kuachana katika 1 Kor. 7:15 linahusu kutoa talaka kwa sababu watu wa kale hawakuwa na mlingano wa dhana ya kisheria ya kisasa ya kuachana" (uk 247).
Hata hivyo suala la kuachana linaonekana kupata suluhu kwa Paulo katika mafundisho ya Yesu (kama vile Marko 10:2-12). Paulo anatetea "useja kwa wale wasio fungwa"!

◙**"Mungu ametuita katika amani"** Hii ni KAULI TIMILIFU TENDAJI YENYE KAURIFU. Inarejea kuwa na amani na Mungu ambayo hupelekea kuwa na amani ndani ya mwamini na nyumba yake. Mungu hupenda watoto wake kuwa na nyumba zenye furaha, kuwa na upendo wa kuridhisha. Hii mara nyingi haiwezekani kwa mwenza mkali asiye amini mara nyingine haiwezekani kwa mwenza Mkristo mchanga, mbinafsi, mdhambi, huku kukosa amani ndiyo sababu hasa kwa nini nyumba nyingi za "Kikristo" huvunjika. Mara nyingi mwenza anaweza kuwa aaminiye, lakini hajakomaa, amani haipo kwenye nyumba zote za Kikristo, siwezi kuamini kwamba Paulo katika muktadha huu anatetea kuishi pamoja kwa gharama yoyote, yapo mazingira ya hatari kimwili na kihisia. Hii haiwezi kuwa amri ngumu na ya haraka kwa watu wote. Lazima itafasiliwe kimazingira na kutazama maandiko mengine. Ni vigumu sana kuweka uwiano, heshima yetu kwenye maandiko na muonekano wa utamaduni wa kihistoria katika ufunuo (yaani, Biblia).
Maandiko ya UBS[4] yanapendelea (B rating) "wewe" WINGI, inayopatikana katika MSS א[*], A, C, K, badala ya "sisi" (MSS P[46], אi[2], B, D, F, G). Kuna tofauti nyingi za kimaandiko kuhusu VIWAKILISHI.

**7:16 "Au wajuaje, wewe mwanamume, kama utamwokoa mkeo"** Kuna tafsiri mbili zinazoweza kuhusika hapa ambazo zinakinzana hasa.

1. ibara hii pengine inafuata 1 Pet. 3:1-12 ambapo uinjilisti ni sababu yenye maana kwa kuendeleza uhusiano wa ndoa (kama vile NRSV, TEV, NJB, NEB, NIV)
2. ndoa kimsingi si kiinjilisti; ni muunganikano na ushirika, kwa hiyo, mwenza aaminiye hapaswi kukaa na mwenza asiye amini kwenye hali ya matusi na ugomvi na bila upendo mradi tu kwa tumaini la uinjilisti (kama vile maelezo mwishoni mwa ukurasa, tafsiri ya Filipi na LB)

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 1 WAKORINTHO 7:17-20**
**[17] Lakini kama Bwana alivyomgawia kila mtu, kama Mungu alivyomwita kila mtu, na aenende vivyo hivyo. Ndivyo ninavyoagiza katika makanisa yote. [18] Je! Mtu fulani ameitwa hali amekwisha kutahiriwa? Asijifanye kana kwamba hakutahiriwa. Mtu fulani ameitwa hali hajatahiriwa bado? Basi asitahiriwe. [19] Kutahiriwa si kitu, na kutokutahiriwa si kitu bali kuzihifadhi amri za Mungu. [20] Kila mtu na akae katika hali ile ile ambayo alikuwa nayo alipoitwa.**

**NASB "Tu"**
**NKJV "lakini"**
**NRSV "Hata kama"**
**TEV "limeondolewa"**

**NJB "basi"**
**NIV "Hata hivyo"**
Hiki kinatambulisha kidokezo kilichosambaa cha mjadala wa Paulo kuhusu maswala ya ngono. Neno la Kiyunani *ei mē* linaweza kumaanisha "mpaka," "isipokuwa," au "lakini."

**NASB, NRSV "Bwana amemgawia kila mtu"**
**NKJV "Mungu amegawa kwa kila mmoja"**
**TEV "vipawa vya Bwana kwako"**
**NJB "Bwana ametoa kwake"**

KITENZI *merizō* kinamaanisha "kugawa ama kugawanya." Imetumika katika maandiko ya kale ya Kiyunani katika ugawaji wa nchi ya ahadi kwa makabila ya Kiyahudi na YHWH (kama vile Kut. 15:9; Hes. 26:53,55,56; Kumb. 18:8), ambayo inafanya sitiari kwa watu wa Mungu kama inavyo fanya KITENZI kinachofuata, "kuitwa." YHWH "aliita" watu wake na wao waliita jina lake. Katika muktadha huu VITENZI vyote vinahusu ukirimiwa maalumu wa Mungu (kama vile 1 Kor. 7:7), ambako kunaruhusu watu kumtumikia (kama vile 1 Kor. 12:7,11). Hali yoyote ya maisha wakati walipoitwa, wakiokolewa na kupewa vipawa, sasa wanawajibika kutumikia (yaani, "kaa kama ulivyo," 1 Kor. 7:8,17,20,24,26,40). Stawi pale ulipopandwa kwa msaada wa Mungu na baadhi ya matarajio.

**NASB "kwa namna hii mwache atembee"**
**NKJV " kwa hiyo mwache atembee so let him walk"**
**NRSV "acha kila mmoja wenu aishi maisha"**
**TEV "endelea kuishi"**
**NJB "acha kila mmoja aendelee kuishi"**
Hii kiuhalisia ni "kutembea" (yaani,KAULI TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO),ambayo ni sitiari ya kibiblia kwa mtindo wa maisha (kama vile Efe 2:2,10; 4:1,17; 5:2,15; Kol. 1:10; 2:6). Palulo anachomaanisha katika 1 Kor. 7:18-20.

▣**"Ndivyo ninavyoagiza katika makanisa yote"** Hiki kifungu kimerudiwa katika 1 Wakorintho (kama vile 1 Kor. 4:17; 7:17; 11:16; 14:33; 16:1). Kanisa la Wakorintho walijifikilia kuwa kama watu"maalumu," "waliopendelewa," na "kupewa karama kwa namna ya kipekee." Paulo anakanusha kiburi cha kupindukia cha majivuno ya uongo kwa madai kwamba yeye hufundisha kweli hizi kwenye makanisa yote. Angalia Mada Maalum: Kanisa katika 1 Kor. 1:2.

**7:18**
**NASB "Hapaswi kuwa kama asiye tahiriwa"**
**NKJV "Usimhurusu kuwa asiye tahiriwa"**
**TEV "asijaribu kuondoa alama ya kutahiriwa"**
**NJB "ikiwa mtu aliyeitwa alikwisha kutahiriwa basi na abaki kama aliyetahiriwa"**
Hii ni KAULI TENDWA SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO (inafanana na 1 Kor. 7:18b pia ni KAULI TENDWA SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO). Hii inahusu mtu ambaye anayeondoa alama za kutahiriwa kwa kufanyiwa upasuaji (kama vile I Wamakabayo 1:15 na Josephus' *Antiq*. 12.5.1).

**7:19 "Kutahiriwa si kitu, na kutokutahiriwa si kitu"** Hii inaonyesha mtazamo wa Paulo juu ya taratibu za ibada katika Agano la Kale (kama vile Matendo 15; Rum. 2:28,29; Gal. 5:6; 6:15; angalia Mada Maalum katika 1 Kor. 9:9). Hili lilikuwa swala lile lile lililompeleka Yesu salemu kwenye baraza katika Matendo 15 na likapelekwa na waliotaka kulifanya kanisa liwe la Kiyahudi kwenye makanisa ya Wagalatia. Thiolojia ya Paulo katika sehemu hii iko wazi kabisa. Mataifa hawataki kufanya ibada za kiyahudi na mambo ya ibada za kidini. Wayahudi waaminio hawapaswi kujivunia au kuonea aibu utendaji wa taratibu za Agano la Kale walioutekeleza(kama vile 1 Kor. 10:16; Kumb. 30:6; Yer. 4:4), (kama vile Yer. 6:10) kumsikia Mungu na kusema ujumbe wake (kama vile Kut. 6:12,30) kusema ujumbe wake katika Kristo (kama vile Yer. 9:25,26).

◙**"bali kuzihifadhi amri za Mungu"** Huu ni msisitizo wa manabii wa Agano la Kale kwamba utii ni bora kuliko taratibu za ibada (kama vile 1 Sam. 15:22; Isa. 1:11-17; Hos. 6:6; Amos 5:21-27; Mik. 6:6-8). Mungu huangalia mwelekeo wetu na nia zetu kabla hajatazama matendo yetu. Mambo yote ambayo Mungu anamfanyia mwanadamu aliyeanguka, wa Agano la Kale ma Agano Jipya yako kwenye msingi wa kimaagano. Utii ni lazima (kama vile Luka 6:46), lakini mwonekano wa mahitaji dhahiri kimaagano umebadilika kutokana na muda.

**7:20 "Kila mtu na akae katika hali ile ile ambayo alikuwa nayo alipoitwa"** NKJV Iko katika maana iliyo wazi na inaruhusu neno "acheni kila mtu abaki kwenye wito ule ule ulioitwa" (kama vile Efe. 4:1,4). Hii ni KAULI TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO. Ni wazo la Paulo linalojirudia katika Muktadha huu (1 Kor. 7:8,17,20,24,26,40). Neno "itwa" (kama vile 1 Kor. 1:20). Angalia MADA MAALUM: ITWA (SPECIAL TOPIC:CALLED) katika 1 Kor. 1:1.

**ANDIKO LA NASB(LILILOBORESHWA):1 WAKORINTHO 7:21-24**
**[21] Je! Uliitwa u mtumwa? Usione ni vibaya lakini kama ukiweza kuwa na uhuru, afadhali kuutumia.[22] Kwa maana yeye aliyeitwa katika Bwana hali ya utumwa, ni huru wa Bwana. Vivyo hivyo yeye naye aliyeitwa hali ya uhuru, ni mtumwa wa Kristo. [23] Mlinunuliwa kwa thamani; msiwe watumwa wa wanadamu. [24] Ndugu zangu, kila mtu na akae mbele za Mungu katika hali iyo hiyo aliyoitwa nayo.**

**7:21 "**mtumwa**"** Angalia Mada Maalum katika 1 Kor. 4:1.

**NASB "kama ukiweza kuwa na uhuru, afadhali kuutumia"**
**NKJV " lakini kama ukiweza kuwa na uhuru, afadhali kuutumia"**
**NRSV "hata kama unaweza kupata uhuru wako, tumia hali yako ya wakati wowote"**
**TEV "lakini kama una nafasi ya uhuru, inakupasa kutumia kikamilifu hali yako kama mtumwa"**
**NJB "hata kama una nafasi ya uhuru, inakupasa kutumia kikamilifu hali yako kama mtumwa"**

Hii ni SENTENSI YENYE MASHARTI DARAJA LA KWANZA, baadhi ya watumwa watapata nafasi ya kuwa huru, ikifuatiwa na, KAULI YA KATI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFU, "fanya kitu!" Kuna tafsiri mbili zinazowezekana.

1. Kwamba mtumwa anapaswa kusalia kwenye kituo ambacho ameitwa, 1 Kor. 7:20,24
2. kwamba ikiwa anayo fursa ya kuwa huru yeye, me/ke lazima afaidi fursa hii (kama vile NASB, TEV, JB)

Hii inapatikana kwenye muktadha wa karibu kuhusu uhuru wa (1) wasio na ndoa wawe na ndoa, 1 Kor. 7:9 na 28 (kama vile NRSV, NJB) na (2) wenza waaminio kuwaacha wenza wasio amini, 1 Kor. 7:15. Hapa kuna ushauri binafsi wa Paulo na uchaguzi wa aaminiye binafsi upande kwa upande. Waaminio wote hupambana sana na "sehemu hizi za kijivuna." Wakati Bwana ama andiko halijaelekeza swala waziwazi, waaminio wanapewa kufanya uchaguzi wa ki-Ungu"! Katika baadhi ya maeneo "kipimo kimoja"!

## MADA MAALUM: MAONYO YA PAULO JUU YA UTUMWA (SPECIAL TOPIC: PAUL'S ADMONITIONS TO SLAVES)

**7:22-23** Katika Bwana waaminio wote wako huru; katika Bwana waaminio wote ni watumishi (kama vile 1 Kor. 8:1-10:33; Rum. 14:1-15:13). Yesu akitenda kama, our *go'el*, alitununua kutoka utumwa wa dhambi na nafsi. Sasa tunamtumikia yeye (kama vile 1 Kor. 6:20; 7:23; Rum. 6; Kol. 2:16-23).

**7:23 "msiwe watumwa wa wanadamu"** Kiyunani ni lugha iliyopindishwa. Wakati mwingine muundo unaweza kuwa na maana mbili zinazowezekana. Hii KAULI SHURUTISHI yawezakuwa

1. KAULI YA KATI YA WAKATI ULIOPO, "msiruhusu nafsi zenu kuwa watumwa wa watu"
2. KAULI TENDWA YA WAKATI ULIOPO, “msifanywe na watu kuwa watumwa”)

Yote yanafaa huu muktadha. Vikundi ndani ya kanisa la Korintho vilikuwa vinajaribu kutawala au kuthibiti waamini wote. Hili bado linatokea leo. Inabidi kuwepo uhuru wenye mipaka; uhuru, sio nafsi na dhambi bali kwa Kristo (kama vile Warumi 6 na 14); uhuru wa chaguzi za mfumo wa maisha ya watu binafsi kuhusu jinsi mtu anavyoweza kumtumikia Yesu vizuri zaidi akiongozwa na vipawa alivyopewa na Mungu pamoja na mazingira ya wakati uliopo.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 1 WAKORINTHO 7: 25-31**

**[25] Kwa habari za wanawali sina amri ya Bwana, lakini natoa shauri langu, mimi niliyejaliwa kwa rehema za Bwana kuwa mwaminifu. [26] Basi, naona hili kuwa jema, kwa ajili ya shida iliyopo, kwamba ni vema mtu akae kama alivyo. [27] Je! Umefungwa kwa mke? Usitake kufunguliwa. Umefunguliwa? Usitafute mke. [28] Lakini, kama ukioa, huna hatia; wala mwanamwali akiolewa, hana hatia; lakini watu kama hao watakuwa na dhiki katika mwili nami nataka kuwazuilia hayo. [29] Lakini, ndugu, nasema hivi, muda ubakio si mwingi; basi tokea sasa wale walio na wake na wawe kama hawana; [30] na wale waliao kama hawalii; na wale wafurahio kama hawafurahi; na wale wanunuao, kama hawana kitu. [31] Na wale wautumiao ulimwengu huu, kama hawautumii sana; kwa maana mambo ya ulimwengu huu yanapita.**

**7:25 "Kwa habari"** Hii ni alama ya maandiko kuonesha kwamba Paulo anaelekea kwenye swali jingine lililoandikwa ambalo alilipokea kutoka ndani ya kanisa la Wakorintho (kama vile 1 Kor. 7:1,25;8:1; 12:1; 16:1,12).

**NASB, NKJV,**
**NRSV, NIV "bikra"**
**TEV "wasiiooana"**
**NJB "watu wanaobaki mabikra"**

Swali kuu kuhusu neno hili ni jinsi matumizi yake katika 1 Kor. 7:25 yanavyohusiana na matumizi yake katika 1 Kor. 7:36 (tazama nukuu katika 1 Kor. 7:36). Muktadha wa 1 Kor. 7:25-35 waonekana kukaa pasipo kuoa dhidi ya ndoa kama hali ya wakati uliopo ambayo ingeweza kuhusu

1. Kuja kwa mara ya pili kunakoelekea kutokea
2. mateso ya kiserikali
3. njaa iliyokumba eneo kubwa
4. uwezo wa mtu mmoja binafsi kuelekea kumtumikia Kristo

◙**"sina amri ya Bwana, lakini natoa shauri"** Baadhi wamejaribu kutumia kauli ya Paulo katika 1 Kor. 7:6 na 25 kushusha mamlaka yake kama mtume ama kufanya hili kuwa na hali ya kutokuwa na uvuvio. Sivyo pia. Hii ni njia ya kimbinu ya kukubali kwamba hajui kama Yesu aliwahi kueleza swala hili dhahiri. Aya ya 25 na 40 zinaonesha kwamba Paulo alihisi utume wake na wito vilimpa yeye mamlaka kueleza maswala ambayo yaliibuka katika maisha ya kanisa la awali la watu wa mataifa.

◙**"mimi niliyejaliwa kwa rehema za Bwana kuwa mwaminifu"** Hii ni KAULI TIMILIFU TENDWA YA HALI YA KUENDELEA. Hii ni njia yenye nahau inayo thibitisha mamlaka yake ya kitume na uelewa unaoongozwa na Roho.

**7:26**
**NASB, NKJV,**
**TEV "mateso yaliyopo"**
**NRSV "machafuko yanayokaribia"**
**NJB "kwa sababu ya mfadhaiko unaotusonga"**

Hii imetafsiriwa katika njia kadhaa lakini ni muhimu sana kuona kwamba idadi kubwa ya matamko katika sura ya 7 sio kanuni kwa watu wote bali ni majibu ya Paulo kwa hali za mahali na za muda. Baadhi waona kwamba kirai hiki kinahusu

1. Machafuko ya utamaduni wa kipagani
2. hali mahususi za mahali katika Korintho
3. njaa eneo lolote
4. ukaaribu wa kuja kwa pili (kama vile 1 Kor. 7:29)

◙**"kwamba ni vema mtu akae kama alivyo"** Kuna mchezo kwenye neno "vizuri" (kama vile 1 Kor. 7:1,18,26), ikimaanisha "enye manufaa." Dhamira inayojirudia ya “kukaa katika hali hiyo hiyo kama ulivyookoka" (kama vile 1

Kor. 7:8,12-13,18,21,24,26,27,37,40) ni kiwango cha kithiolojia cha Paulo cha ndani ya barua hii.

**7:27"Je! Umefungwa kwa mke"**Hii KAULI TIMILIFU TENDWA YENYE KUARIFU kutoka kwenye neno *dēo*, ambayo inamaanisha kufunga. Inatumika kwenye maana ya ki-sitiari kwa ndoa (kama vile 1 Kor. 7:27,39; Rum. 7:2). Kuna mlinganisho kwenye kirai hiki katika aya hii hii ambayo pia ni KAULI TIMILIFU TENDWA YENYE KUARIFU, "Umewekwa huru toka kwa mkeo?" Paulo anataka wasikilizaji wake kubaki kama walivyo.

◙**"Usitake kufunguliwa. . .Usitafute mke"**Zote hizi ni KAULI TENDAJI SHURUTISHI ZA WAKATI ULIOPO zikiwa na KIAMBATA HASI, ambazo zinamaanisha kuzuia kitendo kilicho kwenye mchakato. Hapa tena mtu ana wasiwasi kama vikundi kanisani vilikuwa vinatetea mwelekeo tofauti wa kifamilia (useja, ndoa, uzinzi) ama kusudi la Paulo ni kuzidisha kazi kwa Kristo. Hili ni jambo linalojirudia rudia. Paulo anaonekana kuthibitisha kwamba

1. Wote wanapaswa kubaki walivyokuwa
2. Ikiwa uko pekee, kazia kumtumikia Kristo
3. Ikiwa kuna hamu ya ndoa, hakuna tatizo, lakini tumia ndoa yako kumtumikia Kristo!

Waaminio hubaki maseja kutumika, huoa/huolewa kutumika, huishi katika mateso kutumika, huishi katika uhuru kutumika, huishi kifungo cha kithiolojia kutumika! Waaminio uokolewa kutumika!

**7:28 "Lakini. . . Lakini"** Hizi zote ni SENTENSI YENYE MASHARTI DARAJA LA TATU, inayomaanisha juu ya kitendo muhimu.

◙**"huna hatia"** Paulo anaeleza kwenye hali ya kipekee, sio kufanya matamko kwa watu wote. Ndoa ni ule utaratibu Mungu aliokupatia (kama vile Mwa. 1:28).

◙**"ikiwa, kama…ikiwa bikra"** Swali ni kuwa ni nani hili linamhusu? La kwanza linahusu 1 Kor. 7:27. Wale ambao hawajaoa/kuolewa. La pili lahusu 1 Kor. 7:25, wale ambao hawajaolewa/kuoa. Makundi yote mawili yanaelezwa tena katika 1 Kor. 7:34.

◙**"watakuwa na dhiki katika mwili nami nataka kuwazuilia hayo"** Hili halihusu ndoa kwa ujumla bali kwenye machafuko kwa wakati huo (kama vile 1 Kor. 7:26). Aya ya 32-34 inaelezea ndoa kama kanuni ya jumla.

◙**"dhiki"** Angalia Mada Maalum: Dhiki Kuu katika 2 Kor. 1:4.

◙**"katika mwili"** Hii kiuhalisia ni "mwili." Angalia Mada Maalum katika 1 Kor. 1:26.

**7:29 "muda ubakio si mwingi"** Hii ni KAULI TIMILIFU TENDWA YENYE MAFUMBO. Kumekuwepo tafsiri kadhaa za kifungu hiki; yaonekana ni kimuktadha kuhusisha 1 Kor. 7:26 ("mateso ya wakati uliopo"). Calvin aliamini ilihusu ufupi wa maisha ya mwanadamu; wengine katika mstari huo huo wanaamini kwamba inahusu ufupi wa fursa katika utumishi wetu wa kikristo. Naamini inahusu kuja kwa mara ya pili (kama vile 1 Kor. 7:31; Rum. 13:11-12).
Je? Paulo alitazamia kurudi haraka kwa Yesu ama kuchelewa kurudi? Kuna maandiko kwa pande zote mbili. Sidhani kama theolojia ya Paulo ilibadilika (au ilikoma). Katika moja ya nyaraka zake anafundisha kuja kwa mara ya pili kulichochelewa (kama vile 2 Wathesalonike 2). Paulo (kama waandishi wengine wa Agano Jipya) alitumia tumaini lenye uhakika la kurudi kwa Bwana mara ya pili kama kichocheo cha maisha ya utauwa na utendaji wenye nguvu . Kurudi kwa Kristo ni tarajio la kila kizazi cha waaminio, lakini inabaki kuwa kweli ya mmoja tu! Tazama Mada Maalum katika 1 Kor. 6:14.
Kwa ajili ya mjadala unaovutia kuhusu mafunuo ya kitabu cha ufunuo na mambo ya siku za mwisho na siku ya kiama na maaoni ya Paulo katika 1 Kor. 7:26,28,29, see *Hard Sayings of the Bible*, kur. 593-595.

**7:29-30 "wale waliao"** Hivi vifungu vinavyofanana vinaelezea maisha ya binadamu ya kawaida ya kila siku. Waaminio wanapaswa kubaki wameweka mwelekeo wao kwenye shughuli ya huduma zao kufuatana na vipawa vyao vya kiroho (kama vile 1 Kor. 7:32,35). Waaminio ni raia wa falme mbili, wa kiroho na kimwili ama kanisa na ulimwengu.Mwili sio mwovu bali wa kupita.Waaminio lazima wawe na nia ya kutumika, nia ya injili. Tunautumia

ulimwengu pamoja na rasirimali zake kwa ajili ya kuutumikia ufalme. La sivyo mambo ya kimwili, mambo ya kidunia hututumia! Usiruhu ndoa iwe kama kitu cha kutuzuia fursa za kiroho! Ishi kwenye falme zote mbili kwa hekima ya utauwa.

**7:30 "kama hawana kitu"** Angalia Mada Maalum ifuatayo.

## MADA MAALUM: UTAJIRI (SPECIAL TOPIC: WEALTH)

**7:31 "kwa maana mambo ya ulimwengu huu yanapita"** Manabii wa Agano la Kale (hasa. Isaya 56-66) wanafunua mbingu mpya na nchi mpya. Kizazi kipya kitakuwa kama cha zamani lakini kimetakaswa, kimekombolewa, (kama vile 2 Pet. 3:10-13). Mbingu itakuwa bustani ya Edeni-Mungu, mwanadamu, wanyama wakitimiliza ushirika na utaratibu uliorejeshwa; Mwanzo 1-2 inafanana na ufunuo 21-22.
Kila kizazi cha waaminio kinapitia utaratibu unaopita wa ulimwengu huu (yaani, *schēma*) wanapokua kwenye kufanana na Kristo. Kwa jinsi tunavyomwona Kristo katika njia zilizo wazi zaidi, mambo ya uhai huu yanazidi kuwa ya giza zaidi. Tuko ulimwenguni lakini sisi sio wa ulimwengu huu. Twavitumia vitu vya ulimwengu kwa makusudi ya uinjilisti, sio makusudi yetu binafsi.

**ANDIKO LA NASB(LILILOBORESHWA): 1 WAKORINTHO 7:32-35**
**[32] Lakini nataka msiwe na masumbufu. Yeye asiyeoa hujishughulisha na mambo ya Bwana, ampendezeje Bwana; [33] bali yeye aliyeoa hujishughulisha na mambo ya dunia hii, jinsi atakavyompendeza mkewe. [34] Tena iko tofauti hii kati ya mke na mwanamwali. Yeye asiyeolewa hujishughulisha na mambo ya Bwana, apate kuwa mtakatifu mwili na roho. Lakini yeye aliyeolewa hujishughulisha na mambo ya dunia hii, jinsi atakavyompendeza mumewe. [35] Nasema hayo niwafaidie, si kwamba niwategee tanzi, bali kwa ajili ya vile vipendezavyo, tena mpate kumhudumia Bwana pasipo kuvutwa na mambo mengine.**

**7:32-34** Hii inaelezea kujitoa kwa watu wawili waliooana kila mmoja kwa mwenzake kama "mwili mmoja" (kama vile Efe. 5:24-31). Huu sio uovu unaotumiwa kuelezea uhusiano kati ya Kristo na kanisa lake. Ni dhahiri kwamba wasio na ndoa wanao muda na nguvu zaidi kwa ajili ya kutumika.

Jukumu la Paulo katika muktadha huu limekuwa ni uwezo wa kuwa mwamini mtendaji pasipo jukumu. Paulo anatumia neno *merimnaō*, mara nne kwenye aya mbili. Neno hili linaaweza kuhusu mwenye kukosa makusudi (kama vile Mt. 10:19; Luka 12:25) ama shughuli halali (kama vile 2 Kor. 11:28; 1 Pet. 5:7). Katika muktadha huu inahusu mambo ya kawaida ya maisha ya ndoa yanayoweza kushindana na muda na nguvu ambazo mtu anapaswa kuzitumia kwa Bwana. Inaweza pia kuhusu mashinikizo ya kipekee ya kuwa aaminiye ndani ya jamii ya kipagani (kama vile 1 Kor. 7:26). Paulo anataka waaminio (1) wawe watendaji kwa ajili ya Kristo na (2) waishi kwa amani na kutosheka. Yote mawili ni halali lakini magumu.

**7:34 "mke na mwanamwali Yeye asiyeolewa"**Paulo anazungumzia aina mbili tofauti za wanawake ambao hawajaolewa:

1. Mmoja ana umri mkubwa zaidi, mmoja ni mwenye umri mdogo zaidi
2. wa kwanza alikuwa ameolewa hapo nyuma (yaani, mjane) na wa pili hajaolewa kabisa
3. wa pili yawezekana unahusika na kundi maalum la walioacha kuolewa ama wenza katika huduma (kama vile 1 Kor. 7:36-38)

◙**"apate kuwa mtakatifu mwili na roho"** Hili sio wazo la kushusha hadhi kuhusu suala la kujamiiana kwa binadamu kuwa uovu. Hii ni jinsi mafundisho ya Paulo yalivyokuwa yanatafasiriwa na wale waliokuwa wameathiriwa na utamaduni wa Kiyunani (yaani, wale wenye kuvumilia mateso na shida, wale wenye mafunuo, n.k.). Wazo lake kuu ni kwamba watu walioelekea kwa Bwana wanaweza kutumia Muda wao, nguvu zao, na rasirimali zenye thamani kwenye mambo ya kiroho, wakati wale walioolewa lazima pia washugulikie familia zao majukumu mengine. Angalia MADA MAALUM: TAKATIFU (SPECIAL TOPIC: HOLY) katika 1 Kor.3:17.

[MADA MAALUM: MWILI NA ROHO (SPECIAL TOPIC: BODY AND SPIRIT]

**7:35 "si kwamba niwategee tanzi,"** Neno hili lilitumika kuhusu hatamu ya mnyama.

**NASB "bali kuelekeza kile kilicho sahihi na kuhifadhi umakini usioondolewa kwa Bwana "**
**NKJV "bal ikwa kilicho sahihi na kwamba mnaweza kumtumikia Bwana bila kuondoa umakini wenu mlio utoa kumwelekea Bwana"**
**NRSV "bali kuendeleza utaratibu mzuri na upendo mkubwa usiozuiwa kwa Bwana"**
**TEV "Badala yake nataka ninyi kufanya kilicho haki na sahihi na kutoa nafsi zenu kwa moyo mkunjufu"**
**NJB "lakini kwamba kila jambo lifanyike inavyo paswa nanyi muweze kutoa umakini wenu usiogawika kwa Bwana"**

Kifungu cha Kiyunani ni cha ufasaha zaidi. Maneno mawili ya msingi ni

1. *euschēma*, muunganiko kutoka "nzuri" na "muundo." Linaashiria kwamba kile kilicho sahihi, chenye kupendeza, na kinachofaa (kama vile 1 Kor. 12:23-24; 14:40; Rum. 13:13) chenye kufanana kwenye maana *kalos* katika 1 Kor. 7:1,8,26.
2. *aperispastōs*, HERUFI YA MWANZO KANUSHI ikiwa na neno la kugeuka na hivyo kupoteza lengo

Paulo anataka waaminio wote kuelekea kwenye ufalme, katika huduma! Mimi hakika nakubaliana na hili. Langu "tatizo" na kwenye muktadha huu ni kuonekana kwake kushusha heshima ya ndoa kama huduma iliyo sawa na muundo wa useja. Mungu alianzisha ndoa; ni kanuni; mimi ni mtu mwenye nguvu zaidi na mfanya huduma kwa sababu ya ndoa yangu. Sura hii imekuwa ikitumika na kushambuliwa kwa maneno na wanao shikilia sana sheria na wanaojinyima anasa. Lengo ni huduma iliyoelekezwa sio utawala wa kidini wa sheria zisizo hojiwa wala kujadiliwa kuhusu kuoa au kuwa mseja. Paulo alikuwa na makusudi yaliyoongozwa na Roho lakini haya hayawezi kuzigeuza kuwa kanuni za wote ambazo zinakana maandiko mengine yaliyovuviwa.

**ANDIKO LA NASB(LILILOBORESHWA): 1 WAKORINTHO 7:36-38**

**[36] Lakini mtu awaye yote akiona ya kuwa hamtendei mwanamwali wake vipendezavyo, na ikiwa huyo amepita uzuri wa ujana wake, na ikiwapo haja, basi, afanye apendavyo, hatendi dhambi, na awaruhusu waoane. [37] Lakini yeye aliyesimama kwa uthabiti wa moyo wake, hana sharti, lakini aweza kuyatawala mapenzi yake, tena amekusudia moyoni mwake kumlinda mwanamwali wake, atatenda vema.[38] Basi, hivyo na amwozaye mwanamwali wake afanya vema; na yeye asiyemwoza atazidi kufanya vema.**

**7:36 "ikiwa"** Hii ni SENTENSI YENYE MASHARTI DARAJA LA KWANZA, ambayo inachukuliwa kwamba ni kweli kutokana na mtazamo wa mwandishi ama kutokana na makusudi yake ya uandishi.

**NASB "mtu yeyote. . .kuelekea binti yake bikra"**
**NKJV "Mtu yeyote. . .kuelekea bikra wake"**
**NRSV "awaye yote. . . mwanamwali wake"**
**TEV "ikitokea wenza wamechumbiana ambao wameamua wasioane ikiwa mwanaume. . .kuelekea mwanamwali"**
**NJB "Mtu mwenye hamaki ya mapenzi. . .kuelekea mchumba wake"**

Kuna aya tatu muhimu katika ukurasa huu.

1. kwamba hii inahusu baba Mkristo na binti yake (kama vile NASB na JB)
2. kwamba hii inahusu mwanaume Mkristo na mchumba wake (kama vile NRSV, TEV, NJB)
3. kwamba hii inahusu aina ya ndoa ya kiroho ambayo ingeweza kutafsiriwa wenza katika "useja kwa sababu ya mambo ya kidini" (kama vile NEB)

Neno hili kiuhalisia ni "bikra."

Chaguo #1 linatumia kifungu "yeye atoaye" (1 Kor. 7:38) kama inavyorejea kwa Baba atoapo binti yake kuolewa. Chaguo #2 inachagua juu ya kifungu katika 1 Kor. 7:36, "ikiwa amepita uzuri wa ujana wake." Uchaguzi waonekana bora zaidi katika nuru ya ushahidi wote wa ki-maandiko na wa kihistoria. Chaguo #3 linachukulia hali mahususi la

kihistoria. Baadhi ya wahubiri watembezi wa karne ya kwanza wanaweza kuwa walichukua mabikra Wakristo kama wasaidizi kwenya huduma na kuishi nao lakini walibaki waseja kama ishara yao ya kujithibiti.

◙**"ikiwa"** Hii ni SENTENSI YENYE MASHARTI DARAJA LA TATU, inayomaanisha juu ya tendo muhimu.

**NASB "(ke) amepita uzuri wa ujana wake"**
**NKJV "(ke) amevuka maua ya ujana wake"**
**NRSV "(me) hisia zake za mapenzi ni kali"**
**TEV "(me) hisia za mapenzi ni kali mno"**
**NJB "kwamba mambo yashike mkondo wake"**

Hii inaweza kuhusu (1) muda wa kawaida wa ndoa (kama vile NASB, NKJV, na NJB) au (2) kwa kuwa muundo yawezekana kuwa wa KIUME, sio wa KIKE, iinaweza kurejea kwa mwanaume mwenye ashiki (kama vile NRSV, TEV).

Kwa neno "amepita ujana wake" (*huperakmos*) tazama Mada Maalum: Matumizi ya Paulo ya *Huper* Compounds katika 1 Kor. 2:1.

◙**"basi, afanye apendavyo"** Hili kiuhalisia "hivyo apaswa kuwa kile mtu apendacho." Kifungu kinaweza kuhusu mwanaume ama mwanamke. VIWAKILISHI katika muktadha wote viko tatanishi sana na kiuhakika kuvitafsiri haiwezekani.

**NASB "mwacheni aolewe"**
**NKJV, NRSV "awaruhusu waoane"**
**TEV "wanapaswa kuoana"**
**NJB "wanapaswa kuoana"**

Hii ni KAULI TIMILIFU TENDAJI SHURUTISHI YA MTU WA TATU KATIKA HALI YA WINGI, kiuhalisia "waruhusuni waoane." Hii inahusu (1) mwanaume na mchumba wake (2) "wenza katika useja."

**7:37 "aliyesimama kwa uthabiti"** Angalia Mada Maalum: Simama katika 1 Kor. 15:1.

**7:38 "asiyemwoza atazidi kufanya vema"** Huu sio ushauri unaoshusha hadhi ndoa bali ni maonyo ya kiutendaji katika uwazi wa

1. Mgogoro uliokuwepo Korintho
2. ukaribu wa kuja mara ya pili
3. hali ya kawaida ya ashiki ya tendo la ndoa kwa Wakristo husika

**ANDIKO LA NASB(LILILOBORESHWA): 1 WAKORINTHO 7:39-40**
**39 Mwanamke hufungwa maadamu mumewe yu hai, lakini ikiwa mumewe amefariki, yu huru kuolewa na mtu ye yote amtakaye; katika Bwana tu. 40 Lakini heri yeye zaidi akikaa kama alivyo; ndivyo nionavyo mimi, nami nadhani ya kuwa mimi nami nina Roho wa Mungu.**

**7:39 "Mwanamke hufungwa maadamu mumewe yu hai"** Hii ni KAULI TIMILIFU TENDWA YENYE KUARIFU (kama vile 1 Kor. 7:27). Msitari wa 39 unaonyesha kwamba kuoa/kuolewa baada ya kifo cha mwenza wako sio uovu (kama vile 1 Tim. 5:14). Vile vile inaonyesh pia kwamba Paulo hajaribu kufanya sheria ziwe ngumu na haraka kwa wote.

◙**"katika Bwana tu"** Kuna tafsiri mbili ambazo zaweza kuwepo: (1) Mkristo lazima aoe/aolewe na Mkristo (kama vile 2 Kor. 6:14) au (2) Mwanamke lazima atende kama Mkristo ikiwa anaoolewa tena. Mara nyingi 2 Kor. 6:14 inatumika kama ushahidi wa chaguo namba moja, lakini katika muktadha haielezi mahsusi swala hili.
Hata hivyo kwa njia ya kanuni inaweza kuwa.

**7:40 "ndivyo nionavyo mimi. . .nadhani ya kuwa mimi nami nina Roho wa Mungu"** Paulo anatamka tena dhamira yake inayo jirudia rudia na fikra yake ya uvuvio wa Ki-Ungu (kama vile 1 Kor. 7:12,25).

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujisomea wa fasiri, ambayo inamaanisha kwamba unao wajibu wa tafsiri yako mwenyewe ya Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika nuru tuliyo nayo. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hupaswi kumuachia vitu hivi mfasiri.

Maswali haya ya majadiliano yanatoa tu, msaada wa wewe kufikiria kupitia masuala nyeti ya sehemu ya kitabu hiki. Yamekusudiwa kukuchokonoa mawazo na sio kutoa maana ya mwisho.

1. Tunatumiaje ukweli wa sura ya 7 leo?
2. Ni kwa kiasi gani sura ya 7 iko kitamaduni na kiasi gani iko kwa watu wote?
3. Useja ni hali ya juu ya kiroho kwa Paulo kuliko ndoa? Kama ndivyo kwanini?
4. Biblia inaruhusu kuachana kama ndivyo biblia inaruhusu kuoa/kuolewa tena? (1Kor. 7:28,39)
5. Mgogoro gani uliokuwepo ambao Paulo anaurejea katika "mgogoro wa sasa" 1 Kor. 7:26?
6. Neno "bikra" linatumika tofauti katika 1 Kor. 7:25 na 36?

# 1 WAKORINTHO 8

| MGAWANYO WA AYA WA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **UBS[4]** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB** |
| Chakula kilichotolewa Kwa sanamu | Uwe mwangalifu kwenye dhamiri | Mkristo aweza kula chakula kilichotolewa Kwenye sanamu | Swali kuhusu chakula kilichotolewa kwa sanamu | Chakula kilichotolewa kwa miungu (8:1-11:1) Kanuni za jumla |
| 8:1-6 | 8:1-13 | 8:1-3 | 8:1 | 8:1-6 |
| | | | 8:2-3 | |
| | | 8:4-6 | 8:4-6 | Madai ya ujuzi |
| 8:7-13 | | 8:7-13 | 8:7-8 | 8:7-13 |
| | | | 8:9-13 | |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (Kutoka "**Mwongozo wa Usomaji Mzuri wa Biblia"**) ("**A Guide to Good Bible Reading**")

### *KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo wa usomaji wa fasiri, Ikiwa na maana kwamba unawajibika kwa ukalimani wako wa biblia mwenyewe. Kila mmoja wetu sharti atembee katika nuru tuliyonayo.Wewe, Biblia na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika kutafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua somo. Linganisha mgawanyo wa somo lako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika kiaya sio uvuvio, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la asili la mwandishi ambalo ndilo kiini cha ukalimani. Kila aya ina somo moja na somo ni moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya ya tatu
4. N.k

## UTAMBUZI WA KIMUKTADHA WA 8:1-13

A. Mazingira ya kifasihi yanakwenda toka 8:1 hadi 11:1 kama ufafanuzi hapo juu wa toleo la NJB unavyoonyesha

B. Swala la kula nyama zilizotolewa kwa sanamu linaonekana kuwa geni machoni pa watu wa kisasa. Lakini katika mazingira ya siku za Paulo na watu wa Korintho lilikuwa suala muhimu sana. Zaidi kwenye mikusanyiko ya kijamii palikuwepo na vidokezo vya kidini katika enzi ya siku za Paulo. Pia, nyama iliyokuwa ikiuzwa sehemu za masoko ya Korintho zaidi, lakini sio yote, ilitoka moja ya mahekalu ya kipagani.

C. Kithilojia sura ya 8 inafanana na Warumi 14:1-15:13. Tazama Mada Maalumu: Mtazamo wa Kimktadha toka Rum. 14:1-15:13 ya 1 Kor. 6:12, ambao ni mihtasari zilizochukuliwa toka kwenye fasiri zangu za Rum. 14:1-15:13. Zote kati ya hizo zinashughulika na somo gumu la namna Wakristo wanavyolinganisha uhuru wao katika Kristo na wajibu wao katika upendo kwa wengine.

   Gordon Fee, *To What Exegesis?* Kur. 105-128, anafikiri kuwa mazingira haya yanarejea juu ya kutokula chakula kilichotolewa kwenye sanamu, lakini haswa kujihudhulisha na kushiriki chakulani pa hekalu la sanamu (ambapo mara nyingi inahusianishwa na mambo ya kujamiiana pia, k.v 1 Kor. 10:6-22).

D. Sura hii pia inasisitizia kwamba ujuzi, hata maarifa ya kimafunuo, yasipokuwa na mlinganyo wa upendo kwa wengine kidogo ni kweli (k.v 1 Kor. 13:1-13)

E. Nafikiri D.G Dunn, *Unity and Diversity in The New Testament,* UK. 319, unamaelezo mazuri ya muhtasari. "Hatasimama kwa Wakristo wa Kiyahudi wanaoushusha uhuru wa Mkristo kuelekea kwenye sheria(Gal. 5:1 na kuendelea, Flp 3:2 na kuendelea; lakini wala hatasimama kwa Wakristo wa mataifa wanaopotosha uhuru wa Mkristo wenye kukubarika na tabaka la kiuchaguzi (Rum. 16:17 na kuendelea; 1 Kor. 5-6; 8-10; k.v 2 Thes. 3:6,14 na kuendelea).

Kwa Paulo "injili kwa wote" ilikuwa ni kanuni ya kimwongozo. Hili kwa nguvu zote alilieleza kwa maneno yake katika Wakorintho 9:19-23

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB(LILILOBORESHWA):1 WAKORINTHO 8:1-3**
**[1]Na kwa habari ya vitu vilivyotolewa sadaka kwa sanamu; Twajua ya kuwa sisi sote tuna ujuzi. Ujuzi huleta majivuno, bali upendo hujenga. [2] Mtu akidhani ya kuwa anajua neno, hajui neno lo lote bado, kama impasavyo kujua. [3]Lakini mtu akimpenda Mungu, huyo amejulikana naye.**

**8:1 "Na kwa habari ya vitu vilivyotolewa sadaka kwa sanamu"** Hili ni swali lingine (K.V. 1 Kor. 7:1,25; 8:1; 12:1; 16:1,12) lile lililoulizwa na kanisa la Korintho katika barua waliomwandikia Paulo, iliyoletwa na Stephano, Fortunatus, na Achaicus (k.v 1 Kor. 16:17)

**NASB "Vitu vilivyotolewa sadaka kwa sanamu"**
**NKJB "Vitu vilivyotolewa kwa sanamu "**
**NRSV "Chakula kilichotolewa kafara kwa sanamu"**
**TEV "Chakula kilichotolewa kwa sanamu"**
**NJB " Chakula kilichotolewa kwa miungu"**

Hili ni neno la kimuunganikano *eidōlon*, lenye maana ya umbo, sura au kinyago, na *thuō*, likimaanisha kuuwa au kutoa dhabihu. Neno hili lilitumika kuzuia kula nyama zilizotolewa kwa sanamu katika barua iliyotumwa kwa makanisa ya watu wa mataifa toka kwenye baraza la Yerusalem katika Mdo.15:29 (k.v Mdo. 21:25)

◙ "**Twajua ya kuwa sisi sote tuna ujuzi"** Yumkini hii ni

1. Nukuu toka kwenye barua ile ambayo kanisa la Korintho lilimwandikia Paulo
2. Wito toka kwa moja ya vikundi vidogo vidogo
3. Nukuu toka kwenye mafundisho ya awali ya Paulo, ambayo kanisa la Korintho halikuyaelewa

◙ "**Ujuzi huleta majivuno, bali upendo hujenga"** Paulo alikubaliana na maelezo yaliyokuwemo ndani ya ile barua iliyotoka kwenye kanisa la Korintho lakini yakileta dhana ya ukinzani na kuonyesha ukweli wao na matumaini(hii pia ni kweli yao kwenye wito wa walimu wa uongo katika sura ya 6-7)

Ujuzi ulikuwa ni moja ya mwelekeo wa tamaduni za Kiyahudi ambao baadhi ya makanisa ya Kikorintho walijivunia kwayo. Tatizo la ujuzi ni kuwa unajaribu kumfanya mtu kuwa mshindani na mwenye kujivuna (k.v. 1 Kor. 4:6,18,19; 5:2; 8:1; 13:4; 2 Kor. 12:20). Tazama dokezo zima katika 1 Kor. 4:6. Inatazamisha juu ya ubinafsi, na sio kwenye familia, mwili ambalo ni kanisa.

Neno "hujenga" ni sitiari inayojenga. Paulo mara nyingi anaongea juu ya "kujenga" au "kuinua" kanisa au Mkristo binafsi (k.v. Rum. 14:19; 15:2; 1 Kor. 8:1; 10:23; 14:3,5,12,26; 2 Kor. 10:8; 12:19; 13:10; Efe. 4:12,29; 1 Thes. 5:11). Upendo ni wa muhimu katika uhuru wetu wa Mkristo, ujuzi hautatetea tatizo la kujivuna; ila upendo binafsi wenye ukomo unaweza kulifanya hilo. Waamini wanatakiwa kukitenda kile ambacho kinajenga kanisa, wala sio ambacho kinamtukuza Mkristo binafsi.

### MADA MAALUM: KUJENGA (SPECIAL TOPIC: EDIFY)

**8:2 "Ikiwa"** Hii ni SENTENSI YENYE MASHARTI DARAJA LA KWANZA ambayo inasadikiwa kuwa kweli kutokana na mtizamo wa mwandishi au kusudio lake la kifasihi (1 Kor.8:3,5)

◙ "**Mtu akidhani ya kuwa anajua neno**" Hii ni KAULI TIMILIFU TENDAJI YENYE KUARIFU ikifuatiwa na KAULI TIMILIFU ISIO NA UKOMO. Hii inaaksi majivuno yaliopo ya kanisa la Korintho (k.v 1 Kor. 3:18)

**NASB "Hajui neno lolote bado kama impasavyo kujua"**
**NKJV "Bado hajui chochote kama impasavyo kujua"**
**NRSV "Na bado hana maarifa yampasayo"**
**TEV "Haswa hajui impasavyo kujua"**
**NJB "Na bado hajui kama vile imstahilivyo"**
Paulo anadhihirisha kupungukiwa kwao na maarifa ya kiroho. Hekima ya kidunia (yaani falsafa ya mwanadamu) inasababisha matengano na majivuno, lakini maarifa ya ki-Mungu kwetu (k.v. 1 Kor. 13:12; Gal. 4:9) na ujuzi wetu wa injili unatuweka huru kumtumikia Yeye na watu wake.

**8:3 "Lakini mtu akimpenda Mungu"** Hii ni SENTENSI YENYE MASHARTI DARAJA LA KWANZA. Katika Korintho palikuwepo na wale waliompenda Mungu. Tazama msisitizo wa Paulo ni juu ya upendo (yaani KAULI TENDAJI ELEKEZI YA WAKATI ULIOPO) na sio kwenye ujuzi (k.v 1 Kor. 13:1-13)

◙ **"Huyo anajulikana naye"** Huu waweza kuwa ni mfano mwingine wa miito wa wale waliodai kuwa wameelimika zaidi na ni watu wa rohoni. Ni mfanano na kifungu cha mafunuo ya kale yaliyopatikana katika *Gospel of Truth* 19.33. Mtu mmoja wa kweli aliyeelimika anatambua kuwa hakuna matengano kati ya binadamu, hakuna kati ya

1. Yesu –na watu wa mataifa
2. Watumwa –na uhuru
3. Wanaume –na wanawake
4. Mwenye nguvu –na mdhaifu

Vizingiti vyote viko "chini" ya Kristo!
Maarifa yetu juu ya Mungu ni ya muhimu, lakini maarifa kuhusu Mungu sio mbadala wa mahusiano binafsi, yaliyoanzishwa na Mungu, yaliyotenda katika upendo wetu kwa wengine ambao unaelezea upendo wetu kwake Yeye (k.v. Gal. 4:6; 2 Tim. 2:19; 1 Yoh. 4:19)

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA):1 WAKORINTHO 8:4-6**
**4 Basi kwa habari ya kuvila vitu vilivyotolewa sadaka kwa sanamu; twajua ya kuwa sanamu si kitu katika ulimwengu, na ya kuwa hakuna Mungu ila mmoja tu. 5 Kwa maana ijapokuwa wako waitwao miungu, ama mbinguni ama duniani, kama vile walivyoko miungu mingi na mabwana wengi; 6 lakini kwetu sisi Mungu ni mmoja tu, aliye Baba, ambaye vitu vyote vimetoka kwake, nasi tunaishi kwake; yuko na Bwana mmoja Yesu Kristo, ambaye kwake vitu vyote vimekuwapo, na sisi kwa yeye huyo.**

**8:4** "**sanamu si kitu katika ulimwengu"** Kuna dhihaka juu ya vidokezo katika mistari hii kati ya dhana ya Kiebrania ya neno "twajua" kama uhusiano binafsi (k.v. 1 Kor. 8:3; Mwa. 4:1; Yer. 1:5) na vidokezo vya Kiyunani vya neno "twajua"kama kweli kuhusu kitu ama mtu (k.v. 1 Kor. 8:1,2,4)
Katika agano la kale sanamu zilikuwa "tupu" au "bure." Hakika haikuwa miungu (k.v. 2 Nya. 13:9; Isa. 37:19; 41:29; Yer. 2:11; Mdo. 14:15; Gal. 4:8). Paulo, baadaye katika 1 Wakorintho, anadai kuwa mapepo yanatumia ushirikina wa watu na ibada ya sanamu(k.v 1 Kor. 10:20) lakini hakuna ukweli kwenye sanamu!

◙"**na ya kuwa hakuna Mungu ila mmoja tu"** Huu ni uthibitisho wa kithiolojia wa wale wanoamini uwepo wa Mungu mmoja (k.v. 1 Tim. 2:5-6) kutokana na mafunuo ya biblia kuwa Mungu wa kweli ni mmoja tu (k.v. 1 Kor. 8:6; Kumb. 4:35,39; Zab. 86:8,10). Mara nyingi Agano la Kale linazungumzia juu ya "*Elohim*" wengine (yaani., viumbe vya kiroho) lakini hakuna kinachofanana (yaani kwa namna ile ile, k.v Kut. 20:2-3; Kumb. 32:39) YHWH (k.v. Kut. 15:11; Zab. 86:8; 89:6). Waombaji wa Kiyahudi waliita *Shema* toka Kumb. 6:4, ni uthibitisho wa Kiyahudi ulionukuliwa kila mara kwenye kila ibada ya kuabudu ikidai upekee na umoja wa YHWH (k.v Mark. 12:28-29)

[MADA MAALUM: MUNGU MMOJA (SPECIAL TOPIC: MONOTHEISM)]

**8:6 "Lakini kwetu Mungu ni mmoja tu"** Huu ni uthibitisho wa kithiolojia kwa wale wanaoamini uwepo wa Mungu mmoja. Angalia kwa kifupi 1 Kor. 8:4
Katika historia hii ya kidini, pamekuwepo na aina mbali mbali za imani kuhusu Mungu

1. wanaamini kuwa viumbe vingine vyenye roho vinahusiana na utaratibu wa kiasili au vitu
2. uwepo wa miungu wengi
3. miungu wengi, lakini mmoja kwa ajili yetu (yaani kabila, taifa, maeneo ya kijiografia)
4. uwepo wa Mungu mmoja tu (sio Mungu mkuu wa miungu yote ya dini fulani)

Andiko hili linadai kwamba uwepo wa viumbe vingine vyenye kuishi (k.v 1 Kor.8:5), lakini uwepo wa Mungu mmoja wa kweli (k.v 1 Kor. 8:4, Angalia [MADA MAALUM: MUNGU MMOJA (SPECIAL TOPIC: MONOTHEISM)] katika 1 Kor. 8:4). Kwa wale katika desturi za Wakristo wa Yudea kuna Muumba/Mwokozi mmoja ambaye anaishi katika Utatu mmoja. Angalia Mada Maalumu katika 1 Kor.2:10

◙ **"Baba"** Hii ni sifa ya ki-Ungu ya wazi, binafsi, na ya kawaida. Inasisitiza juu ya uwepo wa Mungu wa kila mahali. Dhana hii ya Mungu inaweza kujulikana kwa watu wake binafsi waliofunuliwa, sio wanadamu wenye falsafa au wavumbuzi. Ingawa sifa hii ya kawaida inatokea katika Agano la Kale kwa uchache (k.v. Kumb. 32:5-6; Isa. 63:16; 64:8; Yer. 31:9,20; Hos. 11:3-4; Mal. 1:6; 2:10), alikuwa ni Yesu, Mwana kwa ukamilifu alidhihirisha huu ufanano wa kushangaza, uliodhahiri (yaani Baba yetu, " Mt. 6:9; 23:9; Efe. 4:6; *Abba*, Mark 14:36). Angalia Mada Maalum katika 1 Kor. 1:3).

◙ **"Ambaye vitu vyote vimetokea kwake"** Huu ni udhihirisho wa Mungu kama Muumbaji (k.v. 1 Kor. 11:12; Rum. 11:36; 2 Kor. 5:18; Kol. 1:16; Ebr. 2:10). Angalia [MADA MAALUM: MZALIWA WA KWANZA (SPECIAL TOPIC: FIRSTBORN)] katika 1 Kor. 15:20

◙ **"Nasi tutaishi kwake"** Mungu aliumba Dunia kama hatua ya Mwanadamu kuwa na ushirika na Yeye. Baada ya matokeo ya Mwanadamu kuasi (k.v Mwanzo 3) ameshinda katika wokovu wetu na kurejeshwa kupitia Kristo, tunatambua kusudi letu tulilokusudiwa. Mara tu taswira ya Mungu katika Mwanadamu kurejeshwa kupitia Kristo, hatimaye ushirika binafsi wa Edeni ulirejeshwa.

◙ **"Bwana mmoja Yesu Kristo, ambaye kwake vitu vyote vimekuwapo"** Neno "Bwana" linaaksi tafasiri ya Agano la Kale la YHWH, ambacho ni KITENZI cha Kiebrania cha neno "kuwa" (k.v. Kut. 3:14, angalia Mada Maalum katika 1 Kor. 2:8). Wayahudi waliogopa kutangaza jina hili takatifu wasije wakalitamka bure, kwa hiyo, walilibadilisha kwa neno lingine la Kiebrania *Adon* au Bwana.

Kumwita Yesu Bwana (yaani., *kurios* ni mfanano wa neno la Kiebrania *Adon*), ni njia ya kuthibitisha Uungu wake na umoja wake na YHWH (K.V Flp. 2:11). Dhana ya umoja pia ni kitu cha muhimu (k.v Efe. 4:5; 1 Tim. 2:5). Ingawa Paulo hatumii neno *Theos* (yaani Mungu) kwa ajili ya Yesu katika muktadha huu, pia hulitumia hilo katika Mdo 20:28; Rum. 9:5; Tit. 2:13 na *Theotētus* katika Kolosai 2:9. Panaweza pasiwepo na shaka kuwa katika fikra za Paulo Yesu anabaki kuwa wa ki-Ungu. Paulo alikuwa ni mnaziri juu ya Mungu mmoja. Kamwe hakuweza kutambua Mungu mmoja anaweza kuishi ndani ya udhihirisho wa watu watatu, lakini hilo ndilo hitimisho lililosahihi. Angalia [MADA MAALUM: UTATU (SPECIAL TOPIC: THE TRINITY)] katika 1 Kor. 2:10

◙ **"Ambaye kwake vitu vyote vimekuwepo, na sisi tupo kwake"** Yesu alikuwa wakala kwenye Uumbaji (k.v. Yoh. 1:3; Kol. 1:16; Ebr. 1:2). Hii ndiyo ilikuwa kazi ya hekima ya kibinadamu katika Mithali 8:22-31. Hekima ni neno linalotumika kwenye Jinsia ya Kike katika Kiebrania (k.v Mith. 8:1-21) kwa sababu NOMINO ya neno "hekima" (BDB 315) ni NOMINO JINSIA YA KIKE. Katika sura hii tunaona mvutano kati ya uthibitisho wetu wa uwepo wa Mungu mmoja na ufunuo wa Agano Jipya wa Utatu. Angalia Mada Maalum katika 1 Kor. 2:10

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 1 WAKORINTHO 8:7-13**
**7 Bali ujuzi huu haumo ndani ya watu wote; ila wengine kwa kuizoelea ile sanamu hata sasa hula kana**

**kwamba ni kitu kilichotolewa sadaka kwa sanamu; na dhamiri zao, kwa kuwa dhaifu, hunajisika. [8]Lakini chakula hakituhudhurishi mbele za Mungu; maana, tusipokula hatupunguziwi kitu, wala tukila, hatuongezewi kitu. [9] Lakini angalieni huu uwezo wenu usije ukawakwaza wale walio dhaifu. [10] Kwa maana, mtu akikuona wewe uliye na ujuzi, umeketi chakulani ndani ya hekalu la sanamu, je! Dhamiri yake mtu huyo, kwa kuwa yu dhaifu, haitathibitika hata yeye naye ale vitu vilivyotolewa sadaka kwa sanamu? [11] Na yule aliye dhaifu aangamizwa kwa ujuzi wako, naye ni ndugu ambaye Kristo alikufa kwa ajili yake. [12] Hivyo, mkiwatenda dhambi ndugu zenu na kuitia jeraha dhamiri iliyo dhaifu, mnamtenda dhambi Kristo. [13] Kwa hiyo, chakula kikimkwaza ndugu yangu, hakika sitakula nyama hata milele, nisije nikamkwaza ndugu yangu.**

**8:7 "Bali ujuzi huu haimo ndani ya watu wote"** Katika mazingira haya hii inarejerea juu ya Mkristo "dhaifu" na "mwenye nguvu" (k.v. Rum. 14:1,2,14,22-23; 15:1). "dhaifu" katika mazingira haya inarejea juu ya ushirikina au uhalali unaohusu mambo ya nyuma ya mtu, maisha yasiyobadilika. Hii kwa ufupi ni kejeli inayorudi hadi kwa 1 Kor. 8:1 na majivuno ya makundi madogo madogo Fulani ya kanisa la Korintho na msisitizo wao juu ya hekima na ujuzi (k.v 1 Kor. 8:11)

◙ **"Na dhamiri zao, kwa kuwa dhaifu, hunajisika"** Waamini lazima watende katika mwanga tulionao (k.v Rum.14:23) hata pale ujuzi huu unapokuwa wa kitoto kiroho. Waamini wanawajibika tu kwa kile wanachokijua.

Paulo anatumia neno "dhamiri" mara zote katika nyaraka za Wakorintho (k.v. 1 Kor. 4:4; 8:7,10,12; 10:25,27,28,29; 2 Kor. 1:12; 4:2; 5:11). Inarejea kwenye maana ya ndani ya uadilifu kwa kila kilichosawa au kisicho sawa (k.v Mdo. 23:1). Kwa hiyo, kwenda kinyume na dhamiri zetu, hata kama ni makosa au udhaifu, linakuwa tatizo kubwa la imani.

Dhamiri ya mwamini inapaswa kuwa zaidi na zaidi kufanywa upya kwa neno la Mungu na Roho wa Mungu (k.v 1 Tim. 3:9). Mungu atawahukumu waamini kwa uelewa walionao (yaani., mdhaifu au mwenye nguvu). Lakini sisi sote tunatakiwa kuwa wazi kwenye biblia na Roho kwa uelewa mkubwa na kukua katika maarifa ya Bwana wetu Yesu Kristo. Angalia dokezo kamili juu ya "dhamiri" katika 1 Kor. 10:25. Angalia MADA MAALUM: UDHAIFU (SPECIAL TOPIC: WEAKNESS)

◙ **"Hunajisika"** Neno hili kiasili linarejea juu ya nguo zilizochafuka (k.v. Zak. 3:3-4; Yud. 23; Ufu. 3:4). Likajakuwa likitumika kitamathali kwa uchafu wa maadili (k.v Ufu. 14:4). Inashangaza kuona kuwa neno hili limechaguliwa kuelezea kile kinachotokea kwa mwamini aliye dhaifu ambaye huenda kinyume na mipaka ya imani yake. Mungu huangalia rohoni katika kila hali. Kuvunjika kwa uelewa wa ufahamu wetu wa imani, hata kama ni dhaifu au haufai, ni uvunjaji mkubwa wa imani.

**8:8 "Lakini hakikuhudhurishi mbele za Mungu"** Hii inaonyesha makosa ya kithiolojia, wote wale wanaodai uthibitisho au uhalalisho wa Kiyahudi, pia wale wanaothibitisha uhuru wa kimsingi. Ikiwa watakula au wasile, lakini itatuleta wote kukubalika mbele za Mungu (k.v. Rum. 14:14,23; Mark 7:18-23). Upendo wa Mungu umeelezewa katika upendo binafsi usio na kizuizi kwa ndugu zetu wengine na dada zetu katika Kristo ambao ni kiini cha amani na ukomavu ndani ya ushirika wa Mkristo.

◙ **"Kuamuliwa"** Angalia mada maalumu "kujaa tele" katika 1 Kor. 2:7

◙ **"Ikiwa……….kama"** kuna vifungu viwili VYENYE MASHARTI DARAJA LA TATU katika 1 Kor. 8:8, vinavyoonyesha tendo muhimu.

**8:9**
**NASB, NRSV "Lakini angalieni uwezo wenu usije ukawakwaza walio dhaifu"**
**NKJV "Lakini iweni waangalifu uwezo wenu usije ukawakwaza walio wadhaifu"**
**TEV "Kuwa mwangalifu usifanye uhuru wa matendo yenu kuwa kikwazo kwa walio dhaifu"**
**NJB "Iweni waangalifu kuwa uhuru wenu kwa namna yeyote usiwe kikwazo kwa wale walio dhaifu"**

Hii ni KAULI TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO, uhuru wa Mkristo (yaani., *exousia*, k.v. 1 Kor. 9:4,5,6,12,18) lazima udhibitiwe kwa upendo au unaweza kuwa kibali (k.v. 1 Kor. 10:23-33; 13:1-13; Rum. 14:1-15:13). Sisi ni waangalizi wa ndugu zetu!

Somo hili la uhuru wa Mkristo na uwajibikaji pia limejadiliwa katika Rum. 14:1-15:13. Angalia mtizamo wa kimktadha wa fasiri yangu juu ya Warumi, sura ya 14 na 15 katika 1 Kor. 6:12.

**8:10 "ikiwa"** Hii ni SENTENSI NYINGINE YENYE MASHARTI DARAJA LA TATU, inayomaanisha juu ya tendo muhimu. Sarufi ya 1 Kor. 8:10 inatarajia jibu la "ndiyo"

**NASB, NKJV "Kwa maana, mtu akikuona wewe uliye na ujuzi, umeketi chakulani ndani la hekalu la sanamu"**
**NRSV "Kwa maana wengine wakikuona wewe uliye na ujuzi, umeketi chakulani ndani la hekalu la sanamu"**
**TEV "Ikiwa mtu mwenye dhamiri iliyo dhaifu akauona wewe mwenye ujuzi, ukila ndani ya hekalu la samau"**
**NJB "ikiwa mtu akauona wewe mwenye ujuzi, umeketi chakulani ndani ya hekalu la miungu wa uongo"**

Kifungu hiki kimetafsiriwa kiutata katika tolea la NASB na NKJV. Kinahau, tafsiri ya mlinganyo wa nguvu wa toleo la TEV na NJB umekamata usikivu. Ujuzi ambao Paulo anaurejerea kwao unarejea mpaka 1 Kor. 8:1-4. Waamini wenye nguvu wanajua kuwa kuna Mungu mmoja (k.v 1 Kor. 8:4). Waumini walio wadhaifu wanaathiriwa na mambo yaliyopita. Waamini wenye nguvu wanawainamia ili kwamba wasiwakwaze kaka au dada zao katika Kristo au watakatifu waaminifu (k.v 1 Kor. 8:1)

Nguvu za kweli za kiroho haziko kwenye ujuzi tu, lakini katika matendo ya upendo dhidi ya waamini wengine, hata wale waliodhaifu, walio washirikina, wenye kushika sheria sana, walio wachanga!

◙ **"Wakila kwenye nyumba ya sanamu"** Angalia ukumbusho katika 1 Kor. 10:14-22

**NASB "Hata mkathibitika"**
**NKJV "Hata mkathibitika kula"**
**NRSV "Hata mkafikia hatua ya kula"**
**TEV "Haitamshawishi hata yeye kula"**
**NJB "Atashawishika kula"**

Hili ni neno la "kujenga'au kuimarisha."Katika mstari huu linatumika hasa

1. Kwa maana ya kejeli kuhusu ushawishi wa uharibifu juu ya matendo ya ndugu mwenye nguvu
2. Yumkini nukuu toka barua ya Korintho inayohusianishwa kwa namna ya kuwasaidia waliodhaifu katika imani.

**8:11**
**NASB "Na yule aliye dhaifu aangamizwa kwa ujuzi wako, naye ni ndugu ambaye Kristo alikufa kwa ajili yake"**
**NKJV "Kwa sababu ya ujuzi wako aliye dhaifu aangamizwa, naye ni ndugu ambaye Kristo alikufa kwa ajili yake"**
**NRSV "Kwa hiyo kwa maarifa yako, yeye mwamini aliye dhaifu ambaye Kristo alikufa kwa ajili yake ataangamia"**
**TEV "Kwa hiyo yeye aliye dhaifu, ndugu yako ambaye Kristo alikufa kwa ajili yake, ataangamia kwa ujuzi wako"**
**NJB "Kutokana na ujuzi wako ambao huyu ndugu Kristo aliye kufa kwa ajili yake, yeye aliye dhaifu, atapotea"**

Mpango wa sentensi ya Kiyunani unasisitiza juu ya neno "wenu" (yaani ujuzi wa juu ulionao). Ikiwa uhuru wa Mkristo unapoharibu uhuru wa mwingine, uhuru huo unakuwa ni angamizo kubwa (k.v Rum. 14:15,20)

Hii ni hoja ya kejeli kama ile ya 1 Kor. 8:10. Kanisa la Korintho lilijivuna juu ya ujuzi wake (8:1). Hapa Paulo anaonyesha kuwa ujuzi waweza kuwa maangamizo. Siku zote Paulo anaonya ndugu "mwenye nguvu"kuwa mtulivu na kuhusika kwa yule "aliye mdhaifu" kwa ajili ya pendo la Kristo kwa wote.

Neno "angamizwa" "potea" au "haribiwa"lazima yote yatafsiriwe katika uelewa wa Rum. 14:22-23, pale yanapomaanisha "kusababisha mtu kutenda dhambi" ambao ni mfanano wa matumizi ya neno hilo hapo. Huu sio uharibifu ulio dhahiri, lakini ni wa muda, usio na uzito wa kurudisha makuzi ya kiroho.

**[MADA MAALUM: MAANGAMIZO (*APOLLUM)* (SPECIAL TOPIC: DESTRUCTION *(APOLLUMI)*]()**

**8:12 "Mkiwatenda dhambi ndugu zenu…….mnamtenda dhambi Kristo"** Haya ni maelezo yenye nguvu. Upendo wetu kwa Mungu unaonekana kwenye upendo wetu wa kupendana sisi kwa sisi. Mara nyingi katika Agano Jipya, matendo ya watu yaliyo kinyume na waamini yanaonekana kama matendo yaliyo kinyume na Kristo (k.v Mdo. 9:4,5) na matendo ya watu kwa waaminio yanaonekana ni kama matendo kwa Kristo (k.v Mt. 25:40,45)

**8:13 "ikiwa"** Hii ni SENTENSI YENYE MASHARTI DARAJA LA KWANZA. Suala la chakula lilisababisha baadhi ya waaminio kwenda kinyume na matarajio ya imani yao binafsi.

◙ **"Kujikwaza"** Hili ni neno la Kiyunani lililotumika kwa ajili ya kuwatega wanyama. Kiuhalisia linarejea juu ya "mti utumikao kunasia wanyama"

◙ **"Hakika sintakula nyama hata milele"** Kifungu hiki kina muundo HASI ulio na nguvu mara tatu (k.v Rum. 14:21). Uhuru katika Kristo lazima ujenge, na sio uharibu. Kidokezo ambacho hakijaelezewa ni kwamba Paulo hatakula nyama zilizotolewa kwa sanamu au hekaluni penye sanamu. Hii haimanishi kuwa Paulo amekuwa mtu asiyekula nyama.

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujisomea wa fasiri, ambao unamaanisha kwamba unao wajibu wa tafsiri yako mwenyewe ya Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika nuru tuliyo nayo. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hupaswi kumuachia vitu hivi mfasiri.

Maswali haya ya majadiliano yanatoa tu, msaada wa wewe kufikiria kupitia masuala nyeti ya sehemu ya kitabu hiki. Yamekusudiwa kukuchokonoa mawazo na sio kutoa maana ya mwisho.

1. Ni dhahiri kuwa tatizo hili hasa sio la wakati ule ule. Hata hivyo, kanuni ya wote hapa ni muhimu. Elezea kanuni hiyo kwa maneno yako.
2. Ni kwa vipi mtu anahusishwa na shughuli za kimapepo kwenye ulimwengu wa kidini katika siku zetu za leo
3. Kama kuna Mungu mmoja, ni kwa vipi Yesu awe wa ki-Ungu?
4. Elezea juu ya uhuru wa Mkristo dhidi ya wajibu wa Mkristo
5. Je ni lazima waamini wote wasile nyama?

# 1 WAKORINTHO 9

| MGAWANYO WA AYA WA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| UBS[4] | NKSV | NRSV | TEV | NJB |
| | | | | Chakula kitolewacho Kwa miungu wa uongo |
| Haki za Mtume | Kielezo cha kujikana | habari za Paulo Kama Mtume | Habari na shughuli za Mtume | Paulo anaomba kwa ajili ya mfano wake |
| 9:1-2 | 9:1-18 | 9:1-2 | 9:1-2 | 9:1-14 |
| 9:3-12a | - | 9:3-7 | 9:3-7 | - |
| - | - | 9:8-12a | 9:8-12a | - |
| 9:12b | - | 9:12b | 9:12b-14 | - |
| | | Paulo yuko huru Kusamehe haki Zake za Kitume | | |
| | Kuokoa watu wote | 9:15-18 | 9:15-18 | 9:15-18 |
| 9:19-23 | 9:19-23 | 9:19-23 | 9:19-22 | 9:19-23 |
| - | Kupambana ili Kupata taji | - | 9:23-27 | - |
| 9:24-27 | 9:24-27 | 9:24-27 | - | 9:24-27 |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (Kutoka **"Mwongozo wa Usomaji Mzuri wa Biblia") ("A Guide to Good Bible Reading")**

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo wa usomaji wa fasiri, Ikiwa na maana kwamba unawajibika kwa ukalimani wako wa biblia mwenyewe. Kila mmoja wetu sharti atembee katika nuru tuliyonayo.Wewe, Biblia na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika kutafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua somo. Linganisha mgawanyo wa somo lako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika kiaya sio uvuvio, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la asili la mwandishi ambalo ndilo kiini cha ukalimani. Kila aya ina somo moja na somo ni moja tu.

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA KWA 9:1-27

A. Sura hii ina uhusiano na sura ya nane katika dhana ya kutafuta uwiano kati ya haki za Mkristo na wajibu katika upendo (kama vile Rum. 14:1- 15:13 na 1 Kor. 8:1-11 na 13:1-13)
B. Ni dhahiri kutoka katika muktadha huu kwamba uongozi wa Paulo ulishambuliwa na baadhi ya kundi ama makundi ndani ya Kanisa pale Korintho.
    1. Wale wenye ufasaha wa kusema waliwafundisha walimu wa Kiyahudi waliokuwa wakisafiri huku na kule
    2. Upokeaji wa mafunuo ya uongo.
C. Kuna aina ya VIWAKILISHI NOMINO vya kibinafsi (na miundo ya VITENZI) vilivyotumika kwenye sura hii
    1. MTU WA KWANZA HALI YA UMOJA, katika 1 Kor. 9:1-3,6,8,15-23,26-27
    2. MTU WA KWANZA HALI YA UWINGI katika 1 Kor. 9:45,10-11,25
        a. Kwa kuwa Barbaba ametajwa hasa katika 1 Kor. 9:6 yeye labda ndiye anapaswa kudhaniwa katika 1 Kor.9:4-5
        b. Katika 1 Kor. 9:10-11 Paulo aonekana kumhusisha Apollo na yawezekana wakawa wahubiri wengine waliokuwa wanakuja kutembelea hata Petro
        c. Mara nyingi Paulo alitumia wingi wa neno "sisi" wa uhariri kusema kumhusu yeye mwenyewe.
    3. MTU WA PILI HALI YA UWINGI, katika 1 Kor. 9:(3) 24 yahusu Wakoritho wanaodai "kujaa" elimu ya mambo ya Mungu.
    4. Matumizi ya Paulo ya VIWAKILISHI NOMINO ambavyo ni vigumu na vyenye sifa mbaya na chanzo cha machapisho mengi ya kinyume yaliyo tofauti.

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 1 WAKORINTHO 9:1-2**
**[1]Je! Mimi si huru? Mimi si mtume? Mimi sikumwona Yesu Bwana wetu? Ninyi si kazi yangu katika Bwana? [2]Kwa maana ikiwa mimi si mtume kwa wengine, lakini ni mtume kwenu ninyi; kwa maana ninyi ndinyi muhuri ya utume wangu katika Bwana.**

**9:1** "**Je Mimi si huru**" kuna mfululizo wa maswali katika muktadha huu.Toleo la UBS4 lina maswali kumi na nne, NASB lina kumi na sita, NKJV lina kumi na tano, NRSV lina kumi na sita, TEV lina kumi na nne, NJB lina kumi na mbili. Hakuna uhakika kama hizi ni taarifa ama maswali (kama vile Ellingwoeth and Halton, *A Hand book on Pauls first letter to the Counthearis*, uk.193). Maswali katika 1 Kor. 9:1-2 yote yanatarajia jibu la "ndiyo." Maswali katika 1 Kor. 9:6,7,10 na 11 yameandaliwa ili yatarajie jibu la "hapana".

Hili ni tumizi la neno "huru" kwenye dhana ya uhuru wa kiroho katika Kristo (kama vile 1 Kor. 9:19;10:29). Siyo uhuru kutoka kwa Warumi (yaani, haki za kisiasa). Katika Kristo aaminiye, sasa anakaliwa na Roho moyoni, sasa anaarifiwa na Injili, ana uhuru "kutoka" nguvu "binafsi iliyoanguka" ya mimi kwanza toka mwanzo 3 imeondolewa na kufidiwa na wengine kwanza "uhuru ulio ndani ya Injili" siyo "uhuru ku………."lakini "uhuru kutoku……"! uko tofauti na uhuru wa kisiasa ambao hasa ni lile tunda la ujuzi wa mema na mabaya. Mwanadamu aliyeanguka hawezi kuukamata "uhuru"! Hata waaminio walio wachanga hawawezi.

◙"**Je sijamuona Yesu Bwana wetu?** Hii ni KAULI TIMILIFU TENDAJI YENYE KUARIFU inayomanisha kwamba kitendo kilichopita kimetokea kwenye hali ya wakati uliopo. Utume wa Paulo ulikuwa unashambuliwa kwa sababu yeye hakuwa mmoja miongoni mwa wale kumi na wawili wa kwanza. Sifa ya mtume ilikuwa kwamba mtu ilimbidi awe aliyekuwa na Yesu wakati wa uhai wake hapa duniani na aliyekuwa amemwona alipofufuka (kama vile Mdo. 1:15-26). Paulo anatetea kwamba alikuwa amemwona Kristo aliyefufuka (kama vile Mdo. 9:3,17,27:22:14, 1 Kor. 15:8. Wito wa Paulo ulikuwa kitendo mahsusi cha Kristo juu ya ujumbe maalum kwa mataifa, uliohitaji ufunuo maalum (kama vile Mdo. 18:9:23:11). Paulo si kwamba alikutana na Yesu ana kwa ana akiwa barabarani akielekea Dameski, bali mara nyingi wakati wa huduma yake Yesu, au malaika kama mwakilishi wa Yesu, na alionekana kwake na kumtia nguvu (kama vile Mdo. 18:9-11; 22:17-21), katika Mdo. 27:23.

◙ "**Ninyi si kazi yangu katika Bwana**" Ushuhuda wa utume wa Paulo ni ule wa wingi wa Makanisa aliyoyaangusha ambayo Korintho lilikuwa mojawapo (kama vile 1 Kor. 4:15; 2 Kor. 3:1-3)

**9:2** "**Ikiwa**" Hii ni SENTENSI YENYE MASHARTI DARAJA LA KWANZA, inayoonyesha kwamba mamlaka ilikataliwa na vikundi vingi makanisani katika kanisa la awali (kama vile Matendo 15 na Wagalatia)

◙ "**Kwa maana ninyi ndinyi muhuri ya utume wangu katika Bwana**" Muhuri katika ulimwengu wa kale ulikuwa tone au bonge la nta la joto ambalo pete ya muhuri iligandamizwa kutia muhuri barua au mzigo/furushi la vitu ili kuthibitisha kwamba kilichomo ndani ya furushi hakijafunguliwa; ulionyesha nani alimiliki furushi/mzigo; na ilionyesha kiuhalisia kuwa kilichokuwa ndani ya furushi kilikuwa limetumwa na mtu sahihi/stahiki. Mfano huu wa muhuri ukawa sitiani ya uhakika wa mkristo (kama vile Yoh. 3:33; Rum. 4:11)

MADA MAALUMU: MUHURI (SPECIAL TOPIC: SEAL)

**ANDKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 1 WAKORINTHO 9:3-7**
**3 Hilo ndilo jawabu langu kwa wale wanaoniuliza. 4 Je! Hatuna uwezo wa kula na kunywa? 5 Hatuna uwezo kuchukua pamoja nasi mke aliye ndugu, kama wao mitume wengine, na ndugu wa Bwana, na Kefa? 6 Au je! Ni mimi peke yangu na Barnaba tusio na uwezo wa kutokufanya kazi? 7 Ni askari gani aendaye vitani wakati wo wote kwa gharama zake mwenyewe? Ni nani apandaye mizabibu asiyekula katika matunda yake? Au ni nani achungaye kundi, asiyekunywa katika maziwa ya kundi?.**

**9:3** "**Jawabu langu**" Neno hili (yaani, *apologia*) lilitumika kwa "utetezi wa kisheria" (kama vile Mdo. 19:33; 22:1; 25:16; Flp. 1:7, 17; 1 Pet 3:15) kisintaksi 1 Kor. 9:3 inaweza kwenda pamoja na 1 Kor. 9:4 Biblia ya USB4 , NRSV, NA TEV inaonyesha kwenda pamoja na 1 Kor. 9:4 wakati toleo la NKJV na NJB hazivunji ubora kwenye sehemu yo yote kati ya mbili.

◙"**Kwa wale wanaoniuliza**" Paulo alikuwa anatafutiwa makosa na makundi kadhaa ama vikundi vya kanisa pale Korintho (kama vile 1 Kor. 2:15; 4:3) walikuwa wanadai

1. Kwamba hakuwa mtume wa kweli
2. Kwamba alibadili ujumbe wa mtume huko Yerusalemu
3. Kwamba alihubiri ili alipwe pesa

Tuhuma hizi hazitamkwi waziwazi bali zinachukuliwa kutokana na mpangilio wa kihistoria na maswala ambayo Paulo alichagua kuyazungumzia.

**9:4** Hili linaanzisha mlolongo wa maswali (kama vile 1 Kor. 9:4) pale ambapo Paulo anadai haki yake kama mtume ili apewe msaada na makanisa ya mahali. Hata hivyo yeye binafsi alichagua kutotumia haki yake (kama vile 1 Kor. 9:15, 18; 1 The. 2:6) lakini anathibitisha haki ya watenda kazi wengine wa Kristo.

**9:5** "**kuchukua pamoja nasi mke aliye ndugu, kama wao mitume wengine**" Muktadha hautetei moja kwa moja haki ya mitume kuwa na wake, ingawa hili kwa uhakika linadokeza, lakini haki ya mitume ni kanisa kuwasaidia na wake zao.

Neno "mitume" linarejea juu ya wale thenashara ama matumizi kwa upana wa neno (kama vile Mdo. 14:4, 14, Rum. 16:6-7; 1 Kor. 4:9; Gal 1:9; Efe. 4:11, Flp. 2:25; 1 The. 2:6. Kwa kuwa Petro ametajwa kitofauti, kundi la baadaye linalodokezwa. Inawezekana pia kwamba kundi (yaani mojawapo ya vikundi vilivyojigawa) kanisani humu vilikuwa vinainua utume wa Petro (kama vile 1 Kor. 1:12; 3:22)

**NASB, NKJV,**
**NRSV, NIV"mke aaminiye"**
**TEV, NJB,**
**NEB"mke wa Kikristo"**

Katika Kiyunani kuna jozi ya NOMINO mara mbili, “dada, mke” ambayo yalikuwa ni ya kinahau kwa “mke aaminiye”

Tatizo la kihistoria ni kwa jinsi gani limehusishwa kwa

1. Wanawake walioambatana na Yesu na kundi la Kitume na wakawasaidia (kama vile Mt. 27:55; Mk. 15:40-41)
2. Mwanamke aliyejadiliwa katika 1 Kor. 7:36-38 (yaani, dada ama mshirika bikira ama mchumba wa kike
3. Huduma ya wake wa viongozi wa kanisa inayofanana na mashemasi wanawake wa Rum.16:1 ama :wajibu wa wajane” wa kichungaji (kama vile 1 Tim. 3:11; 5:9-10)

Kusaidia mitume wote kumi na wawili wa awali waliokuwa wameoa kwa sababu useja miongoni mwa Wayahudi ilikuwa adimu sana. Wayahudi walioa kwa sababu ya amri katika Mwa. 1:28; 9:1,7.

◙ “**kama wao mitume wengine**” Neno “mtume” lina vidokezo kadhaa katika Agano Jipya

1. Wale walioitwa na Yesu na wakamfuata wakati wa uhai wake duniani
2. Paulo aliitwa katika maono maalum njiani akienda Damaski
3. Karama inayoendelea kuwapo kanisani (kama vile Efe. 4:11) ambayo ilihusu watu kadhaa

Suala la kimaandiko hapa ni kuwa tunaafiki lipi juu ya orodha ya Paulo.

1. Mitume waliobaki
2. Ndugu zake Bwana
3. Kefa
4. Barnaba na Sauli

◙ “**Ndugu wa Bwana**” Jerome (mwaka 346-420 B.K) waliamini kuwa walikuwa binamu zake Yesu; Epiphanius ( 310-403 b.k) alisema walikuwa watoto kutoka kwenye ndoa ya Yusufu ya awali. Tafsiri zote mbili ni dhahiri zinahusu dhanio linaloendelea la wakatoliki wa Roma kuhusu mariamu na sio kutoka Agano Jipya (kama vile Mt. 12:26; 13:55; Marko. 6:3; Yoh. 2:12; 7:3, 5, 10; Mdo.1:14; Gal. 1:19. Haimaanishi kwamba nusu ndugu wa Yesu waliokuwa watendaji kanisani walitazamia uongozi, katika hali halisi mmoja wa waliokuwa na uhusiano na Yesu alikuwa kiongozi wa kanisa la Yerusalemu kwa vizazi kadhaa kipindi cha karne ya kwanza kuanzia Yakobo.

◙ “**Kefa**” Huu ni muundo wa Kiaramu wa Petro ambao ni Kiyunani uliomaanisha jabali kubwa au mwamba (kama vile Mt. 8:14; Yoh. 1:42 Kefa alikuwa na ndoa (kama vile Marko. 1:30) Paulo humwita Petro “Kefa” katika 1 Kor. 1:12; 3:22; 9:5; 15:5 Gal. 1:18, 2; 9 lakini katika Gal. 2:7, 8,11, 14 anamwita Petro. Yaonekana kutokuwapo na utofauti wa kithiolojia, yumkini kwenye aina tofauti za kifasihi. Amemwita Petro kila mahali kwenye injili zote isipokuwa Yoh. 1:42. Inapendeza kwamba kanisa limefanya uhusiano kati ya Petro (yaani, *Petros*) na “mwamba huu” (yaani, *Petra*) katika Mt. 16:18. Yesu alizungumza Kiaramu na hapakuwepo na tofauti yo yote kati ya maneno mawili haya katika lugha.

**9:6** “**Barnaba**” Barnaba pia anaitwa mtume, inayoonyesha matumizi mapana zaidi ya neno (kama vile Efe. 4:11) kuliko wale kumi na wawili wa kwanza (kama vile Mdo.14:14, 18:15)

## MADA MAALUM: BARNABA (SPECIAL TOPIC: BARNABAS)

**NASB"Wasio na uwezo wa kutokufanya kazi"**
**NKJV"Wale wasio na uwezo wa kutokufanya kazi**
**NRSV"Wale wasio na uwezo wa kutokufanya kazi kwa ajili ya maisha"**
**TEV"Wale pekee wafanyao kwa ajili ya maisha yetu"**
**NJB"wao pekee wasiokuwa na haki ya kufanya kazi"**

Walimu wa sheria ya Kiyahudi walitetea heshima ya kazi za mikono. Walimu wa sheria ya Kiyahudi walilazimika kuwa na kazi nje ya huduma ya kanisa kwa sababu ilichukuliwa kwamba ni dhambi kupewa malipo kwa kufundisha kweli za YWHH (kama vile Pirke Abot 1:13; 4:7). Paulo alichagua kuacha kuchukua fursa ya haki yake kama mhubiri wa injili (1 Kor. 9:18), yawezekana kwa sababu ya (1) urithi wake wa Kiyahudi ama (2) mashambulizi ya wale waliodai kwamba aliwadai watu wamlipe fedha (kama vile Mdo. 20:33; 2 Kor. 11:7-12; 12:14-18).

**9:7-14** Katika aya hizi ziko mifano kadhaa kutoka katika maisha ya kila siku, imetumiwa kama mifano kuonyesha uhalali wa watenda kazi wa injili kupata malipo kutoka kwenye makanisa walipotumikia (kama vile Rum 15:27) (1)askari, mst.7; (2) shamba la mizabibu, 1 Kor. 9:7; (3) mchungaji, 1 Kor. 9:7; (4) maksai, 1 Kor. 9:9; (5) mkokotaji wa jembe na mpuraji, 1 Kor. 9:10; (6) mpanzi, 1 Kor. 9:11; na (7) kuhani, 1 Kor. 9:13.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 1 WAKORINTHO 9:8-14**

[8]**Je! Ninanena hayo kwa kibinadamu? Au torati nayo haisemi yayo hayo?** [9] **Kwa maana katika torati ya Musa imeandikwa, Usimfunge kinywa ng'ombe apurapo nafaka. Je! Hapo Mungu aangalia mambo ya ng'ombe?** [10] **Au yamkini anena hayo kwa ajili yetu? Naam, yaliandikwa kwa ajili yetu; kwa kuwa alimaye nafaka ni haki yake kulima kwa matumaini, naye apuraye nafaka ni haki yake kutumaini kupata sehemu yake.** [11] **Ikiwa sisi tuliwapandia ninyi vitu vya rohoni, je! Ni neno kubwa tukivuna vitu vyenu vya mwilini?** [12] **Ikiwa wengine wanashiriki uwezo huu juu yenu, sisi si zaidi? Lakini hatukuutumia uwezo huo; bali twayavumilia mambo yote tusije tukaizuia Habari Njema ya Kristo.** [13] **Hamjui ya kuwa wale wazifanyao kazi za hekaluni hula katika vitu vya hekalu, na wale waihudumiao madhabahu huwa na fungu lao katika vitu vya madhabahu?** [1]4 **Na Bwana vivyo hivyo ameamuru kwamba wale waihubirio Injili wapate riziki kwa hiyo Injili.**

**9:8**
**NASB"kulingana na hukumu ya kibinadamu"**
**NKJV"kama mtu tu"**
**NRSV"kwa mamlaka ya kibinadamu"**
**TEV"kujiwekea mipaka katika mifano hii ya kila siku"**
**NJB"hekima ya ulimwengu tu"**

Andiko la Kiyunani lina neno "si kufuatana na mwanadamu" (yaani, *anthrōpos*, ambayo inarejelea kwa wanadamu). Paulo hutumia hii misemo inayofuatana mara kadhaa (kama vile 1 Kor. 3:3; 9:8; 15:32; Rum. 3:5; Gal. 1:11; 3:15).

Ilikuwa njia ya kimbinu ya kulinganisha njia za kibinadamu za duniani na zake mpya zilizotokana na uongozi wa Roho (yaani, mafundisho ya Yesu ama utambuzi wa Roho wa kufasiri na kutenda).

**9:9** "**Kwa maana katika torati ya Musa imeandikwa**" Njia ya Wayahudi ya kusuluhisha swali ilikuwa na nukuu yenye mamlaka, ikiwezekana kutoka kwenye maandiko ya Musa (yaani, Mwanzo – Kutoka) kwa hiyo Paulo ananukuu kumbukumbu 25:4 (kama vile 1 Tim. 5:18)

**MADA MAALUM: MAONI YA PAULO JUU YA SHERIA ZA MUSA (SPECIAL TOPIC: PAUL'S VIEWS OF THE MOSAIC LAW)**

◙ "**Usimfunge kinywa ng'ombe**" Hii ni nukuu kutoka maandiko ya kale ya Kiyunani ya Kumbukumbu 25:4. Neno "usimfunga kinywa" ni *phimōsies,* ambalo linatokea katika miswada ya Kiyunani $P^{46}$, א, A, $B^3$, C, $D^{b,c}$, K, L, P, na sehemu kubwa ya herufi za kiwango cha chini. Huu pia ndo neno lililotumiwa kwenye nukuu ya maandiko hayo hayo katika 1 Tim.5:18. Hata hivyo waandishi wa toleo la Biblia ya $UBS^4$ walichagua neno mbadala *kēmō*seis*,* ambalo linamaanisha usimfunge kinywa linalopatikana katika MSS B $D^*$, F, na G. kufikiri kwao kulikuwa kwamba neno lililotumika kwa uchache (yawezekana ni lugha ya mtaani) yumkini likawa la asili kwa sababu lile lingine lilitazamiwa kutoka kwenye maandiko ya kale ya Kiyunani na nukuu katika 1 Timotheo huenda ndo ikawa sababu waandishi wakalibadili neno hili? Neno lililochaguliwa kama la asili halisababishi tofauti yo yote ya kitafsiri bali linaelezea kwa kielelezo cha kanuni za ki-maandiko ambazo kwazo wachambuzi wa maandiko hutathmini miswada ya ya lugha ya Koine, huko Uyunani katika kujaribu kurejeza uandishi wa asili wa mwandiko binafsi.

**MADA MAALUM: SHUTUMA ZA KIMAANDIKO (SPECIAL TOPIC: TEXTUAL CRITICISM)**

**NASB "Mungu ahusiani na ng'ombe, ni Yeye"**
**NKJV "Ni ng'ombe ambao Mungu anahusika nao"**

**NRSV ”Ni kuhusu nng’ombe Mungu anahusika”**
**TEV ”Sasa Mungu anahusika na ng’ombe”**
**NJB ”Ni habari ya ng’ombe ambayo Mungu anahusika nayo”**

Aya ya 9 na 10 zinaonyesha jinsi maandiko ya Agano la kale yalivyofafanuliwa (yaani, kuongeza umuhimu au matumizi) kutimiza mahitaji ya siku mpya (kama vile Rum. 4:23-24;15:4; 1 Kor. 9:10; 10:6,11). Agano la kale lilionyesha wazi kuwajali wanyama (kama vile Kut. 21:33,35; 27:10-13; 23:5,12; Kum. 5:14; 22:4). Yesu anadokeza kuhusu kujali wanyama (kama vile Luka. 13:15; 14:5, pale anapotumia kanuni za kisheria za Kiyahudi za “nyepesi na nzito.” Hii haimaanishi kwamba Mungu hajali mambo ya wanyama, bali pia huwajali watu wake, na kwenye muktadha huu, pia watenda kazi wa injili (kama vile 1 Tim. 5:18). Hii inafanana na Mt. 6:26-34. Yesu hutumia utoaji wa Mungu katika hali ya asili kama njia ya kuonyesha utoaji wa Mungu kwa binadamu aliyemfanya kwa mfano wake, huu ulikuwa mfano wa mbinu za ualimu wa sheria ya Kiyahudi uliojulikana kama “hali ya udogo hadi ukubwa” ama “chepesi na kizito” ambao ulikuwa mfano mmojawapo ya kanuni za Hillel’s (kama vile Aboth. De Rab. Nathan XXXVII and Tosefta Sanhedrin c. 7). Kumbuka, Gamaliel alikuwa mwalimu wa sharia ya kiyahudi (Kama vile Mdo. 5:34; 22:3). Angalia kiambatanisho namba tatu (mafundisho ya kanuni za ufasiri za sharia ya Kiyahudi) katika Kiebrania katika **www.freebiblecommentary.org.**

**9:10**
**NASB"Ama ananena jumbe kwa ajili yetu? Ndiyo, kwa niaba yetu iliandikwa"**
**NKJV"Ama anasema yote kwa ajili yetu?, bila mashaka hili limeandikwa"**
**NRSV"Ama anasema hasa kwa niaba yetu? Ilikuwa haswa imeandikwa kwa ajili yetu"**
**TEV"Haimaanishi kwa uhakika sisi aliposema hivyo? Bila shaka hayo yalikuwa yameandikwa kwa ajili yetu"**
**NJB"Ama haikuandikwa haswa kwa ajili yetu? Ni dhahiri iliandikwa kwa ajili yetu**"

Mara kadhaa Paulo anathibitisha Agano la kale liliandikwa kama mfano kwa ajili ya waamini wa Agano Jipya (kama vile Rum. 4:23-24; 15:4; 1 Kor. 9:10; 10:6,11). Mafunzo ya Paulo juu ya sheria ya Kiyunani yalikuwa ni kumfundisha kuzitumia sheria katika mazingira ya nyakati husika za sasa. Hapa anatumia mjadala unaoitwa “nyepesi na nzito” au “ndogo zaidi kuelekea kubwa zaidi” Kwenye muktadha wa Kumbukumbu 25:4 matumizi haya yanakuwa hayajulikani yasiyo ya lazima swali la tafsiri ya maandiko ni “Je! Paulo alikuwa anatumia kusudi la asili la mwandishi aliyevuviwa? Jawabu ni wazi hapana! Lakini anatumia matumizi halali ya kanuni? Paulo amevuviwa! Anaona ukweli kwenye kiwango ambacho sisi hatuwezi kuona. Kwa hali yo yote sisi hatutavuviwa bali tumeangaziwa na Roho. Watafsiri wa kisasa hawawezi kutengeneza upya mtindo wa tafsiri ya waandishi wa Agano Jipya. Kwa hiyo ni vizuri kuwaacha waseme, lakini tujizuie wenyewe kwenye mtazamo wa sarufi ya kihistoria ambao unatafuta kusudi la mwandishi wa asili kwa maana iliyokusudiwa lakini ukiruhusu matumizi mengi yanayokaribiana na kusudi la asili.Angalia mada maalum: Nuru na Uvuvio, kwenye Mwanzo wa 1 Wakorintho 2

**9:11** “**Ikiwa, ikiwa**” Zote mbili ni SENTENSI ZENYE MASHARTI ZA DARAJA LA KWANZA ambazo zimechukuliwa kuwa ni kweli kwa mtazamo wa mwandishi ama kwa makusudi yake ya fasihi. Swali halisi ni akina nani wengine waliodai haki ya kupata msaada katika Kanisa la Korintho? Je walikuwa walimu wa uongo waliokuwa wakisafiri ama wale waliokuwa sehemu ya uongozi wa kanisa la mahali, labda inahusu viongozi wa pale kanisani ambao hawakuruhusu kanisa kuwasaidia (kama vile tafsiri ya J. B. Phillips).

◙ "**alipanda. . .vuna**" Utaratibu wa kilimo wa Agano la kale unakuwa kanuni ya Kiroho (kama vile Ayu. 4:8; Mith. 22:8; Hos. 8:7; Hagai. 1:6; Yoh 4:37; 1 Kor. 9:11; 2 Kor. 9:6,10; Gal. 6:7-9).

◙**“vitu vya mwili**” Katika maana halisi neno *ta sarkika,* linamaanisha “vitu vya mwilini”, lakini sio kwa maana ya kutenda dhambi, bali kwa maana ya mwili kama vile ambavyo binadamu anahitaji ili naweze kuishi (yaani maji, chakula, nyumba, mavazi nk (kama vile Rum. 15:27)

9:12 "**ikiwa**" Hii ni SENTENSI nyingine YENYE MASHARTI DARAJA LA KWANZA. Viongozi wengine walikuwa wanadai haki (yaani, *exousia*) kufidiwa vitu vya kimwili.

◙ "**Sisi si zaidi**"? Hiki ni kidokezo kwenye ukweli kwamba Paulo alianzisha kanisa. Alikuwa baba yao wa imani (kama vile 1 Kor. 4:15) sasa walikuwa wanakana haki yake ya kiroho (1 Kor. 9:11, 14; Rum.15:27). Lakini wakiwaruhusu wengine kudai kufidiwa.

◙ "**bali twayavumilia mambo yote**" Hii ni sitiari ya matumizi ya neno la Kiyunani "paa" likimaanisha "kufunika", "kuficha", au "kuvumilia" (kama vile 1 Kor. 13:7)

◙ "**kizuizi"** Hili lilikuwa neno zito la kivita, neno hili lilitumika kwa kuvunja barabara ili kuzuia adui asilitumie

◙ "**habari njema ya Kristo**" Neno injili katika maana halisi "habari njema" linahusisha vipengele kadhaa

1. Habari za kwanza mbaya za dhambi na uasi wa mwanadamu
2. Mwaliko wa wazi kwa ye yote ama wote kukubali utoaji wa Mungu kwa toba na imani.

Habari njema kuhusu Yesu zinahusu vipengele vitatu

1. Ni mtu wa kukaribisha (yaani, Yesu)
2. Ni ukweli kuhusu mtu huyo kumwamini (yaani Agano Jipya)
3. Ni maisha ambayo yanamfanana mtu huyo (yaani, maisha mfano wa maisha ya Kristo)

Ikiwa mojawapo kati ya vipengele hivi vitatu kimedharauliwa basi injili imeharibiwa.

**9:13** "**wale wazifanyao kazi za hekaluni hula katika vitu vya hekalu**" Hii inahusu makuhani wa Agano la kale na Walawi (kama vile Law. 7:6,8-10,14,28-36; Kum. 18:1). Paulo alitumia neno lililotumiwa katika maandiko ya kale ya Kiyunani kwa kazi ya kikuhani (kama vile Hes. 3:7; 8:15) kama vile kazi kwa jumla (kama vile Mwa. 2:5,15; 3:23; 4:2,12; 29:27). Paulo aliona huduma yake ya injili kama huduma ya kikuhani (kama vile Rum. 15:16)

**9:14** "**Na Bwana vivyo hivyo ameamuru**" Hii lazima ihusu maneno ya Yesu katika Mt. 10:10 na Lk. 10:7. Paulo kila wakati alijaribu kurejelea kwenye mafundisho ya Yesu kuhusu somo lililorejerewa.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 1 WAKORINTHO 9:15-18**

[15] **Lakini mimi sikutumia mambo hayo hata moja. Wala siyaandiki hayo ili iwe hivyo kwangu mimi; maana ni heri nife kuliko mtu awaye yote abatilishe huku kujisifu kwangu.** [16] **Maana, ijapokuwa naihubiri Injili, sina la kujisifia; maana nimewekewa sharti; tena ole wangu nisipoihubiri Injili!** [17] **Maana nikiitenda kazi hii kwa hiari yangu nina thawabu; ila ikiwa si kwa hiari yangu, nimeaminiwa uwakili.** [18] **Basi thawabu yangu ni nini? Ni hii, ya kuwa nihubiripo, nitaitoa Injili bila gharama, bila kutumia kwa utimilifu uwezo wangu nilio nao katika Injili.**

**9:15** "**Lakini mimi sikutumia mambo hayo hata moja**" Hii ni KAULI YA KATI TIMILIFU YENYE KUARIFU. Paulo hakupokea fidia kutoka Korintho, huenda kwa sababu kulikuwepo mle kanisani wale ambao walitumia cho chote kumshambulia. Alikubali fedha kutoka Filipi (kama vile 1 Kor. 4:15) na Thesalonike (kama vile 2 Kor. 11:9), lakini baadaye, sio wakati akiwa pale.

◙ "**maana ni heri nife**" Hii ni kauli nzito kiasi gani kuhusu kukubali au kukataa fidia. Pia kuna tatizo la kisarufi kwenye sehemu hii ambalo lilisababisha tofauti kadhaa za miswada ya Kiyunani. Paulo amehamasika sana kuhusu somo hili, alichukua fedha na misaada kutoka Filipi (kama vile Flp. 4:15) na Thesalonike (kama vile 2 Kor. 11:9), kwa nini sio Korintho? Bila shaka kwa sababu ya jambo hili anashambuliwa moja kwa moja na kikundi, vikundi vilivyojiunda ama walimu wa uongo.

Kuna kusimamishwa kwa muda kwa wazo la Paulo katikati ya sentensi baada ya neno "kuliko." Angalia jinsi Biblia ya NRSV na NET zinavyoweka alama ya _ wakati NJB inaweka alama ya vitone ikijaribu kuonyesha mvunjiko

wa sarufi. Jinsi mvunjiko huu unavyoathiri kifungu cha neno unaofuata ni jambo lisilo dhahiri. Yaonekana alimaanisha kuthibitisha kwamba asingechukua fedha yo yote kutoka kanisa la Korintho lakini ameacha hivyo tu bila kusema. Hili ni fungu la maneno ambalo ni lenye hisia yenye nguvu sana. Paulo anaumia, anaonyesha hisia, anatetea hoja, sio kufundisha jambo tu. Maisha yake yanaelezea kanuni hiyo (yaani wote, kila kitu, kila wakati, pamoja na kila mmoja kwa ajili ya injili (kama vile 2 Kor. 4:5-12; 6:3-13; 11:16-33)!

Ni kazi ngumu sana kutafasiri waraka wa Paulo tunapokuwa katika

1. Barua ambayo kanisa walimwandikia ama
2. Utambuzi maalum kuhusu mazingira ya mahali

**9:16** "**ijapokuwa**" Hizi zote mbili ni SENTENSI ZENYE MASHARTI DARAJA LA TATU zinazomaanisha juu ya tendo muhimu.

◙"**Nimewekewa sharti**" Ole wangu nisipoihubiri injili, Paulo alisikia kushurutishwa kuhubiri kwa sababu ya wito maalum wa Yesu alioupata njiani akielekea Dameski (kama vile Mdo. 9:15; Rum. 1:14).
Alikuwa kama Yeremia wa zamani (kama vile Yer. 20:9) aliwajibika kusambaza injili (kama vile Mdo. 4:20)

**9:17** "**Ikiwa ..ikiwa**" Hizi zote mbili ni SENTENSI ambazo zinachukuliwa kwamba ni za kweli kutokana na mtazamo wa mwandishi ama kwa makusudi ya uandishi wake.

◙ "**Nimeaminiwa uwakili**" Hii ni KAULI TIMILIFU TENDWA YENYE KUARIFU, watenda kazi wa injili wana vyote viwili faida ya ki-agano na wajibu wenye heshima (kama vile 1 Kor. 4:1; Gal. 2:7; Efe. 3:2; Kol. 1:25). Angalia maelezo kamili kuhusu uwakili katika 1 Kor. 4:4-11

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 1 WAKORINTHO 9:19-23**

**[19] Maana, ingawa nimekuwa huru kwa watu wote, nalijifanya mtumwa wa wote, ili nipate watu wengi zaidi. [20] Nalikuwa kama Myahudi kwa Wayahudi, ili niwapate Wayahudi; kwa wale walio chini ya sheria, nalikuwa kama chini ya sheria, (ingawa mimi mwenyewe si chini ya sheria), ili niwapate walio chini ya sheria. [21] Kwa wale wasio na sheria nalikuwa kama sina sheria, (si kwamba sina sheria mbele za Mungu, bali mwenye sheria mbele za Kristo), ili niwapate hao wasio na sheria. [22] Kwa wanyonge nalikuwa mnyonge, ili niwapate wanyonge. Nimekuwa hali zote kwa watu wote, ili kwa njia zote nipate kuwaokoa watu. [23] Nami nafanya mambo yote kwa ajili ya Injili ili kuishiriki pamoja na wengine.**

**9:19** "**Ingawa nimekuwa huru kwa watu wote**" Huu ni msisitizo kuhusu uhuru halisi wa Mkristo (kama vile1 Kor. 9:1; 10:29; Gal. 5:13). Martin Luther alisema "Mtu Mkristo ni Bwana aliye huru juu ya vitu vyote na sio chini ya mtu ye yote. Mtu Mkristo ni mtumishi ahudumiaye katika mambo yote akiwa chini ya kila mtu" Tazama maelezo kutoka Rum. 14 na 15 katika 1 Rum. 6:12.

◙ "**Nalijifanya mtumwa wa wote**" Huu ni msisitizo kuhusu wajibu stahiki wa Mkristo (kama vile Rum. 14:1-15:13; 2 Kor. 4:5). Kwa kuwa Paulo alikuwa mtumwa wa Kristo, alikuwa mtumwa wa wote ambao alikuja kuwatumikia na kuwaokoa wote, aaminiye na asiyeamini. Angalia mada maalum uongozi wa ki-utumishi katika 1 Kor. 4:1.

◙ "**Ili nipate watu wengi zaidi**" Hili ni neno "pata" (yaani, *kerdainō*). Limetumika katika maana nyingi katika Agano Jipya. Katika muktadha huu Paulo anatumia neno hili katika maana ya ki-uinjilisti (kama vile 1 Kor. 9:19,20,21,22 na 1 Petr. 3:1). Hili ndilo lengo stahiki la ki-uinjilisti la matendo yetu yote (kama vile 1 Kor. 9:22-23). Kunia kufanya uinjilisti katika kila eneo la maisha yetu sio katika mtindo maalum ndio ufunguo wa kufikia uwiano stahiki kati ya uhuru wa Mkristo na wajibu wa Mkristo.

**9:20** Aya hii inaelezea kunia kwa Paulo. Shughuli kuu ya Paulo ilikuwa uinjilisti (Kama vile 1 Kor. 9:20-23; 10:31-33). Kwa hiyo alimtahiri Timotheo ili afanye kazi na Wayahudi (kama vile Mdo. 16:3), lakini asingemtahiri Tito (kama vile Gal. 2:3-5) ili asishushe hadhi ya uhuru wa injili miongoni mwa mataifa.

◙"**Nalikuwa kama chini ya sharia**" Inafurahisha kwamba ule upokeaji wa maandiko (yaani, ujulikanayo kama andiko la ki-Magharibi), linalojulikana kwa tabia za kiupanukaji, halijumuishi msemo ana fungu la maneno lililo la asili. Unapatikana kwenye miswada Kiyunani P[46], א, A, B, C, D*, F, G, P na toleo la Kilatini, ki-Syria, Coptic,na tafasiri ya Armenia. Lazima tuhusianishe maneno ya Paulo hapa na maneno ya Yesu katika Mt. 5:17-20. Paulo haiondoi sheria ya Musa bali anaona utimilifu wake ndani ya Kristo. Sheria sio njia ya wokovu bali bado ni (1) Ufufuo wa kweli na (2) Urejesho wa mapenzi ya Mungu kwa mwanadamu katika jamii. Inatenda kazi katika utakaso endelevu lakini sio kuhesabiwa haki. Angalia mada maalum katika 1 Kor. 9:9.

**9:21 "bali mwenye sheria mbele za Kristo"** Hii ni njia ya Agano Jipya kurejea kwenye Agano Jipya la Yeremia 31:31-34, Kuna njia kadhaa tofauti ambazo zimeandikwa ki-misemo na Paulo na Yakobo (Sheria ya Roho wa uzima, Rum. 8:2; Yakobo 1:25 na 2:12; sheria ya kifalme Yak. 2:8.

**9:22 "Kwa wanyonge nalikuwa mnyonge, ili niwapate wanyonge"** Maana ya neno"wanyonge" haijulikani hapa kwa sababu imetumika kwenye muktadha huu kwa Wakristo waadilifu sana ama washirikina sana (kama vile 1 Kor 8:7, 10). Yawezekana ikahusu wapagani washirikina (kama vile 1 Kor. 9:21. Tafsiri ya Williams inatafsiri neno hili kama waadilifu wa kupindukia ambapo ni utoaji mzuri) Tazama mada maalumu udhaifu katika 2 Kor. 12:9.

◙ "**Nimekuwa hali zote kwa watu wote, ili kwa njia zote nipate kuwaokoa watu**" Tambua idadi ya neno "wote" "zote" (yaani miundo ya *pas*) kwenye kifungu hiki. Utu wa ndani wa Paulo kubadilishwa kutoka kuiangalia nafsi binafsi kuwa kuiangalia injili. Yuko huru kumtumikia Kristo, kutumikia injili, kuutumikia ufalme (kama vile Rum. 6:11; 7:4)

Uwezo wa kubadili mipango au malengo, hali ya kunia, pamoja na upendo ni vitu muhimu sana katika maisha na huduma ya Paulo. Nia ya Paulo wakati wote ilikuwa kwenye uinjilisti (kama vile Rum. 11:14; 1 Kor. 1:21; 7:16; 10:31-33; 1 Tim. 1:15). Hata hivyo ni huzuni kusema kwamba kiasi cha mwisho kinatupatia fununu kwamba wengi sana hawakutoa mwitikio wa imani kwenye ujumbe wake. Kwa nini baadhi ya watu husikia (kwa masikio ya kiroho) na wengine hawafanyi hivyo, ni siri ya uchaguzi na uamuzi wa hiari.

**9:23** Hii ni aya ya muhtasari, aya ya mpito. Inaweza kwendana na 1 Kor. 9:19-22 au 24-27 ama ikasimama peke yake. Hii aya haitetei wokovu upatikanao kwa kutenda kazi. Paulo hakuokoka kwa sababu anahubiri, yeye hufanya hivyo kwa sababu amekwisha kuikubali injili na anajua amani yake na uhitaji wake.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 1 WAKORINTHO 9:24-27**

**24 Je! Hamjui, ya kuwa wale washindanao kwa kupiga mbio, hupiga mbio wote, lakini apokeaye tuzo ni mmoja? Pigeni mbio namna hiyo, ili mpate. 25 Na kila ashindanaye katika michezo hujizuia katika yote; basi hao hufanya hivyo kusudi wapokee taji iharibikayo; bali sisi tupokee taji isiyoharibika. 26 Hata mimi napiga mbio vivyo hivyo, si kama asitaye; napigana ngumi vivyo hivyo, si kama apigaye hewa; 27 bali nautesa mwili wangu na kuutumikisha; isiwe, nikiisha kuwahubiri wengine, mwenyewe niwe mtu wa kukataliwa.**

**9:25** "**Kila mtu ambaye hushindana kwenye michezo hujizoeza kujizuia katika yote**" Paulo anatumia msemo wa ki-michezo ya riadha, kutoka kwenye michezo iliyofanyika Korintho kila miaka miwili, msisitizo hapa uko kwenye juhudi kubwa inayotumika na wanamichezo washindanao, sio kujaribu ukiwa hujaamua kwa moyo wote (kama vile Ebr. 12:1-3). Mkristo hafanyi mashindano ili pate wokovu, bali kwa sababu amekwishapata uzoefu wa wokovu. Tumeshinda mbio katika Kristo, sasa tunakimbia mbio kwa ajili ya Kristo.

◙ "**Taji iharibikayo**" Washindi kwenye mashindano ya mbio ya Korintho walipewa tuzo ya msonobali (pale Athene taji ya mzeituni, pale Delphi taji ya mdalasini) ambazo baada ya muda tu zilinyauka. Waaminio kupokea taji ya

kufurahia (kama vile 1 Pet. 5:4) hizi ni taji zisizofifia. Je kujitoa kwa waaminio na shauku kunapaswa kuwa chini ya wanariadha? Wanapambana kwa kile kisichodumu, sisi tunapambana kwa ajili ya kisichofifia.

**9:26-27** "**Hata mimi napiga mbio vivyo hivyo**" Hii ni misemo ya mafumbo ya wanariadha kuelezea hitaji la kujidhibiti kwa nguvu na kujitia nidhamu. Maisha ya Kikristo yanazo sheria na mahitaji. Hizi zinahusu thawabu sio wokovu. Paulo lazima atakuwa alifurahia matukio ya riadha katika siku zake, anazitumia mara nyingi kama sitiari kwa maisha ya Kikristo.

**MADA MAALUM: KIWANGO CHA ZAWADI NA ADHABU (SPECIAL TOPIC: DEGREES OF REWARDS AND PUNISHMENT)**

**9:27** "**bali nautesa mwili wangu na kuutumikisha**" Neno hili, nidhamu, kwa maana halisi linarejelea mtu kupigwa usoni chini ya macho. Linatumika kitamathari katika Luka 18:5.
Paulo alikuwa anamaanisha kuhusu kujidhibiti katika maisha ya Kikristo. Mwili sio mwovu bali ni uwanja wa mapambano ya vishawishi. Ikiwa waaminio hawatautiisha mwili wenyewe utawatawala (kama vile Rum. 8:1-11) Huu sio ushindi mwepesi wa mara moja, bali ni mbio ndefu za muda mrefu za kuitawala nafsi kwa ajili ya Kristo. Kujidhibiti (kuwa na kiasi) ndilo tunda la mwisho la Roho katika Gal.5:23.
Neno "mwili" (soma) linahusu Paulo na utu wake wote. Sio moja ya vipengele vitatu vya wanadamu. Mara nyingi linasimama badala ya mtu mzima (kama vile 1 Kor. 7:4; 13:3; Rum.12:2; Flp. 1:20). Biblia humwonyesha mwanadamu kama kitu chenye umoja (kama vile Mwa. 2:7), sio mgao wa sehemu mbili ama mgao wa sehemu tatu (kama vile George E. Ladd, *A Theology of the New Testament*, kr. 464-466. Tazama maelezo zaidi katika 1 Kor. 7:34

**NASB, NKJV "ili kwamba. . .mimi mwenyewe nikakataliwa"**
**NRSV"mimi mwenyewe nisikataliwe"**
**TEV"kuiweka nafsi yangu isikataliwe"**
**NJB"mimi mwenyewe naweza kukataliwa"**

Neno hili "kataliwa" Ni sitiari inayohusu kuvunja sheria za michezo ya riadha na kwa hiyo kutoweza kushinda shindano (kama vile 1 Tim. 6:12; 2 Tim. 4:7). Linatoka kwenye mzizi wa neno "kujaribu" kwa kusudi la kuthibitisha ubora (yaani, *dokimazōi*), lakini ikiwa na KIAMBISHI AWALI KANUSHI ambacho kinakanusha (kama vile 2 Kor. 13:5). Hii aihusu wokovu wa Paulo (ingawa inatumika kwenye dhana hii katika 2 Tim. 3:8); Ingawa kifungu kilichopita kinaonekana kwa (kama vile 1 Kor. 9:19-23). Hili linaingilia mafungu mengi ya maneno ya mafundisho ya kidini ya Paulo hasa Warumi na Wagalatia. Yeye anajadili hofu yake ya kuadhibiwa na kukataliwa kama mhubiri wa injili. Agano jipya linaandika baadhi wale ambao walikataliwa (kama vile 1 Kor. 15:12; 1 Tim.1:20; 2 Tim. 4:10). Paulo alitaka matunda ya uinjilisti kutoka kwa waongofu na makanisa. Mafunzo ya vijana wa kiume kwa ajili ya michezo ya Kiyunani iliyotajwa katika (1) *Ars Poetica*, 412 na (2) *Ad Martyres*, 3. Yalihitaji miezi kumi ya mazoezi yenye kuhitaji nguvu na bidii sana kujitenga na mambo ya kijamii na kanuni za milo, mazoezi, michezo n.k. kwa ajili ya kuleta afya. Lakini bado kuna njia moja halali ya kuangalia andiko hili (kama vile *misemo migumu ya Biblia*, na Kaiser, Davids, Bruce na Branch).
"Katika kuandika hivyo mwandishi anapinga uwiano unaopatikana katika Agano Jipya lote. Waandishi wa Agano Jipya waliandika uzoefu wa neema ya Kristo na imani thabiti kwamba wako kwenye njia yao kuelekea urithi mkuu zaidi mbinguni. Wakati huo huo wanaandika wakiwa na sikitiko kwamba wao ama wasomaji wao wangeweza kuasi kwa hiyo kupoteza kile ambacho wanacho tayari. Kwa kuwa watu wanamfuata Kristo hivyo waandishi wa Agano Jipya hawaelezi tena tumaini lo lote kwamba bila toba watu kama wale hawaingii mbinguni. Hili ni hangaiko tulivu sio lenye kuleta hofu linaloonekana ndani ya Paulo (1 Kor. 9:27; Gal.5:2, 7-10; Flp.3:12; 2 Tim. 4:7 wakati mwingine akizungumzia hangaiko hilo katika maisha yake na wakati mwingine akizungumzia kuhusika kwake na wengine) Yakobo, (Yakobo 5:20 kusudi la waraka likiwa ni "kuokoa" (mwenye dhambi ikimaanisha aaminiye aliyegeukia ulimwengu kutoka mauti) Yuda (Yuda 23 (1 Yoh. 5:16-17 KJV msisitizo ukiwa kuwaombea watu kabla hawajatenda dhambi ya mauti). Wito kwa msomaji wa kisasa ni kuweka umakini kwenye onyo na "kuwaiga wale ambao kwa njia ya imani na subira wanarithi kile kilichokwisha ahidiwa (Ebr. 6:12) ili kwamba

mwandishi angesema juu yetu vile vile, tunayo hakika ya mambo bora katika swala lako – mambo yanayoambatana na wokovu (uk. 683)

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujisomea wa fasiri, ambao unamaanisha kwamba unao wajibu wa tafsiri yako mwenyewe ya Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika nuru tuliyo nayo. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hupaswi kumuachia vitu hivi mfasiri.

Maswali haya ya majadiliano yanatoa tu, msaada wa wewe kufikiria kupitia masuala nyeti ya sehemu ya kitabu hiki. Yamekusudiwa kukuchokonoa mawazo na sio kutoa maana ya mwisho.

1. Sura ya 9 inahusianaje na sura ya 8?
2. Ni sahihi kwa mhubiri kupokea msaada kutoka kanisani?
3. Kwa nini Paulo anatende tofauti kwa makusudi tofauti na asieleweke kama mnafiki?
4. Katika aya 24-27 sitiari ya mwanariadha inasisitizwa. Hii sitiari inatumikaje kwenye maisha yetu ya Kikristo?

# 1 WAKORINTHO 10

| MGAWANYO WA AYA WA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **UBS[4]** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB** |
| | | | | Chakula kilichotolewa kwa miungu ya uongo (8:1-11:1) |
| Onyo dhidi ya kuabudu sanamu | Mifano ya Agano la kale | Onyo dhidi ya kujiamini kupita kiasi | Onyo dhidi ya sanamu | Onyo na mafundisho ya historia ya Israeli |
| 10:1-13 | 10:1-13 | 10:1-5 | 10:1-5 | 10:1-13 |
| | | 10:6-13 | 10:6-10 | |
| | | | 10:11 | |
| | Ikimbieni ibada ya sanamu | Matumizi: kutoa tena sadaka kwa sanamu | 10:12-13 | Sikukuu za dhabihu: hakuna maafikiano na kuabudu sabamu |
| 10:14-22 | 10:14-22 | 10:14-22 | 10:14-17 | 10:14-22 |
| | | | 10:18-22 | |
| Fanya yote kwa Utukufu wa Mungu | Yote kwa Utukufu wa Mungu | Kanuni: Uhuru na wajibu wetu kwa wengine | | Chakula kilichotolewa sadaka kwa sanamu: ufumbuzi wa kiutendaji |
| 10:23-11:1 | 10:23-11:1 | 10:23-30 | 10:23-24 | 10:23-11:1 |
| | | | 10:25-26 | |
| | | | 10:27-29a | |
| | | | 10:29b-30 | |
| | | 10:31-11:1 | 10:31-11:1 | |

**MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (**Kutoka **"Mwongozo wa Usomaji Mzuri wa Biblia") ("A Guide to Good Bible Reading")**

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo wa usomaji wa fasiri, Ikiwa na maana kwamba unawajibika kwa ukalimani wako wa biblia mwenyewe. Kila mmoja wetu sharti atembee katika nuru tuliyonayo.Wewe, Biblia na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika kutafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua somo. Linganisha mgawanyo wa somo lako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika kiaya sio uvuvio, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la asili la mwandishi ambalo ndilo kiini cha ukalimani. Kila aya ina somo moja na somo ni moja tu.

9. Aya ya kwanza
10. Aya ya pili
11. Aya ya tatu
12. N.K

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA KWA 10:1-11:1

A. Sura ya 8 kupia sura ya 10 huhusishwa kukamilisha jaribio la kuleta usawa kwenye mjadala wa uhuru wa Mkristo dhidi ya wajibu wa Mkristo katika upendo. Paulo hakulenga juu ya kanuni ngumu na imara, lakini juu ya vipaumbele vya uhusiano binafsi ambao unaimarisha waminio na kuwavuta wasiomani kwa Yesu.

B. Mjadala wa Paulo juu ya karamu ya Bwana, mwanzoni katika 1 Kor. 10:14 na kuendelea kupitia 1 Kor. 10:22, ni dalili/ishara ya mjadala kamili katika 1 Kor. 11:17-34.
C. Paulo yawezekana alihutubia waaminio "wazaifu" katika 1 Kor. 10:14-22 na waaminio "wenye nguvu" katika 1 Kor. 10:23-33. Kama huu sio muundo, mtu hushangaa jinsi gani aya hizi mbili hazikinzani na nyenzake: 1 Kor. 10:14-22, usile chakula kilichotolewa kidhabihu; 1 Kor. 10:23-33, kuleni pasipo kuuliza maswali. Inawezekana ya kwanza hurejea kwenye chakula cha pamoja katika hekalu la kipagani na cha pili hurejea kwenye chakula binafsi nyumbani.
D. Jamii ya umoja wa Biblia' *Handbook on Paul's First Letter to the Corinthians*, kilichoandikwa na Ellingworth na Hatton kina muhtasari wa kuvutia wa 1 Kor. 10:1-13.
"Muundo wa jumla ni kama ufuatao:
   I. Utangulizi- aya ya 1a.
   II. Vipengele chanya.
      A. Mifano minne chanya kutoka Agano la Kale – aya ya 1b-4a-mfano wa mwisho uliongezewa katika aya ya 4b.
      B. Hitimisho limechukuliwa kutoka kwenye mifano chanya –aya ya 5.
      C. Matumizi kwa wasomaji –aya ya 6a.
   III. Vipengele hasi.
      A. Mifano mitano hasi ya Agano la Kale –aya ya 6b-10.
      B. Matumizi kwa wasomaji –aya ya 11-13.
      Neno **yote** limerudiwa mara tano katika aya ya 1-4, imetoa msisitizo mkubwa kwenye ukweli kwamba watu wote wa Israeli wanahusishwa na ulizi wa Mungu na mibaraka yake wakati wa kutoka na miaka iliyofuatia ya safari ndefu katika jangwa. **Wote** hutofautiana na **mingi kati yao** katika aya ya 5 na pamoja na **baadhi yake**, ambayo ilirudiwa mara nne katika aya ya 7-10" (uk. 214).

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 1 WAKORINTHO 10:1-5**
**[1] Kwa maana, ndugu zangu, sipendi mkose kufahamu ya kuwa baba zetu walikuwa wote chini ya wingu; wote wakapita kati ya bahari; [2] wote wakabatizwa wawe wa Musa katika wingu na katika bahari; [3] wote wakala chakula kile kile cha roho; [4] wote wakanywa kinywaji kile kile cha roho; kwa maana waliunywea mwamba wa roho uliowafuata; na mwamba ule ulikuwa ni Kristo. [5] Lakini wengi sana katika wao, Mungu hakupendezwa nao; maana waliangamizwa jangwani.**

**10:1 "Kwa maana, ndugu zangu, sipendi mkose kufahamu"** Kifungu hiki ni mbinu ya kifasihi ambayo hutumiwa mara nyingi na Paulo kuanzisha hitimisho (kama vile Rum.1:13; 11:25; 1 Kor. 10:1; 12:1; 2 Kor. 1:8; 1 The. 4:13).

◙**"baba zetu"** Hii huaksi (1) kuamini tabia za Kiyahudi katika kanisa au (2) watu wa agano jipya walikuja kupandikizwa ndani ya mti wa asili wa mzeituni, Israeli (kama vile Rum. 10; Gal. 6:16), na sasa tu wamoja katika Kristo (kama vile Efe. 2:11-3:13).

◙ **"wote. . . wote "** Hili neno jumuishi (yaani, *pantes*) hutumika mara mbili katika 1 Kor. 10:1 na mara moja katika 1 Kor. 10:2,3, na 4. Ni njia ya kusisitiza umoja wa Waisraeli wote katika uzoefu wa neema na hukumu ya Mungu, iitwayo kipindi cha Safari ndefu ya kutangatanga Jangwani (yaani., Hesabu).

◙ **"chini ya wingu "** Hii inarejea juu ya alama pekee ya uwepo wa YHWH. Ilikuwa inaitwa na walimu wa sheria za kiyunani wingi wa utukufu la *shekinah* (kama vile Kut. 13:21-22, 14:19). Neno la Kiebrania *shekinah* linamaanisha "kukaa pamoja na." YHWH alikuwa na watu wake wakati huu wa hukumu kwa njia ya karibu na uangalizi ambazo walimu wa sheria za kiyunani walianza kuiita “ kipindi cha fungate” kati ya YHWH na Israeli.

◙ **"wote wakapita kati ya bahari "** Hili ni dokezo la YHWH ikiigawa Bahari ya (kihalisia"mtu asiyeweza kutumainiwa" au"magugu") shamu. Wasomi wa leo hawatambui ni maji yapi walikuwa wanayarejerea. Neno hilo hilo, *yam suph* hutumika katika Agano la Kale kwa kurejea kwa (1) Ghuba ya Aqaba (kama vile Kut. 21:4; Kumb. 2:1; 1 Fal. 9:26; Yer. 49:21) au (2) Bahari ya Hindi. Inavyoonekana walikuwa wanarejelea kwenye maji ya miuujiza kuelekea sehemu za kusini. Inavutia kwamba "maji" hayasemwi kwamba yaliumbwa na Mungu katika Mwanzo 1. Mara nyingi hadithi za uumbaji za Mesopotania zinazungumzia maji (yaani, chumvi na safi) kama miungu ambayo ilitamani uharibifu wa binadamu. YHWH huwaokoa watu wake kwenye machafuko ya maji na wakati wa kushindwa.

**MADA MAALUMU: BAHARI YA SHAMU (SPECIAL TOPIC: THE RED SEA)**

**10:2 "wakabatizwa wawe wa Musa"** Machapisho ya Kiyunani hutofautiana kati ya IRABU TENDWA (yaani, MSS א, A, C, D) na IRABU YA KATI (yaani, MS B). Inaonekana kwangu IRABU YA KATI inafaa kimuktadha katika msisitizo wa maamuzi ta hiari ya Waisrael kumfuata Musa na ukweli wa kihistoria wa kubadili itikadi za Kiyahudi juu ya Ubatizo wanajitawala wenyewe. Hiki ni kifungu kisio cha kawaida,pekee hupatikana hapa katika Agano Jipya.Huonyesha usawa kati ya wajibu na upendeleo wa Agano la Musa, na Agano letu jipya katika Kristo;yote ni kutoka kwa Mungu na kwa namna Fulani ni sawa. Hapa ubatizo hutumiwa kama ishara kwa mtu anayefuta.

Kuna desturi ya walimu wa sheria za kiyunani inayojirudia mpaka kwa Baba wa Abdoni, moja ya waamuzi wa Israel (kama vile b Ker 9a; bYeb 46a) ambaye anahusiana na suala la kubadili itikadi za ubatizo lililotokea Bahari ya Shamu. Tazama Richard N. Longenecker, *Biblical Exegesis in the Apostolic Period*, kr. 102-103.

**10:3 "chakula kile kile cha roho"** Hii yote inarejea kwenye mana (kama vile Kut. 16) na kware (kama vile Kut. 16:13; Hes. 11:31-32), ambavyo vilitolewa kwa nguvu za mwujiza wa Mungu wakati wa safari ya muda mrefu jangwani.

**10:4 "kinywaji kile kile cha roho"** Hii inareja kwenye muujiza wa utoaji wa maji (kama vile Kut. 17:6; Hes. 20:8 na kuendelea).

◙ **"kwa maana waliunywea mwamba wa roho"** Mwamba ni sifa kwa YHWH katika Agano la Kale ambayo husisitiza uwezo na kudumu kwake (kama vile Kumb. 32:4,15; Zab. 18:2; 19:14). Pia hutumiwa na Ufalme wa Kimasihi kama nguvu ya kuharibu (kama vile Dan. 2:45).

◙ **"uliowafuata"** Hii huonekena kurejea kwa hadithi za kale za walimu wa sheria za Kiyunani juu ya Kut. 17:6 na Hes. 20:11 na kuendelea, kwamba mwamba uliwafuata Waisraeli na kwamba alikuwa Masihi. Desturi hii hasa umetajwa katika korani.

◙ **" na mwamba ule ulikuwa ni Kristo "** Hii ni taipolojia ya walimu wa sheri za kiyunani (uhusianishaji wa mwamba wawezakuwa umetoka katika Hes.21:17 au Kumb. 32:4,15,18,30, kama vile Targum Onkelos juu ya Hesabu 21).Mungu alitoa maji yaletayo uzima wakati wa safari ya muda mrefu jangwani. Paulo anaona mfanano kati ya utoaji wa Mungu wakati huo na utoaji jumla wa sasa wa maisha ya Mungu. Theolojia ya Paulo ilimwona Kristo kama alikuwepo kabla na kama wakala wa Baba wa maisha na Baraka. Yesu daima alikuwa Mungu Baba wa utoaji kamili na Baraka kubwa.

**10:5 "Lakini"** Hili ni neno la Kiyunani *alla*, ambalo huonyesha utofauti kubwa.Tazama Utambuzi wa kimktadha, D.

◙ **"wengi sana katika wao, Mungu hakupendezwa nao"** Hii ni dhihaka ya kuvuta usikivu: wote lakini wawili wa kizazi hicho walikufa. Wale tu chini ya umri wa miaka ishirini (yaani, bado sio wakubwa wa kutosha kuwa katika jeshi) na Yoshua and kaleb (yaani, wapelelezi wawili ambao walileta taarifa ya imani hasi) waliingia kwenye nchi ya ahadi (kama vile Yuda 1:5).

◙ **"maana waliangamizwa jangwani"** Neno hilio linamaanisha mifupa yao ilienea/ilitawanyika kando ya njia ya jangwani (kama vile Hes. 14:16). Wao walikuwa watu waliochaguliwa na Mungu, lakini alihukumu kutoamini kwao. Hawa waamini wa Agano la Kale waliona miujiza ya utoaji wa Mungu. Wao walijua mapenzi yake kupitia viongozi wao waliopewa na Mungu (yaani, Musa, Harun, na Mariamu), bado hata hivyo walifanya katika kutokuwaamini na uasi (kama vile Waebrania 3-4).

Paulo amesema tu juu ya jitihada zenye kutumika kwa kujizuia (kama vile 1 Kor. 9:24-27). Katika sura ya 11 anadokeza kwa wale ambao wanajaribu kutenganisha maarifa ya kitheolojia kutoka katika maisha ya ki-Ungu (yaani, mafunuo na wengine wenye akili). Hata chakula cha kawaida cha ushirika (yaani, sikukuu ya *agape*) hakiwezi kuliwa na waamini wasiomcha Mungu (kama vile 1 Kor. 11:27-32). Kifo cha kimwili kinaweza kuwa ni mateso ya muda, hukumu ya Mungu kwa waamini wasiotii.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 1 WAKORINTHO 10:6-13**

**[6] Basi mambo hayo yalikuwa mifano kwetu, kusudi sisi tusiwe watu wa kutamani mabaya, kama wale nao walivyotamani. [7] Wala msiwe waabudu sanamu, kama wengine wao walivyokuwa; kama ilivyoandikwa, Watu waliketi kula na kunywa, kisha wakasimama wacheze. [8] Wala msifanye uasherati, kama wengine wao walivyofanya, wakaanguka siku moja watu ishirini na tatu elfu. [9] Wala tusimjaribu Bwana, kama wengine wao walivyomjaribu, wakaharibiwa na nyoka. [10] Wala msinung'unike, kama wengine wao walivyonung'unika, wakaharibiwa na mharabu. [11] Basi mambo hayo yaliwapata wao kwa jinsi ya mifano, yakaandikwa ili kutuonya sisi, tuliofikiliwa na miisho ya zamani. [12] Kwa hiyo anayejidhania kuwa amesimama na aangalie asianguke. [13] Jaribu halikuwapata ninyi, isipokuwa lililo kawaida ya wanadamu; ila Mungu ni mwaminifu; ambaye hatawaacha mjaribiwe kupita mwezavyo; lakini pamoja na lile jaribu atafanya na mlango wa kutokea, ili mweze kustahimili.**

**10:6 "Basi"** NRSV, TEV, na JB pia inatoa alama kwa mgawanyiko wa aya kwa jambo hili kuonyesha mabadiliko kutoka katika analojia za kitheolojia kuelekea kwenye matumizi ya sasa.

◙**" mambo hayo yalikuwa mifano kwetu"** Neno la Kiyunani *tupoi,* yaani "mifano," (umoja *tupos*) lina uwanja mpana wa kimaana. Ilikuwa alama iliyoachwa kwa kipigo. Hii inaweza kurejea kwa kupigwa kimwili (kama vile Mt. 24:49; 27:30) au sitiari kwa ajili yake (kama vile 1 Kor. 8:12).

Inakuja kutumiwa kwa chapa iliyoachwa kwa kipigo cha nyundo (kama vile Yohana 20:25). Hii chapa inaweza kurejea kwa picha ya kimwili ya sanamu (kama vile Mdo. 7:43) au picha iliyochapishwa (kama vile Mdo. 23:25; Rum. 6:17).Kutoka katika hili inakuja kusimama kwa mpangilio (kama vile Mdo. 7:44; Flp. 3:17; 1 The. 1:7; 2 The. 3:5; 1 Tim. 4:12; Ebr. 8:5; 1 Petro 5:3).

Usawa bora kwa matumizi ya neno hili katika maandishi haya (yaani, "aina" 1 Kor. 10:6) ni 1 Kor. 10:11 na Rum. 5:14, ambapo hurejea kwa (1) aina ya maono; (2) kifanani cha kitamathali; au (3) ishara za mifano.

Aya ya 6 na 11 inakumbusha waaminio wa Agano Jipya kwamba Agano la Kale lina uhusiano wa kiroho kwao (kama vile Rum. 4:23-24; 15:4; 1 Kor. 9:10; 10:6,11). Mafunuo ya Mungu ni ya milele na kanuni ni zenye kuhusu yaliyojadiliwa.

◙ **"kusudi sisi tusiwe watu wa kutamani mabaya, kama wale nao walivyotamani"** Angalia kwamba Paulo analinganisha watu wa Agano la Kale na watu wa Agano Jipya. Uovu ni tatizo la kutokea mara kwa mara. Inaweza kunyang'anya binadamu uzima wa milele, ushirika wa ndani na Mungu. Uovu hupotosha kila ngazi apitiayo mwanadamu. Wokovu hautufungui kwenye mapambano (kama vile Rum. 7; Efe. 6:10-19). Kanisa la Wakorintho lilikuwa katika hatari kwenye maeneo yote mawili ya imanii inayokubalika na tabia sahihi za kirutulujia na kimaadili! Yenye kumcha Mungu, sio taarifa, ni lengo!

Neno "omba" (limetumika mara mbili) kuonyesha ambatani kati ya neno la Kiyunani *epithumeō*, ambalo limeundwa kwa KIHUSISHI "juu ya" na "kuharakisha." Inarejea hisia kali na kupatwa na mihemko na kutawala fikra na moyo wa mtu. Inaweza kutumiwa katika hisia chanya kama katika Flp. 1:23, lakini kawaida hutumiwa katika

hisia hasi (kama vile 2 Tim. 2:22). Paulo anaweza kuonyesha tamaa kubwa na kutotii kwa Waisraeli kuliko nukuliwa katika Hes. 11:31-35, kwa sababu yeye hudokeza kwa Hes. 25:9 katika 1 Kor. 10:8 na Hes. 16:4-5; 17:5,10 katika 1 Kor. 10:10.

**10:7 "Wala msiwe waabudu sanamu "** Hii ni KAULI YA KATI SHURUTISHI (shahidi wa maandishi) YA WAKATI ULIOPO ikiwa na KIAMBATA HASI, ambayo kwa kawaida inamaanisha kusitisha kitendo kilichoko katika mchakato. Nukuu hii ya AK inarejelea juu ya karamu ya ulafi, ulevi na uasherati wa kuabudu sanamu wa Kutoka 32.

Utendaji halisi wa kuabudu sanamu ambao Paulo anaurejelea katika Korintho haujulikani.Kwa maana Fulani waamini walikuwa katika hatari ya kumchukiza Mungu. Kutoka katika sura ya 7 na hali ya kihistoria katika Korintho huenda ikawa ni utendaji wa ibada za kipagani za kujamiiana au kutoka sura ya 8 sadaka ya kuabudu sanamu ya kipagani.

**◙" WATU WALIKETI KULA NA KUNYWA, KISHA WAKASIMAMA WACHEZE "** Hii ni dokezo kwa haruni kufanya ndama ya dhahabu katika Kutoka 32 na wana wa Israeli kusherekea mbele yake na kutenda matendo ya uasherati (kama vile Kut. 32:6,19). Kipengele cha kijinsia cha neno “kucheza” kinaonekana katika neno hilo hilo la kiebrania lililotumika katika Mwa. 26:8 kwa Isaka kufanya mapenzi na Rebeka.

**10:8 "Wala msifanye uasherati"** Hii inaonyesha muundo wa kipagani huko Korintho na pia tabia ya wapagani, hata wapagani waliokombolewa, kuwa sambamba na zinaa kwa jina la dini.

**◙ "wakaanguka siku moja watu ishirini na tatu elfu"** Hii ni rejeo kwa Hes. 25:1-9. Kuna tofauti ya wazi kati ya hili na andiko la Kiebrania la Hes. 25:9, ambayo ina watu ishirini na nne elfu.Hii haionyeshi kuwa kosa la mwandishi aliyekuwa akinakili. Hii tofauti ni katika miswada yote ya kiyunani. Inaweza kuwa ni kuteleza kwa kumbukumbu juu ya sehemu ya Paulo. Hii haimaanishi kudokeza/kuashiria ukosefu wa msukumo au uaminifu, lakini ulimwengu wa kale ulikuwa sio kama sahihi katika matumizi yao ya idadi kama watu wa magharibi wa sasa.

Katika Archer's *Encyclopedia of Bible Difficulties*, kr. 141, 401, yeye huonyesha kwamba kifungu Paulo anachorejelea cha AK sio Hes. 25:1-9, lakini Kutoka 32.Yeye hufanya jambo zuri kwenye nukuu 10:7 kutoka katika Kut. 32:4 na ambayo Kut. 32:35 inataja Bwana alivyowapiga watu wazi wazi hata kushinda watu 3,000 wa 1 Kor. 10:28. Hii ni kwa hakika ni uchaguzi wa taratibu zenye kuweza kujitegemea.

**10:9 "Wala tusimjaribu Bwana"** Hili ni nene *peirazō* na KIHUSISHI *ek*, ambacho huongeza neno (kama vile Mt. 4:7; Luka 4:12; 10:25). Tazama Mada Maalum: maneno ya kiyunani kwa ajili ya majaribu katika 1 Kor. 3:13. Kanisa la Korinto walikuwa wakifanya kwa tabia sawa na Waisraeli jangwani (kama vile Hes. 21:5-6).Mungu anatumia hukumu ya maisha kuwarekebisha watu wake. Neno "Bwana" (kama vile NASB, TEV, NJB, na NIV) linapatikana katika miswada ya kale ya Kiyunani ya א, B, C, P, na tafsiri ya ki-Armenia. Lingeweza kufaa dokezo la Agano la Kale vizuri zaidi, likirejelea kwa YHWH katika Hesabu 21.

Neno "Kristo" (kama vile NKJV, NRSV) linapatikana katika miswada ya $P^{46}$, D, F, G, na tafsiri za toleo la Biblia ya Kilatini na toleo la Biblia la Ki-syria. Inafaa zaidi kwa wasikilizaji wa karibu sana wa Paulo. Wakati $UBS^4$ inapendelea neno "Kristo" na daraja "B" (yaani, karibu na hakika), hoja yenye nguvu kwa neno “Bwana”imetengenezwa na Bart D. Ehrman katika *The Orthodox Corruption of Scripture*, Kr. 89-90.Tazama Mada Maalumu: Maneno ya Kiyunani kwenye neno “kujaribu” na vidokezo vyake katika 1 Kor. 3:13.

**◙ "wakaharibiwa na nyoka"** Hii ni rejeo kwa Hes. 21. Tazama Mada Maalum: *Apollumi* katika 1 Kor. 8:11.

**10:10 "Wala msinung'unike, kama wengine wao walivyonung'unika"** Kifungu cha kwanza ni KAULI TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO kikiwa na KIAMBATA HASI, ambayo kwa kawaida inamaana juu ya kuacha kitendo kilichoko kwenye mchakato. Hii inarejea Hes. 16:41-50, ambayo ilirejelewa katika Hes. 17:5,10. Kanisa la Koritho lilikuwa linanung’unika kama Israeli ya kale.

◙ **"mharabu"** Hili linadokezo kwenye tauni katika Hes. 16:49. Ilikuwa njia ya kitheolojia ya kuonyesha kwamba kifo kilikuwa kwenye mikono ya YHWH (kama vile Kut. 12:23,29; 2 Sam. 24:16; 1 Nya. 21:15; Heb. 11:28). Hakuna "mvunaji mbaya"! Hakuna nafasi, hatima, au bahati! Kuna Mungu, Mungu wa Israeli, Baba wa Bwana Yesu Kristo. Yeye na Yeye pekee ndiye mtawala wa maisha na kifo

**10:11 "wao"** Hii inarejelea watu katika Agano la kale ambao walikufa katika mikono ya waharabu.

◙ **"mifano"** Tazama maelezo katika 1 Kor.10:6. Tazama MADA MAALUMU: MTAZAMO WA PAULO JUU YA SHERIA ZA MUSA (SPECIAL TOPIC: PAUL'S VIEWS OF THE MOSAIC LAW) katika 1 Kor. 9:9.

◙ **" tuliofikiliwa na miisho ya zamani "** Hii ni KAULI TENDAJI ELEKEZI YA WAKATI ULIO TIMILIFU. Ni sitiari juu ya kutabiriwa kwa miisho ya sasa (kifungu sawa katika Ebr. 9:26). Waaminio huishi katika ufalme wa Mungu, kufunguliwa kwa Yesu katika ujio wake wa mara ya kwanza, na kukamilishwa na ujio wake wa mara ya pili. Tunaishi katika wasiwasi wa "utimilifu na ulio bado"! Angalia MADA MAALUMU: ENZI HII NA ENZI INAYOKUJA (SPECIAL TOPIC: THIS AGE AND THE AGE TO COME) katika 1 Kor. 1:20.

**10:12 "anayejidhania kuwa amesimama"** Kujiamini na kiburi cha majivuno ya kikundi kidogo ndani ya kundi zima la Wakorintho lilikuwa tatizo kuu, kama tabia hizo zilivyo leo (kama vile Rum. 11:20; 2 Pet. 3:17). Mungu anao na atahukumu watu wake (kama vile Yer. 25:29; 1 Pet. 4:17). Kujidanganya ni laana kwa watu wa kidini! Wale katika Kristo wanapaswa kutekeleza kwa bidii (kama vile 1 Kor. 9:24-27)!

**10:13 "Jaribu"** Neno hili limetumika mara tatu katika aya hii na namna ya kujaribu kwa mtazamo kuelekea kwenye uharibiifu (tazama Mada Maalumu katika 1 Kor. 3:13). Kuna vyanzo vitatu vya jaribu katika AJ:
1. asili ya dhambi ya mwanadamu aliyeanguka
2. uovu binafsi (yaani, Shetani na pepo mbaya)
3. mfumo wa ulimwengu ulioanguka (kama vile Efe. 2:1-3; Yakobo 4:1,4,7)

**NASB"isipokuwa lililo kawaida ya wanadamu"**
**NKJV"ni ya kawaida kwa binadamu"**
**NRSV"hiyo sio kawaida kwa kila mtu "**
**TEV"aina ambayo kawaida huja kwa watu "**
**NJB"hakuna. . .ni zaidi ya mwandamu kustahimili "**

Wanadamu wengine wamekabiliwa na jaribu sawa kama waaminio wa Kikorintho. Yesu pia amejaribiwa na kushinda majaribu yote ambayo ni ya kawaida kwa Binadamu (kama vile Ebr. 4:15).

◙ **"Mungu ni mwaminifu"** Hii ni kauli muhimu sana ya kutoa wasifu! Imani ya kibiblia inabaki kwenye sifa ya Mungu. Tumaini letu ni katika neema na sifa zake, ahadi za uhakika na matendo ya ukombozi.

Kipengele hiki cha sifa za Mungu kwa mara ya kwanza kilisemwa katika Kumb. 7:9, ambazo ni ukuzaji nguvu kwa Kumb. 5:9-10. Haki ya Mungu inapita kwa muda hadi kizazi cha tatu na nne, lakini fadhili zake (yaani, upendo mwaminifu wa Agano, *hesed*) kwa vizazi elfu. Uthibitisho huu huu unaendelea katika Isa. 49:7.

Hii ni dhamira kuu katika barua za Wakorintho (kama vile 1 Kor. 1:9; 10:13; 2 Kor. 1:18, pamoja na 1 The. 5:24 na 2 The. 3:3). Waaminio ni wa imani ya uaminifu wa Mungu; kuamini uaminifu wa Mungu. Hiki ni kiini cha kiimani ya kibiblia!

**NASB"lakini pamoja na lile jaribu atafanya na mlango wa kutokea, ili mweze kustahimili "**
**NKJV"lakini pamoja na lile jaribu atafanya na mlango wa kutokea, ili mweze kustahimili"**
**NRSV"lakini pamoja na jaribu yeye atatoa mlango wa kutoke ili mweze kustahimili "**
**TEV "ila pamoja na majaribu, yeye atawapeni pia nguvu ya kustahimili na njia ya kutoka humo salama"**
**NJB"na jaribio lolote pia atatoa njia ya kutokea na kukuwezesha kutoka humo salama "**

Neno hili la Kiyunani lilitumika juu ya njia ili kuepuka mtego wa kijeshi. Waaminio hawakabiliani na majaribu peke yake! Tatizo katika maandishi haya ni jinsi gani mtu uhusisha "kutoa mlango wa kutokea" na "kuweza

kustahimili."Je! Baadhi hupata mlango wa kutokea na wengine huvumilia au Mlango wa kutokea wa Mungu kweli ni njia ya kustahimili?Je! Majaribu huacha au Je! Waaminio wanafanya kazi kupitia majaribu kwa imani? Ingawa Utata huu hauwezi kutatuliwa, habari nzuri ni kwamba Mungu yu pamoja nasi katika matatizo (kama vile Zab. 23:4).Mungu hawezi kutuacha sisi au kututelekeza. Utaratibu sahii wa kufanya jambo kwa ushindi haukufunuliwa wazi, lakini ni ushindi!

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 1 WAKORINTHO 10:14-22**

**14 Kwa ajili ya hayo, wapenzi wangu, ikimbieni ibada ya sanamu. 15 Nasema kama na watu wenye akili;
lifikirini ninyi ninenalo. 16 Kikombe kile cha baraka tukibarikicho, je! Si ushirika wa damu ya Kristo? Mkate ule
tuumegao, si ushirika wa mwili wa Kristo? 17 Kwa kuwa mkate ni mmoja, sisi tulio wengi tu mwili mmoja; kwa
maana sisi sote twapokea sehemu ya ule mkate mmoja. 18 Waangalieni hao Waisraeli walivyokuwa kwa jinsi
ya mwili; wale wazilao dhabihu, je! Hawana shirika na madhabahu? 19 Basi niseme nini? Ya kwamba kile
kilichotolewa sadaka kwa sanamu ni kitu? Au ya kwamba sanamu ni kitu? 20 Sivyo, lakini vitu vile wavitoavyo
sadaka wavitoa kwa mashetani, wala si kwa Mungu; nami sipendi ninyi kushirikiana na mashetani. Hamwezi
kunywea kikombe cha Bwana na kikombe cha mashetani. 21 Hamwezi kushirikiana katika meza ya Bwana na
katika meza ya mashetani. 22 Au twamtia Bwana wivu? Je! Tuna nguvu zaidi ya yeye?**

**10:14 " Kwa ajili ya hayo "** Paulo anahitimisha mjadala uliopita na kuendelea na hitimisho.

**NASB, NKJV"wapenzi wangu"**
**NRSV, TEV,**
**NJB"marafiki zangu wpenzi"**

Barua za Paulo kwa Wakorintho (na Wagalantia) ni maneno yake magumu kwa makanisa. Kwa hivyo, alitaka kuwakumbusha jinsi gani wao ni wenye thamani kwake hata wakati akizungumza kwa ukali kwao (kama vile 1 Kor. 4:14; 10:14; 15:58; 2 Kor. 7:1; 12:19).

Neno hili lilitumiwa na Mungu Baba wa Yesu (kama vile Mt. 3:17; 12:18; 17:5). Paulo, Petro, Yuda, na Yohana, katika barua zao, walitumia KIVUMISHI hiki kuonyesha wafuasi wa Mungu. Wao ni wapendwa wake kwa sababu ya uhusiano wao na Kristo;wapendwa na Mungu, na Kristo, na wapendwa na waandishi wa barua za AJ.

◙ **" ikimbieni ibada ya sanamu "** Hii ni KAULI TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO. Angalia neno "kuabudu sanamu" ina KIBAINISHI CHA WAZI. Mungu anatoa njia, lakini waaminio wanapaswa kuchagua kuchukua manufaa yake (kama vile 1 Kor. 6:18). Njia moja ya kushughulikia majaribu ni kukimbia uwepo wake. Waaminio hawapaswi kujiweka katika uwanja wa majaribio.

"Kuabudu sanamu" katikia Agano la kale ilikuwa picha na ibada ya miungu ya kipagani. Katika siku zetu ni kitu chochote kinachomwakilisha Mungu katika kipaumbele cha muundo wetu (kama vile 1 Kor. 10:7,14). Kama Yesu alivyosema, ambapo hazina yako ipo pale moyo wako utakapokuwa (kama vile Mt. 6:21). Watu wa kisasa hufunua vipaumbele vyao kwa muda, fedha, na maisha ya mawazo. Dini mara nyingi ni kiambatanisho muhimu, lakin sio kiini cha kipaumbele. Imani ya kweli haijishughulishi na ziada, lakini inajishughulisha na kiini cha maisha. Kitabu cha 1 Yohana hufunga na "jihadharini na sanamu" (kama vile 1 Yohana 5:21).

**10:15** Hii inaonyesha njia ya Paulo ya uongozi.Yeye alikuwa mtume wa Kristo, bado huonya hawa waaminio wenye majivuno kuhukumu maneno yake kwa wao wenyewe (kama vile 1 Kor. 14:39-40). Ni hakika inawezekana kwamba Paulo alikuwa na kejeli. Hutumia neno hili sawa (yaani, mwenye busara) katika 1 Kor. 4:10 na 2 Kor. 11:19 katika hisia ya kejeli.

**10:16** Aya hii imejengwa kama maswali mawili yasiodai jibu (ingawa TEV huitafsiri kama kauli ELEKEZI).

◙ **"Kikombe kile cha baraka"** Hii yumkini inarejea kwa kikombe cha tatu katika huduma ya pasaka ya Kiyahudi. Ndivyo Yesu aliwatuma kufungua karamu ya Bwana.

Neno "baraka" ni *eulogia* kutoka kwenye KITENZI *eulogeō*, ambacho kinamaanisha "kusifu," "kusifu mno," "kubariki," au"ili kufaidika." Tazama maelezo katika 2 Kor.9:5. Tunapata neno la Kiingereza kwa maneno ya kusifu kutoka katika mzizi huu wa Kiyunani. Wakati Yesu alifanya kuwa sheria amri hii alichukua vyote kikombe na mkate na kutoa shukrani kwa Mungu. Neno la Kiyunani kwa shukrani au kutoa shukrani ni *eucharistia*, ambapo tumepata neno komunyo/meza ya Bwana. Yote mawili kwa maneno haya ya Kiyunani hutumika katika njia ya kufanana katika 1 Kor. 14:16.

Ni ya kuvutia, lakini sio muhimu kitheolojia, kwamba utaratibu wa kawaida ya kikombe na mkate (kama vile 1 Kor. 11:24-27) umegeuzwa hapa. Utaratibu huu sio hoja, isipokuwa ushirika na Kristo katika chakula chake cha jumuia dhidi ya ushirika na miungu ya kipagani katika vyakula vyao vya jumuia.

## MADA MAALUMU: PASAKA (UTARATIBU WA HUDUMA) SPECIAL TOPIC: PASSOVER (ORDER OF SERVICE))

◙ **"ushirika"** Hili ni neno la Kiyunani *koinonia*, ambalo lina maanisha "ushiriki wa pamoja na." Hii ni asili ya neno la kiingereza "ushirikiano" hutumika kwa ishara ya chakula cha komunyo/meza ya Bwana, ambayo husisitiza ushirika sasa, lakini ushirika wa moyoni zaidi baadaye. Tazama Mada Maalumu: *Koinonia* katika 1 Kor. 1:9.

◙ **" wa damu ya Kristo "** Huu ni msisitizo juu ya kifo cha Kristo katika mazingira ya kusilibiwa kwake ya AK (kama vile Mambo ya walawi 1-7). Damu iliashiria maisha (kama vile Law. 17:11,14).

◙ **"Mkate ule tuumegao"** Hiki ni chanzo cha kifungu cha kiingereza tunachotumia kwa karamu ya Bwana, "kuumega mkate" (kama vile Mdo. 2:42).Hii ilikuwa ishara Yesu alichagua kuwasikilisha Agano Jipya katika mwili wake uliomegwa juu ya masalaba. Kwa makusudi hakuchagua mwana kondoo wa Pasaka, ambayo ilikuwa ishara ya uzoefu wa agano la kale (kama vile Kut. 12).

◙ **" ushirika wa mwili wa Kristo"** Ishara ya "mwili wa Kristo" ni wa mara mbili: (1) mwili wake wa asili ulisulubishwa kwa dhambi za mwanadamu na (2) wafuasi wake walikuwa mwili wake wa kiroho, kanisa (ambalo pia lina vipengele viwili katika 1 Wakorintho: [a] kanisa la mahali [b] kanisa la ulimwengu).

**10:17** Huu ni msisitizo juu ya umoja wa Kristo na kanisa lake ulioelezewa katika kuashiria karamu ya Bwana (yaani, mkate mmoja). Umoja huo huo wa mwili wa Kristo uko katika 1 Kor. 12:12-13 kuhusiana na zawadi za kiroho.

**10:18 "Waangalieni hao Waisraeli"** Hii kihalisia "Israeli itokanayo na mwili" (tazama Mada Maalumu katika 1 Kor. 1:26). Hii ni njia nyingine ya ishara (yaani, dokezo la kihistoria) kuonyesha umoja wa wale ambao hushiriki kwenye karamu ya Bwana.

**10:19 " Basi niseme nini "** Maandiko ya Paulo ni baadhi ya maandishi ya kibiblia rahisi kwa kufasiriwa kwa sababu yeye kimantiki huendeleza mawazo yake. Wasahihishaji wenye mantiki kama vile kifungu hiki kinaruhusu wafasiri wa kisasa kueleza kwa muhtasari mawazo ya Paulo katika ngazi za aya, ambazo ni muhimu katika kufasiri vitabu vyake.

Paulo anaendeleza mawazo yake katika mazingira haya kwa mfululizo wa maswali yasiotaka jibu (kama vile NASB, 1 Kor. 10:16 (mbili); 1 Kor. 10:18 (moja); 1 Kor. 10:19 (mbili na tatu); 1 Kor. 10:22 (mbili); 1 Kor. 10:29 (moja); 1 Kor. 10:30 (moja).

◙ **"Au ya kwamba sanamu ni kitu "** Kama mfano kwa jinsi gani waandishi wa kale kwa kutotegemea walibadilisha maandishi ambao walikua wananakili kifungu hiki kilitolewa kwa bahati mbaya katika miswada ya awali ya kale ya kiyunani (yaani, $P^{46}$, א*, A, na C). Kwa majadiliano zaidi ya ukosoaji wa maandiko tazama Kiambatanisho cha pili.

**10:20 " sadaka wavitoa kwa mashetani "** Paulo, anarudi nyuma kwenye Agano la kale, alielewa ibada ya sanamu kama ilivyohusika, sio kwa ukweli wa picha, lakini kwa ukweli wa nguvu za kiroho katika uumbaji wa kimwili (kama vile Law.16:8; 12:7; Kumb.32:17; Zab.96:5; 106:37; Isa. 65:11; Ufu. 9:20; 16:14). Nyuma ya shughuli zote za

binadamu ni utawala wa kiroho (kama vile Kumb. 32:8 [LXX]; Danieli 10; Efe. 6:10-18). Ingawa haijasemwa wazi malaika walioanguka wa AK ni pepo wabaya wa AJ, Paulo anarejea kwa nguvu hizi zilizoanguka za kiroho na maneno mengine katika Rum. 8:38-39; 1 Kor. 15:24; Efe.1:21; 3:10; Kol. 1:16; 2:10,15. Paulo hutumia neno "pepo" hapa pekee na katika 1 Tim. 4:1. Tazama Mada Maalumu: Uovu binafsi katika 1 Kor. 7:5.

**MADA MAALUMU: PEPO WACHAFU (SPECIAL TOPIC: THE DEMONIC (UNCLEAN SPIRITS))**

◙ **"kushirikiana na mashetani"** Fuata analojia ya Paulo. Wakristo ni wamoja na mwili wa Kristo (yaani, kanisa) kwa sababu wao ni wamoja na sadaka yake (yaani, mwili wake umesulubiwa pale Kalvari) kwa sababu wao hushirikiana katika mkate kwenye karamu ya Bwana ambayo inaashiria mwili wake uliomegwa. Kwa hivyo, wapagani wanaoshiriki katika kula nyama iliyotolewa sadaka kwa mashetani yasiyo kuwepo kwenye kushiriki katika ibada ya sanamu ya kiroho inayohusiana na mapepo nyuma ya dini za ulimwengu. Kama waaaminio wanaoshiriki katika matukio ya kihistoria ya maisha ya Yesu na njia ya kawaida za dini (yaani, Warumi 6), hivyo pia, wasioamini wanaoshiriki katika pepo wabaya.

**10:21** kifungu hiki kinarejea kwenye sadaka za kipagani na matambiko katika hekalu za Korintho. Muamini hawezi kuthibitisha upweke wa kikristo (yaani, Mungu mmoja na wa pekee wa kweli na Yesu masihi wake) na bado kushiriki kiroho katika ibada za kipagani. Kama wanafanya, basi ni ibada za kuabudu sanamu!

**10:22 "twamtia Bwana wivu"** Hii inaonekana ni dokezo kwa Kumb. 4:25; 32:16,21; Zab. 78:58; au Isa. 65:3. Neno Bwana katika 1 Kor. 10:21 dhahiri linarejerea kwa Yesu, lakini katika 1 kor. 10:22 kwa YHWH. Aina hii ya uhamisho ni mojawapo ya njia ambayo waandishi wa AJ wanaonyesha Uungu wa Yesu wa Nazareti.

Neno "wivu" ni neno la upendo wa nguvu. Mmoja huwa na wivu tu juu ya mtu anayempenda. YHWH amehusishwa kihisia na watu wake, ambao huaksi sifa yake na kuchukua jina lake ulimwenguni. Ibada ya sanamu huharibu ushirika huu na kusudi la kiinjilisti.

◙ **"Je!Tuna nguvu zaidi ya yeye"** Sarufi hutegemea jibu "hapana." Istilahi hii huonyesha makundi mawili tofauti ya Wakristo yaliyorejelewa: ndugu wadhaifu katika 1 Kor. 10:14-21 na ndugu wenye nguvu katika 1 Kor. 10:23-33. Aya ya 22 huonyesha ugumu wa kujaribu kushughulika na fikra ya haya makundi mawili ya waaminio (kama vile Rum. 14:1-15:13). Paulo anajaribu kutembea kwenye mkazo wa kitheolojia kati ya falsafa mbili za Wakristo/mitazamo wa ulimwengu (yaani, uhuru na utumwa kwa uzoefu wa zamani).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 1 WAKORINTHO 10:23-30**

**[23] Vitu vyote ni halali; bali si vitu vyote vifaavyo. Vitu vyote ni halali; bali si vitu vyote vijengavyo. [24] Mtu asitafute faida yake mwenyewe, bali ya mwenzake. [25] Kila kitu kiuzwacho sokoni kuleni, bila kuuliza-uliza, kwa ajili ya dhamiri; [26] MAANA, DUNIA NI MALI YA BWANA NA VYOTE VIIJAZAVYO. [27] Na mtu asiyeamini akiwaalika, nanyi mnataka kwenda, kuleni kila kitu kiwekwacho mbele yenu bila kuuliza-uliza, kwa ajili ya dhamiri. [28] Lakini mtu akiwaambia, Kitu hiki kimetolewa kiwe sadaka, msile, kwa ajili yake yeye aliyeonyesha, na kwa ajili ya dhamiri. [29] Nasema, dhamiri, lakini si yako, bali ya yule mwingine. Maana kwa nini uhuru wangu uhukumiwe na dhamiri ya mtu mwingine? [30] Ikiwa mimi natumia sehemu yangu kwa shukrani, kwa nini nitukanwe, kwa ajili ya kitu nikishukuriacho?**

**10:23** Huu ni urudiaji wa somo la awali katika sura ya 6:12 kuhusu jinsi gani ya kulinganisha uhuru wa Mkristo na wajibu (kama vile Rum. 14:19).Aya ya 23-33 huhutubia ndugu wenye nguvu.

◙ **"Vitu vyote ni halali"** Kifungu hiki kilirudiwa mara mbili. Baadhi ya tafsiri ziliweka kifungu hiki katika nukuu (kama vile NRSV, TEV, NJB) kwa sababu wao walidhani ilikuwa kauli mbiu ya moja ya kikundi kidogo ndani ya kundi zima la vikundi katika Korintho au mithali ya kitamaduni. Hii ni kukombolewa kwa mtizamo wa ulimwengu wa mkristo" mwenye nguvu" (kama vile 1 Kor. 6:12; 10:26; Rum. 14:14,20).

## [MADA MAALUMU: UHURU WA MKRISTO DHIDI YA WAJIBU WA MKRISTO (SPECIAL TOPIC: CHRISTIAN FREEDOM VS. CHRISTIAN RESPONSIBILITY)]

◙ **"bali si vitu vyote vijengavyo"** Utendaji, jaribio la kiroho ni, "Je! unajenga mwili (yaani, jamii ya waamini)?" (kama vile 1 Kor. 6:12; 14:3-4,26; 2 Kor. 12:19; Rum. 14:19; 15:2). Hili inapaswa kuwa jaribu kwa waamini wote juu ya yale wafanyayo au wasemayo. Uhuru wa mtu katika Kristo haupaswi kumuumiza mwingine ambaye Kristo alikufa kwa ajili yake (kama vile Rum. 14:15).

Neno la kibinafsi tu, hii sio kudokeza kwamba mambo ya kiroho lazima yashauliwe kwenye ngazi ya chini ya muamini aliye dhaifu, lakini waaminio waliokomaa hawapaswi kuringia uhuru wao kwa gharama ya waamini wenzake. Baadhi ya waamini ni wenye kulazimisha kauli, Washikiria sheria wa Kifarisayo. Si lazima kushindwa kwenye sheria zao, lakini napaswa kuwapenda, kuwaombea, kuwakubali kikamilifu, na sio kuwaaibisha hadharani au kuringia uhuru wangu. Ninawajibu kiroho kwa waamini wenzangu! Angalia MADA MAALUMU: KUJENGA MAADILI/ ADILISHA (SPECIAL TOPIC: EDIFY) katika 1 Kor. 8:1.

**10:24 " Mtu asitafute faida yake mwenyewe, bali ya mwenzake "** Hii ni KAULI TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO. Ukristo uliokomaa huweka ustawi wa wengine mbele (kama vile 1 Kor. 10:33; 12:7; 13:5; Rum. 14:7; 15:2; Flp. 2:1-5,21).

**10:25,27** Hii ni sauti ya imani iliyokombolewa. Lakini imani "yeye nguvu" iliyokubali kushindwa hadharani kwa imani "dhaifu" (kama vile 1 Kor. 10:28-29).

**10:25 " dhamiri "** Hakuna kifanani katika AK kwa neno la Kiyunani "dhamiri" isipokuwa neno la kiebrania "kifua" hudokeza ujuzi wa nafsi na nia zake. Kiasili neno la Kiyunani kwa ufahamu huhusishwa na hisia tano. Huja kutumika kwa hisia za ndani (kama vile Rum. 2:15).Paulo anatumia neno hili mara mbili katika majaribio yake katika Matendo (yaani, 23:1 na 24:16). Inarejea kwenye hisia yake kwamba hakutambua kukiukwa kwa kutekeleza majukumu yoyote ya kidini kwa Mungu (kama vile 1 Kor. 4:4).

Dhamiri ni mwendelezo wa uelewa wa makusudi ya mwamini na vitendo vilivyoegemea juu ya (1) mtazamo wa ulimwengu wa kibiblia; (2) Roho akaaye ndani; na (3) Maisha ya maarifaa yaliyoegemea juu ya neno la Mungu. Dhamiri ya Mkristo inawezekana kuumbwa na mapokezi ya kibinafsi ya injili.Tazama maelezo kamili katika 1 Kor. 8:7.

**10:26 "MAANA, DUNIA NI MALI YA BWANA NA VYOTE VIIJAZAVYO"** Huu ni uthibitisho wa uzuri wa vitu vyote vilivyoubwa (kama vile 1 Kor. 6:12; 10:26; Rum. 14:14,20), kuchukuliwa kutoka katika mchanganyiko wa Zab. 24:1 na 50:12, ambao ulikuwa unatumiwa na Wayahudi katika AK kama baraka kwenye vyakula.

Upokeaji wa maandishi hurudia 1 Kor. 10:26 katika mwisho wa 1 Kor. 10:28.Hii sio asili. Haipo katika miswada ya Kiyunani ya א, A, B, C, D, F, G, H*, na P, pia haijaingizwa katika toleo la kibiblia la kilatini, ki-syria, au tafsiri za Coptic.

**10:27** Aya hii ni muhimu katika kufanya utofauti kati ya kushiriki katika kusherekea ibada ya sanamu za wazi dhidi ya kushirikiana kikawaida kila siku na wasioamini. Paulo hana sheria za haraka na ngumu. Yeye hupatia kipaumbele uhusiano wa kibinafsi (yaani, uinjilisti na uwanafunzi). Watu ni kipaumbele chake. Watu ni wa milele. Watu ni kusudi la kifo cha Yesu, sio chakula! Aya ya 29-33 inatuonyesha muhtasari wa Paulo juu ya jambo hili.

**10:27,30 " Ikiwa"** Yote ya haya ni SENTENSI YENYE MASHARTI DARAJA LA KWANZA, ambayo inadhaniwa kuwa kweli kutokana na mtazamo wa waandishi au kwa makusudi ya fasihi hii.

**10:28 "Ikiwa"** Hii ni SENTENSI YENYE MASHARTI DARAJA LA TATU, ambayo ina maanisha kuwezekana kwa kitendo.

◙ **"msile"** Hii ni KAULI TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO ikiwa na KIAMBATA HASI ambayo kawaida ina maanisha kuzuia kula. Ikiwa Mkristo ameambiwa hapaswi kula kwa sababu ukweli hasa wa jambo/suala umetolewa kuonyesha uwepo wa imani dhaifu au kutafuta imani (kama vile 1 Kor. 10:29).

**10:29**
**NASB"kwa nini uhuru wangu uhukumiwe na dhamiri ya mtu mwingine"**
**NKJV"kwa nini uhuru wangu uhukumiwe na dhamiri ya mtu mwingine "**
**NRSV"kwa nini uhuru wangu utegemee dhamiri ya mwingine "**
**TEV"kwa nini uhuru wangu wa kutenda uwe na kikomo kwa dhamiri ya mtu mwingine "**
**NJB"kwa nini uhuru wangu utawaliwe na dhamiri ya mtu mwingine"**

NRSV hii inatenga maneno kama kwamba haya yalikuwa maneno ya Paulo. TEV inatafsiri hili kana kwamba kulikuwepo na swali jingine lililoulizwa na mpinzani. Hii ni mbinu ya kifasihi iitwayo makemeo (kama vile 1 Kor. 6:12,13). Hili ni swali muhimu ambalo unapaswa kujibu kwa nafsi yako. Kila mmoja wetu, chini ya uongozi wa Roho Mtakatifu, lazima kuelezea mipaka ya ukomo wetu kwa wengine, nje ya upendo na heshima kwa Kristo.

**MADA MAALUMU: KUHUKUMU (WAKRISTO WANAPASWA KUHUKUMIANA?) SPECIAL TOPIC: JUDGING (SHOULD CHRISTIANS JUDGE ONE ANOTHER?))**

**10:30** Hii inarejea juu ya chakula kilichotolewa na muumini kama shukrani na kuliwa. Swali limeweka hatua kwa kanuni za pamoja kuhusu jinsi ya kutekeleza haki zetu za Kikristo, ambazo zinafuata katika 1 Kor. 10:31.

**ANDIKO LA NASB(LILILOBORESHWA): 1 WAKORINTHO 10:31-11:1**
**31 Basi, mlapo, au mnywapo, au mtendapo neno lo lote, fanyeni yote kwa utukufu wa Mungu. 32 Msiwakoseshe Wayahudi wala Wayunani wala kanisa la Mungu, 33 vile vile kama mimi niwapendezavyo watu wote katika mambo yote, nisitake faida yangu mwenyewe, ila faida yao walio wengi, wapate kuokolewa. 11:1 Mnifuate mimi kama mimi ninavyomfuata Kristo**

**10:31 "fanyeni yote kwa utukufu wa Mungu"** Hii ni kanuni ya ulimwengu ifaayo katika kila eneo la maisha ya waaminio (kama vile Efe. 6:7;Kol. 3:17,23; 1 Pet. 4:11). Angalia MADA MAALUMU: UTUKUFU *(Agano la Kale)* SPECIAL TOPIC: GLORY (OT) katika 1 Kor. 2:7.

**10:32 "Msiwakoseshe Wayahudi wala Wayunani wala kanisa la Mungu"** Hii inaonekana kureja kwa makundi mawili. Wawili wa kwanza huhusishwa na uinjilisti; kundi la mwisho kwa ushirika katika kanisa.
Neno “kanisa” dhahiri linatumika katika maana ya kiulimwengu kama katika Mt. 16:18. Neno linatumika katika Agano jipya katika
1. maana ya mahali palepale (hutokea mara nyingi)
2. maana ya kimkoa (kama vile Mdo. 9:31; Gal. 1:2
3. maana ya kiulimwengu (kama vile Flp. 3:6; Ebr. 12:23)
4. maana ya ulimwengu mzima wa watakatifu wote wa enzi zote za kuishi na kufa (kama vile Efe. 1:22; 5:23,24,25,27,29,32; Kol. 1:18,24)

◙ **"kanisa" Tazama Mada Maalumu: Kanisa katika 1 Kor. 1:2.**

**10:33 "vile vile kama mimi niwapendezavyo watu wote katika mambo yote. . . wapate kuokolewa "** Uinjilisti, sio haki binafsi, ni kipaumbele cha waaminio waliokomaa (kama vile 1 Kor. 9:19-22).

◙ **"walio wengi"** katika kiingereza hii inaweza kueleweka kama sehemu kubwa ya kundi lote. Hata hivyo, katika mawazo ya Kiebrania ni tofauti ya kifasihi tu ya neno“watu wote.” Mfanano huu inaweza kuonekana katika

1. Isaya 53:11, "wengi"

Isaya53:12, "watu wengi"
Isaya 53:6, "yetu sisi sote"
2. Warumi 5:18, "watu wote . . . watu wote"
   Warumi 5:19, "watu wengi . . . watu wengi"
3. Katika Wakorintho 10:17, "sisi tulio wengi" (hapa Paulo alitumia neno “wengi” kurejea kwa kundi lote la waaminio)

◙ **"wapate kuokolewa"** Hili ni lengo la kuhubiri injili na maisha ya Mkristo (kama vile 1 Kor. 9:19-22). Ahadi ya Mungu ya Mwa.3:15; 12:3 sasa imetimizwa.Ushirika uliovunjika (yaani, picha iliyoharibiwa ya Mungu katika mwanadamu) umerudishwa kupitia Kristo. "Yeyote anayetaka” anaweza kuja (kama vile Eze. 18:23,32; Yohana 1:12; 3:16; 1 Tim. 2:4; 2 Pet. 3:9).

**11:1** Sura hii inaonekana kwenda pamoja na aya ya 10, na sio 11. Nia za uinjilisti za Paulo na matendo zinafanana na maisha na mafundisho ya Yesu. Kama Paulo alivyomuiga Yeye waamini pia katika Korintho walitakiwa kuzingatia juu ya (1) uzuri wa mwili (kanisa) na (2) wokovu wa ulimwengu usioamini.

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujisomea wa fasiri, ambao unamaanisha kwamba unao wajibu wa tafsiri yako mwenyewe ya Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika nuru tuliyo nayo. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hupaswi kumuachia vitu hivi mfasiri.

Maswali haya ya majadiliano yanatoa tu, msaada wa wewe kufikiria kupitia masuala nyeti ya sehemu ya kitabu hiki. Yamekusudiwa kukuchokonoa mawazo na sio kutoa maana ya mwisho.

1. Je! Waisraeli ambao walifariki jangwani walipotea kiroho?
2. Ni nini kusudi kuu la karamu ya Bwana?
3. Jinsi gan mtu analinganisha uhuru wa mkristo na wajibu wa mkristo?
4. Ni nini kinapaswa kuwa lengo kuu la uhuru wetu?

# 1 WAKORINTHO 11

| MGAWANYO WA AYA WA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **UBS[4]** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB** |
| | | Matatizo katika Maisha ya Kijamii (11:2-12:40) | | Staha wakati wa Ibada ya hadhara (11:2-12:40 |
| Kufunika Kichwa Katika Ibada | Kufunika Kichwa | Usahihi wa Kuvaa wakati wa Ibada ya hadhara | Kufunika Kichwa wakati wa Ibada ya hadhara | Mwenendo wa Wanawake katika Huduma |
| 11:2-16 | 11:2-16 | 11:2-16 | 11:2-12 | 11:2-6 |
| | | | | 11:7-12 |
| | | | 11:13-16 | 11:13-15 |
| | | | | 11:16 |
| Matumizi Mabaya ya Chakula cha Bwana | Maadili wakati wa Chakula cha Bwana | Maagizo katika Mwonekano wa Matumizi Mabaya ya Chakula cha Bwana | Chakula cha Bwana | |
| 11:17-22 | 11:17-22 | 11:17-22 | 11:17-22 | 11:17-22 |
| Ushirika wa Chakula cha Bwana | Ushirika wa Chakula cha Bwana | | | |
| 11:23-26 | 11:23-26 | 11:23-26 | 11:23-27 | 11:23-27 |
| Kukionja chakula cha Bwana Isivyostahiri | Kujihoji Wenyewe | | | |
| 11:27-34 | 11:27-34 | 11:27-34 | 11:27-32 | |
| | | | | 11:28-32 |
| | | | 11:33-34 | 11:33-34 |

**MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI** (**kutoka "Mwongozo wa Usomaji Mzuri wa Biblia" (A Guide to Good Bible Reading)**)

## *KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Haya ni maoni ya mwongozo kwa kujisomea, ikiwa na maana kuwa unawajibika binafsi kwa tafsiri ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mtoa maoni tu.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

17. Aya ya kwanza
18. Aya ya pili
19. Aya tatu
20. N.k

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA KWA WAKORINTHO 11:2-34

A. Sura ya 11 mpaka 14 inajishughulisha na mambo yahusuyo kusanyiko la ibada. Mambo haya yanaunda muundo wa umoja wa kimaandishi.
   1. mavazi ya wamaume na wanawake na matendo yao (1 Kor. 11:2-16)
   2. kanuni za Meza ya Bwana (1 Kor. 11:17-34)
   3. zoezi la vipawa vya kiroho (1 Kor. 12-14)

B. Ninaposema "kusanyiko la ibada " kuna uwezekano wa mazingira ya aina mbili.
   1. mikusanyiko ya kimakundi katika nyumba yoyote, wengine katika ujirani wa mali, wengine katika makazi ya watu wa nasaba ile ile, wengine katika makazi ya kiutumwa
   2. kwa wakati mwingine (muda mahsusi haujulikani) makanisa madogo madogo ya nyumbani yalikusanyika kwa pamoja kwa ajili ya tukio la ibada zilizouteka mji mzima (yaani, neno *agapē* chakula cha pamoja na maadhimisho ya Ekaristi)
   3. Mpangilio tofauti wa utaratibu (itifaki) kwa ajili ya makanisa ya nyumbani dhidi ya tukio la kusanyiko haujulikani

C. Kumekuwa na njia kadhaa za kuielewa 1 Kor. 11:2-16.
   1. Muktadha huu kimsingi unajishughilisha na mwenendo mwema (kama vile 1 Kor. 11:13) kusanyiko la ibada, si uhusiano uliopo baina ya wanaume na wanawake (kama vile 1 Kor. 11:11-12).
   2. Muktadha huu unashughulika na uhuru mpya katika Kristo ambapo wanaume wa Kirumi na wanawake katika kanisa la huko Korintho walikuwa wakiutumia kutamba kama hadhi yao ya kijamii (wanaume) na uhuru wao kutoka katika mila na desturi (wanawake).
   3. Muktadha huu unashugulika na uhusiano wa kiuumbaji kati ya wanaume na wanawake (kama vile Efe. 5:22-31; 1 Tim. 2:9-15). Uhusiano kamili umeegemea juu ya Mwanzo 2-3, ambao unaonyesha upendeleo wa wanaume kwa sababu ya uumbaji asilia wa Adamu na uasi asilia wa Eva.
   4. Mjadala wa Paulo wa kufunika vichwa hauwawekei mipaka wanawake, bali umeelekezwa kwa wanaume. Kama ilivvyokuwa kawaida katika Korintho tatizo linatokana na maelekezo. Kama ilivyo ishara ya hadhi yao ya elimu ya kijamii wanaume wenginine walikuwa wakifunika vichwa walipokuwa wakifika katika mikusanyiko ya ibada kama walivyokuwa wakifanya katika dini zao za kutomjua Mungu. Kama ilivyo ishara ya ukombozi wao wa kijamii wanawake walikuwa wakizivua shera zao walipokuwa katika ibada za mikusanyiko (kama vile Bruce W. Winter, *After Paul Left Corinth*, kr. 121-141). Kwa upekee andiko hili linaoanishwa na Wakorintho wa Kirumi. Katika maisha ya Kiyahudi na maisha ya Kiyunani mara nyingi wanawake hawakuvaa vilemba (shera) vya kufunika vichwa vyao.

      Inaonekana kwamba muktadha huu wenye utata u wazi kwa ajili ya tafsiri zilizo nyingi zaidi. Fasiri hizi zinazungumza zaidi kuhusu upendeleo wa mtafsiri kuliko kusudi la Paulo. Muktadha ambao umekuwa ukieleweka au unaoweza kueleweka katika njia nyingi sana kwa waamini walio watiifu kwa uhakika haupaswi kutumika katika ubora, mfumo wa imani ya kanisa uliowekwa kwa ajili ya kuzuia au kuitetea nafasi na kazi ya wanawake katika kanisa au katika uhusiano uliopo kati ya wanaume na wanawake katika zama zote na tamaduni zote. Hii inanishangaza kwamba waamini wengine huushusha daraja mjadala wa sura ya sura 11 unaohusiana na wanaume na wanawake kufunika vichwa kwa jambo la kimapokeo (hata kupitia ombi la Paulo kwa Mwanzo 1-3), ambapo kwa wakati huo huo, sura hii inadai mipaka ya Paulo kuhusu wanawake ndani ya kanisa kama kanuni ya zama zote. Ni huu ukosefu wa ufanano ambao husababisha masumbufu mengi katika fasiri. Mjadala ulio bora na ulio mfupi wa jambo hili lililo na mkanganyiko na la kihisia ni katika kitabu cha *How to Read the Bible for All Its Worth* na Fee na Stuart, kr. 61-77 au *Gospel and Spirit*, na Gordon Fee.

D. Sura hii inatusaidia kuona kwamba ishara nyingine za kitheolojia na haki lazima ziwekewe mipaka au zikuzwe katika uhusiano wa mapokeo ambayo Mkristo aliyekomaa hujikuta akiwa ndani yake. Kitabu kilichonisaidia katika kulielewa eneo hili ni kitabu cha Gordon Fee na Douglas Stuart, *How To Read the Bible For All Its Worth*, kr. 71-89.

E. Haya ni maelezo ya kale yaliondikwa kuhusiana na Karamu ya Bwana/Ekaristi/Komunyo.

F. Madhumuni ya Karamu ya Bwana

1. umoja na ushirika wa kanisa
2. kudhihirisha uwepo wa Yesu
3. kuithihirisha dhabihu ya Yesu ya kihistoria
4. kuudhihirisha uhusiano wetu mpya na Mungu kupitia Kristo
5. tendo la kutangaza tukio lililopita na ubaadae wa kuja kwa Kristo
6. tukio la umakini wa ibada

Kutokana na kitabu cha Kutoka 1 Kor. 10:16-17 ni dhahiri kwamba Paulo aliutazama zaidi uzoefu huu kuliko ishara tu au ukumbusho (kama vile 1 Kor. 11:24-25). Hata hivyo, dhana hii haikuboreshwa. Bila shaka Yohana 6:41-71 (ingawa hakuna cho chote katika muktadha wa sasa kinachohusiana na Chakula cha Bwana ) ni kipengele cha umoja huu wa kiroho. Ukristo ni uhusianao wa imani binafsi ya msingi na Mungu wa Utatu.

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : 1 WAKORINTHO 11:2-16**
**2Basi nawasifu, kwa sababu mmenikumbuka katika mambo yote, nanyi mmeyashika yale mapokeo vile**
**vile kama nilivyowatolea. 3Lakini nataka mjue ya kuwa kichwa cha kila mwanamume ni Kristo, na kichwa cha**
**mwanamke ni mwanamume, na kichwa cha Kristo ni Mungu. 4Kila mwanamume, asalipo, au anapohutubu,**
**naye amefunikwa kichwa, yuaaibisha kichwa chake 5Bali kila mwanamke asalipo, au anapohutubu, bila**
**kufunika kichwa, yuaaibisha kichwa chake; kwa maana ni sawasawa na yule aliyenyolewa. 6Maana**
**mwanamke asipofunikwa na akatwe nywele. Au ikiwa ni aibu mwanamke kukatwa nywele zake au**
**kunyolewa, na afunikwe. 7Kwa maana kweli haimpasi mwanamume kufunikwa kichwa, kwa sababu yeye ni**
**mfano na utukufu wa Mungu. Lakini mwanamke ni utukufu wa mwanamume. 8Maana mwanamume**
**hakutoka katika mwanamke, bali mwanamke katika mwanamume. 9Wala mwanamume hakuumbwa kwa ajili**
**ya mwanamke, bali mwanamke kwa ajili ya mwanamume. 10Kwa hiyo imempasa mwanamke awe na dalili ya**
**kumilikiwa kichwani, kwa ajili ya malaika. 11Walakini si mwanamke pasipo mwanamume, wala mwanamume**
**pasipo mwanamke, katika Bwana. 12Maana kama mwanamke alitoka katika mwanamume, vile vile**
**mwanamume naye huzaliwa na mwanamke; na vitu vyote asili yake hutoka kwa Mungu. Hukumuni ninyi**
**wenyewe katika nafsi zenu. 13Je! Inapendeza mwanamke amwombe Mungu asipofunikwa kichwa? 14Je! Hayo**
**maumbile yenyewe hayawafundishi ya kwamba mwanamume akiwa na nywele ndefu ni aibu kwake? 15Lakini**
**mwanamke akiwa na nywele ndefu ni fahari kwake. Kwa sababu amepewa zile nywele ndefu ili ziwe badala**
**ya mavazi. 16Lakini mtu ye yote akitaka kuleta fitina, sisi hatuna desturi kama hiyo, wala makanisa ya Mungu.**

**11:2** Kutokana na uelewa wa sura zilizotangulia, mtu anaweza kushangaa ikiwa hii ni dhihaka au kejeli. Kanisa hili halikuyakumbuka maneno ya Paulo na pia halikuyafuata mafundisho yake (kama vile 1 Kor. 11:17,22). Inawezekana kuwa hili ndilo swali lingine ambalo kanisa liliandika kumhusu Paulo.

**NASB "mmeyashika yale mapokeo vile vile kama nilivyowatolea"**
**NKJV "mmeyatunza yale maagizo"**
**NRSV "mnayashikilia yale maagizo"**
**TEV "mnayafuata yale mafundisho"**
**NJB "mnafuata yale maelezo"**

Hii ni KAULI TENDAJI ELEKEZI YA WAKATI ULIOPO. Yawapasa waamini kwendelea kuzing'ang'ania zile kweli ambazo Paulo alihubiri (kama vile 2 The. 2:15). Huu ni ulinganifu wa kimaagano kwa ajili ya uteuzi.
Hili neno "mapokeo" (*pardosis*) linatumika katika maana kadhaa:

1. katika 1 Kor. 11:2,23; 15:3 kwa maana ya kweli za injili
2. katika Mt. 15:6; 23:1na kuendelea; Marko 7:8; Gal. 1:14 kwa maana ya mapokeo ya Kiyahudi.
3. katika Kol. 2:6-8 kwa maana ya makisio ya ki-Mafunuo
4. Wakatoriki wa Kirumi (watu wenye imani kamili wa Mashariki na Russia) wanautumia mstari huu kama uhakiki wa maandishi ya kibiblia ya Maandiko na Mapokeo ya kanisa kuwa sawa katika mamlaka

5. katika mazingira haya andiko hili linarejelea juu ya kweli ya ki- Mitume, aidha iliyozungumzwa ama iliyoandikwa (kama vile 2 The. 3:6)

◙ **"yale mapokeo"** Habari nyingi zilizomhusu Yesu zilienea kwa njia ya masimulizi kutoka mtu mmoja hadi mwingine hadi pale zilipoandikwa yapata miaka 30 hadi 60 baada ya kifo chake.

◙**"vile vile kama nilivyowatolea"** Kuna dhihaka ya Kiyunani kati ya neno "mapokeo" (*paradoseis*) na neno "kutolea" (*paredōka*), ambayo yote yanaunda neno *paradidōmi*. Paulo si mwanzilishi, bali kiungo tu katika mfululizo wa ufunuo. Hili neno"mapokeo" lilitumika kwa ajili ya kweli zile za Mkristo kupitia mtu mmoja hadi mwingine (kama vile 1 Kor. 11:23; 15:3).

Paulo alizipokea habari zihusozo injili kutokana na vyanzo kadhaa.

1. hotuba ya Stefano (kama vile Matendo 7)
2. Wakristo aliowatesa (kama vile Matendo 8:1-3; 9:1-2; 22:4,19)
3. Anania (kama Matendo 9:10-18)
4. Wakati alipokuwa na Kristo huko Arabuni (kama vile Gal. 1:11-17)
5. Wakati alipokuwa Yerusalemu akiwa na Petro na Yakobo kama vile Gal. 1:18-19)
6. Barnaba (kama vile Matendo 9:20-27; 11:25-26)

**11:3 "Kristo ndiye kichwa"** Katika Fasiri hii *1 and 2 Corinthians,* uk. 103, F. F. Bruce anadai kwamba katika muktadha huu neno *kephalē* linafuatia neno la Kiebrania *rosh* katika maana ya Asili au chanzo. Hii maana ya neno *kephalē* haikuandikwa katika misamiati ya maneno ya Kiyunani na:

1. Bauer, Arndt, Gingrich, Danker
2. Moulton, Milligan
3. Louw, Nida
4. Moulton

Hili linaonyesha namna muktadha (yaani, 1 Kor. 11) unavyobainisha ufafanuzi, si kamusi. Katika muktadha huu neno "chanzo"au "halisi" linakuwa sawa na 1 Kor. 11:3 katika uhusiano na Mwa. 1:26-27; 2:18 (kama vile Kaiser, Davids, Bruce, na Brauch, *Hard Sayings of the Bible*, kr. 599-602).

Yesu alikuwa mwakilishi wa Baba katika uumbaji (kama vile Yohana 1:3,10; 1 Kor. 8:6; Kol. 1:16; Ebr. 1:2). Wanadamu, wanaume na wanawake, waliumbwa na yeye, kwa mfano wake. Hata hivyo, huyo Mwana ni mnyenyekevu kwa Baba (kama vile 1 Kor. 3:23; 11:2; 15:28). Huu ni unyeyekevu dhahiri unaosambaa kwa wanaume na wanawake. Wote wameumbwa kwa mfano wa Mungu (kama vile Mwa. 1:26-27), lakini kuna mpangilio, mwanamme kwanza, kisha wanawake (kama vile Mwa. 2:18) kulingana na kazi husika (angalau katika mfumo wa familia au ukoo unaoongozwa na mwanamme), lakini si usawa! Angalia Mada Maalum ifuatayo.

**MADA MAALUM: KICHWA *(KEPHALĒ)* (SPECIAL TOPIC: HEAD *(KEPHALĒ)***

◙ **"kichwa cha mwanamke ni mwanamume"** Haya maneno "mwanamme" na "mwanamke" yanaweza kumaanisha mke na mme (kama vile NRSV, TEV). Katika muktadha huu sio msistizo uliokusudiwa, bali mpangilio wa uumbaji ulioakisiwa katika Mwanzo 2.

◙ **"na kichwa cha Kristo ni Mungu"** Hii ni kweli iliyorudiwa katika 1 Wakorintho (kama vile 1 Kor. 3:23; 11:3; 15:28). Huo mpangilio ulio ndani ya Utatu haufanyi kitu cho chote katika hali ya kutokuwepo usawa, bali mgawanyo wa kazi. Kweli hii pia inaweza kudokezwa kutokana ma mjadala wa mke na mme. Mapatano haya kwa hakika yalikuwa yalikuwepo kabla ya lile anguko katika Mwazo 3. Makubaliano yanarejeshwa katika urejesho wa uhusiano wa mwamini na Baba kupitia kwa Mwana (yaani, Yesu ameurejesha ufanano huu kwa waamini wote wanaume na wanawake).

**11:4**

**NASB "Kila mwanamume, asalipo, au anapohutubu, naye amefunikwa kichwa,. . . yuaaibisha kichwa chake”**

**NKJV "Kila mwanamume anayeomba au kutabiri, kichwa chake kikiwa kimefunikwa, hakiheshimu kichwa**

**kichwa chake"**

**NRSV "Kila mwanamume anayeomba au kutabiri akiwa na kitu fulani kichwani pake yuaabisha kichwa chake"**

**TEV "Basi , kila mwanamume anayesali au anayetangaza ujumbe wa Mungu huku akiwa amefunika kichwa chake, huyo anamdharau Kristo "**

**NJB "Kila mwanamume aombaye au kutabiri akiwa amfunika kichwa chakehuyu anaonyesha kuwa hakiheshimu kichwa chake"**

Hii ni dhihaka inayozungumzia neno "kichwa." Matumizi ya pili ya neno "kichwa" yanamrejelea Kristo (kama vile TEV). Paulo anashughulika na mapokeo ya Kirumi ambayo miundo yake na ishara zake ni kinyume na mapokeo ya Kiyahudi (yaani, wanaume kufunika vichwa vyao). Jambo lililosawa si yule anayefunika kichwa chake, bali ile ishara ya (1) uhalisia au (2) unyenyekevu, ambao wote ni muhimu kitheolojia.

Imependekezwa kwamba hali ya kihistoria katika Korintho:

1. kijamii, kisiasa, na viongozi wa kifedha wanaoongoza kwa kufunika vichwa ili kujitofautisha na watu
2. kwamba Wayahudi wanapokuwa ndani ya sinagogi katika Korintho wanawake wavae vilemba na Wayahudi walioamini walitarajiwa kufanya vile vile ndani ya kanisa

Kuna mvutano wa kitheolojia kati ya mstari huu, ambao unaonekana kukiri juu ya wanawake katika kazi ya uongozi katika ibada za hadharani wenye kukubaliwa kijamii juu ya kufunika vichwa kwa kulinganishwa na 14:34-35, ambapo wanawake (au hasa "wake," 1 Kor. 11:35) wanazuiwa kuzungumza ndani ya kanisa.

Baadhi ya makundi yalihakiki sura ya 11, ambapo mengine yalitumia sura ya 14. Lazima iboreshwe kwamba ufunguzi wa kifungu hiki ni mpangilio wa mapokeo ya Korintho ya karne ya kwanza, lakini yenye kipengele maalum ambacho si dhahiri kwetu katika zama hizi. Kanisa la karne la ya kwanza liliufahamu uongozi wa wanawake katika Agano la Kale na lilikuwa na utambuzi uliohusu Paulo kuwatumia wanawake katika huduma yake (kama vile Warumi 16). Hawa walilielewa suala hili katika Korintho na mapokeo ya Kirumi tusivyoyaelewa. Mfumo wa imani unaowekwa kuliongoza kanisa fulani haifai!

Kitabu kipya, *After Paul Left Corinth: The Influence of Secular Ethics and Social Change*, na Bruce W. Winter, kr. 121-141,kinatoa baadhi ya utambuzi wa ndani sana kutokana na fasihi na sanaa ya Kirumi. Kitabu hiki na nakala zingine (yaani, E. Fantham, "The 'New Woman': Representation and Reality," katika *Women in the Classical World*, sura ya 10, na P. W. J. Gill, "*The Importance of Roman Portraiture for Head Coverings* katika 1 Corinthians 11:2-16," TynB 41.2 (1990): kr. 245-260 na "*In Search of the Social Elite in the Corinthian Church*," TynB 44.2 (1993): kr. 323-337), zinaonyesha fasiri mpya namna Korintho ya karne ya kwanza ilivyokuwa ya Kirumi, na si ya Kiyunani, katika mapokeo.

Kwa hizi tambuzi mpya zilizoandikwa kutokana na karne ya kwanza ya Korintho ya Kirumi, inawezekana kuanza kwa kuona masuala ya kimapokeo aliyoyatazamia Paulo katika kitabu hiki.

1. Paulo haelezi kuhusu mapokeo ya Kiyahudi katika muktadha huu hata kidogo.
2. Paulo anaeleza juu ya makundi mawili ya kijamii yenye hadhi ya kielimu.
   a. kundi la wenye mali, wasomi wa kijami, waamini wanaume waliokuwa wakizilingia nafasi zao kwa kufunika vichwa vyao wakati walipokuwa wakiongoza ibada za hadharani, kama ilivyokuwa desturi kwa dalaja hili la kijamii, wakati wa kuongoza ibada za kidini zenye tabia za Kiyunani na Kirumi. Hawa walijivuna.
   b. kundi la wenye mali, wake za wale wasomi walikuwa wakiviondoa vilemba vya yale mapokeo yaliyotarajiwa ili kuuonyesha asawa wao, si katika Kristo pekee, lakini pia kama usemi wa kijamii, kama walivyokuwa wanawake wengine wa Kirumi wa wakati huo.
3. Wazawa wa Korintho ya Kirumi, ambao walikuwa wadadisi kuhusiana na imani ya ki- Kristo na zile taratibu za ibada, wangelituma "wajumbe" (yaani, yule malaika wa 1 Kor. 11:10 anaweza kurejea juu ya wahudumu au wale wawakilishi waliotumwa badala ya wale mabwana) ili kulikagua kusanyiko.

Hii habari ya kihistoria/kimapokeo na ya kijamii inatengeneza maana nzuri ya ugumu ulio mwingi na walakini wa andiko. Pia hii ina ulinganifu na maandiko mengine yaliomo katika 1 Korintho, ambayo kwa uwazi yanaakisi karne ya kwanza ya kipekee, Mazingia ya Korintho!

**MADA MAALUM: WANAWAKE NDANI YA BIBLIA (SPECIAL TOPIC: WOMEN IN THE BIBLE)**

**11:5 "Bali kila mwanamke asalipo, au anapohutubu"** Kwa mkazo hii inamaanisha kwamba kwa kichwa chake kilichofunikwa anaweza kusali au kutabiri awapo katika kusanyiko. Hili neno "kutabiri" katika kitabu hiki limamaanisha"kushirikishana injili" au "kuhubiri hadharani" (kama vile 1 Kor. 14:39). Mistari ya 4 na 5 ina ufanano unahusiana na kile wanachokifanya wanaume na wanawake pale wanaposhiriki katika ibada za makundi. Angalia **MADA MAALUM: UNABII WA AGANO JIPYA (SPECIAL TOPIC: NEW TESTAMENT PROPHECY)** katika 1 Kor. 14:1.

◙ **"bila kufunika kichwa, yuaaibisha kichwa chake"** Korintho ilitawaliwa na Kirumi na iliyafuata utamaduni wa Kirumi. Wanawake wa Kirumi walikuwa wakiolewa katika umri mdogo. Vile vilemba vilikuwa moja wapo ya kipengela cha kiutamaduni cha majukumu ya ndoa. Hiki kilemba kilitarajiwa kuvaliwa na wanawake wa Kirumi nje ya makazi yao. Kutokuwepo kwake kuweza kuonekana kama

1. mwanamke mwenye kujiaibisha
2. kahaba
3. mshiriki mwongozaji wa usagaji (mapenzi ya jinsia moja)
4. mwanamke "mpya" (yaani, umoja wa wapigania haki na uhuru miongoni mwa jamii ya Kirumi katika karne ya kwanza)

Mwanamke ambaye angeweza kujivuna katika hali hii angeweza kumwaibisha mmewe hadharani na kufikiriwa tofauti kulihusu kanisa kwa wale waliokuwa wageni na jumuiya kwa ujumla. Yesu huwafanya wanaume na wanawake kuwa huru, lakini kila mtu anao wajibu wa kuweka mipaka ya uhuru wake kwa ajili ya Kristo. Wanawake na wanaume, wake kwa waume walio waamini wanaitwa kwa ajili ya kuishi maisha yenye afya na kukua katika Ufalme! Hii ndiyo dhamira ya 1 Korintho 8-10 na mwendelezo wake katika sura ya 11.

◙ **"ni sawasawa na yule aliyenyolewa"** Hii ni KAULI TEGEMEZI ENDELEVU YA WAKATI ULIOPO. Kuna uwezekano wa kukielewa kifungu hiki kama .

1. chenye kurejea juu ya vazi maaum la kikahaba
2. kama tendo la kidesturi la kumwaibisha mbele ya umati mwanamke mzinifu
3. hii ilionyesha kwamba wanawake walioaibishwa walikuwa kichocheo katika ulimwengu wa ki-Mediterania kwa wafuasi wa zile "Dini za Siri"
4. hii inarejea juu ya tendo la kidesturi lisilotarajiwa la wanawake wa ki- Kristo wanyoao nywele zao na kuwa fupi sana ili kuuonyesha uhuru wao mpya (yaani, mwelekeo wa kidesturi katika karne ya kwanza ya Kirumi na makoloni yake)

Katika uchaguzi wa fasihi zilizo nyingi #1 imekaziwa. Inadaiwa kwamba hii lazima irejelee juu ya hekalu la makahaba la Diana. Hata hivyo, hekalu hili la Acropolis lilihalibiwa na tetemeko la ardhi yapata miaka 150 kabla ya kipindi cha Paulo na hakuna ushahidi wa kihistoria unaothibitisha kwendelea kufanya kazi kwa hekalu hili. Pia hakuna ushahidi kwamba wale makahaba katika Uyunani walikuwa wamenyoa nywele zao.
Swali la ufunguzi ni "Ni mada gani anayoitolea maelezo Paulo?"

1. vazi la ibada lilnalokubalika au la kidesturi na matendo
2. matumizi mabaya ya uhuru binafsi
3. uhusianno unaokubalika baina ya
   a. wanaume na wanawake
   b. waume kwa wake
   c. malaika na wamawake (1 Kor. 11:10)
   d. desturi na wanawake (1 Kor. 11:13)

Nimekuja kuuelewa #1 kama uchaguzi ulio bora zaidi, unaelezea kuhusu wote waume na wake wasioongozwa na uhuru wao katika Kristo, bali ukaidi wao kwa kuweka kando nyadhifa zao za kidesturi na kazi katika kuujenga umoja na ukuaji wa kanisa.

**11:6 "asipo. . . ikiwa"** Hapa kuna VIFUNGU VYENYE MASHARTI DARAJA LA TATU viwili ambavyo vidhahaniwa kuwa kweli kufuatia mtazamo wa mwandishi au kulingana na kusudi lake. Kulikuwa na wanawake wa ki-Kristo

waliokaidi kufunika vichwa vyao, lakini walihitajika kuwa watendaji katika kuziongoza ibada. Kijamii ilikubalika. Yawapasa waamini kuweka mipaka ya uhuru wao mpya katika Kristo kwa

1. wale walio wanyonge ndani ya kanisa (kama vile Rum. 14:1-15:13)
2. matarajio ya kidesturi ya jamii ambayo kanisa linayahitaji kwa ajili ya kuyahubiri na kuyaambatanisha

**NASB "asipofunika kichwa chake"**
**NKJV " asipofunikwa"**
**NRSV "asipojifunika kwa kilemba"**
**TEV "asipofunikwa kichwa chake"**
**NJB "aendaye pasipo kilemba"**

Data za kihistoria kuhusiana na matumizi ya ufunikaji wa uso (yaani, vilemba) au kujifunika kuanzia kichwani hadi mebagani tendo lilifanywa na watu wa kale wa Mediteranea linasaidia sana. Nimethibitisha ule ushahidi wa kale katika nukuu ya 1 Kor. 11:4. Wanawake wa Kirumi waliokuwa katika ndoa, si walio wajane, na si kahaba, kidesturi walitarajiwa kuvaa vilemba katika mkusanyiko kama alama ya kuwa wanandoa. Katika kipindi cha ulimwengu wa Mediteranea ya kale Kulikuwa na wanawake wachache sana walioishi pasipo ndoa.

Katika desturi za Kiyahudi kitambaa cha kufunika uso kilitumika kama alama ya

1. Ukoma, Law. 13:45
2. Kuomboleza kwa ajili ya yule aliyekufa, Eze. 24:17,22
3. fedheha, Mika 3:7
4. Ndoa, Mwa. 24:65
5. ukahaba, Gen. 38:14-15

Hata hivyo, kumbuka Paulo hairejelei juu ya desturi za Kiyahudi hata kidogo kwa sababu katika desturi za kipindi kile wanaume walifunika vichwa vyao wakati wa kuabudu.

◙ **"na akatwe nywele"** Hii ni KAULI YA KATI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPOITA USIOTIMILIFU. Hili halikumaanisha kwamba andiko hili lichukuliwe kiuhalisia. Paulo hazungumzii kuhusiana na wanawake wa ki-Kristo kuaibishwa hadharani, bali anaweka mkazo juu ya matokeo ya desturi kwa shughuli isiyofaa!

◙ **"na afunikwe"** Hii ni KAULI YA KATI SHUTUTISHI YA WAKATI ULIOPO. Wanawake wa ki- Kristo walio kwa ajili ya Kristo huzitii desturi zinazotazamiwa ili kuwafikiwa watu kwa wokovu na washirika wa kanisa. Hii miundo itabadili desturi hadi desturi na zama hadi zama! Lengo litabaki pale pale (kama vile Mt. 28:18-20; Luka 24:47; Matendo 1:8).

**11:7 "yeye ni mfano na utukufu wa Mungu"** Hii inarejelea Mwa. 1:26-27, bado katika muktadha wa mstari huu wa Mwa. 1:26 hili neno "mwanamume" ni jumuishi. Kitheolojia ni yumkini kabisa kwa kile "mfano na ufanano" kinachorejelewa katika Mwa. 1:26-27. Wasomi wengi wangeweza kulihusianisha andiko hili na hulka ya mtu, kujitambua, mtazamo wa kimaadili, uwezo wa kuchagua, uwezo wa kuhusianisha kwa wengine "wenyewe." Kuna makubaliano dhahiri kati ya wanaume na wanawake pote katika Mwa. 1:26-27 na 2:18. Tatizo linatokea katika Mwa. 3:16! Angalia MADA MAALUM: UTUKUFU *(AGANO LA KALE)* (SPECIAL TOPIC: GLORY *(OT)* katika 1 Kor. 2:7.

**11:8**
**NASB "Maana mwanamume hakutoka katika mwanamke, bali mwanamke katika mwanamume"**
**NKJV "kwa maana mwanamume hatokani na mwanamke, bali mwanamke anatokana na mwanamke"**
**NRSV "naam, mwanamume hakutoka kwa mwanamume, bali mwanamke alitokana na mwanamke"**
**TEV "kwa kuwa mwanamume hakutoka kwa mwanamke, bali mwanamke alitoka kwa mwanamume"**
**NJB "kwa sababu hiyo mwanamume hakutoka katika mwanamume; hakuna mwanamke ambaye hakutokana na mwanamume"**

Hili neno "tokana na" halipatikani katika maandishi ya Kiyunani. Hiki ni KIWAKILISHI pekee *ek* (yaaani, nje ya), kama ni 1 Kor. 11:12. Paulo anautetea mpangilio wa uumbaji katika 1 Kor. 11:7 na 9 kutoka Mwanzo 2 (yaani, Adamu kwanza, kisha Eva). Hata hivyo katika 1 Kor. 11:8-9,11, Paulo anayatetea makubalinao yao anatetea utegemezi (ambao unadokezwa katika Mwa. 1:27 na 2:18).

**11:9 "mwanamume hakuumbwa kwa ajili ya mwanamke"** Yatupasa kukumbuka kwamba usemi wa Paulo katika Gal. 3:28 unaohusiana na usawa wa wanawake haupunguzi utofauti wa uumbwaji kati ya hizi jinsia, hasa katika zama hizi. Usawa kamili wa wanaume na wanawake katika Kristo hauondoi matarajio ya ile kazi ya kiutamaduni. Waamini (waume kwa wake) hawajivunii uhuru binafsi, unaoweza kuiathiri hadhi ya kanisa miongoni mwa desturi zile za wasio amini. Waamni wasiokomaa huweka mipaka ya uhuru wao katika Kristo kwa ajili ya Ufalme wake. Waamini wana jukumu la pamoja kwa ajili ya (1) ule mwili wa Kristo na (2) jamii ile ya wasio amini!

**11:10 "Kwa hiyo imempasa mwanamke awe na dalili ya kumilikiwa kichwani"** Hili andiko, kama yalivyo maandiko mengine yote katika muktadha huu, laweza kueleweka katika njia kadhaa. Swali la ufunguzi ni kwamba neno "kumiliki" (yaani, *exousia*) linawakilisha nini?

Kwanza, yatupasa kukumbuka kwamba neno *exousia* mara nyingi linahusiana na neno *dunamis*. Otto Betz anayo makala yenye kuvutia kuhsiana na neno *exousia* katika *New International Dictionary of New Testament Theology*, juzuu 2, kr. 606-611. Hapa kuna mifano mitano.

> "Hii ni kawaida kwa Agano Jipya kwamba neno *exousia* na *dunamis* yote yanahusiana na kazi ya Kristo, matokeo ya mpangilio mpya wa miundo ya nje yenye nguvu na kuwawezesha waamini" (uk. 609).
>
> "Hili neno *exousia* linawahusu wale waaminio. Kumilikiwa kwa mwani wa ki-Kristo kunapatikana katika Kristo na kunyang'anya madaraka yote. Hili linadokeza vyote yaani uhuru na huduma" (uk. 611).
>
> "Huyu yuko huru kufanya lo lote lile (1 Kor. 6:12; 10:23 *exestin*); dai hili, ambalo lilitengenezwa hapo awali na wale wenye shauku ya kimadhehebu huko Korintho, lilichukuliwa na Paulo ambaye alilikiri kuwa sahihi" (uk. 611).
>
> "Katika hali ya utendaji, hata hivyo, uhuru huu usio na mipaka kwa kanuni unaongozwa na ule wema ulio na msaada kwa Wakristo binafsi wengine na kutaniko kama utimilifu katika wazo kwamba ukombozi kamili bado unakuja (1 Kor. 6:12; 10:23)" (uk. 611).

"'Mambo yote ni halali [*exestin*] kwangu,' lakini si mambo yote yanayosaidia. 'Mambo yote ni halali [*exestin*],' lakini si mambo yote yenye kujenga. Mtu asiyatafute mazuri kwa ajili yake mwenewe, bali mazuri kwa ajili ya jirani yake" (1 Kor. 10:23 na kuendelea). Nukuu iliyo ndani ya nukuu hizi yumkini ni kauli-mbiu ya waasherati wa huko Korintho. Paulo anawakabili kwa kukubaliana na ukweli wao, lakini kwa kuonyesha kwamba si yote yaliyo ya kweli" (uk. 611).

Mara nyingi Paulo anayatumia maneno haya mawili katika nyaraka zake kwa kanisa la huko Korintho.

1. *exousia*, 1 Kor. 7:37; 9:4,5,6,12 (mara mbili) ,18; 11:10; 2 Kor. 13:10
2. *dunamis*, 1 Kor. 1:18; 2:4,5; 4:19,20; 5:4; 15:24,43; 2 Kor. 4:7; 6:7; 8:3 (mara mbili); 12:9; 13:4 (mara mbili)

Haki na nguvu yalikuwa mambo makuu kwa makundi yote yaani kwa wanasheria na waasherati. Paulo anajitahidi kutembea katika mstari ulionyooka baina ya mipaka yote. Katika muktadha huu waamini wa ki-Kristo wanasisitizwa kuukubali mpangilio wa Mungu uliotolewa (yaani, mwanamue-mwanamke-wa ki- Kristo) kwa kusudi la ukuaji wa Ufalme. Paulo anatetea makubaliano halisi (kama vile Mwa. 1:26-27; 2:18) katika mistari ya 11-12. Kitheolojia ni hatari sana kufanya haya

1. kuuweka kando mstari mmojawapo katika muktadha huu
2. kutumia mifumo isiyobadilika ya kimadhehebu yasiyobadilika katika jambo la mahusiano ya wanaume na wanawake/waume kwa wake ya karne ya kwanza kwa kila desturi katika kila karne
3. kuukosa ulinganifu wa Paulo kati ya uhuru wa Mkristo na jukumu la agano la ushirika wa Mkristo

Je! ni wapi wanawake wa ki-Kristo waliupata uhuru wa kushiriki kama viongozi katika kusanyiko (yaani, nyumba-kanisa) la ibada? Kwa hakika uhuru huu hakutoka katika sinagogi. Je! mwelekeo wa kidesturi kutokana na karne ya kwanza ya jamii ya Kirumi? Kwa hakika hii inawezekana na kwa mawazo yangu hii inasaidia kuelezea vipengele vingi vya sura hii. Hata hivyo, pia inawezekana kwamba ile nguvu ya injili, urejesho wa "ufananano wa Mungu" halisi iliopotezwa katika Anguko, ni chanzo. Kuna usawa mpya wenye kushtua katika maeneo yote ya maisha ya

mwanadamu na jamii. Lakini usawa huu unaweza kugeuzwa katika matumizi mabaya ya uhuru na kwa matumizi mabaya binafsi. Upanuzi huu usiokubalika ndio unaoelezwa na Paulo.

F. F. Bruce, *Answers to Questions*, kwa ukweli amenisaidia kufikiri kupitia mambo yenye uelekeo wa ubishi yaliyohusiana na desturi za kanisa la sasa la Ukristo wa mashariki. Kama ulivyo ufafanuzi wa maandiko mara nyingi nimekuwa nikifikiri kwamba wanawake kufunika vichwa kulimaanisha kuonyesha vipawa vya ki-Mungu (au ule usawa wa pande mbili wa Mwa. 1:26,27), si mamlaka ya waume zao. Hata hivyo, nisingeweza kuipata fasiri hii miongoni mwa vyanzo vya kibiblia nilivyovitumia, kwa hiyo, nilikuwa nikisita kuliweka hili katika fasihi au kulihubiri/kulifundisha. Bado nakumbuka msisimko na uhuru niliouhisi pale F. F. Bruce alipofikiria juu ya kitu kile kile (angalia *Answers to Questions*, uk. 95). Nafikiri waamini wote wanaitwa, kwa wakati wote, wahudumu wa Kristo waliokirimiwa!

◙ **"kwa ajili ya malaika"** Kuna mionekano ya aina tatu ya fasiri ya aya hii ambayo inahusiana na malaika.

1. kwamba yale marejeleo yanahusiana na malaika kama wawakilishi wa Mungu ambao wanakuwa katika huduma za ibada zetu kama waangalizi, 1 Kor. 4:9; 1 Tim. 5:21; Zab. 138:1; na pia Magombo ya Kale ya Bahari ya Chumvi
2. kwamba hawa ni malaika waovu wenye shauku ya ki-uasherati sawa na wale malaika wa Mwa. 6:2; 2 Pet. 2:4; na Yuda 6; hawa malaika wanatajwa mara kwa mara katika 1 Wakorintho (kama vile 1 Kor. 4:9; 6:3; 11:10; 13:1)
3. tafsiri ya neno *aňgelous* kama "wajumbe" badala ya "malaika"

Haya maneno yanayohusu mjumbe na malaika ni yale yale katika lugha zote ambazo ni Kiebrania (yaani, *malak*) na Kiyunani (yaani, *aňgelos*). Nadharia hii imeegamia juu ya tamaduni za jamii ya karne ya kwanza (kama vile Bruce W. Winter, *After Paul Left Corinth*, kr. 133-138). Mtu mwenye wadhifa asingeliweza kulitembelea kanisa la nyumbani pasipo kumtuma mtu wa kulikagua kusanyiko kwanza. Hili linajenga maana zaidi kuliko kujaribu kuiunganisha Kor. 11:10 na malaika wa tamaa au wale malaika wanaohusika na heshima (kama vile Zab. 138:1) katika ibada ya kusanyiko.

**11:11-12** "**Walakini si mwanamke pasipo mwanamume, wala mwanamume pasipo mwanamke, katika Bwana"** Mistari hii inasistiza juu ya makubaliano baina ya wanaume na wanawake (kama vile Mwa. 1:26-27; 2:18; Gal. 3:26-29).

Uhuru huu (yaani, ule unarudi katika ule mfano halisi wa uumbaji wa Mwa. 1:26-27) lazima ufafanuliwe katika njia zinazofaa ndani ya desturi za yule aliyeanguka. Hakuna mashaka juu ya ukiri wa Paulo kuhusiana na ukombozi wa Yesu unaobadilisha hadhi ya kila mwamini kwa ujumla! Sisi sote ni wamoja katika Kristo. Lengo letu ni kuwasaidia wale majirani na wazawa walionguka ili waupate ukombozi kama huu. Katika kila mapokeo bado kuna mambo ya kijamii. Kwa kuwa waamini wanaweza, hii haimaanishi kwamba lazima iwe hivyo!

Matumizi ya neno "kutoka" (yaani, *ek*, kifasihi "nje ya") katika muktadha huu (mara mbili) yanaonekana kusistiza matumizi ya neno "kichwa" kama "msingi." Mwanamke yuko nje ya mwanamme; mwanamme yuko nje ya Mungu. Masimulizi ya hiki kitabu cha Mwanzo pia yanatupatia msingi wa neno "kichwa" kama mpangilio sahihi wa uumbaji. Vipengele vyote yaani uhuru katika Kristo na unyenyekevu (kama vile Efe. 5:21) vinafaa pale mambo ya kanisa yaliyo mazuri yanapokuwa na lengo la kudumu.

**11:13-15** Paulo analitumia wazo hili hili katika 1 Kor. 10:15 ambapo lingekuwa la kejeli, ambayo imejikita katika matumizi haya ya neno "watu wenye akili" (kama vile 1 Kor. 4:10; 2 Kor. 11:10), lakini hapa wazo hili halionekani kama lenye kejeli kwa kiasi fulani li katika maana ya "kufikiri kidesturi." Paulo anawatumia Wakorintho wa tabia ya Kiyunani na Kirumi/miiko ya karne ya kwanza.

1. Wanawake walio katika ndoa yawapasa kufunika vichwa vyao wawapo katika umati au wawapo katika matendo ya ibada (1 Kor. 11:13).
2. Vijana waliokuwa Korintho walinyoa nywele zao katika kipindi cha kuuelekea utu uzima (yaani, katika miaka kumi). Kufuga nywele ndefu ilikuwa alama ya kimapokeo ya kutaka hali ya kike au ubasha (1 Kor. 11:14).
3. Wanawake waliokuwa na nywele fupi walitambuliwa kama
    a. yule aliye fedheheshwa mbele ya umati

b. kahaba (1 Kor. 11:15).

Hapa hakuna utambuzi wa ndani wa kiroho wala utambuzi wa ndani wa kibiblia (yaani, hawaendi sawa na desturi za Kiyahudi), bali utambuzi wa ndani wa kidesturi.

**11:13 "Ninyi wenyewe"** Mstari ni wa KIMKAZO.

**11:14-15 "akiwa. . . akiwa"** Hizi haya zote ni SENTENSI ZENYE MSHARTI DARAJA LA TATU, ambazo zinazungumzia tendo lililo mahimu.

Tafsiri mbalimbali za Kiingereza zinaiweka mistari hii katika mfumo wa (ma) swali (yaani, NRSV, NJB); maelezo (yaani, NASB, TEV); au swali moja na usemi mmoja (yaani, NKJV). Hiki kishirikishi kinachomaanisha swali katika 1 Kor. 11:14 chenye kudokeza swali ambalo linatarajia jibu la "ndiyo".

**11:16 "akitaka"** Hii ni SENTENSI YENYE MASHARTI DARAJA LA TATU ambayo inadhaniwa kuwa ya kweli kutokana mtazamo wa mwandishi au makusudi yake ya kiuandishi. Kulikuwa na Wakristo wabishi katika kanisa la huko Korintho.

**NASB "ye yote akitaka kuleta fitina"**
**NKJV "yule aonekanaye kuwa na fitina"**
**NRSV "ye yote aliye tayari kuleta ushindani"**
**TEV "mtu anataka kuleta ubiushi juu ya jambo hili"**
**NJB "ye yote akitaka kuwa mwenye mabishano"**

Hiki KITENZI ni KAULI TENDAJI ELEKEZI YA WAKATI ULIOPO, ambayo inadokeza tendo endelevu. Hali hii yenye kuleta ubishi ni mtazamo endelevu kwa wanaume. Hawa wanapenda migogoro na mashindano!

Hili neno "fitina" ni kiambatishi cha neno *philos* (yaani, upendo) na *veikos* (yaani, mashindano). Lilitumika kwa Mitume katika Karamu ya Mwisho katka Luka 22:24.

◙ **"sisi hatuna desturi kama hiyo, wala makanisa ya Mungu"** (kama vile 1 Kor. 11:4:17). Paulo hawapatii kitu cho chote kilicho muhimu (kama vile 1 Kor. 4:17; 7:17; 11:16; 14:33). Hili kanisa lilijitukuza katika hekima na uhuru wake. Wao walifikiri kuwa walikuwa na haki ya kuishi tofauti na makanisa ya Wakristo wengine. Paulo anadai kuwa wasingefanya hivyo!

◙**"kanisa"** Angalia Mada Maalum: Kanisa (*ekklesia*) katika 1 Kor. 1:2.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : 1 WAKORINTHO 11:17-22**
**[17]Lakini katika kuagiza haya, siwasifu, ya kwamba mnakusanyika, si kwa faida bali kwa hasara. [18] Kwa maana kwanza mkutanikapo kanisani nasikia kuna faraka kwenu; nami nusu nasadiki; [19] kwa maana lazima kuwapo na uzushi kwenu, ili waliokubaliwa wawe dhahiri kwenu. [20]Basi mkutanikapo pamoja haiwezekani kula chakula cha Bwana; [21]kwa maana kila mmoja hutangulia kutwaa chakula chake katika kule kula; hata huyu ana njaa, na huyu amelewa. [22]Je! Hamna nyumba za kulia na kunywea? Au mnalidharau kanisa la Mungu, na kuwatahayarisha hao wasio na kitu? Niwaambieni? Niwasifu? La! Siwasifu kwa ajili ya hayo.**

**11:17** Paulo anaanza na dhana mpya, lakini kwa mtazamo wa baadhi ya waamini wa ki-Korintho wenye majisifu wanaendelea katika matazamio haya. Hii dhana hubadilika, lakini tatizo la msingi halibadiliki.

1. imani yao ya kuliamini tabaka la wasomi kama lenye mamlaka ya kutawala
2. msistizo wao wa uhuru binafsi
3. fikra zao za hekima

Dhana zote alizozieleza Paulo (kama vile 1 Kor. 7:1,25; 8:1; 16:1), ambazo ziliwasilishwa kwake kwa njia ya barua, zinazungukia pale pale na katika mambo yale yale.

Hata sikukuu yao ya upendo iliyojumuishwa (kama vile Yuda 1:12) iliyobadilishwa katika sikukuu "zaidi kwangu! Haki, uwezo, na upendo wenye majivuno ya kiwadhifa, huduma, na afya ya Mwili.

◙ **"siwasifu"** Paulo amekubaliana nao katika 1 Kor. 11:2, lakini katika eneo hili ameweza kuwakaripia tu.

◙ "**mnakusanyika**" Mstari huu ni neno ambatani la Kiyunani *sunerchomai.* Paulo anavipenda sana viambatanishi vya neno *sun*. Hiki KIHUSISHI kimsingi kinamaanisha "pamoja na." Neno hili linawakilisha wazo lile lile kama sinagogi, ambalo linarejelea juu ya mkusanyiko wa waamini wa jumla. Sura za 11-14 zinajikita na ibada za kusanyiko (kama vile 1 Kor. 11:17,18,20,33,34; 14:23,26).

Nashangaa ni jinsi gani huu mstari "kusanyika" ilivyofanya kazi. Inaonekana katika Korintho kulikuwa na makanisa ya nyumbani kadhaa na tofauti tofauti, bila shaka hiki ndicho chanzo cha baadhi ya makundi madogo madogo yenye matengano. Je! hapa Paulo anadokeza kwamba makanisa yote ya nyumbani yanakusanyika kwa furaha kwa ajili ya Karamu ya Bwana?

**11:18 "kwanza mkutanikapo"** Kifungu hiki cha maneno kinaweza kueleweka katika njia mbili.

1. la kwanza lililo muhimu (NKJV)
2. la kwanza kati ya yale mawili au mambo yaliyo zaidi, hata hivyo, hakuna neno "pili," n.k. lililotajwa katika muktadha huu
3. sifa nyingine ya kisarufi inapatikana katika Rum. 1:8

◙ **"kuna faraka kwenu"** Hizi faraka kwanza zimetajwa katika 1 Kor. 1:10-17 na 3:3-4, lakini uwepo wake unadhaniwa katika kitabu kizima. Katika muktadha huu faraka haiko kwa viongozi, bali imeelezwa kwa sababu za kijamii na kiuchumi. Hii inaweza kutoa ufafanuzi wa yale makundi madogo madogo ya utengano kama yenye kuwakilisha matabaka ya kijamii pamoja na msistizo wa kitheolojia.

**11:19**
**NASB, NKJV "kwa maana lazima kuwapo na uzushi kwenu "**
**NRSV "naam lazima kuwepo na faraka miongini mwenu"**
**TEV "(maana lazima fikra tofauti ziweko kati yenu"**
**NJB "ya kwamba lazima kuwapo makundi tofauti miongoni mwenu"**

Kutokana na hili neno "uzushi" (1 Kor. 11:19, yaani, chagua), tunalipata neno la Kiingereza uasi. Asili yake ya msingi ni "kuchagua" au "kuteua," lakini lenye kuongezwa maana nyingine ya kuonyesha upendeleo maalum, kuchagua moja na kuyaacha machaguo mengine (kama vile Matendo 24:14; 1 Kor. 11:19; Gal. 5:20). Hili linaweza kutumika katika kubainisha (1) yule mtu anayeamini mafundisho ya uongo (kama vile Tito 3:10) au (2) mafundisho ya uongo yenyewe (kama vile 2 Pet. 2:1).

Kuna maneno tofauti tofauti yanayotumika katika 1 Kor. 11:18, "faraka" (yaani, *schisma*), ambapo tunalipata neno la Kiingereza farakano. Asili yake ya msingi ni "kutapanya" (kama vile Mt. 27:51). Hili lilitumika kwa yale makundi yaliyogawanyika kutokana na jambo fulani (kama vile Yohana 7:43; 9:16; 10:19; Matendo 14:4; 23:7; 1 Kor. 1:10; 11:18).

Paulo anaitaja sababu ya kitheolojia (yaani, *hina*) na umuhimu (yaani, *dei*) wa kuwepo kwa haya makundi tofauti. Haya yalikuwa muhimu kwa viongozi wa kiroho kwa ajili ya kufunuliwa kwa uwazi. Viongozi waliokomaa watakuwa kama ushahidi katika nyakati za ghalika.

Uchaguzi mwingine ni kwamba baadhi ya makundi mengine na viongozi wao wataonyesha kwa matendo yao kwamba wao si ya Wakristo hata kidogo (kama vile 1 Yohana 2:19; Marko 4:16-19).

◙ **"ili waliokubaliwa"** Angalia Mada maalum: Maneno ya Kiyunani Yanayotumika kuhusu neno Kujaribu katika 1 Kor. 3:13.

**11:20 "haiwezekani kula chakula cha Bwana"** Hizi faraka za kijamii zilizokuwepo kutokana na nyadhifa za kielimu kwa ujumla zilitenda kazi katika namna isiyojulikana kwa jamii, kujitoa kwa Yesu katika karamu ya mwisho akiwa

na wanafunzi wake. Mistari inayofuatia inabainisha hoja yake (kama vile 1 Kor. 11:22).

◙**"chakula cha Bwana"** Huu ni utokeaji pekee wa kifungu hikicha maneno katika Agano Jipya. Huu ni uwezekano wa mfano mwingine wa kejeli. Hakuna jambo linalohusiana na mitazamo na matendo yao ikilinganishwa na mtazamo wa Yesu na matendo katika kujitoa mwenyewe kwa ajili ya mwanadamu mwenye dhambi!

Tukio la kuabudu huendana na majina kadhaa.
1. chakula cha Bwana
2. "meza ya Bwana" (1 Kor. 10:21)
3. "mkate uliomegwa" (Matendo 2:42; 20:7; 1 Kor. 10:16; 11:24 [kama vile Luka 24:30])
4. utoaji wa shukrani (yaani, *eucharist*) au baraka (yaani, *eulogia*, Mt. 26:26-27; 1 Kor. 10:16; 11:24)

**11:21 "kila mmoja hutangulia kutwaa chakula"** Kanisa la mwanzo liliunganisha chakula cha Bwana na ushirika wa chakula ulioitwa "sherehe ya upendo" (kama vile 2 Pet. 2:13; Yuda 12, na bila shaka Matendo 20:7).

Inawezekana kukielewa kifungu hiki katika njia kadhaa.
1. Wale matajiri/wasomi/walio wa muhimu/waliozaliwa mapema na kwa viwango vya juu na kula mapema ili wale maskini wazaliwapo wasikute cho chote, au kwa ugumu wa kupata cho chote, waliochwa kwa ajili ya kula.
2. Kila mtu ilimpasa kuleta chakula chake mwenyewe. Wale waamini waliokuwa wasomi walikula chakula chao kwa haraka huku maskini wakiwepo, au wale washirika watumwa wa kanisa, walileta chakula kidogo au pengine kukosa kabisa.

Tatizo lilikuwa ubinafsi na uchoyo uliojikita katika tofauti za kijamii badala ya pendo la kujitolea, kama matendo ya Yesu na ule mfano dhahiri alioutoa. Kanisa la Korintho halikuenenda kama kitu kimoja katika Kristo. Wao walikuwa kiini cha pande mbili kinzani kati ya

1. wale walionavyo kijamii dhidi ya wasiokuwa navyo
2. matajiri dhidi ya maskini
3. wanaume dhidi ya wanawake
4. wanaume walio huru dhidi ya watumwa
5. Warumi dhidi ya wengine wote
6. wale walioendelea kiroho dhidi ya muumini wa kawaida

Tofauti hizi zinaelezwa vyema katika 1 Kor. 11:21 na 22.

◙ **"hata huyu ana njaa, na huyu amelewa"** Kwa vyo vyote vile hili lilisababishwa na tofauti za jamii ya Kirumi au ubinafsi, hali isiyo na makubaliano inaonyeshwa wazi. Kusudi la chakula hiki cha ukumbusho na ushirika wa pamoja lilikuwa limesahauulika. Hili lilikuwa jambo la umakini (kama vile 1 Kor. 11:23). Mstari huu hauwezi kutumika kutetea zuio la moja kwa moja. Ni wazi kuwa divai ilikuwa sehemu ya tukio hili. Huu ni uonevu kwamba kuna kushutumiwa.

## MADA MAALUM: MITAZAMO YA KIBIBLIA KUHUSU KILEO NA ULEVI (SPECIAL TOPIC: BIBLICAL ATTITUDES TOWARD ALCOHOL AND ALCOHOLISM)

◙**"Je! Hamna nyumba za kulia na kunywea"** Baadhi ya wanasheria na washika sheria wamejaribu kutumia andiko hili lililohakikishwa kwa ajili ya kutokula kanisani. Historia na muktadha mara nyingi ni muhimu katika fasiri ya fasihi ya kale. Kwa kunukuu sehemu ndogo za Maandikio mtu anaweza kuifanya Biblia/Mungu kuongea cho chote! Kama Gordon Fee asemavyo, katika "*A book that can mean anything, means nothing!*"

Kuna mtiririko wa maswali yasiyohitaji majibu yanayozifunua hisia za Paulo alizokuwa nazo wakati akiandika waraka huu. Yeye anashtushwa na matendo ya baadhi ya wale walioko kanisani (kama vile Yakobo 2:6).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : 1 KORINTHO 11:23-26**
**[23] Kwa maana mimi nalipokea kwa Bwana niliyowapa nanyi, ya kuwa Bwana Yesu usiku ule aliotolewa alitwaa mkate,[24] naye akiisha kushukuru akaumega, akasema, Huu ndio mwili wangu ulio kwa ajili yenu; fanyeni hivi kwaukumbusho wangu. [25] Na vivi hivi baada ya kula akakitwaa kikombe, akisema, Kikombe hiki ni agano jipya katika damu yangu; fanyeni hivi kila mnywapo, kwa ukumbusho wangu. [26] Maana kila mwulapo mkate huu na kukinywea kikombe hiki, mwaitangaza mauti ya Bwana hata ajapo.**

**11: 23 "Kwa maana mimi nalipokea kwa Bwana niliyowapa nanyi"** Paulo hakuwepo katika Chakula cha Bwana. Yeye hudai katika Gal. 1:11-17 kuupokea ufunuo moja kwa moja kutoka kwa Yesu na katika Gal. 1:18-19, si kuupokea kutoka kwa Mitume wengine au viongozi wa Yerusalemu. Hata hivyo, hapa maneno yake yanaaksi yale maarifa ya mapokeo ya dokezo la Injili.

◙**"alitwaa mkate"** Ni muhumu kwamba Yesu hakumtumia Mwana-Kondoo wa Pasaka kama ishara. Hii iliunganishwa na Agano la Kale kwa msistizo (kama vile Kutoka 12). Mkate ulikuwa ishara mpya ya umoja (10:16-17).

**11:24 "naye akiisha kushukuru akaumega, akasema"** Mstari huu unaenda moja kwa moja hadi kwenye tukio maalum la kihistoria (yaani, chakula cha Pasaka katika chumba cha gorofani usiku ule kabla ya Yesu kusalitiwa). Wakristo wengi wanayaita maagizo haya *Ekasti*, ambayo inatokana na neno la Kiyunani "kushukuru" (yaani, *eucharisteō*, kama vile Mt. 26:27; Marko 14:22; Luka 22:19).

**NASB "Huu ndio mwili wangu ulio kwa ajili yenu"**
**NKJV "Chukueni, kuleni; huu ndio mwili wangu unaomegwa kwa ajili yenu"**
**NRSV "Huu ndio mwili wangu, ambao ni kwa ajili yenu"**
**TEV, NJB"Huu ndio mwili wangu, ule ulio kwa ajili yenu"**

Kwa uwazi hii ni ya kistiari. Ulaji wa nyama za watu lingekuwa ni suala la kutisha kwa mtu ye yote wa Kiyahudi. Yesu alitumia mkate uliomegwa kama ishara ya mwili wake uliomegwa huko Kalvari. Kama vile mkate ulivyo chakula cha kimwili na uzima kwa wale waulao, hivyo matendo ya Yesu hutoa uzima wa kiroho kwa wale waupokeao.

Kumekuwa na mjadala wa kitheolojia kuhusiana maana ya maneno ya Yesu. Yaliyo mengi katika mjadala huu yanajikita katika (1) asili ya tukio na (2) njia ambayo Mungu hutumia kutoa neema. Wale wanaoliona hili kama sakramenti wanaitegemea sana Yohana 6, ambapo katika muktadha, hawafanyi lo lote kuhusiana na Karamu ya Bwana.

Kuna tofauti kadhaa za Maandiko ya Kiyunani katika kifungu hiki.

1. Upokeaji wa maandiko unaongeza neno "chukueni, kuleni." Hili linapatikana katika MSS $C^3$, K, L, na Kiyunani na P. Hii si halisi.
2. Kifungu cha Paulo kinachodokeza "kwa ajili yenu" (kama vile MSS $P^{46}$, $א^*$, A, B, $C^*$) kimewekewa upanuzi na wale waandishi wa kale katika njia kadhaa:
   a) "uliomegwa kwa ajili yenu" (kama vile MSS $א^2$, $C^3$, $D^2$, F, G)
   b) "iliyomwagika kwa ajili yenu" (kama vile MS $D^*$)
3. c) "uliotolewa kwa ajili yenu" (kama vile Luka 22:19)

$UBS^4$ inaupa mstari huu mfupi sana daraja "A" (kwa neno *huper humōn*) kama (yumkini).

**11:24-25 "fanyeni hivi kwa ukumbusho wangu"** Kwa vyo vyote vile hii ni KAULI TENDAJI ELEKEZI YA WAKATI ULIOPO au KAULI TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO. Huu <u>ushurutishi</u> unaendana sana na muktadha. Chakula hiki cha kiishara lazima kirudiwe mara nyingi hadi pale Yesu atakaporudi.

Inatia shauku kwamba nukuu ya inayohusu chakula cha Bwana katika Injili ya Mathayo na Marko hiki kifungu "fanyeni hivi kwa ukumbusho wangu" hakikuwekwa. Hata hivyo, kifungu hiki kinaonekana katika Luka 22:19 na 1 Kor. 11:24-25. Pia inashangaza kuwa tukio lenye umuhimu ulio dhahiri katika maisha ya Yesu, ambao ulipaswa kurudiwa, umenukuliwa na tofauti hizi katika Injili na katika maandiko ya Paulo.

Kitabu cha Agano Jipya hakibainishi ni mara ngapi tendo hili linapaswa kurudiwa. Makundi mengine ya waamini hayalifanyi tendo hili kamwe (yaani, kutetemeka), mengine hulifanya tendo hili kwa kila juma. Yale makundi ya ki-Kristo ambayo yana mtazamo wa Karamu ya sakramenti kwa udhihirisho hulifanya tendo hili mara kwa mara (yaani, kwa kila juma) na tukio lenye kiini. Waamini wa kale wa Kipalestina wamelijaribu hili mara moja kwa mwaka na kuliunganisha na Pasaka (yaani, walio maskini, kama vile Origen na Epiphanius). Wale Wakristo walio na mashaka na kuhusiana na taratibu hizi zenye kurudiwa huku wakizipoteza nguvu zao na umuhimu na hawalioni hili kama mwongozo wa neema, mara nyingi wanaichukulia hii Karamu kwa uchache (yaani,washirika wa ki-Baptist waliokutana kila baada ya miezi minne).

**11:25 "Kikombe hiki ni agano jipya"** Hili agano jipya linatajwa kwa upekee katika Yer. 31:31-34 (lililoelezwa katika Eze. 36:22-38). Neno la Kiyunani la neno agano kiuhalisia lilimaanisha "ile ijayo" au "usemi wa mwisho," lakini maana yake hapa inaaksi yale matumizi ya maneno ya Maandiko ya Kale kama "agano."
Dhana ya "agano jipya" lazima ingewashtua watu wa Kiyahudi. Wao waliiamini sheria ya Musa kama agano lenye kudumu. Yeremia anawakumbusha kwamba maagano ya YHWH yalikuwa ya amri juu ya mwitikio wa toba ya imani.

## MADA MAALUM: AGANO (SPECIAL TOPIC: COVENANT)

◙**"katika damu yangu"** Mstari huu unarejelea katika dhana ya Kiebrania ya Kifo cha Yesu kama dhabihu (kama vile 2 Kor. 5:21). Damu ni nahau ya Agano la Kale la Kiebrania inayorejelea juu ya dhabihu iliyotolewa kwa Mungu (kama vile Law. 17:11,14; Kut. 12:23). Agano a kwanza lilithibitishwa kwa umwagaji damu (kama vile Kut. 24:8).

**11:26**
**NASB, NKJV**
**NRSV "Maana kila mnapokula. . .kunywa"**
**TEV "Ya kwamba mlapo kila wakati. . .kunywa"**
**NJB "Kila mlapo. . .kunywa"**

Tazama kwamba hapa hakuna wakati maalumu unaoelezwa, au po pote pale, katika Agano Jipya. Katika Matendo kifungu bainishi chenye kutoa ufafanuzi wa Chakula cha Bwana, "kuumega mkate," kinatumika kwa (1) tukio la kila siku (2:42,46) au (2) ibada ya Jumapili (20:7,11). Hata hivyo, kifungu hiki pia kinatumika katika mlo wa kawaida (27:34-35).

◙ **"mwaitangaza mauti ya Bwana"** Kwa udhihirisho hili linaonyesha kipengele cha kifo cha Yesu kama dhabihu. Chakula cha Bwana ni mrejesho wa nyuma wa kifo cha Kristo.

◙ **"hata ajapo"** Chakula cha Bwana ni matarajio ya Ujio wa mara ya Pili (kama vile 1 Kor. 1:7; 4:5; 11:26; Marko 14:25).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : 1 KORINTHO 11:27-32**
**[27] Basi kila aulaye mkate huo, au kukinywea kikombe hicho cha Bwana isivyostahili, atakuwa amejipatia hatia ya mwili na damu ya Bwana. [28] Lakini mtu ajihoji mwenyewe, na hivyo aule mkate, na kukinywea kikombe. [29] Maana alaye na kunywa, hula na kunywa hukumu ya nafsi yake, kwa kutokuupambanua ule mwili. [30] Kwa sababu hiyo wako wengi kwenu walio hawawezi na dhaifu, na watu kadha wa kadha wamelala. [31] Lakini kama tungejipambanua nafsi zetu, tusingehukumiwa. [32] Ila tuhukumiwapo, twarudiwa na Bwana, isije ikatupasa adhabu pamoja na dunia.**

**11:27**
**NASB, NKJV**
**NRSV "aulaye mkate huu au kukinywa kikombe cha Bwana"**
**KJV "Maana kila mnapokula mkate huu na kunywa kikombe hiki cha Bwana"**
**TEV "Kwa maana kila mlapo mkate wa Bwana huu na kukinywea kikombe hiki"**
**NJB "kwa maana hiyo ye yote aulapo mkate huu kukinywa kikombe cha Bwana"**

"Na" si andiko halisi la 1 Kor. 11:27, bali liko katika 1 Kor. 11:28 na 29. "Au" liko katika maandishi ya Kiyahudi. Watafsiri wa Toleo la King James walikuwa na woga juu ya uelewa wa kanisa Kotoriki la Roma ambapo makuhani walikuwa wakinywa divai na mikate ya walei, na kwa makusudi waliutafsri mstari huu visivyo! Lile toleo la NKJV imekusanya tafsiri hii iliyotafsiriwa visivyo na kwa makusudi (angalia Bart Ehrman, *The Orthodox Corruption of Scripture*, uk. 154).

**NASB, NKJV,**
**NRSV "isivyostahili"**
**TEV "katika hali kutokumheshimu"**
**NJB "isiyofaa"**

Mazingira yanayodokeza hili yanarejelea juu ya umoja wa kanisa uliovurugwa kwa kusababishwa na makundi madogo madogo yenye matengano na majisifu, lakini baadhi waliielewa hili kwa kurejelea katika maagizo kwa ajili ya msimamo thabiti wa kiroho wakati wa kuiadhimisha Karamu ya Bwana (kama vile Ebr. 10:29).

**11:28 "Lakini mtu ajihoji mwenyewe"** Hii ni KAULI TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO. Hili neno "kujihoji" lina maana nyingine ya "kujaribu kwa mawazo yenye uelekeo wa ukubalifu." Angalia Mada Maalum: Maneno ya Kiyunani ya neno "Kujaribu" katika 1 Kor. 3:13. Katika maana moja Wakristo wote hawastahili kwa kuwa wote ni wenye dhambi na wanaendelea kutenda dhambi. Katika muktadha huu neno hili kwa muainisho linarejelea zile roho za matengano na matengano za baadhi ya wale waliokuwa ndani ya kanisa huko Korintho (kama vile 2 or. 13:5).

**11:29**
**NASB "kwa kutokuupambanua ule mwili"**
**NKJV "kukuwa na ufahamu wa mwili wa Bwana"**
**NRSV "bilakutambua maana ya mwili"**
**TEV "msipokufahamu ile maana ya mwili wa Bwana"**
**NJB "pasipokuutambua mwili**"

Neno "Mwili wa Bwana" inaonekana kutokuejelea juu ya (1) umbo-mwili la yesu ama (2) wale washiriki, lakini kanisa kama kundi (kama vile 1 kor. 10:17; 12:12-13,27). Matengano ni tatizo. ile roho ya majikwezo au tofauti za kimadaraja huharibu mahusiano.

◙ **"hukumu"** Angalia katika 1 Kor. 4:7 na Mada Maalum katika 1 Kor. 10:29.

**11:30** Paulo anaeleza katika lugha iliyo wazi kwamba wale waamini wanaovuruga umoja wa kanisa wanaweza kuadhibiwa kwa mateso ya mwili ya mfululizo, na hata kifo (kama vile 1 Kor. 3:17). Moja kwa moja hili linahusiana na ule ukosefu wa heshima kwa mwili wa Kristo, kanisa, watu wa Mungu (kama vile Matendo 5; 1 Kor. 5:5; 1 Tim. 1:20).

**11:31 "kama"** Hii ni SENTENSI SHURUTISHI DARAJA LA TATU, ambayo inaitwa "iliyo kinyume na kweli." Hii inapaswa kutafsiriwa kama "ikiwa tumejihoji kwa usahihi, ambapo hatufanya hivyo, kisha haitupasi kuhukumiwa, vile tulivyo." Angalia maelezo katIka 1 Kor. 4:7.

**11:32 "twarudiwa na Bwana"** Ni vigumu kufahamu lini Wakristo wanateseka kwa sababu

1. wanaishi katika ulimwengu ulioanguka

2. wanavuna matokeo ya matendo ya dhambi zao
3. wanapimwa na Bwana kwa ajili ya ukubalifu wa kiroho (kama vile Ebr. 5:8)

Mungu hujaribu na kurudi (kama vile Ebr. 12:5-11). Huu ni ushahidi wa pendo lake na nafasi ya familia yetu.

◙ **"isije ikatupasa adhabu pamoja na dunia"** Hukumu ya dunia hii ya wale waamini ambao wanaliumiza kanisa la Mungu inaweza kuwa tendo la kiupendo katika kuwapiga kwa hukumu kali zaidi inayohusiana na kuliharibu kanisa (kama vile 1 Kor. 3:10-17).

Naipenda nukuu itokayo kwa George Ladd katika *A Theology of the New Testament*.

"Pia ulimwengu una dini yake ambayo imewashikilia wanadamu katika utumwa wa pamoja na uhalali ambao unaweza kuwa na mwonekano wa hekima na msistizo wenye aina ya uaminifu na nidhamu binafsi, lakini ni kushindwa kwa mwisho kwa ajili ya kuleta suluhisho la shaka la maadili ambalo mwanadamu anakumbana nalo (Kol. 2:20 na kuendelea). Ilivyotazamiwa kutokana na hoja hii ya msingi ulimwengu unasimama chini ya hukumu ya Mungu (1 Kor. 11:32) na uko katika uhitaji wa mapatano (2 Kor. 5:19; Rum. 11:15" (uk. 399).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : 1 KORINTHO 11:33-34**
**33 Kwa hiyo, ndugu zangu, mkutanikapo mpate kula, mngojaneni; 34 mtu akiwa na njaa, na ale nyumbani kwake; msipate kukutanika kwa hukumu. Na hayo yaliyosalia nijapo nitayatengeneza.**

**11:33 "mkutanikapo mpate kula, mngojaneni"** Mstari huu unarejelea katika 1 Kor.11:21. Walikuwa wakitenda kama watu wenye ubinafsi, si kama familia, mwili. Walikuwa wakitenda katika njia iliyo kinyume kutokana tendo la upendo la kwa Yesu.

**11:34 "akiwa"** Hii ni SENTENSI YENYE MASHARTI DARAJA LA KWANZA, ambayo inadhaniwa kuwa kweli kutokana na mtazamo wa mwandishi au kwa makusudi yake ya kiuandishi.

◙ **"na ale nyumbani kwake"** Hii ni KAULI TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO. Ikiwa waamini wana njaa sana kwamba wanatenda katika hali ya ghasia, njia ya ubinafsi kataka Karamu ya Bwana, kisha yawapasa kukidhi njaa yao kabla ya kushiriki katika chakula cha ushirika.

**NASB "Na hayo yaliyosalia nijapo nitayatengeneza"**
**NKJV "na yaliyobakia nitayaweka katika mpangiliao pale nijapo"**
**NRSV "kuhusu yale mambo mengine, nitawapeni maelezo nitakapokuja"**
**TEV "Kwa yale masuala mengine, nitayaamua nijapo"**
**NJB "mambo mengine nitayapanga wakati nitakapokuja"**

Tambua kwamba Mungu hakuona vema kuyapitia maelezo yote ya ndani aliyoyatoa Paulo kwa kanisa hili. Hii haina uhakika kama hili linahusiana na Chakula cha Bwana pekee au mambo mengine. Huu muundo wa 1 Korintho (unajibu maswali mengi yasiyohusiana) unamaanisha kwamba maelezo haya yanafanya kazi. Asili ya Chakula cha Bwana haipatikani katika mwongozo wa kitabu cha kanuni za ibada, bali katika uhusiano na Yesu Kristo. Maelezo ya ndani ya taratibu za kidini si muhimu kama moyo mwema umwelekeao Mungu, ambao unatokana na upendo kwa kanisa.

## MASWALI YA MJADALA

Haya ni maoni ya <u>mwongozo</u> kwa kujisomea, ikiwa na maana kuwa unawajibika binafsi kwa tafsiri ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mtoa maoni tu.

Maswali haya ya kujadili yanatolewa kukusaidia mambo muhimu ya kipengele cha kitabu hiki. Yamekusudiwa kukuchokonoa mawazo na sio ya hakika.

1. Je! Wakristo wa sasa wananakili taratibu zote za ibada na miundo ya kanisa la Agano Jipya?
2. Je! Andiko la 11:2-16 linazungumza kuhsiana na ushirikishaji wa wanawake katika zoezi la uongozi katika ibada ya hadhara?
3. Je! Vilemba vinafananishwa na nini katika zama hizi?
4. Toa ufafanuzi kuhusu matatizo ya wanawake wasiofunika vichwa vyao na wanaume waliofunika vichwa vyao katika desturi za karne ya kwanza ya Kirumi.
5. Nini kusudi kuu la Paulo katika kujadili Karamu ya Bwana katika 11?
6. Unafafanuaje 1 Kor. 11:30?

# 1 WAKORINTHO 12

| MGAWANYO WA AYA WA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| UBS[4] | NKJV | NRSV | TEV | NJB |
| | | | | Staha katika Ibada ya Hadharani (11:2-14:40) |
| Karama za Kiroho | Karama za Kiroho Umoja katika Namna Tofauti | Namna Tofauti za Karama za Kiroho | Karama kutoka kwa Roho Mtakatifu | Karama za Kiroho |
| 12:1-3 | 12:1:11 | 12:1-3 | 12:1 | 12:1-3 |
| | | | 12:2-3 | Tofauti Anuwai Na Umoja wa Karama |
| 12:4-11 | | 12:4-11 | 12:4-11 | 12:4-11 |
| Mwili Mmoja Wenye Viungo Vingi | Umoja na kutofautiana Ndani ya Mwili mmoja | Mwili unahitaji Viungo vingi | Mwili Mmoja Sehemu Nyingi | Mshabihiano wa Mwili |
| 12:12:31a | 12:12:31 | 12:12-13 | 12:12-13 | 12:12-17 |
| | | 12:14-26 | 12:14-20 | |
| | | | | 12:18:21 |
| | | | 12:21-26 | |
| | | | | 12:22-26 |
| | | | 12:27-31a | |
| | | | | 12:27-30 |
| | | | 12:31b | |

**MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI** (Kutoka **"Mwongozo wa Usomaji Mzuri wa Biblia"A Guide to Good Bible Reading")**

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Haya ni maoni ya mwongozo kwa kujisomea, ikiwa na maana kuwa unawajibika binafsi kwa tafsiri ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mtoa maoni tu.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa,lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

21. Aya ya kwanza
22. Aya ya pili
23. Aya tatu
24. N.k

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA 12:1-31

A. Sura ya 11-14 inaunda sehemu moja ya fasihi inayoshugulika na ibada ya kusanyiko. Kulikuwa na matatizo mengi katika makanisa ya nyumbani ya Korintho. Paulo anaeleza mengi miongoni mwa maswala haya, ambayo kwa uwazi kabisa kanisa lilikuwa limemwandikia kuhusu maswala hayo (kama vile 1 Kor. 7:1,25; 8:1; 12:1; 16:1,12). Maswala yanayohusu ibada ya kusanyiko yalikuwa:
   1. namna ya kuomba na kutoa unabii
      a. mwanaume kutokufunikwa kichwa
      b. mwanamke kufunikwa kichwa
   2. kiburi na kutumia vibaya karama za roho
   3. namna ya kuzitumia karama katika ibada
      a. wanenaji wa lugha na watafsiri
      b. waimbaji
      c. manabii

B. Kuna vipimo vitatu vinavyohusiana na karama za kiroho.
   1. sura ya 12 – je zinatia hamasa umoja wa kumfanya Kristo kuwa kiini cha ibada?
   2. sura ya 13 - je zinatia hamasa upendo?
   3. sura ya 14 – je zinaujenga mwili?

C. Kuna orodha kadhaa za karama za roho katika Agano Jipya (kama vile Rum. 12; 1 Kor. 12-14; Efe. 4:11; na 1 Pet. 4:10-11). Orodha sio za aina moja, wala mpangilio ama utaratibu wa karama sio ule ule. Zipo sampuli wakilishi, si orodha hitimishi. Baadhi ya karama hutenda kazi katika kusanyiko la ibada ya nje.
   Msisitizo ambao Paulo anaweka kuhusu kukirimiwa karama hizi za roho ni wa kunashangaza, lakini anasema kidogo kuhusu jinsi mtu anavyopata au anavyotambua karama yake. Ninachelea kuthibitisha wingi wa "vipimo vya kiroho" ambavyo vimeendelezwa katika siku zetu. Hivi vimepimwa tu kwa karama zilizo orodheshwa katika Agano Jipya. Karama nyingi zilizoorodheshwa hazijafafanuliwa kwa uwazi. (yaani, karama za kiuongozi katika Efe. 4:11). Mwongozo niliupata kwenye eneo hili ambao unasaidia sana ni kile kijitabu cha *Affirming the Will of God* na Paul Little. Hekima ile ile ya Kikristo inayotusaidia kujua mapenzi ya Mungu pia hutusaidia kutazimbua karama zetu tendaji katika huduma.
   1. omba kwa ajili ya swala maalumu
   2. uliza Wakristo waliokomaa wanaokufahamu wakwambie ni nguvu zipi wanaoziona ndani yako
   3. tafuta milango iliyofunguliwa upate fursa na jaribu maeneo tofauti tofauti
   4. fuata kiu ya moyo wako

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO (LILILOBORESHWA) LA NASB 1 WAKORINTHO 12:1-3**
**[1] Basi, ndugu zangu, kwa habari ya karama za roho, sitaki mkose kufahamu. [2] Mwajua ya kuwa mlipokuwa watu wa Mataifa, mlichukuliwa kufuata sanamu zisizonena, kama mlivyoongozwa. [3] Kwa hiyo nawaarifu, ya kwamba hakuna mtu anenaye katika Roho wa Mungu, kusema, Yesu amelaaniwa; wala hawezi mtu kusema, Yesu ni Bwana, isipokuwa katika Roho Mtakatifu.**

**12:1"kwa habari"** Hiki ni kifungu kinachorudiwa rudiwa katika 1 Wakorintho kinachoonyesha kwamba Paulo anajibu maswali mahususi kutoka kanisa hilo (kama vile 1 Kor. 7:1,25; 8:1; 12:1; 16:1,12).

**NASB, NKJV "karama za Roho"**
**NRSV "watu wa kiroho"**
**(Rejeo/tanbihi)**
**TEV "karama kutoka kwa roho mtakatifu"**
**NJB "karama za Roho"**

Neno la Kiyunani ni KIMILIKISHI CHA UWINGI cha *pneuma*. Hii yaweza kuhusu watu, karama, ama U-kiroho (yaani, mambo ya Kiroho, kama vile 1 Kor. 14:1).

**MADA MAALUM: ROHO KATIKA BIBLIA (SPECIAL TOPIC: SPIRIT IN THE BIBLE)**

◙**"ndugu zangu"** Paulo mara nyingi hutumia neno "ndugu zangu" kuonyesha badiliko kwenye masomo. Aya hii ya kwanza ina alama la kimkutadha tatu za Paulo juu ya badiliko la somo: (1) sasa kwa habari ya; (2) ndugu zangu; na (3) sitaki mkae bila kujua. Sura 11-14 inashugulika na vipengele tofauti tofauti vya ibada ya waliokusanyika.

Jumbe ambazo Paulo alizituma Korintho zilikuwa ngumu kiasi kwamba mara nyingi alitumia "ndugu zangu" kuwakumbusha umoja wao katika familia ya Mungu (kama vile 1 Kor. 1:10,11,26; 2:1; 3:1; 4:6; 6:5,8; 7:24,29; 5:12; 9:5; 10:1; 11:2,33; 12:1; 14:6,20,26,39; 15:1,6,50,58; 16:11,12,15,20; 2 Kor. 1:8; 8:1,23; 9:3,5; 11:9; 13:11).

◙**"' sitaki mkose kufahamu'"** Hiki ni kifungu ambacho kinajirudia rudia katika maandiko ya Paulo (kama vile Rum. 1:13; 11:25; 1 Kor. 10:1; 11:3; 12:1; 2 Kor. 1:8; 1 The. 4:13). Ilikuwa moja ya njia zake za kutambulisha mada mpya yenye umuhimu.

**12:2"mlipokuwa watu wa Mataifa"** Hii ni KAULI YENYE KUARIFU ISIOTIMILIFU. Hawa waaminio huko nyuma walikuwa wapagani, lakini lazima wajue namna hii ya kufikiri utendaji unaohusika na fikra hizo. Kanisa la Korintho lilikuwa limeathiriwa sana na uendeshaji wa (1) ibada za kipagani (2) Utamaduni wa Kirumi. Yote mawili yalikuwa yanailemba injili katika njia zisizostahili.

**NASB "kama mlivyoongozwa"**
**NKJV "mlichukuliwa. . .hata hivyo mliongozwa"**
**NRSV "mlitawaliwa na kupotoshwa "**
**TEV "mlikuwa mmepotoshwa kwa njia nyingi"**
**NJB "mlikuwa mmevutwa kwa njia isiyozuilika"**

Kifungu hiki kina vitenzi viwili vinavyoshabihiana kutoka mzizi wa neno"kuongoza." Cha kwanza ni KAULI ISIOTIMILIFU TENDWA ELEKEZI YENYE MAFUMBO na ya pili ni KAULI TENDWA ENDELEVU YA WAKATI ULIOPO, "mlikuwa na mliendelea kuongozwa."

Neno lingine pia limetiwa nguvu na KIHUSISHI *apo*, kinachomaanisha "kuongoza kama mfungwa" (kama vile Marko 14:44; 15:16). Hawa wapagani wa zamani wamekuwa wakiendelea kutawaliwa na mapepo katika uendeshaji wa ibada yao (kama vile 1 Kor. 10:20) kabla ya kuongoka kwao.

◙**"sanamu zisizonena"** Hii inahusu miungu ambayo haikuweza kuzungumza au kusaidia (kama vile Isa. 46:5-7; Yer. 10:5; Hab. 2:18-19) kinyume na Roho mtakatifu.

**12:3 "hakuna mtu anenaye katika Roho wa Mungu"** Hii ni nahau ya Kiebrania kwa neno uvuvio (kama vile 1 Sam. 10:10; 19:23-24). Hii inawakumbusha waaminio kwamba sio anayedai kunena kwa ajili ya Bwana anafanya hivo kweli. Kila aaminiye lazima awatathimini wale wanaodai kunena ujumbe wa Mungu (kama vile 1 Kor. 12:10; Kumb. 18:20-22; Mathayo 7; 1 Yohana 4:1-3).

**NASB "Yesu analaaniwa"**
**NKJV "amwita Yesu amelaaniwa"**
**NRSV "acha Yesu awe amelaaniwa"**
**TEV, NJB "laana juu ya Yesu"**

Hii ni kauli ya kutisha. Kwanini mtu yeyote isipokuwa (Wayahudi wa kimapokeo) anayedai kunena kwa niaba ya Mungu aseme haya? neno (yaani, *anathema*) lenyewe lilikuwa na asili ya Agano la Kale (yaani, Waebrania, *herem*). Inahusiana na dhana ya vita takatifu, ambapo mji uliwekwa wakfu kwa Mungu, kwahiyo ukawa mtakatifu (kama vile Yos. 6:17; 7:12).

Nadharia ya jinsi neno hili lilivyotumiwa katika Korintho ni

1. kwamba ulikuwa mpangilio wa Kiyahudi uliohusiana na viapo vya sinagogi (kama vile Matendo 26:11, Yaani, baadaye, laana za dini ya Kiyahudi zilitumika kuwaondoa Wakristo ndani ya Sinagogi). Ili kuendelea kuwa mwanachama ilimbidi mtu kumkataa ama kumlaani Yesu wa Nazareti.
2. kwamba ulikuwa na muundo wa Kirumi uliohusiana na kumwabudu mfalme ambapo ni Kaisari pekee aliyeweza kuitwa "Bwana."
3. kwamba palikuwapo na muundo wa ibada ya kipagani ambapo laana zilitamkwa juu ya watu kwa kutumia jina la mungu yeyote. Hii lingaliweza kutafsiriwa "Bwana na akulaani—" (kama vile 1 Kor. 16:22).
4. Kwamba mtu Fulani alihusisha hicho kifungu na dhana ya kitheolojia ya Yesu kubeba laana ya Agano la Kale kwa ajili yetu (kama vile Kumb. 21:23; Gal. 3:13).
5. tafiti za karibu kutoka Korintho (kama vile maelezo ya chini ya ukurasa #1 uk. 164 katika Bruce Winter's *After Paul Left Corinth*) anavithibitisha vibao venye laana maeneo ya kale katika mji Korintho. wataalamu wa Biblia wamechukuliwa kwamba KITENZI, "(kama zilivyo baadhi ya laana katika tafasiri za kale za Kiyunani (LXX) ya Kumb. 22:15-20), kama ilivyo 1 Kor. 12:3. Upo ushahidi zaidi toka maeneo ya zamakale kwamba Wakristo katika Korintho ya Warumi ya karne ya kwanza walitumia utaratibu wa laana katika laana za maziko (yaani, kipindi cha Byzantine), zilizopatikana kwenye makaburi ya Wakristo (J. H. Kent, *The Inscriptions*, 1926-50. Princeton: *American School of Classical Studies,* 1966, juzuu. 8:3, na. 644).

Vikundi vingine vya kanisa vilikuwa vinarejea tena kwenye laana za kipagani kwa jina la Yesu dhidi ya washirika wengine wa kanisa. Sio tu kwa njia ya tatizo, lakini pia kwa sababu ya chuki. Huu ni mfano mwingine wa mvutano ndani ya kanisa. Paulo anawataka kulijenga kanisa, kuliimalisha kanisa. Wao wanataka kulaani sehemu ya kanisa!

**MADA MAALUM: LAANA SPECIAL TOPIC: CURSE *(ANATHEMA)***

◙**"Yesu ni Bwana"** Huu ndio ulikuwa ukiri wa kanisa la kwanza wa imani (kama vile zote mbili Rum. 10:9-13 na Matendo 2:21 zinamnukuu 2:33; pia angalia Flp. 2:11). Ilikuwa njia ya kuuthibitisha Uungu wa Yesu na Umasihi.

◙**"isipokuwa katika Roho Mtakatifu"** Jukumu la Roho Mtakatifu ni kuuhukumu ulimwengu kwa dhambi na kuwavuta watu kwa Kristo (kama vile Yohana 16:8-14). Hakuna binadamu aliyeanguka anaweza kumgeukia Mungu au Yesu bila kupewa msaada (kama vile Yohana 6:44,65). Hilo ndilo fumbo la Mungu mkuu anayewapenda wanadamu wote walioumbwa kwa mfano wake. Mbali ya agano lake ni kwamba lazima waitikie (na kuendelea kuitikia) katika imani, utii, kutumika, na kustahili!

**ANDIKO (LILILOBORESHWA) LA NASB 1 WAKORINTHO 12:4-11**
[4] **Basi pana tofauti za karama; bali Roho ni yeye yule.** [5] **Tena pana tofauti za huduma, na Bwana ni yeye**
**yule.** [6] **Kisha pana tofauti za kutenda kazi, bali Mungu ni yeye yule azitendaye kazi zote katika wote.** [7] **Lakini**
**kila mmoja hupewa ufunuo wa Roho kwa kufaidiana.** [8] **Maana mtu mmoja kwa Roho apewa neno la hekima;**
**na mwingine neno la maarifa, apendavyo Roho yeye yule;** [9] **mwingine imani katika Roho yeye yule; na**
**mwingine karama za kuponya katika Roho yule mmoja;** [10] **na mwingine matendo ya miujiza; na mwingine**
**unabii; na mwingine kupambanua roho; mwingine aina za lugha; na mwingine tafsiri za lugha;** [11] **lakini kazi hizi**
**zote huzitenda Roho huyo mmoja, yeye yule, akimgawia kila mtu peke yake kama apendavyo yeye.**

**12:4-6**
**NASB, NRSV "aina mbali mbali"**
**NKJV "anuwai"**
**TEV "aina tofauti tofauti"**
**NJB "tofauti"**

Neno linamaanisha (1) kugawanya (2) aina mbali mbali (kama vile 1 Kor. 12:4,5,6). Kuna mfanano wa kifasihi ulio dhahiri kati ya 1 Kor. 12:4,5, na 6, ambao unaunganisha kazi ya watu wote watatu wa Utatu (tazama Mada Maalum katika 1 Kor. 2:10).

**12:4-6 "Roho. . .Bwana. . .Mungu"** Angalia utendaji ambao Utatu unahimiza umoja miongoni mwa aina anuwai, na sio zenye kufanana. Kanisa ni kundi la watu waliopewa vipawa. Tunahitajiana! Kila mmoja ni wa muhimu. Kila mmoja amepewa vipawa lakini dhana ni ya kibiblia. Neno "Utatu" sio neno la kibiblia lakini dhana ni ya kibiblia. Angalia Mada Maalum: Utatu katika 1 Kor. 2:10.

**12:4 "karama"** Hili neno ni tofauti kuliko lile lililotumika katika 1 Kor. 12:1. Hili ni neno la Kiyunani *charisma*. Hili linatoka kwenye mzizi wa neno "*chairō,*" linamaanisha kufurahi au kujaa furaha (kama vile 1 Kor. 7:30; 13:6; 2 Kor. 2:3; 6:10; 7:7,9,16 na mchanganyiko wa neno *sun* katika 1 Kor. 12:26 na 13:6). Kutoka hapo zinaendelezwa dhana kadhaa.

1. *chara* – furaha, kufurahia
2. *charis* – karama ya ukarimu (kama vile 1 Kor. 16:3; 2 Kor. 8:4,6)
   a. neema (kama vile 1 Kor. 1:4; 15:10)
   b. shukrani (kama vle 1 Kor. 15:57)
3. *charizomai*
   a. toa kwa ukarimu
   b. samehe (kama vile 2 Kor. 2:7-10; 12:13)
   c. futa deni
4. *charisma* – karama ya bure (kama vile Rum. 5:15,16; 6:23; 2 Kor. 1:11) au kutunuku upambaji wa ki-Ungu (kama vile 1 Kor. 12:4,9,28,30,31)

Mungu ametoa karama kwa Kanisa lake. Karama zipo kwa kuujenga na kuukuza mwili wa Kristo. Kwa kweli kazi ya Kristo imegawanywa miongoni mwa wafuasi wake. Waamini lazima waunganishe karama zao na upendo na ushiririkiano na kila mmoja ili kwamba kanisa liweze kuupata ulimwengu uliopotea na kuwafanya kuwa wanafunzi (kama vile Mt. 28:19-20; Luka 24:47; Matendo 1:8).

**12:5 "huduma"** Hili ni neno la Kiyunani *diakonos*. Lina matumizi kadhaa kwenye Agano Jipya.

1. *diakonos*
   a. mtumishi (kama vile Mt. 20:28; 22:13; 23:11; Yohana 2:5)
   b. mhudumu/mhubiri (kama vile 1 Kor. 3:5; 2 Kor. 3:6; 6:4; 11:15[mara mbili],23)
2. *diakoneō*
   a. kuhudumu (kama vile 1 Pet. 4:11)
   b. Shemasi (kama vile Rum. 16:1; 1 Tim. 3:8,10,13; pia nukuu Flp. 1:1)
   c. tawala (kama vile Matendo 6:2; 2 Kor. 3:3; 8:19,20)
3. *diakonia*
   a. kutoa msaada (kama Matendo 6:1; 2 Kor. 8:4; 9:1,12,13)
   b. huduma kwa injili (kama vile 1Kor. 12:5; 16:15; 2 Kor. 4:1; 5:8; 6:3; 11:8)
   c. ufunuo kutoka kwa Mungu (kama vile 2 Kor. 3:7,8,9)

Wazo kuu ni kuwatumikia na kuwashauri wengine wenye mahitaji (yaani, kiroho na kimwili). Mungu huliandaa kanisa lake kuhudumiana wenyewe na kuhudumia ulimwengu uliopotea na wenye uhitaji.

**12:6**
**NASB "kutenda. . .kazi"**
**NKJV "shughuli. . .kazi"**
**NRSV "shughuli. . .shughuli"**
**TEV "aina za uwezo. . .uwezo"**
**NJB "shughuli. . .kazi"**

Huu ni mchezo juu ya neno *nergēs* ambalo kutokana na hilo tunapata neno la kiingereza. Maana yake ya msingi ni kufanya na kukamilisha kazi kwa matokeo stahiki. Sentensi hii ina NOMINO na KIAMBATA kinachofanana (KAULI TENDAJI YA WAKATI ULIOPO). Alitumia neno hili mara nyingi kwenye nyaraka zake kwa Wakorintho.

4. *energēs*, *energeia, energeō, energēma*, 1 Kor. 4:12; 9:6; 12:6,10,11; 16:9,10; 2 Kor. 1:6; 4:12
5. *ergon* and *sunergeō,* 1 Kor. 3:13,14,15; 9:1; 15:58; 16:10; 2 Kor. 6:1; 9:8; 11:15

Kazi ya Mungu ni kazi inayoonyesha matunda. Hukamilisha makusudi yake. Waaminio wanaitwa kwenye utumishi tendaji, lakini nguvu na kupata matokeo ni kazi ya Mungu.

**12:7**
**NASB "lakini kwa kila mmoja umetolewa udhihirisho wa roho kwa manufaa ya wote"**
**NKJV "lakini udhihirisho wa roho umepewa kwa kila mmoja kwa faida ya wote"**
**NRSV "kwa kila mmoja umepewa udhihirisho wa roho kwa faida ya wote"**
**TEV "uwepo wa roho unaooneshwa kwa namna fulani kwa kila mtu kwa faida ya wote"**
**NJB "Udhihirisho mahususi unaotolewa kwa kila mmoja unapaswa kutumia kwa faida ya wote**"

Kweli hii ni muhimu sana kwa uhai na huduma ya kanisa.

1. Kila aaminiye anacho kipawa cha neema kilichotolewa bure alichopewa na Rho kwa ajili ya huduma alipopata wokovu.
    a. Kila aaminiye ni wa muhimu.
    b. Kila aaminiye amekirimiwa vipawa.
    c. Kila aaminiye ni mhudumu/mtumishi.
2. Kusudi la kipawa cha Mungu sio kumwinua mtu, bali ni kwa afya na kukua kwa mwili wote. Kila mmoja wetu anamhitaji mwenzake!

Ukweli huu ulihitajika kwa kila hali na waaminio wenye vikundi vidogo kanisani, wenye kiburi kilichokithiri, wenye siasa kali kwenye kanisa la Korintho (na kila kizazi). Yale "manufaa ya wote" au "faida" (*sumpheron*, kama vile 1 Kor. 6:12; 7:35; 10:33; 2 Kor. 8:10) ni kwa ajili ya mwili na sio mtu binafsi. Waaminio lazima wawajibike kibinafsi kuhifadhi umoja wa roho katika kifungo cha amani (kama vile Efe. 4:2-3). Jambo hili kimsingi liko tofauti sana na ubinafsi wa magharibi.

### MADA MAALUM: UKRISTO NI KITU CHA SHIRIKA SPECIAL TOPIC: CHRISTIANITY IS CORPORATE

**12:8**
**NASB, NKJV "neno la hekima. . . neno la maarifa"**
**NRSV "matamshi ya hekima. . .matamshi ya maarifa"**
**TEV "ujumbe uliojaa hekima. . .ujumbe uliojaa maarifa"**
**NJB "kipawa cha matamshi yanayojulisha maarifa"**

Haya ni maneno mawili tofauti ya Kiyunani, "hekima" (yaani, *sophia*) na "maarifa" (yaani, *gnōsis*). Yanaaksi tofauti ya Kiebrania kati ya "haekima" na "maarifa." La kwanza ni utendaji na la pili ni maelezo sahihi ya fundisho la Kikristo.

**12:9 "imani"** Hii inarejeea sio kwa imani inayookoa kama Marko 1:15; Yohana 1:12, kwasababu karama zinatolewa kwa waaminio tu, bali kwa imani itendayo miujiza, ambayo imewekwa wazi kutoka 1 Kor. 13:2 (kama vile Mt. 17:20; 21:21).

◙**"kuponya"** Neno (*iaomai*) ni WINGI (kama vile 2 Kor. 12:7-9,28,30), ambao katika uhalisia ni "karama ya uponyaji." Uponyaji ni karama ya roho katika muktadha huu na ni huduma ya "wazee" katika Yakobo 5:14. Uponyaji wa mwili ulikuwa ni ushahidi wa upendo wa Mungu na jinsi anavyo tujali na ishara ya uponyaji wa kiroho (yaani, msamaha wa dhambi, wokovu). Kwa Wayahudi kulikuwa na uhusiano kati ya dhambi na ugonjwa, haki na afya (kama vile Kumbukumbu 27-28). Hata hivyo, Ayubu na na zaburi 73 inafafanua swala hili kama inavyofafanua Yohana 9. Kitendawili hapa ni kwa nini wengine wanapona na wengine hawaponi. Imani ya mtu haiwezi kuwa kiambato kikuu bali mapenzi ya Mungu, Kamwe sio kiasi gani cha imani tunachukua bali kusudi la imani yetu. (imani yenye ukubwa wa mbegu ya haladali kuhamisha milima, kama vile Mt. 17:20).

Mshukuru Mungu kwa uponyaji, waponyaji, na makanisa yanayojari wahitaji!

**12:10 "matendo ya miujiza"** Hii inaonekana kwenda sambamba na 1 Kor. 12:9a (yaani, imani itendayo miujiza). Kwa kuwa hii orodha yote haiwezi kufanana kabisa, tofauti halisi haidhihiriki.

◙**"unabii"** Ziko angalau njia mbili za kuelewa neno hili: (1) katika nyaraka kwa Wakorinto hii inaahusu kushirikisha au kutangaza injili (kama vile 1 Kor. 14:1), (2) kitabu cha matendo kinataja unabii (kama vile 1 Kor. 11:27-28; 13:1; 15:32; 21:10, hata manabii wa kike, 21:9).

Tatizo lililo kwenye neno hili ni, karama ya unabii katika Agano Jipya inahusianaje na manabii wa Agano la Kale? Kwenye Agano la Kale manabii ndio waandikaji wa maandiko. Katika Agano Jipya jukumu hili limekabidhiwa kwa wale Mitume kumi na miwili wa kwanza pamoja na wasaidizi wao. Kama neno "Mtume" litabaki kama karama inayoendelea (kama vile Efe 4:11), lakini likiwa na jukumu lililo badilika baada ya kifo cha wale kumi na wawili, basi vivyo hivyo, na hudumaa ya nabii. Uvuvio umekoma, hakuna maandiko zaidi (kama vile Yuda 1:20). Jukumu kuu la manabii wa Agano Jipya, ni kutengeneza injili lakini. Angalia MADA MAALUM: UNABII KATIKA AGANO JIPYA (SPECIAL TOPIC : NEW TESTAMENT PROPHECY) katika 1 Kor. 14:1.

**MADA MAALUM: UNABII WA AGANO LA KALE (SPECIAL TOPIC: OLD TESTAMENT PROPHESY)**

**NASB "kutofautisha roho"**
**NKJV "kupambanua roho"**
**NRSV "upambanuaji wa roho"**
**TEV "uwezo wa kutambua tofauti kati ya karama zitokazo kwa roho ambazo sizo"**
**NJB "uwezo wa kutofautisha roho"**

Vyanzo vitatu vya mtu kupata karama: (1) kwa asili (yaani, vipawa vya asili); (2) kwa roho na kwa; (3) shetani. Karama ni uwezo wa kutofautisha miongoni mwa vyanzo hivi (kama vile 1 Tim. 4:1; 1 Yohana 4:1-3).

◙**"aina za lugha"** Hili ni neno la Kiyunani kwa "ulimi" (yaani, *glōssa*). Hili lilitumika katika Agano la Kale kama kisawe kwa ajili ya “taifa." Katika Kiyunani lilitumika kwa kuzungumza lugha ya taifa. Hii ingemaanisha kwamba ilikuwa na kidokezo cha lugha inayojulikana ya kibinadamu. Hata hivyo hitaji kwa ajili ya mtafsiri ambalo pia ni karama ya roho badala ya mtafsiri,pamoja na mjadala kamili wa Paulo katika sura ya 14, humwongoza mtu kudhani kwamba huu ulikuwa unenaji wenye furaha iliyopitiliza katika Korintho.

Hakika jinsi "lugha" katika Korintho inayofananishwa na lugha siku ya Pentekoste kama ilivyoandikwa katika Matendo ni jambo lisilo thibitika. Muujiza katika Matendo 2 ulikuwa ni wa sikio (kama vile 1 Kor. 2:6,8,11), sio ulimi. Uzoefu wa ndimi katika Matendo uliwasilisha injili moja kwa moja kwa Wayahudi waliokuwa wakiishi nje waliokuwa wamehudhuria. Pia ulitumika kama njia ya kutambua uwepo, nguvu, na mapenzi ya Mungu ya kushirikisha makundi mengine, kama Wasamaria (kama vile Matendo 8) na Cornelius, afisa jeshi wa Kirumi (kama vile Matendo 10). Ilikuwa ishara kwa Wayahudi waaminio kwamba Mungu alikwishaa fungua mlango kwa mataifa nao wanajumuishwa (kama vile 1 Kor. 15:8). Angalia hapana hitaji la mtafsiri katika matendo!

Unenaji wa lugha katika Wakorintho unafanana na na hotuba za kufurahisha za dini ya Kiyunani (mf, Delphi). Unenaji wa Wakorintho unaonekana wazi uilikuwa ukitumiwa vibaya ama zimetukuzwa zaidi (kama vile 1 Kor. 13:1 na 14:1-33). Unenaji ulikuwa njia ya aaminiye kuwasiliana na Mungu, lakini bila kuelewa. Ni karama halali (kama vile. 1 Kor. 14:39), lakini sio kwa ajili ya waaminio wote (Kama vile 1 Kor. 12:29-30, ambayo ina maswali kadhaa yanayotarajia jibu la “hapana"). Sio karama inayothibitisha kwamba mtu ameokoka ama kuonesha mtu Fulani ni wa kiroho. Unenaji pamoja na kutafsiri ilikuwa njia nyingine ya kuwasilisha injili na kuhitajika kwake.

◙**"tafsiri za lugha"** Korintho lilikuwa jiji la watu wa mataifa mengi, la utamaduni wa Kirumi, Jiografia kwa maana ya Kiyunani. Mahali jiji hilo lilipokuwa pamoja na hatari ya kusafiri merikebuni karibu na rasi ya Ugiriki wakati wa baridi ukifanyika mji wa kibiashara kwenye makutano ya barabara za himaya ya Mashariki na himaya ya Magharibi. Kila utaifa ungalikuwa Korintho, lakini lugha zilihitaji karama za kiroho ili wawasilishe ujumbe wake kwa ajili ya kanisa, sio tu mtafsiri. Lugha katika Korintho haikuwa lugha iliyokuwa inajulikana.

**12:11** Aya hii inasisitiza ukweli kwamba roho hugawa kwa kila aaminiye karama ya kuhudumia (kama vile 1 Kor. 12:7,18). Pia ni karama gani ambayo ni chaguo la roho, na sio la aaminiye. Hakuna mfumo wa ngazi, karama zote ni kwa kutumikia mwili wa Kristo. (kama vile 1 Kor. 12:7). Hazipo kama nembo zenye kustahili heshima, bali ni taulo ya mtumishi.

**MADA MAALUM: UBINADAMU WA ROHO (SPECIAL TOPIC: THE PERSONHOOD OF THE SPIRIT**

**ANDIKO (LILILOBORESHWA) LA NASB 1 WAKORINTHO 12:4-11**
**4 Basi pana tofauti za karama; bali Roho ni yeye yule. 5 Tena pana tofauti za huduma, na Bwana ni yeye yule. 6 Kisha pana tofauti za kutenda kazi, bali Mungu ni yeye yule azitendaye kazi zote katika wote. 7 Lakini kila mmoja hupewa ufunuo wa Roho kwa kufaidiana. 8 Maana mtu mmoja kwa Roho apewa neno la hekima; na mwingine neno la maarifa, apendavyo Roho yeye yule; 9 mwingine imani katika Roho yeye yule; na mwingine karama za kuponya katika Roho yule mmoja; 10 na mwingine matendo ya miujiza; na mwingine unabii; na mwingine kupambanua roho; mwingine aina za lugha; na mwingine tafsiri za lugha; 11 lakini kazi hizi zote huzitenda Roho huyo mmoja, yeye yule, akimgawia kila mtu peke yake kama apendavyo yeye.**

**12:12** Hii inaanza na ibara inayotumia uhusiano wa ndani wa mwili wa mwanadamu kama sitiari kwa kanisa (kama vile Efe. 4:4,16). Inasisitiza umoja kwa namna mbali mbali. Mtazamo sio juu ya sehemu yoyote ile, lakini ni katika utendaji kwa ujumla, sio mtu mtu binafsi, bali familia;

Agano la Kale na Agano Jipya yana msisitizo wa kuungana kuwa kundi moja (tazama Mada Maalum katika 1 Kor. 12:7). Hii haimaanishi kushusha ukweli kwamba watu wanakuwa Wakristo katika msingi wa watu binafsi, lakini mara tu mtu anapokuwa Mkristo, mtazamo wakati wote unakuwa ni afya, umoja na mafanikio ya mwili wote!

**12:13 "katika Roho mmoja"** KIHUSISHI (*en*) chaweza kumaanisha "ndani," "pamoja," au "kwa namna ya." Uwe mwangalifu kwenye utumiaji wa VIHUSISHI vya lugha ya kawaida inayozungumzwa katika Uyunani ili kufanya utetezi wa fundisho la kidini. Hii inafanana na Efe. 2:18; 4:4. Roho ndio njia ambayo kwayo Mungu huwahukumu watu kuhusu dhambi, huwavuta kwa Kristo, huwabatiza ndani ya Kristo na humuunda Yesu ndani yao, (kama vile Yohana 16:8-14). Hiki ni zama za Roho. Kazi yake ni ishara kwamba enzi mpya ya haki kimekwisha kuja. Kipawa ni Roho na Roho hugawa vipawa ambavyo vinaaksi jukumu lake la kumfunua Kristo, kuwavuta waliopotea katika Kristo, ndani ya waaminio.

◙**"sote tulibatizwa kuwa mwili mmoja"** Ubatizo wa maji ni sitiari ya uzoefu wa kiroho ambao ulitokea wakati wa kumpokea yesu (kama vile Efe 4:5). Kwa njia kadhaa Efe. 4:4-6 ina ufanano na fungu hili la maneno, Ubatizo huu unahusu wokovu wa kwanza, unaomfanya aaminiye kuwa mmoja ndani ya mwili wa Kristo, ambalo ni kanisa. Kifungu kinachotumika siku hizi mara kwa mara "ubatizo wa Roho Mtakatifu" kinaleta mkanganyiko kwasababu kibiblia kinamhusu mtu anaye mtumainia Yesu kama mwokozi lakini kinatumika leo kwa kutia nguvu, kujitoa, uzoefu wa baadae katika maisha ya waaminio. Sikatai uhalisia wa huu uzoefu wa baadaye, lakini napendelea neno "uzoefu wa u- Bwana." Katika kusoma wasifu wa maisha ya Wakristo wakuu kipengere huibuka: (1) kumwamini Kristo; (2) kujaribu kumtumikia; (3) kushindwa kuzaa matunda yatokanayo na huduma; (4) kuvunjika moyo katika juhudi ya kibinadamu; (5) kujitoa kwenye hitaji la Mungu ili afanye kazi yake mwenyewe; (6) kutiwa nguvu kwa ajili ya huduma; na (7) utukufu wote kwa Mungu, sio chombo cha mwanadamu.

◙**"kwamba tu Wayahudi, au kwamba tu Wayunani; ikiwa tu watumwa au ikiwa tu huru"** Hakuna tena tofauti na mipaka ya kibinadamu kidunia kati ya wale wanaomtumaini Kristo (kama vile Yoeli 2:28 ilinukuliwa na Petro katika Matendo 2:14-36; Gal. 3:27-28; Kol. 3:11). Kweli hii hakika inatetea usawa wa kuondoa tofauti. Waaminio wote ni watumishi walioitwa waliopewa vipawa, lakini Mkristo anaweza kuwa mtumwa bado.

Usawa uliweza kuwa unashtua jamii ya Warumi pale Korintho ambapo mtu alikuwa mwenye mamlaka juu ya (1)mke wake; (2) watoto wake; na (3) na watumwa wa nyumbani kwake. Palikuwepo na ugumu wa ngazi za kijamii. Thiolojia kuu ya Paulo, iliegamia juu ya mafundisho na matendo ya Yesu, kilikuwa ni kielelezo kikuu

kilichobadili na kushangaza mtazamo mpya wa kidunia ambao ulitakiwa kuondolewa katika ushirika wa kanisa (kama vile Efe. 5:18-6:9). Hii hasa hasa ni katika eneo hili kwamba kanisa la Korintho lilikengeuka.

◙**"nasi sote tulinyweshwa Roho mmoja"** Neno hili lilitumika kwenye umwagiliaji maji. Maana yake halisi ilikuwa "kuloanisha ." Hii ilitafsiriwa kama kuhusisha Meza ya Bwana na Augustine, Luther, na Calvin, lakini kwa sababu ya Yohana 7:37-39 inaweza kumrejelea yule Roho. Hii ni sitiari ya umoja na ushirika ulioletwa na wakala mmoja ambaye ni Roho. Maneno yote mawili "batizwa" na "kunyweshwa" ni KAULI TENDWA YENYE KUARIFU YA WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFU, inayomaanisha kazi iliyomalizika muda uliopita. Njeo na ufanano vinaonyesha havirejei kwenye ubatizo wa maji kwa Mkristo na Ushirika Mtakatifu, lakini ni kwa tukio la mtu lililokwisha timia huko nyuma (yaani, kubadilishwa na Roho, yaani, IRABU TENDWA au na Kristo, kama vile. Mt. 3:11; Luka 3:16; Matendo 1:5, au na Baba, kama vile Matendo 2:33).

**ANDIKO LA NASB(LILILOBORESHWA) : 1 WAKORINTHO 12:14-18**

[14] **Kwa maana mwili si kiungo kimoja, bali ni vingi.** [15] **Mguu ukisema, Kwa kuwa mimi si mkono, mimi si wa mwili; je! Si wa mwili kwa sababu hiyo?** [16] **Na sikio likisema, Kwa kuwa mimi si jicho, mimi si la mwili; je! Si la mwili kwa sababu hiyo?** [17] **Kama mwili wote ukiwa jicho, ku wapi kusikia? Kama wote ni sikio ku wapi kunusa?** [18] **Bali Mungu amevitia viungo kila kimoja katika mwili kama alivyotaka.**

**12:14-26** Paulo anatumia mwili wa asili kama mshabihiano kuonyesha uhusiano wa ndani kati ya viungo vya mwili vilivyo vya lazima ili mwili wote ufanye kazi. Kila kiungo kinahitajika kwa ajili ya afya na utendaji wa mwili.

**12:14** Huu ni ukweli wa ki-muhtasari uliorudiwa mara kadhaa katika sura hii (kama vile 1 Kor. 12:12,13,14,20,25,27).

**12:15-16 "Ikiwa. . .ikiwa"** Hizi zote mbili ni SENTENSI YENYE MASHARTI DARAJA LA TATU, zinazoonyesha utendaji usiodhihirika. Aya hizi zinaonyesha hangaiko lililokuwepo sio katikati ya wale, wanavikundi kanisani, bali kuthamini kupita kiasi karama kadhaa za kiroho. Karama zote zatoka kwa Mungu na kuchagua ni vipi ampe kila aaminiye (kama vile 1 Kor. 12:11,18).

**12:17,19 "kama. . .kama"** Hizi ni SENTENSI YENYE MASHARTI DARAJA LA PILI (yaani hakuna KITENZI katika 1 Kor. 12:17 na hakuna kifungu cha kuhitimisha katika zote tatu). Sehemu ya kwanza ni uongo (yaani, mwili wote sio jicho, 1 Kor. 12:17; mwili wote sio sikio, mst, 17; na mwili wote sio kiungo kimoja, 1 Kor. 12:19, kama vile A. T. Robertson, *A Grammar of the Greek New Testament In Light of Historical Research*, kur. 1015,1023 and *Short Grammar of the Greek New Testament*, uk. 166).

**12:18 "Mungu amevitia"** Hii ni KAULI YA KATI ELEKEZI YA WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFU, Ambayo inamaanisha tendo muhimu. Katika 1 Kor. 12:11 Roho anasemekana kugawa karama. Huu ni utambulisho dhahiri wa Roho kama mwenye Uungu! Angalia Mada Maalum katika 1 Kor. 2:11.

◙**"Mungu amevitia viungo kila kimoja katika mwili kama alivyotaka"** Mahali pa kurejea ni penye uumbaji lakini na kwenye karama za Roho (kama vile 1 Kor. 12:27). Hatuchagui; Mungu hupanga.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : 1 WAKORINTHO 12:19-25**

[19] **Lakini kama vyote vingekuwa kiungo kimoja, mwili ungekuwa wapi?** [20] **Lakini sasa viungo ni vingi, ila mwili ni mmoja.** [21] **Na jicho haliwezi kuuambia mkono, Sina haja na wewe; wala tena kichwa hakiwezi kuiambia miguu, Sina haja na ninyi.** [22] **Bali zaidi sana vile viungo vya mwili vidhaniwavyo kuwa vinyonge zaidi vyahitajiwa zaidi.** [23] **Na vile viungo vya mwili vidhaniwavyo kuwa havina heshima, viungo vile twavipa heshima zaidi; na viungo vyetu visivyo na uzuri vina uzuri zaidi sana.** [24] **Kwa maana viungo vyetu vilivyo na uzuri havina uhitaji; bali Mungu ameuungamanisha mwili, na kukipa heshima zaidi kile kiungo**

**kilichopungukiwa; [25] ili kusiwe na faraka katika mwili, bali viungo vitunzane kila kiungo na mwenziwe.**

**12:22-24 "vinyonge. . .heshimiwa kidogo. . .vyapendeza kidogo. . .kile kiungo chenye upungufu"** Hii yaweza kurejea vile viungo vya mwili vinavyofunikwa na mavazi. Mjadala hu unadhihilisha kwamba baadhi ya karama zisizo dhahiri, zisizo tamaniwa kutokana na utamaduni, karama zisizoonyesha "ufahari" zilikuwa za muhimu kwa ajili ya afya, mwili wenye furaha. Mungu/Roho hugawa vipawa, vipawa vyote vinahitajika, vipawa vyote vina heshima. Angalia MADA MAALUM: UDHAIFU (SPECIAL TOPIC: WEAKNESS) 2 Kor. 12:9.

◙**"heshima zaidi"** Neno hili katika 1 Kor. 12:23 na 24. Angalia Mada Maalum katika 2 Kor. 2:7.

**12:25** Aya hii inafafanua wazo kuu la Paulo (yaani, a *hina* kishazi, kishazi nia). Kanisa lazima liwe kitu kimoja, lisigawanyike. Waaminio lazima kila mmoja amjali mwenzake (kama vile 1 Kor. 12:7), wasifanye kitu chao wenyewe! VITENZI viko kwenye hali ya UTEGEMEZI ambapo vinatambulisha jambo linaloweza kutokea baadaye. Hiki ndicho wanapaswa kufanya lakini kuna mashaka kuhusu utendaji wao.
Neno "jali " kwa kawaida linamaanisha wasiwasi ama hofu (kama vile Mt. 6:25,27; 10:19; 13:22; 2 Kor. 11:28; Flp. 4:6). Linaweza pia kuonyesha swala halali kama katika andiko hili na, 7:32,33,34 na Flp. 2:20.

◙**"faraka"** Hili ni neno la Kiyunani *schisma*, ambalo kwalo tunapata neno la kiingereza faraka au mfarakano. Paulo amekwitaja huu "mfarakano" kabla (kama vile 1 Kor. 1:10; 11:18). Ndilo tatizo kuu katika Korintho.Utengano ulihusu (1) viongozi Fulani; (2) misisitizo Fulani ya theolojia; (3) Misimamo ya kijamii ya Kirumi; (4) Kukuza karama kadhaa; au (5) mabaki ya mtazamo wa kifikra.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 1 WAKORINTHO 12:26**
**[26] Na kiungo kimoja kikiumia, viungo vyote huumia nacho, na kiungo kimoja kikitukuzwa, viungo vyote hufurahi pamoja nacho.**

**12:26 "ikiwa. . .ikiwa"** Hii ni SENTENSI SHURUTISHI DARAJA LA KWANZA (*eite* kikiwa na KIELEKEZI CHA WAKATI ULIOPO, kama vile 2 Kor. 1:6; bila kitenzi, kama vile Rum. 12:6-8; 1 Kor. 3:22; 8:5; 14:27; 2 Kor. 5:10) ambayo inaelezea shauku ya Paulo ya jinsi waaminio wanavyopaswa kutendena kila mmoja na mwingine (kama vile Rum. 12:15).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 1 WAKORINTHO 12:27-31a**
**[27] Basi ninyi mmekuwa mwili wa Kristo, na viungo kila kimoja peke yake. [28] Na Mungu ameweka wengine katika Kanisa, wa kwanza mitume, wa pili manabii, wa tatu waalimu, kisha miujiza, kisha karama za kuponya wagonjwa, na masaidiano, na maongozi, na aina za lugha. [29] Je! Wote ni mitume? Wote ni manabii? Wote ni waalimu? Wote wanatenda miujiza? [30] Wote wana karama za kuponya wagonjwa? Wote wanena kwa lugha? Wote wafasiri? [31] Takeni sana karama zilizo kuu.**

**12:28 "Mungu ameweka"** Hii ni KAULI YA KATI ELEKEZI YA WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFU. Huu ni mfanano 1 Kor. 12:18.

◙**"Kanisa"** angalia Mada Maalum katika 1 Kor. 1:2.

◙**"mitume"** Neno la Kiyunani linatoka kwenye moja ya VITENZI "upelekwa." Ulitumiwa na walimu wa sheria za Kiyahudi mtu aliye tumwa kama mwakilishi rasmi wa mwingine. Katika injili ya Yohana inachukua maana ya Yesu Masihi aliyetumwa na Mungu. Aliyetumwa anawatuma wafuasi wake (Kama vile Yohana 20:21). Tazama Mada Maalum: Upelekwa katika 1 Kor. 4:9.

Kwa asili hii ilihusu wale kumi na wawili, lakini baadaye ilitumiwa kwa wengine: (1)Barnaba (kama vile Matendo 14:4,14); (2) Andronia and Yunia (kama vile Rum. 16:7); (3) Apolo (kama vile 1 Kor. 4:9); (4) Yakobo nusu ndugu (kama ville Gal. 1:19); (5) Epafrodito (kama vile Flp. 2:25; (6 & 7) Sila na Timotheo (kama vile 1 The. 2:6). Karama imetajwa katika Efe. 4:11 kama karama inayoendelea.

◙**"manabii,"** tazama Mada Maalum: Unabii wa Agano Jipya katika 1 Kor. 14:1 na unabii na unabii wa Agano la Kale 1 Kor. 12:10.

◙**"waalimu"** Karama hii imetajwa katika matendo 13:1 ikiunganishwa na unabii, lakini katika Waefeso 4:11 imeunganishwa na wachungaji. Katika 2 Tim. 1:11 Paulo anasema yeye ni mhubiri mtume, na mwalimu. Hapa inaonekana kusimama huru kama inavyosimama katika Rum. 12:7. Imejadiliwa pia pembeni katika Yakobo 3:1 na kuendelea. Hii inamaanisha kwamba karama hizi za uongozi zinaweza kuunganishwa katika njia tofauti katika waamini tofauti kukutana na hitaji la kanisa siku hiyo au mahali. Kila mmoja wa hawa viongozi waliopewa karama alihubiri injilli lakini na msisitizo tofauti.

◙**"miujiza"** Angalia katika 1 Kor. 12:9 na 10 karama hii imetajwa mara mbili, hapa lakini mara moja. Miujiza ilikuwa njia ya kuthibitisha injili. Ni mashuhuri katika Injili na Matendo na imetajwa katika nyaraka za mitume. Bado ziko kwa wingi katika sehemu ambazo injili ni ngeni.

◙**"kuponya"** Karama hii hutenda kazi kuufunua upendo wa Mungu na kuithibitisha injili. Swali sio kwamba kama Mungu bado anaponya, bali kwa nini kwa baadhi na sio wengine? Yakobo 5:13-18 inatoa miongozo mingine zaidi kuhusu jinsi gani hii inapaswa kushugulikiwa katika kanisa la mahali. katika Yakobo ni huduma ya wazee wa manabii, sio karama ya Roho.

**NASB, NKJV "masaidiano"**
**NRSV "miundo ya msaada"**
**TEV "nguvu. . .saidia wengine"**
**NJB "vitendo vinavyosaidia"**

Neno hili linatumiwa juu ya"vitendo vya kimsaada." Ni neno la jumla na linaweza kuhusu huduma ya mara kwa mara ya mashemasi (kama vile Flp. 1:1 na M. R. Vincent, *Word Studies*, juzuu. 2, uk. 793).

**NASB, NKJV "uongozi"**
**NRSV "muundo wa uongozi"**
**TEV "wale wanaopewa nguvu. . .kuwaongoza"**
**NJB "karama za kuelekeza. . .mwongozo"**

Neno hili mwanzoni lilitumiwa na rubani wa meli (kama vile Matendo 27:11; Ufu. 18:17). Lilitumika kimafumbo kwa viongozi wa kanisa wanaotenda kazi kama waelekezaji. Huu ni uwezo wa kuongoza wengine kutimiza majukumu ya kiroho. A. T. Robertson, *Word Pictures In Greek New Testament*, juzuu. 4, inasema kwamba "kusaidiana" kunarejea juu ya kazi ya shemasi kuwasaidia maskini na wagonjwa na “uendeshaji” huo inarejea kazi ya maaskofu/wazee/wachungaji, uk. 173-174.

◙ **"na aina za lugha"** Angalia 1 Kor. 12:10.

**12:29-30** Mlolongo huu wa maswali wote unaanza na KIAMBATA HASI (yaani, *mē*), ambacho huonesha kwamba maswali yanatarajia jibu la "hapana". Hiki ni kifungu muhimu katika kukataa ile thiolojia ya kwamba karama ya “kunena” kwa lugha ni karama ya ya kila aaminiye, namna ya kuthibitisha ishara ya wokovu na /au alama maalum ya hali ya ukiroho wa kweli. Ni kipawa halali, lakini sio kwa kila mtu. Kingine kikubwa ni kukataa “unenaji” kama kitu kilichopita katika kipindi cha Mitume. Huu pia ni utiajichumvi wa kithiolojia. (kama vile 1 Kor. 14:39). Mantiki

yote ya sura hii ni kwamba kuna mwili mmoja lakini viungo vingi, hakuna kiungo kimoja (yaani, karama) iliyo na sifa au heshima.

**12:31a**
**NASB, NIV "Lakini tamanini sana karama zilizo kuu"**
**NKJV "lakini tamanini kwa juhudi karama bora zaidi"**
**NRSV "Lakini tumieni juhudi mpate karama kuu zaidi"**
**TEV "Elekezeni mioyo yenu basi kwa karama muhimu zaidi"**
**NJB "Elekezeni nia zenu kwenye karama za juu zaidi"**

Aidha hii ni (1) KAULI TENDAJI ELEKEZI YA WAKATI ULIOPO (yaani, maelezo ya kweli) au (2) KAULI TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO (yaani, amri inayoendelea). W. Randolph Tate, *Biblical Interpretation*, inapendelea HALI YENYE KIARIFU, "unapania kwa ajili ya karama zilizo njema" kama hoja zingine za Paulo za kejeli (uk 22).

Sehemu ya pili ya aya hii inapaswa kwendana na sura ya 13. Karama bora zingehusu (1) imani, tumaini na upendo 1 Kor. 13:13, (2) karama zinazohusu mwili wote, 1 Kor. 14:1 nakuendelea, ambazo zingekuwa kuhubiri na kufundisha (kama vile 1 Kor. 12:28).

Kuonya kuonekana kurejea kanisa kwa ujumla, na sio mtu binafsi. Kuelekezea juu ya mtu binafsi ni upendeleo wa kawaida Kwa watu wa magharibi. Kuangazia ama kuweka mtazamo mkuu katika sura hii ni kufanya wengi wawe wamoja (yaani, waamini) kwamba wanatangaza injili na wanaujenga mwili.

## MASWALI YA MJADALA

Haya ni maoni kuhusu mwongozo wa kusoma, ambao una maana kuwa, unawajibika kwa tafsiri yako binafsi ya Biblia. Kila moja wetu sharti atembee katika nuru tulionao. Wewe, Biblia na Roho Mtakatifu ni kipaumbele katika tafasiri. Usiachie kazi hii kwa mtoa maoni.

Maswali haya ya kujadili yanatolewa kukusaidia mambo muhimu ya kipengele cha kitabu hiki. Yamekusudiwa kukuchokonoa mawazo na sio ya mwisho.

1. Kanini kulikuwa na tatizo kama hilo kuhusu karama za kiroho kule Korintho?
2. Ni lini aaminiye hupokea karama zake za kiroho? Je kila mmoja anakuwa na karama moja? Mtu anaweza kuwa na zaidi ya moja?
3. Nini kusudi la karama za kiroho?

## BAADHI YA MIONGOZO YA KIUTENDAJI KWA NAMNA MWAMINI MPYA ANAVYOWEZA KUJUA KARAMA ZAKE

1. Muombe Mungu akuonyeshe bayana.
2. Waulize waaminio wengine waliokomaa wanaokufahamu karama gani wanayoiona kwako.
3. Gundua shauku yako ya asili.
4. Tembea kwenye mwelekeo wa nuru yako njema na shauku yako.
5. Fanya jaribio na utafute utoshelevu na tunda la kiroho.

Haya yamechukuliwa kutoka kwenye kijitabu kizuri cha Paul Little, *Affirming the Will of God*, kilichochapishwa na IVP. Hii inatoa hekima ya Kikristo, si Maandiko, kuhusu jinsi ya kuyajua mapenzi ya Mungu, ambayo ni mfanano wa jinsi ya kujua karama za roho ya mtu.

Hata hivyo, waaminio wanahitaji kukumbuka kwamba orodha za karama hazifanani. Kuweza kuzitamka karama zetu si jambo muhimu kama kutambua kwamba sisi tunayo. Waaminio, wote waaminio, wameitwa na kupewa karama ili kufanya huduma (kama vile Efe. 4:11-12).

# 1 WAKORINTHO 13

| MGAWANYO WA AYA WA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **UBS[4]** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB** |
| | | | | Tabia nje katika ibada ya wazi (11:2-14:40) |
| Upendo | Zawadi iliyo kubwa | Upendo, Zawadi iliyo kubwa na njia | Upendo | Utaratibu wa Umuhimu katika Zawadi za kiroho na Upendo |
| 2:31b-13:3 | | | | 2:31-13:3 |
| | 13:1-13 | 13:1-13 | 13:1-13 | |
| 13:4-7 | | 13:4-7 | 13:4-7 | 13:4-7 |
| 13:8-13 | | 13:8-13 | 13:8-10 | 13:8-12 |
| | | | 13:11-12 | |
| | | | 13:13 | 13:13 |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (Kutoka" **Mwongozo Mzuri wa Usomaji Biblia")** **("A Guide to Good Bible Reading")**

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Haya ni maoni ya mwongozo kwa kujisomea, ikiwa na maana kuwa unawajibika binafsi kwa tafsiri ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mtoa maoni tu.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

25. Aya ya kwanza
26. Aya ya pili
27. Aya tatu
28. N.k

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA KWA 13:1-13

A. Sura hii inaunda sehemu ya msingi wa mjadala wa Paulo wa zawadi za kiroho. Hii "sura ya upendo" inaweka haki katikati ya mgogoro juu ya karama za kiroho.
B. Kanisa katika Korintho lilijaribu kuongeza baadhi ya karama. Paulo alithibitisha karama zote na kuweka mipaka kwenye kazi na kusudi yao katika kusanyiko la ibada katika Sura ya 12-14.
C. Jaribio kuu la pili la karama za kiroho (angalia tambuzi za kimuktadha, sur. 12, B) ni, "Je! Wanatekeleza kwa upendo?"

## MAELEZO YA MSINGI

A. Umuhimu wa Upendo kama nia kwa kutekeleza karama za upendo (1 Kor. 13:1-3).
B. Tabia ya upendo inaelezewa katika uhusiano na watu (1 Kor. 13:4-7).
C. Upendo wa ndani kama sifa ya familia ya Mungu (1 Kor. 13:8-13).

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : 1 WAKORINTHO 12:31b-13:3**
**[12:31]Takeni sana karama zilizo kuu. Hata hivyo nawaonyesha njia iliyo bora.[13:1] Nijaposema kwa lugha za wanadamu na za malaika, kama sina upendo, nimekuwa shaba iliayo na upatu uvumao. [2] Tena nijapokuwa na unabii, na kujua siri zote na maarifa yote, nijapokuwa na imani timilifu kiasi cha kuweza kuhamisha milima, kama sina upendo, si kitu mimi. [3] Tena nikitoa mali zangu zote kuwalisha maskini, tena nikijitoa mwili wangu niungue moto, kama sina upendo, hainifaidii kitu.**

**12:31b "Hata hivyo nawaonyesha njia iliyo bora"** Neno "bora" ni neno la Kiyunani lililoumbwa kwa neno *huper* (yaani, juu ya au mbele ya) na neno *ballō* (yaani, kutupa). Ni sitiari kwa kile ambacho kinapitiliza zaidi. Paulo hutumia sitiari hii mara nyingi katika 2 Wakorintho (kama vile 2 Kor. 1:8; 3:10; 4:7; 9:14; 11:23; 12:7). Angalia Mada Maalumu: Matumizi ya Paulo ya muunganiko wa neno *Huper* katika 1 Kor. 2:1.

Neno "njia" ni sitiari ya Agano la Kale kwa maisha ya ki-Mungu (kama vile Kumb. 5:32-33; 31:29; Zab. 27:11; Isa. 35:8). Imani ya Agano la Kale, kama ilivyo imani ya Agano Jipya, haikuwa tu kanuni za imani sahihi (imani halisi), lakini maisha ya utii (tabia nzuri ya kimaadili na kirutulujia). Sifa ya kanisa la kwanza ilikuwa "njia" (kama vile Mdo. 9:2; 19:9,23; 24:14,22). Ubora wa Mungu ni maisha ya upendo binafsi aliyoyatoa, yaliyotolewa na Yeye mwenyewe na Mwanawe.

**13:1 "Ikiwa"** Huu ni mfululizo wa SENTENSI YENYE MASHARTI DARAJA LA TATU, ambayo inamaanisha kuwezekana kwa kitendo, katika 1 Kor. 13:1, 2, na 3 (mara mbili).

| | |
|---|---|
| **NASB, NKJV** | **"nijaposema kwa lugha za wanadamu na za malaika"** |
| **NRSV** | **"nasema kwa lugha za wanadamu na za malaika "** |
| **TEV** | **"hata kama nikinena lugha za watu na hata za malaika "** |
| **NJB** | **"ingawa nazungumza luugha zote za wanadamu na malaika"** |

Hii dhahili ni rejea ya karama za kunena kwa lugha zilizotajwa katika 1 Kor. 12:10,28-29, karama ambayo Kanisa la Korintho lilisababisha kukuzwa kwayo na kumilikiwa na Paulo (kama vile 1 Kor. 14:1,5,6,18-19).

Hapa nadhani kwamba "uneneji wa lugha" katika matendo ulikuwa tofauti kutoka kwa "unenaji wa lugha" katika Korintho, hizi rejeo mbili zinanifanya nishangae kama inawezekana Paulo pia alielewa unenaji wa lugha ilikuwa lugha ya mwandamu (yaani, Pentekoste) na matamshi yaliyojaa furaha (yaani, lugha ya mbinguni). Kwa hakika, yeye uthibitisha kwamba uwezo kujua lugha pekee hautosherezi isipokuwa ukichangamshwa na upendo! Ukristo ni zaidi kuliko ujumbe; ni mtu, anayejitolea, mwenye upendo, mtu wa utiifu-Yesu.

◙ **"upendo"** Hili ni neno la Kiyunani *agapē.* Lilikuwa moja ya maneno kadhaa kwa ajili ya "upendo" katika Uyunani wa sasa, lakini lilitumika mara chache (yaani, muudo wa NOMINO). Kanisa la kwanza huonekana kuchagua neno hili na kulijaza kidokezo kipya cha Mkristo (yaani, Mungu na upendo wa kujitolea wa Kristo, kama vile 1 Yohana 4:10) kwa sababu ya matumizi yake katika tafsiri ya Agano la Kale kwa Kiyunani (mf. Mwa. 22:2) na walimu wa sheria za kiyunani wa dini ya kiyahudi. Katika Agano la Kale upendo wa Mungu wa agano na uaminifu kwa ahadi zake na maagano ulielezewa na neno *hesed*. Katika namna nyingi neno *agapē* huelezea dhana hii kwa "upendo wa Agano" na kuliweka sambamba na "ufalme wa Mungu." Huwa neno la Agano Jipya kwa ajili tabia ya Mungu, ambayo yeye hutumaini wafuasi wake kuihusudu (kama vile 1 Yohana 4:7-21).

Kumbuka tu kuhusu uhusiano wa neno *agapē* kwa *philos*. Katika baadhi ya mazingira kunaonekana kuwa na tofauti (kama vile Yohana 21:15-19). Hata hivyo, katika lugha ya Koine ya huko Uyunani ni ufanano wa kutokea mara kwa mara (kama vile Yohana 3:35 na 5:20).

**MADA MAALUMU: WEMA *(HESED)* (SPECIAL TOPIC: LOVINGKINDNESS *(HESED)***

**NASB, NRSV "shaba iliyo na upatu uvumao"**
**NKJV "kama sauti ya debe tupu au kengele "**
**TEV "sio zaidi ya shaba iliyo na upatu uvumao "**
**NJB "shaba iliyo na upatu uvumao"**

Kihistoria katika karne ya kwanza ya ulimwengu wa Warumi, hii ilitumiwa na madhehebu ya Dionysus na Cybele katika ibada kuvutia miungu yao. Katika mazingira ya tabia mbaya ya Wakorintho inaweza kumaanisha kisitiari "mshindo wa Baragumu" (kama vile Mt. 6:2), ambao ulileta uangalifu kwa mnenaji kama wanaume walivyofanya kwa kufunika nywele zao katika kusanyiko la ibada au wanawake kuweka wazi nywele zao fupi katika kusanyiko la ibada (kama vile 1 Kor. 11:4-5).

Mji wa Korintho ulijulikana katika ulimwengu wa kale kwa vyombo vyao vya shaba. Tumizi moja la nyenzo hii ilikuwa kwa ajili ya "uboreshaji wa sauti yenye kuendelea" katika jumba la maonyesho (kama vile *Dictionary of Paul and His Letters*, uk. 172).

Usambamba wa Paulo honyesha shauku ya hisia zake kuhusu shughuli za kiroho pasipo na upendo.

1. "nimekuwa shaba iliayo na upatu uvumao" (NJEO YA WAKATI TIMILIFU), 1 Kor. 13:1
2. "si kitu mimi" (NJEO YA WAKATI ULIOPO), 1 Kor. 13:2
3. "hainifaidii kitu" (NJEO YA WAKATI ULIOPO), 1 Kor. 13:3

**13:2 "nijapokuwa na unabii"** Katika kitabu hiki neno hili linaeleweka zaidi kama "kushiriki ujumbe wa injili" (kama vile 1 Kor. 11:4,5; 14:39). Maneno ya kwanza matatu ya 1 kor.13:2 yanahusiana na karama ya hekima na maarifa (kama vile 1 Kor. 12:8). Kulikuwepo na tatizo katika eneo hili kama kauli hasi ya Paulo ya 1 Kor. 1:17,19,20,21,22,24; 2:1,4,5,6,13; 3:19 inavyonyesha. Unabii pasipo na upendo, kama hekima na maarifa pasipo na upendo, haipendezi kwa Mungu. Karama za kiroho zinaweza kutumika katika njia sahihi.

Kwa dhana ya "unabii" katika AK tazama Mada Maalumu katika 1 Kor. 12:10 na unabii wa Agano jipya katika 1 Kor. 14:1.

◙ **"na kujua siri zote na maarifa yote"** Paulo analitumia hili katika 1 Kor. 4:1 kwa ajili ya ukweli wa injili na katika 1 Kor. 15:51 kwa ajili ya ukweli maalumu kuhusu ufufuo wa mwili. Katika mazingira haya kifungu hiki cha maneno kinaonesha kurejea kwenye maarifa katika kila muundo wake, ambao waaminio katika Korintho walikitukuza na kukitafuta. Hata maarifa kamili pasipo upendo hayampendezi Mungu. Angalia Mada Maalum: Siri katika 1 Kor. 2:1.

◙ **"imani timilifu"** Mstari huu unarejea kwenye imani itendayo muujiza (kama vile 1 Kor. 12:9,28; Mt. 17:20; 21:21), lakini angalia katika Mt. 7:21-23 kwamba nguvu itendayo muujiza pasipo upendo haimpendezi Mungu au hata kumjua Mungu.

Kwa dhana ya "imani" katika Agano la Kale angala Mada Maaalumu katika 1 Kor. 1:9 na Agano Jipya katika 1 Kor. 2:4.

**13:3**
**NASB "tena nikitoa mali zangu zote"**
**NKJV "nitatoa mali zangu zote "**
**NRSV "nikitoa mali yangu yote "**
**TEV "ninaweza kutoa mali zangu zote "**
**NJB "ninapaswa kutoa. . .mali zangu zote "**

Mstari huu humaanisha kutoa vyote mtu alivyonavyo, kibinafsi, kidogo kidogo (kama vile Yohana 13:26,27,30). Hii inaweza kuwa dokezo kwenye mjadala wa Yesu na yule kijana Mtawala tajili (kama vile Mt. 19:16-29; Marko 10:17-30; Luka 18:18-30).

**NASB, NKJV "kuwalisha masikini "**
**NRSV -inaacha kifungu -**
**TEV -inaacha kifungu-**
**NJB "kuwapa maskini"**

Kifungu hiki cha maneno hakipo katika maandiko ya Kiyunani, lakini kilidokezwa katika kitendo cha KITENZI hiki.

**NASB, NKJV,**
**TEV, NJB "nikijitoa mwili wangu niungue"**
**NRSV "nikiutoa mwili wangu uchomwe"**

Kuna mswada wa chaguzi mbili: "kuungua moto" (yaani, *kauthēsomai*) na "utukufu" (yaani, *kauchēsōmai*) yote yanapatikana katika miswada ya kwanza ya Kiyunani na kwa mkasisi wa kanisa la kwanza. Kifungu cha maneno “ili nipate utukufu” kina machapisho yenye msaada wa nguvu (yaani, MSS $P^{46}$, א, and B), lakini $UBS^4$ haiwezi kufanya maamuzi kati yake.Pia ni neno linalotumiwa na Paulo (kama vile 2 Kor. 8:24; Flp. 2:16; 1 The. 2:19; 2 The. 1:4). Mauaji ya kuchomwa moto hayakujulikana katika kanisa la kwanza, lakini ilikuwa kawaida zaidi katika mateso ya baadaye (yaani, Nero na Domitian). Kwa hiyo, mtu anaweza kuona jinsi gani mwandishi baadaye alivyoweza kubadilisha neno “utukufu” kwenda “kuchoma.”

Kwa mjadala kamili wa utofauti wa maandishi angalia Bruce M. Metzger, *A Textual Commentary on the Greek New Testament*, kr. 563-564. Kwa maoni tofauti tazama *The Expositor's Bible Commentary*, uk. 270 tanbihi chini ya ukurasa.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 1 WAKORINTHO 13:4-7**
**[4] Upendo huvumilia, hufadhili; upendo hauhusudu; upendo hautakabari; haujivuni; [5] haukosi kuwa na adabu; hautafuti mambo yake; hauoni uchungu; hauhesabu mabaya; [6] haufurahii udhalimu, bali hufurahi pamoja na kweli; [7] huvumilia yote; huamini yote; hutumaini yote; hustahimili yote.**

**13:4-7** Mistari hii inaweza kuwa wimbo wa kidini au shairi kuhusu upendo, ulioandikwa au kunukuliwa na Paulo.Maelezo haya yote ya upendo yanafanya kazi. Upendo ni kitendo, sio tu hisia. Yote haya yanaelezea huduma ya Yesu (ufunuo kamili na timilifu wa YHWH) kama Yeye alivyojishughulisha na watu wasio wakamilifu. Upendo ni mtu!

**13:4 "huvumilia"** KITENZI hiki (KAULI TENDAJI ELEKEZI YA WAKATI ULIOPO) kina kidokezo cha uvumilivu wa watu (kama vile Mit. 19:11; 1 The. 5:14; Yakobo 5:7,8; 2 Pet. 3:9) ambao hutenda kwa udhalimu dhidi yetu, pasipo na kulipiza kisasi. Hii ni moja ya matunda ya Roho (kama vile Gal. 5:22). Ni sifa ya Mungu (kama vile Rum. 2:4; 9:22; 1 Tim. 1:16; 1 Pet. 3:20). Inapaswa (NOMINO) elezea sifa ya waaminio wa enzi mpya, wenye Roho wa Mungu (kama vile 2 Kor. 6:6; Kol. 1:11).

◙ **"hufadhili"** KITENZI hiki kinapatikana hapa pekee na pia ni neno lililozingatiwa na watu. Hudokeza “kuwa mpole kwa wote.” Petro pia alitumia neno hilo hilo kwa Yesu katika 1 Pet. 2:3. Pia ni moja ya karama za Roho katika Gal.5:22.

◙ **"hauhusudu"** Mstari huu huelezea shahuku kubwa, kihalisia “kushikwa na ghadhabu.” Upendo hauna shauku kwa ajili yake wenyewe ili kumiliki au kudhibiti watu.

◙ **"hautakabari"** Neno hili la nadra linarejea kwa mtu wa kujipendekeza ambaye anaonekana kwa wengine kama mjisifu au mpiga porojo. Mara nyingi lilihusishwa na wasomi au majivuno ya kutia madoido au kujisifu katika fasihi ya Kiyunani.

◙ **"haujivuni"** Neno hili linarejea kwa wale ambao wana thamini mno na kujishaua wenyewe.Hutumiwa mara nyingi katika 1 Wakorintho (1 Kor.4:6,18,19; 5:2; 8:1) na hapa.Kwa kweli huaksi sifa ya kanisa hili. Angalia maelezo katika 1Kor.4:6.

**13:5 "haukosi kuwa na adabu"** Hili sio neno rahisi kuelezea. Linatumiwa katika 1 Kor. 7:36 kwa hisia chanya zaidi. Hapa kidokezo chake ni hasi. Neno lilitumika katika mafunjo ya Misri likidokeza kulaani au kuchukua kiapo kikihusianishwa na matendo yasiyofaa (kama vile 1 Kor. 12:3). Hudokeza uovu badala ya rehema.

◙ **"hautafuti mambo yake"**Huu ni ukweli uliorudiwa mara nyingi (kama vile 1Kor. 8:9; 10:24,33; Rum. 14:16; Flp. 2:3).Hii laweza kuwa likihusishwa kitheolojia kwa Efe. 5:21, kwa ajili ya kunyenyekeana kutokana na heshima kwa Kristo.

◙ **"hauoni uchungu"** Neno hili kihalisia ni "kutia makali." Linatumika kisitiari kwa niaba ya "kuchochea." Linaweza kuwa chanya kama katika Mdo. 17:16 au hasi, kama hapa. Tafsiri Ya Filipi ina "sio makini" ilitumika katika maana ya "kutokuwa rahisi kukasirishwa au kughadhibishwa." NOMINO hii inatumika kwa Paulo na Barnaba kupingana juu ya Yohana Marko (kama vile Mdo. 15:39).

**NASB "hauhesabu mabaya "**
**NKJV "haufikirii mabaya"**
**NRSV "au yenye chuki "**
**TEV "haweki kumbukumbu ya mabaya "**
**NJB "hauhifadhi mabaya"**

Hili neno la kimahesabu kwa leja ya bili ya bila malipo (kama vile 2 Kor. 3:5; 12:6). Inarejea kwa mtu ambaye huhifadhi rohoni kwa kutaka kulipa kiasi. Mfano inaweza kuwa Mdo 15:36-41 na 2 Tim. 4:11 juu ya Yohana Marko. Inawezekana kwamba hili ni dokezo kwa tafsiri ya Agano la kale kwa Kiyunani ya Zek. 8:17 "wala mtu wa kwenu asiwaze mabaya moyoni mwake juu ya jirani yake." Hata hivyo, tangu wakati ule vifungu vy amaneno vya mazingira sio vidokezo katika Agano la Kale, hudhoofisha uwezekano kwamba huu ndiyo wenyewe.

**13:6** Hizi zote ni kauli za ukweli hasi na chanya . Katika mazingira haya inaweza kurejea juu ya masengenyo ndani ya jamii ya Kikristo. Ni hali isio kawaida kwamba neno "udhalimu" limetofautishwa na"kweli." Yumkini "udhalimu" ni kinyume cha "haki ya kuishi" na "kweli" inarejea kwenye ujumbe wa injili.

◙ **"pamoja na kweli"** Angalia Mada Maalum katika 2 Kor.13:8.

**13:7 "huvumilia yote"** Neno "yote" (yaani, *panta*) limewekwa mbele mara nne katika mstari huu kwa ajili ya kusisitiza. Upendo ni wa wote pamoja. Neno "Yote" linatumika katika hisia ya "wakati wote" (yaani, vitenzi vyote vinne ni NJEO YA WAKATI ULIOPO) na "kwa nafasi zote."

Neno "vumilia" linatoka katika neno la Kiyunani "dari" (kama vile Mt. 8:8). Ni sitiari kwa ajili ya (1) kufunika (kama vile 1 Pet. 4:8, neno tofauti, lakini dhana ile ile) au (2) kustahimili (kama vile 1 Kor. 12:9; 1 The. 3:1,5). Tafsiri ya Moffat ina "mzito kuweka wazi."

◙ **"huamini yote"** Katika muktadha huu mstari huu hudokeza "kuangalia ubora zaidi kwa wengine" au "hutoa faida kwa Mkristo mwingine kwa sababu ya mashaka yake." Daima huendeleza imani (kama vile Gal. 5:22).

◙ **"hutumaini yote"** Katika muktadha huu upendo hushikilia tumaini ya maendeleo ya baadaye ya waaminio wenzio katika imani.Haikati tamaa.

◙ **"hustahimili yote"** Hili ni neno kubwa kwa kustahimili majaribu na kujaribiwa (kama vile Mt. 10:22; 24:13; Ebr. 10:32; Yakobo1:12). Hapa linazungumza kwa hiari, uvumilivu uliositirika. Kifungu hiki husisitiza si kwa ajili ya kulipiza kiasi binafsi au kitu kilichokataliwa, lakini uvumilivu imara, hususani pamoja na watu.

**ANDIKO LA NASB (LILIILOBORESHWA): 1 WAKORINTHO 13:8-13**
**8 Upendo haupungui neno wakati wo wote; bali ukiwapo unabii utabatilika; zikiwapo lugha, zitakoma; yakiwapo maarifa, yatabatilika. 9 Kwa maana tunafahamu kwa sehemu; na tunafanya unabii kwa sehemu; 10 lakini ijapo ile iliyo kamili, iliyo kwa sehemu itabatilika. 11 Nilipokuwa mtoto mchanga, nalisema kama mtoto mchanga, nalifahamu kama mtoto mchanga, nalifikiri kama mtoto mchanga; tokea hapo nilipokuwa mtu mzima, nimeyabatilisha mambo ya kitoto. 12 Maana wakati wa sasa tunaona kwa kioo kwa jinsi ya fumbo; wakati ule tutaona uso kwa uso; wakati wa sasa nafahamu kwa sehemu; wakati ule nitajua sana kama mimi nami ninavyojuliwa sana. 13 Basi, sasa inadumu imani, tumaini, upendo, haya matatu; na katika hayo lililo kuu ni upendo.**

**13:8** Tafsiri kadhaa zinaanza na aya mpya katika 1 Kor. 13:8. Majadiliano ya Paulo kuhusu upendo wa kikristo ni wa kubadilika kidogo na kuendelea katika mwelekeo mpya (yaani, ubora na shughuli ya zama hii dhidi ya kumalizika kwa zama mpya, ambayo ilikuwa imeanzishwa).

◙ **"Upendo haupungui neno wakati wo wote"** Neno hili lina matumizi mawili yanayohusiana kisitiari: (1) lilitumika kwa muigizaji kuzomewa kwenye jukwaa (2) lilitumika kwa ua ambalo lilidondosha petali yake kwa sababu ya dhoruba ya hali ya hewa (kama vile Yakobo 1:11; 1 Pet. 1:24). Upendo wa Mungu kamwe haukatishi tamaa!

**NASB "bali ukiwapo. . .zikiwapo. . .yakiwapo"**
**NKJV "kama. . .kama. . .kama"**
**NRSV "kama kuna. . .kama ni. . .kama kuna"**
**TEV "ukiwapo. . .zikiwapo. . .yakiwapo"**
**NJB "kama kuna. . .kama. . .kama**

Muundo wa kisarufi *eite* (SENTENSI tatu SHURUTISHI DARAJA LA KWANZA) huonyesha kuna zawadi za kiroho.

◙ **" unabii. . . utabatilika. . . lugha. . . zitakoma. . . maarifa. . . yatabatilika"** Tambua mfanano wa muundo. Hizi zilikuwa karama za kiroho ambazo kanisa la Wakorintho walitukuza (kama vile 1 Kor. 13:1-3). Mstari huu mara nyingi inatumika kwa kupunguza thamani ya lugha kwa sababu KITENZI na IRABU tofauti vinatumika.Hata hivyo, muktadha unathibitisha kwamba karama zote za kiroho zitakoma, lakini upendo kamwe hautakoma. Hakuna msisitizo katika muktadha huu juu ya dalili za karama moja kuwa juu dhidi ya nyingine. Karama za kiroho ni za wakati, sio milele. Upendo ni milele!

Neno hili "lililokwisha tendeka" liko katika 1 Kor. 13:8,10, na 11. Angalia Mada Maalumu: *Katargeō* katika 1 Kor. 1:28.

**13:9** Hii huanza na mtiririko wa mistari ambayo husisitiza upendeleo na upungufu wa karama za kiroho. Upendeleo huu ni kutokana na udhaifu wa binadamu, kuanguka, na ukomo, sio ukosefu uliohusianishwa na karama ulizojaliwa na Mungu.

**13:10 "ijapo ile iliyo kamili"** Neno hili (yaani, *teleios*) humaanisha "kukomaa, ukamilifu," au "kuwa tayari kufanya kazi fulani" (kama vile 1 Kor. 2:6; 13:10; 14:20). Swali daima linakuwa,"Je! Inarejea kwenye nini?":

1. Baadhi walionyesha kwamba inarejea kwa Agano Jipya.Hakuna kitu katika muktadha huu kinaonyesha jambo hili. Hii ni nadharia pekee inayotumika kudai kuwa karama za kiroho zimekoma baada ya nyakati za mitume.
2. Baadhi walionyesha kwamba inarejea kwa kukomaa kiroho kwa sababu ya 1 Kor. 13:11 (yaani, mtoto kisha mtu mzima) au matumizi sahihi ya karama za kiroho.
3. Baadhi walionyesha kwamba inarejea kwa Kuja kwa Mara ya Pili kwa Kristo na kutimiliza kwa zama mpya ya haki kwa sababu ya 1 Kor. 13:12 (yaani, "angalia uso kwa uso").

4. Kwangu inaonyesha kuwa uunganishaji wa yote #2 na #3.

   Matumizi tofauti na vidokezo vya neno *teleios* vinaweza kuonekana kwenye matumizi yake katika kitabu cha Waebrania.Tazama Mada Maalumu chini.

**MADA MAALUMU: MWISHO AU UKAMILIFU *(TELOS)* (SPECALTOPIC: END OT FULL *(TELOS)***

**13:11 "nimeyabatilisha"** Hili ni neno la Kiyunani *katargeō*, ambalo Paulo anatumia mara nyingi. Angalia Mada Maalumu katika 1 Kor. 1:28. Katika muktadha huu Paulo anaonyesha kwamba
1. unabii utafikia mwisho, 1 Kor. 13:8 (KAULI TENDEWA ELEKEZI YA WAKATI UJAO)
2. maarifa yatafikia mwisho, 1 Kor. 13:8 (KAULI TENDEWA ELEKEZI YA WAKATI UJAO)
3. kila karama itafikia mwisho, 1 Kor. 13:10 (KAULI TENDEWA ELEKEZI TA WAKATI UJAO)
4. uchanga wa kiroho utafikia mwisho, 1 kor. 13:11 (KAULI TENDAJI ELEKEZI YA WAKATI UJAO)

**13:12 "kioo"** Korinto ilikuwa maarufu kwa kung'arishwa kwake kwa metali ya vioo.Walikuwa watu bora zaidi waliopatikana katika siku hiyo, lakini waliaksi taswira iliyobadilishwa. Binadamu, hata wale waliokombolewa, wanazuiliwa na (1) asili ya dhambi; (2) ukomo; (3) mtazamo ulio na kikomo; (4) mtizamo wa ulimwengu na dhamira iliyoathiliwa na tamaduni (5) wakati kama mfuatano wa utaratibu na matukio; na (6) lugha ya binadamu kwa kuelezea na kufafanua ulimwengu wa kiroho.

Angalia mfanano

1. 1 Kor. 13:9, fahamu kwa sehemu, unabii kwa sehemu dhidi ya wakati timilifu ujapo
2. 1 Kor. 13:11, mtoto mchanga dhidi ya mtu mzima
3. 1 Kor. 13:12, kioo cha Wakorintho dhidi ya mkabiliano na kujua kwa sehemu dhidi ya ninavyojulikana sana

   Hii inaonyesha kuaksi ukweli uliopo dhidi ya uweli wa milele, kwa hiyo, kuja kwa mara ya pili, ambao hutimiliza zama mpya, ndio lengo.

◙ **"fumbo"** Hii kihalisia ni "fumbo" (kama vile NJB). Walimu wa sheria za Kiyahudi waliamini Mungu alizungumza na Musa kwa namna ya mafumbo (kama vile Hes. 12:6,8).

◙ **"uso kwa uso"** Hii ni sitiari kwa maana ya ushirika wa ndani (yaani, kuweza kulinganishwa na Hes. 12:8). Katika Agano la Kale kumwona YHWH ilimanisha kifo (kama vile Mwa. 32:30; Kut. 33:20; Yohana 1:18). Katika zama mpya hii itakuwa kawaida (kama vile Mt. 5:8; 2 Kor. 5:7; 1 Yohana 3:2; Ufu. 22:4).

◙ **"nafahamu kwa sehemu. . . nitajua sana. . . nami ninavyojuliwa sana"** Dhahiri huu ni mchezo unaojishughulisha juu ya kidokezo cha neno la Kiebrania na Kiyunani "kujua." Katika Agano la Kale inarejelea, sio kwa ukweli wa utambuzi (yaani, dhana ya Kiyunani), lakini uhusiano binafsi (kama vile Mwa. 4:1 na Yer. 1:5).

Katika mstari huu pia kuna mzaha juu ya neno la Kiyunani kwa "fahamu" (yaani, *ginōskō*). Matumizi ya kwanza ni msingi wa neno. Ya pili na ya tatu ni neno ambatani (yaani, *epiginōskō*), ambalo linatokana na uzoefu wa mtu, maarifa kamili. Waaminio watamjua Mungu katika zama mpya kama Yeye alivyotujua sisi (kama vile 1 Kor. 8:3; Gal. 4:9). Neno "agano jipya" lilipewa sifa na watu wa Mungu kila mmoja kumjua Yeye (kama vile Yer. 31:31-34). Kutakuwa hakuna uhitaji kwa wahubiri/walimu!

Dhana ya Kitheolojia ya neno "kufahamu" linahusishwa na dhana ya uchaguzi. Siri ya jinsi gani uchaguzi (yaani, chaguo la Mungu) huhusishwa na mwitikio wa agano (yaani, chaguo la binadamu) haujulikani. Kufuata mantiki ya mistari hii ya Agano la Kale: Zab. 1:6;Yer. 1:5; Amosi 3:2 na mistari hii ya Agano Jipya: Rum. 8:29; 11:2; 1 Kor. 8:3; 13:13; Gal. 4:9, waaminio wanajulikana na Mungu kabla ya wakati, kwa wakati, na mbele ya wakati. Waaminio, hata hivyo, humjua Mungu katika hatua sawa sawa na kuhesabiwa haki, utakaso, kutukuzwa. Tunamjua Yeye kwa wakati kupitia Agano la Kale. Yesu, na injili; kupitia wakati na kukua kwetu kuwa kama Kristo kupitia Roho; na

mbele ya wakati tutamjua Yeye uso kwa uso, urafiki wa karibu sana wa jamii na maarifa timilifu kwa zama mpya za haki.

**13:13 "tumaini"** Neno hili la Kiyunani halina ugumu na halijulikani kwenye neno la Kiingereza. Ni imani yenye hakika kwamba ahadi za Mungu zitakuwa kweli katika wakati wake.

**MADA MAALUMU: TUMAINI (SPECIAL TOPIC: HOPE)**

◙ **"Basi, sasa inadumu imani, tumaini, upendo"** KITENZI ni UMOJA (kama vile Gal. 5:22). Paulo mara nyingi hutumia seti hii ya vitu vitatu vinavyohusiana sana (kama vile Rum. 5:2-5; Gal. 5:5-6; Efe. 1:15-18; Kol. 1:4-5; 1 The. 1:3; 5:8; Waebrania) na waandishi wengine pia wa AJ (kama vile Ebr. 6:10-12; 1 Pet. 1:21-22).

◙ **"hayo lililo kuu ni upendo"** Ni jambo kubwa kwa sababu wengine watakoma kwenye utimilizo wa enzi mpya. Imani itageuka kutazama na tumaini litakuwa na ukamilisho wake, lakini upendo utabaki kwa sababu ni msingi wa sifa ya Mungu (kama vile Yohana 3:16; 1 Yohana 4:8,16)

## MASWALI YA MJADALA

Haya ni maoni ya mwongozo kwa kujisomea, ikiwa na maana kuwa unawajibika binafsi kwa tafsiri ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mtoa maoni tu.

Maswali haya ya kujadili yanatolewa ili kukusaidia kufikiri mambo muhimu yaliyoko katika kipengele cha kitabu hiki. Yanamaanisha kuwa maswali ya kichokonozi, yasio ya hakika.

1. Toa wazo kuu la sura hii kwa maneno yako mwenyewe, kwa sentensi moja.
2. Kwa nini Paulo aliingiza sura juu ya upendo kwenye majadiliano ya karama za kiroho?
3. Elezea upendo wa *agapē* kwa maneno yako mwenyewe.
4. Kwa nini 1 Kor. 13:8-13 imekuwa uwanja wa vita juu ya karama za kiroho katika siku zetu?

# 1 WAKORINTHO 14

| MGAWANYO WA AYA WA WATAFSIRI WA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **UBS[4]** | **NKSV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB** |
| | | | | Heshima katika Ibada ya Hadhara (11:2 – 14:40) |
| Kunena kwa Lugha Na unabii | Unabii na Kunena kwa Lugha | Kati ya Karama Unabii ni zaidi ya Kunena kwa Lugha | Mengi zaidi Kuhusu Karama zitokazo Rohoni | Karama za Roho: mtizamo wa Umuhimu wake Katika jamii |
| 14:1-5 | 14:1-5 | 14:1-5 | 14:1-5 | 14:1-5 |
| | Kunena kwa Lugha Lazima Kutafsiriwe | 14:5-6 | | |
| 14:6-19 | 14:6-19 | 14:6-12 | 14:7-12 | 14:6-12 |
| | | 14:13-19 | 14:13-17 | 14:13-19 |
| | Kunena ishara kwa Wasioamini | | 14:18-19 | |
| 14:20-25 | 14:20-25 | 14:20-25 | 14:20-22 | 14:20-25 |
| Mambo yote kufanyika Katika Utaratibu | Utaratibu katika mikusanyiko ya kikanisa | | Utaratibu katika Kanisa | Utiishaji wa Karama za kiroho |
| 14:26-33a | 14:26-40 | 14:26-33a | 14:26-33a | 14:26-33a |
| 14:33b-36 | | 14:33b-36 | 14:33b-35 | 14:33b-35 |
| | | | 14:36-38 | 14:36-38 |
| 14:37-40 | | 14:37-40 | | 14:39-40 |
| | | | 14:39-40 | |

**MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI** (Kutoka **"Mwongozo wa Usomaji Mzuri wa Biblia A Guide to Good Bible Reading")**

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Haya ni maoni ya mwongozo kwa kujisomea, ikiwa na maana kuwa unawajibika binafsi kwa tafsiri ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mtoa maoni tu.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa,lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

29. Aya ya kwanza
30. Aya ya pili
31. Aya tatu

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA KWA 14:1-40

A. Hii inaendeleza miongozo ya Paulo kwenye ibada za mikusanyiko iliyoanza katika sura ya 11. Kanisa la Korintho lilikuwa linaabudu katika njia isiyo sahihi, isiyo na kipimo katika maeneo mengi

B. Kigezo kikuu kwa ajili ya tathmini ya taratibu za ibada ni "Je jambo hili linalijenga kanisa lote?"
Kusanyiko la ibada lina viini viwili;
   1. mahitaji ya wale waliopotea ambao walikuwepo
   2. mahitaji ya waaminio ambao walikuwepo
   
   Hii inafuata agizo kuu la Yesu (kama vile Mt. 28:19-20) *Hard Sayings of the Bible says,*
   
   "Kanuni ya Paulo ya utendaji kazi wa maisha na kusanyiko la waabuduo haibadiliki. Chochote kinachozuia injili kusonga mbele, kusababisha machafuko badala ya ukuaji, uharibifu badala ya kutia moyo ama kuongeza nguvu, kujenga ubinafsi kwa gharama ya wengine wote, hili ni kinyume na kusudi la Mungu. Na kwa vile wanawake katika Korintho na mahali pengine kwenye makanisa machanga walitumia karama zao kinyume na kusudi la Mungu, amri ya kukataza au kunyamazisha sio yenye kufaa neno la mamlaka. Kanuni inayoweka msingi katazo la kunyamazisha ni la mamlaka kwa wote wanaume na wanawake katika makanisa yote" (uk .616)

C. Sasa kwa habari ya swala lenye kuleta ubishi juu ya kushiriki kwa wanawake kwenye makusanyiko ya ibada. Ukisoma wafasiri watano utapata mitazamo mitano tofauti. Tatizo linaonekana kwamba sote tunakuja katika sura hii na ajenda binafsi, ya kimadhehebu, ki-uzoefu, na ki-tafsiri. Hakuna mtu upande wetu ambaye hapendelei upande wo wote. Tuinachukulia Biblia kwa kumaanisha, lakini katika Biblia hata Paulo hunena kwa kauli mbili (kama vile 1 Kor. 11:5 dhidi ya 14:34).

   Wafasiri wengine hata hujaribu kuondoa 1 Kor. 14:34-35 kama nyongeza ya kimaandishi (MSS D, F, G wameweka aya hizi baada ya 1 Kor. 14:40) ama wanazipeleka kwa Paulo akinukuu wito wa walimu wa uongo. Pande zote mbili za mitazamo huifanya sura kunena kinyume kabisa na kile kinachonekana kukisema.

D. Maneno ya Paulo katika 1 Kor. 14:35 yanahusiana na desturi ya Kiyahudi na utamaduni wa Wagiriki – Waroma.

E. Jamii ya ulimwengu wa Mediterania kwnye karne ya kwanza ilisimikwa kwenye utumwa pamoja na mfumo dume. Kwa Yesu ama Paulo kuwa amebadilisha yoyote kati ya misingi ya mifumo ya kijamii iliyokuwepo ingeathiri makuzi ya kanisa, na hata uhai wake. Wote wawili Yesu na Paulo wanathibitisha heshima na thamani ya binadamu wote. Injili katika wakati ujao itaangamiza vipengele vyote vya utendaji mbovu na uhalifu. Ni salama kusema kwamba waliyazungumza haya katika siku zao kwa nguvu iliyovuviwa na kwamba maneno yao yalielekeza kwenye siku ya baadaye kwenye heshima na usawa.

F. Wanawake na viongozi wa watumwa katika kanisa la kwanza wangeathiri uinjilisti kinyume na matarajio. Ni sawa kama ilivyo leo, lakini kutokea upande mwingine katika jamii yetu wanawake wenye kujieleza kwa ufasaha waliona karama za kuhudumu watafikia kipengele cha jamii yetu kwa matokeo mazuri zaidi kuliko wengine. Hii bila njia yo yote ndiyo kutamani kiasi kikubwa cha wanawake kuwa viongozi wa kanisa, lakini utambuzi kwamba wote wameitwa, wamekirimiwa karama, wahudumu wa injili, waaminio wote! mimi sijaribu kuwatetea wanawake kwenye jukumu maalum la huduma, bali ninatetea kwa nguvu huduma ya waaminio wote (kama vile Efe. 4:12)

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : 1 WAKORINTHO 14:1-5**

**1 Ufuateni upendo, na kutaka sana karama za rohoni, lakini zaidi kwamba mpate kuhutubu.**
**2 Maana yeye anenaye kwa lugha, hasemi na watu, bali husema na Mungu; maana hakuna asikiaye; lakini anena mambo ya siri katika roho yake. 3 Bali yeye ahutubuye, asema na watu maneno ya kuwajenga, na kuwafariji, na kuwatia moyo. 4 Yeye anenaye kwa lugha hujijenga nafsi yake; bali ahutubuye hulijenga kanisa.**
**5 Nami nataka ninyi nyote mnene kwa lugha, lakini zaidi sana mpate kuhutubu, maana yeye ahutubuye ni mkuu kuliko yeye anenaye kwa lugha, isipokuwa afasiri, ili kusudi kanisa lipate kujengwa.**

**14:1**"**Ufuateni upendo**" Hii ni KAULI TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO (kama vile Rum. 14:19; 1 The. 5:15; 1 Tim. 6:11; 2 Tim. 2:22) inaonyesha unganisho la ki-muktadha na sura ya 13. Upendo ni tabia ya Mungu na watu wake (kama vile Gal. 5:22; 1 Yohana 4:7-21). Kumbuka, sura ya 11-14 ni maandishi ya aina moja yanayohusu matatizo yanayohusiana na kusanyiko la ibada katika Korintho.

**NASB "tamanini kwa moyo wote *karama* za rohoni"**
**NKJV "tamanini karama za kiroho"**
**NRSV "hangaikieni karama za kiroho"**
**TEV "wekeni mioyo yenu juu ya karama za kiroho"**
**NJB "kuwa na shauku, pia, kwa ajili ya karama za kiroho"**

Hii ni kauli nyingine TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO kutoka kwenye mzizi wa neno "kuchemka" (kama vile 1 Kor. 12:31). Hii inaonyesha ungamanisho la ki-muktadha na sura ya 12. Kwa maana hiyo sura ya 13 inavunja na kuingia kwenye muktadha. Kumbuka kwamba sura ya 12-14 ni taarifa iliyofanywa kuwa moja kuhusu matumizi yanayofaa katika karama za kiroho. Neno "rohoni" ni sawasawa na lile lililotumika katika 1 Kor. 12:1 1 Kor. 12:1 (kama vile 1 Kor. 2:13,15; 3:1; 9:11; 10:3,4; 14:37; 15:44,46). Hili linaweza kuhusiana na karama, watu, vitu nk. Muktadha ubainisha maana

◙ "**lakini zaidi kwamba mpate kuhutubu**" Neno "kuhutubu" limetumika katika 1 Wakorintho katika maana maalum. Haihusu ile shughuli ya kinabii, manabii wa AK (yaani andiko lililoandikwa) bali kwenye mawasiliano ya wazi ya injili yawe ya mahubiri ya hadhara ama ushuhuda wa faragha. Inapaswa kutamaniwa na waaminio wote (kama vile 1 Kor. 14:39), lakini pia ni karama za kiroho (kama vile 1 Kor. 12:10, 28-29). Waaminio wote hushiriki kwa kiwango fulani katika karama zote za Roho, lakini mmoja au mwingine hutiwa nguvu na kuwezeshwa na Roho miongoni mwa waaminio binafsi kwa matokeo maalum yenye kuzaa matunda. Kuhitilafiana kunahitaji roho ya uhusiano na upendo miongoni mwa waaminio. Tunaitwa tuwe na umoja sio kufanana kwa ajili ya injili. Tunakuwa wenye matokeo mazuri tunaposhirikiana kama kitu kimoja. Tunahitaji waaminio wengine kwa kila hali, kanisa ni jumuia ya watumishi wa muda wote walioitwa wenye karama; tumepewa karama kwa ajili ya kueneza injili na afya na uzima wa kanisa. Karama hii inapimwa na kunena kwa kipimo cha "Je inalijenga kanisa lote?" inamaanisha kwenye muktadha huu "kutangaza injili" ambako ni Baraka kwa kanisa lote pamoja na wageni. Kunena kwa lugha ni Baraka kwa aaminiye binafsi pale tu kunapotafsiriwa kwa kanisa lote. Neno hili halipaswi kueleweka katika maana ya ufunuo uliovuviwa (Angalia MADA MAALUM: UNABII KATIKA AGANO LA KALE (SPECIAL TOPIC: OLD TESTAMENT PROPHECY) katika 1 Kor. 12:10)

MADA MAALUM: UNABII KATIKA AGANO JIPYA (SPECIAL TOPIC: NEW TESTAMENT PROPHECY)

**14:2**
**NASB, NKJV,**
**NRSV, NJB"katika lugha"**
**KJV"katika *lugha isiyojulikana*"**
**TEV"katika lugha ngeni"**

Hili ni neno la Kiyunani *glōssa* ambalo lilitumika ki-sitiari kuzungumzia lugha maalum au lahaja. Uzoefu wa kunena kwa lugha siku ya Pentekoste ni dhahiri kulihusu lugha ya kibinadamu inayofahamika (kama vile Matendo 2:6-10) muujiza unaonekana kuwa katika sikio (yaani kila mmoja wao akiwasikia akizungumza katika lugha yake mwenyewe. Tukio hili lilitendeka mara kadhaa kwenye matendo kwa kusudi la kuwathibitishia waaminiuo wa Kiyahudi kwamba Mungu amelikubali kusudi lingine la watu (yaani Wasamaria, maskani wa Kirumi, Mataifa)

Hata hivyo, katika 1 Wakorintho "kunena kwa lugha" kunaonekana kuwa pamoja na matamshi yenye hisia zenye shauku kubwa yenye mwaguzi wa Kiyunani, kama Delphi, ambapo mwanamke alitabiri na mtu mwingine akatafsiri kila alichosema. Watu kutoka katika ulimwengu wote unaoujua walikuwa Korintho, na bado maandiko yanatamka kutafsiri lugha "kama karama za kiroho" (kama vile 1 Kor. 12:10,30; 14:26), sio tu mtu anayetokea kusema kwa lugha ngeni"

◙"**Hasemi na watu, bali husema na Mungu**"Lugha za Wakorintho ni mazungumzo ya faragha kati ya Mungu na aaminiye (kama vile 1 Kor. 14:24) lugha zenyewe sio njia ya mawasiliano bali ushirika wa ndani sana na Mungu. Ni pale tu inapotafsiriwa ndipo mnenaji na msikilizaji wanaelewa.

◙"**Maana hakuna asikiaye**" Lugha katika Korintho yaonekana kuwa sauti isiyojulikana, inayosemwa wazi wazi kwa maneno. Pale Delphi mtu mmoja mahususi (kwa kawaida mwanamke) angetamka maneno yaliyoeleweka waziwazi kisha mwingine angetafsiri kwa ajili ya Yule aliyekuwepo. Utaratibu huu waonekana kufananishwa na uzoefu wa "lugha" katika Korintho. Hakuna anayetafsiri katika matendo.

**14:3**"**Kujenga**" Hiki ni kipimo cha tatu kinachotumika kutathmini karama za rohoni (angalia Tambuzi wa Kimuktadha katika sura ya 12c) Je zinainua nia ama kulijenga kanisa? Dhamira hii inarudiwa tena na tena katika sura hii 1 Wakor 14:3, 4, 5, 12, 17, 26. Ndiyo maana "kuhutubu" kukieleweka kama kushirikisha injili, kunapaswa kutamaniwa zaidi ya kunena "lugha" kuhutubu, kutangaza injili kwa watu waliopo wakati lugha hubariki mnenaji isipokuwa zitafsiriwe. Kama zitatafsiriwa lugha pamoja na tafsiri zake kutimiza kusudi lile lile la kutangaza injili (yaani kuhutubu) Angalia. MADA MAALUM: KUADILISHA ( SPECIAL TOPIC: EDIFY) katika 1 Kor. 8:1

◙"**Na kuwafariji, na kuwatia moyo**" Kusudi la kutangaza injili sio kwa uinjilisti pekee lakini pia kwa kuhamasisha kanisa (yaani kujenga, kufariji na kutia moyo)

**14:4**"**Yeye anenaye kwa lugha hujijenga nafsi yake**" Lugha za Wakorintho bila nkutafsiriwa ni karama zitokanazo na mtu binafsi.

◙"**Kanisa**" Hili ni neno *ekklesia* bila KIBAINISHI linalorejea mwili mzima wa mwamini. Shauku kuu ya Paulo ni kwamba, waaminio wote wala sio wateule wachache wabarikiwe kwenye kusanyiko la ibada. Angali Mada Maalum katika 1 Kor. 1:2

**14:5**"**Nami nataka ninyi nyote mnene kwa lugha**" Pamoja na 12:30 nakumbuka kirai hiki ni KISHAZI KINACHOJITEGEMEA kwa kile kinachofuata. Paulo hashushi hadhi ya kunena kwa lugha lakini (1) anatetea uhusiano wao sahihi na karama nyingine za rohoni na (2) anaweka miongozo ya kutekelezwa. yaonekana Wakorintho walikuwa wanatafuta karama hii kwa ajili ya furaha, utukufu binafsi na heshima yao.

◙ "**Maana yeye ahutubuye ni mkuu kuliko yeye anenaye kwa lugha**" Hii ni tathmini iliyoegemea ile sifa ya Paulo kwamba kunena kwa lugha ni kwa thamani ya chini katika kulijenga kanisa lililokusanyika. Lakini kumbuka kwamba kunena kwa lugha ni karama halali ya roho (kama vile 1 Kor. 14:18,39)!

◙"**Isipokuwa afasiri**" Hii ni SENTENSI YENYE MASHARTI DARAJA LA TATU inayotambulishwa na *ei* badala ya *ean*, Je yawezekana mtu mmoja kuwa na karama zote mbili ya kunena na ya kutafsiri? Ni dhahiri kutoka maandiko mengine kwamba viongozi wa kanisa walikuwa na karama za kiroho zaidi ya moja (kama vile Matendo 13:1; 2 Tim. 1:11). Hata hivyo kama ingewezekana kwa mtu yule yule kunena kwa lugha na kisha kufasiri kwa nini mtu

anahitaji mfasiri? Ni kwa jinsi gani huu muunganiko utofautiane na kuhutubu. Labda yawezekana kwamba aaminiye mmoja kuwa na karama zote mbili ambazo hutumika kwa nyakati tofauti tofauti lakini sio mara nyingi (kama vile 1 Kor. 14:13). Uwezekano mkubwa zaidi ni kwamba Paulo anatumia mbinu ya kifasihi kusisitiza hitaji la kuelewana kimawasiliano kwenye kusanyiko la ibada.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : 1 WAKORINTHO 14:6-12**

**6 Ila sasa, ndugu, nikija kwenu na kunena kwa lugha, nitawafaidia nini, isipokuwa nasema nanyi kwa njia ya ufunuo, au kwa njia ya elimu, au kwa njia ya hotuba, au kwa njia ya fundisho? 7 Hata vitu visivyo na uhai vitoapo sauti, ikiwa ni filimbi, ikiwa ni kinubi, visipotoa sauti zilizo na tofauti, itatambulikanaje ni wimbo gani unaopigwa kwa filimbi au kwa kinubi? 8 Kwa maana baragumu ikitoa sauti isiyojulikana, ni nani atakayejifanya tayari kwa vita? 9 Vivyo hivyo na ninyi, msipotoa kwa ulimi neno lililo dhahiri, neno lile linenwalo litajulikanaje? Maana mtakuwa mkinena hewani tu. 10 Yamkini ziko sauti za namna nyingi duniani, wala hakuna moja isiyo na maana. 11 Basi nisipoijua maana ya ile sauti nitakuwa kama mjinga kwake yeye anenaye; naye anenaye atakuwa mjinga kwangu. 12 Vivyo hivyo na ninyi, kwa kuwa mnatamani sana kuwa watu wenye karama za roho, takeni kwamba mzidi sana kuwa nazo ili kulijenga kanisa.**

**14:6** "**isipokuwa**" Kuna SENTENSI nne zenye MASHARTI DARAJA LA TATU kwenye ibara, 1 Kor. 14:6-12 inaonyesha utendaji usiodhihirika (kama vile 1 Kor. 14:6,7,8,11) 1 Kor. 14:6 na 7 zote mbili ni maswali yanayotarajia jibu "hapana" (kama ilivyo 1 Kor. 14:9)

◙"**Kwa njia ya ufunuo, au kwa njia ya elimu, au kwa njia ya hotuba**" Neno hili linaonekana kuaksi karama tofauti,lakini tofauti haidhihiriki labda kwa kuwa viongozi wengi waliokirimiwa karama wametajwa katika Waefeso 4;11 kila mmoja akitangaza injili lakini akiwa na msisitizo tofauti, basi ndivyo hata hapa. Mungu huzifunua kweli zake kwa njia zinazotofautiana lakini maudhui ni yale yale, karama nyingi, injili moja; waaminio wengi walipewa karama; kusudi moja (yaani uadilishaji wa ukuaji wa kanisa kama vile Mt. 28:19-20; Luka 24:47; Matendo 1:8).

**14:7-8** Paulo anatumia vyombo vya muziki kujenga hoja, filimbi na vinubi katika 1 Kor. 14:7 na tarumbeta la jeshi katika 1 Kor. 14:8. Vyombo vya muziki vinatumika kwa makusudi tofauti tofauti (yaani kutoa muziki ama kutoa ishara) ikiwa chombo kitatoa sauti isiyo sahihi husababisha machafuko. Sauti ya mwanadamu imekusudiwa kuwakilisha habari kwa wanadamu wengine. Kama itatoa sauti ambayo haitakuwa na maana yo yote kwa wanadamu wengine itashindwa kutimiza kusudi lake (kama vile 1 Kor. 14:9).

**14:10** Hii ni SENTENSI YENYE MASHARTI YA DARAJA LA NNE isiyo ya kawaida. Aya hii haiwezi kutumika kuthibitisha kwamba lugha ni lugha zinazojulikana. Paulo anatumia neno tofauti (yaani *phōne* na sio *glōssa*) katika 1 Kor. 14:10 na 11. Hiki ni kielezo kilicho kigumu katika kuelewa lugha iliyotamkwa visivyo ama lugha ngeni. Lugha ya binadamu imekusudiwa kueleweka.

**14:11**
**NASB, NJB "mshenzi"**
**NKJV, NRSV,**
**TEV "mgeni"**

Hili lilikuwa neno la kuiga sauti au mlio wa kitu (yaani, *barbarous)* kwa sauti ngeni za lugha nyingine za Wayunani na Warumi, hasa kwa makundi ya kikabila kule kaskazini mwa himaya ya Warumi. Walisema kwamba lugha hizi za kikabila zilitoa matamshi yenye sauti kama "bar, bar" kwao. Ndiyo mwanzo wa neno "mshenzi"

**14:12** "**Kwa kuwa mnatamani sana kuwa watu wenye karama za roho**" Paulo hahukumu shauku yao (kama vile 1 Wakor 14:1) lakini anajaribu kuelekeza kwenye kulijenga kanisa lote (kama vile 1 Kor. 12:7)

**NASB, NKJV,**
**NRSV, NIV "karama za Rohoni"**

**RSV "udhihirisho wa Roho"**
**TEV "karama za Roho"**
**NJB"nguvu za kiroho"**

Hili silo neno lile lile la Kiyunani kama katika 1 Kor. 12:1 (yaani, *pneumatikōn)*, bali KIMILIKISHI CHA WINGI cha neno *pneuma* (angalia mada maalum: Roho katika Biblia 1 Kor. 12:1) ambayo ina maana ya "pumzi" "upepo" "roho." Muundo huu pia unapatikana 1 Kor. 12:10 ambapo unahusu karama maalum (yaani kupambanua roho kama vile 1 Yohana 4:1). Ki-muktadha yaonekana kwamba hili linahusu karama za rohoni tofauti tofauti zilizotolewa na Roho (kama vile 1 Kor. 12:11) kwa faida ya mwili wote (kama vile 1 Kor. 12:7)

◙ "**Takeni kwamba mzidi sana kuwa nazo ili kulijenga kanisa"** Hii ni KAULI TENDAJI SHURUTISHI YENYE UWINGI YA WAKATI ULIOPO. Lengo la karama za rohoni sio kuinuliwa na kutukuzwa kwa mtu binafsi bali afya na kukua kwa mwili wa Kristo, ambalo ni kanisa.
Kwa neno "kujazwa" Angalia Mada Maalum katika 2 Kor. 2:7

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : 1 WAKORINTHO 14:13-19**

**13wa sababu hiyo yeye anenaye kwa lugha na aombe apewe kufasiri. 14 Maana nikiomba kwa lugha, roho**
**yangu huomba, lakini akili zangu hazina matunda. 15 Imekuwaje, basi? Nitaomba kwa roho, tena nitaomba**
**kwa akili pia; mtaimba kwa roho, tena nitaimba kwa akili pia. 16 Kwa maana wewe ukibariki kwa roho, yeye**
**aketiye katika mahali pa mjinga ataitikaje, Amina, baada ya kushukuru kwako, akiwa hayajui usemayo? 17**
**Maana ni kweli, wewe washukuru vema, bali yule mwingine hajengwi. 18 Namshukuru Mungu ya kuwa**
**nanena kwa lugha zaidi ya ninyi nyote; 19 lakini katika kanisa napenda kunena maneno matano kwa akili**
**zangu, nipate kuwafundisha wengine, zaidi ya kunena maneno kumi elfu kwa lugha.**

Katika muktadha hili linamaanisha kuwa kuwaiwasilisha injili kwa wote ni bora zaidi kwa hisia binafsi (kama vile 1 Kor. 14: 15). Je! Mstari huu unamaanisha kwamba waamini wanapokea karama moja katika wokovu (kama vile 1 Kor. 12:11), lakini anaweza kuomba apate nyingine? Swali hili lazima libaki bila kujibiwa. Ni hakika kwamba baadhi walikuwa na karama kadhaa (kama vile Mdo. 13:1; 1 Tim. 2:7; 2 Tim. 1:11).

**14:14 "Ikiwa"** Hii ni SENTENSI YENYE MASHARTI DARAJA LA TATU nyingine kama ilivyo 1 Kor. 14:6,7,8,11,23,24,28, na 29

◙ "**Roho yangu huomba**" Hii inarejelea roho ya binadamu. Hii Ilikuwa sitiari ya kifasihi kwa ubinadamu.

◙ "**lakini akili zangu hazina matunda**" Paulo alikuwa akiomba juu ya upendo wa Wakorintho kwa hekima. Pia alikuwa anathibitisha kwamba kunena pekee hakukuweza kufanya mawasiliano hata kwa msemaji.

**14:15**
**NASB "matokeo yake ni nini basi"**
**NKJV "Matokeo yake ni nini basi"**
**NRSV, TEV "Nifanye nini basi"**
**NJB "Nini basi"**

Hii ni nahau (1 Kor. 14:26; Matendo. 21:22) Paulo anataka kuweka hitimisho kwenye mjadala wake.

◙"**Nitaimba kwa roho**" Hii inamaanisha kudokeza karama nyingine ya rohoni? (kama vile 1 Kor. 14:26; Kol. 3:16; Efe. 5:19)

**14:16** "**Ikiwa**" Hii ni SENTENSI nyingine YENYE MASHARTI DARAJA YA TATU, KAMA N1 Ko. 14:6, 7, 8, 11 na 14.

**NASB "yeye aketiye katika mahali pa mjinga"**
**NKJV "yeye ajazaye mahali pa asiyehabarishwa"**
**NRSV "awezaje aliye katika nafasi ya nje"**
**TEV "Hawa wa kawaida waliokuja kwenye kusanyiko"**
**NJB "mtu asiyefundishwa"**

Neno lilitumiwa kuhusu mtu ambaye hakuwa na habari ama asiyepata mafunzo kwenye maeneo maalum, kwa hiyo, si mwenye weledi (kama vile Matendo 4:13; 2 Kor. 11:6). Matumizi hapa ya 1 Kor. 14:23-24 yaweza kuwa na moja ya maana mbili zinazowezekana.

1. Mgeni wa mara kwa mara kwenye kusanyiko la Kikristo wakati katika 1 Kor. 14:23 yawezekana mgeni aliyekuja kwa mara ya kwanza.
2. bila shaka Mkristo mpya, lakini ambaye hana karama ya kunena au kutafsiri

Kifungu cha neno "mahali pa" kinakuwa kati ya (1) wageni ama yawezekana Wakristo wapya waliopewa vitu maalum ili waweze kusikia sawasawa ama (2) lahaja kwa mtu ambaye hajaelewesha.

◙"**Sema Amina"**Angalia Mada Maalum hapa chini

Inawezekana kwa hakika kwamba neno lililopo juu lingeweza kuhusu mwamini asiye na karama (Angalia F.F. Bruce, *Answers, to Question*, uk. 98). Kama ni kweli basi Paulo alitaka waaminio wachunguze ama "kupitisha hukumu juu ya" maneno ya kinabii yaliyozungumzwa kwenye makusanyiko ya ibada (kama vile 1 Kor. 2:12,15; 14:29,37; 1 The. 5:20-21; pia angalia 1 Yoh. 4:1). Hapana ambaye angeweza kusema "amina" mpaka

1. waliewa kile kilichokuwa kinanenwa
2. walikuwa na njia (yaani, yule Roho) kutathmini kile kilichokuwa kinanenwa

## MADA MAALUM: AMINA (SPECIAL TOPIC: AMEN)

**14:16, 17 "kwenye kutoa kwako shukrani"** Kifungu hiki chaweza kuhusu meza ya Bwana iliyoitwa the *Eucharist* kutoka katika neno la Kiyunani "toa shukrani." Aya ya 17 hata hivyo yaonyesha kwamba kinahusu maombi.

◙"**mtu mwingine**" Angalia maelezo katika 1 Kor. 6:1

**14:18** "**Namshukuru Mungu ya kuwa nanena kwa lugha zaidi ya ninyi nyote**" Paulo alijua alichokuwa anazungumzia. Aya hii ikiunganishwa na 1 Kor. 14:39, inafanya Wakristo wa kisasa kufikiri mara mbili kabla hawajahoji kwa nia ya kutafuta makosa kuhusu dhana ya kunena kwa lugha kwenye siku zetu. Pia inapaswa kuwafanya wale wanaosisitiza kufikiri mara mbili. Paulo anaikubali ili kuishushia hadhi.

Inapendeza jinsi surah ii inavyobadilika katikati ya UMOJA 1 Kor. 14:2,4,9,13,14,19,26,17, na WINGI, 1 Kor. 14:5,6,18, 22,23,39.

Wasiwasi katika kanisa hili ulikuwa (1) Katikati ya vikundi vya kijamii na (2) katikati ya watu binafsi waliokuwa na karama ujengaji wa shirika lote. Ndani ya kanisa mtu binafsi wakati wote anahudumia shirika (kama vile 1 Kor. 12:7). Huu ni mfano mwingine wa Paulo akijaribu kujifananisha angalau kwa kipimo fulani, na waaminio wa Korintho waliokuwa na shauku kupindukia kwani alithibitisha elimu, lakini alisisitiza upendo, sasa anathibitisha kunena kwa lugha lakini anasisitiza kujengana.

**14:19** Lakini kanisani natamani kunena maneno kwa akili zangu kuliko kunena maneno elfu kumi kwa lugha. Baadhi ya maandishi ya sura ya 11-14 yanahusu hadhara ya kusanyiko la ibada (kama vile 1 Kor. 14:23,28,34). Katika mpangilio huu kuabudu kwa mtu binafsi katika lugha kuna Kor. 14:24-25) ama kujengwa ("ili kwamba niweze kuwafundisha wengine pia" kama vile 1 Kor. 14:3,4,5,12,1,19,26)

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : 1 WAKORINTHO 14:20-25**
**[20]Ndugu zangu, msiwe watoto katika akili zenu; lakini katika uovu mgeuzwe watoto wachanga, bali katika akili zenu mkawe watu wazima. [21] Imeandikwa katika torati, Nitasema na watu hawa kwa watu wa lugha nyingine,**

**na kwa midomo ya wageni, wala hata hivyo hawatanisikia, asema Bwana. [22]Basi, hizi lugha ni ishara, si kwao waaminio, bali kwao wasioamini lakini kuhutubu si kwa ajili yao wasioamini, bali kwa ajili yao waaminio. [23]Haya! Ikiwa kanisa lote limekusanyika pamoja, na wote wanene kwa lugha, kisha ikawa wameingia watu wajinga au wasioamini, je! Hawatasema ya kwamba mna wazimu? [24]Lakini wote wakihutubu, kisha akaingia mtu asiyeamini, au mjinga, abainishwa na wote, ahukumiwa na wote; [25] siri za moyo wake huwa wazi; na hivyo atamwabudu Mungu, akianguka kifudifudi, na kukiri ya kuwa Mungu yu kati yenu bila shaka.**

**14:20** "**Msiwe watoto**" Hii ni KAULI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO ikiwa na KIAMBATA HASI ambacho kwa kawaida kinamaanisha kukoma kufanya kitendo kinachoendelea. Walikuwa watoto kwenye eneo hili (kama vile Efe. 4:14), ingawa walidhani kwamba walikuwa wa kiroho sana na wenye hekima.

◙ "**Katika akili zenu**" Hili ni kutoka kwenye neno la Kiyunani kiwambo ama fumbatio. Hili, na sio wenye akili, palifikiliwa kuwa mahali pa kisaikolojia pa watu wa kale wenye kufikiri.

◙" **lakini katika uovu mgeuzwe watoto wachanga**" katika baadhi ya maeneo waaminio lazima wasifahamishwe (kama vile Mt. 10:16; Rum. 16:19) mojawapo ya kinga kuu dhidi ya uovu ni kuwa mjinga ama mshamba

◙ "**Mkawe watu wazima**" Paulo anatumia neno hili (yaani *telecos*) kumwelezea aaminiye ambaye anaelewa injili kikamilifu na anaishi kwayo (kama vile 1 Kor. 2:6; 13:10; 14:20; Efe. 4:13; Flp. 3:15; Kol. 1:28). Waaminio wote huanza kama Wakristo watoto wachanga na lazima wakue. Kuna viwango vya kuelewa na kuishi maisha ya utawa. Hata hivyo neno hili haumaanishi kutokuwa na dhambi kabisa bali kukamilika kiroho na kutengenezwa tayari kwa kutumika.

**14:21-22** Hii sehemu ya nukuu kutoka Isa. 28:11-12. Hii inahusiana na Ashuru iliyovamia Israeli, Mstari 22 inahusu nukuu na sio muktadha wote. Sentensi hii ni kinyume na yote ambayo Paulo anayasema katika muktadha lazima ihusu nukuu ya Agano la Kale tu. Paulo anatumia "ishara" katika njia mbili; hukumu na neema. 14:21 "katika torati" kwa kawaida katika muktadha wa Kiyahudi, hii ingekuwa maandiko ya Musa (Mwanzo-Kumbukumbu la Torati) lakini sio kila wakati. Katika Yohana 10:34; 12:34 na 15:25, kirai hiki kinarejea nukuu kutoka katika Zaburi kama ilivyo katika Rum. 3:9, kirai hiki hiki kinatumika katika 1 Kor. 14:34 lakini hakuna uhakika kinarejea juu ya maandiko yapi labda Mwanzo 3.

Walter Kaiser, katika *Toward An Exegetical Theology*, uk. 110 anatoa maoni yenye kupendeza kwamba mistari ya 34 na 35 ni nukuu kutoka kwenye barua ambayo Paulo aliipokea kutoka kanisa la Korintho. Kwa kawaida majibu ya Paulo kwa maswali yao yaliyoandikwa yanatambulishwa kwa kirai "sasa kuhusiana" (kama vile 1 Kor. 7:1,25; 8:1; 12:1; 16:1), lakini si nyakati zote (yaani nukuu inayoonekana kutoka kwenye barua iliyopatikana katika 1 Kor. 6:12 na 10:23) kama hiyo ni kweli basi "torati nayo yasema" yaweza kuhusu Zab. 68:11 ambayo inarejelewa bila nukuu 1 Kor. 14:36; Zab. 68:11 inathibitisha kutangazwa kwa habari njema kwenye makusanyiko na wanawake. Gordon Fee katika fasihi yake juu ya 1 Kor. (New International Commentary) pia anadai kwamba Paulo hakuandika 1 Kor. 14:34,35 uk. 699-708)

**14:23 "ikiwa"** Hii ni SENTENSI nyingine DARAJA LA TATU (kama vile 1 Kor. 14:6,7,8,11, na 14).

◙ **"Kanisa lote limekusanyika pamoja"** Muktadha wa kifasihi wa sura ya 11-14 inashughulika na miongozo ya makusanyiko ya ibada. Kwa kawaida makanisa haya ya awali (tazama mada maalum katika 1 Kor. 1:2) yalikutana kwenye nyumba za faragha yaani makanisa ya majumbani)

Mara nyingi kwa ukubwa wa mji kama Korintho kungekuwa majumba mengi sana yaliyohusika. Hii yaweza kuwa mojawapo ya sababu ya kushamiri kwa vikundi vidogo vidogo ndani ya kanisa. Maneno ya Paulo yanaashiria huenda ni kundi kubwa la kusanyiko lililokuwa likisheherekea sherehe ya upendo 1 Kor. 11:17-34 na meza ya Bwana. Ni mara ngapi na wapi walikutania hakuna hakika yoyote. Kutokana na aya hii ni wazi wageni waliruhusiwa, ambavyo inaonyesha kwamba haikuwa siri au kusanyiko la kujifungia ndani.

**NASB "kwamba mna wazimu"**
**NKJV, NRSV"ninyi mmechanganyikiwa"**
**TEV "ninyi nyote ni vichaa"**
**NJB "ninyi nyote mu wapaukaji"**

Neno hili (yaani, *mainomai*) limetumika katika Matendo 12:15 na 26:24-25. Katika Yohana 10:20 hili limetumika kueleza juu ya kupagawa na pepo. Neno hili halimaanishi ukichaa, bali kupagawa na roho. Katika utamaduni wa Kiyunani jambo hili lingeonekana kama hali ya kiroho yenye upendeleo, lakini sivyo katika Ukristo.

**14:24 "ikiwa"** Hii ni SENTENSI nyingine YENYE MASHARTI DARAJA LA TATU (kama vile 1 Kor. 14:6,7,8,11,14,23,24,28,29).

**NASB "hukumiwa. . .itwa kutoa maelezo"**
**NKJV "hakikishwa. . .kuhukumiwa"**
**NRSV "kemewa. . .itwa kutoa maelezo"**
**TEV "hakikishwa juu ya dhambi yao. . .hukumiwa"**
**NJB "kujikuta umewekwa katika jaribio. . .hukumiwa"**

Unabii huleta kuelewa na kusadiki; kunena huleta machafuko kwa wasioamini ama waaminio wapya.

◙**"wote… wote… wote"** Hii haimaanishi kwamba kila aaminiye alinena katika kila huduma ya ibada, bali kwamba kila kilichofanyika kwenye huduma ya ibada kiliongezea kwenye kuthibitika kiroho jambo ambalo wageni na ikiwezekana waaminio wapya walipata uzoefu. Neno "wote" hakika linajumuisha waaminio wanawake walihudhuria.

**14:25 "Siri za moyo wake huwa wazi"** Hii yaweza kuhusu ukweli kwamba
1. Mungu hujua mawazo ya binadamu na huleta hukumu kwa kutumia Roho Wake (kama vile 1 Kor. 24)
2. Kukiri/kuungana dhambi ilikuwa sehemu ya ibada kwenye karne ya kwanza (kama vile Mt. 3:6; Mk. 1:53; Matendo. 19:18 na Yakobo. 5:16.

## MADA MAALUM: MOYO (SPECIAL TOPIC: MOYO)

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : 1 WAKORINTHO 14:26-33**
**26Basi, ndugu, imekuwaje? Mkutanapo pamoja, kila mmoja ana zaburi, ana fundisho, ana ufunuo, ana lugha, ana tafsiri. Mambo yote na yatendeke kwa kusudi la kujenga. 27Kama mtu akinena kwa lugha, wanene wawili au watatu, si zaidi, tena zamu kwa zamu, na mmoja na afasiri. 28 Lakini asipokuwapo mwenye kufasiri na anyamaze katika kanisa; aseme na nafsi yake tena na Mungu. 29 Na manabii wanene wawili, au watatu, na wengine wapambanue. 30Lakini mwingine aliyeketi akifunuliwa neno, yule wa kwanza na anyamaze. 31Kwa maana ninyi nyote mwaweza kuhutubu mmoja mmoja, ili wote wapate kujifunza, na wote wafarijiwe. 32Na roho za manabii huwatii manabii. 33 Kwa maana Mungu si Mungu wa machafuko, bali wa amani; vile vile kama ilivyo katika makanisa yote ya watakatifu.**

**14:26-33** Hii hutupatia utambuzi ndani ya huduma ya ibada yenye nguvu isiyowekewa miundo ya kanisa la awali. Yaonekana kufikia muda huo hapatakuwepo watumishi wa kanisa wasomi. Mtu ye yote aliweza na alizungumza kwa uhuru. Matatizo yalitokea kwenye maeneo mawili
1. kulikuwa na vurugu kwa sababu watu wengi walipenda kusema
2. walikuwa wakiingiliana katika kusema

Paulo anajaribu kuweka muundo kwenye huduma ya ibada ya waliokusanyika kwa jinsi ambavyo hataki kuweka kizuizi katika uhuru wa roho lakini kusisitiza kusudi la kusanyiko ambalo ni wokovu wa wasiookoka na kukomaa kwa waliookoka (kama vile Mt. 28:19-20). Huu sio mpangilio mzuri kwa minajiri ya kupangilia kitu (kama vile 1 Kor. 14:32)! Paulo hatafuti namna ya kudhibiti ibada!

**14:26 "Matokeo ni nini"** Angalia nukuu katika msitari wa 15.

◙ **"Kila jambo litendeke kwa ajili ya kujenga"** Hili ni agizo linalojirudia rudia (yaani, KAULI TENDWA [shahidi] SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO. Kusudi la karama za rohoni sio kumpa utukufu mtu, bali ukuaji (ki-idadi na kukomaa) wa kanisa. Kwa maneno mengine "Je kitendo hiki au muundo huu unakamilisha kusudi la Agizo kuu la Yesu" (kama vile Mt. 28:19-20)?

**14:27"ikiwa"** Hii ni SENTENSI YENYE MASHARTI DARAJA LA KWANZA. Paulo hathibitishi vitendo vyao, bali anaangalia vitendo vyao.

**14:28"ikiwa"** Hii ni SENTENSI YENYE MASHARTI DARAJA LA TATU. Paulo anatamani kwamba kusanyiko la ibada litoe habari za kiroho kwa wote walio hudhuria. Kunena kwa lugha kunaafikiwa ikiwa kunatafsiriwa. Kusanyiko la ibada sio wakati na mahali kwa ajili ya uzoefu wa faragha na kuabudu ili kutawala kusudi la ushirika.

◙ **"kufasiri na anyamaze katika kanisa"** Hii ni KAULI TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO. Kunena kwa lugha na unabii ni vitu vinavyodhibitiwa na mtu aliyekilimiwa (kama vile 1 Kor. 14:30). Uadilishaji wa mwili wa Kristo na uinjilist, na sio uhuru binafsi, ndio mlengo wa ibada ya hadhara.

**14:29** Manabii hawana uhuru usiohojiwa (yaani, somo, muda, au maudhui) katika kuzungumza. Wanapaswa kutathiminiwa na waaminio wengine wenye karama (kama vile 1 Kor. 14:30 na 12:10; 1 Yohana 4:1-3). Kumbuka waliopagawa na mapepo walikuwemo ndani ya sinagogi wakati Yesu alipokuwa anasema na kwenye mahubiri ya nje.

◙**"wengine wapambanue"** Angalia nukuu katika 1 Kor. 4:7 na Mada Maalum katika 1 Kor. 10:29.

**14:30 "ikiwa"** Hii ni SENTENSI YENYE MASHARTI DARAJA LA TATU (kama vile 1 Kor. 6,7,8,11,23,24,28,29).

◙**"yule wa kwanza na anyamaze"** Hii ina ufanano na 1 Kor. 14:28 (yaani, KAULI TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO). Hii inamaanisha kwamba mnenaji anaweza kuingiliwa kati na mwamini mwingine na kwamba mnenaji anayeendelea amsikilize mnenaji mpya kabla hajajibu ama kuongeza kwenye ufunuo. Huduma hizi za awali zilikuwa zenye tabia ya msukumo na zenye kuruhusu kunena bila kujiandaa. Hii inahitajika kwa baadhi ya tabia kuwepo na hitaji la utaratibu thabiti wenye nguvu kwa ajili ya tabia zingine!
Sasa swali ni "huu ulikuwa mfumo wa kawaida kwenye makanisa yote ya Paulo ama ni kipengele cha pekee cha kanisa la Korintho? Je tunachukua mjadala huu kama shahidi wa Agano Jipya wa jinsi ibada zote zinavyopaswa kupangiliwa au ni mfano tu wa jinsi ya kushugulikia tatizo kwenye eneo hili ?

**14:31"ninyi nyote mwaweza kuhutubu mmoja mmoja" Kifungu hiki kiknaweza kuchukuliwaje ki-fasihi**? Je Paulo anaanzisha mfumo ama fursa isiyo na mipaka kwa mmoja wa waaminio na wote kuzungumza kwenye huduma ya ibada? Je hapakuwa na mipaka ya muda kwenye huduma za makusanyiko siku hiyo? Huu ni mfano wa kauli halisi!
Hata hivyo neno "wote" inamaanisha kwamba wote wanawake na wanaume waweze kuhutubu (kama vile 1 Kor. 11:5). Waaminio wote wamepewa karama kwa nia njema (kama vile 1 Kor. 12:7; 14:26). Hili linaongeza ufafanuzi zaidi katika 1 Kor. 14:34!

◙**"ili wote wapate kujifunza, na wote wafarijiwe"** Hiki kishazi nia (yaani, *hina*) kinaelezea juu ya hitaji kuu la Paulo, sio kwamba wote wanaweza kunena, lakini wote wakapate kujengeka, kuadilishwa, na kukua! Hili ni somo linalorudiwa katika sura hii.

**14:32**
**NASB, NKJV,**
**NRSV "Roho za manabii huwatii manabii"**
**TEV "karama ya kutangaza ujumbe wa Mungu unapaswa kuwa chini ya mnenaji"**
**NJB "roho ya kinabii inapaswa kuwa chini ya roho ya nabii"**

Uchaguzi wa tafsiri waonyesha njia mbili tofauti ambazo kifungu hiki kinaweza kueleweka.

1. Wale wanao hutubu ujumbe wa Mungu wanawajibika kwa (yaani, KAULI TENDWA YENYE KUARIFU YA WAKATI ULIOPO) wengine ambao huhutubu ujumbe wa Mungu (yaani manabii huwapima manabii, 1 Kor. 14:29).
2. Yeye Yule ahutubuye ujumbe wa Mungu anajitawala (yaani, KAULI YA KATI YENYE KUARIFU YA WAKATI ULIOPO) juu ya kile anacho kinena na wakati anapokinena (kama vile 1 Kor. 14:30).

Neno "roho" linatumika katika njia hiyo hiyo kama katika 1 Kor. 14:2,14,15 (mara mbili), 16. Ni njia ya nahau ya kurejea kwenye ubinadamu wa mtu (kama vile 1 Kor. 2:11; 5:3-4; 7:34; 16:18). Tazama nukuu katika "kujiweka chini ya" katika 1 Kor. 16:16 na Mada Maalum katika 2 Kor. 9:13.

**14:33**
**NASB "kwani Mungu sio Mungu wa machafuko bali wa amani"**
**NKJV "kwani Mungu sio mwangalishi wa machafuko bali wa amani"**
**NRSV, NJB "kwani Mungu ni Mungu sio wa uvurugu bali wa amani"**
**TEV "kwa sababu Mungu hapendi sisi tuwe kwenye uvurugu bali kwenye upatanifu na amani"**

Hii hairejerei kwenye uumbaji. Hii sio agizo dhidi machafuko, bali ugomvi wa ndani wa vikundi ndani ya kanisa ama binafsi/umimi dhidi ya amani. Hii sio kushusha hadhi ya tabia ya ibada yenye nguvu ya karne ya kwanza (kama vile 1 Kor. 14:39-40), lakini tabia ya wivu, ubinafsi wa baadhi ya wasemaji waliokuwa na vipawa (kama vile 2 Kor. 6:5; 12:20; Yakobo 3:16). Mtindo wa kuabudu na tabia vinaaksi juu ya Mungu tunayedai kuwa tunamwabudu (kama vile 1 Kor. 11:17-34).

◙**"vile vile kama ilivyo katika makanisa yote ya watakatifu"** Hakuna hakika kama kirai hiki kinaenda sambamba na 1 Kor. 14:33a (NASB, NKJV) ama na 1 Kor. 14:34 (NRSV, TEV, NJB). Kwasababu kirai "katika makanisa" kinarudia 1 Kor. 14:33b hufanya maoni ya kuhitimisha kama ifanyayo katika 33b ambayo hufanya maoni ya kuhitimisha kama ifanyayo katika 1 Kor. 4:17 na 7:17. Hiki kifungu chaeleza dhahiri kwa makanisa yote ya nyumbani kwamba wao hawako maalumu, wenye hadhi kubwa zaidi ama kwamba wana karama za kipekee (kama vile 1 Kor. 4:17; 7:17; 11:16; 14:33,36; 16:1). Angalia MADA MAALUM: WATAKATIFU (SPECIAL TOPIC: SAINTS) katika 1 Kor. 1:2.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : 1 WAKORINTHO 14:34-36**
**[34] Wanawake na wanyamaze katika kanisa, maana hawana ruhusa kunena bali watii, kama vile inenavyo torati nayo. [35] Nao wakitaka kujifunza neno lo lote, na wawaulize waume zao wenyewe nyumbani mwao; maana ni aibu wanawake kunena katika kanisa. [36] Au je! Neno la Mungu lilitoka kwenu? Au kuwafikia ninyi peke yenu?**

**14:34"Wanawake na wanyamaze katika kanisa"** Aya hii imekuwa hoja kuu ya kithiolojia miongoni mwa makundi mbalimbali katika kanisa la siku hizi. Mtindo wa kimagharibi wa kisasa, kijamii, na kitamaduni kuelekea haki za mtu binafsi na usawa umelifanya Agano Jipya na hasa Paulo, aonekane kuwa mwenye kuhukumu na kuwa kinyume katika hoja hii. Wakati wa siku za Paulo theolojia yake kuhusu wanawake ilikuwa chanya kimsingi. (kama vile Efe. 5:22-23). Paulo bila shaka alifanya kazi na wanawake wengi, kama anavyo orodhesha watenda kazi wenza katika Warumi 16 inavyoonekana. Pia angalia Mada Maalum: Wanawake katika Biblia 1 Kor. 7:5.

Hata kwenye muktadha huu, Paulo anatamka uwiano wa 1 Kor. 11:5 dhidi ya 14:34. Kwa namna Fulani 1 Kor. 14:34-35 inahusiana kipekee na Korintho na karne ya kwanza. Nadharia ni kikosi cha askari wa Kirumi (tazama Mada Maalum) jinsi inavyohusiana na siku zetu ni matatizo. Hali ya kuweka kauli kwa njia ya nguvu kimamlaka ya kidini na kuhakiki maandiko ni jambo lisilo sahihi, "ushahidi wa kibiblia sio swala la kufanana wala mfumo wa mawazo ya aina moja kwenye hoja hii," 1 Kor. 14:28,30,34.

Palikuwepo na tatizo katika kusanyiko la ibada huko Korintho. Wanawake wa Kikristo walikuwa sehemu ya tatizo. uhuru wao pya katika Kristo (au kuwa kwao kundi huru la wanawake wa jamii ya Kiroma) kulisababisha matatizo kitamaduni, kithiolojia, na kiinjilisti. Katika siku zetu za leo kinyume na hayo yaweza kuwa kweli.

Wanawake viongozi waliokilimiwa watalisaidia kanisa la karne ya 21 kuufikia ulimwengu kwa injili. Hii hauathiri utaratibu wa uumbaji uliotolewa na Mungu, lakini unaonyesha kipaumbele cha uinjilisti (kama vile 1 Kor. 9:22). Hili suala si suala la injili wala la kimaandiko.

## MADA MAALUM: WANAWAKE KATIKA HUDUMA (SPECIAL TOPIC: WOMEN IN MINISTRY

## MADA MAALUM: NADHARIA ZIHUSUYO "WANAWAKE KUKAA KIMYA" (SPECIALA TOPIC: THEORIES RELATED TO "WOMEN KEEP SILENT")

**NASB "wako chini ya nafsi zao"**
**NKJV "wanapaswa kuji nyenyekeza"**
**NRSV "lazima wawe wadogo"**
**TEV "lazima wasiwe viongozi"**
**NJB "sehemu yao ni ya kuwa wadogo"**

Hii ni KAULI TENDWA SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO. "paswa kutii" lilikuwa neno la kijeshi likielezea mnyororo wa maagizo. Umetumika kwa Yesu (kama vile Luka 2:51 kwa wazazi wake wa kidunia na 1 Kor. 15:28 kwa Baba yake wa mbinguni ) na ni kweli ya ulimwengu (kama vile Efe. 5:21).
MADA MAALUM: KUTII *(HUPOTASSŌ)* SPECIAL TOPIC: SUBMISSION *(HUPOTASSŌ)*

◙**"kama vile inenavyo torati nayo"** Je Paulo anarejea kwenye andiko maalum ama kanuni ya jumla? Hakuna andiko la Agano la Kale linalosema hivi. Inawezekana kwamba kwa namna ya uelewa wa 1 Kor. 11:8-9 kwamba Mwa. 2:20-24 ndio rejeo (kama vile 1 Tim. 2:13). Wengine hudhani kwamba matokeo ya anguko na kuwa andiko la Mwa.3:16 ndiyo rejeo. Inawezekana pia ki-muktadha kwamba "kujitiisha" kunahusiana na matumizi ya neno hilo katika 1 Kor. 14:32, ambapo lingerejea kujitiisha kwa manabii wengine (kama vile *Hard Sayings of the Bible*, uk . 616). Kuna mtiririko katika maandiko ya kutumia neno hili "torati." Mara nyingi ilihusu sheria ya Musa, Agano la Kale, lakini nyakati nyingine inahusu dhana ya sheria kwa jumla, ".

Kama wanawake wangeruhusiwa kuwa watangulizi hata kwenye mwonekano, ingeumiza utendaji wa huduma ya Kristo kwenye ulimwengu wa Wagiriki-Warumi. Kwa maana hiyo inafanana kwa namna Agano Jipya linavyochukulia suala la utumwa. tazama maelezo katika 1 Kor. 14:21 kwa uelewa tofauti wa kifungu hiki.

**14:35** Aya hii inaonesha kwamba neno "mwanamke" katika 1 Kor. 14:34 inarejea juu ya "wake." Je hii inamaanisha mwanamke mmoja anaweza kusema? Utata ule ule uko katika sura ya 11:5.
Aya hii inahusiana na 1 Tim. 2:11-12 na Tito 2:5. Je ni kithiolojia ama kitamaduni katika 1 Tim. 2:13-14? Je imefungiwa ndani ya mpangilio wa kipekee wa kihistoria ama ni ukweli wa ulimwengu kwa tamaduni zote? Ushahidi wa kibiblia anazungumza na sauti mbili (kama vile *How to Read the Bible For All Its Worth* na Gordon Fee na Douglas Stuart, kr. 15,63,72.74).

**"kama"** Hii ni SENTENSI YENYE MASHARTI DARAJA LA KWANZA. Wake wa Kikristo walikuwa wanauliza maswali kwenye makusanyiko ya ibada pale Korintho. Mikutano ya kanisa tayari ilikuwa inaingiliwa na waimbaji, wanenao kwa lugha, watafsiri wa lugha, na manabii. Sasa wake waliokuwa watafiti ama wake waliokuwa wanadai uhuru wao kwa kiburi walikuwa wameanza kujishugulisha kwa juhudi kwenye vurugu!

◙**"na wawaulize"**Hii ni KAULI TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO. Hawa wanawake wanaambiwa wamuulize nani na lini waulize na kwasabu gani! Vitendo vyao vilikuwa vinaathiri matokeo ya makusanyiko ya ibada. Tafadhali soma ujumbe juu ya uelewa wa Walter C. Kaiser wa 1 Kor. 14:34-36 katika 1 Kor. 14:21, aya ya pili.

**14:36** Hili lilikuwa swali la kejeli la kushutua kanisa la Korintho lenye kiburi ndani ya uhalisia wa kiroho na mahali pao miongoni mwa makusanyoko mengine. Muundo wa kisarufi wa maswali mawili katika 1 Kor. 14:36 unatarajia jibu la "hapana".

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 1 WAKORINTHO 14:37-38**
**37 Mtu akijiona kuwa ni nabii au mtu wa rohoni, na ayatambue hayo ninayowaandikia, ya kwamba ni maagizo ya Bwana. 38 Lakini mtu akiwa mjinga, na awe mjinga.**

**14:37-38** Paulo anathibitisha kwamba wale walio na karama za kiroho za kweli lazima wawatambue wengine wanaonena na wamepewa karama kutoka kwa Mungu (kama vile 1 Kor. 14:32; Mt. 11:15; 13:9,15,16,43). Maelezo ya Paulo ya utambuzi wa uongozi yameelezwa katika 1 Kor. 7:40 na 14:38. Paulo alitambua karama yake ya kitume pamoja na mamlaka yake ya kunena kwa ajili ya Kristo. Utume wake ulikuwa unahojiwa na kushambuliwa na baadhi ya watu pale Korintho.
Aya 38 inadokeza laana ya kiungu (KAULI TENDWA YENYE KUARIFU YA WAKATI ULIOPO) kuhusu wale wanaokataa mamlaka ya kitume (kama vileWayne Grudem, *The Gift of Prophecy in 1 Corinthians*, uk. 52 footnote #104).

◙**"ikiwa. . .ikiwa"** Hizi zote ni SENTENSI ZENYE MASHARTI DARAJA LA KWANZA, ambazo zimethibitika kuwa kweli kwa mujibu wa mtazamo wa mwandishi ama kwa kusudi lake la fasihi. Baadhi ya watu pale Korintho "wanadhani" kwamba wao ni wa "kiroho" (yaani, *pneumatikos*, kama vile 1 Kor. 12:1), lakini vitendo vyao na uhusiano wao na mamlaka ya kiutume (yaani, mamlaka ya Paulo.) yaonyesha kwamba sivyo.

**14:38**
**NASB "hatambuliwi"**
**NKJV "acha awe mjinga"**
**NRSV "hapaswi kutambuliwa"**
**TEV "msimjari"**
**NJB "mtu huyo hatambuliwi mwenyewe"**
Ipo hitilafu kwenye NJEO ZA VITENZI katika mswada wa Kiyunani, kati ya KAULI TENDWA YENYE KUARIFU YA WAKATI ULIOPO (MSS א*, A*) na KAULI TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO (MSS P[46], אi[2], A[c], B, D[2]). KAULI TENDWA YENYE KUARIFU inadokeza "liokataliwa." The IMPERATIVE kinaamuru waaminio pale Korintho kumkataa mtu anaye kataa mamlaka ya Paulo ikiwezekana mamlaka ya Paulo ikiwakilishwa katika mtetezi na mwakilishi wake, Timotheo. UBS[4] hukipa kiwango cha "B" karibu (hakika).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : 1 WAKORINTHO 14:39**
**39 Kwa ajili ya hayo, ndugu, takeni sana kuhutubu, wala msizuie kunena kwa lugha. 40 Lakini mambo yote na yatendeke kwa uzuri na kwa utaratibu.**

**14:39 "takeni sana kuhutubu"** Hili ni neno la Paulo lenye shauku nzito (kama vile 1 Kor. 12:31; 14:1). TEV ina maneno "elekeza moyo wako kwenye." Kwa Paulo katika mpangilio wa kitamaduni, shauku inaelekezwa kwenye kutangaza injili kwa manufaa ya aaminiye na asiye amini. Linganisha hii na Hes. 29: 11.
Yaonekana kwamba ufunguzi wa kauli ya Paulo katika 1 Kor. 14:1 pia ni kauli inayohitimisha katika 1 Kor. 14:39. Neno la Kiyunani *ōste,* ukifuatiwa na kishurutishi, yaweza kuwa njia ya kutambulisha mihutasari (kama vile. 1 Kor. 10:12; 11:33; 14:39; 15:58; Flp. 2:12; 1 The. 4:18).

◙**"wala msizuie kunena kwa lugha"** Huu ni uwiano unaohitajiwa kwenye matatizo pale Korintho na siku za leo. Tunaelekea kujibu kwa hisia kali kuliko inavyostahili katika tabia zetu kuhusu mambo ya kiroho. Barabara la ukweli lina mfereji wa wa makosa kila upande (yaani., wale wanenao kwa lugha dhidi ya wale wasionena kwa lugha)!

**NASB "ipasavyo na kwa utaratibu"**
**NKJV, NRSV "kiungwana na kwa utaratibu"**
**TEV "njia sahihi na yenye utaratibu"**
**NJB "mtindo sahihi na wenye utaratibu"**

Neno la kwanza linatoka kwenye muungano wa KIELEZI cha neno"vyema" (*eu*) na NOMINO ya neno “mtindo" ama "muundo" (kama vile Rum. 13:13; 1 The. 4:12).

Neno la pili linamaanisha "kupanga kwa njia sahihi, kutoa utaratibu" (kama vile Kol. 2:5). Kirai hiki kinafanana na 1 Kor. 14:33. Linapaswa kufanya, pasipo na utaratibu ulioandaliwa kabla (yaani agenda inayotawala), lakini likiwa na kusudi la huduma ya kusanyiko la ibada ambalo ni uinjilisti na kuwafanya watu kuwa wanafunzi (kama vile Mt. 28:19-20).Hili ni hitimisho la maelezo ya Paulo Kuhusu swala la kusanyiko la ibada ambalo lilianza katika sura ya 11.

## MASWALI YA MJADALA

Haya ni maoni ya <u>mwongozo</u> kwa kujisomea, ikiwa na maana kuwa unawajibika binafsi kwa tafsiri ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mtoa maoni tu.

Maswali haya ya kujadili yanatolewa kukusaidia mambo muhimu ya kipengele cha kitabu hiki. Yamekusudiwa kukuchokonoa mawazo na sio ya mwisho.

1. Vigezo vitatu vitumikavyo katika kupima karama za rohoni ni vipi?
   a.
   b.
   c.
2. Kwa nini kunena kwa lugha kunapewa umuhimu mdogo zaidi kuliko kuhutubu kwenye sura hii?
3. Ni kwa jinsi gani akili inahusianishwa na kunena kwa lugha?
4. Aya ya 22 ina tatizo gani?
5. Je kanisa la Korintho linapaswa kutumika kama mwongozo kwa makanisa yote?
6. Je wanawake wanapaswa kunyamaza kanisani? Fafanua jibu lako ukilinganisha 11:5 na 14:34.

# 1 WAKORINTHO 15

| MGAWANYO WA AYA WA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **UBS[4]** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB** |
| Ufufuo wa kristo | Kristo aliyefufuliwa, ukweli wa imani | Injili ya kifo cha Kristo na ufufuo | Ufufuo wa Kristo | Ukweli wa ufufuo |
| 15:1-11 | 15:1-11 | 15:1-11 | 15:1-2 | 15:1-8 |
| | | | 15:3-7 | |
| | | | 15:8-11 | |
| | | | | 15:9-11 |
| Ufufuo wa wafu | Kristo aliyefufuliwa, tumaini letu | Umuhimu wa ufufuo kwetu | Ufufuo wetu | |
| 15:12-19 | 15:12-19 | 15:12-19 | 15:12-19 | 15:12-19 |
| | Adui wa mwisho Atabatilishwa | | | |
| 15:20-28 | 15:20-28 | 15:20-28 | 15:20-28 | 15:20-28 |
| | Madhara ya kukataa ufufuo | | | |
| 15:29-34 | 15:29-34 | 15:29-34 | 15:29-34 | 15:29-34 |
| | | | 15:33-34 | |
| Mwili wa ufufuo | Mwili wa Rehema | Asili ya Rehema | Mwili wa Rehema | Njia ya ufufuo |
| 15:35-41 | 15:35-49 | 15:35-41 | 15:35-38 | 15:35-38 |
| | | | 15:39 | 15:39-44a |
| | | | 15:40-41 | |
| 15:42-49 | | 15:42-49 | 15:42-49 | |
| | | | | 15:44b-49 |
| | Ushindi wetu wa mwisho | | | |
| 15:50-58 | 15:50-58 | 15:50-57 | 15:50 | 15:50-53 |
| | | | 15:51-57 | Nyimbo ya |
| hitimisho | | | | |
| | | | | la ushindi |
| | | | | 15:54-57 |
| | | 15:58 | 15:58 | 15:58 |

**MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI** (Kutoka" **Mwongozo mzuri wa kusoma biblia"( A Guide to Good Bbible Reading**

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILIA LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo wa usomaji wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako binafsi ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika nuru tuliyonayo. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hupaswi kumwachia kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo. Linganisha mgawanyo wa masomo yako na tafsiri tano hapo juu. Kugawanya katika aya hakuna uvuvio, isipokuwa ni ufunguo wa kufuatilia kusudio la asili la mwandishi ambalo ndilo kiini cha ukalimani. Kila aya ina somo moja na ni moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya ya tatu

4. N.K

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA

A. Ni dhahiri kutoka katika mazingira kwamba Paulo anaonyesha hisia kwenye uasi wa mahali unaoweza kutokea ambao ulikataa ufufuo wa wafu (ambao Wayahudi wengi wangekubaliana nao). Nadharia kadhaa zilisadikiwa kama asili inayowezekana:
   1. Mafunuo ya kwanza (tazama ufafanuzi) ya mawazo ambayo yalisisitiza kwenye matumizi mawili kati ya roho (yaani, Mungu, ambacho ndio kitu kizuri) na jambo (yaani, vitu vya kimwili, ambavyo ni uovu)
   2. Wale wanaoonyesha kuwa ufufuo umetokea tayari (kama vile 2 Tim. 2:17-18).

B. Hiki ni kifungu cha hakika katika Agano Jipya juu ya ufufuo wa Kristo na ufufuo wa waaminio.Ni lazima ikumbukwe kwamba kifungu hiki labda kiliandikwa kabla ya injili yoyote iliyoandikwa.

C. Angalia msisitizo wa Paulo wa kiuchungaji kwa namna sura ya mafundisho haya unavyoishia, 1 Kor. 15:58. Hii ni sawa na 1 The. 4:18. Paulo daima huyaondolea hadhi mafundisho ya kila siku na kutumikia. Ukweli huarifu stadi ya maisha!

D. Inasaidia kuona muundo wa jumla wa sura hii ndefu. Dr. David King, mwanachuo katika chuo kikuu cha mashariki cha Texas Baptisti, ina ufafanuzi mzuri kutoka kwenye maelezo yake ya darasani:

"IV. Kukua kwa Wakristo waliokomaa kunahitaji ufahamu wa imani katika ufufuo (1 Kor.15:1-58).

1. Utangulizi: (1 Kor. 15:1-11)
   a. Injili yenyewe inategemea uthibiti juu ya ufufuo wa Yesu (1 Kor. 15:1-8).
      (1) Msingi wa ukweli wa injili (mafundisho ya awali) inayojishughulisha na kifo, kuzikwa, na ufufuo wa Yesu (1 Kor. 15:3-4).
      (2) Kuonekana baada ya ufufuo wa Yesu kumethibitisha pasipo shaka yoyote kwamba Yesu alifufuka kutoka kwa wafu (1 Kor. 15:5-7).
      (3) Paulo hukuza neema ya Mungu ambayo ilimruhusu yeye kuwa miongoni mwa mashuhuda wa ufufuo wa Yesu (1 Kor. 15:8-11).
2. Msingi wa mafundisho ya ufufuo wetu ni ufufuo wa Yesu (1 Kor. 15:12-34).
   a. Baadhi yenu husema kwamba hakufufuka toka katika wafu. Ni nini maana yake (1 Kor. 15:12-19)?
      (1) kuhubiri kwetu ni bure (1 Kor. 15:12-14).
      (2) imani yenu ni bure (1 Kor. 15:14 & 17).
      (3) sisi ni mashahidi wa uongo wa ukweli wa Mungu (1 Kor. 15:15).
      (4) mngalimo katika dhambi zenu (1 Kor. 15:17).
      (5) wale waaminio ambao wamekufa wamepotea milele (1 Kor. 15:18).
      (6) waaminio wote wanapaswa kuhurumiwa (1 Kor. 15:19).
   b. Lakini Kristo (na bado ni!) amefufuka! Ni nini maana yake (1 Kor.15:20-34)?
      (1) Yeye ni limbuko la mavuno yajayo (1 Kor. 15:20).
      (2) Kristo,binadamu,kushinda mauti ambayo yaliletwa katika ulimwengu na mtu wa kwanza, Adamu (1 Kor. 15:21-22, kama vile Rum. 5:12-21).
      (3) Ufufuo umegawanywa katika sehemu mbili: ufufuo wa Kristo na ufufuo wa wengine (1 Kor. 15:23).
      (4) Mauti itashindwa na ufufuo na <u>wote</u> watakuwa chini ya Mungu, muumba wa wote (1 Kor. 15:24-28).
      (5) Waaminio watabatizwa katika imani wakiamini katika yote ya kiroho na kimwili (1 Kor. 15:29).
      (6) Tunaweza kumbana na aina zote za hatari pasipo na uwoga, ikiwa tukifa, <u>tutaishi</u> tena na kuhukumiwa, kulingana na matendo yetu (kudokezwa) hiivyo tunapaswa kuwa makini na jinsi tunavyoishi (1 Kor. 15:30-34).

3. Mafundisho ya ufufuo wa waaminio ni wa maana. Paulo alijibu baadhi ya maswali yao (1 Kor. 15:35-57).
   a. Je! ni jinsi gani wafu walifufuliwa? Jibu:Kwa nguvu za Mungu, kama Mungu anavyoinua mimea kutoka kwenye mbegu (1 Kor. 15:35-38).
   b. Je! wana mwili wa aina gani? Jibu: Aina tofauti ya mwili wa kufaa kwa aina tofauti ya maisha tutakayo ishi milele (1 Kor. 15:39-41).
      (1) Mungu aliumba aina tofauti za miili kwa ajili ya maisha katika ulimwengu huu (1 Kor. 15:39-41).
      (2) Ufufuo wa mwili ni aina mpya ya mwili (1 Kor. 15:42-44).
         Usio angamia dhidi ya ule unao angamia,
         Wenye utukufu badala ya ule wenye kufedheheshwa
         Wa nguvu badala ya ule ulio dhaifu
         Wa Kiroho badala ya ule wa nyama (au kimwili)
      (3) Asili ya ufufuo wa mwili ilifafanuliwa na utofauti na mwili wa asili ambao humuongoza Paulo kwa kutofautisha kati ya Adamu na Kristo (1 Kor. 15:45-49, kama vile Rum. 5:12-21).
   c. Je! haya yote yatafanyika lini? Jibu: Wakati Yesu atakapokuja tena (1 Kor. 15:50-57).
      (1) Mabadiliko ni muhimu kwa <u>wote</u> (1 Kor. 15:50).
      (2) Sisi wote tutabadilishwa mara moja (1 Kor. 15:51-52, kama vile 1 The. 4:14-17).
      (3) Itatokea wakati parapanda ya Mungu itakapolia (1 Kor. 15:52-kama vile 1 The. 4:16).
      (4) Wakati mabadiliko yakifanyika ushindi kamili juu ya mauti utakuwa wetu katika Yesu Kristo (1 Kor.15:53-57).
4. Hitimisho: Matokeo ya kuamini katika mafundisho haya ni ukamilifu katika huduma kwa sababu tunajua kwamba huduma yetu sio bure (1 Kor. 15:58)"

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 1 WAKORINTHO 15:1-2**
**[1] Basi, ndugu zangu, nawaarifu ile injili niliyowahubiri; ambayo ndiyo mliyoipokea, na katika hiyo mnasimama, [2] na kwa hiyo mnaokolewa; ikiwa mnayashika sana maneno niliyowahubiri isipokuwa mliamini bure.**

**15:1**
**NASB"basi nawaarifu "**
**NKJV"zaidi ya hayo. . .ninatangaza kwako"**
**NRSV"Sasa ningependa kuwakumbusha"**
**TEV"napenda kuwakumbusha "**
**NJB"napenda kuweka wazi "**

Paulo aliandaa barua yake kuhusu maswali kadhaa ambayo kanisa la Korintho lilimtumia (kama vile 1 Kor. 7:1,25; 8:1; 12:1; 16:1) ikiwa na kifungu “sasa kuhusiana” (yaani, *peri de*). Sura ya 15 huanza na *de*. Inawezekana kwamba mjadala huu kuhusiana na ufufuo ulikuwa sio swali ambalo kanisa liliuliza, lakini hali ambayo Paulo alifanywa kuitambu na pia alitaka kuielezea.

Hii ni aina ya KAULI TENDAJI ELEKEZI YA WAKATI ULIOPO ya neno *gnōrizō*, ambayo inamanisha kufanya kujulikana, kudhihirisha, au kutangaza. Hata hivyo, Paulo hakuwa akitoa taarifa mpya (kama vile 1 Kor. 12:3), bali muhtasari wa mafundisho ya kuandaa injili ambayo awali aliwahubiria.

### <u>MADA MAALUM: *MAFUNDISHO* YA KANISA LA AWALI (SPECIAL TOPIC: THE *KERYGMA* OF THE EARLY CHURCH)</u>

◙ **" ndugu zangu "** Paulo mara nyingi hutumia neno hili kumaanisha kipengele kipya cha mada hii au mabadiliko ya somo, kama alivyofanya hapa (kama vile 1 Kor. 1:10; 2:1; 3:1; 4:6; 8:12; 10:1; 11:33; 12:1; 14:6,20,26; 15:1,58; 16:12,15).

◙ **"injili"** Paulo hufananisha dhana ya "injili" na "neno nililowahubiria ninyi" (1 Kor. 15:2). Katika mawazo ya Waebrania kulikuwa na nguvu ya neno la Mungu (mf. Mwa. 1:3,6,9,11,14,20,24; Zab. 33:6,9; Isa. 55:11; Yohana 1:1). Hii basi ni sitiari ya maudhui ya mahubiri ya Paulo, si njia tu ya kurejelea kwa kauli ya mnenaji.

Aya hii ina KISHAMIRISHO CHENYE SHUTUMA, kihalisia ni lile neno "injili ambayo niliwahubiria."

Haya ni maoni yangu juu ya "injili" kutoka kwa fasiri yangu, *Gospel According to Peter*, juzuu. 2 (angalia mtandaoni katika **www.freebiblecommentary.org**

> "Pamoja na Marko yumkini ilikuwa injili ya kwanza kuandikwa, haya ni matumizi ya kwanza ya neno *euangelion* (kama vile Mk. 1:14,15; 8:35; 10:29; 13:10; 14:9) na mwandishi wa injili (matumizi ya Paulo katika Gal. 2:2 na 1The. 2:9 yangalikuwa ya kimakuzi ya awali).Ni kawaida kwa "habari njema" au "ujumbe mzuri." Hii dhahiri huaksi Isa. 61:1 na inawezekana Isa. 40:9 na 52:7. Muundo wake wa kisarufi unaweza kueleweka kama (1) ujumbe uliotolewa na Yesu au (2) ujumbe kuhusu Yesu. Namba 2 labda ni maana iliyokusudiwa. Hata hivyo, the *Dictionary of Jesus and the Gospels*, iliyochapishwa na IVP, inasema"kimilikishi ('cha') yumkini ni kwa kiima na kishamilisho: Yesu alitangaza injili na injili itatangaza historia yake " (uk. 285). The *Jerome Biblical Commentary* inasema" matumizi ya Marko ya neno 'injili' ni ya kufanana na hayo ya Paulo ambapo yanaweza kumaanisha ama kitendo cha kutangaza au maudhui ya kile kinachotangazwa."

◙ **"ambayo ndiyo mliyoipokea"** Neno hili linatumiwa na Wayahudi kwa namna ya "kupitishwa kwenye mila" (kama vile 1 Kor. 15:3; 11:23; 15:3; Mk 7:4; Flp. 4:9; 1 The. 4:10; 2 The.3:6). Paulo alikuwa anapitia kwenye kile alichokipokea (yaani, injili, kama vile 1 Kor. 15:3) kutoka kwa Kristo kama vile Gal. 1:12,16; Mdo. 9:1-22; 22:3-16; 26:7-18). Kabla ya Paulo kuwa Mtume kwa watu wa mataifa, yeye mwenyewe alikuwa mpokeaji wa injili. Hii ni KAULI TENDAJI ELEKEZI YA WAKATI ULIOPO USIOTIMILIFU. Ingawa Yesu alikufa kwa dhambi zote za Wanadamu, ni wazi kutoka katika kifungu hiki na vingine (kama vile Yohana 1:12; 3:16; Rum. 10:9-13) kwamba kila mtu anapaswa kibinafsi kupokea utoaji wa Mungu (kama vile 1 Kor. 15:11) wa wokovu wa bure. Injili inahusisha (1) ukaribishaji wa mtu; (2) kuamini ukweli kuhusu huyo mtu; na (3) kuishi maisha yenye kumfanana na huyo mtu.

◙ **"na katika hiyo mnasimama"** Hii ni KAULI TENDAJI ELEKEZI YA WAKATI TIMILIFU, ambayo humaanisha kitendo kilichokamilika katika wakati uliopita kikaja kuwa kwenye hali ya kudumu. Inazungumzia umuhimu wa uvumilivu (angalia Mada Maalumu katika 1 Kor. 1:21).

**MADA MAALUM: KUSIMAMA *(HISTĒMI)* [SPECIAL TOPIC: STAND *(HISTĒMI)***

**15:2 "mnaokolewa"** Hii ni KAULI TENDEWA ELEKEZI YA WAKATI ULIOPO, ya neno "kuokolewa" (kama vile 1 Kor. 1:18; 2 Kor. 2:15; 1 Pet. 3:21; 4:18). Wokovu ni mchakato wa kuelekea kwenye mfanano wa kuwa kama Kristo.

Angalia MADA MAALUM: WOKOVU (NJEO ZA KITENZI CHA KIYUNANI ( SPECIAL TOPIC: SALVATION [GREEK VERB TENSES) katika 1 Kor. 3:15.

◙ **"ikiwa"** Hii ni SENTENSI YENYE MASHARTI DARAJA LA KWANZA, ambayo inamaanisha kwamba wangaliweza "kushikamana" kwenye ukweli wa injili, ambao aliwahubiria, lakini inaongezea ujmbe wa tahadhari kwa mara ya pili "*ei*" (yaani, isipokuwa). Hii inaonekana kufananisha mfano wa Yesu juu ya udongo (kama vile Mt. 13) na majadiliano ya Paulo katika 1 Yohana 2:19 wa wale ambao walikuwa katika ushirika, lakini waliondoka.

Kulikuwapo na wale waliokuwa kwenye vikundi vidogo ndani ya kundi zima katika Korintho ambao kwa matendo yao, mitazamo, na theolojia ilionyesha kuwa hawakuwa waamini! Walikataa (1) injili ya Paulo; (2) mamlaka ya kitume ya Paulo; na (3) kuunganishwa injili kwenye utamaduni wa Warumi, ambapo utamaduni ndio ungetawala! Ukristo wa kitamaduni daima ni dhaifu na wakati mwingine sio ukristo!

Hata hivyo, tafadhali kumbuka kwamba kimazingira Paulo anaonyesha imani yake ambayo inadhihilisha waaminio wa Korintho ni waamini wa kweli.

1. NJEO YA WAKATI ULIOPO USIOTIMILIFU, 1 Kor. 15:1, " mliyonipokea"
2. NJEO YA WAKATI TIMILIFU, 1 Kor. 15:1, " na katika hilo mnasimama"
3. SENTENSI SHURUTISHI DARAJA LA KWANZA , 1 Kor. 15:2, "ikiwa mnayashika sana"

◙ **"isipokuwa mliamini bure "** " **ikiwa mnayashika sana**. . . **bure**." Neno "bure" (*eikē*) linamaanisha "bila kusudi" (kama vile Gal. 3:4; 4:11). Ni dhahiri kutoka katika Mt. 13:1-9,18-23, na Yohana 8:31-59 kwamba weledi wa uongo ni kweli ya maisha ya kidini (angalia MADA MAALUM: UASI *(APHISTĒMI)* SPECIAL TOPIC: APOSTASY *(APHISTĒMI)* katika 1 Kor. 6:9). Kifungu hiki kinaunda kitu cha nne katika mfululizo unaofafanua mambo muhimu ya maisha ya kikristo: ukubalifu, nafasi, maendeleo, na uendelevu wa kudumu. Wokovu ni njia ambayo inahusisha toba, imani, utii (yote ya awali na yenye kuendelea), pamoja na Ustahimilivu. Angalia Mada Maalumu: Hitaji la Kustahimili katika 1 Kor. 1:21.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 1 WAKORINTHO 15:3-11**

**3 Kwa maana naliwatolea ninyi hapo mwanzo yale niliyoyapokea mimi mwenyewe, ya kuwa Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zetu, kama yanenavyo maandiko; 4 na ya kuwa alizikwa; na ya kuwa alifufuka siku ya tatu, kama yanenavyo maandiko; 5 na ya kuwa alimtokea Kefa; tena na wale Thenashara; 6 baadaye aliwatokea ndugu zaidi ya mia tano pamoja; katika hao wengi wanaishi hata sasa, ila baadhi yao wamelala; 7 baadaye akamtokea Yakobo; tena na mitume wote; 8 na mwisho wa watu wote, alinitokea mimi, kama ni mtu aliyezaliwa si kwa wakati wake. 9 Maana mimi ni mdogo katika mitume, nisiyestahili kuitwa mitume, kwa sababu naliliudhi Kanisa la Mungu. 10 Lakini kwa neema ya Mungu nimekuwa hivi nilivyo; na neema yake iliyo kwangu ilikuwa si bure, bali nalizidi sana kufanya kazi kupita wao wote; wala si mimi, bali ni neema ya Mungu pamoja nami. 11 Basi, kama ni mimi, kama ni wale, ndivyo tuhubirivyo, na ndivyo mlivyoamini.**

**15:3 "Kwa maana naliwatolea ninyi"** Hii inarejea juu ya (1) ushahidi wa Wakristo ambao Paulo aliupokea (yaani,kutoka kwa Stefano, Mdo. 7; kutoka kwa Anania, Mdo. 9:10-18; na kutoka kwa wakristo walioteswa, Mdo. 9:1-2; 1 Kor. 15:9) au (2) ufunuo wa moja kwa moja kutoka kwa Bwana (kama vile 1 Kor. 11:23; Mdo. 9:1-22; 22:3-16; 26:9-18; Gal. 1:12). Paulo alipita kwenye ukweli wa injili aliokwisha kuipokea. Paulo alikuwa sio mvumbuzi, lakini mashahidi waaminifu ambao walitumia ukweli wa injili kwa hali ya mataifa mapya.

◙ **"hapo mwanzo"** Huu ni muhtasari pekee wa injili ya kitume. Mihtasari ya kisasa ya injili yetu, kama njia ya Warumi (yaani, 3:23; 5:8; 6:23; 10:9-13), ni chaguzi za kisasa zilizochukuliwa kutoka kwa maandiko makuu yaliyovuviwa. Paulo anataka kuwakumbusha mambo ya msingi ya injili (angalia Mada Maalum: Mafundisho ya awali katika 1 Kor. 15:1).

Muhtasari wa injili ya Paulo:

1. Kristo alikufa kwa dhambi zetu
2. Kristo alikufa kiukweli na alizikwa
3. Kristo alifufuka kutoka kwa wafu
4. Tunajua hayaa ni kweli kwa sababu Yeye alionekana kwa watu wengi kwa siku nyingi

◙ **"Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zetu"** Neno “Kristo” ni tafsiri ya Kiyunani ya neno la kiebrania Masihi, ambalo lina maanisha mtiwa mafuta. Neno hili, pasipo kawaida neno “ Yesu Kristo” au “Bwana Yesu Kristo” au “ Kristo Yesu” huonyesha asili ya kale ya utamaduni wa Paulo, ambapo Yesu alithibitishwa kama Masihi wa Wayahudi, aliyeahidiwa angalia MADA MAALUM: MASIHI (SPECIAL TOPIC: MESSIAH) katika 1 Kor. 1:23). Katika

uelekeo wote, Paulo alipokea hili kutoka kwa Anania na waaminio wengine walioko Dameski kabla ya ubatilishaji wake.

Hii ni KAULI TENDAJI ELEKEZI YA WAKATI ULIOPO USIOTIMILIFU, “Yesu alilipa deni ambalo hakuwiwa na sisi tunawiwa deni ambalo hatuwezi kulilipa” (kama vile Gal. 3:13; 1 Yohana 4:10).

KIHUSISHI cha neno“kwa” (*huper*) kinamanisha “kwa niaba ya”; mara nyingi kilitumika sawa na KIHUSISHI kingine cha Kiyunani, *anti*, ambacho kinamaanisha “badala ya.” Hii ilikuwa rejeo dhahili, kwa upatanisho mbadala (kama vile Isa. 53; Marko 10:45). Kifo cha Kristo lilikuwa ni somo lililojirudia mara kwa mara katika maandiko ya Paulo. Yeye alitumia maneno na vifungu kadhaa kurejelea kifo mbadala cha Yesu:

1. Damu (kama vile 1 Kor. 11:25,27; Rum. 3:25; 5:9; Efe. 1:7; 2:13; Kol. 1:20)
2. Akajitoa (kama vile Efe. 5:2,25)
3. Alitolewa (kama vile Rum. 4:25; 8:32)
4. Sadaka: (kama vile 1 Kor. 5:7)
5. Alikufa (kama vile Rum. 5:6; 8:34; 14:9,15; 1 Kor. 8:11; 15:3; 2 Kor. 5:15; Gal. 5:21; 1 The. 4:14; 5:10)
6. Msalaba (kama vile 1 Kor. 1:17-18; Gal. 5:11; 6:12-14; Efe. 2:16; Flp. 2:8; Kol. 1:20; 2:14)
7. Aliyesulibiwa (kama vile 1 Kor. 1:23; 2:2; 2 Kor. 13:4; Gal. 3:1)

◙ **" kama yanenavyo maandiko "** Hii inarejelea kwenye Agano la Kale kwa sababu hakuna Agano Jipya lililoandikwa kwa wakati huo huenda isipokuwa kwa Wagalatia na Wathesalonike. Matumizi ya kifungu hiki katika 1 Kor. 15:3-4 huonyesha unabii (kama vile Luka 24:27) na mpango wa ukombozi ulioamuliwa kabla na Mungu (kam a vile Mdo. 2:23; 3:18; 4:28; 13:29, tazama Mada Maalumu katika 1 Kor. 1:21).

Hata hivyo, inawezekana kwamba maandiko hapa yanarejelea kwenye moja ya injili (au maneno ya Yesu yaliyokuwa yakienea kipekee toka kwenye vidokezo vya mwanzo). Haijulikani ni wakati gani iliandikwa, na wakati gani ilianza kuzungushwa kwenye makanisa ya mwanzo. Ikiwa kifungu kinarejelea kwa maelezo ya injili, basi “siku ya tatu” inaweza kurejelea kwa Yesu kufufuliwa siku ya jumapili, siku ya kwanza ya juma na, kwa Wayahudi kutegemea, siku tatu.

**15:4 "alizikwa"** Yeye alikufa kweli!

◙ **"siku ya tatu"** Hakuna uthibitisho wa wazi kwenye Agano la Kale juu ya neno “siku ya tatu.” Hata hivyo, ilikuwa sehemu ya *mafundisho ya awali* (kamavile Marko 10:34; Luka 24:46; Mdo.10:40, angalia Mada Maalumu katika 1 Kor. 15:1). Baadhi wanaona inarejelea kwa Yoh. 1:17 au Zab. 16:10, hata hivyo, maoni ya Yesu (kama vile Mt. 12:40) yanaonekana kuyahusianisha na uzoefu wa Yona ndani ya samaki mkubwa.

◙ **" alifufuka "** Hii ni KAULI TENDEWA ELEKEZI YA WAKATI TIMILIFU, inayotumika mara nyingi katika aya hii (kama vile 1 Kor. 15:4,12,13,14,16,17,20). Hii njeo ya kitenzi cha kiyunani inazungumza juu ya hadhi endelevu ya Kristo kama “aliyefufuliwa” na IRABU TENDWA huzungumzia matendo ya Mungu Baba katika kumfufua kutoka kwa wafu. Hii huonyesha idhini ya Baba juu ya maisha, mafundisho, na dhabihu ya kifo cha Yesu. Agano Jipya mara nyingi hufikiria kazi za ukombozi kwa utatu wote wa kiungu:

1. Mungu Baba alimfufua Yesu (kama vile Mdo. 2:24; 3:15; 4:10; 5:30; 10:40; 13:30,33,34,37; 17:31; Rum. 6:4,9; 10:9; 1 Kor. 6:14; 2 Kor. 4:14; Gal. 1:1; Efe. 1:20; Kol. 2:12; 1 The. 1:10)
2. Mungu Mwana alijifufua (kama vile Yohana 2:19-22; 10:17-18)
3. Mungu Roho alimfufua Yesu (kama vile Rum. 8:11).

**MADA MAALUMU: UFUFUO (SPECIAL TOPIC: RESURRECTION)**

**15:5 "alimtokea "**Angalia Mada Maalum chini.

MADA MAALUMU: KUONEKANA KWA YESU BAADA YA UFUFUO (SPECIAL TOPIC: JESUS` POST – RESURRECTION APPEARENCES)

◙ **"Kefa"** Mara nyingi Paulo humuita kwa jina hili katika barua zake za Wakorintho (kama vile1 Kor. 1:12; 3:22; 9:5; 15:50, lakini katika Wagalatia humuita kwa majina yote Kefa (kama vile 1 Kor. 2:9) na Petro (kama vile 1 Kor. 1:18; 2:7,8,11,14).Paulo kamwe hakumwita Simioni**.**

Inastaabisha kwamba mtu wa kwanza (baada ya wanawake pale kaburini) Kristo kumtokea baada ya kufufuka ni yule aliyemkana mara tatu, yule aliyehubiri mafundisho ya mwanzo ndani ya kanisa siku ya Pentekoste. Yesu anamuonyesha kwa msisitizo maalumu katika Marko 16:7, ambapo mitume waliambiwa kukutana na Yesu huko Galilaya. Hii hakika huonyesha upendo, uelewa, msamaha, na kurejesha nguvu za Kristo. Mengi juu ya Yohana 21 inaelezea marejesho ya Petro kwenye uongozi.

◙ **"wale Thenashara"** Jamii ya ki-Magharibi ya machapisho ya Kiyunani (yaani, MS D [kitabu cha miswada ya kale cha Bezae]), pamoja na toleo la biblia ya kilatini, yana wanafunzi "kumi na moja." Neno "wale thenashara" likawa neno la kiufundi kwa kikundi cha mitume.Paulo kamwe hakutumia neno hili katika sehemu yoyote ya maandiko yake mengine. Baadhi wanadhani hii hudokeza kwamba 1 Kor. 15:3-7 huenda ikawa muhtasarfi wa katekisimu ya kanisa la awali.

MADA MAALUM: NAMBA KUMI NA MBILI (SPECIAL TOPIC: THE NUMBER TWELVE)

**15:6 "aliwatokea ndugu zaidi ya mia tano "** Hii inaweza kurejea kwa Mt. 28:16-20, hasa 1 Kor. 15:17, ambayo huonyesha kwamba amri kuu ilitolewa kwa kanisa lote, sio kwa viongozi wa chache tu. Msisitizo wa Paulo katika 1 Kor. 15:6 ni ukweli wa kihistoria wa ufufuo. Kama mtu hakuamini, kulikuwa na mashahidi wengi wa macho kwa ajili ya kushuhudia.

◙ **"hata sasa"** Yesu alisulibiwa katikati ya miaka 30 na kuendelea na 1 Wakorintho waliandika katikati ya miaka 50 na kuendelea, hivyo katika hii miaka ishirini ya muda mrefu ya wale walioathiriwa binafsi na maneno na matendo ya Yesu walikuwa bado hai na kushuhudia!

◙ **"wamelala"** Paulo anafuata matumizi ya Yesu (kama vile Mt. 27:52; Yohana 11:11,13) na matumizi ya Agano la Kale (kama vile Dan. 12:2) juu ya kulala kama tafisida kwa kifo.

**15:7 "Yakobo"** Hii inarejelea kwa ndugu wa Bwana ambaye hakumuamini mpaka baada ya ufufuo (kama vile Marko 3:21; Yohana 7:5). Wote wa familia hii walikuwepo katika chumba cha gorofani (kama vile Mdo 1:14). Yakobo huyu alijulikana kama nduguye Bwana (kama vile Mt. 13:55; Mk 6:3), ili kumtofautisha kutoka kwa mtume Yakobo, sehemu ya mzunguko wa ndani, ambaye aliuawa mwanzoni sana (kama vile Mdo 12). Kwa vizazi kadhaa kanisa ndani ya Yerusalemu lilikuwa na ndugu wa kimwili wa Yesu kama kiongozi wao. Vifungu kadhaa vya kibiblia (kama vile Mdo. 12:17; 15:13; 21:18; 1 Kor. 15:7; na Yakobo 1:1) vinaonyesha kwamba Yakobo alikuwa kiongozi muhimu sana wa kanisa katika Yerusalemu.Paulo ndiye peke yake ametaja kuonekana. Hii huonyesha jinsi gani maelezo mengi yameondolewa katika Agano Jipya kuhusu mafundisho na matendo ya Yesu. Tuna kila kitu tunachohitaji kumtumaini na kumfuata, lakini haitoshi kwa kukamilisha historia ya maisha yake.

MADA MAALUM: YAKOBO, NDUGUYE YESU (SPECIAL TOPIC : JAMES, THE HALF BROTHER OF JESUS)

◙ **"tena na mitume wote"** Tangu thenashara wametajwa katika 1 Kor. 15:5, hii inaonekana kurejea kwenye matumizi mapana ya neno hili. Yakobo anaonekana kuwa "mtume" kwa maana sawa kama Barnaba (kama vile Mdo. 14:4, 14); Androniko na Yuniasi (au Yunia, kama vile Rum. 16:7); Apollo (kama vile 2 Kor. 4:9); Epafrodito (Flp. 2:25); au Silvana na Timotheo (kama vile 1 The. 2:6; Mdo; 18:5). Inawezekana kutoa hoja kuwa Kefa ametajwa tofauti na thenashara hivyo "mitume wote" wanaweza kurejea kwa wale thenashara pia.

**15:8**

**NASB, NRSV"kama ni mtu aliyezaliwa si kwa wakati wake "**

**NKJV"kama mtu kuzaliwa nje ya wakati wake "**

**TEV"hata mimi niliyekuwa kama mtu ambaye aliyezaliwa kabla ya wakati "**
**NJB"kama nilikuwa mtoto aliyezaliwa kabla ya wakati"**

Tafsiri hii ya kingereza inaonyesha maana ya jumla ya neno hili la nadra.Limetumika mara tatu pekee katika maandiko ya kale ya Kiyunani (kama vile Hes. 12:12; Ayu 3:16; na Mhu. 6:3) juu ya utoaji wa mimba.Neno linadokeza juu ya mimba za utotoni. Hata hivyo, katika muktadha huu, Paulo anaonekana kuelezea maongezeko yake ya kuchelewa kwa kundi la mitume (yaani, Barabara ya ubadilishaji wa Damaski, kama vile Mdo 9).

Yumkini inawezekana kwamba hii ilikuwa moja ya sababu iliyoumiza kikundi kimoja au makundi zaidi ndani ya kanisa waliokataa mamlaka ya Paulo (yaani, hakuwa mtume wa kawaida). Paulo alithibitisha neema ya Kristo kwa kuonekana kwake katikati ya mateso yake kwa kanisa (kama vile 1 Kor. 15:10; Gal. 1:23). Hata hivyo, yeye bado yuko kwenye orodha ya kuchagua wale ambao Kristo aliwatokea baada ya ufufuo wake.Paulo hata anaweza kudai kwamba yeye ndiye pekee ambaye Kristo aliyetukuzwa (yaaani, aliyepaa) alimtokea (kama vile Gal. 1:15-16).

Pia inawezekana kwamba neno lina maana ya pili ya "ukatili" ambayo ingekuwa inarejelea kwenye makosa ya Paulo na mashambulizi ya mara kwa mara juu ya waaminio wasio na hatia (yaaani, Mdo 9:1-2, tazama *Jerome Biblical Commentary,* uk. 273). Paulo anaweza kuunda neno hili mwenyewe tangu lilipoelezea ubadilishaji wake wa kabla kwenye kufurahia maisha ya Wayahudi.

**15:9 "Maana mimi ni mdogo katika mitume"** Paulo aliyenyekezwa sana na neema ya Mungu hata katikati ya mateso yake ya Kanisa la Yesu. Mara nyingi hutumia vifungu kama hivi kujielezea mwenyewe (kama vile 2 Kor. 12:11; Efe. 3:8; 1 Tim. 1:15).

◙ **"kwa sababu naliliudhi Kanisa la Mungu"** (kama vile Mdo 9:1,13,21; Mdo 22:4,19; Mdo 26:10-11; Gal. 1:13,23; Flp. 3:6; 1 Tim. 1:13).

**15:10 "kwa neema ya Mungu nimekuwa hivi nilivyo"** Neno "neema" limewekwa mbele kwa ajili ya msisitizo (kama vile Rum. 12:3; Efe. 2:8-9). Waaminio wote ndivyo walivyo kwa neema ya Mungu, lakini angalia uwiano unaohitajika juu ya kitendo/hatua ya kibinadamu yenye kusudi (kama vile Flp. 2:12-13).

◙ **"ilikuwa si bure"** Hili ni neno tofauti kutoka katika 1 Kor. 15:2. Paulo alitumia maneno matatu tofauti yaliyotafsiriwa kwa maana ya "bure" au "tupu" katika aya hii.

1. *eikē*, 1 Kor. 15:2
2. *kenos*, 1 Kor. 15:10,14,48; 2 Kor. 6:1
3. *mataios*, 1 Kor. 15:17; 1 Kor. 3:20

**Jambo lake ni kwamba neema ya Mungu imethibitisha ufanisi katika huduma ya Paulo, ambayo kanisa la Wakorintho lenyewe lilikuwa shahidi wa matokeo.**

◙ **"bali nalizidi sana kufanya kazi kupita wao wote"** muktadha huu unaamuru kwamba hii inarejelea kwa mitume wengine. Paulo anajilinganisha na mitume wengine katika Galatia kwa sababu mamlaka yake ya kitume ilikuwa inatiwa changamoto.Inawezekana kwamba moja au zaidi ya kikundi kidogo ndani ya kundi zima walikuwa wanafanya jambo lile lile katika Korintho. Paulo alikuwa hana ugomvi na thenashara.Yeye alionyesha wazi tu wito wake na mamlaka yake mwenyewe!

**Angalia Mada Maalum juu ya "ipitayo kiasi" katika 2 Kor.2:7.**

◙ **"wala si mimi, bali ni neema ya Mungu pamoja nami"** Kuna uwiano kwenye theolojia ya Paulo kati ya wito, kukirimiwa, na huduma ihusianayo na utawala wa Mungu. Daima kuna uwiano wa kimaagano kati ya hizi njia mbili za kuangalia ufanisi wa mtu. Paulo anaonyesha kwamba alifanya kazi kwa bidii kuliko mitume wengine, lakini pia alijua kwamba Mungu alikuwa chanzo, sio mwenyewe. Uwiano huo huo unaonekana kati ya Yohana 15:5 na Flp. 4:13, au Flp. 2:12-13.

**15:11** Paulo anaonyesha kwa uthabiti sana kwamba injili aliyopokea na kuihubiri ilikuwa sawa kama waliyohubiri mitume wa awali.Ukweli kwamba yeye anafanya madai kuonyesha upinzani upi aliokuwa anakabiliana nao katika Korintho. Wengine walikuwa wanakataa mamlaka yake ya kitume, na hata ikiwezekana, habari zake za injili.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 1 WAKORINTHO 15:12-19**
**[12] Basi, ikiwa Kristo anahubiriwa ya kwamba amefufuka katika wafu, mbona baadhi yenu husema kwamba hakuna kiyama ya wafu? [13] Lakini kama hakuna kiyama ya wafu, Kristo naye hakufufuka; [14] tena kama Kristo hakufufuka, basi, kuhubiri kwetu ni bure na imani yenu ni bure. [15] Naam, na sisi tumeonekana kuwa mashahidi wa uongo wa Mungu; kwa maana tulimshuhudia Mungu ya kuwa alimfufua Kristo, ambaye hakumfufua, ikiwa wafu hawafufuliwi. [16] Maana kama wafu hawafufuliwi, Kristo naye hakufufuka. [17] Na kama Kristo hakufufuka, imani yenu ni bure; mngalimo katika dhambi zenu. [18] Na hapo wao nao waliolala katika Kristo wamepotea. [19] Kama katika maisha haya tu tumemtumaini Kristo, sisi tu maskini kuliko watu wote.**

**15:12 "ikiwa"** Hii ni SENTENSI YENYE MASHARTI DARAJA LA KWANZA, ambayo hudokeza kuwa Kristo alihubiriwa (kama vile 1 Kor. 15:11).

◙ **"mbona baadhi yenu husema kwamba hakuna kiyama ya wafu"** Chanzo cha kukana ufufuo wa Kristo yumkini ina asili yake Katika falsafa ya Kiyunani (yaani, watu wa mafunuo ya uongo, angalia faharasa), ambao walidhani mwili wa asili ulikuwa chanzo cha uovu. Haijulikani kimaandiko kama wao walikataa ufufuo wa Kristo au ufufuo wa waaminio wote. Hii ilikuwa sio tatizo la pekee katika kanisa la awali (kama vile 2 Tim. 2:18).

**15:13 "kama"** Hii ni kauli nyingine YENYE MASHARTI DARAJA LA KWANZA. Mara nyingi inaitwa na wanasarufi muundo"rahisi" au "wenye mantiki" (kama vile 1 Kor. 15:13,14,15,16,17,19). Dhahiri katika aya hii Paulo anaitumia kukuza hoja yake ya maandishi na sio kuonyesha kwamba Kristo hakufufuliwa! Lakini mantiki katika maandiko haya ya aya chache ndio zilizo na nguvu. Ikiwa Kristo hakufufuliwa basi:

1. Hakuna ufufuo kabisa, 1 Kor. 15:13,16
2. Kuhubiri kwetu ni bure, 1 Kor. 15:14
3. Imani yenu ni bure, 1 Kor. 15:14
4. Wao ni mashahidi wa uongo, 1 Kor. 15:15
5. Imani yenu ni bure, mst 17
6. Mngalimo katika dhambi zenu, 1 Kor. 15:17
7. Wao na waliolala katika Kristo wamepotea, 1 Kor. 15:18
8. Sisi tu watu wa kuhurumiwa sana, 1 Kor. 15:19

Jambo hili la kitheolojia la ufufuo wa Kristo sio jambo dogo! Yeye yu hai au Ukristo ni uwongo! Haya ni mafundisho ya kumwagwa kwa maji!

**15:14,17 "imani yenu ni bure. . . imani yenu ni bure"** Haya maneno mawili tofauti hudokeza tupu au isio na matunda. Haya ni mafundisho ya kuvunja moyo!

**15:19 "Kama katika maisha haya tu tumemtumaini Kristo"** Hii ni SENTENSI YENYE MASHARTI DARAJA LA KWANZA.Paulo anajenga hoja kwamba kama Kristo hakufufuliwa tuna tumaini pekee (KAULI TENDAJI TIMILIFU YENYE MAFUMBO) katika maisha haya kwa sababu hakuna maisha baada ya kifo-kama Kristo hakufufuliwa

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 1 WAKORINTHO 15:20-28**
**[20] Lakini sasa Kristo amefufuka katika wafu, limbuko lao waliolala. [21] Maana kwa kuwa mauti ililetwa na mtu, kadhalika na kiyama ya wafu ililetwa na mtu. [22] Kwa kuwa kama katika Adamu wote wanakufa, kadhalika na katika Kristo wote watahuishwa. [23] Lakini kila mmoja mahali pake; limbuko ni Kristo; baadaye walio wake Kristo, atakapokuja. [24] Hapo ndipo mwisho, atakapompa Mungu Baba ufalme wake; atakapobatilisha utawala wote, na mamlaka yote, na nguvu. [25] Maana sharti amiliki yeye, hata awaweke maadui wake wote**

**chini ya miguu yake. [26] Adui wa mwisho atakayebatilishwa ni mauti. [27] KWA KUWA, ALIVITIISHA VITU VYOTE CHINI YA MIGUU YAKE. Lakini atakaposema, Vyote vimetiishwa, ni dhahiri ya kuwa yeye aliyemtiishia vitu vyote hayumo. [28] Basi, vitu vyote vikiisha kutiishwa chini yake, ndipo Mwana mwenyewe naye atatiishwa chini yake yeye aliyemtiishia vitu vyote, ili kwamba Mungu awe yote katika wote.**

**15:20 "Lakini"** Ni tofauti gani muhimu!

◙ **"sasa Kristo amefufuka"** Sura hii mara nyingi inaitwa "sura ya ufufuo." Ufufuo wa Kristo na wa wafuasi wake ni mada inayojirudia mara kwa mara. Matokeo ya uhakika na ya kudumu ya hii yanaweza kuonekana katika KITENZI *egeirō*, ambacho kinamaanisha kuamka, kuinuka:
mst. 12, KAULI TENDEWA ELEKEZI YA WAKATI TIMILIFU
mst. 13, KAULI TENDEWA ELEKEZI YA WAKATI TIMILIFU
mst. 14, KAULI TENDEWA ELEKEZI YA WAKATI TIMILIFU
mst. 15, KAULI TENDWAN ELEKEZI YA WAKATI ULIOPO USIOTIMILIFU (mara mbili)
mst. 16, KAULI TENDEWA ELEKEZI YA WAKATI TIMILIFU
mst. 16, KAULI TENDEWA ELEKEZI YA WAKATI TIMILIFU
mst. 17, KAULI TENDEWA ELEKEZI YA WAKATI TIMILIFU
mst. 20, KAULI TENDEWA ELEKEZI YA WAKATI TIMILIFU
mst. 32, KAULI TENDEWA ELEKEZI YA WAKATI TIMILIFU
mst. 35, KAULI TENDEWA ELEKEZI YA WAKATI TIMILIFU
mst. 42, KAULI TENDEWA ELEKEZI YA WAKATI TIMILIFU
mst. 43, KAULI TENDEWA ELEKEZI YA WAKATI TIMILIFU
mst. 44, KAULI TENDEWA ELEKEZI YA WAKATI TIMILIFU
mst. 52, KAULI TENDEWA ELEKEZI YA WAKATI UJAO

Angalia uendeleaji wa IRABU TENDWA. Mungu wa Utatu huwafufua wafu. NJEO YA WAKATI TIMILIFU huzungumzia juu ya ufufuo wa Yesu uliopita, ambao ukajakuwa kwenye hali ya ubinadamu. Waaminio hushiriki ukweli wa ufufuo wake na kwa imani, hakikisho lao!

◙ **"lao waliolala"** Hii ni KAULI YA KATI ENDELEVU YA WAKATI TIMILIFU (kama vile Mt. 27:52), ambayo ilikuwa nahau ya Kiebrania kwa kifo.

◙ **"limbuko"** Huu utaratibu wa Agano la Kale wa kila mwaka wa utoaji dhabihu umejadiliwa katika Law. 23:10 na kuendelea. Limbuko katika Agano la Kale yalikuwa matita yaliyokomaa ya mavuno ya ngano iliyopepetwa huletwa mbele ya Bwana katika hekalu siku baada ya sabato takatifu ya juma la pasaka, ambayo itakuwa jumapili ya ufufuo.Yalitolewa kuonyesha umiliki wa Mungu juu ya mazao yote. Hii ni aina ya ahadi ya agano la Kale kwa ajili ya ufufuo kwa wafuasi wote wa Kristo! Paulo alitumia neno hili tena katika 1 Kor. 16:15 kwa kuelezea waaminio wa kwanza katika Akaya. Pia aliliitumia katika Rum.8:23 kuelezea juu ya waamini kumpokea Roho, lakini wakisubiri kwa hamu ule ufufuo. Yesu ni wa kwanza kufufuliwa (kama vile Kol. 1:18), lakini kwa wakati unaofaa wafuasi wake wote watapitia hali ile ile.Katika maana ya kiroho tayari tuna maisha ya ufufuo (kama vile Efe. 2:5-6).

**MADA MAALUM: MZALIWA WA KWANZA (SPECIAL TOPIC: FIRST BORN)**

**15:21-22** Huu ni uainishi kipindi cha Adamu -Kristo ambacho ilifuatwa katika 1 Kor. 15:45-48 (kama vile Rum. 5:12-21; Flp. 2:6-11). Katika Adamu ubinadamu wote umeathiriwa na dhambi (yaani, kifo). Katika Kristo, kuna uwezekano wa wanadamu wote kuathiriwa na neema. Aya hizi zenye utata mwingi pamoja na Rum. 5:18-19, zilisababisha baadhi ya wanathiolojia hatimaye kudai wokovu kwa wanadamu wote. Wengine wanaona kama inarejelea juu ya ufufuo wa wote waliookolewa na walipotea (kama vile Dan. 12:2).Katika adamu wote walikufa; katika Yesu wote watafufuliwa (yaani, baadhi kwa thawabu, baadhi kwa hukumu). Inaonekana wazi kwangu

kwamba maandiko ya Paulo, yaliochukuliwa katika muktadha, yanahitaji mwitikio wa imani ya toba ili kuweza kuokolewa!

**15:23-25** wanatheolojia wengine wanadai ya kwamba aya hizi zinathibitisha dhana ya kabla ya milenia ya matukio ya siku za mwisho. Hata hivyo, haya maandiko sio majadiliano ya milenia, bali ufufuo. Kifo kilishindwa katika kaburi tupu, si utawala wa baaadaye wa dunia hii. Tunapaswa kuwa makini na ajenda zetu za kitheolojia kuelezea tafsiri ya muktadha. Paulo kamwe hakujadili milenia, hata katika majadiliano ya kuwa na shauku (kama vile 1 The. 4:13-18) wala wa mpinga Kristo (kama vile 2 Wathesalonike 2).Wala Yesu hakujadili milenia, hata katika mahubiri ya matukio ya siku za mwisho (kama vile Mt. 24; Mk. 13; Lk. 21). Kuna vitabu vizuri kadhaa ambavyo vinatoa muhtasari wa nafasi ya kila milenia ya sasa na ambayo huacha nafasi nyingine zionyeshe uwezo na udhaifu wa kila mmoja.

1. Robert G. Clouse (tl.), *The Meaning of the Millennium, Four Views*
2. C. Marvin Pate (tl.), *Four Views on the Book of Revelation*
3. Darrell L. Boch (tl.), *Three Views on the Millennium and Beyond*

Angalia maoni yangu katika ufunuo, sura ya 20, mtandaoni katika **www.freebiblecommentary.org**

**15:23 "atakapokuja "** Angalia Mada Maalum hapo chini.

**MADA MAALUM: MANENO YA AGANO JIPYA JUU YA KURUDI KWA YESU (SPECIAL TOPIC: NT TERMS FOR CHRIST'S RETURN)**

**15:24 "ufalme"** Inastajabisha kuona ni mara ngapi dhana hii inatumiwa na Yesu katika vidokeza vya injili. Ni suala la mahubiri yake ya mwanzo na ya mwisho pamoja na msukumo wa mifano zaidi.Ni ya kustajabisha kutumika mara mbili pekee katika injili ya Yohana. Ni utawala wa Mungu katika kuamini mioyo ya binadamu sasa ambayo siku moja itabadilishwa juu ya dunia yote (angalia Mada Maalum katika 1 Kor. 4:20).

Linatumiwa na Yesu kama uwepo wa sasa wa ufalme wa ufalme ya Mungu na kupitia uwepo wake mwenyewe binafsi na mafundisho yake (kama vile Mt. 3:2; 4:17; 10:7; 11:12; 12:28; Mk. 1:15; Lk.9:9,11; 11:20; 21:31-32). Hata hivyo, pia iliunganishwa na kutimiliza kwa utukufu wa baadaye katika kurudi kwake (kama vile Mt. 6:10; 16:28; 26:64). Ni "tayari/bado" ya wasiwasi wa matukio ya siku za mwisho za injili!

Rejeo maalumu kwa neno"ufalme" ni nadra kiasi katika maandiko ya Paulo.
Warumi - 14:17
1 Wakorintho - 4:20; 6:9; 15:24,50
Wagalatia- 5:21
Waefeso- 5:5
Wakolosai- 1:13; 4:11
1 Wathesalonike - 2:12
2 Wathesalonike - 4:1,18

**◙" atakapobatilisha utawala wote, na mamlaka yote, na nguvu "** Hii inarejea kwenye nguvu za kimalaika (*eons* katika mawazo ya mafunuo ya uongo) za zama za uovu huu wa sasa (kama vile Rum. 8:38; Efe. 1:21; 3:10; 6:12; Kol. 1:16; 2:10,15). Ubatilishaji huu inavyoonekana hutokea

1. Kitheolojia katika msalaba na ufufuo
2. Kwa wakati katika kurudi kwa Kristo

Ikiwa hii ni kweli, basi 1 The. 4:13-18 ni mfanano wa karibu sana katika maandiko ya Paulo. Tazama kwamba baada ya kuwa na shauku, waaminio wako pamoja na Mungu milele (kama vile 1 The. 4:17), ambao ni ufalme wa milele wa Baba (kama vile Dan. 7:13-14).

Kwa "utawala" angalia Mada Maalum hapo chini.

MADA MAALUM: *ARCHĒ* (SPECIAL TOPIC: *ARCHĒ*)

Kwa neno “mamlaka” angalia Mada Maalum inayofuata.
MADA MAALUM: MAMLAKA *(EXOUSIA)* [SPECIAL TOPIC: AUTHORITY (*EXOUSIA*)]

Muktadha huu unaweza kurejelea juu ya mafunuo ya uongo *eons.* Angalia Mada Maalum inayofuata.
MADA MAALUM: MALAIKA KATIKA MAANDIKO YA PAULO (SPECIAL TOPIC: ANGELS IN PAUL’S WRITINGS)

**15:25 " hata awaweke maadui wake wote chini ya miguu yake "** Hii ni lahaja ya Agano la kale kwa ushindi kamili (kama vile Zab. 8:6; 110:1). Katika Agano la kale maadui walikuwa ni yale mataifa ya kipagani yaliyokuwa yamewazunguka, lakini katika Agano jipya ni wale malaika, nguvu za kiroho zenye uadui na Mungu na Kristo wake. Hizi nguvu za uovu zinamshawishi mwanadamu kwa kutokuamini na kuasi. Yesu alizishinda kikamilifu nguvu hizi kwa msalaba na ufufuo wake. Ufufuo wa mwisho wa waaminio wote utaweka alama ya kutimiliza kwa ushindi huu!
Kuna vitabu viwili vya kupendeza ambavyo vimeelezea hasa ni nini hizi “nguvu” zinarejelea kwayo.

1. Hendricus Berkhof, *Christ and the Powers*
2. Oscar Cullmann, *Christ and Time*

**15:26 " Adui wa mwisho atakayebatilishwa ni mauti "** Hii inamaanisha “kufanya batili na tupu.” Kifo kimeshindwa (kama vile 2 Tim. 1:10; Ufu. 21:4). Kifo hakikuwa mapenzi ya Mungu kwa mwanadamu, lakini ni matokeo ya anguko (yaani, Mwanzo 3). Laana itaondolewa (kama vile Ufu. 21:3) kama ilivyoshindwa sasa. Kwa neno "batilishwa" katika 1 Kor. 15:24 na 26 angalia Mada Maalumu: *Katargeō* katika 1 Kor. 1:28.

**15:27-28** KIWAKILISHI vitangulizi ni vyenye utata. Dhahiri hii inarejelea uhusiano wa karibu ndani ya Uungu (kama vile 1 Kor. 3:23; 11:3). Kristo, Mwana, ni msaidizi (lakini asiyelingana, kama vile Kol. 3:11) kwa Baba katika kazi yake ya ukombozi ndani ya wakati (kama vile Rum. 11:33-36).

**15:27** Hii ni nukuu kutoka katika Zab. 8:6 pamoja na dokezo lililoongezwa kwa Zab. 110:1. Kwenye neno “kutiisha” tazama maelezo katika 1 Kor. 16:16 na Mada Maalum katika 2 Kor. 9:13.

**15:28 "Basi, vitu vyote vikiisha kutiishwa chini yake"** Je! ni lini hili litatokea? Hili ni swali! Kuna wakati dhahiri wa kuashiria kupitia aya hii.

1. Baadaye (*epeita*), 1 Kor. 15:23
2. Hatimaye (*eita*), 1 Kor. 15:24
3. Atakapo (*hotav*, mara mbili), 1 Kor. 15:24
4. Hapo (*achri*), 1 Kor. 15:25
5. Atakapo (*hostan*), 1 Kor. 15:27
6. Basi (*hostan*), 1 Kor. 15:28

Je! Hii inarejea kwenye

1. Kifo cha Yesu na ufufuo
2. Kupaa kwa Yesu
3. Kurudi kwa Yesu/kuwa na shauku
4. Baadhi ya kipengele cha milenia
   Kuna wakati dhahiri wa utaratibu, lakini Paulo ana maeneno yenye utata sana kwa mfasiri yoyote kutamka bila shaka. Mara nyingi madhanio yetu na theolojia za hatua kwa hatua zimeelezea kifungu hiki katika sura yoyote iliyotakiwa!

ANDIKO **LA NASB (LILILOBORESHWA): 1 WAKORINTHO 15:29-34**
**29 Au je! Wenye kubatizwa kwa ajili ya wafu watafanyaje? Kama wafu hawafufuliwi kamwe, kwa nini kubatizwa kwa ajili yao? 30 Na sisi, kwa nini tumo hatarini kila saa? 31 Naam, ndugu, kwa huku kujisifu kwangu niliko nako juu yenu katika kristo yesu bwana wetu, ninakufa kila siku. 32 ikiwa, kwa jinsi ya kibinadamu, nalipigana na hayawani wakali kule efeso, nina faida gani? Wasipofufuliwa wafu, NA TULE, NA TUNYWE,**

**MAANA KESHO TUTAKUFA.** [33] **Msidanganyike; mazungumzo mabaya huharibu tabia njema.** [34] **Tumieni akili kama ipasavyo, wala msitende dhambi; kwa maana wengine hawamjui Mungu. Ninanena hayo niwafedheheshe.**

**15:29** Aya hii imesababisha matatizo makubwa katika kufasiri. Hatuna ufanano wa vifungu katika maandiko. Tuna rejeo lingine kwa utaratibu huu katika kanisa la awali, ingawa kuna ushaidi kadhaa wa kihistoria kuhusu kitu kile kile kutekelezwa miongoni mwa wasioamini wa karne ya kwanza na ya tatu. Tunapaswa kukubali kwamba hatujui Biblia hasa kwa yale ambayo hii inarejelea. Baadhi ya nadharia ni:

1. Wakristo wapya walibatizwa kuchukua nafasi ya Wakristo waliokufa
2. Waongofu wapya walibatizwa kwa sababu ya heshima yao kwa wapendwa waliokufa
3. Watu katika katekisimu waliokufa kabla ya kubatizwa wakawa mbadala kwa kuwabatiza Wakristo wanaoishi
4. Waongofu wapya walibatizwa juu ya makaburi ya wakristo wenye kusimama imara.

Mawazo kadhaa ya kanuni za kiufasiri huitaji kutumika kwenye fasiri ya aya hii.

1. Kimsingi ni katika mfululizo wa mifano/vielezo vya ukweli wa ufufuo.
2. Mtu hajengei juu ya theolojia/mafundisho.
3. Kwa kuwa hakuna dalili ya rejeo halisi la kihistoria, maandishi haya hayapaswi kusisitizwa au kutumiwa na hakika hayakugeuka kuwa mafundisho (yaani, imani ya wamomosi)
4. Hata haijulikani kimazingira kama Paulo anathibitisha utekelezaji huu au ni kufanya tu dokezo juu yake (kama vile TEV, NJB)

◙**"Kama"** Hii ni SENTENSI YENYE MASHARTI DARAJA LA KWANZA hutumika kufanya utumbuizaji wenye nguvu. Maandiko ya Kiyunani yana neno *holōs* (kwa kweli) katika kishazi hiki.Angalia maelezo katika 1 Kor. 5:1.

**15:31**
**NASB, NKJV"naam"**
**NRSV"hiyo ni hakika"**
**TEV"natangaza hili"**
**NJB"naapa"**

Neno hili halipo katika Kiyunani, lakini katika muktadha, kifungu kifuatacho kinaweza kuwa kanuni ya kiapo.Paulo anatumia kanuni/maagizo ya kiapo mara nyingi kwa kuonyesha ukweli wa kauli zake (kama vile Rum. 9:1; 2 Kor. 1:18,23; 11:10-11,31).

◙ **"kwa huku kujisifu kwangu niliko nako juu yenu katika kristo yesu"** Paulo anaonyesha kwamba kazi yake katika Korintho ni ushahidi wa kazi yake kwa Kristo.Kazi yake imekuwa yenye thamani yake (kama vile 2 Kor. 3:1-2; 7:4; 9:2-3).makanisa ya Paulo yalikuwa ushahidi wa utume na ufanisi wake.

◙ **"ninakufa kila siku"** Kifungu hiki kimewekwa cha kwanza katika sentensi kwa ajili ya kusisitiza (kama vile 2 Kor. 5:14-15; Gal. 2:20; 1 Yohana 3:16). Aya ya 30-32 inarejelea kwenye ugumu/matatizo ambayo Paulo alikumbana nayo katika huduma kwa Kristo (kama vile 2 Kor. 1:8-10, 4:8-12; 6:3-10; 11:23-27). Yeye alijua ilikuwa yenye thamani yake kwa sababu yeye kibinafsi alimwona Kristo aliyetukuzwa njiani wakati akienda Dameski (kama vile Mdo. 9:1-22; 22:3-16; 26:9-18). Theolojia ya Paulo ilielezwa na uzoefu binafsi na ufunuo binafsi (kama vile Mdo 9:1-22; Gal. 1:11-12) na Agano la Kale (mafunzo yake ya walimu wa sheria za Kiyahudi).

**15:32 "ikiwa"** Paulo anatumia SENTENSI MBILI ZENYE MASHARTI DARAJA LA KWANZA kufanya jambo.Kama hakuna ufufuo na hakuna malipo ya Kikristo, kwanini Paulo alikuwa tayari kuteseka kila siku kwa ajili ya injili?

◙ **"nalipigana na hayawani wakali kule efeso"** Paulo hakutaja uzoefu huu katika litania yake ya mateso katika 2 Kor. 11:23-27, na kwa sababu Paulo alikuwa raia wa Kirumi, hapaswi kulazimishwa kupigana na hayawani

wakali.Hii inapaswa kuwa sitiari ya hali ngumu ya kiroho ambayo Paulo alikabiliwa nayo katika Efeso (kama vile 1 Kor. 1:8-10). Baadhi walichukua maandiko haya kikawaida na kuonyesha kifungo katika Efeso.

◙ **"nina faida gani"** Kazi ya Paulo kwa ajili ya Kristo haina athari za kiroho kama hakuna ufufuo, ama kwa Kristo na kwa hivyo hakuna ufufuo kwa Paulo. Kazi zake kwa ajili ya injili, lakini kama injili sio kweli, hakuna malipo (yaani, hakuna wokovu, hakuna ufufuo, hakuna maisha ya milele, hakuna ushirika na Mungu, hakuna kuunganishwa tena na wapendwa mbinguni, kama vile1 Kor. 15:12-19).

◙ **"NA TULE, NA TUNYWE, MAANA KESHO TUTAKUFA"** Hii ilikuwa kauli mbiu ya wenye kupenda anasa.Pia ni nukuu kutoka katika Isa. 22:13 (kama vile Isa. 56:12; Lk. 12:19). Hii ni sawa sawa na msemo wa sasa "Unapita mara moja tu katika maisha, hivyo pata furaha yote unayoweza!" Lakini, Je! kama kuna ufufuo? Je! kama tukisimama mbele za Mungu Mtakatifu kutoa hesabu ya dhabihu ya maisha? (kama vile Dan. 12:2)?!

**15:33 "Msidanganyike"** Hii ni KAULI TENDEWA SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO. Kanisa la Korintho lilikuwa linaongozwa na upotoshaji wa theolojia ya uongo (kama vile 1 Kor. 6:9).

◙ **"mazungumzo mabaya huharibu tabia njema"** Hii inaonekana kuwa nukuu kutoka katika nabii wa Kiyunani, Menander's *Thais*, ikihusianishwa na ukahaba. Baadhi ya kikundi kidogo ndani ya kundi zima katika Korintho kilikuwa wenye fahari ya (1) urithi wa kipindi cha Wagiriki- Warumi au (2) uhuru wa kijinsia. Paulo anaongeza mitazamo yao na kunukuu kutoka kwa wanafalsafa wao wenyewe (kama vile 1 Kor. 15:32 na33). Paulo alilelewa huko Tarso, ambako kulikuwa kunajulikana vizuri kwa shule zake za falsafa ya Kiyunani (kama vile Mdo. 17:28 naTito1:12). Kipekee alijifunza chini ya walimu wa sheria za kiyahudi na mawazo ya Kiyunanai ya kidunia.

◙ **"huharibu" Angalia Mada Maalum katika 1 Kor. 15:42.**

**15:34**
**NASB "tumieni akili kama ifuatavyo"**
**NKJV "amkeni! anzeni kusishi vyema"**
**NRSV "njoeni katika busara na haki"**
**TEV "rudini kwenye akili zenu"**
**NJB "amkeni kutoka kwa kuotojitambua kwako kama unapaswa"**
Hii ni KAULI TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO USIOTIMILIFU. Hii inaonekana kumanisha "kurudi kwenye ufahamu wako wa kimaadili jumla."

◙ **"msitende dhambi"** Hii ni KAULI TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO ikiwa na KIAMBATA HASI ambacho kawaida kinamaanisha kuzuia kitendo kilichoko kwenye mchakato. Ni dhahiri kwamba wale ambao walikataa ufufuo pia walikuwa wanaishi maisha yasiyo ya Mungu. Paulo anatumia uovu wao kama njia ya kuonyesha mwendelezo wa kosa juu ya madai yao ya kithiolojia (yaani, hakuna ufufuo).

◙ **"hawamjui Mungu"** Katika kiingereza hili ni neno "yule ajuaye asili ya Mungu." Hii ilikuwa kejeli ya kutatiza kusema kwa wale ambao waliheshimu maarifa sana!

**ANDIKO LA NASB(LILILOBORESHWA): 1 WAKORINTHO 15:35-41**
**35 Lakini labda mtu atasema, Wafufuliwaje wafu? Nao huja kwa mwili gani? 36 Ewe mpumbavu! Uipandayo haihuiki, isipokufa; 37 nayo uipandayo, huupandi mwili ule utakaokuwa, ila chembe tupu, ikiwa ni ya ngano au nyingineyo; 38 lakini Mungu huipa mwili kama apendavyo, na kila mbegu mwili wake. 39 Nyama yote si nyama moja; ila nyingine ni ya wanadamu, nyingine ya hayawani, nyingine ya ndege, nyingine ya samaki. 40 Tena kuna miili ya mbinguni, na miili ya duniani; lakini fahari yake ile ya mbinguni ni mbali, na fahari yake ile ya duniani ni mbali. 41 Kuna fahari moja ya jua, na fahari nyingine ya mwezi, na fahari nyingine ya nyota; maana iko tofauti ya fahari hata kati ya nyota na nyota.**

**15:35 "labda mtu atasema"** Haya ni matumizi ya Paulo ya mbinu ya kifasihi itwayo tahakiki makemeo. Huu muundo wa swali/jibu pia unaonekana katika Agano la kale kwa Malaki na katika Agano jipya kwa Warumi na 1 Yohana. Suala la kazi ya fasihi imefanyika mbele na mazungumzo kati ya waandishi na mpinzani anayefikiriwa. Hapa mabishano yanaendelea juu ya tofauti ndogo ya mada. Kwanza, baadhi ya vikundi vidogo ndani ya kundi zima walikataa ufufuo wa Kristo na hivyo kukataa ufufuo wa waamini wote. Sasa Paulo anahutubia wale ambao waliuliza utaratibu wa ufufuo wa mwili.

◙ **"Nao huja kwa mwili gani "** Moja ya chanzo cha mgogoro kuhusiana na kufufuliwa kwa mwili huja kutoka kwa mtazamo hasi wa mwili wa asili katika baadhi ya shule za falsafa ya Kiyunani. Wayunani mara nyingi walitazama nyenzo kama uovu (yaani, watu wa mafunuo ya uongo) na mbaya zaidi, mwili wa asili kama gereza la kimeto cha Uungu wa milele au nafsi ndani ya wanadamu wote. Utamaduni huu / historia ya falsafa inakuja katika mgogoro wa moja kwa moja na historia ya Kiebrania ya Paulo (yaani, Mfarisayo) ya uthibitisho wa kimwili, mwili baada ya uhai.

**15:35-41** Paulo anatumia mfuatano wa vielezo ambavyo vinaonyesha kuendelea, na utofauti bado, kati ya mwili wa asili na mwili wa roho.

1. Mbegu dhidi ya mmea uliokomaa, 1 Kor. 15:37
2. Mwanadamu dhidi ya hayawani , 1 Kor. 15:39
3. Miili ya mbinguni dhidi ya miili ya duniani, mst 40
4. Mwezi dhidi ya jua , 1 Kor. 15:41

**15:36 "Ewe mpumbavu"** Watu ambao walidai kumjua Mungu, lakini wanafikiria kutenda katika njia zisizifaa mara nyingi wanaainishwa kama masikini wa akili! Maoni ya kejeli ya Paulo, ya mara kwa mara sana katika 1Wakorintho na 2 Wakorintho, yanafunua aina hii ya mtu. Wao walikuwa wanajiamini sana kwamba walikuwa na maarifa ambayo hawakuweza kuona wala kutambua maarifa ya kweli!

**MADA MAALUM: MANENO KWA WATU WAPUMBAVU (SPECIAL TOPIC: TERMS FOR FOLISH PEOPLE)**

**15:37 "Uipandayo haihuiki, isipokufa"** Paulo tena anafuata maneno ya Yesu (kama vile Yohana 12:24). Haya ni matumizi ya lugha ya ajabu (yaani, namna mambo yanavyojitokeza kupitia milango mitano ya fahamu). Hii haimanishi kuwa kauli ya kisayansi, lakini sitiari ya mambo ya kilimo kwa maisha mapya kutoka kwenye ugumu, anaonekana kwa mbegu kufa.

Neno "isipokuwa" humaanisha SENTENSI YENYE MASHARTI DARAJA LA TATU, ambayo inamaanisha kuwezekana kwa kitendo.

◙ **"ikiwa"** Hii ni KAULI YENYE MASHARTI DARAJA LA NNE isio kamilifu (kama vile 1 Kor. 14:10). Paulo anadai uwepo wa mbegu tofauti za nafaka.

**15:39-40 "nyingine. . . nyingine"** Ya kwanza, imetumika mara nne katika 1 Kor. 15:39 na ya tatu katika 1 Kor. 15:41, ni *allos* na inayofuata "nyingine" imetumika mata tatu katika 1 Kor. 15:40 na ni *heteros*. Utofauti kati ya hizi mbili ulikuwa ni wazi katika Kiyunani cha kale, lakini yamekaribia kupotea katika lugha ya kawaida Koine ya Kiyunani. Katika muktadha huu tofauti inaonekana kubaki:

1. *allos*, nyingine ya aina ile ile (kama vile 1 Kor. 15:39,41)
2. *heteros*, nyingine ya aina tofauti (kama vile 1 Kor. 15:40)

**15:40,41,43 "fahari"** Angalia MADA MAALUMU: UTUKUFU *(AK)* [SPECIAL TOPIC: GLORY (OT)] katika 1 Kor. 2:7.

| |
|---|
| **ANDIKO LA NASB(LILILOBORESHWA): 1 WAKORINTHO 15:42-49**<br>**42 Kadhalika na kiyama ya watu. Hupandwa katika uharibifu; hufufuliwa katika kutokuharibika; 43 hupandwa katika aibu; hufufuliwa katika fahari; hupandwa katika udhaifu; hufufuliwa** |

**katika nguvu; [44] hupandwa mwili wa asili; hufufuliwa mwili wa roho. Ikiwa uko mwili wa asili, na wa roho pia uko. [45] Ndivyo ilivyoandikwa, Mtu wa kwanza, Adamu, akawa nafsi iliyo hai; Adamu wa mwisho ni roho yenye kuhuisha. [46] Lakini hautangulii ule wa roho, bali ule wa asili; baadaye huja ule wa roho. [47] Mtu wa kwanza atoka katika nchi, ni wa udongo. Mtu wa pili atoka mbinguni. [48] Kama alivyo yeye wa udongo, ndivyo walivyo walio wa udongo; na kama alivyo yeye wa mbinguni, ndivyo walivyo walio wa mbinguni. [49] Na kama tulivyoichukua sura yake yule wa udongo, kadhalika tutaichukua sura yake yeye aliye wa mbinguni.**

**15:42-49** Biblia haikufunua kwa uhalisi au kikamilifu mambo yaliyohusishwa na maisha baada ya kifo. Labda kwa sababu hatuwezi katika kuanguka kwetu, kwa dunia hii, hali ya kidunia kwa kuwatambua. Aya hii hujadili ufufuo wa mwili na kuulinganisha na mwili wa kidunia.Bado, hata hivyo si sahihi. Yote yanayoweza kusemwa ni kwamba miili yetu mipya itatayarishwa kikamilifu kwa maisha, ushirika, ibada, na huduma ya Mungu wetu katika zama mpya. Katika uwelewa wa hili, sura halisi ni isiofaa (kama vile Fipl. 3:21; 1 Yohana 3:2).

**15:42**
**NASB, NRSV,**
**NJB"uharibifu. . .kutoharibika"**
**NKJV"uharibifu. . .kutoharibika”**
**TEV"uharibikao. . .usioharibika"**

Mara nyingi neno hili linatumika katika muktadha sawa kama kunusho lenye kinyume (kama vile Rum. 1:23; 1 Kor. 9:25; 15:50,53). Angalia mfanano unaotofautisha kati ya miili yetu ya asili ya kidunia na miili yetu ya milele ya mbinguni.

1. Uharibifu dhidi ya kutokuharibika, 1 Kor. 15:42,50
2. Aibu dhidi ya fahari, 1 Kor. 15:43
3. Udhaifu dhidi ya nguvu, 1 Kor. 15:43
4. Mwili wa asili dhidi ya mwili wa roho, 1 Kor. 15:44
5. Adamu wa kwanza dhidi ya Adamu wa mwisho, 1 Kor. 15:45
6. Sura yake yule wa udongo dhidi ya sura yake yeye alie wa mbinguni, 1 Kor. 15:49

**MADA MAALUM: HARIBU, UTILIFU, UHARIBIFU *(PHTHEIRŌ)* [SPECIAL TOPIC: DESTROY, RUIN, CORRUPT**) ***(PHTHEIRŌ)***

**15:43 "udhaifu"** Angalia MADA MAALUM: UDHAIFU (SPECIAL TOPIC: WEAKNESS) katika 2 Kor. 12:9.

**15:44 "Ikiwa"** Jamii ya umoja wa Biblia *Handbook on Paul's First Letter to the Corinthians* inasema hii sio SENTENSI SHURUTISHI DARAJA LA KWANZA, lakini kauli ya ukweli (kama vile uk. 361). Hata hivyo, A. T. Robertson katika *Word Pictures in the New Testament* huonyesha kwamba ni SENTENSI SHURUTISHI DARAJA LA KWANZA (kama vile uk. 197).Sarufi sio sayansi.

**15:45 "Mtu wa kwanza, Adamu"** Hii ni nukuu kutoka katika Mwa. 2:7. Yesu kumtaja Adamu (kama vile Mt. 19:4; Mk 10:6; Lk 3:38) humaanisha tabia yake ya historia. Yesu alidhani uharibifu wa seti ya kwanza kuitwa Adamu na Hawa.Matumizi ya Paulo ya uainishi wa kipindi cha Adamu- Kristo, hapa pote na katika Rum. 5:17-21, hudai uumbaji maalumu wa Adamu na Eva. Hii inaweza kuwa uumbaji wa baadaye (tazama fasiri yangu juu ya Mwanzo 1-11 (mtandaoni katika **www.freebiblecommentary.org**), ambapo ninaonyesha dunia ya zamani, lakini uumbaji wa hivi karibuni wa Edeni), lakini inaonekana kwangu unapaswa kuwa uumbaji maalumu.

◙ **"Adamu wa mwisho ni roho yenye kuhuisha"** Hii inapaswa kurejea kwenye ufufuo wa Yesu. Haimaanishi kukataa kipengele cha umwili kwa Yesu baada ya kuonekana kwa ufufuo, lakini kwa kutofautisha Adamu wa kwanza ambaye matendo yake yalisababisha kifo, na Adamu wa mwisho, ambaye matendo yake yalisababisha

maisha, maisha ya milele, maisha ya ufufuo! Huu ni mfano wa uainishaji wa kipindi cha Adamu- Kristo (kama vile Rum. 5:12-21; 1 Kor. 15:21-22,45-49; Flp. 2:6-8).

◙ **"roho yenye kuhuisha"** Huu ni mfano mzuri wa ugumu wa kujua katika baadhi ya mazingira kama "roho" inapaswa kuwa na herufi ndogo "s" (kama vile Rum. 8:9; 2 Kor. 3:3; Gal. 4:6; 1 Pet. 1:11).Biblia inatumia neno *pneuma* katika aya kadhaa tofauti. Angalia Mada Maalumu: *Pneuma* katika 1 Kor. 12:1.

**15:46** Hii sio kauli ya ihusianayo na asili ya viumbe, lakini kauli ya wakati kuhusisha na Adamu wa kwanza na Adamu wa pili (kama vile 1 Kor. 15:47). Maisha ya kimwili ya mwanadamu hutangulia maisha ya kiroho!

**15:47 "Mtu wa pili atoka mbinguni"** Kuna nyongeza kadhaa kwenye kifungu hiki katika miswada ya Kiyunani. Wengi wao wanajaribu kutia mkazo kwamba Yesu ni mwanadamu kama Adamu, lakini zaidi kuliko mwanadamu.Bart D. Ehrman, *The Orthodox Corruption of Scripture*, kr. 94-95, ufikiri wa mabadiliko haya ulikuwa ni matokeo ya mkanganyiko ndani ya kanisa kipindi wakati machapisho haya yalikuwa wakiyadurufu.Yeye alipendekeza kuwa nyongeza iwe nyenye makusudi, yenye kufafanua kithiolojia juu ya sehemu ya waandishi wa ki-Orthodox.

**15:49 "Na kama tulivyoichukua sura yake yule wa udongo"** Neno hili hutokea katika miswada ya awali ya Kiyunani P[46], א, A, C, D (yaani, _KAULI TENDAJI TEGEMEZI YA WAKATI ULIOPO USIO TIMILIFU). Muktadha unaonekana kudai maandiko ya miswada B ya awali ya Alexandrian, ambayo ilikuwa, "Tunapaswa kubeba..." (yaani, KAULI TENDAJI ELEKEZI YA WAKATI ULIOPITA). Maneno yote ya Kiyunani yalikuwa yanatamkwa sawa.Miswada ya awali mara nyingi ilinukiliwa katika wakati mmoja na mtu mmoja kusoma maandiko kwa sauti na wanaume kadhaa kufanya nakala za maandishi. Kitheolojia KAULI ELEKEZI YA WAKATI UJAO ni bora. VITENZI vingine katika muktadha ni WAKATI UJAO. Ni muktadha wa kiufafanuzi, sio wa kutia moyo (yaani, kushawishi kwa kitendo)

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 1 WAKORINTHO 15:50-57**
**[50] Ndugu zangu, nisemayo ni haya, ya kuwa nyama na damu haziwezi kuurithi ufalme wa Mungu; wala uharibifu kurithi kutokuharibika. [51] Angalieni, nawaambia ninyi siri; hatutalala sote, lakini sote tutabadilika, [52] kwa dakika moja, kufumba na kufumbua, wakati wa parapanda ya mwisho; maana parapanda italia, na wafu watafufuliwa, wasiwe na uharibifu, nasi tutabadilika. [53] Maana sharti huu uharibikao uvae kutokuharibika, nao huu wa kufa uvae kutokufa. [54] Basi huu uharibikao utakapovaa kutokuharibika, na huu wa kufa utakapovaa kutokufa, hapo ndipo litakapokuwa lile neno lililoandikwa, Mauti imemezwa kwa kushinda. [55] Ku wapi, Ewe mauti, kushinda kwako? U wapi, Ewe mauti, uchungu wako? [56] Uchungu wa mauti ni dhambi, na nguvu za dhambi ni torati. [57] Lakini Mungu na ashukuriwe atupaye kushinda kwa Bwana wetu Yesu Kristo.**

**15:50 "Ndugu zangu"** Hii ni sitiari kwa ubinadamu (kama vile Mt. 16:17; Gal. 1:16; Efe. 6:12; Ebr. 2:14).

◙ **"kuurithi"** Hii ni sitiari ya familia kufafanua ushirika wetu wa milele na Mungu. Katika Agano la kale Walawi walipokea sio ardhi kubwa ya urithi (miji 48 tu ya kilawi), hivyo wao walisemekana kuwa na YHWH kama urithi wao. Agano jipya lilihamisha hili (kama lilivyofanya shughuli nyingi za kuhani) kwa waaminio wote. Angalia MADA MAALUMU: URITHI WA WAAMINIO (SPECIAL TOPIC: BELIEVERS' INHERITANCE) katika 1 Kor. 6:9.

◙**" ufalme wa Mungu"** Angalia maelezo katika 1 Kor.15:24.

**15:51 "siri"** Angalia Mada Maalumu ifuatayo.

**MADA MAALUMU: MPANGO WA MUNGU KWA UKOMBOZI, "SIRI" (SPECIAL TOPIC: GOD'S PALN FOR REDEMPTION "MYSTERY")**

Mungu anakusudi la pamoja kwa ajili ya ukombozi wa mwanadamu ambao ulikuwepo hata kabla ya anguko (Mwanzo3). Dokezo la mpango huu lilifunuliwa katika Agano la kale (Mwanzo 3:15; 12:3; Kutoka 19:5-6; na vifungu vya watu wote katika manabii).Hata hivyo, agenda hii yote pamoja haikuwa wazi (1 Kor. 2:6-8). Na ujio wa Yesu na Roho ulianza kuwa wazi zaidi. Paulo alitumia neno "siri" kuelezea mpango wa ukombozi wa jumla, ambao mwanzo ulifichwa, lakini sasa umefunuliwa kikamilifu (1 Kor. 4:1; Efe. 6:19; Kol. 4:3; 1 Tim. 1:9).Hata hivyo, yeye aliitumia katika maana kadhaa tofauti.

1. Kuimarisha kwa sehemu ya Israeli kuruhusu mataifa kuwekwa pamoja. Huku kuingia kwa wingi kwa mataifa utafanya kazi kama utaratibu wa kufanya jambo (wivu) kwa Wayahudi kumkubali Yesu kama Masihi wa unabii( Rum. 11:25-32).
2. Injili ilifanywa kujulikana kwa mataifa, yote ambayo yana uwezekano kuwekwa pamoja katika Kristo na kupitia katika Kristo(Rum. 16:25-27; Col. 2:2).
3. Waaminio watakuwa na miili mipya katika kuja kwa mara ya pili (1 Kor. 15:5-57; 1 The. 4:13-18).
4. Kuvijumlisha vitu vyote katika Kristo (Efe. 1:8-11).
5. Mataifa na Wayahudi ni warithi wenza (Efe. 2:11-3:13).
6. Urafiki wa karibu sana wa uhusiano kati ya Kristo na kanisa ulielezewa katika maneno ya ndoa (Efe. 5:22-33).
7. Mataifa yaliwekwa pamoja katika Agano la watu na wenye kukaa na Roho ya Kristo ili kuzalisha ukomavu wa kuwa kama kristo, hiyo ni, sura iliyolejeshwa katika kuanguka kwa mwanadamu (Mwa. 1:26-27; 5:1; Kol. 1:26-28).
8. Wakati wa mwisho wa Mping Kristo (2 The. 2:1-11).
9. Muhtasari wa kanisa la awali wa siri hupatikana katika 1 Tim. 3:16.

◙ **"hatutalala sote, lakini sote tutabadilika"** Hii inaonekana kuonyesha kwamba kutakuwepo na Wakristo waliohai katika kuja kwa mara ya pili (kama vile 1 The. 4:13-18). Kulala ni tasifida ya kibiblia kwa kifo.

Je! Paulo alitarajia kuwa hai katika kuja kwa mara ya pili au hii ni namna ya kiuhariri ya neno "sisi" (hai katika kurudi kwa Yesu, 1 Kor. 15:51-52; 1 The. 4:15,17 au atafufuliwa katika kurudi kwa Yesu, 1 Kor. 6:14; 2 Kor. 4:14; 5:1-10)? Kama wandishi wote wa Agano jipya na Yesu, yeye anaonekana alitarajia kurudi kwa karibu sana kwa Kristo aliyetukuzwa. Lakini Baba pekee ndiye aliyejua wakati (kama vile Mt. 24:36; Mk. 13:32; Mdo. 1:7). Waaminio wanatakiwa kuishi kila siku katika mwanga wa tumaini la kurudi kwa mara ya pili, lakini kupanga na kujifunza kwa shughuli za ufalme kama itabidi kucheleweshwa.

## MADA MAALUMU: KURUDI KWA YESU MUDA WOWOTE DHIDI YA KUTORUDI (FUMBO LA AGANO JIPYA) [SPECIAL TOPIC:THE ANY –MOMENT RETURN OF JESUS VERSUS THE NOT YET (NT PARADOX)]

**15:52 "kwa dakika moja"** Tunapata neno la kiingereza "chembe" kutoka katika neno la Kiyunani "isiyoweza kugawanyika."

◙ **"kufumba na kufumbua"** Hii inatumika kwa maana ya kupepesa kwa nyota au mwendo wa haraka wa mbawa za aina ya visubi. Maana ya haya maneneo mawili ni kwamba kurudi kwa Yesu kutatokea haraka sana mara itakapoanza. Hakuna wakati wa sala za dakika za mwisho.

◙ **"wakati wa parapanda ya mwisho"** Hii ilikuwa njia ya Agano la Kale ya kutangaza matukio ya siku za mwisho na njia ya *shophar* (yaani, pembe ya kushoto ya kondoo dume, kama vile Isa. 27:13; Zek. 9:13; Mt. 24:31; 1 The. 4:16).Ni hakika inawezekana kwamba parapanda ilikuwa sitiari kwa sauti ya Mungu (kama vile Kut. 19:16,19; 20:18; Ufu. 1:10), pia ilitumiwa kwa sauti za manabii (kama vile Isa. 58:1; Ebr. 12:19).

## MADA MAALUM: PEMBE ZILIZOTUMIWA NA WAISRAELI (SPECIAL TOPIC: HORNS USED BY ISRAEL)

**15:54** Hii ni rejeo kwa Isa. 25:8, ambayo pia lidokezwa katika Mt. 5:11; 1 Pet. 4:14; Ufu. 7:17; 21:4. Aya ya 54 na 55 dhahiri ni njia ya Paulo ya kudhihaki adui mkuu wa mwisho wa wanadamu kifo, ambaye alishindwa kabisa katika

ufufuo wa Kristo kutoka katika wafu na wafuasi wake kuwekwa huru kutoka katika adhabu ya dhambi na wanasubiri ufufuo wenyewe.

**15:55** Hii ni rejeo kwa Hosea 13:14, ambayo hurudisha nyuma amri na kunukuu andiko la Agano la Kale. Nukuu nyingi za Agano la kale katika Agano jipya ni kutoka katika tafsiri ya Kiyunani ya Agano la kale. Ilikuwa ni Biblia ya kanisa la karne ya kwanza.

**15:56** Katika aya hii Paulo anaonyesha kuvunjika kwa uhusiano wa binadamu na Mungu uliosababishwa na dhambi (kama vile Mwanzo 3; Warumi 2-3). Uasi huu ulitusababisha sisi kujisikia kutenganishwa kutoka kwa yule mmoja hasa aliyetufanya sisi kwa mfano wake.

Dhambi iliingia ulimwenguni kupitia katika kitendo cha hiari cha kutotii.Neno "sheria" hairejelei kwa sheria za Musa, lakini kwa makatazo ya Mungu kwa ujumla. Sisi ni waharibifu, lakini Mungu alichagua kurejesha ushirika kupitia Kristo. Ni dhambi gani iliyoharibu, Kristo hurejesha (yaanii, ushirika wa milele na Mungu; sura iliyoharibiwa imerekebishwa).

**15:57 "Mungu na ashukuriwe"** Hii inanikumbusha kulia kwa Paulo katika Rum. 6:17 na 7:25. Ni ishara ya sitiari kuu ya Paulo ya kushangilia matukio ya Warumi katika 2 Kor. 2:14, pamoja na mlipuko wake wa shukrani katika 2 Kor. 9:15. Angalia Mada Maalum: Kusifu kwa Paulo, sala, na shukrani katika 2 Kor. 2:14.

◙ **"kushinda kwa Bwana wetu Yesu Kristo"** ushindi wote wa kiroho unakuja kupitia Kristo na Kristo pekee! Tayari umekuja! Waaminio wanaishi katika nuru ya ushindi kamili na ukamilifu wa Kristo!

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 1 WAKORINTHO 15:58**
**58 Basi, ndugu zangu wapendwa, mwimarike, msitikisike, mkazidi sana kutenda kazi ya Bwana sikuzote, kwa kuwa mwajua ya kwamba taabu yenu siyo bure katika Bwana.**

**15:58** Paulo alihitimisha mjadala huu mkubwa mno wa Kitheolojia wa ufufuo na kutia moyo kwa utendaji wa mchungaji kwa uhitaji thabiti na uvumilivu katika maisha yote ya kila siku ya Ukristo. Kuishi milele kuna sifa ya kuonekana! Kuna KAULI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO Moja iliyofuatwa na KAULI ENDELEVU mbili iliyotumika kama KAULI SHURUTISHI. Itakuwa na thamani yake wakati wote tutakapomwona yeye na kukaribishwa kwa nadra katika ufalme wa milele!

◙ **"mkazidi"** Angalia Mada Maalum katika 2 Kor.2:7.

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa maoni ya usomaji, ukiwa na maana kuwa, unawajibika kwa fasiri binafsi ya Biblia. Kila mmoja wetu yampasa atembee katika nuru tulionayo, na Roho Mtakatifu ndiye kipaumbele katika fasiri yetu. Usimwachie hili mtoa maoni pekee.

Maswali haya ya kujadili yanatolewa ili kukusaidia kufikiri mambo muhimu yaliyoko katika kipengele cha kitabu hiki. Yanamaanisha kuwa maswali ya kichokonozi, yasio na ukomo.

1. Orodhesha vipengele vinne vya maisha ya Kikristo vinavyopatikana katika 1 Kor. 15:1 na 2.
2. Orodhesha mafundisho makuu ya injili yanayopatikana katika 1 Kor. 15:3 na 4.
3. Kwa nini Paulo alijiona kuwa ni aliye mdogo kwa mitume?
4. Je! nini kilikuwa msingi wa waumini wa kanisa la Korintho kukataa ufufuo.
5. Ni nini uainishaji wa kipindi cha Adamu -Kristo?
6. Je! Inamaanisha nini juu ya kubatizwa kwa wafu?
7. Je! Miili yetu ya ufufuo itakuwa inafanana na ya binadamu?

# 1 WAKORINTHO 16

| MGAWANYO WA AYA WA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **UBS[4]** | **NJKV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB** |
| Mchango kwa ajili ya Watakatifu | Changizo kwa Ajili ya Watakatifu | Jumbe za Mwisho | Sadaka kwa Ajili ya Waamini walio Wahitaji | Salamu zenye sifa |
| 16:1-4 | 16:1-4 | 16:1-4 | 16:1-4 | 16:1-4 |
| Mipango ya safari | Mipango Binafsi | | Mipango ya Paulo | |
| 16:5-9 | 16:5-12 | 16:5-9 | 16:5-7 | 16:5-9 |
| | | | 16:8-9 | |
| 16:10-11 | | 16:10-11 | 16:10-11 | 16:10-12 |
| 16:12 | | 16:12 | 16:12 | |
| Nasaha na Salamu za Mwisho | Ushawishi wa Mwisho | | Maneno ya Mwisho | |
| 16:13-14 | 16-13-18 | 16:13-14 | 16:13-14 | 16:13-14 |
| 16:15-18 | | 16:15-18 | 16:15-16 | 16:15-18 |
| | Salamu na Maagano ya Dhati | | 16:17-18 | |
| 16:19-20 | 16:19-24 | 16:19-20 | 16:20a<br>16:20b | 16:20 |
| 16:21-24 | | 16:21-24 | 16:21 | 16:21 |
| | | | 16:22a<br>16:22b | 16:22 |
| | | | 16:23 | 16:23 |

**MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI** (kutoka "**Mwongozo wa Usomaji Mzuri wa Biblia**" **(A Guide to Good Bible Reading)**

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILIA LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo wa usomaji wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako binafsi ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika nuru tuliyonayo. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hupaswi kumwachia kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo. Linganisha mgawanyo wa masomo yako na tafsiri tano hapo juu. Kugawanya katika aya hakuna uvuvio, isipokuwa ni ufunguo wa kufuatilia kusudio la asili la mwandishi ambalo ndilo kiini cha ukalimani. Kila aya ina somo moja na ni moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

## UTANGULIZI

A. Sura ya 15 imeibua mjadala mkubwa wa kitheolojia unashughulika na ile kweli ya ufufuo, ambapo sura ya 16 inahusika na utendaji wa Kristo wa kila siku. Paulo hakuwa na tatizo lililoendelea kati ya kweli na uzima. Hivi lazima vingewekwa kwa pamoja. Aina hii ya mabadiliko ya ghafla kutoka somo moja kwenda somo lingine yanaeleza maandiko ya Paulo.
B. Ufafanuzi Fasaha:
    1. 1 Kor. 16:1-4, changizo la maskini wa huko Yudea
    2. 1 Kor. 16:5-9, mpango wa safari isiyotarajiwa ya kuelekea Korintho
    3. 1 Kor. 16:10-12, watenda kazi wengine walio Wakristo
    4. 1 Kor. 16:13-18, mahusia ya mwisho
    5. 1 Kor. 16:19-24, salamu za mwisho
C. Uhusiano wa Paulo na Akila na Priska:
    1. Hawa walikuwa watengeneza mahema ya Kiyahudi (au watengeneza ngozi) katika Roma. Amri ya Claudio ya mwaka 49-50 B.K iliyoziondoa desturi zote za Kiyahudi (ambapo kwa wakati huo shughuli za kanisa zilijumuishwa), na kuwalazimisha wao kuondoa.
    2. Hawa walikutana na Paulo katika Korintho, Matendo18:2.
    3. Baadaye walihamia Efeso na kuanzisha kanisa la nyumbani, 1 Kor. 16:19.
    4. Walirudi Rumi baada ya kifo cha Claudio katika mwaka 54 B.K na hivyo amri ilivunjwa, Rum. 16:6.

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LIILOBORESHWA) : 1 WAKORINTHO 16:1-4**

[1] **Kwa habari ya ile changizo kwa ajili ya watakatifu, kama vile nilivyoamuru makanisa ya Galatia, nanyi fanyeni vivyo.** [2] **Siku ya kwanza ya juma kila mtu kwenu na aweke akiba kwake, kwa kadiri ya kufanikiwa kwake; ili kwamba michango isifanyike hapo nitakapokuja;** [3] **nami nitakapofika nitawatuma kwa nyaraka wale mtakaowachagua, wachukue hisani yenu mpaka Yerusalemu.** [4] **Na kama ikifaa niende na mimi, watasafiri pamoja nami.**

**16:1 "Kwa habari ya"** "*Peri de"* hiki ni kifungu cha Kiyunani ambacho kinalitambulisha jibu la Paulo kuhusiana na maswali ambayo yalitumwa na kanisa la Korintho kwenda kwa Paulo (kama vile1 Kor. 7:1,25; 8:1; 12:1; 16:1,12).

◙ **"ile changizo"** *Logia* ni neno liliopatikana katika mafunjo ya Kiyunani huko Misri kama zawadi ya fedha kwa ajili ya kusudi la kidini, lakini halikuhusiana na kodi ya kawaida (kama vile Moulton, Milligan, *The Vocabulary of the Greek Testament*, uk. 377). Kwanza Pulo anautaja woga huu kwa ajili ya wale maskini katika Uyahudi kwenye mazungumzo na Yakobo, Petro, Yohana, na Barnaba katika Gal. 2:10; 6:10. Sadaka maalum ilianzishwa na kanisa la huko Antiokia ambapo Paulo na Barnaba walihudumu, Matendo 11:27-30. Sadaka inatajwa katika vitabu kadhaa vya Agano Jipya (kama vile Rum. 15:26; 2 Kor. 8-9; 1 Kor. 16:1). Hizi zilikuwa juhudi za kuufuta uhusiano baina ya kanisa mama la Kiebrania na makanisa ya Mataifa.

Paulo analiita hili changizo kwa maana kadhaa.

1. sadaka (zawadi za msaada ), Matendo 24:17
2. ushirika, Rum. 15:26,27; 2 Kor. 8:4; 9:13
3. yenye deni, Rum. 15:27
4. hudumu, Rum. 15:27; 2 Kor. 9:12

◙ **"kwa ajili ya watakatifu"** Neno "Watakatifu" (*hogioi*) linatokana na neno la Agano la Kale "takatifu," (*kados*h) ambalo lilimaanisha "kutenga kwa ajili ya huduma ya ki-Mungu" (kama vile 1 Kor. 1:2; 2 Kor. 1:1; Rum. 1:1; Efe. 1:1; Flp. 1:1; Kol. 1:2). Katika Agano Jipya mara nyingi neno hili ni WINGI isipokuwa limetokea mara moja katika Wafilipi (4:21), lakini hata hapa, linatumika kwa namna ya umoja. Kuokolewa ni kuwa sehemu ya jamii ya agano la imani, familia ya waaminio.

Watu wa Mungu ni watakatifu kwa sababu ya haki ya Yesu iliyogharimiwa (kama vile Warumi 4; 2 Kor. 5:21). Ni mapenzi ya Mungu kwamba hawa waishi maisha matakatifu (kama vile 1 Kor. 1:4; 4:1; 5:27; Kol. 1:22; 3:12). Waamini wote wanaelezwa kama walio watakatifu (utakaso wa mahali) na wanaitwa katika maisha ya utakatifu (utakaso endelevu). Uthibitisho na utakaso kwa pamoja lazima ushikiliwe kwa uthabiti! Angalia Mada Maalum: Watakatifu katika 1 Kor. 1:2 na Utakaso katika 1 Kor. 1:2.

◙ **"kama vile nilivyoamuru makanisa ya Galatia"** Paulo hakulichukulia kanisa la huko Korintho kwa utofauti. Kulikuwa na viwango vya kawaida (kama vile 1 Kor. 4:17; 7:17; 11:34; 14:33; Tito 1:5) katika sadaka hii. Hatufahamu ni kwa jinsi gani Paulo alilizungumza hili kwa makanisa ya Galatia. Ikiwa jambo hili ni la kweli hatuna uhakika ni kanisa lipi linarejelewa na neno hili. Wengine wanafikiri kuwa hili linarejea juu ya dora ya Kirumi ambapo wengine wanafikiri kuwa hii ni lugha tu au kwa ajili ya kabila fulani.

◙ **"makanisa"** Angalia Mada Maalum katika 1 Kor. 1:2

**16:2 "Siku ya kwanza ya juma"** Mpangilio wa ibada uliwekwa na mwonekano wa awali wa ufufuo wa Yesu uliotangulia usiku wa manane wa siku ya Jumapili (kama vile Yohana 20:19,20). Hii iliboreshwa kwa ajili ya siku ya kawaida ya kutaniko la ibada ya kanisa (kama vile Matendo 20:7; Ufu. 1:10). Siku ya Jumapili ilikuwa siku ya kwanza ya juma ya kazi hadi kipindi cha Constantine (Mfalme wa Milki ya Kirumi kuanzia mwaka 306-337 B. K). Wakristo walikutana kabla ya kazi katika siku za Jumapili kwa ajili ya ibada, kuhubiri, na kwa ajili ya Karamu ya Bwana.

Viongozi wa Kiyahudi waliliboresha upya baada ya kuanguka kwa Yerusalemu mnamo mwaka 70 B. K na kufanya marekebisho kadhaa. Moja kati ya hayo lilikuwa kile kiapo kilichomlaani na kumkana Yesu kama Masihi. Waamini wa kale walikuwa wakikutana katika sinagogi katika siku za Sabato na kanisa siku ya Jumapili. Hata hivyo, kiapo hiki kililazimisha mgawanyiko na waamii waliifanya siku ya Jumapili kuwa siku yao iliyochaguliwa kwa ajili ya ibada.

◙ **"kila mtu kwenu na aweke akiba kwake"** Hii ni KAULI TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO ikifuatiwa na KAULI TENDAJI YA WAKATI ULIOPO ENDELEVU inayotumika kama YENYE USHURUTISHI. Andiko hili linaonekana kumaanisha kwamba kama lilivyokuwa juma la kwanza, kila mtu aliitunza sadaka yake mahali salama huko nyumbani, na baadaye kupelekwa kanisani. Hata hivyo, ukweli ni kwamba siku ya Jumapili ndipo walipokuwa wakiziweka hadharani fedha zote zilizokuwa zimekusanywa kwa siku katika juma la huduma ya ibada (kama vile Justin Martyr, *Apology* 1.67-68). Tambua kwamba mstari huu mfupi uliounganishwa na 2 Wakorintho 8 na 9 unatupatia mwongozo wa msingi kwa utoaji wa Agano la Kale: (1) kwa ukawaida; (2) kama upendeleo; (3) kwa hiari; (4) kwa furaha; ana (5) kwa uwiano.

Inashangaza kuwa waandishi wa Agano Jipya hawaujadili utoaji wa kiwango cha kawaida cha Mkristo. Maneo ya Paulo ya msistizo na utaratibu wa wakati ule ule wa makanisa ya Mataifa kwa kanisa mama katika Yerusalemu ni mwongozo pekee unaohusiana na somo hili. Wakristo walitambua kwamba hawakumiliki cho chote na wasimamizi wa mali zao zote. Uelewa huu wa herufi mbalimbali za ile dhana ya Agano la Kale "kutoa zaka." Kwa uhakika hii ni kweli kwamba unaweza kuusemea upendeleo wa mtu kwa kutazama kitabu chake cha hundi na kalenda yake! Utoaji wa Mkristo ni jambo la kuwa na moyo uliomiminika, si jambo la kupigia mahesabu!

**MADA MAALUM: UTOAJI WA ZAKA (SPECIAL TOPIC: TITHING)**

**NASB, NKJV "kwa kadiri ya kufanikiwa kwake"**
**NRSV "vyo vyote uwezavyo kuzidisha"**

**TEV "katika kiasi kile mlichokipokea"**
**NJB "vyo vyote vile mtu awezavyo kuongeza**

"Kifasihi hii ni "kwa vyo vyote vile ikiwa atakuwa amefanikiwa" (A. T. Robertson, *Word Pictures In the New Testament*, anasema, "hakuna uyakini wenye kuonyesha nini muundo wa kisarufi cha neno *eudō tai*, KAULI TEGEMEZI TENDEWA YA WAKATI ULIOPO, KAULI TENDEWA ELEKEZI YA WAKATI TIMILIFU, au tena KAULI TENDEWA TEGEMEZI YA WAKATI TIMILIFU" uk. 200). Hii ilikuwa nahau ya Kiyunani yenye kumtakia mtu furaha, safari yenye mafanikio (kwa makusudi ya kibiashara). Paulo anaitumia nahau hii kama kanuni ya utoaji wa Mkristo (yaani, kulingana na uwezo wako, kama vile 2 Kor. 8:3,11).

◙ **"ili kwamba michango isifanyike hapo nitakapokuja"** Paulo mara kadhaa alikuwa akitahadharisha kuhusiana na matumizi mazuri ya pesa. Bila shaka (1) alikuwa ameyaona matatizo yakiendelea katika eneo hili au (2) kibinafsi alikuwa amelaumiwa katika eneo hili. Yeye hakuwa na kawaida ya kuchukuwa fedha kutoka katika makanisa aliyokuwa akiyahudumia na pia wakati hisani hii ilipokuwa ikitolewa kwenda Yerusalemu yeye alihitaji wawakilishi kutoka makanisa mbalimbali kwa ajili ya kuambatana pamoja naye. Hata yeye hakuwa na uhakika wa kwenda peke yake (kama vile 1 Kor. 16:4).

**16:3 "nami nitakapofika nitawatuma kwa nyaraka wale mtakaowachagua, wachukue hisani yenu"** Mstari huu una mchanganyiko wenye kuvutia wa mamlaka ya kiutume na mamlaka ya kimakusanyo. Imejadiliwa kama yule aliyeandika nyaraka za nasaha, Paulo au lile kanisa (kama vile Matendo 18:27). Kisarufi vyote vinawezekana. Toleo la King James na lile la RSV hufikiri kuwa hili lilikuwa kanisa ambapo lile toleo la Williams NT, TEV, NIV, NJB, na REB hufikiri kuwa ni Paulo. Paulo alilitaka kanisa kuwachagua wawakilishi wa kwenda na sadaka zilizokuwa zikibaki ambazo kwazo yeye alikuwa akishutumu kwa matumizi mabaya, kama ilivyokuwa kawaida kwa kanisa hili (kama vile 1 Kor. 9:3-18).

Mara nyingi Paulo aliandika nyaraka za nasaha kwa watendaazi waliokuwa pamoja naye (kama vile Rum. 16:1; 2 Kor. 3:1; ;8:18-24; na mifano mingine, Matendo 9:2; 22:5; 3 Yohana). Paulo anaitumia dhana hii kwa njia ya istiari katika 2 Kor. 3:1 katika maana kwamba makanisa yake yaliyokuwa yakitenda kazi yalikuwa yakilengwa na waraka wa nasaha. Inavyoonekana Mtume Yohana pia anaishughulikia aina hii ya waraka (kama vile 3 Yohana 9). Katika maana iliyodhahiri hii ilikuwa njia ambapo makanisa ya awali yalikuwa yakiri juu ya injili ya wale wahudumu waliokuwa wakihama hama.

**16:4 "kama"** Hii ni SENTENSI YENYE MASHARTI DARAJA LA TATU, ambayo ilimaanisha tendo lenye uwezekano.

**NASB "ikifaa niende na mimi"**
**NKJV "ikinibidi nami niondoke"**
**NRSV "ikiwa bora"**
**TEV "ikionekana vema"**
**NJB "kama ni mimi kuondika"**

Hii inaonekana kuhusiana na (1) kiwango cha sadaka; (2) yule aliyeanzisha kuiunga mkono sadaka hii; au (3) hitaji laPaulo kwa kanisa hili, ambalo linapitia matatizo kama haya kwa mamlaka yake, ni kuitambua kazi yake iliyo sahihi na uaminifu.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : 1 WAKORINTHO 16:5-9**
**[5] Lakini nitakuja kwenu, nikiisha kupita kati ya Makedonia; maana napita kati ya Makedonia. [6] Labda nitakaakwenu; naam, labda wakati wote wa baridi, mpate kunisafirisha ko kote nitakakokwenda. [7] Maana sipendi kuonana nanyi sasa, katika kupita tu, kwa sababu nataraji kukaa kwenu muda kidogo, Bwana akinijalia. [8] Lakini nitakaa Efeso hata Pentekoste; [9] kwa maana nimefunguliwa mlango mkubwa wa kufaa sana, na wako wengi wanipingao.**

**16:5-9** Paulo alikuwa akiisubiri Efeso katika safari yake ya tatu ya umisheni. Baaadaye alishambuliwa na kundi lililokuwa ndani ya kanisa huko Korintho kwa sababu ya kudhaniwa kama "kigeugeu" mipango ya kusafiri (kama vile 2 Kor. 1:15na kuendelea). Kwanza alikuwa akielekea kuishika njia ya bahari kwenda Korintho na kupita Makedonia, lakini kwa sababu alitaka kukaa sana, kwanza aliamua kuishika njia ya nchi kavu kupitia Makedonia na kIsha Korintho. Alikaa pale kwa wakati wote wa baridi (kama vile Matendo 20:2,3). Katika kanisa wengine waliitumia ile mipango ya safari ya Paulo iliyokuwa na mashaka kuishambulia theolojia yake (yaani, injili).

**16:6 "mpate kunisafirisha ko kote nitakakokwenda"** Hiki KITENZI *propempō* kinatumika kama neno la kiufundi kwa ajili ya kutoa mahitaji kwa wale wahudumu wa Mungu wanaozunguka sehemu mbali mbali (kama vile 1 Kor. 16:11, "kusafirisha," kama vile Matendo 15:3; Rum. 15:24; 2 Kor. 1:16; Tito 3:13; 3 Yohana 6).

**16:7 "Bwana akinijalia"** Hii ni SENTENSI YENYE MASHARTI DALAJA LA TATU, yenye kumaanisha tendo lenye uwezekano. Hiki si kifungu cha kawaida kwa Wakristo wa Agano Jipya. Wao waliamini ya kwamba hatua zao zinaongozwa na Bwana kwa majaliwa yake (kama vile Matendo 18:21; 1 Kor. 4:19; Yakobo. 4:14; Ebr. 6:3).

**16:8 "Pentekoste"** Mara nyingi neno hili linamaanisha "hamsini." Hili linarejelea juu ya sikukuu ya mavuno ya ngano (yaani, Sikukuu ya Majuma, kama vile Hes. 28:26) ya Wayahudi ambayo ilikuwa ikitokea siku 50 baada ya siku ya pili ya Sikukuu ya Mikate Isiyochachwa (yaani, *Nisan* 16). Katika muktadha huu inaonekana kwamba neno hili linatumika kama njia ya kuweka kipindi maalum cha mipango ya safari za Paulo na si kueleza kuwa Paulo alikuwa akiendelea kuzishikilia sikukuu hizi ya Kiyahudi.

**16:9**
**NASB "kwa maana nimefunguliwa mlango mkubwa wa kufaa sana"**
**NKJV "kwa kuwa umefunguliwa mlango mkubwa na wenye mafanikio kwangu"**
**NRSV "naam mlango mkubwa kwa ajili ya kazi iliyo njema umefunguliwa kwangu"**
**TEV "mlango uko wazi kabisa kwa ajili ya kazi yangu muhimu hapa"**
**NJB "mlango mkubwa uliohaidiwa uliohimarika kwa upana umefunguliwa kwangu"**

Hii ni KAULI TENDAJI ELEKEZI YA WAKATI TIMILIFU. Matumizi ya hili neno "mlango"kama sitiari kwa maana ya fursa ni ya kawaida katika Agano Jipya (kama vile Matendo 14:27; 2 Kor. 2:12; Kol. 4:3; Ufu. 3:8).

**MADA MAALUM: MATUMIZI YA NENO "MLANGO" KATIKA AGANO JIPYA (SPECIAL TOPIC: USE OF "DOOR" IN THE NT)**

◙ **"na wako wengi wanipingao"** Upendeleo wa ki-Mugu mara nyingi unaendena na upinzani. Kwa mazingira ya kihistoria soma Matendo 19:19-20; 20:19,23.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : 1 KORINTHO 16:10-11**
**10 Lakini, Timotheo akija, angalieni akae kwenu pasipo hofu; maana anaifanya kazi ya Bwana vile vile kama mimi mwenyewe; 11basi mtu ye yote asimdharau, lakini msafirisheni kwa amani, ili aje kwangu; maana ninamtazamia pamoja na ndugu zetu.**

**16:10 "akija"** Hii ni SENTENSI YENYE MASHARTI DALAJA LA TATU, yenye kumaanisha tendo lenye uhakika. Inaonekana kwamba Paulo tayari alikuwa ameshamtuna Timotheo na Erasto (kama vile Matendo 19:22),na bila shaka Tito (kama vile 2 Kor. 2:13; 7:6,7) huko Korintho kwa safari ya nchi kavu. Yeye aliutuma waraka wake kupitia njia ya bahari na ungeweza kufika haraka sana.

◙ **"angalieni akae kwenu pasipo hofu"** Paulo analiweka hili katika mfumo wa masharti (yaani, KAULI TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO). Kibinafsi alijua kanisa lisilokuwa na upendo ambavyo lingekuwa. Hakutamka msaidizi wake aliye mchanga kupuuzwa kwa sababu ya (1) umri wake; (2) mwonekano wake; au (3) hasira yao inayomhusu Paulo (kama vile 1 Kor. 16:11).

**16:11**
**NASB, NKJV,**
**NRSV "Hivyo asitokee ye yote wa kumdharau"**
**TEV "Asiwepo mtu ye yote wa kumbeza"**
**NJB "hakuna mtu anayepaswa kumchukulia visivyo"**

Hii ni KAULI YA TENDAJI TEGEMEZI YA WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFU, ambacho kinamaanisha "kutofanya cho chote kabisa juu ya" (kama vile 1 Kor. 1:28; 1 Tim. 4:12; Tito 2:15).

◙ **"pamoja na ndugu"** Hatuna uhakika kama huyu amehusishwa. Yawezekana huyu ni Erasto (kama vile Matendo 19:22, na Tito, 2 Kor. 2:13; 7:6-7), lakini po pote pale, ikiwa ye yote yule, si dhahiri.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : 1 WAKORINTHO 16:12**
[12] **Lakini kwa habari za Apolo, ndugu yetu, nalimsihi sana aende kwenu pamoja na hao ndugu; ambaye si mapenzi yake kwenda sasa; lakini atakuja atakapopata nafasi.**

**16:12 "Lakini kwa habari"** Hili ni jibu lingine la swali lililoulizwa na kanisa la Korintho (kama vile 1 Kor. 7:1,25; 8:1; 12:1; 16:1,12).

◙ **"Apolo"** Huya alikuwa ameelimika sana na mhubiri aliyekuwa na ushawishi kutoka Alexandria,Misri. Hapo mwanzo alikuwa katika Korintho (kama vile Matendo 18:24-19:1), lakini alikataa kurudi (kama vile 1 Kor. 16:12).

◙ **"ambaye si mapenzi yake kwenda sasa"** Hili andiko linaweza kufasiriwa katika njia mbili: (1) hayakuwa mapenzi ya Apolo kuja au (2) hayakuwa mapenzi ya Mungu kwa yeye kuja. Kutokana na mstari huu inaonekana kwamba Apolo aliwaacha Waefeso kati ya kile kipindi ambacho Paulo ailikuwa akizungumza kumhusu na kuandika waraka huu.

**ANDIKAO LA NASB (LILILOBORESHWA) : 1 WAKORINTHO 16:13-14**
[13] **Kesheni, simameni imara katika Imani, fanyeni kiume, mkawe hodari.** [14] **Mambo yenu yote na yatendeke katika upendo.**

**16:13-14** Huu ni mpangilio wa KAULI TANO SHURUTISHI ZA WAKATI ULIOPO. Hizi zinafanana sana na yale mahusia ya 1 Kor. 15:58. Zile nne za kwanza ni <u>nafsi ya tatu wingi</u> na zina usuli wa kijeshi. Ile ya mwisho ni NAFSI YA PILI UMOJA na inaonekana kueleza juu ya ushirika wa kanisa.

**16:13**
**NASB " Kesheni,**
**NKJV "jichungeni"**
**NRSV "kaa tayari"**
**TEV "iweni imara"**
**NJB "iweni macho**"

Hii ni KAULI TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO. Ile maana yake ya kimsingi ni kuzinduka, linatumika katika maana ya neno "kujihadhari" (kama vile Mt. 24:42; 25:13; 26:38,40,48; Marko 13:35,37; 14:34,37,38). Paulo anawaasa ya kuwa wawe imara na wenye kujihadhari dhidi ya roho ya matengano, uasi, ufisadi, na majisifu!

**NASB, TEV " simameni imara katika Imani""**
**NKJV "simameni kwa uthabiti katika imani"**
**NRSV "simameni imara katika imani tenu"**
**NJB "kaeni kwa uhodri katika imani"**

Hii ni KAULI nyingine iliyo TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO. Hili ni neno la kijeshi lenye kumuasa mtu kushikilia nafasi aliyonayo. Aya ya neno "Katika imani" inarejelea ile kweli ya Mkristo au yale mafundisho ya Mkristo (kama vile Yuda 1:3, 20).
Angalia Mada Maalum: Kusimama (*Histēmi*) katika 1 Kor. 15:1.

◙ **"fanyeni kiume"** Hii ni KAULI SHURUTISHI (shahidi)YA WAKATI ULIOPO . Haya ni matumizi pekee ya hili neno ndani ya Agano Jipya pekee. Huu ni muundo wa KITENZI cha neno *anēr*, kinachomaanisha mtu aliyekomaa au mwaname.Hili limeonekana katika Tafsiri ya Agano la kale ya Kiyunani (LXX) katika Yos. 1:6. Hili si jumuishi (yaani, inarejelea kwa wanaume pekee), bali inalisistiza kanisa zima kutenda kwa usahihi kama waamini waliokomaa na wenye ushujaa.

◙ **"mkawe hodari"** Hii ni KAULI TENDEWA SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO.

**MADA MAALUM: IWENI HODARI (SPECIAL TOPIC: BE MADE STRONG)**

**16:14 "Mambo yenu yote na yatendeke katika upendo"** Tazama neno "yote" limewekwa kipaumbele katika maandishi ya Kiyunani kwa ajili ya msistizo. Katika hali ya kidini na kitamduni kama iliyo na nguvu, ya namna mbali mbali, na yenye utatanishi kama Korintho, upendo ni mhumu. Hii ni KAULI nyingine YA KATI (shahidi) SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO ). Imani sahihi na utendaji sahihi wa kimaadili na kiluturujia pasipo upendo hiyo si kwa ajili ya mapenzi ya Mungu au njia (kama vile 1 Kor. 14:1)! Ni vigumu kutambua kwamba maana (kwa Wakristo) ni nini kama ulivyo umuhimu kama zilivyo hatima.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : 1 KORINTHO 16:15-18**
**15 Tena ndugu, nawasihi; (mnawajua watu wa nyumbani mwa Stefana kwamba ni malimbuko ya Akaya, nao wamejitia katika kazi ya kuwahudumu watakatifu); 16 watiini watu kama hawa, na kila mtu afanyaye kazi pamoja nao, na kujitaabisha. 17 Nami nafurahi kwa sababu ya kuja kwao Stefana na Fortunato na Akaiko; maana hawa wamenikirimia kwa wingi yale niliyopungukiwa kwenu. 18 Maana wameniburudisha roho yangu, na roho zenu pia; basi wajueni sana watu kama hao.**

**16:15 "nawasihi"** Aya hii ni sawa na 1 Kor. 16:16. Paulo ameingiza wazo la kipekee kuhusiana na nyumba ya Stephana.

◙**"ndugu"** Toleo la NRSV limetumia maneno "kaka na dada," ambayo ni kusudio la Paulo kulihutubia kanisa lote. Paulo analitumia neno hili katika nyaraka zake kulitambulisha jambo jipya au mwendelezo wa uwasilishaji wake.

◙ **"nyumbani mwa Stefana"** Wale wa kwanza kubadilishwa (yaani, matunda ya mwanzo) walikuwa viongozi dhahiri katika kanisa la mahali. Paulo anawataja waamini wa awali katika Matendo 17:34.

Hii dhana ya "nyumbani" ni ile ya kuwabadilisha wote kwa wakati mmoja wakati yule aliye kama kichwa cha familia anapobadilika (kama vile Kornelio, Matendo 11:14-17; Lidia, Matendo 16:14-15; Mfilipi mfungwa, Matendo 16:31-33) mara nyingi ni vigumu kwa wainjilisti wenye kumsistiza mtu abadili dini yeye peke yake. Bado desturi ni muhimu katika kuelewa haijalishi imani ya familia hutenda kazi kwa namna gani, bali pia imani ya kimbari. Mungu hana mipaka wala hakandamizwi sana na nadharia mpya ya ubinafsi ya magharibi! Hili linaumiza sana kwa fikra zetu zilizo finyu na kulingana na mfumo wetu wa imani.

Hii dhana ya "nyumbani" kubadili inatumiwa na madhehebu kwa wale wabatizwa wachanga. Taratibu za tohara za Israeli mara nyingi zinanukuliwa kama zenye kuunganisha umri wa mtoto mwenye miaka minane katika familia ya Israeli. Bila shaka kibiblia mwanzo lazima utazamwe kutoka mwisho. Imani ya kweli hukua, hutubu, huamini, hutii, na ustahimilivu. Imani ya kweli huonaoneka kwa matunda yake, si utaratibu wake pekee (kama vile 1 Kor. 16:16b na Yakobo na 1 Yohana).

◙ **"wamejitia katika kazi ya kuwahudumu"** Hiki ni kifungu kinachotia hamasa sana. Hili neno "kujitia" ni *tassō*, ambalo mara nyingi linamaanisha "kuchagua." Imani, imani ya kweli, huliona kusudi katika huduma! Ili kuyaelewa mahitaji ya injili ni kuwa na shauku ya kujitoa sisi wenyewe katika huduma kwa ajili ya wengine kama vile Yesu alivyojitoa mwenyewe kwa ajili yetu (kama vile 1 Yohana 3:16). Huu ni ukuaji wa kawaida wa imani, si uchaguzi. Kama vile yale makundi ya matengano (yaani, wasomi wa ki-Korintho) walivyokuwa wakiyafuata manufaa ya vyeo vyao binafsi, mwongozo wao binafsi, imani ya kweli hufuata upendo (kama vile 1 Kor. 14:4; 16:14). Waamini wameokolewa na kukarimiwa kwa Agizo Kuu (kama vile Mt. 28:19-20; Luka 24:47; Matendo 1:8) na yale mazuri ya mwili wa Kristo, kanisa (kama vile 1 Kor. 12:7).

Stefana na nyumba yake waliamua kuzitumia mali zao kwa ajili ya ufalme. Ikiwa Stefana alikuwa mmoja wa wale matajiri na wasomi wenye daraja la kijamii aidha matendo yake yalikuwa mfano wa mafundisho ya Paulo. Yeye alikuwa mfano wa wasomi wengine waliokuwa matajiri katika kanisa (kama vile Bruce W. Winter, *After Paul Left Corinth*, kr. 184-205). Angalia Mada Maalum katika 1 Kor. 4:1.

◙ **" kuwahudumu"** Angalia MADA MAALUM: UONGOZI WA MTUMISHI (SPECIAL TOPIC: SERVANT LEADERSHIP katika 1 Kor. 4:1.

◙ **"watakatifu"** Angalia MADA MAALUM: WATAKATIFU (SPECIAL TOPIC: SAINTS) katika 1 Kor. 1:2.

**16:16 "watiini watu kama hawa"** Hii ni KAULI TENDEWA TEGEMEZI YA WAKATI ULIOPO. Neno "Kutii" (*hupotassō*) ni neno la kijeshi lenye kumsistiza mtu katika mfululizo wa amri. Katika waraka wa Paulo neno Wakorintho linatumika kwa

1. roho za manabii kuwatii manabii, 1 Kor. 14:32
2. vitu vyote kumtii Yesu, 1 Kor. 15:27
3. Yesu kumtii Baba, 1 Kor. 15:28
4. waamini kuwatii viongozi wa ki- Mungu, 1 Kor. 16:16

Bila shaka kungekuwa na dhihaka baina ya viongozi "kujitoa wenyewe katika kuhudumu" (kutokana na neno *tassō*) na "waamini kuwa na utii (*hupo* plus *tassō*) kwa viongozi wa ki-Mungu" (kama vile 2 Kor. 9:12-13). Angalia Mada Maalum: Utii katika 2 Kor. 9:13.

Kanisa hili lilikuwa na matatizo katika maeneo ya mwenendo sahihi na heshima kwa viongozi wake wa kweli (kama vile 1 Kor. 16:18; 1 The. 5:12; Ebr. 13:17). Waraka wa Clementi wa Roma, ulioandikwa kwa kanisa hili hili miaka 40 baadaye, unaonyesha kwamba hawa bado wana tatizo lile lile.

**16:17 "Stefana na Fortunato na Akaiko"** Wengine wamedai kuwa haya majina mawili ya mwisho, ambayo kwayo hatusikii cho chote katika Agano Jipya, walikuwa miongoni mwa familia ya Stephana. Baadhi hudai kuwa wote watatu walikuwa watumwa, lakini hili haliwezi kuthibitishwa. Hawa wanaonekana kuuleta waraka kutoka katika kanisa la Korintho kwenda kwa Paulo. Pauo alipokea habari zilizolihusu kanisa kutoka kwa watu wa Kloe. Clementi wa Roma aliwandikia Wakorintho yapata miaka 40 baadaye na kumtaja mzee wa kanisa aitwaye Fortunato.

◙**"wamenikirimia kwa wingi yale niliyopungukiwa kwenu"** Kifungu hiki kina maana hasi katika lugha ya Kiingereza, lakini hakina maana hiyo. Taarifa zao zilimfahamisha Paulo habari kutoka katika kanisa hili ambalo alilipenda, pamoja na matatizo yake yote (kama vile 1 Kor. 16:24). Hawa walitenda kazi kama wawakilishi wa Paulo katika kanisa. Hakika kile walichokifanya kwa Paulo, hatimaye kilimpa furaha (kama vile 1 Kor. 16:18) uwepo wao, si haba.

**16:18 "roho yangu, na roho zenu"** Hili liko wazi kutokana na muktadha anaoutumia Paulo kwa neno "roho" kama njia ya kujirejelea yeye mwenyewe (kama vile 1 Kor. 2:11; 5:4; 2 Kor. 2:13; 7:13; Rum. 1:9; 8:16; Fil. 4:23).

**NASB, NKJV " wajueni sana watu kama hao"**
**NRSV "hivyo toa ushirikiano kwa watu kama hao"**

**TEV "watu kama hawa wanatazamia faida"**
**NJB "yawapasa kuwakubali watu kama hawa"**

Hii ni KAULI TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO ya neno "*ginōskō*" katika maana ya kukiri (kama vile 2 Kor. 3:2) au kujua ili kukubali (kama viile 1 Kor. 8:3).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : 1 WAKORINTHO 16:19-20**
**19 Makanisa ya Asia wawasalimu. Akila na Priska wawasalimu sana katika Bwana, pamoja na kanisa lililoko**
**ndani ya nyumba yao. 20 Ndugu wote wawasalimu. Salimianeni kwa busu takatifu.**

**16:19 "Makanisa ya Asia"** Aya hii inarejelea juu ya karne ya kwanza ya utawala wa Kirumi wa magharibi wa moja ya tatu ya nchi ya sasa Uturuki.

◙ **"Akila na Priska"** Akila alikuwa mtengeneza mahema (au mtengeneza ngozi), kama Paulo. Wayahudi wote, hata walimu wa sheria za Kiyahudi, hawa walifundishwa elimu ya biashara ili kwamba wasichukue fedha wakati wa mafundisho yao. Mke wa Akila, Prisila au Priska, wameorodheshwa mara nne za mwanzo kati ya zile sita ambazo wametajwa (kama vile Matendo 18:2,18,26; Rum. 16:3; 1 Kor. 16:19; 2 Tim. 4:19). Wengi wametoa hoja kuwa jina la huyu mwanamke ni la kifalme (*gens Prisca*). Tangu lilipotajwa hapo awali, limechunguzwa sana na watu wa Kiyahudi, wengi wameiona simulizi kuu na yenye upendo ndani yake ya mwamamke wa Kirumi aliye tajiri wa Kirumi na Myahudi mwenye kutengeneza mahema!
Lile toleo lenye Maandiko ya Kale lina jina Prisila, ambapo jina lake liko katika Matendo 18:2,18,26. Pia hili limeonekana katika Rum. 16:3 na hapa. Hili linafuata machapisho ya Kiyunani A, C, D, F, G, K, L, zile tafsiri za Kisiria, na baadaye yale machapisho yenye jinsia ya kiume. Hata hivyo, Paulo anamuita Priska, jina ambalo linapatikana katika machapisho P[46], א, B, M, na zile tafsiri za lile Toleo la Kiyunani na and Coptic. Angalia Bruce Metzger, *A Textual Commentary on the Greek New Testament*, uk. 570.

◙ **"kanisa lililoko ndani ya nyumba yao"** Kanisa la kale halikuwa na majengo. Watu walikutana majumbani. Hii ilikuwa ni kwa sababu ya

1. uhaba wa fedha
2. uhitaji wa kuwepo siri, kwa kuwa Ukristo ulikuwa kama dini haramu katika utawala wa Kirumi kwa wakati ule.
3. uhutaji wa mwonekano wa haki tangu makanisa yale ya kwanza yaliyokusanyika kama jamii ya jumuiya ya Kirumi

Dhana ya kanisa la nyumbani inaanza katika Matendo 2:46; 5:4. Hii inaendelezwa na kukuzwa katika Warumi 16:5,23, Kol. 4:15; Filemoni 2.

◙ **"Ndugu wote wawasalimu"** Kwa uwazi aya hii inarejelea juu ya kanisa zima, si kanisa zima tu.

**16:20 "Salimianeni kwa busu takatifu"** Huu ni muundo wa salamu za umati (kulibusu shavu moja la mtu au yote mawili) na ile ishara ya ushirika inaweza kuonekana katika Agano la Kale ndani ya kitabu cha Kut. 4:27. Hili pia linaweza kuonekana katika Injili katika Marko14:45. Hili lilikuja kutambulishwa katika kanisa la mwanzo (kama vile Rum.16:16; 2 Kor. 13:12; 1 The. 5:26; 1 Pet. 5:14), ambalo liliufuata ule utaratibu wa Sinagogi. Wanaume waliwabusu wanaume na wanawake waliwabusu wanawake. Hili lilikuja kutumiwa vibaya na baadhi ya Wakristo na kutoeleweka kwa wale ambao hawakuwa waamini na kukomeshwa na lile kanisa la kwanza. Hata hivyo, hili bado linaendelea katika matukio maalum katika makanisa ya magharibi. Usawa wake wa magharibi ungeweza kuwa kushikana mikono au kukumbatiana.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : 1 WAKORINTHO 16:21-24**
**21 Hii ni salamu yangu Paulo kwa mkono wangu mwenyewe. 22 Mtu awaye yote asiyempenda Bwana, na**

**awe amelaaniwa. Maranatha. [23] Neema ya Bwana Yesu na iwe pamoja nanyi. [24] Pendo langu na liwe pamoja nanyi nyote katika Kristo Yesu.**

**16:21 "Hii ni salamu yangu Paulo kwa mkono wangu mwenyewe"** Hili lilikuwa zoezi la kawaida la Paulo la baada ya yeye kutoa ufafanuzi wa nyaraka zake. Hii ilikuwa ni njia ya kuhakikisha ule uhalisia wake (kama vile Gal. 6:11; 2 The. 2:2; 3:17; Kol. 4:18; Filemoni 19).

**16:22 "asiye"** Hii ni SENTENSI YENYE MASHARTI DALAJA LA TATU. Inaonekana kuwa katika kanisa la Korintho wengine hawakumpenda Bwana!

◙ **"asiyempenda "** Hili ni neno la Kiyunani "*phileō.*" Paulo hakulitumia neno hili mara nyingi kueleza juu ya upendo (kama vile Tito 3:15). Kwa sababu ya hili, inaweza kudhaniwa kuwa yeye ananukuu wimbo wa kumsifu Mungu au kanuni za ibada. Huu sawa na mzizi wa neno "kubusu" (*philēma*). "*Phileō*" ni lugha ya Kiyunani ya mawasiliano kwa sababu lina maana nyingine ya "*agapaō*" kama vile Yohana 5:20; 16:27), lakini kwa wakati mwingine bado kunaweza kuwako utofauti wa kimuktadha (kama vile Yohana 21:15-17).

◙ **"amelaaniwa"** "*Anathema"* ni neno la Kiyunani ambalo linaaksi neno la Kiebrania "*herem*" au kile kilichotolewa kwa Mungu, ambacho kimekuwa kitakatifu na lazima kiharibiwe (mf. Yeriko katika Yos. 6:17-19). Hili limekuja kutumika katika maana ya laana takatifu (kama vile Matendo 22:12,14; Rum. 9:31; 1 Kor. 12:3; 16:22; Gal. 1:8-9). Usemi huu wenye nguvu unaweza kuaksi ule uwepo wa walimu wa uongo huko Korintho (kama vile 1 Kor. 12:3). Inawezekana kwamba hili linaaksi zile desturi za sasa katika Korintho. Tazama nukuu kuhusiana neno hili katika 1 Kor. 12:3.

◙ **"Maranatha"** Yesu na wale mitume wa kwanza walikuwa wakizungumza lugha ya Kiaramu (si Kiebrania). Hii ilikuja kuwa lugha ya kawaida tokea kipindi cha Dola ya Kiajemi. Kuna maneno kadhaa ya Kiaramu/vifungu katika Agano Jipya.

1. *talitha kum* – Marko 5:41
2. *ephphatha* - Marko 7:34
3. *abba* - Marko 14:36; Rum. 8:15
4. *maranatha* - 1 Kor. 16:22.

Angalia Mada hapo chini.

## MADA MAALUM: *MARANATHA* (SPECIAL TOPIC: *MARANATHA*)

**16:23 "Neema ya Bwana Yesu"** Hatua ya kwanza katika kuifasiri Biblia ni kuimarisha yale maneno halisi. Chanzo kinachosaidia kwa huu Umoja wa Vyama vya Biblia *A Textual Commentary on the Greek New Testament*, na Bruce M. Metzger. Kuonyesha namna inavyosaidia inaweza kunipa mwangaza wa kunukuu kifungu hiki katika mstari huu.

"Ule Upokeaji wa Maandiko, ulifuatiwa na א$^{c}$ A C D F G K L M zilizo nyingi ziliandikwa kwa herufi ndogo, ikiwemo 6 424$^{c}$ 920 1739, it$^{d,g,r}$ syr$^{p,h}$ cop$^{8a,bo}$ arm eth, inasoma Ἰησοῦ Χρισκοῦ. Kwa usomaji ulio mfupi Ἰησοῦ, ambayo inasaidiwa na א$^{*}$ B 2 33 35 226 356 442 823 1611 1908 2002 vg goth *al,* ni ya kuzingatiwa. Katika hoja ya kuwepo kwa usomaji mrefu katika fadhila zingine za Pauline (Ro 16.24; 2 Kor 13.13; Ga 6.18; Flp. 4.23; I Th 5.28; 2 Th 3.18; Phm 25), pamoja na uelekeo wa waandishi kwa ajili ya kukuza jina lililotakaswa, huenda hii ikaeleweka kwamba ushahidi wo wote lazima uwe umedhbitiwa na nguvu kama hii" (uk. 570).

**16:24 "Pendo langu na liwe pamoja nanyi nyote"** Hii ni moja ya semi haba za Paulo kuhusu pendo binafsi. Tazama pendo lililoelezwa na kuwapenda wote ambao wamekuwa wakijitenga sana na kuwa chukizo ndani ya kanisa.

◙ **"Amina"** Angalia nukuu katika 1 Kor. 14:16.

## MASWALI YA MJADALA

Haya ni maoni kuhusu mwongozo wa kusoma, ambao una maana kuwa, unawajibika kwa tafsiri yako binafsi ya Biblia. Kila moja wetu sharti atembee katika nuru tulionao. Wewe, Biblia na Roho Mtakatifu ni kipaumbele katika tafasiri. Usiachie kazi hii kwa mtoa maoni.

Maswali haya ya kujadili yanatolewa kukusaidia mambo muhimu ya kipengele cha kitabu hiki. Yamekusudiwa kukuchokonoa mawazo na sio ya mwisho.

1. Orodhesha maswali ambayo Kanisa la huko Korintho yaliandika kwa Paulo.
2. Ni vyanzo gani tofauti tofauti vya habari za Paulo kuhusu amri ya sasa katika Kanisa la Korintho?
3. Orodhesha mwongozo wa utoaji katika Agano Jipya.
4. Kwa nini Paulo alikuwa na shauku ya kulichangia Kansa la Yerusalemu?
5. Kwanini Paulo aliendelea kuzishikilia sikukuu za Kiyahudi baada ya kuokolewa?
6. Ni kwa namna gani 16:15 inasuluishwa na Matendo 17:34?
7. Akila na Priska walikuwa akina nani?
8. Kwa nini Paulo anatumia kifungu cha Kiarama katika waraka kwa kanisa la Kiyunani?

# UTANGULIZI WA 2 WAKORINTHO

## MAELEZO YA UFUNGUZI

A. Kitabu hiki , zaidi ya barua zote za Paulo kinatuonesha moyo na mawazo ya Mtume kwa Mataifa. Kiko karibu sana na sisi kuliko vitabu vingine vinavyozungumzia maisha yake mwenyewe ya kiroho na kichungaji.

B. Kitabu hiki kinaweza kuwa kazi kuu iliyomalizwa yenye hotuba za Paulo. Raymond E. Brown, *An Introduction to the New Testament*, anasema "inawezekana ikawa kazi kuu zaidi yenye hotuba za Paulo za ushawishi katika maandiko yake yote" ukurasa wa 541. Hata hivyo, hii ilifanyika kuwapinga wapotoshaji waliokuja Korintho na kushambulia mbinu za Paulo za hotuba pamoja na injili yake (kama vile alivyoshambuliwa juu ya hekima yake katika 1 Wakorintho 1-4).

**MADA MAALUMU: WAPOTOSHAJI (SPECIAL TOPIC: SOPHISTS)**

C. Kitabu hiki kina muunganiko wa ajabu, kama Paulo mwenyewe, ya kupanda na kushuka kiroho, ya hisia zinazotiririka kwa uhuru kuanzia hasira na furaha kubwa.

D. Kitabu hiki kiukweli ni barua na kama ni barua kwa hiyo kina sehemu moja nusu ya mazungumzo. Wingi wa hisia/sababu/hukumu za mwanzo na mazingira yaliyosukuma mwitikio wa Paulo yamepotea. Huu ni mfano mzuri wa kweli kwamba nyaraka za Agano Jipya kwa asili ziliandikwa kama ujumbe wa kujibu mahitaji fulani, na sio tafiti huru za kithiolojia.

E. Kitabu hili kimekuwa kikiwekwa kando na wanataaluma na katika mahubiri. Kuna maandiko ya fasiri machache kuhusu 2 Wakorintho kuliko vitabu vingine vyote katika Agano Jipya. Hii ni bahati mbaya kwasababu kitabu hiki ni chanzo cha majadiliano mengi yenye maana ya Paulo kuhusu mateso katika maisha ya Mkristo.

F. Kwa Wachungaji,kitabu hiki kinatoa mwongozo wa ufahamu juu ya namna ya kushughulikia matatizo ya ndani ya makanisa ya nyumbani. Paulo anatupatia sisi sote mfano wa kuigwa katikati ya mashambulizi binafsi na hali ya kutoelewana.

## MWANDISHI

A. Hata katikati ya kukataliwa kote kunakofanywa na wanataaluma wa kisasa kwa waandishi wa kale walioandika vitabu vya biblia, kitabu hiki hakijawahi kukataliwa kuwa hakikuandikwa na Paulo.

B. Kimekuwa kinazungumzia maisha ya mtu mwenyewe binafsi sana na ngumu sana kuelewa baadhi ya vifungu vya maneno kiasi kwamba uwezekano wa mtu mwingine kujaribu kumuigilizia Paulo kwa kuandika kitabu hiki haupo kabisa. Ugumu na uelekeo wa barua unazungumza juu ya upekee wake. Ni kweli kwamba wasomi wengi wa Agano Jipya wanafikiri kwamba 2 Wakorintho ni barua ya muunganiko inayounganisha barua kadhaa za Paulo na kuzifanya iwe moja. Nakubaliana na umoja wake kwasababu

   1. Hakuna dokezo la kutokuwa na umoja katika nyaraka za kale za Kiyunani
      a. Hakuna kutofautiana katika vipengele vya uandishi
      b. Hakuna nyaraka ambayo haijumuishi sura zote kumi na tatu.
   2. Japokuwa 2 Wakorintho 13 ilikuwa haijulikani kwa Clement wa Rumi katika 96 Baada ya Kristo, inanukuliwa na Polycarp katika mwaka 105 Baada ya Kristo
   3. Kitabu kinaeleweka kama kipengele. Inaonekana kuwepo kwa mada fulani zinazoonyesha umoja wake kama vile "mateso."
   4. Ushahidi wa ndani haujitoshelezi kulinda uchambuzi wa ndani wa 2 Wakorintho.

C. Paulo anatajwa kuwa ndiye mwandishi katika 2 Wakorintho 1:1 na 10:1

## TAREHE

A. Tarehe ya 2 Wakorintho inaunganishwa bila kutenganishwa na 1 Wakorintho na kitabu cha Matendo ya Mitume.
B. Matendo ya Mitume 18:1-18 and 20:2-3 yanahusianisha kuwepo kwa Paulo katika Korintho, lakini inaonekana kuwepo angalau kwa safari ambayo haikuwekwa katika kumbukumbu 2 Wakorintho 2:1; na safari yake ya tatu inayotajwa katika 2 Wakorintho 12:14; 13:1-2).
C. Swali kubwa ni uhusiano wa muda kati ya safari za kuwatembelea za Paulo na barua zake kwa Korintho.
D. Tatizo kubwa kuhusu kuweka tarehe kwa matukio yanayohusiana na Korintho ni kwamba hatuna ushahidi wa nje au taarifa kati ya Matendo ya Mitume 18:1-18 na Matendo ya Mitume 20:2-3,isipokuwa utata wa ushahidi wa ndani wa barua za Wakorintho zenyewe.
E. Paulo anatofautiana na kanisa la Wakorintho-mapendekezo ya kutengeneza upya

| **TAREHE** | **SAFARI** | **WARAKA** |
|---|---|---|
| 50-52 B.K safari ya pili ya Paulo | a. katika safari ya pili ya Paulo alikaa Miezi 18 (k.v Mdo. 18:1-11) | |
| 52 B.K Gallio alikuwa Gavana wa Rumi mwaka 51 B.K (k.v Mdo.18: 12-17) | | a. 1 Kor. 5:9-11 inaonekana kurejea kwenye waraka kuhusu hali isiyo ya kiadilifu katika kanisa. Waraka Huo haujulikani isipokuwa<br>(1) Baadhi wanadai kuwa 2 Kor. 6:14-7:1 ni moja ya sehemu yake au<br>(2) Kuwa 2 Kor. 2:3,4,9 ni nyaraka za wakati uliopita usiotimilifu na unarejerea kwenye 2 Korinto |
| Mwaka wa 56 B.K (majira ya kuchipua) | b. Paulo anayosikia kuhusu matatizo ndani ya kanisa wakati akiwa Efeso toka kwa vyanzo viwili<br>(1) Watu wa Chloe,1 Kor. 1:11 na<br>(2) Stephano, Fortunatus, na Achaicus 1 Kor. 16:17. Inaonekana kuwa walileta Waraka toka makanisa ya Korinto ukiwa Na maswali | |
| Mwaka wa 56 B.K (majira ya baridi) au Mwaka wa 57 B.K (majira ya baridi) | | b. Paulo anajibu maswali haya (k.v 1 Kor. 7:1,25; 8:1; 12:1; 16:1,2) kwa kuandika 1 Wakorinto, Timotheo (k.v 1 Kor. 4:17) anawajibika toka kwa Waefeso kwenda kwa wakorinto. Timotheo hakuweza kuleta Suluhu ya matatizo ndani ya Kanisa |
| | c. Paulo anafanya safari ya dharura yenye maumivu huko Korinto (haikuwekwa kumbu kumbu katika matendo, k.v 2 Kor. 2:1). Haikuwa na mafanikio lakini aliapa kurudi | |
| | | c.Paulo anaandika waraka mchungu (k.v 2 Kor. 2:3-4:9; 7:8-12) kwa |

Makanisa ya Korinto uliopokelewa Na Tito (k.v 2 Kor. 2:3; 7:13-15). Waraka huu haujulikani isipokuwa baadhi wanadhani moja ya sehemu yake ipo katika 2 Kor. 10-13

d.Paulo anapanga kumwona Tito huko Troa, lakini Tito hakuonekana, kwa hiyo Paulo akaamua kwenda Makedonia (k.v 2 Kor. 2:13; 7:5,13), yumkini Filipo(k.v Mss $B^c$,L,P)

d.Alimpata Tito na kusikia kuwa kanisa limeitikia kwenye uongozi wake na tena akaandika 2Korinto katika shukrani kubwa(k.v 7:11-16) ukapokelewa na Tito.

Mwaka 57-58 B.K (majira ya baridi)

e. Safari ya mwisho ya Paulo kwenda Korinto iliyoandikwa inaonekana kurejerewa Kwenye Mdo. 20:2-3. Ingawa haitaji Jina la Korinto, kama ilivyofikiliwa aliamua Kubaki huko kipindi cha majira ya baridi

e. Hali ya alama inayobadilika kati ya sura ya 1-9 na 10-13 imeelezewa na wasomi kama taarifa mbaya (yumkini ufufuaji wa upinzani wa Kale na kuongeza upinzani mpya) Kutoka kwa makanisa ya Korinto Baada ya sura ya 1-9 kuwa Imeandikwa.

## BARUA NGAPI AMBAZO PAULO ALIWAANDIKIA WAKORINTHO

A. Ni mbili tu, 1 na 2 Wakorintho
B. Tatu, pamoja na barua moja iliyopotea
C. Nne, pamoja na barua 2 zilizopotea
D. Baadhi ya wanataaluma wa kisasa wamepata barua zilizopotea katika 2 Wakorintho
   1. Barua ya kabla (1 Wakorintho 5:9) katika 2 Wakorintho 6:14-7:1
   2. Barua kali (2 Wakorintho 2:3-4,9; 7:8-12) katika 2 Wakorintho 10-13
E. Tano, pamoja na 2 Wakorintho 10-13 kuwa barua ya tano,iliyotumwa baada ya ripoti ya Tito kuhusiana na habari mbaya
F. Nashikilia C (angalia pia H. C. Thiessen, *Introduction to the New Testament*, ukurasa wa 209)
   1. Barua ya kabla-ilipotea ( 1 Wakorintho 5:9)
   2. 1 Wakorintho
   3. Barua kali-ilipotea (2 Wakorintho 2:1-11, 7:8-12)
   4. 2 Wakorintho

## MAADUI WA PAULO WALIOKUWA KORINTHO

A. Katika 2 Wakorintho matatizo yanaonekana kuwa na makundi kadhaa yanayomiliki makanisa mbalimbali ya nyumbani (sio kuwa lazima ni yale yale ya 1 Wakorintho, lakini inawezekana).
   1. Kundi la waaminio wanaounga mkono mila na desturi za Kirumi
   2. Kundi la waaminio wanaounga mkono mafunzo hotuba ya kigiriki
   3. Kundi la waaminio wanaounga mkono mila na desturi za Kiyahudi

    4. Kundi la waaminio kutoka katika jamii ya wanyonge waliosahaulika

B. Kuwasili kwa wafanya fujo wa Kiyahudi kutoka Palestina kulisababisha mtafaruku wa ziada(rejea 2 Wakorintho 10-13). Wao ni tofauti wakitokea kwa wana wa Yuda wa Galatia na wanasheria wa Kigiriki na Kiyahudi wa Wakolosai. Yawezekana walikuwa na mafunzo ya kunena na utoaji wa hotuba, walimu wenye ushawishi sawa na wakina Apolo.

C. Hapa ni baadhi ya madai yaliyotolewa dhidi ya Paulo ambayo aliyajibu
    1. Paulo alikuwa ni kigeugeu (kama vile mipango yake ya safari ilibadilika, 2 Wakorintho 1:15).
    2. Paulo alikuwa ni mwandishi mzuri lakini dhaifu katika hotuba zake(rejea 2 Wakorintho 10:10).
    3. Paulo hakuwa mnenaji mzuri (rejea 2 Wakorintho 10:10; 11:6).
    4. Paulo hakuwa anapokea fedha (rejea 2 Wakorintho 11:7; 12:13).
    5. Paulo hakuwa Mtume wa kweli (rejea 2 Wakorintho 11:5, 13; 12:4).
    6. Paulo hakuwa Myahudi halisia (rejea 2 wakorintho 11:21)
    7. Paulo hakuwa na ufunuo wa moja kwa moja na maono ya kiroho kama ambavyo wao walikuwa nayo (rejea 2 Wakorintho 12:1).

## MAZINGIRA NA KUSUDI LA II WAKORINTHO

A. Shukurani kwa mwitikio chanya wa kanisa kuupokea uongozi wa Paulo (rejea 2 Wakorintho 2:12,13; 7:11-16)
B. Maandalizi ya safari ya tatu ya Paulo(rejea (10:1-11). Safari yake ya pili ilikuwa ya maumivu na bila mafanikio. Mabadiliko ya hisia katika sauti kwa sura ya 10-13 ni wazi. Wengine wanatoa maelezo kuwa ni matokeo ya barua kadhaa za Paulo kwenda kanisa la Korintho kuunganishwa katika 2 Wakorintho. Pia inawezekana kwamba Paulo aliandika barua hizi baada ya kusikia kuhusu mfumuko wa upinzani mpya ndani ya ushirika wa Wakorintho. Ni hisia zilizochochewa.
C. Kuwapinga walimu wa Kiyahudi wa uongo (rejea 2 Wakorintho 10-12) ambao walimkataa Paulo;
    1. Mtu
    2. Sababu
    3. Mamlaka
    4. Namna yake ya uwasilishaji
    5. Jumbe zake za injili

## VIPENGELE VYA FASIHI VINAVYOWEZA KUAINISHWA

A. Kuainisha kitabu hiki ni kazi ngumu sana kwasababu ya
    1. Kubadilika kwake kihisia
    2. Aina nyingi za mada zinazotofautiana
    3. Maelezo mengi ya kimalezi ya mzazi (2 Wakorintho 2:14-7:1 au 7:4)
    4. Ufahamu wetu finyu wa mazingira ya kienyeji
B. Hata hivyo, kuna migawanyo mitatu mikubwa ya mada:
    1. Paulo anajibu ujumbe wa Tito na anahusianisha mipango yake ya kusafiri, sura 1-7 (kuna maelezo makubwa yanayoshughulikia huduma ya kitume ya Paulo, 2 Wakorintho 2:14-7:1 au 7:4)
    2. Kutiwa moyo kwa Paulo kwa ajili ya kumaliza mchango wake kwa kanisa la Yerusalemu, sura ya 8-9
    3. Paulo anavyojitetea na kujilinda juu ya uongozi wake,sura 10-13

## MZUNGUKO WA KWANZA WA USOMAJI

Huu ni mwongozo wa kujisomea wa fasiri wenye maana kuwa unawajibika kwa tafsiri zako za Biblia mwenyewe. Kila mmoja wetu lazima atembee katika nuru tuliyopewa. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hupaswi kumuachia kazi hii mfasiri.

Soma kitabu chote cha Biblia kwa mara moja. Eleza dhamira kuu ya kitabu kizima kwa maneno yako mwenyewe.

1. Dhamira kuu ya kitabu kizima

2. Aina ya fasihi (aina ya fasihi aliyotumia katika kuwasilisha ujumbe wake).

**MZUNGUKO WA PILI WA USOMAJI** (kutoka **"Mwongozo wa Usomaji Mzuri wa Biblia ("A Guide to Good Bible Reading")**

Huu ni mwongozo kujisomea wa fasiri wenye maana kuwa unawajibika kwa tafsiri zako za Biblia mwenyewe. Kila mmoja wetu lazima atembee katika nuru tuliyopewa. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hupaswi kumuachia kazi hii mfasiri.

Soma kitabu kizima cha Biblia kwa mara ya pili kwa mara moja. Ainisha somo kuu na zielezee mada kwa sentensi moja.

1. Somo la kipengele cha kwanza cha fasihi
2. Somo la kipengele ya pili cha fasihi
3. Somo la kipengele cha tatu cha fasihi
4. Somo la kipengele cha nne cha fasihi
5. Na mengineyo.

# 2 WAKORINTHO 1

| MGAWANYO WA AYA WA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **UBS4** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB** |
| Salamu | Salamu | Salamu na Shukrani | Salamu | Utambulisho na Salamu |
| 1:1-2 | 1:1-2 | 1:1a | 1:1a | 1:1-2 |
| | | 1:1b | 1:1b | |
| | | 1:2 | 1:2 | |
| Shukrani ya Paulo Baada ya Maumivu | Faraja ndani ya mateso | | Paulo anatoa Shukrani kwa Mungu | Kutoa Shukrani |
| 1:3-7 | 1 :3 -7 | 1:3-7 | 1:3-7 | 1:3-7 |
| | Kukombolewa Kutoka kwenye Mateso | | | |
| 1:8-11 | 1:8-11 | 1:8-11 | 1:8-11 | 1:8-11 |
| Kuahirishwa kwa Safari ya Paulo | Uaminifu wa Paulo | Uhusiano wa Karibuni na kanisa | Mabadiliko ya mipango ya Paulo | Kwanini Paulo alibadili Mipango yake |
| | | (1:12-2:13) | (1:12-2:4) | (1:12-2:11) |
| 1:12-14 | 1:12-14 | 1:12-14 | 1:12-14 | 1:12-14 |
| | Kulihurumia Kanisa | | | |
| 1:15-22 | 1:15-24 | 1:15-22 | 1:15-22 | 1:15-22 |
| 1:23-2:4 | | 1:23-24 | 1:23-2:4 | 1:23-2:4 |

* Ingawa hazijavuviwa, migawanyo ya aya ndiyo ufunguo wa kuelewa na kufuata kusudio la awali la mwandishi. Kila tafsiri ya kisasa imegawanya na kufanya muhtasari wa aya. Kila aya ina mada kuu, kweli, au wazo. Kila toleo hufupisha mada hiyo kwa namna yake ya pekee. Unaposoma andiko, jiulize ni tafsiri gani inashabihiana na uelewa wako wa mada na mgawanyo wa aya. Katika kila sura lazima tusome Biblia kwanza na kujaribu kutambua somo (aya), kisha tulinganishe uelewa wetu na matoleo ya kisasa. Ni pale tu tunapoelewa kusudio la asili la mwandishi kwa kufuata mantiki yake na uwasilishaji wake, ndipo tunapoweza kuielewa Biblia kiukweli. Ni mwandishi wa asili tu aliyevuviwa—wasomaji hawana haki ya kubadili au kurekebisha ujumbe. Wasomaji wa biblia wana wajibu wa kutumia kweli iliyovuviwa kwenye siku na maisha yao. Fahamu kwamba maneno yote ya kiufundi na vifupisho vimefafanuliwa kikamilifu kwenye nyaraka zifuatazo: Maelezo Fasaha ya Muundo wa Sarufi za Kiyunani (Brief Definitions of Greek Grammatical Structure), Uhakiki wa Tofauti za Kiuandishi (Textual Criticism) na Ufafanuzi (Grossary).

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (kutoka "**Mwongozo wa Usomaji Mzuri wa Biblia"("A Guide to Good Bible Reading")**

### *KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo wa usomaji wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako binafsi ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika nuru tuliyonayo. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hupaswi kumwachia kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo. Linganisha mgawanyo wa masomo yako na tafsiri tano hapo juu. Kugawanya katika aya hakuna uvuvio, isipokuwa ni ufunguo wa kufuatilia kusudio la asili la mwandishi ambalo ndilo kiini cha ukalimani. Kila aya ina somo moja na ni moja tu.

32. Aya ya kwanza
33. Aya ya pili
34. Aya tatu
35. N.k

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA

A. 2 Wakorintho iliandikwa karibu miezi sita hadi kumi na minane baada ya 1 Wakorintho, kufuatia ujio wa Paulo Makedonia akiwa na Tito, aliyotoa taarifa mwitikio wa kanisa kwa mazungumzo ya awali (kama vile 2 Kor. 2:12-13; 7:11-16).
B. Hii ni barua ya Mtu binafsi kali sana. Hali ya msukumo ya Paulo inatambulika katika sarufi (yaani, sentensi kutokuwa na muungano na kutokuwa na muungano na kutokukamilika).
C. Paulo alikuwa ameshambuliwa kwa uovu na wachache miongoni mwa kanisa. Kikundi cha wachache hawa chaonekana kutoka ndani ya kundi la kanisa la Korintho pamoja na kundi la Wayahudi wanaozunguka zunguka mashitaka yao yalikuwa:
    1. Paulo alikuwa na nia chafu, 2 Kor. 1:12
    2. Paulo alikuwa hana msimamo, 2 Kor. 1:15 na kuendelea
    3. Paulo alikuwa dhaifu, 2 Kor. 10:10
    4. Paulo alikuwa mbaya kimaumbile, 2 Kor. 10:10
    5. Paulo hakuwa msemaji mzuri, 2 Kor. 10:10; 11:16
    6. Paulo alihubiri ili kupata fedha 2 Kor. 11:7 na kuendelea; 12:13 na kuendelea
    7. Paulo hakuwa mtume wa kweli, 2 Kor. 11:5,13; 12:4
    8. Paulo hakuwa Myahudi halisi, 2 Kor. 11:21 na kuendelea
    9. Walikuwa na Ufunuo wa Moja kwa Moja lakini Paulo hakuwa nao, 2 Kor. 12:1na kuendelea.

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 2 WAKORINTHO 1:1a**
**[1a] Paulo, mtume wa Kristo Yesu kwa mapenzi ya Mungu,**

**1:1a "Paulo"** Sauli wa Tarso anaitwa Paulo kwa mara ya kwanza katika Matendo 13:9. Yaelekea kwamba wengi miongoni mwa Wayahudi walio uhamishoni "diaspora" walikuwa na jina la kiebrania na jina la Kiyunani. Kama ndivyo basi wazazi wa Paulo walimpa jina hili lakini kwa nini Katika Matendo 13? Yawezekana (1) wengine walianza kumwita kwa jina hili ama (2) mwenyewe alianza kujitambulisha kwa neno "mdogo" au "mdogo kuliko wote." Jina la Kiyunani *Paulos* lilimaanisha "mdogo." Nadharia mbalimbali zimewekwa mbele kuhusu chanzo cha jina hili la Kiyunani.

1. Maumbile yake kimwili, desturi za karne ya pili kwamba Paulo alikuwa mfupi, mnene, mwenye upaa, mwenye matege, na miguu iliyopinda, mwenye nyusi nyingi sana na macho yaliyotokeza ni uwezekano wa chanzo cha jina hili Thessalonika aliyeitwa *Paul and Thekla*
2. Aya ambazo Paulo hujiita "mdogo miongoni mwa watakatifu" kwasababu alilitesa kanisa kama katika Matendo 9:1-2 (kama vile 1 Kor. 15:9; Efe. 3:8; 1 Tim. 1:15). Wengine wameuona huu "udogo" kama chanzo cha cheo cha kujipatia mwenyewe. Hata hivyo, kwenye kitabu kama Wagalatia ambapo anasisitiza kujitegemea kwake na usawa, na wale wa Yerusalemu Thenashara hii kwa sababu ya msingi kwa namna fulani haielekei kuaminika (kama vile 2 Kor. 11:5; 12:11; 15:10).

◙ **"mtume"** Hili ni neno la kawaida kwa neno "tuma" (yaani, *apostellō*). Angalia Mada maalum katika 1 Kor. 4:9. Neno hili lina matumizi kadhaa ya kithiolojia.

1. Walimu wa Kiyahudi Walilitumia kama mtu aliyeitwa na kutumwa kama mwakilishi rasmi wa mwingine,kitu fulani kama "balozi"kwa lugha yetu ya kiingereza (kama vile 2 Kor. 5:20).

2. Injili mara nyingi hutumia neno hili kwa Yesu akiwa ametumwa na Baba (kama vile Mt. 10:40; 15:24; Marko 9:37; Luka 9:48).Katika Yohana neno hilo huchukua mazungumzo ya ki-Masihi (kama vile Yohana 4:34; 5:24,30,36,37,38; 6:29,38,39,40,57; 7:29; 8:42; 10:36; 11:42; 17:3,8,18,21,23,25; 20:21). Inatumika kwa Yesu kuwatuma waaminio (kama vile Yohana 17:18; 20:21).
3. Agano Jipya alilitumia kwa mitume wake.
   a. Wale thenashara wa kwanza waliokuwa kiini cha wanafunzi (kama vile Luka 6:13; Matendo 1:21-22)
   b. Kundi maalum la wasaidizi wa mitume na watenda kazi wenza
      1) Barnaba (kama vile Matendo 14:4,14)
      2) Androniko na Yunia (KJV, Yunia, kama vile Rum. 16:7)
      3) Apolo (kama vile 1 Kor. 4:6-9)
      4) Yakobo, nduguye Yesu (kama vile Gal. 1:19)
      5) Silvanus na Timotheo (kama vile 1 The. 2:6)
      6) Yawezekana Tito (kama vile 2 Kor. 8:23)
      7) Yawezekana Epaphroditus (kama vile Flp. 2:25)
   c. Huduma inayoendelea kanisani (kama vile 1 Kor. 12:28-29; Efe. 4:11)
4. Paulo hutumia nomino hii kama cheo kwake mara nyingi miongoni mwa barua zake kama njia ya kutetea wito wake aaliopewa na Mungu na mamlaka kama mwakilishi wa Kristo (kama vile Rum. 1:1; 1 Kor. 1:1; 2 Kor. 1:1; Gal. 1:1; Efe. 1:1; Kol. 1:1; 1 Tim. 1:1; 2 Tim. 1:1; Tito 1:1).

◙ **"Kristo"** Hili ni neno la Kiyunani lililosawa na neno *Masihi* (angalia mada maalum katika 1 Cor. 1:23), ambalo lilimaanisha “mpakwa mafuta.” Linadokeza “mtu aliyeitwa na kuandaliwa kwa ajili ya shughuli maalum." Katika agano la kale makundi matatu ya viongozi ndio yalitiwa mafuta: makuhani, wafalme na manabii. Yesu alikamilisha yote haya kati ya ofisi tatu zilizotiwa mafuta (kama vile. Heb. 1:2-3).

◙ **"Yesu"** Jina la Kiebrania lilimaanisha "YHWH huokoa" au "YHWH huleta wokovu." Jina hili lilifunuliwa kwa wazazi wake na malaika (kama vile Mt. 1:21). Jina "Yesu"limetokana na neno la Kiebrania Wokovu, *hosea*, lenye kiambishi awali cha jina la Mungu, YHWH. Ni sawa na jina la Kiebrania Yoshua.
Maandiko ya Kiyunani yamegawanyika kufuatana na utaratibu wa maneno haya.
1. Yesu Kristo, A, D, G, K, L (Peshita, KJV, NKJV)
2. Kristo Yesu, P[46], א, B, M, P (NASB, NRSV, TEV, NJB, NIV)

Yaonekana kutokuwepo umuhimu wa kithiolojia kwenye utaratibu. Angalia MADA MAALUM: MAJINA YA UUNGU (SPECIAL TOPIC: NAMES FOR DEITY) katika 1 Kor. 2:8.

◙ **"kwa mapenzi ya Mungu"** Kifungu hiki hiki cha utambulisho kinatumika katika 1 Kor. 1:1; 2 Kor. 1:1; Efe. 1:1; Kol. 1:1 na 2 Tim. 1:1. Paulo alikuwa amehakikishiwa kwamba Mungu alikuwa amemchagua awe mtume. Hii namna mahsusi ya kutambua wito ilianza pale alipoongoka akiwa njiani kuelekea Dameski (kama vile Matendo 9:1-22; 23:3-16; 26:9-18). Paulo mara nyingi alitetea mamlaka yake aliyopewa na Mungu na wito kuthibitisha maandiko yake kama yalitoka kwa Mungu kwa namna isiyo ya kawaida (yaani, yaliyovuviwa, kama vile 2 Tim. 3:16; 1 Kor. 2:9-13; 1 The. 2:13).

◙ **"Timotheo ndugu yetu"** Katika 1 Kor. 1:1 "Sostenes" ametajwa; hapa Timotheo ametamkwa, yawezekana kama mtenda kazi mwenza, mwandishi mwenza, au mnakiri wa maandishi. Pia yawezekana kwamba Paulo alimtaja Timotheo kwa sababu kanisa hili lilikuwa halina mwitikio kwake alipowapelekea barua ya 1 Wakorintho kutoka kwa Paulo.

MADA MAALUM: TIMOTHEO (SPECIAL TOPIC: TIMOTHY)

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 2 WAKORINTHO 1:1b**
**[1b] na Timotheo ndugu yetu; kwa kanisa la Mungu lililoko Korintho,**

**1:1b "kanisa"** Hili ni neno la Kiyunani *ekklesia* (Angalia Mada Maalum katika 1 Kor. 1:2). Linatokana na maneno mawili, "kutoka kwa" na "kuitwa," kwahiyo neno linamaanisha wale walioitwa kwa utaratibu wa Mungu. Kanisa la kwanza walichukua neno hili kutoka matumizi ya kilimwengu (kama vile Matendo 19:32,39,41) na kwa sababu ya matumizi ya ya neno hili kwa "kusanyiko" la Israeli (kama vile Hes. 16:3; 20:4). Walilitumia kwa ajili yao kama mwendelezo wa watu wa Mungu. Wao ndio walikuwa Israeli mpya (kama vile Rum. 2:28-29; Gal. 6:16; 1 Pet. 2:5,9; Ufu. 1:6), utimilifu wa kazi maalum ya Mungu ulimwenguni pote (kama vile Mwa. 3:15; 12:3; Kut. 19:5:6).

◙ **"la Mungu lililoko Korintho"**Kifungu hiki kinafafanua dhana mbili tofauti kuhusu "kanisa."

1. Kanisa la mahali la waamini waliozaliwa mara ya pili na kubatizwa. Sehemu nyingi katika Agano Jipya ambapo neno *ekklesia* limetumika kuaksi dhana hii ya mahali pamoja.
2. Ni utambulisho wa kijumla juu ya mwili wa Kristo. Hili laonekana katika Mt. 16:18 (yaani, matumizi machache ya neno hili la awali lililotumiwa na Yesu, kama vile Mt. 18:17 [mara mbili]); Matendo 9:31 inatumia "kanisa" katika hali ya umoja kwa makusanyiko yote katika Uyahudi, Galilaya, na Samaria; na hatimaye matumizi ya neno hilo katika Waefeso, ambayo ni barua ya kuzunguka kwenye makanisa ya Asia Ndogo (kama vile 2 Kor. 1:22; 3:10,21; 5:23-32).

Kuna mwili mmoja mkubwa wa Kristo uliotokana na waaminio (baadhi wameisha kufa, baadhi wako hai) na kuna vielelezo vya mahali husika vya huo mwili wa ulimwengu wote.

◙ **" pamoja na watakatifu wote walioko katika nchi yote ya Akaya"** Salamu hii yaonyesha kwamba barua ilikuwa kwa ajili ya umati mpana zaidi kuliko kanisa moja (kama vile barua za Paulo zilivokuja zikawa). Ingeweza kutumika kama barua ya kuzungumza jimbo lote la Galatia na Efeso. Hata hivyo, inakabiri matatizo ya Korintho kwa namna ya kipekee.

◙ **"watakatifu"** Hii inamaanisha wametamkwa watakatifu kwa kazi ya Yesu kwa uwakili wa Roho Mtakatifu (kama vile 2 Kor. 6:11). KITENZI (*hagiazō*) linahusiana na neno "takatifu" (*hagios*) na "watakatifu" (yaani, "aliye mtakatifu" *hagioi*). Inazungumzia kuhusu kutengwa kwetu kwenye huduma kwa ajili ya Mungu. Hapa inahusu sehemu yetu ndani yake kama 2 Kor. 1:3 inavyosema, lakini katika mahali pengine katika Agano Jipya waaminio lazima wahangaike kuutafuta "utakatifu." Ni hali ya kumilikiwa. Paulo analihimiza kanisa lenye vikundi vidogo vidogo na lenye majivuno kwa kuwaita, "watakatifu," pamoja na kushindwa kwao na dhambi! Angalia MADA MAALUM: WATAKATIFU (SPECIAL TOPIC: SAINTS) katika 1 Kor. 1:2.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 2 WAKORINTHO 1:2**
**1 Paulo, mtume wa Kristo Yesu kwa mapenzi ya Mungu, na Timotheo ndugu yetu; kwa kanisa la Mungu lililoko Korintho, pamoja na watakatifu wote walioko katika nchi yote ya Akaya. 2 Neema na iwe kwenu na amani, zitokazo kwa Mungu Baba yetu na kwa Bwana Yesu Kristo.**

**1:2 "Neema na iwe kwenu na Amani zitokazo kwa Mungu"** Desturi za uandishi wa barua za Kiyunani ilikuwa ni kuanza na "salam" [cf Matendo 23:26; Yakobo1:1 sio "neema" Paulo alifanya kejeli kwenye neno "*chairein*" kwenda "*charis*," ambao uliifanya neno kuwa ukristo wa kipekee [kama vile 1The 1;1; Gal 1:3. Baadhi wanadai kwamba "amani" linaaksi neno la kiebrania "shalom" [Angalia Mada Maalum katika Kor 1:3, Yawezekana kwamba Paulo huku kuunganisha maneno kutoka kwenye Baraka za ki-haruni za Hesabu 6:24-26. Barua nyingi zaidi za kiyunani za kizazi kile na nyaraka za Agano Jipya zilianza na maombi ya shukrani, lakini kutokana na matatizo kati ya Paulo na kusanyiko lake, sala ya kufungua na kutoa shukrani inaelekezwa kwa Mungu (kama vile2 Kor. 1:3-7).

◙ **"zitokazo kwa Mungu Baba yetu"** Hii inaweka msisitizo kwa uhusiano wa mtu na mtu wa ndani wa kifamilia (kama vile Mt. 6:9). Katika Agano la Kale Mungu ni Baba wa Israeli (kama vile Isa. 64:8; Hos. 1-3;11). Kwa kuwa Mungu yu katika nafsi ya kibinadamu sitiari iliyo bora zaidi kufafanua uhusiano wake na zile nafsi nyingine za utatu

na watu wake uko kwenye utaratibu wa familia ya Kiyahudi, kama vile Baba anavyohusiana na Yesu katika njia ya kulingana. Angalia Mada Maalum: Ubaba wa Mungu katika 1 Kor. 1:3.
"neema" na "amani" pamoja huja kutoka kwa Baba na Mwana. Baba na Yesu wanaunganishwa kisarufi kama kitu cha pamoja (yaani, KIHUSISHI kimoja , lakini VISHAMILISHO viwili). Hii ni njia ya kawaida kwa waandishi wa Agano Jipya kutetea Uungu wa Yesu (kama vile 1 The. 1:1; 3:11; 2 The. 1:2,12; 2:16).

◙ **"na kwa Bwana Yesu Kristo"** Maneno haya ni sehemu ya cheo kamili "Bwana Yesu Kristo" (kama vile 2 Kor. 1:2,3,7,8,9,10). Hivi vyeo vyote vitatu kila kimoja kina umuhimu wake.

1. "Kristo" ni tafsiri ya Kiyunani ya neno la Kiebrania *Messiah* (yaani, aliyepakwa mafuta). Linatetea cheo cha Yesu katika Agano la Kale kama aliyeahidiwa na YHWH akitumwa kuanzisha enzi mpya ya haki.
2. "Yesu" ni jina alilopewa mtoto pale Bethlehemu na malaika (kama vile Mt. 1:21). Linatokana na nomino mbili za Kiebrania: "YHWH," jina la Agano kwa Uungu, na " wokovu" (yaani, *hosea*). Ni jina la Kiebrania lililo sawa na Yoshua. Linapotumika pekee mara nyingi huwa linamtambulisha mwanadamu, Yesu wa Nazarethi, mwana wa Maria ( Mt. 1:16, 25; 2:1; 3:13,15,16).
3. "Bwana" (limetumika katika 2 Kor. 1:1 katika KJV) ndio tafsiri ya neno la Kiebrania *adon*, lililomaanisha "mmiliki, mume, mkuu wa kaya, au bwana." Wayahudi walihofu kutamka jina takatifu YHWH vinginevyo wangelitaja bure na kuvunja mojawapo ya amri kumi. Kila waliposoma maandiko, waliweka *Adon* badala ya YHWH. Hii ndiyo sababu tafsiri zetu za kiingereza hutumia herufi kubwa zote BWANA kwa YHWH katika Agano la Kale. Kwa kuhamisha cheo hiki (*kurios* Kiyunani) kwenda Yesu, waandishi wa Agano Jipya wanatamka Uungu na usawa wake na Baba.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 2 WAKORINTHO 1:3-7**
**3 Na ahimidiwe Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, Baba wa rehema, Mungu wa faraja yote; 4 atufarijiye katika dhiki zetu zote ili nasi tupate kuwafariji wale walio katika dhiki za namna zote, kwa faraja hizo, tunazofarijiwa na Mungu. 5 Kwa kuwa kama vile mateso ya Kristo yanavyozidi kwetu, vivyo hivyo faraja yetu inazidi kwa njia ya Kristo. 6 Lakini ikiwa sisi tu katika dhiki, ni kwa ajili ya faraja yenu na wokovu wenu; au ikiwa twafarijiwa, ni kwa ajili ya faraja yenu; ambayo hutenda kazi yake kwa kustahimili mateso yale yale tuteswayo na sisi. 7 Na tumaini letu kwa ajili yenu ni imara, tukijua ya kuwa kama vile mlivyo washiriki wa yale mateso, vivyo hivyo mmekuwa washiriki wa zile faraja.**

**1:3 "ahimidiwe"**Tunapata neno la kiingereza " kusifu" kutoka kwenye neno hili la Kiyunani. Neno hili (ikifuatilia tafsiri ya maandiko ya kale ya Kiyunani) kila wakati hutumika kwa wanadamu wanapombariki Mungu (kama vile Luka 1:68). Katika Marko 14:61 ni kutaja jina la Mungu kwa kuzunguka zunguka (yaani, "yule aliyebarikiwa"). Paulo anatumia neno hili kwa Baba katika Rum. 1:25; 9:5; 2 Kor. 1:3; 11:31; na Efe. 1:3.

◙ **"Mungu"** Sala hii ya sifa, 2 Kor. 1:3-11, inafafanua Mungu kwa njia tatu.

1. Yeye ni Baba yake Yesu
2. Yeye ni Baba wa rehema zote
3. Yeye ni Mungu wa faraja yote

Mfumo wa kawaida wa barua ulikuwa kutoa shukrani kwa walioandikiwa barua, lakini kwenye sala ya shukrani ilielekezwa kwa Mungu.

YHWH kama Baba wa *Yeshua* (yaani, Yesu kwa Kiebrania), linajulikana tu kwa Ufunuo. Hakuna mjadala toka ulazima wa kifalsafa ama muundo ungeweza kutoa thiolojia ya kiuhusiano. Jihadhari na "uthibitisho" kuhusu Mungu ambao umejikita kwenye mantiki badala ya kujikita kwenye neno, lakini yanawasaidia watu wengi wanaokataa kuyakubali maandiko kama ukweli. Tazama Elton Trueblood, *The Logic of Belief*.

◙ **"Baba wa rehema"** Kuna maneno matatu ya Kiyunani yanayokaribiana na "Rehema" au "huruma."

1. *eleos*, mara nyingi likirejerea kwenye hisia za rehema ama huruma (kama vile 2 Kor. 4:1; Rum. 9:15, ambayo ni nukuu toka Kutoka. 33:19)

2. *splanchna*, ambalo linarejea mahali panapopasa kuwa na huruma ama rehema katika hisia ya ndani (kama vile Flp. 2:1; Col. 3:12)
3. *oiktirmos*, kuhisi ama kujulisha dhana ya rehema ama huruma juu ya hali ya mtu mwingine (kama vile 2 Kor. 1:3,4-6; Rum. 12:1)

Neno hili linathibitisha tabia ya matendo ya Mungu na hisia kuhusu mwadamu aliyeanguka. Hili ni tumaini letu kuu rehema na neema ya Mungu isiobadilika.

Agano Jipya mara nyingi hutumia "Baba"pamoja na KIMILIKISHI kufafanua Uungu.

1. Baba wa rehema (kama vile 2 Kor. 1:3)
2. Baba wa utukufu Efe. 1:17 (kama vile Matendo 7:2; 1 Kor. 2:8)
3. Baba wa wote (kama vile Efe 4:6)
4. Baba wa roho (kama vile Hebr. 12:9; Ufu. 22:6)
5. Baba wa nuru (kama vile Yakobo 1:17)
6. Tena na tena katika maandiko ya Paulo, "Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo"

**1:4-11 "faraja"** Neno hili, *paraklēsis*, katika miundo yake tofauti, limetumika mara kumi katika 2 Kor. 1:3-11. Ndilo neno la ufunguo katika aya yote na pia katika sura 1-9, ambapo limetumiwa mara ishirini na tano. Neno lamaanisha "kuita pamoja na" mara nyingi lilitumika katika dhana ya kimahakama kwa wakili aliyetoa msaada wa kisheria, faraja na uangalizi.

Katika muktadha huu limetumika katika dhana ya kutia moyo na kuliwaza. Neno linalokaribiana, *paraklētos*, limetumika kwa Roho mtakatifu katika Yohana 14:16,26; 15:26; 16:7; na Yesu katika 1 Yohana 2:1. Kwenye muktadha huu limetumika kwa Baba.

Muundo wa Kitenzi cha *parakaleō* umetumika katika dhana kadhaa.

1. Agano la Kale la Kiyunani
   a. sihi, Kumb. 3:28
   b. fariji, Mwa. 24:67; 37:35; Zab. 119:50 (katika dhana ya Ki-masihi; Isa. 40:1; 49:13; 51:3; 61:2)
   c. uwe na huruma, Kumb. 32:36; Amu. 2:18; Zab. 135:14
   d. liwaza, Isa. 35:4
   e. ita, Kut. 15:13
2. Maandiko ya Paulo kwa Wakorintho
   a. Sihi, 1 Kor. 1:10; 4:16; 14:30-31; 16:15-16; 2 Kor. 2:8; 5:20; 6:1; 8:4,6; 10:1
   b. fariji, changamka, 2 Kor. 1:4,6; 2:7; 7:6,7,13; 13:11
   c. kuwa na huruma, liwaza, 1 Kor. 4:13
   d. sihi sana, sihi hata kwa mihemko, omba, 1 Kor. 16:12; 2 Kor. 9:5; 12:18

**1:4 "ili nasi tupate kuwafariji wale walio katika dhiki za namna zote"** Kuna sababu mbili zilizotajwa katika muktadha huu kwa nini Wakristo wanateseka: (1) ili waweze kuwafariji wengine, 2 Kor. 1:4 na (2) kutufanya tusitegemee nafsi zetu, 2 Kor. 1:9. Waamini wanaishi kwenye ulimwengu ulioanguka. Mambo mabaya hutokea; baadhi ni ya kitakwimu, mengine ni uovu wa mtu binafsi, lakini yote yaweza kutumwa (sio kutumwa, bali kuruhusiwa) na Mungu kwa kukomaa kwetu na huduma (kama vile. Rum. 8:28-29). Tazama W. Wenham, *The Goodness of God*

Neno, mateso, (yaani, *thlipsis*), kiasili lilimaanisha "kusongamana ama kuseta " ( yaani., utengenezaji wa zabibu ama kusaga ngano iwe unga)" lakini lilikuja kutumika kisitiari kwa mwili (kama vile 2 Kor. 1:6) ama mihemko (kama vile 2 Kor. 2:4; 11:28) kiwewe (kama vile 2 Kor. 4:8; 7:5).

Kuna maoni binafsi kidogo. Ni vigumu sana katika kitabu hiki kujua Paulo anamhusianisha nani kwa viwakilishi nomino vya wingi, "sisi," "sisi," na "vyetu." Yaweza kuhusu yeye (1) yeye peke yake; (2) yeye na kikundi chake; (3) yeye na mitume wengine; (4) au waaminio wote.Ni mazingira tu yanaweza kuamua na wakati mwingine inaleta utata.

MADA MAALUMU: DHIKI KUU (SPECIAL TOPIC: TRIBULATION)

**1:5 " mateso ya Kristo yanavyozidi kwetu"** Neno la Kiyunani *pathēma* limetumika hapa kwa mateso ya Kristo (kama vile Luka 22:15) na katika 2 Kor. 1:6 na 7 kwa mateso ya waaminio. Paulo anatumia neno tofauti kwa mateso/dhiki (*thlipsis*) katika 2 Kor. 1:4.

Paulo anataja waamini kama washiriki wenza wa mateso pamoja na Kristo mara kadhaa (kkama vile 2 Kor. 4:10-11; Rum. 8:17; Flp. 3:10; Kol. 1:24). Kama tunavyoshiriki kufa na kufufuka kwake vivyo hivyo twashiriki kuteseka, na kuadhibiwa kwake. Dhana ya Mkristo anayeteseka inazungumziwa mara nyingi (kama vile Matendo 14:22; Rum. 5:3-4; 8:17; Gal. 6:17; Flp. 1:29; 3:10; Kol. 1:24; 1 The. 3:3-4; 2 Tim. 3:12; Hebr. 13:13; Yakobo 1:1-4; 1 Pet. 2:19-23; 3:14; 4:12-19). Hii ni kawaida kwa Wakristo wote. Somo hili laonekana kuwa maudhui unganishi ya 2 Wakorintho. Utoshelevu wa Yesu pia ni mwingi na wa kujaa pomoni! Ndiyo, waaminio watateseka katika ulimwengu ulioanguka kwa kuwa ni Wakristo, Lakini Mungu wetu atatupatia kila hitaji, kimwili, kihisia na kiroho kupitia Kristo. Kifo na ufufuo wa Yesu Kristo sio kwa ajili ya mbingu bali kwa ajili ya wakati huu pia!

◙ **" inazidi"** Muundo wa kawaida wa Paulo katika 2 Wakorintho waweza kuelezeka kwa matumizi yake ya "utele."

1. *perissos*, juu na zaidi (kama vile 2 Kor. 2:7; 9:1)
2. *perissoterōs*, kwa wingi zaidi (kama vile 2 Kor. 2:4; 7:13)
3. *perisseuō*, juu na zaidi (kama vile 2 Kor. 1:5; 3:9; 4:15; 8:2; 9:8)
4. *perisseauma*, zaidi ya utoshelevu (kama vile 2 Kor. 8:13,14)
5. *perisseia*, Wingi mkuu (kama vile 2 Kor. 8:2; 10:15)

Inapokuja kwa kile Mungu katika Kristo alichokifanya kwa waaminio, kila wakati ni "Mungu mkuu," "zaidi ya mahitaji," "kuzidi na kupitiliza"! Tazama nukuu katika 2 Kor. 2:7**.**

**1:6 " ikiwa. . . ikiwa"** Hizi ni SENTENSI SHURUTISHI DARAJA LA KWANZA. Katika ulimwengu ulioanguka viongozi wa Kristo watapata maumivu lakini hili huleta utajiri wa msaada na wokovu kwa wale wanaosikia kuteseka, kuna kusudi la ki-Ungu,(kama vile 2 Kor. 1:7).

◙ **"ni kwa ajili ya faraja yenu na wokovu"** Kwakuwa faraja imeshirikishwa na wokovu, inaonekana kwamba hii inafuatisha maana ya Agano la Kale ya neno *sosō*, inayomaanisha ukombozi wa mwili (cf. Matt. 9:22; Mark 6:56; James 5:20). Kuna utofauti wa machapisho ya Kiyunani yanayohusiana na 2 Kor. 1:6-7. Sababu kubwa ya wazi ni kwamba neno "faraja" (*paraklēseōs*) katika 2 Kor. 1:6a limechanganywa na muundo huo huo wa 6b, ambao andiko lililoingia. Kati limeachwa nje. Pamoja na kuachwa, maneno mengine yameongezwa na waandishi kulifanya andiko lieleweke.

◙ **"kustahimili mateso"** Katika tafsiri ya Agano la Kale la Kiyunani neno hili lilitumika kama tumaini ama tazamio (kama vile Yer. 14:8; 17:13; 50:7). Katika maandiko ya Paulo linamaanisha ustahimilivu wa hiari ulio katika "utendaji, na wenye kudumu," ambao unatokana na mateso yanayosababishwa na injili: ikiwa tutaaminika, tunaishi, na ikiwa tutaitangaza. Kuna ushirikiano kwenye maandiko ya Paulo kati ya neno "tumaini" (kama vile 2 Kor. 1:7) na "ustahimilivu wenye subira" (kama vile Rum. 5:3-5; 8:25; 15:4-5; na 1 The. 1:3; 1 Tim. 6:11).

**1:7** Kama waaminio wanavyoshiriki mateso, jinsi Yesu alivyoshiriki, vilevile wanashiriki faraja ya Mungu, kama Yesu alivyoshiriki.
Tumaini la Paulo kwao lilikuwa:

**NASB "limewekewa mzizi"**
**NKJV "mathubuti"**
**NRSV "usiotikisika"**
**TEV "usiotikisika kamwe"**
**NJB "salama"**

Hili ndilo neno hilo hilo (*bebaios*) lililotumika katika 1 Kor. 1:8 na 2 Kor. 1:21.

MADA MAALUM: DHAMANA (SPECIAL TOPIC: GUARANTEE

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 2 WAKORINTHO 1:8-11**
**8 Maana ndugu, hatupendi, msijue habari ya dhiki ile iliyotupata katika Asia, ya kwamba tulilemewa mno kuliko nguvu zetu, hata tukakata tamaa ya kuishi. 9 Naam, sisi wenyewe tulikuwa na hukumu ya mauti katika nafsi zetu ili tusijitumainie nafsi zetu, bali tumtumaini Mungu, awafufuaye wafu, 10 aliyetuokoa sisi katika mauti kuu namna ile; tena atatuokoa; ambaye tumemtumaini kwamba atazidi kutuokoa; 11 ninyi nanyi mkisaidiana nasi kwa ajili yetu katika kuomba, ili, kwa sababu ya ile karama tupewayo sisi kwa msaada wa watu wengi, watu wengi watoe shukrani kwa ajili yetu.**

**1:8 "hatupendi, msijue habari"** Paulo anatumia mara nyingi kifungu hiki kutambulisha ama habari mpya au hitimisho (kamavile Rum. 1:13; 11:25; 1 Kor. 10:1; 12:1; 2 Kor. 1:8; 1 The. 4:13).

◙ **"habari ya dhiki ile iliyotupata katika Asia, ya kwamba tulilemewa mno kuliko nguvu zetu"** Haijulikani ni kitu gani hasa ambacho Paulo anarejelea kutokana na msemo huu.

1. Fujo iliyosababishwa na Demetrius katika Matendo 19:23-41
2. "wakati wa kupigana na wanyama kule Efeso" ya 1 Kor. 15:32
3. Kifungo gerezani, yawezekana na hukumu ya kifo (kama vile 2 Kor. 1:9-10)
4. Aina Fulani ya magonjwa ya mwili

Vyovyote vile ingekuwa, ilikuwa ni changamoto ya Paulo ama kuishi au kufa (kama vile 2 Kor. 1:8-10) na yawezekana kanisa la Korintho walikuwa wamekwisha kusikia habari hiyo kwasababu Paulo hahisi hitaji la kutambulisha habari hiyo. Kwa "zaidi inavyohitajika" (*huperbolē*) Angalia Mada Maalum: matumizi amabatani ya Paulo ya neno *Huper* katika 1 Kor. 2:1.

**1:9 "tulikuwa na hukumu ya mauti katika nafsi zetu ili tusijitumainie nafsi zetu"** Hii ni kauli isiyo ya kawaida. Kwanza, neno " hukumu" linatumika kwenye uandishi wa Kiyunani cha kale tu, baadaye kumaanisha "hukumu ya kifo" (kama vile Josephus, *Antiquities* 14:10:6). Paulo haonekani kuwa anarejerea hukumu ya kimahakama, bali namna ya kifo chake kilichokuwa kinakaribia. Hili lilimlazimisha yeye pamoja na washiriki wenzake kujitupa mbele za Mungu kwa msaada wake, huruma yake, na uweza wake.

KITENZI ni KAULI TIMILIFU TENDAJI YENYE KUARIFU. Wengine wameliona hili kama njia ya kurejerea ugonjwa ambao Paulo na kundi la wamisheni wenzake walipambana nao, ambalo lilikuwa na matokeo endelevu. Hata hivyo, inaweza kutafsiriwa kama WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFU, muundo sawa na 2 Kor. 2:13.
Hii yote inakifanya kifungu hiki kuwa chenya utata sana kikiwa na tafsiri tofauti. Ingawa mazingira halisia hayaonekani kuwa ya hakika, maana ya Paulo kiroho ni kwamba mateso yaliyo wazi husaidia waaminio kumtumaini Mungu, kwa nguvu zaidi na kwa utimilifu zaidi katika Kristo!

◙ **"tusijitumainie nafsi zetu"** Kama 2 Kor. 1:4 inavyofafanua kusudi la kwanza la kuteseka kwa Wakristo, aya hii inafafanua kusudi la pili. Ukweli huu waweza kuonekana katika " mwiba ndani ya mwili" (kama vile 2 Kor. 12:7-9). Katika utawala wa roho udhaifu wa kibinadamu ukiambatana na imani huachilia uweza wa Mungu.

◙ **" Mungu, awafufuaye wafu"** Je Paulo anafikiria juu ya

1. Mifano ya Agano la Kale ya watu ambao Mungu aliwarejeshea uhai wa kimwili ( kama vile 1 Fal. 17:17-22; 2 Fal. 4:32-37)
2. Maelezo ya Kitheolojia ya Agano la Kale (kama vile Kumb. 32:39; 1 Sam. 2:6; 2 Fal. 5:7)
3. Mjadala wake wa Ufufuo katika 1 Wakorintho 15

**1:10 "ambaye tumemtumaini kwamba atazidi kutuokoa"** KIWAKILISHI kinamrejea Mungu Baba (kama vile 2 Kor. 1:9; 1 Tim. 4:10). Cheo hiki cha Mungu kimefafanuliwa kwa namna ya kupendeza sana. Paulo mara kwa mara huunda vyeo vya Mungu vinavyoelezeka vya ajabu, vyenye nguvu (Tazama orodha kamili katika 2 Kor. 1:3), kama vile

1. "Baba wa Rehema" (kama vile. 2 Kor. 1:3)
2. "Mungu wa faraja" (kama vile 2 Kor. 1:3)
3. "kwake yeye awezaye" (kaama vile Rum. 16:25; Efe. 3:20)

KITENZI ni KAULI TIMILIFU TENDAJI YENYE KUARIFU, ambayo inamaanisha tendo lililokamilishwa wakati uliopita lenye matokeo ya kudumu (kama vile 1 Kor. 15:19; 1 Tim. 5:5; 6:17).

◙ **"atatuokoa"** Neno hili limetumika mara tatu katika 2 Kor. 1:10. Hii inafuata dhana ya Agano la Kale ya ukombozi kimwili, kijamii, kimhemko, na kiroho. Paulo alitumia neno hili mara kadhaa (kama vile Rum. 7:24; 11:26; 15:31; 2 Kor. 1:10; Kol. 1:13; 1 The. 1:10; 2 The. 3:2; 2 Tim. 3:11; 4:17-18). Hakika alidhani kwamba alikuwa anakwenda kufa huko Efeso (kama vile 2 Kor. 1:8-10).

**NASB " kutoka katika hatari kubwa ya kifo"**
**NKJV "kutoka kwenye mauti kuu namna hiyo"**
**NRSV "kutoka hatari kubwa ya kifo kiasi hicho"**
**TEV "kutoka kwenye hatari kubwa za kifo"**
**NJB "kutoka kwenye kifo kama hicho"**

Kuna utofauti wa maandiko ya asili ya Kiyunani kati ya HALI YA UMOJA ya neno "mauti kuu namna ile" (yaani, MSS א, A, B, C, D, F, G) na wingi (yaani, MS $P^{46}$ Na tafsiri ya shamu, pia maandiko ya Kiyunani yaliyotumiwa na Origen, Basil, Chrysostom, Theodoret, Jerome, na Augustino). Katika hali ya WINGI (kama vile TEV) zaidi ni yale yasio ya kawaida na ni ya kale. WINGI huu waweza kuonekana kwenye orodha ya Paulo ya matatizo aliyopambana nayo kwa ndani na kwa nje katika 2 Kor. 4:8-12; 6:3-10; 11:23-29. Toleo la $UBS^4$ huipa WINGI daraja la "B" (karibu hakika).

**1:11**
**NASB "jiunga kutusaidia kwa njia ya maombi"**
**NKJV "mkisaidia pamoja katika maombi kwa ajili yetu"**
**NRSV "jiunge katika kutusaidia kwa maombi yenu"**
**TEV "tusaidieni kwa njia ya maombi yenu kwetu"**
**NJB "maombi yenu kwa ajili yetu yatasaidia sana jambo hili"**

Wanafunzi kadhaa wanaamini kwamba muundo huu wa ki-sarufi (Murry J. Harris in *The Expositor's Bible Commentary*, juzuu. 10, uk. 322) unatumika katika dhana ya mashariti (The Anchor Bible, juzuu. 32A, uk. 115). Kama waaminio hawaombi kwa namna fulani Mungu mwenye mamlaka amechagua kuacha kutenda, (kama vile Ykobo 4:2). Hii inaonyesha manufaa ya maombi yenye aina ya maombezi (kama vileEfe 6:18-20). Paulo alihisi kwamba maombi ya Wakristo yakiunganishwa na neema ya Mungu yanweza kumwokoa kutoka mautini na kuendelea kumlinda na kumkomboa. Ukombozi wa Paulo kwa Mungu ungetambuliwa na kusifiwa na wengi ambao wangebarikiwa na huduma ya Paulo inayoendelea.

◙ **" watu"** Kikawaida hili neno ni "uso" (yaani, *prosōpon*) Paulo hutumia neno hili mara kwa mara katika 2 Wakorintho (kama vile 2 Kor. 2:10; 3:7 [mara mbili],13,18; 4:6; 5:12; 8:24; 10:1,7; 11:20). Laweza kuwa kidokezo cha Agano la Kale kuhusiana na kiwango cha nafasi ya mtu kutokana na maombi ya Kiyahudi akiwa ameinua kichwa juu jambo ambalo hutosheleza hasa kwenye mukutadha huu,.
Paulo hutumia neno hili katika dhana kadhaa katika 2 Korintho:

1. Kwa watu, 2 Kor. 1:11; 2:10; 4:6
2. Kwa uso wa mtu, 2 Kor. 3:7 (mara mbili), 2 Kor. 13,18; 10:1,7; 11:20
3. Sitiari kabla ya dhana ya "mbele ya" (yaani, mahali, sio muda), 2 Kor. 8:24

4. Sitiari kwenye mwonekano wa nje (kama vile NRSV), 2 Kor. 5:12

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 2 WAKORINTHO 1:12-14**

**12 Kwa maana kujisifu kwetu ni huku, ushuhuda wa dhamiri yetu, ya kwamba kwa utakatifu na weupe wa moyo utokao kwa Mungu; si kwa hekima ya mwili, bali kwa neema ya Mungu; tulienenda katika dunia, na hasa kwenu ninyi. 13 Maana hatuwaandikii ninyi neno, ila yale msomayo, au kuyakiri; nami nataraji ya kuwa mtayakiri hayo hata mwisho; 14 vile vile kama mlivyotukiri kwa sehemu, ya kwamba sisi tu sababu ya kujisifu kwenu, kama ninyi mlivyo kwetu sisi, katika siku ile ya Bwana wetu Yesu.**

**1:12 "kujisifu kwetu ni huku"** Maneno haya ya Kiyunani *kauchaomai, kauchēma,*na *kauchēsis* yanatumika kama mara mbili tu kwenye sehemu yote iliyobaki kwenye Agano Jipya (zote mbili ni katika Yakobo). Matumizi yake yaliyozidi yako kwenye I na 2 Wakorintho.

Kuna kweli kuu mbili kuhusiana na kujivuna:

1. Hakuna mwenye mwili atakayejitukuza/jivuna mbele za Mungu (kama vile 1 Kor. 1:29; Efe. 2:9)
2. Waaminio wanapaswa kujisifu katika Bwana (kama vile 1 Kor. 1:31; 2 Kor. 10:17, ambacho ni kidokezo kwa Yer. 9:23-24)

Kwahiyo kuna kujivuna, kunakofaa/kusiko faa (yaani, kiburi).

1. Kunakofaa
   a. Katika tumaini la utukufu (kama vile Rum. 4:2)
   b. Katika Mungu kwa njia ya Bwana Yesu (kama vile Rum. 5:11)
   c. Katika msalaba wa Bwana Yesu Kristo (yaani, dhamira kuu ya Paulo, kama vile 1 Kor. 1:17-18; Gal. 6:14)
   d. Paulo anajisifu katika
      (1) Huduma yake bila kufidiwa (kama vile 1 Kor. 9:15,16; 2 Kor. 10:12)
      (2) Mamlaka yake kutoka kwa Kristo (kama vile 2 Kor. 10:8,12)
      (3) Kutokujisifia kazi ya watu wengine (kama Wakorintho wengine walivyo kuwa wanafanya, kama vile 2 Kor. 10:15)
      (4) Urithi wake wa kimbali (kama wengine walivyo kuwa wanafanya pale Korintho, kama vile 2 Kor. 11:17; 12:1,5,6)
      (5) Makanisa yake
         (a) Korintho (kama vile 2 Kor. 7:4,14; 8:24; 9:2; 11:10)
         (b) Wathesalonike (kama vile 2 The. 1:4)
      (6) Ujasiri wake katika faraja na ukombozi wa Mungu (kama vile 2 Kor. 1:12)
2. Kusikofaa
   a. Katika uhusiano na urithi wa Kiyahudi (kama vile Rum. 2:17,23; 3:27; Gal. 6:13)
   b. Wengine katika kanisa la Korintho walijisifu
      1) Katika wanadamu (kama vile 1 Kor. 3:21)
      2) Katika hekima (kama vile 1 Kor. 4:7)
      3) Katika uhuru (kama vile 1 Kor. 5:6)
   C. Walimu wa uongo kujisifu kanisani pale Korintho (kama vile 2 Kor. 11:12)

◙ **"ushuhuda wa dhamiri yetu"** Paulo hutumia neno "dhamiri" mara nyingi kwenye barua za Wakorintho (kama vile 1 Kor. 4:4; 8:7,10,12; 10:25,27,28,29; 2 Kor. 1:12; 4:2; 5:11). Inarejea ile maana ya ndani ya dhana ya uadilifu wa kile kinachofaa au kisichofaa (kama vile Matendo 23:1; Rum. 2:15). Dhamiri yaweza kuathiriwa na maisha yetu ya zamani, uchaguzi wetu usiofaa, ama Roho wa Mungu. Sio mwongozo ulio kamili (kama vile 1 Kor. 4:4; 8:7; 1 Tim. 4:2), lakini unabainisha mipaka ya imani binafsi (kama vile 1 Tim. 1:5,19). Kwa hiyo, kwenda kinyume na dhamiri zetu, hata kama zimeikosea ama ni dhaifu, hubaki kuwa tatizo kubwa la imani.

Dhamiri ya aaminiye inahitaji kuwa inatengenezwa na neno la Mungu na Roho wa Mungu (kama vile 1 Tim. 3:9). Mungu atawahukumu waaminio kutokana na nuru waliyonayo, lakini waaminio wote wanahitaji kuwa wazi kwa

biblia na Roho kwa nuru zaidi na kusudi waendelee kukua katika kumjua bwana Yesu Kristo. Katika muktadha huu, hukumu ya nyakati za mwisho inakaribia (kama vile 2 Kor. 1:13-14). Mungu atahukumu wanadamu kulingana na uelewa wao, dhamiri yao (kama vile Rum. 2:15-16; 9:1; 13:5).
Nia na matendo ya Paulo vilichunguzwa na kuhukumiwa na idadi ndogo ya walimu wa uongo pale Korintho (kama vile sura 10-13). Yaonekana kulikuwa na makundi mawili: (1) kundi la mahali la wapinzani na (2) kundi la Waalimu wa uongo Wayahudi wa Ki – Palestina waliokuwa wanazunguka.

◙ **"utakatifu"** Baadhi ya maandiko ya asili ya Kiyunani yana "utakatifu" (yaani $P^{46}$, א*, A, B, C, K, P, na toleo la Coptic NASB, NIV, na tafsiri za NJB ). Mengine yana "urahisisho" (yaani, אi[2], D, F, G, na Vulgate, Peshitta, NKJV, NRSV, na tafsiri ya TEV). Bruce Metzger in *A Textual Commentary on the Greek New Testament*, inatoa maoni kwamba kamati ya tafsiri kwa toleo la $UBS^3$ ilipenda zaaidi "urahisi" (*haplotēti*), iliweka daraja "D", ikimaanisha kiwango cha hali ya juu cha mashaka (uk. 575). Hata hivyo, toleo la $UBS^4$ huweka daraja "B" ikimaanisha karibu hakika, (uk. 612). Uhakika huu ulioongezeka unakuja kutoka kwenye ukweli kwamba Paulo hutumia neno "urahisi" katika 2 Kor. 11:3 (na neno kama hilo lililotafsiriwa "ukarimu" katika 2 Kor. 8:2; 9:11,13), lakini hakuna kamwe katika maandiko yake anapotumia *hagiotēti*.

◙ **"uaminifu"** Neno hili lilikuwa na vidokezo viwili, "mkarimu" au"aminifu." Ilikuwa sitiari iliyohusiana na maono. Kwenye Agano la Kale jicho lilitumika kama sitiari kwa njia mbili (1) jicho ovu (uchoyo, BDB 949, kama vile Kumb. 15:9-10) na (2) jicho jema (karimu, BDB 373 III, kama vile Mith. 22:9). Yesu alifuata matumizi haya (kama vile Mt. 6:22-23; 20:15). Paulo alitumia neno hili katika dhana mbili.

1. "urahisi, uaminifu, usafi" (yaani, hakuna agenda ya siri ama maigizo ya uongo, kama vile 2 Kor. 1:12; 11:3; Efe. 6:5; Col. 3:22)
2. "ukarimu" (kama vile Rum. 12:8; 2 Kor. 8:2; 9:11,13)

◙ "**si kwa hekima ya mwili"** Paulo anajadili hekima ya kiulimwengu kwa upana sana katika 1 Wakorintho (kama vile 1 Kor. 1:18-31; 2:1-16; na 3:18-23 na kwa kejeli katika 2 Kor. 4:10; 6:5 na yawezekana 10:15). Paulo hutumia vifungu vya namna hiyohiyo kurejerea hekima katika 1 Kor. 1:17; 2:4,13-14. Kwenye Ibara hii anafanya mzaha baina ya hekima ya kiulimwengu dhidi ya kuishi kwa neema ulimwenguni. Ushahidi wa Paulo katika uongozi wake sio katika mantiki ama ujuzi wa kuongea tu bali maisha ya utauwa pamoja na dhamiri mbele za Mungu. Paulo anadai kuwa amekwisha kuwaandikia kwa uwazi maneno dhahili, yenye kueleweka.Kama wangekuwa wenye hekima, wangekwisha kuelewa maneno yake. Madhumuni na vidokezo vya mtindo wa maisha bila kutumia juhudi yoyote lakini hawakuelewa. Paulo anatumia neno "mwili" katika njia kadhaa. Angalia Mada Maalum katika 1 Kor. 1:26.

**1:13-14** Aya hizi ziko katika muundo mlingano na zaonekana kurejerea barua za Paulo za awali kwa Korintho (ni ipi kati ya hizo haijulikani). Aliandika ili aeleweke. Hata hivyo, lakini mwelekeo wao na mtindo wa maisha yao waonyesha kuwa walielewa kidogo tu.
Je neno *telous* kwenye muktadha huu lamaanisha "kamili" (TEV, NJB, NIV) au "mwisho" (NASB, NKJV, NRSV)? Yote yaleta maana. Ikiwa "kamili" (yaani, kikamilifu ikilinganishwa na kisehemu kidogo tu) ingeungana na sehemu ya kwanza ya 2 Kor. 1:14. Ikiwa "mwisho" lingefanana na "siku wa Bwana wetu Yesu" kwenye ile ya mwisho wa 2 Kor. 1:14.
Kanisa la Korintho ni uthibitisho wa utendaji wenye matokeo ya utume wa Paulo. Paulo anatamani kwamba maneno yao, nia yao na vitendo vyao viwe chanzo cha kujisifu na kujigamba, ambako ni halali wakati Bwana arudipo kuhukumu (yaani, "siku ya Bwana wetu Yesu," kama vile 1 Kor. 1:8; 5:5; Flp. 1:6,10; 2:16; 1 The. 5:2; 2 The 2:2).

**1:14 " katika siku ile ya Bwana wetu Yesu"** Kifungu "siku ile" ni nahau ya Agano la Kale. Angalia maelezo kutoka maoni yangu katika Amosi 2:16.

MADA MAALUM: SIKU ILE (SPECIAL TOPIC: THAT DAY)

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : 2 Wakorintho 1: 15-22**

[15] **Nami nikiwa na tumaini hilo nalitaka kufika kwenu hapo kwanza, ili mpate karama ya pili;** [16] **na kupita kwenu na kuendelea mpaka Makedonia; na tena toka Makedonia kurudi kwenu na kusafirishwa nanyi kwenda Uyahudi.** [17] **Basi, nilipokusudia hayo, je! Nalitumia kigeugeu? Au hayo niyakusudiayo, nayakusudia kwa jinsi ya mwili kwamba iwe hivi kwangu, kusema Ndiyo, ndiyo, na Siyo, siyo?** [18] **Lakini kama Mungu alivyo mwaminifu, neno letu kwenu si Ndiyo na siyo.** [19] **Maana Mwana wa Mungu, Kristo Yesu, aliyehubiriwa katikati yenu na sisi, yaani, mimi na Silwano na Timotheo, hakuwa Ndiyo na siyo; bali katika yeye ni Ndiyo.** [20] **Maana ahadi zote za Mungu zilizopo katika yeye ni Ndiyo; tena kwa hiyo katika yeye ni Amin; Mungu apate kutukuzwa kwa sisi.** [21] **Basi Yeye atufanyaye imara pamoja nanyi katika Kristo, na kututia mafuta, ni Mungu,** [22] **naye ndiye aliyetutia muhuri akatupa arabuni ya Roho mioyoni mwetu.**

**1:15 "nikiwa na tumaini"** Angalia maelezo kamili katika 2 Kor. 3:4.

◙ **"I intended at first to come to you"** "Kuja kwenu" ni NJEO YA WAKATI USIOTMILIFU inayodokeza vitendo vinavyo rudiwa mara kwa mara, fikra zilizopo, katika wakati uliopita. Katika 1 Kor. 16:2-8 Paulo aliwaambia kuhusu mipango ya safari aliyokusudia. Kwasababu ya vitendo vyao, baadaye alibadili nia yake kwasababu hakutaka kuingia kwenye hukumu, bali kwenye furaha! Idadi ndogo ya wasemaji walimshitaki kwa habari ya kutokuwa na msimamo, sio tu katika mipango yake ya safari bali katika injili yake (kama vile 2 Kor. 1:18-20).

**NASB "ili kwamba mpokee Baraka maradufu"**
**NKJV "kwamba mpate faida ya pili"**
**NRSV "ili kwamba mpate upendeleo mara mbili"**
**TEV "ili kwamba muweze kubarikiwa mara mbili"**
**NJB "ili kwamba mfaidi mara mbili"**

Kuna chapisho la Kiyunani lililo tofauti hapa. Baadhi ya machapisho yana *charin*, litokanalo na *charis*, ambalo linamaanisha faida ama upendeleo (yaani, א*, A, C, D, F, G, na tafsiri za shamu na Armenian).

Maandiko mengine yana *charan*, inayotokana na *chara*, ambayo inamaanisha furaha ama kufurahia, (yaani, א[2], B, L, P). Toleo la UBS[4] la maandiko ya Kiyunani huweka daraja *charin* a "B" (karibu hakika), Kwenye muktadha (yaani, 2 Kor.1:16). Inahusu kuja kwa Paulo mara ya pili Korintho na wao wakipata fursa ya kumpa mahitaji yake anapoendelea kusafiri (kama vile cf. Gordon D. Fee, *To What End Exegesis?*, pp. 99-104).

**1:16 "kurudi kwenu na kusafirishwa nanyi kwenda Uyahudi"** Paulo asingechukua fedha yoyote kutoka kanisa la Korintho wakati alipokuwa anawahudumia. Aliogopa angeweza kushambuliwa kuhusu swala hili. Kama jinsi ilivyojitokeza kushambuliwa kwa yeye kutochukua fedha kutoka kwao.

Kifungu hiki kinadokeza kwamba alikuwa anakwenda kuruhusu kanisa hili limpatie mahitaji yake ya safari ya kimisheni (kama vile 1 Kor. 16:6; Rum. 15:24). Hii ingeweza kuwa njia ya kujaribu utii wao kwake na injili na kugawanyisha wapinzani wake.

**1:17 "nayakusudia kwa jinsi ya mwili"** Kifungu hiki chaweza kuaksi wapinzani wa Paulo (kama vile 2 Kor. 10:2-3; 11:18) ama Paulo anatafuta mapenzi ya Mungu katika yote anayofanya ikiwa ni pamoja na safari (kama vile 1 Kor. 4:19; 16:7; Matendo 18:21; Rum. 1:10; 15:32).

Chaguo la pili lenye kufaa muktadha huu vizuri linaweza kuonekana kutoka 2 Kor. 1:18a. Uaminifu wa Mungu ni dhana ya Paulo inayojirudia mara nyingi katika maandiko yake (kama vile 1 Kor. 1:9; 10:13; 1 The. 5:24; 2 The. 3:3).

Kuhusu “mwili" Angalia Mada Maalum katika 1 Kor. 1:26.

**1:18 "Mungu alivyo mwaminifu"** Mwaminifu limewekwa kwanza kwa ajili ya msisitizo (kama vile 1 Kor. 1:9; 10:13; 1 The. 5:24; 2 The. 3:3). Katika Agano la Kale imani kwa kawaida inaeleweka kama uaminifu. Hii ndiyo tabia ya Mungu iliyo muhimu sana (kama vile Kumb. 7:9; Isa. 49:7). Tabia yake ya neema na uaminifu haibadiliki,

tumaini la mwanadamu halipo katika utendaji wa kibinadamu ama moyo wa kufanya ibada (kama vile Mal. 3:6). Bali ni katika tabia na ahadi za Mungu (kama vile 2 Kor. 1:12,15,20)!

**1:19 "Mwana wa Mungu, Kristo Yesu"** Paulo hatumii kifungu "Mwana wa Mungu" mara nyingi (kama vile Rum. 1:4; hapa na Gal. 2:20). Hata hivyo, dhana hiyo pamoja na kutumia vifungu vya maneno hayo ni ya kawaida sana.Angalia Mada Maalum katika 1 Kor. 1:9.

▣ **"Silwano"** Silas, ama Silvanus, alikuwa mtu ambaye Paulo alimchagua kwenda naye kwenye safari ya pili ya umisheni baada ya Barnaba na Yohana Marko kurudi Kipro.

1. Anatajwa kwanza katika biblia Matendo 15:22 anapoitwa kiongozi miongoni mwa ndugu wa kanisa la Yerusalemu.
2. Pia alikuwa nabii (kama vile Matendo 15:32).
3. Alikuwa na uraia wa Kirumi kama Paulo (kama vile Matendo 16:37).
4. Yeye pamoja na Yuda Barsaba walitumwa antiokia na kanisa la Yerusalemu kufuatilia hali iliyokuwa (matendo 15:22,30-35).
5. Paulo anamtaja katika 2 Kor. 1:19 kama mshiriki mwenza muhubiri wa injili.
6. Baadaye anatambulishwa na Petro kwenye maandiko katika 1 Petro. (kama vile 1 Pet. 5:12).
7. Wote wawili Paulo na Petro wanamwita Silivanusi wakati Luka anamwita Silas (Muundo wa Kiaramu kwa Sauli). Yawezekana kwamba Silas lilikuwa jina la Kiyahudi na Silvanus jina lake la Kirumi (kama vile F. F. Bruce, *Paul: Apostle of the Heart Set Free*, uk. 213).

**1:19-20 "bali katika yeye ni Ndiyo"** Aya ya 19 na 20 zimefungwa kithiolojia! Paulo anatamka kama kweli kwamba timu yake (Yeye mwenyewe, Silvanus, na Timotheo) walimhubiri Yesu kama ahadi ya Mungu iliyotimilizwa kama mwana wa Mungu kama tumaini pekee la mwanadamu kwao kama kilele cha Ufunuo cha Agano la Kale! Kuhubiri kwao hakukuwa dhaifu bali kuliko wazi na bila makosa (kama vile 2 Kor. 1:18). Yesu ndiye "ndiyo" wa Baba kwa kila ahadi, kila tendo, (yaani, KAULI TIMILIFU TENDAJI YENYE KUARIFU ya neno *ginomai*). Kwa kumthibitisha Yesu wanampa Baba utukufu kwa ajili ya kumtoa Yeye.
Maarifa yote ya kanisa la Korintho juu ya (1) Mungu, (2) na Mwana wake, (3) ahadi zake (kama vile Rum. 9:4) na (4) neema ya utoaji wake vinakuja kupitia timu ya umisheni ya Paulo. Ikiwa wataanza kutia shaka juu ya mienendo na ujumbe wa Paulo, basi watapoteza imani katika injili!

**1:20 "Amina"** Angalia maelezo zaidi 1 Kor. 14:16c.

◙ **"kutukuzwa"** Angalia MADA MAALUM: UTUKUFU (SPECIAL TOPIC: GLORY)Agano la Kale katika 1 Kor. 2:7.

**1:21-22** Kuna muundo ulio wazi usio na makosa kwenye aya hizi unaofafanua kile ambacho Mungu (yaani, "Yeye ambaye") amekwisha kukifanya na kuthibitisha timu ya umisheni.

1. Mungu hututhibitisha, 2 Kor. 1:21 (kama vile 1 Kor. 1:8). Hii ni KAULI TENDAJI ENDELEVU YA WAKATI ULIOPO ambayo inahusu tendo linaloendelea. Inamaanisha kuthibitisha, kuimalisha, kufanya endelevu muda wote, paspo myumbo (kama vile 2 Kor. 1:7; Rum. 4:16). Neno hili linatumika kwenye magombo kuelezea dhamana ya kisheria (kama vile Moulton na Milligan, uk. 107).
2. Mungu alitupaka mafuta, 2 Kor. 1:21 (kama vile 1 Yohana 2:20,27). Hii ni KAULI TENDAJI ENDELEVU YA WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFU. NJEO inalenga kwenye kitendo kilichokamilika, cha mara moja. Neno lenyewe linaaksi dhana ya Agano la Kale ya uchaguzi na uaandaji wa Mungu, wa viongozi maalum wa Israeli kwa ajili ya huduma
    a. Manabii, kama vile 1 Fal. 19:16 na yawezekana kufanana na 1 Nya. 16:22; Zab. 105:15
    b. makuhani, kama vile Kut. 40:15; Law. 4:3; Zab. 105:15
    c. Wafalme, kama vile. 1 Sam. 9:16; Zab. 2:2; 18:50; 20:6; Hab. 3:13)
    Ni neno ambalo katika Kiyunani limetafsiriwa "Kristo" wanaporejerea kwa Masihi (yaani, aliyetiwa mafuta). Waaminio pia wamechaguliwa na kuandaliwa na Mungu kutumikia makusudi ya ufalme wake.

3. Mungu alitutia muhuri, 2 Kor. 1:22 (kama vile Yohana 3:33; 6:27; Rum. 4:11; 15:28; 1 Kor. 9:2; Efe. 1:13; 4:30; 2 Tim. 2:19; Ufu. 7:3-8). Hii ni KAULI YA KATI ENDELEVU YA WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFU Inayomaanisha kuweka alama juu ya kitu ama mtu kama mali ya mtu ama kitu cha mtu. Waaminio Ni mali ya Mungu.
4. Mungu aliweka Roho ndani ya mioyo yetu kama dhamana, 2 Kor. 1:22 (kama vile 2 Kor. 5:5; Rum. 8:9-16,23,26-27; Efe. 1:13-14).

Neno "pewa" ni kauli nyingine TENDAJI ENDELEVU YA WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFU, ikionyesha kitendo kilicho kwisha kukamilika. Mungu amekwisha kuwapa watoto wake.

1. anawaimarisha (NJEO YA WAKATI ULIOPO)
2. Amewatia Mafuta (NJEO YA WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFU)
3. Ameisha Watia Muhuri (NJEO YA WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFU)
4. Amekwisha Wapa Roho (NJEO YA WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFU)

Utoaji wote huu unahusu imani ya Paulo katika 2 Kor. 1:15,19-20. Imani ya Paulo ilikuwa katika vitendo na utoaji wa Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu.

◙ **"Kristo. . . Mungu. . . Roho"** Tambua kwamba utatu uko katika utendaji kwenye kujiamini kwetu (Angalia Mada Maalum inayofuata). Ingawa neno "Utatu" halionekani kwenye biblia dhana hiyo ni yenye kujirudia rudia (kama vile 1 Kor. 12:4-6; 2 Kor. 13:14). Ukristo ni imani ya Mungu mmoja (kama vile Kumb. 6:4). Hata hivyo, ikiwa Yesu ni mwenye Uungu na Roho Mtakatifu ni mtu, tunao watu watatu wa usababisho wa Kiungu wa kufanya kitu kwa jinsi kilivyo. Umoja wa nafsi tatu! Angalia Mada Maalum katika 1 Kor. 2:10.MADA MAALUM: UHAKIKA (SPECIAL TOPIC : ASSURANCE)

**1:22 "aliyetutia muhuri"** Angalia MADA MAALUM: MIHURI (SPECIAL TOPIC: SEAL) Katika 1 Kor. 9:2.

◙ **"mioyoni"** Angalia Mada Maalumu katika 1 Kor. 14:25.

◙ **"arabuni"** Inazungumzia kuhusu vyote viwili yaani malipo kamili wakati ujao pamoja na sehemu ya malipo ya sasa. Malipo ya Mungu ya kwanza yalikuwa uhai wa mwanamke pamoja na uwepo wa Roho wake (kama vile Efe. 1:3-14). Angalia maelezo kamili katika 2 Kor. 5:5.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 2 WAKORINTHO 1:23-24**
**[23] Lakini mimi namwita Mungu awe shahidi juu ya roho yangu, ya kwamba, kwa kuwahurumia sijafika Korintho. [24] Si kwamba tunatawala imani yenu; bali tu wasaidizi wa furaha yenu; maana kwa imani yenu mnasimama.**

**1:23**
**NASB "Lakuni nmwita Mungu kama shahidi kwa nafsi yangu"**
**NKJV 'Zaidi ya Hayo namwita Mungu kuwa shahidi wangu dhidi ya nafsi yangu"**
**NRSV "Lakini namwita Mungu kama shahidi dhidi yangu"**
**TEV "Namwita Mungu kama shahidi wangu anajua moyo wangu"**
**NJB "Kwa maisha yangu namwita Mungu kuwa shahidi wangu"**

Hiki ni kiapo cha hali ya kuwa mkweli. Paulo mara nyingi hutumia viapo kuthibitisha maneno yake (kama vile 2 Kor. 11:11,31; Rum. 1:9; Gal. 1:20; Flp. 1:8; 1 The. 2:5).

◙ **"kuwahurumia"** Shitaka la Paulo Kuhusu mipango ya safari haukuwa mfano wa kutokuwa na msimamo, bali wa upendo wake. Alichagua kutokurudi kwenye mazingira ambavyo chaguo lake lilibadilishwa kuwa hukumu ama ushindani, ugomvi ama ukinzani. Walimu wa uongo walikwisha kutilia shaka nia yake na Matendo ya kale. Paulo anaweka sawa taarifa waliyokuwa wamepewa!

◙ **"sijafika Korintho"** Kuna mjadala mkubwa kuhusu idadi ya safari ambazo Paulo alizifanya kutoka Efeso hadi Korintho na idadi ya barua aliyoandika kwa kanisa la Korintho. Kwa maelezo zaidi tazama utangulizi katika 2 Korintho, D.

**1:24 "Si kwamba tunatawala imani yenu"** Hapa tunaona uwiano kati ya Paulo kama mtume mwenye mamlaka, 1:1, na uhuru wa hili kusanyiko la mahali. Imani ya kibiblia, imani ya Agano, huanza na kukua kuongezeka kwa njia ya maamuzi ya hiari ambayo yamekusudiwa, kuleta furaha, na kukomaa.

◙ **"maana kwa imani yenu mnasimama"** Paulo anataja dhana hii katika 1 Kor. 15:1 (kama vile Rum. 5:2; 11:20). Hii yaweza kuwa na historia ya Agano la Kale (kama vile Zab. 76:7; 130:3; Nah. 1:6; Mal. 3:2; Angalia Mada Maalum katika 1 Kor. 1:9). Inazungumzia imani ya ujasiri katika uwepo wa Mungu. Uwepo wa matatizo katika Korintho ni maelezo ya kutatanisha. Kanisa la Korintho halikuwa limeathiriwa na ujio wa waalimu wa uongo kama makanisa ya Galatia yalivyokuwa. Baadhi ya makanisa ya nyumbani yalikuwa imara na safi (yaani, NJEO YA WAKATI TIMILIFU "mmekuwa na mnaendelea kusimama imara"). Angalia Mada Maalum: Simama (*Histēmi*) [Special Topic: Stand (*Histēmi*) katika 1 Kor. 15:1.

## MASWALI YA MJADALA

Haya ni maoni kuhusu mwongozo wa kusoma, ambao una maana kuwa, unawajibika kwa tafsiri yako binafsi ya Biblia. Kila moja wetu sharti atembee katika nuru tulionao. Wewe, Biblia na Roho Mtakatifu ni kipaumbele katika tafasiri. Usiachie kazi hii kwa mtoa maoni.
Maswali haya ya kujadili yanatolewa kukusaidia mambo muhimu ya kipengele cha kitabu hiki. Yamekusudiwa kukuchokonoa mawazo na sio ya mwisho.

1. Ikiwa Paulo alikuwa anaandika kwa tatizo la mahali katika Korintho, kwanini barua ilikuwa isomwe Achaia yote? (2 Kor. 1:1)
2. Ni faida zipi mbili za kuteseka zilizotajwa katika 2 Kor. 1:4 na 9?
3. Ni matatizo gani ambayo Paulo aliyapata Asia ambayo yalikaribia kumwua? (mst.8-10)
4. Kwanini Paulo alishambuliwa kwa kubadili kwake mipango ya safari? (1Kor. 16:1-8 dhidi ya 2 Kor. 1:12-20)
5. Kwanini tunaamini katika Utatu?

# 2 WAKORINTHO 2

| MGAWANYO WA AYA WA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| UBS[4] | NKJV | NRSV | TEV | NJB |
| Kuahirisha kwa Ziara Ya Paulo | Kulihudumia Kanisa | Uhusiano Mpya na Kanisa | Mabadiliko katika Mipango ya Paulo | Kwa nini Paulo Alibadili Mipango Yake |
| (1:12-2:4) | | (1:12-2:13) | (1:12-2:4) | (1:12-2:11) |
| | 1:15-2:2 | | | |
| 1:13-2:4 | Kumsamehe Mkosaji | 1:23-2:4 | 1:23-2:4 | |
| Wasiwasi ya Paulo Faraja | Furaha ya Ushindi Ndani ya Kristo | | Wasi wasi wa Paulo Pale Troa | Kutoka Troa Kwenda Makedonia Utume Umuhimu Wake |
| 2:12-13 | 2:12-13 | 2:12-13 | 2:12-13 | (2:12-4:6 |
| | | Huduma Yetu | | |
| | | (2:14-3:6) | Ushindi Kupitia Kristo | |
| 2:14-17 | 2:15-17 | 2:14-17 | 2:14-17 | 2:12-3:3 |

**MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI** (kutoka "Mwongozo wa Usomaji Mzuri wa Biblia"(A Guide to Good Bible Reading")

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Haya ni maoni ya mwongozo kwa kujisomea, ikiwa na maana kuwa unawajibika binafsi kwa tafsiri ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mtoa maoni tu.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa,lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

36. Aya ya kwanza
37. Aya ya pili
38. Aya tatu
39. N.k

A. Kuna mjadala mkubwa miongoni mwa wafasiri kuhusu idadi ya ziara alizozifanya Paulo na barua alizoziandika kwa kanisa hili. Sura hii ndio kiini cha mjadala huu kwa sababu inaonekana kurejelea ile barua ya awali na ile ziara yenye maumivu. Kuna utata mkubwa katika vyote viwili yaani andiko na ule ufahamu wetu kuhusu maisha ya Paulo. Ule Mfumo wa Imani wenye mamlaka haufai.

B. Eneo lingine lenye ukinzani linalohusisha sura hii ni aidha mkosaji aliyetajwa katika 2 Kor. 2:5 na 6 ni
   1. mwenye maana ya yule mwanamme aliyefanya uzinzi wa kimbari wa 1 Wakorintho 5

2. kiongozi wa moja ya vikundi vidogo vidogo vya kiutengano au makanisa ya nyumbani yaliyonenwa katika 1 Wakorintho 1-4.
3. Kiongozi wa waasi wa waalimu wa uongo kutoka Yerusalemu waliomkabili Paulo ana kwa ana kuhusiana na ziara hii yenye maumivu 2 Wakorintho 10-13.

C. Mgawanyo wa sura ni dhahiri kuwa haufai. Sura ya 2 lazima iunganishwe na ule mjadala wa mipango ya safari za Paulo zilizotajwa katika 2 Kor. 1:15 na kuendelea.

D. Kuna uwezekano mkubwa wa kuwa na mawazo tofauti ama mwanzo wa utengano katika 2 Kor. 2:14. Paulo harejei katika mjadala wake unaohusu yeye kukutana na Tito kule Makedonia hadi 2 Kor. 7:5. Namshukuru Mungu kwa ajili ya fikra tofauti kwa sababu kunatuonyesha moyo wa Paulo na upendo wake mkuu kwa Yesu Kristo

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : 2 WAKORINTHO 2:1-4**

[1]**Lakini nafsini mwangu nalikusudia hivi, nisije kwenu tena kwa huzuni.** [2]**Maana mimi nikiwatia huzuni, basi ni nani anifurahishaye mimi ila yeye ahuzunishwaye nami?** [3]**Nami naliwaandikia neno lilo hilo, ili nijapo nisitiwe huzuni na wale ambao ilinipasa kuwafurahia; nikiwatumaini ninyi nyote kwamba furaha yangu ni yenu nyote pia.** [4]**Maana katika dhiki nyingi na taabu ya moyo niliwaandikia na machozi mengi; si kwamba mhuzunishwe, bali mpate kujua upendo wangu nilio nao kwenu jinsi ulivyo mwingi.**

**2:1**
**NASB, NKJV "Lakini"**
**NRSV, TEV,**
**NIV, REB "Hivyo"**
**NJB "Hata hivyo"**
**RSV "Kwa maana"**

Kuna tofauti ya Machapisho ya Kiyunani kati ya neno **"kwa**" (yaani, *gar*, kama vile $P^{46}$ na B) na "lakini" (yaani, *de*, kama vile א, A, C, D, F, G). Toleo la $UBS^4$ inatoa daraja"C" likimaanisha hawawezi kuamua. Mara nyingi VIHUSISHI ni muhimu kati ufasiri, lakini katika suala hili maana ya sentensi hufafanua hoja.

**NASB "nafsini mwangu nalikusudia hivi"**
**NKJV "naliliazimia hili rohoni mwangu"**
**NRSV, TEV,**
**NJB "naliitengeneza akili yangu"**

Hii inaonyesha kwamba Paulo hakuwa na utambuzi maalum kutoka kwa Roho kuhusiana na suala hili. Yeye anataja mara kadhaa namna Roho alivyoiongoza mipango ya ziara zake ((kama vile Matendo 16:9-10; 18:21; Rum. 1:10; 15:32; 1 Kor. 4:19), lakini wakati huu hana mwongozo mahsusi na anaamua kutokuja.

◙**"nisije kwenu tena kwa huzuni"** Paulo anatamka ziara ya tatu ya kwenda Korintho katika 2 Kor. 12:14; 13:1. Kitabu cha Matendo hakikuweka kumbu kumbu ya ziara hii ya pili yenye huzuni. Kukaa kwake kwa awali katika Korintho kumenukuliwa katika Matendo 18:1-11. Angalia jedwali lenye utangulizi, tarehe, E. "ziara" C. Bila shaka hili lilitokea kati ya uandishi wa I na 2 Wakorintho.

**2:2"nikiwatia"** Hii ni SENTENSI YENYE MASHARTI DARAJA LA TATU, ambayo inadhaniwa kuwa ya kweli kutokana na mtazamo wa mwandishi ama kwa ajili ya makusudi yake ya kiuandishi. Ziara ya pili ya Paulo ililifanya kanisa kuwa lenye majonzi. Naipenda tafsiri ya NJB ya mstari huu, "

**2:3"Nami naliwaandikia neno lilo hilo"** Kuna nadharia nyingi zinazojaribu kufafanua aya hizi.

1. wengine wanauita huu WARAKA WA WAKATI ULIOPITA USIO TIMILIFU ambao ungalimaanisha kurejelea 2 Wakorintho (kama vile NJB)

2. wengine wanaamini kwamba hili linarejea kwa 1 Wakorintho
3. wengine wanaamini kwamba hili linarejelea ile barua ya awali iliyopotea iliyotajwa katika 1 Kor. 5:9.
4. Wengine wanadhani kwamba hili linarejelea ile barua kali iliyopotea, bila shaka ilihifadhiwa kwa ukamilifu katika 2 Wakorintho 10-13.

**2:4** Kwa uwazi sana aya hii inafunua moyo wa Paulo na hisia za maumivu makubwa aliyoyapata kuhusu kile kilichotokea wakati wa ziara yake yenye maumivu. Bado, alizungumza ukweli, kwa namna maumivu yalivyokuwa. Kama daktari mzuri Paulo alifahamu kwamba wakati mwingine maumivu ni ya lazima kwa ajili ya uponyaji wa muda mrefu.
Paulo alitumia VITENZI TEGEMEZI viwili katika sentensi hii kwa sababu wakaiti mwingine watu hawayaitikii vizuri marekebisho. Mungu amewaumba wanadamu wote wakiwa na utashi ambao ni kitu chenye thamani na cha hatari pia. Hii inabeba uwezo wa furaha na urejesho ama inachukiza na kuendeleza uasi.

**NASB "mwingi"**
**NKJV, NRSV "tele"**
**NJB "jinsi ulivyomwingi"**
Pia aya hii inajumuisha moja ya maneno yanayomtambulisha Paulo anayotumia mara nyingi katika barua zake kwa Wakorintho ( yaani, *perissoterōs*). Angalia maelezo kamili katika 2 Kor. 1:5 ama ile Mada Maalum katika 2 Kor. 2:7.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : 2 WAKORINTHO 2:5-11**
**[1]Lakini nafsini mwangu nalikusudia hivi, nisije kwenu tena kwa huzuni. [2] Maana mimi nikiwatia huzuni, basi ni nani anifurahishaye mimi ila yeye ahuzunishwaye nami? [3] Nami naliwaandikia neno lilo hilo, ili nijapo nisitiwe huzuni na wale ambao ilinipasa kuwafurahia; nikiwatumaini ninyi nyote kwamba furaha yangu ni yenu nyote pia. [4] Maana katika dhiki nyingi na taabu ya moyo niliwaandikia na machozi mengi; si kwamba mhuzunishwe, bali mpate kujua upendo wangu nilio nao kwenu jinsi ulivyo mwingi. [5] Lakini iwapo mtu amehuzunisha, hakunihuzunisha mimi tu, bali kwa sehemu (nisije nikalemea mno), amewahuzunisha ninyi nyote. [6] Yamtosha mtu wa namna hii adhabu ile aliyopewa na walio wengi; [7] hata kinyume cha hayo, ni afadhali mmsamehe na kumfariji, mtu kama huyo asije akamezwa katika huzuni yake ipitayo kiasi. [8] Kwa hiyo nawasihi kumthibitishia upendo wenu. [9]Maana naliandika kwa sababu hii pia, ili nipate bayana kwenu kwamba mmekuwa wenye kutii katika mambo yote. [10] Lakini kama mkimsamehe mtu neno lo lote, nami nimemsamehe; kwa maana mimi nami, ikiwa nimemsamehe mtu neno lo lote, nimemsamehe kwa ajili yenu mbele za Kristo, [11] Shetani asije akapata kutushinda; kwa maana hatukosi kuzijua fikira zake.**

**2:5** Aya hii ni ngumu sana kutafsiriwa! Naamini maana ya toleo la RSV na ile tafsri ya Phillips inaweza kuwa bora zaidi.“lakini ikiwa mtu ye yote amesababisha maumivu,hakuyasababisha kwa ajili yangu, bali kwa kiwango fulani (sikulichukulia kupita kiasi) ni kwenu ninyi nyote.” Hakuna SHAMIRISHO lililotajwa katika sentensi hii, kwa hiyo, wengine hulihusianisha hili na (1) kanisa lote kama vile matoleo ya NKJV, NJB, RSV, Phillips, NIV, NEB) au (2) mtu aliyetenda kosa (kama vile tafsri ya KNOX).

Ni nani “huyu”aliyesababisha matatizo? Kumekuwepo na maoni kadhaa.

1. hili linarejelea ile 1 Kor. 5:9 na mtu yule aliyemwoa mke wa baba yake
2. hili linarejelea mmoja wa viongozi wa waasi wa moja ya yale makundi madogo madogo ya utengano ama makanisa ya nyumbani
3. hili linahusu yule msemaji wa kundi la wale wanaofikiriwa kuwa “viongozi” kutoka Palestina waliomkabili Paulo kuhusu kurudi kwake Korintho na kwa hali iliyo dhahiri kanisa halikumtetea Paulo kama ilivyopaswa kuwa.

◙**"ikiwa"**Hii ni SENTENSI YENYE MASHARTI DARAJA LA TATU. Mtu fulani alikuwa amesababisha huzuni kwa Paulo na kwa kanisa lote. (KAULI TIMILIFU TENDAJI YENYE KUARIFU) na matokeo yalidumu.

**2:6"hii adhabu ile aliyopewa na walio wengi"** Maamuzi hayakuwa ya pamoja. Paulo, aliposhambuliwa, hata kumjali mshambuliaji (kama vile 2 Kor. 2:7) na yale matokeo ya kiroho ambayo yanaweza kusababshwa na ukinzano na makabiliano ((kama vile 2 Kor. 2:11).

Kutajwa kwa "wale walio wengi" kunaonyesha namna Paulo alivyoutazama utawala wa kanisa. Yeye alishindwa kujiita kama Mtume kwa Mataifa, lakini hili halikuundoa ule mwonekano wa kusanyiko juu ya wajibu wa kuongoza. Pauli anao mlinganyo mkubwa katika barua zake kati ya ushurutishi wa kimamlaka (yaani, Wagalati na 1 Korintho), na uhitaji wa uongozi wa mahali. Kitabu cha Agano Jipya kina miundo mitatu ya utawala: ule wa ki-utume (yaani, mamlaka ya ki-askofu); viongozi wa mahari (yaani, chini ya uongozi wa wazee); na ushirika wa pamoja (yaani, kila mwamini). Matendo 15 ina viwango vitatu vilivyohusishwa katika lile tendo la matukio ya siku za mwisho. Hili si jambo lile ambalo mojawapo ni la kibiblia; haya yote ndivyo yalivyo. Hili ni suala la waamini wenye kumcha Mungu kuongoza kwa kufuata mwongozo ulio ndani ya biblia, si agenda binafsi!

**2:7"afadhali mmsamehe na kumfariji"** Hizi zote ni AORIST INFINITIVES. Nidhamu ya kanisa kamwe haiwezi kuwa katika hali ya kutosamehe, bali mara nyingi kuwa ya kiukombozi (Gal. 6:1). Dhambi lazima iwekwe wazi, lakini pia ifunikwe (yaani, kusamehewa na Mungu, kusamehewa na kanisa) baada ya kuwa imewekwa wazi.

Kwa neno "fariji" angalia maelezo kamili katika 2 Kor. 1:4-11.

**NASB "mtu kama huyo asije akamezwa katika huzuni yake ipitayo kiasi"**
**NKJV "kumwezwa na ile huzuni iliyo kuu"**
**NRSV "ili asije akamezwa na huzuni ipitayo kiasi"**
**TEV "ili asije akahuzuka mno na kukata tama kabisa"**
**NJB "anaweza kumezwa na dhiki yake iliyo kuu"**

Kifungu cha kwanza ni cha kifashi " kwa huzuni iliyopita kiasi mtu aweza kumezwa" Angalia Mada Maalum hapo chini. Neno la pili, *katapinō*, pia ni stiari yenye nguvu. Hili kikawaida ni "kugugumia." Hili linatumika katika maana chanya kwenye 2 Kor. 5:4 (yaani, kumezwa kimaisha). Katika hali hasi hili lazima limaanishe kuharibu (kama vile 1 Kor. 15:54; 2 Kor. 2:7; Ebr. 11:29; 1 Pet. 5:8).
Uzoefu binafsi wa Paulo na ufundi wa kitheolojia vilimfanya kuwa na utambuzi zaidi juu ya kina cha dhambi na upana wa neema na huruma ya Mungu. Uchaguzi wake wa maneno unafunua kile kina cha hisia zake.

## MADA MAALUM: UTELE (SPECIAL TOPIC: ABOUND [*perisseuō*] )

**2:8"nawasihi kumthibitishia upendo wenu"** Hii inarejelea juu ya urejesho ama kitendo cha kisheria cha kwa kura maalum (kama vile matumizi ya neno katika Gal. 3:15) ya kanisa kwa njia ya upendo. Inawezekana kuwa hii ni stiari ya ule ukweli wa kitu fulani (kama vile Louw ana Nida, uk. 668).

**2:9"naliandika"** Angalia maelezo katika 2 Kor. 2:3.

◙**"jaribio"**Hii inarejelea jaribio la sarafu za chuma kwa ajili ya kuhakikisha uhalisia wake. Katika kitabu cha Agano Jipya hii inaonekana kuwa na maana nyingine ya "kupima kwa vigezo vya kuuelekea ukubalifu. Angalia Mada Maalum kuhusiana na "Kujaribu" katika 1 Kor. 3:13.

◙**"kwamba mmekuwa wenye kutii katika mambo yote"**Hili lilikuwa jaribu la uaminifu wao kwa utawala wa Paulo. Hili lilikuwa LILE jambo (kama vile 2 Kor. 7:15; 10:6).
Kuna tofauti ya chapisho la Kiyunani inayohusiana na "kwa vyovyote."

1. *ei* - א, C, D, F, G
2. *η* - A, B

3. linaondoa - P[46]

Inaonekana kwamba P[46], inafikiriwa kuwa ya kale sana, na ilifanywa kwa haraka sana, na mara nyingi iliondoa maneno ama vifungu. Kama zilivyo chaguzi nyinginezo, Hizi zilitamkwa sawasawa. Machapisho ya kale ya Kiyunani yaliyo mengi yalinukuliwa na mtu mmoja aliyesoma andiko na wengine kadhaa kuliandika hilo hilo. Hivyo, tofauti kama hii inayohusiana na sauti, ni ya kawaida. Toleo la UBS[4] linatoa uchaguzi #1 lile daraja "A" (yumkini).

**2:10"mkimsamehe"**Neno hili, *charizomai* (kama vile 2 Kor. 2:7,10; 12:13) linatokana na mzizi wa neno *chairō*, ambalo linamaanisha kufurahia, kuwa na shangwe. Katika muktadha huu hili linamaanisha kusamehe kwa neema ama kuachilia (kama vile 2 Kor. 2:7,10 [mara mbili]).
Paulo anawasihi walio wengi kusamehe katika 2 Kor. 2:7 (KAULI YA KITENZI CHA KATI KISICHO NA UKOMO CHA WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFU); katika 2 Kor. 2:10 anaendelea kwa ombi hili endelevu (KAULI YA KATI ELEKEZI YA WAKATI ULOPO); katika 2 Kor. 2:10 anawahakikishia juu ya (yaani, KIWAKILISHI cha nafsi, *egō*) neema yake na msamaha endelevu wa yule mkosaji (KAULI MBILI ZA KATI TIMILIFU ZENYE KUARIFU)

◙**"ikiwa"** Hiii ni SENTENSI YENYE MASHARTI DALAJA LA KWANZA. Paulo anarudia kusema kuhusu msamaha wake binafsi kwa mkosaji.

◙**"kwa ajili yenu mbele za Kristo"** Hii ni njia ya Paulo ya kudai kwamba urejesho wa mtenda mabaya utalitia nguvu kanisa. Yeye binafsi aweza kulifanya hilo kwa sababu ya upendo wake kwa Kristo.

**2:11**
**NASB "Shetani asije akapata kutushinda"**
**NKJV "Shetani asipate manufaa kwa kutushinda"**
**NRSV "ili tusimpe nafasi Shetani atudanganye"**
**TEV "ili kukaa mbali na mkono wa Shetani"**
**NJB "ili kuepuka kushindwa na Shetani"**

Mstari huu unakiri nguvu binafsi ya uovu katika ulimwegu wetu kuzuia mpango wa Mungu . Paulo anamwita huyu kwa majina kadhaa katika 2 Wakorintho.

1. Shetani katika 2 Kor. 2:11; 11:14; 12:7
2. "mungu wa zama hizi (ulimwengu)"katika 2 Kor. 4:4
3. "Beliari" katika 2 Kor. 6:15
4. "yule nyoka" katika 2 Kor. 11:3

Lile neno "sisi" linamrejelea Paulo mwenyewe na kanisa la Korintho. Hili linatia shauku kufahamu kwamba Shetani huwajaribu watu kwa ule uelekeo wa uovu na kwa kupotosha wema. Mwelekeo usio sahihi, kutosamehe, wa hasira, ama wenye mtazamo ya majivuno kwa upande wa kanisa unaweza kufungua mlango wa Shetani kuvuruga kanisa. Angalia MADA MAALUM; UOVU BINAFSI (SPECIAL TOPIC: PERSONAL EVIL) katika 1 Kor. 7:5.

◙**"hatukosi kuzijua fikira zake"** Yule mwovu hujaribu kuyaangamiza maisha yetu (kama vile Efe. 4:14; 6:10-18). Mara nyingi waamini hushindwa kujizuia (yaani, *agnoeō*) katika fikra zake.

MADA MAALUM: MPANGO (SPECIAL TOPIC: SCHEME)

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : 2 KORINTHO 2:12-13**
**[12] Basi nilipofika Troa kwa ajili ya Injili ya Kristo, nikafunguliwa mlango katika Bwana, [13] sikuona raha nafsini mwangu, kwa sababu sikumwona Tito ndugu yangu, bali niliagana nao, nikaondoka kwenda Makedonia.**

**2:12"nilipofika Troa"**Aya hii inafuatia ule mpango wa 1 Kor. 16:5 (Kana vile Matendo 16:8-11). Kwa uwazi kabisa Paulo alishambuliwa na baadhi ya Wakorintho kwa sababu mipango yake ya safari haikutimia. Paulo anajaribu kuelezea sababu.

◙**"nikafunguliwa mlango katika Bwana"**Hii ni KAULI TIMILIFU TENDEWA YENYE HALI YA KUENDELEA inayomaanisha kwamba Mungu aliifungua fursa hii kwa ajili ya injili na kwamba ilibaki wazi! "kufungua mlango" ni stiari maarufu ya Paulo (kama vile 1 Kor. 16:9; Kol. 4:3; na pia ,Matendo 14:27 na Ufu. 3:8).Kifungu hiki kinasistiza nguvu ya Mungu ya utendaji kupitia huduma ya ukombazi wa Masihi na kule kuugua kwa Roho Wake kwa ajili ya uinjilisti na uanafunzi wa Ukristo (kama vile Mt. 28:19-20 na Matendo 15:3-4,12; 21:19). Angalia Mada Maalum katika 1 Kor. 16:9.

**2:13"sikuona raha nafsini mwangu"** Haya ni matumizi ya neno "nafsi" kama lenye ufanano na mtu ama mwanadamu mwenyewe (kama vile 2 Kor. 7:13; 1 Kor. 16:18). Paulo aliendelea kuwa na wasiwasi (KAULI TIMILIFU TENDAJI ELEKEZI) kuhusu Korintho (kama vile 2 Kor. 7:5) fikra za Paulo zilimpa shida; nawe kuwa makini na fikra zako. Yeye aliuacha mlango wazi huko Troa kwa sababu ya kuhusika kwake na woga wake ulihusu kanisa kule Korintho. Paulo alilipenda kanisa hili lenye vikundi vya kimatengano, kanisa lililokuwa na majivuno.

◙**"sikumwona Tito"**Paulo alikuwa amemtuma Timotheo mapema kule Koritho, lakini alionekana kutopokelewa vyema na kanisa kwa hiyo Paulo alimtuma Tito aende na barua kali (kama vile 2 Kor. 2:3-4). Paulo alikuwa hajasikia lo lote kutoka kwake kwa wakati aliotegemea na hivyo akawa na wasiwasi sana.

Tito anatajwa mara kadhaa katika 2 Wakorintho (kama vile 2 Kor. 2:13; 7:6,13,14; 8:6,16,23; 12:18).

MADA MAALUM: TITO (SPECIAL TOPIC: TITUS)

◙**"nikaondoka kwenda Makedonia"** Katika fikra za Paulo kuna mawazo tofauti ambayo yanayoelekea hadi 2 Kor. 7:5. Ni sifa ya kudhikika kwa ajili ya Kristo! Dhiki hii ni nzuri na ya msaada kwamba kwamba tumshukuru Mungu kwa hilo. Nyingi ya nukuu za Paulo zenye kukumbukwa zatokana na kudhikika huku.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : 2 WAKORINTHO 2:14-17**
**14 Ila Mungu ashukuriwe, anayetushangiliza daima katika Kristo, na kuidhihirisha harufu ya kumjua yeye kila mahali kwa kazi yetu. 15 Kwa maana sisi tu manukato ya Kristo, mbele za Mungu, katika wao wanaookolewa, na katika wao wanaopotea; 16 katika hao wa pili harufu ya mauti iletayo mauti; katika hao wa kwanza harufu ya uzima iletayo uzima. Naye ni nani atoshaye kwa mambo hayo? 17 Kwa maana sisi si kama walio wengi, walighoshio neno la Mungu; bali kama kwa weupe wa moyo, kama kutoka kwa Mungu, mbele za Mungu, twanena katika Kristo.**

**2:14 "Mungu ashukuriwe"** Angalia Mada Maalum ifuatayo.

MADA MAALUM: MAOMBI YA PAULO, SIFA NA SHUKRANI (SPECIAL TOPIC: PAULO'S PRAYER, PRAISE AND THANKSGIVING)

◙ **"daima"** Mungu hutuongoza kwa wakati wote (1) kupia Kristo (2) ushindi wa Kristo; na (3) kwa kusudi la ushuhuda (yaani, "kudhirisha kupitaia kwetu" KAULI TENDAJI ENDELEVU YA WAKATI ULIOPO, kama vile 2 Kor. 2:15-16).

**NASB, NKJV "anayetushangiliza daima katika Kristo"**
**NRSV "anayetuongoza daima katika msafara wa ushindi wa Kristo"**
**TEV "Mungu atuongozaye kama wafungwa wake katika msafara wa ushindi wa "Kristo"**
**NJB "ambaye daima hutuleta katika Kristo katika msafara wake wa ushindi"**

Kifungu hiki kinarejelea zoezi la maonyesho ya msafara wa jeshi la Kirumi kwa ajili ya ushindi wa halaiki ya makamanda kupitia mitaa ya Roma, ambalo lilikuwa likisistiza Kristo kama mshindi (kauli ya wakati uliopo endelevu ni UMOJA). Yeye ameangamiza nguvu zote za uadui (kama vile Kol. 2:15, hiki KITENZI kinaonekana katika

mistari hii miwili pekee katika Agano Jipya). Waamini humfuata Yeye, si kama wafungwa ( matoleo ya TEV, NEB, na REB yanalitafsri hili kwa usahihi kama "wafungwa," lakini linakinzana na ule ushindi dhahiri wa muktadha, hadi Paulo aliporejelea yale mateso na unyanyaswaji wake kama mwinjilisti ikilinganishwa na wafungwa walio katika msafara wa Kirumi), lakini kama wanajeshi wenzao! Sisi ni washindi kwa sababu hiyo na kupitia Yeye! Ushindi wetu ni zaidi ya kushinda, lakini yatupasa kuchagua kuudai na kuenenda katika huo kila siku.

◙**"sisi"**Hiki KIWAKILISHI CHA WINGI katika 2 Kor. 2:14-17 inarejelea (1) wale Mitume; (2) Paulo na kundi la watedakazi wake; ama (3) waamini wote ambao wanaieneza injili. Kwangu mimi uchaguzi #2 ni mtazamo, lakini uchaguzi #3 umehusishwa

◙**"kuidhihirisha"** Paulo anatumia neno hili mara nyingi katika 2 Wakorintho (kama vile 2 Kor. 2:14; 3:3; 4:10,11; 5:10,11[mara mbili]; 7:12; 11:6).Hili neno linamaanisha kuonyea wazi ama kufanya jambo lijulikane. Shauku kubwa ya Paulo iilikuwa ni kutimiza, kutangaza, na kumfunua Mungu kupitia mtu wa Kristo na kazi (yaani injili).

◙**"harufu ya kumjua yeye kila mahali"** Kanisa la Korintho lilijivunia urithi wa watu wenye akili sana. Paulo alijivunia maarifa yake yaliyotoka kwa Mungu kupitia Kristo. Maarifa si kwa ajili ya heshima binafsi, bali kwa ajili ya uinjilisti. Kama tulivyo "daima" (yaani, *pantote*) tunaelekea katika shangwe iliyo ndani ya Kristo, sisi pia tunatarajia kufunua kwa usahihi (yaani, kudhihirisha) ule ujumbe wa Kristo "kila mahali" (yaani, *panti*). Injili ya Kristo ya ki-ulimwengu lazima waishiriki wafuasi wake walio washindi wa kila mahali (kama vile Mt. 28:19-20; Luka 24:47; Matendo 1:8).

Paulo anatumia kifungu hiki kidogo "kila mahali" mara nyingi (kama vile 1 Kor. 1:2; 1 The. 1:8; 1 Tim. 2:8). Nashangaa ikiwa hili si dokezo la Mal. 1:11, ambayo inatabiri juu ya kumsujudia Masihi wa Mungu dunia nzima?

**2:15"Kwa maana sisi tu manukato ya Kristo, mbele za Mungu"** Kifungu hiki kina uwezekano wa kuwa na usuli wa aina mbili.

1. Katika Kitabu cha Agano Jipya ule moshi uliotoka katika dhabihu na uvumba ulipanda moja kwa moja kwa Mungu na kukubaliwa kama manukato mazuri (kama vile Mwa. 8:21; Kut. 29:18,25; katika LXX katika Law. 1:9,13,17; 2:2; pia inatumika kistiari na Paulo katika Flp. 4:18)
2. Katika karne ya kwanza uvumba ulifukizwa kando kando ya njia ya gwaride la jeshi la Kirumi huko Roma.

Uenezaji wa injili ni sadaka ya sifa ya YHWH iliyokubaliwa. Waamini wanakubaliwa katika Kristo kwa kusudi la kuwa kama Kristo na kuishiriki injili Yake.

◙**"wanaookolewa, na katika wao wanaopotea"** Tofauti inaonekana kana kwamba wale wanaopotea kwa matendo endelevu ya matakwa yao wenyewe (kauli tendaji endelevu ya wakati uliopo), na wale waliokolewa wanaokolewa kwa mapenzi ya Mungu kupitia Kristo (KUALI TENDEWA ENDELEVU YA WAKATI ULIOPO). Kwa ule umuhimu wa kitheolojia wa aya "wanaokolewa." Angalia **MAALUM: WOKOVU [VITENZI VYA KIYUNANI] (SPECIALA TOPIC: SALVATION [GREEK VERB TENSES])** katika 1 Kor. 3:15.

Kwa dhana ile ya "kupotea" anagalia mjadala kamili wa kitheolojia katika 1 Kor. 1:18, amabao unafanana na andiko.

**2:16"nani atoshaye kwa mambo hayo"** Kuihubiri injili huugawanya ubinadamu milele. Kutokana na 2 Kor. 3:5-6 yatupasa kuelewa kwamba Mungu huwatenga watoto Wake kwa ajili ya jukumu la ushuhuda wa ukuu huu. Kila maisha ya mwamini ni manukato kwa Mungu ambayo wengine huwajibika kwayo, aidha katika kumwamini Kristo ama kumkana Kristo. Maisha tunayoishi ni muhimu; wengine wanayatazama (kama vile 2 Kor. 2:16; 3:2,3).

Kama nilivyosoma mstari huu nafikiri ni mara ngapi na sehemu ngapi nina upendeleo wa kuishiriki injili. Mwingine kamwe hawezi kufahamu nani yupo ama kipi kinaendelea! Baadhi ya hotuba zangu zimefanya vema na nyingine zina kishindo kikubwa! Ni namna gani mpiga mbiu anaweza kusimama na ule uzito ambao msikilizaji wa mtu

mwingine anao na ule uchaguzi wa milele wa kufanya mambo yaliyoegemea katika kile anachokisikia kutoka kwa mwanadamu anenaye? Hawawezi! Huduma ni ya Roho, si mpiga mbiu! Yatupasa kuwa waaminifu katika kuinena injili lakini wajibu wetu wa kiroho una mipaka! Hii ni ijili ya Mungu! Huu ni ulimwengu Wake! Hakuna awezaye kuokolewa bila mguso wa Roho (kama vile. Yohana 6:44,65). Mantiki ya mwanadamu ama ile lugha ya ushawishi si sababu muhimu!

**2:17"sisi si kama walio wengi "** Paulo anarejelea (1) waalimu watembeao katika ulimwengu wa Wagiriki -Waroma ambao wanazunguka kutoka sehemu hadi sehemu wakihubiri na (2) wanafalsafa ambao walilinganishwa na waalimu wa uongo waliokuja kutoka Palestina (kama wale walio katika Gal. 1:6-9) na kumshambulia Paulo, injili yake,na ule utume wake (kama vile 2 Kor. 4:2).

Kuna uhusiano tofauti wa neno "wengi" (MSS א, A, B, C, K, P). MSS ($P^{46}$, D, F, G, L) nyingine za kale zina neno "waliobaki" (NKJV, NRSV tanbihi). Bruce Metzger, *A Textual Commentary of the Greek New Testament*, uk. 577, anasema uchaguzi wa pili ni neno "chukiza" ambalo Paulo asingeweza kulitumia katika muktadha huu. Lile toleo la $UBS^4$ linatoa uchaguzi wa kwanza amabao ni daraja "B" (takariban yumkini).

◙**"walighoshio neno la Mungu"** Hili ni neno linalotokana na kiwanda cha mvinyo. Hili lilitumika katika njia mbili:

1. Kuongeza maji/kufifisha mvinyo ili kuzalisha fedha nyingi zaidi (iyaani, kughushi)
2. kutembeza bidhaa ya mtu fulani kwa ajili ya faida (yaani, mchuuzi)

Paulo hakuubadili ujumbe wake (injili) kwa hadhira zilizokuwa tofauti (yaani, Wayunani, Wayahudi), bali aliboresha mtazamo wake (angalia hotuba za Paulo katika Matendo na usemi wake katika 1 Kor. 9:19-23).

◙**"bali kama kwa weupe wa moyo"** Neno hili linatokana na mzizi "kutochanganywa" (kama vile 2 Kor. 1:12). Hiki kinaweza kuwa kinyume cha neno "kuchuuza." Hili neno adimu linalohusu weupe wa moyo bila shaka ni neno ambatani kutoka "mwanga wa jua" na "mtaalamu." Hili linahusiana na ile dhana ya kile kisichofichika, nia safi (kama vile 1 Kor. 5:8; 2 Kor. 1:12; 2:17; Flp. 1:10; 2 Pet. 3:1). Tambua ufanano kati ya "bali kwa weupe wa moyo" na "bali watoka kwa Mungu."

◙**" neno la Mungu. . . kutoka kwa Mungu. . . mbele za Mungu"** Paulo anaukiri ujumbe wa injili yake ni ujumbe wa Mungu na kwamba huo ujumbe ni Kristo! Paulo anamshukuru Mungu (kama vile 2 Kor. 2:14) kwa:

1. shangwe yetu katika Kristo (kama vile 2 Kor. 2:14)
2. kuthibitisha kwetu maarifa Yake kila mahali (kama vile 2 Kor. 2:14)
3. ujumbe wetu kumhusu Yeye unaoleta uzima ama kifo (kama vile 2 Kor. 2:15-16)
4. ujumbe wetu usiochanganywa unaotoka kwa Mungu, mbele za Mungu, kuhusu Kristo, na katika Kristo (kama vile 2 Kor. 2:17)

◙**"twanena katika Kristo"** Kifungu hiki halisi kimerudiwa katika 2 Kor. 12:19. Inaonekana kuwa njia ya kinahau ya kudai uaminifu wa injili.

## MASWALI YA MJADALA

Haya ni maoni ya <u>mwongozo</u> kwa kujisomea, ikiwa na maana kuwa unawajibika binafsi kwa tafsiri ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mtoa maoni tu.

Maswali haya ya mjadala yametolewa ili kukusaidia wewe kufikiri juu ya masuala muhimu ya kipengere cha kitabu hiki. Yanamaanisha kuwa ya kichokonozi, na sio ya kumalizia

1. Kwa nini Paulo anaijadili mipango ya ziara zake kwa mapana sana?
2. Je! ni barua ngapi alizoziandika Paulo kwa kanisa la Korintho?
3. Eleza usuli wa ile shangwe iliyo katika 2 Kor. 2:14.
4. Je! ni namna gani mtu anasimama na uzito wa kiroho uliohusishwa katika 2 Kor. 2:15-16 tunapofahamu kwamba kuishiriki Injili kunaweza kumaanisha ile tofauti kati ya mbingu na jehanamu

# 2 WAKORINTHO 3

| MGAWANYO WA AYA WA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| UBS[4] | NKJV | NRSV | TEV | NJB |
| Wahudumu wa Agano Jipya | Barua ya Kristo | Huduma yetu | Watumwa wa Agano Jipya | Kutoka Troa mpaka Makedonia |
| | | | | Utume: Umuhimu wake |
| | | (2:14-3:6) | | (2:12-4:6) |
| 3:1-3 | 3:1-3 | 3:1-3 | 3:1-3 | 3:1-3 |
| | Roho, sio barua | | | |
| 3:4-6 | 3:4-6 | 3:4-6 | 3:4-6 | 3:4-6 |
| | Utukufu wa | Huduma ya | | |
| | Agano Jipya | Agano Jipya | | |
| 3:7-11 | 3:7-18 | 3:7-11 | 3:7-11 | |
| 3:12-18 | | 3:12-18 | 3:12-18 | 3:12-1 |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (Kutoka "Mwongozo wa Usomaji Mzuri wa Biblia"("A Guide to Good Bible Reading")

### *KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo wa kusoma fasiri, hii ina maana kwamba unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe kutoka katika Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika nuru tuliyonayo, wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele. Hautakiwi kumuachia vitu hivi mfasiri

Soma Sura kwa mara moja.Tambua masomo yanayozungumzwa. Linganisha mgawanyo wa masomo yako na tafsiri tano hapo juu. Aya zaweza kuwa hazina uvuvio lakini ni msingi kupata au kufuatilia kusudio la asili la mwandishi ambalo ndilo moyo wa tafsiri. Kila aya ina somo moja na somo ni moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya ya tatu
4. Na nyinginezo

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA

**A.** Msisitizo wa Sura hii ni sawa na msisitizo wa kitabu cha Waebrania. Ni ulinganifu kati ya Agano la Kale na Agano Jipya. Namna wanadamu wenye dhambi wanavyopatanishwa na Mungu.
   1. Kutekelezwa kwa Sheria ya Musa
   2. Imani katika kazi ya Mungu ya upatanisho

Ulinganisho huu unatumika na Paulo kulinda Injili yake na yeye mwenyewe dhidi ya walimu wa mafundisho ya uongo wa Kiyahudi waliowasili Korintho.

B. Kutumika kwa neno “roho” katika sura hii kunaleta utata mwingi sana. Kumekuwa na mjadala mkubwa juu ya 2 Wakorintho 3:6, 8, 17 na 18. Je wanahusiana na “Roho Mtakatifu” au dhana ya “ukiroho”? Hapa panaonekana pana hali ya kutotukia kwa makusudi kati ya mawili. Kizazi kipya ni kizazi cha Roho (rejea Yeremia 31:31-34; Ezekieli 36:22-38), kinachoweka rasmi uhusiano wa kiroho kati ya Mungu dhidi ya uhusiano wenye misingi ya utekelezaji iliyo halali.

C. Matumizi ya Paulo ya neno “sheria” (angalia Mada Maalumu katika 1 Wakorintho 9:9)

1. Sheria=ghadhabu; Warumi 3:204:15; Wagalatia 3:10-13; Wakorintho 2:14
2. Sheria=hali nzuri ya kiroho; Warumi 7:14
3. Totauti kati ya Warumi 1:5; 2:13; Wagalatia 3:12; na Warumi. 3:2 au 8:7; 2 Wakorintho 3:6; Wagalatia 3:21
4. Paulo anamtumia Ibrahimu na Musa kama wawakilishi wa uhusiano kati ya “imani” na “sheria”
   Sheria ni nzuri. Inatoka kwa Mungu, na inaendelea kutumikia kusudi la kiungu (rejea Warumi 7:7,12,14,22,25). Haiwezi kuleta amani au wokovu. Katika kitabu cha James Stewart*, A man in Christ,* anaonesha fikra na maandishi yenye mkanganyiko:

“kwa asili ungetegemea mtu anayejipanga mwenyewe kutengeneza mfumo wa mawazo na mafundisho kutengeneza maana za maneno aliyoyatumia kwa uimara kama inavyowezekana. Ungemtegemea kulenga katika ubora wa vifungu vya maneno vya mawazo yanayomuongoza. Ungetamani kwamba neno, mara linapotumika na mwandishi wako kwa maana fulani ingeendelea kumaanisha kitu hicho hicho mpaka mwisho. Lakini kwa kuliangalia hili kutoka kwa Paulo ni kujikatisha tamaa. Vifungu vyake vingi vinaelea wala sio imara…..’Sheria ni takatifu,’ anaandika,’naifurahia sheria ya Mungu kwa namna ya mtu wa ndani’ (rejea Warumi 7:12-13) lakini ni wazi sehemu nyingine ya *nomos* inayomfanya aseme sehemu nyingine ‘Kristo ametukomboa kutoka katika laana ya torati’ (rejea Wagalatia 3:13)” (Ukurasa wa 26).

D. Paulo anatumia ulinganifu mkuu wa aina tatu katika Sura hii
   1. Barua, 2 Wakorintho 3:1-3
      a. Barua za mapendekezo, 2 Wakorintho 3:1
      b. Wao ni barua, 2 Wakorintho 3:2
      c. Meza za Agano la Kale, 2 Wakorintho 3:3
   2. Agano la Kale na Agano Jipya, 2 Wakorintho 3:6-11
      a. Lililoandikwa dhidi ya rohoni, 2 Wakorintho 3:3, 6
      b. Kuua dhidi ya kuhuisha, 2 Wakorintho 3:6
   3. Pazia, 2 Wakorintho 3:7, 12-12
      a. Mussa, 2 Wakorintho 3:12
      b. Wayahudi wa siku za Paulo, 2 Wakorintho 3:14
      c. Waaminio, 2 Wakorintho 3:14-1

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 2 WAKORINTHO 3:1-3**
**[1]Je! Tunaanza tena kujisifu wenyewe? Au tunahitaji, kama wengine, barua zenye sifa kuja kwenu, au kutoka kwenu? [2] Ninyi ndinyi barua yetu, iliyoandikwa mioyoni mwetu, inajulikana na kusomwa na watu wote; [3] mnadhihirishwa kwamba mmekuwa barua ya Kristo tuliyoikatibu, iliyoandikwa si kwa wino, bali kwa Roho wa Mungu aliye hai; si katika vibao vya mawe, ila katika vibao ambavyo ni mioyo ya nyama.**

**3:1** Aina ya Sarufi ya maswali yote katika 2 Wakorintho 3:1 inatarajia jibu la "hapana." Ni ngumu kujua kama Paulo alikuwa anakebehi ama alikuwa amevunjika moyo.
◙**"tunaanza"** Neno hili ni muunganiko wa "kuweka" na "kwa pamoja," linalotumika kiulinganifu kuonesha, kuweka pamoja, au kupendekeza.

1. Kuonyesha (rejea Warumi. 3:5; 5:8; 2 Wakorintho 7:11; Wagalatia 2:18)
2. Kuvumilia (rejea Wakorintho 1:17)
3. Kuanza (rejea Warumi 16:1; 2 Wakorintho 3:1; 4:2; 5:12; 6:4; 10:12,18; 12:11)

◙**"kama wengine"** Paulo anatumia neno hili mara nyingi katika 2 Wakorintho kwasababu ya mgogoro na walimu wachochezi wa uongo kutoka Palestina waliojaribu kujiinua wenyewe kwa kujitofautisha wenyewe na Paulo na historia yake na Injili yake (rejea 2 Wakorintho 4:18; 15:12).

◙**"barua zenye sifa"** Kanisa la kwanza lilipitisha utaratibu wa barua zenye sifa kuwahakikishia wa imani halisi na uaminifu wa wahudumu wa ratiba (Matendo ya Mitume 18:27; Warumi 16:1; 1 Wakorintho 16:3,15-18; Wafilipi. 2:29-30; 3 Waraka wa Yohana 1:12).

**3:2"Ninyi ndinyi barua yetu, iliyoandikwa mioyoni mwetu,"** Paulo anadai kuwa haitaji barua kujidhibitisha mwenyewe kwa kanisa hili (au kutoka katika hili kanisa), kwasababu yeye ndiye muasisi wa kiroho kama Kristo alivyo Mkombozi wake na Bwana. Wao walikuwa barua yake ya damu na nyama (2 Wakorintho 3:3)

Kifungu cha maneno haya "iliyoandikwa mioyoni mwetu" ni KAULI TIMILIFU TENDEWA YA WAKATI UNAOENDELEA. Paulo alilipenda kanisa hili. Walikuwa wa kudumu ndani ya moyo wake na akili. IRABU TENDEWA inamaanisha kwamba Mungu/ Kristo/ Roho ni wakala (2 Wakorintho 3:3), anayezaa upendo wa Paulo.

Angalia MADA MAALUMU: MOYO (SPECIAL TOPIC: THE HEART) katika 1 Wakorintho 14:25.

◙**"inajulikana na kusomwa"** kuna sauti ya kimchezo kati ya maneno haya mawili ya Kiyunani (ambayo ni, *ginōskomenē* and *anaginōskomenē*, rejea 2 Wakorintho 1:13). Zote ni KAULI TENDEWA ENDELEVU YA WAKATI ULIOPO

◙**"na watu wote"** Haya ni matumizi ya neno "wote" ambapo si kwa kujumuisha (rejea Warumi 11:26). Huku kweli ni kutia chumvi, kunatumika sana katika fasihi ya Kiyahudi (rejea Mathayo 5:29-30, 38-42; 6:24; 7:3-5; 23:23-24).

**3:3"mnadhihirishwa"** angalia Angalizo katika 2 Wakorintho 2:14

◙**"mmekuwa barua ya Kristo"** Waaminio wanapaswa kwa kumfunua Kristo kwa uhakika kabisa kwa nia, maneno, na vitendo. Tunavyoishi tunafunua tabia yake!

◙ "**tuliyoikatibu"**Angalia MADA MAALUMU: UONGOZI WA KITUMISHI (SPECIAL TOPIC: SERVANT LEADERSHIP) katika 1 Wakorintho 4:1

◙"**kwa Roho wa Mungu aliye hai"** Neno hili humaanisha Mungu wa Utatu linaelea sana. Roho mara nyingi inamaanisha Roho wa Yesu (rejea Warumi 8:9; 2 Wakorintho 3:17; Wagalatia 4:6; 1 Waraka wa Petro 1:11). Hapa pia ni aina ingine ya kuelea tena inayoelekezwa kwa Baba. Hiki cheo "Mungu aliye hai" lipo katika YHWH, linalotokana na KITENZI cha Kiebrania "kuwa"(rejea Kutoka 3:14). Cheo hiki kinachofunua ni kawaida kwa Baba katika Agano Jipya (rejea Mathayo 16:16; 26:63; Matendo ya Mitume 14:15; Warumi 9:26; 2 Wakorintho 6:16; 1 Wathesalonike 1:9; 1 Timotheo 3:15; 4:10; Waebrania 3:12; 9:14; 10:31; 12:22; Ufunuo 7:2). Katika Agano la kale miungu ya wapagani haikuwa na uhai. Hawakuweza kuitikia au walikuwa wamekufa kwa sehemu ya mwaka (mfano wakati wa baridi) kufuatia mzunguko wa rutuba wa asili. YHWH alikuwa mmoja tu aliyekuwa hai kweli kweli,Mungu aliye hai siku zote!

◙"**si katika vibao vya mawe ila katika vibao ambavyo ni mioyo ya nyama"** hii inataka kufanana na kutolewa kwa sheria katika Kutoka 31:18 na kwenye ahadi ya Agano Jipya (rejea Yeremia 31:31-34 na Ezekieli 36:22-38). Huku ni kutofautiana kwa wazi kati ya Agano la Kale kama sheria ya nje dhidi ya Agano Jipya kama sheria ya ndani (kama moyo mpya, ufahamu mpya na roho mpya, rejea Ezekieli 11:19; 36:26)

> **ANDIKO LA NASB(LILILOBORESHWA): 2 WAKORINTHO 3:4-6**
> **4 Na tumaini hilo tunalo mbele za Mungu kwa njia ya Kristo. 5 Si kwamba twatosha sisi wenyewe kufikiri neno lo lote kwamba ni letu wenyewe, bali utoshelevu wetu watoka kwa Mungu. 6 Naye ndiye aliyetutosheleza kuwa wahudumu wa agano jipya; si wa andiko, bali wa roho; kwa maana andiko huua, bali roho huhuisha.**

**3:4"tumaini"** Hili ni neno lingine la Paulo analolitumia sana katika 2 Wakorintho. Inatoka katika mzizi mmoja kama imani, uaminifu, ujasiri, au kuamini (kama vile *peithō* and *pistis, pisteuō*) kimsingi limaanisha uaminifi, ujasiri au kutumaini.

1. Mazingira chanya
   a. Mipango ya Paulo ya kusafiri, 2 Wakorintho 1:15
   b. Ujasiri wa Paulo katika Mungu kupitia Kristo, 2 Wakorintho 3:4
   c. Ujasiri wa Paulo kwa Tito, 2 Wakorintho 8:22
   d. Ujasiri wa Paulo katika Kristo, Waefeso 3:12
2. Mazingira hasi
   a. Paulo anataka awachukulie kwa upole, 2 Wakorintho 10:2
   b. Hali ya kuchukuliana ya Paulo ukiilinganisha na sifa zake kwa walimu wa uongo, Wafilipi 3:4

**3:5" Si kwamba twatosha sisi wenyewe"** Neno la Kiyunani *hikanos* linatumika katika Agano Jipya na inatumika katika namna mbili.

1. Hali ya ukubwa wa kitu Fulani (2 Wakorintho 11:30), wakati wote
2. Kinachotosheleza vizuri kabisa (2Wakorintho 2:6), bobezi, yenye sifa, inayoweza, au toshelevu
   Namna hii ya tatu inatumika hapa. Paulo anatumia namna yake ya kutostahili akitumia neno hili 1 Wakorintho 15:9. Pia anadai kwamba wahudumu wa Injili hawastahili wao wenyewe katika 2 Wakorintho 2:16 na 3:5
   Hata kama hatujitoshelezi sisi wenyewe, Mungu ametuita na ametutia nguvu kama wawakilishi wake (rejea 2 Wakorintho 3:6; 2 Timotheo 2:2). Utoshelevu wetu upo katika Yeye (rejea 1 Wakorintho 1:12)

◙**"kufikiri"** Hili ni neno *logizomai*, lililotumika mara mara thelathini na nne na Paulo, lakini chini ya mara saba katika sehemu zilizobaki za Agano Jipya(2 Wakorintho 3:5; 5:19; 10:2,7; 11:5; 12:6). Inaakisi mantiki ya uwasilishaji wa Paulo wa kweli na pia kama kutia moyo, kufikiri mambo kwa uzuri.

Neno kwa sehemu kubwa ni la Kithiolojia kwa sababu ya;

1. Matumizi yake katika maandiko ya tafsiri ya Agano la Kale la Kiyunani kwa kweli iliyobinafsishwa (rejea *New International Dictionary of NT Theology*, Toleo la 3, ukurasa wa 823)
2. Matumizi yake katika Mwanzo 15:6, ambayo Paulo anatumia kuhalalisha haki ya Agano la Kale iliyojikita katika zawadi ya bure ya Mungu kupitia imani(rejea Warumi 4:3)
3. Inawezekana limekuwa neno la kiufundi lililotumiwa na wapotoshaji katika mawasilisho yao yenye nia ya kushawishi au kupendezesha (angalia Bruce W. Winter, *Philo and Paul Among the Sophists*)

Waamini wa kisasa wanatakiwa wawe waangalifu pia kuangalia wanachokiamini kuhusu imani na kwanini wanaamini. Uwezo wetu wa mdomo na akili ni sehemu taswira ya Mungu kwa mwanadamu. Lazima tumuabudu Mungu kwa akili zetu (rejea LXX Kumbukumbu la Torati 6:5; Mathayo 22:37). Tunaitaji kuwa na uwezo wa kutoa hesabu ya tumaini letu lililo ndani yetu (rejea 1 Waraka wa Petro 3:15). Lazima tutafakari kwa kuzipitia imani zetu kwa ajili ya kusimama kwetu imara na kwa ajili ya uinjilisti. Angalia video "Why I Trust the NT" mtandaoni katika

**www.freebiblecommentary.org**, bonyeza "Biblical Interpretation Sermons," alafu bonyeza tena Video Seminar, Dallas, TX, 2009" alafu upande wako wa kulia wa kioo angalia somo la tatu ( lesson 3).

**3:6**" **wahudumu wa Agano jipya"** Angalia Mada Maalumu: Uongozi wa Kutumikia katika 1 Wakorintho 4:1.

◙**"si wa andiko,bali wa roho"** Kuna mfululizo wa ulinganisho.

1. Iliyoandikwa dhidi ya kiroho, 2 Wakorintho 3:3 na 6
2. Barua dhidi ya Roho, 2 Wakorintho 3:6
3. Huduma ya Kale dhidi ya huduma ya kiroho, 2 Wakorintho 3:7
4. Huduma yenye muunganiko wa hukumu dhidi ya huduma iliyo na muunganiko wa kusimama vyema, 2 Wakorintho 3:9
5. Yale yaliyopita dhidi ya yale yadumuyo, 2 Wakorintho 3:11
6. Pazia kuinuliwa dhidi ya pazia kuondolewa, 2 Wakorintho 3:14
   Paulo anatofautisha Agano la Kale na Jipya, lakini ukweli imani ya moyo (rejea Warumi 2:29; 7:6) dhidi ya imani ya kichwani (kama vile uhalali, kutekelezwa kibinadamu, hakibinafsi).

◙**"andiko huua"** Hii inataka kufanana na na kusudi la msingi la sheria ya Mussa. Ilitolewa si ihuishe, bali kufanya kuonekana au kufunua hali yetu ya dhambi (rejea Warumi 7:9-11; Wagalatia 3:10). Sheria inaleta hukumu (rejea Warumi 5:13), ghadhabu (rejea Warumi 4:15), na kifo (Warumi 7:19; 2 Wakorintho 3:6). Angalia George E. Ladd's *A Theology of the New Testament*, ukurasa wa 495-510. Nafasi ya sheria pia inaonekana wazi katika Warumi 3:20; 5:20; 10:4; Wagalatia 3:24-25. Uhusiano kati ya Waaminio wa Agano Jipya na Agano la Kale la sheria imekuwa jambo la kuchanganya sana. Inaonekana kwangu, kulingana na vifungu vya habari vya Agano Jipya, kwamba Mkristo hayuko chini ya sheria ya Agano la Kale (rejea Warumi 6:14; Wagalatia 5:18). Hii si kwasababu sheria ya Agano la Kale imepitwa na wakati, lakini kwakuwa Mkristo wa Agano Jipya anatimiza sheria ya Agano la Kale katika uhusiano wa upendo wa Mungu pamoja na sisi tunaoonekana katika upendo wa waaminio kwa wengine (rejea Warumi 13:8-10; Wagalatia 5:14). Kusudi la sheria ni kumleta mwanadamu aliyeanguka kwa Kristo, ili awaokoe wote. Hata hivyo, kwakuwa tu Agano la Kale si njia ya kufikia wokovu haimaanishi kuwa si mapenzi ya Mungu kwa wanadamu katika jamii (rejea Mathayo 5:17; Warumi 8:4). Angalia MADA MAALUMU: MAONI YA PAULO KUHUSU SHERIA YA MUSSA (SPECIAL TOPIC: PAUL'S VIEWS OF THE MOSAIC LAW) katika 1 Wakorintho 9:9.

◙**"roho huuisha"** Mazingira haya hayatoi mwanga wa mbinu za utafsiri! Aya hii haifanani na mbinu za kisarufi ya kihistoria ya Kibiblia ya utafsiri dhidi ya mbinu za kutumia viwakilishi vya ishara. Inahusiana kimsingi kwenye utofauti kati ya kusudi la Agano la Kale na kusudi la Agano Jipya.

Na zaidi sana, nafasi ya imani ya moyoni katika mali za Mungu (rejea Yohana 6:63) dhidi ya kuamini mali za kibinadamu (kama maarifa, kazi, hali za kabila). Msingi ni upendo wa Mungu, kazi ya Kristo, na uwezesho wa Roho. Angalia kuwa kuua kwa barua na kuhuisha kwa Roho zote ziko katika KAULI TENDAJI ELEKEZI YA WAKATI ULIOPO.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 2 WAKORINTHO 3:7-11**
**[7] Basi, ikiwa huduma ya mauti, iliyoandikwa na kuchorwa katika mawe, ilikuja katika utukufu, hata Waisraeli hawakuweza kuukazia macho uso wa Musa, kwa sababu ya utukufu wa uso wake; nao ni utukufu uliokuwa ukibatilika; [8] je! Huduma ya roho haitazidi kuwa katika utukufu? [9] Kwa maana ikiwa huduma ya adhabu ina utukufu, siuze huduma ya haki ina utukufu unaozidi. [10] Maana hata ile iliyotukuzwa haikuwa na utukufu hivi, kwa sababu ya utukufu uzidio sana.[11] Kwa maana, ikiwa ile inayobatilika ilikuwa na utukufu, zaidi sana ile ikaayo ina utukufu.**

**3:7"ikiwa"** Hii ni SENTENSI YENYE MASHARTI DARAJA LA KWANZA, inayokadiriwa kuwa kweli kutoka katika muono wa mwandishi au katika kusudi la maandiko yake.

◙**"huduma ya mauti, iliyoandikwa na kuchorwa katika mawe"** Kusudi la sheria ilikuwa kuonesha hali ya dhambi(rejea Wagalatia 3:24). Sehemu hii, 2 Wakorintho 3:7-18, ni neno la kiualimu *Midrashon* Kutoka 34:23-35. Kuna matumizi ya aina tatu ya kiwakilishi cha "pazia": (1) Mussa; (2) Wayahudi wa leo; (3) Waamini
Agano la Kale limeandikwa kwa kidole cha Mungu katika mawe juu ya Mlima Sinai (rejea Kutoka 19-20). Agano Jipya pia liliandikwa na Mungu, liko katika mioyo ya wafuasi waaminifu(Yeremia. 31:31-34; Ezekieli 36:22-38). La kwanza linatabia ya kufuatwa kwa utii kwa mambo ya nje, lakini la pili, linafuatwa kwa utii wa mahusiano ya ndani.
◙**"ilikuja katika utukufu"** angalia katika 1 Wakorintho 2:7

◙**"hawakuweza kuukazia macho uso wa Musa, kwa sababu ya utukufu wa uso wake; nao ni utukufu uliokuwa"** Hii inafanana na Kutoka 34:30-35. Kumekuwa na mjadala mwingi kuhusu kifungu hiki cha habari. Wengine wanafikiri Musa alifunika uso wake kuzuia Waisraeli kuona utukufu wa muda(rejea 2Wakorintho 3:7, 13). Wengineo, hatahivyo wanafikiri kuwa Musa alifunika uso wake na kitambaa kwasababu Waisraeli hawakuweza kustahimili utukufu wa Mungu kwasababu ya dhambi zao.
**3:8** Mstari huu unapingana na huduma ya Musa, ambayo inaakisi Utukufu wa Mungu pamoja na huduma ya Roho anayetushirikisha utukufu wa Baba.

**3:9"ikiwa"** Hii ni SENTENSI YENYE MASHARTI DARAJA LA KWANZA, inayodhaniwa kuwa kweli kutoka katika muono wa mwandishi au katika makusudi ya kazi zake za uandishi.

◙ "**huduma ya adhabu"** Namna gani mbaya, ya ajabu na kushangaza ya kufunua Agano la Kale hii.

◙**"huduma ya haki"** Agano la Kale lilizalisha hukumu kwa watoto wengi wa Ibrahimu. Agano Jipya linazalisha haki kwa watoto wote wa Adamu ikiwa tu wataamini kazi iliyokwisha kamilika katika Kristo na kuugua kwa Roho. Angalia Mada Maalumu: Haki katika 1 Wakorintho 1:30

◙**"ina"** Hii ni KAULI TENDAJI ELEKEZI YA WAKATI ULIOPO ya *perisseuuō*,inayosisitiza hali yake ya kuendelea. Angalia angalizo kamili katika 2 Wakorintho 1:5 na Mada Maalumu katika 2 Wakorintho 2:7.

**3:10**
**NASB "Kwa kweli, lile lililokuwa na utukufu,kwa namna hii halina utukufu kwasababu ya utukufu unaozidi sana"**
**NKJV "Hata lile lililofanywa kuwa na utukufu halikuwa na utukufu kwa namna hiyo kwa sababu ya utukufu uzidio"**
**NRSV "Kwakweli, iliyo na utukufu hapo mwanzo ilipoteza utukufu wake kwasababu ya utukufu mkuu"**
**TEV "Tunaweza kusema kwamba kwa ajili ya utukufu ug'aao zaidi sasa ule utukufu uliokuwa ukig'aa sana mwanzo umeondoka"**
**NJB "Kwakweli,lile lililokuwa linasemekana kuwa na utukufu limepoteza madai yake yote ya utukufu, kwa tofauti ya utukufu unaopita kawaida"**

Agano la Kale lina tabia ya "kulikuwako na utukufu" (KAULI TENDEWA ELEKEZI YA WAKATI ULIOTIMILIFU). Hakika lilitoka kwa Mungu na lilimuakisi Mungu. Hata hivyo Ufunuo kamili upo katika Kristo, utukufu wa Agano Jipya (KAULI TENDWA TIMILIFU YA HALI YA KUENDELEA). Ulinganifu huu wa maagano ya YHWH pia yameendelezwa katika kitabu cha Waebrania. Angalia MADA MAALUMU:UTUKUFU (AGANO LA KALE) (SPECIAL TOPIC: GLORY (OT) katika 1 Wakorintho 2:7.

KIBAINISHI CHA WAZI "to" (UHUSIKA WA KIIMA, ISIYO NA JINSI,UMOJA) imetumika kama kishikilio sehemu ya sarufi kwa jili ya "agano la kale"(Tafsiri nyingi za Kingereza zina "nini"). Katika mazingira haya limekuwa na tabia kama

1. "kuandikwa katika vibao vya mawe," 2 Wakorintho 3:3, 7
2. "barua," 2 Wakorintho 3:6

3. “huduma ya mauti,” 2 Wakorintho 3:7
4. “huduma ya hukumu,” 2 Wakorintho 3:9

◙**”uzidio”** Hili ni neno la ndani sana kutoka “zaidi” au “kupita kawaida” na “kutupa.” Paulo analitumia hapa na kama katika 2 Wakorintho 9:14(kama “neema ya Mungu izidio”). Pia anatumia yote *perisseuō* na *huperballō* katika 2 Wakorintho 11:23, ambapo analinganisha maisha yake ya nyuma na huduma na sifa za walimu wa uongo. Paulo anazungumza kwa uchungu wa hisia na misamiati yenye kutiwa chumvi! Angalia Mada Maalumu: Matumizi ya Paulo ya *Hupe*r ambatani katika 1 Wakorintho 2:1

**3:11”ikiwa”** Hii ni nyingine SENTENSI YENYE MASHARTI DARAJA LA KWANZA.

◙“**ile inayobatilika”** Hili ni neno *katargeō*,linalotumika mara nyingi na Paulo katika barua zake za Wakorintho(rejea 1 Wakorintho 1:28; 2:6; 6:13; 13:8,10,11; 15:24,26; 2 Wakorintho 3:7,11,13,14). Kwa ajili ya Mada Maalumu angalia 1 Wakorintho 1:28.

◙**” ile ikaayo ina utukufu”** Tofauti si kati ya lile linalotoka kwa Mungu au lenye utukufu wa Mungu, lakini lile lenye utukufu zaidi na linalokaa katika utukufu. Jibu ni Agano Jipya katika Kristo, Kizazi Kipya cha Roho, na mpango mkamilifu wa sasa wa ukombozi wa milele ulioandaliwa kabla (rejea Matendo ya Mitume 2:22-24; 3:18-21; 4:28; 13:29-41).

**ANDIKO LA NASB(LILILOBORESHWA): 2 WAKORINTHO 3:12-18**
**[12] Basi, kwa kuwa mna taraja la namna hii, twatumia ujasiri mwingi; [13] nasi si kama Musa alivyotia utaji juu ya uso wake, ili kwamba Waisraeli wasitazame sana mwisho wa ile iliyokuwa ikibatilika; [14] ila fikira zao zilitiwa uzito. Kwa maana hata leo hivi, wakati lisomwapo Agano la Kale, utaji uo huo wakaa; yaani, haikufunuliwa kwamba huondolewa katika Kristo; [15] ila hata leo, torati ya Musa isomwapo, utaji huikalia mioyo yao. [16] Lakini wakati wo wote watakapomgeukia Bwana, ule utaji huondolewa. [17] Basi ndiye Roho; walakini alipo Roho wa Bwana, hapo ndipo penye uhuru. [18] Lakini sisi sote, kwa uso usiotiwa utaji, tukiurudisha utukufu wa Bwana, kama vile katika kioo, tunabadilishwa tufanane na mfano uo huo, toka utukufu hata utukufu, kama vile kwa utukufu utokao kwa Bwana, aliye Roho.**

**3:12” Basi, kwa kuwa mna taraja la namna hii”** Hii inaonekana kufanana na utukufu wa siku za mwisho (2 Wakorintho 3:11). Angalia MADA MAALUMU: TUMAINI (SPECIAL TOPIC: HOPE) katika 1 Wakorintho 13:13.

◙ “**twatumia ujasiri mwingi katika kunena”** angalia Mada Maalumu hapa chini.

## MADA MAALUMU: UJASIRI (*PARRHĒSIA*) (SPECIAL TOPIC: BOLDNESS *(PARRHĒSIA)*)

3:13 Mstari huu unaturejesha katika mstari wa 7, ambayo ni maelezo kwa Kutoka 34:29-35. Katika Agano la Kale sababu ya Mussa kuvaa kitambaa kwa kuhofia madhara ya kile kilichokuwa kikig’ara usoni mwake kuwaathiri waisraeli (rejea Kutoka 34:30). Paulo anatafsiri sababu ili kuweka mwendelezo wake wa kulishusha Agano la Kale. Kama sura ya Musa ilivyokuwa ya kupita kwa muda tu, pia na agano la Musa!
Paulo anatengeneza ulinganifu kadhaa kati ya Agano la Musa na Agano la Yesu.

1. Bwana wa Kutoka=Roho ya Yesu
2. Ni musa tu ndiye angemsogelea Mungu kwa ukaribu dhidi ya waamini wote katika Kristo wanavyoweza kumkaribia Mungu
3. Utukufu wa Musa ulikuwa wa kitambo tu wakati Utukufu wa Yesu hauwezi kupita kamwe
4. Wafuasi wa Musa hawawezi kumuona Kristo katika Agano la Kale dhidi ya Wafuasi wa Yesu kupitia Roho wanaweza kutafsiri kwa usahihi Agano la Kale katika ufahamu wa Kristo.
5. Mussa alileta kifungo cha utekelezaji wakati Kristo ameleta uhuru wa neema

6. Nyaraka za sheria ya Mussa huleta mauti wakati Roho wa Agano Jipya huleta uhai, maisha ya milele na uhai tele.
7. Agano la Mussa lilishindwa kuzalisha watu wenye haki wakati agano la Yesu linazalisha watu wenye haki (wote wenye kusudi la kuhesabiwa haki na kwa kibinafsi kutakasa)

**3:14"ila fikira zao zilitiwa uzito"** Hiki ni KITENZI TENDEWA ELEKEZI CHA WAKATI ULIOPITA. Neno hili la Kigiriki linatoka katika wazo la "ngozi nzito" au "moyo mgumu" (Marko 6:52; 8:17; Warumi. 11:7, 25). Upofu wa kiroho una asili zote ya kiroho (kama [1] Mungu kwa kutumia IRABU TENDEWA, rejea Isaya 6:9-10; 29:10; Yohana 12:40; Warumi 9:18 na [2] Shetani, rejea 2 Wakorintho 4:4) na asili ya kibinadamu (rejea Yohana 3:19-20). Kwa ajili ya mjadala mzuri wa siri ya kithiolojia ya Waisraeli kufanya ugumu mioyo yao soma Warumi 9-11 na *Hard Sayings of the Bible* from Inter Varsity Press, ukurasa wa 619-621.

KITENZI "huikalia" katika 2 Wakorintho 3:15 inaweza kuwa aidha KAULI TENDWA (kama vile, #1) au WAKATI ULIOPO WA KATI (Kama vile #2
Angalia **MADA MAALUMU: MIKAKATI (SPECIAL TOPIC: SCHEMES)** katika 2 Wakorintho 2:11

◙**"utaji uo huo wakaa"** Musa alitumia kitambaa halisi; neno hili kwa sasa linatumika kuelezea upofu wa ndani wa Dini ya Kiyahudi ya sasa. Wayahudi wali/wanatembea katika hukumu ya Isaya 6:9-10 na 29:10. Hii pia inafanana kwa Wayahudi wa siku za leo wanaokataa kumkubali Yesu kama Masihi (rejea 2 Wakorintho 3:15).

◙**"huondolewa katika Kristo"** Ni neema ya Mungu tu inayoweza kuondoa upofu wa desturi, kujiona wenye haki, na dhambi. Watu wa dini wako hatarini kupata upofu wa kiroho kama ilivyo kwa wasioamini. Tumaini pekee kwa binadamu walioanguka ni

1. Rehema zisizobadilika za baba
2. Kupatanishwa kamili kulikomalizika kwa Mwana
3. Kuugua kwa Roho/Kazi ya Roho ulimwenguni

   Wokovu ni kipawa cha roho na sio suala la familia, desturi, akili, uwezo au upendeleo!

Kile ambacho Paulo anaweza akawa anaeleza katika mazingira haya ni uwezo wa Mwamini kupitia Roho kuona maisha, mafundisho, na kazi ya Yesu katika Agano la Kale. Yesu mwenyewe alifungua ufahamu wa watu wawili kutoka katika kijiji cha Emau wa barabarani (Luka 24:13-35, hasa 2 Wakorintho. 3:25-27).

**NASB, TEV"inaondolewa"**
**NKJV"chukuliwa"**
**NRSV"kuwekwa kando"**
**NJB"inafutwa"**

Angalia Mada Mallumu: *Katargeō* katika 1 Wakorintho 1:28.

**3:15"Mioyo"** Angalia MADA MAALUMU: MOYO (SPECIAL TOPIC: THE HEART) katika 1 Wakorintho 14:25

**3:16" Lakini wakati wo wote watakapomgeukia Bwana, ule utaji huondolewa"** Hii inawezekana ikawa ni nukuu kutoka Kutoka 34:34. Kama ndivyo hivyo inahusiana na vitendo vya Musa kumkaribia Mungu. Inaonekana pia kama wito wa kiujumla wa yeyote na kila mmoja kumgeukia Bwana. Neno "kugeuka" kwa Kiebrania ni *shub* inayomaanisha kutubu. Neno, "Bwana" inaweza kumaanisha mazingira aidha kwa YHWH au kwa Yesu. Utata inawezekana ukawa ni kwa makusudi. Angalia muunganiko wa msisitizo kwenye utashi wa uchaguzi wa binadamu na kitendo cha kiungu (kama vile agano)

**3:17" Basi <Bwana> ndiye Roho"** Huduma ya Yesu na Roho vinaunganishwa bila kuachanishwa (2 Wakorintho3:17). Huduma ya Roho ni ya kumtukuza Yesu (rejea Yohana 16:8-14).

Katika mazingira haya inawezekana Paulo hatoi maoni yake kwenye muunganiko wa Yesu na Roho, lakini anatoa maana ya neno "Bwana" (kurios) katika 2 Wakorintho 3:16, ambayo katika mazingira ya Kutoka 34:34, yanamaanisha YHWH (angalia Mada Maalumu katika 2 Wakorintho 1:1), lakini Paulo analitumia katika maana ya tafsiri ya REB, "kwa hiyo Bwana ambaye habari hii inamzungumzia ni Roho." Kama hii ni sahihi kwahiyo sehemu yote haimzungumzii Yesu kwa neno la "Bwana,"lakini kwa roho (rejea Mwanzo 1:2 pia angalia Gordon D. Fee, *To What End Exegesis*, ukurasa 218-239). Hii kwahiyo ingekuwa ni sehemu pekee ambapo Paulo anatumia *Kurios* kwa ajili ya Roho. Ni tofauti kati ya sheria ya Agano la Kale na ile Injili isiyoandikwa kama iliyoandikwa dhidi ya inayoishi).

**MADA MAALUMU: YESU NA ROHO (SPECIAL TOPIC: JESUS AND THE SPIRIT)**

◙**"penye uhuru"** Hii inamaanisha uhuru kutoka katika upofu wa kiroho, kujihesabia haki, na uhalali wa kisheria unaosababishwa na imani ya uhusiano binafsi na Yesu Kristo(rejea Yohana 8:32,36; Warumi 14: 1 Wakorintho 8; 10:23, Wagalatia 5:1,13).

Mmoja wa watoa maoni ninayempendelea zaidi, F. F. Bruce, in his book, *Paul: Apostle of the Heart Set Free*, anasema

> "Paulo kwa hakika alijua upendo wa Kristo kuwa ndiyo nguvu ya kufanya vyote katika maisha .Palipo na upendo pana nguvu ya uwezesho, hakuna maumivu au migogoro au kifungo katika kufanya kile kilichosawa: mwanaume au mwanamke aliyewezeshwa na upendo wa Yesu na kutiwa nguvu na Roho wake anayafanya mapenzi ya Mungu kutoka ndani ya moyo. Kwakuwa (kama Paulo alivyosema kutika katika uzoefu) 'palipo na Roho wa Bwana, pana moyo ulio huru'" (ukurasa 21).

**3:18 "kwa uso usiotiwa utaji"** Hii ni KAULI TENDWA ENDELEVU YA KUENDELEA inayomaanisha kutotiwa taji kwa kudumu. Pia angalia ujumuisho "sisi sote" ikimaanisha waaminio wa kanisa la Korintho walio katika hali ya kuchanganyikiwa na kutoelewa.

◙**"tukiurudisha utukufu wa Bwana, kama vile katika kioo,"** Injili imefunua kabisa vyote YHWH na Yesu wa Nazareti(rejea 2 Wakorintho 4:6). Tunapoitikia katika toba na imani ufunuo unatubadilisha katika taswira yake. Ulinganifu huu huu unapatikana katika 2 Wakorintho 4:4. Wakorintho hawa wa Korintho walikuwa kwa wazi kabisa wamemuona Mungu ndani ya Kristo kupitia Injili.

Neno "tukiurudisha" ni neno nadra. *The Greek-English Lexicon of the New Testament and Other Early Christian Literature* cha Bauer, Arndt, Gingrich na Danker, anaorodhesha matumizi yanayowezekana yaliyojikita katika sauti (ukurasa wa 424).

1. TENDAJI, inazalisha uaksi
2. TENDEWA, kile kinachoonekana katika kioo
3. KATI, kujiangalia mwenyewe katika kioo

◙**"tunabadilishwa"** Hii ni KAULI TENDWA ELEKEZI YA WAKATI ULIOPO. VITAMKWA vyote katika mazingira haya ni IRABU SAUTI TENDEWA, ikimaanisha vitendo vya Mungu kwa niaba yetu, kuwabadilisha waamini kwenda katika kufanana na Kristo(Warumi 12:2). KITENZI hikihiki kinatumika katika Kugeuzwa (rejea Mathayo 17:2; Marko 9:2). Tunapata neno la kingereza metamorphosis (ugeuzaji kabisa wa umbo au tabia) kutoka katika neno hili la Kiyunani.

◙**"tufanane na mfano uo huo"** Yesu ni sura ya Mungu (rejea 2 Wakorintho 4:4; Yohana 1:14-18; 14:9; Wakolosai 1:15; Waebrania 1:3). Wanadamu waliumbwa kwa sura ya Mungu (rejea Mwanzo 1:26-27). Waaminio ni sura ya Kristo (Warumi 8:29-30). Kufanana na Kristo ni lengo la kwanza la msingi la Mungu kwa waaminio wote (Wagalatia 4:19; Waefeso 1:4).

◙**"toka utukufu hata utukufu"** Kuna hatua katika mpango wa urejesho wa Mungu na kufanywa upya. Waaminio wako katika mchakato (angalia Mada Maalumu katika 1 Wakorintho 3:15) inayopelekea kufanana na Kristo (rejea 1 Waraka wa Yohana 3:2). Angalia Mada Maalumu: Utukufu katika 1 Wakorintho 2:7)

◙**"kwa Bwana, aliye Roho"** baadhi ya tafsiri:

1. King James, "kama kwa Roho wa Bwana"
2. Vulgate, "kama kutoka kwa Bwana(ambaye) ni Roho"
3. Westcott and Hort, "kama kutoka kutoka kwa Roho mwenye uweza wote"
4. Kutoka katika mazingira ya 2 Wakorintho 3:16-17, "kama kutoka kwa Bwana ambaye ni Roho" (rejea TEV, NJB, na NIV)
5. Herufi kubwa ya "R" katika "Roho ikimaanisha Roho Mtakatifu, nafsi ya tatu ya Utatu wa milele (rejea 2 Wakorintho 3:3; Warumi 8:9; Wagalatia 4:6; 1 Waraka wa Petro 1:11)

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni <u>mwongozo</u> wa kujisomea wa fasiri, hii ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika nuru tuliyonayo. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hupaswi kumuachia vitu hivi mfasiri!

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuchokonoa mawazo na sio kutoa maana ya mwisho.

1. Eleza tofauti kati ya Agano la Kale na Agano Jipya?
2. Kwanini Agano la Kale linasemekana kuwa la mauti/ Je inamaanisha kuwa Agano la Kale ni ovu?
3. Kuna uhusiano gani kati ya Agano la Kale na Agano Jipya?
4. Je habari hii inazungumzia Roho Mtakatifu au ulimwengu wa roho?
5. Je ulinganifu wa "pazia/kitambaa" unajaribu kuzungumza nini kwa Wakristo wa siku za leo?

# 2 WAKORINTHO 4

| MGAWANYO WA AYA ZA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **UBS[4]** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB** |
| Hazina katika vyombo vya udongo | nuru ya injili ya Kristo | hazina za kweli wahudumu waharibikao | Hazina za rohoni katika vyombo vya mfinyanzi | Kutoka Troa mpaka Makedonia Utume: Umuhimu wake (2:12-4:6) |
| 4:1-6 | 4:1-6 | 4:1-6 | 4:1-6 | 4:1-6 |
| | Tunatupwa chini Lakini Hatuangamizwi | | | Magumu na Matumaini ya Utume (4:7-5:10) |
| 4:7-15 | 4:7-15 | 4:7-12 | 4:7-12 | 4:7-12 |
| Kuishi kwa Imani | Kuona Visivyoonekana | 4:13-15 | 4:13-15 | 4:13-15 |
| | | | Kuishi kwa Imani | |
| (4:16-5:5) | | | (4:16-5:5) | |
| | 4:16-18 | 4:16-18 | 4:16-18 | 4:16-18 |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (Kutoka "Mwongozo wa Usomaji Mzuri wa Biblia")("A Guide to Good Bible Reading")

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo wa kujisomea wa fasiri, ambao una maana kwamba unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe kutoka katika Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika nuru tuliyonayo, wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele. Hupaswi kumuachia vitu hivi mfasiri.

Soma Sura kwa mara moja. Tambua masomo yanazozungumzwa. Linganisha mgawanyo wa mada zako na tafsiri tano za kisasa hapo juu. Aya hazina uvuvio lakini ni msingi kupata au kufuatilia kusudio la asili la mwandishi ambalo ndilo moyo wa tafsiri. Kila aya ina somo moja na somo ni moja tu.

5. Aya ya kwanza
6. Aya ya pili
7. Aya ya tatu
8. Na nyinginezo

## UTAMBUZI WA KIMUKTADHA

A. Uwasilishaji wa ujumbe, 2 Wakorintho 4:2
B. Kupingwa kwa ujumbe, 2 Wakorintho 4:3-4a
C. Ujumbe unakingwa, 2 Wakorintho 4:4b-6
D. Mkanganyiko wa ujumbe, 2 Wakorintho 4:7-13
E. Matokeo ya ujumbe, 2 Wakorintho 4:14-18

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB(LILILOBORESHWA): 2 WAKORINTHO 4:1-6**
**[1] Kwa sababu hiyo, kwa kuwa tuna huduma hii, kwa jinsi tulivyopata rehema, hatulegei; [2] lakini tumekataa mambo ya aibu yaliyositirika, wala hatuenendi kwa hila, wala kulichanganya neno la Mungu na uongo; bali**

**kwa kuidhihirisha iliyo kweli twajionyesha kuwa na haki, dhamiri za watu zikitushuhudia mbele za Mungu. 3 Lakini ikiwa injili yetu imesitirika, imesitirika kwa hao wanaopotea; 4 ambao ndani yao mungu wa dunia hii amepofusha fikira zao wasioamini, isiwazukie nuru ya injili ya utukufu wake Kristo aliye sura yake Mungu. 5 Kwa maana hatujihubiri wenyewe, bali Kristo Yesu ya kuwa ni Bwana; na sisi wenyewe kuwa tu watumishi wenu kwa ajili ya Yesu. 6 Kwa kuwa Mungu, aliyesema, Nuru itang'aa toka gizani, ndiye aliyeng'aa mioyoni mwetu, atupe nuru ya elimu ya utukufu wa Mungu katika uso wa Yesu Kristo.**

**4:1"Tu.."** Ni wazi kwamba Paulo anatumia KIWAKILISHI CHA WINGI kujimaanisha yeye mwenyewe, kama afanyavyo katika sura nzima.

◙**"tuna huduma hii"** Paulo anamaanisha "huduma ya Roho" (rejea 2 Wakorintho 3:8), pia inaitwa "huduma ya haki" (rejea 2 Wakorintho 3:9). Paulo anatumia neno hili kwa ajili ya huduma, *diakonia,* mara nyingi katika 2 Wakorintho.

1. *diakonēo*, 2 Wakorintho 3:3; 8:19,20
2. *diakonia*, 2 Wakorintho 3:7,8,9; 4:1; 5:18; 6:3; 8:4; 9:1,12,13; 11:8
3. *diakonos*, 2 Wakorintho 3:6; 6:4; 11:15,23

Wakristo wameokolewa kuhudumu (rejea Waefeso 2:10). Ukristo sio "kuna nini kwa ajili yangu" weka shabaha kwamba "naweza kufanya nini kwa ajili ya wengine kwasababu Kristo alifanya hivyo kwa ajili yangu" weka shabaha. Paulo alitumikia na aliitwa kwa ajili ya huduma (rejea Wagalatia 2:20). Angalia MADA MAALUMU: UONGOZI WA KUTUMISHI (SPECIAL TOPIC: SERVANT LEADERSHIP)) katika 1 Wakorintho 4:1

◙**"kwa jinsi tulivyopata rehema"** Rehema za Mungu kwa Paulo aliyekuwa kikwazo kikubwa, anayetumia nguvu ya jeshi, mpinga wakristo (rejea 1 Timotheo 13, 16), njiani Dameski (KITENZI TENDEWA ELEKEZI CHA WAKATI ULIOPITA USIO TIMILIFU) alimtia moyo kuendelea kuhubiri habari njema mbele kwa kukabiliana na hali ngumu.

Paulo aliandika kwa Kiyunani, lakini alifikiri kwa Kiebrania. Neno la Kiyunani *eleeō* (kama vile rehema, huruma na kujali) inatumika katika maandiko ya tafsiri ya Agano la Kale la Kiyunani kutafsiri neno la Kiebrania *hesed* (angalia Mada Maalumu katika 1 Wakorintho 13:1), ambayo inahusiana na uaminifu wa agano. YHWH ni mwaminifu kwa ahadi za agano lake, hata pale ambapo mwanadamu sio! Kule kuongoka kwa Paulo kunaonesha vizuri kuhusu huruma ya Mungu. Anatenda rehema kwa Wayahudi (rejea Warumi 9:15, 16,18,23-24; 11-30) na kwa Mataifa (rejea Warumi 11:32) kwa ajili ya kusudi la agano lake yeye mwenyewe ambalo ni kurejeshwa kwa sura yake kwa mwanadamu kupitia kazi ya Kristo na huduma ya Roho. Uaminifu wa Mungu kwa agano lake na tabia yake ya rehema ya kutobadilika ni tumaini pekee kwa mwanadamu.

◙**"hatulegei"** Hii ni KAULI TENDAJI ELEKEZI YA WAKATI ULIOPO. Hii lazima ieleweke katika ufahamu wa huduma ya Paulo kwa ujumla wake na hasa katika muktadha huu (2 Wakorintho 4:16). Paulo alijisikia kukata tamaa mara kadhaa. Yesu alimtokea katika maono mara kadhaa kwa ajili ya kumtia moyo (rejea Matendo ya Mitume 18:9-10; 23:11; 27:24; 2 Timotheo 4:17). Na katika muktadha huu, kwa kukabiliana na majaribu na matatizo na kanisa pale Korintho, Paulo alikuwa na ujasiri kwamba mwenye rehema, Mungu wa maagano alikuwepo na alikuwa akihusika na yote (rejea 2 Wakorintho 3:12). Kazi ilikuwa ya muhimu sana kiasi cha kutokuikatia tamaa (Mathayo 28:19-20; Luka 24:47; Matendo ya Mitume 1:8).

**4:2" tumekataa"** Hiki ni KITENZI TENDAJI CHA KATI ELEKEZI. Kuna mfululizo wa vitu ambavyo Paulo mwenyewe anakataa kutumia katika huduma yake mwenyewe.

1. Hakuna mambo ya uongo
2. Hakuna mbinu za kujidhalilisha
3. Hakuna dhuluma
4. Hakuna kuchezea au kupuuzia ujumbe wa Mungu
   Kila moja ya mbinu hizi zinaakisi tuhuma za walimu wa uongo au matendo yao

**NASB"vitu vilivyofichwa kwasababu ya aibu"**
**NKJV"Vitu vilivyofichwa vya aibu"**

**NRSV"matendo ya aibu ambayo mtu huficha"**
**TEV"siri na matendo ya aibu"**
**NJB"usiri wa aibu"**
Paulo anatumia vifungu vya maneno hayohayo kuelezea utumwa wa dhambi katika Warumi 6:21 na dhambi za mwanadamu ambazo zitafunuliwa katika 1 Wakorintho 4:5 (pia angalia 1 Wakorintho14:25). Katika muktadha huu vifungu vya maneno vinaonekana kuelezea mbinu za walimu wa uongo.

**NASB, NKJV"bila kutembea katika dhuluma"**
**NRSV"tunakataa kufanya kazi kwa ujanja ujanja"**
**TEV"hatutendi kwa udanganyifu"**
**NJB"si namna yetu kuwa waovu"**
Hii ni KAULI TENDAJI ENDELEVU YA WAKATI ULIOPO. Paulo anatumia neno "dhuluma" (kama vile "yote" na pia "kazi") mara kadhaa katika barua zake kwa Korintho (rejea 1 Wakorintho 3:19; 2 Wakorintho 4:2; 11:3;12:16). Lazima tuwe makini na mbinu zetu na vilevile malengo yetu. Kwakuwa katika Ukiristo njia inaamua mwisho. Neno hilohilo linatumiwa na Paulo.

1. Katika nukuu kutoka Ayubu 5:13 ikimaanisha hekima ya kibinadamu (1 Wakorintho 3:19)
2. Shetani kumjaribu Hawa (rejea 2 Wakorintho 11:3)
3. Mbinu za uongo wa shetani na walimu wa uongo (rejea Waefeso 4:14)
4. Mbinu za hapa za walimu wa uongo

**NASB"au kwa kulikuza neno la Mungu"**
**NKJV"si kwa kushika neno la Mungu kwa dhuluma"**
**NRSV"kulifanya neno la MUngu kuwa uongo"**
**TEV"Na wala hatujaribu kulifanya neno la Mungu uongo"**
**NJB"au kulifanya neno la Mungu kuwa uongo"**

Hili neno na aina zake zinazofanana linamaanisha

1. Kupuuza (rejea 2 Wakorintho 2:17)
2. Kutegwa kwa chambo (rejea Mathayo 26:4; Marko 14:1)
3. Kuhongwa au kudanganywa (rejea 2 Wakorintho 11:13; Warumi 3:13)

Inamaanisha ujumbe unaobadilika kulingana na usikivu wa wasikilizaji au kujaribu kuwarubuni wasikilizaji (1 Wakorintho 1:23).

**NASB"Kwa udhihirisho wa kweli"**
**NKJV" Kwa udhihirisho wa kweli"**
**NRSV"Kwa kauli ya wazi ya ukweli"**
**TEV"Katika ufahamu kamili wa kweli"**
**NJB"Kwa kuonesha ukweli kwa uwazi"**
Kwa ajili ya "udhihirisho" angalia angalizo kamili katika 2 Wakorintho 2:14. Neno kweli lina KIBAINISHI na linamaanisha Injili ya Kristo, Agano Jipya. Walimu wa uongo walifanya vitendo kwa njia ya aibu, njia za siri, lakini Paulo alihubiri kweli kamili hadharani. Angalia MADA MAALUMU:"UKWELI" KATIKA MAANDIKO YA PAULO (SPECIAL TOPIC: "TRUTH" IN PAUL'S WRITINGS) katika 2 Wakorintho 13:8.

◙**"dhamiri za watu zikitushuhudia mbele za Mungu"** Paulo anamaanisha ukomo wake binafsi wa upendo wake yeye mwenyewe kwa wengine (1 Wakorintho 9:19-23). Hii haimaanishi kujichanganya kuacha imani bali kwa hiari yake mwenyewe akijizuia uhuru kwasababu ya kutojichanganya na mila au upendeleo wa wengine. Kusudio lake ilikuwa ni uinjilisti na sio uhuru wake binafsi (rejea Warumi 14:1-15:13; 1 Wakorintho 8:10:23).

Paulo anayatumia maneno haya haya katika 2 Wakorintho 5:11-21 ambayo yanasisitiza Injili na sehemu yetu katika kuitangaza. Angalia angalizo kamili kuhusu "kushuhudiwa" katika 2 Wakorintho 3:1. Angalia angalizo kamili kuhusu "dhamiri" katika 1 Wakorintho 8:7 na 10:25.

◙**”mbele za Mungu”** Hii imekaa kama kifungu cha maneno cha nahau sambamba na “Mungu ni shahidi yangu.” Katika maandiko mengine ya Paulo anatumia maneno haya kwa njia hii hii (rejea Wagalatia 1:20; 1 Timotheo 5:21; 6:13; 2 Timotheo 2:14; 4:1), lakini tazama kanuni ya kiapo cha Paulo katika 2 Wakorintho 1:23; 11:31; na 1 Wathesalonike 2:5, 10).

**4:3”ikiwa”** Hii ni SENTENSI YENYE MASHARTI DARAJA LA KWANZA, ambayo inadhaniwa kuwa kweli. Baadhi ya watu hawaielewi (rejea Mathayo 13)

◙**”injili yetu imesitirika”** Hii ni KAULI TIMILIFU TENDWA ENDELEVU YENYE MAFUMBO ya “kusitirika” (rejea 2 wakorintho 3:14, 16). Ni wazi kwa Paulo kwamba alipohubiri Injili baadhi ya watu hawakuitikia hata kidogo. Kama ilivyo kuwa Wayahudi wamekuwa “wagumu” (rejea 2 Wakorintho 3:14; na Isaya 6:9-10), wasikiaji wa kila kizazi pia “wamepofushwa” (rejea 2 Wakorintho 4:4). Hii ni siri ya kuamuliwa kabla na utashi huru, mkanganyiko wa injili (rejea Yohana 1:12; 3:16 dhidi ya Yohana 6:44,65).

◙ “**hao wanaopotea”** Paulo anaendelea na mfanano wake wa Injili kama manukato ya Uzima na mauti (rejea 2 Wakorintho 2:15; 1 Wakorintho 1:18-19; 8:11; 10:9-10; 15:18). Kutangaza Injili ni suala nyeti sana, kwa wengine uhai lakini kwa wengine ni mauti.
Kwa dhana ya “wanaopotea” angalia Mada Maalumu katika 1 Wakorintho 8:11 na mjadala katika 1 Wakorintho 1:18

**4:4”mungu wa dunia hii”** Sifa hii ya uovu imetajwa kwa majina kadhaa na Paulo.

1. Shetani (rejea Warumi 16:20; 1 Wakorintho 5:5; 7:5; 2 Wakorintho 2:11; 11:14; 12:7; 1 Wathesalonike 2:18; 2 Wathesalonike 2:9; 1 Timotheo 1:20; 5:15).
2. Muovu (rejea Waefeso 4:27; 6:11-12; 1 Timotheo 3:6,7; 2 Timotheo 2:26; WINGI unatumika kipepo, 1 Wakorintho 10:20-21; 1 Timotheo 4:1)
3. “mkuu wa nguvu za anga” (rejea Waefeso 2:2)
4. “mungu wa kizazi hiki/dunia” (Yohana anamuita “mtawala wa kizazi hiki/dunia,” Yohana 12:31; 14:30; 16:11)
5. “mjaribu” (rejea 1 Wathesalonike 3:5)
6. “yule muovu” (rejea 2 Wathesalonike 3:3, cheo hiki kimepatikana sana katika maandiko ya Mathayo na Yohana)
7. “malaika wa nuru” (rejea 2 Wakorintho 11:14)

Mstari huu umesababisha kuwekewa umakini sana na Mababa wa Kanisa la kwanza kwasababu ulionekana kuchochea moto wa kwa walimu wa uongo akina Gnostic na Arian. Kwahiyo kwa bahati mbaya, wao (Irenaeus, Tertullian, Origen, Chrysostom, Ambrose, Theodoret, na Augustine) wakabadilisha Kiyunani cha andiko hili kuwa: “ambao Mungu amewapofusha akili zao wasioamini wa dunia hii.” Sasa shetani anatajwa kwa uwazi kama mfalme na nguvu ya dunia hii (Yohana 12:31; 14:30; Waefeso 2:2). Mababa wa Makanisa haya hawakuwa wanafanya hivyo kwa dhana ya nguvu binafsi ya uovu, bali kwa dhana ya kithiolojia ya Gnostic Demiurge na mawazo ya Arian yaliyokuwa yanashusha uungu wa Kristo. Angalia MADA MAALUMU: UOVU BINAFSI (SPECIAL TOPIC: PERSONAL EVIL) katika 1 Wakorintho 7:5

◙**”wa dunia hii”** Hili pia ni neno la Kiyunani kwa ajili ya “kizazi” (kama vile *aiōnos*) Hii inaonekana kumaanisha namna Wayahudi wanavyomaanishwa vizazi viwili: kizazi cha sasa kilichojaa dhambi na kizazi kijacho, kuandaliwa na kutawaliwa na Mesiya (Mathayo 28:20; Waefeso 2:2). Kwa ajili ya mjadala mpana wa vizazi viwili angalia Mada Maalumu katika 1 Wakorintho 1:20. Maneno “dunia hii” (*kosmos houtos*) na "kizazi hiki" (*aiōn houtos*) yanatumika kwa pamoja kwa kubadilishana (rejea George E. Ladd's *A Theology of the New Testament*, ukurasa wa 223).

◙**”amepofusha fikira zao wasioamini”** Hii ni KAULI TENDAJI ELEKEZI YA WAKATI USIOTIMILIFU. Neno hutumika katika upofu wa kiroho katika Mathayo 15:14; 23:16; 1 Waraka wa Yohana 2:11 na dhana ipo katika Yohana 9. Neno hilihili limetumika katika kunukuu kutoka katika maandiko ya tafsiri ya Agano la Kale ya Kiyunani ya Isaya

6:10 katika Yohana 12:40. Ni neno nadra katika maandiko ya Paulo (rejea Warumi 2:19 na hapa), lakini lipo sana katika vitabu vya Injili.

Katika habari ya Isaya (kama vile 6:9-10) ni hukumu ya Mungu iliyowapofusha macho ya kiroho ya Waisraeli kwasababu ya kuendelea kwao kutokuamini. Ukweli huu huu unaelezwa katika Warumi 1:21, ambapo IRABU SAUTI TENDEWA inamaanisha Mungu (rejea Warumi 11:8-10, nukuu Isaya 29:10 na Zaburi 69:22-23). Ni ngumu kuweka usawa

1. Hali ya kutokuamini ya kibinadamu
2. Kufanywa ugumu kiungu
3. Kupofushwa kishetani

Kuamini ni kipawa na mwitikio muhimu! Mkanganyiko wa kimaagano ni siri iliyoamuliwa na utashi huru. Lazima tumuache Mungu awe Mungu na tutake kuwajibika kibinadamu. Angalia MADA MAALUMU: KUCHAGULIWA/KUAMULIWA KABLA NA UHITAJI WA ULALI WA USAWA WA KITHIOLOJIA (SPECIAL TOPIC: ELECTION/PREDESTINATION AND THE NEED FOR A THEOLOGICAL BALANCE)

Unaweza kuwaza nguvu ambayo Yule muovu ambayo lazima anayo kiasi kwamba ana uwezo wa kupofusha macho ya binadamu kwa nguvu ya ushawishi ya kupendeza ya injili (rejea Mathayo 13:19) na kuugua kwa Roho Mtakatifu ili kufanya kuiitikia (rejea Yohana 6:44, 65)? Paulo anatumia ulinganifu kadhaa kuelezea hali ya kutokuamini: (1) mioyo migumu; (2) ufahamu uliopofushwa; (3) dhamiri ziwakazo; na (4) macho yaliyopofushwa. Kuna mgogoro wa kiroho unaoendelea (rejea Waefeso 6:10-19).

**NASB"ili kwamba wasione nuru ya Injili ya utukufu wa Kristo"**
**NKJV"isije nuru ya injili ya utukufu wa Kristo….ikawaangazia"**
**NRSV"kuwakinga wasione nuru ya injili ya utukufu wa Kristo"**
**TEV"Anawakinga wasione nuru ikiwazukia, nuru inayokuja kutoka kwa habari njema ya utukufu wa Kristo"**
**NJB"ili kwamba wasione nuru ig'aayo ya injili ya utukufu wa Kristo"**

Kama utagundua katika muktadha huu, yako maneno kadhaa ambayo yanafanana na nuru. Hii inamaanisha

1. Yesu, mara nyingi aliita "nuru" (rejea Yohana 1:4, 9; 3:19; 8:12)
2. Yawezekana ile hali ya Paulo alokutana nayo njiani akienda Dameski (rejea Matendo ya Mitume 9)
3. Yawezekana maelezo kwa *Shekinah* utukufu wa Mungu kutoka Kutoka kunakotajwa katika 2 Wakorintho 4:6; 3:7)

Kutomuona Kristo katika maandiko ni kuukosa wokovu. Agano Jipya linatangaza utukufu wa Kristo, Injili. Agano la Kale linatimizwa na kukamilishwa katika Yeye. Yeye ni msingi muhimu,jiwe kuu la pembeni, jiwe la msingi, jiwe la juu. Kumkosa yeye ni sawa na mtu kupatwa dhoruba ya imani yake.

◙**"aliye sura yake Mungu"** Kumuona Yesu ni kumuona Baba (rejea Yohana1:18; 14:8,9; Wakolosai 1:15; Waebrania 1:3). Agano Jipya linaeleza kwamba Yesu alivaa mwili ili kutumikia makusudi matatu.

1. Kumfunua Baba kiukamilifu
2. Kupatanisha dhambi
3. Kuwapa waaminio mfano wa kufuata

**4:5" hatujihubiri wenyewe"** Kujaribu kutafsiri barua ya Paulo ni kama kusikiliza nusu tu ya mazungumzo ya simu. Tunadhani kutoka katika kauli za Paulo vitu ambavyo vinaweza kuwa vilisababisha. Kutoka 3:1, hapa na sura za 10-13 ni wazi kuwa Paulo alikuwa nao Korintho wale waliomshambulia binafsi na injili yake. Paulo kwa nguvu anakiri u-Bwana wa Yesu na utumishi wake (rejea 1 Wakorintho 3:5-9). Anajilinda tu yeye mwenyewe (kama vile "sisi wenyewe" ni ya nguvu) au anakuza sifa zake(rejea sura ya 12) kwa ajili ya kulinda mamlaka ya injili yake. Kwa ajili ya majadiliano mazuri kuhusu ukomo wa mamlaka ya utume angalia George Ladd's *A Theology of the New Testament*, ukurasa wa 382.

◙**"Kristo Yesu ya kuwa ni Bwana"** kifungu hiki cha maneno kilikuwa ndiyo kauli ya imani ya kanisa la kwanza katika ubatizo (rejea Warumi 10:9-13; 1 Wakorintho 12:3; Wafilipi 2:9-11). Yote matatu yalitumika katika agano Jipya kumhalalisha Yeye Aliyeahidiwa, Mtumwa aliye katika mateso, yanatumika katika kifungu hiki cha maneno.

1. Kristo – Hili ni Kiyunani sawa na neno la Kiebrania *messiah,* linalomaanisha "aliyepakwa mafuta". Linamaanisha "aliyeitwa na Mungu na kuwezeshwa kwa ajili ya kusudi fulani". Katika makundi matatu ya viongozi katika Agano la Kale yaani : makuhani, wafalme, na manabii walipakwa mafuta. Yesu alitimiza ofisi zote tatu za kutiwa mafuta (rejea Waebrania 1:2-3)
2. Yesu – Hili jina la Kiebrania lina maanisha "YHWH anaokoa" au "YHWH analeta wokovu". Ilifunuliwa kwa wazazi wake na malaika (rejea Mathayo 1:21). "Yesu" linatoka katika neno la Kiebrania kwa ajili ya wokovu, *hosea,* likiwa na viambishi tamati kwenye jina la agano kwa Mungu, "YHWH". Ni sawa na jina la Kiebrania la Yoshua.
3. Bwana – neno "bwana" *(kurios)* linaweza kutumika kwa namna ya kiujumla au katika namna fulani maalumu ya kithiolojia. Inaweza kumaanisha "bwana," "mheshimiwa," "mkuu," "mmiliki," "mume," au "mtu kamili wa Mungu." Matumizi ya Agano la Kale ya neno hili *(adon*) lilitokana na hali ya kustarehe ya Wayahudi kutangaza jina la agano la Mungu, YHWH (angalia Mada Maalumu katika 2 Wakorintho 1:1), lililokuwa linatoka katika KITENZI "kuwa"cha Kiebrania (rejea Kutoka 3:14). Walikuwa na hofu ya kuvunja amri ambayo ilisema "hutolitaja jina la Bwana Mungu wako bure" (rejea Kutoka 20:7; Kumbukumbu la Torati 5:11). Walifikiria ikiwa hawakulitaja, basi hawakulitaja bure. Kwahiyo, wakatafuta jina mbadala la kutoka Kiebrania, *Adonai* ambalo lilikuwa na maana sawa ikimaanisha neno la Kiyunani, *Kurios* (Bwana). Waandishi wa Agano Jipya walilitumia hili neno kuelezea uungu kamili wa Kristo.

Kuna vifungu vya maneno kadhaa vya ukiri vilivyotumiwa na Yesu.

1. Yesu ndiye Masiya/Kristo – Matendo ya Mitume 5:42; 9:22; 17:3; 18:5,28; 1 Wakorintho 1:23
2. Yesu ni mwana wa Mungu – Matendo ya Mitume 9:20; Warumi 1:3-4; Waebrania 4:14
3. Yesu ni Bwana – Matendo ya Mitume 2:36; 10:36; 11:20; Warumi 10:9; 2 Wakorintho 4:5; Wafilipi 2:11; Wakolosai 2:6

Kwa namna fulani haya yanajumuisha uelewa wa kanisa la kwanza la Yesu wa Nazareti.

**4:6"Kwa kuwa Mungu aliyesema, Nuru itang'aa toka gizani"** Haya ni maelezo kwa Mwanzo 1:3 na maelezo binafsi hali aliyokutana nayo Paulo njiani akielekea Dameski (rejea Matendo ya Mitume 9:1-22; 22:3-16; 26:9-18). Kwa Petro aina hii hii ya kufunuliwa baada ya kupita mto Yordani kuingia katika nchi ya Ahadi. YHWH anajulikana vizuri sana, sio kwa kuona, wala kwa mwili, lakini katika Yesu, kufanyika mwili kwa kiungu. Angalia <u>MADA MAALUMU: UTUKUFU (AGANO LA LAKE (SPECIAL TOPIC: GROLY (OT)</u> katika 1 Wakorintho 2:7.

◙**"uso wa Yesu Kristo"** Huuni mwendelezo wa kulinganisha kati ya kitambaa cha Mussa (rejea 2 Wakorintho 3:130 na kuaksiwa kamili kwa Yesu Kristo (rejea Waebrania 1:3). Waaminio wameona utukufu wa Yesu Kristo katika injili (rejea 2 Wakorintho 3:18).

**ANDIKO LA NASB(LILILOBORESHWA): 2 WAKORINTHO 4:7-12**
**[7] Lakini tuna hazina hii katika vyombo vya udongo, ili adhama kuu ya uwezo iwe ya Mungu, wala si kutoka kwetu. [8] Pande zote twadhikika, bali hatusongwi; twaona shaka, bali hatukati tamaa; [9] twaudhiwa, bali hatuachwi; twatupwa chini, bali hatuangamizwi; [10] siku zote twachukua katika mwili kuuawa kwake Yesu, ili uzima wa Yesu nao udhihirishwe katika miili yetu. [11] Kwa maana sisi tulio hai, siku zote twatolewa tufe kwa ajili ya Yesu, ili uzima wa Yesu nao udhihirishwe katika miili yetu ipatikanayo na mauti. [12] Basi hapo mauti hufanya kazi ndani yetu, bali uzima ndani yenu.**

**4:7"lakini tunazo hazina"** Hii inamaanisha Roho wa Mungu akaaye ndani yetu anaye kuza, kufunua, na kumtengeneza mtu wa Kristo katika maisha yetu (rejea Yohana 16:8-14; Warumi 8:9; Wakolosai 1:27; 2 Waraka wa Petro 1:3-4).

◙**"vyombo vya udongo"** Huu ni msisitizo kwa mwili wa binadamu (rejea 2 Wakorintho 4:10,16; 5:1; Mwanzo 2:7; 3:19; 18:27). Muktadha huu wote ni wa kilahaja kati ya hali ya nje ya mwili ya Paulo na nguvu ya kiroho ya injili na Roho Mtakatifu akaaye ndani katika maisha yake.

◙**"adhama kuu ya uwezo"** *Huperbolē*, angalia Mada Maalumu:Matumizi ya *Huper* ambatani ya Paulo katika 1 Wakorintho 2:1

**4:8-11" Pande zote twadhikika bali hatuangamizwi"** Mstari 8-10 una mfululizo wa njeo za WAKATI ULIOPO (zaidi TENDEWA) ENDELEVU ambazo ni kuchezeshwa kwa maneno ya Koine maneno ya Kiyunani yakieleza ugumu wa huduma ya Paulo. Tungo ENDELEVU nane za kwanza ziko katika safu zinazotofautiana. Ya kwanza inaelezea hali alizokutana nazo Paulo katika huduma na ya pili inazungumza ukomo wa matokeo yake. Mfano wa kuchezeshwa huku kwa maneno ni: (1)"hasara lakini si katika kila kitu" na "kuangushwa chini lakini si kushindwa." Sehemu hii inaweza kulinganishwa na 2 Wakorintho 1:6; 6:4-10; 11:23-28.

**4:9"kuangamizwa"** Kwa ajili ya dhana ya "uangamivu" angalia Mada Maalumu katika 1 Wakorintho 8:11 na mjadala katika 1 wakorintho 1:18

**4:10"siku zote twachukua katika mwili kuuawa kwake Yesu"** Hii inamaanisha mkanganyiko wa sisi kuhusianishwa kuwa vizuri na Mungu, lakini tukiwekwa wazi kwa matatizo kwasababu ya ulimwengu ulioanguka. Tunao uzima wa milele, lakini miili yetu ipo katika hali ya kufa (rejea 2 wakorintho 1:8). Kama Yesu alivyokataliwa na kudhikika (rejea Yohana 15:20), hivyo sisi pia waamini (1 Wakorintho 15:31; Wagalatia 2:20; Wafilipi 3:10; Wakolosai 1:24; 1 Waraka wa Petro 4:12-19).

◙**"ili uzima wa Yesu"** Hii ina maanisha (1) Kristo aliyefufuka, ambalo lililokuwa tumaini la Paulo au (2) uaminifu wa Yesu wakati akipitia dhiki. Paulo alitaka kufunua uaminifu wa Yesu (rejea 2 Wakorintho 4:11) na kushiriki katika ufufuo wa wafuasi wake (rejea 2 Wakorintho 4:14; 1 Wakorintho 15).

◙**"udhihirishwe katika miili yetu"** Hii ni KAULI TENDWA TEGEMEZI YA WAKATI ULIOPITA. Soma Wagalatia 6:17, ambayo kwa uwazi inamaanisha alama za vidonda katika huduma ya Yesu. Kama vyombo vyetu vya udongo vinavyovunjika, hazina ya ndani inaonekana zaidi (rejea 2 Wakorintho 12:9-10)

Paulo anatumia neno la Kiyunani *sarx* (kama vile nyama/mwili) katika namna kadhaa.

1. Mwili wa mwanadamu ("mwili" ya 2 Wakorintho 4:10 sambamba na "nyama" ya 2 Wakorintho 4:11; pia 2 Wakorintho 7:5; 10:3; 12:7)
2. Uanadamu wa mtu (2 Wakorintho 5:16; 11:18)
3. Sifa ya uanadamu (kama vile baba- mwana, rejea Warumi 1:3; 4:1)
4. Ubinadamu kwa ujumla wake (rejea 1 Wakorintho 1:26, 29)
5. Dhambi ya kibinadamu (rejea Warumi 7:5,18; 8:3,4,5,8,9,12,13; 2 Cor. 7:1; 10:2)

**4:11" sisi tulio hai, siku zote twatolewa tufe kwa ajili ya Yesu"** Ufahamu wa Kibiblia katika mstari huu unaweza kuonekana katika 1 Wakorintho 4:9, pale Mitume wanaoneshwa kwa wote, malaika na wanadamu. Waaminio pia wapo kwenye maonesho kwa ulimwengu unaopotea na ulimwengu wa malaika (rejea Waefeso 2:7; 3:10).

Neno "siku zote" (rejea 2 Wakorintho 6:10) ni sambamba na "muda wote" ya 2 Wakorintho 4:10. Wito wa huduma ni wito wa makusudi wa kujitoa kila siku kwa kujikana nafsi (rejea 2 Wakorintho 5:14-15; warumi 6:76:7; 1 Wakorintho 15:31; Wagalatia 2:20; Wafilipi 3:8, 10; 1 Waraka wa Yohana 3:16). Huu mtazamo ni kurudishwa nyuma kwa kuanguka kwa mwanadamu katika Mwanzo 3. Ni ushahidi wa kufanana na Kristo, ambaye ni urejesho wa sura ya Mungu katika ubinadamu.

Neno "twatolewa" (*paranididōmi*) lilitumika na Yuda kumkabidhi Yesu kwa mamlaka (Mathayo 20:18-19; Marko 10:33). Inatumika na Yesu katika namna ya kutabiri akiwaelezea wanafunzi wake katika Mathayo 10:17; 24:9; Marko 13:11-12.

Kifungu cha maneno "kwa ajili ya Yesu" ni kuelewa kama kisababishi. Mizigo ya huduma yetu haimpi faida Kristo, bali ni kwa ajili yetu kwakuwa tunamfuata Yeye. Kama walivyomtesa, watatutesa nasi pia. Hatahivyo, ni

kweli kwamba vitu tunavyopitia kama wafuasi wa Kristo ni vitu ambavyo vinaweza kutusaidia kukua zaidi na zaidi kama yeye.

Utambulisho wa Paulo na kifo cha Yesu kunafanya kazi kithiolojia katika ngazi kadhaa.

1. Thiolojia ya Sakramenti (rejea Warumi 6:3-5; Wakolosai 2:12; 3:1,3-5)
2. Mafundisho ya kanisa (rejea 1 Wathesalonike 4:14-15)
3. Uzoefu binafsi (rejea 2 Wakorintho 4:10-11; Wagalatia 2:20; Wafilipi 3:10)

◙**"miili yetu ipatikanayo na mauti"** angalia Mada Maalumu katika 1 Wakorintho 1:26.

**4:12" Basi hapo mauti hufanya kazi ndani yetu, bali uzima ndani yenu"** Hii ni KAULI YA KATI YA WAKATI ULIOPO ELEKEZI inayoipa mauti sifa za uhai. Hii inamaanisha dhiki ya mwili kwa Paulo na timu yake ya huduma (2 Wakorintho 4:16) na maisha ya kiroho ndani yao wale awahubirio injili.

Katika mfululizo wa *Anchor Bible* katika 2 Wakorintho , Victor Furnish anaamini ni SAUTI IRABU TENDEWA (ukurasa wa 257) kwasababu hiyo SAUTI inatawala 2 Wakorintho 4:10-11, ambapo mada inayojulikana ni nguvu ya Mungu (rejea 2 Wakorintho 4:7). Hii ingemaanisha kwamba Mungu anatumia majaribu na dhiki kama njia ya kuzalisha mfanano wa Kristo ndani ya wafuasi wake. Maisha ya viongozi yanatoa nguvu kwa jumbe zao (2 Wakorintho 1:3-11; 2 Timotheo 2:9-10).

**ANDIKO LA NASB(LILILOBORESHWA): 2 WAKORINTHO 4:13-15**
***13*** **Lakini kwa kuwa tuna roho ile ile ya imani; kama ilivyoandikwa, Naliamini, na kwa sababu hiyo nalinena; sisi nasi twaamini, na kwa sababu hiyo twanena;** ***14*** **tukijua ya kwamba yeye aliyemfufua Bwana Yesu atatufufua sisi nasi pamoja na Yesu, na kutuhudhurisha pamoja nanyi.** ***15*** **Kwa maana mambo yote ni kwa ajili yenu, ili neema hiyo ikiongezwa sana, kwa hao walio wengi shukrani izidishwe, na Mungu atukuzwe.**

**4:13" tuna roho ile ile ya imani"** Jambo la muhimu hapa ni kwamba ile imani iliyomfanya mtu akubalike kwa Mungu katika Agano la Kale (kama vile mwandishi wa Zaburi 116) ni imani ambayo inamfanya mtu awe kimahusiano vizuri na Mungu katika Agano Jipya (kama vile Ibrahimu katika Mwanzo 15:6, ikinukuliwa na Paulo katika Warumi 4:3, 9, 22)

Paulo anatumia neno "roho"kwa namna nafsi ya mtu. Mara nyingi anatumia "roho" kama njia ya kumaanisha sifa ya ndani ya mtu mwanadamu (angalia angalizo katika 2 Wakorintho 4:21). Hii haina uhusiano na kifungu cha maneno hicho kinachopatikana katika 1 Wakorintho 12:9, ambayo inamaanisha Roho akitoa vipawa kwa waaminio kwa imani. Hii inamaanisha imani iokoayo kama ya Ibrahimu (rejea Mwanzo 15:6). Cha kushangaza, katika *Word Studies in the New Testament*, vol. 2, M. R. Vincent anasema, "si kwa upekee wa Roho Mtakatifu, wala sio kwa upande mwingine akili ya mwanadamu au tabia yake, lakini vikiunganishwa vyote viwili; imani kama kipawa cha Roho wa Mungu" (ukurasa 82).

Katika *Synonyms of the Old Testament*, Robert Girdlestone analeta mjadala mzuri sana wa matumizi ya "roho" katika Agano Jipya (ukurasa 61-63).

1. Roho ovu
2. Roho ya binadamu
3. Roho Mtakatifu
4. Vitu ambavyo Roho huzalisha ndani na kupitia roho za binadamu
   a. 'si roho ya utumwa dhidi roho ya kufanywa' – Warumi 8:15
   b. 'roho ya upole' – 1 Wakorintho 4:21
   c. 'roho ya imani' – 2 Wakorintho 4:13
   d. 'roho ya hekima na ufunuo katika maarifa yake' – Waefeso 1:17
   e. 'si roho ya hofu dhidi ya nguvu, upendo na nidhamu' – 2 Timotheo 1:7
   f. 'roho ya makosa dhidi ya 'roho ya kweli – 1 Waraka wa Yohana 4:6

◙**"kama ilivyoandikwa"** Hii ni KAULI TIMILIFU TENDWA ENDELEVU YA WAKATI ULIOPO, inayotumika na waandishi wa Agano la Kale kumaanisha hali ya kupewa na umuhimu wa maandiko (rejea Mathayo 5:17-19)

◙**"NALIAMINI, NA KWA SABABU HIYO NALINENA"** Hii ni nukuu kutoka katika Septuagint ya Zaburi 116:10, iliyozungumzia kuokolewa kunakoletwa na Mungu kwa watakatifu.

**4:14" kwamba yeye aliyemfufua Bwana Yesu"** Kifungu hiki cha maneno ni fursa nzuri sana kuonesha kwamba Agano Jipya lina sifa za kazi ya ukombozi kwa nafsi tatu za Kichwa cha Mungu.

1. Mungu Baba alimfufua Yesu (rejea Matendo ya Mitume 2:24; 3:15; 4:10; 5:30; 10:40; 13:30,33,34,37; 17:31; Warumi 6:4,9; 10:9; 1 Wakorintho 6:14; 2 Wakorintho 4:14; Wagalatia 1:1; Waefeso 1:20; Wakolosai 2:12; 1 Wathesalonike 1:10)
2. Mungu mwana alijifufua mwenyewe (rejea Yohana 2:19-22; 10:17-18)
3. Mungu Roho alimfufua Yesu (rejea Warumi 8:11)
   Kuna aina za mbadala yanayohusiana na kifungu cha maneno, "Bwana Yesu"
   a. "Bwana Yesu" - MSS א, C, D, F, G
   b. "Bwana Yesu Kristo" - MS 436
   c. "Bwana Yesu kutoka katika wafu" - MSS 104, 459
   d. "Yesu" - MSS $P^{46}$, B
      The UBS[4] inatoa chaguo #1 a "B" ikiipa alama (karibia na hakika), lakiniBruce Mketzger anapendelea chaguo la #4 (kama ambavyo inasema Biblia ya NET). Kama kuna aina za mbadala mwingi, ipi ilikuwa ndio ya asili ya kwanza kabisa haiathiri nguvu ya habari.

◙**"atatufufua sisi………….. kutuhudhurisha"** Hizi zote KAULI TENDAJI ELEKEZI YA WAKATI UJAO. Waaminio watafufuliwa kutoka katika wafu (*syn* na Yesu) na kutuhudhurisha kwa Baba (*syn* na waaminio wote).
Uelewa wa Paulo kuhusu muda wa Kuja kwa Mara ya Pili una utata. Katika baadhii ya maandiko inaonekana kwamba anategemea kuwa hai katika *parousia* (rejea 1 Wathesalonike 4:15, 17; 1 Wakorintho 15:51-52; na Wafilipi 3:20; 4:5), lakini katika maandiko mengine anaonekana kujiweka yeye mwenyewe na wale waamini waliokwisha kufa(rejea 1 Wakorintho 6:14; 2 Wakorintho 4:14; 5:1-10). Ni Baba tu pekee anayejua muda wa Kuja kwa Mara ya Pili (rejea Mathayo 24:36; Marko 13:32; Matendo ya Mitume 1:7). Kuja kwa Mara ya Pili ni tumaini kwa kila kizazi cha waamini, lakini uhalisia wa kizazi kimoja tu. Waaminio wanatakiwa kuishi kwa utayari, tayari kutumika katika huduma ya Kristo.

**4:15** Moyo wa Paulo ulitakiwa kuwasaidia watu wenye dhambi kuja katika imani katika Kristo na kutafuta amani ya kweli na furaha na kumpa Mungu sifa (rejea 2 Wakorintho 1:11 na NASB, NRSV, TEV, NJB). Toleo la NKJV kidogo ni halisi kwa "wengi."Hii inaweza kumaanisha wanaomuunga mkono Paulo katika kanisa la Wakorintho. Inaweza ikawa totauti kwa "baadhi" 2 Wakorintho 3:1; 10:12; 1 Wakorintho 4:18; 6:11; 8:7; 10:7,8,9,10; 15:6,12,34,35). Mstari wa 15 kwa wazi ni ujumuisho kwa ufupi wa namna zimsifuzo Mungu.

▣**"Mungu atukuzwe"** angalia MADA MAALUMU:UTUKUFU (SPECIAL TOPIC:GROLY)

**ANDIKO LA NASB(LILILOBORESHWA): 2 WAKORINTHO 4:16-18**
***16*** **Kwa hiyo hatulegei; bali ijapokuwa utu wetu wa nje unachakaa, lakini utu wetu wa ndani unafanywa upya siku kwa siku.** ***17*** **Maana dhiki yetu nyepesi, iliyo ya muda wa kitambo tu, yatufanyia utukufu wa milele uzidio kuwa mwingi sana;** ***18*** **tusiviangalie vinavyoonekana, bali visivyoonekana. Kwa maana vinavyoonekana ni vya muda tu; bali visivyoonekana ni vya milele.**

**4:16" Kwa hiyo hatulegei"** Hii ni mada inayojirudia katika maandiko ya Paulo (rejea. 2 Wakorintho 4:1; Wagalatia 6:9; Waefeso 3:13; 2 Wathesalonike 3:13). Mazingira ni kuwa, kiuhalisia, kwa ajili ya kuimarishwa kiroho chetu, nguvu na kuzaa matunda.

◙**"ijapokuwa utu wetu wa nje unachakaa, lakini utu wetu wa ndani unafanywa upya siku kwa siku."** Hizi zote ni KAULI TENDWA ELEKEZI YA WAKATI ULIOPO, ambayo inaashiria kitendo kinachoendelea. PASIVE SAUTI IRABU TENDAJI ni ngumu kuitafsiri na kuielewa katika muktadha huu. Tafsiri nyingi za Lugha ya Kingereza inatafsiri zote kama SAUTI IRABU TENDAJI, lakini zinaweza pia zikaashiria kitendo cha kiungu katika kutumia matatizo ya kimwili na dhiki kama namna ya kuimarisha na kufanya makuzi kwa wafuasi wa Yesu (Mathayo 5:10-12; Yohana 15:18-21; 16:1-2; 17:14; Matendo ya Mitume 14:22; Warumi 5:3-4; 8:17; 2 Wakorintho 4:16-18; Wafilipi 1:29; 3:11; 1 Wathesalonike 3:3; 2 Timotheo 3:12; Waebrania 5:8; Yakobo 1:2-4; 1 Waraka wa Petro 4:12-19). Katika Waefeso 3:16 na 4:24 kuna kulinganisha kwa mtu wa kale na mtu mpya, lakini utofauti hapa ni baina ya utu wetu wa nje wa mwili na utu wetu wa ndani wenye asili ya roho.

◙**"unafanywa upya"** Angalia Mada Maalumu ifuatayo

## MADA MAALUMU: Kufanywa upya *(ANAKAINŌSIS)* (SPECIAL TOPIC: Renew *(ANAKAINŌSIS)*)

◙ "**siku kwa siku"** Paulo anatumia nahau ya Kiebrania (rejea Mwanzo 39:10; Esta 3:4; Zaburi 68:19) marudio katika 2 Wakorintho 4:16, "siku kwa siku," na sawa na marudio ya Kiaramaiki katika 2 Wakorintho 4:17, "zaidi kwa zaidi" (kama vile *huperbolēn eis hperbolēn*). Kumbuka, waandishi wa Agano Jipya (isipokuwa Luka) ni ya Kiebrania/Kiaramaiki maandiko yaliyofikiriwa katika Kiyunani cha Koine. Kuna nahau nyingi za Kiebrania na tungo za kisarufi, na pia maelezo kadhaa ya Agano la Kale na nukuu katika Agano Jipya.

**4:17-18** Mstari wa 17 unafanana na Warumi 8:18, wakati 2 Wakorintho 4:18 ni sawa na Warumi 8:24. Paulo aliwaandikia Warumi kutoka Korintho! Alikuwa akifikiria juu ya wito wake na matatizo yanayoambatana nae. Kulikuwa, kiuhalisia, hakuna ulinganifu baina ya mateso kidogo ya muda na utukufu wa milele! Huu ni muono wa Kibiblia wa kiulimwengu unaowapa watu wa Mungu nguvu ya kuendelea licha ya kuwa katika ulimwengu wenye anguko. Yeye yupo pamoja nasi na atatuleta sisi katika uwepo wake binafsi kukaa naye milele!

**4:17" yatufanyia"** KITENZI hikihiki kimetumika katika Warumi 5:3-4 na Yakobo 1:2-4, ambayo pia inazungumzia faida za mateso na dhiki.

◙**"utukufu wa milele"** Angalia MADA MAALUMU: UTUKUFU *(AGANO LA KALE)* (SPECIAL TOPIC: GROLY (OT)) katika 1 Wakorintho 2:7.

◙**"uzidio kuwa mwingi sana"** *Huperbolē*. Angalia Mada Maalumu: Matumizi ya Paulo ya *Huper* ambatani katika 1 Wakorintho 2:1.

**MASWALI YA MJADALA**

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, ambao una maana maana kuwa unawajibika kwa tafsiri zako za Biblia mwenyewe. Kila mmoja wetu lazima atembee katika nuru tuliyopewa. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hupaswi kumuachia vitu hivi mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuchokonoa kimawazo na sio kutoa maana ya mwisho.

1. 2 Wakorintho 4:1 inazungumza vipi juu ya mbinu za walimu wa uongo?
2. Je mababa wa kanisa la kwanza walipewa haki ya kubadili andiko la Kigiriki la 2 Wakorintho 4:4 kukabiliana na tatizo walilokuwa nalo katika siku zao?
3. Je ina maanisha nini kuwa Shetani ni "mungu" wa ulimwengu huu)
4. Kwanini Paulo anataka tuone matatizo yake ya kimwili dhidi ya nguvu zake za kiroho?

# 2 WAKORINTHO 5

| MGAWANYO WA AYA WA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **UBS[4]** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB** |
| Kuishi kwa Imani na Kifo | Uhakika wa ufufuo | Ujasiri wa kukabiliana | Kuishi kwa Imani | Ugumu na Matumaini ya Huduma ya Mitume |
| (4:16-5:10 | | | (4:16-5:10) | (4:7-5:10) |
| 4:16-5:5 | | | | |
| | 5:1-8 | 5:1-5 | | 5:1-5 |
| 5:6-10 | Kiti cha Hukumu Cha Kristo | 5:1-10 | 5:6-10 | 5:5-10 |
| Huduma ya Upatanisho | 5:9-11 | Ulinzi wa Baadaye wa Huduma yake ya Upatanisho | Urafiki na Mungu Kupitia Kristo | Huduma ya Mitume katika Tendo |
| 5:11-15 | | 5:11-15 | 5:11-15 | 5:11-15 |
| | Kupatanishwa na Mungu | (5:11-6:13) | 5:11-6:13 | |
| | 5:12-21 | | | |
| 5:16-6:10 | | 5:16-6:10 | 5:16-19 | 5:16-19 |
| | | | 5:20-6:3 | 5:20:6:10 |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (**Kutoka "Mwongozo wa Usomaji Mzuri wa Biblia" A Guide to Good Bible Reading**)

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Haya ni maoni ya mwongozo kwa kujisomea, ikiwa na maana kuwa unawajibika binafsi kwa tafsiri ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mtoa maoni tu.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa,lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

40. Aya ya kwanza
41. Aya ya pili
42. Aya tatu
43. N.k

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA

A. Paulo anzungumzia juu ya mauti yake katika 2 Kor. 5:1-10
   1. Yeye anatumia sitiari mbili.
      a. Maskani ya kidunia dhidi ya yale ya kudumu, yaliyotengenezwa na Mungu
      b. Wale waliovikwa dhidi ya wale wasio na mavazi yaani, walio uchi)
   2. Ni vigumu kuyafuata mawazo ya Paulo yaliyo katika utangulizi wake. Yeye anazungumza kuhusu
      a. Kuvikwa kwetu katika Kristo kupitia ubatizo (kama vile 2 Kor. 5:2-4)
      b. yule Roho akaaye ndani ya wokovu (kama vile 2 Kor. 5:5)
      c. kuupokea mwili mpya wa kiroho wakati wa kurudi kwa Kristo (kama vile mst. 3 na 10)
   3. Ufanano bora wa Pauline katika kulifasiri hili andiko unapatikana katika Rum. 8:18-25,26-30 (yaani, kuwa na majonzi ya ndani na 1 Kor. 15:53-54 (yaani, "kule kumezwa").
   4. Kwa kiasi fulani andiko hili lazima lihusiane na mjadala wa Paulo wa sura za 4 na 6. Uaminifu, maisha ya ki-Mungu katikakati ya mambo magumu ndiyo dhana ya mara kwa mara.

B. Paulo anatengeneza dai kubwa la kitheolojia katika 2 Kor. 5:6 na 8. Hapo mwanzo waamini na wale wasioamini walikuwa wakifikiri kwenda *Kuzimu* pale wanapokumbwa na mauti ili kuingoja hukumu (angalia MADA MAALUM: Wafu wako Wapi? (PECIAL TOPIC: Where Are the Dead?) katika 2 Kor. 5:6). Sheria za Dini za Kiyahudi nazo pia zilionyesha mgawanyiko ndani ya ya eneo linalowahifadhi wale waliokufa (yaani, Agano la Kale *Sheol*) kati ya wale wenye haki na na waovu. Paulo anadai kuwa Yesu alipofufuka aliichkua ile haki huko mbinguni. Na sasa wale waaminio haendi *kuzimu*, bali hukaa na Bwana. Kwa vyo vyote vile hili linamaanisha ushirika kamili au ushirika wenye mipaka usio yumkini. Biblia haifunui undani wa habari hii kuhusiana na maisha baada ya kifo.

C. Paulo anatengeneza usemi mwingine wenye kushangaza katika 2 Kor. 5:10. Kwa uwazi kabisa wamini wote na wale wasioamini watasimama mbele ya Kristo kama Hakimu. Je, huu ni ufanano wa ile ukumu ya kondoo na mbuzi ya Mt. 25 au ile Hukumu ya kile Kiti cha Enzi Kikubwa Cheupe ya Ufunuo 20? Ikiwa waamini wanasamehewa dhambi zao zote kupitia Kristo, Je, watahukumiwa kwa jambo gani? Tena maswali haya ya muhimu hayawezi kujibiwa kibiblia. Dhahanio la kimantiki ni kuwa hawa wanalazimika kwa ajili ya
   1. ile habari ya injili
   2. karama zao za kiroho
   3. matumizi yao ya mapato yao ya kimwili
   4. upatikanaji wao kwa ajili ya huduma

   Lakini, hili ni kisio pekee lilijikita katika ile maudhui ya 2 Kor. 5:11-21.

D. Mjadala wa Paulo ule wajibu ywa kiroho katika 2 Kor. 5:11-21 kwa uwazi kabisa unaakisi ule ubinafsi wa wale walimu wa uongo, bila shaka yale matendo maovu/mafundisho.

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : 2 WAKORINTHO 5:1-5**
[1] **Kwa maana twajua ya kuwa nyumba ya maskani yetu iliyo ya dunia hii ikiharibiwa, tunalo jengo litokalo kwa Mungu, nyumba isiyofanywa kwa mikono, iliyo ya milele mbinguni.** [2] **Maana katika nyumba hii twaugua, tukitamani sana kuvikwa kao letu litokalo mbinguni;** [3] **ikiwa tukiisha kuvikwa hatutaonekana tu uchi.** [4] **Kwa sababu sisi tulio katika maskani hii twaugua, tukilemewa; si kwamba twataka kuvuliwa, bali kuvikwa, ili kitu kile kipatikanacho na mauti kimezwe na uzima.** [5] **Basi yeye aliyetufanya kwa ajili ya neno lilo hilo ni Mungu, aliyetupa arabuni ya Roho.**

**5:1"twajua"** Ni vigumu katika kitabu hiki kuuufahamu utangulizi wa VIWAKILISHI vya Palo vilivyo katika hali ya UWINGI. Wakati mwingne alirejelea (1) kwake mwenyewe; (2) watendakazi wa huduma yake; au (3) waamini wote. Ni muktadha pekee unaopaswa kukitambua kile kinachomaanishwa. Hapa nukuu hii ni #3.

◙**"ikiharibiwa "** Hii ni SENTENSI SHURUTISHI DARAJA LA TATU ambayo inamaanisha tendo muhimu. Kifo cha Paulo kilikuwa cha mashaka mpaka pale Ujio wa Pili ungetokea kwanza. Yeye alifikiri kuwa angeenda kufia huko (kama vile 2 Kor. 1:8-10). Maisha yake yeye kama Mtume hayakuwa na wepesi au kukosa mwiba (kama vile 2 Kor. 4:7-12; 6:3-10; 11:24-28). Paulo kwa hakika hakuufahamu wakati wa kufa kwake au mambo ambayo yangepelekea kifo chake. Yeye angefikiri au kutumaini kwamba atakuwa hai wakati Kristo atakaporudi (kama vile 1 Kor. 15:51-52; Flp. 3:20; 1 The. 4:15,17). Hata hivyo, katika vifungu vingine alitarajia kufufuka kutoka katika wafu (kama vile 1 Kor. 6:14; 2 Kor. 4:14. Kwa mjadala mzuri tazama F. F. Bruce's *Answers to Questions*, kr. 200-201). Lile tumaini la kuwa hai wakati wa kurudi kwa Kristo ni tumaini la kila kizazi cha waaminio lakini ukweli pekee ni kwa kile kizazi kilichokumbwa na mateso.

◙**"maskani"** Hii ni moja miongoni mwa zile stiari kadhaa za kibiblia kwa ajili ya ule udhaifu wa mwili wa mwanadamu (yaani, majani, ushairi). Paulo alifahamu kwamba mwili wake ulikuwa umechakaa. Yeye alijaribu kuyatengeneza makazi ya zamani!

**NASB, TEV "ikiharibiwa"**
**NKJV, NRSV "itakapong'olewa"**
**NJB "itakaposhindwa**"

Hii ni KITENZI TENDEWA TEGEMEZI CHA WAKATI ULIOPITA USIO TIMILIFU. Paulo alifahamu kwamba uzima na kifo vilikuwa mikononi mwa Mungu (yaani, KAULI TENDEWA). Yeye alifahamu kuwa angekufa, lakini hakufahamu ni lini au kwa namna gani (yaani, DHAMIRA TEGEMEZI).

Neno hili lina uwanja mpana wa kimaana. Katika Agano la Kale na Agano Jipya neno *kataluma* katika maeneo ya makazi ya muda na neno *katal*ū*ō* lilimaanisha eneo la kuishi au kupumzika. Hata hivyo, pia linatumika kumaanisha uharibifu au ubatilifu wa kitu (ambalo upanuzi wa kistiari wa neno *luō*, yaani, kupoteza, kama vile Mt. 24:2). Katika Isa. 38:12 hili linatumika kumaanisha kuiharibu maskani. Hapa hili linaonekana kuwa ufanano bora wa matumizi ya Paulo.

◙ **"tunalo jengo litokalo kwa Mungu"** Hili ni jengo la kudumu (kama vile Yohana 14:2-3; Ebr. 11:10) ikilinganishwa na ile inayohamishika, isiyo ya kudumu (kama vile Ebr. 11:9). Huu ni WAKATI ULIOPO. Paulo anaianza ile kweli ya kinabii kama ilivyokuwa kawaida ya kweli.

◙**"nyumba isiyofanywa kwa mikono"** Miili yetu mipya itakuwa ya kiroho (kama vile 1 Kor. 15:35-49), kama ule wa Yesu (kama vile Marko 14:58; 1 Yohana 3:2).

◙**"iliyo ya milele mbinguni"** Aya hii inarejelea lile eneo la makazi ya Mungu. Hili neno "mbiguni" ni UWINGI kwa sababu Walimu wa Sheria za Kiyahudi walikuwa na mdahalo uliohusu ni "mbingu" ngapi zilizokuwepo. Katika Mwanzo 1 hili neno mbingu linarejelea ile sehemu ya juu ya uso wa dunia. Hivyo Walimu hawa walitumia maarifa yao ya elimu ya hesabu za kibiblia kuitetea mbingu ya tatu au mbingu ya saba kama mahali ambapo Mungu anaishi. Agalia Mada Maalum" Mbingu katika 2 Kor. 12:2.

Mbingu haikojuu au nje. Bila shaka hiki ni kipimo kingine kisichokuwa na wakati na nafasi. Baada ya ufufuo Yesu alionekana na kutoweka, pamoja na kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine. Kipimo cha ulimwengu unaoonekanao kinapofahamika ile kweli ya kiroho inashangaza.

**5:2"katika hii"** Hii ni aya ISIYO na jinsi, ambayo inarejelea juu ya "nyumba" katika 2 Kor. 5:1.

◙ **"twaugua"** Neno hili ni KITENZI TENDAJI ELEKEZI CHA WAKATI ULIOPO, waamini wanaendelea kuugua au kuwa na majonzi ya ndani kwa ajili ya mpangilio mpya wa Mungu na miili mipya ya kiroho (kama vile Rum. 8:18-27; uumbaji wa kuugua kwa majonzi ya ndani 2 Kor. 5:22; kuugua kwa waamini, 2 Kor. 5:23; na kule kuugua kwa Roho, 2 Kor. 5:26).

◙ **"tukitamani "** Hili ni neno lenye nguvu kwa maana ya shauku (kama vile 2 Kor. 9:14). Muundo wa NOMINO ni 2 Kor. 7:7 na 11. Paulo alikuwa mtu wa hisia zenye nguvu.

**5:3-4 "tukiisha kuvikwa "** Paulo mara kwa mara anatumia neno kuvikwa kama stiari ya maisha ya kiroho. Hili vazi linalorejelewa hapa ni lile la je au lile la juu (*ependutēs*, kama vile Yohana 21:7). Yeye anatumia vazi kama stiari ya kumaanisha zile chaguzi wa maisha za mtu. Waamini wanasistizwa kuachana na yale maisha ya zamani na kuyatupilia mbali kama lile vazi (kama vile 2 Kor. 3:8,9; Efe. 4:22,25,31; Yakobo 1:21; 1 Pet. 2:1). Hawa yawapasa kumvaa Kristo (kama vile 2 Kor. 3:10,12,14; Efe. 4:24; Rum. 13:14; Gal. 3:27). Hawa waamini walikuwa wakiongozwa na kutawaliwa na shauku ya maovu yao, lakini kwa sasa, kupitia Kristo, hawa wanaweza kubadilika (kama vile Warumi 5-6). Hii asili ya matumizi ya neno kumvaa Kristo pia imehusianishwa na ile kanuni ya ubatizo katika lile kanisa la awali, ambapo wale waliokuwa wamebadili dini walivalishwa mavazi yaliyo safi, mavazi meupe baada ya ubatizo. Paulo hakutaka kukumbana na hali ya mwili kutengana na roho kati ya kifo na ufufuo, bali alitaka kushiriki katika ya matukio ya yaliyohusiana na Ujio wa mara ya Pili (kama vile 1 The. 4:15-17), ambao ni moja ya mwili wa kiroho.

Hii dhana ya kitheolojia ya hali ya mwili kutengana na roho haitajwi kwa ubayana katika Andiko, bali kidokezo pekee cha ukaidi kwa sababu hii dhana ilitumika katika falsafa ya Kiyunani kama hali ya kudumu iliyopokelewa kama hadhi ya juu kwa roho kutengana na mwili kimwonekano. Katika *Word Pictures in the New Testament* A. T. Robertson anasema "Paulo hatarajii kuwa katika hali ya mwili kutengana na roho tu vazi lake la kiroho" (juzuu. 4, uk. 228).Ufuatao ni ufupisho wa maelezo kutokana na maoni yangu, juzuu. 7, 1 The. 4:16 (angalia www.freebiblecommentary.org).

"'Na wale waliokufa katika Kristo watanyakuliwa kwanza' Kifungu hiki kinasababisha mkanganyiko kuhusiana na wapi wafu huenda baina ya siku ya kifo na ufufuo wao. Kifungu hiki kinamaanisha kwamba hawa watabaki katika makaburi (kama vile Mt. 27:52-53).

Hata hivyo, 2 Kor. 5:8 inamaanisha kwamba hawa wako katika Bwana. Suluhisho linaweza kuwa katika ile dhana ya hali ya mwili kutengana na roho. Hilo umbo mwili hubaki kaburini, nguvu ya maisha inaenda kuwa na Bwana. Hapa kuna maswali mengi yasiyojibiwa. Biblia haitoi kifungu cha mafundisho yaliyo wazi kuhusiana na jambo hili.

Tafsri zilizo nyingi zinakitafsiri kifungu hiki kama ikiwa watakatifu wako na Mungu/na Yesu atakaporudi watakuwa pamoja naye (kama vile NASB). Mtazamo mwingine unapatika na katika TEV, "Wale waliokufa huku wakiamini katika Kristo watanyakuliwa kwanza."

**5:3** Mstari wa tatu bila shaka umetengwa. Ni vigumu kufahamu kile alichokirejelea Paulo kwa ufasaha kwa sababu

1. aliandika kwa kuchanganya stiari
2. ule uyumkini wa namna "uchi" unavyohusiana na "kuvikwa"
3. ule uhusianao wa kimuktadha na yale mateso ya ki- Mitume (kifo) au upinzani (mafundisho ya uongo)
4. pia kuna tatizo lililoongezeka ju ya tofauti ya kimuktadha. Ushahidi bora wa kimuktadha uko nyuma ya neno *eudusamenoi* ("kuvua," yaani, MSS $P^{46}$, א, B, C, $D^2$), lakini neno lenye ufanano sana *ekdusamenoi* ("kuvikwa," yaani, MS $D^*$) linatengeneza maana zaidi katika muktadha. Ikiwa mmoja atachagua kwa sifa ya ukosoaji wa kimuktadha
    a. mpangilio wa machapisho ya Kiyunani ni bora
    b. andiko lake lisilo la kawaida bila shaka ni halisi

kisha Paulo ameandika maneno yale yale (yaani, "kuvua. . .uchi"). $UBS^4$ haiwezi kuamua (utaoji wa daraja "C"), bali inaweka "kuvika" katika andiko. Ile Biblia Net pia inapendelea uchaguzi #2, "vika."

◙**"uchi"** Neno hili mara nyingi linatumika katika fasihi ya Kiyunani kwa ajili ya hali ya mwili kutengano na roho iliyokubaliwa katika kifo (kama vile Vincent, *Word Studies*, juzuu 2, uk. 822; Frank Stagg, *New Testament Theology*, kr.322-324; George E. Ladd, *A Theology of the New Testament*, uk. 552-554). Wayunani walitamani sana kwa utangulizi huu wa kwanza kutoka mwili wa asili, hata hivyo, Ukristo, kama ile dini ya Kiyahudi, inayodai kuwa sisi tutaonekana katika umbo mwili (wote waamini na wasio amini, kama vile. Dan. 12:1-2; Mt. 25:46; Yohana 5:28-

29). Bila shaka anakanusha kwa mara nyingine yale mafundisho ya uongo (yaani, kiini cha yale Mafunuo ya Uongo).

**5:4** Huu mstari mfupi na wenye kufumbwa lazima ufasiriwe sambamba na Rum. 8:18-25,26-30 (yaani, "kuugua") na 1 Kor. 15:53-54 (yaani, "kufa," "kutoweka"). Huu unaonekana kunenwa tena katika mstari wa 2.

**5:5 "aliyetufanya"** Paulo analitumia neno hili mara nyingi katika 2 Wakorintho (kama vile 2 Kor. 4:17; 5:5; 7:10,11; 9:11; 12:12). Maisha yetu hayaongozwi kwa bahati, nasibu, majaliwa, bali yanaongozwa na Mungu. Hata majaribu yetu yanaweza kumaanisha ukomavu na ile imani iliyo kubwa sana (kama vile Rum. 8:28-30; Ebr. 5:8).

Utoaji wa yule Roho ni

1. ishara kuwa zile Zama Mpya zimeanza
2. uthibitisho wa wokovu binafsi
3. maanisho la huduma
4. yeye anamaanisha ule ukomavu
5. uhakika wa mbingu

**NASB, NJB "arabuni"**
**NKJV, NRSV,**
**TEV "dhamana"**

Hii dhana ya arabuni ina utangulizi wa Agano la Kale (kumbuka, waandishi wa Agano la Kale ni Waebrania wenye fikra kubwa walioandika katika lugha ya kawaida na ya kienyeji inayozungumzwa katiki Ugiriki).

1. ahadi ya kulipa deni (kama vile Mwa. 38:17,18,20; Kumb. 24:10-13)
2. ahadi ya kutoa mahitaji (kama vile 1 Sam. 17:18
3. ahadi binafsi (kama vile 2 Flp. 18:23; Isa. 36:8)

Neno hili la Kiyunani linarejelea tendo la "malipo ya awali" au ile fedha ya awali (kama vile 2 Kor. 1:22; 5:5). Katika Ugiriki ya sasa neno hili linatumika kama pete ya uchumba, ambayo ni ahadi ya ndoa inayotarajiwa. Roho ni utimilifu wa ile ahadi ya enzi mpya za haki. Hiii ni sehemu ya "kile kilicho tayari" na "kile kisicho tayari" mvutano wa Agano Jipya, ambalo linapishana na zile zama mbili za Kiyahudi kwa sababu ya zile zama mbili za Kristo zijazo (tazama mjadala mzuri sana katika *How to Read the Bible for All Its Worth* na Fee ana Stuart, uk. 129-134). Roho ni arabuni atolewaye sasa kwa ajili ya ule ukamilifu wa baadaye.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : 2 WAKORINTHO 5:6-10**
**[6] Basi siku zote tuna moyo mkuu; tena twajua ya kuwa, wakati tuwapo hapa katika mwili, tunakaa mbali na Bwana. [7] (Maana twaenenda kwa imani, si kwa kuona.) [8] Lakini tuna moyo mkuu; nasi tunaona ni afadhali kutokuwamo katika mwili na kukaa pamoja na Bwana. [9] Kwa hiyo, tena, ikiwa tupo hapa, au ikiwa hatupo hapa, twajitahidi kumpendeza yeye. [10] Kwa maana imetupasa sisi sote kudhihirishwa mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo, ili kila mtu apokee ijara ya mambo aliyotenda kwa mwili, kadiri alivyotenda, kwamba ni mema au mabaya.**

**5:6**
**NASB "tuna moyo mkuu"**
**NKJV, NRSV "tuko imara"**
**TEV "tumejaa matumaini"**
**NJB "tunao ujasiri"**

Neno hili limetumika mara kadhaakatika 2 Wakorintho katika maana mbili.

1. uhakika, matumaini mema (kama vile 2 Kor. 5:6,8; 7:16)
2. ujasiri (kama vile 2 Kor. 10:1,2)

Lile tumaini letu endelevu (yaani, KAULI TENDAJI ENDELEVU YA WAKATI ULIOPO) katika Kristo litupali ujasiri katika maombi na huduma.

◙ **" hapa. . . tunakaa mbali"** Hapa kuna dhihaka katika ya haya maneno mawili yenye kuhusiana (pia katika 2 Kor. 5:8, 9).

1. *endēmountes*, kuwa hapa (KAULI TENDAJI ENDELEVU YA WAKATI ULIOPO)
2. *ekdēmoumen*, tuko mbali na mahali hapa (KAULI TENDAJI ELEKEZI YA WAKATI ULIOPO)

Unapofahamu mahali ulipo katika Yeye, mara nyingi unakuwa nyumbani pamoja naye, ingawa, tunapokuwa duniani, tunaishi kwa imani (kama vile mst.7).

**MADA MAALUM: Wafu Wako Wapi? (SPECIAL TOPIC: Where Are the Dead?)**

**5:7 "Maana twaenenda kwa imani, si kwa kuona"** Hii ni dhana ya Agano Jipya ya mara kwa mara (kama vile 2 Kor. 4:18; Ebr. 11:1,10,27; 1 Pet. 1:8). "kuenenda" ni stiari ya kibiblia inayomaanisha ule mtindo wa maisha. Waamini wanaishi katika ufalme wa kimwili, lakini kwa imani wanatambua na kuamini katika ufalme usionekana.

**5:8** Huu ni mstari wenye kushangaza kwa Wakristo. Huu unadai kuwa tutakuwa na Bwana katika hsia fulani pale tutakoapokuwa tumekumbwa na mauti. Mstari huu unakanusha ile dhana ya kulala kwa nafsi. Ingwa ushirika wetu pamoja na waamini wengine hauna mashaka katika hatua hii na ushirika wetu na Bwana si wa moja kwa moja huu utakuwa ni wa baada ya kuipokea miili mipya katika Siku ya Ufufuo, uhakika mkuu tulionao ni kuwa tutakuwa pamoja naye! Kweli hii haifundishwi kwa uwazi sehemu yo yote ile isipokuwa katika Flp. 1:21-23, ambalo inaufanya mstari huu kuwa wa muhimu! Katika upande wa hii kweli Paulo na waamini wote wangeweza kukumbana na jambo lo lote katika maisha.

**5:9"tena, ikiwa tupo hapa. . . kumpendeza yeye"** Hili ni lengo na shauku kwa ajili ya waamini (kama vile Efe. 5:8-10; Kol. 1:10).

Hili neno "kumpendeza sana" linapatikana katika maandiko kadhaa ya kumbukumbu, hata kabla ya siku za Paulo. Hii ilikuwa kaulimbiu ya utiifu na uaminifu katika Uyunani wa Mazingira ya karne ya kwanza (kama vile Moulton na Milligan, *The Vocabulary of the Greek Testament*, uk. 259). Paulo msomi na msomaji mzuri wa vyote yaani mawazo ya Kiyunani na Kiebrania.

**5:10"sisi sote kudhihirishwa mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo"** ile muktadha ya papo kwa papo inaandikwa kwa waamini; hata waamini watasimama mbele ya Mungu (kama vile Rum. 14:10; 1 Kor. 3:10-17). Kwa uwazi kabisa, sisi tutahukumiwa/kupewa thawabu kwa ajili ya zile shauku zetu, apatikanaji, na yale matumizi ya karama za kiroho. Dhambi na zile dhambi kwa ukamilifu kabisa zimekuwa zikihusika na kule kufa katika Kristo, lakini jambo la msingi ni ule uanafunzi!

Kuhusiana na ile dhana ya Yesu kaka Hakimu, hapa kuna maelezo mafupi kutokana na maoni yangu kuhusiana na Yohana 3:17 (angalia mtandaoni katika www.freebiblecommentary.org).

"Kuna vifungu kadhaa katika Yohana ambavyo vinadai kuwa Yesu alikuja kama Mwokozi, si kama Hakinmu (kama vile Yohana 3:17-21; 8:15; 12:47). Hata hivyo, kuna vifungu vingine katika Yohana ambavyo vinadai kuwa Yesu alikuja kuhukumu, atahukumu (kama vile Yohana 5:22-23,27; 9:39; na katika sehemu nyingine za Agano Jipya Matendo 10:42; 17:31; 2 Tim. 4:1; 1 Pet. 4:5).

Maoni kadhaa ya kitheolojia yako katika mpangilio: (1) Mungu alimpa Yesu kazi ya hukumu, kama alivyoifanya ile kazi ya uumbaji na ukombozi, kama ishara ya heshima (kama vile Yohana 5:23); (2) Yesu hakuja kwa mara ya kwanza kuhukumu, bali kuokoa (kama vile Yohana 3:17), lakini kwa ukweli kwamba watu waliomkataa, wanajihukumu wao wenyewe; (3) Yesu atarudi kama Mfalme wa Wafalme na Hakimu (kama vile Yohana 9:39).

Hizi semi zinazoonekana kuwa na mkanganyiko ni sawa na zile semi zinazomhusu Yohana Mbatizaji kuwepo au si kuwapo kwa Eliya."

◙**"kadiri alivyotenda, kwamba ni mema au mabaya"** Hii ni kanuni ya kiulimwengu kuwa wanadamu wanawajibika kwa ajili ya matendo yao na wataoa hesabu kwa Mungu (kama vile Ayubu 34:11; Mit. 24:12; Mhu. 12:14; Yer. 17:10; 32:19; Mt. 16:27; 25:31-46; Rum. 2:6; 14:12; 1 Kor. 3:8; Gal. 6:7-10; 2 Tim. 4:14; 1 Pet. 1:17; Ufu. 2:23; 20:12; 22:12). Hata waamini watatoa hesabu ya maisha yao na huduma kwa Kristo (yaani, "kile kitabu cha kumbukumbu"). Waamini hawaokolewi kwa kazi bali wanaokolewa katika kazi (kama vile Efe. 2:8-10; Yakobo na 1 Yohana). Angalia Mada Maalum: Uhuru wa Mkristo dhidi ya Wajibu wa Mkristo katika 1 Kor. 10:23.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : 2 WAKORINTHO 5:11-15**

***11*** **Basi tukiijua hofu ya Bwana, twawavuta wanadamu; lakini tumedhihirishwa mbele za Mungu. Nami natumaini ya kuwa tumedhihirishwa katika dhamiri zenu pia.** ***12*** **Maana hatujisifu wenyewe mbele yenu tena, bali tunawapa sababu ya kujisifu kwa ajili yetu, ili mpate kuwa nayo mbele yao wanaojisifu kwa mambo ya nje tu, wala si kwa mambo ya moyoni.** ***13*** **Maana ikiwa tumerukwa na akili zetu, ni kwa ajili ya Mungu; au ikiwa tunazo akili zetu timamu, ni kwa ajili yenu.** ***14*** **Maana, upendo wa Kristo watubidisha; maana tumehukumu hivi, ya kwamba mmoja alikufa kwa ajili ya wote, basi walikufa wote;** ***15*** **tena alikufa kwa ajili ya wote, ili walio hai wasiwe hai tena kwa ajili ya nafsi zao wenyewe, bali kwa ajili yake yeye aliyekufa akafufuka kwa ajili yao**

**5:11"hofu ya Bwana"** Hiki kifungu kinahusiana na kile kiti cha Kristo cha hukumu kilichotajwa katika 2 Kor. 5:10. Kuna heshima na ukuu (kama vile Matendo 5:11; 9:31) kwa sababu ya Hukumu ya Ulimwengu (kama vile Ebr. 10:31; 12:29; Yuda 22-23)! Waamini wanashawishiwa kuishi maisha ya ki-Mungu na kuishiriki injili kwa maarifa ambayo kwayo kila mtu atayatolea hesabu kwa Mungu.
Ule wadhifa wa "Bwana" unaweza kurejelea kwa YHWH au Yesu. Hiki kifungu "hofu ya Bwana" ni cha kawaida katika Maandiko ya Kiyunani ya Kale, yaliyomrejelea YHWH. Hata hivyo, huu ni wadhifa wa kawaida kwa Yesu katika Agano Jipya. Hukumu ni ya YHWH, lakini yeye ameigawa kwa Mwanae aliyechukua umbo-mwili.

◙**"twawavuta wanadamu"** Katika muktadha huu hili lingeweza kurejelea juu ya makundi kadhaa ya watu.
wale wasiomini (kama vile 2 Kor. 5:10)

1. wale manabii wa uongo (kama vile 2 Kor. 5:12)
2. waamini walio wadhaifu (kama vile 2 Kor. 5:11-12)

Huduma ya Paulo ilitimiza lile Agizo Kuu katika vipengele vyote yaani katika uinjilsti (kama vile Mt. 28:19) na pia uanafunzi (kama vile Mt. 28:20).

◙**"tumedhihirishwa mbele za Mungu "** Hiki ni KITENZI TENDEWA ELEKEZI CHA WAKATI TIMILIFU. Paulo kwa ujasiri anaeleza kuwa kwa utimilifu na ukamilifu Mungu anaijua nia makusudi yake (kama vile 2 Kor. 4:2). Tazama maelezo katika 2 Kor. 2:14.

◙**"tumedhihirishwa katika dhamiri zenu pia"** Hii ni KAULI TIMILIFU TENDEWA ISIO NA KIKOMO. Paulo anayarudia mawazo yake ya awali yaliyoelezwa katika 2 Kor. 4:2. Huduma yake pamoja na watenda kazi wake imekuwa ya wazi na ya uaminifu kikamilifu. Paulo alilitaka kanisa hili kuielewa nia ya huduma na matendo yake kwa uwazi kama vile Mungu alivyowafahamu.

◙**"dhamiri"** Angalia maelezo katika 2 Kor. 1:12

.

**5:12 "hatujisifu wenyewe"** Angalia maelezo kamili katika 2 Kor. 3:1.

◙**"ili mpate kuwa nayo mbele yao wanaojisifu kwa mambo ya nje tu, wala si kwa mambo ya moyoni"** Nia ya huduma na njia ni muhimu! Kwa uwazi kabisa Paulo anailinganisha huduma yake na viongozi wengine katika kanisa la Korintho (kama vile 2 Kor. 4:2, pia nukuu 1 Kor. 3:10-15). Viongozi wengine wote walijionyesha na hawakuwa na ile kweli.

◙**"hatujisifu. . . kujisifu"** Hii yote ni miundo ya neno *kauchēma*. Kuna kujisifu kwenye manufaa (yaani, kanisa linajisifu kwa sababu ya Paulo) na kule kujisifu kusikokuwa na manufaa (yaani, kule kujisifu kwa walimu wa uongo). Angalia MADA MAALUM: KUJISIFU (SPECIAL TOPIC: BOASTING) katika 1 Kor. 5:6.

◙**"mambo ya nje"** Angalia maelezo kamili katika 2 Kor. 1:11.

**5:13 "ikiwa. . . ikiwa"** Hizi zote ni SENTENSI SHURUTISHI DARAJA LA KWANZA, ambazo zinatazamiwa kuwa za kweli kutokana na mtazamo wa mwandishi au makusudi yake ya kifasihi.
**NASB, NKJV,**
**NRSV "tumeonekana kuwa wendawazimu"**
**TEV "vichaa halisi"**
**NJB "kutojihuuliza"**

Hili ni neno la Kiyunani "kusimama" (*histēmi*, Angalia Mada Maalum katika 1 Kor. 15:1) yenye KIHUSISHI "nje ya" (*ek*). Hiki kinaweza kutumika kuhusiana na

1. mshangao (kama vile Mt. 12:23; Marko 5:42)
2. woga (kama vile Marko 16:8; Luka 5:26)
3. mpagao (kama vile Matendo 10:10; 11:5; 22:17)
4. kurukwa na akili au kichaa (kama vile Marko 3:21; 2 Kor. 5:13)

Ni vigumu kuelewa kwa uthabiti kile anachokirejelea Paulo. Watoamaoni wengi wanalihusianisha hili na 11:1,16; 12:11. Hata hivyo, neno tofauti linatumika: "mpumbavu." Katika sura hizi Paulo anailinganisha desturi yake ya kiroho na zile sifa za wale walimu wenye vipaji vya uongo. Bila shaka hili ni oni kwamba hawa walimu wa bandia wamerejea kwa Paulo.

◙**"tunazo akili zetu timamu, ni kwa ajili yenu"** Paulo kwa uyumkini kabisa alikuwa na uhayawani wa kiroho wa muda mfupi (kama vile Matendo 9; 1 Kor. 14:5,18; 2 Kor. 12), lakini kwa upande wa huduma yeye aliishi na kuiwasilisha injili kwa ufasaha na kufikiri kwa hali ya juu, katika mstari ulionyooka pamoja na yale matarajio ya kitamaduni ya lile kundi ambalo aliliongoza (kama vile 1 Kor. 9:19-23).

**5:14 "Maana, upendo wa Kristo"** Kisarufi kwa vyo vyote vile hii ni: "upendo wa Kristo kwetu sisi" (yaani, KIIMA MILIKISHI) au "pendo letu kwa Kristo" (yaani, KISHAMILISHO MILIKISHI). Katika muktadha huu uchaguzi #1 ni bora.

**NASB "watubidisha"**
**NKJV "watushurutisha"**
**NRSV "watusistiza"**
**TEV "watutawala"**
**NJB "twashinda"**

Neno hili linamaanisha "kufunga kwa pamoja katika hali ya mbanano." Upendo hutawala ule uchaguzi na matendo yetu. Ile asili ya mwongozo wa injili wa yale matendo yaliyo sahihi; katika kipengele hiki kifo hadi lile kusudi la ubinafsi na ule mtindo wa maisha.

◙**"mmoja alikufa kwa ajili ya wote"** Ule upendo wa Mungu wa kiulimwengu unaonekana katika Kristo kama alivyomfia Myahudi na Mataifa (kama vile Efe. 2:11-3:13). Wanadamu wote kwa uwezekano walikombolewa katika Kristo (kama vile 2 Kor. 5:19; Yohana 3:16-18; 4:42; Rum. 5:18; 1 Tim. 2:4; 2 Pet. 3:9; 1 Yohana 2:2; 4:14). Mistari 14-15 iko katika uhusiano unaofanana. Uwakilishi wa upatanisho wa Kristo (kama vile Isaya 53) umehimizwa mara tatu. Kweli hii iliyo sawa inaelezwa katika Rum. 5:12-21. Mara nyingi hili linaitwa Adam/uainishi wa Kristo (kama vile 1 Wakorintho 15).

◙**"basi walikufa wote"** Kitheolojia waamini wanaungana na kifo cha Kristo katika ubatizo wao. Kifo chake kilitupatia msamaha na uzima wa milele (kama vile Warumi 6).

Kama tulivyorasimishwa katika kifo chake pia tunarasimishwa katika maisha ya kusulibiwa kwake kwa ajili ya wengine (kama vile 1 Yohana 3:16). Ubinafsi, maisha ya kujiendesha mwenyewe ni usahihi wa ile damu iliyonunuliwa kwa wale waaminio (kama vile 2 Kor. 5:15).

Katika *Synonyms of the Old Testament*, Robert B. Girdlestone ana mjadala mzuri kuhusianana na hii maana mpya ya neno "kifo" kwa waamini.

"Bwana wetu aliwaambia wanafunzi wake (Mt. 16. 28), 'Pana watu katika hawa wasimamao hapa, ambao hawataonja mauti kabisa, hata watakapomwona Mwana wa Adamu akija katika ufalme wake.' Haya maneno yanaelezwa katika mfumo mwingine na Mt. Marko (9. 1), 'Pana watu katika hawa wasimamao hapa, ambao hawataonja mauti kabisa, hata watakapouona ufalme wa Mungu umekuja kwa nguvu.' Pia angalia Luka 9. 27.

Kusudi la kifungu hiki lilikuwa kwa ajili ya kuandaa fikra za wanafunzi kwa ajili ya ile kweli iliyo kuu na ile mauti, ambayo mpaka sasa yule gaidi wa ulimwengu, inamlazimu kuupoteza *utamu* au *uchungu* katika upande wa wale walioungana wao kwa wao kwa Bwana katika imani. Kristo mwenyewe ilimpasa kufa, ilimpasa kuyapitia maumivu ya mateso ya kifo, Nafsi yake ilipaswa kuukabili uchungu kupita kiasi hata mauti, na kuwakomboa wale ambao kupitia woga wa kifo maisha yao yote yametawaliwa na utumwa. Hivyo yeye aliliweka wazo jipya la uzima na kifo, kwa kuwaambia wanafunzi wake ya kuwa ye yote atakaye taka kuyasalimisha maisha yake kwa kumkana Bwana, atayapoteza, ambapo ye yote atakeyeyatoa maisha yake kwa ajili ya Bwana atayasalimsha, naye atawasalimisha vile vile. Bwana atamwaibisha mtu katika Siku ile Kuu, bali atawakiri wengine.

Kule kuingia katika uzima mpya ambao hutokea kupitia imani katika Kristo katika maana nyingine kunahusisha kifo. Huku kunaitenga ile asili ya mwanadamu itokanayo na ile mifumo ya awali na zile kanuni za kuwepo kwake kwa maana nyingine, hiki ni kifo cha kuifia dhambi. Hivyo kama ilivyo hatima ya mwonekano ule mwili huacha kuhisi, hali ya mapigo ya moya hukoma, mikono huacha kufanya kazi, na miguu huacha kutembea, hivyo katika siri hii ya kifo mwili pamoja na viungo vyake vyote havina tena uwezo wa kuitumikia dhambi; uvunjaji ulio sawa au tofauti kubwa lazima iwepo kati ya Mkristo na dhambi kama ilivyo kati ya mwanadamu aliyekumbwa na kifo ile sura ya nje ya ulimwengu ambayo aliitumia kuishi na kujongea na kuwepo kwake. Kifo hiki kinahusiana kusulibiwa kwa Kristo, ambaye 'aliifia dhambi.' Muumini anabatizwa katika kifo cha Kristo, anakufa pamoja na Kristo, anaimarishwa kwa kifo chake, anasulibishwa na Kristo (Rum. 6. 5; 2 Kor. 5. 14; Gal. 2. 19, 20; kol. 2. 20, 3. 3)" (kr. 285, 286).

**5:15** Mstari wa 15 una ufanano na unatoa ufafanuzi wa 2 Kor. 5:14. Huu ndiyo ukweli wenyewe. Wokovu ni huru, bali maisha ya kumfanana Kristo yanaghalimikia kila kitu tulicho nacho na namna tulivyo (kama vile Gal. 2:20)!

**NASB, NKJV "kafufuka"**
**NRSV, TEV,**
**NJB "alifufuka"**

Hii ni KAULI YA KITENZI TENDEWA ENDELEVU yenye uwakala usioelezeka. Mara nyingi kitabu cha Agano Jipya kinazipa sifa kazi za ukombozi kwa nafsi zote za Uungu.

1. Mungu Baba aliyemfufua Yesu (kama vile Matendo 2:24; 3:15; 4:10; 5:30; 10:40; 13:30,33,34,37; 17:31; Rum. 6:4,9; 8:11; 10:9; 1 Kor. 6:14; 2 Kor. 4:14; Gal. 1:1;Efe. 1:20; Kol. 2:12; 1 The. 1:10)
2. Mungu Mwana alifufuka mwenyewe (kama vile Yohana 2:19-22; 10:17-18)
3. Mungu Roho aliyemfufua Yesu (kama vile Rum. 8:11)

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : 2 WAKORINTHO 5:16-19**

**16 Hata imekuwa, sisi tangu sasa hatumjui mtu awaye yote kwa jinsi ya mwili. Ingawa sisi tumemtambua Kristo kwa jinsi ya mwili, lakini sasa hatumtambui hivi tena. 17 Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya; ya kale yamepita tazama! Yamekuwa mapya. 18 Lakini vyote pia vyatokana na Mungu, aliyetupatanisha sisi na nafsi yake kwa Kristo, naye alitupa huduma ya upatanisho; 19 yaani, Mungu alikuwa ndani ya Kristo, akiupatanisha ulimwengu na nafsi yake, asiwahesabie makosa yao; naye ametia ndani yetu neno la upatanisho.**

**5:16"Hata imekuwa, sisi tangu sasa"** Maisha ya Kristo na kifo yameanzisha enzi mpya. Kila kitu ni tofauti katika nuru yake (kama vile Gal. 3:28; Kol. 3:11).

**NASB " hatumjui mtu awaye yote kwa jinsi ya mwili "**
**NKJV "hatumtambui ye yote kwa namna ya mwili"**
**NRSV "sisi hatupimi mtu yeyote kibinadamu"**
**TEV "hatuwezi kamwe, kuhukumu"**
**NJB "hatumfikirii mtu aweye yote kwa viwango vy mwili"**

Hili linaweza kuaksi 1 Sam. 16:7; Isa. 11:3; Yohana 7:24; 8:15. Yesu amebadili kila eneo la wokovu. Viwango vya mwanadamu sasa havitosherezi ile maana ya hukumu (kama vile Rum. 3:22; 1 Kor. 12:13; Gal. 3:28; Kol. 3:11). Kumjua Kristo hutubadilisha (kama vile 2 Kor. 5:17).
Hili linaweza kuaksi kuwa wengine waliokuwa miongoni mwa kanisa la Korintho wakafikia hatua ya kumtathimini Paulo, injili yake, na huduma yake (kama vile sura ya 4, 11, na 12).

Hili halimaanishi kuwa Paulo alifikiri kuwa historia ya Yesu haikuwa ya muhimu au hata kutofautishwa kwa kumtukuza Kristo. Paulo anayataja maisha ya Yesu ya hapa duniani, mafundisho, na yale matendo ya ukombozi (yaani, msalaba, ufufuo) wa mara kwa mara. Paulo anarejelea juu ya ile tathimini ya mwanadamu (yaani, kufahamu kulingana na mwili). Ukombozi huwaruhusu waamini kuyatazamia mambo yote ya maisha na historia kati nuru mpya iliyojikita katika Kristo. Historia ya mwanadamu inageuka kuwa katika historia ya wokovu. Mwanamume Yesu ndiye aliyekuwa Masihi, yule aliyeahidiwa. Maisha na mafundisho yake yalikuja Andiko lililovuviwa. Historia ya Israeli yapaswa kufasiriwa tena katika nuru yake!

Kwa neno "mwili" angalia Mada Maalum katika 1 Kor. 1:26.

**5:17 "akiwa "** Hii ni SENTENSI SHUTUTISHI DARAJA LA KWANZA nyingine kama zile zilizo katika 2 Kor. 5:13 na 16.

◙**"ndani ya Kristo"** Hii ni moja ya stiari za Paulo anazozipendelea kwa ajili ya kumbainisha Mkristo. Hii inazungumza juu ya ile nafasi yetu katika Kristo.

**NASB "kiumbe kipya"**
**NKJV, NRSV,**
**NJB, NIV "uumbaji mpya"**
**TEV "kuwa wapya"**

Paulo anafananisha uumbaji katika Rum. 8:18-25. Yeye anaubainisha uumbaji wa Mungu mpya, zama mpya, zile zama za Roho katika 2 Kor. 5:17 na Gal. 6:15. Waamini wanapaswa kuishi kama watu wa zile enzi mpya (kama vile Rum. 6:4).

**MADA MAALUM: *KTISIS* (SPECIAL TOPIC: *KTISIS*)**

◙ **"ya kale yamepita tazama! Yamekuwa mapya"** Angalia mwingiliano wa makusudi wa NYAKATI ZA VITENZI.

1. "ya kale yamepita" Hii ni kauli ya wakati uliopo katika DHAMIRA TEGEMEZI ambayo mara nyingi hurejerelea juu ya tendo lililotimilifu katika wakati uliopita. Kauli hii inarejelea juu ya mabadiliko.
2. "yamekuwa mapya" Huu ni WAKATI TIMILIFU wenye kurejelea tendo la wakati uliopita timilifu lenye matokeo ya kudumu. Kauli hii inaurejelea uwanafunzi.

Kuna tofauti ya machapisho ya Kiyunani ambayo yanaaksi hii aya ya "mambo yote" katika kifungu cha mwisho (yaani, MS $D^2$). Aina hii ya kubainisha ongezeko ni kawaida kwa weredi wa maandishi ya baadaye. Machapisho ya kale ya Kiyunani (yaani, MSS $P^{46}$, א,B, C, $D^*$, F, G) yanayoishia na *kaina*. $UBS^4$ inaupa usomaji huu dalaja "A" (yumkini).

Dhana hii ya "upya" ni sehemu ya asili ya maneno ya Agano la Kale ya neno *eschaton.* Manabii wa Agano la Kale walizungumzia hizi zama mpya.

1. "mambo mapya" (kama vile Isa. 42:9; 43:19; Yer. 31:22)
2. "agano jipya" (kama vile Yer. 31:31-34)
3. "moyo mpya, roho mpya" (Eze. 11:19; 18:31; 36:26)
4. "jina jipya" (kama vile Isa. 62:2; 56:5; 65:15)
5. "wimbo mpya" (kama vile Zab. 96:1; Isa. 42:10)
6. "mbingu mpya na nchi mpya" (kama vile Isa. 65:17; 66:22)

Huu upya wa matukio ya siku za mwisho umekuja katika Yesu, lakini yale ya kale yalikuwa yakiendelea. Yale yaliyo mapya bado hayajatimizwa kwa ukamilifu. Kupishana kwa hizi "zama mbili " za Kiyunani (angalia Mada Maalum katika 1 Kor. 1:20) kupitia huu Ujio wa Yesu wa mara ya Pili haukutabiriwa na manabii wa Agano la Kale ijapokuwa walitabiri juu ya Masihi katika maneno machache kabisa ya kitumishi pamoja na maneno ya ushindi wa utiifu

**5:18"Lakini vyote pia vyatokana na Mungu "** Hili ni pendo la Mungu ambalo lilimtuma mwana katika ulimwengu (kama vile Yohana 3:16). Wokovu ulitoka kwa Mungu moja kwa moja (angalia Mada Maalum katika 2 Kor. 8:16-17, kama vile Yohana 6:44,65; Efe. 1:4; 2:8-9), lakini waamini yawapasa kuitikia na kuendelea kuitikia juu ya Agano Jipya katika toba, imani, utii, na ustahimilivu.

◙**"aliyetupatanisha"** Huu ndiyo ukweli wa kitheolojia ulio mkuu. Kimsingi neno linamaanisha kubadilishana au kubadilisha na kukiweka kitu kwa pamoja kile kilichotengwa. Wanadamu wa uasi wamerejeshwa katika ushirika na Mungu kupitia Kristo. Mungu alibadilishana na haki ya Kristo (kama vile 2 Kor. 5:21) kwa ajili ya dhambi zao. Kristo kwa ajili yetu (kama vile 2 Kor. 5:14,21).

Muktadha huu (yaani, 2 Kor. 5:16-21) na Rum. 5:10-11 ni vifungu vyenye uhakika vya neno hili la kitheolojia. Wale watenda dhambi sasa ni marafiki, hata wanafamilia, kwa yule Aliye Mtakatifu. Urejesho wa huu ushirika ulivunjwa katika lile Anguko (kama vile Mwanzo 3) ambao umefanywa kwa ukamilifu katika Kristo.

Mjadala wa "upatanisho" kama ilivyo dhana ya yale matukio ya siku za mwisho katika Frank Stagg's *New Testament Theology*, kr. 102-104, 142.

◙**"naye alitupa huduma ya upatanisho"** Kitheolojia hii inafanana na 2 Kor. 5:14-15. Yesu alikuwa upatanisho wa waamini, sasa yawapasa kuwa njia ya ushiriki wa injili ya ipatanisho na wengine. Waamini hushiriki katika kifo cha Kristo na tunashiriki katika huduma Yake (kama vile 2 Kor. 5:19). Utumishi wa ufanano wa Kristo ndiyo lengo (kama vile 1 Yohana 3:16). Angalia MADA MAALUM: UONGOZI WA KITUMISHI (SPECIAL TOPIC: SERVANT LEADERSHIP) katika 1 Kor. 4:1.

**5:19"Mungu alikuwa ndani ya Kristo"** Hili ndilo jambo kuu la Ukristo. Mungu alikuwa (yaani, yule Mungu, yule YHWH wa Agano la Kale), katika yesu wa Nazarethi, kuupatanisha ulimwengu pamoja Naye (kama vile Gal. 1:3-4)? Kama ndivyo hivyo, Ukristo ni kweli; kama si hivyo, ni uongo. Je! Yesu ni utimiifu wa Mungu kweli (kama vile Yohana 1:1-14; Kol. 1:15-16; Flp. 2:6-11; Ebr. 1:2-3)? Je! Yeye ndiye njia pekee ya upatanisho na msamaha wa kweli (kama vile Yohana 14:6)? Kama ndivyo, hata injili ni habari ya muhimu sana kwa watu ambao hawakuwahi kuisikia! Yatupasa kuzungumza ukweli; yatupasa kuihubiri injili; yatupasa kumwinua Kristo; yatupasa kujitolea kwa ajili ya wokovu wa bure kwa ule ulimwengu uliopotea.

◙**"ulimwengu"** Mungu aliupenda ulimwengu (kama vile Yohana 3:16). Ulimwengu unaweza kuokolewa (kama vile 1 Tim. 2:4; 2 Pet. 3:9). Angalia Mada Maalum: Matumizi ya Paulo ya neno *Kosmos* katikt 1 Kor. 3:21b-22.

◙**"asiwahesabie makosa yao"** Hili linaweza kuaksi Zab. 32:2, ambayo imenukuliwa katika Rum. 4:6-8. Kabla ya Sheria, dhambi haikuhesabiwa kwa watu (kama vile Rum. 4:15; 5:13-14; Matendo 17:30). Lakini andiko hili lina ukweli mkuu pia. Katika sura ya uasi wa mwanadamu usiojulikana kuna masamaha katika Kristo. Damu ya Yesu husafisha dhambi zote! Dhambi si mpaka tena wa Mungu na mwanadamu, bali sasa ni

1. kutokuamini

2. kukana imani katika Kristo
3. kutokuwa tayari kuitikia juu ya kule kujitoa kwa Mungu

◙**"asiwahesabie"** Hili ni neno *logizomai*, ambalo limetumiwa na Paulo mara thearathini na nne, lakini katika ukamilifu wa maana mbili tofauti tofauti. Ile ya kwanza inaweza kuonekana katika 2 Kor. 3:5, "kufikiri" Angalia maelezo kamili pale.

Ile ya pili "kuhesabu" au "kuhesabia." Maana hii inaonekana vema katika Rum. 4:3,4,5,6,8,9,10,11,22,23,24, na Gal. 3:6. Tumizi hili la kitheolojia linamaanisha kuweka kitu fulani katika akaunti ya mtu katika benki fulani. Mungu aliiweka haki ya Yesu katika akaunti yetu (kama vile 2 Kor. 5:21). Pia Mungu hahesabu wala kuweka dhambi katika akaunti yetu. Jinsi gani Mungu alivyo wa ajabu! Jinsi gani alivyo Mwokozi wa kufaa!

◙**"naye ametia ndani yetu neno la upatanisho."** Ulimwengu uliopotea si hatua ya Mungu kukosa nguvu, upendo, bali ni hatua ya kutojali, kanisa lisilojali. Tunao ujumbe; tunazo funguo za Ufalme (kama vile Mt. 16:19; Ufu. 1:18; 3:7). Tunaye Roho Mtakatifu akaaye ndani yetu (kama vile Rum. 8:9,11; 1 Kor. 3:16; 6:19; 2 Tim. 1:14). Tunao mpangilio wa maagizo ya Yesu (kama vile Mt. 28:18-20). Je! Tutafanya nini?

**ANDIKO LA NASB (LILLILOBORESHWA) : 2 WAKORINTHO 5:20-21**
**[20] Basi tu wajumbe kwa ajili ya Kristo, kana kwamba Mungu anasihi kwa vinywa vyetu; twawaomba ninyi kwa ajili ya Kristo mpatanishwe na Mungu. [21] Yeye asiyejua dhambi alimfanya kuwa dhambi kwa ajili yetu, ili sisi tupate kuwa haki ya Mungu katika Yeye.**

**5:20"tu wajumbe kwa ajili ya Kristo"** Je! neno "sisi" na "ninyi" yaliyo katika mstari huu yanamrejelea nani? Je! Paulo ananena na kanisa? Kama ni hivyo neno"sisi" ni Paulo pamoja na kundi lake la umisheni na "ninyi," waamini wa kule Korintho. Watu hawa hawakuhitaji kuokolewa, bali walihitaji kurejeshwa katika umoja.

Zingatia kuwa haneni kuwa waamini lazima wawe wajumbe, bali kwamba hawa ni wajumbe. Hili ni sawa na ule usemi wa Yesu katika Mt. 5:13-16. Waamini ni chumvi na nuru. Swali ni aina gani ya chumvi na nuru. Hili ndilo swali hapa. Waamini ni wawakiishi wa Kristo, lakini ni aina gani ya wajumbe: yale makundi madogo madogo ya matengano, ya uasi, wasioshirikiana n.k.?

◙**"omba"** Angalia maelezo kamili katika 2 Kor. 1:4-11.

◙**"mpatanishwe na Mungu"** Hiki ni KITENZI TENDEWA CHENYE MASHARTI CHA WAKATI ULIOPO. Hii ni amri kwa watu waliopotea ama wale waliokolewa? Muktadha uliyo mpana ni kutoa amri juu ya maisha yenye kufaa kwa upande wa waamini. Yesu alituokoa kautoka dhambini na migongano; tumeokolewa ili yutumike! Tunaitwa katika ile huduma ya kumfanana Kristo, si agenda binafsi.

Muktadha huu una ujumbe kwa yule aliyepotea, mhitaji wa yule Kristo aliyeufia ulimwebgu kwa ajili yenu (haki ya mahali). Muktadha huu unao ujumbe kwa ajili ya yale makundi madogo madogo ya matengano, kanisa lisiloshiriki ambapo Kristo alkufa kwa ajili yenu (haki endelevu).

Hii IRABU TENDEWA inaweza kutafsiriwa kama "Mungu na awapatanishe ninyi pamaja Naye"; "jiruhusuni wenyewe kwa ajili ya kupatanishwa" (kama vile *The Jerome Biblical Commentary*, uk. 281); au "Mungu na awabadilishe kutoka katika uhadui kwenda katika urafiki wake" (kama vile TEV). Waamini wanaitangaza ukweli, Roho humfanya yule aliyepotea kuona hatia, Mwana hutoa maana, Baba hukamilisha Mapenzi Yake kupitia mwitikio wa agano.

**5:21** Muktadha huu una kweli kuu kadhaa.

1. Mungu alimtuma Yesu kwa ili kutufia sisi (kama vile Yohana 3:16). Yesu alikuja ili kutufia (kama vile. Marko 10:45).
2. Yesu alijua kuwa hana dhambi (kama vile Yohana 8:46; Ebr. 4:15; 7:26; 1 Pet. 1:19; 2:22; 1 Yohana 3:5).
3. Lengo ni ile haki binafsi, kutumika katika ufanano na Kristo (kama vile Rum. 8:28-29; 2 Kor. 3:18; Gal. 4:19; Efe. 1:4; 1 The. 3:13; 4:3; 1 Pet. 1:15). Hata hivyo, kuna maelezo ya dhahanio (DHAMIRA TEGEMEZI). Waamini wote hawatambui kwa ukamilifu sababu kamili ya Mungu katika wokovu. Huu ni wito kwa ajili ya kutumika, wito kwa ajili ya kijikataa wenyewe, wito kwa ajili ya utakatifu. Ukristo huanza tu mtu anapomwamini Kristo. Imani ndiyo hatua ya kwanza pekee ya ile safari ndefu.

**NASB "kuwa dhambi kwa ajili yetu"**
**NKJV "kuwa dhambi kwetu"**
**NRSV "kuwa dhambi"**
**TEV "kuzishiriki dhambi yetu"**
**NJB "mshindi kwa ajili yadhambi"**

Ni kwa jinsi gani Mungu alimfanya Yesu kuwa dhambi? Hili linaweza kuwa dokezo la Agano la Kale kwa sadaka ya dhambi (kama vile Isaya 53; Rum. 8:3). Mungu alimtoa Yesu kama mwanakondoo asiye na dhambi (kama vile Yohana 1:29,36).

Nafikiri maneno ya Yesu alipokuwa msalabani, "Mungu Wangu, Mungu Wangu, mbona Umeniacha" (kama vile Marko 15:34), ambayo ni nukuu kutoka Zaburi 22, inaaksi ule ukweli wa kiroho wa Baba kumwelekea Mwana (yaani, hali iliyoashiriwa na lile giza, kama vile Marko 15:33), kama Yeye alivyozichimba dhambi za ulimwengu. Kitheolojia hili linafanana na Gal. 3:13, "kufanyika laana kwa ajili yetu"!

## MASWALI YA MJADALA

Haya ni maoni ya mwongozo kwa kujisomea, ikiwa na maana kuwa unawajibika binafsi kwa tafsiri ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mtoa maoni tu.

Maswali haya ya kujadili yanatolewa kukusaidia mambo muhimu ya kipengele cha kitabu hiki. Yamekusudiwa kukuchokonoa mawazo na sio ya mwisho.

1. Je! sura hii inafundisha juu ya kile kipindi cha utengano baina ya kifo na ufufuo?
2. Je! 2 Kor. 5:10 inamaanisha kuwa waamini watahukumiwa? Kama ni hivyo, kwa ajili gani?
3. Orodhesha shauku mbili za Paulo kwa ajili unjilisti (2 Kor. 5:11,14).
4. Eleza kwa nini mistari ya 14-15 ni ya muhimu kwa ajili ya uaelewa sahhi wa Maisha ya Mkristo.

# 2 WAKORINTHO 6:1-7:1

| MGAWANYO WA AYA WA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **UBS[4]** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB** |
| Huduma ya Upatanisho | Alama za huduma | Ulinzi zaidi wa huduma yake ya Upatanisho | Urafiki pamoja na Mungu kupitia Kristo | Utume katika utendaji |
| (5:11-6:13) | | (5:11-6:13) | (5:11-6:13) | (5:11-6:13) |
| 5:11-6:10 | | | | |
| | 6:1-10 | | | |
| | Kuwa Mtakatifu | | 6:3-10 | Onyo |
| 6:11-13 | 6:11-7:1 | 6:11-13 | 6:11-13 | 6:11-13 |
| Hekalu la Mungu aliye hai | | Msifungiwe nira pamoja na wasioamini | Onyo dhidi ya ushawishi wa Kipagani | |
| 6:14-7:1 | | 6:14-7:1 | 6:14-7:1 | 6:14-7:1 |

**MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI** (Kutoka" **Mwongozo Mzuri wa Kusoma Biblia" (A Guaide to Good Bible Reading)**

## *KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Haya ni maoni ya mwongozo kwa kujisomea, ikiwa na maana kuwa unawajibika binafsi kwa tafsiri ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mtoa maoni tu.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA

A. Mstari wa 1 wa sura hii ni kiini kwa fasiri ya sura yote. Muktadha huwahusisha waaminio wa kanisa katika Korintho na kwa hiyo, haihusishi uasi (angalia Mada Maalumu katika 1 Kor. 6:9), Lakini walishindwa kuishi maisha ya Kikristo yenye kustahili.
B. Mwanzoni katika mstari wa 4 kuna mfululizo wa vihusishi.
   1. *en* na UHUSIKA WA WAKATI, mara kumi na nane, 2 Kor. 6:4-7

2. *dia* na UHUSIKA MILIKISHI, mara tatu , 2 Kor. 6:7-8
3. *hōs* na WAKATI ULIOPO ENDELEVU, mara saba, 2 Kor. 6:9-10
   Hii inaonekana kuhusisha ufafanuzi wa Huduma ya Paulo mbali na matatizo na shinikizo, yote ya ndani na ya nje, pamoja na neema ya Mungu inayofaa.

C. Kweli kinzani zilizo hitimishwa za 2 Kor. 6:8-10 zinaonekana kuelezea maisha ya Paulo, yote kutoka katika mtazamo wa wakosoaji na kutoka katika mtazamo wa Mungu.

D. Sehemu ya 6:14-7:1 inaonekana kuwa nje ya muktadha. Mstari wa 7:2 Huchukua istilahi na mjadala wa 2 Kor. 6:13. Sehemu hii kiasili ni ya Uyahudi. Ni onyo dhidi ya mtu mwenyewe kujitambulisha kuwa karibu na utamaduni wa Kipagani. Maonyo yanatoka kwenye muundo wa Agano la Kale (yaani, Wayahudi dhidi ya Mataifa au watu wa Mungu dhidi ya waabudu sanamu). Hata hivyo, Paulo anayatumia katika njia sawa na 1 Kor. 10:14-33, ambapo alijadili kushiriki kwa wakristo katika ibada ya Kipagani.

   Kuonekana kwa ukinzani kwenye aya hii kumesababisha nadharia za 2 Wakorintho kuwa barua yenye sehemu zaidi ya moja toka kwenye nyaraka kadhaa za Paulo alizozituma kule Korintho

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB(LILILOBORESHWA): 2 WAKORINTHO 6:1-10**

**[1] Nasi tukitenda kazi pamoja naye twawasihi msiipokee neema ya Mungu bure. [2] (Kwa maana asema, WAKATI ULIOKUBALIKA NALIKUSIKIA, SIKU YA WOKOVU NALIKUSAIDIA;tazama,WAKATI ULIOKUBALIKA ndiyo sasa; tazama SIKU YA WOKOVU NI SASA) [3] Tusiwe kw-azo la namna yo yote katika jambo lo lote, ili utumishi wetu usilaumiwe; [4] bali katika kila neno tujipatie sifa njema, kama watumishi wa Mungu; katika saburi nyingi, katika dhiki, katika misiba, katika shida; [5] katika mapigo, katika vifungo, katika fitina, katika taabu, katika kukesha, katika kufunga; [6] katika kuwa safi, katika elimu, katika uvumilivu, katika utu wema, katika Roho Mtakatifu, katika upendo usio unafiki; [7] katika neno la kweli, katika nguvu ya Mungu; kwa silaha za haki za mkono wa kuume na za mkono wa kushoto; [8] kwa utukufu na aibu; kwa kunenwa vibaya na kunenwa vema; kama wadanganyao, bali tu watu wa kweli; [9] kama wasiojulikana, bali wajulikanao sana; kama wanaokufa, kumbe tu hai; kama wanaorudiwa, bali wasiouawa; [10] kama wenye huzuni, bali siku zote tu wenye furaha; kama maskini, bali tukitajirisha wengi; kama wasio na kitu, bali tu wenye vitu vyote.**

**6:1 "Nasi tukitenda kazi pamoja naye"** Hii ni KAULI TENDAJI ENDELEVU YA WAKATI ULIOPO. Hakuna SHAMIRISHO iliyoelezwa, lakini muktadha unamaanisha “pamoja na Mungu” (kama vile 2 Kor. 5:20; 1 Kor. 3:9). Paulo hutumia neno hili hili kuelezea watendaji wenza katika injili (kama vile 2 Kor. 1:24; 8:23; 1 Kor. 16:16; Rum. 16:3,9,21), lakini hapa muktadha humaanisha hasa Mungu. Ni wazo gani la ajabu kwamba waaminio ni watendaji wenza kwa ajili ya Mungu (kama vile 1 Kor. 3:5-9).

◙ **"naye twawasihi"** Paulo alitumuia KITENZI kile kile katika Kor. 5:20. Angalia maelezo kamili katika 2 Kor. 1:4-11.

◙ **"msiipokee neema ya Mungu bure "** KITENZIJINA ni NJEO YA WAKATI ULIOPO USIOTIMILIFU, ambayo inarejelea kwa waaminio wa Korintho kumpokea Kristo. Lakini neno“bure” linarejelea kwa dhumuni la wokovu, ambao ni wenye kuzaa matunda kwa Ufalme, sio wokovu binafsi tu. Paulo mara nyingi anatumia neno hili kuelezea huduma hii iliyotarajiwa ya Ufalme (kama vile 1 Kor. 15:10,14,58; Gal. 2:2; Flp. 2:16; 2 The. 2:1; 3:5). Dhana hii ni mfanano na Matumizi ya Paulo ya neno “mwenende” katika Waefeso (kama vile Efe. 4:1,17; 5:2,15).

**6:2 "Kwa maana asema"** Paulo ananukuu kifungu cha maneno cha Agano la Kale kinachohusiana na Israeli, lakini matumizi ya kauli hii TENDAJI ELEKEZI YA WAKATI ULIOPO (yaani, asema), anaonyesha Kwamba ahadi hiyo ni muhimu kwa nyakati zote na kwa watu wote. Paulo anatumia nukuu hii kama rufaa ya moja kwa moja kutoka kwa Mungu hadi kwa kanisa la Wakorintho. Maandiko ni ya wakati uliopo na ni ya Muhimu!

◙ **"'WAKATI ULIOKUBALIKA"** Hii ni nukuu kutoka kwenye tafsiri ya andiko la agano la kale la Isa. 49:8 (yaani, moja ya shairi/nyimbo za mtumishi), ambayo inajishughulisha na Mungu kumkaribisha na kumwandaa (1) Masihi na (2) jumuiya ya Kimasihi. Mara nyingi kuna wasiwasi katika Isaya 40-53 kati ya ushirika (yaani, Israeli ya Kitaifa) na Mfalme bora wa Israeli (yaani, Masihi).

◙ **"' WAKATI ULIOKUBALIKA. . . WAKATI ULIOKUBALIKA'"** Nukuu ya kwanza kutoka katika tafsiri ya andiko la agano la kale la Kiyunani katika Isa. 49:8, akitumia *dektos*,lakini Paulo hutumia muundo wenye mkazo zaidi (iyaani, *eurosdektos*, kama vile Rum. 15:16) wakati anatumia unabii huu kwa hali ya Wakorintho (kama vile 2 Kor. 6:2b). Masihi amekuja na sasa ule ukaribisho wa moja kwa moja toka kwa Mungu umewaajilia. Wanapaswa kutwaa mara moja. Wanapaswa kuwa jamii ya Ki-Masihi ya matukio ya siku za mwisho.

Siku ya wokovu wa mtu ni wa kustaajabisha, na matukio ya kushangaza, lakini mara nyingi yalifuatana na mateso na matatizo (kama vile 2 Kor. 6:4-10).

**NASB, NKJV "Tazama"**
**NRSV "Angalia"**
**TEV "Sikiliza"**
**NJB "vizuri"**

Hiki ni KIAMBATA cha Kiyunani *idou*, ambayo hutumika kuleta uangalifu kwa kauli ya kweli. Paulo alilitumia mara nyingi katika 2 Wakorintho (kama vile 2 Kor. 5:17; 6:2,9; 7:11; 12:14).

◙ **"ndiyo sasa 'SIKU YA WOKOVU NI SASA'"** Sentensi hii ya mwisho katika 2 Kor. 6:2 ni maoni ya Paulo juu ya nukuu kutoka Isaya. Hii inaweza kurejelea kwa vyote mwaliko binafsi wa kuitikia injili, pamoja na maisha ya huduma kwa Ufalme wa Kimasihi.

**6:3 "Tusiwe kw-azo la namna yo yote"** Hii ni HASI MARADUFU yenye nguvu katika Kiyunani. Paulo alikusudia, vyote katika maisha yake binafsi na utumishi, sio kuweka vizuizi vyovyote kati yake na wasikilizaji wa injili (kama vile 1 Kor. 9:19-23). Alitumia maisha yake kutimiza mambo mawili: (1) kuwapatia mfano wa kufata katika utumishi wao na (2) kushinda mashtaka ya walimu wa uongo (kama vile 2 Kor. 11:12).

“Kikwanzo” pekee kilikuwa Kristo mwenyewe (kama vile 1 Kor. 1:18-25). Injili ilikataliwa na

1. wayahudi kwa sababu ya kuteswa kwa Masihi
2. mataifa kwa sababu ya ufufuo wa mwili
3. walimu wa uongo wa Korintho kwa sababu ya mapungufu ya Paulo ya uwasilishaji kiufasaha

Kwa sababu ya shetani kuwapofusha (kama vile 2 Kor. 4:4) na mvutano wa ujumbe wa injili wenyewe, Paulo hakuhitaji kufanya chochote ili kusababisha watu kukataa mahubiri yake (kama vile 1 Kor. 9:19-23,24-27).

**NASB "ili utumishi wetu usilaumiwe "**
**NKJV "ili utumishi wetu usiweze kulaumiwa"**
**NRSV "kusudi tusiwe na lawama yoyote katika utumishi wetu"**
**TEV "hatuhitaji mtu yeyote kupata lawama katika kazi yetu"**
**NJB "ili tuswe na lawama inayoweza kuwekwa kwenye kazi yetu ya huduma"**

Neno “yetu” (kama vile NKJV, NRSV, TEV, NJB) halipo katika maandiko ya Kiyunani, ambalo lina KIBAINISHI CHENYE UKOMO, “utumishi.” Mstari huu unahusiana kithiolojia na 1 Tim. 3:2-10, ambayo inaonyesha kwamba watumishi hawapaswi kushughulikia ukosoaji/uhakiki. Waaminio wanaishi na kutumikia kwa maendeleo ya Ufalme wa Kimasihi, sio kujiongezea wenyewe au ajenda za kibinafsi (kama vile 1 Kor. 9:12). Angalia MADA MAALUMU: UONGOZI WA KITUMISHI (SPECIAL TOPIC: SERVANT LEADERSHIP) katika 1 Kor. 4:1.

**6:4-7** Huu ni mfululizo wa maneno yaliyowasilishwa na KIHUSISHI cha Kiyunani *en*. Imerudiwa mara kumi na nane kwa msisitizo. Kuna orodha kadhaa katika maandiko ya Paulo juu ya matatizo ambayo alikumbana nayo (kama vile 1 Kor. 4:9-13; 2 Kor. 7:5; 11:23-29). Aliyataja kuhamasisha uaminifu na kupunguza thamani ya madai ya walimu wa uongo. Angalia Mada Maalumu: Uovu na Wema wa Agano Jipya katika 1 Kor. 5:9.-

**VIFUNGU VYA MANENO YA KIYUNANI VINAVYOWASILISHWA NA *EN***

| | NASB | NKJV | NRSV | TEV | NJB |
|---|---|---|---|---|---|
| v. 4, *hupomonē* | Saburi nyingi | Subira nyingi | Saburi kubwa | Saburi ya kuvumilia | Uvumilivu thabiti |
| v. 4, *thliphis* | Dhiki | Dhiki | Dhiki | Matatizo | Misiba |
| v. 4, *anagkē* | Misiba | Umaskini | Misiba | Misiba | Matatizo |
| v. 4, *stenochōria* | Shida | Shida | Maafa | Matatizo | Shida |
| v. 5, *plēgē* | Mapigo | Mapigo | Mapigo | Mapigo | Kupigwa |
| v. 5, *phulakē* | Vifungo | Vifungo | Vifungo | Kifungo | Peleka kifungoni |
| v. 5, *akatastasia* | Fitina | Fitina | Vurugu | Ghasia ya watu | Ghasia ya watu |
| v. 5, *kopos* | Taabu | Taabu | Taabu | Angamizwa | Taabika |
| v. 5, *agrupnia* | Kukesha | Kukesha | Kukesha usiku | Bila kulala | Kukesha |
| v. 5, *nēsteia* | Kufunga | Kufunga | Kufunga | Bila chakula | Kushinda na njaa |
| v. 6, *hagnotēs* | Kuwa safi | Kuwa safi | Kuwa safi | Kuwa safi | Kuwa safi |
| v. 6, *gnōsis* | Elimu | Elimu | Elimu | Elimu | Elimu |
| v. 6, *makrothumia* | Uvumilivu | Uvumilivu sana | Uvumilivu | Uvumilivu | Uvumilivu |
| v. 6, *chrēstotēs* | Utu wema | Utu wema | Utu wema | Utu wema | Utu wema |
| v. 6, pneumati hagiō | Roho Mtakatifu | Roho Mtakatifu | Utakatifu wa roho | Roho Mtakatifu | Roho Mtakatifu |
| v.6, agatiē anuplkritō | Upendo usio na unafiki | Upendo wa kweli | Upendo usio na unafiki | Upendo wa kweli | Upendo bure wa huba |
| v. 7, *logō aletheias* | Neno la kweli | Neno la kweli | Hotuba ya kweli | Ujumbe wa kweli | Neno la kweli |
| v. 7, *dunamei theou* | Nguvu ya Mungu | Nguvu ya Mungu | Nguvu ya Mungu | Nguvu ya Mungu | Nguvu ya Mungu |

**6:4 "bali katika kila neno tujipatie sifa njema, kama watumishi wa Mungu "** Hili ndilo jambo. Mstari huu ni rejeo la Kifungu cha neno "bure" cha 2 Kor. 6:1. Paulo anathibitisha kipaumbele cha huduma ya Ufalme. Waaminio wote ni (kama vile 1 Kor. 12:7,11) watumishi wenye vipawa (kama vile Efe. 4:12). Injili ina malengo yote lengo la mtu binafsi (yaani, wakovu wa kibinafsi) na lengo la ushirika (yaani, utangazaji wa injili na huduma ya injili, kama vile 1 Kor. 12:7). Angalia Mada Maalumu: Uongozi wa kitumishi katika 1 Kor. 4:1.

**6:6 "katika kuwa safi"** Mstari huu unarejelea ama kwa (1) maana ya mzizi wa neno hili, ukosefu wa kusudi au (2) maadili ya Paulo, maisha ya kimaadili.

◙ **"katika uvumilivu"** Neno hili mara nyingi linatumika kurejelea kuwa mvumilivu na watu, hata hivyo, pia limetumika katka Agano Jipya kurejelea kwa sifa ya Mungu (kama vile Rum. 2:4; 9:22; 2 Pet. 3:9,15).

◙ **"katika utu wema"**Hili neno mara nyingi limetafsiriwa "uzuri wa roho." Ni mtazamo kwamba afadhali aumie mmoja kuliko kuumiza wengine, afadhali kuwawezesha wengine kujipendeza kuliko kujipendeza wenyewe.

◙ **"katika Roho Mtakatifu"** The New English Bible hutafsiri hili kama "karama ya Roho Matakatifu." The *Jerome Biblical Commentary* ina kifungu cha maneno "katika Roho Mtakatifu" (uk. 282). Sababu ambayo walibadilisha tafsiri ni kwamba ni kawaida kwa Paulo kutaja mtu wa tatu ambaye ni Roho Mtakatifu katikati ya mfululizo wa maelezo. Nakubali kwamba inarejelewa kwa roho biafsi ya Paulo ya utakatifu uliozalishwa na Roho Mtakatifu, hata hivyo, mmoja hawezi kuwa mwenye kutangazwa kama imani ya kanisa kwa hili kwa sababu ya Rum.9:1; 14:17; 15:16; 1 Kor. 12:3; 1 The.1:5.

◙ **"katika upendo usio unafiki"** Kifungu hiki cha maneno sawa kimetumika katika Rum. 12:9.Paulo ametumia KIVUMISHI kile kile kuelezea imani katika 1 Timotheo 1:5 na 2 Tim. 1:5. Petro ametumia KIVUMSHI kile kile pamoja na KISAWE cha *agapē*, *philadelphia* katika1 Pet. 1:22.

**6:7 "katika neno la kweli"** NI lazima ikumbukwe kwamba historia ya Kiebrania kwa neno hili sio "ukweli dhidi ya uwongo," bali "utiifu na uaminifu," kama katika uhusiano wa kibinafsi (kama vile 1 Yohana 8:32; 14:6). Angalia MADA MAALUMU: "UKWELI" KATIKA MANDIKO YA PAULO (SPECIAL TOPIC: "TRUTH" IN PAUL'S WRITINGS) Katika 2 Kor. 13:8.

**Vifungu vya maneno ya Kiyunani vilivyowasilishwa na *dia***

| | NASB | NKJV | NRSV | TEV | NJB | NIV |
|---|---|---|---|---|---|---|
| v.7,hoplōntēs *dikaiosunēs* | Silaha za Haki | Silaha ya Haki | Silaha za Haki | Uadilifu ndiyo Silaha yetu | Silaha za Haki | Silaha za Haki |
| v.8,*dozēs kai atimias* | Utukufu na aibu | Heshima na kudharauliwa | Heshima na kudharauliwa | Kuheshimiwa na kudharauliwa | Nyakati za heshima na kudharauliwa | Utukufu na aibu |
| v.8,*dusphēmias kaieuphēmias* | Kunenwa vibaya na kunenwa vema | Kunenwa vibaya na kunenwa vema | Kulaumiwa na kusifiwa | Sifa mbaya na sifa njema | Kulaumiwa na kusifiwa | Kunenwa vibaya na kunenwa vema |

◙ **"kwa silaha za haki za mkono wa kuume na za mkono wa kushoto"** Mstari huu unarejea kwa utoaji wa Mungu kwa ajili ya vita vyetu vya Kiroho vya Dunia (kama vile 2 Kor. 2:11; Rum. 6:13; Efe. 2:2; 4:14,27; 6:10-18; 1 Pet. 5:8). Inawezekana kwamba mkono wa kuume unarejea juu ya silaha za kudhuru na mkono wa kushoto unarejea juu ya silaha za kujikinga. Angalia MADA MAALUMU: HAKI (SPECIAL TOPIC: RIGHTEOUSNESS) katika 1 kor. 1:30.

**6:8 "aibu"** Neno hili linatumika kwa mkazi kupoteza haki ya uraia.

Vifungu vya Kiyunani vilivyowasilishwa na *hōs*

| | NASB | NKJV | NRSV | TEV | NJB |
|---|---|---|---|---|---|
| v. 8, *planoi kai alētheis* | Kama wadanganyao, bali tu watu wa kweli | Kama wadanganyao, bali tu watu wa kweli | Twadhaniwa kuwa waongo kumbe twasema kweli | Kama waongo bali twasema kweli | Twachukuliwa kwa uongo bali sio wanafiki |
| v. 9, *agnooumenoi kai epigninōskomenoi* | Kama wasiojulikana, bali wajulikanao sana | Kama wasiojulikana, bali wajulikanao sana | Kama wasiojulikana, bali wajulikanao sana | Kama wasiojulikana, kumbe twajulikana kwa wote | Kama wasiojulikana bali tumekubaliwa |
| v. 9, *apothnēskontes kai idou zōmen* | Kama wanaokufa, kumbe tuhai | Kama wanaokufa, kumbe tu hai | kama wanaokufa bali tunaishi | Kama waliokufa lakini mwonavyo, sisi ni hai kabisa | Tunakufa bali tu hai |
| v. 9, *paideuomenoi kai mē thanatoumenoi* | Kama wanaorudiwa, bali wasiouawa | Kama wanaorudiwa bali wasiouawa | Kama wanaorudiwa, bali wasiouawa | Ingawa tumeadhibiwa, hatukuuawa | Tumeadhibiwa bali hatukuuawa |
| v. 10, *lupoumenoi aei de chairontes* | Kama wenye huzuni, bali siku zote tu wenye furaha | Kama wenye huzuni, bali siku zote tu wenye furaha | Kama wenye huzuni, bali siku zote tu wenye furaha | Ingawa tunayo huzuni, twafurahi daima | Tunayo maumivu bali siku zote tu wenye furaha tele |
| v. 10, *ptōchoi pollous de ploutizontes* | Kama maskini, bali tukiwatajirisha wengi | Kama maskini, bali tukiwatajirisha wengi | Kama maskini, bali tukiwatajirisha wengi | Ingawa tu maskini, twatajirisha watu wengi | Maskini bali twatajirisha watu wengi |
| v. 10, *mēden echontes kai panta katechontes* | Kama wasio na kitu, bali tu wenye vitu vyote | Kama wasio na kitu, bali tu wenye vitu vyote | Kama wasio na kitu, bali tu wenye kila kitu | Twaonekana kuwa watu tusio na chochote, kumbe tuna kila kitu | Hatuna chochote bali tu wenyekumiliki kila kitu |

**6:8-9 "bali tu. . . bali"** Maandiko ya Kiyunani yana neno *kai*, ambalo kawaida humaanisha "na," lakini katika baadhi ya maandiko linaweza kumaanisha "bali tu" (kama vile Yohana 20:29). Kumbuka mazingira huamua maana, sio msamiati.

**6:10 "kama wenye huzuni, bali siku zote tu wenye furaha"** (kama vile Rum. 5:3-5; Flp. 2:17-18; 3:1; 4:4; 1 The. 5:16)

◙ **"bali tu wenye vitu vyote"** Mfululizo huu wa kweli zilizo kama uwongo huonekana kutofautisha mtazamo wa ulimwengu na mtazamo wa Mungu. Waaminio ni warithi wa vitu vyote kupitia Kristo (kama vile Rum. 8:17,32; 1 Kor. 3:21).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 2 WAKORINTHO 6:11-13**

**11 Vinywa vyetu vimefumbuliwa kwenu, enyi Wakorintho; mioyo yetu imekunjuliwa. 12 Hamsongwi ndani yetu, bali mwasongwa katika mioyo yenu. 13 Basi, ili mlipe kadiri ile mliyopewa (nasema nanyi kama na watoto), nanyi pia mkunjuliwe mioyo.**

**6:11** VITENZI viwili vyote ni NJEO YA WAKATI ULIPO. Paulo amewashirikisha wote, ukweli kamili wa injili na maana zake pamoja na Wakorintho waamini katika uwazi kamili na uaminifu.

◙ **"enyi Wakorintho"** Hii ni moja ya sehemu tatu tu katika maandiko ya Paulo kwamba yeye binafsi anasema kanisa fulani analoliandikia (kama vile Gal. 3:1; Flp. 4:15). Vifungu vyote hivi vinaonyesha mkazo wa mioyo ya Mitume.

**6:12**
**NASB "Hamsongwi ndani yetu"**
**NKJV "hamsongwi ndani yetu"**
**NRSV "hakuna kusongwa"**
**TEV "sio sisi tuliofunga mioyo yetu kwenu"**
**NJB "kama mnaona kizuizi chochote kile, kiko kwenu nyinyi, na si kwa upande wetu"**

Mtindo wa NOMINO (JINA) wa KITENZI hiki umetumika katika 2 Kor. 6:4 na 12:10 (kama vile Rum. 2:9; 8:35). Kiuhalisia inarejea kwa kitu fulani au watu fulani waliosongamana pamoja katika sehemu ndogo, na hivyo wakawa duni. Ilitumika kisitiari kwa "kusongwa," "duni," au "uchungu" (kama vile 2 Kor. 4:8; 6:12).
**NASB, NKJV,**
**NRSV "mioyo yenu"**
**TEV "kufungw mioyo yenu"**
**NJB "maumivu"**
Hii ni sitiari ya Agano la Kale kutoka kwenye neno "matumbo." Wazee walifikiri viungo vya ndani au viungo vikuu (yaani, moyo, ini, mapafu) vilikuwa mahali pa hisia (kama vile Andiko la agano la kale Mith. 12:10; 26:22; Yer. 28:13,51; II Macc. 9:5-6; IV Macc. 10:8; Baruch 2:17). Paulo hutumia sitiari hii mara nyingi (kama vile 2 Kor. 6:12; 7:15; Flp. 1:8; 2:1; Kol. 3:12; Filemoni 1:7,12,20).

**6:13**
**NASB "bali, ili mlipe kadri ile mliyopewa"**
**NKJV "wekeni mioyo yenu wazi kama nasi tulivyofanya"**
**NRSV "kwa kurudisha"**
**NJB "kwa kubadilishana kwa haki"**
Katika kifungu hiki neno kuu ni *antimisthia*, ambalo ni neno *misthos* (yaani, fidia kulingana na kile ambacho mtu anastahili, kama vile. 1 Kor. 3:8,14; 9:17-18; 1 Tim. 5:18) na KIHUSISHI *anti*. Mtindo huu unapatikana hapa tu na katika Rum. 1:27.Neno hili linaweza kutumika katika maana chanya au hasi; Mazingira yanapaswa kuamua.Katika Rum.1:27; ni hasi, lakini hapa inanekana kuwa imetumika vizuri kwa maana ya Gal. 4:12.

◙ **"na watoto"** Paulo, kama Yohana, anawaelezea waamini wapya kama watoto (kama vile 1 Kor. 4:14,17; Gal. 4:19; 1 Tim. 1:2,18; 2 Tim. 1:2; 2:1; Tito 1:4; Filemoni1:10).

◙ **"nanyi pia mkunjuliwe mioyo"** Kama Paulo alivyoukunjua moyo wake kuwajumuisha, kama kikundi kidogo ndani ya kundi kubwa na ushindani kama walivyokuwa, yeye alitaka kwa bidii wao kurudi. Hii ni KAULI TENDEWA SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO USIOTIMILIFU. Angalia wazo TENDWA kwamba hawawezi kulifanya wenyewe, lakini wanapaswa kumruhusu Mungu kulifanya.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 2 WAKORINTHO 6:14-18**
**[14] Msifungiwe nira pamoja na wasioamini, kwa jinsi isivyo sawasawa; kwa maana pana urafiki gani kati ya haki na uasi? Tena pana shirika gani kati ya nuru na giza? [15] Tena pana ulinganifu gani kati ya Kristo na Beliari? Au yeye aaminiye ana sehemu gani pamoja na yeye asiyeamini? [16] Tena pana mapatano gani kati ya hekalu la Mungu na sanamu? Kwa maana sisi tu hekalu la Mungu aliye hai; kama Mungu alivyosema, ya kwamba,**

**NITAKAA NDANI YAO, NA KATI YAO NITATEMBEA, NAMI NITAKUWA MUNGU WAO, NAO WATAKUWA WATU WANGU. [17] Kwa hiyo, TOKENI KATI YAO, MKATENGWE NAO, asema Bwana, MSIGUSE KITU KILICHO KICHAFU, Nami nitawakaribisha. [18] Nitakuwa Baba kwenu, Nanyi mtakuwa kwangu wanangu wa kiume na wa kike,**

**6:14**
**NASB "Msifuungiwe nira pamoja na wasioamini"**
**NKJV "Msilinganishwe nira pamoja na wasioamini"**
**NRSV "Msichukuane pamoja na wasioaminis"**
**TEV "Msiambatanishwe na watu wasioamini"**
**NJB "Msishirikiane katika usawa pamoja na wasioamini"**

Paulo mara nyingi hutumia nukuu za kilimo za Agano la Kale kueleza kwa mifano ukweli wa Wakristo (kama vile 1 Kor. 9:9; 1 Tim. 5:18) kutafakari Kumb. 22:10. Ni KAULI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO pamoja na KIAMBATA HASI, ambacho humaanisha "walikuwa wakifanya" uhusiano huu usiofaa, wa ndani, wa kibinafsi pamoja na wasioamini. Neno la Kiyunani ni ambatani kwa neno"kutiwa nira" (*zugeō*) na "lingine la aina tofauti" (*heteros*, yaani, aina tofauti za wanyama). Mstari huu umekuwa maandiko yaliyothibitishwa katika uhusiano kwa waaminio kuoa wasioamini. Hata hivyo, maandiko haya hayaonekani kujishughulisha dhahiri na ndoa, ingawa kwamba kwa hakika imehusishwa katika kauli hii pana. Waaminio wanapaswa kuzuia uhusiano wao binafsi wa ndani zaidi kwa waaminio wenzao. Hii hutusaidia upiganaji wa tamaduni zilizo anguka kuwa mbali na Kristo. Imani katika Yesu na Roho yenye kukaa imesababisha mpasuko uliowazi na uliowekwa ndani sana miongoni mwa familia, biashara, matamanio, furaha, hata makanisa.

Mtu anapaswa kuweka katika hesabu vifungu kama 1 Kor. 5:9-13; 7:12-16; 10:27 kupata uwiano wa kitheolojia wa ukweli huu. Tunapaswa kukumbuka udhaifu wa utamaduni wa kipagani wa karne ya kwanza. Huu sio uthibitisho wa kuishi kwa utawa, lakini jaribio la kupunguza uhusiano binafsi wa ndani na mfumo wa ulimwengu ulioanguka (kama vile 1 Yohana 2:15-17).

◙**" kwa maana pana urafiki gani kati ya haki na uasi "** Ukweli huu unaofanana umerudiwa katika mfuatano wa waraka ya Waefeso (kama vile 2 Kor. 5:7,11). Tofauti ya Paulo ya haki na uasi huonyesha wazi kwamba katika muktadha huu haki hairejelei kwa haki iliyodhaniwa (katika Warumi 4; Wagalantia 3), lakini kuisha kwa haki (kama vile Mt. 6:1). Angalia MADA MAALUMU: HAKI (SPECIAL TOIPIC: RIGHTEOUSNESS) katika 1 Kor. 1:30.

◙ **" shirika:** Angalia Mada Maalumu katika 1 Kor. 1:9.

**6:15**
**NASB, NKJV "Beliaril"**
**NRSV, NJB "Beliari"**
**TEV "Ibilisi"**

Hili ni neno la Kiebrania (yaani, *beli* na *ya'al*, angalia BDB 116) ambalo asili yakeya neno kwa namna fulani inatia shaka. *Beliar* ni matamshi tofauti kutoka katika baadhi ya maandiko ya Kiyahudi. Historia zinazowezekana ni:

1. kutokuwa na thamani (yaani, ufafanuzi wa watu waovu, kama vile Kumb. 13:13; 2 Sam. 23:6; 1 Kgs. 21:10,13)
2. uasi (kama vile 2 Sam. 22:5)
3. mahali pale ambapo hakuna upaaji (yaani, *Sheol*, kama vile Zab. 18:4)
4. Neno lingine kwa Shetani (kama vile Nah 1:15; Jubilii 1:20; 15:33; na Magombo ya Bahari ya Chumvi [ex. IQS 1:18,24; 2:5,19])

**6:16 " Tena pana mapatano gani kati ya hekalu la Mungu na sanamu "** Mstari huu unapaswa kulinganishwa na Kor. 3:16, ambapo kanisa la mahali linaitwa hekalu la Mungu. Katika 1 Kor. 3:16 hakuna KIBAINISHI kilicho na "hekalu" (yaani *naos*, madhabahu kuu yenyewe). KIWAKILISHI NOMONO "wewe" ni WINGI, wakati "hekalu' ni UMOJA, kwa

hiyo, katika muktadha huu neno"hekalu" linapaswa kurejea kwa kanisa lote katika Korintho (kama vile Efe. 2:21-22).

Lengo la imani ya Wayahudi liliendelezwa katika taratibu za ibada na kawaida ya Ushirika Mtakatifu (kama vile Yeremia 7) badala ya imani binafsi kwa YHWH. Sio wapi au lini au namna gani mtu husujudu, lakini ni nani ambaye ana uhusiano na, Mungu. Yesu aliona mwili wake kama Hekalu la Mungu (kama vile Yohana 2:21). Yesu ni mkuu kuliko hekalu la Agano la Kale (kama vile Mt. 12:6). Shughuli ya Mungu imehama kutoka jengo takatifu kuingia mwili wa waaminio (yaani, alikombolewa, mtakatifu) watakatifu.

Sanamu na waaminio wamejadiliwa kimamilifu katika 1 Kor 8 na 10:14-22. Haya yanapaswa kuwa maalum kwa pande zote! Njia zote haziongozi kwenda mbinguni!

◙ **"Mungu aliye hai"** Jina la agano kwa Mungu kwenye Agano la Kale lilikuwa YHWH (angalia Mada Maaalumu katika 1 Kor. 2:8), ambao ulikuwa mtindo wa KITENZI cha neno "kuwa." Waandishi wa Agano la Kale mara nyingi wametumia KIVUMISHI "aliye hai" kuaksi Yeye aishiye milele, Mungu aliye hai pekee. Vidokezo vya Agano la Kale katika 2 Kor. 6:16-18 vina istilahi ya agano ndani yake, "nami nitakuwa Mungu wao, nao watakuwa watu wangu" (kama vile Ezek. 37:27).

Kifungu cha maneno "nitakwenda kati yenu" huonekana kutoka Law.26:12. Maandiko ya Agano la Kale katika 2 Kor. 6:16 yanaaksi enzi mpya wakati YHWH atakaa pamoja na watu wake kama ilivyo kusudiwa katika Mwanzo 2 na ilitokea kwa muda na kwa upendeleo katika kipindi cha safari ndefu ya jangwani, lakini itatambulika kikamilifu katika mbigu mpya na dunia mpya (kama vile Ufunuo 21-22).

◙ **"Mungu alivyosema"** Huu ni ushirikiano uliofunguka wa Law. 26:11-12 na Ezek. 37:27 Kutoka andiko la agano la kale. Katika muktadha huu Paulo anatumia ahadi hizi kiasilia kwa agano la Israeli na kanisa ambalo ni Israeli ya Kiroho (kama vile Rum. 9:6; Gal. 6:16).

**6:17 "TOKENI KATI YAO. . . MKATENGWE NAO"** Hizi zote ni KAULI SHURUTISHI ZA WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFU. Hivi ni vidokezo kwa Isa. 52:11 katika andiko la agano la kale. Watu wa Mungu wanajitenga wenyewe kutoka kwa watenda dhambi na wasioamini wala wasihukumiwe katika hukumu zao (kama vile. Ufu.18:4).

Mara nyingi nasikia mstari huu umenukuliwa katika uhusiano kwa madhehebu ambayo mtu hustahili kuwa. Napenda kumnukuu F. F. Bruce katika *Answers to Questions*, " Matumizi ya maneno haya kuthibitisha utengano wa kanisa la Kikristo kati ya wakristo wenye dalili ya ubaya walioshindwa kusomwa kwenye muktadha huu " (uk. 103).

◙ **"MSIGUSE KITU KILICHO KICHAFU"** Hii ni KAULI YA KATI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO. Waaminio hawapaswi kushiriki katika matendo ya dhambi kulingana na utamaduni wao. Kama waliokombolewa tunapaswa kudhihirisha na kutangaza mioyo mipya na fikra mpya ya watu wa Mungu. Kila kitu kimebadilika katika Yeye!

**6:18** Mstari huu huaksi ukweli wa manabii wengi, lakini kikamilifu zaidi, ni Hosea (au yumkini 2 Sam. 7:14). Ukristo ni shauri ya familia.

◙ **"mungu mwenyezi"** Hii huaksi neno la Agano la Kale kwa Mungu, YHWH (kama vile Kut. 3:14), na *El Shaddai* (kama vile Kut. 6:3). Katika andiko la agano la kale hutafsiri kifungu kama "Bwana wa Majeshi." Angalia MADA MAALUMU: MAJINA YA UUNGU (SPECIAL TOPIC: NAMES FOR DEITY) katika 1 Kor. 2:8

**ANDIKO LA NASB (LILILOBPRESHWA): 2 WAKORINTHO 7:1**
[1] **Basi, wapenzi wangu, kwa kuwa tuna ahadi hizo, na tujitakase nafsi zetu na uchafu wote wa mwili na roho, huku tukitimiza utakatifu katika kumcha Mungu.**

**7:1 "kwa kuwa tuna ahadi hizo"** Hii ni KAULI TENDAJI ENDELEVU YA WAKATI ULIOPO. Paulo alinukuu maneno ya kitume ya agano la kale kutoka kwa Mungu kama vile waliyatumia kwa wakati uliopo kwa Wakorintho (kama vile 2

Kor. 6:2). Agano la Kale pia limenukuliwa katika2 Kor. 6:16-18, Kuonyesha shauku ya kuendelea ya YHWH kwa watu ambao wanaaksi tabia yake. Paulo anajaribu kuwasababisha waaminio wa Korintho kuishi maisha ya ki-Ungu, maisha tofauti. Walikuwa na "neema" (kama vile 2 Kor. 6:1), sasa wanapaswa kuishi ndani yake. Mstari huu ni wito kwa utakatifu wa kuishi kama Kristo (kama vile Efe. 1:4; 2:10).

◙ **"wapenzi wangu"** Kifungu hiki cha maneno kimetumika katika Mt. 3:17 na 17:5 kama sifa kwa Yesu. Paulo hutumia neno hili hili kuelezea wafuasi wa Yesu (kama vile 2 Kor. 12:19; 1 Kor. 10:14; 15:58; Rum. 12:19; Flp. 2:12; 4:1). Neno hili huzungumzia uaminifu wa upendo wa agano ulioimarishwa na Mungu (Kiebrania, *hesed*; Kiyunani, *agapē*) Kwa ajili yetu katika Kristo, lakini hapa linazungumzia upendo wa Paulo kwa kanisa hili, lenye kikundi kidogo, wenye kiburi, na wenye kujitenga.

◙ **"na tujitakase nafsi zetu"** Hii ni KAULI TENDAJI TEGEMEZI YA WAKATI ULIOPITA USIOTIMLIFU. Njeo ya WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFU ni njia ya kuthibitisha kitendo katika lunga ya kawaida ya Kiyunani inayozungumzwa Koine. Ina weza kuwa na maana nyigi tofauti (angalia D. A. Carson, *Exegetical Fallacies*, 2nd ed., kr. 68-73). Hapa ni wito kwa kitendo chenye maamuzi (yaani, KAULI YENYE MASHARTI TEGEMEZI YA WAKATI ULIOPO imetumika kama KAULI SHURUTISHI. DHAMIRA TEGEMEZI hutoa ishara ya tukio la nasibi/bila kutarajiwa. Waamino wanapaswa kushirikiana na Mungu katika wokovu na kisha kushirikiana katika ukomavu.

◙ **"wa mwili na roho"** Mstari huu huzungumzia ubinadamu wetu wote. Watu wengi walikataa mstari huu kuwa halisi kwa sababu ya matumizi ya kiufundi ya Paulo ya maneno haya mawili katika mazingira mengine. Hata hivyo, 2 Kor. 7:5, wakati inaunganishwa na 2 Kor. 2:13 (ambao ni mwanzo na mwisho wa Muendelezo wa Paulo uliotengwa), ilitumia maneno haya mawili kwa maana sawa katika hali tofauti (soma *A Man in Christ* by James S. Stewart, Harper and Row).

◙**"huku tukitimiza utakatifu katika kumcha Mungu"** Hii ni KAULI TENDAJI ENDELEVU YA WAKATI ULIOPO. Ni kweli ki-theolojia kwamba wakati tunakombolewa, sote tunathibitishwa na kutakaswa papo hapo (kama vile 1 Kor. 1:30, pia angalia MADA MAALUM: UTAKATIFU WA AGANO JIPYA/UTAKASO (SPECIA TOPIC: NEW TESTAMENT HOLINESS/SANCTIFICATION katika 1 Kor. 1:2). Hii huzungumzia nafasi yetu katika Kristo. Hata hivyo, tunapaswa kuishi katika nuru ya nafasi yetu. Kwa hiyo, tunaaswa kutimiliza wito wetu kwa kuendeleza utakaso au kuishi kama Kristo (kama vile Rum. 8:28-29; Efe. 4:1). Haya ni mapambano yanayoendelea (kama vile Warumi 7). Kama ilivyo wokovu ni zawadi ya bure na wajibu wa gharama, vivyo hivyo pia, hata utakaso. Dhana hii sawa ni ya kweli kwa waaminio kuitwa watakatifu (KAULI ELEKEZI) na kisha kuitwa kuwa watakatifu (KAULI SHURUTISHI). Siamini katika uwezekano wa kuwa wenye dhambi katika maisha haya, lakini ninaamini katika kufaa kwa waaminio kutenda dhambi ndogo na ndogo zaidi! Hii ni ki-theolojia na wasiwasi wa utendaji uliosababishwa na waaminio kuwa katika Ufalme,lakini Ufalme haujakamilishwa (kama vile. Fee, Stewart, *How to Read the Bible For All Its Worth*, kr. 131-134).

## MASWALI YA MJADALA

Haya ni maoni ya mwongozo kwa kujisomea, ikiwa na maana kuwa unawajibika binafsi kwa tafsiri ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mtoa maoni tu.

Maswali haya ya kujadili yanatolewa ili kukusaidia kufikiri mambo muhimu yaliyoko katika kipengele cha kitabu hiki. Yanamaanisha kuwa maswali ya kichokonozi, yasio ya hakika.

1. Je 2 Kor. 6:1 inafundisha kwamba tunaweza kupoteza wokovu wetu?
2. Ni jinsi gani Wakristo wanaweza kuishi ili kutoweka vikwazo vyovyote mbele ya wenzao?
3. kwanini maisha ya Paulo yalikuwa magumu?
4. Je kifungu cha maneno "mkatengwe nao" kina maanisha nini?
5. Je wokovu ni bure bila shaka au unatugharimu kila kitu?

# 2 WAKORINTHO 7:2-16

| MGAWANYO WA AYA WA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| UBS[4] | NKJV | NRSV | TEV | NJB |
| | | | | Onyo (6:11-7:4) |
| Furaha ya Paulo kwa ajili ya toba ya kanisa | Mwitikio wa Wakorintho | Furaha ya Paulo | Furaha ya Paulo | |
| 7:2-4 | 7:2-12 | 7:2-4 | 7:2-4 | 7:2-4 |
| | | | | Paulo Makedonia: Tito aliungana na Paulo |
| 7:5-13a | | 7:5-13a | 7:5-7 | 7:5-7 |
| | | | 7:8-11 | 7:8-13a |
| | Furaha ya Tito 7:13-16 | | 7:12-13a | |
| 7:13b-16 | | 7:13b-16 | 7:13b-16 | 7:13b-16 |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (Kutoka" **Mwongozo Mzuri wa Kusoma Biblia" (A Guide to Good Bible Reading)**

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Haya ni maoni ya mwongozo kwa kujisomea, ikiwa na maana kuwa unawajibika binafsi kwa tafsiri ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mtoa maoni tu.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

5. Aya ya kwanza
6. Aya ya pili
7. Aya tatu
8. N.k

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 2 WAKORINTHO 7:2-4**
**2 Tupeni nafasi mioyoni mwenu. Hatukumdhulumu mtu ye yote, wala kumharibu mtu, wala kumkaramkia mtu. 3 Sisemi neno hilo ili niwahukumu ninyi kuwa na hatia; kwa maana nimetangulia kusema, ya kwamba ninyi mmo mioyoni mwetu hata kwa kufa pamoja, na kuishi pamoja. 4 Ninao ujasiri mwingi kwenu; naona fahari kuu juu yenu. Nimejaa faraja, katika dhiki yetu yote nimejaa furaha ya kupita kiasi.**

**7:2 "Tupeni nafasi mioyoni mwenu"** Aya hii huchukua wazo la 2 Kor. 6:13. Ni KAULI TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFU, amri yenye maamuzi, lakini ikiwa na msisitizo endelevu. Paulo hutaja wazo hili hili katika 2 Kor. 6:13. Yeye hutumia KINYUME katika 2 Kor.6:12 (yaani, kuzuia). Paulo hutamani kwamba wajiweke wazi kwake kama alivyokwisha kujiweka wazi kwao.

Neno “moyo” katika 2 Kor. 6: 11 ni njia ya kujirejelea mwenyewe. Paulo anafanya jambo hilo hilo likiwa na neno “mwili” katika 2 Kor. 7:5 na “roho” katika 2 Kor. 7:13b. Angalia maelezo kamili katika 2 Kor.7:5.

◙**"Hatukumdhulumu mtu ye yote, wala kumharibu mtu, wala kumkaramkia mtu"** Hizi zote ni KAULI TENDAJI ELEKEZI ZA WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFU. Neno “mtu ye yote” limerudiwa na kuandikwa mbele ya kila kifungu cha maneno kwa ajili ya kusisitiza. Vifungu hivi vinahusishwa na vitendo vya walimu wa mafundisho ya uongo ama mashtaka yaliyofanywa na wakosoaji wa Paulo kuhusu yeye pamoja na huduma yake (kama vile 2 Kor. 12:17-18).

◙ **"kumharibu"** Angalia Mada Maalum katika 1 Kor. 15:42.

**7:3 "kwa kufa pamoja, na kuishi pamoja"** Kiyunani kina “Ningekufa na wewe ama kuendelea kuishi na wewe” KITENZI cha kwanza ni KAULI TENDAJI ISIYO NA UKOMO YA WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFU na cha pili ni KAULI TENDAJI ISIYO NA UKOMO YA WAKATI ULIOPO. Hii inaweza kurejea kwa 6:1. Paulo anatamani kanisa lililokomaa, lenye kutenda kazi katika Korintho. Ikiwa watafuata uongozi na mamlaka yake watazaa matunda, ila kama hawatafanya hivyo, watakuwa wamekuwepo bure. Inawezekana pia kwamba hii ni lahaja ya kitamaduni ya kujitoa hadi mwisho.

**7:4 "ujasiri"** Angalia Mada Maalum: *Parrhēsia* katika 2 Kor. 3:12.

◙**"fahari"** Angalia usomaji wa neno kamili katika 1 Kor. 5:6 na Mada Maalum katika 2 Kor. 1:12.

◙ **"Nimejaa faraja; nimejaa furaha ya kupita kiasi"** Mstari huu unaonekana kurejea kwa taarifa ya Tito katika 2 Kor. 7:6-13a. Paulo alikuwa amehamasika sana kuhusu hali ya kiroho ya makanisa yake (kama vile Gal. 4:19).
Neno kujaa kupita kiasi/kufurika (yaani, *huperperisseuomai*, kama vile Rum. 5:20) ni mtindo uliotiwa nguvu wa *perisseuō*. Yenyewe na mitindo yake iliyohusishwa imetumiwa mara nyingi na Paulo katika barua zake kwa Wakorintho. Angalia Mada Maalum: Matumizi ambatani ya Paulo ya neno *Huper* katika 1 Kor. 2:1.

1. *perissos/perissoteros*
   a. Kubwa kuliko inavyohitajika (kama vile 1 Kor. 12:23,24; 15:10)
   b. wingi uliozidi mpaka (kama vile 2 Kor. 2:7; 10:8)
   c. liozidi/kupita kiasi (kama vile 2 Kor. 9:1)
2. *perissoterōs*, kwa wingi zaidi (kama vile 2 Kor 1:12; 2:4; 7:13,15; 11:23; 12:15)
3. *perisseuō*
   a. Kuwa na wingi (kama vile 2 Kor. 1:5; 3:9; 9:8,12)
   b. kujazwa karama (kama vile 1 Kor. 14:12; 2 Kor. 8:7)
   c. Kuwa na wingi katika utendaji (kama vile 1 Kor. 15:58)
   d. wingi katika chakula (kama vile 1 Kor. 8:8)
   e. kusababisha kujazwa wingi (kama vile 2 Kor. 4:14; 9:8)
4. *perisseuma*, wingi wa kuzidi kiasi (kama vile 2 Kor. 8:13,14)
5. *perisseia*, wingi wa kuzidi kiasi (kama vile 2 Kor. 8:2; 10:15)

◙ **"katika dhiki yetu yote"** Angalia MADA MAALUM: DHIKI KUU (SPECIAL TOPIC: TRIBULATION) katika 2 Kor. 1:4

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 2 WAKORINTHO 7:5-13A**

**5 Kwa maana hata tulipokuwa tumefika Makedonia miili yetu haikupata nafuu; bali tulidhikika kote kote; nje palikuwa na vita, ndani hofu. 6 Lakini Mungu, mwenye kuwafariji wanyonge, alitufariji kwa kuja kwake Tito. 7 Wala si kwa kuja kwake tu, bali kwa zile faraja nazo alizofarijiwa kwenu, akituarifu habari ya shauku yenu, na maombolezo yenu, na bidii yenu kwa ajili yangu, hata nikazidi kufurahi. 8 Kwa sababu, ijapokuwa naliwahuzunisha kwa waraka ule, sijuti; hata ikiwa nalijuta, naona ya kwamba waraka ule uliwahuzunisha, ingawa ni kwa kitambo tu. 9 Sasa nafurahi, si kwa sababu ya ninyi kuhuzunishwa, bali kwa sababu**

**mlihuzunishwa, hata mkatubu. Maana mlihuzunishwa kwa jinsi ya Mungu, ili msipate hasara kwa tendo letu katika neno lo lote. [10] Maana huzuni iliyo kwa jinsi ya Mungu hufanya toba liletalo wokovu lisilo na majuto; bali huzuni ya dunia hufanya mauti. [11] Maana, angalieni, kuhuzunishwa kuko huko kwa jinsi ya Mungu kulitenda bidii kama nini ndani yenu; naam, na kujitetea, naam, na kukasirika, naam, na hofu, naam, na shauku, naam, na kujitahidi, naam, na kisasi! Kwa kila njia mmejionyesha wenyewe kuwa safi katika jambo hilo. [12] Basi, ijapokuwa naliwaandikia, sikuandika kwa ajili yake yeye aliyedhulumu, wala si kwa ajili yake yeye aliyedhulumiwa, bali bidii yenu kwa ajili yetu ipate kudhihirishwa kwenu mbele za Mungu. [13] Kwa hiyo tulifarijiwa.**

**7:5 "Kwa maana hata tulipokuwa tumefika Makedonia"** Paulo anarudia tena habari kuhusu taarifa ya Tito aliyoianza katika 2 Kor.2:13. Kumekuwapo na tabia ya kustaajabisha ya kwenda nje ya mada kuhusu maandiko na mafundisho ya Mtakatifu Paulo kati ya 2:13 na 7:5, ambapo anajadili furaha na huzuni katika huduma ya Kitume.

◙**"miili yetu haikupata nafuu"** Paulo alikuwa ameugua kutokana na wasiwasi juu ya kanisa hili (kama vile 2 Kor. 2:12-13, zote mbili ni KAULI TENDAJI ELEKEZI YA WAKATI TIMILIFU). Inanisaidia katikati ya wasiwasi na mashaka yangu kujua kwamba mtume mkuu kwa mataifa pia alipata adha na mashaka yake kuhusu matokeo yaliyodumu katika huduma yake (kama vile 2 Kor. 6:1).

Paulo anatumia neno "mwili" kama kisawe kwa ajili yake mwenyewe (angalia Mada Maalum katika 1 Kor. 1:26). Yeye hufanya kitu kile kile katika kuhusiana na roho katika 2 Kor. 7:13b (angalia mlinganisho katika 2 Kor. 2:13, "pumzika katika roho yangu"), akirejelea kwa Tito. Agano Jipya haliungi mkono mtazamo wa mwanadamu kuwa na nafsi tatu. Mwanadamu ni kitu kimoja (kama vile Mwa. 2:7). Paulo hufafanua huu umoja wa sura nyingi kwa njia kadhaa.

◙ **"bali tulidhikika kote kote"** Hii ni KAULI TENDEWA ENDELEVU YA WAKATI ULIOPO**.** Mstari huu ni kifupi cha muhtasari wa matatizo ambayo Paulo ameyataja katika 2 Kor. 1:4-10; 4:7-12; na 6:3-10.

◙ **"nje palikuwa na vita, ndani hofu"** Tangu wakati wa Mtakatifu Yohana, Kifungu hiki cha maneno kimefasiriwa kama kinachorejelea kwa matatizo yanayohusu wasioamini na waaminio (kama vile 2 Kor. 11:28). Paulo alihofu kuhusu mbinu za shetani (kama vile 2 Kor. 11:3; 1 Kor. 7:5).

**7:6 "Lakini Mungu, mwenye kuwafariji wanyonge, alitufariji"** Ni sifa gani ya kustaajabu kwa Mungu "yeye aendeleaye kuwafariji" (KAULI TENDAJI ENDELEVU YA WAKATI ULIPO). Angalia maelezo kamili kuhusu faraja katika 2 Kor. 1:4-11.

**7:7** Maombi ya Paulo na barua zake yalithibitika kuzaa matunda. Idadi kubwa zaidi ya kanisa iliitikia inavyopaswa kwenye mamlaka yake ya kitume na uwasilishaji wa injili. Walikataa uovu na walimu wapotoshaji (kama vile 2 Kor. 7:8-13a).

**7:8**
**NASB "Kwa kuwa ingawa naliwasababishia huzuni"**
**NKJV, NRSV "kwa kuwa ingawa naliwafanya kuhuzunika"**
**TEV "kwani hata kama. . .liwafanya kuhuzunika"**
**NJB "hivyo sasa ingawa naliwahuzunisha"**

Hii ni SENTENSI YENYA MASHARTI DARAJA LA KWANZA, ambayo inadhaniwa kuwa kweli.

◙ **"waraka ule"** Mstari huu unaonekana kurejelea kwa barua ya tatu ya Paulo kwa Korintho ambayo iliitwa na wasomi "waraka mchungu" (kama vile 2 Kor. 2:3.4.9). Hii ni mojawapo ya barua mbili zilizopotea isipokuwa sura ya 10-13 yawe mabaki kutoka kwa barua hiyo.

**7:8-11 "huzuni. . . majuto. . . toba"** Kuna maneno matatu ya Kiyunani ambayo yana umuhimu sana yaliyotumika kufafanua huzuni na toba. Neno la kwanza (yaani, *lupeō*) ni neno la jumla kwa "huzuni kuu" au "mateso." Ni neno la kithiolojia lisilopendelea upande wowote linalopatikana mara mbili katika 2 Kor. 7:8: mara tatu katika 2 Kor. 7:9: mara mbili katika 2 Kor. 7:10: na mara moja katika 2 Kor. 7:11 (kama vile 2 Kor. 2:2,4,5; 6:10).

Neno majuto (yaani, *metamelomai*), linapatikana mara mbili katika 2 Kor. 7:8 na limekanushwa katika 2 Kor. 7:10, ni neno ambalo humaanisha "utunduizi wa jambo." Hii inaonekana kumaanisha huzuni juu ya matokeo ya matendo yaliyopita: Mfano: (1) wale ambao hawakutubu kiukweli katika mifano ya Yesu, Mat. 21:29, 32; (2) Yuda, Ebr 12:16-17; na (3) Esau, Mt. 27:3.

Neno la mwisho (yaani, *metanoeia*), linapatikana katika 2 Kor. 7:9 na 10, ni la muhimu sana kitheolojia. Kiuhalisia, lina maanisha "baada ya fikra." Haikuhusu kubadili mtazamo tu, bali badiliko la matendo (kama vile Mk. 1:15; Mdo. 3:16; 20:21). Mifano ya aina hii ya toba inaweza kupatikana kwa Mfalme Daudi na Mtume Paulo.

Paulo anarejelea barua yake ya "maumivu" ambayo ilikuwa imekwisha kuandikwa kwa kanisa la Korintho. Alijieleza kikamilifu na kiukweli, lakini alikuwa na wasiwasi kwamba barua hiyo ingeweza kusababisha wasiwasi mkubwa badala ya toba yenye afya, ambayo ingetoa matokea katika ushirika uliorejeshwa. Walimlazimisha Paulo kutenda kama daktari wa upasuaji wa kiroho badala ya baba wa Kiroho. Paulo alitambulisha vitendo visivyofaa na kazitazamia ziwe na mwitikio unaostahili. Lakini , kama Baba anavyowaadilisha watoto wake kwa huzuni, Paulo aliandika katika huzuni na alihofu sana, kwamba wasingeitikia kwa toba ya kweli na kwamba ushirika usingeweza kurejeshwa na kazi yake pale ingekuwa bure (kama vile 2 Kor. 6:1).

### [MADA MAALUM: TOBA KATIKA AGANO LA KALE (SPECIAL TOPIC: REPENTANCE IN THE OLD TESTAMENT)]

**7:9**
**NASB "kwa kuwa mlihudhunishwa kwa kusudi la Mungu"**
**NKJV "Kwa kuwa mlihudhunishwa kwa kumcha Mungu"**
**NRSV "Kwa kuwa mlihisi huzuni ya Mungu"**
**TEV "kwamba huzuni ilitumiwa na Mungu"**
**NJB "Maumivu yenu sawa nay ale Mungu anayakubali"**

Katika hali halisi mstari huu unatakiwa kuwa "kwani mlihuzunishwa kwa makusudi na Mungu." Unaweza kuona mitazamo tofauti ya kithiolojia katika tafsiri tofauti tofauti. Je, Mungu anatumia huzuni, maumivu, hata uovu, kwa makusudi yake? Baadhi wangenukuu Rum. 8:28 na kusema "ndiyo." Wengine wangenukuu Yakobo 1:13, 17 na kusema "hapana." Paulo anaorodhesha matatizo na mateso anayokutana nayo kama Mtume. Yeye huorodhesha vyanzo vya haya katika Efe. 2:2-3 kama shetani, utaratibu wa ulimwengu ulioanguka, na asili ya Adamu ya mwandamu aliyeanguka. Mungu yuko tayari kusamehe, kufanya kazi pamoja, na kuwakaribisha watu wenye dhambi. Yeye hutumia uovu kwa madhumuni yake, lakini yeye kibinafsi hahusiki katika hilo. Kuteseka na matatizo mara nyingi huleta matokeo chanya. Katika mazingira haya huleta toba (kama vile 2 Kor. 7:9-11).

◙ **"ili msipate hasara kwa tendo letu katika neno lo lote"** Hii ni KAULI TENDEWA TEGEMEZI YA WAKTI ULIOPITA USIOTIMILIFU. Tambua kwamba kuna ishara ya tukio la bila kutarajiwa. Paulo alitaka awe Baraka kwa kanisa sio kikwazo kwa namna yoyote. Hata hivyo, kanisa linapaswa kumpokea Paulo na huduma yake.

**7:10 "liletalo wokovu"** Toba ni mojawapo ya ishara- muhimu ya wokovu. Toba ilitajwa kama hitaji la lazima na Yohana Mbatizaji (kama vile Mt. 3:2), Yesu (kama vile Mt. 4:17), Petro (kama vile Mdo. 2:38), na Paulo (kama vile Mdo. 26:20). Toba ni kurudi kutoka dhambini na imani ni kurudi kwa Kristo: vyote vinahitajika (kama vile Mk. 1:15; Mdo. 3:16, 19: 20:21). Nimefikia kuamini kwamba kuna mahitaji kadhaa yanayosanifisha wokovu uliokomaa: toba, imani, ubatizo, utii, huduma na ustahimilivu. Ukristo ni mtindo wa maisha ya uhusiano, sio kundi la vikwazo vya kulazimisha kuvivuka, wakati uzima wa milele unazo sifa zinazoonekana!

Wasiwasi wa kiagano kati ya utawala wa Mungu na mwitikio wa mwanadamu aliyeamriwa waweza pia kuonekana katika eneo hili la thiolojia kwa sababu Matendo 11:18 huonyesha kwamba Mungu huwapa watu toba. Wokovu waweza kuonekana kibiblia kama yote kwa Mungu na bali pia unahitaji mwitikio wa mwanadamu. Hii ni kweli kinzani ya wokovu wa bure na na kugharimu kila kitu kwa maisha ya Mkristo.

Dhana ya Agano Jipya ya wokovu imelezewa kama mwanzo wa matendo ya imani yakifuatiwa na imani ya mahusiano yanayokuwa na kufikia hatua ya mwisho ya kuja kwa Kristo siku zijazo. Andiko hili linaonekana kumaanisha hali ya kukamilishwa ya baadaye. Angalia Mada Maalum: Njeo za Kitenzi za Kiyunani kwa wokovu katika 1 Kor. 3:15.

◙ **"bali huzuni ya dunia hufanya mauti "** Sentensi hii ina maneno matatu muhimu ambayo yanapaswa kueleweka katika muktadha wao wa Agano Jipya.

1. Neno "huzuni" Mstari huu unayo maneno yote matatu ya Kiyunani kwa huzuni, majuto, toba, katika kifungu hiki cha neno huzuni *lupeō*, ambalo linamaanisha huzuni kuu. Wanadamu huhuzunika kwa ajili ya matendo yaliyopita, lakini kwa sababu za ubinafsi.
2. Neno "ulimwengu" Hii ni rejeo kwa jamii ya mwanadamu waliojiongoza na kutenda kinyume na Mungu. Huyu ni mwandamu aliyeanguka!
3. Neno "Kifo" Matumizi ya neno hili yawezekana ni tata lenye maana. Linarejelea kwa kifo cha kiroho (kama vile Mwanzo 3) na kifo cha asili (kimwili) (kama vile Mwanzo 5).

**7:11** Huzuni ya kumcha Mungu (yaani, *lupeō*) hufanya matokeo ya kiroho (yaani, toba ya kweli, *metanoeō* na matunda yake). Matokeo ya kumcha Mungu yameorodheshwa katika Mstari wa 11.

◙ **"na kisasi"** Neno katika uhalisia ni "lipiza kisasi," lakini linatumika katika maana ya kugawa haki. Kumekuwapo na muachano wa maoni miongoni mwa wasomi kuhusu kile ambacho aya hii inarejelea. Baadhi wanadai kwamba (1) linarejelea kwa 1 Kor. 5:5, wakati wengine wanaamini (2) linarejelea kwa kikundi kidogo au walimu wa mafundisho ya uongo (kama vile 2 Kor. 7:12).

**7:12** Mstari wa 12 unaonekana kuwa lahaja ya Kiebrania ya ulinganisho, sio kauli hasi (kama vile *The Jerome Biblical Commentary*, uk. 283).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 2 WAKORINTHO 7:13b-16**
**[3b] Tena katika kufarijiwa kwetu tulifurahi sana kupita kiasi kwa sababu ya furaha ya Tito; maana roho yake imeburudishwa na ninyi nyote. [14] Kwa maana, ikiwa nimejisifu mbele yake katika neno lo lote kwa ajili yenu, sikutahayarishwa; bali, kama tulivyowaambia mambo yote kwa kweli, vivyo hivyo na kujisifu kwetu kwa Tito kulikuwa kweli. [15] Na mapenzi yake kwenu yamekuwa mengi kupita kiasi, akumbukapo kutii kwenu ninyi nyote, jinsi mlivyomkaribisha kwa hofu na kutetemeka. [16] Nafurahi, kwa sababu katika kila neno nina moyo mkuu kwa ajili yenu.**

**7:13b " tulifurahi sana kupita kiasi kwa sababu ya furaha ya Tito; maana roho yake imeburudishwa na ninyi nyote"** Kanisa hili lilimtendea wema Tito (yaani, yeye alifarijiwa, KAULI TENDEWA ELEKEZI YA WAKATI TIMILIFU). Yaonekana Paulo alikuwa na wasi wasi kuhusu hili kwa sababu ya alivyotendewa Timotheo awali.

Tambua Paulo anatumia neno "roho" kama kisawe cha utu wa Tito, sio kipengele tu (yaani, mwili, nafsi, roho, kama vile Elwell's *Evangelical Dictionary of Theology*, kr. 676-680). Angalia maelezo kamili juu ya neno "roho' katika 2 Kor. 4:13.

Kwa neno "zaidi" angalia Mada Maalum katika 2 Kor.2:7.

**7:14 "ikiwa"** Hii ni SENTENSI YENYE MSHARTI DARAJA LA KWANZA, ambayo imedhaniwa kuwa kweli kutokana na mtazamo wa mwandishi ama kwa kusudi la fasihi. Paulo alijisifu kuhusu kanisa la Wakorinto kwa Tito.

◙ **"nimejisifu"** Angalia Mada Maalum: Kujisifu katika 1 Kor. 5:6.

◙ **"kwa kweli"** Angalia Mada Maalum katika 2 Kor.13:8.

**7:15 "mapenzi"** Hili kwa uhalisia ni neno la Kiyunani, *splagchna*. Angalia maelezo kamili katika 2 Kor. 6:12.

◙ **"mengi kupita kiasi"** Angalia Mada Maalum katika 2 Kor.2:7.

◙ **"akumbukapo kutii kwenu ninyi nyote"** Hii ni KAULI YA KATI ENDELEVU YA WAKATI ULIOPO (yaani, Moulton's *Analytical Greek Lexicon Revised*, uk. 24) au KAULI TENDEWA ENDELEVU YA WAKATI ULIOPO (yaani, Friberg's *Analytical Greek New Testament*, uk. 562). Jinsi gani makanisa yanatendea Watumishi wa Mungu husema kitu kuwahusu wao (kama vile 1 Kor. 16:16; 1 The. 5:12; Ebr. 13:17).

**7:16** Kauli hii huhitimisha kitengo hiki cha fasihi (kama vile 2 Kor. 2:14-7:16) pamoja na maelezo yenye uhakika yenye kujiamini.

◙ "**moyo mkuu"** Angalia maelezo katika 2 Kor.5:6.

## MASWALI YA MJADALA

Haya ni maoni ya <u>mwongozo</u> kwa kujisomea, ikiwa na maana kuwa unawajibika binafsi kwa tafsiri ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mtoa maoni tu.

Maswali haya ya kujadili yanatolewa ili kukusaidia kufikiri mambo muhimu yaliyoko katika kipengele cha kitabu hiki. Yanamaanisha kuwa maswali ya kichokonozi, yasio ya hakika.

1. Kwa nini taarifa ya Tito ilikuwa ya muhimu kwa Paulo?
2. Fafanua maneno matatu tofauti kwa neno "huzuni" yanayopatikana katika mst. 8-11 na kuhusisha umuhimu wao wa kithiolojia.

# 2 WAKORINTHO 8

| MGAWANYO WA AYA WA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **UBS[4]** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB** |
| Utoaji wa Ukarimu | Kuzidi katika utoaji | Makusanyo kwa ajili ya kusaidia kanisa la Yerusalemu<br>(8:1-9:15) | Utoaji wa Kikristo | Kwanini Wakorintho wawe wakarimu |
| 8:1-7 | 8:1-7 | 8:1-7 | 8:1-7 | 8:1-15 |
| | Kristo mfano wetu | | | |
| 8:8-15 | 8:8-15 | 8:8-15 | 8:8-9 | |
| | | | 8:10-12 | |
| | | | 8:13-15 | |
| Tito na wenzake | Makusanyo kwa ajili ya watakatifu wa Yudea | | Tito na wenzake | Watu walio pendekezwa kwa Wakorintho |
| 8:16-24 | 8:16-24 | 8:16-24 | 8:16-19 | 8:16-9:5 |
| | | | 8:20-21 | |
| | | | 8:22-24 | |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (kutoka **"Mwongozo wa Usomaji Mzuri wa Biblia" ("A Guide to Good Bible Reading")**

### *KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, hii ina maana kwamba unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe kutoka katika Biblia. Kila mmoja wetu anatembea katika nuru tuliyonayo, wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele. Hupaswi kumuachia mfasiri vitu hivi.

Soma Sura kwa mara moja. Tambua mada zinazozungumzwa. Linganisha mgawanyo wa mada zako na tafsiri tano hapo juu. Aya zaweza kuwa hazina uvuvio lakini ni msingi kupata au kufuatilia kusudi la asili la mwandishi ambao ndio moyo wa tafsiri. Kila aya ina mada moja na mada ni moja tu.

9. Aya ya kwanza
10. Aya ya pili
11. Aya ya tatu
12. Na nyinginezo

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA

A. Sura ya 8 na 9 zinatengeneza kipengele cha fasihi kinachohusiana na sehemu ya Wakorintho katika mchango wa makanisa ya mataifa kwa ajili ya masikini walio katika makanisa ya Yerusalemu (kama vile 1 Wakorintho 16:1-3).

B. Historia ya kipawa cha Paulo kwa kanisa la Yerusalemu
   1. Katika Matendo ya Mitume 11:27-30 Kanisa la Antiokia lilianza taratibu za kazi ya kusaidia Yerusalemu. Ilikuwa ni njia ya kuunganisha makanisa ya Wayahudi na yale ya Mataifa.
   2. Katika Wagalatia 2:10 na 6:10 Paulo alianza msisitizo huo huo katika kazi yake ya umisheni
   3. Katika 1 Wakorintho 16:1-4 inaoneshwa kuwa mchango huu ulikuwa umeshaanza pale Korintho
   4. Katika Warumi 15:26 michango ya Makedonia na Akaya inatajwa.

C. Mijadala yote ya Paulo kuhusu utoaji wa Wakristo
   1. Mifano ya wengine (Wamakedonia) 2 Wakorintho 8:1-5
   2. Utoaji ni sehemu ya ukuaji wa kiroho, 2 Wakorintho 8:7-8
   3. Mfano wa Kristo, 2 Wakorintho 8:9; 9:15
   4. Mwanzo wao wenyewe, 2 Wakorintho 8:6,10
   5. Kutiwa moyo kuchochea shauku yao katika matendo, 2 Wakorintho 8:10
   6. Dhamiri na si kiwango, ndiyo msingi 2 Wakorintho 8:12
   7. Kutoa sawasawa nje, 2 Wakorintho 8:14

D. Miongozo ya Agano JIpya kwa utoaji wa Wakristo unaojikita katika mfano wa makanisa ya Makedonia
   1. Kwa furaha na kwa dhati, hata katikati ya umaskini, 2 Wakorintho 8:2; 9:7
   2. Kutoa kadiri ya uwezo, 2 Wakorintho 8:3
   3. Kutoa kwa kujidhabihu zaidi ya uwezo, 2 Wakorintho 8:3, 12
   4. Kutoa kwa uhuru, 2 Wakorintho 8:3; 9:7
   5. Kutoa kwa dhati, 2 Wakorintho 8:4
   6. Kutoa zaidi ya fedha, 2 Wakorintho 8:5

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB(LILILOBORESHWA): 2 WAKORINTHO 8:1-6**
**1Tena ndugu zetu, twawaarifu habari ya neema ya Mungu, waliyopewa makanisa ya Makedonia; 2 maana walipokuwa wakijaribiwa kwa dhiki nyingi, wingi wa furaha yao na umaskini wao uliokuwa mwingi uliwaongezea utajiri wa ukarimu wao. 3Maana nawashuhudia kwamba, kwa uwezo wao, na zaidi ya uwezo wao, kwa hiari yao wenyewe walitoa vitu vyao; 4 wakituomba sana pamoja na kutusihi kwa habari ya neema hii, na shirika hili la kuwahudumia watakatifu. 5Tena walitenda hivi si kama tulivyotumaini tu, bali kwanza walijitoa nafsi zao kwa Bwana; na kwetu pia, kwa mapenzi ya Mungu. 6Hata tukamwonya Tito kuwatimilizia neema hii kwenu kama vile yeye alivyotangulia kuianzisha.**

**8:1"neema ya Mungu"** Hili neno "neema" (*charis*) linatumika zaidi ya mara kumi katika sura ya 8 na 9. Linatumika kwa maana ya

1. Upendo wa Mungu usiostahilishwa katika kristo, 2 Wakorintho 8:1, 9; 9:8, 14
2. Upendeleo/kupendelewa, 2 Wakorintho 8:4
3. Sadaka ya Yerusalemu, 2 Wakorintho 8:1, 6, 7, 19
4. Shukrani, 2 Wakorintho 8:16; 9:15

   Angalia kwamba neema inaeleweka ikimaanisha kwa Wasiostahili wa Mungu, upendo usiostahili katika Kristo au kama njia ya kumaanisha mchango kutoka kwa makanisa ya mataifa ya Paulo kwenda kwa kanisa mama katika Yerusalemu. Neno la Kiyunani lina wigo mpana wa ki-maana.

◙**"makanisa ya Makedonia"** Hii ingemaanisha Filipi, Thesalonike na Beroya (kama vile Matendo ya Mitume 16-17). Kulikuwa na hali ya kitamaduni ya mashindano kati ya Akaya na Makedonia. Angali Mada Maalum: Kanisa katika 1 Wakorintho 1:2

**8:2 "maana walipokuwa wakijaribiwa kwa dhiki nyingi"** Tunaona kitu kikubwa cha dhiki hii kutoka Matendo ya Mitume 17:1-15 na Wathesalonike 1:6; 2:14. Kuna maneno mawili ya Kiyunani ambayo yanafasiriwa kuwa

“majaribu,” ”mtihani” au “jaribu” (hapa “mateso”). Moja linamaanisha jaribu kwa muono wa kuelekea uharibifu, wakati lingine linamaanisha jaribu kwa muono wa kuelekea kuthibitishwa (kama vile 2 Wakorintho 8:2,8,22; 9:13). Angalia Mada Maalum katika 2 Kor. 3:13.

Kwa “mateso” angalia MADA MAALUM: DHIKI katika 2 Wakorintho 1:4

◙**”wingi wa furaha yao”** inashangaza sana kwamba kifungu hiki cha maneno kinatokea kati ya “taabu za mateso makubwa” na “umaskini wao mwingi.” Furaha hii katikati ya mazingira magumu ni tabia ya Mwamini (kama vile Mathayo 5:10-12; Warumi 5:3; Yakobo 1:2). Furaha ni tunda la roho (kama vile Wagalatia 5:22) na haiusiani na mazingira! Kwa matumizi ya Paulo ya kurudiarudia kwa “wingi” au “kujaa kuzidi” angalia angalizo katika 2 Wakorintho 1:5.

◙**”umaskini wao uliokuwa mwingi uliwaongezea utajiri wa ukarimu wao”** Neno, “umaskini” (yaani *ptōchos)* ni neno imara la Kiyunani lililotumika kwa (1) umaskini uliopitiliza katika maandiko ya kale ya Kiyahudi katika Kumbukumbu la Torati 8:9 Waamuzi 6:6; 14:15 (2) waombaji (kama vile 2 Wakorintho 6:10; Warumi 15:26; Ufunuo 2:9; 3:17). Hawakutoa katika ziada zao.  Walimwamini Mungu kukidhiwa kwa mahitaji yao (kama vile Marko 12:42; Luka 21:2). Katika muktadha huu "umaskini wao mwingi”inaonekana kufanana na kupatwa kwao kwa dhiki kwa ajili ya injili (kama vile 2 Wakorintho 8:13-18).

◙**”ukarimu”** Mzizi wa neno hili unamaanisha “kuwa na nia moja,” ambao unaweza kumaanisha “dhati” au “kweli” (kama vile Andiko la kale la Kiyahudi 2 Samweli 15:11; 1 Mambo ya Nyakati 29:17). Lakini linatumika katika Agano Jipya (yaani neno tu katika maandiko ya Paulo) katika namna ya “ukarimu” au “utu wema” (kama vile 2 Wakorintho 9:11, 13). *Jerome Biblical Commentary* (ukurasa 284) unafikiri neno linaaksi neno la Kiebrania lenye maana ya “ukamilifu” au “sifa njema” na kwa hiyo kumaanisha usafi  wa nia zao. Nia ya kutoa kwetu ndiyo ufunguo (kama vile 2 Wakorintho 8:12). Angalia angalizo kamili katika 2 Wakorintho 1:12.

**8:3** Paulo alikuwa amekwisha uona umaskini wao tayari hapo mwanzo

**NASB"walitoa kwa kupenda kwao wenyewe"**
**NKJV"walikuwa tayari kwa uhuru"**
**NRSV"walitoa kwa kupenda"**
**TEV"kwa uhuru wao wenyewe"**
**NJB"ilikuwa kwa kupenda kwao"**

Hili neno linatoka *autos* and *haireomai*, linalomaanisha “maamuzi binafsi.” Linatumika kote katika 2 Wakorintho 8:3 na 17. Mzizi wa neno una maana ya ziada ya kuchagua kwa upendo na furaha (kama vile Mathayo 12:18, ambayo ni nukuu kutoka katika wimbo wa Mtumishi wa Isaya 42:1-3). Unatumika katika (1) Maccabees 6:19 na Maccabees 6:6; 7:10 na (2) lugha ya Koine kwenye mafunjo kutoka Misri ya mtu anayefanya kazi kwa matakwa yake mwenyewe kwa uhuru.

*A Handbook on Paul's Second Letter to the Corinthians* cha Roger L. Omanson na John Ellington kinaonesha namna tafsiri za kingereza zinavyotofautiana kisarufi juu ya tungo ya kuweka katika kifungu hiki cha neno.

> “Maneno haya yanaweza kuhesabiwa kama sehemu ya sentensi ambayo inatangulia, ambayo Wamakedonia walitoa kwa utashi wao wenyewe (hivyo RSV, NRSV, NJB, SPCL), au kwa sentensi inayofuatia katika mstari wa 4, ambayo kwa utashi wao wenyewe waliomba kuhusika katika makusanyo (kwahiyo TEV, NIV, REB, NJB, TNT, FRCL). Kalimani ya mwisho inafuata alama ya nukta ya Agano Jipya la Kiyunani la toleo la UBS (UBS *Greek New Testament* ) na inawezekana ikawa hivyo zaidi” (ukurasa wa 142).

**8:4” wakituomba sana”** Angalia angalizo kamili katika kifungu hiki cha neno katika 2 Wakorintho 1:4-11.

◙ “**neema hii, na shirika hili la kuwahudumia”** kwa “neema” angalia angalizo katika 2 Wakorintho 8:1. Neno “kushiriki” (yaani *koinōnia*) linatumiwa mara nyingi na Paulo katika barua zake za Wakorintho katika hali kadhaa zinazofanana. Angalia Mada Maalum katika 1 Wakorintho 1:9.

1. Uhusiano wa karibu, wa ndani wa binafsi (neno linalofanana *koinōneō* ni mara nyingi linatumika katika kuanzisha kuingia katika dini za siri)
   a. Pamoja na mwana, 1 Wakorintho 1:9
   b. Pamoja na Roho, 2 Wakorintho 13:14
   c. Si pamoja na uovu, 2 Wakorintho 6:14
   d. Tito pamoja na Paulo katika huduma, 2 Wakorintho 8:23
2. Ukarimu (neno linalohusiana *koinōnikos* maana kushirikiana kwa ukarimu wa mali ya mtu fulani mwenyewe), 2 Wakorintho 9:13

3. Kushiriki katika jambo fulani
   a. 1 Wakorintho 10:16 (yaani katika damu ya Kristo)
   b. 2 Wakorintho 8:4 (katika kuchangia kwa watakatifu maskini walioko Yerusalemu)
   c. 2 Wakorintho 1:7 (yaani katika mateso)
   Kuna mchezo wa ugeuzaji wa maneno kati ya ushirikiano (*koinōnia*) na kuungwa mkono (au huduma, *diakonia*). Neno hili kwa huduma linatumika mara nyingi katika 2 Wakorintho.
      1) *diakonos* (mtumwa), 2 Kor. 3:6; 6:4; 11:15,23
      2) *diakoneō* (kutumika), 2 Kor. 3:3; 8:19,20
      3) *diakonia* (huduma), 2 Kor. 3:7,8,9; 4:1; 5:18; 6:3; 8:4; 9:1,12,13; 11:8

Ukristo ni kutumikia. Tuliokolewa ili tutumike!

◙**”na shirika hili”** Angalia angalizo katika 1 Wakorintho 16:1

◙**”watakatifu**”Angalia MADA MAALUMU: WATAKATIFU (SPECIAL TOPIC: SAINTS) katika 1 Wakorintho 1:2

**8:5 “kwanza walijitoa nafsi zao kwa Bwana; na kwetu pia, kwa mapenzi ya Mungu.”** Uwakili unajumuisha kila kitu tulivyo na tulivyo navyo. Kama ukijitoa mwenyewe kwa Bwana basi kunakuwa hakuna kilichobaki kukitoa! Uwakili wa Wakristo ni kipimajoto cha kukua kwetu kiroho. Waamini hawana chochote wanachomiliki isipokuwa ni mawakili wa kila kitu cha Mungu. Ukweli huu mara nyingi ni rahisi kwa maskini kuuelewa na kuutii kuliko watu walio na mali nyingi.

**8:6 “Tito”** Katika *Paul: Apostle of the Heart Set Free*, F. F. Bruce anatoa maoni yake kwenye nadharia kuwa sura ya 10-13 ni vipengele vya barua iliyotangulia, “lakini hii inaonekana haiwezekaniki kwa 12:18, ambayo kwa uwazi inaonekana kurejea nyuma kwa 8:6, 16-19” (ukurasa 274 tanbihi chini ya ukurasa 51).

◙**”neema hii”** Hii inamaanisha michango kutoka kwa makanisa ya mataifa ya Paulo kwa ajili ya kanisa mama katika Yerusalemu (kama vile 1 Wakorintho 16:1-4; Warumi 15:26). Katika *Jesus and the Rise of Early Christianity*, Paul Barnett anatoa pointi nzuri kuhusu maneno mengineyo ambayo Paulo anayatumia kufunua sadaka hii ya upendo kwa waamini waskini katika Yerusalemu

> “ Wito unapewa tabia na msamiati wake wenyewe: ‘mchango kwa jili ya watakatifu’ (1 Wakorintho 16:1); “kipawa” (1 Wakorintho 16:3); ); 'neema' (2 Wakorintho 8:6, 7, 9; 9:14); 'huduma' (2 Wakorintho 9:12; kama vile Warumi 15:27) na 'ushirika' (2 Wakorintho 8:4; 9:13; Warumi 15:26)" (ukurasa 344).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 2 WAKORINTHO 8:7-15**
**[7]Lakini kama mlivyo na wingi wa mambo yote; imani, na usemi, na elimu, na bidii yote, na upendo wenu kwetu sisi; basi vivyo hivyo mpate wingi wa neema hii pia. [8] Sineni ili kuwaamuru, bali kwa bidii ya watu**

**wengine nijaribu unyofu wa upendo wenu. [9] Maana mmejua neema ya Bwana wetu Yesu Kristo, jinsi alivyokuwa maskini kwa ajili yenu, ingawa alikuwa tajiri, ili kwamba ninyi mpate kuwa matajiri kwa umaskini wake. [10] Nami katika neno hili natoa shauri langu; maana neno hili lawafaa ninyi mliotangulia, yapata mwaka, licha ya kutenda hata na kutaka pia. [11] Lakini sasa timizeni kule kutenda nako, ili kama vile mlivyokuwa tayari kutaka, vivyo hivyo mkawe tayari na kutimiza, kwa kadiri ya mlivyo navyo. [12] Maana, kama nia ipo, hukubaliwa kwa kadiri ya alivyo navyo mtu, si kwa kadiri ya asivyo navyo. [13] Maana sisemi hayo, ili wengine wapate raha nanyi mpate dhiki; [14] bali mambo yawe sawasawa; wakati huu wa sasa wingi wenu uwafae upungufu wao, ili na wingi wao uwafae ninyi mtakapopungukiwa; ili mambo yawe sawasawa. [15] Kama ilivyoandikwa, Aliyekusanya vingi, hakuzidi, wala yeye aliyekusanya vichache hakupungukiwa.**

**8:7"kama mlivyo na wingi wa mambo yote;"** Tazama kwamba orodha (yaani imani, usemi, maarifa, bidii, upendo) haihusiani na umiliki wa mali. Hatutoi ili kupata vitu zaidi kwa ajili yetu. Tunatosheleza katika Yeye (kama vile 1 Wakorintho 1:5). Yeye anatutosheleza kila kitu tunachokihitaji (kama vile 2 Wakorintho 9:8).

◙**"wingi"** Neno hili linatumika mara mbili katika mstari huu. Ya kwanza ni KAULI TENDAJI ELEKEZI YA WAKATI ULIOPO, walikuwa wanatoshelezwa katika Baraka za injili. Ya pili ni <u>kauli tendaji tegemezi ya wakati uliopo</u> inayoongeza angalizo la uwezekano. Kama walivyokuwa na wingi wa Baraka za Agano Jipya, wanatakiwa wakae katika wingi wa majukumu. Msaada wao kwa maskini katika kanisa la Yerusalemu ni moja ya "kazi zenye neema."

**NASB "katika upendo tuliyowavuvia ndani yenu"**
**NKJV, TEV "katika upendo wenu kwa ajili yetu"**
**NRSV "katika upendo wetu kwa ajili yenu"**
**NJB "na upendo kwa ajili yetu"**

Fasiri hizi zinafunua aina tofauti za Kiyunani.

1. "katika upendo wetu kwa ajili yenu" (NRSV) kutoka MSS $P^{46}$, B
2. "katika upendo wenu kwa ajili yetu" (NKJV, TEV, NIV) from MSS א, C, D, F, G
3. NASB inachukua mbadala #1, lakini kuna mabadiliko kidogo kwenye shabaha, "pendo tulilovuvia ndani yenu"
4. UBS[4] inaweka mbadala #1 katika andiko lakini alitoa alama ya "C".

Mkanganyiko wa KIWAKILISHI hicho hicho unaonekana katika aina za Kiyunani katika 2 Wakorintho 8:9.

**8:8" Sineni ili kuwaamuru"** Amri sio sawa na hazitakiwi katika eneo la uwakili wa Mkristo. Nia sahihi ni muhimu katika eneo hili la maisha ya Mkristo.

## <u>MADA MAALUMU: UTOAJI WA ZAKA (SPECIAL TOPIC: TITHING)</u>

**NASB"kama kuthibitisha kupitia bidii kwa wengine juu ya upendo wenu wa dhati"**
**NKJV"ila najaribu upendo wen wa dhati kwa bidii ya wengine"**
**NRSV"lakini najaribu upendo wenu wa dhati dhidi ya bidii ya wengine"**
**TEV"lakini kwa kuonesha jinsi shauku ya kusaidia wengine, najaribu kutafta upendo wenu una ukweli kiasi gani"**
**NJB"lakini nikijaribu dhati ya upendo wenu dhidi ya kujali wengine"**

Paulo anatoa changamoto kwa makanisa ya Akaya kufuatilia uongozi wa makanisa ya Makedonia (kama vile 2 Wakorintho 8:1-5) kupitia safari ya Tito (kama vile 2 Wakorintho 8:6, 16-24)

◙**"kuthibitisha"** Angalia Mada Maalum katika 1 Wakorintho 3:13.

**8:9 "neema"** Angalia angalizo katika 2 Wakorintho 8:1

◙ “**ya Bwana wetu Yesu Kristo”** Angalia angalizo katika 2 Wakorintho 1:2

◙**”ingawa alikuwa tajiri”** Hii inamaanisha utukufu wa Yesu Kristo uliokuwepo hapo mwanzo (kama vile Yohana 1:1; 8:56-59; 16:28; 17:5,24; 2 Kor. 8:9; Filip. 2:6-7; Kol. 1:17; Ebr. 1:3; 10:5-8; 1 Waraka wa Yohana 1:1).

◙**”jinsi alivyokuwa maskini kwa ajili yenu”** Huu ni msisitizo wa kufanyika mwili wa uwepo wa kabla wa *Logos* katika hori la ng’ombe huko Betlehemu. Alizaliwa na mwanamke binti, mkulima na bikira katika maisha ya fundi selemara wa kijijini, lakini alikuwa Mungu katika mfano wa binadamu (kama vile George Ladd, *A Theology of the New Testament*, kurasa 241-242)

◙**”ili kwamba ninyi mpate kuwa matajiri kwa umaskini wake”** Paulo anatumia kuvaa mwili kwa Yesu katika namna mbili.

1. Alikuja kufa katika nafasi yetu ya dhambi (kama vile Marko 10:45).
2. Alikuja kutupatia mfano wa kufuata (kama vile 1 Waraka wa Yohana 3:16).

Usambamba wa mawazo haya mazuri ya 9:15. Kanisa hili lilidhani walikuwa tayari ni matajiri (kama vile 1 Wakorintho 4:8). Sasa maana ya kweli wa utajiri ni wazi kuwa ni kiroho na utoaji wa huduma, sio kutafuta masilahi binafsi au akili au mali.

**8:10”natoa shauri langu”** Ingawa Paulo anasema kwamba hili ni shauri lake kwa sababu ya maoni mengi katika 1 Wakorintho 7:25,40 imekuwa na kauli ya mamlaka (yaani iliyovuviwa).

◙**”mliotangulia, yapata mwaka”** 2 Wakorintho iliandikwa kati ya miezi 6 mpaka 8 baafa ya 1 Wakorintho (kama vile 2 Wakorintho 16:1-4).

**8:11” Lakini sasa timizeni kule kutenda nako”** Hii ni wakati TENDAJI SHURUTISHI ULIOPITA USIOTIMILIFU. Yalikuwa ni moja ya makanisa ya kwanza kwa shauku ya asili kusaidia wahihati katika Yerusalemu. Sasa ni wakati wa kufanya hivyo (kama vile TEV).

**NASB, NKJV"utayari"**
**NRSV"shauku"**
**TEV"kuwa kama na shauku"**
**NJB"ari"**

Hili ni neno la Kiyunani *prothumia*, ambalo pia linatumika katika 2 Wakorintho 8:12 na 8:19 pia vilevile 9:2. Maana yake ya msingi ni “utayari, kwa wakati ufaao” (kama vile Matendo ya Mitume 17:11).

▣**”kutimiza, kwa kadiri ya mlivyo navyo”** Tazama Paulo anarudi tena katika mada hii tena . Inashangaza sana kwangu kwamba Paulo hakuwahi kujadili utoaji wa kila siku wa Mkristo. Maoni yake pekee kuhusu “utoaji” yanahusiana na kipawa hiki cha mara moja kwa jili ya kanisa katika Yerusalemu. Anakiri kwamba mfanyakazi anastahili na makanisa yanatakiwa yasaidie wamishionari kusafiri, lakini hatoi miongozo mingine.

Waamini wa Agano Jipya lazima awe mwangalifu kuhakiki andiko lenye Agano la Kale la kigezo cha kidini katika mazingira ya Agano Jipya (kama vile *Hard Sayings of the Bible*, kurasa 539 tanbihi #1). Kama tunakubali kwamba utoaji wa zaka ni mapenzi ya Mungu,nini kinawazuia wengine kufanya dhabihu au kuabudu Sabato. Yesu hakutaja utoaji wa zaka katika mazungumzo yake kwa walimu wa Kiyahudi(Mathayo 23:23; Luka 11:42), lakini hatuwezi kudai kuwa ushahidi pekee wa Agano Jipya kwamba huu utaratibu wa Agano la Kale ni wa kweli ya milele(angalia Mada Maalumu katika 2 Wakorintho 8:8).

Sijaribu kupunguza kile ambacho waamini wanatakiwa kutoa lakini kusisitiza miongozo ya Paulo katika 2 Wakorintho 8-9 kama taarifa pekee ya Agano Jipya (pia angalia 1 Wakorintho 16:2). Waamini hawatakiwi kuridhika na viwango vya Agano la Kale! Msome Paulo tena (kama vile Frank Stagg, *New Testament Theology*, kurasa 285-293).

**8:12"kama"** Hii ni SENTENSI YENYE MASHARTI DARAJA LA KWANZA. Paulo anadhania kwamba walikuwa tayari na wenye shauku ya kutoa.

◙**"hukubaliwa kwa kadiri ya alivyo navyo mtu, si kwa kadiri ya asivyo navyo"** Ufunguo kwa uwakili wa Mkristo ni mtazamo na nia,sio kiasi au asilimia (kama vile Marko 12:41-44).

**8:13-14** Neno la ufunguo katika mistari hii miwili ni "usawa" na dhana ya ufunguo ni kujirudiarudia. Familia ya Mungu inatakiwa tusaidiane na wenye mahitaji (kama vile Waefeso 4:28). Kanisa la Yerusalemu limesambaza habari njema ya Kristo (Warumi 15:27). Makanisa ya mataifa yanaweza kusaidia katika utoaji kwa maskini waaminio wa Yeruslemu. Wengine wanaweza kuwa maskini kwa sababu ya imani yao katika Kristo.

◙**"dhiki"** Angalia Mada Maalum: Dhiki katika 2 Wakorintho 1:4

**8:15"kama ilivyo andikwa"** Hii KAULI TIMILIFU TENDEWA YENYE KUARIFU (msemo wa Kiebrania) ulitumika kutambulisha nukuu ya Agano la Kale. Inamaanisha uvuvio wa ki-Ungu na umuhimu wa milele wa maandiko. Andiko lililonukuliwa linahusiana na miujiza ya kila siku ya ukusanyaji wa manna ambapo kila Muisraeli alipata ya kutosha (Kutoka 16:17, 18). Mungu atatimiliza mahitaji ya waaminio kama wanavyotafuta na kumtii Yeye (kama vile Mathayo 6:19-34).

**ANDIKO LA NASB(LILILOBORESHWA): 2 WAKORINTHO 8:16-24**
**[16] Lakini ahimidiwe Mungu atiaye bidii ile ile kwa ajili yenu katika moyo wa Tito. [17] Maana aliyapokea kweli yale maonyo; tena, huku akizidi kuwa na bidii, alisafiri kwenda kwenu kwa hiari yake mwenyewe. [18] Na pamoja naye tukamtuma ndugu yule ambaye sifa zake katika Injili zimeenea makanisani mwote. [19] Wala si hivyo tu, bali alichaguliwa na makanisa asafiri pamoja nasi katika jambo la neema hii, tunayoitumikia, ili Bwana atukuzwe, ukadhihirike utayari wetu. [20] Tukijiepusha na neno hili, mtu asije akatulaumu kwa habari ya karama hii tunayoitumikia; [21] tukitangulia kufikiri yaliyo mema, si mbele za Bwana tu, ila na mbele ya wanadamu. [22] Nasi pamoja nao tumemtuma ndugu yetu tuliyemwona mara nyingi katika mambo mengi kuwa ana bidii, na sasa ana bidii zaidi sana kwa sababu ya tumaini kuu alilo nalo kwenu. [23] Basi mtu akitaka habari za Tito, yeye ni mshirika wangu, na mtenda kazi pamoja nami kwa ajili yenu; tena akitaka habari za ndugu zetu, wao ni mitume wa makanisa, na utukufu wa Kristo. [24] Basi waonyesheni mbele ya makanisa hakika ya upendo wenu, na ya kujisifu kwetu kwa ajili yenu.**

**8:16-17 "Lakini ahimidiwe Mungu atiaye bidii ile ile kwa ajili yenu katika moyo wa Tito"** Tazama uelewa wa Paulo wa kuwezesha na Mungu (kama vile katika Waefeso 4:12) na kuwahimiza kwa ajili ya huduma. Uelewa huu huu wa uongozi mkuu wa Mungu katika mambo ya mwanadamu pia inaonekana katika Ufunuo 17:17. Hii ni siri ya ukuu wa ki-Ungu na utashi huru wa kibinadamu.

## MADA MAALUMU: Uchaguzi/Kukusudiwa kabla na Hitaji la Mlinganyo wa Kithiolojia (SPECIAL TOPIC: Election/Predestination and the Need for a Theological Balance)

**8:16-24** Mstari wa 16-24 unaonekana kuwa barua ya kupendekezwa kwa Tito. Angalia angalizo kamili katika 2 Wakorintho 3:1. Mchoro mfupi wa maisha ya Tito unafuata.

1. Tito alikuwa ni mmoja wa watendakazi walioaminiwa zaidi sana na Paulo. Hii inathibitishwa na ukweli kuwa Paulo alimtuma katika maeneo yenye migogoro ya Korintho na Krete.
2. Alikuwa ni Mtu wa Mataifa kamili (Timotheo alikuwa ni Myunani nusu tu), aliyeongoka kutokana na mahubiri ya Paulo. Paulo alikataa kumtahiri (kama vile Gal 2).
3. Anatajwa mara kwa mara katika barua za Paulo (kama vile 2 Kor. 2:13; 7:6-15; 8:6-24; 12:18; Gal. 2:1-3; 2 Tim. 4:10). Na inashangaza kwamba Luka hamtaji yeye katika Matendo ya Mitume. Baadhi ya fasiri zinakuwa na nadharia kwamba (1) anawezekana alikuwa ni ndugu wa Luka (yawezekana kaka) na

kumjumuisha jina lake ingeonekana kiutamaduni kuwa si sawa kwa upande wa Luka au (2) Tito ni chanzo kikubwa cha taarifa kwa Luka kuhusu maisha ya Paulo na huduma na kwa hivyo Luka asingetajwa.

4. Aliambatana na Paulo na Barnaba katika mabaraza yote muhimu ya Yerusalemu yanayotajwa katika Matendo ya Mitume 15.
5. Barua kwenda kwa Tito ina shabaha kwenye ushauri wa Paulo anaoutoa kuhusu kazi yake huko Krete. Tito anatenda kazi kama mpasha habari rasmi wa Paulo.
6. Taarifa ya mwisho katika Agano Jipya kuhusu Tito ni kwamba alitumwa kufanya kazi Damaltia (kama vile 2 Timotheo 4:10)

**8:16"moyo"** Paulo anatumia neno hili mara nyingi katika 2 Wakorintho (kama vile 2 Kor. 1:22; 3:2-3,15; 4:6; 5:12; 6:11; 7:3; 8:16; 9:7). Angalia Mada Maalumu katika 1 Wakorintho 14:25.

**8:18" tukamtuma ndugu yule ambaye sifa zake katika Injili zimeenea makanisani mwote"** Desturi za kanisa zimesisitiza kuwa huyu anaweza akawa mtenda kazi pamoja na Paulo, Luka. Luka hatajwi katika orodha ya waliosafiri na Paulo wanaotajwa katika Matendo ya Mitume 20:4, lakini kwa sehemu "tu", ambayo inamaanisha uwepo wa Luka na kuanza katika Matendo ya Mitume 20:5-6,inatokea katika wakati huu katika muktadha (kama vile Origen recorded in Eusebius' *Hist. Eccl.* 6:25:6; A. T. Robertson' *Word Pictures in the New Testament*, kurasa 245).

F. Bruce, *Paul: Apostle of the Heart Set Free*, anatoa maoni yake kuhusu Tito and Luka kuwa ndugu wa damu.

> "Maelezo ya ukimya wa Luka kuhusu Yule aliyekuwa askari aliyeaminiwa wa Paulo ni kwamba Tito alikuwa ni ndugu wa Luka; kama vile W. M. Ramsay, *St. Paul the Traveller and the Roman Citizen* (London, 1895), ukurasa 390; *Luke the Physician and Other Studies* (London, 1908), kurasa 17 na kuendelea; A. Souter, 'A Suggested Relationship between Titus and Luke', *Expository Times* 18 (1906-7), ukurasa 285, na "The Relationship between Titus and Luke', *ibid*., kurasa. 335 na kuendelea. Lakini ikiwa huu ni uhusiano unaolindwa, kuna uwezekano kuwa Luka ni 'ndugu' wa 2 Wakorintho 8:18 na kuendelea (angalia kurasa 320) inavyoamuriwa. Kusudi la Paulo katika kutuma huyu ndugu pamoja na Tito ilikuwa ni kwamba awe ni mfadhili wa kujitegemea wa utauwa wa uongozi wa mfuko wa kusaidia wenye mahitaji, na kusudi hili lingekuwa limeparanganyishwa iwapo wakosoaji wangepewa fursa ya kuangazia kwenye uhusiano wa damu kati ya hawa wawili. Hakuna ambacho kingepigiwa gharama kuweza kuendeleza mashaka ambayo yalikuwa yamekwisha jengeka" (ukurasa 339 Tanbihi#5).

M.R. Vincent katika *Word Studies* anataja nadharia nyingine.

> "Mtu anayetajwa amekwisha kwa namna mbalimbali kutambuliwa kuwa ndugu wa Tito, Barnaba, Marko, Luka, na Epaeneto, wanaotajwa katika Warumi 16:5. Mrejeo wa Epaeneto umesisitizwa kwa msingi wa yumkini, mchezo uliopo katika maneno *praise, epainos*; Epaeneto ikimaanisha anayestahili kusifiwa; na usambamba unawekwa katika namna ya *Onesimus profitable* ambao Paulo anasema kuanzia sasa aktakuwa *mwenye kufaa* na matumizi mema.

**8:19" bali alichaguliwa na makanisa"** KITENZI ni *cheirotoneō*, ambacho kinatoka katika ambatani kutoka "mkono" na "kuvuta." Kwa asili inamanisha kupiga kura kwa kunyoosha mkono. Haiwezi kumaanisha hili katika Matendo ya Mitume 14:23, lakini haimaanishi hapa katika 2 Wakorintho 8:19

Hapa ni mfano mwingine wa kimkusanyiko wa dola inayounganishwa na makusanyiko kadhaa tofauti. Angalia angalizo kamii katika 1 Wakorintho 16:3

**NASB"kusafiri nasi katika kazi ya neema"**
**NRSV"kusafiri pamoja nasi kwa kipawa hiki"**
**NKJV"kusafiri pamoja nasi tunapofanya kazi hii ya ukarimu"**

**TEV"kusafiri pamoja nasi tunapofanya huduma hii ya upendo"**
**NJB"kuwa mmoja wetu katika safari ya kazi ya ukarimu"**

Paulo siku zote alikuwa anawasiwasi na kutuhumiwa kwake kwa matumizi mabaya ya fedha (kama vile 2 Wakorintho 8:20; 11:9, 12). Kwa hiyo, alitaka wachukue wawakilishi kadhaa wa kutoka katika makanisa mbalimbali pamoja naye ili kutoa mchango uliotoka kwa makanisa ya Mataifa kwenda kwa kanisa mama huko Yerusalemu.

◙**"ili Bwana atukuzwe, ukadhihirike utayari wetu"** Kipawa hiki cha kifedha kilikuwana makusudi kadhaa. Mawili yanatajwa hapa.

1. Kumtukuza Bwana
2. Kuonesha utayari wa makanisa ya mataifa kusaidia kanisa mama lililopo Palestina
   Yawezekana ilimsaidia Paulo kuonesha kujitoa kwake na uaminifu kwa jamii ya waaminio wa Kiyahudi iliyo sehemu ya kanisa la wote la ulimwengu. Angalia MADA MAALUMU: UTUKUFU (AGANO LA KALE) (SPECIAL TOPIC: GLORY *(OT)*) katika 1 Wakorintho 2:7.

Kuna aina za machapisho ya Kiyunani yanayounganishwa na "Yeye mwenyewe." Kiwakilishi hiki chenye pande mbili kinajitokeza katika namna mbili,

1. *auto* - MSS א, D[1]
2. *autēn* - MS P
3. Iliyotolewa katika the uncial MSS B, C, D*, F, G, and L (NJB)

Toleo la UBS[4] inatoa mbadala #1. Alama ya "C" ambayo inamaanisha kamati ya maandiko haiwezi kuamua.

**8:20" Tukijiepusha"** Kifungu cha maneno "kujiepusha au tukichukua tahadhali" (yaani "kujiepusha," KAULI YA KATI ENDELEVU YA WAKATI ULIOPO linatumika hapa tu na katika 2 Wathesalonike 3:6) ilikuwa ni sitiari ya ubaharia kwa kujali zaidi katika kujishughulisha na safari wanapokaribia bandari (kama vile Moulton and Milligan, ukurasa 587 from *Homer*).

**NASB"kushusha hadhi"**
**NKJV, NRSV"kulaumu"**
**TEV"kuchochea manug'uniko yoyote"**
**NJB"kuweza kufanya tuhuma"**

Hii ni neno la Kiyunani *mōmos*, ambayo kimsingi linamaanisha, kebehi, aibu au majeraha (kama vile 2 Petro 2:13). KITENZI hapa (yaani KAULI YA KATI TEGEMEZI YA WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFU) inamaanisha "kutafuta kosa," "kukosoa," au "kulaumu" (kama vile 2 Wakorintho 6:3; 8:20).

**NASB, NRSV,**
**TEV"kipawa hiki cha ukarimu"**
**NKJV"kipawa hiki cha ukarimu"**
**NJB"kiasi hiki kikubwa"**

Hili si neno la kawaida kwa ajili ya kipawa. Lilitumika katika tafsiri ya Agano la Kale la Kiyunani kwa jili ya watu wazima waliokomaa (kama vile 2 Samweli 15:18; 1 Wafalme 1:9) na viongozi (kama vile 2 Samweli 15:18; 2 Wafalme 10:6,11; Isaya 34:7). Kutoka katika fasihi ya Kiyunani ilitumika kwa ngano iliyokwisha iva au kitu kinene. Inapatikana hapa tu katika Agano Jipya.

**8:21" tukitangulia kufikiri yaliyo mema"** Hii inaonekana kuwa nukuu kutoka katika Mithali 3:4 katika tafsiri ya Agano la Kale la Kiyunani. Waamini wanahitaji kuwa juu ya mashaka katika kila kitu (Mathayo 10:16; Warumi 12:17; 1 Wathesalonike 5:22).

Neno "mheshimiwa" (NASB) au "sawa" (NKJV, NIV) ni neno la Kiyahudi, *kalos,* ambalo lina aina mbalimbali za viwango.

1. Ya kupendeza

2. Nzuri
3. Ya maana
4. Yenye ubora
5. Ya kiwango sawa
6. Yenye heshima
7. Ya uzuri wa tofauti
8. Yenye ubora zaidi
9. Inayostahili
10. Yenye thamani nzuri
11. Yenye staha

◙**"mbele za Bwana"** Hii inamaanisha nia ya mtu na maarifa ya maandiko. Kama 2 Wakorintho 8:21 inatoka Mithali 3:4, kwa hiyo Bwana anamaanisha YHWH.

◙**"ila na mbele ya wanadamu"** Hii inamanisha shahidi yetu (Warumi14:18; Wafilipi 2:15; 4:8; 1 Timotheo 3:7; 1 Petro 2:12).

**8:22" Nasi pamoja nao tumemtuma ndugu yetu"** Hii inaonekana kuwa ya pili kwa kuwa na mtu aliyefuatana nao asiyejulikana kutimiza matakwa ya Agano la Kale ya mashahidi wawili (kama vile Kumbukumbu la Torati 17:6; 19:15). Hii inamaanisha kwamba Paulo anamaanisha kwa muktadha huu watu watatu.

1. Tito
2. Ndugu wa 2 Wakorintho 8:18
3. Ndugu wa 2 Wakorintho 8:22

◙**"tuliyemwona mara nyingi"** Neno hili *dokimazō* pia linaonekana katika 2 Wakorintho 8:8 na mfumo mwingine wa neno ni 2 Wakorintho 8:2. Angalia Mada Maalum: Maneno ya Kiyunani ya "kujaribu" na maana zake katika 1 Wakorintho 3:13

◙**"kwa sababu ya tumaini kuu alilo nalo kwenu"** Angalia angalizo kamili katika 2 Wakorintho 3:4.

**8:23**
**NASB, NKJV,**
**NRSV"wao ni wajumbe wa makanisa"**
**TEV"wanawakilisha makanisa"**
**NJB"wao ni mabalozi wa makanisa"**

Hili ni neno *apostolos,* ambalo linamanisha "mjumbe" au "wakala." Kwa sababu ya upekee wa matumizi ya neno hili katika Injili ya Yohana ikimaanisha Yesu kama "Aliyetumwa" na Awatumaye Wafuasi wake, neno limechukua maana yake ya kipekee ya uwakilishi wa kiofisi (yaani Mtume). Hapa linatumika katika hali yake ya kawaida wa yale (Tito na ndugu wawili wasiotajwa) waliotumwa kuwakilisha makanisa katika safari ya Yerusalemu pamoja na sadaka. Angalia Mada Maalumu: Tuma katika 1 Wakorintho 4:9

◙**"utukufu wa Kristo"** Hii lazima inahusu 2 Wakorintho 8:19. Angalia MADA MAALUMU:UTUKUFU (AGANO LA KALE) (SPECIAL TOPIC: GLORY *(OT)* katika 1 Wakorintho 2:7. Inawezekana kuwa kifungu hiki cha maneno kinahusu makanisa yaliyotuma matoleo.

**8:24** Swali la kujiuliza ni nani fungu hilo la neno "wa.." linawamaanisha?

1. Inaweza kuwa ilimaanisha maskini walioko katika kanisa huko Yerusalemu. Kanisa la Wakorintho lilidhihirisha upendo wake kwa kipawa chao kwa kanisa mama. Ukarimu wao uliwaonesha makanisa mengine ya mataifa kuwa walikuwa wakishiriakiana na kufuata uongozi wa Paulo.
2. Ingemaanisha makanisa mengine yenyewe. Mbadala bora kimuktadha na kisarufi ni #2

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa usomaji wa fasiri, ambayo inamaanisha kwamba unao wajibu wa tafsiri yako mwenyewe ya Biblia. Kila mmoja wetu lazima aenende katika nuru tuliyo nayo. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hupaswi kumuachia vitu hivi mfasiri.

Maswali haya ya kujadili yanatolewa ili kukusaidia kufikiri mambo muhimu yaliyoko katika kipengele cha kitabu hiki. Yamekusudiwa kukuchokonoa akili, na sio kutoa maana ya mwisho.

1. Utoaji wa Agano Jipya unatofautianaje na utoaji wa Agano la Kale?
2. Je utoaji wa Zaka ni kweli ya jumla ya watu wote au ni kweli ya kitamaduni? Kwanini au kwaninii sio?
3. Je utoaji unawakwazaje Wamakedonia?
4. Elezea tofauti kati ya utoaji na uwakili?
5. Je huyu ndugu ni nani anayetajwa katika 2 Wakorintho 8:18?

# 2 WAKORINTHO 9

| MGAWANYO WA AYA WA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **UBS[4]** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB** |
| Matoleo ya Watakatifu | Kuongoza vipawa | Ukusanyaji wa misaada ya kanisa la Yerusalemu<br>(8:1-9:15) | Msaada kwa Waamini wahitaji | Watu waliopendekezwa kwa Wakorintho<br>(8:1-9:5) |
| 9:1-5 | 9:1-5 | 9:1-5 | 9:1-5 | Baraka Zinazotegemewa kutoka katika makusanyo |
| | Atoaye kwa furaha | | | |
| 9:6-15 | 9: 6-15 | 9:6-15 | 9:6-15 | 9:6-9<br>9:10-15 |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (Kutoka "**Mwongozo wa Usomaji Mzuri wa Biblia" ("A Guide to Good Bible Reading")**

### *KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, hii ina maana kwamba unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe kutoka katika Biblia. Kila mmoja wetu anatembea katika nuru tuliyonayo, wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele. Hupaswi kumuachia mfasiri vitu hivi.

Soma Sura kwa mara moja. Tambua masomo yanayozungumzwa. Linganisha mgawanyo wa mada zako na tafsiri tano hapo juu. Aya zaweza kuwa hazina uvuvio lakini ni msingi kupata au kufuatilia kusudio la asili la mwandishi ambao ndio moyo wa tafsiri. Kila aya ina somo moja na somo ni moja tu.

13. Aya ya kwanza
14. Aya ya pili
15. Aya ya tatu
16. Na nyinginezo

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA

A. Ni lazima ikumbukwe kwamba sura ya 8 na 9 zinatengeneza umoja wa kifasihi. Pia kwa namna nyingine ni sambamba. Yawezekana Paulo ameunganisha hotuba mbili kuhusu utoaji wa Mkristo.

B. Sura hizi mbili zikiwekwa pamoja, kwa maoni yangu zinatengeneza mjadala wa maana wa uwakili wa Agano Jipya.

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 2 WAKORINTHO 9:1-5**
**[1] Kwa habari za kuwahudumia watakatifu sina haja ya kuwaandikia. [2] Maana najua utayari wenu, ninaojisifia**

**kwa ajili yenu kwa Wamakedonia, kwamba Akaya ilikuwa tayari tangu mwaka mzima; na bidii yenu imewatia moyo wengi wao. [3] Lakini naliwatuma hao ndugu, ili kujisifu kwetu kwa ajili yenu kusibatilike katika jambo hili; mpate kuwa tayari, kama nilivyosema; [4] kusudi, wakija Wamakedonia pamoja nami, na kuwakuta hamjawa tayari, tusije tukatahayarika sisi, (tusiseme ninyi), katika hali hiyo ya kutumaini. [5] Basi naliona ya kuwa ni lazima niwaonye ndugu hawa watangulie kufika kwenu, na kutengeneza mapema karama yenu mliyoahidi tangu zamani, ili iwe tayari, na hivi iwe kama kipawa, wala si kama kitu kitolewacho kwa unyimivu.**

◙**"haja ya kuwaandikia"** Si kawaida kwa Paulo kusema hivyo wakati amewaandikia wao punde kuhusu jambo hilo (yaani makusanyo kutoka kwa makanisa ya Mataifa kwa kanisa mama lililopo Yerusalemu, kama vile sura ya 8). Sura hizi mbili ni sambamba katika kanuni ya kiroho kuhusiana na uwakili wa Mkristo. Yawezekana ziko hotuba mbili zilizounganishwa au sehemu mbili za Katekisimu.

◙**"kuwahudumia"** Neno hili (*diakonia*) mara nyingi limetumika kwa uwakili wa Mkristo (kama vile Matendo ya Mitume 6:1; 11:29; Warumi 15:31; 2 Wakorintho 8:4; 9:1,12,13). Hapa linamaanisha utumishi. Uhusiano wa Waaminio kwa Mungu mwenye neema na utoaji binafsi wa Masihi anahitaji maisha ya kuwahudumia watu wengine (kama vile Yohana 17:18; 20:21; 1 Waraka wa Yohana 3:16). Angalia MADA MAALUMU: UONGOZI WA KUTUMIKIA WENGINE (SPECIAL TOPIC: SERVANT LEADERSHIP) katika 1 Wakorintho 4:1.

◙**"kwa watakatifu"** Angalia Mada maalumu: Watakatifu (Special topic: Saints)

**9:2"najua utayari wenu"** Paulo ameeleza kuhusu hili katika 2 Wakorintho 8:8-12, 20

◙ "**ninaojisifia kwa ajili yenu kwa Wamakedonia"** Hii ni KAULI YA KATI ELEKEZI YA WAKATI ULIOPO. Paulo anaendelea kujivunia kuhusu watu wa Akaya. Katika 2 Wakorintho 8:1-5, Paulo anatumia Wamakedonia kutia moyo Wakorintho; sasa, katika Sura ya 9 Paulo anasema kwamba anawatumia wa Akaya kuwatia moyo wa Makedonia.

◙**"kujisifia"** Angalia Mada Maalumu: Majivuno (special topic : boasting) katika 1 Wakorintho 5:6

◙**"Akaya"** Hili lilikuwa ni Jimbo la Rumi pembeni mwa bahari mwa Ugiriki. Hii inakubaliana na 2 Wakorintho 1:1, ambapo barua inaandikwa kwa ajili ya watu wote wa Mungu katika Akaya. Hiyo inaonesha kwamba barua ilisomwa katika makanisa kadhaa ya eneo au kwamba Kanisa katika Korintho lililokuwa mji mkuu wa jimbo lenye ushawishi mpana wa kijiografia.

◙**"ilikuwa tayari tangu mwaka mzima"** Inaonekana kuwepo na mkanganyiko wa sura ya 8. Hata hivyo, Wakorintho walitaka kuanza matoleo ya mwaka mapema lakini hawakuwahi kuimaliza. Tatizo halisi ni tafsiri (aina ya mgeuzo ni ileile) ya KITENZI.

1. Ikiwa ni KAULI YA KATI ELEKEZI YA WAKATI TIMILIFU,inatakiwa ifasiriwe "wamefanya maandalizi"
2. Ikiwa ni KAULI TENDEWA ELEKEZI YA WAKATI TIMILIFU, kwasababu ya muktadha na kufanana ENDELEVU katika 2 Wakorintho 9:3 (yaani KAULI YA KATI YA WAKATI TIMILIFU).

◙**"bidii yenu imewatia moyo wengi wao"**KITENZI katika sentensi hii inaweza kutumika katika namna hasi (kama vile Tafsiri ya Agano la Kale la Kiyunani la Kumbukumbu la Torati 20:21; Wakolosai 3:21) au namna chanya (kama vile 2 Wakorintho 9:2). Ni muktadha tu unaoweza kuamua maana.

**9:3 "mpate kuwa tayari"** KAULI TENDEWA TEGEMEZI. NJEO na IRABU vinafanana na 2 Wakorintho 9:2, lakini DHAMIRA TEGEMEZI inaonesha kuna viashiria vya dharura iliojikita katika maamuzi ya waaminio wa Korintho unaohusiana na makusanyo (fasihi. "suala hili")

**9:4"wakija Wamakedonia pamoja nami"** Hii ni SENTENSI DARAJA LA TATU SHURUTISHI inayomaanisha kitendo kinachowezekana. Wawakilisha hawa wanatajwa katika 2 Wakorintho 8:19-24. Katika Matendo ya Mitume 20:4 ambapo wawakilishi kwa Yerusalemu wa matoleo haya wanatajwa, hayuko anayetajwa katika orodha kutoka Korintho. Baadhi wameeleza kwamba ilikuwa inawezekana kwamba Tito aliyetangulia mapema alikuwa mwakilishi wao lakini hatajwi popote katika Matendo ya Mitume.

◙ Kuna VITENZI TEGEMEZI VYA WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFU vitatu katika 2 Wakorintho 9:4 inatoa utangulizi wa kiashiria cha uwezekano kwa kujikita kwenye matendo ya Makanisa ya Akaya.

**NASB"sisi - tusije tukawazungumzia ninyi"**
**NKJV"sisi (tusije tukawataja ninyi!)"**
**NRSV"sisi….tusiseme kitu juu yenu"**
**NJB"sisi - tusiseme kitu juu yenu wenyewe"**

Tatizo linalotafsiriwa kwa njia hizi tatu tofauti inahusiana na KIWAKILISHI na namna kinatakiwa kifanane na KITENZI kilichotangulia ("inatakiwa kuaibishwa "*kataischunthōmen*, KAULI TENDEWA YA WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFU TEGEMEZI, WINGI). UBS[4] inaonesha mbadala tatu.

1. "*lego*" (KAULI YA WAKATI ULIOPO TENDAJI TEGEMEZI, UMOJA) - MSS P[46], C[*], D, F, G
2. "*legōmen*" - (KAULI YA WAKATI ULIOPO TENDAJI TEGEMEZI, WINGI) - MSS א, B, C[2]
3. Ondoka - MS K

UBS[4] inatoa mbadala #1 a "B" alama (karibu na kutimia). Paulo anatumia NAFSI YA KWANZA UMOJA katika 2 Kor. 9:1, 2, 3, na 5 (Metzger, ukurasa 582).

**NASB"kwa ujasiri huu"**
**NKJV"kwa ujasiri huu wa majivuno"**
**NRSV"katika kufanya hili"**
**TEV"kwa kujiskia uhakika wa ninyi"**
**NJB" kwa ujasiri wetu juu yenu"**

Kwa nini Paulo na kanisa la wakorintho waone aibu? Neno *hupostasis* (yaani NASB, "ujasiri"), kulingana na Bauer, Arndt, Gingrich and Danker's *Greek-English Lexicon*, haiwezi kutafsiriwa "ujasiri," lakini lazima iwe "namna ya ufahamu" au yawezekana "kutambua" kwa ukusanyaji kwa ajili ya maskini katika Yerusalemu (kama vile NRSV) (ukurasa 847#2 na #3). Paulo alikuwa na hofu kuhusu matoleo na sio kujivuna. Hii inarandana na matumizi ya neno katika Waebrania 1:3. Hata hivyo, unapolinganisha na matumizi ya neno hilohilo katika 2 Wakorintho 11:17, "kujivuna kwa ujasiri," hivyo mtu anaelewa kwa nini NASB inatafsiriwa namna hii katika mstari huu.

Neno "kujivuna" (NKJV) linakosekana katika maandiko mengi ya mwanzo ya Kiyunani (yaani MSS P[46], א[*], B, C, D[*], F, G). Inapatikana katika MSS א[2], D[1]. Toleo la UBS[4] inatoa kuondolewa kwake alama ya "B" (inakaribia kwa hakika).

**9:5** Yapo maneno matatu katika mstari huu ambayo yanaanza na kiambishi awali *pro* (yaani kabla).

1. Paulo aliwatanguliza wawakilishi wa kanisa (*proerchomai*, kama vile Matendo 20:5,13)
2. Paulo aliwataka waandae kabla (*prokatartizō*, kama vile Matendo 3:18,24; 7:52)
3. Paulo alitaka kutimiza ahadi yao ya mwanzo (*proepēngellomai*, kama vile Warumi 1:2)

**◙"kipawa kisicho na unyimivu"** Hii ni *eulogia*(yaani kiuwazi "neno zuri"). Neno hili pia linatumika katika 2 Wakorintho 9:6 kwa maana ya "utele."

Neno hili ni pana kimaana. Louw na Nida, *Greek-English Lexicon*, wanaorodhesha maana sita (vol. 2, ukurasa wa 108).

1. Sifa (kama vile Yakobo 3:9)
2. Mazungumzo matamu (kama vile Warumi 16:18)

3. Baraka (kama vile 1 Wakorintho 10:16; Yakobo 3:10)
4. Faida (kama vile Warumi 15:29)
5. Zawadi/kipawa (2 Wakorintho 9:5)
6. Kiasi kikubwa (kama vile 2 Wakorintho 9:6)

Haya matumizi ya #3 yanafuata tafsiri ya maandiko ya Agano la Kale ya Kiyunani (Waamuzi 1:15)

**NASB"kama zawadi isiyo na unyimivu na isiyo athiriwa na wivu"**
**NKJV" suala la ukarimu na sio kama kulazimisha uchungu"**
**NRSV"kama kipawa tulichopewa pasipo kustahili na sio kama tulikipata kwa nguvu zetu"**
**TEV"mnatoa kwasababu mnataka kufanya hivyo na sio kwasababu mnalazimika"**
**NJB"kama kipawa cha kweli na si kama mzigo"**

Kiuhalisia "kwahivyo kama Baraka na sio tamaa binafsi." Mjadala mzima wa Paulo kuhusu kutoa katika kipengele hiki cha fasihi (yaani 2 Wakorintho 8-9) unaandikwa katika njia chanya na ya kimkakati, lakini kifungu hiki cha neno kinaonesha kwamba kulikuwa na kiashiria cha upinzani kanisani. Paulo alitaka kanisa la Korintho kujihisi ni sehemu ya ushirika mkubwa wa makanisa yake na kuwa naye kama sehemu yake ya huduma ya huruma. Hata hivyo alijua kwamba baadhi wangechukua hii kama fursa ya kumtuhumu yeye juu ya kustahimili kwake kuhusu matoleo. Kwa hiyo kuzuia mashambulizi yanayowezekana kumpata, akasema "fanyeni kabla sijafika huko!"

*Jerome Biblical Commentary* (Fasiri ya Biblia ya Jerome) inasema kwamba NOMINO mara nyingi ilitafsiriwa "tamaa ya ubinafsi," inatakiwa kwa muktadha huu, kutafsiriwa "kipawa kinachotolewa kwa machungu" (ukurasa wa 285).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 2 WAKORINTHO 9:6-15**
**[6] Lakini nasema neno hili, Apandaye haba atavuna haba; apandaye kwa ukarimu atavuna kwa ukarimu. [7] Kila**
**mtu na atende kama alivyokusudia moyoni mwake, si kwa huzuni, wala si kwa lazima; maana Mungu**
**humpenda yeye atoaye kwa moyo wa ukunjufu. [8] Na Mungu aweza kuwajaza kila neema kwa wingi, ili ninyi,**
**mkiwa na riziki za kila namna siku zote, mpate kuzidi sana katika kila tendo jema; [9] kama ilivyoandikwa,**
**Ametapanya, amewapa maskini, Haki yake yakaa milele.[10] Na yeye ampaye mbegu mwenye kupanda, na**
**mkate uwe chakula, atawapa mbegu za kupanda na kuzizidisha, naye atayaongeza mazao ya haki**
**yenu; [11] mkitajirishwa katika vitu vyote mpate kuwa na ukarimu wote, umpatiao Mungu shukrani kwa kazi**
**yetu. [12] Maana utumishi wa huduma hii hauwatimizii watakatifu riziki walizopungukiwa tu, bali huzidi sana**
**kuwa na faida kwa shukrani nyingi apewazo Mungu; [13] kwa kuwa mkijaribiwa kwa utumishi huo,**
**wanamtukuza Mungu kwa ajili ya utii wenu katika kuikiri Injili ya Kristo, na kwa ajili ya ukarimu wenu**
**mliowashirikisha wao na watu wote. [14] Nao wenyewe, wakiomba dua kwa ajili yenu, wawaonea shauku kwa**
**sababu ya neema ya Mungu iliyozidi sana ndani yenu. [15] Mungu ashukuriwe kwa sababu ya kipawa chake,**
**tusichoweza kukisifu kama ipasavyo.**

**9:6" Apandaye haba atavuna haba"** Haya yanaonekana ni maelezo ya Mithali 11:24-25 (kama vile Mithali 19:17; 22:9). Inaaksi mafundisho ya Yesu kuhusu utoaji (kama vile Mathayo 7:2; Marko 4:24; Luka 6:38). Sitiari ya kilimo ya kupanda mara nyingi hutumika katika Biblia; mara nyingi katiko maandiko ya nyakati za mwisho, katika namna za kimahakama (kama vile Wagalatia 6:7). Lakini pia kama njia ya kumaanisha matendo yasiyokuwa ya kawaida ya kiungu kama ufufuo (kama vile 1 Wakorintho 15:35-37). Katika muktadha huu inazungumzia mbegu moja kuzaa mbegu nyingi kama njia ya kumaanisha utele. Lakini mbegu ya kwanza lazima itolewe (yaani ipandwe)!

**9:7 "Kila mtu na atende kama alivyokusudia moyoni mwake"** Hii ni KAULI YA KATI ELEKEZI YA WAKATI TIMILIFU. Hii ni moja ya kanuni ya msingi katika utoaji wa kiroho. Ipo kiwango kimoja na 8:12 katika kuwapa waamini miongozo mikuu kuhusu uwakili.

◙**"moyo"** Angalia angalizo kamili katika 1 Wakorintho 14:25

◙"**si kwa huzuni, wala si kwa lazima"**Utoaji wa kiroho lazima uwe ni wa kujitolea na nia njema sahihi (kama vile 2 Wakorintho 8:12). Binafsi nashtuka ninaposikia utoaji wa zaka wa Agano la Kale ukihubiriwa (mara nyingi ni kutoka Malaki au Mambo ya Walawi) kama (1) mwongozo/amri ya mali binafsi zao (2) kitisho cha afya ya mwili au ustawi. Angalia MADA MAALUMU: ZAKA (SPECIAL TOPIC: TITHING) katika 2 Wakorintho 8:8.

◙**"Mungu humpenda yeye atoaye kwa moyo wa ukunjufu"** Hii inaonekana kutoka Mithali 22:8 katika tafsiri ya maandiko ya Agano la Kale. Kauli haionekani kutoka katika MT. Tunapata neno la Kingereza "kifurahishi," kutoka katika mzizi wa Kiyunani. Neno hilohilo linatumika katika muunganiko wa rehema katika Warumi 12:8. Katika mafunjo yenye lugha ya Koine huko Uyunani (maandiko ya kimiujiza) neno *hilaros* (furaha) ni neno lenye maana sawa na *hileōs* (rehema). Kwa sababu ya hili Moulton na Milligan, katika *The Vocabulary of the Greek New Testament,* wanafikiri linatumika katika maana ya neema (ukurasa wa 303).

**9:8"Mungu aweza"** Huu ni ushuhuda mkubwa sana wa tabia ya Mungu na cheo chema (yaani "kwake Yeye kuna uweza," kama vile Warumi 16:25; Waefeso 3:20; Yuda 24). Waamini wanaamini, wanapenda, na kutumikia Mungu anayetenda kazi!

◙**"kuwajaza kila neema kwa wingi"** Kifungu hiki cha neno hakirejerei utoaji wa Wakorintho, kinarejelea asili ya misingi ya Mungu ambayo ni neema. Kwa sababu ya asili ya Mungu na kipawa cha Mungu (yaani Yesu), waaminio lazima watoe. Waamini wanaaksi tabia za familia ya Mungu.

◙ **"mkiwa na riziki za kila namna siku zote"** Angalia hesabu ya ujumuisho "zote" (yaani *pas*).

1. Neema yote (*pasan)*
2. Siku zote (*pantote*)
3. Zote toshelevu (*panti*)
4. Katika kila tendo jema (*pan*)
   Utoaji wa Mkristo unaathiri maisha yote! Mungu anatoa kwa mahitaji yote ( kama vile Mathayo 6:19-34)

Neno "utoshelevu" linatoka katika maneno mawili ya Kiyunani "binafsi" na "kuridhika" (kama vile 1 Timotheo 6:6-10; Wafilipi 4:11-12,19; Waebrania 13:15) A. T. Robertson's *Word Pictures In The New Testament*, vol. 4, ukurasa wa 248 na M. R. Vincent's *Word Studies*, ukurasa wa 831, wote wanadai kwamba matumizi ya neno yanaonesha Paulo alikuwa anafahamu mawazo na maneno ya ukakamavu. Lakini anatoa maana yake upya katika ufahamu wa Injili. Angalia Bruce Winter, *Philo and Paul Among the Sophists*.

◙**"mpate kuzidi sana katika kila tendo jema"** Mungu atawapa wale walioshirikiana nae katika mali zao, mali nyingi zaidi. Utele huu hata hivyo sio kwa ajili ya matumizi binafsi ya mtu mmoja mmoja bali kwa ajili ya Kristo (kama vile Waefeso 4:28). Utoaji wa Kikristo unakuwa mfereji wa Mungu wa kupitishia mahitaji kwa ajili ya mahitaji ya wengine. Huu ndiyo ukweli ambao umepotezwa katika mafundisho yetu ya uwakili wa Kikristo. Ndio, agano la Baraka na utele vitatokea lakini vinatakiwa viendelee kwa ajili ya ufalme na sio kushikiliwa au kuzuiwa! Waamini wameokolewa ili kutumikia na wanabarikiwa ili kutoa!

**9:9 "kama ilivyoandikwa"** Hii ni nukuu kutoka Zaburi 112:9 kutoka katika tafsiri ya maandiko ya Agano la Kale (yaani 111:9). Nukuu hii inajumuisha moja ya matumizi nadra ya neno "haki" (angalia Mada Maalum: katika 1 Wakorintho 1:30) ikirejelea matendo ya kibinadamu (kama vile Mathayo 6:1). Katika dini ya Kiyahudi ilikuja kurejelea matendo ya kila wiki ya Kiyahudi ya utoaji sadaka kwa maskini walioko katika Sinagogi (kama vile Zaburi 112:1-6) mara nyingi katika Agano Jipya, haki ni kipawa cha Mungu katika Kristo kutoka katika tabia za binadamu.

## MADA MAALUMU: UTOAJI SADAKA (SPECIAL TOPIC: ALMSGIVING)

◙**"milele"** angalia Mada maalumu hapa chini.

## MADA MAALUMU: MILELE (*'OLAM*) (SPECIAL TOPIC: FOREVER (*'OLAM*))

**9:10** Sehemu ya kwanza inaonekana kuwa nukuu kutoka Isaya 55:10, na sehemu ya pili inaonekana kunukuliwa kutoka Hosea 10:12. Mstari huu unaelezea

1. Umiliki wa Mungu na utoaji wake wa vitu vyote
2. Uwakili wa waaminio

   Mungu ndiye chanzo, lakini waaminio wanapokea Baraka wanapowashirikisha wengine.
   Umiliki wa Mungu unazungumzwa kupitia neno la Kiyunani "kuwasambazia" (yaani *chorēgeō),* inayokuja katika Kingereza kama "kiitikio."

   Neno hili katika Kiyunani cha Koine lilitumika kwa kumaanisha mfadhili wa utele anayesambazia kwaya za eneo fulani. Mara nyingi waamini wa kisasa wanayaona mafanikio yao kuwa yametokana na ubunifu wao wenyewe, kazi, maadili, na maarifa waliojikusanyia, au nguvu binafsi. Hata hivyo, muono wa kibiblia wa ulimwengu unakubiliana kuwa mali zote ni za Mungu. Angalia Mada Maalum: Uongozi wa kutumika katika 1 Wakorintho 4:1

**NASB, NRSV"kuongeza mavuno ya haki yako"**
**NKJV"kuongeza matunda ya haki yako"**
**TEV"kuzalisha mavuno mazuri ya ukarimu ya ukarimu wako"**
**NJB"tengeneza mavuno ya haki yako kuwa kubwa"**

Katika 2 Wakorintho 8:5 neno "neema" linatumika katika maana mbalimbali, kama ilivyo pia haki. Sitiari ya Kithiolojia ni namna waaminio wanapokea Baraka au zawadi kwa vitu ambavyo Mungu anavitoa au anavivuvia? Hii ni siri ya Mungu Mtawala na mwitikio wa mamlaka ya kiagano! Waamini wanatoa kwa sababu

1. Mungu hutoa
2. Mfano wa Yesu
3. Mahitaji ya kibinadamu
4. Mtazamo mpya wa kiulimwengu
5. Roho akaaye ndani

Utoaji ni matokeo ya asili ya wokovu. Mkristo bahili ni mkanganyiko wa kimsamiati!

**9:11 "mkitajirishwa katika vitu vyote"** Hii ni KAULI TENDEWA ENDELEVU YA WAKATI ULIOPO ya *ploutizō* "katika kila kitu" ikiwekwa mbele kwa ajili ya msisitizo. Kutoka 8:7-9, ni wazi kuwa hili halirejelei vitu kama Baraka tu, bali pia Baraka za rohoni (kama vile 2 Wakorintho 6:10; 1 Wakorintho 1:5).

◙**"ukarimu wote"** Angalia hapa maneno zaidi ya *pas* mjumuisho (kama vile 2 Wakorintho 9:8). Neno hili la Kiyunani linaweza kumaanisha pia kuwa na nia moja (yaani ukweli, usafi) na dhati (kama vile 2 Wakorintho 8:2; 9:11, 13). Angalia katika 2 Wakorintho 1:12

◙**"umpatiao Mungu shukrani"** Msisitizo wa kufunga sehemu ya sura ya 9 upo kwa Mungu kupokea utukufu unaotokana na washirika kushirishana (kama vile 2 Wakorintho 9:11-13). Hii inanikumbusha mimi habari ya Mathayo 5:16, ambapo inasema "wataziona kazi zenu njema na kumtukuza Baba yenu aliye mbinguni." Kusudi kubwa la Paulo katika kuunganisha kanisa mama la Yeusalemu na makanisa yake mengine ya mataifa ilikuwa kwamba hali ya upendo na shukrani iweze kujengeka (kama vile 2 Wakorintho 9:14)

**9:12"huduma"** Hili ni neno la Kiyunani *leitourgia* (muunganiko wa jamii na kazi) ambapo kutokana na hilo tunapata neno la lugha ya Kingereza "liturgy." (liturujia)

Kiasili ilimaanisha mtu aliyefanya kazi za jamii kwa gharama yake mwenyewe. Katika maana hii ni sawa na *chorēgeō* ya 2 Wakorintho 9:10.

◙ **"kuwatimizia watakatifu riziki walizopungukiwa"** Hili ni neno la Kiyunani *prosanaplēroō,* (KAULI TENDAJI ELEKEZI YA WAKATI ULIOPO YENYE UMBO), ambalo ni *pros* pamoja na *anaplēroō*, ambayo yanamaanisha kujaza au kukamilisha (kama vile 1 Wakorintho 14:16; 16:17). Paulo anatumia Vitamkwa vingi vyenye kina vyenye muundo

wa *pros* (kama vile 2 Wakorintho 9:5), hata hivyo matokeo halisi yatokanayo na maana sio hakika Paulo anatumia maneno hayo hayo yenye muundo wa ndani katika 2 Wakorintho 11:9.

Neno "riziki/mahitaji" lina maana halisia "vitu vinavyokosekana" (kama vile 1 Wakorintho 16:17; 2 Wakorintho 8:8, 13, 14; 11:8). Maskini waaminio katika Yerusalemu walikuwa na mahitaji ya kweli ambayo makanisa haya ya Mataifa walikuwa na uwezo wa kuyatimiza. Kwa "watakatifu" angalia Mada Maalum katika 1 Wakorintho 1:2.

◙**"huzidi sana kuwa na faida kwa shukrani nyingi apewazo Mungu"** Wahitaji wa Yerusalemu na waaminio wote katika Palestina walikuwa wakimpa shukurani Mungu kwa hali ya kujali na msaada wa kujitoa wa makanisa ya Mataifa (kama vile 2 Wakorintho 9:13).

**9:13"uthibitisho"** Hili ni neno linalosimama kwa "jaribu" (yaani *dokimē*) lililotumika katika 2 Wakorintho 2:9; 8:2; 13:3. Angalia Mada Maalum katika 1 Wakorintho 3:13.

◙**"huduma hii"** Hii inarejerea michango ya makanisa ya Mataifa ya Paulo kwa kanisa mama katika Yerusalemu. Hii ni neno lilelile lililotumika katika 2 Wakorintho 9:1.

**MADA MAALUMU: UKIRI (SPECIAL TOPIC: CONFESSION)**

**NASB, NKJV,**
**NRSV, NJB"utii"**
**TEV"uaminifu"**

Hili neno kiuhalisia linamaanisha "unyenyekevu" (yaani *hupotagē*, Wagalatia 2:5; 1 Timotheo 2:11; 3:4), lakini likitumika kwa maana ya utii kwa sababu Kusudio ni "Injili," na sio mtu.

**MADA MAALUMU: UNYENYEKEVU (*HUPOTASSŌ*) (SPECIAL TOPIC: SUBMISSION *(HUPOTASSŌ)*)**

◙**"kuikiri Injili ya Kristo"** Ukiri maana yake ni "kukubaliana na" (kama vile 1 Timotheo 6:12-13; 1 Waraka wa Yohana 1:9). Katika muktadha huu ukiri wao wa kisitiari ni mchango wao wa ukarimu unaothibitisha uhusiano wao na makanisa mengine ya Mataifa na Kristo . Maisha ya milele yana tabia zinaonekana!

◙**"Michango"** Hili neno *koinōnia* (kama vile Warumi 15:26), ambalo humaanisha "ushirikiano wa pamoja." Hapa inamaanisha pesa itolewayo kwa ajili ya maskini wa kanisa katika Yerusalemu (angalia angalizo katika 1 Wakorintho 16:1) angalia Mada Maalum katika 1 Wakorintho 1:9.

◙**"na watu wote"** Hiki ni kifungu cha neno ambacho kina ugumu katika kukifasiri. Inalazimika kwa namna fulani kumaanisha ushawishi wa Wakorintho katika kuwatia moyo makanisa mengine ya mataifa kushiriki katika makusanyo (kama vile 2 Wakorintho 9:2)

**9:14** Mstari huu unawarejelea wale wote waliopokea makusanyo (yaani maskini wa kanisa la Yerusalemu na washirika wake). Paulo alitaka matawi haya mawili ya kanisa la mwanzo kuungana bila kuachana.

◙**"iliyozidi"** *Huperballō*. Mada Maalum: matumizi ambatani ya Paulo ya *Huper* katika 1 Wakorintho 2:1.

**9:15" Mungu ashukuriwe kwa sababu ya kipawa chake"** wengine wanachukulia muktadha huu kumaanisha kipawa cha kifedha cha Wakorintho, lakini kwasababu

1. Kujidhabihu kwa kiasi kikubwa kwa Yesu kunakotajwa katika 2 Wakorintho 8:9
2. Injii ya Kristo inayotajwa katika 2 Wakorintho 9:1

Yawezekana inamaanisha huduma ya Yesu wa Nazareti, Masihi. James D. G. Dunn, *Unity and Diversity in the New Testament* (ukurasa wa 184) anataja kwamba “kipawa cha Mungu” katika Matendo ya Mitume kinamaanisha Roho Mtakatifu (yaani nyakati mpya, kama vile Matendo ya Mitume 2:38; 8:20; 10:45; 11:17).

Injili ya kujitolea ya Mwana (kama vile 2 Wakorintho 8:9) ilikusudiwa

1. Kuwavuvia waamini hawa kushukuru (yaani *eucharistia*, 2 Wakorintho 9:11,12; *charis*, 2 Wakorintho 9:13) kwa Mungu
2. Kuwalazimisha kuwashirikisha mali zao za kifedha pamoja na wahitaji waaminio.

**NASB, NKJV,**
**NRSV"isiyoelezeka"**
**TEV"isiyo na thamani"**
**NJB"zaidi ya maelezo"**

Hili ni neno *ekdiēgeomai*, ambalo linamaanisha kuelezea kwa ukamilifu au kutaja maelezo yote, pamoja na KIAMBISHI AWALI HASI, kinachokanusha. Katika namna ya upendo wa Mungu ni jambo la ajabu kwa binadamu kukamata pande zote( kama vile Kumbukumbu la torati 30:11; Ayubu 11;7; Zaburi 139:6; Mithali 30:18; Isaya 55:8-9; Warumi 11:33).

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa usomaji wa fasiri, ambayo inamaanisha kwamba unao wajibu wa tafsiri yako mwenyewe ya Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika nuru tuliyo nayo. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hupaswi kumuachia vitu hivi mfasiri.

Maswali haya ya kujadili yanatolewa ili kukusaidia kufikiri mambo muhimu yaliyoko katika kipengele cha kitabu hiki. Yamekusudiwa kukuchokonoa akili, na sio kutoa maana ya mwisho.

1. Ainisha kwa maneno yako mwenyewe kanuni za uwakili unaotajwa katika sura ya 8 na 9.
2. Kwa maneno yako mwenyewe, elezea nukuu ya 2 Wakorintho 9:6 na 2 Wakorintho 9:10 zilivyo na maana kwenye maisha yako.

# 2 WAKORINTHO 10

| MGAWANYO WA AYA WA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **UBS[4]** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB** |
| Paulo Anatetea Huduma Yake | Vita ya Kiroho | Utetezi kwa Utume wa Kweli | Paulo Anatete Huduma Yake | Paulo alijibu kuhusu Tuhuma ya Udhaifu |
| 10:1-6 | 10:1-6 | 10:1-6 | 10:1-6 | 10:1-11 |
| | Uhalisia wa Mamlaka ya Paulo | | | |
| 10:7-11 | 10:7-11 | 10:7-11 | 10:7-11 | |
| | Mipaka ya Mamlaka ya Paulo | | | Majibu yake juu ya Tuhuma |
| 10:12-18 | 10:12-18 | 10:12-18 | 10:12-161 | 0:12-18 |
| | | | 10:17-18 | |

**MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI** (kutoka"**Mwongozo Mzuri wa Usomaji Biblia ( A Guide to Good Bible Reading**")

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI ZA AYA*

Haya ni maoni ya mwongozo kwa kujisomea, ikiwa na maana kuwa unawajibika binafsi kwa tafsiri ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mtoa maoni tu.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa,lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

9. Aya ya kwanza
10. Aya ya pili
11. Aya tatu
12. N.k

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA

A. Sura ya 10 hadi ya 13 zinatoa muundo wa umoja wa mwandishi ambapo Paulo anajitete kuhusu mashtaka ya walimu wa uongo. Walimu wa uongo walikuwa wamemfanya Paul kuwa kiini cha mjadala. Kwa hiyo, bila hiari yake, anajitetea kwa misingi ya kibinadamu, akitumia maneno yao ya uzushi na mtindo wa elimu yao ya usemaji. Kusudi lake hatimaye lilikuwa kuitete injili.
B. Baadhi ya mifano ya mashitaka yaliyomkabili Paulo.
   1. Alikuwa muoga alipokuwa amekutana nao macho kwa macho, lakini alikuwa mjasiri katika barua yake, 2 Kor. 10:1, 9, 11.

2. Alikuwa anaenenda katika nia ya kibinadamu ya hali ya chini sana, 2 Kor. 10:2.
3. Mwonekano wake binafsi haukuwa unapendeza na mtindo wake wa usemaji ulikuwa wa hali ya chini; 2 Kor. 10:2, 10
4. Alihubiri ili mradi apate fedha tu, 2 Kor. 11:8, 12; 12:16.

C. Maadui wa Paulo
   1. Yaonekana kuwa makundi matatu yalikusudiwa
      a. Mkorintho mmoja mwenyeji ambaye angeweza kutoka( makundi ya kanisa la 1 Wakorintho 1-4)
      b. Myahudi ambaye angeweza kutoka Palestina (mfano wa dini ya Kiyunani, 2 Kor. 10-13).
      c. Yawezekana ni chotara wa wote
   2. Kutoka 1 Wakorintho kunaonekana kuwepo makundi yanayoshambulia kwa ajili ya sehemu za upinzani na kutoka sehemu hiyo.
      a. Kundi la wanaokazia sheria (kujima anasa)
      b. Kundi la antinomia (waasherati)

D. Kwa sababu Paulo anataja barua kadhaa ambazo alikwisha kuwaandikia kanisa la Wakorintho, ambazo yaonekana hazikuhifadhiwa, kumekuwepo na kisio kuhusu 2 Wakorintho yenye sehemu zaidi ya moja ikiwa moja wapo ya barua hizi zilizopotea. Ni ukweli wenye hakika kwamba matumizi ya WARAKA WA WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFU katika kurejelea barua zake mbalimbali zimesababisha kanganyiko pamoja na vifungu vya maandishi pamopja na tofauti dhahiri ya kitengo cha fasihi vinavyokamilisha 2 Wakorintho, ambavyo mara nyingi huonekana kuwa nje ya mpangiliao na utaratibu wa kimantiki.

   Yawezekana kwa uhakika kwamba miachano iliyosababishwa na Paulo kuandika barua hii kwa muda na kwamba habari mpya zilizoendelea kufika baada ya yeye kuwa ameandika vifungu vya maandishi. Barua inaanza kwa uthibitisho chanya, lakini kisha inabadilika kuwa hasi.

   Binafsi, uwezekano kwamba baadhi ya barua za Paulo zilipotea hainipi shida (yawezekana zilikuwa na taarifa ambazo Roho hakutaka ziwe maandiko), lakini hali iliyokusudiwa yenye sehemu zaidi ya moja yenye asili ya 2 Wakorintho, ambayo haina ushahidi katika miswada ya mapokeo ya Kiyunani au ya kanisa, bali makisio ya wasomi wa kisasa wa magharibi hainipi shida mimi! Hatupaswi kulazimisha watu wenye fikra nyingi na waandishi wa mashariki ya kale katika aina za fasihi za sasa za madharibi.

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 2 WAKORINTHO 10:1-6**

**[1]Basi, mimi Paulo mwenyewe nawasihi kwa upole na utaratibu wa Kristo; mimi niliye mnyenyekevu nikiwapo pamoja nanyi, bali nisipokuwapo ni mwenye ujasiri kwenu; [2] naam, naomba kwamba nikiwapo, nisiwe na ujasiri kwa uthabiti ambao nahesabu kuwa nao juu ya wale wanaodhania ya kuwa sisi tunaenenda kwa jinsi ya mwili. [3] Maana ingawa tunaenenda katika mwili, hatufanyi vita kwa jinsi ya mwili; [4] (maana silaha za vita vyetu si za mwili, bali zina uwezo katika Mungu hata kuangusha ngome) [5] tukiangusha mawazo na kila kitu kilichoinuka, kijiinuacho juu ya elimu ya Mungu; na tukiteka nyara kila fikira ipate kumtii Kristo; [6] tena tukiwa tayari kupatiliza maasi yote, kutii kwenu kutakapotimia.**

**10:1 "Basi, mimi Paulo mwenyewe nawasihi"** Paulo hatumii neno "sisi" katika sura zilizopita kwa sababu anajitetea mwenyewe binafsi mbele ya mashtaka ya walimu wa uongo. Paulo alitumia *autosna ego* (kama vile Kor. 12:13; Rum. 7:25; 9:3; 15:24; na katika Gal. 5:2 *egō* na *Paulos*) kusistiza kwamba hili lilikuwa ombi lake binafsi.

Kawa neno "sihi" angalia maelezo kamili katika 2 Kor. 1:4-11.

◙ **" kwa upole na utaratibu wa Kristo"** Paulo alitumia mtazamo unaofaa na methodolojia hata pamoja na hawa walimu wa uongo ( kama vile Mt. 11:29). Unyenyekevu haukuonekana kama kitu cha heshima kwa Wayunani wenye fikra nyingi (yaani, Socrates, Aristotle, Wavumilivu). Hili linaaksi moja wapo ya lawama zao kwa Paulo. M. R. Vincent's *Word Studies*, juzuu 2, anaonyesha kwamba katika tafsiri ya agano la kale kwa Kiyunani kwamba “unyenyekevu” (*praus*, 2 Kor. 10:1), "mnyenyekevu" (*tapeinos*, 2 Kor. 10:1), na “masikini” (*penēs*, mst. 9:9) yametumika kutafsiri maneno hayo hayo ya Kiebrania . Inaweka wazi tofauti baina ya tajiri na wenye nguvu dhidi ya wenye hali ya chini na aliyekanywagwa chini (uk. 832).

◙ **"niliye mnyenyekevu nikiwapo pamoja nanyi, bali nisipokuwapo ni mwenye ujasiri kwenu"** Tathmini hii yaweza kuhusu barua ya Paulo ambayo ni kali iliyopotea (kama vile 2 Kor.1:9-11). Angalia mzaha wake kwenye dhana ya ‘unyenyekevu.” Yeye humuita Kristo mnyenyekevu (yaani, *praus*iliyotumika kwa Masihi katika Mt. 21:15 na waaminio katika Mt. 5:5; 1 Pet. 3:4, 15). Katika kifungu hiki cha neno anatumia kisawe *tapeinos* (kama vileLouw na Nida, *Greek-English Lexicon*, juzuu 1, uk. 748), amabcho pia kimetumika kwa Yesu (kama vile Mt.11:29) na kwa Paulo (kama vile 2 Kor. 11:7; 12:21).

◙**"ujasiri"** Angalia maelezo katika 2 Kor. 5:6.

◙ **"naam, naomba"** Hili ni neno la Kiyunani *deomai*, linalomaanisha kuomba kwa haraka au kusudi. Ni kisawe cha neno (yaani, *parakaleō*, kama vile Louw na Nida, *Greek-English Lexicon*, juzuu. 1, uk. 408) Paulo alilitumia katika 2 Kor. 10:1 (kama vile 2 Kor. 2:8; 5:20; 6:1; 8:6; 9:5; 12:8,18; 13:11). Anahisi kwa haraka hawa waaminio kutathimini tena kile walichokwisha kusikia kutoka kwa walimu wa mafundisho ya uongo.

◙ **"kwamba nikiwapo"** Paulo hakupenda kurudi Korintho hadi pale mambo yangekwisha badilika. Hakutaka kuwa jasiri, bali mpole.

◙**"nisiwe na ujasiri kwa uthabiti ambao nahesabu kuwa nao juu ya"** Kuna mzaha juu ya neno la Kiyunani kwa “mwili.” Walimu wa mafundisho ya uongo walikuwa wanamshutumu Paulo kwa utenadaji wa kiwango cha hali ya chini sana katika msingi wa nia ya kibinadamu (yaani, katika mwili). Wakati Paulo anakiri kwamba yu katika mwili (yaani, mwili wa asili, kama vile 2 Kor. 10:3), anadai kwa nguvu kwamba hatendi mambo kwa kuongozwa na nia za kibinadamu (kama vile 2 Kor. 1:17; 2:17; 4:3; 7:2; 10:3-4).

Kwa neno “ujasiri” anagalia maelezo katika 2 Kor. 3:4.

◙**"nahesabu. . . wanaodhania"** Huu ni mzaha juu ya neno la Kiyunani *logizomai*. Paulo hutumia KITENZI (KAULI YA KATI [shahidi wa maandishi] ELEKEZI YA WAKATI ULIOPO) kuelezea mawazo yeke na KAULI ENDELEVU (KAULI YA KATI YA WAKATI ULIOPO (shahidi wa maandishi) kuelezea walimu wa mafundisho ya uongo na mashtaka ya uongo. halingeweza kuwa neno la kitaalamu kutoka kwa wapotoshaji( angalia Bruce W. Winter, *Philo and Paul Among the Sophists*). Angalia maelezo kamili ya neno katika 2 Kor. 3:5.

◙**"tunaenenda"** Hii ni lahaja ya Kiebrania kwa tabia ya mtindo wa maisha (mf. Efe. 4:1,17; 5:2,1).

◙ **"kwa jinsi ya mwili"** Walimuhukumu Paulo katika nuru ya kanuni za jamii zao (kama vile 1 Kor. 9:8; 15:32; Rum. 3:5; Gal. 1:11; 3:5). Waaminio wanaviwango tofauti-walifunua neno la Mungu: (1) Agano la Kale; (2) Kristo; na (3) Agano Jipya. Angalia Mada Maalumu katika 1 Kor. 1:26.

**10:3-6** Paulo hutumia mfuatano wa sitiari za Kijeshi kuelezea mapambano ya kila siku baina ya Mkristo na udhaifu wa Kiroho (kama vile Rum. 7; 8:3-11). Udhaifu huu wa Kiroho umeelezewa katika 2 Kor. 10:5 kama mantiki ya binadamu, hekima, na kuhojiana dhidi ya injili (kama vile Efe.6:10-18).

**10:3 "katika mwili"** Angalia Mada Maalum katika 1 Kor. 1:26.

◙ **"vita"** Hili ni neno *strateuō*, ambapo tunapata mkakati wa neno la Kiingereza. Hili lilitumika kwa askari (kama vile 1 Kor. 9:7: 2 Tim. 2:4) au kisitiari kwa vita ya kiroho (kama vile hapa na 1 Tim. 1:18). Kuna mgogoro unaoendelea katika ufalme wa kiroho.

1. kuharibu ngome (*ochurōma*)
2. kuharibu fikra (*logizomai*)
3. kuharibu kila mawazo yajiinuayo (*huphōma*)
4. kuteka nyara za kila fikra (*noēma*)

Mambo haya, yawezekana yanarejea kwa werevu wa walimu wa mafundisho ya uongo wa kunena kwa njia ya kushawishi wasikilizaji ambao Paulo alikwisha washusha hadhi katika 1 Kor. 1-4 (kama vile Bruce W. Winter, *Philo and Paul Among the Sophists*, kr. 180-202).

**10:4"silaha za vita vyetu"** Paulo amekwisha kudokeza kwenye hii vita ya kiroho awali katika 2 Kor. 6:7.Kitabu cha warumi kiliandikwa kutoka Korintho kuhusu wakati ule ule.Yeye pia hutaja vita hii katika Rum. 6:13 na13:12. Petro hutumia mfano wa kitenzi hiki katika 1 Pet. 4:1, pale anapowatia moyo waaminio kujivika silaha katika kupambana kwao kimwili.

Chanzo kizuri cha kitabu katika eneo hili ni *Three Crucial Questions About Spiritual Warfare* by Clinton E. Arnold, kilichochapishwa na Baker.

◙**"hata kuangusha ngome"** Hili linaweza kuwa dokezo kwa Mit .21:22 (muktadha mkuu zaidi 2 Kor. 10:13-31). Kumekuwepo na majadiliano mengi kuhusu maana ya kifungu hiki cha maneno miongoni mwa watoa maoni, lakini ni hakika kwamba 2 Kor. 10:5 ni maelezo kuhusu zile ngome za Kiroho anazozirejelea Paulo. Hii inaonekana kuwa yeye anahutubia theolojia ya wale walimu wa mafundisho ya uongo.

**10:5**
**NASB "tukiangusha mawazo"**
**NKJV "kushusha chini mabishano"**
**NRSV "kuharibu mabishano"**
**TEV "shusha chini"**
**NJB "ni mawazo ambayo turiangusha"**

Angalia maelezo katika 2 Kor.3:5.

**NASB "na kila kitu kinachofikirika"**
**NKJV "na kila kitu kilicho juu"**
**NRSV "na kila kikwazo cha kiburi"**
**TEV "kila kiburi cha kikwazo"**
**NJB "na kila wazo lenye kiburi"**

Hili ni neno "urefu" lililotumika katika maana ya kujisifu, fikra za kibinadamu. Hii huaksi walimu wa mafundisho ya uongo kuzidisha msisitizo juu ya

1. maarifa na fikra za kibinadamu (kama vile 1 Kor. 1:18-25; Kol. 2:8)
2. ushikiriaji sana wa sheria (kama vile Kol. 2:16-23)

◙ **"na tukiteka nyara kila fikira ipate kumtii Kristo"** Hiki ni KITENZI amabatani cha neno "mkuki" na "kuteka mateka vitani." Hawa Wakorintho walikuwa wanateka fikra na mawazo ya Wakorintho waaminio. Paulo angekuwa nasi "kufanya upya fikra zetu" (kama vile Rum. 12:2; Efe. 4:23): linda fikra zetu (kama vile Flp. 4:7). Wokovu ni bure, lakini maisha ya ukristo yanajidhihirisha kwa utii, huduma, ibada na ustahimiivu. Haya ni majukumu ya kiagano. Kuna mgogoro wa kiroho unaoendelea!

Paulo hutumia neno “wazo” (*noēma*) mara nyingi katika 2 Wakorintho (kama vile 2 Kor. 2:11; 3:14; 4:4; 11:3), lakini mara moja tu kwa wakati mwingine, katika Flp. 4:7. Kusisitiza kulikozidi kwa Wakorintho juu ya maarifa yangeweza kuwa ndiyo sababu ya yeye kurudiarudia neno hilo. *The Analytical Greek Lexicon Revised*, Harold K. Moulton, ed., orodha ya vidokezo kadhaa (uk. 280).

1. fikra, uelewa, akili- 2 Kor. 3:14; 4:4
2. moyo, nafsi, mapenzi, hisia, tabiaa- 2 Kor.11:3
3. utungaji wa fikra, wazo, kusudi, hila- 2 Kor. 2:11; 10:5

**10:6** Paulo huwaonya walimu wa mafundisho ya uongo pamoja na wafuasi wao kwamba siku yao ya kiama inakuja. Walimtuhumu kwamba yeye yu dhaifu, lakini walielewa tu uvumilivu wake pamoja nao (1) kwa ajili ya Kristo na (2) kwa ajili ya afya ya ushirika wa kanisa hili. Paulo analionya kanisa hili lishughulikie matatizo yake kabla hajawasili ama sivyo atawashughulikia (kama vile 1 Kor 5:3-5).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 2 WAKORINTHO 10:7-11**

**[7]Yaangalieni yaliyo mbele ya macho yenu. Mtu akijitumainia mwenyewe ya kuwa ni mtu wa Kristo, na afikiri hivi pia nafsini mwake, ya kwamba kama yeye alivyo mtu wa Kristo, vivyo hivyo na sisi. [8] Maana, nijapojisifu zaidi kidogo kwa ajili ya mamlaka yetu, (tuliyopewa na Bwana, tupate kuwajenga wala si kuwaangusha), sitatahayarika; [9] nisije nikaonekana kana kwamba nataka kuwaogofya kwa nyaraka zangu. [10] Maana wasema, Nyaraka zake ni nzito, hodari; bali akiwapo mwenyewe mwilini ni dhaifu, na maneno yake si kitu. [11] Mtu kama huyo na afikiri hivi, ya kwamba jinsi tulivyo kwa maneno katika nyaraka tusipokuwapo, ndivyo tulivyo kwa matendo tukiwapo.**

**10:7 "Yaangalieni"** Katika Kiyunani muundo uliobadilishwa ungeweza kuwa KAULI SHURUTISHI (kama vile NRSV, NJB) au KAULI ELEKEZI (kama vile NASB, TEV, NIV). Toleo la NKJV na ASV yanaitafsiri kama swali.

Kanisa la Korintho lilikuwa linachanganua na kukosoa kwa kipimo cha kimwili/kiulimwengu/ngazi ya asili badala ya lengo la injili.

◙ **"ikiwa"** Hii ni SENTENSI YENYE MSHARTI DARAJA LA KWANZA. Kumekuwepo na baadhi katika kanisa la Korintho ambao walikuwa wamejidanganya wenyewe (kama vile 1 Kor. 14:37) kama kwenye hali na msimamo wao wa kiroho (yaani, “yu jasiri,” KAULI TENDAJI ELEKEZI YA WAKATI ULIOPO).

◙ **"mwenyewe"**Paulo hutumia neno hili, *eautou*, mara mbili kwenye mstari huu. Hawa walimu wa mafundisho ya uongo walikuwa wamejidanganya wenyewe. Hii ndio hali ya kiroho iliyo ngumu zaidi kuliko zote kufikiria ama kuathiri.

◙**"ya kwamba kama yeye alivyo mtu wa Kristo, vivyo hivyo na sisi"** Walimu wa mafundisho ya uongo walikuwa wanadai mamlaka yao ya kiroho na msimamo, lakini walikuwa wanayakana mamlaka ya Paulo.

**10:8 "ikiwa"** Hiii ni SENTENSI YENYE MASHARTI DARAJA LA TATU, ambayo huonyesha kuwezekana kwa kitendo (kama vile 2 Kor. 11:1-12:13).

◙ **"nijapojisifu"** Neno hili (yaani, *kauchaomai* na miundo yake mingine) limetumika mara nyingi katika barua za Paulo.

1. *kauchaomai* (utukufu, kujisifu, kama vile 1 Kor.r. 1:29,31; 3:21; 4:7; 13:3; 2 Kor. 5:12; 7:14; 9:2; 10:8,13,15,16,17; 11:12,16,18,30; 12:1,5,6,9)
2. *kauchēma* (kma vile 1 Kor. 5:6; 9:15,16; 2 Kor. 1:14; 5:12; 9:3)
3. *kauchēsis* (kama vile 1 Kor. 15:31; 2 Kor. 1:12; 7:4,14; 8:24; 11:10,17)

Angalia maelezo kamili juu ya matumizi ya neno hilo katika 2 Kor. 1:12 na Mada Maalum katika 1 Kor. 5:6.

◙**"kwa ajili ya mamlaka yetu, tuliyopewa na Bwana"** Hii hurejea kwa uzoefu wa Paulo akiwa njiani kuelekea Dameski (kama vile Mdo. 9:15,16; Rum. 1:5; Gal. 2:9).

◙**"tupate kuwajenga wala si kuwaangusha"** Paulo anarudia kifungu hiki cha neno katika 2 Kor. 13:10. Hili linafanana na wito wa Isaya (kama vile Isaya 6) na Yeremia (kama vile Yeremia 1), isipokuwa waliitwa kufanya yote! Paulo hutumia KITENZI kile kile (yaani, *kathairesis*), ambacho alitumia katika 2 Kor. 10:4 (mara mbili) kwa kuangusha ngome za fikra za kibinadamu. Paulo ameitwa kuangusha baadhi ya vitu na mawazo, lakini sio kanisa lenyewe. Yeye ameitwa kulitetea na kulilinda kanisa (kana vile 2 Kor. 10:9). Angalia MADA MAALUM: ADILISHA (SPECIAL TOPIC: EDIFY) katika 1 Kor. 8:1.

◙**"sitatahayarika"** Paulo anakwenda kujitete kwa sababu walimu wa mafundisho ya uongo walikwisha kufanya kuwa hoja. Yeye hujitetea kwa kutetea (1) mamalaka aliyokwisha kupewa na (2) injili aliyohubiri.

Hii inaweza kuaksi ahadi za Mungu za Angano la Kale (kama vile Rum. 9:33 na 10:11, Ikinukuu Isa. 28:16), ambapo wale wanaomtumaini Mungu hawatatahayarika au kufadhaishwa. Paulo alitambua katika Yule anayemuamini!

Hata kama Paulo angalikuwa amejisifu kupita kiasi (kama vile NRSV, TEV) katika wito na uteuzi wake, bado alikuwa kweli na Mungu angemtete yeye! Wale wanaokataa mamlaka ya Paulo wamelaaniwa (kama vile 1 Kor. 14:37-38).

**10:9** Barua za Paulo zilikusudiwa kuhamasisha toba yao, si kuleta lawama (kama vile 2 Kor. 7:5-13a).Lakini kwa walimu wa mafundisho ya uongo hiki kilikuwa kisa kipya (kama vile 2 Kor. 10:8, 11; 13:10).

**10:10 "Maana wasema"** "Wasema" hufuata MSS B, toleo la Biblia la Kilatini, na tolea la Biblia la ki-Shamu (tafsiri ya ki-shamu ya karne ya tano). Machapisho mengine mengi ya Kiyunani yana "yeye," ambayo ingeweza kurejelea kwa kiongozi wa kikundi cha walimu wa mafundisho ya uongo (kama vile 2 Kor. 10:7, 11: 11:4).

◙**"akiwapo mwenyewe mwilini ni dhaifu"** Maelezo ya maumbile ya Paulo ya mapokeo ya karne ya pili yanatoka Thesalonike kwenye sehemu ya kitabu kiitwacho *Paul and Thekla*. Kinasema kwamba alikuwa mfupi mwenye upaa, mwenye matege, alikuwa na nyusi nyingi sana na macho makubwa yaliyotokeza. Paulo hakuwa mtu aliyekuwa anavutia ki-maumbile (kama vile Gal. 4;14). Baadhi ya sifa hizi za kimwili zaweza kuwa na uhusiano na mwiba katika mwili wake (kama vile 2 Kor. 12:7), ambavyo nadhani yalikuwa matatizo ya macho, labda kuhusiana na kupofuka kwake akiwa "njiani kuelekea Dameski."

Yawezekana kwamba kifungu hiki cha maneno, kama kinachofata, hurejelea kwa ujuzi wa Paulo wa kunena hadharani, ambao ulikuwa kipengele kikubwa cha upinzani (kama vilke 1 Kor. 1:17). Kifungu hiki cha neno mara nyingi kilitumika kwa "uwepo wa kipindi" (kama vile Bruce W. Winter, *After Paul Left Corinth*, uk. 35).

◙**"na maneno yake si kitu"** Hii ni KAULI TENDEWA ENDELEVU YA WAKATI TIMILIFU. Hili ni neno lenye nguvu la Kiyunani kama vile 1 Kor. 1:28; 6:11; Rum. 14:3, 10). Paulo hakuwa mzungumzaji wa hadharani aliyepata mafunzo ya kuzungumza (yaani, mtindo wa Kiyunani wa elimu ya usemaji, kama vile 1 Kor. 1:17; 2 Kor. 11:6). Apollo alikuwa jasiri wa kunena, mhubiri aliyepata elimu ya usemaji kutoka Isakandria. Hata hivyo, Paulo anadai kwamba ingawa hana ufundi katika mtindo wa elimu ya usemaji (kama vile 2 Kor. 11:6), ujumbe na mamlaka yake vimetoka kwa Kristo.

**10:11** Walimu wa mafundisho ya uongo wamekwisha kumtuhumu Paulo kwa kuwa na barua nzito, lakini mwonekano wake wa kimaumbile ni dhaifu. Paulo anathibitisha kwamba nguvu ambayo walithibitisha katika barua zake ingelinganishwa na nguvu ya uwepo wake binafsi kama angekuwa amekuja binafsi kuyanyoosha mambo mwenyewe!

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 2 WAKORINTHO 10:12-18**
**[12]Kwa kuwa hatuthubutu kujihesabu pamoja na baadhi yao wanaojisifu wenyewe, wala kujilinganisha nao; bali wao wenyewe wakijipima nafsi zao na nafsi zao, na wakijilinganisha nafsi zao na nafsi zao, hawana akili.**
**[13]Lakini sisi hatutajisifu zaidi ya kadiri yetu; bali kwa kadiri ya kipimo tulichopimiwa na Mungu, yaani, kadiri ya kufika hata kwenu.**
**[14]Maana hatujitanui nafsi zetu kupita kadiri yetu, kana kwamba hatuwafikii ninyi; kwa sababu tulitangulia kufika mpaka kwenu katika injili ya Kristo;**
**[15]wala hatujisifu zaidi ya kadiri yetu, yaani, katika taabu za watu wengine; bali tukiwa na tumaini ya kwamba, imani yenu ikuapo, tutakuzwa kwenu kwa kadiri ya kipimo chetu, na kupata ziada;**
**[16]hata kuihubiri Injili katika nchi zilizo mbele kupita nchi zenu; tusijisifu katika kipimo cha mtu mwingine kwa mambo yaliyokwisha kutengenezwa.**
**[17]LAKINI, YEYE AJISIFUYE, NA AJISIFU KATIKA BWANA.**
**[18]Maana mtu mwenye kukubaliwa si yeye ajisifuye, bali yeye asifiwaye na Bwana.**

**10:12"bali wao wenyewe wakijipima nafsi zao na nafsi zao, na wakijilinganisha nafsi zao na nafsi zao"** Paulo amekwisha dokeza sifa za kibinadamu katika 2 Kor. 3:1 (kama vile 2 Kor. 10:18); sasa analiongeza hadi kwenye ulinganisho wa kibinadamu. Yaonekana dhahiri kwamba hawa walimu wa mafundisho ya uongo walikuwa wanajilinganisha wenyewe kwa Paulo kwa njia ambayo walipandisha nafasi yao na kuidhihilisha nafasi yake.

Paulo alijua kutokana na mafunzo yake ya Agano la Kale (kama vile 1 Sam. 16:7; Mit. 21:2) jinsi gani hili lilivyokuwa halina matunda. Huenda pia alikuwa na ufahamu wa mafundisho ya Yesu kuhusu watu wanaojihesabia haki wenyewe (kama vile Luka 10:29; 16:15: 18:9, 14).

Kuna maneno machache ya kejeli katika aya hii kama ilivyo katika 2 Kor. 10:1. Paulo alitumia mtindo huu wa fasihi mara nyingi katika 1 Wakorintho.

Kuna zihaka dhahiri kati ya kauli mbli KAULI TENDAJI ISIYO NA UKOMO YA WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFU.

1. *egkrinai* (*en* na *krinō*), zinahukumu kama tunatoka kwenye kundi moja
2. *sugkrinai* (*sun* na *krinō*),zinahukumu kwa kulinganisha

Katika kitabu cha miswada ya kale cha Bezae (maandishi ya herufi kubwa ya MS ya karne ya tano) kuna kifungu cha nane kimeachwa katika mwisho wa 2 Kor. 10:12 na mwanzoni mwa 2 Kor. 10:13. Yaonekana kwamba jicho la mwandishi lilitembea kutoka "*ou*" ya 2 Kor.10:12 kwenda "*ouk*" ya 2 Kor. 10:13 na liliacha maneno yaliyoingilia kati (“haelewei, lakini hatutajua”). Angalia kiambatanisho cha pili juu ya Uhakiki wa Maandishi. Toleo la UBS[4] hutoa nyongeza ya daraja "B" kwenye kifungu cha neno (karibu na hakika).

◙**"hawana akili”**Hii ilikuwa kauli inayoshtua hasa.
1. kwa Wanafalsafa wa Kiyunani ingeshusha dai lao kwa elimu ya kiroho ya hali ya juu
2. kwa Waebrania wenye akili nyingi ingekuwa ni dokezo kwa wanyama.

**10:13** Paulo anadokeza wito wake wa ki-Ungu na mamlaka yake (yaani, uzoefu wake “ njiani kuelekea Dameski” , kama vile Mdo. 9; 22:3-16; 26:9-18) kuwa Mtume wa Mataifa. Yeye alikuwa halinganishi au kuamuru, lakini kutamka wito wa Mungu. Wito wa Mungu kwake kama mwakilishi maalum kwa Mataifa hata alijumuisha kanisa la Korintho (kama vile 2 Kor. 10:14-15).

◙ **"kipimo tulichopimiwa na Mungu"** *The NASB Study Bible* (uk. 1701) ina maoni mazuri kuhusu kifungu hiki cha maneno.

**"10:13** *kipimo tulichopimiwa na Mungu.* Taswira ambayo Paulo anayo kwenye fikra yaweza kuwa ya mashindano ya mbio ambayo mistari ya ndani imechomwa kwa ajili ya wakimbiaji mabilmbali. Katika swala hili “kipimo” kinapaswa kipewe “mistari ya ndani” (pia katika 2 Kor. 10:15-16). Kwa kujipenyeza mwenyewe ndani ya Korintho,

hawa mitume wa uongo walikwisha kuvuka na kuingia kwenye uchochezi wa Paulo ambao Mungu alikwisha uwekea alama na kwamba zilizokuwa zimemleta kwa Wakorintho kama mtume wao stahiki. Yeye hana nia ya kuwania Himaya iliyowekewa alama kwa ajili ya wengine na kudai kazi yao kana kwamba ni yake yeye, kama hawa walimu wa mafundisho ya uongo walivyokuwa wanafanya. Wengine wanalielewa neno la Kiyunani lililo kwenye swali kwamba linarejelea kwenye kipimo kilichopangiwa cha mamlaka."

**10:14"Maana hatujitanui nafsi zetu kupita kadiri yetu"** Hili ni neno lingine ambatani *"huper*", na *huperekteinō*. Angalia Mada Maalum: Matumizi ya Paulo ya Vimabatani vya neno *Huper* katika 1 Kor.2:1.

◙**"kwa sababu tulitangulia kufika mpaka kwenu katika injili ya Kristo"** Paulo alikuwa mwanzilishi wa kanisa la Korintho, bali walimu wa mafundisho ya uongo walikuwa wanajaribu kutwaa sifa (kama vile 2 Kor. 10:18b).

**10:15 "wala hatujisifu zaidi ya kadiri yetu, yaani…katika taabu za watu wengine"** Walimu wa Mafundisho ya uongo wanatwaa sifa kwa ajili ya kanisa la Korintho, ambalo Paulo alilianzisha.

**10:16"hata kuihubiri Injili katika nchi zilizo mbele kupita nchi zenu"** Hii yaonekana kurejelea kwa shauku la Paulo kwenda Roma na/au Hispania (kama vile Mdo. 19:21; Rum. 15:22 na kuendelea). Yeye alitaka makanisa yaliyoanzishwa kumsaidia yeye pamoja na changizo kwa ajili ya Yerusalemu na kumwezesha kusafiri hadi Magharibi ya Mediterrania kwa ajili ya kuanzisha makanisa mengine.

Kwa neno "mbele," hili ni neno lingine ambatani la neno "*huper*" (*huperekeinē*), anagalia Mada Maalum: Matumizi ya Paulo ya viambatani vya neno *Huper* katika 1 Kor. 2:1.

**10:17"YEYE AJISIFUYE, NA AJISIFU KATIKA BWANA"** Hii ni nukuu kutoka Tafsiri ya agano la kale kwa Kiyunani ya Yer. 9:23-24. Imenukuliwa pia katika 1 Kor. 1;3. Kujisifu kote kwa binadamu ni ujinga. Angalia Mada Maalum: Kujisifu katika 2 Kor.1:12.

**10:18** Swali halisi ni kikundi kipi, mwalimu yupi, ama thiolojia ipi ambayo Yesu anathibitisha (kama vile 1 Kor. 4:1-5).

## MASWALI YA MJADALA

Haya ni maoni ya <u>mwongozo</u> kwa kujisomea, ikiwa na maana kuwa unawajibika binafsi kwa tafsiri ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mtoa maoni tu.

Maswali haya ya kujadili yanatolewa ili kukusaidia kufikiri mambo muhimu yaliyoko katika kipengele cha kitabu hiki. Yanamaanisha kuwa maswali ya kichokonozi, yasio ya hakika.

1. Eleza utengano ulio dhahiri kati ya sura ya 9 na 10.
2. Je! ni zipi zilikuwa baadhi ya tuhuma za walimu wa mafundisho ya uongo dhidi ya Paulo?
3. Je! Kwa nini Paulo anatumia maneno ya kijeshi kuelezea mapambano yake dhidi ya walimu wa mafundisho ya uongo?
4. Je! Hawa walimu wa mafundisho ya uomgo walikuwa Wakristo waaminifu ambao walikuwa wamekosea katika mambo madogo ya Kitheolojia ama walikuwa viongozi wa imani potofu waliokuwa wanajaribu kuwapotosha watu kutoka kwenye kweli ya injili?

# 2 WAKORINTHO 11

| MGAWANYO WA AYA WA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **UBS[4]** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB** |
| Paulo na Mitume Wa Uongo | Kuhusika na Uaminifu Wao | Jibu la Paulo kwa Wapinzani Wake | Paulo na Mitume wa Uongo | Paulo alazimishwa kutamka Sifa zake Mwenyewe |
| 11:1-6 | 11:1-4 | 11:1-6 | 11:1-4 | 11:1-6 |
| | Paulo na Mitume wa Uongo | | | |
| | 11:5-15 | | 11:5-6 | |
| 11:7-11 | | 11:7-11 | 11:7-11 | 11:7-15 |
| 11:12-15 | | 11:12-15 | 11:12-15 | |
| Mateso ya Paulo Kama Mtume | Asiyetaka kujisifu | | Mateso ya Paulo kama Mtume | |
| 11:16 -19 | 11:16-21 | 11:16-21a | 11:16-21a | 11:16-21a |
| | Kuteseka Kwa ajili ya Kristo | | | |
| | | 11:21b -29 | 11:21b -29 | 11:21b -29 |
| | 11:22-33 | | | |
| 11:30-33 | | 11:30-33 | 11:30-33 | 11:30-33 |

**MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI** (kutoka "**Mwongozo Mzuri wa Usomaji wa Biblia" ("A Guide to Good Bible Reading")**

## *KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI ZA AYA*

Huu ni mwongozo wa usomaji wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako binafsi ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika nuru tuliyonayo. Wewe, Biblia na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hupaswi kumwachia kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo. Linganisha mgawanyo wa masomo yako na tafsiri tano hapo juu. Kugawanya katika aya hakuna uvuvio, isipokuwa ni ufunguo wa kufuatilia kusudio la asili la mwandishi ambalo ndilo kiini cha ukalimani. Kila aya ina somo moja na ni moja tu.

1. Aya ya kwanza
44. Aya ya pili
45. Aya tatu
46. N.k

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA

A. 2 Wakorintho 10-13 huunda kitengo cha fasihi. Katika sehemu hii ambayo ni tofauti sana na sura zilizopita katika 2 Wakorintho, Paulo anajitetea dhidi ya mashambulizi ya walimu wa uongo. Walimfanya Paulo mwenyewe kuwa kitu cha dhihaka katika kujaribu kwao kuaibisha injili yake.

B. Paulo anajibu mashitaka ya wapinzani wake katika sura ya 2 Kor. 11:4,8,12-15,18-20.

C. Paulo hutumia kejeli na kupinga vijembe kuendesha kumbukumbu ya Wakristo wa Korintho kuhusu huduma yake (kama vile 2 Kor. 11:5, 7, 19, 20, 21).

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 2 WAKORINTHO 11:1-6**
**1 Laiti mngechukuliana nami katika upumbavu wangu kidogo! Naam, mchukuliane nami. 2 Maana nawaonea**
**wivu, wivu wa Mungu; kwa kuwa naliwaposea mume mmoja, ili nimletee Kristo bikira safi. 3 Lakini nachelea;**
**kama yule nyoka alivyomdanganya Hawa kwa hila yake, asije akawaharibu fikira zenu, mkauacha unyofu na**
**usafi kwa Kristo. 4 Maana yeye ajaye akihubiri Yesu mwingine ambaye sisi hatukumhubiri, au mkipokea roho**
**nyingine msiyoipokea, au injili nyingine msiyoikubali, mnatenda vema kuvumiliana naye! 5 Maana nadhani ya**
**kuwa mimi sikupungukiwa na kitu walicho nacho mitume walio wakuu. 6 Lakini nijapokuwa mimi ni mtu**
**asiyejua kunena, hii si hali yangu katika elimu; ila katika kila neno tumedhihirishwa kwenu.**

**11:1 "Naam, mchukuliane nami"** Hii ni KAULI YA KATI ELEKEZI YA WAKATI USIOTIMILIFU. SAUTI IRABU YA KATI inakwenda sambamba na utambulisho binafsi wenye mkazo wa sura ya 10. Njeo ya <u>wakati ulio timilifu</u> yaweza kumaanisha (1) kitendo kinachorudia katika wakati uliopita au (2) mwanzo wa kitendo. Namba mbili inafaa zaidi kwenye muktadha huu. Angalia Maelezo kamili kuhusu "chukuliana" katika 2 Kor. 11:4.

◙ **"katika upumbavu wangu kidogo"** Paulo hapo awali alisema kwamba kulinganisha kimwili ni ujinga, lakini walimu wa uongo walikwisha kumtumia kama kitu cha dhihaka. Kwa hiyo, anatumia mtindo wa usemaji wa wale wapotoshaji (yaani, kujisifu) dhidi yao (yaani, mwigo wa kubeza). Ilimbidi ajitetee mbele ya kanisa hili kwa manufaa yao. Alijisikia mjinga kwa kulazimisha kufanya hili kama mistari ya 17 na 21 inavyothibitisha.

◙ **"Laiti mngechukuliana nami"** Mstari huu ama ni KAULI YA KATI ELEKEZI YA WAKATI ULIOPO (NASB, NKJV,NJB) au KAULI YA KATI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO (NRSV, TEV). Kuna sababu tatu zilizotajwa katika 2 Kor. 11:2, 4, 5 kwa mimi lazima wasikilize. Kila moja ya sababu hizi inatambulisha neno la Kiingereza "kwa" (*gar*).

**11:2 "kwa kuwa naliwaposea mume mmoja"** Paulo kama mwanzilishi wa kanisa hili anasimama kama mzazi kuwaposa kwa Kristo (kama vile Efe. 5:22-33; Ufu. 19:9; 21:2,9; 22:17). Wazo la Agano la Kale la Mungu kama mume linapatikana katika Isa. 54:5; 62:5; na Hosea 1-3; 11:1-4.

◙ **"ili nimletee Kristo bikira safi"** Hii ni istilahi ya Agano la Kale kwa ajili ya sherehe ya ndoa. Paulo anarudia dhamira hiyo hiyo katika Efe.5:25-27. Paulo anawakemea Wakristo wa Korintho hata kwa wale walimu wa uongo waliokuwa wanazungukazunguka. Katika busara wale waliowatetea walikwisha kuwa wasio waaminifu kiroho (yaani, uzinzi wa kiroho wa Agano la Kale).

**11:3 "kama yule nyoka alivyomdanganya Hawa kwa hila yake"** Hii inarejea maelezo ya lile jaribu linalopatikana katika Mwanzo 3 (kama vile 1 Tim. 2:14). Kumbuka nyoka alimwondoa Hawa kwa YHWH kidogo kidogo kwa kumfanya kuwa na madai binafsi ya kuwa huru!

Neno alidanganya (*exapataō*) linatumiwa na Paulo pekee katika Agano Jipya (kama vile Rum. 7:11; 16:18; 1 Kor. 3:18; 2 Kor. 11:3; 2 The. 2:3; 1 Tim. 2:14). Mtindo usioongezwa, *apataō*, ulitumiwa na tafsiri ya agano la kale kwa Kiyunani katika Mwa.3:13 kuhusu Hawa. Paulo anautumia katika Efe.5:6 na 1 Tim. 2:14 (mara mbili). Udanganyifu huja kutoka ndani na nje. Waaminio lazima wakati wote wawe macho.

Neno Nyanja (*panourgia*) ni ambatani kutoka neno"ote" (*pan*) na "kazi" (*ergon*). Paulo amelitumia hili mara mbili hapo awali katika barua zake kwa Wakorintho (kama vile 1 Kor. 3:19; 2 Kor. 4:2). Paulo aliielewa vita ya kiroho ambayo waaminio walikabiriwa nayo (kama vile Efe. 4:14). Anaeleza matokeo ya uovu kwa mwanadamu waziwazi katika Warumi 1-3 na juu ya waamino katika Warumi 7; Efe. 6:10-19. Thiolojia ya Paulo inaanza na uasi wa malaika na mwanadamu.

Angalia MADA MAALUM: MIPANGO ( SPECIAL TOPIC: SCHEMES) katika 2 Kor. 2:11.

◙ **"asije akawaharibu fikira zenu"** KITENZI *phtheirō* ni KAULI TENDEWA TEGEMEZI YA WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFU. Katika dokezo zaidi la Mwanzo 3 Paulo alitumia neno hili kwa "angamiza" au "haribu" katika dhana ya uadilifu mara kadhaa (kama vile 2 Kor. 7:2; 11:3; 1 Kor. 3:17; 15:33; Efe. 4:22). Angalia Mada Maalum katika 1 Kor. 15:42. Waaminio waweza kudanganywa, kumilikiwa, kwa werevu au hila na kushindwa na uovu!

◙ **"mkauacha unyofu"** Angalia maelezo katika 2 Kor. 1:12.

◙ **"na usafi"** Kuna machapisho tofauti ya Kiyunani ambayo huongeza neno"na usafi." Hupatikana katika MSS P[46], א[*], B, na G (kama vile NASB, NRSV, TEV, NIV). Halipo katika MSS א[c], D[c], H, K, na P (kama vile NKJV, NJB, REB). Toleo la MS D[*] pia lina usomaji mrefu, japo maneno yapo katika utaratibu wa kinyume. Wasomi wa maandiko wamegawanyika kwenye asili ya maneno yenyewe. Kujumuishwa kwa neno“usafi” huchukuliwa kutoka 2 Kor. 11:2 na baadhi yamejumuishwa vizuri na kijiografia ni tofauti na machapisho ya kale.

**NASB"ya moyo wa ibada kwa Kristo"**
**NKJV "iliyo ndani ya Kristo"**
**NRSV, TEV,**
**NJB, NIV "Moyo wa ibada kwa Kristo"**

KIHUSISHI CHENYE UHUSIKA WA KUONDOA, *apo*, Huanzisha VISHAMIRISHO vitatu.

1. Kutoka unyofu
2. Kutoka utakatifu
3. Kutoka "kwa Kristo"

Ni kitu gani cha kutafakari katika 2 Kor. 11:3? Tafsiri kadhaa za kiingereza hutoa neno"moyo wa ibada," lakini ingeweza kurejerea "kwa Kristo," ambayo ni kifungu cha maneno maarufu ya Paulo ya imani binafsi katika Kristo.

**11:4 "Maana yeye ajaye"** Hii ni SENTENSI YENYE MASHARTI DARAJA LA KWANZA, ambayo ilidhaniwa kuwa ya kweli kwa mtazamo wa mwandishi ama kwa kusudi lake la kifasihi. Neno "Mtu" linaonekana kurejelea kwa Yule mkuu wa walimu wa uongo aliyedokezwa katika 2 Kor. 10:7,10.

◙ **"Yesu mwingine ambaye sisi hatukumhubiri"** Hawa walimu wa uongo hawakuwa wanapinga kuhusu swala dogo la pembezoni, bali kuhusu mtu na kazi ya Yesu Kristo (kama vile 1 Kor. 3:11). Ni dhahiri katika kuweka ushahidi wote pamoja na kwamba hawa waalimu wa uongo walikuwa mchanganyiko wa Wayahudi waliolazimisha desturi za Kiyahudi kama ilivyo katika kitabu cha Wagalatia na fikra za Kiyunani (yaani, *Wapotoshaji*). Hawa manaibu kutoka Yerusalemu walileta mkazo wa kutahiriwa, yumkini kwa sababu ya matokeo ya baraza la Yerusalemu katika Matendo 15, lakini waliendelea na sheria zao za Kiyahudi kwa namna fulani zilizounganishwa pamoja au kusafishwa na fikra za (yaani, wapotoshaji) Uyunani.

Yawezekana kwamba Paulo anatumia mashitaka ya walimu wa uongo dhidi yake. Wangeweza kumshtaki kwa "kuhubiri injili nyingine."

Wale miongoni mwetu ambao wanaamini kwamba Biblia ni neno la Mungu lililovuviwa tunayo maswali kadhaa ya kujibu.

1. Je, tunasoma Agano Jipya kupitia nuru ya Agano la Kale au Je Agano Jipya lina tafsiri zinazoshinda nyingine?
2. Je! Maneno ya Paulo (au mwandishi yeyote wa Agano Jipya) yamevuviwa kama maneno ya Yesu?
3. Je! Uwepo wa baadhi ya hali ya tofauti miongoni mwa wandishi wa Agano Jipya unaruhusu wafasiri wa kisasa kupata nafasi ya kuchezesha chezesha maswala fulani fulani? Je! Tunaruhusu jambo hili hili miongoni mwa wafasiri wa awali wa kanisa (yaani, makasisi, wa Kiyunani na Kilatini; viongozi wa badaye wa kanisa [Augustine, Aquinas, Luther, Calvin, nk.])? Ama kwa kuliweka kwa njia nyingine, jinsi gani mtu anaelewa (fafanua, weka mipaka) imani halisi inayokubalika?

◙ **"au mkipokea roho nyingine msiyoipokea"** Wengine huliona hili kama rejeo kwa Roho mtakatifu (kama vile Gal. 4:6; TEV), lakini yaonekana afadhari kuhusisha hili aidha kwa (1) "roho ya uwoga na utumwa" (kama vile Rum. 8:15; 2 Tim. 1:7) au (2) "roho ya amani na furaha" (kama vile Rum. 14:17). Kwa maelezo kamili zaidi kuhusu "Roho" angalia 1 Kor. 2:11.

Neno "tofauti" ni *heteros*, ambalo linamaanisha kingine cha namna ya tofauti. Paulo anaonyesha tofauti inayoshtua pale ujumbe wa walimu wa uongo na ujumbe wake vinapolinganishwa (kama vile Gal. 1:6). Kuna kufanana kwingi kati ya matatizo yaliyotajwa hapa katika Gal.1:6-9.

◙ **"mkipokea. . . msiyoikubali"** Vitenzi vya Kiyunani *lambanō* na *dechomai* ni vyenye maana sawa. Maana zote za msingi ni kung’ang’ania kitu fulani. Maelezo mawili katika Louw na Nida's *Greek-English Lexicon*, juzuu. 1, ni yenye msaada.

1. "Kupokea ama kukubali kitu ama manufaa ambayo kwayo moyo wa kujituma huwa ndani ya mtoaji, lakini kusudi la usikivu katika uhamisho ni juu ya mpokeaji" (uk. 572).
2. Tanbihi 31, "yaweza kuwepo na tofauti katika maana kati ya *dechomai* na *lambanō* pamoja na mwisho kumaanisha kushiriki utendaji zaidi kwa upande wa yule anayepokea kipawa, lakini hili haliwezi kutambulika kutokana na mazingira yaliyopo" (uk. 572).

Kwangu mimi kama Mkristo wa ki-injili, maneno haya ni muhimu sana katika mwitikio halali kwa injili (kama vile Yohana 1:12). Ahadi za Mungu, kazi za Kristo, na ushawishi wa roho lazima vipokee mwitikio pale mwanzoni na kuendelea. Hili linaunda msingi wa dhana ya kiagano (yaani, Mungu huanzisha, lakini mwanadamu lazima aitikie).

*Lambanō* linarudiwa rudiwa katika muktadha huu (kama vile 2 Kor. 11:4,8,20,24; 12:16).

NASB **"mnachukuliana naye vizuri tu"**
**NKJV "mnaweza tu kukubaliana nalo"**
**NRSV "mnajitia chini yake kwa utayari kiasi cha kutosha"**
**TEV "mnavumilia kwa furaha"**
**NJB "mnachukuliana nalo kwa utayari kupindukia"**

Hii aidha ni KAULI YA KATI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO na KAULI YA KATI ELEKEZI YA WAKATI ULIOPO. Hii ni kejeli inayoumiza iliyoelekezwa kwenye utayari wa Wakristo wa Korintho kwa kuwasikiliza walimu wa uongo.
Paulo hutumia neno hili, *anechomai*, mara kadhaa katika sura hii (kama vile 2 Kor. 11:1,4,10,20). Katika 2 Kor. 11:1 limetumika katika dhana ya "ustahimilivu" (kama vile 1 Kor. 4:12), lakini katika 2 Kor. 11:4,19,20 limetumika kikejeli kwa maana ya "vumilia."

**11:5 "Maana nadhani"** Katika kitengo hiki cha fasihi Paulo hutumia KITENZI, *logizomai*, mara nyingi (kama vile 2 Kor. 10:2,7,11; 11:5; 12:6). Yawezekana lilikuwa neno la kumtega mtu ama neno lililo tumika mara kwa mara na walimu wa uongo walio wapotoshaji.

◙ **"sikupungukiwa na kitu"** KITENZI katika kifungu hiki cha maneno ni KAULI TIMILIFU TENDAJI ISIYO NA UKOMO. Hakuna wakati wowote, uliopita ama wakati uliopo, ambapo Paulo alikwisha kujidhania kuwa mnyonge kuliko wawakilishi wenye mamlaka kutoka Yerusalem (kama vile 2 Kor. 12:11). Mtazamo huu pia umejadiliwa katika Gal. 1:11-2:14, ambapo pia Paulo anatetea utume wake.

**NASB, NKJV "kwa mitume walio maarufu"**
**NRSV "kw hawa mitume wa hali ya juu sana"**
**TEV "kwa hawa waitwao mitume wenu maalum sana"**
**NJB "kwa mitume wa hali ya juu sana"**

Maelezo ya kejeli ni mchanganyiko wa maneno mawili ya Kiyunani, *huper* (yaani, juu na kupitiliza) na *lian* (yaani, kuu ama yakuzidi sana). Kifungu hiki cha maneno kinachojieleza ni adimu na Paulo analitumia hapa tu na katika 2 Kor. 12:11. Mstari wa 5 umeunganishwa kimuktadha na kisarufi na 2 Kor. 11:4, ambayo dhahiri inahusu walimu wa uongo (kama vile 2 Kor. 11:13-15). Paulo anatumia neno "mitume" kwa kejeli katika dhana mbili: (1) wale kumi na wawili (2) wajumbe waliotumwa kutoka makanisani (kama vile 2 Kor. 11:13). Yaonekana hawa walimu wa uongo walikuwa na uhusiano na kanisa la Yerusalem (kama vile 2 Kor. 11:22 inavyoonyesha kwamba walidai kuwa na msingi wa Kiyahudi na ; 12:1 inavyoonyesha uzoefu wa vipawa kutoka kwa Mungu).

◙ **"walio wakuu"** (*huperlian)* Angalia Mada maalum: Matumizi ya Paulo ya viambatani vya neno *Huper* katika 1 Kor.2:1.

**11:6 "Lakini nijapokuwa"** Hii ni SENTENSI YENYE MASHARTI DARAJA LA KWANZA. Paulo alikiri kwao kwamba ujuzi wa kunena wa Kiyunani haukuwa uwezo wake. Uwezo wake ulikuwa ni maudhui yaliyovuviwa ya ujumbe wake.

◙ **"Lakini nijapokuwa mimi ni mtu asiyejua kunena"** Neno hili linatumika katika dhana ya "asiyefunzwa" au "sio stadi" (kama vile Matendo 4:13, ambapo lilitumiwa kwa Petro na Yohana au 1 Wakorintho 14, ambapo limetumika kwa wale ambao hawajafundishwa kuhusu karama za rohoni). Yaonekana kuhusiana na ukiri wa Paulo kwamba hakuwa stadi katika kuvuta wasikilizaji kwa kutumia maneno (kama vile 2 Kor. 10:10; 1 Kor. 1:17).

Maoni haya, yaonekana kutoka kwa walimu wa mafundisho ya uongo, huonyesha kwamba walitukuza uzungumzaji wa ufasaha. Hii humaanisha msingi (yaani, wapotoshaji) wa Uyunani. Angalia Bruce W. Winter, *Philo and Paul Among the Sophists*.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 2 WAKORINTHO 11: 7-11**

**7 Je! Nalifanya dhambi kwa kunyenyekea ili ninyi mtukuzwe, kwa sababu naliwahubiri Injili ya Mungu bila ujira? 8 Naliwanyang'anya makanisa mengine mali yao, nikitwaa posho langu ili niwahudumie ninyi. 9 Nami nilipokuwa pamoja nanyi na kuhitaji sikumlemea mtu. Maana hao ndugu waliokuja kutoka Makedonia walinipa kadiri ya mahitaji yangu; nami katika mambo yote najilinda nafsi yangu nisiwalemee hata kidogo; tena najilinda. 10 Kama vile ile kweli ya Kristo ilivyo ndani yangu, hakuna mtu atakayenifumba kinywa katika kujisifu huku, katika mipaka ya Akaya. 11 Kwa nini? Je! Ni kwa sababu siwapendi ninyi? Mungu anajua.**

**11:7 "Je! Nalifanya dhambi kwa kunyenyekea ili ninyi mtukuzwe"** Mstari wa 7 ni swali linalotarajia jibu la "hapana". Huu ni mfano mwingine wa kejeli za Paulo zihusianazo na ubishi wa muda mrefu wa yeye kutokubali malipo ya kifedha kutoka katika kanisa la Wakorintho (kama vile 1 Kor. 9:3-18).

Neno "dhambi" (*hamartia*) latumika kwenye dhana isiyo ya uadilifu ya neno"nilifanya kosa" au "nilifikilia vibaya." Kumbuka muktadha, muktadha, muktadha – unabainisha maana ya neno. Kuwa mwangarifu kuhusu ufafanuzi wa kithiolojia wa maneno ya kusisitiza yanayosomwa kila mara yatokeapo!

◙ **"Injili ya Mungu"** Tazama injili ya Kristo (kama vile 2 Kor. 2:12; 9:13; 10:14) na pia ni injili ya Mungu!

**11:8 "naliwanyang'anya makanisa"** Wayunani na warumi walizoea kuwa wanawalipa walimu wao waliokuwa wanazungukazunguka, lakini Paulo alijua kwamba hiki kingekuwa chanzo cha ukosoaji wa walimu wa uongo na alikataa kukubali msaada wa kifedha kutoka kwenye kanisa hili (ama kanisa lolote wakati alipofanya kazi kati yao, kama vile 1 The. 2:5-9; 2 The. 3:7-9). Paulo hakukubali msaada kutoka kwa Wafilipi wa Wathesalonike baada ya kuwa amekwisha ondoka (kama vile flp. 4:15-18 na yawezekana 1 the. 3:6). Inaonekana iliumiza hisia ya kanisa (kama vile 2 kor. 11:11; 12:13,14; 1 kor. 9:12,15,18).

◙ **"makanisa"** Angalia Mada Maalum katika 1 Kor. 1:2.

◙ **"niwahudumie ninyi"** Angalia Mada Maalum: Uongozi wa watumishi katika 1 Kor. 4:1.

**11:10 "Kama vile ile kweli ya Kristo ilivyo ndani yangu"** Hii ni njia yenye nahau ya kutetea uaminifu wa dhana ya Paulo ya uvuvio (kama vile Rum. 9:1). Angalia MADA MAALUM: "UKWELI" KATIKA MAANDIKO YA PAULO (SPECIAL TOPIC: "TRUTH" IN PAUL'S WRITINGS) katika 2 Kor. 13:8.

◙**"hakuna mtu atakayenifumba kinywa katika kujisifu huku, katika mipaka ya Akaya"** Hili ni neno muhimu la Kiyunani linalotumika katika tafsiri ya agano la kale la Kiyunani kwa ajili ya kuzuia maji ya mto. Paulo alikataa kuchukua fedha kutoka Kanisa la Korintho na wazi kabisa alilifanya hili lijulikane hadharani na mara zote. Kwa "kujisifu" angalia maelezo kamili katika 2 Kor. 1:12.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 2 WAKORINTHO 11:12-15**
**12 Lakini nifanyalo nitalifanya, ili niwapinge hao watafutao nafasi wasipate nafasi; ili kwamba katika neno hilo wajisifialo waonekane kuwa kama sisi. 13 Maana watu kama hao ni mitume wa uongo, watendao kazi kwa hila, wanaojigeuza wawe mfano wa mitume wa Kristo. 14 Wala si ajabu. Maana Shetani mwenyewe hujigeuza awe mfano wa malaika wa nuru. 15 Basi si neno kubwa watumishi wake nao wakijigeuza wawe mfano wa watumishi wa haki, ambao mwisho wao utakuwa sawasawa na kazi zao.**

**11:12** Paulo aliwajua wapinzani wake. Alijaribu kuondoa kila fursa kwa mashambulizi yao. Aliweka mipaka katika uhuru wake na haki za kulinda na kueneza injili (kama vile Rum. 14:1-15:13).

**11:13 "Maana watu kama hao ni mitume wa uongo"** Hawa viongozi wa dini waliokuwa wakitoka nje ya mji, yawezekana kutoka Yerusalem, walidai mamlaka. Paulo anawaita mitume wa bandia ama ndugu wa bandia (kama vile 2 Kor. 11:26).

◙ **"watendao kazi kwa hila"** Hili neno litokanalo na NOMINO iliyomaanisha "chombo cha kulowea samaki." Walijaribu kuwakamata waaminio kwa madhumuni yao wenyewe na kujizihirishia sifa njema.

◙ **"wanaojigeuza wawe mfano wa mitume wa Kristo"** Hawa hawakuwa Wakristo waaminifu ambao walipotoshwa. Hawa walikuwa watu ambao walikuwa wamepotea kiroho (kama vile 2 Kor. 11:14) wakijaribu kuligawa kanisa la Mungu (kama vile 1 Kor. 3:10-15). Walikuwa mbwa mwitu waliovaa ngozi ya kondoo (kama vile Mathayo 7; Matendo 20:29; 2 Pet. 2:1-22; Yuda 1:3-16).

Neno "wakajigeuza" (yaani, *metaschēmatizō*) limetumika katika 2 Kor. 11:13,14,15. Linazungumzia juu ya muundo wa kubadilika kwa nje kwa kitu ama mtu (kama vile Flp. 3:21). Hawa (yaani, walimu wa uongo na shetani) huonekana kuwa vile wasivyo!

**11:14 "Maana Shetani mwenyewe hujigeuza awe mfano wa malaika wa nuru"** Huu ni ukweli ulio dhahiri, lakini haupo mahali pengine popote kwenye Biblia ukitajwa kwa maneno hayo. Hii yaweza kuwa kutokana na mapokeo

ya walimu wa sheria za Kiyahudi kuhusu Mwanzo 3 (kama vile DSS cave 1, *Manual of Discipline* 3:20,24). Hila kuu ya shetani ni kujifanya yeye kama kweli (kama vile Mwa. 3). Uovu kila wakati hujaribu kuiga ama kugushi lile jema. Walimu wa uongo kila wakati hutoka ndani ya kanisa (kama vile 2 Pet. 2; 1 Yohana 2:18-19). Angalia MADA MAALUM: UOVU BINAFSI (SPECIAL TOPIC: PERSONAL EVIL) katika 1 Kor. 7:5.

**11:15 "ikiwa"** Hii ni SENTENSI YENYE MASHARTI DARAJA LA KWANZA. Walikuwa waalimu wa uongo waliokuwa wamevuviwa na shetani ndani ya kanisa la Korintho. Wako pamoja nasi leo!

◙ **"watumishi wa haki"** Paulo hatumii neno "haki" mara nyingi katika dhana anayotumia hapa. Hapa ina kidokezo cha "wema" au "haki" (kama vile Mt. 6:1), lakini sio katika dhana ya kithiolojia ya imani (kama vile Warumi 4). Angalia Mada Maalum: Haki katika 1 Kor. 1:30. Angalia MADA MAALUM: UONGOZI WA KITUMISHI (SPECIAL TOPIC: SERVANT LEADERSHIP) katika 1 Kor. 4:1.

◙ **"ambao mwisho wao utakuwa sawasawa na kazi zao"** Hili huonekana kuwa dokezo kwa Mith. 24:12. Pia ni ukweli wa msingi wa Biblia. Angalia maelezo kamili katika 2 Kor. 5:10.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 2 WAKORINTHO 11: 16-21a**

**16 Nasema tena, mtu asidhani ya kuwa mimi ni mpumbavu; lakini mjaponidhania hivi, mnikubali kama mpumbavu; ili mimi nami nipate kujisifu ngaa kidogo. 17 Ninenalo silineni agizo la Bwana, bali kama kwa upumbavu, katika ujasiri huu wa kujisifu. 18 Kwa sababu wengi wanajisifu kwa jinsi ya mwili, mimi nami nitajisifu. 19 Ninyi, kwa kuwa mna akili, mnachukuliana na wajinga kwa furaha. 20 Maana mwachukuliana na mtu akiwatia utumwani, akiwameza, akiwateka nyara, akijikuza, akiwapiga usoni. 21 Nanena kwa jinsi ya kujidhili kana kwamba sisi tulikuwa dhaifu.**

**11:16 "Mtu yeyote asidhani kwamba mimi ni mpumbavu. . .ili mimi nami nipate kujisifu ngaa kidogo"** Paulo hakuwa na raha juu ya kujisifu binafsi (kama vle 2 Kor. 11:1,17). Walimu wa uongo walikwisha kumlazimisha kutumia mitindo yao (yaani, miundo ya sura ya 10-13 yaaksi tabia ya miundo ya wapotoshaji wa Utaifa wa Myunani).

Kwa neno "ujinga" angalia Mada Maalum katika 1 Kor. 15:36. Kwa neno "kujisifu" Anagalia Mada Maalum: Kujisifu katika 1 Kor. 5:6.

◙ **"ikiwa"** Hii ni SENTENSI YENYE MASHARTI DARAJA LA KWANZA isiyotimilifu (yaani, hakuna KITENZI).Hawa Wakristo waaminio walishangazwa na barua ya Paulo.

**11:17** Paulo alidokeza kwa maisha na mtazamo wa Yesu katika 2 Kor. 10:1 (yaani, kwa unyenyekevu na upole wa Kristo), lakini ilipokuja wakati wa kujisifu ama kujilinganisha kibinadamu, Paulo lazima akiri kwamba hakuna kitangulizi cha jambo ndani ya Kristo.

**11:18 "Kwa sababu wengi wanajisifu kwa jinsi ya mwili, mimi nami nitajisifu"** Hili ndilo kusudi kuu la sura 10-13. Hawa walimu wa uongo walikwisha kumshambulia kwa kulinganisha Paulo na injili yake kwa kulinganisha urithi wake na vipawa alivyokirimiwa ukilinganisha na vyao (kama vile 2 Kor. 11:8). Paulo aliteseka moyoni kwamba kanisa lilikuwa limewasikiliza na lilikwisha kuyumbishwa na mabishano yao. Kwahiyo aliamua kushuka hadi kwenye kiwango chao kwa kusudi la kulipata kanisa lirejee kuwa na imani na uongozi wake na injili yake.

**11:19-20** Hii ni kejeli inayoumiza iliyoelekezwa kwenye kanisa la Korintho. Kila kitu ambacho walimu wa uongo walimshtakia Paulo, walikifanyia utendaji na kanisa liliitikia mwitikio chanya kwao!

◙ **"kuvumilia"** Angalia maelezo katika 2 Kor.11:4.

**11:20 "Maana mwachukuliana na mtu akiwatia utumwani"** Hili linaanzisha mfululizo wa SENTENSI YENYE MASHARTI DARAJA LA KWANZA tano. KITENZI hiki (yaani, *katadouloō*) kimetumika hapa tu na katika Gal. 2:4 ambapo hurejelea wale wanaolazimisha tabia za Kiyahudi. Watu waliofuata taratibu za Kiyahudi walidai kwamba ilibidi mtu awe Myahudi kikamilifu kabla hajawa Mkristo. Jinsi gani walimu hawa wa uongo wanahusiana na hawa wanaoshurutisha mila za Kiyahudi haijulikani. Sheria kamili au taratibu zilizowekwa na hawa walimu wa uongo huko Korintho kuwa kama zenye umuhimu kwenye wokovu pia hazijulikani.

◙ **"akiwameza"** Paulo alitumia KITENZI hiki mara mbili tu, hapa na katika Gal. 5:15, ambacho pia huelezea kanisa lililoko kwenye mgogoro na walimu wa uongo.

**NASB, NRSV,**
**TEV "watumia kwa manufaa yake"**
**NKJV "chukua kutoka kwenu"**
**NJB "atawaweka ninyi chini ya mamlaka yake"**

Hiki ni KITENZI cha kawaida *lambanō*, lakini kikiwa na upanuzi wa ki-sitiari wa maana halisi ya neno"kushikilia." Hapa ni kumiliki kwa hila kwa manufaa ya mtu binafsi.

**NASB, NKJV "akijiinua mwenyewe"**
**NRSV "anavaa hewa"**
**TEV "anawadharau"**
**NJB "anajiweka juu yenu"**

Paulo alitumia neno hilo hilo katika 2 Kor. 10:5 kuelezea kiburi cha hoja na makisio ya walimu wa uongo. Neno hili kikawaida ni "kuinua juu" (kama vile 1 Tim. 2:8). Lakini, 1 Wakorintho ina vidokezo hasi vya majivuno na kiburi cha binadamu.

◙ **"akiwapiga usoni"** Maneno ya Paulo yanakuwa na kejeli kibao (kama vile 2 Kor. 11:21). Alikuwa mpole na mnyenyekevu (kama vile 2 Kor. 10:1) kwao, lakini walimkataa; walimu wa uongo walikuwa wabinafsi na wenye hila lakini waliwapenda.

**11:21 "kwa aibu yangu"** Hili kikawaida ni "kutokana na fedheha." Paulo alihisi kwamba unyenyekevu na upole wake ulieleweka vibaya na waalimu wa uongo wakatumia fursa hiyo. Huu waweza kuwa mfano mwingine wa kejeli.

◙ **"dhaifu"** Angalia Mada Maalum: Udhaifu katika 2 Kor. 12:9.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 2 WAKORINTHO 11:21b-29**

**[21]bWalakini, akiwa mtu anao ujasiri kwa lo lote, (nanena kipuuzi), mimi nami ninao ujasiri. [22] Wao ni Waebrania? Na mimi pia. Wao ni Waisraeli? Na mimi pia. Wao ni uzao wa Ibrahimu? Na mimi pia. [23] Wao ni wahudumu wa Kristo? (Nanena kiwazimu), mimi ni zaidi; katika taabu kuzidi sana; katika vifungo kuzidi sana; katika mapigo kupita kiasi; katika mauti mara nyingi. [24] Kwa Wayahudi mara tano nalipata mapigo arobaini kasoro moja. [25] Mara tatu nalipigwa kwa bakora; mara moja nalipigwa kwa mawe; mara tatu nalivunjikiwa jahazi; kuchwa kucha nimepata kukaa kilindini; [26] katika kusafiri mara nyingi; hatari za mito; hatari za wanyang'anyi; hatari kwa taifa langu; hatari kwa mataifa mengine; hatari za mjini; hatari za jangwani; hatari za baharini; hatari kwa ndugu za uongo; [27] katika taabu na masumbufu; katika kukesha mara nyingi; katika njaa na kiu; katika kufunga mara nyingi; katika baridi na kuwa uchi. [28] Baghairi ya mambo ya nje, yako yanijiayo kila siku, ndiyo maangalizi ya makanisa yote. [29] Ni nani aliye dhaifu, nisiwe dhaifu nami? Ni nani aliyekwazwa nami nisichukiwe?**

**11:21b** Paulo yuko tayari kupambana jino kwa jino. Wanataka kulinganisha sifa zao, basi na iwe!

**11:22 "Wao ni Waebrania? Na mimi pia"** Hili ni swali la kwanza miongoni mwa maswali manne yasiyo hitaji majibu. "Waebrania" kinahau inarejelewa kwa uwezo wa kuzungumza Kiaramu (kama vile Matendo 6:1), lakini pamoja na maana ya utaifa wa kweli wa Kiyahudi. Huu ni ushahidi mwingine kwamba kundi hili la walimu wa uongo walikuwa na asili ya Palestina/Uyahudi.

Hili neno "na mimi pia" (yaani, *kagō*) limerudiwa mara tatu katika 2 Kor. 11:22.

◙ **"Wao ni Waisraeli? Na mimi pia"** Inaonekana walikuwa wanajigamba kwamba wao walikuwa sehemu ya ahadi ya Agano la Kale la watu wa Mungu (kama vile Flp. 3:5; Yohana 8:31-59).

**11:23 "Wao ni wahudumu wa Kristo?"** Paulo hadai hapa kwamba wao ni Wakristo. Yeye anasema tu, kwa ajili ya mabishano kwamba anao utambulisho wa kiroho kama ule wanaojigamba kuwa nao, Hata walidai kuwa na hali ya kiroho iliyo ya juu zaidi kuliko ya Paulo.

◙ **"mimi ni zaidi"** Paulo alikuwa na mfululizo wa ulinganisho ukiwa na *en*.
1. Nimefanya kazi zaidi, 2 Kor. 11:23
2. Nimefungwa gerezani zaidi, 2 Kor. 11:23
3. Nimechapwa viboko visivyo na hesabu, 2 Kor. 11:23
4. Mara nyingi nimekuwa karibu ya kufa, 2 Kor. 11:23
   a. Nimechapwa viboko arobaini kasoro kimoja (mara 5), 2 Kor. 11:24
   b. Nimechapwa kwa chuma (mara 3), 2 Kor. 11:25
   c. Mawe (mara moja), 2 Kor. 11:25
   d. Jahazi (mara 3), 2 Kor. 11:25

   Baadhi ya haya yameandikwa katika Matendo, lakini sio yote. Kwa hakika tunajua kidogo sana kuhusu kanisa la karne ya kwanza. Paulo alikwisha kulipia gharama za kuinena injili!

**11:24 "Kwa Wayahudi mara tano nalipata mapigo arobaini kasoro moja"** Mstari huu hurejelea kwenye adhabu iliyotolewa na baraza la Sinagogi (kama vile Kumb. 25:1-3). Mapigo yumkini yalitolewa kwa kumnyima mtu haki yake (kama vile Kut. 21:20; Mith. 10:13; 19:29; 26:3) na yalitolewa hadharani. Adhabu ya aina hii ilijulikana na kufanyika nchini Ashuru na Misri. Ilifanyika katika Israeli (kama vile Isa. 50:6; Yer. 20:2; 37:15).

Walimu wa sheria za Kiyahudi baadaye waliweka kanuni kwamba ilibidi viwe viboko arobaini kasoro moja (yaani, idadi kubwa zaidi, kama vile Josephus, *Antiq.* 4:8:21,23). Walieleza bayana kwamba mapigo kadhaa yapigwe mgongoni na mengine mbele, mabega ya kushoto na kulia (kama vile *Maccoth* 3:10 na kuendelea).

**11:25 "nalipigwa kwa bakora"** Mstari huu unarejea kwa aina ya adhabu ya mahakama ya Kirumi (yaani, *verberatio*), bila shaka ilisimamiwa na mahakama ya mji (kama vile Matendo 16:22-40; 1 Kor. 4:21) hadharani.

◙ **"mara moja nalipigwa kwa mawe"** Katika Matendo 14:19 washambuliaji wake walidhani alikuwa amekufa! Hili tukio laweza kuwa ndilo lenyewe.

◙ **"mara tatu nalivunjikiwa jahazi"** Mstari huu huonyesha jinsi gani historia ya matendo ilivyo. Mabaki ya jahazi la Paulo yaliyonukuliwa katika kitabu cha Matendo ya Mitume. Kitabu cha Matendo sio historia iliyokamilika, bali ni maelezo ya kithiolojia ya injili ikitembea kutoka Palestina hadi Roma, kutoka kwa Wayahudi kwenda kwa watu wa Mataifa.

**11:26**
**NASB "Nimekuwa katika safari nyingi"**
**NKJV "katika safari mara kwa mara"**
**NRSV "kwenye safari za mara kwa mara"**
**TEV "katika safari nyingi "**
**NJB "kusafiri kwa kuendelea"**
Hii inaanza orodha nyingine ya UWINGI WA WAKATI au ni muundo wa UHUSIKA mara nane kama wa A. T. Robertson's, Huu ni UHUSIKA WA MAHALI uliotambulishwa. Hakuna KITENZI, ENDELEVU,au KISICHO NA UKOMO,katika 2 Kor. 11:26,27,28. Hii huelezea huduma ya Paulo kwa Kristo.

1. Hatari kutoka kwenye mito
2. Hatari kutoka kwa wanyanganyi
3. Hatari kutoka kwa watu wa nchi yangu (kama alivyo kuwa pale Korintho)
4. Hatari kutoka kwa mataifa
5. Hatari mijini
6. Hatari nyikani
7. Hatari baharini
8. Hatari kutoka kwa ndugu wa uongo (kama alivyokuwa pale Korintho)

**11:27 "*nimekuwa*"** Paulo huanza orodha nyingine akitumia UHUSIKA WA WAKATI/UHUSIKA WA MAHALI.

1. Katika kazi ngumu
2. Katika taabu
3. Bila usingizi
4. Katika njaa
5. Katika kiu
6. Katika kufunga mara nyingi (ki sitiari. "mara nyingi bila chakula")
7. Katika baridi
8. Bila nguo (ki sitiari. "katika utupu")

Sisi wote tunaodai kuwa watumishi wa injili lazima tuache kunung'unika!

**11:28** Kitu kingine ambacho kilimfanya Paulo aumie kila siku ni wasiwasi wa kisaikolojia/ na kiroho WASIWASI KWA afya ya kanisa na upatikanaji wa matokeo mazuri ya kanisa yawezekana haya ndiyo yalikuwa maumivu makali kuliko yote!

**11:29 "Ni nani aliye dhaifu, nisiwe dhaifu nami"** Msitari wa 29 una maswali mawili yasiyodai majibu. Wakati Paulo anapoona makanisa na waaminio wakiumia, inamuumiza yeye na kumfanya kupata gadhabu juu ya wale wanaoweza kuwakwaza walio wadogo (kama vile Mt. 18).

**NASB "nisichukiwe"**
**NKJV "kuchomwa na ghadhabu"**
**NRSV "ghadhabu"**
**TEV "huwa na wasiwasi"**
**NJB "kuchomwa na masumbuko makali"**
Paulo hutumia neno hili, choma, kwa maana maalum katika barua zake za Korintho. Sio hasi au uharibifu (kama vile Efe 6:16), lakini sitiari kwa shauku lenye jaziba (kama vile 1 Kor. 7:9).

**NASB, TEV "kuhangaishwa kwa nguvu sana"**
**NKJV, NRSV "kuwaka kwa hasira"**
**NJB "mefanywa kuanguka"**
Hili ndilo neno la Kiyunani *skandalon*, ambalo kiuhalisia linarejelewa kwa fimbo iliyowekewa ndoano yenye chambo (kama vile Rum. 11:9). Limetumika katika maana ya kushindwa katika maadili (hapa na 1 Kor. 8:13) ama

yawezekana kushawishiwa na thiolojia ya uongo ya "mitume walio kiwango cha juu" (kama vile 1 Kor. 1:23; Gal. 5:11).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 2 WAKORINTHO 11:30-33**
**30 Ikinibidi kujisifu, nitajisifia mambo ya udhaifu wangu. 31 Mungu, Baba wa Bwana Yesu, aliye mtukufu hata milele, anajua ya kuwa sisemi uongo. 32 Huko Dameski liwali wa mfalme Areta alikuwa akiulinda mji wa Wadameski, ili kunikamata; 33 nami nikatelemshwa ndani ya kapu, katika dirisha la ukutani, nikaokoka katika mikono yake.**

**11:30 "Ikinibidi"** Hii ni SENTENSI YENYE MASHARTI DARAJA LA KWANZA.

◙ **"nitajisifia mambo ya udhaifu wangu"** Majaribu ya Paulo na kukosolewa vilimsababishia Paulo kutambua kwamba nguvu zake zilitoka kwa Mungu na udhaifu wake ulikuwa fursa kwa Mungu kupokea utukufu (kama vile 2 Kor. 12:1-10).

**11:31 "Mungu, Baba wa Bwana Yesu"** Aya hii ni kiapo. Paulo hutumia jina la Mungu kutetea ukweli wa kauli zake mara nyingi (kama vile Rum. 1:9; 2 Kor. 1:18; 11:10,11; Gal. 1:20; 1 Tim. 2:7).

◙ **"milele"** Hii katika uhalisia "ni kwa vizazi" (kama vile Rum. 1:25; 9:5; 11:36; 16:27). Fungu la maneno, hilo hilo lakini UMOJA, laonekana katika 1 Kor. 8:13 na 2 Kor. 9:9. Angalia Mada Maalum: Zama hizi na Zama zijazo katika 1 Kor. 1:20.

**11:32-33 "Huko Dameski liwali wa mfalme Areta"** Wengine husema kwamba hii ni kinyume na hali ya hewa, lakini huu ulikuwa unaonekana kuwa wakati wenye kuaibisha sana (yaani, dhaifu kuliko) katika maisha ya Paulo. Ingeweza kurejea shitaka jingine la walimu wa uongo. Mfalme Areta (yaani, *Harethath*) alikuwa Mfalme wa Falme ya Nabatean kutoka 9 K.K. hadi B.K. 40. Alikuwa baba mkwe wa Herode Antipas. Neno "Areta" ni sawa na neno "Farao," cheo cha wafalme wote wa Nabatean waliotawala Petra. "Liwali" angeweza kuwa mwakilishi wa Areta kule Dameski. Maelezo katika matendo 9:23-25 yako tofauti kwa namna fulani; yawezekana walimu wa uongo walitumia tukio hili kushambulia tabia ya Paulo.

## MASWALI YA MJADALA

Haya ni maoni ya <u>mwongozo</u> kwa kujisomea, ikiwa na maana kuwa unawajibika binafsi kwa tafsiri ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mtoa maoni tu.

Maswali haya ya kujadili yanatolewa ili kukusaidia kufikiri mambo muhimu yaliyoko katika kipengele cha kitabu hiki. Yanamaanisha kuwa maswali ya kichokonozi, yasio ya hakika.

1. Kwanini Paulo anajitetea dhidi ya walimu hawa wa uongo?
2. Je 2 Kor. 11:3 inahusu kuanguka kutoka kwenye neema ama kupotoshwa kutoka kwenye mamlaka ya mitume?
3. Kwanini Paulo asingekubali kupokea fedha kutoka kwa kanisa la Wakorintho?
4. Hawa mitume wa uongo walikuwa akina nani?
5. Fafanua thiolojia ya hawa waalimu wa uongo?
6. Kwanini maisha ya Paulo yakufanyiwa ukatili yalikuwa ishara ya mamlaka yake ya kitume? (kama vile 1 Kor. 4:9-13: 2 Kor. 4:8-12; 6:4)

# 2 WAKORINTHO 12

| MGAWANYO WA AYA WA TAFSRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **USB[4]** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB** |
| Maono na Mafunuo | Yale Maono ya Paradiso | Kujisifu kwa Baadaye: Nguvu Katika Udhaifu | Maono ya Paulo na Mafunuo | Paulo anabanwa Kudadisi sifa zake Mwenyewe |
| | | | | (11:1-12:18 |
| 12:1-10 | 12:1-10 | 12:1-10 | 12:1-6 | 2:1-6 |
| | | | 12:7-10 | 12:7-10 |
| Kuhusika kwa Paulo kwa Kanisa La Korintho | Ishara za Mtume | | Kuhusika kwa Paulo kwa Wakorintho | |
| 12:11-18 | 12:11-13 | 12:11-13 | 2:11-13 | 12:11-13 |
| | Upendo kwa Kanisa | Mipango ya Paulo Kuzuru Korintho Tena | | |
| | | (12:14-13:10) | | |
| | 12:14-21 | 12:14-18 | 12:14-15 | 12:14-15 |
| | | | 12:16-18 | 12:16-18 |
| | | Wito wa Kujipima na Kubadilika Mwenyewe | Woga wa Paulo na Wasiwasi | |
| | | (12:19-13:10) | | (12:19-13: 10) |
| 12:19-21 | | 12:19-21 | 12:19-21 | 12:19-21 |

**MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI** (kutoka "Mwongozo wa Usomaji Mzuri wa Biblia" A Guide to Good Bible Reading")

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Haya ni maoni ya mwongozo kwa kujisomea, ikiwa na maana kuwa unawajibika binafsi kwa tafsiri ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mtoa maoni tu.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa,lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA

A. Maono maalum na matatizo ya kimwili vyote viwili vinashughulikiwa kwenye muktadha huo huo, bila shaka yote mawili yalitukia huko Tarso miaka 14 kabla (42 ama 43). Hili haliwezi kurejelea ule uzoefu wa Paulo wa kubadilika kwake kulikotokea kiasi cha miaka 20 kabla, ingawa nafikiria "mwiba" wake ilikuwa tatizo la macho, ambalo laweza kuwa limeanza pale alipokutana na Yesu njiani kuelekea Damaski (kama vile Matendo 9:22,26).

B. Paulo anaendelea kwa kejeli yake inayochoma katika 2 Kor. 12:11,13 na 15 kama alivyofanya katika 2 Kor. 11:4-5,7,19-21. Naamini sura ya 10-13 zimeandikwa kwa mtindo wa kutumia maneno ya kuwavuta wasikilizaji wa lugha na utamaduni wa Kiyunani wa miaka 400-100 K.K. Kwa kusudi la kuwaonyesha walimu wa uongo namna alivyokuwa, Wayahudi walifundishwa lugha na utamaduni wa Kiyunani wa miaka 400-100 K.K. kwamba yeye pia alijua na aliweza kutumia mtindo walioupendelea katika fasihi.

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : 2 WAKORINTHO 12: 1-10**
**1 Paulo, mtume wa Kristo Yesu kwa mapenzi ya Mungu, na Timotheo ndugu yetu; kwa kanisa la Mungu**
**lililoko Korintho, pamoja na watakatifu wote walioko katika nchi yote ya Akaya. 2 Neema na iwe kwenu na**
**amani, zitokazo kwa Mungu Baba yetu na kwa Bwana Yesu Kristo. 3 Na ahimidiwe Mungu, Baba wa Bwana**
**wetu Yesu Kristo, Baba wa rehema, Mungu wa faraja yote; 4 atufarijiye katika dhiki zetu zote ili nasi tupate**
**kuwafariji wale walio katika dhiki za namna zote, kwa faraja hizo, tunazofarijiwa na Mungu. 5 Kwa kuwa**
**kama vile mateso ya Kristo yanavyozidi kwetu, vivyo hivyo faraja yetu inazidi kwa njia ya Kristo. 6 Lakini ikiwa**
**sisi tu katika dhiki, ni kwa ajili ya faraja yenu na wokovu wenu; au ikiwa twafarijiwa, ni kwa ajili ya faraja**
**yenu; ambayo hutenda kazi yake kwa kustahimili mateso yale yale tuteswayo na sisi. 7 Na tumaini letu kwa**
**ajili yenu ni imara, tukijua ya kuwa kama vile mlivyo washiriki wa yale mateso, vivyo hivyo mmekuwa**
**washiriki wa zile faraja. 8 Maana ndugu, hatupendi, msijue habari ya dhiki ile iliyotupata katika Asia, ya**
**kwamba tulilemewa mno kuliko nguvu zetu, hata tukakata tamaa ya kuishi. 9 Naam, sisi wenyewe tulikuwa**
**na hukumu ya mauti katika nafsi zetu ili tusijitumainie nafsi zetu, bali tumtumaini Mungu, awafufuaye wafu,**
**10 aliyetuokoa sisi katika mauti kuu namna ile; tena atatuokoa; ambaye tumemtumaini kwamba atazidi**
**kutuokoa;**

**12:1"Sina budi kujisifu"** Neno la Kiyunani *dei* linamaanisha "haja." Waalimu wa uongo walikuwa wanamshambulia Paulo. Yeye alijitetea kuhifadhi ujumbe wake. Neno "kujisifu" lilitumika mara kwa mara katika sura ya 10 -13 (kama vile 2 Kor. 10:8,13,15,16,17; 11:12,16,18,30; 12:1,5,6,9, angalia maelezo kamili katika 2 Kor. 1:12 na Mada Maalum katika 1 Kor. 5:6), lililobainisha namna ya kutumia maneno ya kuwavuta wasikilizaji kwa mtindo uliopendwa sana katika karne ya kwanza. Paulo aliwaonyesha walimu wa uongo wenye kujisifu, kwamba aliweza kucheza mchezo wao.

Sentensi hii ilikuwa inachanganya waandishi weredi wa kale, walioiboresha katika njia mbali mbali.

1. wengine waliongeza "ikiwa" (MSS $\aleph^2$, H)
2. wengine walibadili neno *dei* (lazima) kuwa *de* (lakini), (MSS ℵ na D
3. mfumo wa toleo la UBS[4] unaungwa mkono na $P^{46}$, B, $D^2$, F, G ( lenye kutoa dalaja "A")
   Namba 2 na 3 zinaonyesha ni mapema kiasi gani haya maandiko ya Kiyunani ya asili ya Kiyunani yaliyoboreshwa na waandishi waliokusudia vema.

**NASB "ijapokuwa haipendezi"**
**NKJV "hakuna mashaka ya kuwa na faida"**
**NRSV "ingawa haifai"**

**TEV "hata kama haifanyi lo lote lililo jema"**
**NJB "si kwamba imefanya lo lote jema"**

Ikiwa kujisifu kwa Paulo hakuleti faida yo yote, kwa nini ajisifu? Analifanya hili katika kejeli ili matunda yapatikane, akitumia maneno pamoja na njia hiyo ya walimu wa uongo (yaani Wayahudi waaminio waliotawanyika waliofungwa kutumia maneno kuvuta wasikilizaji ambao kwa namna fulani walikuwa na uhusiano na kanisa la Yerusalemu, sawa sawa na wale waliozifuata desturi za Kiyahudi za huko Galatia pamoja na chembe chembe za Kifarisayo zinazoonekana katika Baraza la Yerusalemu la Matendo 15).

◙**"maono na mafunuo"** Bila shaka hakuna tofauti kati ya haya maneno mawili; yote mawili yanafafanua aina ya ufunuo wa moja kwa moja. (kama vile 1 Kor. 2:10; 11:23; Gal. 1:12; 2:2; Efe. 3:3). Hawa walimu wa uongo bila shaka walikuwa wanadai mfumo maalum wa moja kwa moja. Neno "ufunuo" ni matukio ya siku ya mwisho, ambalo linamaanisha "kufunua."

Walimu wa uongo, wakati ule na sasa, wanabainishwa na
1. unyonywaji wa kijinsia
2. unyonyaji wa kifedha
3. lile dai la mafunuo ya kipekee na maalum

◙**"ya Bwana"** Hiki kinaweza kuwa KIIMA MILIKISHI "ufunuo kutoka kwa Bwana" ama KISHAMILISHO MILIKISHI, "kuhusu Bwana." Muktadha ufuatao unamaanisha "kutoka kwa Bwana" (SAUTI IRABU TENDEWA, 2 Kor. 12:2,4,7).

**12:2"Namjua mtu"** Hii ni njia ya mtu kujinenea wenyewe kisheria kwa walimu wa Kiyahudi. Paulo anaonekana kusita hata kutamka tukio, lakini anafanya hivyo kwa sababu ya upendo wake kwa kanisa na madai ya walimu wa uongo juu ya maono ya kiroho.

◙"**katika Kristo** "Hiki kilikuwa cheo cha kwanza alichokipenda Paulo cha kuwa Mkristo. Waamini wana tambulishwa na maisha/ kifo/ ufufuo Wake. (kama vile Warumi 6). Lengo la waamini ni kuwa kama Yeye (kama vile Rum. 8:29; 2 Kor. 3:18; Gal. 4:19; Efe. 1:4; 1 The. 3:13; 4:3; 1 Pet. 1:15).

George Ladd, *A Theology of the New Testament*, anatengeneza usemi wenye kuvutia kwamba

"mtu katika Kristo pia yu ndani ya Kristo. Ikiwa kinyume cha 'katika Kristo' kinapaswa kuwa katika Adamu,kinyume cha 'katika Roho' kinapaswa kuwa 'katika mwili.'

Maisha katika Kristo inamaanisha maisha ya uwepo wa matukio ya siku za mwisho katika zama mpya" (uk. 483).

◙**"miaka kumi na minne"** Bila shaka hiki kilikuwa kipindi cha huduma ya awali ya Paulo ambayo haikuchukuliwa kumbukumbu katika Tarso, muda mfupi kabla ya Barnaba kuja kumchukua ili asaidie kule Antiokia. (kama vile Matendo 11:25-26). Fahamu kwamba maono maalum hayakuwa tukio la kila siku kwa Paulo, bali yeye alikuwa na mengi kati ya hayo (kama vile Mtendo 9:4; 18:9; 23:11; 27:23).

◙**"kwamba alikuwa katika mwili sijui; kwamba alikuwa nje ya mwili sijui"** Paulo mwenyewe hata hakuwa na uhakika hasa ni nini kilichotokea (kifungu hiki cha maneno kimerudiwa mara mbili katika 2 Kor. 12:2 na 3). Inawezekana kama ulivyo uzoefu wa Ezekieli 8 ama kama uzoefu wa Yohana katika kitabu cha Ufunuo (kama vile Ufu. 1:10; 4:2; 17:3; 21:10). Tambua kwamba mwili hauwekwi kando kutoka mbinguni katika Ukristo kama ilivyokuwa katika falsafa ya Kiyunani.

◙ **"alinyakuliwa juu"** Neno hili hili linatumika kwa (1) Filipo katika 8:30; (2) "kunyakuliwa" katika 1 The. 4:17; (3) mtoto wa kiume katika Ufu. 12:5. Ile maana yake ya msingi ni kumnyakua kama yule mnyama alaye nyama afanyavyo kwa mawindo yake. Bila kutarajia kabisa Paulo alirejeshwa katika mwili ama ufahamu katika uwepo wa Mungu (kama vile 2 Kor. 12:4).

◙**"mbingu ya tatu"** Angalia Mada Maalum ifuatayo.

## MADA MAALUM: MBINGU NA MBINGU YA TATU (SPECIAL TOPIC: THE HEAVENS AND THE THIRD HEAVEN)

**12:3-4** Mistari hii baaaye inaeleza lile tukio lililotajwa katika 2 Kor. 12:2.

**12:4"Peponi"** Hili ni neno la mkopo la lugha ya Kiajemi lenye maana ya "bustani ya mtu mwenye cheo kikubwa, iliyowekewa ukuta" Neno la Kiyunani linatumika katika Maandiko ya Agano la Kale juu ya neno "Bustani ya Edeni" (kama vile Mwa. 2:8; 3:1; Eze. 28:13; 31:18). Hili neno linatumika katika Luka 23:43 kwa maana ya kuwa na sehemu ya mwenye haki kule Kuzimu ama Shimoni. Katika kitabu cha ziada kinachohusu sheria za kanisa *The Secrets of Enoch*, au *II Enoch*, sura 8, hili neno linatumika kwa mbingu ya tatu ama uwepo wa Mungu. Mbingu ya tatu na Peponi ni njia zote za kurejelea uwepo wa Mungu.

◙**"akasikia maneno yasiyotamkika, ambayo haijuzu mwanadamu ayanene"**Shauku ya mwanadamu haipaswi kutumika katika maeneo yote ya ile kweli. Kama Lazaro alivyokaa kimya kuhusu uzoefu wake alioupata mle kaburini, Paulo asingeweza (yaani, takatifu sana), asingeweza (yaani, hakuna msamiati wa kibinadamu unaoweza kutoshereza), kushiriki uzoefu huu. Kuna mchezo kwenye neno "isiyosemeka"; *arrētos*, "kunena," na *hrētos* ama huenda hii ilikuwa nahau ya kiufundi ya uanzilishi wa taratibu za dini za siri. Bila shaka hapakuwa na msamiati wa kibinadamu uliotosheleza kueleza kile alichokiona (kama vile 1 Kor. 2:9).

**12:5** Paulo hajisifu katika kukamilisha mambo yake binafsi (angalia maelezo kamili katika 2 Kor. 1:12), bali katika ufunuo wa Mungu Mwenyewe kupitia vyote yaani uzoefu binafsi na ile kweli ya injili. Huu ni upungufu wa Paulo upungufu ambao unamruhusu Mungu kutukuzwa katika yeye (linganisha Yohana 15:5 na Flp. 4:13).

◙**"udhaifu"** Angalia Mada Maalum katika 2 Kor. 12:9.

**12:6"kama"** Hii ni TENTENSI YENYE MASHARTI DARAJA LA KWANZA, ambayo inamaanisha tendo lililo muhimu.

◙**"mpumbavu"** Angalia Mada Maalum katika 1 Kor. 15:36.

◙**"ili mtu asinihesabie zaidi ya hayo ayaonayo kwangu au kuyasikia kwangu."** Hili linaangukia upande wa kejeli. Hawa manabii wa uongo walitamba kwa uzoefu na sifa zilizopita, ambapo Wakorintho walizisikia tu. Paulo anasema, "msinisifu kwa kile ambacho sikuwaonyesha ninyi, bali kwa kile nilichokifanya miongoni mwenu. Tazama historia yangu"

**12:7"kwa wingi wa mafunuo"** Kifungu hiki kisarufi kinaweza kuhusiana na "mtu asinihesabie" cha 2 Kor. 12:6 ama "nisije nikajivuna kupita kiasi" cha 2 Kor. 12:7. Ikiwa neno *dio* liko katika andiko halisi la 2 Kor. 12:7 (kama vile MSS א, A, B, F, G) kisha huenda ikaendana na 2 Kor. 12:6, lakini neno *dio* linaachwa na machapisho mengi ya kale ya Kiyunani (kama vile MSS $P^{46}$, D, na zile tafsiri za lile Toleo la Kilatini, Armenia, na Toleo la Ashuru). Toleo la $UBS^4$ linatoa hitimisho la daraja "C" (ni vigmu kafikla maamuzi).

Kwa aya ya "wingi wa mafunuo" (*huperbolē*) angalia Mada Mada Maalum: Matumizi ya Paulo ya neno Ambatani *Huper* katika 1 Kor. 2:1.

◙**"nisije nikajivuna kupita kiasi"** Neno hili hili linatumika katika 2 The. 2:4 kueleza kujisifu kwa majivuno ya "Mwanadamu wa Dhambi" ama Mpinga Kristo. Tena Paulo anajitofautisha mwenyewe na wale manabii wa uongo. Hawa walijisifu kwa njia ya mtindo wa maneno ya Kiupotoshaji (ambao Paulo anauiga katika sura 10-13).

Paulo aliamini kwamba Mungu (yaani, SAUTI IRABU TENDEWA ya neno "kupewa") amempa huu "mwiba katika mwili" kwa makusudi (yaani, kishazi *hina*). Hii inaweza kuwa maana ya Rum. 8:28 (yaani, baadhi ya machapisho ya Kiyunani yanasoma "Mungu husababisha mambo yote"), lakini jambo jema ni kule kufanana na Kristo kunakoelezwa kwa uwazi kabisa katika Rum. 8:29 (yaani, kuthibitika kwa sura na mfano wa Mwana Wake). Shetani ni mtumishi!

◙**"mwiba katika mwili"** Hili neno "mwiba" linaweza kumaanisha "mambo" (yaani, kimaandishi "kuchongoka"). Katika Kiyunani cha sasa hili neno linatumika katika maana ya kile kitu chenye ncha kali ambapo katika Maandiko ya Kale ya Kiyunani hili linatumika kwa mwiba wa mmea (kama vile Num. 33:55; Eze. 28:24; Hos. 2:6). Baadhi ya nadharia zinauchukulia mwiba katika mwili wa Paulo kama:

1. Mababa wa kanisa la kale, Luther na Calvin, wanasema kuwa haya yalikuwa matatizo ya kiroho pamoja na ile asili yake iliyoanguka (yaani, "katika mwili")
2. Chrysostom anasema hili lilikuwa tatizo lake pamoja na wale watu (kama vile Hes. 33:55; Amu. 2:3)
3. Wengine wanasema kuwa hiki kilikuwa kifafa
4. Bwana William Ramsay anasema hii ilikuwa malaria
5. Nafikiri huu ulikuwa ugonjwa wa macho, lile tatizo la ugonjwa wa kawaida wa macho (linganisha Gal. 4:13-15 na 6:11) lililochochewa ama kusababishwa na upofu hali akiwa njiani kuelekea Dameski (kama vile Matendo 9, bila shaka hili ni dokezo la kitabu cha Agano la Kale katika Yos. 23:13)

Kwa neno "mwili" angalia Mada Maalum katika 1 Kor. 1:26.

◙**"mjumbe wa Shetani"** Mungu huruhusu kumtumia yule mwovu (kama vile Ayu 2:6; 1 Kor. 5:5; 1 Tim. 1:20). Hili neno "mjumbe" linaonekana kurejelea yule wakala wa kipepo. Hili neno"mjumbe" katika lugha zote za Kiebrania na Kiyunani linaweza kutafsiriwa "malaika." Kama ndivyo, tunaona kwamba waamini wanaweza kuathiriwa na huyo pepo mbaya, lakini tambua hii ni kwa ajili ya makusudi ya Mungu. Mungu humtumia yule mwovu kwa makusudi ya haki Yake Mwenyewe.

**MADA MAALUM: SHETANI (SPECIAL TOPIC: SATAN)**

◙**"ili anipige"** Hii ni KAULI TENDAJI TEGEMEZI YA WAKATI ULIOPO. Hili neno kimaandishi linamaanisha "kupiga kwa ngumi" Tatizo hili lilikuwa la kimaumivu na la mara kwa mara.

◙**" nisije nikajivuna kupita kiasi"** Hili ni kusudi (yaani, *hina*) la hiki kishazi. Yale madai ya kiroho ya wale waalimu wa uongo yanasisitiza juu ya waliosisitiza juu ya majisifu yao. Kujinyenyekesha kwa Paulo.

**12:8 "nalimsihi Bwana"** Kimuktadha hili linaweza kurejelea (1) YHWH ama (2) Yesu (kama vile Yohana 14:13-14). Mara nyingi Paulo aliomba kwa Baba. Wakristo wanaweza kuomba kwa Nafsi yo yote ya Uungu wa Utatu, japo mara kwa mara tunaomba kwa Baba, katika jina la Mwana, kupitia kwa Roho.

◙**"hicho"** Inawezekana kwamba neno "hicho" linarejerelea (1) hali hii; (2) taabu hizi; (3) mjumbe huyu wa Shetani; ama (4) huu ugonjwa wa kimwili.

◙**"mara tatu"** Ombi la Yesu pale Gethsemane lilirudiwa mara tatu (kama vile Mt. 26:42; Marko 14:39,41). Marudio matatu fungamano yanadokeza msistizo. Hii haikuwa sababu ya uhaba wa kuamini, bali kuonyesha kwamba tunaweza kuomba cho chote kinachotuhusu kama tujisikiavyo kimahitaji. Marudio haya, matatizo yenye kuumiza yalimfundisha Paulo somo kubwa la kiroho (kama vile 2 Kor. 12:9). Hapa lazima niseme kwamba idadi ya majeraha inatoa nuru ya msistizo mkubwa katika maisha yetu kuhusiana na uponyaji wa imani inayoamriwa katika kiwango cha imani ya mtu anayehitaji uponyaji. Kwa uwazi kabisa Paulo alikuwa na imani kubwa sana. Pia, yale mafundisho ya kusikitisha kwamba Mungu hutaka kila mtu aponywe na kukombolewa kutoka kila tatizo yana elezwa katika kifungu hiki. Yale maombi ya wote yaani Yesu na Paulo hayakujibiwa katika njia ile walioitaka. Mungu huyatumia

matatizo na maradhi katika maisha yetu kwa ajili ya makusudi Yake (kama vile Rum. 8:17; 2 Kor. 1:5,7; Phil. 3:10; 1 Pet. 4:12-17). Mahitaji yetu ni fursa ya Mungu ya kujifunua Mwenyewe na mapenzi yake kwetu!

**12:9"Naye akaniambia"** Hii ni KAULI YA WAKATI ULIOPO, iliyo katika nahau ya aya "hatimaye alisema."

◙**"Neema yangu yakutosha"** Hii sifa na uwepo wa Mungu ni mahitaji yote ya Paulo. Nafikiri Paulo angeliweza kufikiri juu ya 1 Fal. 8:27. Hii ni moja ya sehemu katika kitabu cha Agano la Kale ambapo kifungu "mbingu na mbingu ya mbingu" kinatumika, ambapo kinaweza kuwa chanzo cha "mbingu ya tatu" ya Paulo katika 2 Kor. 12:2. Ombi la Suleimani lilizungumzia vyoye yaani "mbingu kuu sana" ya Mungu isiyokuwa na mipaka na kuwepo Kwake daima kila mahali katika Hekalu. Paulo hakuishi katika ukuu wa mbingu ya tatu, bali katika asili ya neema na uwepo binafsi uliokuwa pamoja naye kila siku.

◙**"uweza wangu hutimilika"** Hii ni KAULI TENDEWA YA WAKATI ULIOPO. Nguvu ya Mungu hutenda kazi kwa sifa tofauti kuliko ile ya mwanadamu. Mungu hupokea utukufu wakati kiungo cha mwanadamu kinapokuwa dhaifu na kutokuwa na uwezo wa kukutana na mahitaji yake. Nguvu ya Mungu ndiyo sifa Yake isiyobadilika!

Kifungu hiki kinaweza kuwa kimemkumbusha Paulo juu ya 1 Kor. 2:5 ama 2 Kor. 4:7 na kwa upekee hakihusiani na ule msistizo wa walimu wa uongo juu ya utendakazi wa mwanadamu ama yale manufaa.

◙**"nitajisifia udhaifu wangu "** Angalia Mada Maalum hapa chini.

## MADA MAALUM: UDHAIFU (SPECIAL TOPIC: WEAKNESS)

◙**"uweza wa Kristo"** Tambua huu ni uweza wa Mungu! Huu ni uweza wa Kristo! Kristo ni Mungu!

**NASB, NRSV "ukae juu yangu"**
**NKJV, NJB "na ukae juu yangu"**
**TEV "najikia ulinzi. . .juu yangu"**

Hili neno la Kaiyunani *piskēnoō*, ambalo ni *epi* huongeza *skēnē* (nyumba ya maskani, kama vile 2 Kor. 5:1), hivyo, kistiari ni kwa ajili ya kuweka kivuli ama kukaa ndani yake. Neno hili linapatikana hapa katika Agano Jipya pekee. Mzizi huu wenye kufanana unatumika kwa Yesu aliyezaliwa katika ubikra (kama vile 1:35) yale mabadiliko ya Yesu (kama vile Mt. 17:5), na kwa kile kivuli cha Mitume kiangukiacho juu ya watu na wao kuupokea uponyaji (kama vile Matendo 5:15).

Paulo alifahamu kwamba lile wingu la kile kipindi cha kutangatanga jangwani (kama vile Kut. 40:35) liliitwa na wale Waalimu wa Sheria za Dini ya Kiyahudi "*shekinah*. Lile wingu la utukufu." Neno *Shekinah* linamaanisha "kuishi katika hali ya kudumu" Paulo alitaka uwepo binafsi wa Mungu, ulio kamili na uliofunuliwa kwa utimilifu na kuunganishwa katika Kristo, pamoja naye. Hili ndilo lengo la Ukristo, si nguvu binafsi, hadhi binafsi, maarifa maalum ama uzoefu (yaani, "Ili nimjue Yeye kutokana na udhaifu na mateso," kama vile Flp. 3:10).

**12:10"Kwa hiyo napendezwa na udhaifu"** Paulo anafahamu kutokana na uzoefu binafsi (yaani, barabarani akielekea Dameski) zile dhamira njema na juhudi binafsi hazitoshi. Tunahitaji neema (kama vile 2 Kor. 12:9), si uweza. Hakuna mwanadamu atayejitwalia utukufu wa Mungu (kama vile 1 Kor. 1:29; Efe. 2:9). Neema ya Mungu, uweza, na utukufu vinasisitizwa katika kujitoa, hali ya kutotosheleza, viungo vya mwanadamu.

◙**"napendezwa na udhaifu"** Katika ukumbusho wa mstari huu Paulo anatoa muhtasari mfupi sana wa majaribu ya huduma yake, ambao ameutaja kabla katika 2 Kor. 4:7-11; 6:3-10; 11:24-28. Paulo alifahamu kwa ukamilifu ile maana ya yale maneno ya Yesu katika Mt. 5:10-12!

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : 2 WAKORINTHO 12:11-13**
[11] **Nimekuwa mpumbavu, ninyi mmenilazimisha. Maana ilinipasa nisifiwe na ninyi; kwa sababu sikuwa duni ya**

**mitume walio wakuu kwa lo lote, nijapokuwa si kitu. [12] Kweli ishara za mtume zilitendwa katikati yenu katika saburi yote, kwa ishara na maajabu na miujiza. [13] Maana ni kitu gani mlichopungukiwa kuliko makanisa mengine, ila kwa kuwa mimi sikuwalemea? Mnisamehe udhalimu huu.**

**12:11"Nimekuwa mpumbavu"** Hii ni KAULI TENDAJI ELEKEZI YENYE KUARIFU. Baadhi ya makundi (yaani, 1 Wakorintho 1-4) ama baadhi ya makundi ya walimu wa uongo yaliyotapakaa sehemu mbali mbali (yaani, 2 Kor. 10-13) yamemshambulia Paulo, uongozi wake, mamlaka yake, mtindo wake wa kuongea, na injili. Hivyo, Paulo ilimpasa kujitetea. Alilifanya hili katika njia kadhaa.

1. kuyalinganisha maisha yake na wengine
2. kutumia mtindo wao wa uzungumzaji, lakini kwa unyenyekevu
3. alitumia kejeli ili kuziunda hoja zake

Angalia MADA MAALUM: MANENO KWA WATU WALIO WAPUMBAVU (SPECIAL TOPIC: TERMS FOR FOOLISH PEOPLE) katika 1 Kor. 15:36.

◙**"Nime"** Hili ni neno la mkazo "Nime" (yaani, *egō*) inatumika katika 2 Kor. 12:11,13,15, na 16.

◙**"mmenilazimisha"** Angalia maelezo kamili katika 2 Kor. 3:1.

◙**"sikuwa duni ya mitume"** Angalia maelezo kamili katika 2 Kor. 11:5.

◙**"Kama"** Hii ni SENTENSI YENYE MASHARTI DALAJA LA KWANZA inayotumika kwa makusudi ya kuiunda hoja hii, si uhalisia. Paulo hakuwa duni kwao katika maana yo yoe ile.

◙**"nijapokuwa si kitu"** Paulo aliifahamu na aliielewa nafasi yake katika neema tu (kama vile 1 Kor. 15:9; Efe. 3:8; 1 Tim. 1:15). Yeye pia aliifahamu nafasi yake kama aliyeitwa, Mtume aliyeitwa (kama vile Matendo 8,22,26)!

**12:12"kwa ishara na maajabu na miujiza"** Huduma ya Paulo ilithibitishwa na nguvu ya Mungu (kama vile 1 Kor. 2:4; 4:20; Rum. 15:19). Hata hivyo, hii haikuwa katika miujiza, bali katika mtazamo na matendo yake kulielekea kanisa lake ambalo lilithibitishwa kuwa lilitoka kwa Mungu.

**12:13"ila kwa kuwa mimi sikuwalemea"** Paulo asingelihusu kanisa hili lenye makundi ya kimatengano kumsaidia. Yeye aliyangojea makanisa ya kule Filipi (Flp. 4:15) na Thesalanike (1 The. 3:6), lakini ni baada tu ya kuondoka katika miji ile. Hili linaumiza fikra za kanisa la kule Korintho (kama vile 2 Kor. 12:13a), lakini Paulo asingebadili mawazo kwa sababu ya wale walimu wa uongo (kama vile 2 Kor. 11:8-20). Hata hivyo, Paulo aliunga mkono (kama kanuni) msaada wa kanisa wa kifedha kwa wahudumu (kama vile 1 Kor. 9:3-18).

◙**"makanisa"** Angalia Mada Maalum katika 1 Kor. 1:2.

◙**"Mnisamehe udhalimu huu"** Hii ni kejeli inayochoma.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : 2 WAKORINTHO 12:14-18**
**[14]Tazama, hii ni mara ya tatu ya mimi kuwa tayari kuja kwenu, wala sitawalemea. Maana sivitafuti vitu vyenu, bali nawatafuta ninyi; maana haiwapasi watoto kuweka akiba kwa wazazi, bali wazazi kwa watoto. [15] Nami kwa furaha nyingi nitatapanya, tena nitatapanywa kwa ajili ya roho zenu. Je! Kadiri nizidivyo kuwapenda sana, ninapungukiwa kupendwa? [16] Lakini na iwe hivyo, mimi sikuwalemea; bali kwa kuwa mwerevu naliwapata kwa hila. [17] Je! Mtu ye yote niliyemtuma kwenu, kwa mtu huyo naliwatoza kitu? [18] Nalimwonya Tito, nikamtuma ndugu yule pamoja naye. Je! Tito aliwatoza kitu? Je! Hatukuenenda kwa Roho yeye yule na katika nyayo zile zile?**

**12:14**
**NASB, NRSV,**
**NJB "hapa"**
**NKJV "sasa kwa"**
**TEV-imeachwa-**

Hiki ni KIBAINISHI kisisitizi cha neno *idou*, cha Kiyunani chenye nguvu kitumikacho mara nyingi katika Injili, kwa kawaida hutafsiriwa "tazama." Hiki kinatumika kuvuta umakini wa usemi unaofuatia. Paulo hukitumia mara chache (kama vile Rum. 9:23 [nukuu ya Agano la Kale]; 1 Kor. 15:51; 2 Kor. 5:17; 6:2 [nukuu ya Agano Jipya], 9; 7:11; 12:14; Gal. 1:20).

◙ **"hii ni mara ya tatu"** Kitabu cha Matendo kinaandika ziara mbili tu za kwenda Korintho (kama vile Matendo 18:1; 20:2-3; 2 Kor. 1:15; 13:1,2). Hata hivyo, KItabu cha Matendo sio historia kamili ama iliyosimulia habari zote, bali waraka wa kithiolojia unaoonyesha kusambaa kwa Ukristo kutoka kundi la watu, kutoka Palestina hadi Roma.

◙ **"wala sitawalemea"** Hii inahusu kufidiwa kifedha (kama vile 2 Kor. 11:9; 12:13; 1 Kor. 9:12,18). Paulo anathibitisha wahudumu kupokea fidia, lakini binafsi alikataa kwa sababu (1) alishambuliwa na walimu wa uongo kuhusu swala hili (kama vile 2 Kor. 12:14b) au (2) msingi wake kama rabbi uliiweka kando fidia hiyo.

◙ **"bali ninyi"** Paulo hataki fedha yao, bali uaminifu na usafiri wao.

◙ **"watoto. . . wazazi"** Paulo anatumia analojia ya familia. Alijifikiria kuwa baba yao wa kiroho (kama vile 1 Kor. 4:14-15; Gal. 4:19).

**12:15 "nitatapanya"** Neno hili la Kiyunani laweza kueleweka kwa njia mbili: (1) maana halisi "kulipa fedha" (kama vile Matendo 21:24) au (2) kitamathali "kutumia kitu kizima" au "kulipa kitu ama cho chote" (kama vile Marko 5:26). Paulo alikuwa tayari kutoa rasilimali zake zote na/ama nafsi yake kwa ajili ya Kristo miongoni mwa waaminio wa Korintho. Kwa uwazi kabisa Paulo anatumia maneno ya mzaha kuhusu fedha. Hakutaka wao watumie fedha kwa mahitaji yake, bali angejitumia kwa ajili yao.

◙ **"ajili ya roho zenu"** "Nafsi" (yaani, *psychē*) limetumika katika maana ya watu katika maandishi ya Paulo kama "roho" (kama vile *pneuma*, kama vile Flp. 1:27).

Hii sio analojia yenye mgao wa sehemu mbili ya Mwanadamu, bali uhusiano wa mara mbili wa sayari hii na kwa Mungu. Neno la Kiebrania *nephesh* (BDB 659) linatumika kwa mwanadamu na mnyama pamoja katika kitabu cha Mwanzo, ambapo neno "roho" (*ruah*, BDB 924) linatumika kipekee kuhusu mwanadamu. Huu sio uthibitisho – andiko juu ya asili ya mwanadamu kama kiumbe chenye nafsi tatu (trichotomous). Mwanadamu kimsingi anawakilishwa katika biblia kama umoja (kama vile Mwa. 2:7). Kwa ajili ya muhtasari wa nadharia za mwanadamu kama kiumbe kilichogawanyika katika sehemu tatu, angalia Millard J. Erickson's *Christian Theology* (toleo la pili) kur. 538-557 na Frank Stagg's *Polarities of Man's Existence in Biblical Perspective*.

◙ **"ikiwa"** Hii ni SENTENSI SHURUTISHI DARAJA LA KWANZA, ambayo inachukuliwa kuwa ya kweli kutokana na mtazamo wa mwandishi kwa kusudi la uandishi wake.

◙ **"zaidi"** Hili ni kundi la maneno yanayohusiana kueleza sifa za Paulo za mihemko na mtindo wa kutumia fasihi kupita kiasi katika 2 Wakorintho. Angalia nukuu katika 2 Kor. 2:7.

◙ **"Kadiri nizidivyo kuwapenda sana"** Kadri Paulo alivyozidi kutoa vitu kwao, ndivyo walivyozidi kumpunguzia heshima na upendo. Hii ilikuwa hali ambayo haikuweza kuvumilika.

**12:16 "Lakini na iwe hivyo, mimi sikuwalemea; bali kwa kuwa mwerevu naliwapata kwa hila"** Hili lingeweza kuhusiana na ule mchango kwa ajili ya kanisa la Yerusalemu katika sura 8-9. Walimu wa uongo bila shaka walimtuhumu yeye kwa kuwatuma wengine kukusanya fedha kwa ajili yake (kama vile 2 Kor. 12:17-18).
Hoja ya Paulo hapa ni zile kejeli zinazoumiza!

**12:18 "Tito"** Inashangaza kwamba Tito hakutajwa kamwe katika kitabu cha Matendo (labda alikuwa mdogo wake Luka). Alikuwa mmoja wa wasaidizi wa Paulo waaminifu waliotumainiwa sana. (Angalia Mada Maalum katika 2 Kor. 2:13). Inaonekana Tito pia hakupokea fedha yo yote kutoka katika kanisa hili, aliufuata mfano wa Paulo.

◙ **" ndugu yule pamoja naye"** Hii huenda ni sawa na ile ya katika 2 Kor. 8:18. Wengine wanadhani alikuwa Luka (yaani, Origen). Hali hii ya kwenda pamoja na mwakilishi mmoja kutoka kwenye makanisa ilikuwa njia ya Paulo kuondoa mashtaka yaliyohusu changizo hili kwa ajili ya kanisa la Yerusalemu.

◙ Aya ya 17 na 18 zina mlolongo wa maswali manne. Muundo wa kisarufi wa majibu mawili ya kwanza unatarajia jibu la "hapana" ambapo yale mawili ya mwisho yanatarajia jibu la "ndiyo". Kusudi la maswali haya ni kuonyesha kwamba si Paulo ama Tito aliyepata manufaa katika njia yeyote, kama baadhi yao walivvyokuwa wametoa tuhuma.

◙**"Roho yeye yule"** Hii inahusu roho ya mtu iliyokombolewa ya Tito (yaani, UHUSIKA WA MAHALI) sio Roho Mtakatifu (UHUSIKA WA KUTUMIKA). Paulo hutumia " Roho" kujirejerea mara nyingi (kama vile 2 Kor. 2:13; 7:13; 1 Kor. 2:11; 5:4; 16:18; Rum. 1:9; 8:16; Flp. 4:23). Angalia nukuu katika 2 Kor. 7:13b.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 2 WAKORINTHO 12:19-21**
**19 Mwadhani hata sasa ya kuwa najidhuru kwenu! Mbele za Mungu twanena katika Kristo. Na hayo yote, wapenzi, ni kwa ajili ya kuwajenga ninyi. 20 Maana nachelea, nisije nikawakuta si kama vile nitakavyo kuwakuta, nikaonekana kwenu si kama vile mtakavyo; nisije nikakuta labda fitina na wivu, na ghadhabu, na ugomvi, na masingizio, na manong'onezo, na majivuno, na ghasia; 21 nami nitakapokuja tena, Mungu wangu asije akanidhili kwenu, nami nikawasikitikia wengi waliokosa tangu hapo, wasiutubie uchafu, na uasherati, na ufisadi walioufanya.**

**12:19 "hata sasa"** Paulo anarejerea barua yake ya wakati huo (yaani, 2 Wakorintho).

◙**"Na hayo yote, wapenzi, ni kwa ajili ya kuwajenga ninyi"** Huu ni msemo wa kejeli. Paulo alilijua kanisa hili vyema. Walikuwa na makisio yaliyojazwa kujiona wenye thamani na uhuru mkubwa.

◙ "**Mbele za Mungu**" Paulo anatumia fungu hili hili la maneno katika 2 Kor. 2:17, anapofanya kiapo cha uaminifu mbele za Mungu.

◙ **"Na hayo yote"** Paulo anatamka mamlaka yake akitumia neno hili 2 Kor. 10:8. Alijitetea mwenyewe ili kutetea na kulilinda kanisa hili ambalo lilikuwa limepotoshwa. Matendo yake yalikuwa kwa ajili yao, sio kwa ajili ya nafsi yake. Angalia MADA MAALUM: ADILISHA (SPECIAL TOPIC: EDIFY) katika 1 Kor. 8:1.

◙ "**wapenzi**" Paulo anawatambulisha kanisa lake katika kweli  na wazi, lakini na upendo mkuu. Hili lilikuwa neno la kuonyesha upendo (kama vile 1 Kor. 10:14; 15:58; 2 Kor. 7:1; 12:19).

**12:20** Hii kwa usahihi inaaksi maelezo ya 1 Wakorintho kulihusu kanisa hili kumwelekea kila mmoja na mwenzake na kwa Paulo pia kama inavyoonyesha 1 Wakorintho.

◙**"ugomvi"** Angalia nukuu kamili katika 1 Kor. 2:11.

Neno hili na lile linalofuatia ni UMOJA (kama vile MSS P[46], א, A), lakini maneno mengine yaliyo katika orodha ni WINGI.

◙"**wivu**" Katika muktadha huu linahusu roho ya chama ama vikundi vinavyo azimiana (kama vile 1 Kor. 3:3). Angalia nukuu katika 2 Kor. 9:2.

◙**"ghadhabu"** Hili linahusu tabia ya hasira kali (kama vile Gal. 5:20; Efe. 4:31; Kol. 3:8).

◙**"masingizio"** Neno hili (yaani, *eritheia*) kwa asili lilimaanisha "kuzunguka kwa ajili ya kukodisha" Hili lilikuja kutumika kwa kiburi cha mamlaka ya kifalme dhidi ya wale waliokuwa wakifanya kazi kwa ajili ya kupata mahitaji yao. Tabia hii inafanana na kuazimiana kwa vikundi vya 1 Wakorintho, hasa sura ya 11. Neno hili linatumiwa mara nyingi na Paulo (kama vile Rum. 2:8; Gal. 5:20; Flp. 1:17; 2:3; na pia angalia matumizi ya Yakobo katika Yakobo 3:14,16).

◙**"fitina "** Hili linahusu kumsema mtu mwingine vibaya, kumharibia jina (kama vile Rum. 1:30; 2 Kor. 12:20; Yakobo 4:11; 1 Pet. 2:1,12; 3:16). Kazi hii inatumika kufafanua ile kazi ya shetani.

◙ **"manong'onezo "** Neno hili "nong'ona," ambalo lahusu kueleza habari za mtu wakati amewapatia mgongo kwa faragha.

◙"**majivuno**" Neno la Kiyunani *phusioō* kwa asili lilimaanisha kujaza ama kupuliza kitu (yaani, Robertson, *Word Pictures in the New Testament*, uk. 105 na Vincent, *Word Studies*, uk. 766, kutoka *phusa* - viriba). Lilikuja kutumiwa na fasihi ya Kikristo (yawezekana ilibuniwa na Paulo) Kisitiari badala ya kiburi ama majigambo. Hili lilikuwa tatizo kubwa katika kanisa la Korintho. Paulo hutumia neno hili katika 1 Kor. 4:6,18,19; 5:2;; 8:1; 13:4; na kwenye orodha ya dhambi katika 2 Kor. 12:20. Hili linatumika tu nje ya nyaraka za Korintho katika Agano Jipya kwenye Kol. 2:18, ambapo linahusu yale mafunuo ya maono ya walimu wa uongo ya elimu maalum.

**NASB "ghasia"**
**NKJV "msuko suko"**
**NRSV, TEV "uasi"**
**NJB "maasi"**

Angalia katika 1 Kor. 14:33. Hili lilikuwa kanisa lenye vikundi vinavyoazimiana. Neno hili limetumika pia katika Yakobo 3:16.
Kuna orodha kadhaa ya tabia mbaya katika maandiko ya Paulo (kama vile Rum. 1:29-31; 1 Kor. 5:11; 6:9; Gal. 5:19-21; Efe. 4:31; 5:34; Kol. 3:5-9). Katika njia nyingi walifanana na orodha ya tabia mbaya ya wa-Staiko. Ukristo unadai mwitikio wa kiuadilifu. Uzima wa milele, una tabia inayowezekana ya uadilifu.

**12:21** Paulo alihofu kwamba kama kanisa hili halikutubu angelazimika kutumia mamlaka yake ya kitume wakati angerudi (kama vile 2 Kor. 13:2). Baadhi ya vikundi vilivyo azimiana (yaani, 1 Wakorintho) na walimu wa uongo (yaani, 2 Wakorintho ) yaonekana waliishi maisha yasiyomcha Mungu na kujihusisha na ubinafsi.

**NASB, TEV,**
**NJB "fedhehesha"**
**NKJV, NRSV**
**NIV "unyenyekevu"**

Paulo hutumia mzizi huu wa neno katika maana kadhaa kwenye barua zake kwa Wakorintho (imechukuliwa kutoka Harold K Moulton, *The Analytical Greek Lexicon Revised*, uk. 397.

1. *tapeinos*
    a. ya hali ya chini, huzuni (2 Kor. 7:6)
    b. kupenda kwa upole ama bila kuzidi kiasi (2 Kor. 10:1)

2. *tapeinoō*
    a. (SAUTI IRABU YA KATI) kuishi katika hali ya unyenyekevu (2 Kor. 11:7)
    b. Kuwa mnyenyekevu na heshima kwa matumaini na matarajio; kuhuzunishwa na kukatishwa tamaa (2 Kor. 12:21)

◙ **"nikawasikitikia"** Angalia nukuu katika 1 Kor. 5:2.

◙ **"wengi waliokosa tangu hapo"** Kifungu hiki chote cha maneno kinatafsiri kibainishi na badiliko la KIBAINISHI na HALI YA KUENDELEA kilichotumika hapa tu na katika 2 Kor. 13:2. Hii ni kauli ya kitenzi tendaji endelevu cha hali ya kuendelea ya KIWAKILISHI CHA Kiyunani *pro* (yaani, kabla) na *hamartanō* (yaani, kutenda dhambi). Maana iliyoambatanishwa ni wale waliotenda dhambi na wanaendelea kutenda dhambi. Dhana ya "zamani" haikuwekwa ndani, bali ni nyongeza ya watafsiri. Muda pekee ndiyo uliowekwa katika DHAMIRA ELEKEZI

◙ **"wasiutubie"** Aya hii kwa uwazi kabisa inawarejelea wale Wakristo ambao huendelea kutenda dhambi. Toba ni muhimu sana, sio ya mwanzoni tu (kama vile Marko 1:15; Matendo 2:38,41; 3:16,19; 20:21), bali ni endelevu (kama vile 1 Yohana 1:9). Toba kwa aaminiye hurejesha ushirika, sio wokovu! Toba ni mtazamo kuelekea kwa Mungu na nafsi zaidi ya seti ya vitendo vya kiroho au hatua. Angalia maelezo kamili katika 2 Kor. 7:8-11

◙ **"uchafu, na uasherati, na ufisadi"** Lazima tuwatambue wasio mjua Mungu, mila ambazo hawa waaminio wapya katika Korintho walitokea. Hawa wamekulia kwenye zinaa ya kupita kiasi. Hata hivyo, tambua kwamba aya hii pia inataja njia ambazo kwazo Wakristo hushugulikia dhambi maishani mwao —toba (kama vile 1 Yohana 1:9; Zab. 19:12-14). Imani na toba vyote viwili ni vile vinavyotendeka mwanzoni na ni uzoefu endelevu wa kiroho katika maisha ya Mkristo.
Orodha hii inaweza kuaksi vitendo vya walimu wa uongo ambao wanatia mkazo mtindo wa Kiyunani na ujuzi wa kutumia maneno ili yavute wasikilizaji hadharani, jambo ambalo linaonyesha kwamba pia walikuwa wanashirikishwa na mafundisho ya Kiyunani ya kimafunuo, yanayosisitiza elimu, lakini yanashusha tabia ya uadilifu. Maneno haya yote yameorodheeshwa kwenye dhambi ambazo Paulo ameziita za mwili katika Wagalatia Gal. 5:19. Kuhesabiwa haki lazima kusitengwe na hakuwezi kutengwa na utakatifu!

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa usomaji wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako binafsi ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika nuru tuliyonayo. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hupaswi kumwachia kazi hii mfasiri.
Maswali haya ya kujadili yanatolewa kukusaidia mambo muhimu ya kipengele cha kitabu hiki. Yamekusudiwa kukuchokonoa mawazo na sio ya mwisho.

1. Kwa nini Paulo anataja mafunuo yake ya kipekee na kisha hatuelezi kuyahusu?
2. Kwa nini udhaifu ni ufunguo kuelekea kwenye kutumika?
3. Mungu hutumia uovu kukamilisha maksudi yake?
4. Kwa nini Paulo alikuwa mgumu kupokea fedha kutoka kanisa hili? (kama vile 2 Kor. 12:20-21).

# 2 WAKORINTHO 13

| MGAWANYO WA AYA WA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **UBS[4]** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB** |
| Maonyo na Salama za Mwisho | Kuja na Mamlaka | Wito wa kujipima na kujisahihisha | Maonyo na Salamu za Mwisho | Hofu na wasiwasi wa Paulo |
| | | (12:19-13:10) | | (12:19-13:10) |
| 13:1-4 | 13:1-6 | 13:1-4 | 13:1-4 | 13:1-4 |
| 13:5-10 | Paulo anawashtaki watu wa Mataifa | 13:5-10 | 13:5-10 | 13:5-10 |
| | 13:7-10 | | | |
| | Salamau na Baraka | Hitimisho | | Hitimisho |
| 13:11-12 | 13:11-14 | 13:11-12 | 13:11 | 13:11 |
| | | | 13:12a | 13:12 |
| | | | 13:12b | |
| 13:13 | | 13:13 | 13:13 | 13:13 |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (Kutoka" Mwongozo Mzuri wa Usomaji Biblia" (A Guide to Good Bible Reading)

### *KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Haya ni maoni ya mwongozo kwa kujisomea, ikiwa na maana kuwa unawajibika binafsi kwa tafsiri ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Biblia na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mtoa maoni tu.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

13. Aya ya kwanza
14. Aya ya pili
15. Aya tatu
16. N.k

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 2 WAKORINTHO 13:1-4**

**[1] Hii ndiyo mara ya tatu ya mimi kuja kwenu. KWA VINYWA VYA MASHAHIDI WAWILI AU WATATU KILA NENO LITATHIBITISHWA.[2] Nimetangulia kuwaambia; na, kama vile nilipokuwapo mara ya pili, vivyo hivyo sasa nisipokuwapo, nawaambia wazi wao waliotenda dhambi tangu hapo, na wengine wote, ya kwamba, nikija, sitahurumia; [3] kwa kuwa mnatafuta dalili ya Kristo, asemaye ndani yangu, ambaye si dhaifu kwenu, bali ana uweza ndani yenu. [4] Maana, alisulibiwa katika udhaifu, lakini anaishi kwa nguvu za Mungu. Maana sisi nasi tu dhaifu katika yeye; lakini tutaishi pamoja naye kwa uweza wa Mungu ulio kwenu.**

**13:1 “Hii ndiyo mara ya tatu ya mimi kuja kwenu”** Hii hutoa utambulisho wa ki-muktadha kwa nadharia ya Paulo yenye maumivu kutembelea Korintho kati ya uandishi wa 1 na 2 Wakorintho (kama vile 2 Kor.12:14). Ziara hii haikuandikwa katika kitabu cha Matendo.

◙ “**KILA NENO”** Hii huanza na nukuu kutoka Kumb.19:15 (kama vile Hes. 35:30; Kumb. 17:6; Mt. 18:16; 1 Tim. 5:19), ambayo hujishughulisha na utaratibu wa Mahakama. Je inarejelea kwenye nini katika sura hii? Kuna uwezekano wa aina mbili.

1. Hurejea kwa tathmini ya Paulo juu ya kanisa. Alikwisha kuwa pale mara mbili na alishiriki nao. Waliwajibika na wangetoa hesabu kama wasikilizaji wa ukweli.
2. Hurejea kwa nidhamu ya kanisa inayohusiana na kikundi ndani ya kanisa
    a. Vikundi vya kiitikadi vya 1 Kor. 1-4 (kama vile 2 Kor. 12:20)
    b. Kikundi cha waasherati (kama vile 2 Kor. 12:21)
    c. Neno “mitume waliotukuka”au Walimu wa mafundisho ya uongo walikuwa na uhusiano na Yerusalemu pamoja na kule Uyahudi (kama vile sura ya 10-13, hasa 11:13-15)

**NASB "litathibitishwa"**
**NKJV "litaanzishwa"**
**NRSV "litaendelezwa"**
**TEV "litatatuliwa"**
**NJB "litahitajika"**

Muundo wa KITENZI hiki ni KAULI TENDEWA ELEKEZI YA WAKATI UJAO (kama vile NKJV), lakini Barbara na Timothy Friberg, *Analytical Greek New Testament*, uk 573, wanasema inafanya kazi kama KAULI TENDEWA SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFU (kama vile NRSV, NJB). Angalia Mada Maalum: Simama (*Histēmi*) katika 1 Kor. 15:1.

**13:2 "wao waliotenda dhambi tangu hapo, na wengine wote"** Hii inaonekana kuhusisha makundi mawili. La kwanza “wale waliokwisha tenda dhambi huko nyuma” (KAULI TENDAJI ENDELEVU YA WAKATI TIMILIFU), lazima irejelee kwa wale waaminio katika Korintho waliomsikia Paulo mara mbili, lakini bado waliendelea kuasi uongozi wake. Hili lingekuwa lile kundi la kiitikadi la 1 Wakorintho 1-4 au kundi la waasherati (kama vile 2 Kor. 12:20-21; 1 Wakorintho 5).

Kifungu cha maneno “na wengine wote” kinaonekana kuwahusisha wale ambao hawakuwepo nyakati zote mbili, yawezekana mitume wa uongo kutoka Yerusalemu na wale wanaowaunga mkono, ambao ni walengwa wa sura ya 10-13. Hata hivyo, makundi yote mawili wanatahadharishwa kwamba Paulo anawataka washughulikie matatizo hayo lakini ikiwa hawatafanya hivyo, yeye atayashughulikia!

◙ **"ikiwa"** Hii ni SENTENSI YENYE MASHARTI DARAJA LA TATU, lakini imetumika katika maana ya “ikiwa” (kama vile Yohana 16:7 na 1 Yohana 3:2).

◙ **"sitahurumia"** Paulo hutumia neno hili kwa maana chanya katika 1 Kor. 7:23 na 2 Kor. 1:23, lakini kwenye maana ya ki-mahakama hapa na katika 2 Kor. 12:6 (kama vile Kor. 10:11).

**13:3 "dalili"** Dhana hii ya kujaribu inarudiwa rudiwa katika muktadha huu. Kuna muendelezo wa dhihaka kati ya vdokezo viwli vya maneno ya Kiyunani, *dokimazō* na *peirazō*.

1. mst. 3, dalili- *dokimē* (kama vile 2 Kor. 2:9; 8:2; 9:13; 13:3)
2. mst. 5, Jijaribuni - *peirazō* (kama vile 2 Kor. 13:5)

3. mst. 5, jithibitisheni - *dokimazō* (kama vile 2 Kor. 8:8,22; 13:5)
4. mst. 5, mmekataliwa – *adokimos*
5. mst. 6, msikataliwe – *adokimos*
6. mst. 7,kukubaliwa - *dokimos* (kama vile 2 Kor. 10:18)
7. mst. 7, kutokukubaliwa – *adokimos*

Kwa usomaji wa neno kamili angalia Mada Maalum katika 1 Kor. 3:13.

◙ **"ya Kristo, asemaye ndani yangu"** Wengine katika Korintho walikuwa wanapinga mamlaka ya Paulo. Walikuwa "wanamjaribu" Paulo! Katika 2 Kor. 13:5 Paulo atawajaribu! Uwepo wa Kristo ndani ya Paulo ulikwisha kuthibitishwa (kama vile 2 Kor. 12:12).

◙ **"si dhaifu"** Udhaifu ni njia ya Mungu kuelekea ushindi kama ilivyo wekwa wazi katika maisha ya Yesu (kama vile 2 Kor.13:4) na maisha ya Paulo (kama vile 2 Kor. 10:1, 11; 12:9; 13:9). Hakuna mwanadamu atakaye jisifu mbele za Mungu kwa habari ya kufanikisha kwenye mambo ya Kiroho ambayo moja kwa moja ni matokeo ambayo yanatoka kwa Mungu na sio sisi ni nani. Ni rasilimali za Mungu ndizo zinakamilisha matokeo ya Kiroho! Waaminio wanapaswa kuruhusu nguvu yake itiririke kupitia uhitaji wao na kutokuwa na msaada kwao. Angalia MADA MAALUM: UDHAIFU (SPECIAL TOPIC: WEAKNESS) katika 2 Kor. 12:9.

Mstari wa 3-4 ni muhtasari wa kinyume cha kiburi cha usemaji wa walimu wa mafundisho ya uongo. Walidai ukuu kutoka

1. jamii ya ukoo
2. Uzoefu binafsi wa kipaji
3. Upotoshaji mkuu, mafunzo ya usemaji
4. Kujilinganisha na wengine

◙ **"kwenu. . . ndani yenu"** Huu UWINGI wa neno "ninyi" huonesha kwamba Paulo anarejelea kwenye uzoefu wa ki-kusanyiko, na sio uzoefu binafsi (kama vile 2 Kor. 13:5). Yawezekana tafsiri ya toleo la TEV, "miongoni mwenu" linaleta ladha.

**13:4 "alisulibiwa"** Paulo hutumia maneno kadhaa kufafanua kifo cha Yesu:

1. Kifo ( kama vile Rum. 5:6,nakuendelea; 8:34; 14:15; 1 Kor. 8:11; 15:3; 2 Kor. 5:15; Gal. 2:21; 1 The. 4:14; 5:10)
2. Damu (kama vile 1 Kor.1:17-18; Gal. 5:11; 6:12,14; Efe. 2:16; Flp. 2:8; Kol. 1:20; 2:14)
3. Kusulibiwa (kama vile 1 Kor. 1:23; 2:2; 2 Kor. 13:14; Gal. 3:1)

◙**"lakini anaishi kwa nguvu za Mungu"** Ni vifungu vya maneno kama hivi vilivyosababisha mabishano ya thiolojia yanayohusu Kristo katika kanisa la kwanza. Je! Yesu sio Mungu pia? Je! Mtu huyu Yesu anaishi kwa nguvu ya Uungu tofauti (yaani, YHWH)? Mtu hawezi kujenga uelewa wa kiutaratibu juu ya mstari mmoja na mistari iliyochaguliwa, lakini lazima ajaribu kuziunganisha ziwe kitu kizima kilichofungamanishwa. Angalia Mada Maalum: Imani ya uwepo wa Mungu mmoja tu katika 1 Kor. 8:4.

Kwa kawaida istilahi ya mstari huu hutumika kuthibitisha kwamba Mungu Baba, kama mtendaji wa idhini, alimfufua mwana ( kama vile Matendo 2:24; 3:15; 4:10; 5:30; 10:40; 13:30,33,34,37; 17:31; Rum. 1:4; 6:4,9; 8:11; 10:9; 1 Kor. 6:14; 2 Kor. 4:14; Gal. 1:1; Efe. 1:20; Kol. 2:12; 1 The. 1:10). Hata hivyo, kuna maandiko mengine yaliyovuviwa yanayothibitisha kuwa (1) Roho alimfufua mwana (kama vile Rum. 8:11) au (2) Mwana alijifufua Mwenyewe (kama vile Yohana 2:19-22; 10:17-18).

◙ **"sisi nasi tu dhaifu katika yeye; lakini tutaishi pamoja naye"** Uelewa wa Paulo kuhusu Ukristo ulikuwa kitambulisho cha waaminio katika uhai, kifo, na ufufuo wa Yesu. Kama alivyoishi maisha ya unyenyekevu, upole, na maisha ambayo watu waliyaelewa visivyo, ndivyo nasi tutaishi; kama alivyokufa akiwatumikia wengine, ndivyo itupasavyo nasi tuwe (yaani, uhai mpya sasa) na ndivyo tutakavyo kuwa (yaani ufufuo wa mwili atakavyokuja Mara ya Pili).
Thiolojia ya utambulisho iko dhahiri sana katika Warumi 6. Paulo aliwaandikia Warumi alipokuwa anashughulikia Korintho. Uelewa wa Mfumo wa Paulo wa Ukristo (yaani, Warumi) uliondolewa katika hali ya mwili alipokuwa anafanya kazi na kanisa hili ambalo lilikuwa halienendi inavyostahili.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 2 WAKORINTHO 13:5-10**
**5 Jijaribuni wenyewe kwamba mmekuwa katika imani; jithibitisheni wenyewe. Au hamjijui wenyewe, kwamba Yesu Kristo yu ndani yenu? Isipokuwa mmekataliwa. 6 Lakini natumaini kama mtajua ya kuwa sisi hatukukataliwa. 7 Nasi twamwomba Mungu, msifanye lo lote lililo baya; si kwamba sisi tuonekane tumekubaliwa, lakini ninyi mfanye lile lililo jema, tujapokuwa sisi tu kama waliokataliwa. 8 Maana hatuwezi kutenda neno lo lote kinyume cha kweli, bali kwa ajili ya kweli. 9 Maana twafurahi, iwapo sisi tu dhaifu, nanyi mmekuwa hodari. Tena twaomba hili nalo, kutimilika kwenu. 10 Kwa sababu hiyo, naandika haya nisipokuwapo, ili, nikiwapo, nisiutumie ukali kwa kadiri ya uwezo ule niliopewa na Bwana, kwa kujenga wala si kwa kubomoa.**

**13:5 "Jijaribuni"** Hii ni KAULI TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO. Hili ni neno *peirazō*, ambalo humaanisha "kujaribu kukiwa na mtazamo wa uharibifu" Angalia maelezo kamili katika 1 Kor. 3:3. Walikuwa wamekwisha kumjaribu Paulo, sasa lazima wajijaribu wenyewe!

◙ **"Ikiwa"** Hii ni SENTENSI YENYE MASHARTI DARAJA LA KWANZA, ambayo inachukuliwa kuwa kweli. Paulo hatilii mashaka imani yao, bali anawahamasisha waamke!

◙ **"imani"** Neno la Kiyunani "imani" (*pistis*) limetafsiriwa kwa kiingereza katika maneno matatu: imani, amini ama tumaini. Angalia Mada Maalum katika 1 Kor.2:4. Imani imetumika katika maana tatu katika Agano Jipya (1) mtu binafsi kumkubali Yesu kama Kristo wa Mungu; (2) kama anayeishi kwa uaminifu kwa ajili yake; na (3) kama mwili wa kweli kuhusu yeye (kama vile 2 Kor. 13:3; Gal. 1:23; 3:23-25). Ukristo uliokomaa unahusisha maana zote tatu.

◙ **"jithibitisheni wenyewe"** Paulo anarudia agizo lake (yaani, KAULI TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO nyingine), lakini anatumia neno jingine (yaani, *dokimazō*) kwa kujaribu, ambayo inaonyesha kujaribu kwa mtazamo wa kuelekea kupewa kibali. Angalia Mada Maalum katika 1 Kor. 3:13.

◙ **"hamjijui"** Hili ni neno la Kiyunani *epigniōskō* (yaani, KAULI TENDAJI ELEKEZI YA WAKATI ULIOPO), ambayo kwa kawaida huonyesha ujuzi wa uzoefu kamili.

◙ **"Yesu Kristo yu ndani yenu"** Kama 3 Kor. 13:4 iliyolenga kwenye mwonekano wa pamoja, kifungu hiki cha maneno ( kikitumia KIHUSISHI kile kile na KIWAKILISHI NOMINO CHA UWINGI ) chaweza kurejelea kwenye kipengele binafsi zaidi. Kristo kwa hakika yu miongoni mwa watu wake, lakini pia ndani ya kila mmoja wa watu wake. Huduma za Yesu na za Roho zinahusiana kwa karibu kiasi kwamba mara nyingi Roho anaitwa Roho wa Kristo (kama vile Rum. 8:9; 1 Pet. 1:11). Yesu hata anasema kukaa ndani ya waaminio ( kama vile Yohana 14:23; Rum. 8:10; Kol. 1:27. Pia tazama Mt. 28:20) Angalia MADA MAALUM: YESU NA ROHO (SPECIAL TOPIC: JESUS AND THE SPIRIT katika 2 Kor. 3:17.

◙ **"Isipokuwa mmekataliwa"** Kifungu hiki cha maneno ni ufanano na " ikiwa mu katika imani" katika 2 Kor. 13:5. Paulo amekwisha kusema kwa njia kadhaa (yaani, SENTENSI YENYE MASHARTI DARAJA LA KWANZA katika 2 Kor. 13:5 na matumizi ya *dokimazō*) kwamba anaamini wasomaji wake ni waaminio, lakini sio wote. Kuna uwezekano

wa kuwepo walimu wa uongo wasiomjua Kristo (angalia MADA MAALUM: UTUME (APHISTĒMI)    ( SPECIAL TOPIC: APOSTASY*(APHISTĒMI)* katika 1 Kor. 6:9). Kishazi hiki kinawahusu.

Kishazi hiki hakihusishi waaminio watendao dhambi kwa sababu Paulo anawatambulisha katika 2 Kor. 12:20-21. Wanahitaji kutubu, lakini walimu wa uongo wanamhitaji Kristo (kama vile Mathayo 7).

Paulo alitumia neno hili hili katika 1 Kor. 9:27 kama sababu iliyomfanya apambane kujiweka chini ya utawala wa Mungu. Paulo hakutaka "kuondolewa ustahili" ama kukataliwa. Waaminio wanapewa changamoto ya kujikagua mwenyewe (kama vile Flp. 2:12).

**13:6** Paulo anasema kwamba yeye pamoja na wasaidizi wake wamekwisha kushinda jaribio (yaani, sio wa bandia, *adokimos*, kama vile 2 Kor. 13:7) hasa katika uhusiano wa kanisa katika Korintho. Ikiwa mwanaye Kristo akikaa ndani yao, basi huduma ya Paulo ilikuwa yenye matatizo yaliyotarajiwa.

**13:7** Kwa namna fulani kwa kanisa lenye nguvu huko Korintho lingalithibitisha uongozi wa Paulo na sifa ya Utume wake. Yeye anahusika zaidi kwamba wafanye kile kilicho haki na stahiki kwa sababu ya Mungu na injili, sio tu kumwonyesha hali za utambulisho wa Paulo ama kuthibitisha uongozi wake (kama vile 2 Kor. 13:9).

◙ **"tumekubaliwa. . . waliokataliwa"** Paulo anaendeleza dhihaka hii kwenye maneno *dokimos* na *adokimos*.

**13:8** Ukweli kwenye muktadha huu hurejelea kwenye injili kama mtu (yaani Yesu Masihi), kama ujumbe (yaani, injili kumhusu Yesu), na kama matendo ya maisha (yaani kufuatisha ama kuiga maisha ya Yesu).

**MADA MAALUMU: "UKWELI" KATIKA MAANDIKO YA PAULO   (SPECIAL TOPIC: "TRUTH" IN PAUL'S WRITINGS)**

**13:9 "Maana twafurahi, iwapo sisi tu dhaifu, nanyi mmekuwa hodari"** Hii ni kweli kinzani ya Paulo. Anajua kwamba nguvu ya Kristo huachiliwa kupitia udhaifu wa binadamu (kama vile 2 Kor. 12:10; 13:4). Kwa hiyo, yeye huhitaji kubaki mdhaifu. Hata hivyo, kwa kanisa la Korintho kuwa na nguvu hata lenyewe pia lazima liwe dhaifu. Hii ni kinyume sana na watu wanavyotathmini maisha. Walimu wa uongo wamekwisha kudai nguvu kwa njia ya elimu, nasaba, uzoefu, lakini Paulo anatetea nguvu kwa njia ya mfano wa Kristo (kama vile 2 Kor. 13:4).

◙ **"kutimilika kwenu"** Muundo wa NOMINO wa neno hili hili unapatikana hapa tu katika Agano Jipya. KITENZI hiki kinamaanisha "unga pamoja." Paulo alitumia muundo wa KITENZI katika 1 Kor. 1:10, ambacho kinaagiza kanisa la Korintho kumaliza migawanyiko yao ya vikundi vya ki-itikadi. Sasa mwishoni mwa 2 Wakorintho anarudi kwenye agizo hili (yaani, umoja utakaoishia kwenye kuwepo kwa maisha ya Kiroho).

Louw na Nida, *Greek-English Lexicon of the New Testament*, juzuu. 1, uk. 680, hudai kwamba *artios* (yaani, kamili, ya kutosha, iliyoandaliwa kwa ajili ya kazi aliyotolewa), pamoja na tofauti zake zote za viambati vya kihusishi yaaani, *epi* na *kata*), yote ni yenye maana sawa (kama vile Luka 6:40; 2 Kor. 13:9,11; Efe. 4:12; 2 Tim. 3:17).

Paulo anataka kanisa ambalo linatenda kazi, lenye muungano, na upendo katika Korintho (kama vile 2 Kor. 13:11). Ili jambo hili litendeke lazima kuwepo na msamaha, upatanisho pamoja na nidhamu ya kanisa (kama vile Gal. 6:1).

**13:10** Paulo hakutaka kufanya ziara yenye maumivu tena kule Korintho (kama vile 2 Kor. 2:3-4). Hakutaka kuja amefungashwa ndani ya mamlaka yake ya Kitume, bali katika upendo wa mzazi. Hata hivyo, mwitikio wa kanisa ndio uliamua jinsi ambavyo atakavyo lazimika kutenda.

◙ **"kwa kadiri ya uwezo ule niliopewa na Bwana"** Kifungu hiki hasa cha maneno huonekana katika 2 Kor. 10:8. Mamlaka hii ya Kitume, iwe ni kuwepo kiuhalisia ama kutoka mbali (kama vile 1 Kor. 5:4), kuna mamlaka ya Kristo (kama vile 2 Kor. 12:19; 13:3). Mamlaka hii ilitolewa kwa Paulo katika tukio lile la njiani akielekea Dameski (kama vile Mdo. 9, 22,26).

◙ **"kwa kujenga"** Angalia Mada Maalum: Adilisha katika 1 Kor. 8:1.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 2 WAKORINTHO 13:11-13**
**11 Hatimaye, ndugu, kwaherini; mtimilike, mfarijike, nieni mamoja, mkae katika amani; na Mungu wa upendo na amani atakuwa pamoja nanyi. 12 Salimianeni kwa busu takatifu. 13 Watakatifu wote wawasalimu.**

**13:11 "Hatimaye"** Ki-uhalisia hili neno ni "kwa wengine wote" (kama vile Gal. 6:17). Hii ni sifa ya kuhitimisha kifungu cha maneno kwa Paulo (kama Efe. 6:10; Flp. 3:1; 4:8; 2 The. 3:1), kwa kawaida huwa kinaweka alama ya mpito kuelekea mwisho wa wazo kuu.

◙ **"ndugu"** Ni njia nzuri na ya kufariji kiasi gani kuhitimisha barua hii ngumu kwa kanisa hili lenye matatizo. Pia inatumika kama chombo cha ki-fasihi cha kuashiria mapito kuelekea somo jipya.

◙ Kuna mfuatano wa kauli tano SHURUTISHI ZA WAKATI ULIOPO.

1. "furahia" (KAULI TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO). Paulo mara nyingi hutumia neno hili katika 2 Wakorintho (kama vile 2 Kor. 2:3; 6:10; 7:7,9,13,16; 13:9,11). Neno hili linaweza kumaanisha "kwa heri" (kama vile Flp. 3:1; 4:4), lakini hili halitoshelezi mifuatano ya KAULI SHURUTISHI.
2. "mkamilishwe" (KAULI TENDEWA SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO). Hili huzungumzia umoja na huduma (kama vile mst.9).
3. "farijiweni" (KAULI TENDEWA SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO). Paulo hutumia neno hili mara nyingi katika 2 Wakorintho (kama vile 2 Kor. 1:4,6; 2:7,8; 5:20; 6:1; 7:6,7,13; 8:6; 9:5; 10:1; 12:8,18; 13:11).
4. "iweni na nia moja" (KAULI TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO). Neno hili la kiyunani lina vidokezo vingi (kama vile Louw na Nida, juzuu. 2, uk. 259), lakini katika muktadha huu lina ufanano na "mkamilishwe." Hii inarejelea umoja kwa kusudi la injili. Hii haimaanishi kwamba waaminio lazima wakubaliane katika kila hoja bali lazima wasikubaliane huku wakiendelea kupendana na kwamba injili lazima ipewe kipaumbele juu ya uchaguzi au upendeleo wa mtu binafsi!
5. "ishi kwa amani" (KAULI TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO). Hii kwa hakika inaaksi 1 Wakorintho 1-4 na 2 Wakorintho 10-13. Hakuna uthibitisho wa jinsi matatizo haya yanahusiana, lakini yote mawili yalisababisha utengano na ukinzani. Paulo anaamuru amani, sio kwa maafikiano bali kwa mfanano wa Kristo. Mungu wa amani (kama vile 2 Kor.13:11) atatusaidia katika udhaifu wetu!

◙ **"Mungu wa upendo na amani"** Ni sifa gani ya kustaajabu kiasi gani inayoweza kuelezeka kwa YHWH. YHWH mara nyingi imeunganishwa na "amani" (kama vile Rum. 15:33; 16:20; 1 Kor. 14:33; Flp. 4:9; 1 Thes. 5:23; Ebr. 13:20). Yeye anaitwa "Bwana wa amani" katika 2 The.3:16. Upendo na amani vyote viwili vimetajwa katika Efe. 6:23.

Waaminio wanapaswa waige tabia hizi katika uhusiano wao wenyewe kwa wenyewe.

**13:12 "Salimianeni"** Hii inaweza kutafsiriwa "takia heri" (kama vile Mdo. 20:1; 21:6). Ina wasilisha mtazamo wa kukubalika na ushirikiano. Mtazamo ulio kinyume chake unafafanuliwa katika Mt. 5:47.

Kwa muda kidogo tu kuhusu kuweka namba kwenye mistari hii miwili ya mwishoni. Baadhi ya tafsiri za kiingereza zinamaanisha 2 Kor. 13:12-13 (TEV, NJB, RSV, NRSV), wakati nyingine zinagawa neno hilo katika mistari miwili (KJV, NKJV, NASB, NIV).

◙ **"busu takatifu"** Mila hii (yaani, miongoni mwa wanafamilia na marafiki) baadaye ilisimama kwa sababu ya kuchanganya na kutokuelewa kwa wapagani (yaani, Kubusu kwa nia ya mapenzi ya kikahaba). Katika kanisa la awali wanaume walikuwa wanawabusu wanaume na wanawake waliwabusu wanawake ( yaani, kufuatisha mila ya sinagogi, kama vile Rum. 16:16; 1 Kor. 16:20; 1 The. 5:26). Angalia maelezo katika 1 Kor.16:20.

Hii ni KAULI SHURUTISHI. Je inamaanisha kwamba wakristo lazima wasalimiane kwa mtindo huu uliodhahiri? Hapa ndipo kuna mfano mzuri wa jinsi gani mila na mazingira ya wakati ujao lazima uathiri fasiri. Muundo sio hoja, bali mtazamo. Waaminio ni familia.

**13:13 "Watakatifu wote"** Kifungu hiki cha maneno hakirejelei kwa Paulo pekee na timu yake ya umisionari, bali "watakatifu wote" (yaani makanisa yote ya Paulo). Kulikuwepo na mgogoro kati ya kanisa la Korintho na haya makanisa mengine.. Kulikuwepo matangazo ya hali ya kuwa wakubwa kuhusu kanisa hili. Paulo anatambulisha suala hili kwa kutaja mara kadhaa viwango alivyofundisha katika makanisa yote (kama vile 1 Kor.4:17; 7:17; 11:16,34: 14:33) Korintho lazima iwe sehemu ya familia, sio mshirika msomi aliyepata upendeleo. Angalia MADA MAALUM: WATAKATIFU (SPECIAL TOPIC: SAINTS) katika 1 Kor. 1:2.

Katika mzozo wao wa wakati uliopo, makusanyiko yote yaliyoanzishwa na Paulo yalituma salamu zao, jambo linaloonyesha ushirika, kuhusika, ushirikiano, maombi na kukubaliana.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 2 WAKORINTHO 13:14**
**14 Neema ya Bwana Yesu Kristo, na pendo la Mungu, na ushirika wa Roho Mtakatifu ukae nanyi nyote.**

**13:14** Paulo kila mara huhitimisha barua zake kwa maombi na kutoa Baraka, lakini katika barua hii ni ya kipekee. Inaunganisha vipengele vitatu vya sifa ya Mungu pamoja na watu watatu wa Utatu. Pia sio kawaida Yesu kutajwa kwanza. Kwa maelezo kamili kuhusu "Utatu" angalia Mada Maalum katika 1 Kor. 2:10. Vipengele vitatu vya Mungu: neema, upendo na ushirika, ni kwa waaminio "wote" katika Korintho. Hii ni sehemu muhimu sana ya maombi. Paulo anataka kurejesha umoja miongoni mwa waaminio pia akiwatambua na kuwakataa waamini wa uongo.
Paulo alitumia mwandishi kuandika barua zake, lakini huenda aliandika sala ya mwisho yeye wenyewe (kama vile 2 The. 3:17) Paulo alilipenda kanisa lake!

◙**" ushirika wa Roho Mtakatifu "** Angalia Mada Maalum katika 1 Kor. 1:9 na 12:11.

## MASWALI YA MJADALA

Haya ni maoni ya mwongozo kwa kujisomea, ikiwa na maana kuwa unawajibika binafsi kwa tafsiri ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mtoa maoni tu.

Maswali haya ya kujadili yanatolewa ili kukusaidia kufikiri mambo muhimu yaliyoko katika kipengele cha kitabu hiki. Yanamaanisha kuwa maswali ya kichokonozi, yasio ya hakika.

1. Waaminio wanajijaribu wenyewe?
2. Kwa nini Paulo anazungumza mara kwa mara katika sura ya 11-13 kuhusu udhaifuwake?
3. Je ni jinsi gani imani ilihusianishwa na ustahimilivu?
4. Je ni jinsi gani Mungu anaweza kuwa nafsi moja na nafsi tatu kwa wakati huo huo?

# TAFASIRI SAHIHI ZA ISTILAHI ZA VISARUFI VYA KIYUNANI

Lugha ya kawaida ya Koine mara nyingi inafahamika kama Kiyunani kilichobobea, ilikuwa ni lugha ya kawaida ya ulimwengu wa Meditarania ilianzishwa na Alexanda mkuu (336-323 B.C) na ikadumu mpaka miaka ya (300 B.C-A.D 500). Haikuwa rahisi, Kiyunani kuwa cha daraja la juu, lakini kwa njia nyingi ni dhana ya Kiyunani ambayo ilikuja kuwa lugha ya pili karibu na mashariki ya kale na ulimwengu wa Mediterania.

Kiyunani cha Agano Jipya kilikuwa ni cha kipekee kwa njia kadhaa kwa watumiaji wake, isipokuwa Luka mwandishi wa kitabu cha Waebrania, yamkini alitumia lugha ya Kiarama kama lugha ya msingi. Kwa hiyo, uandishi wao uliathiliwa na dhana ya muundo wa Kiarama. Pia, walisoma na kunukuu wandishi wa maandiko ya kale (tafasiri ya Kiyunani ya maandiko ya kale) ambayo pia yaliandikwa kwa lugha ya Koine. Lakini maandiko ya kale pia yaliandikwa kwa wasomi wa Kiyahudi ambao lugha yao ya asili ilikuwa sio ya Kiyunani.

Hii ilisaidia kuwa kama kumbukumbu ambayo haiwezi kulipeleka Agano Jipya kwenye muundo mgumu wa kisarufi. Ni wa kipekee na bado una mambo mengi yaliyo pamoja na (1) maandiko ya kale (2) maandiko ya kale kama yale ya Yusufu na (3) mafunjo yaliyopatikana Misri. Kwa hiyo tunakabilianaje na uchambuzi wa visarufi vya Agano Jipya.

Muundo wa kisarufi wa lugha ya Koine na Agano Jipya la lugha ya Koine ulibadilika. Kwa njia tofauti ulikuwa ni urahisishaji wa sarufi. Mazingira ndio yatakuwa mwongozo wetu mkuu. Maneno pekee yana maana katika upanuzi wa mazingira, kwa hiyo, muundo wa kisarufi unaweza tu kueleweka katika mwanga wa (1) aina mahsusi ya mwandishi, na (2) mazingira mahsusi

Hapana hitimisho la fasiri ya dhana na muundo wa Kiyunani unaowezekana. Kimsingi lugha ya Koine ilikuwa ni lugha ya maneno tu. Mara nyingi msingi wa utafasiri ni aina na dhana ya maneno. Mara nyingi vishazi vikuu hutokea kwanza, vikionyesha kushinda vingine vyote. Katika kueleza kitenzi cha Kiyunani, vipande vitatu vya habari lazima vizingatiwe (1) kiini cha msisitizo wa njeo, sauti na dhamira (tukio au umbo); (2) kiini cha maana husika ya kitenzi (usawidi kamusi); na (3) mtiririko wa mazingira yenyewe (isimu ya mpangilio wa maneno)

## I. NJEO

A. NJEO au sura inajumuisha uhusiano wa VITENZI ili kukamilisha kitendo au kutokamilisha kitendo. Mara nyingi huitwa “utimilifu” au “utoutimilifu”
   1. Njeo timilifu zinaangazia juu ya utoaji wa kitendo. Hakuna taarifa nyingine zilizotolewa isipokuwa ya kile kilichotokea! Kuanza kwake, mwendelezo au ukomo wake haukueiezwa.
   2. Njeo zisizo timilifu zinaangazia juu ya mchakato endelevu wa kitendo. Zinaweza kuelezewa dhidi ya unasaba wa kitendo, kudumu kwa kitendo, mwendelezo wa kitendo, n.k.

B. Njeo zaweza kugawanywa kwa jinsi mwandishi anavyoona kitendo kinavyoendelea.
   1. Kimetokea-KITENZI TIMILIFU
   2. Kilivyotokea au matokeo yake-KITENZI CHA WAKATI ULIOPITA
   3. Kilivyokuwa kikitokea nyuma na matokeo yake yakastahimili, lakini sio sasa-KITENZI CHA WAKATI ULIOPITA TIMILIFU
   4. Kinatokea –WAKATI ULIOPO
   5. Kilikuwa kikitokea- WAKATI USIOTIMILIFU
   6. Kitatokea –WAKATI UJAO

Mfano thabiti wa jinsi njeo hizi zinasaidia katika utafasiri ungalikuwa wa neno “okoa.” Lilitumika katika NJEO nyingi tofauti kuonyesha kwa pamoja mchakato na ukomo.

1. KITENZI CHA WAKATI TIMILIFU- “okolewa” (Rum 8:24)
2. KITENZI CHA WAKATI ULIOPITA- “ameokolewa na matokeo yake yanaendelea” (Efe 2:5,8)
3. KITENZI CHA WAKATI ULIOPO- “anaokolewa” (cf. 1Kor 1:18; 15:2)
4. KITENZI CHA WAKATI UJAO- “ataokolewa” (cf. Rum 5:9,10; 10:9)

C. Katika kuzingatia juu ya VITENZI VYA NJEO, mfasiri huangalia sababu za mwandishi wa kwanza alichagua kuelezea yeye binafsi NJEO fulani. Tarajio la NJEO “hakuna madoido” lilikuwa ni la KITENZI CHA WAKATI TIMILIFU. Kilikuwa ni muundo wa KITENZI cha kawaida “kisichoainishwa” “kisichotambulika” “kisichochoka.” Chaweza tumika katika Nyanja pana ambamo mazingira lazima yaelezee. Kwa kawaida kilikuwa kinaelezea kuwa kitu fulani kimetendeka. Sura ya muda uliopita ulikusudia tu katika DHAMIRA ELEKEZI. Kama pana NJEO nyingine zilizotumika, uainishaji wa kitu fulani ulikuwa unasisitizwa. Lakini ni nini?
   1. NJEO YA WAKATI ULIOPITA. Hii inaongelea juu ya tendo lililokwisha tendeka na matokeo yakiendelea kuwepo. Katika namna fulani ilikuwa ni muunganikano wa NJEO ZA WAKATI TIMILIFU na ZA WAKATI ULIOPITA. Mara kwa mara mlengo ulikuwa juu ya matokeo yalioendelea kuwepo au kumalizika kwa kitendo. Mfano: Efe 2:5 & 8, “umekuwa na unaendelea kuokolewa.”
   2. NJEO YA WAKATI ULIOPITA AINISHI. Hii ilikuwa kama njeo ya WAKATI ULIOPITA isipokuwa matokeo yalishakoma. Mfano: “Petro alikuwa akisimama nje mlangoni” (Yoh 18:16)
   3. NJEO YA WAKATI ULIOPO. Hii inazungumzia juu ya kitendo kisichokiwisha au kisichotimilifu. Mtizamo mara nyingi ni juu ya uendelezaji wa tukio. Mfano: “kila mmoja ashikamanae ndani yake haendelei kutenda dhambi”, “kila mmoja aliyesamehewa na Mungu haendelei kutenda dhambi” (1Yoh 3:6 & 9).
   4. NJEO YA WAKATI USIOTIMILIFU. Katika njeo hii uhusiano na NJEO YA WAKATI ULIOPO ni mwendelezo wa uhusiano kati ya WAKATI ULIOPITA na WAKATI ULIOPITA AINISHI. WAKATI USIOTIMILIFU unaongea juu ya kitendo ambacho hakijaisha kutendeka ambacho kilikuwa kinatokea lakini sasa kimekoma au mwanzo wa kitendo awali. Mfano: “kwa hiyo Yerusalemu yote waliendelea kumwacha” au “ Yerusalemu yote wakaanza kumwacha”(Mt3:5)
   5. NJEO YA WAKATI UJAO. Hii inaongelea juu ya kitendo ambacho kawaida kilijitokeza ndani ya muda mwafaka. Inaangazia juu ya umuhimu wa jambo kutokea kuliko utokeaji wa uhalisia. Mara nyingi unazungumzia juu ya ualakini wa tukio. Mfano: “Heri wale….wata...”(Mt 5:4-9).

## II IRABU

A. Irabu inaelezea mahusiano kati ya kitendo cha KITENZI na KIIMA

B. IRABU TENDAJI ilikuwa ni njia ya kawaida, tarajiwa, isiosisitiza utetezi wa kwamba kiima kilikuwa kikitenda kitendo cha KITENZI.

C. IRABU TENDEWA ina maana kuwa KIIMA kilikuwa kikipokea kitendo cha KITENZI kilichotolewa na mtu wan je. Mtu wa nje anayetoa kitendo alionyeshwa katika Agano Jipya la Kiyunani kwa mambo na VIHUSISHI vifuatavyo:
   1. Mtu binafsi wa moja kwa moja wa *hupo* kukiwa na UHUSIKA WA KUONDOA (cf. Mt 1:22; Mdo 22:30)
   2. Mtu binafsi wa kati na *dia* kukiwa na UHUSIKA WA KUONDOA (cf. Mt 1:22)
   3. Mtu wa kawaida asiyehusika na *en* kukiwa na UHUSIKA WA JAMBO
   4. Wakati mwingine ni mtu binafsi au asiyehusika kukiwa na UHUSIKA WA JAMBO pekee.

D. IRABU YA KATI inamaanisha kuwa KIIMA kinatoa tendo la KITENZI na pia moja kwa moja kinahusishwa katika kitendo cha KITENZI. Mara nyingi huitwa irabu ya kurefusha matakwa binafsi. Muundo huu unasisitizia KIIMA cha kishazi au sentesi kwa namna nyingine. Muunganikano huu haupatikani katika

Kiingereza. Una uwezekano mpana wa maana na ufasiri katika Kiyunani. Baadhi ya mifano ya dhana hizi ni;

1. YENYE KUJIREJEA – kitendo cha moja kwa moja cha kiima chenyewe. Mfano: “kajiangika mwenyewe” (Mt 27:5)
2. YENYE KUTIA MKAZO- kiima kinazaa kitendo chake chenyewe. Mfano: “shetani mwenyewe anajifanya kama malaika wa nuru” ( 2Kor 11:14)
3. Kukubaliana – mwingiliano wa viima viwili. Mfano: “walishauliana wao kwa wao” (Mt 26:4)

## III. DHAMIRA (au “NAMNA”)

A. Kuna namna nne za DHAMIRA katika lugha ya Koine. Zinaashiria uhusiano wa KITENZI kuwa kweli, haswa ndani ya wazo la mwandishi mwenyewe. DHAMIRA hizi zinagawanyika katika namna pana mbili: ile inayoonyesha ukweli (ELEKEZI) na ile inayoonyesha umuhimu (UTEGEMEZI, KUAMURU/KUSHURUTISHA na HALI Y A UCHAGUZI).

B. DHAMIRA ELEKEZI ilikuwa ni NAMNA ya kawaida ya kuelekeza kitendo ambacho kimekwisha tokea au kilikuwa kinatokea, haswa kwenye wazo la mwandishi. Ilikuwa namna <u>pekee</u> ya Kiyunani ya kueleza ukomo wa muda na hata hapa sura hii ilikuwa daraja la pili.

C. DHAMIRA TEGEMEZI kinaelekeza yumkini kitendo kitakachotokea mbeleni. Kitu fulani ambacho hakijawahi tokea lakini nafasi ya kutokea ingaliwezekana. Ina vitu vingi vinavyofanana na KITENZI CHA WAKATI UJAO ELEKEZI. Utofauti ni kuwa UTEGEMEZI unaelezea kiwango fulani cha mashaka. Katika Kiingereza hii mara nyingi inaelezewa na neno “ingalikuwa”, “ingaliweza”, “yawezekana” au “yenye uwezo”.

D. DHAMIRA YA UCHAGUZI inaelezea utashi ambao kinadharia unawezekana. Ilifikiliwa ni hatua moja mbele kutoka katika ukweli kuliko HALI YA UTEGEMEZI. HALI YA UCHAGUZI inaelezea uwezekano chini ya hali fulani. HALI YA UCHAGUZI ilikuwa ni nadra katika Agano Jipya. Utumikaji wake mara nyingi kilikuwa ni kifungu maarufu cha Paulo. “yawezekana isiwe” (KJV, Mungu anakataza), kimetumika mara kumi na tano ( cf. Rum 3:4,6,31; 6:2,15; 7:7,13; 9:14; 11:1,11; 1Kor 6:15; Gal 2:17; 3:21; 6:14) mfano mwingine unapatikana katika Thes 1:38, 20:16, Mdo 8:20 na 1Thes 3:11

E. DHAMIRA SHURUTISHI inasisitizia juu ya amri ambayo iliwezekana, lakini msisitizo ulikuwa juu ya dhamira ya mnenaji. Inatetea juu ya uwezekano wa hiari na ilishurutishwa juu ya chaguzi za wengine. Kulikuwa na matumizi ya kipekee ya HALI YA KUSHURUTISHA katika maombi na hitaji la mtu wa tatu. Amri hizi zinapatikana tu katika WAKATI ULIOPO na njeo ya WAKATI TIMILIFU katika Agano Jipya.

F. Baadhi ya visarufi vinabainisha VIAMBATA kama moja aina ya NAMNA. Ni vya kawaida katika Agano Jipya la Kiyunani, mara nyingi vikielezewa kama KIVUMISHI CHA TENDO. Vinatafasiriwa kama muunganiko wa VITENZI vikuu ambavyo vinafanana. Tofauti pana iliwezekana katika utafasiri wa viambata. Ni vizuri kuzirejea tafasiri nyingi za Kiingereza. *The Bible in Twenty Six Translation* kilichochapishwa na Baker ni msaada mkubwa hapa.

G. KITENZI TENDAJI TIMILIFU ELEKEZI kilikuwa ni njia ya kawaida au “kisichotambulika” cha Kuingiza matokeo. Njeo nyingine, irabu au zilikuwa na ufasiri mahususi ambao mwandishi wa kwanza alihitaji kuwasilisha.

IV. Kwa mtu ambaye hayuko na uzoefu na lugha ya kiyunani, msaada wa usomaji unaofuata utatoa taarifa inayohitajika;

A. Friberg, Barbara na Timothy. Analytical Greek New Testament. Grand Rapids: Baker 1988
B. Marshall, Alfred. Interlinear Greek-English New Testament. Grand Rapids: Zondervan 1976
C. Mounce, William D. The Analytical Lexicon to the Greek New Testament. Grand Rapids: Zondervan 1993

D. Summer Ray. Essential of the New Testament Greek Nashville: Broadman 1950
E. Kitaaluma mtangamano wa kozi ya lugha ya Koine unapatikana kupitia taasisi ya Moody Bible iliyoko Chikago II

## V. NOMINO

A. Ki-isimu, NOMINO zinaainishwa kwa jambo. Jambo ni lile lililoshurutisha dhana ya NOMINO ambayo ilionyesha kuwa na uhusiano na KITENZI na sehemu nyingine ya sentesi. Katika lugha ya Koine kazi nyingi za uhusika zilionyeshwa na VIHUSISHI. Tangu dhana ya uhusika iliweza kutambua tofauti ya mahusiano mbali mbali, VIHUSISHI vilitokea kutoa utengano mzuri wa kazi hizo.
B. Uhusika wa Kiyunani uliainishwa kwa njia nane zifuatazo;
   1. UHUSIKA WA KIIMA ulitumika kwa ajili ya kutaja na kawaida kilikuwa ni kiima cha sentesi au kishazi. Pia ilitumika kwa NOMINO ARIFU na VIVUMISHI vikiunganishwa na VITENZI “kuwa” au “kufaa”
   2. UHUSIKA MILIKISHI ulitumika kwa ajili ya kuelezea na kawaida ulitoa kivumishi au thamani ya nenolililofanana nalo. Ulijibu swali, “aina gani?” mara nyingi ulielezewa na utumiaji wa KIHUSISHI cha Kiingereza “ya/za”
   3. UHUSIKA WA KUONDOA ulitumia dhana ile ile ya kushurutisha kama ya UMILIKISHI, lakini ulitumika kuelezea utenganifu. Kawaida ulidokeza utengano wa alama kwenye muda, nafasi, kiini, chanzo au degrii. Mara nyingi ulielezewa na matumizi ya KIHUSISHI cha Kiingereza “kutoka”.
   4. UHUSIKA WA WAKATI ulitumika kuelezea matwaka ya mtu binafsi. Hii ingalidokeza mtizamo chanya au hasi. Mara nyingi hiki kilikuwa si kitu cha moja kwa moja. Mara nyingi ulielezewa na KIHUSISHI cha Kiingereza “ya”.
   5. UHUSIKA WA MAHALI ilikuwa dhana shurutishi ya WAKATI, lakini ilielezea mahali au eneo kwenye nafasi, muda au ukomo. Mara nyingi ulielezewa na KIHUSISHI cha Kiingereza “ndani, juu, ni, kati, kwa, juu ya na mbali na”
   6. UHUSIKA WA KUTUMIKA ilikuwa ni dhana shurutishi kama uhusika wa WAKATI na MAHALI. Unaelezea namna au uhusiano. Mara nyingi ulielezewa na KIHUSISHI cha Kiingereza cha neno “kwa” au “enye”
   7. UHUSIKA WA KUSHUTUMU ulihusika kuelezea hitimisho la kitendo. Unaelwzea ukomo. Haswa utumikaji wake ulikuwa kwenye dhana ya moja kwa moja. Ulijibu maswali “kwa umbali gani” au “kwa namna gani”
   8. UHUSIKA WA KAULI ulitumika kuelezea moja kwa moja.

## VI. VIUNGO NA VIUNGANISHO

A. Kiyunani ni lugha sahihi kwa sababu ina viunganishi vingi. Viunganisho fikra ( vishazi, sentesi na aya). Ni vya kawaida kwamba utouwepo wao mara nyingi unakuzwa. Kama jambo la uhakika, viunganisho na viungo hivi vinaonyesha muelekeo wa fikra za mwandishi. Mara nyingi ni vya maana kupima ni kipi haswa anajaribu kukiwakilisha.
B. Hapa pan orodha ya baadhi ya viunganishi na viungo na maana zake (taarifa hizi zimekusanywa haswa toka kwa H.E Dana na Julius K. Mantery. A Manual Grammar of the Greek New Testament
   1. Viunganishi vya wakati
      (a)*epei, epedē,hopote, hōs, hote, hotan (*TEGEMEZI)- “lini”
      (b) *heōs- “*wakati”
      (c)*hotan, epan (*TEGEMEZI)- “kila, wakati wowote”
      (d) *heōs, achri, mechri (*Tegemezi)- “mpaka”
         a. *priv (*kitenzijina)- “kabla”

b. *hōs*- “tangu”, “lini”, “kama”.

2. Viunganishi venye mantiki
   a. Kusudi/dhumuni
      1) *hina* (TEGEMEZI) *hopōs (*TEGEMEZI) *hōs*- “ya kwamba”, “kuwa”
      2) *hōste(*KIUNGO SHUTUMU KISICHO NA UKOMO)- “kuwa”
      3) *pros(*KIUNGO SHUTUMU KISICHO NA UKOMO) au *eis* (KIUNGO SHUTUMU KISICHO NA UKOMO)- “kuwa”
   b. Tokeo (kuna uhusiano wa karibu kati ya kusudio la dhana ya kisarufi na tokeo)
      (1) *hōste(*ISIYO NA KIKOMO, hasa hiki ni cha kawaida)- “ili kwamba”, “hivyo”
      (2) *hiva(*TEGEMEZI)- “ya kwamba”
      (3) *ara*- “kwa kiasi hicho”
   c. Chanzo au sababu
      1) *gar(*chanzo/athari au sababu/hitimisho)- “kwa”, “kwa sababu ya”
      2) *dioti, hotiy*- *“*kwa sababu ya”
      3) *epei, epeidē, hōs*- “tangu”
      4) *dia(*ikiwa na SHUTUMA) na (ikiwa na KIUNGO KISICHO NA UKOMO)- “kwa sababu ya”
   d. Maamuzi
      (1) *ara, poinun, hōste*- “kwa hiyo”
      (2) *dio(*KIUNGO HITIMISHO chenye nguvu)- “kwa sababu ipi”, “kwa nini”, “kwa hiyo basi”
      (3) *oun*- *“*kwa hiyo basi”, “kwa kiasi hicho”, “hatimaye”, “hivyo basi”
      (4) *tinoun*- “kufuatana na”
   e. –a kinyume au tofauti
      (1) *alla(* yenye KINYUME thabiti)-“lakini”, “isipokuwa”
      (2) *de*- *“*lakini”, “ingawa”, “bado”, “kwa upande mwingine”
      (3) *kai*- *“lakini”*
      (4) *mentoi, oun*- *“ingawa”*
      (5) *plēn*- “hata hivyo” (haswa katika Luka)
      (6) *oun*- *“ingawa”*
   f. Ulinganifu
      (1) *hōs,kathōs (*ingiza vishazi linganifu)
      (2) *kata(*kwa muunganiko, *katho, kathoti, kathōsper, kathaper)*
      (3) *hasos(*katika Kiebrania)
      (4) *ē*- *“kuliko”*
   g. Enye mlolongo au mtiririko
      (1) *de*- *“*na”, “sasa”
      (2) *kai*- *“*na”
      (3) *tei*- “na”
      (4) *hina, oun*- *“*kile”
      (5) *oun*- *“*kasha”(katika Yohana)

3. Matumizi yenye mkazo
   a. *alla*- *“*kwa hakika”, “naam”, “kwa kweli”
   b. *ara*- *“*hakika”, agharabu”, “kweli”
   c. *gar*- *“*lakini kweli”, “agharabu”, “hakika”
   d. *de*- *“*hakika”
   e. *ean*- *“*hata”

f. *kai*- “hata”, “hakika”, “kweli”
g. *mentoi*- “hakika”
h. *oun*- “kweli”, “kwa hali zote”

VII.

A. SENTESI SHURUTISHI ni ile iliyo na kishazi kimoja au zaidi. Muundo huu wa kisarufi unaongeza utafasiri kwa sababu unatoa amri, sababu au chanzo kwa nini kitendo cha KITENZI kikuu kimetokea au hakikutokea. Palikuwa na aina nne za sentesi shurutishi. Zilitoka kwa zile zilizofikiriwa kuwa kweli toka kwa mtizamo wa mwandishi au kwa kusudio lake kwa lile alilokuwa na utashi nalo.
B. SENTESI SHURUTISHI DARAJA LA KWANZA ilielezea kitendo au kile kilichofikiliwa kuwa kweli toka kwa mtimamo wa mwandishi au kusudio lake. Ingawa ilielezewa kwa neno “kama.” Katika mazingira tofauti lingeweza kutafasiriwa “tangu”(cf. Mt 4:3, Rum 8:31). Ingawa hii haimaanishi kudokeza kuwa MADARAJA YA KWANZA yote ni ya kweli. Mara nyingi yalitumika kuweka alama kwenye hoja au kuangazia kosa(cf. Mt 12:27)
C. SENTESI SHURUTISHI DARAJA LA PILI mara nyingi huitwa “inayopingana na ukweli”. Inaelezea kitu ambacho kilikuwa ni cha uongo kwenye ukweli wa kufanya jambo. Mfano:
    1. “kama kweli alikuwa nabii, ambapo sio, alikuwa sasa nani na mwanamke wa tabia gani anaye mng’ang’ania yeye, lakini hawezi (Thess 7:39)
    2. Kama kweli Musa, lakini hamkumwamini, mngaliniamini na mimi lakini hamkuniamini (Yoh 5:46)
    3. Kama ningalitaka kuwapendezesha wanadamu lakini sivyo, nisingalikuwa mtumwa wa Christo hata sasa(Gal 1:10)
D. DARAJA LA TATU linaongelea juu ya tukio lijalo ambalo laweza kutokea. Mara nyingi unafikirika uwezekanao wa kitendo kutokea. Kawaida inaashiria tahadhari. Kitendo cha KITENZI kikuu ni tahadhari juu ya tendo la kishazi “hiki”. Mfano toka 1Yoh 1:6-10; 2:4,6,9,15,20,21,24,29; 4:20; 5:14,16
E. DARAJA LA NNE ni daraja la mbali lililoondolewa kwenye uhakika. Ni adimu katika Agano Jipya. Kama jambo la kweli, hakuna SENTESI SHURUTISHI DARAJA LA NNE lililokamilika ambamo pande zote za jambo zinastahili maelezo. Mfano wa DARAJA LA NNE ni ufunguzi wa kishazi katika 1Pet 3:14. Mfano wa sehemu DARAJA LA NNE ni katika kuhitimisha kishazi katika Mdo 8:31.

## VIII. VIZUIZI

A. KITENZI CHA KUAMURU CHA WAKATI ULIOPO kikiwa na KIAMBATA MĒ mara nyingi (lakini hakitengwi) kina msisitizo wa kusimamisha tendo ambalo liko kwenye mchakato. Baadhi ya mifano: “msijiwekee hazina yenu duniani…………”(Mt 6:19); “msisumbukie maisha yenu……….” ( Mt 6:25); “wala msiendelee kuvitoa viungo vyenu kuwa silaha za dhuluma kwa dhambi…….”(Rum 6:13); “wala msimhuzunishe Yule Roho Mtakatifu wa Mungu (Efe 4:30) na “tena msilewe kwa mvinyo…………………”(Ef 5:18)
B. KITENZI TEGEMEZI TIMILIFU kina mkazo wa “udhahanifu au mwanzo wa kutenda kitendo” baadhi ya mifano: “msidhani ya kuwa……..”(Mt 5:17); “msisumbuke………”(Mt 6:31); “msiuonee haya………..”(2Tim 1:8)
C. KITENZI HASI CHENYE JOZI kikiwa na DHAMIRA TEGEMEZI ni chenye msisitizo hasi. “kamwe, katu” au “kwa hali yeyote ile”. Baadhi ya mifano: “kamwe, hataonja mauti………”(Yoh 8:51); “hakika, kamwe………..”(1Kor 8:13)

XI

A. Katika lugha ya Koine, KIBAINISHI CHA WAZI cha neno “wale, Yule,ile” kina matumizi mfanano na kwenye Kiingereza. Kazi yake kuu ilikuwa ni ya “muonyeshwaji”, ni njia ya kukamata hisia ya neno, jina au kirai. Utumiaji unatofautiana kati ya mwandishi na mwandishi kwenye Agano Jipya. KIBAINISHI CHA WAZI pia chaweza kutenda
   1. Kama chombo cha kutofautisha mfano cha kuonyesha
   2. Kama alama ya kurejea KIIMA kilichowekwa awali au mtu
   3. Kama njia ya kutambua kiima kwenye sentesi kikiwa na KITENZI kinchounganisha. Mfano: “Mungu ni Roho” Yoh 4:24, “Mungu ni nuru” 1Yoh 1:5; “Mungu ni upendo” 4:8,16

B. Lugha ya Koine haina KIBAINISHI KISICHO CHA WAZI kama ilivyo kwenye Kiingereza cha neno “a” herufi ya kwanza ya alfabeti au “an” mbadala wa “a” kwenye irabu zinazoanza na herufi kama “e”, “h”. Kutokuwepo na KIBAINISHI CHA WAZI chaweza kumaanisha;
   1. Mlengo juu ya tabia au thamani ya kitu
   2. Mlengo juu ya aina ya kitu

C. Waandishi wa Agano Jipya walitofautiana sana kwa jinsi KIBAINISHI kilivyotumiwa.

## X NJIA ZA KUONYESHA MKAZO KWENYE AGANO JIPYA LA KIYUNANI

A. Mbinu za kuonyesha msisitizo zinatofautiana toka kwa mwandishi mmoja hadi mwingine kwenye Agano Jipya. Waandishi waendelezaji na warasimishaji walikuwa ni Luka na mwandishi wa Waebrania.

B. Mwanzo kabisa tumesema ya kuwa KITENZI TENDAJI TIMILIFU ELEKEZI kilikuwa ni kipimo na kisichoangaliwa kwenye msisitizo, lakini njeo nyingine, irabu au dhamira zina umuhimu wa ufasiri. Hii sio kumaanisha kuwa KITENZI TENDAJI TIMILIFU ELEKEZI mara nyingi hakikutumika kwenye umakinishaji wa kisarufi. Mfano: Rum 6:10 (mara mbili)

C. Upangiliaji wa neno kwenye lugha ya Koine.
   1. Lugha ya Koine ilikuwa ni lugha ngumu isiyo tegemezi, kama vile Kiingereza, kwenye mpangilio wa maneno. Kwa hiyo mwandishi angaliweza kutofautiana kwenye mpangilio wa kawaida aliotegemea kuonyesha.
      a. Kile mwandishi alihitaji kusisitiza kwa viongozi
      b. Kile mwandishi angalikishangaza kwa viongozi
      c. Kile mwandishi alichosikia toka ndani
   2. Mpangilio wa kawaida wa neno kwenye Kiyunani bado ni jambo ambalo halijatulia ingawa mpangilio wa kawaida unaokusudiwa ni
      a. Kiunganishi cha VITENZI/Vitenzi unganishi
         (1) KITENZI
         (2) KIIMA
         (3) SIFA
      b. VITENZI elekezi
         (1) KITENZI
         (2) KIIMA
         (3) KISHAMILISHI
         (4) KISHAMILISHI KISICHO DHAHIRI
         (5) KIRAI HUSISHI
      c. Virai vya NOMINO
         (1) NOMINO

(2) KIVUMISHI
(3) KIRAI HUSISHI

3. Mpanglio wa neno waweza kuwa muhimu mno kwenye upangiliaji wake. Mfano:
   a. "walinipa mimi na Barnaba mkono wa kuume wa shirika" (Gal 2:9) kirai "mkono wa kuume wa shirika" imegawanyika na kuwekwa mbele kuonyesha umuhimu wake.
   b. Pamoja na Kristo (Gal 2:20), iliwekwa kwanza kifo chake kilikuwa kiini.
   c. "ni sehemu nyingi na kwa njia nyingi" (Ebr 1:1), iliwekwa kwanza. Ilikuwa ni kwa namna Mungu alivyojidhihilisha mwenyewe kwa tofauti na sio ukweli wa mafunuo.

D. Kawaida kwa kiasi fulani cha degrii ya msisitizo ulionyeshwa na
1. Urudiaji wa KIWAKILISHI ambacho tayari kilikuwepo katika KITENZI kilichonyambulika. Mfano: "mimi mwenyewe, hakika nitakuwa nawe……."(Mt 28:20)
2. Ukosekanaji wa KIUNGO tarajiwa, au kitu kingine cha kuunganisha maneno, virai, vishazi au sentesi. Hii inaitwa (isiofungamana). Kitu unganishi kilikuwa ni
   a. Ibada ya kubarikiwa kwa Kristo, Mt 5:3 ff(ikisisitizia orodha)
   b. Yohana 14:1 (maada mpya)
   c. Rumi 9:1 (kifungu kipya)
   d. 2Kor 12:20 ( inasisitizia orodha)
3. Urudiaji wa maneno au virai vilivyomo katika mazingira tajwa. Mfano: "usifiwe utukufu wa neema yake" (Efe 1:6, 12 & 14). Kirai hiki kilitumika kuonyesha kazi ya kila mtu wa utatu.
4. Utumiaji wa nahau au neno (sauti) unakaa kati ya istilahi.
   a. Tasifida- maneno mbadala kwa viima vyenye miiko kama "lala" kwa kifo (Yoh 11:11-14) au "nyayo" kwa viungo vya uzazi vya kiume (Ruth 3:7-8; 1Sam 24:3)
   b. Maneno ya kuzunguka- mbadala wa maneno kwa jina la Mungu, kama "ufalme wa mbingu" (Mt 3:21) au "sauti toka mbinguni" (Mt 3:17)
   c. Maumbo ya hotuba
      (1) Kutowezekana kuyakuza (Mt 3:9; 5:29-30; 19:24)
      (2) Upole wa maelezo (Mt 3:5; Mdo 2:36)
      (3) Mfano halisi wa (1Kor 15:55)
      (4) Kejeli (Gal 5:12)
      (5) Dondoo za kishairi (Flp 2:6-11)
      (6) Mvumo unaokaa kati ya maneno
         (a) "kanisa"
            i. "kanisa" (Efe 3:21)
            ii. "Kuitwa" (Efe 4:1,4)
            iii. "Kuitwa" (Efe 4:1,4)
         (b) "huru "
            i. "Mwanamke huru" (Gal 4:31)
            ii. "uhuru" (Gal 5:1)
            iii. "huru" (Gal 5:1)
   d. Lugha ya kinahau- ni lugha ambayo mara nyingi ni ya kitamaduni na lugha bayana
      (1) Hii ilikuwa ni matumizi ya kistiari ya neno "chakula" (Yoh 4:31-34)
      (2) Hii ilikuwa ni matumizi ya kiistiari ya neno "hekalu" (Yoh 2:19; Mt 26:61)
      (3) Hii ilikuwa ni nahau ya Kiebrania ya kuonyesha huruma, ya neno "chukia" (Mwa. 29:31; Kumb.21:15; Thess 14:36; Yoh 12:25; Rum 9:13)

(4) “wote” dhidi ya “wengi”. Linganisha Isa. 53:6 (“wote”) na 53:11 & 12 (“wengi”). Istilahi hizi zina maneno sawa kama Rum 5:18 na 19 kama inavyoonyesha.

5. Utumiaji wa kifungu cha isimu moja kwa moja badala ya neno moja. Mfano: “Bwana Yesu Kristo”.
6. Utumiaji maalumu wa neno *autos*
    a. Wakati likiwa na KIFUNGU (nafasi ya kivumishi angama) kilichofasiliwa “sawa”
    b. Wakati bila KIFUNGU (nafasi ya kuarifu) kilitafasiliwa kama KIWAKILISHI CHENYE MKAZO CHA KUJIREJEA- “mwenyewe jinsia ya ME” “mwenyewe jinsia ya KE” au “yenyewe/chenyewe”

E. Wanafunzi wa Biblia wasio weza soma Kiyunani waweza kutambua mkazo katika Nyanja tofauti:
    1. Utumiaji wa misamiati ya kichambuzi na andiko nasaba la Kiyunani/ Kiingereza.
    2. Mlinganyo wa fasili za Kiingereza, hasa toka kwa nadharia za fasiri zinazotofautiana. Mfano: ufasiri mlinganyo wa “neno kwa neno” (KJV, NKJV, ASV, NASB, RSV, NRSV) na “mfanano wa karibu” (William, NIV, NEB, REB, JB, NJB, TEV)

       Msaada mzuri hapa ungalikuwa ni ule toka *The Bible in Twenty-Six Translation* kilichochapishwa na Baker.
    3. Utumiaji wa *The Ephasized Bible* cha Joseph Bryant Rotherham (Kregel, 1994).
    4. Utumiaji wa tafasiri yenyewe.
        a. *The American Standard Version* ya mwaka 1901
        b. Young’s Lateral Translation of the Bible cha Robert Young (Guardian Press, 1976)

Usomaji wa kisarufi unachosha lakini unafaa kwa ufasiri mzuri. Maelezo hasa sahihi, maoni na mifano inahamasisha na kuwaamusha watu wasiojua Kiyunani kutumia mihitasari ya kisarufi iliyotumiwa kwenye juzuu hii. Hakika maana hizi zimerahisishwa zaidi. Zisingaliweza kutumika katika hali madhubuti nay a kulazimisha, lakini kama ngazi ya kupandia kwenda kwenye uelewa mkubwa wa isimu za Agano Jipya. Kimatumaini maana hizi zitawawezesha wasomaji kuelewa maoni ya msaada mwingine wa usomaji kama vile maoni ya kiufundi juu ya Agano Jipya.

Ni lazima tuweze kuthibitisha ufasiri wetu uliolenga kwenye habari iliyopatikana kwenye maandishi ya Biblia. Sarufi ni moja ya msaada mkubwa wa vipengere hivi, vipengere vingine vingalijumuisha muundo wa kihistoria, maandishi ya kifasihi, utumiaji wa neno la wakati ule ule na dondoo zinazorandana.

# Uhakiki wa Tofauti za Kiuandishi

Somo hili litajikita kwa namna moja kutoa maelezo yanayopatikana katika maoni haya.
Mhutasari ufuatao utahusika

I. Vyanzo vya maelezo ya Biblia zetu za Kiingereza
   A. Agano la Kale
   B. Agano Jipya
II. Maelezo mafupi ya matatizo na nadharia ya "maoni dhaifu" pia yanaitwa "uhakiki wa maandiko"
III. Vyanzo vilivyopendekezwa kwa ajili ya usomaji wa badaye

I. Vyanzo vya maandiko ya Biblia yetu ya Kiingereza

A. Agano la Kale
1. Machapisho ya kale ya Kiebrania ya karne ya kumi na tisa (MT)-maandiko ya konsonanti za Kiebrania yalipangwa na Rabbi Aquiba miaka 100 Baada ya Kristo. Nukta za irabu na lafudhinukuu za pembeni, vituo vya uandishi na alama za nukta zilizoongezwa katika karne ya sita Baada ya Kristo na vilihitimishwa katika karne ya tisa Baada ya Kristo. Yalifanywa na familia ya wasomi wa Kiyahudi wajulikanao kama Wana-maandiko ya Kale ya Kiebrania. Muundo wa maandiko walioutumia ulikuwa sawa na ule katika Mishnah, Talmud, Targums, Peshitta, na Vulgate.
2. Tafsiri ya Kiyunani ya Agano la Kale la Kiebrania (LXX) –Utamaduni unasema Tafsiri ya Kiyunani ya Agano la Kale la Kiebrania ilitengenezwa na wasomi wa Kiyahudi 70 katika siku 70 katika maktaba ya Alexandria chini ya ufadhili wa Mfalme Ptolemy wa II (285-246 K.K). Tafsiri ilidhaniwa kuwa matakwa ya kiongozi wa Kiyahudi aliyeishi katika Alexandria. Utamaduni huu unatokana na "Herufi Aristeas." Mara kwa mara Tafsiri ya Agano Kale(LXX) ilijikita katika kutofautiana kwa utamaduni wa maandishi ya Kiebrania kutoka katika maandishi ya Rabbi Aquiba (MT).
3. Mafunjo ya Bahari ya Chumvi (MBC)-Michoro ya Bahari ya Chumvi -iliandikwa huko Ruma kipindi cha K.K(200 Kabla ya Kristo hadi Baada ya Kristo 70) na madhehebu ya Kiyahudi waliojitenga waitwao " Esene". Machapisho ya Kiebrania, yalikutwa katika sehemu nyingi kandokando ya Bahari ya Chumvi yakionyesha baadhi ya zile tofauti za machapisho ya familia za Kiebrania nyuma ya Machapisho ya Kale ya Kiebrania (MKK)na Tafsiri za Kale za Kiebrania (70).
4. Baadhi ya mifano ya mahususi ni kwa namna gani ulinganifu wa maandishi haya imewasaidia wakalimani kulielewa Agano la Kale.
   a. Tafsiri za Kale za Kiebrania zimewasaidia watafsiri na wasomi kuyaelewa maandishi ya Kale ya Kiebrania.
      (1) Tafsiri za Kale za Kiebrania za Isa. 52:14, "Kama vile wengi watakavyo shangazwa <u>Naye</u>."
      (2) Maandishi ya Kale ya Kiebrania ya Isa. 52:14, "Bado kama vile wengi walivyo staajabishwa <u>Nawe</u>."
      (3) Katika Isa. 52:15 tofauti ya kiwakilishi cha Tafsiri za Kale za Kiebrania imehakikishwa
         (a) Tafsiri za Kale za Kiebrania, "hivyo mataifa mengi yatashangazwa naye"
         (b) Maandishi ya Kale ya Kiebrania, "hivyo yeye ameyatapakaza mataifa mengi"
   b. Mafunjo ya Bahari ya Chumvi (DSS) yamewasaidia watafsiri na wasomi kuyaelewa Maandishi ya Kale ya Kiebrania
      (1) Mafunjo ya Bahari ya Chumvi ya Isa. 21:8, "ndipo akalia Karibu na mlinzi wa mnara nilipo simama."
      (2) Maandishi ya Kale ya Kiebrania (MT) ya Isa. 21:8, "ndipo akalia kama simba, Ee Bwana, mimi nasimama daima juu ya mnara wakati wa mchana……"
   c. Tafsiri za Kale za Kiebrania (LXX) na Mafunjo ya Bahari ya Chumvi (DSS) zote zilisaidia kuichuja Isa. 53:11
      (1) Tafsiri za Kale za Kiebrania (LXX) na Mafunjo ya Bahari Chumvi (DSS), "Baada ya kutaabika sana, mtumishi wangu atafurahi. Kwa kuwajibika kwake kikimilifu, atatosheka na matokeo hayo.''

(2) Maandishi ya Kale ya Kale ya Kiebrania (MT), “Ataona —ya taabu ya nafsi yake, na kuridhika. Kwa maarifa yake mtumishi wangu mwenye haki Atawafanya wengi kuwa wenye haki.”

B. Agano Jipya

1. Maandishi yapatayo 5,300 yote au sehemu za Agano Jipya la Kiyunani yapo hadi leo. Yapatayo 85 yameandikwa katika karatasi za mafunjo na 268 ni maandishi yaliyoandikwa yote kwa herufi kubwa (maandiko adimu) Baadaye, mnamo karne ya tisa B.K., maandishi yaliyo somwa (madogo sana) yalikuzwa. Maandishi ya Kiyunani yaliandikwa kutoka namba zipatazo 2,700. Pia tunazo nakala zipatazo 2,100 za orodha ya Machapisho ya maandiko Matakatifu yalitumika katika kuabudu ambayo tunaiita misale ya waumini.
2. Machapisho ya Kiyunani yapatayo 85 yaliyokuwa na sehemu za Agano Jipya zilizoandikwa katika karatasi za mafunjo yamejengewa katika makumbusho. Baadhi yao yamewekwa katika kipindi maalumu kutoka karne ya pili A.D., yaliyo mengi ni kuanzia karne za tatu na nne A.D. Hakuna kati ya machapisho ya kale. Hizi zilizo na Agano Jipya Kamili. Hii ni kwa sababu hizi ni nakala za kale za Agano Jipya hazimaanishi kuwa sio ya kujiendesha yenyewe zina tofauti chache. Zilizo nyingizilinukuliwa kwa kasi kwa matumizi ya kawaida. Utunzaji haukuzingatiwa katika utendaji. Hivyo, zina utofauti mwingi.
3. Kitabu cha miswada ya kale chenye maandishi ya Kale ya Kiyunani ya karne ya nne B.K. kinachojulikana kwa herufi ya Kiebrania א (*aleph*) au (01), iliyokutwa katika nyumba ya Mt. Katarina juu ya Mlima Sinai na Tischendorf. Tarehe yake imeandikwa kuanzia karne ya nne B.K. iliyokuwa na zote Tafsiri za Kale za Kiebrania (LXX) na za Agano Jipya la Kiyunani. Ni aina ya“Maandishi ya Kialekzandria.”
4. Kitabu cha miswada ya Kale cha Alexandrianus, kijulikanacho kama “A” au (02), machapisho ya Kiyunani ya karne ya tano ambayo ilipatikana katika Alexandria, Misri.
5. Kitabu cha miswada ya Kale cha Machapisho ya Kiyunani cha karne ya nne, kijulikanacho kama “B” au (03), iliyopatika katika maktaba ya Vatikani katika Roma na imeandikiwa tarehe kuanzia katikati ya karne ya nne B.K. Ina zote Tafsiri za Kale za Kiebrania za Agano la Kale na Agano Jipya la Kiyunani. Yalikuwa aina ya “Maandishi ya Kialekzandria.”
6. Kitabu cha miswada ya kale cha Ephraemi, kijulikanacho kama “C” au (02), machapisho ya Kiyunani ya karne ya tano ambayokwa makusudi yaliaribiwa.
7. Kitabu cha miswada ya Kale cha Bazae, kijulikanacho kama “D” au (05), machapisho ya Kiyunani ya karne ya karnre ya tano au sita. Ni mwakilishi mkuu wa kile kinachojulikana kama “Maandishi ya Magharibi.” Ina maongezeko mengi ulikuwa ushahidi mkuu wa tafsiri ya Mfalme James.
8. Agano Jipya la machapisho ya kale yanaweza kuwekwa katika makundi matatu, kadria nne, familia ambazo zimeshiriki sifa fulani.
   a. Maandishi ya Kialekzandria kutoka Misri
      (1) $P^{75}$,$P^{76}$ ( yapata 200 B. K.), ambayo inachukua kumbukumbu ya Injili.
      (2) $P^{46}$ (yapata 225 B. K.), ambayo ilichukua kumbukumbu ya barua za Paulo
      (3) $P^{72}$(yapata 225-250 B. K.), ambayo ilichukua kumbukumbu ya Petro na Yuda
      (4) Kitabu cha miswada ya Kale B, kiitwacho Viticanus (mnamo 325 B. K), ambacho kimebeba Agano la Kale zima na Agano Jipya
      (5) Origen alinukuu kutoka aina hii ya maandiko
      (6) Machapisho ya kale mengine ambayo yanaonyesha aina hii ya maandishi ni א,C, L, W, 33
   b. Maandishi ya Magharibi kutoka Afrika ya Kaskazini
      (1) alinukuu kutoka wakuu wa kanisa wa Afrika ya Kaskazini, Tertullian, Cyprian, na tafsiri za Kale za Kilatini
      (2) yalinukuliwa kutoka Irenaeus
      (3) ilinukuliwa kutoka Kilatini na tafsri za kale za Kisiria
      (4) Andiko D la Machapisho ya kale “Bezae” ilifuata aina ya maandishi haya
   c. Byzantine Mashariki kutoka Constantinople
      (1) aina ya maandishi inaakisiwa katika 80% ya 5,300 MSS

(2) ilinukuliwa na kanisa la mapadre wa Antiokia ya Silia, Cappadoceans, Chrisostom, natherodoret
(3) Andiko A la machapisho ya kale, katika Injili tu
(4) Andiko E la machapisho ya kale, (karne ya nane) ya Agano Jipya

d. aina ya nne iwezekanayo ni ya "Kikaizari" kutoka Palestina
(1) kwanza inaonekana katika Mrko tu
(2) baadhi ya shuhuda zake ni $P^{45}$ na W

II. Matatizo na nadharia ya "ukosoaji dhaifu."

A. Ni kwa namna gani tofauti zilitokea

1. isio angalifu au bila kukusudia (matukio mengi mno)

a. makosa madogo madogo ya macho katika kunakili kwa mkono ambapo ulisomwa mfano wa pili wa maneno yanayofanana na pale ambapo yanaondoa maneno yote katikati (mfanano wa maneno)
(1) makosa madogo madogo ya macho katika kuondoa maneno ya herufi jozi au vifungu (urudiaji wa maneno)
(2) makosa madogo madogo ya kumbukumbu katika kurudia kifungu au msitari wa maandishi ya Kiyunani (mshabaha ule ule)

b. makosa madogo madogo ya masikio katika kunakili maneno ya imla ambapo makosa ya kiuandishi hutokea (itacism). Mara nyingi makosa ya kiuandishi hudokeza au kutaja herufizenye mfananowa sauti za maneno ya Kiyunani.

c. maandishi ya Kiyunani ya kale hayakuwa na sura au mgawanyo wa mistari, chache au alama za uandishi na hakuna mgawanyo kati ya maneno. Inawezekana kuzigawa herufi katika nafasi kuunda maneno tofauti.

2. makusudi

a. mabadiliko yalifanywa ili kufanikisha muundo wa kisarufi wa maandishi yaliyo nakiliwa
b. mabadiliko yalifanywa ili kuyaleta maandiko katika ulinganifu na maandiko mengine ya kibiblia (mlinganyosambamba)
c. mabadiliko yalifanywa kwa kuuunganisha masomo mawili au zaidi yaliyokuwa tofauti katika muungano mmoja wa maandishi marefu (conflation)
d. mabadiliko yalifanywa kusahihisha makosa yaliyotambuliwa katika maandishi ( cf. I Kor. 11-27 na I Yohana 5:7-8)
e. baadhi ya taarifa za nyongeza kama mpangilio wa kihistoria au ufafanuzi sahihi wa maandishi uliwekwa pembezoni kwa nakala moja lakini zilihamishiwa katika maandishi kwa kuzinakili mara ya pili ( Yohana 5:4)

B. Mafundisho muhumu ya ukosoaji wa maandiko (mwongozo wa kimantiki ili kubainisha usomaji halisi wa maandishi wakati tofauti inapojitokeza)

1. maandishi ambayo hayakuwa na ustadi zaidi au ambayo hayakuwa muhimu kisarufi yamkini ni halisi
2. maandishi mafupi zaidi yamkini ni halisi
3. maandishi ya kale yamepewa uzito zaidi kwa sababu ya ukaribu wake kihistoria katika uhalisia, kila kitu kuwa sawa zaidi
4. Machapisho ya kale ni namna mbali mbali ya kijiografia mara nyingi yana usomaji halisi
5. Kimafundisho maandishi ya wanyonge, hasa yale yanayohusiana na majadiliano makuu ya kitheolojia ya kipindi cha mabadiliko ya machapisho kama Utatu katika Yohana 5:7-8, yanapaswa kupendelewa.
6. maandishi ambayo yanaweza kuelezea zaidiasili ya tofauti zingine
7. nukuu mbili ambazozinzsaidia kuonyesha usawa katika tofauti zinazotaabisha

*a.* kitabu cha J. Harold Greenless, *Inroduction to New Testament Textual Criticism*, "Hakuna mafundisho ya Kikristo yanayoning'inia juu ya maandishi yenye kujadiliwa; na mwanafunzi wa

Agano wa Jipya anapaswa kuyatambua maandiko yake anayoyataka kuwa mwenye imani zaidi au kuwa mwenye nguvu kimafundisho kuliko msukumo asilia" (uk. 68).

*b.* W. A. Criswell alimwambia Greg Garrison ya *The Birmingham News ambayo yeye* ( Criswell) haamini kila neno katika Biblia ni la kutia moyo "angalau si kila neno ambalo limekwisha kutolewa kwa alaiki ya kisasa kwa karne za watafsiri." Criswell alisema "Mimi ni mwamini sana katika ukosoaji wa maandishi. Kama vile, Nafikiri, nusu ya sura ya 16 ya Marko ni uasi: haitii moyo, imebuniwa…Unapolinganisha machapisho hayo kwa kurudi huko nyuma, hakukuwa na kitu kama hicho kama lilehitimisho la Kitabu cha Marko. Mtu fulani alikiongeza…" Mababa wa uzao wa SBC wasio wakosaji walidai kuwa "kutia maneno yasiokuwepo katika kitabu" pia ni dhahiri katika Yohana, uwajibikaji wa Yesu katika bwawa la Bethesda. Na alijadili tofauti mbili za uwajibikaji wa kujinyonga kwa Yuda ( Mt. 27 na Matendo 1): "Ni maoni tofauti ya kujinyonga," Criswell alisema "Kama iko katika Biblia, kuna maelezo yake. Na hatia mbili za kujinyonga kwa Yuda ziko katika Biblia."Criswell aliongeza, "Ukosoaji wa Maandishi nisayansi ya ajabu ndani yake yenyewe. Si ya muda mfupi kupita, si isiyo husiana.Ni yenye nguvu na kuu…"

III. Matatizo ya machapisho (ukosoaji wa maandishi)

A. Vyanzo vilivyopendekezwa kwa ajili ya kusoma zaidi

1. *Biblical Critcism, Historical, Literary and Textual*, na R. H. Harrison
2. *The Textual of the New Testmemt: Its Transmission, Corruption and Restoration*, na Bruce M. Metzger
3. *Introduction to New Testament Txtual Critism*, na J. H Greenlee

# FAHARASA

**Uasilishaji.** Hili ni moja kati ya maoni ya kale ya uhusiano wa Yesu na Uungu. Kimsingi inadai kwamba Yesu alikuwa mwanadamu wa kawaida kwa kila namna na alichukuliwa na Mungu kwa kazi maalumu katika ubatizo wake (Mt. 3:17; Marko 1:11) au katika ufufuo Wake (cf. Rum.1:4).Yesu aliyaishi maisha haya kama mfano ambao Mungu, kwa kiasi chake, (ubatizo, ufufuo) uliyomuasilisha Yeye kama "mwana" Wake (Rum.1:4 Flp. 2:9). Hili lilikuwa kanisa la mwanzo na maoni ya watu wa karne ya nane. Badala ya Mungu kuwa mwanadamu (umbo la kibinadamu) akalirejeresha hili na sasa mwanadamu anakuwa Mungu!
Ni vigumu kusema namna gani Yesu, Mungu Mwana, Uungu uliokuwepo kabla alivyozawadiwa au kuwa mbadala kwa ajili ya maisha yenye mfano. Kama Yeye alikuwa tayari ni Mungu, ni kwa namna gani Yeye alitolewa kama zadiwa? Kama Yeye alikuwa na utukufu wa Kiungu wa awali ni kwa namna gani Yeye angeliheshimiwa zaidi? Ingawa ni vigumu kwetu sisi kutambua, kwa namna Baba alivyomuheshimu Yesu katika dhana maalumu ya ukamilifu Wake wa kuyatimiza mapenzi ya Baba.

**Shule ya Alexandria.**Njia hii ya ukalimani wa kibiblia ilikuzwa katika Alexandria, Misri katika karne ya pili B.K. Inatumia misingi ya kanuni za ukalimani ya Philo, ambaye alikuwa mfuasi wa Pilato, mara nyingi inaitwa njia ya kiistiari. Ilitawaliwa katika kanisa hadi wakati wa Marekebisho. Watetezi wake zaidi walikuwa Origen na Augustine. Tazama Moisea Silva, *Has The church Misred The Bible?* (Academic, 1987)

**Ufuasi wa Alexandria.**Haya ni machapisho ya Kiyunani ya karne ya tano kutoka mji wa Alexandria, Misri ikijumuisha Agano la Kale, lililothibitishwa, pamoja na Agano Jipya. Ni moja ya ushahidi wetu mkubwa katika Agano Jipya zima la Kiyunani (isipokuwa sehemu za kitabu cha Mathayo, Yohana, na II Wakorintho). Wakati ambapo machapisho haya, ambayo yanapewa alama "A, na machapisho ya alama "B" (ya Vatican) yanaafiki juu ya usomaji unaofikiriwa kuwa ya mwanzo na baadhi ya wasomi.

**Istiari.** Hii ni aina ya ukalimani wa kibiblia ambayo kiasili ulianzishwa ndani ya dini ya Kiyahudi huko Alexandria. Ilienezwa na Philo wa Alexandria. Msukumo wake wa msingi ni shauku ya kufanya uhusiano wa Maandiko na utamaduni wa mtu au mfumo wa kifalsafa kwa mpangilio wa historia ya Biblia na/ au muktadha wa maandishi. Inatafuta uficho au kweli ya kiroho nyuma ya kila kifungu cha maandiko. Inapaswa kukubaliwa kwamba Yesu, katika Mathayo 13, na Paulo, katika Wagalatia 4, alitumia istiari kuiwasilisha kweli. Kwa hali yoyote, hii, ilikua katika muundo wa taipolojia (uanishi), na si istiari halisi.

**Uchanganuzi wa misamiati.** Hii ni aina ya chombo cha utafiti ambacho kinamruhusu mtu kutambua kila muundo wa Kiyunani katika Agano Jipya. Ni mkusanyiko, katika mpangilio wa alfabeti za Kiyunani, wa kimuundo na maelezo ya msingi. Katika muunganiko kwa tafsiri mbalimbali, unaruhusu usomaji wa wasio Wayunani kuchambua visarufi vya Agano la Kale la Kiyunani kimsamiati na kimuundo.

**Ushabihiano wa Maandiko.** Hiki ni kifungu kinachotumika kueleza wazo kwamba Biblia nzima imefunuliwa na Mungu, na ni, kwa hiyo sio mkanganyiko bali ukamilifu. Ukubalifu wa dhanio hili ni msingi kwa matumizi yanayo fanana na vifungu vya maneno katika kufasiri maandiko ya biblia.

**Utata.**Hii inarejea juu ya mashaka ambayo yanaleta matokeo katika nyaraka zilizoandikwa ambapo kuna maana mbili ziwezekanazo au zaidi au wakati vitu viwili au zaidi vinakuwa vikirejewa kwa wakati mmoja. Inawezekana kwamba Yohana anatumia utata huu kwa makusudi.

**Elimu ihusuyo tabia ya mwanadamu.** Inamaanisha kuwa na "tabia zinazohusiana na wanadamu." neno hili linatumika kueleza lugha zetu za kidini kumuhusu Mungu. Linatokana na neno la Kiyunani kumuhusu mwanadamu. Inamaanisha kwamba tunazungumza kuhusiana na Mungu kana kwamba Yeye alikuwa mwanadamu. Mungu anaelezwa katika umbo la mwili lionekanalo, kijamii, maneno ya kisaikolojia ambayo

yanahusiana na wanadamu (cf. Mwa. 3:8; II Wafalme 22: 19-23). Hii, hakika ni mshabihiano pekee. Hata hivyo maarifa yetu kumhusu Mungu, ingawa ni kweli, lakini yamewekewa mipaka.

**Shule ya Antiokia.**Hii njia ya ufasiri wa kibiblia ilianzia huko Antiokia, Syria katika karne ya tatu B.K. kama kuonyesha hisia juu ya utaratibu wa kiistiari wa Alexandria, huko Misri. Msingi wa msukumo wake uliangalia maana ya kihistoria ya Biblia. Ilitafasiri Biblia kama fasihi ya kawaida ya mwaadamu. Shule hii ilikuwa imejumuishwa katika ubishi kumhusu Kristo kama alikuwa na asili mbili (mafundisho kuhusu uwili wa Yesu) au asili moja (Mungu kamili na mwanadamu kamili). Ilitambuliwa kama maoni ya kupinga Ukristo kwa Kanisa Katoriki la Rumi na kuhamishiwa Uajemi lakini shule ilikuwa na umuhimu mdogo. Misingi ya kanuni zake za ufasili wa kibiblia baadaye ikawa kanuni za ufasili wa watu walioleta mageuzi kwenye dini ya Kiprostanti (Luther and Calvin).

**Kutabaini.** Hii ni moja miongoni mwa njia tatu za uwasilishaji wa neno uliotumika kudokeza uhusiano kati ya misitari ya ushairi wa Waebrania. Unahusiana na misitari ya ushairi yenye kukinzana kimaana (cf. Mit. 10:1; 15:1).

**Fasihi ya mafunuo.** Hii ilikuwa ni namna tanzu ya Wayahudi wenye nguvu, hata kuonekana ya kipekee. Ilikuwa ni aina ya uandishi wenye mafumbo uliotumika nyakati za uvamizi na umiliki dola yenye nguvu ya Kiyahudi. Inafikiriwa kwamba mtu, muumbwaji aliyekombolewa na Mungu na kuyatawala matukio ya ulimwengu, na kwamba Israeli ina upendeleo maalumu na uangalizi kutoka Kwake. Fasihi hii inahaidi ushindi mkuu na kupitia juhudi pekee za Mungu.

Ni ishara kuu na ya ubunifu sana yenye maneno ya mafumbo. Mara nyingi ilieleza ukweli katika rangi, tarakimu, maono, ndoto, upatanishi wa kimalaika, alama za siri za maneno, mara nyingi uwili wa vitu kati ya mema na mabaya.

Baadhi ya mifano tanzu hapa ni (1)katika Agano la Kale, Ezekieli (sura ya 36-48), Danieli (sura ya 7-12), Zekaria; na (2) Katika Agano Jipya, Mathayo 24;Marko 13; II Wathesalonike 2 na Ufunuo.

**Mtetezi.**Hili linatoka katika mzizi wa neno la Kiyahudi "ulinzi wa kisheria." Haya ni mafundisho ndani ya theolojia ambayo yanatafuta kutoa ushahidi na uwiano wa hoja za kifikra kwa imani za Kikristo.

**Haki ya kutangulia.**Kimsingi huu ni ukaribu wa maana ya neno "dhanio." Inahusisha ufikiliaji wa wa maana za awali zilizokubalika, kanuni au nafasi iliyosadikika kuwa kweli paspo uchambuzi au uchunguzi.

**Ufuasi wa Arius.**Arius alikuwa mhudumu ndani ya kanisa huko Aexandria, Misri katika karne ya tatu na mwanzoni mwa karne ya nne. Alikubali kwamba Yesu alikuwepo hapo kabla lakini si kwa Uungu (si sawa na asili ya Baba), huenda kwa kufuata Mithali8:22-31. Alipingwa na askofu wa Alexandria, ambaye alianza (B.K. 318) mabishano yalidumu kwa miaka mingi. Ufuasi wa Arius ulikuja kuwa kanuni rasmi katika Kanisa la huko Mashariki. Baraza la Nicaea katika 325 B.K.walimshtumu Arius na kuutetea usawa na Uungu kamili wa Mwana.

**Jamii ya watu wakuu.** Alikuwa mmoja wa wanafalsafa wa kale wa Ugiriki, mwanafunzi wa Pilato na mwalimu wa Iskanda Mkuu.Ushawishi wake, hata sasa, umefika maeneo mengi yanayofundisha mafunzo ya kisasa. Hii ni kwa sababu alisistiza maarifa ni kupitia uchunguzi na upambanuzi. Hii ni moja ya itikadi ya njia za kisayansi.

**Miandiko binafsi.** Hili ni jina lililotolewa kwa maandishi ya mwanzo ya Biblia. Maandiko haya asilia yaliyoandikwa kwa mkono yote yamepotea. Baadhi tu ya nakala zimesalia. Hiki ndio chanzo cha utofauti wa maandishi mbalimbali katika machapisho ya Kiebrania na Kiyunani.

**Maandiko ya asili ya karne ya sita.** Haya ni machapisho ya Kiyunani na Kiratini ya karne ya sita B.K. Yanasanifiwa na alama "D." Imejumuisha Injili na Matendo na baadhi ya Nyalaka za Jumla. Inabainishwa na nyongeza nyingi za maandishi yenye ueledi. Inaunda msingi wa "uundaji wa maandiko"ambayo ni tamaduni za machapisho makuu ya Kiyunani nyuma ya toleo la King James Version.

**Upendeleo.** Hili ni neno linalotumika kueleza maelezo yenye nguvu kuhusiana na jambo au mtazamo fulani. Ni mtizamo ambao uadilifu ndani yake hauwezekani kungalia kitu au maoni Fulani. Ni madhara ya kieneo.

**Mamlaka ya Kibiblia.** Ni neno lililotumika katika maana maana ya kipekee. Linaelezwa kama uelewa wa kile alichokisema mwandishi asilia katika siku zile zake na kutumia ukweli huu katika siku zetu. Mamlaka za Kibiblia mara nyingi zinaelezwa kuitazama Biblia yenyewe kama kiongozi chetu chenye mamlaka. Hata hivyo, katika hali ya sasa, utafasiri sio sahihi. Nimeweka mipaka juu a dhana ya Biblia kama ilivyotafsiriwa na kanuni za njia ya historia ya kisarufi.

**Orodha ya vitabu vya Agano Jipya.**Hili ni neno linalotumika kuelezea maandishi yanayosadikiwa kuvuviwa kipekee. Limetumika kuangalia maandiko yote ya Agano la kale na Agano jipya.

**Kristo kama kitovu.**Ni neno lililotumika kuonyesha Kristo kama kitovu cha mambo yote. Na lilitumiwa kuunganisha dhana ya kwamba Yesu ni Bwana wa Biblia zote, Mawazo ya Agano la Kale dhidi yake na utimilifu wa malengo yake.

**Fasiri.**Hii ni aina pekee ya utafiti wa kitabu. Inatoa kwa pamoja usuli wa kitabu cha Biblia. Pia inajaribu kuelezea maana ya kila kipengele cha kitabu. Baadhi inatazamisha matumizi, wakati mwiingine zinahusiana na andiko katika hali ya kiufundi. Vitabu hivi ni vya manufaa, lakini lazima vitumike baada ya mtu kufanya uchunguzi wake wa awali. Tafsiri za watoa maoni lazima zisikubalike kuhakiki. Ukilinganisha fasiri nyingi toka kwa mitizamo ya wanathiolojia tofauti utaona inasaidia.

**Itifaki.** Hii ni aina ya chombo cha utafiti kwa usomaji wa Biblia. Inaorodhesha kila utokeaji wa neno katika Agano Jipya na la Kale. Inasaidia katika njia tofauti: (1) kubainisha maneno ya Kiebrania au Kiyunani yaliyoko nyuma ya maneno ya kiingereza: (2) kulinganisha kurasa ambapo neno lile lile la Kiebrania au Kiyunani limetumika: (3) kuonyesha mahali ambapo maneno mawili tofauti ya Kiebrania au Kiyunani yametafasiriwa kwa neno lie lile la kiingereza: (4) kuonyesha mwendelezo wa kutumia maneno fulani katika vitabu fulani au maandishi: (5) inasaidia mtu kupata somo katika Biblia (cf. Walter Clark's *How to use New Testament Greek Study Aids*. kurasa za 54-55).

**Magombo ya Bahari ya Chumvi.** Inarejerea mlolongo wa maandiko ya kale yaliyoandikwa katika Kiebrania na Kiarama ambayo yalipatikana karibu na Bahari ya Chumvi mwaka 1947. Palikuwepo na maktaba za kidini ya Kiyunani ya karne ya kwanza. Msukumo wa umilikaji toka Rumi na vita ya kinazi vya miaka ya sitini viliwasababisha wao kuficha magombo yaliyokuwa yamefungashwa ndani ya vyungu kwenye mapango au mashimo. Inatusaidia sisi kuelewa muundo wa kihistoria wa palestina ya karne ya kwanza na kuthibitisha maandiko ya mossoretes kuwa yako sahihi kwa kiasi fulani enzi ya awali kabla ya Yesu B.C.

**Mambo yaliyofasiliwa.** Njia hii ya kimantiki au ufikiliaji inatokana na kanuni ya pamoja ya matumizi maalumu kwa njia ya wazo. Hii ni kinyume toka ufikiliaji wa mambo yaliyofasiriwa, ambayo yanaangazia njia ya kisayansi toka kwenye uchunguzi maalumu kwenda hitimisho la pamoja (nadharia)

**Mbinu pembuzi.**Hii ni njia ya kufikilisha ambapo kile kinachoonekana kuleta mkanganyiko au mafumbo huwekwa pamoja katika hali ya mkazo, ikitafuta jibu la pamoja ambalo linajumuisha pande zote za fumbo. Mafundisho mengi ya Biblia yana upembuzi unaofanana, kuamuliwa kabla-mapenzi huru, ulinzi-ustahimilivu, imani-kazi; uwamuzi-ufuasi; uhuru wa Mkristo-uwajibikaji wa Mkristo

**Wayahudi waliotawanyika katika mataifa mengine.**Hili ni neno la kiufundi la Kiyunani lililotumiwa na wapalestina wa Kiyahudi kuelezea wayahudi wengine walioishi nje ya mipaka ya kijiografia ya nchi ya ahadi.

**Mlinganyo wa nguvu.** Hii ni nadhalia ya ufasili wa Biblia. Tafasili ya Biblia inaweza kuangaliwa kama mwendelezo toka ushirika wa "neno kwa neno", mahali ambapo neno la Kiingereza lazima liwekwe kwa kila neno la Kiyunani au Kiebrania, kwenye "ufasili" ambapo tu wazo limetafasiliwa kwa angalizo la chini ya neno au kifungu cha awali.

Katika nadharia hizi mbili ndipo pana "mlinganyo wa nguvu" unaojaribu kuchukua neno la mwanzo kwa umakini wake, lakini limefasiliwa katika miundo ya visarufi vya kisasa  na nahau. Majadiliano mazuri ya kweli ya hizi nadharia mbali mbali za fasili zinapatikana katika makala ya Fee na Stuart *How to Read the Bible For Its Worth,* uk. 35 na katika Robert Bratcher's utangulizi katika Biblia ya TEV.

**Kutofuata mfumo.** Neno hili linatumika katika mahusiano ya uhakiki wa maandiko. Unarejerea kitendo cha kuchagua usomaji toka machapisho tofauti tofauti ya Kiyunani ili kufika kwenye neno linalotakiwa kuwa karibu na maandiko ya mwanzo.

**Kupotosha maana.** Hili neno ni kinyume cha neno fasili ya maandiko. Kama fasili ya maandiko ni "kuondoa" kulingana na  kusudio la mwandishi wa awali, basi neno hili litamaanisha "kuingiza" wazo la kigeni.

**Elimu ya asili na historia ya neno.** Hii ni dhana ya usomaji wa neno unaojaribu kuyakinisha maana ya awali ya neno. Kutokana na chanzo cha maana hii, utumiaji wa kipekee unaotambulika kirahisi katika ufasili, elimu ya asili na historia ya neno sio kiini cha mtizamo, mbali na maana ya wakati ule ule na utumiaji wa neno.

**Fasili ya maandiko.** Hili ni neno la kiufundi kwa utendaji wa kutafasili kifungu maalumu. Inamaanisha "uondoaji nje" (wa neno) ukidokeza kwamba dhumuni letu ni kuelewa kusudi la mwandishi wa mwanzo katika uelewa wa muundo wa kihistoria, mazingira ya kifasihi, sintaksi na maana ile ile ya neno.

**Namna ya Uwasilishaji.** Hili ni neno la Kifaransa ambalo limedokeza aina mbali mbali ya fasihi. Msukumo wa neno hili ni mgawanyiko wa miundo ya fasihi katika namna mbali mbali ambazo zinashirikishana tabia za aina moja. Usimuliaji wa kihistoria, mashairi, mithali, ufunuo na uandikishaji.

**Maarifa ya utambuzi/mafunuo.** Zaidi ya maarifa tulionayo kuhusu imani potofu yameletwa toka maarifa ya utambuzi wa maandiko katika karne ya pili. Ingawa mawazo ya awali yalikuwepo katika karne ya kwanza (na kabla). Baadhi ya maelezo ya mafunuo ya kinazi ya Valentino na Cerinthin ni (1) mwili na roho vyote vilikuwepo kabla. mwili ni mwovu, na Roho ni nzuri. Mungu, ambaye ni Roho hawezi kuhusishwa moja kwa moja na mwili mwovu (2) kuna asili (*eons au* daraja la kimalaika*)* kati ya Mungu na mwili. Wa mwisho au wa chini alikuwa YAHWE wa Agano la kale, ambaye aliuumba ulimwengu (*kosmos*); (3) Yesu alikuwa mwanzilishi kama YAHWE lakini akiwa juu ya viwango, karibu na Mungu wa kweli. Wengine walimweka juu zaidi lakini bado yu chini kuliko Mungu na hakika asiye na mwili wa Kiungu (cf. 1:14). Kwa vile mwili ni mwovu, Yesu asingelikuwa na mwili wa kibinadamu na bado akawa na hali ya Kiungu. Alikuwa ni nafsi ya kufikirika (cf. 1Yoh 1:1-3; 4:1-6); na (4) wokovu ulipatikana kupitia imani katika Yesu pamoja na maarifa maalumu, yaliyojulikana na watu maalumu. Maarifa (maneno ya siri) yalihiiitajika kupitia ulimwengu wa kimbingu. Washikiliaji sana wa kisheria za Kiyahudi nao pia walihitaji kumfikia Mungu. Walimu wa uongo wenye maarifa ya utambuzi walitetea miundo miwili kinzani ya kimaadili (1) baadhi ya stadi za maisha hazikuhusiana na wokovu. Kwao wokovu na utakaso ulifumbwa kwenye maarifa ya siri (neno la siri) kupitia ulimwengu wa kimalaika (*eons)*; au (2) kwa wengine stadi ya maisha ilikuwa muhimu katika wokovu. Walisisitiza miundo ya maisha kama kielelezo cha utakaso wa kweli.

**Kanuni za ufasili.** Hili ni neno la kiufundi kwa kanuni zinazoongoza ufasili wa maandiko. Ni seti ya mwongozo maalumu na sanaa/kipawa. Kibiblia, au takatifu, kanuni za ufasili zimegawanyika kwa namna mbili; kanuni za ujumla na kanuni maalumu. Hizi zinahusiana na aina tofauti za fasihi zinazopatikana katika Biblia. Kila aina tofauti (tanzu)zina mwongozo wake wa kipekee lakini zinashirikiana na baadhi ya dhana na namna ya utafasili.

**Uhakiki juu ya maandiko.** Hii ni namna ya utafasili wa kibiblia ambao unatazamisha kwenye muundo wa kihistoria na umbo la fasihi hasa hasa katika kitabu cha Biblia.

**Nahau.** Neno hili linatumika kwenye vifungu vinavyopatikana katika tamaduni tofauti zenye maana maalumu na sio vilivyohusiana na maana ya kawaida ya maneno binafsi. Maana ya mifano ya kisasa ni: "ilikuwa ni vizuri sana" au "umeniua". Biblia pia inajumuisha aina hizi za vifungu.

**Nuru.**Hili ni jina lililotolewa kwenye dhana kuwa Mungu aliongea na mwanadamu. Dhana nzima kwa kawaida imeelezewa kwa namna tatu: (1) ufunuo-Mungu ametenda kwenye historia ya binadamu: (2) uvuvio-ametoa utafasili sahihi wa matendo yake na maana yake kwa watu fulani waliochaguliwa kuweka kumbukumbu ya mwanadamu: na (3) nuru –ametoa roho wake kumsaidia mwanadamu kuelewa mafunuo yake.

**Kudukiza.** Hii ni njia ya kimantiki au kufikiria inayotoka sehemu Fulani na kuenea sehemu yote. Ni njia ya kutegemea majaribio ya kisasa. Kimsingi, huu ni mjongeo wa watu wenye hadhi ya juu.

**Unasaba.** Hii ni aina ya chombo cha uchunguzi kinachoruhusu wale wasiojua lugha za kibiblia kuchunguza maana yake na muundo. Inaweka tafasili ya kiingereza kwenye ngazi ya neno kwa neno chini ya lugha ya awali ya kibiblia. Chombo hiki kinajumuishwa na "misamiati ya kiuchunguzi" ambayi inatoa miundo na maelezo ya msingi ya Kiebrania na Kiyunani.

**Uvuvio.**Hii ni dhana ya kwamba mungu aliongea na mwanadamu kwa kuwalinda waaandishi wa kibiblia kwa usahihi na uwazi ili kuweka kumbukumbu ya mafunuo yake. Dhana nzima imeelezewa kwa namna tatu: (1) ufunuo-Mungu ametenda katika historia ya mwanadamu (2) uvuvio-ametoa utafasiri wasahihi wa matendo yake na maana yake kwa watu Fulani waliochaguliwa kuweka kumbukumbu ya mwanadamu: na (3) Nuru-ametoa roho wake kumsaidia mwanadamu kuelewa mafunuo yake.

**Lugha ya maelezo.** Hii inatumika pamoja na nahau pale Agano la Kale lilipoandikwa. Inaongelewa juu ya dunia kwa namna jinsi vitu vinavyotokea kwenye milango mitanmo ya fahamu. Sio maelezo ya kisayansi hata yakamaanisha kuwepo.

**Ushikiliaji sana wa sheria.** Mwenendo huu umeainishwa kwa msisitizo zaidi juu ya sheria au matambiko. Unajaribu kutegemea juu ya utendaji wa mwanadamu kama njia ya ukubalifu kwa Mungu. Unajaribu kushusha uhusiano na kuinua utendaji, mwote ambamo dhana muhimu ya mahusiano ya kimaagano kati ya Mungu mtakatifu na mwanadamu mtenda dhambi.

**Tafasili sisisi.** Hili ni jina jingine la mlengo wa kimaandiko na njia za kihistoria za za kanuni za ufasili toka Antiokia. Ina maana kwamba utafasili unahusika katika maana dhahili za lugha ya mwanadamu, ingawa inaendelea kutambua uwepo wa lugha za kitamathali.

**Fasihi tanzu.** Hii inarejerea kwenye miundo ya utofauti ili kwamba mawasiliano ya uwanadamu yanaweza kuchukuliwa kama vile ushairi au simulizi za kihistoria. Kila aina ya fasihi ina nji/namna yake maalumu ya kanuni ya ufasili kwa kuongezea kwenye kanuni za pamoja kwa fasihi zote zilizoandikwa.

**Sehemu ya fasihi.** Hii inarejerea mgawanyo wa lengo kuu la kitabu cha Kibiblia. Inaweza kuundwa na misitari, aya, au ibara chache. Ni kijumuishi pekee chenye kiini cha somo.

**Lower criticism- Uhakiki wa kawaida wa maandiko.**

**Maandiko ya asili.** Neno hili linahusiana na nakala mbali mbali za Agano jipya la Kiyunani. mara nyingi limegawanyika katika aina tofauti kwa (1) nyenzo iliyotumika kuandikiwa kwayo (mafunjo, ngozi) au (2) muundo wenyewe wa uandishi. Limefupishwa kwa neno "MS" (umoja) au "MSS" (wingi).

**Andishi la kidesturi la Kiebrania la Biblia ya Kiyahudi.** Hii inarejerea karne ya nane A.D. maandiko ya asili ya Kiebrania ya Agano la kale yalitolewa na vizazi vya wasomi wa Kiyahudi ambayo yalijumuisha alama za irabu na mihtasari mingine ya maandiko. Yanatengeneza msingi wa neno kwa Agano letu la kale la Kiingereza.

**Mshabihiano wa neno.** Huu ni namna ya msemo ambao jina la kitu linatumika mbadala wa kitu kingine kinachofanana nacho. Kwa mfano " birika linachemka" ki uhalisia inamaanisha "maji yaliyeko kwenye birika yanachemka".

**Orodha ya vitabu vya Agano jipya.** Hii ni orodha ya vitabu vya sheria za kanisa la Agano jipya. Iliandikwa huko Rumi kabla ya mwaka 200 A.D. Inatoa vitabu ishirini na saba kama vile vile vya Agano Jipya la Waporostanti. Hii wazi kabisa inaonyesha makanisa madogo madogo ya mahali katika sehemu mbali mbali za milki ya Rumi kulikuwa "kiutendaji" pamewekwa sheria za kanisa kabla ya baraza kuu la kanisa la karne ya Nne.

**Ufunuo wa asili.** Hii ni namna ya Mungu mwenyewe kujifunua kwa mwanadamu. Unajumuisha utaratibu wa kiasili (Rum 1:19-20) na dhamila adilifu (Rum 2:14-15). Umeongelewa katika Zaburi 19:1-6 na Warumi 1-2. Unatofautishwa toka kwenye mafunuo maalumu, ambayo kwa mungu mwenyewe ni muhimu kujifunua katika Biblia na mwanae pekee Yesu wa Nazareti. Uangaliaji huu wa kithiolijia unasisitizwa tena na mwenendo wa "dunia ya zamani" kati ya wanasayansi wa Kikristo (cf. maandishi ya Hagh Ross) wanatumia uangaliaji huu kwa kuthibitisha kuwa kweli yote ni kweli ya Mungu. Ulimwengu ni mlango ulio wazi wa maarifa ya kumjua Mungu; ni tofauti toka kwa ufunuo maalumu (Biblia); unawapa wanasayansi uhuru wa kufanya uchunguzi juu ya utaratibu wa kiasili. Kwa maoni yangu , hii ni fursa mpya ya ajabu kushuhudiwa juu ya wanasayansi wa ulimwengu wa magharibi.

**Ufuasi wa Nestory.** Nestory alikuwa ni mkuu wa familia ya Constantino kwenye karne ya tano. Alifundishwa huko Antiokia ya Syria na kuthibitisha kwamba Yesu ana asili mbili, moja ni mwanadamu kamili na nyingine ni Mungu kamili. Maoni haya yalichepushwa toka kwenye mtizamo wa asili wa mtu mmoja wa Orthodox kutoka Alexandria. Kusudio kubwa la Nestory lilikuwa ni cheo cha "mama wa Mungu" alichopewa Maria Magdalena. Nestory alipingwa na Cycil wa Alexandria na, kwa kuwekwa matatani juu ya mafundisho yake huko Antiokia. Antiokia yalikuwa makao makuu ya mtazamo wa kihistoria wa visarufi vya maandiko kwa utafasili wa Kibiblia, wakati Alexandria yalikuwa makao makuu ya shule Nne zilizotengwa kwa ajili ya utafasili. Nestory hatimaye aliondolewa toka ofisini na kukimbilia mafichoni.

**Mwandishi wa awali.** Hii inarejerea wandishi halisi wa maandiko

**Mafunjo/Magombo.** Haya yalikuwa aina mojawapo ya nyenzo toka Misri zilizotumika kuandikiapo maandiko. Yalitengenezwa kwa majani au magome ya miti. Ni nyenzo ambazo nakala za zamani Agano la Kale la Kiyunani zilihifaziwapo.

**Vifungu Mlinganyo**. Ni sehemu ya mtazamo kuwa yote yaliyomo kwenye Biblia yametoka kwa Mungu na, kwa hiyo, ni ufafili wake mahsusi na mlinganyo wa kweli wa kimafumbo. Hili pia ni la msaada pale mtu anapojaribu kutafasili kifungu kisicho wazi au kigumu. Pia inamsaidia mtu kupata kifungu kilicho wazi juu ya somo husika vile vile mtazamo wote wa kimaandiko juu ya somo husika.

**Ufafanuzi/fasili.** Hili ni jina la nadhalia ya utafali wa Biblia. Utafasili wa Biblia unaweza kuangaliwa kama mwendelezo wa mahusiano wa "neon kwa neon" ambapo neon la Kiingreza laweza kuweka kwa kila neon la Kiebrania au Kiyunani kwenye "fasili" ambapo tu wazo limetafasiliwa kwa mtizamo wa kawaida wa neon au kifungu cha awali. Kati ya nadhalia mbili hizi "mlinganyo wa nguvu" ambao unajaribu kuchukuawa kwa umakini andiko la awali lakini likatafasiliwa katika muundo wa kisasa wa kisarufi na nahau. Kweli kabisa mjadara mzuri wa nadhalia hizi mbali mbali za utafasili zinapatikana katika chapisho la Fee na Stuart *How to Read the Bible For All Its Worth, Uk. 35.*

**Aya.** Huu ni msingi wa ufasili wa fasihi moja kinadhalia. Unajumuisha wazo moja kuu na mwendelezo wake. Tukibaki na musukumo wake mkuu hatutatazama juu ya udogo wake au uzuri wa kusudi la mwandishi wa awali.

**Uparokia.** Hii inahusiana na mapendeleo yaliyofungiwa kwenye muundo wa tamaduni/ thiolojia ya kawaida. Haitambui asili ya mapokeo ya kweli yaliyobadilika ya Kibiblia au matumizi yake.

**Fumbo.** Hii inarejerea kweli zile zinazoonekana kuleta mkanganyiko, nab ado zote zikabaki kuwa kweli, ingawa bado zinakinzana. Zinaunda kweli kwa kuwakilisha toka pande zilizo kinyume. Kweli nyingi za Kibiblia zinawakilishwa kimafumbo (au kiupembuzi). Kweli za Kibiblia sio kama nyota zilizotengana, zimetengenezwa kwa ukilimio wa sehemu za nyota.

**Pilato.** Alikuwa ni mmoja ya wanafalsafa wa Ugiriki ya kale. Falsafa yake kwa kiasi kikubwa ulisababisha kanisa la mwanzo kupitia wasomi wa Alexandria, Misri na baadaye, Augustino. Alituma ujumbe kuwa kila kitu duniani ni kiini macho na ni mfano tu wa kielelezo asili wa vitu vya rohoni. Baadaye wanathiolojia wakasawazisha "mtizamo/mawazo" ya Pilato na ulimwengu wa kiroho.

**Dhanio.** Hili linarejerea uelewa wa jambo tulilowaza kabla. Mara nyingi tunaunda wazo au hukumu kuhusu mambo hata kabla hatujatazamisha maandiko yenyewe. Uelekezaji huu vile vile hujulikana kama upendeleo, kujitanguliza mbele, kudhania au kuelewa kabla.

**Uhakiki wa maandishi.** Hiki ni kitendo cha kutafasili maandiko kwa nukuu za kifungu bila kuangalia mazingira ya haraka au ukubwa wa mazingira katika fahisi moja. Hii inaondoa vifungu toka kwa kusudio la mwandishi wa awali na mara nyingi unahusha jaribio la kuhakiki maoni binafsi wakati huo likithibitisha mamlaka ya Kibiblia.

**Ualimu wa dini ya Kiyahudi.** Ngazi hii ya maisha ya watu wa Uyahudi yalianza walipokimbilia Babel (586-538 B.C). kama ushawishi wa makuhani na hekalu ulivyoondolewa, masinagogi ya kawaida yakawa mtizamo wa maisha ya Kiyahudi. Hivi vitovu vya kawaida vya tamaduni za Kiyahudi, ushirika, kuabudu na elimu ya Biblia ikawa mtizamo wa maisha ya kidini kitaifa. Katika siku za Yesu, hii "dini ya wandishi" ilikuwa sambamba na ile ya makuhani. Katika kuanguka kwa Yerusalem mwaka wa 70 A.D muundo wa kiandishi, ukitawaliwa na mafalisayo, walidhibiti mwelekeo wa maisha ya kidini ya Kiyahudi. Inachagizwa na utafasili wa kiutendaji, na wa kisheria wa Torah kama ulivyoelezwa katika tamaduni za Talmud.

**Ufunuo.** Hili ni jina lililopewa kwenye dhana ya kwamba Mungu amesemezana na mwanadamu. Wazo zima mara nyingi limeelezewa katika maneno matatu- (1) Ufunuo-Mungu ametenda katika historia ya mwanadamu (2) Uvuvio-Ametoa tafasili sahihi ya matendo yake na maana yake kwa mtu Fulani aliyemchagua kuweka kumbukumbu ya mwanadamu (3)Nuru-Amempa Roho wake kumsaidia mwanadamu kuelewa ukaribu wake.

**Elimu-maana.** Hii imerejerea kipimo halisi cha maana kinachohusiana na neno. Kimsingi ina vidokezo mbali mbali vya neno katika mazingira tofauti.

**Maandiko ya kale ya Kiyunani.** hili ni jina lililopewa tafasili ya Kiyunani ya Agano la kale la Kiebrania. Mafundisho ya zamani yanasema kuwa yaliandikwa kwa siku 70 na wasomi sabini wa Kiyahudi kwa ajili ya maktaba ya Alexandria, Misri. Tarehe ya kimapokeo ilikuwa 250 B.C (kiukweli yawezekana ilichukua zaidi ya miaka Mia kumaliza kuandika). Tafasili hii ni muhimu kwa sababu (1)inatupatia andiko la kale kulinganisha na andiko la Kiebrania (2) inatuonyesha sisi hali ya utafasili wa Kiyahudi katika karne ya pili nay a tatu B.C (3) inatupatia uelewa wa umasihi wa Kiyahudi kabla ya kumkataa Yesu. Kifupi chake ni "LXX".

**Machapisho ya asili.** Haya ni machapisho ya asili ya Kigiriki ya karne ya Nne A.D. Yalivumbuliwa na msomi wa Kijerumani, Tischendorf, katika nyumba ya mtawa Catheline, kwenye eneo la kimila la mlima Sinai. Maandishi haya yameundwa na herufi ya kwanza ya Kiebrania ya alfabeti inayoitwa "*eleph*" (א). Yanajumuisha Agano la Kale na Agano Jipya kwa pamoja.

**Kujitakasa.** Hili neno ni kisawe chenye istiari katika maana kuwa linakwenda mpaka kwenye historian a mazingira ya fasihi ya kifungu na kulifasili katika msingi wa jambo lingine.

**Visawe.** Hii inarejerea maana yenye kariba au mfano wa maana moja (ingawa kiukweli hakuna maneno mawili yenye elimu-maana kamili iliyopishana). Kwa karibu sana yanahusiana kiasi kwamba moja linaweza kuwa mbadala wa lingine katika sentesi bila kupoteza maana. Pia yanatumika kuunda moja kati ya miundo mitatu ya mlinganyo wa ushairi wa Kiebrania. Kwa maana hii inarejesha mistari miwili ya ushairi ambayo inaelezea kweli ile ile (cf. Zab 103:3).

**Sintaksi.** Hili ni neno la Kiyunani linalirejeresha muundo wa sentesi. Inahusiana na namna ya sehemu ya sentesi zinaweza wekwa pamoja kuleta maana kamili.

**Usanisi.** Hii ni moja ya maneno matatu yanayohusiana na aina ya ushairi wa Kiebrania. Neon hili linaongelea juu ya mistari ya ushairi uluojengwa juu ya mwingine katika maana moja, wakati mwingine huitwa "taaluma ya mabadiliko ya hali" (k.v. Zab 19:7-9).

**Thiolojia mpangilio.** Hii ni hatua ya utafasili ambayo inajaribu kuhusisha ukweli wa Biblia katika hali ya pamoja na mlingano. Ina mantiki zaidi kuliko historia tupu, ni uwasilishaji wa thiolojia ya Kikristo kwa namna ( Mungu, mtu, dhambi,wokovu).

**Buku la taratibu na kanuni za Kiyahudi.** Ni wadhifa uliokuwapo kwa ajili ya upangaji wa simulizi za kanuni na taratibu za Kiyahudi. Wayahudi wanaamini ulitolewa kwa Musa kwa kusimuliwa na Mungu kwenye mlima Sinai. Ki-ukweli inaelekea kuwa ni mkusanyiko wa hekima za walimu wa Kiyahudi kwa miaka mingi. Kuna matoleo mawili tofauti yaliyo andikwa juu ya Talmud: ya Babel na fupi la kiparestina ambalo halikwisha.

**Uhakiki wa tofauti za kiuwandishi.** Huu ni usomaji wa maandiko wa Biblia. uhakiki wa maandiko ni muhimu kwa sababu hakuna maandiko ya mwanzo yaliyopo na nakala zilizopo zinatofautiana toka moja hadi nyingine. Unajaribu kuelezea utofauti na kufika (karibu iwezekanavyo) na maneno ya awali kabisa ya miandiko ya Agano la kale na jipya. Mara nyingi unaitwa "uhakiki wa asili ya neno".

**Upokeaji wa Maandiko.** Usanifishaji huu ulianzia kwenye toleo la Elzevir la Agano jipya la Kiyunani katika mwaka wa 1633 A.D. Kimsingi ni muundo wa Agano jipya la Kiyunani lililozalishwa toka kwenye maandiko machache ya asili ya Kiyunani na matoleo machache ya Erasmo ya Kilatini (1510-1535), Stephano (1546-1559) na Elzevir (1624-1678). Katika *An Introduction to the Textual Criticism of The New Testament uk. 27 cha A.T Robertson* anasema "andiko la Byzantine kiutendaji ni aina ile ile ya uundaji wa maandiko. Andiko la Byzantine ni la thamani ya chini kati ya familia tatu ya maandiko ya awali ya Kiyunani (Kimagharibi, Alexandria na Byzantine). Inajumuisha mkusanyiko wa makosa ya karne nyingi za maandiko na nakala za mkono. Hata hivyo, A.T Robertson alisema uundaji wa maandiko umetunza kwa ajili yetu andiko sahihi kimalidhawa (uk.21). Mapokeo haya ya maandiko ya asili ya Kiyunani (hasa Erasmo, toleo la tatu la 1522) yanatengeneza msingi wa toleo la King James la mwaka 1611 A.D.

**Sheria za Musa.** Hili ni neno la Kiebrania lenye maana ya "ufundishaji". Lilitokea kuwa wadhifa rasmi wa maandishi ya Musa (Mwanzo mpaka Kumbu kumbu la Torati). Kwa Wayahudi ulikuwa ni mgawanyo wa kimamlaka wa kanuni za kanisa la Kiebrania.

**Uanishaji.** Hii ni aina ya urasimishaji wa wa utafasili. Mara nyingi unahusisha kweli ya Agano jipya inayopatikana katika vifungu vya kale kwa njia ya analojia. Namna hii ya kanuni za ufasili ilikuwa ni dalili kubwa ya njia za Alexandria. Kwa sababu ya matukano ya aina hii ya utafasili, mtu lazima aweke ukomo wa matumizi yake kwa mfano mahsusi ulioandikwa katika Agano jipya.

**Maandiko ya Vatican.** Haya ni maandiko ya asili ya Kiyunani ya karne ya Nne A.D . Yalipatikana kwenye maktaba ya Vatican. Uwasili wake unajumuisha vitabu vyote vya Agano la kale, ufunuo na Agano jipya. Hata hivyo, sehemu

zingine zilipotea( Mwanzo, Zaburi, Waebrania, Filemon na Ufunuo). Inasaidia maandiko ya asili kubadilisha miandiko ya maneno ya awali. Tena yameundwa kwa herufi kubwa "B".

**Tafasili ya Biblia ya Kilatini.** Ni jina la tafasili ya Biblia ya Kilatini ya Jerome. Ilikuwa ndio msingi au utafasili wa "kawaida"wa kanisa Katoriki la Rumi. Lilifanyika mwaka 380 A.D.

**Hekima ya Fasihi.** Hii ni fasihi tanzu iliyozoeleka enzi za kale karibu na pande za Mashariki (na ulimwengu wa kisasa). Kimsingi lilikuwa ni jaribio la kuelekeza kizazi kipya juu ya mwongozo wa maisha ya ushindi kupitia ushairi, mithali, au insha. Ilielezewa zaidi kwa watu binafsi kuliko kwenye jumuiya iliyoungana. Haikutumia viini macho kuweka historia, lakini ilisimamia uzoefu na uchunguzi wa maisha katika Biblia, Ayubu kupita Wimbo ulio Bora, anasadiki uwepo na ibada ya YAHWE, lakini mtizamo huu wa ulimwengu wa kidini sio wa wazi kwa uzoefu wa kila mtu kila wakati.

**Picha ya ulimwengu na Mtizamo wa Kidunia.** Haya ni maneno mwandani. Yote yana dhana ya kifalsafa kuhusiana na uumbaji. Neno "picha ya ulimwengu" inarejerea "kwa namna gani" juu ya uumbaji wakati "mtizamo wa kidunia" unahusiana na "nani." Maneno haya yote ni muhimu kwenye utafasili pale mwanzo 1-2 inaposhughulika hasa hasa na nani, na sio kwa namna gani juu ya ulimwengu.

**YAHWE/YEHOVA.** Hili ni jina la Agano la Mungu katika Agano la kale. Linaelezewa katika kitabu cha Kutoka 3:14. Ni muundo wa KISABABISHAJI wa neno la Kiebrania "kuwa" ambalo Wayahudi waliogopa kulitamka jina hili ili wasilitamke bure; kwa hiyo, walitumia jina lingine badala yake yaani "Adonai" likimaanisha "Bwana". Hivi ndivyo jina la Agano limetafasiliwa katika Kiingereza.

# MAELEZO YA KIMAFUNDISHO YA BOB

Mimi siangalii hasa habari za imani au kanuni za imani. Napendelea kuthibitisha Biblia yenyewe. Ingawa, natambua kuwa habari ya imani itawaleta wale tusiojuana ili kupima mtizamo wa mafundisho yangu. Katika siku zetu za leo zenye makosa mengi ya kithiolojia na upotofu, natoa muhtsari mfupi wa thiolojia yangu kama ufuatavyo.

1. Biblia, yote katika Agano la Kale na Agano Jipya, ni neon la Mungu lililovuviwa, lenye uhakika, lenye uzima na lenye mamlaka. Ni ufunuo pekee wa Mungu ulioandikwa na watu chini ya uongozi wa nguvu za ajabu (Angalia MADA MAALUM: UVUVIO[SPECIAL TOPIC: INSPIRATION). Ni kiini pekee cha ukweli sahihi kuhusu Mungu na Kusudi Lake (Angalia Mada Maalum: Mpango wa YHWH wa Ukombozi (Special Topic: YHWH's Eternal Redemptive Plan). Pia ni kiini pekee cha imani na utendaji wa kanisa lake.
2. Kuna Mungu mmoja tu wa uzima, uumbaji na ukombozi (Angalia MADA MAALUM: UWEPO WA MUNGU MMOJA (SPECIAL TOPIC: MONOTHEISM). Yeye ndiye muumbaji wa vitu vyote, vionekanavyo na visivyo onekana. Amejidhihilisha mwenyewe kama Mungu wa upendo na anayejali ingawa pia ni Mungu asiye na upendelea. Amejidhihilisha mwenyewe katika nafsi tatu tofauti: Baba, Mwana na Roho; haswa wanatengana lakini wanafanya kazi moja (Angalia MADA MAALUM: UTATU(SPECIAL TOPIC: TRINITY).
3. Muda wote Mungu yuko hai kuangalia ulimwengu huu. Kuna mpango wa ndani wa uumbaji wake usiobadilika na mtazamo wa kipekee unaomfanya binadamu kutenda mapenzi huru. Hakuna kinachoweza kutokea pasipo ruhusa na maarifa ya Mungu, bado anaruhusu uchaguzi kwa wote malaika na wanadamu. Yesu ni chaguo la Baba na wote kimanufaa wamechaguliwa katika Yeye. Ufahamu wa mbele wa Mungu kuhusu matukio hayampunguzii binadamu kubainisha maandiko yaliyoandikwa kabla. Wote tunahusika kwa mawazo yetu na matendo (Angalia Majaaliwa (Calvinism) Dhidi Ya Mapenzi Huru Ya Kibinadamu (Arminianism) Predestination (Calvinism) vs Human Free Will (Arminianism)
4. Binadamu, japo aliumbwa kwa sura ya Mungu na mbali na dhambi, aliamua kumwasi Mungu. Ingawa alijaribiwa na kitu chenye nguvu ya ziada (Angalia MADA MAALUM: UOVU BINAFSI (SPECIAL TOPIC: PERSONAL EVIL). Adamu na Hawa waliwajibika kwa utashi wao wenyewe kuamua. Uasi wao umeathiri utu wa uumbaji. Watu wote tunahitaji rehema na huruma ya Mungu yote kwa hali ya ushirika katika Adamu na uasi binafsi wa hiari.
5. Mungu anatoa aina ya msamaha na urejesho kwa binadamu aliyeanguka. Yesu Kristo, Mwana pekee wa Mungu Baba, akawa mwanadamu, akaishi maisha yasio na dhambi, na kwa kifo chake mbadala, akalipa malipo ya dhambi ya mwanadamu. Ndiyo njia pekee ya kurejesha ushirika wetu na Mungu. Hakuna njia nyingine ya wokovu isipokuwa kupitia imani ya kazi yake aliyoimaliza.
6. Kila mmoja wetu binafsi yampasa kupokea ahadi ya msamaha na urejesho katika Kristo. Hilo linatimizwa kwa njia ya imani ya hiari katika ahadi za Mungu kupitia Kristo Yesu na kugeuka kwa mapenzi huru kwa dhambi inayojulikana Tazama Mada Maalum:Ina Maana Gani "Kupokea" "Kusadiki" "Kukiri/Kutubu" na "Kusihi"? (Special Topic: What Does It Mean to "Receive," "Believe," "Confess/Profess," and "Call Upon"?)
7. Sisi sote tumesamehewa jumla na urejesho umelenga juu ya kuamini(Mada Maalum: "Kuamini" Katika Agano Jipya(Special Topic: "Believe" in the NT)katika Kristo na toba toka dhambini (MADA MAALUM: TOBA[AGANO JIPYA] SPECIAL TOPIC: REPENTANCE (NT) Ingawa, ushahidi wa mahusiano mapya unaonekana katika mabadiliko na badiliko endelevu. Dhumuni la Mungu kwa wanadamu sio tu kwenda mbinguni siku moja, lakini kufanana na Kristo kwa sasa. Wale wote ambao wanakombolewa kweli ingawa wakati mwingine wanatenda dhambi, wataendelea katika imani na toba siku zao zote za maisha.

8. Roho Mtakatifu ni "Yesu mwingine"(Mada Maalum: Yesu na Roho(Special Topic: Jesus and the Spirit) Yuko duniani kuwaongoza wale wote waliopotea katika Kristo na kujenga ufanano wa Kristo katika kuokolewa. Karama za rohoni zinapewa toka kwenye wokovu. Ni maisha na huduma ya Yesu yaliyogawiwa katika mwili wake, yaani kanisa. Vipawa 358 ambavyo kimsingi ndio mwelekeo na msukumo wa hitaji la Yesu likihamasishwa na tunda la Roho. Roho yu hai katika siku zetu kama alivyokuwa katika enzi za Biblia.
9. Baba amemfanya Yesu Kristo aliyefufuka kama mwamuzi w vitu vyote. Atarudi duniani kuhukumu wanadamu wote. Wale wote walioamini Yesu na majina yao yameandikwa katika kitabu cha uzima cha mwanakondoo watapata mwili na utukufu ataporudi. Wataishi nae milele. Ingawa, wale wote walioikataa kweli ya Mungu watatengwa milele toka katika furaha ya ushirika wa Mungu wa Utatu. Watahukumiwa pamoja na shetani na malaika zake. Hii hakika haijaisha au kukamilika lakini natarajia itakupa ladha ya kithiolojia ya moyo wangu, nafurahia maelezo:

"Katika mambo ya msingi-umoja, mambo yaliyo ukingoni-uhuru, katika mambo yote-upendo.